
Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya UNESCO kwa ajili ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika

# HISTORIA KUU YA AFRIKA •

Juzuu Lililofupishwa

## V Afrika kuanzia Karne ya Kumi na Sita hadi ya Kumi na Nane

MHARIRI B.A. OGOT



TUKI • CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM • UNESCO

Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika (UNESCO)

Historia Kuu ya Afrika · V

# Afrika Kuanzia Karne ya Kumi na Sita Hadi ya Kumi na Nane

MHARIRI B. A. OGOT

Toleo Lililofupishwa

TUKI . CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM . UNESCO

Jina la Asili: **GENERAL HISTORY OF AFRICA, VOL V**

© UNESCO 2000
ISBN 9976 911 22 X

*Maelezo yaliyotolewa na uwasilishaji wa matini zote kwenye chapisho hili haumaanishi maoni yoyote yale kwa upande wa UNESCO kuhusu sheria ya nchi yoyote ile, mji au eneo au mamlaka yake, au kuwekea mipaka eneo lolote lile.*
*Waandishi wanahusika na uteuzi na uwasilishaji wa taarifa za kweli zilizopo kwenye kitabu hiki na kwa maoni yaliyoelezewa ndani, ambayo si lazima yawe yale ya UNESCO na hayalifanyi Shirika liwajibike.*
*Toleo la Tafsiri ya Kiswahili limechapishwa kwa msaada wa kifedha wa UNESCO.*

Historia Kuu ya Afrika · V

# Afrika Kuanzia Karne ya Kumi na Sita Hadi ya Kumi na Nane

## Toleo Lililofupishwa

UNESCO Historia Kuu ya Afrika

| | |
|---|---|
| **Juzuu I** | *Mbinu na Historia ya Awali ya Afrika*<br>Mhariri **J. Ki-Zerbo** |
| **Juzuu II** | *Staarabu za Kale za Afrika*<br>Mhariri **G. Mokhtar** |
| **Juzuu III** | *Afrika kuanzia Karne ya Saba hadi ya Kumi na Moja*<br>Mhariri **I. Hrbek** |
| **Juzuu IV** | *Afrika kuanzia Karne ya Kumi na Mbili hadi ya Kumi na Sita*<br>Mhariri **J. Ki-Zerbo na D.T. Niane** |
| **Juzuu V** | *Afrika kuanzia Karne ya Kumi na Sita hadi ya Kumi na Nane*<br>Mhariri **B.A. Ogot** |
| **Juzuu VI** | *Afrika kuanzia Karne ya Kumi na Tisa hadi miaka ya 1880*<br>Mhariri **J.F. Ade Ajayi** |
| **Juzuu VII** | *Afrika Chini ya Utawala wa Kigeni 1880 - 1935*<br>Mhariri **A. Adu Boahen** |

## Toleo Lisilofupishwa la Jalada Jepesi

| | |
|---|---|
| **Juzuu VIII** | *Afrika Kuanzia 1935*<br>Mhariri **A.A. Mazrui**<br>Mhariri Msaidizi **C. Wondji** |

Toleo lililofupishwa la
HISTORIA KUU YA AFRIKA YA UNESCO

**Limechapishwa na:**

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI)
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
S.L.P. 35110
Dar es Salaam, Tanzania

Pamoja na:
UNESCO Publishing
7 Place de Fontenoy, 75700, Paris

Kimepangwa na kuchapwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, S.L.P. 35110, Dar es Salaam, Tanzania.

*YALIYOMO*


| | | |
|---|---|---|
| | *Dibaji* ............................................. | *vii* |
| | *Wasifu wa Mradi* .................................. | *xii* |
| | *Maelezo ya Wendo* ................................. | *xv* |
| | *Wana Kamati* ...................................... | *xvi* |
| | *Wasifu wa Waandishi* .............................. | *xviii* |
| *1* | *Mapambano kwa ajili ya biashara ya Kimataifa na taathira zake kwa Afrika* ........................ | *1* |
| *2* | *Miundo ya Kiafrika ya kisiasa, kiuchumi na kijamii katika kipindi hiki* ..................................... | *14* |
| *3* | *Miguro ya watu na kuibuka kwa miundo mipya ya jamii na siasa katika Afrika* ........................... | *27* |
| *4* | *Afrika katika historia ya ulimwengu* ................ | *42* |
| *5* | *Diaspora ya Waafrika katika dunia kongwe na mpya* ............................................. | *61* |
| *6* | *Ushindi wa Waturuki nchini Misri* .................. | *77* |
| *7* | *Nchi ya Sudani, 1500 – 1800* ........................ | *97* |
| *8* | *Moroko* ............................................. | *114* |
| *9* | *Algeria, Tunisa na Libya* ............................ | *131* |
| *10* | *Senegambia kuanzia karne ya kumi na sita hadi ya kumi na nane* ...................................... | *147* |
| *11* | *Mwisho wa himaya ya Songhay* ..................... | *169* |
| *12* | *Kutoka mto Niger hadi Mto Volta* .................. | *184* |
| *13* | *Madola na tamaduni za pwani ya Guinea ya Juu* ... | *206* |
| *14* | *Madola na tamaduni za pwani ya Guinea ya Chini* | *224* |
| *15* | *Wafon na Wayoruba* ................................. | *243* |
| *16* | *Madola ya Kihausa* .................................. | *255* |

| | | |
|---|---|---|
| *17* | *Kanem – Borno* ……………………………………… | *272* |
| *18* | *Kuanzia mbuga za Kameruni hadi Nili ya Juu*……. | *284* |
| *19* | *Ufalme wa Kongo na Majirani zake* ………………… | *301* |
| *20* | *Mfumo wa kisiasa wa Waluba na Walunda* ………… | *319* |
| *21* | *Zambezi ya Kusini* ………………………….. | *347* |
| *23* | *Utegemezi na kutegemeana kusini mwa Afrika* …… | *369* |
| *24* | *Pembe ya Afrika* ……………………………………… | *380* |
| *25* | *Afrika Mashariki: pwani* ………………………………… | *405* |
| *26* | *Ukanda wa Maziwa Makuu* …………………………… | *419* |
| *27* | *Bara ya Afrika Mashariki* ……………………………… | *447* |
| *28* | *Bukini na visiwa vya Bahari ya Hindi* ……………… | *460* |
| *29* | *Historia ya jamii za Kiafrika toka 1500 – 1800: hitimisho* ………………………………….. | *485* |
| | *Bibliografia* ……………………………………………… | 493 |
| | *Faharasa* ………………………………………………… | 508 |
| | *Sherehe* ……………………………………………… | 522 |

# *Dibaji*

**AMADOU - MAHTAR M'BOW**
*Mkurugenzi Mkuu wa Zamani wa UNESCO (1974-1987)*

Kwa muda mrefu, aina zote za uzushi na kashfa zilificha historia halisi ya Afrika kwa dunia nzima. Jamii za Kiafrika zilionekana kama jamii zisizoweza kuwa na historia. Licha ya kazi muhimu zilizofanywa na waasisi kama Leo Frobenius, Maurice Delafosse na Arturo Labriola tangu miongo ya mwanzoni mwa karne hii, wataalamu wengi wasio Waafrika hawakuweza kuondoa fikra fulani za awali walizozishikilia na wakadai kwamba kukosekana kwa kumbukumbu za maandishi kulifanya isiwezekane kufanya utafiti wowote wa kisayansi wa jamii kama hizo.

Ingawa tenzi za *Iliad* na *Odyssey* kwa usahihi zilichukuliwa kama kumbukumbu muhimu za historia ya Ugiriki ya kale, mapokeo simulizi ya Kiafrika, ambayo ndiyo kumbukumbu za pamoja za watu yanayounganisha matukio mengi yenye kuonyesha maisha yao, yanakataliwa kuwa hayana thamani. Kwa kuandika historia ya sehemu kubwa ya Afrika, kumbukumbu tu zilizotumika ni zile za kutoka nje ya bara. Matokeo yake ni kuwa kile walichoandika kilitoa sura ambayo sio ya njia halisi walizopita Waafrika, bali zile ambazo waandishi walifikiria kuwa pengine ndimo walimopita. Kwa kuwa Enzi za Kati za Ulaya mara nyingi ndizo zilizotumika kama kipimo, njia za uzalishaji, mahusiano ya kijamii na asasi za kisiasa zilitazamwa tu kwa kurejelea zama za Ulaya.

Kwa hakika, waandishi hao walikataa kuwachukulia Waafrika kama waumbaji wa tamaduni za asili ambazo zilichanua na kudumu kwa karne nyingi katika ruwaza walizozibuni na ambazo wanahistoria hawawezi kuzibaini isipokuwa pale tu watakapokubali kuachana na mawazo yao ya kashfa.

Zaidi ya hayo, bara la Afrika halikutazamwa hata kidogo kama eneo moja kihistoria. Kinyume chake, mkazo uliwekwa kwenye kila kitu kilichoelekea kuhalalisha wazo kwamba mgawanyiko ulikuwepo toka zama za kale, kati ya 'Afrika ya weupe' na 'Afrika ya Weusi', kila upande ukiwa haujui kuwa kuna watu wa upande mwingine. Mara nyingi Sahara ilielezewa kama eneo lisilopitika na hivyo kuzuia kuchanganyikana kwa makundi ya kimbari na watu au mabadilishano ya bidhaa, imani, desturi na mawazo baina ya jamii zilizozidi kukua katika kila upande wa jangwa. Mipaka iliyofungwa kabisa iliwekwa baina ya staarabu za Misri ya Kale na Unubi na ile ya watu wa kusini mwa Sahara.

Ni kweli kwamba historia ya Afrika kaskazini mwa Sahara imehusishwa kwa karibu mno na ile ya nchi za bonde la Bahari ya Mediterani kuliko ilivyokuwa kwa historia ya Afrika Kusini mwa Sahara, lakini hivi sasa inafahamika zaidi kwamba staarabu mbalimbali za bara la Afrika, pamoja na tofauti zao za lugha na tamaduni, zinawakilisha, kwa kiasi kikubwa au kidogo, michepuo ya kihistoria ya makundi ya watu na jamii yanayounganishwa na mahusiano ya karibu yenye umri wa karne nyingi.

Jambo jingine ambalo halikutendea haki utafiti wa uhakika wa Afrika ya Kale ilikuwa ni tokeazaji wa ubaguzi wa rangi, ikiwa ni pamoja na biashara ya utumwa na ukoloni, ambao ulizaa dharau na kutokuelewana na hata kupata mashiko kiasi kwamba hisia hizo kuvuruga hata dhana za msingi za uandikaji historia. Tokea wakati dhana za "mweupe" na "mweusi" zilipoanza kutumika kama vitambulisho vya jumla na wakoloni, ambao walichukuliwa kuwa watu wa daraja la juu, ilibidi Waafrika waliotawaliwa wapambane dhidi ya utumwa wa kiuchumi na wa kisaikolojia. Waafrika wulitambuliwa kwa rangi ya ngozi zao, walifanywa kama bidhaa, walitayarishwa ili kufanya kazi ngumu na hatimaye, katika fikra za waliowatawala, waliishia kuashiria mbari ya *kinegro* ambayo ilibuni wa na kudaiwa kuwa mbari duni. Ruwaza hii ya utambulisho wa uwongo ilidhalilisha historia ya watu wa Afrika katika fikra za watu kufikia kiwango cha historia ya kimbari, ambamo ufahamu wa ukweli wa kihistoria na kitamaduni ulikuwa lazima upotoshwe.

Hali imebadilika vya kutosha tangu mwishoni mwa Vita Vikuu vya Pili vya Dunia na hasa toka nchi za Kiafrika zipate uhuru na kuanza kushiriki kikamilifu katika maisha ya jumuiya ya kimataifa na katika mabadilishano ambayo ndiyo sababu ya kuwepo kwake. Idadi kubwa ya wanahistoria wamejitahidi kukabili utafiti wa Afrika kwa mtazamo thabiti, usiopendelea na wa wazi kwa kutumia - pamoja na tahadhari zote - kumbukumbu halisi ya Kiafrika. Kwa kutumia haki yao ya kuchukua jitihada za kihistoria, Waafrika wenyewe wameihisi haja kubwa ya kuanzisha upya ukweli wa kihistoria wa jamii zao kwenye misingi thabiti.

Katika muktadha huu, umuhimu wa majuzuu haya nane ya *Historia Kuu ya Afrika,* ambayo UNESCO inachapisha unajieleza wenyewe.

Wataalamu kutoka kwenye nchi nyingi ambao wanashughulikia mradi huu walianza kwa kuweka misingi ya kinadharia na ya kimbinu kwa ajili ya *Historia* hii. Wamekuwa katika hali ngumu ya kuutilia shaka urahisishaji mno wa historia ya Afrika unaotokana na dhana ya wazo la upande mmoja na finyu kuhusu historia ya dunia na kuanzisha upya taarifa za kweli kila ilipolazimu na ilipowezekana. Wamejitahidi kuonyesha bayana data za kihistoria zinazotoa picha ya wazi kuhusu mabadiliko ya watu tofauti wa Afrika katika mandhari yao maalum ya kijamii na kitamaduni.

Ili kuikabili kazi hii kubwa, ambayo ilifanywa kuwa yenye utata na ngumu zaidi na wingi wa kumbukumbu za aina nyingi na ukweli kwamba nyaraka zilikuwa zimesambaa sana, imebidi UNESCO iende hatua kwa hatua. Hatua ya kwanza, kuanzia 1963 hadi 1969, ilikuwa ni ya kukusanya nyaraka na kutayarisha mpango wa kazi. Migawanyo ya kazi ilifanyika uwandani na ilijumuisha kampeni za kukusanya mapokeo simulizi, uundaji wa vituo vya nyaraka vya kikanda kwa ajili ya mapokeo simulizi, ukusanyaji wa miswada isiyochapishwa ya Kiarabu na Kiajemi (lugha za Kiafrika

zilizoandikwa kwa hati za Kiarabu), utengenezaji wa orodha ya kumbukumbu za kale na utayarishaji wa Kiongozi cha Kumbukumbu za Historia ya Afrika (*A guide to the sources of the History of Africa)* kutokana na hifadhi za nyaraka na maktaba ya nchi za Ulaya na baadaye kuchapishwa katika majuzuu kumi na moja. Zaidi ya hayo, mikutano iliandaliwa kuwawezesha wataalamu kutoka Afrika na mabara mengine kujadili masuala ya mbinu, na kuweka misingi wazi ya utekelezaji wa mradi huu baada ya uchunguzi makini wa kumbukumbu zilizokuwepo.

Hatua ya pili, ambayo ilianza 1969 hadi 1971, ilihusika na uwekaji sawa wa *Historia* na kuunganisha sehemu zake tofauti. Madhumuni ya mikutano ya kimataifa ya wataalamu iliyofanyika huko Paris mwaka 1969 na Addis Abbaba mwaka 1970, yalikuwa ni kuchunguza na kufafanua matatizo yaliyopo kwenye kusawidi na kuchapisha *Historia;* kuitoa historia hiyo katika majuzuu manane, kuwa na chapa kuu katika Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu, kuitafsiri katika lugha za Kiafrika kama vile Kiswahili, Kihausa, Kifulfulde, Kiyoruba au Kilingala, matarajio ya chapa za baadaye kwa Kijerumani, Kirusi, Kireno, Kihispania na Kichina na vilevile chapa zilizofupishwa kwa ajili ya umma mpana wa Kiafrika na Kimataifa.

Hatua ya tatu imehusu usawidi wenyewe na uchapishaji. Hatua hii ilianza kwa kuteuliwa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi yenye wajumbe 39, theluthi mbili miongoni mwao wakiwa Waafrika na theluthi moja wasio Waafrika, ambayo ndiyo Kamati inayochukua jukumu la kitaaluma kwa *Historia* hii.

Mbinu iliyotumika ni ya taaluma fungamano na imekitwa kwenye mkabala wenye jiha za namna tofauti na kumbukumbu za aina nyingi. Ya kwanza miongoni mwa hizi ni akiolojia, ambayo ndiyo taaluma yenye ufumbuzi kwa mambo mengi ya historia ya tamaduni na staarabu za Afrika. Kutokana na akiolojia, inakubalika sasa kuwa Afrika huenda ndio ilikuwa chanzo cha wanadamu na eneo - katika kipindi cha Neolithi — la moja ya mapinduzi ya kitekuolojia ya kwanza katika historia. Akiolojia pia imeonyesha kwamba Misri ilikuwa mahali ambapo kulikuwa na mojawapo ya tamaduni za kale maarufu mno duniani. Lakini kumbukumbu nyingine muhimu sana ni mapokeo simulizi ambayo baada ya kudharauliwa kwa muda mrefu, sasa yameibuka kama chombo muhimu cha kuvumbulia historia ya Afrika, kwa kufanya iwezekane kufuatilia mijongeo ya watu wake mbalimbali katika kitambo cha nafasi na wakati, kuelewa maono ya Kiafrika kuhusu dunia kutokea ndani mwake na kuzingatia sifa za asili za amali ambamo ndimo zilipokitwa tamaduni na asasi za bara hili.

Tunaishukuru Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi inayosimamia *Historia Kuu ya Afrika,* na kwa Waandishi, Wahariri na Watunzi wa majuzuu mbalimbali na sura zake, kwa kuipatia mwanga mpya ukale wa Afrika katika uasilia na muundo wake mzima na kwa kuepukana na inadi katika utafiti wa masuala muhimu. Miongoni mwa masuala haya tunaweza kutaja: biashara ya watumwa, "jeraha lisilopona", ambayo ilisababisha mojawapo ya uhamishaji wa kikatili wa watu wengi katika historia ya mwanadamu, ambao ulifyonza uhai wa bara la Afrika na papo hapo kuchangia sana katika upanuzi wa uchumi na biashara huko Ulaya. Masuala mengine ni ukoloni na athari zake zote kwa idadi ya watu, uchumi, saikolojia na utamaduni, mahusiano kati ya Afrika kusini mwa Sahara na ulimwengu wa Kiarabu; na mwisho, harakati za kutokomeza ukoloni na za

ujenzi wa taifa ambazo ziliamsha akili na hisia za watu ambao baadhi yao wangali hai na pengine wangali wakiendesha harakati. Masuala haya yote yametajwa kwa kuzingatia ukweli na umakini aambazo ni sifa kubwa za *Historia* hii.Kwa kuchunguza ujuzi wetu wote wa Afrika, kutoa mawazo ya namna mbalimbali juu ya tamaduni za Afrika na kwa kutoa mtazamo mpya wa historia, *Historia* hii ina faida ya pekee ya kubainisha mwanga na kivuli na ya kudhihirisha wazi tofauti za maoni ambazo yawezekana zikawepo kati ya wataalamu.

Kwa kuonyesha kasoro katika mikabala ya kimbinu iliyotumika kwa muda mrefu katika kufanya utafiti kuhusu Afrika, *Historia* hii inadai kufanyike utafiti mpya na wenye uangalifu kwa maeneo ya matatizo ya namna mbili ya uandikaji wa historia na mahusiano yaliyopo kati yake, namna ambazo zinaunganishwa na uhusiano wa kutegemeana. Kama vile ilivyo kazi yoyote ya kihistoria yenye thamani, *Historia* hii inaandaa njia kwa ajili ya utafiti mwingi zaidi kuhusu mada za aina mbalimbali.

Ni kwa sababu hiyo kwamba Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi, ikishirikiana kwa karibu na UNESCO, iliamua kuanzisha tafiti za ziada katika kujaribu kuyaingia kwa kina masuala kadhaa yatakayowezesha kueleweka kwa vipengele fulani vya kale ya Afrika. Matokeo ya tafiti hizo yanayochapishwa katika mfululizo wa *Mitaala na Nyaraka za UNESCO- Historia Kuu ya Afrika*[1] yatakuwa kijalizo muhimu kwa *Historia* hii kama zitakavyokuwa pia kazi zilizopangwa kufanyika juu ya vipengele vya historia ya taifa au ya majimbo ya Afrika.

*Historia Kuu* inatoa mwanga kuhusu umoja wa kihistoria wa Afrika na pia mahusiano ya bara hili na mabara mengine, hasa Amerika na Caribbean. Kwa muda mrefu mambo ya kibunifu ya vizazi vya Waafrika katika Amerika yalilundikwa pamoja na baadhi ya wanahistoria kama mkusanyo wa mambo mchanganyiko wa *Uafrika.* Kwa hakika huu si mtazamo wa wandishi wa *Historia* hii ambamo upinzani wa watumwa waliosafirishwa kwenda Amerika, kushiriki mfululizo na kwa wingi kwa vizazi vya Waafrika katika mapambano kwa ajili ya uhuru wa mwanzo wa Amerika na katika harakati za ukombozi wa kitaifa, yanatazamwa vizuri kama yalivyokuwa: utetezi wa dhati wa kujitambua, uliosaidia kuunda dhana ya kilimwengu ya jamii ya watu. Ingawa jambo hili linaweza likatofautiana katika sehemu mbalimbali ni dhahiri sasa kuwa namna za kuhisi, kufikiri, kuota ndoto na kutenda katika mataifa fulani ya magharibi zimeathiriwa na urithi wa Kiafrika. Urithi wa kitamaduni wa Kiafrika unaonekana kila mahali kutoka kusini mwa Marekani hadi kaskazini mwa Brazil, katika Caribbean na

---

[1] Majuzuu kumi na mbili yafuatayo yamekwishachapishwa katika mfululizo huu: *Kukaliwa kwa Misri ya Kale na ufasiri wa hati za Kimeroi; Biashara ya Utumwa Afrika tangu karne ya kumi na tano hadi karne ya kumi na tisa; Mahusiano ya kihistoria kuvuka Bahari ya Hindi. Uandikaji wa historia wa Kusini mwa Afrika; Kuondoka katoka ukaloni Afrika Kusini mwa Afrika na Pembe ya Afrika; Majina ya mbari na ya sura ya nchi ya Afrika; Mahusiano ya kihistoria kijamii na kitamaduni baina ya Waafrika weusi na Waarabu tangu 1935 hadi leo; Mbinu za historia ya sasa ya Afrika; Afrika na vita vya Pili vya Dunia; Uelimishaji na uandikaji historia Afrika Kale ya Libya; Dhima ya Vyama vya Wanafunzi wa Kiafrika kwenye mabadiliko ya kisiasa na kijamii ya Afrika kuanzia 1900 hadi 1975.*

kwenye pwani ya Bahari ya Pacific. Katika sehemu fulani urithi huo ni msingi wa ubainisho wa kitamaduni wa baadhi ya vipengele muhimu kabisa vya watu.

*Historia* hii pia huonyesha dhahiri mahusiano ya Afrika na kusini mwa bara la Asia kupitia Bahari ya Hindi na michango ya Kiafrika katika staarabu nyinginezo kutokana na mabadilishano baina yake na maeneo hayo.

Nina hakika kuwa juhudi za watu wa Afrika za kutwaa kwa nguvu au kuimarisha uhuru wao, za kupata maendeleo yao na kutetea maumbile yao ya kitamaduni lazima zitokane na utambuzi wa kihistoria uliohuishwa, wenye kushabikiwa na wa kuzingatiwa na kila kizazi.

Kwa kuangalia historia ya maisha yangu, uzoefu nilioupata kama mwalimu na kama mwenyekiti, toka siku za awali za uhuru, wa tume za mwanzo zilizoundwa kurekebisha mitaala ya historia na jiografia katika baadhi ya nchi za Afrika Magharibi na Kati, ulinifundisha jinsi ilivyokuwa muhimu kwa elimu ya vijana na kwa taarifa kwa watu wote kwa jumla, kuwa na vitabu vilivyochapishwa na wataalamu wenye ujuzi wa ndani kuhusu matatizo na matumaini ya Afrika na wenye uwezo wa kuyaelewa mambo yote ya bara zima.

Kutokana na sababu zote hizi, shabaha ya UNESCO itakuwa ui kuhakikisha kwamba hii *Historia Kuu ya Afrika* inasambazwa katika lugha nyingi na kutumiwa kama msingi wa kuandaaa vitabu vya watoto, vitabu vya kiada na vipindi vya radio na televisheni. Hivyo vijana wakiwa watoto wa shule au wanafunzi, na watu wazima katika Afrika na penginepo, wataweza kupata picha kamili ya kale ya bara la Afrika na vipengele vinavyoelezea picha hiyo na vilevile kuelewa vizuri urithi wake wa kitamaduni na mchango wake katika maendeleo ya jamii ya watu. Kwa hivyo, *Historia* hii itaweza kuchangia katika ushirikiano bora wa kimataifa na mshikamano imara miongoni mwa watu katika matumaini yao ya kupata haki, maendeleo na amani. Hii, walau, ndio tumaini langu kubwa.

Kinachohakia ni kwa mimi kutoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi, mwandishi, wahariri wa majuzuu mbalimbali, waandishi na wale wote walioshiriki katika kazi hii kubwa. Kazi waliyoikamilisha na mchango walioutoa unadhihirisha jinsi watu wenye usuli tofauti lakini wenye moyo mmoja wa ridhaa na hamasa wa kuhudumia ukweli wa kilimwengu wanavyoweza, ndani ya kiunzi cha kimataifa kilichotolewa na UNESCO, kufanikisha mradi wenye umuhimu mkubwa kisayansi na kitamaduni. Natoa shukrani pia kwa mashirika na serikali ambazo ukarimu wake umeiwezesha UNESCO kuchapisha *Historia* hii katika lugha tofauti na hivyo kuhakikisha kwamba itapata uzito inaostahiki duniani kote, na kwa jinsi hiyo kuhudumia jumuiya nzima ya kimataifa.

# *Wasifu wa Mradi*

*B.A. OGOT*[1]
*Rais wa Zamani, Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi kwa ajili ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika (1978-1983)*

Mkutano Mkuu wa UNESCO katika Kikao chake cha 16 ulimwagiza Mkurugenzi Mkuu kushughulikia usawidi wa *Historia Kuu ya Afrika*. Kazi hii kubwa ya kutekeleza mradi ilikabidhiwa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi ambayo ilianzishwa na Bodi ya Utendaji mnamo 1970. Kamati hii kwa mujibu wa Sheria iliyopitishwa na Bodi ya Utendaji ya UNESCO mnamo mwaka 1971, ina wajumbe thelathini na tisa (theluthi mbili miongoni mwao wakiwa Waafrika na theluthi moja ni watu wengine wasio Waafrika) wanaoshiriki kwa nafasi zao binafsi na kuteuliwa na Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO kwa kipindi ambacho Kamati itadumu.

Kazi ya kwanza ya Kamati ilikuwa ni kufafanua sifa kuu za kazi hii. Hizi zilifafanuliwa katika kikao cha kwanza cha Kamati kama ifuatavyo:

(a) Ingawa lengo lake ni kiwango cha juu kabisa cha kisayansi, Historia hii hainuii kuwa timilifu na ni kazi ya usawidi inayoepukana na inadi. Katika hali zake nyingi, historia hii ni tamko juu ya matatizo yanayoonyesha hali ya sasa ya maarifa na mikondo mikuu ya utafiti, na haisiti kuonyesha hitilafu za mtazamo pale ambapo zipo. Kwa namna hii inaweka msingi kwa kazi za siku zijazo.

(b) Katika kazi hii Afrika inatazamwa katika ujumla wake. Nia ni kuonyesha mahusiano ya kihistoria kati ya sehemu zote za bara ambazo mara nyingi hutengwa katika kazi ambazo zimechapishwa hadi sasa. Mahusiano ya kihistoria ya Afrika na mabara mengine yanashughulikiwa ipasavyo kwa kuchanganuliwa kuzingatia mabadilishano baina yake na athari kutoka pande zote na kudhihirisha, katika mwanga halisi, mchango wa Afrika kwa historia ya mwanadamu.

(c) Kwa mahususi, *Historia Kuu ya Afrika* ni historia ya mawazo na staarabu, jamii na asasi. Imetegemezwa kwenye vyanzo vingi vya aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na mapokeo simulizi na namna za sanaa.

---

[1] Wakati wa Mikutano Mkuu wa Sita wa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi kwa ajili ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika (uliofanyika Brazaville Agosti 1983), uchunguzi wa wajumbe wapya ulifanyika na nafasi ya Profesa Ogot ilichukuliwa na Profesa Albert Adu Boahen.

(d) Kimsingi, *Historia* inatazamwa kutokea ndani. Ingawa ni kazi ya kitaalamu, pia kwa kadri kubwa, inaakisi kwa uaminifu jinsi waandishi wa Kiafrika wanavyotazama ustaarabu wao wenyewe. Pamoja na kuandaliwa kwa mtazamo wa kimataifa, na ikichota maarifa yote ya kisayansi yaliyopo wakati huu, yapaswa pia iwe kipengele muhimu kabisa katika utambuzi wa urithi wa Kiafrika na yapaswa kudhihirisha vipengele vinavojenga umoja barani. Juhudi hii ya kutazama mambo kutokea ndani ni sifa mpya ya mradi huu na pamoja na thamani yake ya kisayansi, inapaswa kuipatia mradi umuhimu wa kujadiliwa vipana. Kwa kuonyesha sura halisi ya Afrika, *Historia* inaweza, katika enzi iliyozama kwenye mapambano ya kiuchumi na kiufundi, kutoa dhana mahsusi ya amali za mwanadamu.

Kamati imeamua kuwasilisha kazi ya miaka milioni tatu ya historia ya Afrika katika majuzuu manane, kila moja likiwa na karibu kurasa mia nane za matini na mifano, picha, ramani na michoro.

Mhariri Mkuu akisaidiwa, pale inapolazimu, na wahariri wasaidizi wawili, ana jukumu la kuandaa kila juzuu. Wahariri wanachaguliwa na Kamati ama kutokana na wajumbe wake au kutoka nje kwa wingi wa theluthi mbili. Hawa wana jukumu la kuandaa majuzuu kulingana na maamuzi na mipango iliyokubaliwa na Kamati. Kuhusu mambo ya kisayansi wanaiwajibikia Kamati, au kati ya mikutano miwili ya Kamati watawajibikia Idara kuhusiana na maudhui ya majuzuu, miswada ya mwisho ya matini, mifano na kwa jumla, vipengele vote vya kisayansi na kiufundi vya *Historia*. Idara mwishowe huthibitisha muswada wa mwisho. Inapoona kwamba muswada uko tayari kuchapishwa inaukabidhi kwa Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO. Hivyo, katika kipindi kati ya Vikao Viwili, Kamati au Idara huendelea kusimamia mradi.

Kila juzuu lina kama sura thelathini. Kila sura ni kazi ya mwandishi mkuu, akisaidiwa, inapolazimu, na mshiriki mmoja au wawili. Waandishi wanachaguliwa na Kamati kutokana na sifa na uzoefu wa kitaaluma. Waandishi wa Kiafrika hupewa upendeleo alimradi wawe na sifa zinazohitajika. Juhudi maalumu pia hufanywa kuhakikisha kwamba kila inapowezekana kanda zote za bara na vile vile kanda nyingine zenye historia au utamaduni unaohusiana na Afrika zinapata uwakilishi sawa miongoni mwa waandishi.

Pale mhariri wa juzuu anapothibitisha matini za sura, zinapelekwa kwa wajumbe wote wa Kamati kwa uhakiki. Zaidi ya hayo, matini ya mhariri wa juzuu inawasilishwa kwa uchunguzi, kwa Kamati ya Wasomaji, iliyoundwa ndani ya Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi kulingana na uwezo wa wajumbe wake katika uwanja wa kitaaluma. Kamati ya Wasomaji inachanganua sura kimaudhui na kimuundo. Kisha Idara hutoa uthibitisho wa mwisho kwa miswada.

Utaratibu kama huu unaoonekana mrefu na mgumu, unaonekana kuwa wa lazima kwani unatoa uthibitisho bora kabisa wa uhakika wa kisayansi wa *Historia Kuu ya Afrika*. Kwa hakika, kumewahi kuwepo matukio ambapo Idara imeikataa miswada au kusisitiza ifanyiwe marekebisho makubwa au hata mwandishi mwingine kuombwa

asawidi sura. Hutokea pia wataalamu wenye ujuzi wa kipindi fulani cha historia au wa swali fulani mahsusi kuombwa ushauri ili kukamilisha juzuu fulani.

Kazi hii itachapishwa kwa mara ya kwanza katika matoleo ya jalada gumu kwa lugha za Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu na baadaye katika matoleo ya jalada laini kwa lugha hizo. Matoleo yaliyofupishwa kwa lugha za Kiingereza na Kifaransa ndiyo yatatafsiriwa kwa lugha za Kiafrika. Kamati imechagua lugha za Kiswahili na Kihausa kama lugha za kwanza za Kiafrika za kufanyia tafsiri za kazi hii.

Aidha, kila juhudi itafanywa kuhakikisha *Historia Kuu ya Afrika* inachapishwa katika lugha nyingine kubwa kimataifa kama vile Kichina, Kireno, Kirusi, Kijerumani, Kiitaliano, Kihispania, Kijapani, n.k.

Hivyo, ni dhahiri kwamba hii ni kazi nzito inayotoa changamoto kubwa kwa wanahistoria wa Kiafrika na kwa wasomi kwa jumla, na vilevile kwa UNESCO ambayo kazi hii inafanywa chini yake. Hii ni kwa kuwa ni jukumu kubwa mno kuandika historia ya bara la Afrika ya miaka milioni tatu iliyopita kwa kutumia kanuni makini kabisa za kitaaluma na kulazimika kuwahusisha wataalamu kutoka nchi, tamaduni, itikadi na mahusiano ya kihistoria tofauti. Mradi huu unabeba peo kubwa za mambo ya bara, ya kimataifa na ya taaluma mbalimbali.

Kwa kuhitimisha, ningependa kusisitiza umahimu wa kazi hii kwa Afrika na dunia. Katika kipindi ambamo watu wa bara la Afrika wanajitahidi kuunda umoja na ushirikiano mkubwa ili kutoa mwelekeo kwa mwenendo wa maisha yao, uelewa muafaka wa kale ya Afrika na utambuzi wa uhusiano miongoni mwa Waafrika na baina ya Afrika na mabara mengine, usingekuwa tu mchango mkubwa kwa maelewano miongoni mwa watu duniani bali pia chanzo cha maarifa ya urithi wa kitamaduni ambacho ni cha wataalamu wote.

# *Maelezo kuhusu Wendo*

Imekubaliwa kufuata utaratibu ufuatao wa kuandika tarehe. Ama kuhusu kipindi kabla ya historia, tarehe zinaweza kuandikwa kwa njia mbili.

Njia ya kwanza ni kwa kurejea enzi ya sasa yaani tarehe KS (Kabla ya Sasa), mwaka unaorejewa ukiwa ni + 1950; tarehe zote zinakuwa hasi kuhusiana na + 1950.

Njia nyingine ni kwa kurejea mwanzo wa enzi ya Ukristo. Kuhusiana na enzi hii, tarehe huwakilishwa kwa kutumia alama + au - kabla ya tarehe. Zinaporejewa karne, vifungu KK na WK nafasi yake huchukuliwa na `kabla ya enzi ya Ukristo' na `-a enzi ya Ukristo'.

Baadhi ya mifano ni kama hii Ifuatayo:

(i) 2300 KS = - 350

(ii) 2900 KK = - 2900
1800 WK = + 1800

(iii) Karne ya tano KK = Karne ya tano kabla ya enzi ya Ukristo
Karne ya tatu WK = Karne ya tatu ya enzi ya Ukristo.

# Wanakamati wa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika

*Tarehe zilizotajwa zinawakilisha tarehe za wanachama.*

Profesa J.F.Ade Ajayi
(Nigeria), tangu 1971
Mhariri Juzuu VI

Prof. F.A. Albuquerque Mourão
(Brazil), tangu 1975

Profesa D. Birmingham
(Uingereza), tangu 1985

Profesa A. Adu Boahen
(Ghana), tangu 1971
Mhariri Juzuu VII

Hayati H.E. Boubou Hama
(Niger), 1971-8 (alijiuzulu 1978);
alifariki 1982

Dakta (Bibi) Mutumba M. Bull
(Zambia), tangu 1971

Hayati Profesa D. Chanaiwa
(Zimbabwe), tangu 1975;
alifariki 1993

Profesa P.D. Curtin
(Marekani), tangu 1975

Profesa J. Devisse
(Ufaransa), tangu 1971

Profesa M. Difuila
(Angola), tangu 1978

Profesa H. Djait
(Tunisia), tangu 1975

Hayati H.E.M. El Fasi
(Morocco), tangu 1971; alifariki 1991
Mhariri Juzuu III

Profesa J.D. Fage
(Uingereza), 1971- 81 (alijiuzulu)

Hayati Profesa J.L. Franco
(Cuba), tangu 1971; alifariki 1989

Hayati Bw. M.H.I. Galaal
(Somalia), 1971 - 81; alifariki 1981

Profesa Dakta V.L. Grottanelli
(Italia), tangu 1971

Hayati Profesa E. Haberland
(Ujerumani Magharibi), tangu 1971; alifariki 1992

Dakta Aklilu Habte
(Ethiopia), tangu 1971

Hayati H.E.A. Hampâté Bâ
(Mali), 1971 - 8; (alijiuzulu); alifariki 1991

Dakta I.S. El-Hareir
(Libya), tangu 1978

Hayati Dakta I. Hrbek
(Czechoslovakia), tangu 1971; alifariki 1993
Mhariri Msaidizi Juzuu III

Hayati Profesa Cheikh Anta Diop
(Senegal),1971- 86; alifariki 1986

Hayati AbbéAlexis Kagame
(Rwanda), 1971 - 81; alifariki

Profesa I.N. Kimambo
(Tanzania), tangu 1971

Profesa J. Ki-Zerbo
(Burkina Faso), tangu 1971
Mhariri Juzuu I na IV

Bw. D. Laya
(Niger), tangu 1979

Dakta A. Letnev
(Urusi), tangu 1971

Dakta G. Mokhtar
(Misri), tangu 1971
Mhariri Juzuu II

Profesa P. Mutibwa
(Uganda), tangu 1975

Profesa L.D. Ngcongco
(Botswana), tangu 1971

Profesa D.T. Niane
(Senegal), tangu 1971
Mhariri Juzuu IV

Profesa T. Obenga
(Jamhuri ya Watu wa Kongo),
tangu 1975

Profesa Bethwell A. Ogot
(Kenya), tangu 1971
Mhariri Juzuu V

Profesa C. Ravoajanahary
(Madagascar), tangu 1971

Dakta (Bibi) A. Jones
(Liberia); tangu 1971

Hayati Profesa W. Rodney
(Guyana), 1979 - 80; alifariki 1980

Hayati Profesa M. Shibeika
(Sudan), 1971 - 80; alifariki 1980

Profesa Y.A. Talib
(Singapore), tangu 1975

Hayati Profesa A. Teixeira da Mota
(Ureno), 1978 - 82; alifariki 1982

Mgr T. Tshibangu
(Zaire), tangu 1971

Profesa J. Vansina
(Ubelgiji), tangu 1971

Hayati Mheshimiwa Dakta E. Williams
(Trinidad na Tobago), 1976-8;
alijiuzulu 1978; alifariki 1980

Profesa A.A. Mazrui
(Kenya)
Mhariri Juzuu VIII,
Siyo Mwanakamati

Profesa C. Wondji (Côte d'Ivoire)
Mhariri Msaidizi Juzuu VIII
Siyo Mwanakamati

*Ukatibu wa Kamati ya*
*Kimataifa ya Kisayansi*
C. Wondji
Sekta ya Utamaduni
Mkurugenzi, *Chargé de mission*
Msimamizi wa Miradi ya Historia
1, rue Miollis
75015 Paris

# Wasifu wa waandishi waliochangia makala kwenye juzuu kuu

*Toleo lililofupishwa lilitayarishwa kutoka kwenye toleo kuu lililoandikwa na waandishi wafuatao:*

SURA YA 1 — M. Maliwist (Poland): Mtaalamu wa uchumi na historia ya jamii ya Enzi ya Kati ya baadaye na mapema kipindi cha sasa; ni mwandishi wa machapisho na makala mengi kwenye somo hili, alikuwa Profesa wa Historia, Chuo Kikuu cha Warsaw; alikuwa mjumbe wa Clare Hall, Cambridge na mgeni wa Taasisi ya Taaluma ya Juu, Princeton; amefariki.

SURA YA 2 — P. Diagne (Senegal): Daktari wa Sayansi ya Siasa na Uchumi; mwanauchumi na mtaalamu wa Isimu; mwandishi wa kazi nyingi kuhusu makala ya kisiasa Afrika na sarufi mpya ya Kiwolof; hivi sasa ni Profesa na Mshauri.

SURA YA 3 — J. Vanstina (Ubelgiji): mtaalamu wa historia ya Afrika; mwandishi wa kazi nyingi na makala kuhusu historia ya Afrika kabla ya ukoloni; Profesa wa Historia na Anthropolojia; Chuo Kikuu cha Wisconsin.

SURA YA 4 — J.E. Inikori (Nigeria): Mtaalam wa historia ya kiuchumi; mwandishi wa machapisho na makala mengi kwenye somo hili; hivi sasa ni Profesa na Mkuu wa Idara, Chuo Kikuu cha Ahmadu Bello, Zaria.

SURA YA 5 — J.E. Harris (Marekani); Mtaalamu wa historia ya Afrika; mwandishi wa machapisho na makala mengi kwenye somo hili, hivi sasa ni Profesa, Chuo Kikuu cha Howard, Washington DC.

SURA YA 6 — R. Vesely (Chekoslovakia) : Mtaalamu wa historia ya Misri, diplomasia, matatizo ya kiuchumi ya nchi za Kiarabu Enzi ya Kati; mwandishi wa kazi nyingi kuhusu taaluma za historia na diplomasia ya kipindi cha kale cha nchi za Kiarabu (hasa Misri) na za Kiislamu; mhadhiri wa nchi za Kiarabu na Kiislamu na historia yao kwenye Kitivo cha Falsafa cha Chuo Kikuu cha Charles, Idara ya Taaluma za Mashariki na Afrika, Prague.

SURA YA 7 — Y.F. Hasan (Sudan): Mtaalamu wa historia ya Sudan; mwandishi wa kazi nyingi kwenye somo hili; alikuwa Profesa wa Historia, Chuo Kikuu cha Sudan na Mkurugenzi wa Kitengo cha Utafiti cha Sudani, Chuo Kikuu cha Khartoum; alikuwa Makamu wa Mkuu wa Chuo, Chuo Kikuu cha Khartoum

B.A. Ogot (Kenya) : Mtaalamu wa historia ya Afrika; mwanzilishi wa mbinu za historia simulizi; mwandishi wa machapisho mengi kwenye historia ya Afrika Mashariki; alikuwa Mkurugenzi wa Taasisi ya Kimataifa ya Kumbukumbu ya Louis Leakey; alikuwa Naibu Makamu wa Mkuu wa Chuo, Chuo Kikuu cha Nairobi, Profesa wa Historia, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

SURA YA 8 — M. El Fasi (Moroko): mwandishi wa kazi nyingi (kwa Kiarabu na Kifaransa) kuhusu historia ya Kiisimu na uhakiki wa fasihi, alikuwa Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Karawiyyin, Fez.

SURA YA 9 — M.H. Cherif (Tunisia): mtaalamu wa historia ya jamii na siasa ya Afrika ya Kaskazini; mwandishi wa makala mengi kuhusu historia ya Afrika ya Kaskazini; Profesa na Mkuu wa Kitivo cha Sayansi ya Jamii, Tunis.

SURA YA 10 — B.Barry (Senegal) : Daktari wa Historia, mwandishi wa kazi nyingi kuhusu Waalo, Senegambia na Futa Jallon; alikuwa Katibu Mkuu wa chama cha wanahistoria wa Afrika; ni mhadhiri kwenye Kitivo cha Sanaa, Chuo Kikuu cha Cheikh Anta Diop, Dakar.

SURA YA 11 M. Abitbol (Israel): mtaalamu wa Sudan ya Nigeria; mwandishi wa kazi nyingi kuhusu historia ya Sudani; Mchunguzi Mwandamizi, Chuo Kikuu cha Kihebrenia, Jerusalem.

SURA YA 12 M. Izard (Ufaransa): mtaalamu wa historia ya himaya ya Mossi (Burkina Faso) kabla ya ukoloni; mwana anthropolojia na historia; mwandishi wa machapisho na makala mengi, hasa kuhusu himaya ya kale ya Yatenga; Mchunguzi Mwandamizi katika Kituo cha Taifa cha Utafiti wa Kisayansi (Maabara ya Anthropolojia Jamii), Paris.

J. Ki-Zerbo (Burkina Faso); mtaalamu wa mbinu za historia ya Afrika; mwandishi wa makala mengi kuhusu Afrika ya Watu Weusi na historia yake; Profesa wa Historia, Chuo Kikuu cha Dakar.

SURA YA 13 C. Wondji (Côte d'Ivoire): mtaalamu wa historia ya sasa ya Afrika, mwandishi wa kazi nyingi za utamaduni wa Afrika na historia ya Côte d' Ivore; alikuwa Mkuu wa Idara ya Historia, Kitivo cha Sayansi ya Jamii, Chuo Kikuu cha Taifa cha Côte d' Ivore (Abidjan) na Naibu Mkurugenzi wa Taasisi ya Sanaa na akiolojia, Chuo Kikuu cha Abidjan; alikuwa Mshauri kwenye Ujumbe wa Kudumu wa Côte d' Ivore huko UNESCO, Paris.

SURA YA 14 A.A. Boahen (Ghana): mtaalamu wa historia ya Afrika Magharibi; mwandishi wa makala na machapisho mengi kuhusu historia ya Afrika, alikuwa Profesa na Mkuu wa Idara ya Historia, sasa ni Profesa Mstaafu, Chuo Kikuu cha Ghana.

SURA YA 15 E.J. Alagoa (Nigeria): mtaalamu wa historia ya Afrika na maandishi ya kihistoria; mwandishi wa taaluma nyingi za Ijo, mbinu na mapokeo simulizi na akiolojia; Profesa wa Historia, Chuo Kikuu cha Port Harcourt.

SURA YA 16 D. Laya (Niger): mtaalamu wa tamaduni za Afrika Magharibi; mwanaelimujamii, mwandishi wa kazi zinazohusu somo hili, alikuwa Mkurugenzi wa Kituo cha Taaluma za Lugha na Historia kutokana na mapokeo simulizi (CELHTO), Niamey.

SURA YA 17 B. Barkindo (Nigeria): mtaalamu wa uundaji dola wa uhusiano baina ya dola kwenye eneo la Chad; mwandishi wa kazi nyingi kuhusu somo hili; Profesa Mshiriki wa Historia, Chuo Kikuu cha Bayero, Kano.

SURA YA 18 E. M'Bokolo (Zaire): mtaalamu wa historia ya Afrika ya Watu Weusi; mwandishi wa kazi nyingi kuhusu somo hili; Mchunguzi mwandamizi huko EHESS; mhadhiri kwenye taasisi ya taalamu za siasa (IEP),Paris; mtangazaji kwenye Redio ya Kimataifa ya Ufaransa.

SURA YA 19 J. Vansina

T.Obenga (Jamhuri ya Watu wa Kongo): mtaalamu wa lugha za Afrika; mwandishi wa makala mengi kuhusu historia ya Afrika na Afrika kwenye dunia ya kale; alikuwa Profesa kwenye Kitivo cha Sanaa cha Chuo Kikuu cha Marien N'Gouabi, Brazzaville; Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Kimataifa cha Staarabu za Wabantu (CICIBA) Libreville.

SURA YA 20 Ndaywel è Nziem (Zaire): mtaalamu wa historia ya Afrika ya Kati; mwandishi wa kazi nyingi kwenye somo hili; anafundisha historia kwenye Chuo Kikuu cha Kinshasa na kwenye Taasisi ya Elimu ya Taifa; Mkurugenzi Mkuu wa Maktaba ya Taifa ya Zaire.

SURA YA 21 K.M. Phiri (Malawi) : mtaalamu wa historia ya Malawi na Afrika ya Kati na kusini; alikuwa mhadhiri na mhadhiri mwandamizi wa historia, Chuo Kikuu cha Malawi.

O.J.M. Kalinga (Malawi): mtaalamu wa historia ya eneo la Ziwa Malawi; mwandishi wa kazi juu ya somo hili; Profesa wa Historia, Chuo Kikuu cha Taifa cha Lesotho.

H.H.K. Bhila (Zimbabwe): mtaalamu wa historia ya Kusini-Mashariki ya Afrika; mwandishi kuhusu Kusini mwa Afrika; alikuwa Mkuu wa Idara ya Historia, Chuo Kikuu cha Zimbabwe; hivi sasa ni Naibu Katibu wa Bunge la Zimbabwe.

SURA YA 22 H.H.K. Bhila.

SURA YA 23 D. Denoon (Uingereza): mtaalamu wa Kusini na Mashariki ya Afrika; mwandishi juu ya somo hili; alikuwa mhadhiri wa kualikwa Chuo Kikuu cha Ibadan; hivi sasa ni Profesa kwenye Chuo Kikuu cha Taifa cha Australia, Canberra.

SURA YA 24 E. Haberland (Ujerumani): mtaalamu wa Ethiopia kabla ya ukoloni na Afrika Magharibi, mwandishi kuhusu Ethiopia, Mkurugenzi wa Taasisi ya Frobenius, Frankfurt; Profesa wa Ethnolojia na Historia ya Afrika, Chuo Kikuu cha Frankfurt; Mkurugenzi, Kituo cha Taaluma za Afrika huko Frankfurt.

SURA YA 25 A.I. Salim (Kenya): mtaalamu wa historia ya Afrika Mashariki; mwandishi wa makala mengi kuhusu Waswahili; Profesa na Mkuu wa Idara ya Historia, Chuo Kikuu cha Nairobi.

SURA YA 26 J.B. Webster (Kanada): mtaalamu wa historia kabla ya ukoloni, akizingatia mazingira; mwandishi kuhusu historia ya Waacholi na Wateso pamoja na *Shajara, Uhamaji na Ukame Afrika*; alikuwa Profesa na Mkuu wa Historia, Chuo Kikuu cha Makerere na cha Malawi; sasa ni Profesa wa Historia ya Afrika, Chuo Kikuu cha Dalhousie.

B.A. Ogot

J.P. Chrètien (Ufaransa): mtaalamu wa historia ya Burundi; mwandishi wa kazi nyingi kuhusu himaya za Maziwa Makuu na Afrika Mashariki ya Ujerumani; mtafiti mwandamizi kwenye Kituo cha Utafiti wa Afrika (CRA), Chuo Kikuu cha Paris 1.

SURA YA 27 W.R. Ochieng' (Kenya); mtaalamu wa historia ya Kenya, mwandishi wa kazi nyingi kuhusu somo hili; alikuwa mhadhiri mwandamizi wa historia ya Kenya; Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi. Hivi sasa yuko Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret, Kenya.

SURA YA 28 R.K. Kent (Marekani): mtaalamu wa historia ya Madagaska; mwandishi wa kazi nyingi kuhusu somo hili; Profesa wa Historia ya Afrika, Chuo Kikuu cha California, Berkeley.

SURA YA 29 B.O. Ogot


# 1 Mapambano kwa ajili ya biashara ya Kimataifa na taathira zake kwa Afrika

## *Utangulizi*

Mnamo mwaka 1500 ramani ya kijiografia na kisiasa ya dunia ilionyesha kuwepo kwa kanda kadhaa kubwa, ambazo kwa kiasi fulani zilikuwa huru: Mashariki ya Mbali, Mashariki ya Kati, Ulaya na hatimaye Afrika na fukwe zake za Mediterania, Bahari ya Shamu na Bahari ya Hindi, ambazo zilifungua milango ya biashara iliyokuwa ikiongezeka na Nchi za Mashariki. Kipindi cha kuanzia mwaka 1500 hadi 1800 kilishuhudia kuanzishwa kwa mfumo mpya wa kijiografia na kiuchumi wenye mwelekeo wa Bahari ya Atlantiki na ruwaza yake ya biashara ya pembe tatu iliyounganisha Afrika na Ulaya na nchi za Amerika. Kufunguliwa kwa biashara ya kuvuka Bahari ya Atlantiki, kulifanya Ulaya- hususan Ulaya Magharibi - kuwa juu ya Amerika na jamii za Kiafrika.

Katika nchi nyingi za Ulaya, kipindi cha tangu mwaka 1450 hadi mwaka 1630 kilishuhudia upanuzi mkubwa wa kiuchumi, kisiasa na kitamaduni. Upanuzi katika nchi za ng'ambo ulifikia hadi kwenye nchi kubwa zinazopakana na Bahari ya Atlantiki na hata kufikia mwamhao wa Bahari ya Pasifiki. Toka mwanzo pwani ya Afrika ilikuwa mojawapo ya maeneo hayo, lakini hali ya huko Afrika Kaskazini ilitofautiana na ile katika maeneo ya kusini mwa Sahara. Mediterania ilikuwa mandhari ya ushindani mkali baina ya Hispania, Ureno, Ufaransa na Afrika Kaskazini ya Kiislamu kwa upande mmoja na kwa upande mwingine himaya ya Waturuki (Wa-*Ottoman*) ambayo ilikuwa ikizidi kuwa mashuhuri. Mnamo mwaka 1517 Waturuki waliteka Misri. Baadaye waliteka sehemu kubwa ya peninsula ya Uarabuni na polepole kuanzisha utawala wao huko Tripoli, Tunis na Algiers. Hata hivyo, huko Moroko, Wareno waliweza kutawala sehemu kubwa ya pwani hadi kufikia Agadir na Safi, na Wakastile walianzisha vituo huko Tilimsan na Oran.

Ushindi huu uliwawezesha Wareno kudhibiti njia zilizoanzishwa zamani na zile njia muhimu za biashara ya dhahabu na watumwa kutoka Sudan Magharibi kupitia Sahara na Maghrib hadi Mediterania. Wazungu walichepua sehemu ya biashara hii, ambayo awali ilikuwa ikipelekwa nchi za Kiislamu, kwa faida yao, na hivyo kupunguza kiasi cha dhahabu kilichokuwa kikifika Maghrib. Hii yaweza kuelezea kutekwa kwa pindi la




*1.1 Afrika: vituo vikuu vya mahusiano ya biashara na Ulaya kuanzia Karne ya kumi na sita hadi ya kumi na nane*

Niger na Wamoroko mnamo mwaka 1591, kulikowawezesha kudhibiti njia kadhaa za biashara ya dhahabu na watumwa kutoka Afrika Magharibi hadi Maghrib na Misri. Kampeni maarufu ya kijeshi ya Judar Pasha, ambaye wenyewe alikuwa mwasi wenye asili ya Kiiberia, ni mfano halisi wa utamalaki katika karne ya kumi na sita.

Kwa muda wote katika karne ya kumi na tano na mwanzoni mwa karne ya kumi na sita, Wareno walianzisha vituo vingi vya biashara katika pwani ya Afrika Magharibi na kuwafanya watu wa pwani na watawala wao kuwa washiriki kwenye biashara na Wazungu. Baada ya mwaka 1481-2 ngome ya El Mina ilitokea kuwa kituo mashuhuri cha biashara huko Gold Coast. Huko Afrika Mashariki, Wareno walitumia mbinu tofauti: walibomoa ngome za Sofala, Mombasa na miji mingine ya pwani, wakaweka vituo vya kijeshi pale na kutoza kodi kwa ajili ya mfalme wa Ureno. Wakati huo huo, walijaribu kutwaa biashara ya dhahabu, pembe za ndovu na metali kati ya pwani, bara na India.

Mwanzoni mwa karne ya kumi na sita, biashara huko El Mina, pale Mto Gambia unapoingilia baharini, huko Sierra Leone na huko Sofala, iliingiza faida kubwa hasa kutokana na kununuliwa kwa dhahabu kwa bei ya chini, na kwa kiasi kidogo, kutokana na biashara ya watumwa kutoka bara. Biashara hii mwanzoni iliingizia Ureno faida kubwa. Kuingia kwa kiasi kikubwa cha dhahabu nchini humo kulifanya iwezekane kwa Mfalme Yohana II na mrithi wake, Manuel, kupiga chapa sarafu ya *cruzado* – sarafu ya dhahabu ya thamani kubwa – na muhimu zaidi, kuongeza idadi ya meli na kuimarisha utawala wa makoloni na dola. Hatua hii ya mwisho ilitoa fursa kwa makabaila na waungwana kupata nyadhifa nyingi za kifahari na zenye faida. Biashala na Afrika, na baadaye na India, iliharakisha maendeleo ya tabaka la wafanyabiashara wa Kireno ambalo lilikuwa lingali dhaifu mnamo karne ya kumi na tano. Hivyo, Ureno yaweza kufikiriwa kuwa ilikuwa imeingia kwenye upanukaji wa kudumu wa kiuchumi na kisiasa. Hata hivyo, muundo wake wa kijamii na kiuchumi uliokuwa duni na goigoi ulizuia upanukaji huo kufanyika. Upanukaji nchi za ng'ambo ulihitaji matumizi makubwa ya fedha na ununuzi wa dhahabu na watumwa ulitegemea kuipatia Afrika kiasi kikubwa cha bidhaa za chuma, shaba nyeupe na kupri (shaba nyekundu); nguo za bei nafuu, fedha, vyakula na chumvi. Bidhaa hizi zilikuwa hazizalishwi Ureno, lakini ilikuwa lazima zinunuliwe kutoka kwa wafanyabiashara wa kigeni au huko Bruges, na baadaye kutoka kwenye vituo vikubwa vya biashara vya Ulaya vya wakati huo. Zaidi ya hayo, kuongezwa kwa idadi ya meli kulitegemea uingizaji wa mbao, hasa kutoka nchi za Baltiki. Ureno haikuweza kuendeleza uzalishaji wake kwa sababu ya uwezo wake hafifu katika idadi ya watu na ushindani mkubwa kutoka ng'ambo, hususan katika bidhaa za viwanda.

Ustawi wa haraka wa uchumi wa Ulaya ulichochea kupanda kwa bei polepole kuanzia miaka ya 1470. Katika nusu ya pili ya karne ya kumi na sita, ongezeko hili lilikuwa kubwa mno hata kuathiri mazao ya kilimo na bidhaa za viwandani. Uhusiano kati ya ongezeko la bei na ongezeko la faida kwa Ureno kutokana na biashara ya nchi za ng'ambo yaelekea haukuinufaisha Ureno. Matumizi makubwa yanayohusiana na upanukaji nchi za ng'ambo yalikuwa na faida tu pale ilipowezekana kununua kwa bei

nafuu na kuuza kwa bei ghali. Hata hivyo, kufanya hivyo kulikuwa na maana ya kuwabana au hata kuwaondoa kabisa washindani wa Ulaya, na hivyo kulihitaji jeshi imara la meli za kivita. Hiyo ilikuwa shughuli ya gharama kubwa. Kufikia miaka ya 1470, Ureno tayari ilikuwa imekwishaingia vitani na Kastile, nchi ambayo iliondolewa kutoka Afrika Magharibi kutokana na nguvu za meli za kivita za Kireno na ujanja wa kidiplomasia. Kugunduliwa na kutamalakiwa kwa Amerika kulifanya Kastile igeukie huko badala ya Afrika, jambo ambalo halikufanywa na nchi nyingine za Ulaya ambazo zilikuwa na uchumi imara kuliko Ureno, na hivyo kuwa tishio zaidi.

Watawala wa Ureno, Yohana II na Manuel, walilazimishwa kutafuta fedha kutoka kwa matajiri wakubwa wa Italia na Ujerumani kwa ajili ya harakati zao za kikoloni. Akaunti za Mfalme wa Ureno huko Bruges na baadaye Antwerp, zilionyesha kwamba Mfalme alikuwa akitegemea mno makampuni makubwa kama yale ya *Frescobaldi*, *Affaitati* na *Fuggers*. Katika hatua ya kwanza ya upanuzi, watawala wa Kireno waliweza kuwa na ukiritimba katika uingizaji wa dhahabu kutoka Afrika, na kwa kiasi kikubwa, biashara ya watumwa - au walau zile faida zake zisizo bayana.

Katikati ya miaka ya 1520, Wareno walikabiliana na matatizo yao ya mwanzo katika kupata dhahabu hata katika eneo la El Mina. Yaelekea kwamba wakati huo tayari walikuwa hawawezi kutoa bidhaa za kutosha kwa ajili ya mabadilishano na walikuwa wakikabiliwa na ushindani kutoka kwa washindani wao wa huko Ulaya ambao walikuwa katika nafasi nzuri kwa sababu haikuwa lazima kwao kuagiza kutoka nje bidhaa walizowauzia Waafrika. Zaidi ya hayo, Ufaransa, Uingereza na Uholanzi zilikuwa bado hazijajitwisha mzigo mkubwa wa utawala mkubwa na mpana sana wa kudhibiti biashara ya nchi za ng'ambo. Wafanyabiashara wao walikuwa na fedha za kununulia kiasi kikubwa zaidi cha bidhaa na kuuza kwa bei nafuu.

## Biashara ya watumwa

Ureno mwanzoni ilivutiwa na Afrika kwa sababu ya dhahabu yake, ambayo awali ilikuwa ikipelekwa kwenye nchi za Kiislamu. Hata hivyo, muda si mrefu waligundua zao la pili la Kiafrika lililopendelewa na Wazungu, yaani watumwa. Watumwa walipelekwa nchi za Kiarabu kwa miaka mingi kutoka sehemu kubwa ya bara, hususani Sudan. Katika karne ya kumi na tano na ya kumi na sita, Wareno walinufaika kutokana na desturi hii, na walikuwa wakiwanunua watumwa kutoka Afrika Magharibi, hususani Senegambia, ambayo ilikuwa mshirika wa kiuchumi wa siku nyingi wa Maghrib. Walitumia kwa ufanisi mbinu za biashara zilizokuwa zikitumika Senegambia, na kwa kutambua kuwa ushirikiano wao na watawala na wafanyabiashara wenyeji ulikuwa muhimu kwa ajili ya ufanisi, walifaulu kuwaingiza katika biashara ya watumwa.

Baada ya muda mfupi Wareno waliviacha vipingamizi vyovyote vile vya kimaadili dhidi ya biashara ya watumwa wakiamini, kama walivyofanya wazungu wengi, kwamba iliwasaidia watu weusi kupata wokovu ambapo kama wangebakia katika nchi zao, wakiwa sio Wakristo, wangelaaniwa. Hata hivyo, yafaa iongezwe kwamba watumwa weusi walionekana Ulaya wakati ambapo biashara ya watumwa weupe kutoka Black Sea ilikuwa inakaribia kufikia mwisho wake, na kwamba kutoka wakati huo istilahi za

"mtumwa" na "Mnegro" zilitumika kwa maana inayolingana.

Katika karne ya kumi na tano yote na mwanzoni mwa karne ya kumi na sita, soko kuu la "bidhaa nyeusi" lilikuwa Ulaya, hususan Hispania na nchi zilizokuwa zikitawaliwa na Hispania; na kwa kiasi fulani visiwa katika Bahari ya Atlantiki kama vile Madeira, Kanari, visiwa vya Rasi Verde (Cape Verde) na kisiwa cha St. Thomas. Kichocheo kikubwa cha biashara ya watumwa katika visiwa hivi kilikuwa ni kuanzishwa kwa kilimo cha miwa na pamba. Utumwa usingeweza kukua sana Ulaya kwa vile hakukuwa na sababu za kiuchumi za kukua kwake. Kulingana na maelezo ya Curtin, idadi ya watumwa waliochukuliwa kutoka Afrika na Wazungu kati ya mwaka 1451 na mwaka 1600 ilifikia karibu 274,900. Miongoni mwa hawa, Ulaya na visiwa katika Bahari ya Atlantiki vilichukua karibu watumwa 149,000, Amerika ya Kihispania kiasi cha 75,000 na Brazil kiasi cha 50,000 hivi. Tarakimu hizi ndizo zinazoelezea hali halisi ya kipindi cha awali cha biashara ya watumwa ya kuvuka Bahari ya Atlantiki kabla ya kuendelezwa sana kwa mfumo wa mashamba makubwa kwenye Dunia Mpya uliochochea haja kubwa ya nguvu kazi ya watu weusi.

Waafrika wa kwanza Amerika walipelekwa huko na watiishaji wa Kihispania (*conquistadores*) ambao ndio waliowamiliki. Wengi wao walitoka Senegambia na ama walipelekwa Ulaya kwanza au walizaliwa huko. Waliitwa *ladinos* (Walatino) huko Amerika kwa sababu walijua Kihispania na Kireno na kwa kiasi walikuwa wameathiriwa na ustaarabu wa nchi za Iberia. Walithaminiwa sana, tofauti na *bozales* ambao waliletwa moja kwa moja kutoka Afrika na hivyo kuwa na utamaduni tofauti kabisa.

Katika karne ya kumi na tano Wareno walizidi kuvutiwa na biashara ya watumwa na katika karne iliyofuata, walianza kutafuta nchi ambazo zingewaletea watumwa wengi. Huu ndio ulikuwa msingi wa Wareno kujipenyeza Kongo mwanzoni mwa karne ya kumi na sita na baadaye kutamalaki kwao Angola. Walowezi kwenye kisiwa cha St. Thomas nao walikuwa wakiwatafuta watumwa, si kwa ajili ya mashamba yao tu bali pia kwa ajili ya kuwauza kwenye makoloni ya Kihispania huko Amerika, na vilevile huko Brazil ya Wareno kuanzia mwishoni mwa karne ya kumi na sita. Idadi ya watu weusi wa Brazil wakati huo ilikuwa elfu chache tu, lakini katika karne iliyofuata idadi hii iliongezeka hadi kufikia 400,000-450,000kufuatia kuanzishwa kwa mashamba ya miwa.

Kutamalakiwa kwa Amerika kuliuibulia matatizo Ufalme wa Kastile ambao ulikuwa unawapa wakoloni watumwa. Hata hivyo, hazina ya kifalme ilipata chanzo cha fedha nyingi kwenye mfumo wa leseni zilizokuwa zikitolewa kwa wafanyabiashara waliokuwa wakiingiza watumwa kwa ajili ya walowezi, hasa kadri bei ya leseni ilivyopanda kulingana na kukua kwa mahitaji ya watumwa. Miongoni mwa waliokuwa wa kwanza kupata leseni ni makabaila waliokuwa na uhusiano wa karibu na mfalme, na pia mabepari wakubwa, pengine kwa sababu ya mapendekezo yao ya kulowea na kuchimba madini huko Venezuela. Kama inavyotarajiwa, wale waliokuwa wakifikiria kufanya biashara ya watumwa walitaka kuondoa zile ofisi ghali za Wareno. Kwa hilo, ilikuwa lazima kwao kuvuka vikwazo vilivyowekwa na Wareno huko Afrika, wakati huko Amerika walilazimika kufanya magendo kwa kuwa Ufalme wa Kastile uliwaruhusu tu

wale ambao uliwapa leseni ya kuagiza watumwa. Lakini wakoloni wa Kihispania huko Amerika daima walihitaji wafanyakazi, hivyo walikuwa tayari kushirikiana na wafanya magendo ambao walishusha shehena zao katika bandari haramu.

Hivyo, hali zote zilielekea kupendelea uingizwaji zaidi wa Waafrika huko Amerika, ingawa biashara ya watumwa, kwa hakika, ilikua tu kutokana na kuanzishwa kwa mashamba makubwa ya miwa. Ilijitokeza kwa haraka sana kwamba katika Amerika ya Wahispania na baadaye huko Brazil, Wahindi "Wekundu" hawakuweza kuhimili kazi ngumu mfululizo kwenye mashamba, wakati ambapo Waafrika walikuwa na sifa zote zilizohitajika.

Kwa hiyo tangu mwanzoni mwa miaka ya 1500, lakini hasa hasa tangu mwaka 1550, Afrika ilikuwa na dhima kubwa, japo isiyostahiki, ya kupeleka nguvukazi na kiasi fulani cha dhahabu kwenye uchumi wa dunia uliokuwa umeshamiri.

Lakini nafasi ya Wareno ilikuwa ikiendelea kufifia. Huko Moroko, walipata mapigo makubwa kwenye vita vya jihadi vya masharifu wa Kisa'adi dhidi ya "makafiri." Mnamo mwaka 1541 walipoteza Agadir, na muda mfupi baadaye matatizo ya kifedha yaliwalazimisha kuziachia karibu bandari zote za Moroko. Mwaka 1560 ulishuhudia kufilisika kwa mara ya kwanza kwa Ufalme wa Ureno. Gharama ya himaya ya kikoloni, wakati ikiingiza faida kubwa kwa baadhi ya makabaila, mabwenyenye na baadhi ya wafanyabiashara, iliikomba Hazina ya Mfalme na kuwatwisha wananchi wengi mzigo uliokuwa ukizidi kuwa mzito.

## Kuwasili kwa madola mapya ya Ulaya

Wafaransa tangu miaka ya 1520, na Waingereza tangu miaka ya 1550, walitokea kuwa washindani hatari wa Wareno barani Afrika, na tangu mwishoni mwa karne ya kumi na sita Waholanzi wakawa washindani hatari zaidi. Awali wafanyabiashara binafsi wa Kifaransa au makampuni ya kibiashara ndiyo yaliyojishughulisha. Mfalme wa Ufaransa na mfalme wa Uingereza hawakujihusisha moja kwa moja katika biashara na Afrika. Francis I hata alijaribu bila mafanikio kuwazuia watu wake kusafiri kwenda Afrika ili wasihatarishe mahusiano yake na Ureno wakati Ufaransa ilipokuwa na mgogoro na viongozi wa Kihabsburg wa Hispania. Wafaransa walikuwepo kwa wingi katika eneo la Rasi Verde na Senegal. Wafaransa mara nyingi walipora meli za Wareno baharini zilipokuwa zikirudi kutoka Afrika zikiwa na shehena ya dhahabu au zikitoka India zikiwa na bidhaa za Mashariki. Kufikia robo ya mwisho ya karne ya kumi na sita, Wafaransa walikuwa wamejiimarisha sana katika Senegambia, hususani kwenye vituo kama Goree, Portudal, Joal na Rufiski (Rio Fresco) kwenye nchi ya Wawolof. Wafaransa walileta nguo kutoka Normandy na Brittany, vinywaji vikali, bidhaa za metali na silaha. Biashara ya silaha yaelekea ilifanya mambo yawe mazuri zaidi kwa Ufaransa, wakati mfalme wa Ureno, kwa muda mrefu na kwa ukaidi, alipozuia biashara ya silaha kwenda Afrika, ingawa watawala wa huko walikuwa na hamu nazo. Wafaransa walinunua dhahabu na pembe za ndovu na vilevile pilipili, ngozi na mafuta ya mawese. Biashara ya watumwa ilikuwa haijawavutia bado. Kufikia katikati ya karne ya kumi na sita, Wafaransa walikuwa washindani hatari wa Wareno huko Pepper Coast

na Gold Coast, kwa kuwa walipeleka bidhaa nyingi Afrika kuliko Wareno, na kuwaathiri vibaya, hasa katika eneo la El-Mina. Hatimaye waliwafukuza Wareno kutoka kwenye mlango wa mto Senegal na Gambia, na wao kutimuliwa hapo na Waingereza mwishoni mwa karne ya kumi na sita.

Upanuzi wa Waingereza Afrika katika karne ya kumi na sita ulifanana na ule wa Wafaransa. Walianza kwa kuanzisha mahusiano imara ya kiuchumi na Moroko, baada ya kuondoka kwa Wareno mnamo mwaka 1541. Kati ya mwaka 1550 na mwaka 1565, makampuni ya biashara ya Kiingereza yalituma safari maalum kadhaa ambazo taarifa zake bado zinapatikana. Walizipeleleza pwani za Afrika Magharibi hadi kwenye ghuba ya Benin,waliponunua dhahabu, ngozi na watumwa wachache. Maelezo ya Wareno yanaonyesha kwamba kufikia mwishoni mwa karne ya kumi na sita Waingereza walikuwa na mawasiliano na watu wa Gold Coast, lakini hawakupendelea sana biashara ya watumwa. Kufikia mwishoni mwa karne nafasi yao ilikuwa imeimarika sana pembezoni mwa Senegambia walipopatumia kuwatimua Wareno na Wafaransa. Mnamo mwaka 1588 kampuni ya kwanza ya Kiingereza kwa ajili ya kufanya biashara na Guinea ilianzishwa hasa na mabepari kutoka London na Exeter. Hakuna ushahidi kwamba kampuni hii ilifikia popote. Pengine, mnamo mwishoni mwa karne ya kumi na sita, Waingereza waligundua kwamba kupora meli za Wakastile kwenye Bahari ya Atlantiki kulikuwa na faida kubwa kuliko kufanya biashara na Afrika.

Wakati huo huo ndipo Waholanzi walipojitokeza kwa mara ya kwanza kwenye mwambao wa bara la Afrika. Walikuwa vitani na Wahispania na waliichukulia Ureno, ambayo ilikuwa ikitawaliwa na Filipo II, kama adui. Mtaji mkubwa uliokuwa umelimbikizwa na wafanyabiashara wake na nguvu ya meli zao za kivita viliwawezesha kufanya upanuzi huko India na Afrika. Kati ya mwaka 1593 na 1607, meli 200 hivi zilifunga safari kwenda Afrika kutoka Uholanzi. Mnamo mwaka 1594 na mwaka 1595, Waholanzi waliingia Goree, na miaka michache baadaye walifika Benin ambapo walinunua bidhaa za pamba na kauri ambavyo walivibadilisha na dhahabu na fedha huko Gold Coast. Mnamo mwaka 1611 walijenga Ngome ya Massau (Mouri) huko Gold Coast, ambayo ilikuwa kituo chao cha kwanza cha biashara kwenye pwani ya Afrika Magharibi. Vilevile walianzisha biashara na eneo la Akkra. Walisafirisha nje vyombo vya kupri na bati, nguo za bei nafuu, vileo, silaha, mapambo ya aina mbalimbali, vitu vya matumizi ya kila siku na hata mvinyo iliyokuwa maarufu kwa namna tofauti. Pia waliagiza sukari kutoka kisiwa cha St. Thomas na kusafirisha bidhaa isiyosafishwa hadi kwenye viwanda vyao vya kusafishia huko Amsterdam.

Kufikia mwaka 1617, Waholanzi walikuwa wamejiimarisha huko Senegambia kiasi cha kutamalaki Goree na waliwaondoa si tu Wareno bali pia Waingereza na Wafaransa huko Joal, Portudal na Rufiski. Walidumisha nguvu zao hizi kwa zaidi ya miaka hamsini. Wakati huo huo meli zao zilitembelea miambao ya Kongo na Angola. Waholanzi, kama Waingereza na Wafaransa, mwanzoni hawakuvutiwa na biashara ya watumwa. Lakini mambo yalibadilika mwanzoni mwa karne ya kumi na sita wakati Waholanzi walipoanza kuwanunua watumwa huko El Mina, Akkra, Arda na Benin na pia huko Kalabari, Gabon na Kameruni. Hawa watumwa waliuzwa, kwa kubadilishwa

na sukari, kwa wenye mashamba kwenye kisiwa cha St. Thomas, au kusafirishwa hadi Brazil. Kutekwa kwa Angola mwaka 1641 kulihusiana sana na mahitaji ya nguvukazi ya Brazil. Japokuwa Waholanzi walipoteza eneo la kaskazini mashariki mwa Brazil na kufukuzwa Angola mnamo mwaka 1648, uhusiano wa karibu wa nchi hizo mbili uliotegemezwa kwenye biashara ya watumwa uliendelea hadi karne ya kumi na tisa.


Katika kipindi hiki chote, Afrika Mashariki haikuwavutia sana Wazungu. Wareno, ambao walishikilia Sofala na kudhibiti kisiasa miji mingine ya pwani, hawakuingia ndani ya nchi. Kiasi cha dhahabu kilichokuwa kikifika pwani kutokea bara kilikuwa kimekwisha anza kupungua katikati ya karne ya kumi na sita. Kupungua kwa kiasi cha dhahabu ndiko kulikochangia katika kufifia kwa miji kama Kilwa, Mombasa na Malindi, ambayo kabla ya kufika kwa Wareno, ilikuwa ikitoa dhahabu na bidhaa nyingine kwa wafanyabiashara kutoka India na Arabia. Wakazi wa maeneo ya pwani walijaribu bila mafanikio kuwashawishi Waturuki kutoka Musoma wa Arabuni kuwasaidia dhidi ya Wareno. Upanuzi wa nchi uliofanywa na Uimamu wa Omani katika mwambao wa Afrika Mashariki na kwenye visiwa mwishoni mwa karne ya kumi na saba ulileta mabadiliko kisiasa, yaliyowabakiza Wareno huko Msumbiji tu, lakini ni mnamo mwishoni mwa karne ya kumi na nane na karne ya kumi na tisa ndipo mabadiliko dhahiri yalipotokea.

Kwenye ncha ya kusini ya Afrika, dalili za mwanzo za upanuzi wa Wazungu zilionekana mnamo karne ya kumi na saba, wakati kampuni ya Kidachi ya India Mashariki ilipohimiza kuwepo kwa makazi ya wakulima wadogo wa Kiholanzi (na wa Kidachi), ambao baadaye walijulikana kama Makaburu. Shinikizo la Makaburu lililowafanya Wasan kuwa watumwa au kuondolewa kwenye nchi yao lilitoa ishara mbaya kwa wenyeji.

## Afrika kama hodhi ya nguvukazi

P.D Curtin anakadiria kwamba kati ya mwaka 1541 na mwaka 1600, watu weusi 274,900 walipelekwa Amerika. Katika miaka michache iliyofuata, idadi hii iliongezeka hadi kufikia 1,341,100 na hadi milioni 6 katika karne ya kumi na nane, milioni mbili miongoni mwao wakiwa wameingizwa Brazil. Katika karne ya kumi na nane, idadi ya watu weusi waliopelekwa katika visiwa vya West Indies vya Waingereza na Wafaransa iliongezeka mno na idadi ya waliopelekwa Kuba nayo iliongezeka. Afrika, ambayo mwanzoni ilitazamwa na Wazungu kama chanzo kikuu cha dhahabu, sasa ilibadilika kuwa hodhi ya nguvukazi kwa ajili ya mashamba makubwa ya Wazungu huko Amerika, hususani kwenye mashamba ya miwa yaliyokuwa yakikua kwa kasi. Kuingizwa kwa watu weusi huko kaskazini mashariki mwa Brazil, ambako kulifanyika kwa wingi wakati wa utawala wa Wareno, kuliongezeka zaidi wakati wa utamalaki wa Waholanzi. Hali ilibadilika tu pale Waholanzi walipofukuzwa Brazil na wao kuanza kutumia mbinu zao za kusafisha sukari kwenye visiwa vya Karibiani, ambavyo mashamba yake yalishindana na yale ya Brazil.

Katika makoloni ya Waingereza huko Karibiani, idadi ya watumwa walioingizwa humo iliongezeka kutoka 263,700 katika karne ya kumi na saba hadi 1,401,300 katika



1.2 *Watumwa wa Kinegro wakisafisha almasi huko Brazil*

karne ya kumi na nane. Hali ilikuwa hivyo hivyo katika visiwa vilivyokaliwa na Wafaransa ambako San Domingo pekee iliingiza karibu watumwa 790,000 katika karne ya kumi na nane. Kilimo cha miwa kilianzishwa pia huko Kuba na kupelekea kuwepo kwa mahitaji yanayofanana ya nguvukazi. Surinam ya Waholanzi, na mashamba ya Waingereza na Wafaransa katika Amerika ya Kati na katika sehemu ya kaskazini ya Amerika Kusini pia mliingizwa idadi kubwa ya watumwa weusi. Huko Amerika Kaskazini, mashamba ya tumbaku huko Virginia na mashamba ya mpunga huko Maryland pia yalisaidia kupanua biashara ya watumwa. Mnamo karne ya kumi na tisa kuendelezwa kwa mashamba ya pamba kuliigeuza kusini ya Marekani kuwa eneo kubwa ambalo uchumi wake ulitegemea utumwa.

Mahitaji ya nguvukazi ya watu weusi yaliipa Ulaya ya Magharibi jukumu ambalo ilikuwa haijawahi kuwa nalo, wakati ambapo mabadiliko makubwa ya kiuchumi na kisiasa yalikuwa yakitokea. Katika nusu ya pili ya karne ya kumi na saba, kufifia kwa Hispania na Ureno kulizidi kudhihirika kwa uwazi zaidi. Uholanzi wakati huo ikiwa kwenye kilele cha nguvu zake, ilianza kutimuliwa na Ufaransa na Uingereza, ambazo uchumi wake ulikuwa unakua kwa kasi. Kuanzia mwishoni mwa karne ya kumi na saba nchi hizi mbili zilikuwa zikiiathiri sana Afrika, wakati ambapo Wahispania na Waholanzi walikuwa na dhima ndogo tu. Ama kuhusu Wareno, ushindi wao huko Angola uliwaruhusu kuendelea kushikilia nafasi nzuri katika biashara ya watumwa.

Katika karne ya kumi na saba, Uholanzi, Uingereza na baadaye Ufaransa na nchi nyingine ziliunda makampuni ya kufanya biashara na Afrika na kusafirisha watumwa kwenda Amerika. Makampuni haya yalipata, kutoka kwa serikali zao, haki za ukiritimba kwenye biashara na Afrika, ambazo ziliwawezesha kudhibiti bei. Kwa upande wao, walilazimika kutunza ngome kongwe na kujenga nyingine mpya ili kulinda vituo vya biashara vya Wazungu katika pwani ya Afrika. Idadi ya ngome za Wazungu iliongezeka katika karne zote za kumi na saba na kumi na nane, hususan katika Gold Coast na sehemu jirani.

Wakati huohuo, watu weupe katika Afrika walikuwa na mikwaruzano miongoni mwao. Wafanyabiashara na makampuni ya biashara yalitaka kujipatia udhibiti wa vituo vya biashara vilivyokuwa kwenye sehemu nzuri katika pwani ya Afrika. Kila moja ya makundi tofauti ya Wazungu yaliyokuwa yakishindana liliungwa mkono na serikali yake. Madola yenye nguvu yasingeacha kuvutiwa kuingia Afrika kwani eneo hili lilikuwa na madau makubwa. Hata madola ambayo hayakuwa na nguvu sana kama Sweden, Denmark na Prussia yalijaribu kujiingiza katika mambo ya Afrika.

Hata hivyo, makampuni ya biashara hayakufaulu kama yalivyotarajiwa. Makampuni mawili ya kwanza ya Waingereza hayakujishughulisha vilivyo. Kampuni la Kifalme la Afrika, lililoanzishwa mnamo mwaka 1672, lilidhibiti sehemu kubwa ya biashara ya Afrika ya nje iliyopitia pwani ya Afrika Magharibi katika robo ya mwisho ya karne ya kumi na saba, lakini sera yake ilipingwa na wakulima wa Amerika na wafanyabiashara wengi wa Kiingereza. Baada ya mwaka 1689, fadhila lilizokuwa likizipata zilipunguzwa polepole na hatimaye kupoteza ukiritimba wake.

Enzi ya biashara huru na Afrika ilikuwa imekwishaanza miaka michache mapema

huko Uingereza. Wafanyabiashara wa Liverpool ndio walikuwa na nguvu zaidi. Mafanikio yao makubwa katika karne ya kumi na nane yaliwezekana kutokana na maendeleo ya haraka ya viwanda vya maeneo ya kati ya Uingereza (Midlands), hususani viwanda vya metali vya Birmingham na vile vya nguo vya huko Manchester vilivyowawezesha kupeleka Afrika bidhaa za bei nafuu kama vile visu, silaha na bidhaa nyingine za metali na pia nguo. Wafanyabiashara wa Kiingereza walibadilishana bidhaa hizi kwenye pwani ya Afrika kwa watumwa ambao waliwapeleka Amerika kuwauzia wenye mashamba kwenye makoloni.

Katika karne ya kumi na nane, Uingereza ilikuwa nchi iliyoongoza katika biashara kwenye pwani ya Afrika. Athari zake zilidhihirika kutoka Senegal hadi kwenye mipaka ya Kameruni. Ingawa Uingereza ilibidi itoe kwa Wafaransa ngome zake huko Senegal mnamo mwaka 1799, nafasi yake huko Gambia na Sierra Leone ilizidi kuimarika. Pia ilishika nafasi ya kwanza katika biashara ya watumwa ya Gold Coast ambayo ilikuwa ikikua tangu karne ya kumi na saba. Lakini Waingereza hawakuwa wazungu pekee waliohusika hapa. Uholanzi na Ufaransa nazo zilizidi kujishughulisha kwenye Slave Coast, huko Senegal, katika eneo la Kameruni na huko Lwango.

Majaribio ya kulowea yalianza huko Angola, ambako Wazungu wachache walianza kuweka makazi. Hata hivyo, kwenye pwani ya kutoka Rasi Verde hadi Kongo, Wazungu walijihusisha tu na biashara. Vituo vya biashara na viwanda vilivyoanzishwa na Wazungu (kama vile Saint Louis mnamo mwaka 1626) vilisambaa kote pwani, karibu na ghuba zilizokuwa nzuri na, kwa kawaida, karibu na miji ya Kiafrika. El Mina, Akkra, Whydah, Porto Novo, Badagri na Kalabari Kongwe na Mpya – yote ikiwa maarufu katika karne ya kumi na nane – ilikuwa sehemu za kukutania ambako watu weusi waliwaletea Wazungu watumwa ili kupata bidhaa za Kizungu. Kwa jumla, watawala wa Kiafrika walijiwekea aula katika kufanya biashara na Wazungu, lakini wafanyabiashara weusi nao walikuwa na dhima muhimu. Hata huko Angola Wareno waliteka watumwa wachache tu wenyewe, na kuwaachia mawakala wenyeji kazi ya kununua au kuteka watumwa huko bara.

Ni vigumu kujua kiasi cha eneo la biashara ya watumwa Afrika. Lakini si maeneo ya pwani tu yaliyohusika. Mapema mnamo karne ya kumi na sita kulikuwa na taarifa za safari ndefu ambazo watumwa ilibidi wazifanye kutoka makwao hadi kwenye bandari ambako wangesafirishwa kwenda ng'ambo. Katika karne ya kumi na nane, wakati usafirishaji wa Waafrika ulipoongezeka, wenye biashara walikuwa ni watawala wa nchi zenye nguvu, kama vile Asante au Dahomey, au wafanya biashara wa Kalabari. Madola kongwe ya Afrika kama vile Benin au Oyo, hayakuhusika sana. Kongo ambayo ilisambaratika kabisa katika karne ya kumi na nane, haikuwa mtoaji muhimu wa watumwa.

Wazungu walikuwa hawajawa tayari kuanza kutamalaki Afrika, hasa kwa sababu hali ya hewa ilikuwa ngumu kwao na walidhurika sana na magonjwa ya ukanda wa joto. Wazungu wa awali, Wabrazil na Waamerika Kaskazini, waliojitokeza mwanzoni barani Afrika, walipendelea kufanya urafiki na watawala wa Kiafrika kwa kuwapa kwa wingi bidhaa zozote walizozitaka. Maslahi yaliyofanana yaliwaunganisha wale waliokuwa

wakifanya biashara ya watumwa, yaani watawala wa Kiafrika, waadhamu na wafanyabiashara. Yafaa itajwe kwamba harakati za kukomesha utumwa, zilizoanza katika nusu ya pili ya karne ya kumi na nane, zilipingwa vikali huko Uingereza, si tu na wenye mashamba wa West Indies, bali pia na mabepari wa Uingereza kwenyewe. Baadaye ilidhihirika kwamba Wafalme wa Asante na Dahomey nao walipinga vikali ukomeshaji wa biashara ya watumwa.

Ilikuwa ni katika karne ya kumi na nane tu ndipo Wazungu wafanyabiashara ya watumwa walipojitokeza katika pwani ya mashariki ya Afrika. Umbali mkubwa kutoka hapo hadi kwenye masoko ya Amerika ulifanya usafirishaji wa Waafrika kwenda kwenye makoloni katika Dunia Mpya kuwa mgumu zaidi ingawa wenye kuwezekana. Kwa mujibu wa P.D Curtin, idadi ya watumwa walioingizwa Amerika kutoka Afrika ya kati na ya kusini mashariki kati ya mwaka 1711 na mwaka 1810 ilikuwa 810,100 hivi au asilimia 24 ya jumla ya watumwa waliosafirishwa. Katika Afrika Mashariki watumwa waliopelekwa Bara Arabuni na watu wa Imam wa Oman waliongezeka katika karne ya kumi na nane. Lakini ni katika karne ya kumi na tisa ndipo maeneo haya yalipoanza kuingiliwa na Waarabu wafanya biashara ya watumwa.

Huko Afrika Kaskazini, safari kwenda kwenye Mto Niger ya Chini mnamo mwaka 1591, yaelekea haikuwa na athari ya kudumu kwa Moroko. Watamalaki haraka haraka walijipatia uhuru wao kutoka nchi zao za asili, na warithi wao, Waarma, waliunda madola madogo yaliyodumu kwa muda mfupi. Hakuna ushahidi wa kutokea kwa mabadiliko muhimu katika biashara kati ya Moroko na pindi la Niger. Biashara ya watumwa yaelekea ilikuwa kubwa kwani, mwishoni mwa karne ya kumi na saba, masultani wa Moroko walikuwa na jeshi la watumwa ambalo, kwa kipindi fulani, lilikuwa pia na athari kubwa kwenye siasa za nchi.

## *Hitimisho*

Yafuatayo yanaweza kutajwa kuhusu mawasiliano ya Afrika na nchi za nje kuanzia karne ya kumi na sita hadi ya kumi na nane:

(1) Sehemu kubwa ya mawasiliano hayo ilitokea kwenye pwani na bara ya magharibi ya Afrika.

(2) Mwanzoni, Wazungu walivutiwa na dhahabu ya Afrika, lakini tangu nusu ya pili ya karne ya kumi na sita, biashara ya watumwa ikapata umuhimu mkubwa. Ilisaidia kuhakikisha maendeleo ya kiuchumi ya sehemu kubwa ya Amerika na Karibiani, na vilevile kasi ya malimbikizo ya mtaji huko Ulaya (hasa Uingereza) na Afrika.

(3) Papo hapo upanuzi wa Wazungu Afrika ulikuwa wa ukoloni mkongwe lakini uliokitwa zaidi kwenye biashara. Mabadilishano kati ya wahusika hayakuwa sawa, kwa kuwa watu weupe walikuwa wakiuza bidhaa za bei nafuu kwa idadi kubwa ya watumwa. Hivyo, ingawa hawakujaribu wakati huo kutamalaki bara, walivuruga mno demografia ya bara hili.

(4) Dhima ya Afrika kama soko kwa bidhaa nyingi za viwanda vya Ulaya katika

karne ya kumi na sita na ya kumi na saba, pengine ni kubwa kuliko ilivyofikiriwa.

(5) Faida ilizopata Afrika kutokana na mawasiliano haya ilikuwa tu kuingizwa kwa kilimo cha mahindi na mihogo. Hii kwa kweli haifidii upotevu mkubwa wa watu, achilia mbali mateso waliyoyapata watu waliokamatwa kwa nguvu kutoka nchi zao na kupelekwa nchi za mbali kufanya kazi ngumu kwenye mashamba.

# 2 Miundo ya Kiafrika ya kisiasa, kiuchumi na kijamii katika kipindi hiki

Kutokana zaidi na vipengele vya ndani kama vile demografia na ekolojia, au kwa sababu ya dhurba ya kani za nje kama vile biashara ya watumwa, Ukristo, Uislamu na ubepari, miundo ya Kiafrika ya kijamii, kiuchumi na kisiasa iliendelea kubadilishwa kati ya mwaka 1500 na 1800.

## *Miundo mipya ya kijamii*

### Uislamu na Ukristo

Katika mambo ya dini, falsafa na dini za Ulaya na Mashariki ya Kati zilianza kutia athari zake Ukristo na Uislamu ulipoanza kuwa na nguvu za kisiasa kwenye maeneo ambako dini hizo hazikujulikana hapo kabla.

Hatua yoyote iliyofikiwa na Ukristo katika maeneo ya pwani ya Afrika Mashariki ilipotezwa kutokana na kuuawa kwa Padri Gonçalo da Silveira, kasisi wa Kireno ambaye alikuwa akijaribu kumuingiza Mwene Mutapa katika Ukristo mnamo mwaka 1560. Uislamu, kwa upande mwingine, ulipiga hatua kutokana na utamalaki wa Ahmad Grañ (1531-35) huko Ethiopia, na utamalaki wa Mai wa Borno na *maaskiya* wa Songhai huko Sahara na Sudan Magharibi.

### Mpito kutoka jamii zenye mateka hadi jamii zenye watumwa

Badiliko la pili muhimu lilikuwa ni la nafasi ya mfumo wa *jonya* wa Waafrika weusi katika sehemu kubwa ya Afrika kuchukuliwa na mfumo wa Kizungu na wa Kimashariki ya Kati wa kumiliki watumwa.

*Jonya* (kutoka neno la Kimande *jon* lenye maana ya "mateka") ilienea zaidi huko Sudan Magharibi na katika eneo la Niger na Chad. *Jon* (au mateka) hakuweza kuhamishiwa kwa bwana mwingine, alimiliki sehemu kubwa ya kile alichokizalisha, alikuwa sehemu ya nasaba, na alikuwa katika kundi la kijamii-kisiasa lililokuwa sehemu ya tabaka tawala. Jonya alikuwa na dhima kubwa katika madola na himaya za Ghana, Takrur, Mali, Kanem-Borno, Asante, Yoruba na Mutapa. Kundi la waali miongoni mwa watumwa wa kifalme lilikuwa sehemu ya tabaka tawala; walikuwa na kiasi fulani cha mamlaka, walitajirika na waliweza pia kumiliki watumwa.

Utumwa wa Mashariki na Magharibi, kwa upande mwingine, katika muundo wake wa kale na pia wa kikoloni, uliwafanya watumwa wawe viumbe wasiokuwa na haki kabisa na ambao wangeweza kununuliwa au kuuzwa kama mali ya kuhamishika.

Kutokana na kuanzishwa kwa madola ya Kiislamu, ambayo yalichukua Sudan Magharibi yote mnamo karne ya kumi na nane, sharia na desturi za Kiislamu zilianzishwa katika eneo hilo, na mfumo wa kuwamiliki watumwa ulichukua nafasi ya mfumo wa jonya. Hata hivyo, mfumo wa jonya uliendelea kudumu miongoni mwa watawala wa kijadi wa Sudan Magharibi na eneo la Niger na Chad ambazo ysliathiriwa kidogo tu na Uislamu. Hadi wakati wa utamalaki wa kikoloni, mfumo wa jonya uliendelea kuwa na athari kiasi katika madola ya Wolof, Serer, Uhausa, Kanembu na Uyoruba.

## Kuenea kwa miundo ya kikabaila

Badiliko la tatu lilikuwa ni kuenea kwa miundo ya kikabaila katika ama umbo lake halisi au potofu miongoni mwa wenye staarabu za kilimo wa Afrika.

Ukabaila kama muundo wa kisiasa, mtindo wa uzalishaji au mfumo wa kijamii na kiuchumi ulihusu sio tu mfungamano wa kiapo na kiutawala bali pia fursa ya kubahatisha na kupata faida kutokana na njia za uzalishaji. Milki ya ardhi ilikuwa sifa muhimu ya mifumo ya kikabaila ya Ulaya na Mashariki ambayo ilipata mashiko katika staarabu za kilimo za Afrika. Athari zake zilionekana popote pale ambapo umilikaji wa ardhi au udhibiti juu ya nchi ulipelekea katika kutozwa kwa ushuru, kodi na kodi za pango.

Lakini kabla ya majilio ya sharia za Kiislamu au ya mfumo wa *mailo* (mfumo wa ardhi) uliotiwa msukumo na nchi za Magharibi, ardhi haikuwa chanzo cha mapato katika Afrika ya watu weusi. Wale waliojitwalia au kugawa kiwanja au eneo la kuwindia, la kuvulia samaki au la kukusanyia chakula, walifanya hivyo kwa kuzingatia haki za utumiaji ambazo hazikuhusu utafutaji wa faida kubwa wala uwezekano wa eneo kuuzwa. Jamii za wakulima kusini mwa Sahara ziliibua mfumo wa *lamana* ambao ni mfumo wa kumiliki ardhi uliozuia ukodishaji wa ardhi, upangishaji wa ardhi ya kilimo, na mgawano wa mazao. Muundo wa uchumi uliokuwa wa pekee kwa Afrika ya watu weusi ulihusu mno uzalishaji mazao kwa ajili ya matumizi. Watu walizalisha walichokihitaji lakini hawakumiliki njia za uzalishaji.

Mwingiliano baina ya miundo tofauti ya kijamii iliibua jamii mchanganyiko zenye makundi yanayotofautiana. Kutoka karne ya kumi na sita hadi karne ya kumi na nane, jamii ya Kiafrika ilikuwa na maeneo madogo yenye ukabaila hafifu uliochanganyika na mfumo wa lamana. Ukabaila ulishamiri pale ambapo uzalishaji ulikuwa ni kwa ajili ya mabadilishano, na mfumo wa lamana ama uliachwa au kurekebishwa.

Huko Misri, mfumo wa Kituruki wa *beylik* ulisaidia kuendeleza mfumo wa kikabaila. Makabaila wa vijijini walilindwa, kama ilivyokuwa katika Enzi za Kati huko Ulaya, na *ojak* (ambazo ni ngome na vituo vya kijeshi vya Kituruki). Watemi wakuu walitawala *`arsh* (ambalo ni eneo la kabila) na ma-*dwar* (makambi ya mahema) kulingana na mfumo msonge. Katika Sahel na huko Sahara ya Mauritania, familia za

kidini na ma- *juad* (yaani watemi wapiganaji) walichukua madaraka na kuingiza utumwani miungano ya jumuiya ndogo kwa kutumia kisingizio cha udugu wa kidini au haki ya kutamalaki.

Waadhamu wakubwa wa Kituruki na wa kienyeji huko Maghrib mara nyingi walikuwa wakipewa mashamba makubwa. Kama ilivyokuwa huko Misri, shughuli za kiuchumi zilikuwa mikononi mwa *beylik* ambazo zilihodhi viwanda na kudhibiti biashara za nafaka, mafuta, chumvi na nguo na vilevile njia za biashara. Vyama vya mafundi stadi na wafanyabiashara navyo vilikuwa chini ya usimamizi wa *beylik.*

Katika sehemu zilizobakia za Afrika Kaskazini na kaskazini mwa Ethiopia, mfumo wa kikabaila ulikua kwa namna tofauti kwa sababu ya hali za kiekolojia ambazo katika baadhi ya maeneo zilifanya umiliki wa ardhi usiwe wa msongamano. Mashamba makubwa ya *beylik* ya huko Maghrib yalienea katika maeneo mapana na yakaibua kushamiri kwa ugawaji wa *azel* (ardhi) iliyokuwa ikilimwa kwa mfumo wa *khammasat* (yaani wa wakulima wapangaji ardhi) kwa malipo ya moja kwa tano ya mazao. Katika kiwango cha ukanda, ruwaza iliendelea kuwa ile ya *milk* (yaani mashamba madogo ya familia) na *'arsh* (yaani mashamba ya jumuiya), lakini ambayo siku zote ilijumuishwa ndani ya muundo mkuu wa kikabaila uliokuwa ukitumiwa kwa ajili ya kupata faida.

Huko Misri na katika sehemu zilizobakia za Afrika Kaskazini, karne kadhaa za utawala wa Wayunani na Warumi zilikuwa zimekwishaweka msingi wa mpito kuelekea kwenye ukabaila, yaani mfumo wa *ikta* wa Mamamluk. Kusini mwa Sahara, mpito kwenda katika ukabaila ulifanyika kutokana na athari kutoka nje.

Kwa mfano, huko kaskazini mwa Ethiopia, kulijitokeza tabaka la waungwana wenye kumiliki ardhi ambao walilima mashamba makubwa, kwa sababu ufalme wa Ethiopia ulibadilisha kanuni za ukoo-kuwili na urithi wa mgawano sawa na hivyo kuunda miongoni mwao "familia" za vizazi vingi. Nguvu za kisiasa polepole ziliingia mikononi mwa wanaomiliki ardhi, na ulimbikazaji huu wa ardhi kama mali na nguvu za kisiasa ulileteleza tofauti kubwa za kitabaka kaskazini mwa Ethiopia.

Utawala huu uliokuwa si wa kikabaila kamili, ulienezwa na Waethiopia Wakristo wa kaskazini hadi katika maeneo ya kusini ambapo *ketema* (miji yenye ngome) ilianzishwa, na *neftenia* (tabaka la wenye ardhi), lilizifanya *gasha* (ardhi zilizokaliwa) kuwa makazi yake. Wakulima wadogo au *gabar* waliokuwa wakilima kwa faida ya tabaka la wenye ardhi, walikuwa kama watwana au walau wapangaji waliolazimika kulipa *gabir* au *siso* kutegemea kama walikuwa na mkataba wa kugawana mazao au wa kukodi ardhi.

Katika eneo la Maziwa Makuu, hasa sehemu za kusini zilizopo kaskazini magharibi mwa nchi za sasa za Tanzania, Burundi, Rwanda, na Uvira kaskazini mashariki mwa Kongo, asasi za uteja ziliunda mapatano yasiyokuwa ya kikabaila kamili ambayo yaliongoza mahusiano baina ya mfugaji na mkulima. Mapatano haya yalikuwa kama mkataba baina ya wahisani (yaani mfugaji) waliotoa ng'ombe na mpokeaji (yaani mkulima) aliyetoa huduma zake na zile za familia yake na vizazi vyake kwa mhisani na warithi wake. Mikataba hii ilitofautiana toka jamii hadi jamii na ilibadilika baada ya miaka fulani.

Sababu kubwa zilizochangia katika kuchukuliwa kwa mfumo wa kikabaila wa kijamii na kiuchumi wa Waturuki, zilikua ni kuenea kwa tawala za Kiislamu kutokana na majilio ya ma-*askiya* huko Sudan Magharibi, upanuzi wa himaya ya *mai* wa Borno ambayo ilikuwa imesilimishwa, na kuingizwa kwa sharia ya Kiislamu kutokana na usilimishaji na jihadi. Huko Songhai, ma-*askiya* walidumisha sehemu ya muundo wa kijamii na kiuchumi wa jadi.

Katika sehemu zilizotawaliwa na Waislamu, sharia ya Kiislamu ya jihadi ilitumika na hivyo kusimika kwa uthabiti zaidi miundo ya kijamii na ya kiuchumi ya nusu-ukabaila. Mifumo ya *almamia* ya Futa Toro, Futa Jallon na ya ukhalifa wa Sokoto ilinakiliwa tu kutoka kwa mfumo wa Waturuki wa kumiliki ardhi na kutoza kodi.

Mfumo mpya wa sharia ulioanzishwa chini ya watawala wa Kiislamu, ulileta mtindo wa kikabaila wa kupangisha ardhi ili kupata faida. Miundo kama ya *njoldi* (malipo ya kiishara kwa mwenye ardhi), *kawngal* (maeneo ya uvuvi), *yial* (maeneo ya uwindaji), *hare kosam* (machungani) na *gobbi* (migodi), ilibadilishwa kuwa ushuru wa mwaka uliolipwa kwa wale wenye mamlaka, na kukusanywa chini ya usimamizi wa dola. Wadhifa wa mkusanya kodi uliweza kupatikana kwa kutoa ada, kama ilivyokuwa kwa nyadhifa nyingi rasmi katika mfumo huo. Mgawano wa mazao, kilimo kwa kupanga ardhi na ukodishaji ardhi vikawa ndiyo kawaida. Katika maeneo yaliyosilimishwa, wakulima wadogo wengi waliopoteza ardhi kutokana na kutiishwa au kwa sababu ya mfumo mpya wa sheria, walifanywa watwana na vibaraka chini ya mfumo wa Waturuki.

Hivyo, kuanzia karne ya kumi na sita na kuendelea, mifumo ya kijamii na ya kiuchumi yenye usuli tofauti ilikuwa inaunganika. Matokeo yalikuwa ni kujitokeza kwa utaratibu mpya wa kijamii ambamo miundo ya kikabaila ililazimishwa juu ya *lamana* za Kiafrika. Huko Sudan ya Magharibi na Nigeria ya Kaskazini, ambazo zilikuwa zikisilimishwa, asasi ya Kiislamu ya utawala wa kiamiri ilichukua nafasi ya *umansaya* au kulazimishwa juu yake. Katika Ghuba ya Guinea na Afrika ya Kati na Mashariki ambako watawala wa Kikristo walijitokeza, athari za ufalme wa kikabaila wa Ukristo zilizidi kuonekana.

## Maendeleo ya usanifu majengo na usanii

Kulikuwa na mafanikio fulani muhimu ya kiusanifu majengo na ya kisanii. Watu waliojenga miji katika Bonde la Nili, Maghrib na Sudan, na huko pwani, na wale waliojenga majumba ya kifalme ya Yoruba, majumba yajulikanayo leo hii kama magofu ya Zimbabwe, majumba ya kifalme na misikiti ya pwani ya Afrika Mashariki na *tata* (ngome) zinazozunguka miji ya Kihausa, walikuwa wakati huohuo ni wasanifu majengo, waashi, warembaji na wapanga miji. Vibanda miviringo au vya kipiramidi vilivyotengenezwa kwa mawe au udongo wa mfinyanzi na nyumba za ghorofa za Jolla zilikuwa za jadi moja ya kiusanifu majengo na Kutubia ya Marrakesh, kaburi la maaskiya huko Gao na lile la makhalifa huko Kairo.

Baada ya karne ya kumi na sita mbinu mpya katika usanifu majengo zilizidi kugunduliwa, labda zaidi huko Sudan ya Magharibi na Nigeria, lakini miji ya Afrika

Kaskazini na bonde la Nili ilififia. Hata hivyo, maaskiya ambao waliendeleza jadi hiyo huko Afrika ya Magharibi, walikuwa wajenzi hodari kama yule mjenzi wa Moroko wa enzi zao, aliyejulikana kama Abu l-Abbas al-Mansur, ambaye kutwaa kwake madaraka kulitokea wakati mmoja na mtindo wa majenzi makubwa nchini. Jadi za usanifu majengo za Sahel na za Nchi za Kiislamu zilizidi kuenea kuelekea kusini. Mtindo wa usanifu majengo wa Kisudani, ambao mifano yake ilikuwa ni ile ya misikiti ya Sankore na Jenne, ulienea tangu karne ya kumi na sita.

Huko Ethiopia, kipindi cha Gondar (t.1632- 1750) kilishuhudia maendeleo ya mitindo mipya ya usanifu majengo iliyohimizwa na mfalme. Huko Gondar na katika miji mingine, familia za kifalme zilijenga makasri makubwa na mazuri, ngome, makanisa na maktaba zenye mapambo ya nakshi ndani. Katika maeneo ya pwani ya Afrika kulikosemwa Kiswahili, kulikuwa na ubunifu mkubwa wa kiusanifu majengo katika kipindi kati ya mwaka 1700 na mwaka 1850 kuhusiana na ruwaza na michoro ya nyumba. Maendeleo haya ya kiusanifu majengo yaliandamana na tija kubwa katika nyanja zenye kuhusiana kama vile uchongaji na utengenezaji samani.

## *Miundo mipya ya kiuchumi*

Miundo mikubwa ya kiuchumi ilikua katika kipindi hiki: mfumo wa tabaka-amali, ambao ulichukua nafasi ya mfumo wa vyama vya kifani au mashirika; uchumi wa kiporaji, hasa huko Afrika Kaskazini na Mashariki, na uchumi wa vituo vya biashara au vya kibohari, hasa huko Afrika ya Kati na Magharibi.

### Uchumi wa ufundistadi na jamii ya matabaka-amali na vyama vya kifani

Ustaarabu wa mijini wa Enzi za Kati ulichangia kuchipuza mgawanyo wa kazi kwa kuendeleza ufundistadi na shughuli za utengenezaji vitu. Lakini katika karne ya kumi na sita maendeleo haya yalianza kupitana; mikondo tofauti ilijitokeza katika miktadha tofauti ya kijamii.

Katika staarabu za Sudan ya Magharibi, eneo la Niger-Chad na Sahara, mathalan, ufundistadi na shughuli za kutengeneza vifaa ziliendelezwa, kwa kiasi kikubwa au kidogo, kwa misingi ya matabaka amali ya kisiri, yaliyotundwa kwa msingi wa kinasaba. Chini ya athari ya staarabu za Takrur na Sahara, mfumo wa matabaka ulielekea kudhihirika zaidi, hasa huko kusini mwa Senegal, katika nchi ya Wamande na Uhausa. Mfumo wa matabaka wa Wamande uliojulikana kama *nyamankala* kwa muda mrefu uliinua hadhi ya wahunzi hadi Watakruri walipokalia eneo hilo baada ya jihadi. Wafua metali waliheshimika sana miongoni mwa Wafon na Wayoruba, lakini hapo pia, athari ya wahamiaji toka Takrur na Sahara ilivuruga utaratibu uliokuwapo. Huko Songhai, maaskiya tayari walikuwa wakiiongoza jamii ambamo mfumo wa matabaka ulikuwa umekwishapata mashiko na kukua.

Mapinduzi ya Torodo mwishoni mwa karne ya kumi na nane yaliushadidisha mfumo wa matabaka-amali huko Takrur kwa kukuza migawanyiko ya kitabaka. Wakulima wadogo wa Sebbe, wavuvi wa Subalbe na hata wafugaji wanoinadi wa Buruure

walishushwa hadhi kila kukicha. Hawa hawakuhusishwa na kundi la *benangatoobe* (lililojumuisha washona viatu, wahunzi na mayeli), na walitengwa mbali na *nangatoobe* (tabaka-amali la juu). Warabiti (*marabouts*) waali wa Torobo baadaye waliwatweza watawala walioshindwa na wakashika nafasi kubwa za uongozi. Katika jamii za Kinegro-Kiberiberi za Sahara, migawanyiko ya kidini, kikabila na kijamia polepole ilijengeka katika misonge ya matabaka-amali.

Kipengele kikubwa katika uendeshaji wa viwanda au ufundistadi wakati huo kilikuwa ni kiwango cha udhibiti wa dola. Katika staarabu za Mediterania, kwa jumla, kulikuwa na ukritimba wa dola katika shughuli kadhaa kama vile ufumaji, uundaji meli, utengenezaji silaha, usafishaji bidhaa na biashara ya nje, lakini madola katika Afrika ya watu weusi, hayakutumia sana udhibiti kama huo hata wakati wa kupanuka kwa viwanda vya silaha.

Kipindi hiki kilidhihirishwa na tofauti ya ujuzi wa mambo mengi wa watu wa vijijini na ubobezi finyu wa wakazi wa mijini. Viwanda vya dola vilikua, vikitenegeza silaha na hata kuunda vyombo vya kusafiria mitoni na baharini huko Sudan ya Magharibi, katika pwani ya Magharibi ya Bahari ya Atlantiki, na vilevile katika nchi za Mediterania na za Bahari ya Hindi.

Wingi wa vita wakati mwingine ulitia msukumo mpya kwenye utengenezaji wa bidhaa za metali. Mnamo karne ya kumi na sita Sonni Ali alizatiti viwanda vya zana za vita vya Songhai kwa kuziwekea karakana malengo ya uzalishaji ya kila mwaka. Misri ilibobea katika ufuaji metali na ikaanza kutengeneza chuma cha pua cha Damasko. Wahunzi wa Kimande wakiwa wamejipanga kitabaka-amali, walipeleka mbinu zao kwenye miji mipya iliyoibuka kutokana na biashara ya kuvuka Bahari ya Atlantiki. Tasnia ya metali za thamani huko Misri na Afrika Kaskazini iliendelea kupata dhahabu kutoka Nubia, Sofala na Sudan Magharibi. Mafundistadi waliofua dhahabu na fedha walichochea biashara katika masoko mijini huko Maghrib, Misri na Sudan Magharibi. Masonara wa Kiberiberi na Kiwolof walisifika kwa dhahabu yao na kwa kazi ya kutia nakshi vito. Waswahili nao walitengeneza vito vizuri na vitu vingine vya fedha na dhahabu. Vyombo vya udongo navyo viliibua viwanda, huku ufinyanzi (kama usukaji vikapu) ukibakia kuwa kazi ya wanawake. Viwanda vya kioo navyo viliendelea kukua huku vikienea katika nchi yote ya Wayoruba, Nupe, Uhausa, Misri na Maghrib. Miongoni mwa Washona kwenye eneo la kusini mwa Zambezi, uchimbaji migodi ulienea sana, na migodi ya dhahabu na shaba nyekundu ilikuwa mhimili wa uchumi wa eneo hilo hadi karne ya kumi na nane.

Utengenezaji wa bidhaa za ngozi ulishamiri zaidi Nigeria ambako ufugaji ulitoa malighafi ya kutosha. Kutoka karne ya kumi na sita hadi ya kumi na nane, usukaji vikapu na ufumaji vilichukua nafasi muhimu miongoni mwa viwanda vya eneo la Niger-Chad. Utengenezaji wa karatasi, ambayo ilichukua nafasi ya mafunjo, ulikua zaidi huko Misri kutokana na athari ya Samarkand. Sudan nayo haikubaki nyuma sana na polepole ikaanza kutengeneza miswada; Kanem ikawa inatengeneza Kurani zilizouzwa katika nchi zote za Kiislamu. Shughuli zilizohusiana na viwanda vya vyakula, zilizoanza kukua katika Enzi za Kati kwenye miji huko kaskazini na katika Sudan Magharibi, pia

zilianzishwa katika miji ya Nigeria. Katika eneo la utengenezaji nguo, kilimo cha pamba na ufumaji wa nguo za pamba ulikwisha imarika katika nyanda za juu za Zimbabwe na kwenye bonde la Zambezi kufikia karne ya kumi na sita. Madola ya miji ya Waswaili nayo yalipata umaarufu kutokana na aina zake za vitambaa. Huko Afrika ya Kati nguo za viramba (rafia) za Kongo zilivuma tangu karne ya kumi na tano hadi ya kumi na tisa.

## Uchumi wa kiporaji

Kabla ya karne ya kumi na sita, biashara ya masafa marefu ilikuwa na dhima kubwa katika uchumi wa Afrika. Biashara hii ilihimiza tija kubwa na ilipelekea kuibuka kwa staarabu za mijini na kuimarika kwa mahusiano kati ya maeneo ya mijini na vijiji. Hata hivyo, kati ya mwaka 1500 na mwaka 1800, uchumi wa kiporaji, uliokuwa matokeo ya upanuzi wa Wahispania na Wareno, uliingia na kuimarika.

Kati ya mwaka 1495 na mwaka 1523, Hispania na Ureno zilieneza mamlaka yake kote Maghrib. Wareno walipokalia Azemmur, mnamo 1513, Waberiberi wa Kiarabu na watawala wa Uturuki (*Sublime Porte*) waliamua kupinga uchokozi wa Wazungu, na maharamia wa baharini, wakisafiri chini ya bendera ya Waturuki, walisaidia kurekebisha uwiano wa mamlaka. Mwaka 1514, mmoja wa ndugu wa Barbarossa, aliyeitwa Abu Yusuf, aliitwaa tena miji ya Jijelli na Algiers, na ndugu yake, Khayr al-Din, aliimarisha utamalaki huo. Tunisia na Algeria ziliingia chini ya utawala wa Kituruki kwa mara nyingine na zikabakia hivyo, walau kwa jina, hadi karne ya kumi na tisa, licha ya mashambulizi ya Charles V wa Hispania. Mnamo mwaka 1551, Sinan Pasha alikalia Tripoli kwa kutumia jina la utawala wa Uturuki na kisha Tunis mnamo mwaka 1574. Katikati ya miaka ya 1500, Moroko iliimarisha uhuru wake baada ya kuteka tena Agadir, Safi na Azemmur kutoka kwa Wareno.

Licha ya mapigano yao na mataifa ya Ulaya, madola ya Afrika Kaskazini yaliendelea kudumisha uhuru wao, lakini maendeleo yao yalikwamishwa mnamo karne ya kumi na sita kutokana na kuporomoka kwa utaratibu wa uchumi wa dunia. Kuanzia wakati huo na kuendelea, bandari za Maghrib na sehemu zilizobakia za Afrika Kaskazini ziliishi zaidi kwa kutegemea uharamia na kwa ushuru na kodi, badala ya kuendesha biashara au kuanzisha viwanda vipya. Bandari za Sale (Moroko), Algiers, Tunis na Tripoli zililindwa na merikebu za mamluki, ambazo mnamo karne ya kumi na saba; zilishamiri mno huko Mediterania. Maharamia wa baharini walieneza vitisho, na katika karne ya kumi na nane yote pia kulikuwa na kuyumba kwingi huko magharibi mwa Mediterania. Makaimu wa watawala wa Kituruki wa Algiers na Tunis daima walikuwa vitani na taifa mojawapo la Ulaya, na hali hii kwa hakika iliumiza ubepari wa kibiashara na tabaka la wafanyabiashara.

Ni kutokana na usuli huu ndio yafaa yatazamwe mashambulizi ya Moroko dhidi ya Songhai huko Sudan Magharibi. Mtawala wa Moroko, Abdu'l'Abbas al-Mansur, alijaribu, baada ya kutamalaki Songhai mnamo mwaka 1591, kufungua tena njia za biashara za dhahabu na watumwa. Mnamo mwaka 1593, kutekwa kwa Timbuktu kulifanya iwezekane kuleta watumwa 1,200 kupitia Sahara, lakini mashambulizi yaliyoongozwa na Judar Pasha yalileteleza tu kuanguka kwake na kukwama kwa

biashara hii. Huu ndio ulikuwa mwisho wa himaya iliyokuwa kubwa kuliko zote Sudan ya Magharibi mnamo karne ya kumi na sita. Tripolitania na Misri zilidhurika kidogo tu kutokana na matokeo ya kufifia kwa biashara katika Sahara na zilidumisha njia zao za kawaida za kuvuka Sahara. Utawala wa Kituruki, ambao ulikwisha jisimika Misri na Tripoli, ulitia sahihi mkataba wa ushirikiano na Kanem-Borno, na hivyo kuweza kudumisha mtiririko wa biashara ya kaskazini-kusini, uliokuwa muhimu kwake kwa kupatia bidhaa, hadi karne ya kumi na tisa.

Uchumi wa kiporaji kwa hakika ulichangia katika kupunguza kasi ya ukuaji wa kiuchumi na kiteknolojia huko kusini mwa Mediterania, lakini miundo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa nayo ilichangia katika kudumaa kwa eneo hilo na maeneo yake ya bara.

Nchi zote za Nili na Afrika Mashariki, na vilevile nchi za eneo la Niger-Chad na Sudan Magharibi, ziliathirika kwa namna tofauti. Kwa mfano, huko magharibi mwa Bahari ya Hindi miaka ya 1680 hadi 1720 ilijulikana kama "kipindi cha maharamia." Nchi zilizokuwa na mahusiano ya moja kwa moja na nchi za Ulaya zilizokuwa na mamlaka, zilivurugwa kabisa na uchumi wa kiporaji, ingawa kufifia kwao kulitokana pia na kushindwa kwao kutia uhai mpya katika muundo wa kiuchumi na kijamii uliokuwa ukizidi kusthiriwa na nchi za Mashariki ambazo zilikuwa nyuma kimaendeleo. Nchi hizi pia zilikuwa zimekwamishwa na kushindwa kwao kuunda mahusiano ya kimamlaka ambayo yangewawezesha kuepuka upogo wa mfumo wa biashara uliokuwepo katika kipindi hicho.

## Kufifia kwa maeneo ya vijijini: umaskini na ukosefu wa usalama miongoni mwa wakulima wadogo

Uchumi wa kiporaji ulisababisha biashara baina ya miji na vijiji kusimama na hivyo kuathiri mahusiano kati yao. Hapo awali, shughuli zao na mazao yao yalikamilishana. Miji ilikuwa imevunja utaratibu uliokwama wa kilimo cha kijungujiko, iliimarisha mgawanyo wa kazi na ilibeba mbegu za ujenzi wa jamii mpya. Viwanda na ufundisadifu wa mijini ndivyo vilivyochochea kupanuka sana kwa shughuli za kilimo, ufugaji, uvuvi na uwindaji. Miji pia ndiyo ilisababisha kilimo cha miwa na pamba kwa kiwango cha kutosheleza mahitaji ya viwanda, na kilimo cha mimea ya rangi na manukato. Vyombo vilivyoendeshwa kwa nguvu ya maji, barabara na ufugaji kwa ajili ya kupata sufu, maziwa na nyama - yote yaliwezekana kutokana na kukua kwa miji.

Karne ya kumi na sita ilileta vurugu na zahama kwenye dunia hiyo. Kupungua kwa watu mijini kulisababisha kufifia kwa uchumi wa vijijini, kukapelekea kuenea kwa umaskini miongoni mwa wakulima wadogo na maeneo makubwa ya ardhi ya kilimo kugeuka kuwa pori. Kutokana na hali ya usalama kuzidi kupungua, watu wa maeneo ya vijiji walikimbilia katika misitu, mbali na utamaduni wa mijini, na kurudia kilimo cha kijungujiko cha kifamilia au cha kijijini. Mabadilishano ya mazao ndiyo yakawa tena namna kuu ya biashara.

Biashara ya watumwa ilisababisha mabadiliko mapya. Kutokana na kupungukiwa na

watu wenye uwezo, uchumi wa vijiji ulififia. Katika maeneo fulani, watu ambao kila mara walikabiliwa na bughudha za kushambuliwa, waliingia kwenye uchumi wa kinomadi wa kuwinda na kuhemea, na kufanya wengi wao wahame ukanda wa nyika na kuingia misituni.

Tabaka tawala la kijeshi lilitumia nguvukazi kubwa ya wakulima wadogo kwa faida yake, hali ambayo ilikuwa na matokeo mabaya kwa demografia ya maeneo ya vijijini. Tabaka la watawala liliacha kilimo na badala yake kutegemea mashambulizi kwa kutumia huduma za raia na watumwa liliowateka. Wakulima wadogo waliathirika zaidi huko Sudani ya Magharibi na katika eneo la Niger-Chad.

Ukandamizwaji wa wakulima wadogo wa Kiafrika na matabaka tawala ya vijijini na mijini uliongezeka kadri hali ya uchumi ilivyozidi kubana. Chini ya sharia ya Kiislamu ya Kituruki, kodi ingeweza kuongezwa kwenye nchi ambazo hazikusilimishwa. Waislamu walitakiwa kulipa si tu zaka (kodi pekee ambayo Waislamu walipaswa kulipa) bali pia *kharaj*. Kadri magendo katika haki za utozaji kodi kwenye nchi za Kiislamu yalivyozidi kuenea, ndivyo mzigo wa kodi ulivyozidi kuwalemea watu.

Katika hali hiyo viongozi wa jihadi na wana-vuguvugu la wokovu la Kikristo waliweza, kwa urahisi, kuungwa mkono na wakulima wadogo. Viongozi wa dini waliahidi kupatikana kwa usawa mara tu mambo yakiisha tulia. Waliwalaumu watawala wa kijadi na Wazungu kwa vurugu zote na udhalimu.

Kuanzia karne ya kumi na saba, dhima ya kisiasa ya wakulima wadogo iliongezeka. Maasi ya wakulima wadogo yalienea barani kote kama mapinduzi ya kidini na hivyo kusafisha njia kwa ajili ya ukinzani dhidi ya utamalaki wa kikoloni. Maasi hayo hayakufanywa na mateka na watumwa, bali na tabaka kubwa lililokuwa likinyonywa zaidi, yaani wakulima wadogo.

## Nchi za Nili na Bahari ya Hindi

Taathira ya uchumi wa kiporaji juu ya nchi zilizo kwenye Bonde la Nili na zile zinazopakana na Bahari ya Hindi ilikuwa na uharibifu sawa na ule uliojadiliwa juu. Bandari za Afrika Mashariki zilikuwa zikijulikana kwa shughuli zake za kibiashara tangu karne ya kumi na moja na zilikuwa na mawasiliano ya moja kwa moja na Bara Arabuni, Uajemi, India, China na Mediterania. Uvamizi wa Wareno ulikuwa mwanzo wa kuporomoka kwa utamaduni huu wa kibiashara wa mijini. Mwaka 1502, Kilwa na Zanzibar zilianza kutozwa kodi na Ureno. Mwaka 1505, Francesco d'Almeida alipora Kilwa na Mombasa na kisha kujenga ngome ya Santiago huko Kilwa. Alizuia biashara yote baina ya miji na wafanyabiashara waliihama hiyo kwenda Malindi na Visiwa vya Ngazija. Miji ya Lamu na Pate ilikaliwa.

Ukiacha Luanda na Msumbiji, hakuna vituo vyovyote vilivyojengwa na Wareno na baadaye na Waholanzi, Waingereza na Wafaransa ambavyo vililingana kwa ukubwa na miji ya huko Sudan Magharibi au hata na bandari za Waswahili na za Afrika Mashariki za karne ya kumi hadi ya kumi na sita.

## Uchumi wa mabohari au wa vituo vya biashara

Wakati ambapo uchumi wa kiporaji ulienea katika maeneo yanayopakana na

Mediterania, Nili na Bahari ya Hindi, uchumi wa mabohari au wa vituo vya biashara ulishamiri kwenye mwambao wa Bahari ya Atlantiki. Miji mipya ya mabohari sehemu za pwani ilikuwa ni ngome kabla ya kuwa vituo vya ustaarabu wa kibiashara vikiwa mandhari ya jefule na unyang'anyi.

Katika pwaa za Guinea na Ikweta, Wareno, ambao walikuwa wameanzisha uchumi wa mabohari katika karne ya kumi na sita, walipora kuliko walivyonunua vitu. Hawakuwa na chochote kikubwa cha kiuchumi kutoka upande wao; mbali na mvinyo na mikuo ya chuma, bidhaa zao nyingine ziliagizwa kutoka sehemu nyingine. Walibadilishana bidhaa hizi kwa dhahabu, watumwa, ngozi, gundi, pembe za ndovu, kaharabu, fungo manjano, kauri, pamba na chumvi. Katika Ghuba ya Guinea, Wareno walinunua bidhaa kutoka kwa Waakan na kuziuza tena kwenye pwani ya Nigeria au huko Kongo au Angola. Huko Senegambia waliishi kwenye bandari na wakawa wafanyabiashara wenye mafanikio. Mnamo karne ya kumi na saba, wakati ambapo viwanda vya Ulaya vilianza kutengeneza nguo na vifaa, kasi ya kufifia kwa miji kiuchumi iliongezeka.

Vituo vya biashara havikuchangia chochote katika kuleta ustawi wa kijanibu. Kabla ya mwaka 1800, Albreda, Cacheu, Santiago de Cape Verde, El Mina, Ketu, Kalabari na San Salvador vilikuwa vituo muhimu kabisa vya biashara na vyote vilikuwa na wakazi chini ya 5,000. Mbali na Wazungu, wengi wa wakazi wa vituo vya biashara walikuwa ma-*lapto* (wakalimani wenyeji). Uchumi wa vituo vya biashara ulitegemezwa kwenye biashara ya watumwa kuvuka Bahari ya Atlantiki. Katika kilele cha biashara hii, hakuna kituo chochote cha biashara kilichokuwa soko kwa ajili ya mazao ya mahali hapo au kilichokuza shughuli za kibiashara na za viwanda za wenyeji. Kituo cha biashara ya watumwa mno mno kilikuwa ni chombo cha kupunguza idadi ya watu.

Hata hivyo, mchango wa moja kwa moja na usio wa moja kwa moja wa uchumi wa vituo vya biashara kwa ustawi wa dunia ulikuwa mkubwa. Baada ya kugunduliwa kwa migodi ya Amerika, vituo vya biashara vilitoa sehemu kubwa ya dhahabu na fedha duniani. Aidha sehemu kubwa ya nguvukazi iliyoendeleza bara la Amerika ilitokana navyo. Kwa msemo mmoja, vituo hivi vilisukuma mbele biashara duniani. Vilikuwa ni chimbuko la viwanda, fedha na ubepari wa Ulaya na wa kimataifa. Biashara ya Wafaransa, mathalani, ilikua mno katika karne ya kumi na nane.

Kwa kujiimarisha katika mtandao (huu) wa kiuchumi, manahodha wa Kizungu walivuruga ruwaza ya kawaida ya biashara baina ya sehemu mbalimbali za Afrika na kuweka ukiritimba wao wenyewe wa wafanyabiashara wa kati waliokuwa kwenye vituo vya biashara. Waafrika hawakuweza tena kufanya biashara kati ya Saint-Lonis na Portendick, Grand Lahou na El Mina, Angola na Kongo au Sofala na Kilwa.

Mtandao wa Wareno ulitumiwa na nchi nyingine zilizotamalaki bahari kutoka karne ya kumi na sita na kuendelea. Vyanzo vingi vya taarifa juu ya biashara kwenye ngome-bohari na vituo vya biashara vya msimu toka wakati wa Wareno hadi kuwasili kwa Waholanzi, Wafaransa na Waingereza, vinaeleza hadithi za jefule na migogoro iliyodumu. Vituo vya biashara vya Bahari ya Atlantiki na Bahari ya Hindi viliharibiwa na kujengwa upya, na umiliki wake kubadilika mara kadhaa wakati wa mapambano ya

Wazungu, Waturuki na Waomani dhidi ya upinzani mkali wa watawala wa kienyeji waliotoza ushuru au *curva*. Mwisho uvumbuzi wa kiteknolojia uliobadilisha Ulaya ulikuwa na taathari ndogo tu. Uchumi wa Kiafrika uliathirika zaidi kutokana na ushindani kutoka kwa viwanda na shughuli za kibiashara za Kizungu. Kwa kuzisakama bandari, wafanyabiashara Wazungu walififisha mahusiano baina ya pwani na maeneo ya ndani ya nchi. Hivyo madola ya Ulaya yaliyoteka maeneo ya pwani yaliweka maeneo ya mamlaka ya Kireno, Kiholanzi, Kifaransa na Kiingereza hata kabla ya utamalaki wa kikoloni, na kwa kufanya hivyo, yaliamua maendeleo na jiografia ya kisiasa ya maeneo haya katika karne ya kumi na nane. Kutoka harakati za kiupanuzi wa Moroko dhidi ya Songhai hadi kwenye patapotea za vita vyenye madhara kwa pande zote huko Sudan Magharibi, tafrani nyingi katika mandhari ya kisiasa ya Afrika zilianzia katika vurugu zilizochochewa na mataifa ya Ulaya kunako karne ya kumi na sita.


## *Miundo mipya ya kisiasa*

Mandhari ya kisiasa ya Afrika yalikuwa yamekwishafikia kiwango cha uwiano na utengemano katika kipindi cha kati ya karne ya kumi na mbili na karne ya kumi na sita. Katika karne ya kumi na sita, Afrika ya Mediterania ilikuwa mfumo mdogo ndani ya himaya ya Waarabu-Waturuki, Moroko, Ifrikiya na Tripolitania zikiwa sehemu yake. Misri ilikuwa nchi pekee. Eneo la Nili lililojumuisha Nubia na Ethiopia lilienea kusini hadi kwenye dola la Bunyoro Kitara katika eneo la Maziwa Makuu, madola miji ya Waswahili, na eneo la kusini mwa Zambezi lililotawaliwa katika karne ya kumi na sita na dola la Mutapa. Kusini mwa Afrika hadi wakati huo ilikuwa na miundo michache ya dola. Huko Afrika ya Kati, mfumo mmoja ulitawaliwa na falme za Kongo na Tio, na mwingine na ufalme wa Luba. Lakini watu wa misituni hawakuunda madola. Sudan ya Magharibi na eneo la Niger na Chad zilipakana, mipaka yake ikiwa inabadilika mara kwa mara.

Maendeleo ya ramani ya kisiasa yalikuja kuakisi shinikizo kutoka nje na matokeo yake. Madola mapya yaliibuka ama kwa kuwa yalikuwa na silaha madhubuti kama vile Kanem Borno, au kwa sababu yalikuwa na njia nyingi za kufikia baharini, kama vile Kayor huko Senegambia, Dahomey katika Ghuba ya Guinea, Angola huko Afrika ya Kati au ufalme wa Changamire kusini mwa Zambezi.

Maumbile ya dola la Kiafrika nayo yalibadilika. Maeneo makubwa yasiyokuwa na watawala au wafalme, yaliyokuwa yamekaliwa na wakulima, wafugaji wa kinomadi na wawindaji, yalitekwa na kugeuzwa madola yenye miundo unganifu ya uongozi. Miundo ya vijijini ya Wabantu na ya Wa-Kabyle na Waberiberi wa Sahara, ilindoshwa na badala yake kuwekwa miundo ya *Makhzen* ya Maghrib, *mansaya* au *farinya* ya Afrika ya watu weusi, ukabaila wa makaimu wa Waturuki, au mfumo wa kiamiri wa Kiislamu.

Kutoka karne ya kumi na sita na kuendelea, maisha ya kisiasa yalijizatiti zaidi katika maeneo ya pwani, bandari za mamluki na vituo vya biashara. Utawala ulikusanya zaka katika maeneo hayo; serikali za Kiafrika zilijiundia idara za mapato ili kukusanya kodi kwenye biashara za kigeni. Mikataba mingi ilifanywa katika kujaribu kurasimisha




**2.1** *Maeneo ya kisiasa kuanzia Sahara hadi Ikweta kwenye karne ya kumi na saba*

mfumo huu wa utozaji kodi.

Moroko, Tunisia, Algeria na Tripolitania zilitia sahihi makubaliano mengi ya kibiashara na mikataba ya kirafiki na Wazungu na hata Waamerika iliyodumu kwa muda mfupi. Mnamo mwaka 1780, vita kati ya Moroko na Hispania vilimalizwa na Mkataba wa Aranjuez, ambao ulibainisha mipaka yao na kuyawekea kanuni mahusiano yao ya kibiashara. Karibu wakati huo huo, Algeria na kisha Moroko ziliilazimisha Marekani kulipa fidia kwa maharamia ili kuachiwa huru kwa baadhi ya raia wake.

Vilitumika vita, uharibifu wa vituo vya biashara na uzuiaji wa biashara kuzishawishi nchi za Ulaya kulipa kodi. Lakini vyanzo hivi vya mapato, ambavyo, kwa kiasi kikubwa au kidogo, vilikuwa vya kawaida, ndivyo vilikuwa chanzo cha vita miongoni mwa watawala na matabaka tawala barani kote.

Tawala "huru" za kisiasa zilikuwa ni maeneo ambamo uwiano ulikuwa umefikiwa na ambayo yalikuwa yameendelea kulingana na hali halisi za ndani. Maeneo haya yalitofautiana kwa ukubwa na kwa uimara wa mipaka yake na serikali zake. Mengine yalikuwa mashirikisho ya madola, wakati mengine yalikuwa dola au temi unganifu zenye mamlaka kidogo. Wakati mwingine yalikuwa ni ukoo tu au *lamana* huru ambamo wakazi wa mwanzo walikuwa wakiendesha mambo yao wenyewe.

Hivyo kukosekana utengemano kulikoletwa na uchumi wa kiporaji na wa vituo vya biashara, kutoka karne ya kumi na sita hadi ya kumi na nane, kuliunda ruwaza ya madola au chumi ambazo hazikuweza tena kutegemeza maendeleo yake kwenye msingi thabiti na wenye mpangilio.

# 3

# Miguro ya watu na kuibuka kwa miundomipya ya jamii na kisiasa katika Afrika

## Aina ya miguro ya watu

Tofauti kuu moja kati ya historia ya Afrika ya kabla ya ukoloni na historia ya Ulaya na ya sehemu nyingi za Asia inahusu miguro (uhamaji) ya watu, hasa miguro ya wakulima. Wakulima wa Kiafrika wa ukanda wa tropiki na ule unaokaribia tropiki walikuwa wakihamahama zaidi kuliko wakulima wa Ulaya na Asia kwa kuwa walitumia kilimo-panuzi na hawakuweza kulima ardhi ileile kila mwaka. Kwa hiyo hawakufungika kwenye eneo maalumu la ardhi. Ilikuwa ni hivyohivyo kwa wafugaji, ingawa mbinu zao za kuhimili mazingira zilifanana sana na za wafugaji wa Asia na uhamaji wa msimu wa Ulaya. Miguro hii ya watu ndio tabia ya msingi inayofaa kuangaliwa katika kuchunguza au kuunda upya historia ya Afrika.

Juzuu hili linatoa ushahidi wa wingi wa uhamaji, kutoka uhamaji wa Makaburu huko kwenye Rasi ya Kusini hadi ule wa Wasomali na Waoromo katika Pembe ya Afrika, Wangbandi wa Ubangi, Wajaga wa Afrika ya Kati, Watuareg wa ukanda wa Niger, Wamane wa Sierra Leone, Wafalbe wa Afrika Magharibi yote na watu wote wa Bukini. Uhamaji huu haukuwa tu wa kawaida kwa kipindi cha kati ya mwaka 1500 na 1800, bali pia kwa vipindi vingine. Lakini ilipofika mwishoni mwa karne ya kumi na sita wasafiri wa Kireno walidhani kwamba miguro hiyo ilihusiana, kwani waliiiona kuwa kawaida ya makabila yote ya "washenzi" - dhana potofu ambayo imedumu katika historia ya Kiafrika hadi miaka ya karibuni. Zaidi ya kuwa ni dharau, mawazo hayo hayaruhusu kuelewa nini kilichotokea hasa.

Neno "uhamaji" lina maana ya kugura kwa watu kutoka sehemu moja na kwenda kufanya maskani yao mahali pengine. Uhamaji basi ni dhana inayoeleza mabadiliko ya uhusiano baina ya watu, mahali na wakati. Kwa maana hii ya jumla, ni bora kuzungumzia miguro ya watu. Miguro hiyo huweza kutokana na mabadiliko ya uwiano wa watu na raslimali au kwa sababu ya watu kujaribu kupangilia upya nafasi yao na raslimali walizo nazo kwa mapana zaidi. Katika Afrika, mipangilio mikubwa ya maeneo ilikuwa ni madola na mitandao ya biashara.

Waafrika walisisitiza umuhimu wa uhamaji katika mapokeo simulizi yao. Mapokeo mengi yanapojaribu kueleza juu ya asili ya ulimwengu hurejelea jamii za wahenga au

waasisi binafsi ambao walitokea sehemu nyingine. Visasili vingine vinadai kuwa watu walitoka kwenye udongo na hivyo walikuwa wamiliki wa ardhi. Nadhariatete ya kwanza ilikubaliwa na wasomi wa Kizungu waliokuwa wakithibitisha mawazo waliyokuwa nayo tangu awali. Walikuwa na taswira ya mashambulizi ya mara kwa mara ambapo watu wa Afrika walikuwa wakisukumana mithili ya vipira vya biliadi, kila ushindi mpya ukianzisha wimbi la wakimbizi lililotafuta amani mahali pengine, au labda wao wenyewe kuzifukuza jamii nyingine kutoka mahali pao.

Ingawa ilionekana hivyo, mawazo kuwa Waafrika walihama daima ni kalautala na hayana msingi. Katika makala muhimu, P.E.H. Hair aliandika juu ya utengemavu usio kifani wa lugha zote za pwani kutoka Senegali hadi Kameruni, na mawazo hayo yanaweza kuchukuliwa kuwa ni kweli kwa jamii nyingi za wakulima wa Afrika baada ya karne ya kumi na sita.

Kama ilivyokuwa dhana ya "uhamaji", dhana ya "utengemavu" inaeleza juu ya uhusiano baina ya watu, wakati na mahali; inaelezea kutokuwepo kwa mabadiliko. Lakini dhana zote mbili zinafungwa na matumizi. Ukipewa eneo kubwa la kutosha, kama vile eneo linaloenea mashariki na kaskazini ya Nili Nyeupe, uhamaji wa watu kama vile ule wa Wajie, unakuwa ni utengemavu, ni kujirekebisha tu kwa watu kuhusiana na udongo na hali ya hewa. Kwa upande mwingine ulio tofauti mno, hajira ya kijiji kwenda kilometa kumi mbali zaidi huweza kuelezwa kuwa ni "uhamaji." Ni hivyohivyo kulingana na wakati: ni kwa kuangalia tu vipindi virefu vya muda ndio tunaweza kuona "uhamaji" wa baadhi ya watu wanaojongea polepole kwa karne kadhaa (kama vile uhamaji wa Wabantu, kwa mfano, ambao huenda uliendelea kwa miaka elfu mbili).

Kwanza ni lazima tuangalie miguro ya kawaida inayotokana na kutafuta maisha bora zaidi ili tuweze kuelewa vyema zaidi miguro isiyo ya kawaida na kuona jinsi miguro mbalimbali ya watu ilivyotokea. Baada ya hapo tunaweza kuangalia ushahidi ainaaina wa miguro isiyo ya kawaida na kisha kuangalia hajira kubwa za watu katika Afrika kati ya 1500 na 1800.

## Miguro na matumizi ya ardhi

Kwa kuwa kuna njia nne za kutumia mazingira kupatia chakula - kuwinda na kuhemea, kufuga, kilimo na uvuvi - halikadhalika kuna ruwaza nne kubwa za uhamaji wa kawaida unaohusiana na shughuli hizo.

Wawindaji na wahemeaji hutangatanga kwenye nchi ambayo kwa kiasi ina utengemavu, mradi wingi wa watu unatosheleza mahitaji ya maisha ya namna hiyo. Huishi katika makambi na kutembeatembea ndani ya nchi hiyo, kama wafanyavyo Mbilikimo wa Ituri na Wakung San wa Botswana. Inabidi wafanye hivyo ili kufuata wanyama na kupata kiasi cha kutosha cha mimea ya kula. Uhamahamaji wao hubadilika kufuatana na majira. Miguro yao ni mikubwa, lakini bado wakazi huweza kutumia nchi hiyohiyo kwa muda mrefu.

Wachungaji pia huhamahama. Wanyama wao huhitaji maji, nyasi na chumvi na kupatikana kwa vitu hivyo kunabadilika kulingana na hali ya hewa. Katika Sahara, kwa

mfano, wahamaji mara nyingi huishi karibu na ukingo wa jangwa au kwenye oasisi wakati wa kiangazi na wanakwenda ndani jangwani wakati wa mvua. Miguro hii hujulikana kama uhamaji wa kimsimu, na aghalabu hufuata njia ileile mwaka hadi mwaka. Miguro hiyo huweza kuwa za masafa marefu sana kwa wachunga ngamia kama vile Warigeibati wa Sahara Magharibi. Aghalabu kunakuwepo na miguro changamani ya kupishana baina ya wachungaji wahamaji wenye mifugo mbalimbali, kulingana na mahitaji tofauti ya ngamia, mbuzi, ng'ombe na kondoo. Zaidi ya hayo, Wanomadi walilima mazao machache na kubadilishana chakula na wawindaji wabobezi na wahemeaji, kama walikuwepo - kama ilivyokuwa kwa msafara wa Makaburu wa karne ya kumi na nane huko Afrika Kusini. Hivyo maliasili ilitumiwa kwa njia tofauti zinazowiana na makundi mbalimbali yaliyoishi pamoja, kila moja likiwa na nyendo zake katika eneo lilelile. Isitoshe, uchungaji uliathirika kwa urahisi zaidi na mabadiliko ya hali ya hewa, hasa ya muda mfupi, kuliko uwindaji na uhemeaji.

Wakulima pia walikuwa waguraji kwa sababu walilima kwa kuhamuhama, wakiacha ardhi iliyolimwa mwaka uliotangulia kupoa. Vijiji ilibidi visogezwe iwapo mashamba yalianza kuwa mbali mno na makazi ya watu. Katika miaka ya karibuni, hali hiyo ilikuwa ikitokea takriban kila baada ya miaka kumi. Ardhi nzuri zilikuwa ni zile zilizorutubishwa kwa umwagiliaji na tope la mashapo la kila mwaka. Katika ardhi kama hiyo, kungeweza kuwa na ulimaji wa kudumu uliosababisha kuwepo kwa watu waliofanya makazi ya kudumu. Lakini, zaidi ya Misri na ukanda wa kinamo wa kilimo cha mpunga wa pwani ya magharibi ya Guinea, maeneo ya kilimo cha kudumu yalikuwa adimu katika Afrika, kutokana na kutokuwepo kwa njia zinazofaa za urutubishaji.

Vijiji vingi vilihamahama wakati huo, lakini mradi watu hawakuwa wengi, vilifuata njia za kuzungukazunguka katika eneo lilelile. Miguro ya vijiji haikutegemea ardhi peke yake. Katika maeneo mengi, kwa mfano katika misitu yote ya tropiki ya Afrika ya Kati, wakulima walikuwa pia wawindaji na wategaji wa wanyama, na wahemeaji pia. Hivyo, miongoni mwa Wanzabi wa Gabon, kwa mfano, sehemu za kujenga vijiji zilihamuliwa na mahitaji ya wategaji wanyama na wakulima pia. Tishio kubwa la njia hii ya kuishi lilikuwa ni mabadiliko ya hali ya hewa, hasa mvua zisizotabirika. Njaa iliwezekana kutokea hata karibu na Ikweta, hata kama kulikuwa na maeneo yenye maji ya kutosha. Kutokuwa na mvua baada ya kupanda kulikuwa ni balaa lakini pia mvua isiyokwisha iliyozuia upandaji wa mbegu ilikuwa balaa vilevile. Ukame ulitokea zaidi kwenye maeneo yaliyokuwa karibu na jangwa, lakini hakuna eneo lililokwepa kabisa hali hiyo.

Kwa ufupi, kwa wakulima, kama ilivyokuwa kwa wachungaji au wahemeaji, kulikuwa na idadi ya juu kabisa ya watu iliyoweza kuishi katika eneo fulani, na pia kulikuwa na idadi ya watu iliyostahili kuishi katika eneo hilo, na ambayo ilibadilika kulingana na mazingira - aina ya udongo, kiasi cha mvua, taswira ya nchi, upatikanaji wa chakula cha ziada, hali ya teknolojia na mipango ya ugawanyaji au usambazaji wa raslimali.

Wavuvi walikuwa ni watu waliokaa mahali pamoja na walihamisha vijiji vyao kwa nadra sana. Hata hivyo, mabadiliko ya kimsimu ya viwango vya mito yangeweza

kuwalazimisha kwenda mbali. Katika hali hiyo wangepiga kambi kwenye mafungu ya mchanga kwenye mto Kongo au Kasai, mara nyingine kilometa nyingi kutoka kwenye vijiji ambako wameacha familia zao. Makazi ya kudumu yalikuwa ni jambo la kawaida zaidi kwa wavuvi wa pwani na kwenye maziwa makubwa. Wavuvi walikuwa na njia rahisi ya usafiri kwa kuwa walikuwa na mitumbwi, ambayo iliwafanya wengi wawe wafanyabiashara na walanguzi baina ya makundi mbalimbali yaliyotamakani kwenye maeneo yao.

Ni dhahiri pia kuwa watu waliohamahama hawakufanya hivyo kwa sababu za kiuchumi tu. Kuondoka kwa kikundi cha watu kutoka sehemu fulani kungeweza kuwa ni matokeo ya kuongezeka kwa vifo au ugomvi na vikundi vingine au kwa ajili ya kujilinda. Palikuwa pia na miguro mingi ya watu binafsi. Wanawake mara nyingi waliolewa kwenye vijiji vingine; watoto wa kiume walikwenda kuishi na ndugu wa mama zao. Watumwa, waweka rehani, wafanyabiashara, mahujaji, waganga wakubwa na wawindaji mara nyingi walihamahama. Dhana kwamba baadhi ya makabila ya Kiafrika hayakuhusiana na ulimwengu wa nje ni uwongo kama ilivyo dhana ya kuwa makabila mengi yalikuwa yakitangatanga daima. .

Ni lazima isisitizwe kwamba tofauti baina ya hajira ya kawaida na isiyo ya kawaida ilikuwa ndogo sana kwa watu binafsi, ingawa ujumla wake ungeweza kuwa ni jambo kubwa. Biashara ya watumwa ya baada ya 1660 ingeweza kuonekana kama jambo la kawaida la miguro ya watu. Lakini usafirishaji wa watumwa kwenda Amerika ulikuwa ndio hajira kubwa kabisa ya watu iliyopata kuisibu Afrika.

Ujenzi wa miji pia unawakilisha miguro ya watu. Kufikia mwanzoni mwa karne ya kumi na nne, idadi ya watu wa mji wa Zimbabwe ingeweza kufikia 10,000, ikiwa na maana kuwa kulikuwa na uhamiaji wa watu mjini hapo awali. Ardhi ilipochoka, wakazi wake walihama mji na kurudi kwenye vijiji vyao. Kutawanyika kwao pia kunawakilisha dhana muhimu vilevile ya miguro ya watu. Lakini zaidi ya ujenzi wa miji na biashara ya watumwa, hakuna taarifa nyingi kuhusu hajira za watu binafsi na hata familia. Tunaweza kufahamu zaidi juu ya habari zao tutakapoweza kujua idadi ya watu ilivyobadilika kutoka muongo mmoja hadi mwingine na kutoka eneo moja hadi jingine. Lakini uhamaji wa watu binafsi ulikuwepo na ungeweza kuwa mkubwa kiasi cha kuwa na taathira kwenye mabadiliko ya wingi wa watu katika eneo fulani.

## *Aina za miguro ya watu isiyo ya kawaida*

Miguro isiyo ya kawaida ya jumuiya inaweza kuainishwa katika makundi mawili – mzururo na uhamaji. Mzururo huwa ni wa polepole, lakini uhamaji ni hajira ya mara moja. Zaidi ya hayo, mzururo hauna maana ya kuacha kabisa makazi ya mwanzo, ingawa mwishowe inaweza ikawa hivyo, ilhali uhamaji mara nyingi huwa na maana ya kuacha makazi ya awali. Aina hizi mbili za miguro ya watu zinaweza kugawanywa zaidi katika aina kadhaa. Mzururo huitwa upanuzi pale ambapo eneo linalokaliwa na kikundi cha watu huongezeka, na huwa diaspora unapokuwa mtawanyiko wenye kuzua makazi mapya. Kwa upande mwingine, kuna uhamaji wa halaiki, uhamaji wa makundi

maalumu (mara nyingi huwa ni makundi ya wapiganaji) na uhamaji wa waali ambao huwa ni wa vikundi vidogo ambavyo kufika kwake huleta mabadiliko makubwa katika jamii ya wenyeji.

Umuhimu wa kihistoria na ukubwa wa mguro wa watu hutegemea idadi ya watu waliojihusisha nao, umbali waliosafiri, urefu wa muda wa mguro huo, sababu zake na matokeo yake. Sababu hizo zote ni lazima zitiliwe maanani katika kila tukio, lakini haziwezi kutumika katika kuainisha uhamaji kwani maana zake hutofautiana sana. Kwa hiyo tutaangalia sifa za kila mguro katika aina tano za uhamaji zilizoelezwa hapo juu.

## Upanuzi

Upanuzi umetokea mara zisizohesabika kwa sababu ya miguro ya kawaida ya watu wengi wa Afrika, na tabia yake hutofautiana kulingana na maisha ya jamii inayoangaliwa. Kilimo cha kuhamuhama huwa upanuzi pale ambapo kuna mzururo wa kuelekea upande mmoja badala ya mzururo wa shaghalabaghala au wa mzunguko. Upanuzi huo huweza kuwa wa muda mrefu na bado watu wakaonekana kama wametulia kwenye makazi yao.

Katika eneo la msitu, upanuzi wa Wamongo kuelekea kusini kutoka kwenye pindi la Mto Kongo ulianza mapema sana kabla ya karne ya kumi na sita, na ulikuwa bado unaendelea hata mwishoni mwa karne ya kumi na tisa katika maeneo mengi kati ya Mto Kongo kwa upande wa magharibi na Mto Lomami kwa upande wa mashariki. Upanuzi huu ulisababisha mtiririko wa watu kutoka kitovu cha wingi wa watu karibu na ikweta na digrii moja kusini, kwenda kwenye mabonde ya mito na kingo za msitu.

Upanuzi uliweza kufanywa haraka zaidi kwa kuongeza umbali unaosafiriwa wakati wa kila mguro au kwa kuhamahama mara nyingi zaidi. Upanuzi wa namna hiyo ulikuwa na kusudi mahsusi, mara nyingi kwa kuvutiwa na jambo maalumu. Hivyo, katika kipindi cha nusu karne Wanzabi wa Gabon/Kongo walihama kutoka kwenye nchi yao mashariki ya pindi kuu la Mto Ogowe na kwenda kusini magharibi ili wawe karibu na njia za biashara na ili waweze kuchimba madini mapya. Wafang wa Komoe ya juu walifikia mlango wa Mto Gabon katika miaka ishirini tu na kisha waliendelea kwa miaka arubaini mingine kuelekea delta ya Mto Ogowe. Hawakuyaacha maisha yao ya kawaida kamwe, vijiji vilihama kimoja baada ya kingine, kila kimoja kikitambuka kijiji kilichotangulia.

Upanuzi wa wafugaji ulifuata ruwaza tofauti. Kwa kawaida marika ya vijana yaliacha mzingo wa miguro ya kimsimu ya kikundi na kufanya makazi yao na ya mifugo yao katika sehemu mpya za malisho. Wamasai walihama kwa njia hiyo katika karne za kumi na saba na kumi na nane mpaka ardhi yote iliyofaa ilipokaliwa. Mfano mwingine ni ule wa njia kuu ya Makaburu wa Afrika Kusini. Kizazi cha pili cha masetla wa Kizungu kilikaa karibu na Rasi tangu takribani mwaka 1680 na kuendelea. Tangu mwanzo wachungaji walilalamikia wingi wa watu uliokithiri, ingawa kwa kweli watu walikuwa wachache. Wakichukua baadhi ya mifugo, vijana waliondoka na kuanza makazi mahali pengine. Mpaka 1780 upanuzi huu uliendelea katika maeneo ya wachungaji wengine (makundi ya Wakhoi) ambayo wahamaji wa Kikaburu

waliyachukua. Lakini walikuja kugota kwenye mpaka wa ardhi yenye maji zaidi ya wakulima na wachungaji wa Kixhosa.

Hata wawindaji nao walionyesha mzururo. Hii inaweza kuwa ndiyo sababu ya kuwepo kwa wawindaji Wabaka huko Kameruni ya mashariki. Mbilikimo hao wanazungumza lugha za Kiubangi, lakini wanaishi magharibi zaidi ya wakulima walio kwenye kundi hilohilo la lugha. Sababu ya hali hii pengine ni mguro wa kutoka bonde la juu la mto Sanga ambao ulilipanua taratibu, kuelekea magharibi zaidi, eneo ambamo Wabaka waliwindia.

Miguro ya upanuzi mkubwa huonyesha mgawanyo mpya wa watu. Mwelekeo wenye mashiko sana na uliochukua muda mrefu katika historia ya Afrika ni mjongeo usiobadilika na wa idadi kubwa ya watu kwa ajili ya kuteka maeneo mapya na kubadili mazingira kulingana na maisha yao kuliko kutawaliwa nayo. Hivyo upanuzi wa Waigbo mashariki ya Niger ya chini ulisababisha mabadiliko kamili ya taswira ya msitu na kuwepo kwa ongezeko kubwa la watu. Upanuzi wa aina hiyo katika maeneo yaliyokuwa na watu wachache ulisababisha ongezeko la watu katika bara lote kwa jumla.

Miguro ya upanuzi ni lazima ilitokea mapema katika Afrika. Wawindaji na wahemeaji ndio waliokuwa wa kwanza kujipanua katika maeneo waliyofanyia shughuli zao, wakifuatiwa na watu waliotumia mazingira yao kishadidi zaidi. Katika matukio mengine, uharibikaji wa muda mrefu wa raslimali kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa ulisababisha upanuzi, tukio kubwa likiwa ni lile la kukauka kwa Sahara ambako kuliwasukuma polepole wakulima wa Mauritania kuelekea kusini.

Si lazima kuwa watu waliokuwa wakipanua makazi yao waliwafukuza watu waliowakuta njiani. Aghalau mchanganyiko wa watu ulitokea, wale wa zamani wakiiga utamaduni wa wageni, kama ilivyokuwa kwa Wafang; au jamii na utamaduni mpya kutokea kutokana na mchanganyiko huo. Kwa hiyo, upanuzi wa Wamongo kuelekea kusini ulisababisha kutokea kwa jamii mbalimbali, pamoja na jamii maarufu kama Wakuba. Kama hakukuwa na kuchanganyika, wenyeji waliacha nchi yao polepole. Inaonekana kuwa haikuwa kawaida kwa watu waliofukuzwa nchini kwao kushambulia majirani zao. Upanuzi ulisababisha wakimbizi wachache kutokana na idadi ndogo ya watu waliohusika.

## Diaspora

Diaspora ni hajira za watu zisioendelea mfululizo ambazo husababisha kuundwa kwa makazi mapya yaliyotengwa na makazi ya asili. Diaspora zote huhusishwa na biashara au hija, isipokuwa labda ile ya wachungaji wa Kifulbe walioenea Afrika Magharibi yote.

Diaspora za kawaida zaidi zilikua kutokana na biashara. Makazi ya Wafoeniki, Wayunani na Waarabu yaliyokuwa pwani ya Pembe ya Afrika na upwa wa Afrika ya Mashariki, ngome za Wazungu na koloni la Cape Town, vilianzishwa na wafanyabiashara kutoka ughalbuni. Biashara ya kwenye mito na uvuvi vilikuwa muhimu katika historia ya diaspora. Kwa mfano, kati ya 1750 na 1850 wakazi wa kijiji kikubwa kwenye mlango wa Mto Ubangi walianzisha vituo vya biashara na makazi kandokando

ya Mto Kongo hadi kufikia kwenye mlango wa Mto Kasai; walichanganyika na makundi mengine ya watu na walianzisha kabila jipya la Wabobangi. Katika Afrika Mashariki Waswahili na utamaduni wao ulienea kwa njia hiyohiyo, kutoka pwani ya Somalia na Kenya hadi visiwa vya Ibo kando ya Msumbiji na Ngazija. Diaspora zilifuata pia njia za bara. Wafanyabiashara wa Kimande waliunda diaspora za Jahaka kutoka Niger ya juu hadi makazi ya pwani ya Senegal na ya Wajuula kuanzia Niger ya Juu hadi upwa wa Akan.

Diaspora nyingine zilitokana na kuhiji kulikofanywa kila mwaka Maka. Pale ambapo, kwa sababu moja au nyingine, mahujaji hawakuweza kuendelea na safari yao, walitamakani pale walipoweka kambi. Hivyo ndivyo Watakruri, kutoka Afrika ya Magharibi, walivyotamakani Sudani mnamo karne ya kumi na tisa. Vivyo hivyo, *marabtin bilbaraka* wengi wa huko Barka walitokana na mahujaji wa Afrika Kaskazini.

Aghalabu diaspora ziliendelea kujihusisha na nchi zao za awali, ama kwa biashara au kwa sababu waliishi karibu na njia za mahujaji. Katika baadhi ya mifano, hata hivyo, walikwenda mbali polepole. Kwa mfano, ilipofika karne ya kumi na tano wakazi wa Sofala hawakuwa tena na uhusiano maalumu na Lamu au visiwa vya Bajuni katikati ya Uswahilini. Hata makoloni ya Wazungu yalielekea kujitenga na nchi zao za awali na kuunda uhusiano wa kibiashara na makoloni mengine. Hivyo wakoloni wa Cape Town walikuwa karibu zaidi na Visiwa vya Mashariki vilivyokuwa chini ya Uholanzi, ambavyo mji wake mkuu ulikuwa Batavia, kuliko walivyokuwa na Uholanzi.

Diaspora ni hajira za watu zilizokuwa dhahiri zaidi. Zilikuwa ni dalili za kuwepo kwa mitandao ya mawasiliano ya masafa marefu, na zilistawi kutokana na maendeleo ya njia za biashara. Zilidhihirisha mafanikio ya watu katika kudhibiti maeneo.

## Uhamaji wa halaiki

Uhamaji wa halaiki hutokea pale ambapo kabila lote - wanaume, wanawake na watoto - huacha nchi yao, wakachukua mali zao zote na kusafiri mwendo mrefu kwa mwaka au zaidi. Uvamizi mkuu kabisa wa Afrika Kaskazini ulikuwa ni ule wa makabila ya Banu Hilal na Banu Sulaym wa 1052 na kuendelea, ambao unahusishwa hivi sasa na kuwepo kwa ukame wa mara kwa mara Arabia. Uvamizi huu uliendelea hadi takriban 1500 ambapo ulifika Mauritania. Ulibadili mazingira ya kiutamaduni ya Afrika ya Kaskazini na kuyafanya kuwa ya Kiarabu kabisa.

Uhamaji wa kweli wa halaiki ni tukio la kusisimua, lakini hutokea mara chache. Katika kipindi kati ya 1500 na 1800, uhamaji wa kweli wa halaiki ulikuwa ni ule wa Waoromo ambao uliwahusisha hata watu wengine katika kuhama. Katika karne ya kumi na tisa kulikuwa na uhamaji wa Wanguni uliohusisha Afrika tangu Rasi ya Kusini hadi Nyanza.

Hajira za halaiki zilikuwa ni matukio magumu. Hajira hizo zilihitaji miundo mipya ya kuongoza jamii na siasa, aghalabu ikiwa ya kijeshi. Mara nyingi wahamaji walijiingiza kwenye mashambulizi na uporaji. Watu wengine, waliosumbuliwa na kupita kwao, mara nyingi walijiunga nao, na polepole kuongeza idadi yao. Uhamaji huo huweza kusababisha ugomvi na kuwepo kwa wakimbizi na kuanzisha uhamaji mwingine

au upanuzi wa haraka. Hata kama uhamaji wa awali ulikuwa wa ghafla, mjongeo wa watu ulioanzishwa uliweza kuendelea kwa karne au zaidi. Hivyo uhamaji wa Waoromo labda ulianza miaka ya 1530, lakini utengemano haukuwepo katika maeneo yaliyoathiriwa hadi takriban 1700.

Maelezo haya yanahusu hali ambazo ni za aina ya pekee sana. Mapema, wakati hakuna nyaraka za kutosha, ni vigumu kubainisha kati ya uhamaji wa halaiki na ueneaji wa haraka uliohusisha watu wengi, hasa wafugaji. Hivyo ueneaji wa Waluo mara nyingi hutambuliwa kama uhamaji wa halaiki. Ulihusisha watu wote na ulianzisha miguro kadha mingine, na kuleta misukosuko katika eneo kubwa, hasa mashariki ya Nili Nyeupe. Lakini hajira za Waluo ziliendelea kwa muda mrefu, labda nusu ya milenia, na ushahidi uliopo unaonyesha kuwepo kwa mizururo kuliko uhamaji wa halaiki, kwani Waluo aghalabu walihama na mifugo yao na walipiga kambi kulima. Sehemu ya uhamaji wa Waoromo inaonyesha hali hiyohiyo. Mifano hii inaonyesha kwamba uhamaji wa halaiki mara nyingine ulifanana na ueneaji wa umma na kwamba mzururo huweza kutokea katika wakati huo. Jambo linaloubainisha ni uwezo wa kuzalisha mali na miundo ya kijeshi ya halaiki iliyo katika mwendo.

Uhamaji wa halaiki aghalabu husukumwa na sababu nzito, kwa mfano mabadiliko ya ghafla ya hali ya hewa yanayofuatiwa na njaa na magonjwa ya mlipuko. Mara nyingine hata hivyo, uhamaji hautokani na maafa ya asili. Uhamaji wa Wavandali, kwa mfano, unahusiana na miguro mingine na kuanguka kwa himaya ya Roma. Ongezeko la watu linaelezwa kuwa ni sababu ya kuwepo kwa uhamaji wa Banu Hilal, Waoromo na *mfekane,* lakini hadi sasa hakuna ushahidi wa kutosha wa sababu hiyo. Shinikizo la idadi ya watu linaweza kuhusika katika uhamaji wote wa halaiki, lakini si sababu ya kutosha au kamili kuelezea hali ilivyokuwa.

## Uhamaji wa makundi

Uhamaji wa makundi, mara zote yakiwa na silaha, huhusisha idadi ndogo ya watu, hasa vijana, wakiwa sehemu tu ya wakazi. Kwa kawaida makundi ya wapiganaji yaliondoka kwa lengo la kuvamia na kuteka nchi mpya, mara nyingine, lakini si mara zote, wakiwa chini ya kiongozi mmoja. Katika matukio mengine, kama yale ya Wajaga na Wazimba, kwa mfano, makundi hayo yalisambaa baada ya kushindwa; katika matukio mengine, kama vile ya Wamane, Watyokosi na Waimbangala, walifanikiwa kuanzisha temi au falme.

Makundi yaliweza kuleta uharibifu mkubwa lakini kutokana na udogo na muda mfupi wa shughuli zao ikilinganishwa na uhamaji wa halaiki, hayakusababisha vurugu kubwa. Mara nyingi sababu za nje ziliyasukuma kuliko sababu za ndani, kwa mfano, wakati upanuzi wa Makaburu ulipowasukuma Wakorana na Wagonakwa kuhamia Mto Orange na Mto Kaledón. Uhamaji wa makundi mara nyingine ulisababishwa na kuundwa kwa dola au upanuzi wa biashara ambao wahamaji walitaka kufaidika nao, kama ilivyokuwa kwa Wajaga.

Mfano mzuri ni ule wa Waimbangala. Makundi yalijiunga karibu na Mto Kwango, labda baada ya mabadiliko yaliyotokea katika dola la Lunda lililokuwa likipanuka.

Makundi haya yalijichanganya na watu wanyonge katika tawala za Waovimbundu na Wambundu. Waimbangala walijihusisha na uporaji kwa miaka kadhaa wakiwa marafiki wa Wareno ambao walikuwa wakilitayarisha koloni la Angola. Ilipofikia takriban 1620 walitamakani karibu na Mto Kwango, wakiwa nje kidogo ya mafikio ya Wareno. Uhamaji wao ulisababisha kuundwa kwa dola, ufalme wa Kasanje, ambao ukawa ndio kituo kikubwa cha kupitishia watumwa waliosafirishwa kutoka barani Afrika kwenda Luanda. Mfano wa Waimbangala ulikuwa tu ni uratibu wa miundo ya kijamii na kisiasa na biashara, na si kitu kingine zaidi.

### Uhamiaji wa waali

Uhamiaji wa waali ni suala linalopendwa katika mapokeo simulizi kuhusu uundwaji wa madola. Mfalme wa kwanza huwa ni mgeni, aghalabu mwindaji, anayekuja kutoka mahali pengine, akiwa peke yake au na wenzake wachache; na japo hajira ya watu katika matukio ya aina hii huwa ni ndogo, lakini matokeo yake ya kijamii na kiutamaduni huwa ni makubwa.

Baadhi ya hadithi hizi huweza kuwa ni za kubuni kabisa na hazina sababu nyingine ila kuonyesha mawazo ya kuwa mfalme ni lazima awe mgeni kwani ni mtu aliye tofauti na wengine, mwenye sifa za utukufu na usirisiri. Hadithi nyingine, hata hivyo, zina msingi. Kwa mfano katika hadithi ya Wakaba inaelezwa jinsi mkimbizi Mbushoong, Shyaam a Mbul a Ngoong, alivyorudi nyumbani kutoka magharibi na kuunda ufalme kutokana na temi zilizokuwa zikizozana. Imeonyeshwa jinsi athari za lugha kutoka magharibi zilivyoingia katika eneo la Ukuba na kuenea kutoka kwenye kitala, hali ambayo inaunga mkono wazo la kuwapo kwa utamalaki wa utamaduni. Hata hivyo, haiyamkini kwamba athari kama hiyo inaweza kupatikana kwa kuja kwa mtu mmoja, na zaidi kwa mtu aliyekuwa uhamishoni.

Katika kuchunguza hajira za watu, uhamaji wa waali unaweza ukapuuzwa, lakini katika kuchunguza maendeleo ya miundo ya jamii na utamaduni, hasa uundaji wa madola, uhamaji wa waali huweza kuwa na umuhimu mkubwa.

## *Uhifadhi wa taarifa za uhamaji wa watu*

Marejeo makubwa yanayohifadhi historia ya uhamaji wa Afrika ni masimulizi, lugha, akiolojia na maandishi. Lakini matumizi yake ni magumu na yanahitaji uangalifu mkubwa.

Mapokeo simulizi hayawezi kuweka kumbukumbu za muda mrefu za upanuzi, kwani maisha ya kila siku hayasumbuliwi sana na upanuzi huo na mwendo wake ni wa polepole kiasi kwamba watu huwa hawautambui. Hakuna mapokeo simulizi yanayoweza kujumuisha uhamaji wa halaiki, kwani ukubwa wa matukio umekithiri; mapokeo simulizi huweza tu kuhifadhi kumbukumbu za matukio madogomadogo katika uhamaji huo. Zaidi ya hayo, mapokeo simulizi huelekea kuchanganya uhamaji wa halaiki na uhamaji wa makundi ya watu, ambayo huwa ni ya eneo dogo, lakini huwa na athari zinazofanana, ambazo hubaki katika kumbukizi. Watu mara nyingi hukumbuka diaspora

kutokana na wakazi wa kijiji kujua walikotoka wahenga wao. Mwisho, uhamaji wa waali mara nyingi hukumbukwa kwa undani. Miguro ya familia na watawala wa Mangbetu, kwa mfano, ilisimuliwa kwa karne mbili kabla ya kuundwa kwa ufalme wao.

Lakini kama mchunguzi hatilii maanani ukweli kwamba jadi hueleza itikadi na malimwengu, anaweza akakosea. Kama watu wakiamini kwamba kila kitu kina chimbuko moja, wataamini pia kuwa walihama kutoka mahali hapo pa asili na kuishi waliko sasa. Kuwepo kwa paradiso kunamaanisha kuwa kulikuwa na uhamaji wa asili.

Itikadi inahusika pia na dhamira (mada) zihusuzo asili kama ile ya mwindaji mgeni anayekuwa mfalme. Dhamira hii inakutwa miongoni mwa Waigala wa Niger ya chini, katika falme za savana ya kusini na eneo la Maziwa Makuu, ufalme wa Shambaa Tanzania na dola la Ufipa kati ya maziwa ya Tanganyika na Rukwa. Hadithi hizi zote hazionyeshi uhamaji wa waali bali huonyesha itikadi ya dola. Lakini dola huweza kuwa lilianzishwa na mgeni au kikundi kidogo cha wageni. Kwa hiyo hadithi hizi huhitaji kuhakikishwa kwa njia nyingine, kwa kutilia maanani maana yake mahsusi ya kiishara, na thamani yake kiitikadi.

Kosa jingine linalofanywa kila mara katika kuafsiri mapokezi ni lile la kuichukulia sehemu ya kitu kuwa inawakilisha kitu kizima. Mapokezi yanayohusu asili ya Wakamba, Wameru na Wagikuyu wa Kenya yanaelekea, katika kila moja ya jamii hizo, kuikweza hadithi ya sehemu ndogo ya watu iwe ya watu wote.

Kwa ujumla, kadiri mapokezi simulizi yanavyokuwa na dhamira za kikalamala (kidesturi), ndivyo yanavyokuwa ya mashakamashaka. Na mapokezi ya kikalamala hupatikana katika historia za koo, nasaba, vijiji au familia.

Aghalabu, kimbilio huwa katika isimu ya lugha, lakini taarifa za lugha pia ni ngumu kuzifasili. Kanuni ya kawaida ni kuwa wazungumzaji wa lugha mbili wanapochanganyika, wale walio wengi hulazimisha lugha yao itumike na wachache. Ndio maana uhamaji au upanuzi mkubwa mara nyingi husababisha kuenea kwa lugha ya wahamaji. Na kinyume chake, wageni wachache wanapokutanishwa na wenyeji walio wengi, ama kutokana na diaspora au uhamaji wa kundi, lugha ya wageni ndiyo inayotoweka. Mifano mingi inayodhaniwa kutozingatia kanuni hii kwa kweli haijaikiuka. Jamii ya watu huweza kubaki na lugha yao kwenye diaspora pale tu inaposhikamana sana na kuendelea kuwa na uhusiano na kule ilikotoka. Makundi ya wahamiaji pia hubaki na lugha yao iwapo hawachanganyiki na watu wengine: hali hii ilitokea kwa Watyokosi na Wamende wa Sierra Leone, tofauti na makundi ya Wambangala, ambao waliiacha lugha yao kwa kuwa ilitoweka katika nchi yao ya asili.

Lakini kuna mifano ya kweli ya ukiukaji wa kanuni hii ya usimilishaji wa kilugha unaofanywa na walio wengi kwa wachache, ambao unaweza kutokana na heshima iliyopata lugha ya wachache. Kindebele na Kikololo zilidumu Zimbabwe na Zambia kwa sababu zilikuwa lugha za washindi, kuliko sababu ya kuwa ziliandikwa na kutumiwa mashuleni mara baada ya ushindi. Vinginevyo, zingemezwa na lugha za walio wengi za Kishona na Kiluyi.

Kanuni ya pili ya msingi ni kwamba lugha inayomezwa mara zote huacha alama

katika lugha inayoimeza, kwa njia ya maneno ya mkopo, misemo, majina ya watu na mahali, au tofauti za maumbo na miundo ya lugha. Uchunguzi wa alama hizo huweza kutoa taarifa juu ya uhusiano miongoni mwa jamii za watu.

Taaluma ya isimu huwezesha kutofautisha uhamaji wa jamii mbalimbali uliotokea. Diaspora ndizo zilizo rahisi kuzitambua kwani husababisha kuwepo kwa lugha nyingi kwa kipindi kirefu katika eneo, au mara nyingine kuundwa kwa krioli. Kiafrikaani ni krioli, kama inavyoonyeshwa na mabadiliko makubwa katika maumbo na miundo yake, pamoja na mchango wa Kimalaya, Kireno, Kibantu na Kikhoi au Kisan. Kibobangi ni krioli ya lugha kadha za Kibantu zinazohusiana. Lugha za diaspora hujitambulisha kwa sarufi yake sahili na msamiati unaotokana na lugha nyingi. Upanuzi huwa na mikopo michache ya lugha. Husababisha lugha kuenea katika eneo pana zaidi kuliko lile lililoathiriwa na uhamaji wenyewe, ambako hulingana na udugu unaoaminiwa kuwepo baina ya watu. Kwa upande mwingine, katika uhamaji wa halaiki, ueneaji huo hauhusiani sana na udugu. Uhamaji wa halaiki mara nyingi huleta mchanganyiko wa zaidi ya lugha mbili. Walangi hawawezi kuwa walihusika na uhamaji wa halaiki kwani lugha yao, Kiluo, imeathiriwa na lugha moja tu, Kikarimojong. Kundi la wahamaji linapokuwa kubwa la kutosha, hulazimisha lugha yake kutumika katika eneo linamotamakani na kuacha alama zake katika maeneo lilimopitia, mradi tu lugha hiyo haifanani sana na lugha zinazokutwa hapo.

Lakini tatizo kubwa la matumizi ya uchambuzi wa kiisimu ni kuwa iwapo maneno ya mkopo hayatachunguzwa kwa undani kwa kutumia njia ya kulinganisha "maneno na vitu," haitawezekana kujua kama mikopo hiyo haipaswi kunasibishwa na sababu nyingine zaidi ya uhamaji wa watu kama vile uhusiano wa kibiashara, athari za dola pale ambapo lugha hiyo huzungumzwa na familia ya watawala au heshima ya lugha ya kidini. Uchunguzi kama huo unaweza kuwa mgumu lakini huweza kuwa na matokeo yenye manufaa sana.

Akiolojia mara nyingi imetumiwa kusaidia kuthibitisha kuwepo kwa upanuzi au uhamaji pale ambapo vifaa vinavyofanana au vilevile vya utamaduni wa vitu au mila za namna moja (kama vile mabuli ya mazishi) vinapatikana katika sehemu mbalimbali. Lakini wana-akiolojia hawafuati tena nadharia hii ya "uhamaji" kwa kutambua kwamba uvumbuzi huria hutokea mara nyingi kuliko ilivyofikiriwa awali, na kuwa vifaa huweza kuenea kwa njia nyingi zaidi ya uhamaji.

Hata hivyo, katika mifano mingi uhamaji wa watu ndio ulikuwa chanzo kikubwa cha kuenea kwa vifaa. Inapoonekana kuwa aina mpya ya ufinyanzi, iliyo tofauti sana na ile ya mwanzo, inaenea katika maeneo mbalimbali, ni sawa tu kufikiria kwamba imetokana na mtawanyiko wa polepole. Hivyo, akiolojia inaelekea kuthibitisha uhamaji wa watu, unaoitwa *kutama*, kutoka kusini mashariki ya Afrika kwenda Zimbabwe takriban mwaka 1000. Ni bahati mbaya kwamba kuna mifano mingi ya mashaka ya namna hiyo.

Baadhi ya waandishi bado wanatumia mtawanyiko wa makabila kama ushahidi wao wa uhamaji. Mtazamo huu, ambao ulikuwa mtindo uliokubalika wakati fulani, sasa unapingwa kabisa. Hivyo ni hoja isiyoingia akilini kudai kuwa Wafang walihama kutokea Ubangi kwa kuwa tu walikuwa na pinde kama watu wengine wa eneo la

Ubangi. Tabia za kikabila huweza kuenea bila watu kuhama. Kufanana kwao kunaweza kutokana na nasibu tu au uvumbuzi huria. Hakuthibitishi chochote kama hakuhusishwi na mshabaha wa lugha.

## *Uhamaji mkubwa wa watu wa 1500-1800*

Sehemu mbili tu za Afrika ndizo zilizohusika na mtawanyiko mkubwa wa watu uliofuatiwa na kuundwa kwa jamii na tamaduni mpya katika kipindi hiki. Sehemu hizo zilikuwa ni eneo la Pembe ya Afrika, kusini mwa Abbay au Nili ya Bluu ya Juu, likijumuisha sehemu kubwa ya Somalia ya sasa na kaskazini ya Kenya, na pia eneo la mashariki ya Nili Nyeupe kaskazini ya Nyanza na kusini mwa Sabat. Kulikuwa na miguro kadha ya watu katika eneo hili. Uhamaji mashuhuri ni ule wa Waoromo kuingia Ethiopia katika takriban 1535. Ilipofika 1700 sehemu kubwa ya Ethiopia ilikuwa chini ya Waoromo. Wakristo na Waislamu walikuwa wamepoteza mamlaka kabisa katika eneo la kusini magharibi. Wasomali na Waoromo walikuwa wakishindana kupata ardhi nzuri hadi kufikia Mto Tana, na jamii ndogo za watu wasiohamahama zilikuwa zimefukuzwa kutoka Shungwaya, eneo la pwani kaskazini kidogo tu ya mpaka wa Somalia na Kenya. Jamii hizo, wahenga wa Wamiji-kenda, zilitamakani kwenye vijiji vikubwa vyenye ngome (kaya) nyuma ya miji ya bandari kuu za Kenya.

Magharibi zaidi, miguro ya watu ilianza mapema zaidi, labda takriban mwaka 1000, wakati wa uhamaji wa Waluo kandokando ya Nili Nyeupe. Makundi mengi yalikuwa yakihama, hasa wale wanaoitwa Wakaramojong, Waturkana, mashariki zaidi, na Wamaasai na Wanilo wa kusini. Watu wote hawa, isipokuwa Waluo, walikuwa wafugaji hasa, kama Waoromo na Wasomali. Wote walikuwa wakitafuta ardhi "tupu" - ardhi ambayo haikuwa na watu wengi. Uhamaji wao ulitegemea sana mazingira asilia. Hivyo, Waluo walihitaji ardhi yenye maji ya kutosha, ilhali wanomadi waliofuga ngamia, Wasomali na Waoromo wa kusini, wangeweza kuishi kwenye maeneo makame. Ni mara chache sana kwa watu kubadili mtindo wao wa maisha. Katika sehemu nyingine, wakati upanuzi ulipokuwa ukifikia mwisho, mapambano ya kijeshi yalitokea baina ya watu wenye aina moja ya uchumi. Hivyo, Waluo wa Kenya waligombea ardhi na majirani zao mnamo karne ya kumi na nane, na makundi mbalimbali ya Wamaasai yalipigania ardhi mnamo karne ya kumi na tisa. Ni dhahiri kuwa shinikizo la wingi wa watu lililohusika hapa.

Uhamaji huu wa watu ulikuwa ndio hasa hadithi ya kukaliwa kwa ardhi zilizo pembezoni, angalau hadi karne ya kumi na nane. Ardhi nzuri zenye maji ya kutosha, kandokando ya Nili, ndizo zilikuwa za kwanza kuchukuliwa na wakulima ambao walifuga pia. Waliwafukuza wageni waliotaka kupanua maeneo yao jinsi idadi yao ilivyoongezeka. Uhamaji huu ulibainisha utengemano uliokuweko mahali kwingineko katika bara hili, ambako watu walikuwa wameyadhibiti vizuri maeneo.

Imewahi kudokezwa kuwa ukame uliachangia sana katika kuleteleza hajira hizi za watu huko kaskazini mashariki ya Afrika, lakini sababu hiyo haitoshi kuelezea miguro hiyo ya watu, na kuanguka kwa himaya yenye nguvu ya Ethiopia vilevile si sababu ya

kutosha. Sababu za msingi zinaweza kupatikana kwenye mivutano baina ya maeneo yaliyokuwa na watu wengi zaidi, kama ilivyokuwa katikati ya nchi ya Waoromo na labda miinuko ya Ethiopia, na yale yasiyokuwa na watu wengi kama Uganda na Kenya ya kaskazini na Mabonde ya Ufa ya Kenya na Tanzania. Ilipofika 1700 maeneo haya yanayoelezewa yalikuwa yamekwisha kaliwa na makundi mapya yaliyokuwa na uchumi na jamii zenye kuruhusu watu wengi zaidi kuishi mahali pamoja.

Kwingineko, hajira za watu zilikuwa zikitokea kwa kiwango kidogo zaidi. Kusini kabisa mwa Afrika makaburu wahamaji walikuwa wakichukua kwa nguvu nyanda za Karroo kwa kuwafukuza au kuwaua wafugaji waliozikalia, na huko Namibia Waherero na Wanamib walijipanua kwa kuwadhulumu wenyeji Wasan na Wadama. Kandokando ya Kalahari kulikaliwa, kama ilivyokaliwa ardhi kame ya Uganda na Kenya kaskazini. Lakini kusini mashariki eneo kubwa lililokuwa na ukosefu wa urari lilikuwa likijengeka jinsi idadi ya watu ilivyoongezeka na kumaliza raslimali. Dalili za kwanza za ukosefu wa utengemano, labda, zilionekana katika mguro wa Watonga kuelekea kaskazini hadi kusini mashariki mwa Zimbabwe, na uhamaji wa vikundi vya washambulizi kuingia Zimbabwe yenyewe.

Katika msitu wa mvua wa Afrika ya Kati na katika savana za inayojulikana sasa kama Jamhuri ya Afrika ya Kati, miguro ya halaiki ilikuwa ikiendelea, lakini polepole, ikiweka urari unaoridhisha baina ya idadi ya watu na raslimali zilizokuwepo. Mzururo wa makundi ya Wamongo kuelekea kusini ulisababisha kuundwa kwa ufalme wa Kuba na temi zenye nguvu za kaskazini mwa Kasai ya chini. Kati ya Mto Kongo na Ubangi watu waliongezeka lakini katika viungaviunga. Bado iliwezekana kwa watu kama Wangbandi wa bonde la Ubangi kuzururia kusini, kuvuka mto. Lakini ilipofika karne ya kumi na nane kulikuwa na dalili ya kuzidi mno kwa idadi ya watu na katika nusu ya pili ya karne kulizuka watu wapya, Wazande. Walienea haraka mashariki kuelekea mto Nili, wakiunda temi kadhaa. Magharibi ya msitu wa mvua wa Afrika ya Kati uhamaji wa mizururo wa mara kwa mara uliwachukua watu waliotamakani kwenye makutano ya mto Mbam na Sanaga hadi kwenye maeneo yasiyokuwa na watu wengi ya kusini, na mara nyingine, magharibi.

Miguro mingi midogomidogo ya watu ilitokea kutokana na kuundwa au kuanguka kwa madola. Katika Afrika Magharibi, kudidimia kwa himaya ya Mali kunaelekea kulisababisha Wasusu, Wabaga na Wanalu kuondoka Futa Jallon na Wamane kuhama kwa makundi kuelekea Liberia na Sierra Leone. Kukua kwa madola ya Wamossi kunaweza kuhusishwa na kuhamia kaskazini kwa Wadogon, waliotamakani kwenye genge la Bandiagara, na kuundwa, kusini zaidi, kwa dola ya Gonja kutokana na makundi ya Wamande. Kuundwa kwa dola la Asante kulisababisha kupanukia magharibi kwa makundi ya Wabaule na Waagni.

Miguro michache ya namna hiyo inajulikana kutokea Afrika ya Kati. Upanuzi wa himaya ya Lunda kwanza, baadaye ufalme wa Yaka kwenye mto Kwango, ulianzisha uhamaji wa makundi ya majeshi. Miguro ya Lunda ya kusini, na ule ulioanzisha ufalme wa Kazembe, inajulikana zaidi. Huko Malawi, kuibuka kwa makundi ya watu wenye silaha kulitokana na kuundwa kwa madola ya Maravi na Lunda mnamo takriban mwaka

1600. Hajira ndogo ndogo kwa ajili ya upanuzi na uvamizi huko Zimbabwe haziwezi kuelezwa kwa uthabiti kuwa zilitokana na kukua au kudhoofika kwa madola. Baadhi ya miguro ya watu ilihusu zaidi utwaaji wa ardhi zilizokaliwa na wachache huko kusini. Bukini labda ndio mfano muhimu wa miguro ya watu inayotokana na kuibuka kwa falme na temi: uhamaji wa Wamaroserana ni mfano mzuri wa miguro ya namna hiyo. Ilipofika 1500 watu wa kisiwa hiki bado walikuwa wakihamahama, na bado kulikuwa na ardhi tupu. Ilipofika mwaka 1800 karibu kisiwa chote kilikuwa kimekwishagawanywa katika madola anuwai. Wakati wa kuundwa kwa madola hayo maeneo yalidhibitiwa. Huko bara, uundwaji wa madola ulikuwa umekomea sehemu za Tanzania ya kati na kusini, na kaskazini ya Msumbiji.

Ukuaji mkubwa wa njia za biashara za kusini mwa Sahara ulisababisha kuundwa kwa diaspora mpya na kuzikomaza zile za zamani. Kutoka magharibi hadi mashariki diaspora za Wajahanka, Wajuula, Wayarse, Wahausa, Wabobangi, Wavili, Wahungaan, Wabisa, Wayao na Waswahili zilijulikana sana. Zaidi ya diaspora hizo ziongezwe zile za Kizungu: Wafaransa kwenye pwani ya Senegali, Wareno huko Lnanda na Msumbiji na Waholanzi kwenye Ras waliathiri sana bara ya Afrika katika kipindi hiki. Diaspora za Wazungu na Waafrika zilikuwa na jukumu kubwa katika biashara ya watumwa jinsi njia za biashara zilivyoendelea kukua. Watu walioishi karibu na njia hizo kuu mara nyingine walizisogelea au kuzikimbia. Hivyo Waitsekiri walienea hadi pwani ya karibu ili kudhibiti njia za bahari kwenda Benin na wakazi wengi wa Gabon walienea polepole kuelekea delta ya Ogowe ili kufanya biashara huko. Lakini watu walioishi baina ya Kwango na Kasai walielekea kuwakimbia wafanyabiashara na wavamizi, na watu wengi huko Zimbabwe walielekea kuhama kutokana na fujo zilizosababishwa na wapiganaji wa Kireno. Lakini miguro hii yote ya watu ilikuwa ni midogomidogo. Iliwakilisha tu urekebishaji wa matumizi ya nafasi kulingana na maendeleo mapya ya biashara na uhusiano wa kijamii na kisiasa.

## *Hitimisho*

Maeneo ya kuishi yalikwishadhibitiwa katika sehemu kubwa ya Afrika muda mrefu kabla ya mwaka 1500, na wingi wa watu ulikuwa mdogo kiasi cha matatizo yaliyotokana na shinikizo juu ya ardhi kuweza kutatuliwa kwa njia za upanuzi tu. Sehemu hasa iliyokuwa na mwenendo tofauti ni Afrika ya Mashariki, tangu kwenye Pembe ya Afrika hadi Zambezi, ikiwemo Bukini lakini bila kuhusisha eneo la Maziwa Makuu. Nusu ya kaskazini ya eneo hili kulikuweko na uhamaji wa halaiki, aina mpya za maskani na upanuzi wa haraka wa wafugaji. Katika nusu ya kusini na Bukini, aina mpya ya utawala, ikihusisha uundwaji wa falme na temi, ilisaidia kuleta utengemano kwenye makazi na kushadidisha matumizi ya ardhi.

Ongezeko la watu halikuwa na athari kubwa kwa Afrika ya kipindi hiki kwani lilifidiwa kwa urahisi na miguro ya watu. Ni katika sehemu chache tu tunapoona kuibuka kwa teknolojia mpya iliyowezesha matumizi bora zaidi ya ardhi na matokeo yake – ongezeko kubwa zaidi la idadi ya watu. Kasamansi ya chini, nchi ya Igbo, mbuga za Kameruni, milima ya maeneo ya Maziwa Makuu, kandoni mwa bonde la ufa

la magharibi kulikokuwa na mifumo ya asili ya umwagiliaji mashamba na kilimo kikubwa cha migomba, uwanda wa juu wa Kukuya na aina zake za kipekee za urutubishaji ardhi au bonde la Zambezi ya juu - haya yalikuwa na bado ni maeneo yaliyotofautiana na mengine katika Afrika ya magharibi na kati. Bila ya kueleza kwa kina hapa kwa nini ongezeko la watu halikuwa kubwa zaidi, inabidi angalau tueleze kwamba idadi kubwa ya Waafrika iliondoka barani kutokana na biashara ya watumwa ya kuvuka Atlantiki.

Nje ya Afrika ya mashariki, miguro ya watu iliathiriwa hasa na kuibuka na kuanguka kwa madola na upanuzi wa mitandao ya biashara. Ingawa baadhi ya madola makubwa ya Saheli ya Afrika Magharibi yalianguka, asilimia ya maeneo yaliyodhibitiwa na madola ilikuwa juu zaidi mwaka 1800 kuliko ilivyokuwa mwaka 1500.

Mtandao mpana wa njia za biashara na makazi ulikuwepo Afrika Kaskazini na Magharibi muda mrefu kabla ya karne ya kumi na sita. Kulikuwepo pia njia chache za biashara Afrika ya Kati, lakini zilikua tu mnamo karne za kumi na saba na kumi na nane, zikiunganisha Bahari za Atlantiki na Hindi. Kuenea kwa mitandao ya biashara kuliwezesha raslimali zitumike kwa wingi kama ambavyo, kisiasa, madola yalidhibiti maeneo makubwa kuliko temi na miungano ya vijiji. Kwa kuiunganisha Afrika na mabara mengine, njia za biashara ziliiingiza bara hili kwenye mpangilio msonge wa ulimwengu, mfumo ambao kuanzia mwaka 1500 na kuendelea, ulikuwa ukitawaliwa zaidi na Ulaya.

Karne hizi tatu hazina budi kuonekana kuwa ni sehemu ya mlolongo mrefu wa mabadiliko. Kwa kulinganishwa na nusu ya milenia iliyotangulia, kipindi hiki watu wa Afrika walitengemaa zaidi na walidhibiti nafasi yao vyema zaidi.

Lakini bado tunajua mambo machache sana kuhusiana na miguro ya watu. Taaluma za demografia ya kihistoria na historia ya teknolojia bado ni changa katika Afrika. Tunahitaji data zaidi na tunahitaji hasa kubadilisha dhana kama "uhamaji" ambazo si dhahiri, kwa kufanya uchambuzi ulio makini zaidi. Hapo ndipo tutakapoweza kuielezea kikronolojia dhamira ya msingi katika historia ya Afrika: ile ya kutwaliwa na kukaliwa polepole na taratibu kwa bara hili na wakazi wake.

# 4 *Afrika katika historia ya ulimwengu: uuzaji nje wa watumwa kutoka Afrika na kuibuka kwa mfumo wa uchumi wa Atlantiki*


## *Utangulizi*

Ijapokuwa katika enzi za Wayunani-Warumi biashara ya watumwa ilikuwa jambo lililojulikana wazi katika maeneo yaliyozunguka bahari ya Mediterania, uuzaji nje wa watumwa kutoka bara la Afrika kwenda nje unarudi nyuma hadi kwenye karne ya tisa. Biashara hii ilihudumia zaidi maeneo yaliyoizunguka bahari ya Mediterania (yakijumnisha sehemu za kusini za Ulaya), Mashariki ya Kati na sehemu za Asia, na ilendelea kwa karne kadhaa, ikidumu hadi mwanzoni mwa karne ya ishirini, lakini idadi ya watumwa waliosafirishwa nje kila mwaka haikuwa kubwa sana. Hata hivyo kutokana na kuanzishwa kwa unyonyaji wa Wazungu katika Dunia Mpya, kulikofuatia safari ya Kristofa Kolumba (Christopher Columbus) mwaka 1492, biashara kubwa ya watumwa kutoka Afrika, ikihusisha idadi kubwa zaidi ya watu, iliongezwa kwenye biashara ya zamani: hii ndio iliyokuwa biashara ya watumwa ya kuvuka Atlantiki ambayo ilidumu kuanzia karne ya 16 hadi katikati ya karne ya 19. Nafasi ya biashara hii katika historia ya ulimwengu bado haijaonyeshwa kwa usahihi.

Kwanza ni lazima ifahamike kwamba biashara ya watumwa sio kitu kilichofanyika Afrika pekee. Dunia imeshuhudia utumwa wa kibiashara tangu enzi ya utawala wa Warumi. Rekodi za kihistoria zinaonyesha wazi kwamba mataifa yote ya ulimwengu kwa kipindi kimoja au kingine yamehusika katika kuuza watu wake wenyewe utumwani katika nchi za mbali. Kwa karne nyingi vikundi asili vya watu huko Ulaya ya mashariki na kati (hasa watumwa wa Ki-*Slav* ambao jina lao ndilo limeipa lugha ya Kiingereza neno *slave* lenye maana ya "mtumwa") vilitoa watumwa kwa ajili ya Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini.

Ingawa hivyo, kwa upande wa historia ya ulimwengu, biashara nje ya watumwa kutoka Afrika, hasa biashara ya kuvuka Atlantiki, ni ya pekee, hasa kwa kuzingatia ukubwa wake, kuenea kwake kijiografia na uchumi wake.

Ugumu wa kuukilia nafasi halisi ya biashara hiyo katika historia ya ulimwengu umefungamana na tatizo la chimbuko la kihistoria la utaratibu wa uchumi wa dunia wa wakati ule. Ubishani juu ya jambo hili unatokana na mambo kadhaa: Kwanza ni udhibiti wa ruwaza za mawazo ya wanazuoni mbalimbali unaotokana na mitazamo




4.1 *Biashara ya Atlantiki kwenye karne ya kumi na nane na mapema karne ya kumi na tisa*

tofauti ya kitaaluma inayowaongoza; pili, athari za kisiasa kuingilia maelezo ya kitaalamu; na tatu, upungufu wa taarifa za kutosha za kuweza kutumiwa na wanazuoni wengi.

Katika sura hii, jitihada zitafanyika ili kuchanganua athari za biashara ya watumwa kutoka Afrika katika muktadha wa mabadiliko ya utaratibu wa uchumi wa ulimwengu kuanzia karne ya 16. Utaratibu wa uchumi unaweza kufasiliwa kuwa ni mfumo wa mahusiano ya uchumi unaokumbatia nchi kadhaa, na wakati huohuo ukigawa majukumu na maslahi miongoni mwao kupitia mtandao wa biashara. Uendelezaji wa mfumo wa namna hiyo wa mahusiano ya uchumi wa kimataifa unamaanisha mabadiliko ya miundo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa katika nchi wanachama ambayo yanawezesha utendaji wa mfumo huo kudumishwa moja kwa moja kwa nguvu za soko. Mara ukishafikia hatua hiyo, marekebisho yoyote muhimu ya mfumo huo yanaweza tu kutokana na vitendo vya makusudi vya kisiasa, labda vikisahabishwa na mabadiliko ya utawala kwenye nchi moja au zaidi katika mfumo huo.

Hapa, mahali pa kuanzia ni kwenye dhana kwamba utaratibu wa uchumi unaounganisha eneo kubwa linalojumuisha kanda anuwai za ulimwengu ulizaka katika zoni ya Atlantiki katika karne ya 19. Kanda hizo zilikuwa Ulaya ya Magharibi, Amerika ya Kaskazini, Amerika ya Kilatino, na visiwa vya Karibiani na Afrika. Kitovu cha utaratibu huo kilikuwa ni Ulaya ya Magharibi na baadaye Amerika ya Kaskazini, wakati Amerika ya Kilatino, visiwa vya Karibiani na Afrika zikiwa pembezoni, na zote zikiwa na miundo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa yenye kuoana na dhima yao. Upanuzi wa utaratibu wa uchumi wa Atlantiki kwenda Asia na sehemu zilizobakia za Ulaya katika karne ya 19 na ya 20 ulileteleza utaratibu wa uchumi wa dunia wa kisasa, ambao hadi sasa umefanyiwa mabadiliko kidogo sana. Kanda ziliyokuwa kitovu na zile za pembezoni katika utaratibu wa uchumi wa Atlantiki katika karne ya 19, zimeendelea katika nafasi zile zile tangu wakati huo, japo katika utaratibu mpana zaidi.

Sura hii inadhamiria kuonyesha kwamba biashara ya watumwa kutoka Afrika ilikuwa ni kichokoo muhimu kabisa katika maendeleo ya utaratibu wa uchumi wa Atlantiki katika karne ya 19. Katika kuimarisha hoja hii, kutafanyika jitihada za kuonyesha, kwa upande mmoja, dhima ya biashara ya watumwa ya Afrika na utumwa huko Marekani katika mageuzi ya kibepari ya Ulaya ya Magharibi na Amerika ya Kaskazini na, kwa upande wa pili, dhima ya mambo hayohayo katika kuibuka kwa miundo tegemezi katika Amerika ya Kilatino, visiwa vya Karibiani na Afrika hadi katikati ya karne ya 19.

## *Methodolojia*

Mara nyingi wanazuoni wanatumia viunzi tofauti vya taamuli ambavyo huwafanya wawe na mitazamo tofauti kwa hakika za kijamii zinazofanana. Jambo hili linasaidia kuelezea mengi kuhusiana na ubishani kuhusu kukwama kwa maendeleo na

utegemezi. Kwa upande mmoja yapo maoni yasiyopambanua (aina za maendeleo ya kijamii) yaonayo kuwa mabadiliko yote ya kijamii hupelekea kwenye maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kwa upande mwingine, hasa miongoni mwa wanazuoni wa tapo la "kukwama kimaendeleo na utegemezi," mabadiliko ya kijamii, yanatofautishwa: upambanuzi unafanywa kati ya mielekeo miwili ya mabadiliko ya kijamii, moja likielekea kwenye maendeleo ya kiuchumi na jingine kwenye ukwamishaji wa maendeleo na utegemezi. Yote haya ni mabadiliko, na kwa hali hiyo yanaweza kuchunguzwa kihistoria.

Kwa kuzingatia hatua za kihistoria zinazoleteleza hali ya sasa ya uchumi wa mataifa, maoni yasiyotofautishwa ya mabadiliko ya kijamii yameshindwa kutoa maelezo ya kutosheleza kuhusu jambo hili. Mabadiliko ya kijamii yamekuwa yakiendelea katika jamii zote kwa karne nyingi. Kama mabadiliko yote ya kijamii hatima yake ingekuwa ni maendeleo ya kiuchumi, basi ni dhahiri kwamba hadi wakati huu uchumi wa dunia nzima ungekuwa umeendelea. Bali, hata kwa fasili yoyote ile ya dhana ya "maendeleo ya kiuchumi" ni nchi chache tu humu duniani ambazo leo zimeendelea. Idadi kubwa ya nchi zilizobakia zinaweza tu kutarajia kuendelea kwa kuchukua hatua kali kama zile zilizochukuliwa na China. Hivyo ni wazi kwamba mabadiliko ya kijamii ambayo kwa karne kadha yameupeleka uchumi wa nchi hizi kwenye hali yake ya sasa, hayakuwa mchakato wa maendeleo bali kitu kingine kabisa. Ni mchakato wa kihistoria ambao wachanganuzi wengine wameuita mwenendo wa ukwamishaji wa maendeleo na utegemezi.

Mtazamo wa wananadharia ya ukwamishaji wa maendeleo na utegemezi unahitaji kuchunguzwa kwa makini zaidi. Mabadiliko ya kijamii yanamaanisha kuweka miundo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Mchanganyiko wa aina fulani za miundo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa huleta maendeleo ya uchumi, lakini mchanganyiko mwingine husababisha vikwazo vya maendeleo. Hivyo, kiuchanganuzi, aina tatu za uchumi zinaweza kubainishwa: usioendelea, ulioendelea, uliokwamishwa.

Uchumi ulioendelea uchukuliwe kumaanisha uchumi wenye muundo imara wa ndani wenye kuhusisha sekta mbalimbali, unaosaidiwa na teknolojia iliyoendelea pamoja na miundo ya kijamii na kisiasa yenye kuruhusu ukuaji unaojihimili. Uchumi uliokwamishwa na tegemezi ni uchumi ambao haukuratibiwa vizuri kimuundo na kisekta kwa sababu ya miundo kadhaa ya ndani inayotokana na mahusiano ya awali ya kimataifa, ambayo inasababisha ugumu mkubwa katika kuleta maendeleo ya teknolojia na kutoa mwanya kwa hali ambamo kupanuka au kunywea moja kwa moja kwa uchumi kunategemea sekta ya nje. Mwishowe, uchumi usioendelea ni ule ambao hauna miundo ya kuleta maendeleo wala ya kukwamisha maendeleo, hivyo bado upo huru kuelekea upande wowote ule kulingana na fursa zitakazojitokeza.

Hivyo, ili kuelewa athari za kiulimwengu zilizosababishwa na mchakato ulioúnda uchumi wa kimataifa, tunahitaji kuchunguza aina za miundo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa ambayo mchakato huo uliivyaza katika uchumi (wa mataifa) mbalimbali. Katika hilo, litakuwa jambo la busara kutumia nadhariatete ya ukwamishaji na utegemezi, ambayo ni kwamba, wakati wa enzi ya biashara iliyotangulia ubepari,

mageuzi ya kibepari ya nchi zilizotokea kuwa kiini cha uchumi wa dunia yalisababisha, wakati huo huo, uimarishaji na upanuzi zaidi wa mifumo ya kijamii ya kabla ya ubepari katika maeneo yaliyokuja kuwa ya pembezoni. Kama hivyo ndivyo mambo yalivyokuwa, basi ni dhahiri kuwa maendeleo ya nchi za kiini yalisababisha kuzuka kwa miundo ya ukwamishaji na utegemezi katika nchi za pembezoni. Sura hii imepangiliwa kwa kufuata nadhariatete hii ili kuitathmini dhidi ya ushahidi wa kihistoria.

## *Kiwango cha biashara ya watumwa kutoka Afrika*

Ili kufanya tathmini ya haki kuhusu dhima ya biashara ya watumwa kutoka Afrika katika historia ya ulimwengu, ni muhimu kupata kadirio sahihi iwezekanavyo la kiwango cha biashara hiyo kwa karne zote. Katika hili, maendeleo ya kuridhisha yamepatikana katika tawi muhimu zaidi la biashara hii, yaani biashara ya watumwa ya kuvuka Atlantiki, kwa kuanzia na makadirio yaliyochapishwa na Philip Cartin mwaka 1969. Tangu 1976 wataalamu wengine (J.E. Inikori, C.A. Palmer, E. Vila Vilar, L.B. Rout Jr, D. Eltis na R. Stein) wamechapisha matokeo ya uchunguzi wa kina yaliyozingatia sehemu mbalimbali za makadirio haya.

Ijapokuwa kazi hii ya utafiti haijakamilika, matokeo yote yanaelekea kuonyesha kwamba takwimu za biashara yote ya watumwa ya kuvuka Atlantiki zilizotolewa na Curtin zilikuwa chini mno na zinahitaji kuongezwa kwa asilimia 40. Hivyo makadirio ya Curtin yanayoonyesha jumla ya watumwa milioni 11 waliosafirishwa nje yanahitaji kupanda na kufikia milioni 15.4. Kwa ile biashara ya kuvuka Sahara, Bahari ya Sham na Bahari ya Hindi, makadirio yaliyopo hayana msingi imara. Raymond Mauny alikadiria watumwa milioni 10 kwa kipindi cha kati ya 1400-1900, na Ralph Austen alifikia idadi ya 6,856,000 kwa kipindi cha kati ya 1500-1890; 3,956,000 kwa biashara ya kuvuka sahara na 2,900,000 kwa biashara ya kuvuka Bahari ya Sham na Bahari ya Hindi. Kwa kutumia makadirio ya Austen ambayo yanaonyesha kuwa na msingi mzuri zaidi, basi kiasi cha watu milioni 22 walisafirishwa kutoka Afrika kwenda kwingineko duniani kati ya 1500 na 1890.

## *Mageuzi ya ubepari ya Ulaya ya Magharibi na Amerika ya Kaskazini katika enzi ya biashara ya watumwa na utumwa*

Wakati Kristofa Kolumba alipowasili huko Karibiani mwaka 1492, uchumi wa Ulaya ya Magharibi ulikuwa haujaendelea. Kilimo cha kujikimu na utengenezaji wa sanaa za ufundi kwa njia ya kujiajiri bado zilikuwa ndizo shughuli muhimu zilizokuwa zikifanywa na umma wa wafanyakazi. Miundo ya kijamii na kisiasa iliyokuwepo ni ile iliyowezesha mgawanyo wa pato la jamii ufanywe zaidi kwa kutumia njia za mabavu zisizokuwa za kiuchumi.

Hata hivyo, mabadiliko muhimu yamekuwa yakitendeka huko Ulaya ya Magharibi katika karne tatu au nne za nyuma. Ukuaji wa idadi ya watu na mgawanyo mpya wa

wakazi kikanda wakati wa Enzi za Kati uliamsha maendeleo ya biashara kati ya kanda, na biashara kati ya mataifa. Bidaa kuu zilikuwa zimekwisha ingizwa katika taratibu za (utumiaji wa) ardhi na nguvukazi, na mabadiliko haya yaliandamana na mabadiliko fulani katika miundo ya kijamii. Kwa hiyo mazingira ambayo yaliruhusu uchumi wa Ulaya ya Magharibi kutumia fursa iliyojitokeza kutokana na mfumo wa Atlantiki yalikuwa yameandaliwa.

Bila shaka sio kila uchumi wa Ulaya ya Magharibi ulipitia mabadiliko hayo kwa kiwango hicho hicho mwishoni mwa Enzi za Kati. Uingereza hasa ilishuhudia mabadiliko makubwa kutokana na mchanganyiko wa athari za biashara ya sufu na ongezeko la idadi ya watu. Tofauti hizi bayana za viwango vya mabadiliko kati ya nchi na nchi ndizo sababu ya kuwepo kwa kasi tofauti za mageuzi ya kibepari ya nchi za Ulaya ya Magharibi kati ya karne ya 16 na 19.

Ili kuweza kuchanganua taathira za kuibuka kwa mfumo wa Atlantiki kwenye uchumi wa Ulaya ya Magharibi, tutatofautisha vipindi viwili: 1500-1650 na 1650-1820.

Katika kipindi cha kwanza, uchumi na jamii za ukanda wa Atlantiki hazikuwa zimekwisha ibua muundo ambao ungeruhusu nguvu za soko kuhimili kikamilifu opereshreni ya mfumo mmoja wa uchumi ambao ungeweza kugawa majukumu na kutawanya maslahi miongoni mwa nchi wanachama. Matokeo yake, Ulaya ya Magharibi ilitumia ubora wake wa kijeshi kudai rasilmali kutoka chumi na jamii nyingine katika ukanda huo.

Rasilimali muhimu ambazo ziliingia Ulaya ya Magharibi kutoka sehemu nyingine za eneo la Atlantiki katika kipindi hiki zilikuwa almasi na dhahabu. Hizi zilitoka hasa Amerika ya Hispania (makoloni ya Hispania katika Dunia Mpya), biashara ya dhahabu kutoka Afrika ya Magharibi ikiwa imepungua kasi kutokana na ongezeko la biashara ya watumwa. Kutoka Hispania, almasi na dhahabu kutoka Dunia Mpya zilitawanywa kote Ulaya ya Magharibi, na kuchapusha mchakato wa kuugeuza uchumi uwe wa kibiashara. Mwingiliano kati ya ongezeko la haraka la kiasi cha fedha iliyokuwa kwenye mzunguko na ukuaji wa idadi ya watu ulileteleza kile kilichojulikana katika historia ya Ulaya kama mapinduzi ya bei katika karne ya 16.

Kuagizwa kwa dhahabu ya Marekani kuliamsha ukuaji wa biashara ya kimataifa ndani ya Ulaya. Huko Hispania walioruhusiwa kubeba bidhaa kutoka na kuingia Amerika ya Kihispania walikuwa ni raia wa Hispania pekee pamoja na meli zao; na biashara hiyo ilibaniwa kwenye bandari mbili tu Ulaya nzima, Cadiz na Seville. Hata hivyo mipango mbalimbali ya chinichini iliwawezesha wafanyabiashara kutoka nchi nyingine za Ulaya kushiriki katika biashara hii na Amerika ya Kihispania.

Kwa hiyo, katika karne ya 16, Hispania ilikuwa kitovu cha biashara kubwa ya kimataifa iliyotawaliwa na Uholanzi, Ufaransa na Uingereza. Almasi na dhahabu kutoka Amerika ya Kihispania iliondoka Hispania miezi michache tu baada ya kuingia huko na kuingizwa katika uchumi mkuu wa ukanda huo, ikichochewa na hatua za mageuzi. Kama alivyoandika A. Christelow: "Hispania ilitunza ng'ombe na sehemu

nyingine za Ulaya zilikunywa maziwa." Hali hii iliendelea moja kwa moja kwenye karne ya 17 na 18.

Katika kipindi cha pili, miaka ya 1650-1820, uundaji wa uchumi na jamii za eneo la Atlantiki ulifikia upeo wake, na mchakato wa mageuzi ya kibepari katika Ulaya ya Magharibi ulianza kutegemea mfumo wa Atlantiki. Dhima ya mfumo huu wa Atlantiki katika maendeleo ya uchumi wa Ulaya ya Magharibi inaweza tu kutambuliwa iwapo itatazamwa dhidi ya usuli wa zahama ya jumla ya Ulaya ya Magharibi katika karne ya 17.

Uingizwaji wa dhahabu ya Marekani ulifikia kilele chake kwenye miaka ya 1590 na kisha ulipunguza kasi yake. Kadhalika, kasi ya ongezeko la watu ilipungua. Sera ya utaifa wa kiuchumi iliyofuatwa na nchi kadhaa za Ulaya katika karne ya 17 ilifanya hali iwe mbaya zaidi. Kuta za ushuru zilizojengwa na Ufaransa, Uingereza na nchi nyingine ili kulinda viwanda vyao vya ndani zilileteleza kudidimia kwa hali ya uchumi hadi kuwa zahama ya kijumla, na kusababisha kuanguka kwa biashara kati ya kanda mbalimbali. Hatua za mageuzi ya kibepari zilisitishwa katika nchi kadhaa, wakati katika nchi nyingine kinyume chake kilifanyika, Italia ikiwa imeathirika zaidi kuliko nchi nyingine.Asili na chanzo cha zahama ya karne ya 17 inadhihirisha kuwa,ili hatua za mageuzi ya kibepari ziweze kukamilika, ukanda huo ulihitajifursa kubwa zaidi za kiuchumi kuliko zile ambazo ziliweza kupatikana Ulaya peke yake.

Mabadiliko yaliyotokea wakati wa kutengeneza miundo ya uchumi na ya jamii katika maeneo ya Atlantiki yasiyokuwa ya Ulaya kati ya 1650 na 1820 yalitoa fursa kubwa pamoja na changamoto, ambazo zingebadilisha kabisa hali ya uchumi katika Ulaya ya Magharibi. Katika Dunia Mpya, uzalishaji wa vito vya thamani uliendelea kuimarika, lakini kiini cha muundo wa uchumi pamoja na jamii za ukanda huo kilikuwa ni kustawi kwa mashamba makubwa ya kilimo. Katika bara la Amerika ya Kaskazini, mazao yalikuwa hasa ni tumbaku na pamba; lakini katika Amerika ya Kilatino na nchi za Karibiani, sukari ndiyo iliyotawala. Kiwango cha utendaji wa uchumi mpya kilikuza haja ya kuipatia Dunia Mpya wakazi wapya kabisa.

Kiasi kikubwa cha biashara kilihusiana na shughuli za usafirishaji wa bidhaa kwa meli kutoka Afrika na Amerika, watumwa kutoka Afrika kwenda Amerika, na mazao ya kilimo na vito vya thamani kutoka Amerika kwenda Ulaya ya Magharibi. Kwa vile wamiliki wa makoloni kutoka Ulaya ya Magharibi walizuia usafirishaji huria wa bidhaa, udhibiti wa usambazaji wa bidhaa kutoka Amerika huko Ulaya lilikuwa ni jambo muhimu katika ukuaji wa biashara miongoni mwa mataifa ya Ulaya kwenye karne ya 17 na 18. Wanufaikaji wakuu wa maendeleo haya walikuwa Waingereza, Wafaransa na Waholanzi. Kufuatana na maoni ya F. Crouzet, mwana historia mchumi wa Ufaransa, "kwa kweli karne ya 18 inaweza kuitwa ni hatua ya Atlantiki ya maendeleo ya Ulaya."

Fursa mpya za uchumi zilizoletelezwa na upanuzi wa mfumo wa Atlantiki ziliongeza ajira na kusisimua ongezeko la idadi ya watu Ulaya ya Magharibi kote baada ya poromoko la karne ya 17. Ukuaji wa masoko ya ndani huko Uingereza, Ufaransa na Uholanzi, ukichanganywa na ukuaji wa bidhaanje, ulisababisha shinikizo

la mahitaji ambalo lilichochea ugunduzi na bidaa za kiteknolojia za karne ya 18 pamoja na mageuzi ya viwanda Ulaya ya Magharibi katika karne ya 19. Kwa njia hii, upanuzi mkubwa katika uzalishaji wa bidhaa, biashara, mitaji ya fedha na usafirishaji wa madini uliotokea kwenye eneo la Atlantiki kati ya 1650 na 1820 uliziwezesha nchi za Ulaya ya Magharibi kuishinda zahama ya karne ya 17, kuvunja minyororo ya uchumi na miundo ya jadi ya kijamii na kukamilisha mchakato wa mageuzi ya kibepari. Nchi ya kwanza kufaulu kufanya jambo hili ni Uingereza.

Ile sehemu ya Dunia Mpya ambayo katika mwaka 1783 ilikuja kuwa Muungano wa Madola ya Amerika (yaani Marekani), lakini ambayo katika karne ya 17 na hadi 1776 ilikuwa bado ni mkusanyo wa makoloni, ilitoa mchango mkubwa sana pia katika upanuzi huu hata katika kipindi hiki cha awali. Wakati Kolumba alipowasili Amerika, labda nchi hizi zilikuwa miongoni mwa nchi zisizoendelea kiuchumi. Msongamano wa watu ulikuwa mdogo sana na nchi hizo zilitawaliwa na shughuli za kujikimu ambazo ziliendelea hata baada ya kukaliwa na walowezi wa Kizungu.

Kuhusika kwa nchi hizi katika mfumo wa Atlantiki katika miaka iliyotangulia kidogo tu Tangazo la Uhuru kulibadilisha kwa kiasi kikubwa hali hii. Katika miaka hii jumla ya thamani ya biashara ya Atlantiki ya Amerika ya Kaskazini ya Waingereza kwa mwaka ilikuwa pauni milioni 8.4. Idadi ya watu ilikuwa milioni 2.2 mnamo mwaka 1770, hivyo thamani hiyo inawakilisha pauni 3.8 kwa kila mtu mmoja. Kukua kwa ushiriki katika mfumo wa Atlantiki kulichochea ukuaji wa soko la ndani na uzalishaji kwa ajili ya kubadilishana sokoni, kwani kulihimiza ubobezi, kuongeza pato la kichwa, na kuathiri kiwango cha uhamiaji katika eneo hili.

Jinsi makoloni ya Waingereza ya Amerika ya Kaskazini yalivyosogea taratibu kutoka shughuli za kujikimu kwenda kwenye uzalishaji kwa ajili ya soko chini ya athari za mfumo wa Atlantiki, kanda tatu za kiuchumi, zikijumuisha makoloni ya kusini, kati na kaskazini (hasa New England) zilijidhihirisha. Mchanganyiko wa rasilimali maridhawa za asili na nguvukazi rahisi ya watumwa wa Kiafrika ulihimiza makoloni ya kusini kupanua kilimo cha viunga, yakianza na mpunga na tumbaku, kisha pamba. Makoloni ya kati yalijihusisha na uzalishaji wa mazao ya chakula kwenye mashamba ya kifamilia. Makoloni ya kaskazini kwa kiasi fulani yalikuwa maskini kwa rasilimali asilia za kilimo, lakini yalikuwa yametunukiwa bandari za asili na maliasili ya misitu kwa ajili ya kujengea meli, na hali hii iliyafanya yabobee katika biashara na shughuli za meli. Kwa hali hii, eneo la kusini lilizalisha karibu bidhaa zote za mashambani ambazo zilisafirishwa kwenda Ulaya, wakati eneo la kaskazini lilizalisha idadi kubwa ya bidhaanje zisizoonekana (meli, wafanyabiashara, huduma, bima n.k), na makoloni ya kati yalizalisha vyakula kwa ajili ya kuuza nje pamoja na kutoa huduma za usafirishaji.

Tofauti hizi za kishughuli katika mfumo wa Atlantiki zilizua miundo ya kiuchumi na kijamii yenye kutofautiana. Katika makoloni ya kati na yale ya kaskazini, uzalishaji ulifanywa na nguvukazi huru ya watu weupe, umiliki wa mali ulikuwa umeenea na mapato kugawanywa kwa usawa. Katika makoloni ya kusini, kilimo cha

mashamba makubwa kilichotegemea nguvukazi ya watumwa wa Kiafrika, kilisababisha kuwepo kwa idadi kubwa ya watumwa miongoni mwa wakazi, ulimbikizaji wa mali nyingi mikononi mwa watu wachache, na mgawanyo wa mapato usiokuwa na usawa hata kidogo. Kati ya watumwa 697,000 waliokuwepo Marekani mwaka 1790, watumwa 642,000 walikuwa kwenye nchi za kusini ambako walifanya asilimia 36 ya jumla ya watu wote. Wakati miundo ya kwenye makoloni ya kati na yale ya kaskazini ilihimiza ukuaji wa soko la nyumbani kwa ajili ya bidhaa za matumizi ya halaiki, miundo katika makoloni ya kusini ilizuia ukuaji wa aina hiyo ya soko la nyumbani na kuhimiza uingizaji wa bidhaa za anasa za kigeni. Kwa hali hii, wakati msingi wa ukuaji wa uchumi wa kujitosheleza wenyewe uliwekwa kwenye makoloni ya kati na ya kaskazini wakati wa ukoloni, miundo tegemezi ilijengwa huko kusini.

Baada ya kupata uhuru, uchumi wa nchi za kusini uliendelea kutegemea nguvukazi ya watumwa wa Kiafrika, ambao ndio wanawawia ule upanuzi mkubwa wa uzalishaji wa pamba kati ya 1790 na 1860. Matokeo yake ni kwamba miundo ya kiuchumi na ya kijamii iliyokuwepo wakati wa ukoloni iliendelea kudumishwa.

Hata hivyo, serikali huru kisiasa ya Marekani ilichukua hatua za kiuchumi ambazo polepole ziliondoa eneo la kusini kutoka hali ya kuitegemea Ulaya na kuwa tegemezi kwa majimbo ya kaskazini. Wakiwa na ulinzi wa serikali, wamiliki wa meli na wafanyabiashara wa majimbo ya kaskazini-mashariki walichukua shughuli za kusafirisha kwa meli pamba ya kusini kuipeleka Ulaya, na kuwaletea wakulima wa kusini na watumwa wao bidhaa za viwandani kutoka Ulaya. Wakati huo huo upanuzi wa uzalishaji wa pamba huko kusini ulisababisha ukuaji wa soko la chakula ambalo nalo lilisisimua ongezeko la uzalishaji wa mazao ya chakula huko magharibi pamoja na mtiririko wa wahamiaji. Kuanzishwa kwa soko kubwa la ndani kulihimiza ukuaji wa viwanda vibadala huko kaskazini mashariki kwa bidhaa zilizokuwa zinaagizwa kutoka nje. Kwa njia hii nchi ya Marekani ilitumia fursa iliyokuwepo ya uhuru wa kisiasa kwa wakati muafaka kudhibiti kwa hila kani (za uchumi na biashara) katika eneo la Atlantiki kwa manufaa ya uchumi wake, ikisaidiwa na miundo sadifu iliyoanzishwa katika makoloni ya kati na yale ya kusini wakati wa kipindi cha ukoloni. Kwa hiyo miundo tegemezi ya nchi za kusini ilijenga mazingira muhimu ya kuleta mageuzi ya kibepari kwa majimbo ya kaskazini na ya magharibi.

## *Kuibuka kwa miundo ya ukwamishaji Amerika ya Kilatino na nchi za Karibiani*

Kwa fasili yetu, nchi za Amerika ya Kilatino na Karibiani zilikuwa na uchumi usioendelea wakati Kolumba alipowasili katika eneo hilo. Mambo matatu yalileteleza kukosekana kwa maendeleo hayo kwa jumla: idadi ya watu, jiografia na hali ya kutengwa na sehemu nyingine za dunia.

Makadirio ya idadi ya watu katika Amerika nzima katika mwaka 1492 yanatofautiana sana, kutoka milioni 8.5 hadi 112. Hata hivyo, utafiti wa hivi karibuni


uliofanywa na shule ya Berkeley, unaonyesha kwamba kiasi cha milioni 50 hadi 100 ndiyo idadi inayokubalika zaidi. Kwa kuwiana na upana wa Amerika kijiografia hata ile idadi ya juu bado inaonekana ndogo. Zaidi ya hayo, kulikuwa na mkusanyiko mkubwa kwenye maeneo matatu: Amerika ya kati, ikijumuisha falme za Azteki na Maya; ufalme wa Inka wa Peru ya kale; na kisiwa cha Hispaniola huko Karibiani, ambacho sasa kina nchi mbili za Haiti na Jamhuri ya Dominika. Maeneo mengine ya Dunia Mpya yalikaliwa kwa uchache sana.

Msongamano mdogo wa watu haukuwa na athari nzuri kwa maendeleo ya biashara na mgawanyo wa nguvukazi. Ilikuwa vigumu kuyafikia maeneo ya msongamano mkubwa kwa sababu ya topografia (maumbile ya nchi), na jambo hili lilipunguza mahusiano ya kibiashara miongoni mwa jamii za Amerika. Zaidi ya hayo Amerika iliendelea kutengwa na sehemu nyingine za dunia hadi 1492, na matokeo yake, utajiri wao mkubwa wa rasilimali asilia ulikuwa na thamani ndogo kibiashara, na hivyo kuwa na mchango mdogo sana katika kupanua idadi ya watu na biashara. Hili linaelezea ni kwa nini mwaka 1492 ustaarabu wa kale wa Amerika ya Kati na ya Kusini ulikuwa umefikia kiwango cha juu cha maendeleo ya kitamaduni lakini nchi hizo zilikuwa hazikuendelea kiuchumi hata kidogo.

Fursa ya kufanya biashara iliyoanzishwa na kuwasili kwa Wazungu ilifika katika hali ambayo ilisababisha kuibuka kwa miundo ya ukwamishaji badala ya ile ya kuendelea. Kwanza, nchi za Ulaya Magharibi zilichukua kwa nguvu udhibiti wa rasilimali asilia ya Amerika ya Latino na Karibiani. Wahindi wenyeji walifedheheshwa na kuvunjwa moyo, kisha walifanyishwa kazi nyingi na kuangamizwa kwa magonjwa yasiyo ya kawaida yaliyoletwa na Wazungu hao na hatimaye idadi yao kuporomoka kabisa katika ukanda mzima. Hivyo idadi ya watu wa Mexico ya kati iliyokadiriwa kuwa milioni 18.8 hadi 26.3 kabla ya kutekwa na Wazungu, ilianguka na kufikia milioni 6.3 mwaka 1548 na ilipofikia 1580 ilikuwa ni milioni 1.9. Ilipofikia 1605 idadi hiyo ilikuwa milioni 1.1 tu.

Angamizo hili kubwa la jamii ya Wahindi lilikuwa na matokeo makubwa mawili. La kwanza ni uingizaji mkubwa wa nguvukazi ya watumwa Waafrika, waliotarajiwa kuchukua nafasi za Wahindi hao; na la pili ni uchukuaji wa ardhi ya kilimo na walowezi hawa wa Kizungu na kuigeuza mashamba makubwa (*hacienda* au *fazenda*). Mabadiliko haya yalitoa fursa ya kufanya biashara ambayo ilisisimua mageuzi ya kibepari ya Ulaya ya Magharibi na Amerika ya Kaskazini, na wakati huo huo kusababisha ukwamishaji na utegemezi katika Amerika ya Latino na Karibiani.

Kiasi kikubwa cha magendo ya uingizaji wa watumwa Amerika ya Kihispania katika karne ya 16 na ya 17 kimesababisha ugumu mkubwa katika kujaribu kupima mchango wa nguvukazi ya watumwa wa Kiafrika katika uzalishaji wa vito vya thamani kwenye eneo hilo katika kipindi hicho. Hata hivyo, sensa iliyofanywa na mapadre huko Amerika ya Kihispania mwaka 1796 inaonyesha kwamba kulikuwa na kiasi cha watu 679,842 wenye asili ya Kiafrika huko Mexico na 539,628 huko Peru. Huko Brazil, uzalishaji wa sukari ya kusafirisha nje katika karne hizi moja kwa moja ulitegemea nguvukazi ya watumwa wa Kiafrika; na wakati mfumko mkubwa wa



*4.2 Watumwa wa Kinegro wakitaka miwa kwenye shamba huko West Indies, 1883*

dhahabu ulipotokea katika karne ya 18 kazi hii ilitegemea tena nguvukazi ya watumwa weusi.

Hili linathibitishwa na uwiano wa kimbari wa jamii ya watu wa Brazil katika karne za 18 na 19. Katika mwaka 1798 watu wa asili ya Kiafrika walikuwa asilimia 61.2 ya umma wote wa Brazil, na 1872 waliunda asilimia 58. Idadi kubwa zaidi ya watumwa ilikuwa kwenye mikoa sita iliyozalisha dhahabu na mazao ya shambani kwa ajili ya biasharanje: Bahai, Pernambuko, Rio de Janeiro, Sao Paulo, Minas Gerais na Rio Granda do Sul.

Huko Karibiani, kuanzia nusu ya pili ya karne ya 17, uingizaji wa idadi kubwa ya watumwa wa Kiafrika na upanuzi wa mashamba makubwa ya kilimo uliua kilimo cha kujikimu wakati uzalishaji wa mazao ya biasharanje ukiongezeka kwa kasi kubwa. Uwiano wa kimbari pia ulibadilika sana. Kwa hivyo, kwa kuchukua jumla ya watu wa Barbados, Jamaika na Visiwa vya Leeward, idadi ya watumwa iliongezeka kutoka asilimia 40.5 mwaka 1660 kufikia asilimia 80.2 mwaka 1713. Vivyo hivyo, idadi ya watu wenye asili ya Kiafrika katika West Indies ya Wafaransa, iliongezeka kutoka asilimia 52 ya wakazi wote mwishoni mwa karne ya 17 na kufikia asilimia 88 mwaka 1780.

Upandikizwaji huu mkubwa wa nguvukazi ya Waafrika katika Amerika ya Kilatino, Karibiani na nchi za kusini za Amerika ya Kaskazini ndio uliosababisha upanuzi mkubwa wa uzalishaji wa bidhaa na biashara katika eneo la Atlantiki kati ya karne ya 16 na ya 17. Hata hivyo, jambo hili halikuleta athari katika maeneo haya kama zile zilizopatikana huko Ulaya ya Magharibi na Amerika ya Kaskazini. Kwa vile idadi ya watu katika Amerika ya Kilatino na Karibiani ilijumuisha idadi kubwa ya watumwa, kipato cha watu wengi kilikuwa kidogo mno kuweza kustawisha soko la ndani la walaji. Na kwa kuwa faida iliyopatikana kutokana na machimbo na mashamba ya viunga haikuweza kutumika ndani ya nchi, ilibidi itumike kununulia vifaa vilivyotengenezwa Ulaya au ipelekwe Ulaya kugharamia uwekezaji na matumizi ya huko huko. Hali hii ilichochewa na sheria za kikoloni ambazo zilizuia uanzishaji wa viwanda katika Amerika ya Kilatino na Karibiani.

Kukosekana kwa maendeleo ya viwanda katika Amerika ya Kilatino na Karibiani kulichipuza uchumi usio na uwiano mzuri, huku sekta za uchimbaji madini na kilimo zikiwa zimehusishwa kwa karibu sana na uchumi wa Ulaya ya Magharibi, na pia, baadaye, na uchumi wa Marekani. Maendeleo haya yalizua pia himaya za kiuchumi zilizofungamana kwa karibu sana na biasharanje, shughuli pekee ambayo iliwavutia matajiri wa migodi na wamiliki wa ardhi wa Amerika ya Kilatino na Karibiani. Tabaka la wafanyabiashara matajiri vileviele lilijitosa kwenye shughuli za kuingiza na kusafirisha bidhaa nje. Hata baada ya nchi kuu za Amerika ya Kilatino kupata uhuru wa kisiasa katika karne ya 19, serikali ziliendelea kupendelea uzalishaji wa bidhaa za msingi kwa ajili ya kusafirisha nje na kuagiza kutoka nje bidhaa zilizokwisha kusindikwa. Pamoja na hayo, mapinduzi ya viwanda katika Ulaya ya Magharibi na Marekani katika karne ya 19 yalipunguza gharama za uzalishaji na hivyo kurahisisha bei za bidhaa za viwandani ambazo zilikuwa zinauzwa kwenye eneo

la Atlantiki, kiasi cha kuzifanya nchi mpya za Amerika ya Kilatino zilizopata uhuru zilishindwe kuanzisha viwanda vya uzalishaji vya taifa kwa ajili ya soko la ndani. Kwa hiyo, ilipofikia katikati ya karne ya 19, uchumi na jamii za Amerika ya Kilatino na Karibiani zilikuwa zimepata muundo ambao uliimarisha ukwamishaji wa maendeleo na utegemezi.

## *Uwekaji wa misingi ya miundo tegemezi katika Afrika*

Data zilizopo zinaonyesha kwamba jamii zilikuwa zinapitia kwenye hatua kubwa za mabadiliko wakati Wazungu walipowasili mwishoni mwa karne ya 15. Ugunduzi wa akiolojia wa hivi karibuni, kama vile mabaki ya Igbo-Ukwu, unaonyesha kwamba kiwango cha juu cha mabadiliko ya kijamii na ya kiuchumi tayari kilikwisha kupatikana katika maeneo kadhaa wakati huo. Hata hivyo, mchakato wa mabadiliko ulikuwa ndio unaanza, na miundo ya kijamii kimsingi ilikubaliana bado na fasili yetu ya kutoendelea. Idadi ya watu ikilinganishwa na ardhi ya kilimo iliyokuwepo bado ilikuwa ni ndogo sana, na zaidi ya hayo, wakazi walitapanywa kwenye kontinenti pana, vikundi vikiwa vimeteganishwa na vingine kwa masafa marefu na mandhari magumu kupitika. Kuwepo kwa jangwa kubwa kati ya Afrika ya Weusi na Mediterania na Mashariki ya Kati (vituo vya biashara ya kimataifa kwa karne nyingi) kulipunguza bidhaa za biashara kati ya Afrika ya Weusi na sehemu nyingine za dunia na kubakiza zile tu zilizokuwa na thamani kubwa na gharama ndogo ya usafirishaji, yaani dhahabu na watumwa.

Hapo mwanzoni, kuanzishwa kwa biashara ya baharini kati ya Afrika na Ulaya ya Magharibi kuanzia nusu ya pili ya karne ya 15 kulionekana kana kwamba kungetoa fursa ya kuleta aina ya mabadiliko ya haraka ya kijamii na kiuchumi yaliyokuwa yanahitajika katika Afrika ya Weusi. Biashara ya dhahabu ilipanuka. Biashara ya mazao ya kilimo kama vile pilipili, ilianzishwa, na kichocheo kilitolewa kwa watengezaji wa nguo wa Afrika, kwani Wareno na Waholanzi walishiriki katika kusambaza nguo hizo hadi sehemu mbalimbali za pwani ya Afrika.

Hata hivyo, maendeleo haya ya mwanzoni hayakudumu kwa muda mrefu. Wakati kiasi kikubwa cha rasilimali za Marekani zilipoanza kupatikana huko Ulaya ya Magharibi, dhima ya Afrika katika mfumo wa uchumi wa Atlantiki iligeuka. Idadi ya watu ambayo Afrika ilihitaji kuongeza ili kuweka mazingira ya ndani yenye kuruhusu mabadiliko kamili ya kimuundo ya uchumi na jamii zake ilihawilishwa kwa wingi kwenda Marekani. Hali hii iliyojengwa kwa kipindi cha karne tatu kutokana na uhawilishaji huu mkubwa wa watu ilizuia maendeleo ya uzalishaji wa bidhaa katika Afrika na badala yake kuweka msingi wa miundo tegemezi.

Hasara ya kwanza iliyotokana na uhamaji huu wa kulazimishwa nikufutika kwa ongezeko la idadi ya watu na kupungua kwa watu kwenye maeneo makubwa ya kontinenti hili. Ilikadiriwa kwamba zaidi ya watu milioni 22 walisafirishwa kutoka Afrika ya Weusi kwenda kwingineko duniani kati ya 1500 na 1890.

Ili kuukilia ni kwa kiasi gani usafirishaji nje wa watumwa ulipunguza uwezo wa

watu wa Afrika ya Weusi kuzaliana, uchanganuzi wa umri na jinsi za watu waliosafirishwa nje unatakiwa kufanywa, maana kilicho muhimu hapa ni idadi ya wanawake waliokuwa wamefikia umri wa kuzaa.


Kuhusiana na biashara ya kuvuka Sahara na Bahari ya Sham, wanawake vijana na wazuri ndio waliochukuliwa kwa wingi kutokana na mahitaji ya masuria. Kwa kawaida inaaminika kwamba uwiano wa kijinsia ulikuwa ni wanawake wawili kwa mwanamme mmoja. Kwa biashara ya kuvuka Atlantiki, utafiti wa hivi karibuni sasa unatoa data ambazo zinaweza kutumika kuonyesha uwiano wa kijinsia kwa Waafrika 404,705 waliosafirishwa kwenda nchi za Dunia Mpya katika karne za 17,18 na 19; yaani kiasi cha asilimia tatu ya jumla kuu ya biasharanje huko Marekani. Kwa ujumla wanawake waliunda asilimia 32.9 ya sampuli hiyo.

Uchunguzi wa data za biashara ya kuvuka Atlantiki daima huonyesha tofauti za uwiano wa kijinsia kulingana na kanda za Afrika ambamo watumwa hao wamechukuliwa. Eneo la Nigeria kuanzia Ghuba ya Benin hadi Ghuba ya Biafra, ilitoa idadi kubwa zaidi ya wanawake, kuanzia mbili ya tano hadi nusu ya watumwa wote waliosafirishwa nje. Hata hivyo, eneo jingine muhimu la kusafirisha nje watumwa, lile la Kongo-Angola, mara nyingi lilisafirisha kiwango kikubwa zaidi cha wanaume kuliko wastani wa kawaida. Tofauti hizi za kikanda ni muhimu sana katika kukadiria taathira za kidemografia za usafirishaji nje wa watumwa katika kiwango cha kanda ndogo.

Kwa Afrika yote ya Weusi ushahidi uliochanganuliwa unaonyesha kwamba idadi ya wanawake waliosafirishwa kwa mwaka ilikuwa kubwa sana kiasi cha kupunguza kwa kiwango kikubwa uwezo wa kuzaliana kwa watu. Kwa kuzingatia upotevu zaidi wa idadi ya watu uliosababishwa na kusafirishwa kwenda Amerika (yaani kiasi cha vifo kati ya kipindi cha kutekwa na kipindi cha kusafirishwa nje), pamoja na watu weusi milioni 6.9 waliosafirishwa kwenda sehemu nyingine duniani, ushahidi unaonyesha kwamba idadi ya watu katika Afrika ya Weusi ilipungua sana, angalau kati ya 1650 na 1850. Kadhalika, yale maeneo yaliyotoa idadi kubwa ya watumwa waliosafirishwa kupitia Ghuba ya Benin, Ghuba ya Biafra na Kongo-Angola, hayakosi yaliathiriwa sana na upungufu wa idadi ya watu.

Aidha, kwa vile ushikwaji utumwa kwa idadi kubwa ya waliosafirishwa nje ulifanywa kwa nguvu, biasharanje ya watumwa ilikuwa na athari za uharibifu kwenye miundo ya kijamii na ya kisiasa ya Afrika. Ni kweli idadi kubwa ya wachunguzi wa wakati ule wanadai hivyo. Mwaka 1730 afisa wa kampuni ya *Dutch West India* aligundua kwamba Gold Coast yote ilikuwa imegeuka na kuwa Pwani ya Watumwa, na kwamba tangu kuingizwa silaha za Kizungu, wafalme na wanamfalme walijiingiza katika vita vikali vya wao kwa wao kwa lengo la kuteka mateka ambao waliuzwa papo hapo utumwani. Baadaye katika karne ya 18 mchunguzi Mwafrika, Olaudah Equiano aliandika:

> Kutokana na yale ninayoweza kukumbuka kuhusu vita hivi, yaelekea vilikuwa ni mashambulio ya nchi au wilaya moja ndogo kwa nchi au wilaya nyingine ili kupata



**4.3** *Watumwa wakipakiwa kwenye meli ya Wazungu ya watumwa*

> mateka au mali. Labda yalichochewa na wale wafanyabiashara walioingiza miongoni mwetu bidhaa za Kizungu nilizozizungumzia hapo juu. Njia hii ya kupata watumwa katika Afrika ni ya kawaida, na ninaamini wengi wanapatikana kwa njia hii, na kwa kuteka nyara, kuliko njia nyingine yoyote.

Maelezo haya yanaonyesha uhusiano mkubwa uliokuwepo kati ya biasharanje ya watumwa na vita vya mara kwa mara katika Afrika kwenye kipindi hiki. Upotoshaji mkubwa uliofanywa ni ule wa kuanzisha matabaka ya waungwana wa kijeshi ambayo yalikuwa na ushawishi mwingi kisiasa na kuukilia mwelekeo wa sera ya nchi karibuni katika madola yote makuu ya Afrika katika kipindi hicho. Kuwepo kwa soko kubwa la kuuza nje mateka kuliwafanya wavione vita kama njia ya kupatia mateka wa kuuza badala ya kuwa njia ya kupata eneo kubwa zaidi la nchi ambalo rasilimali zake za asili na watu wake wangeweza kujumuisha (katika himaya) na kunyonywa. Jambo hili lilikuwa na athari mbili hasi kwa madola haya: Kwanza ni kwenye ukubwa wao kieneo, ambao haukupanuka; pili, ni kwenye utengemano wao wa ndani wa kisiasa, ambao ulitetereka sana.

Kwenye jamii kadhaa za Kiafrika kuwepo kwa matabaka haya ya kijeshi, kukiungana na hali ya uchumi iliyokuwepo, kulisisimna ukuaji wa mtindo wa kitumwa wa uzalishaji mali. Idadi kubwa ya jamii za Kiafrika zilikuja kutawaliwa na watu ambao, wakiwa wafanyabiashara au watendaji wa serikali, walihusika moja kwa moja au kwa kificho na biashara ya kusafirisha nje watumwa. Kutokana na upungufu wa rasilimali ya watu ikilinganishwa na ardhi ya kilimo, miundo ambayo ilikuwa imeanzishwa ilibakia hata baada ya kuzima mahitaji ya nje ya watumwa.

Matokeo ya jumla ya michakato hii ya kihistoria ya kipindi cha zaidi ya karne tatu yalikuwa ni kugeuza mwelekeo wa hatua za kiuchumi katika Afrika kutoka kwenye kuendelea na kuelekea kwenye ukwamishaji na utegemezi. Uenezaji wa mtindo wa kitumwa wa uzalishaji katika maeneo makubwa ya Afrika ulikuwa na athari ya kukwaza maendeleo ya masoko ya ndani na uzalishaji kwa ajili ya soko. Zaidi ya hayo, biashara ya kuvuka Atlantiki kwa namna mbalimbali ilizuia maendeleo ya biashara ya bidhaa na Ulaya, jambo ambalo lingechochea ukuaji wa biashara miongoni mwa nchi za Afrika, na uzalishaji kwa ajili ya soko. Hivyo hadi katikati ya karne ya 19, uzalishaji wa kujikimu wa mazao ya chakula uliendelea kutawala uchumi wa Afrika. Hali hii ilizuia limbikizo la mtaji katika kilimo, na hivyo, ongezeko lolote lile la tija katika kilimo cha uzalishaji wa chakula kwa ajili ya soko la ndani. Tija ndogo ya wakulima wa mazao ya chakula katika Afrika leo ni matokeo ya mirathi ya karne tatu za historia, ambayo sura yake ilifanywa kuwa mbaya zaidi na athari za uchumi wa kikoloni katika karne ya 20.

Kiwango cha chini cha mgawanyo wa kazi na udogo wa soko la ndani havikufaa kwa maendeleo ya utengenezaji wa bidhaa zaidi ya hatua ya ufundisadifu. Aidha, maendeleo ya utengenezaji wa bidhaa yalikwazwa na kukosekana kwa udhibiti wa bidhaa za Ulaya na za mashariki zilizobadilishwa na watumwa. Hivyo, hali hii ya ufinyu wa soko la ndani, sekta za kilimo na viwanda zisizo na mtaji, na madola


madogo madogo yenye kutawaliwa na wafanyabiashara na wanajeshi wanaotegemea muundo wa kitumwa wa uzalishaji, iliweka msingi imara wa kuifanya Afrika kuwa tegemezi kwa uchumi wa viwanda wa eneo la Atlantiki. Na kuanzia mwishoni mwa karne ya 19 mfumo mzima (wa utegemezi) ulikamilishwa na utawala wa kikoloni.

## *Hitimisho*

Sasa ushahidi na uchanganuzi unaweza kutolewa muhtasari wake. Wakati Kristofa Kolumba alipowasili Amerika, uchumi wa eneo lote la Atlantiki ungefasilika kuwa ulikuwa haujaendelea. Huko Ulaya, kama ilivyokuwa Afrika na Amerika, utengenezaji wa vifaa ulikuwa katika hatua ya ufundisadifu, na ulikuwa ni sehemu ya kilimo, sekta kuu kabisa ya wakati huo. Mitindo ya uzalishaji ya kabla ya ukabaila ilikuwa imetawala pote. Ilipofikia katikati ya karne ya 19 ufa mkubwa ulishajitokeza kati ya uchumi wa kanda mbalimbali za eneo la Atlantiki. Kwa upande mmoja, viwanda vilivyoendeshwa kwa mashine vilijikusanya kandokando ya Atlantiki, kaskazini-magharibi mwa Ulaya na kaskazini-mashariki mwa Marekani. Kwa upande wa pili, sehemu kubwa ya eneo la Atlantiki ilitawaliwa na bidhaa za msingi: Uzalishaji wa vyakula vya biashara na kilimo cha mashamba makubwa magharibi na kusini mwa Marekani; mashamba makubwa ya kilimo ya Karibiani, uchimbaji madini, ufugaji wa wanyama kwa wingi na mashamba makubwa ya kilimo katika Amerika ya Kilatino; na kilimo cha kujikimu na ukusanyaji usio wa kudumu wa mazao pori kwa ajili ya kusafirisha nje ya Afrika (baada ya kusitishwa kwa biashara ya watumwa). Uchumi na jamii za eneo la Atlantiki tayari ulikwishaunganishwa katika mfumo mmoja wa uchumi uliotawaliwa na nguvu za soko. Hali hii ingeweza, ama kujiendeleza na kujidumisha, ama kubadilishwa kwa vitendo vya makusudi vya kisiasa vya kuleta mageuzi makubwa katika nchi moja au zaidi.

Taarifa zinaonyesha wazi kwamba hali hii hatimaye ilitokana na usafirishaji wa watumwa kutoka Afrika. Mapinduzi ya viwanda huko Uingereza katika karne ya 18 na mwanzoni mwa karne ya 19 na kaskazini-mashariki mwa Marekani katika karne ya 19 yasingeweza kutokea bila upanuzi mkubwa wa uzalishaji wa bidhaa na biashara katika eneo la Atlantiki kuanzia karne ya 16 hadi karne ya 19. Hakuna shaka yoyote kwamba ni nguvukazi ya watumwa wa Kiafrika waliopatikana kutoka Afrika kwa njia ya biashara ya watumwa iliyowezesha upanuzi huu mkubwa.

Wakati upanuzi huu ulichochea ukuaji wa nguvukazi ya ujira huria kuwa ndio mtindo wa msingi wa shughuli za uchumi huko kaskazini-magharibi mwa Ulaya na kaskazini-mashariki mwa Marekani, katika maeneo mengine ya Atlantiki mtindo wa uzalishaji wa kitumwa ulipanuka. Katika Amerika ya Kilatino, Karibiani na kusini mwa Marekani, upanuzi huu ulijenga mazingira yaliyoruhusu maendeleo yasiyolingana ambayo yalisuhulisha ustawi wa haraka wa ubepari katika Ulaya ya kaskazini-magharibi, na pia kaskazini-mashariki mwa Marekani. Mchakato wa kihistoria uliozaa ubepari katika maeneo haya kando kando ya Atlantiki ulisababisha, wakati huo huo, kuimarika na kupanuka kwa mtindo wa uzalishaji wa kabla ya




4.4 Vyanzo vya biashara ya watumwa ya Atlantiki kutoka Afrika katika karne ya 18 na 19 (na J.E. Inkari).

ubepari katika Afrika, Amerika ya Kilatino, Karibiani na kusini mwa Marekani.

Ni muhimu kutambua kwamba wakati utaratibu wa uchumi wa Antlantiki ulipokuwa unaundwa, Ulaya ya Magharibi haikuweza kuanzisha biashara imara na Asia kwa msingi wa kile kilichozalishwa na nchi hizo. Ulaya ilikuwa na bidhaa chache sana za kuuza, zaidi ya dhahabu na almasi iliyotoka Amerika. Hata hivyo ilipofikia karne ya 19, Ulaya ya Magharibi na Amerika ya Kaskazini ziliweza kuoanisha imara uchumi wa Asia kwenye utaratibu wa uchumi wa Atlantiki. Asia iliona ugumu kujizuia kununua bidhaa za viwanda vya mashine, hasa nguo kutoka viwanda vya Uingereza na vya Amerika ya Kaskazini.

Kwa hali hii, kwa msaada wa utawala wa kikoloni, utaratibu wa uchumi wa Atlantiki ulienezwa katika maeneo mengine ulimwenguni, na kuchipuza utaratibu wa uchumi wa ulimwengu wa karne ya 20, ambao mwanzoni ulijengwa kwa jasho na damu ya Waafrika.

# 5

# Diaspora ya Waafrika katika Dunia Kongwe na Mpya

## *Ulaya na Amerika*

Kukosekana kwa nyaraka kunaleta ugumu wa kujua kwa uhakika ni lini Waafrika walifika kwa mara ya kwanza nchini Iberia au sehemu nyingine za Ulaya. Hata hivyo, huenda Waafrika kadhaa kutoka kaskazini na kusini mwa Sahara waliingia wenyewe katika peninsula ya Iberia na Tunisia enzi za kale wakati biashara ya kuvuka Sahara ilipokuwa imestawi.

Waafrika pia walishiriki katika kampeni ya Uislamu huko Iberia mnamo 711, na karne zilizofuata za vita baina ya Waislamu na Wakristo zilishuhudia Waafrika wakipigana kama askari na kutumikia kama watumwa. Ni kweli, mapema katika karne ya 13, wafanyabiashara wa Kimoori (machotara wa Kiberiberi na Kiarabu) walikuwa wakiuza watumwa kutoka kusini mwa Sahara kwenye magulio ya Guimaraes huko kaskazini mwa Ureno.

Kutekwa kwa Sabta (*Ceuta*) mwaka 1415 na Wareno kulifungua enzi ya kujipenyeza kwa Wazungu ndani ya Afrika. Waafrika walichukuliwa na kupelekwa Lisbon mwaka 1441, na hiki ndicho kilikuwa kitangulizi cha biashara ya watumwa ambayo iliendelea hadi kwenye euzi za sasa. Kati ya 1450 na 1500 Ureno iliingiza kiasi cha watumwa wa Kiafrika 700 hadi 900 kila mwaka. Katika mwaka 1468 ufalme wa Ureno ulianzisha ukiritimba (*asiento*) juu ya biashara ya watumwa kusini mwa mto Senegal.

Matangazo ya Papa Nikolas V (1454) na Kalikstus III (1456) ambayo yalielezea upanuzi wa Wareno katika Afrika kama vita vya msalaba vya kueneza Ukristo ndani ya kontinenti, kwa kiwango fulani yalihalalisha kuwatia Waafrika utumwani. Hoja hii iliungwa mkono zaidi na kisasili cha Kibiblia cha Ham, mtoto wa Noah, ambaye wahenga wake walisemekana kuwa walilaaniwa na kutupwa utumwani.

Huko Hispania na Ureno watumwa weusi walifanya kazi kwenye machimbo, mashambani, kwenye majenzi, kama maaskari, walinzi, watumishi wa majumbani, vijumbe, makuli, na vibarua wa viwandani; wanawake walikuwa masuria. Wale ambao hawakuwa watumwa walijikuta wakifanya kazi duni na za kuchosha kuliko zote.


Uuzaji na utumiaji wa watumwa ulikuwa hasa ni ada ya mjini, kwa vile nguvukazi ya Waafrika ilipatikana zaidi kupitia bandari na miji hasa Barselona, Kadiz, Seville na Valensia huko Hispania, na Lisbon huko Ureno. Maisha ya mjini yalitoa fursa kadhaa kwa watumwa kutoroka, na katika maeneo mengine waliweza kujinunulia uhuru wao. Waafrika "huru" walikutana na kujaribu kuanzisha moyo wa kijumuiya na kulinda maslahi yao. Udugu wa kidini ulianzishwa huko Barselona 1455, Valensia 1472 na Seville 1475. Vyama hivi vilifadhili shughuli za burudani, vilikusanya fedha za kuwanunulia watumwa wengine uhuru na kununua viwanja vya kuzikana, kwa vile watu weusi walitakiwa kuzikwa kwenye maeneo tofauti.

Watu huru wengine weusi walipata heshima katika jamii ya Hispania. Kristobal de Menesses alifanywa kuwa padre mashuhuri wa shirika la Dominika; Juan de Pareja na Sebastian Gomez walikuwa wachoraji/wapaka rangi; Leonardo Ortez alikuwa mwanasheria. Mwaka 1475 Juan de Valladolid aliteuliwa kuwa msimamizi wa watu weusi wa Seville. Jambo la kusifika zaidi ni lile la Juan Latino, mwanazuoni mweusi, aliyetunukiwa digrii mbili kwenye chuo kikuu cha Granada na kuwa mhadhiri wa chuo hicho hicho.

Hakukuwepo na sera rasmi kuhusu biashara ya watumwa kwenda Dunia Mpya hadi mwaka 1518, wakati Charles I wa Ureno alipotangaza sera ya *Asiento de Negroes* ambayo ilikuwa na athari ya kushadidia ushindani katika biashara ya watumwa wa Afrika. Ijapokuwa ilikuwa chini ya utawala wa Hispania, Ureno ilianzisha ukiritimba kamili wa biashara ya watumwa kwa ajili yake yenyewe mnamo 1600, ikifanya mikataba na Wahispania, Waholanzi na Wafaransa. Mwaka 1713, kufuatia vita vya urithi vya Hispania, ukiritimba huu ulikwenda Uingereza, nchi ambayo kuanzia wakati huo ilikuwa mwuzaji mkuu wa watumwa duniani.

Ingawaje, idadi ya Waafrika waliokuwa wakiishi Uingereza kwenyewe ilikuwa ikiongezeka wakati wote. Mwaka 1556 Elizabeth I alinena kwamba kulikuwa na "Wamoori-weusi" wengi mno nchini Uingereza, na kwamba walitakiwa kurejeshwa Afrika. Kuanzia karne ya 18, wakulima wa West Indies walianzisha tabia ya kuandamana na watumwa wao wa majumbani wa Kiafrika wakati waliporejea nyumbani kwa matembezi. Maofisa wa kijeshi, mabaharia na makapteni wa meli za watumwa nao walifanya vivyo hivyo. Polepole umiliki wa watumwa weusi ulikuja kutambulika kama alama ya hadhi ya kijamii. Magazeti ya London, Bristol, Liverpool na kwingineko yalitoa orodha ya watumwa wa kuuchuzwa na kuchapisha matangazo ya watumwa waliotoroka. Huko Uingereza wasaka watumwa walipata uzoefu mkubwa wa kukamata Waafrika wasiokuwa na hifadhi ya kisheria. Wengi wao walitambuliwa kwa alama za moto zilizotiwa kwenye miili yao na wamiliki wa watumwa hao. Athari za kisaikolojia za udhibiti huu wa watu weupe kwa watu weusi hazikadiriki. Mchakato wa kumdhalilisha Mwafrika ulikuwa tayari umeanza kufikia karne ya 18.

Lakini lilizuka suala la kutaka kujua hadhi ya Waafrika waliokuwa wanaishi Uingereza. Waingereza wengine walifikiri kwamba kuingia katika Ukristo kulitakiwa kuandamane na uhuru na haki za binadamu waliostaarabika pia. Granville Sharp




*51. Marekani na Afrika (ilichukuliwa kutoka kwenye mwami iliyochorwa na Dkt. Dulal C. Goswami, Idara ya Jiologia na Jiografia, Chuo Kikuu cha Howard, Washington D.C.*

alikuwa mmoja kati ya wale waliopigania ukomeshaji wa utumwa.

Alitetea kesi za watumwa wa Kiafrika kwenye mahakama, hasa mwaka 1772, wakati wa kesi ya James Summerset ambaye alikuwa ametoroka na kukamatwa tena. Lord Mansfield, ambaye alihukumu kesi hii, hakukomesha utumwa bali alitoa hukumu ya kwamba bwana wa mtumwa kisheria hakuweza kumlazimisha mtumwa kuandamana naye kwenda ng'ambo. Uamuzi huu ulitoa ishara ya mwanzo wa kuporomoka kwa utumwa huko Uingereza.

Huko Ufaransa watu walianza kutambua kuwepo kwa Waafrika katika karne ya 15. Hiki kilikuwa kipindi ambacho mabaharia wa Kifaransa walitembelea sehemu kadhaa za pwani ya Afrika ya Magharibi, na kuwapeleka Waafrika weusi huko Ufaransa, kwanza kama ushuhuda wa safari zao na baadaye kwa lengo la kuwauza kama watumwa.

Mwanzoni kuanzishwa kwa utumwa huko Ufaransa hakukuwa kumekusudiwa. Kwa hakika mahakama ya kifalme mwaka 1571 ilitangaza: "Ufaransa, mama wa uhuru, haipokei watumwa." Hata hivyo vitendo vilitofautiana kutoka tukio moja hadi jingine. Baadhi ya Waafrika walifanywa watumwa, wakati wengine walibakia huru kwenye mazingira ya chuki kali. Watazamaji kadhaa walishuhudia kuwepo kwa Waafrika kwenye miji kama vile Angers, Lyon, Orleans, Nantes na Paris. Walikuwa wakifanya kazi za utumishi, kwenye majumba ya watu na hata kama matarishi kwenye nyumba za malodi. Wengine walikuwa askari, kama wale waliokuwa kwenye kikosi cha *Saxe-Volontaires*, ambacho kiliundwa na watu kutoka Guinea, Kongo na Bukini; askari hawa walishinda katika mapigano mengi Ulaya katika karne ya 18. Mtu mweusi mashuhuri katika jeshi la Ufaransa alikuwa Jenerali Alexandre Davy Dumas (1762-1806), aliyezaliwa na baba Mfaransa na mama wa Kiafrika, ambaye mwanaye na mjukuu wake walipata sifa kuu katika ulimwengu wa sanaa.

Kuanzia mwishoni mwa karne ya 17, Waafrika walikuwa wakiingia Ufaransa kwa idadi ya kutosha, na wakati wa karne ya 18, sera ya kifalme iliruhusu Wafaransa waliomiliki watumwa huko Marekani kuwaleta watumwa wao Ufaransa.

Ni machache sana yameandikwa kuhusu kuwepo kwa Waafrika katika maeneo mengine ya Ulaya. Hata hivyo, inajulikana kwamba, kiasi fulani cha Waafrika, hasa wajumbe wa serikali ya Ethiopia na mahujaji, walitembelea Ulaya kipindi cha mwishoni mwa Enzi za Kati, na Waafrika wengine walikuwa wakiishi Venisi, Vatikani na miji ya jirani.

Watu wa Venisi walikuwa ni wafanyabiashara ya watumwa na wamiliki wa watumwa pia. Ijapokuwa watumwa wengi wanaonekana walikuwa na asili ya Kizungu na Kiasia, wengine walikuwa ni Waafrika. Nyaraka zilizopo ni chache mno kuweza kutoa picha halisi ya maisha ya Waafrika huko Venisi na maeneo ya jirani. Ripoti nyingine zinadai kwamba waliingizwa kwenye familia za wenyeji, kitu ambacho kinaweza kuelezea kutoweka kwao kabisa mwishoni mwa karne ya 18. Wote walitakiwa kubatizwa, na hilo huenda lilisaidia kuinua hali zao.

Athari za kusisimua zaidi za kutawanyika kwa Waafrika zilitokea upande wa pili wa Bahari ya Atlantiki, huko Amerika. Kwa karibu kipindi chote cha karne ya 15,

biashara ya watumwa ilifanyika tu katika nchi za Karibiani na Amerika ya Kati na ya Kusini. Biashara hii ilihusishwa na maendeleo ya mashamba makubwa ya Wareno huko Brazil na yale ya Waholanzi huko Guyana. Awamu ya karne ya 16 ya biashara hii ilitukia sawia na kushiriki kwa Afrika katika upelelezi wa Amerika. Waafrika mia mbili waliandamana na Alvarado kwenye ziara yake ya kwenda Kito, na wengine walijiunga na ziara ya Pizarro kwenda Peru. Mashuhuri miongoni mwao alikuwa Estervaniko, ambaye alitoa mchango mkubwa katika upelelezi wa Wahispania huko New Mexico na Arizona. Waafrika pia walishiriki katika ziara ya Wafaransa ya huko Kanada na katika utiishaji wa bonde la Mississippi.

Mwaka 1619 merikebu ya Waholanzi ilileta "Wanegro" ishirini huko Jamestown wakiwa ni vibarua wa mkataba. Kuanzishwa huku kwa nguvukazi ya Waafrika kuliamsha ari ya kutaka kuwa na wafanyakazi weusi na kanuni mbalimbali ziliwekwa ili kudhibiti uhuru wao. Hili lilihitimishwa kwa kuanzishwa rasmi kwa utumwa katika makoloni ya Waingereza ya Amerika ya Kaskazini mwaka 1660, na ilipofikia mwishoni mwa karne, Waafrika walishushwa hadhi kisheria na kuwekwa katika kundi la watumwa, wakifananishwa na mali ambayo iliweza kuuzwa au kutendewa vinginevyo kwa matakwa ya mabwana zao, bila kuzingatia kuwa nao pia walikuwa wanadamu.

Wakati huo huo, Uingereza na Hispania zilikuwa zikigombea utawala huko Karibiani. Mashamba ya sukari yalihitaji idadi kubwa ya nguvukazi na watumwa wengi waliagizwa kutoka Gold Coast, Angola, Kongo, Nigeria, na Dahomey, na ilipofikia miaka ya 1690 walitakiwa pia huko Bukini.

Kufikia miongo ya mwisho ya karne ya 17, Waingereza na Wafaransa walikwishatamalaki huko Karibiani na utumwa uliendelezwa huko Jamaika na Barbados, na kuwa mfano kwa Amerika ya Kaskazini. Zaidi ya hayo, huko Karibiani vituo vya "kuzoeshwa," mahali ambapo watumwa "walitiwa adabu," vilianzishwa. Maasi ya watumwa hawa "waliozoeshwa" yaliigwa na vuguvugu la upinzani miongoni mwa watumwa wa Amerika ya Kaskazini.

Maeneo yaliyokuwa yamekaliwa kwa wingi na watumwa weusi kama vile British Guyana, Jamaika, Brazil na San Domingo (Haiti), ndiyo yaliyoshuhudia njama na maasi makali ya mara kwa mara. Maasi ya kwanza yalikuwa yale ya vita vya Maroon ambavyo vilianzia huko Jamaika 1725, wakati vikundi vya watumwa vilipotorokea milimani na kuanzisha jumuiya zao huko. Guyana iliatilika na maasi kadhaa kwenye karne ya 18. Katika miaka ya 1740, upinzani wa weusi uliwafanya Waholanzi watiliane sahihi mkataba wa urafiki na kiongozi wa Kikoromante, Adoe. Miaka ya 1760 ilijulikana kwa maasi makubwa ya 1763-4 ya Waafrika na Wakrioli yaliyoongozwa na Cuffy.

Lakini ilikuwa huko Brazil ambako mapambano ya silaha ya Waafrika yalifikia kiwango kisichotarajiwa na kudumu kwa muda mrefu zaidi, angalau katika karne ya 17. Katika nchi ya Palmares, jumuiya huru ya Waafrika waliokadiriwa kuwa 20,000, wengi wao wakiwa Wabantu kutoka eneo la Kongo-Angola, ilidumu kuanzia 1605 hadi 1695. Walijitahidi kuipangilia jamii yao kulingana na muundo wa jamii za

nyumbani walikotokea, wakapigana na Waholanzi na Wareno pia kabla ya kushindwa kabisa mwaka 1695.

Mapambano haya ya kutafuta uhuru yanaonyesha kuzinduka kwa utaifa wa Kiafrika miongoni mwa watumwa huko Karibiani na Amerika ya Kilatino. Katika mapambano haya, dini za Kiafrika kama vile *obeah* na *vodum* zilikuwa ni zana zenye nguvu katika kupanga mipango. Uislamu pia ulichukua wajibu uliofanana na huo wa dini hizo, hasa kule Bahia ambako Uislamu ulisaidia kuwaunganisha Wahausa na Wayoruba. Katika kipindi hicho hicho, huko Amerika ya Kaskazini, Waafrika waliandaa njama na kuanzisha maasi kadhaa. Mashamba mengi yalikuwa mbali na maeneo yaliyofaa kwa shughuli za maasi, maeneo kama yale ya milima ya Jamaika au misitu ya Guyana. Lakini watumwa wengi kutoka makoloni ya kusini mwa Amerika ya Kaskazini walitoweka na kwenda kuishi miongoni mwa Wahindi, na kwa pamoja wakashirikiana kuvamia mashamba ya jirani. Pia maasi yalitokea huko Virginia na Maryland mwanzoni mwa karne ya 18 mara baada ya kubainikia wazi kwamba mfumo wa ajira ya mkataba ulikuwa ubadilishwe na utumwa wa maisha.

Katika mwaka 1730 njama za watumwa zilifichuliwa katika makoloni matatu ya Virginia, Karolina na Luisiana. Mwaka 1731 maasi yalianza kwenye meli ya watumwa iliyokuwa imetia nanga nje kidogo ya Rhode Island, na miaka minne baadaye, watumwa waliokuwa ndani ya meli ya *Dolphin* walijiangamimza wao pamoja na watekaji wao. Maasi makubwa zaidi kuliko mengine ni yale ya Karolina ya Kusini mnamo 1739, wakati uleule Kudjoe alipokuwa amelizuia jeshi la Waingereza kwenye milima ya Jamaika. Haya yalijulikana kama maasi ya Kato.

Matatizo ya aina hiyo hiyo yalitokea kwenye makoloni ya kaskazini ya Amerika ya Kaskazini, ambako kulikuwa na Waafrika wachache wasiozidi 3,000 miongoni mwa idadi ya watu weupe iliyokuwa mara sita zaidi, na ambako hakukuwa na mashamba. Mwaka 1712 kikundi kilichoongozwa na Mwafrika kutoka Gold Coast kilijaribu kuangamiza kwa moto mji wa New York. Jitihada za aina hiyo hiyo zilifanywa huko Boston mnamo 1723. Mwaka 1741 Waafrika walijaribu tena kuchoma moto jiji la New York, na tukio hili lilitangazwa sana sehemu nyingi. Ilipofikia 1772 ilikuwa inapendekezwa katika makoloni ya Amerika kwamba watu wote weusi waliokuwa huru warejeshwe Afrika au wapelekwe West Indies, kwani walionekana kuwa ndio wachochezi wa upinzani uliokuwepo. Wale walionaswa wakijihusisha na shughuli za kimapinduzi walinyongwa ama kuteswa kikatili.

Kati ya 1750 na 1775, matukio ambayo yangeamua kudra ya Waafrika yalikuwa yanaelekea kwenye upeo wake huko Amerika ya Kaskazini na Karibiani. Jinsi nguvu za Uingereza zilivyozidi kuimarika ndivyo vuguvugu dhidi ya utumwa lilivyoanza kujitokeza huko Uingereza. Mwaka 1772 Lodi Mansfield alifanya uamuzi wake mashuhuri kwamba ilikuwa marufuku kumshikilia mtu utumwani ndani ya visiwa vya Uingereza. Katika makoloni ya Amerika, vuguvugu la kudai uhuru wa kisiasa kutoka kwa Waingereza lilikuwa linaanza kujitokeza miongoni mwa Wazungu.

Mwaka 1776 makoloni ya Amerika ya Kaskazini yalijitangazia Uhuru wao. Waafrika waliojua kusoma na kuandika, bila kujali kwamba walikuwa watu huru au

watumwa, waliungana na Wazungu katika kudai haki ya uhuru. Wengine walipigana bega kwa bega na weupe hao dhidi ya Waingereza. Kikundi cha kujitolea cha weusi na machotara kilitoka koloni la Wafaransa la San Domingo kuja kuunga mkono walowezi waliokuwa wakipigana na Waingereza huko Savannah, Georgia. Huko Amerika ya Kaskazini, mapambano ya uhuru yalikuwa yameanza: Wazungu walikuwa wakitafuta uhuru wao kutoka utawala wa Waingereza, wakati Waafrika walitaka uhuru wao kutoka kwa Waingereza na pia kutoka kwa walowezi wa Kimarekani.

Waafrika katika diaspora ya Amerika walikuwa ni sehemu ya dunia iliyotawaliwa na mataifa ya Ulaya ambamo misukumo mikali ya kiuchumi na kisomi ilikuwa inaunda upya miundo ya kisiasa na kijamii. Wakiwa wamekabiliwa na shinikizo hizo, Waafrika waligawanyika: Wengine waliamini kwamba ukombozi wao ungepatikana kwa kujitambulisha na amali za Kizungu; wengine walitafuta kugundua upya Uafrika wao na walikuwa tayari kuhatarisha maisha yao katika kupinga ukandamizaji wa Wazungu.

Jaribio la huko Sierra Leone liliakisi imani ya kundi la kwanza. Huko London kulikuweko na jumuia kubwa kiasi ya watu weusi, na watetezi wa ukomeshaji wa utumwa walikuwa na wazo la kuwapatia Waafrika huru makazi mapya huko Afrika ili waanzishe jamii zao kwenye misingi ya nguvukazi huru, jamii ambayo ingeeneza Ukristo, kuanzisha mtindo wa uchumi wa Magharibi na kuchangia katika ukomeshaji wa utumwa. Kwa hiyo, mwaka 1787, zaidi ya Waafrika 400 walioachiwa huru walisafirishwa kutoka Uingereza na kupatiwa makazi mapya huko Sierra Leone. Hili lilikuwa jaribio la kwanza la kuwarejesha watumwa wa zamani wa Kiafrika. Jaribio hili lilitoa changamoto kwa jitihada za Waafrika walioungana chini ya uongozi wa Paul Cuffee huko Marekani na kujigharamia kwa lengo la kuwaunganisha upya watu weusi waliotaka kurejea Afrika. Mwaka 1814, jitihada za Paul Cuffee zilifanikiwa kuwarejesha Waafrika 38, na mfano wake ulikuwa kichocheo kwa vizazi vilivyofuata.

Wakati Wazungu waliokuwepo Marekani walikuwa wakiunda asasi za kudhihirisha utamaduni na uhuru wao, Waafrika nao walianzisha idadi kadhaa ya asasi zao. Ijapokuwa Waafrika hao walikuwa na mambo machache sana ya kushikilia utambulisho wao wa asili, kwa vile walikuwa wamekatazwa kuzungumza lugha za Kiafrika, au hata kufuata dini zao, walianza kujiita "Waafrika". Mwaka 1787 mchungaji Mwafrika wa Kimethodi huko Marekani, Richard Allen, katika kupinga ubaguzi wa sera katika kanisa lake, alijiondoa na kuanzisha Chama cha Waafrika Huru, ambacho kilikuwa na malengo ya kidini na ya kijamii. Waafrika wengine waliiga mfano huu katika maeneo mengine huko Marekani. Wakati huo huo, mhubiri mzaliwa wa Barbados, Prince Hall, ambaye alikuwa ameingizwa katika imani ya Kimasoni (inatokana na *Free Masons,* yaani udugu wa siri wa upendo na kusaidiana) na askari kadhaa wa Kiingereza wakati wa Vita vya Uhuru vya Marekani, alijaribu kutafuta haki ya kuanzisha tawi la Wamasoni weusi waliokuwa huru. Wamasoni wa "Haki ya Waskoti" walimpatia kibali cha kuanzisha tawi la Waafrika ambalo yeye alifanywa kuwa Kiongozi Mkuu wake. Hiki ndicho chama cha kwanza cha mtindo wa

udugu wa Magharibi miongoni mwa watu weusi. Jumuiya hizi na vyama hivi vya kidini vilikuja kuwa asasi zenye nguvu kubwa za Wamarekani Weusi katika karne ya 19, kwa vile viliwaunganisha watu weusi kitaifa.

Ingawa vyama hivi vilijitambulisha na mila na utamaduni wa Kiafrika, lakini pia vilikuwa vinaeneza amali za Magharibi kama vile uwekevu (katika matumizi ya fedha), teolojia ya kujinyima, maendeleo ya binafsi kupitia elimu na kazi, na kuwajali wale wasiobahatika kama wao. Hayo ndiyo mambo yaliyomsukuma George Liele, kwa mfano, ambaye alianzisha Kanisa la Kibaptisti huko Marekani na Jamaika mwishoni mwa karne ya 18. Bidaa hizi za mwanzo miongoni mwa Wamarekani Weusi baadaye zilisaidia kuweka msingi wa kuanzishwa kwa utambulisho wa kijamii huko Marekani, Karibiani na Afrika.

Viongozi wengi wa Kiafro-Amerika wa kipindi hiki walikuwa wamejielimisha wenyewe. Phyllis Wheatley, aliyezaliwa Afrika 1753, alikuwa mshairi mashuhuri, Gustavus Vassa, aliyezaliwa Benin 1745 na kupelekwa Marekani na kisha Uingereza, alijihusisha sana na mwenendo wa kupinga utumwa na aliandika kumbukumbu zake (*Simulizi ya Kuvutia ya Maisha ya Olaudah Equiano au Gustavus Vassa)*. Benjamin Benneker, aliyepangwa jina la "Muethiopia" alikuwa mwana-mahesabu na mnajimu mashuhuri.

Waafrika walioishi Ulaya walitoa mchango wao pia katika mapambano ya uhuru na heshima ya binadamu. Baada ya kusomea katika chuo kikuu cha Halle na kile cha Wittenberg, Anton Azmo alirudi kuwasaidia wananchi wenzake huko Gold Coast; Ottobah Cagoano, aliyeachiwa huru kwa uamuzi wa Mansfield, aliandika *Mawazo na Hisia Juu ya Biashara Mbaya na Ovu ya Kusafirisha Watumwa na Kuuza na Kununua Spishi ya Wanadamu.* Barua za Ignatius Sancho zilizochapishwa baada ya kufa kwake zilimthibitisha kama msemaji mkuu wa Waafrika waliokuwa ng'ambo. Huko Ulaya, kama ilivyokuwa huko Marekani, wapinzani Waafrika walipata marafiki weupe kama vile Chama cha Marafiki wa Watu weusi (*Societe des Amis des Noirs)* kilichokuwa huko Paris.

Hata hivyo, ni huko Marekani ambako mapambano ya uhuru yalichukua sura ya kimataifa kwa matukio ya visiwa vya San Domingo. Wakati mapinduzi yalipotokea huko Ufaransa mnamo 1789 kwa kilio cha "Uhuru! Usawa! Udugu!", vuguvugu hilo lilitikisa koloni la Kifaransa la San Domingo, lililojaa mashamba ya miwa yaliyostawi, ambako watumwa nusu milioni na machotara huru 24,000 waliishi chini ya utawala wa masetla 32,000 wa Kifarausa, waliojulikana kwa ukatili mkubwa waliowatendea watumwa wao. Umma wa Waafrika huru ulidai usawa kamili na watu weupe. Kisha mwaka 1791 umma wote wa watu weusi ulianza kuleta vurugu chini ya kiongozi mfanyakazi wa mashambani asiyejua kusoma wala kuandika, Boukman, ambaye aliwaunganisha wafuasi wake kwa miviga ya *voodoo* na viapo vya siri vya mtindo wa Kiafrika ili kufanya maasi dhidi ya mabwana zao. Serikali ya mapinduzi huko Paris ilituma jeshi la kurejesha amani visiwani humo. Ilikuwa ni katika kipindi hiki ambapo mtu mashuhuri alijitokeza katika uwanja wa kisiasa, msomi, mtumwa Mkristo, aliyezaliwa na baba Mwafrika aliyekuwa katika diaspora - Toussaint,



5.2 *Toussaint L'Ouverture wa Haiti*

ambaye alichukua jina la L'Ouverture.

Toussaint aliitisha vita vya msituni ili kuunga mkono jeshi lake dogo; na katika muda wa miaka mitano aliweza kuvishinda vikosi vya Napoleon kwa kusaidiwa na homa ya manjano. Alirejesha amani na ustawi huko Haiti na alisifika duniani kote kwa uwezo wake mkubwa wa kijeshi, ujuzi wa kiutawala, utu na ustadi katika siasa. Haiti na Toussaint L'Ouverture kwa pamoja wakawa ishara iliyotoa mwamko kwa watu weusi waliotamani uhuru, na hata kujitawala, katika maeneo mengine ya Amerika na Karibiani.


Mwanzoni mwa karne ya 19, mhubiri mweusi, Gabriel Prosser, aliandaa maandamano huko Richmond, Virginia, akiongoza watumwa elfu moja. Walitarajia kutumia maandamano haya kupata uhuru wao, lakini gavana aliitisha mgambo. Waafrika wengi, Prosser akiwa mmojawapo, walikamatwa na kunyongwa; lakini mfano wa Haiti ulibakia hai.

Kuingia kwa karne ya 19 kulileta enzi mpya kwa Waafrika waliokuwa wakiishi Ulaya na Amerika. Ni kweli kwamba mifumo mbalimbali ya kisheria huko Ulaya na Amerika haikuwapatia watu weusi usawa wala uhuru wa kweli, lakini kulikuwepo na unyumbufu mkubwa zaidi. Walijifunza kusoma na kuandika hata pale ambapo sheria zilikataza kufanya hivyo; kulikuwepo na kuoana bila kujali rangi, ijapokuwa mambo hayo yaliwachukiza watu wengi; na kusafiri kuliwezesha kuundwa kwa mitandao. Hata hivyo, katika diaspora Waafrika walitambua kwamba hadhi yao duni ilitokana na wao kuwa jamia tofauti, yenye utamaduni tofauti, na hivyo waliona umuhimu wa kujitahidi kuwaokoa ndugu zao pamoja na urithi wao. Umoja huu wa kisaikolojia uliendelea kudumishwa, na kwa kweli uliwapa Waafrika nguvu ambazo hatimaye ziliwawezesha kuanzisha Vuguvugu la Umoja wa Waafrika Wote (*Pan African Movement*), katika karne ya kumi na tisa na ya ishirini.

Hata hivyo, katika kutawanyika Waafrika hawakuweza kukwepa athari za mazingira ambamo walipandikizwa upya, au karne kadhaa za kuatilika na utamaduni wa Kizungu na wa Kimarekani. Lugha yao na mtindo wa maisha vilibadilika na vivyo hivyo amali na malengo yao. Kwa hali hiyo katika kutawanyika huko Ulaya na Amerika, Waafrika walijikuta wakiwa kiungo kati ya Waafrika wa asili na Wazungu-Waamerika.

## *Asia*

Wakati uhamaji wa kushurutishwa wa Waafrika kwenda Ulaya na Amerika ni tukio la karibuni kiasi katika historia ya ulimwengu, biashara ya watumwa kwenda Asia ina historia ndefu zaidi. Kitabu cha *Periphus of the Erythrean Sea* kilichoandikwa katika takriban mwaka 50, kinarejelea watumwa waliochukuliwa kutoka Pembe ya Afrika, na huenda biashara kati ya watu wa pande hizi mbili za Bahari ya Shamu inarudi nyuma kwenye kipindi cha kabla ya kuandikwa kwa historia. Kuanzia karne ya 7, yaani kuanzia kuzaliwa kwa Uislamu, aina fulani ya umoja wa kiutamaduni ulizuka kote kuzunguka Bahari ya Hindi na eneo la Bahari ya Shamu. Miji kadhaa pwani ya




5.3 *Ramani ya Afrika, Ulaya na Asia*

Afrika Mashariki ilisilimis' a, na Waislamu waliendelea kutawala biashara, ikijumuishwa biashara ya wa nwa.

Kwa karne nyingi Utur a na nchi za jirani zilikuwa ndizo vituo vikuu vya kuhifadhia watumwa kutoka Benghazi na Tripoli, na zoni ya kupumzishia misafara iliyokuwa ikitoka bara. Manunuzi ya vijana kadhaa wa Kiafrika huko Konstantinople kwa ajili ya Maliki Petro Mkuu wa Urusi mnamo mwaka 1696 yafaa kutajwa, kwani mmoja kati yao alikuwa Abram Petrovich Hannibal, babu mkuu wa Aleksander Pushkin (mtunzi mashuhuri wa vitabu huko Urusi kwenye karne ya 19).

Inaonekana kama kwamba Hannibal alizaliwa Ethiopia ambako alitekwa na Waturuki. Idadi kamili ya Waafrika wengine waliofika Urusi na maeneo ya jirani kupitia Uturuki haijulikani, lakini huenda hawakuwa wengi. Kwa vile utumwa ulikomeshwa huko Urusi kwenye robo ya kwanza ya karne ya 18, huenda Waafrika waliokuwa nchini humo hawakuwa watumwa bali walikuwa ni watumishi tu.

Watumwa wengi walioingizwa Asia walikuwa ni watoto, na wengi wao walikuwa

ni wasichana. Kutoka bandari za Afrika ya Mashariki, kwa kawaida watumwa walipelekwa kwenye bandari ya Arabia ya Mocha kwenye pwani ya Bahari ya Sham. Kutoka pale wengi walipelekwa Hodeida, Jeddah, Maka na vituo vingine vya kusambaza watumwa huko Arabia. Wengine walisafirishwa kwa meli kwenda bandari za Ghuba ya Uajemi. Mara nyingi bandari za India kama vile Bombay, Goa, Surat, Karikal, Pondicherry na Kalkuta zilipokea watumwa wao kutoka Mocha au kutoka Ghuba ya Uajemi, lakini wengine walifika moja kwa moja kutoka Afrika ya Mashariki.

Huko Arabia, Oman ndiyo iliyoshika nafasi muhimu katika mkakati wa kibaharia na kibiashara huko Mashariki ya Kati. Maskati, mji wake mkuu, ndio uliotawala njia ya kuingia Ghuba ya Uajemi, ambapo idadi kubwa ya watumwa wa Kiafrika walisafirishwa. Waarabu wa Oman waliteka bandari za Afrika Mashariki za Kilwa na Zanzibar mwaka 1784 na 1785 kwa mfuatano huo; na kutokea hapo walidai kutawala maeneo kadhaa ya pwani na kupata watumwa wa kuvuna karafuu na nazi kwenye mashamba ya Waarabu kwenye eneo hilo.

Huko Yemen na Hadramaut, watu weusi wenye asili ya Ethiopia walikuwa wakiishi humo tangu enzi za kale. Huko Aden, watu hawa weusi waliunda kikundi kinachoweza kufananishwa na tabaka-amali la chini kabisa la "wasioguswa" la huko India. Katika maeneo kadhaa mengine ya Arabia ya kusini, watumwa weusi kutoka Afrika walitumikia katika majeshi ya masultani wenyeji, pia waliweza kutumika kama masuria na watumishi wa ndani, matowashi, mabaharia, makuli na vibarua wa mashambani waliofanya kazi kwenye mabwawa ya chumvi na mashamba ya miwa na ya mitende.

Waafrika walikuwa wametapanywa kwenye visiwa vingi vya Bahari ya Hindi. Waholanzi walipata watumwa kutoka Afrika ya Mashariki na Bukini na kuwapeleka Indonesia. Waingereza na Wafaransa waliwahamishia watu wa Afrika Mashariki kama watumwa kwenye visiwa vya Maskarene vya Bourbon na Mauritius. Kupanuka kwa biashara ya watumwa katika karne ya 19 kulizipanua jumuiya za Kiafrika kwenye visiwa hivyo, lakini hata kabla ya kipindi hicho, kulikuwa kumezuka jumuiya ya Wakrioli ambao athari yao iliweza kuhisiwa moja kwa moja kwenye karne ya 19 na ya 20.

Kulikuwa na watumwa wengi zaidi wa Kiafrika kusini mwa Asia kuliko sehemu nyinginezo za Asia, labda kwa kuwa biashara yake na Afrika ilikuwa ya siku nyingi zaidi na yenye shughuli nyingi. Waislamu walidhibiti pwani ya Magharibi ya India na Wahindi walikuwa tayari wamekwisha kulowea Afrika Mashariki. Kulikuweko na watumwa wengi wa Kiafrika nchini India mapema kwenye karne ya 13.

Nusu ya pili ya karne ya 15 ilishuhudia kujitokeza kwa Waafrika katika sehemu moja kaskazini mwa India, Bengal. Waafrika walikuwa wamehamia huko kutoka mkoa wa pwani wa Kalkuta, eneo la Dakha na mikoa kadhaa ya bara. Mtawala wa Bengal, Rukn-ud-din-Barbak (1459-1474), alizoea kuwapandisha vyeo vya juu vya kijeshi na vya kiutawala Waafrika waliokuwa waaminifu. Baada ya kifo cha Barbak 1486, Shahzada, towashi aliyekuwa kamanda wa walinzi wa jumba la kifalme, aliteka

madaraka na kuchukua cheo cha Barbak Shah. Aliuawa na nafasi yake ilichukuliwa na Mwafrika mwingine, ambaye alibakia mwaminifu kwa kiongozi aliyetangulia. Waafrika waliendelea kuwa madarakani hadi 1493 na kutia athari yao katika kipindi hiki kifupi.

Huko Gujarat Waafrika walitumika jeshini, angalau kuanzia karne ya 13, na labda mapema zaidi. Mwaka 1537 mji wa Ahmadabad ulikuwa umewaajiri kiasi cha Waafrika 5,000 katika huduma za serikali. Huko Gujarat Waafrika kadhaa walijitambulisha kwa umashuhuri katika karne ya 16. Wengine kati yao walikuwa makamanda wa kijeshi. Iktitiyar-ul-Mulk, kwa mfano, aliunda jeshi la wanaume 20,000 na kupinga vikosi vya Maliki Akbar wa Mughul. Ikhtiyar alishindwa, lakini aliheshimiwa na Akbar.

Mwafrika mmoja ambaye hapo mwanzoni alikuwa mtumwa, Shaykh Sayyid al Habshi Sultani, alitumikia kama askari katika jeshi la Jhujhar Khan. Alipostaafu alinunua ardhi, akaenda kuhiji Maka na kisha akafanya kazi kwenye mashamba yake, ambayo yalimsaidia kulisha mamia ya watu maskini kila siku. Alianzisha maktaba ambayo iliwavutia wanazuoni wengi. Mwaka 1573 Sayyid (Sa'id) alijenga msikiti huko Ahmadabad ambao ulisifika kwa usanii wake sahili: paa la matao na madirisha mazuri yenye matundu yaliyopekechwa na mabombwe ya mapambo bora ya mana.

Mwafrika mwingine Sidi Bashir, alijenga msikiti wa kusifika huko Ahmadabad, ambao ni pekee kwa maana ya kwamba una minara miwili" inayotikisika." Mnara mmoja unapotikiswa mtikisiko wake huambukiza mnara wa pili.

Karibu sana na Gujarat kulikuwa na Kisiwa cha Janjira, ambacho katika enzi za kale kilikuwa sehemu ya shughuli za biashara ya utajiri mkubwa kaskazini-magharibi ya India, ikijumuisha Bombay ya leo na pwani ya Konkan. Kama tunaweza kuamini mapokeo ya wenyeji, Wasiddi wa Janjira walitokana na Waafrika waliowasili kutoka Gujarat mnamo 1489.

Kuanzia miaka ya 1530, Wareno walianzisha udhibiti wa kisiasa na wa kiuchumi kwenye sehemu ya pwani ya magharibi ya India, hasa pwani ya Konkan, mahali ambapo watumwa wengi wa Kiafrika walipelekwa. Wengi wa watumwa hawa walitoka Msumbiji, na Wareno waliwatumia katika biashara, kwenye mashamba au kama watumishi wa majumbani. Wengine walifunzwa na kuwa mapadre na walimu wa shule za dini, hasa huko Goa, mahali ambapo palikuwa ndio makao makuu ya Wareno kwa makoloni yao ya Afrika Mashariki na Asia.

Kwa kipindi chote hiki, kisiwa cha Janjira kilikuwa na uhuru wake. Ilipofikia karne ya 17, Wasiddi, ambao waliunda idadi kubwa ya Waislamu katika kisiwa hiki, walikuwa ndio wamiliki wakuu wa ardhi. Baraza la wazee la viongozi mashuhuri wa Siddi, walimchagua *nawab*, ambaye alipewa wadhifa wa kiongozi wa kidunia na kiroho. Baada ya kujiwekea msingi wa kisiasa, Wasiddi wa Janjira walitumia nguvu zao za jeshi la majini kupanua madaraka yao na kuenea hadi pwani ya kaskazini-magharibi.

Mwaka 1616 waliunda ushirika na Malik Ambar, mfalme wa *Kihabshi* wa Dekkan huko India ya kati. Majeshi yote mawili yalipigana na Mughul kwa miaka mingi.

Katika karne ya 17, Kampuni ya Kiingereza ya India Mashariki ilifanya jitihada za mara kwa mara za kujaribu kufanya urafiki na Wasiddi waliotawala pwani ya Konkan. Wasiddi waliendelea kulitawala eneo hilo, na Waingereza hawakuweza kudhibiti mamlaka yao hadi baada ya mwaka 1759. Janjiraililetwa moja kwa moja chini ya utawala wa Waingereza katika karne ya 19.

Wasiddi wa Janjira walikuwa na dhima kubwa katika historia ya India. Hakuna shaka yoyote kwamba dini yao (Uislamu) na ujuzi wao wa kibaharia na wa kijeshi viliwasaidia sana. Ni jambo lenye umuhimu mkubwa kwamba kikundi hiki kidogo cha wahamiaji Waafrika kilikuwa na athari kubwa kiasi hicho kwenye sera na vitendo vya Uingereza, Ureno na Uholanzi, na pia kwenye madola ya wenyeji ya Kihindi.

Waafrika pia walilowea kwenye sehemu za ukanda wa pwani ya Malabar kwenye karne ya 17 na 18. Hawa walikuwa ni Wayahudi weusi, madhuria wa watumwa wa Kiafrika, ambao walikuwa wamehama Kochin na Kerala huko India ya Kusini, na kuja kustakimu sehemu za pwani. Wengi wao walikuwa watumishi wa ndani na walioana na wenyeji wao na Wayahudi wengine. Wareno walihusika katika kuwapatia watumwa wa Kiafrika makazi mapya kwenye sehemu kadhaa kandokando ya pwani ya Malabar, hasa maeneo yaliyozunguka Goa, ambayo baadaye katika karne ya 16, yalikuja kuwa moja ya makao yao makuu.

Mwanazuoni na msafiri wa Kiitaliano, Pietro della Valle, aliripoti kwamba watu weusi kutoka Afrika Mashariki na Afrika Magharibi (Waguinea na Wanamsumbiji) walipelekwa kwenye nchi za Wareno kupitia njia za baharini. Wareno waliwafanya watumwa wao wa Kiafrika kuwa watumishi wa ndani, wachukuzi na walinzi wa wasindikizaji wao katika safari zao. Mara nyingi wanawake walichukuliwa kuwa mahawara.

Sehemu nyingine ya India huko Dekkan ilishuhudia kuibuka ghafla na kushika madaraka kwa Mwafrika Malik Ambar, Mhabeshi ambaye alikuwa ameuzwa utumwani mara kadhaa kabla ya kufika India. Umashuhuri wa Ambar katika historia ulitokana na kuwa kamanda wa jeshi lenye nguvu lililopigana chini ya bendera ya mfalme wa Ahmadnagar na kupinga vikali mashambulizi kadhaa ya Wamughul, na hivyo kufanikiwa kuwazuia watawala wa Mughul kuiteka Dekkan katika kipindi chote cha maisha yake. Alikuwa mtawala mkuu wa eneo lililozunguka Ahmadnagar walimokuwa wakiishi maelfu kadhaa ya Waafrika, kutoka 1602 hadi 1626. Alianzisha miji, alijenga mifereji na taratibu za umwagiliaji maji, alichangamsha biashara na Asia na Ulaya na kuwakaribisha wanazuoni na washairi kwenye kitala chake.

Shughuli za Malik Ambar zinathibitisha mambo makuu mawili: mosi, kwamba Waafrika binafsi walikuwa na dhima kubwa na yenye athari katika historia ya India; na pili, kwamba Waafrika waliweza kupata heshima na kuungwa mkono na Wahindi wakati wao wenyewe wakibakia na hisia ya utambulisho wao.

## *Hitimisho*

Historia ya watu wa Afrika imeathiriwa sana na maono yaliyotokana na biashara ya



5.4 *Maliki Ambar, mfalme wa Kiafrika huko India kwenye karne ya kumi na saba*

watumwa kiasi kwamba ni muhimu kusisitiza kuwa Waafrika kwa ridhaa yao wenyewe walihamahama baina ya makontinenti wakiwa ni wafanyabiashara, makasisi, mabaharia, majasuri n.k. Kuwepo kwa watu weusi huru huko ng'ambo kunahitaji kufanyiwa uchunguzi zaidi ili kutoa picha halisi ya ustaarabu wa ulimwengu.

Hata hivyo ni biashara ya watumwa baina ya makontinenti, kuliko kitu kingine chochote, iliyosababisha kuweko kwa watu weusi duniani kote.

Hulka ya biashara hii na matokeo yake ndiyo yaliyowafanya Waafrika, hasa huko Amerika na Karibiani, kuanzisha mapambano ya kudai uhuru. Hatua hii ilianza mwanzoni mwa enzi ya sasa na kuchukua mwelekeo tofauti kabisa wakati Toussaint L'Ouverture alipoibuka kama ishara ya kimataifa ya ukombozi wa Mtu Mweusi kweye miaka ya 1800. Mchakato wa ukombozi uliendelea, licha ya kuwepo kwa utawala wa kikoloni, na huenda ukawa ndilo tokeo muhimu zaidi la kihistoria la diaspora ya Waafrika.

# 6

# *Ushindi wa Waturuki nchini Misri*

Mwanzoni mwa karne ya 16 dola kuu jipya la Kiislamu, yaani himaya ya Kituruki, liliingia katika historia ya Afrika na Uarabuni. Himaya hiyo ilianzia sehemu za Asia Ndogo na katika peninsula ya Balkan, baadaye ikasonga mbele na kuteka sehemu kubwa ya nchi za Kiarabu za Asia Magharibi na Afrika Kaskazini.

Mwaka wa 1516 tawala za Kimamluki za Shamu na Misri zilianguka kutokana na mashambulizi ya jeshi la Uturuki. Mahusiano baina ya Wamisri na Waturuki yalikuwa ni ya mvutano tangu miaka ya 1480, lakini katika mwaka 1514, baada ya ushindi wa kwanza wa Sultani Selim I katika kampeni yake ya kukomesha nguvu za Uajemi, watawala wa Misri walichukua msimamo thabiti dhidi ya utawala wa Kituruki. Selim aliamua kuvunja moja kwa moja ushirika wa usultani wa Kimamluki na wa Kisafavi.

Mwezi Agosti 1516 jeshi la Uturuki liliyafukuza majeshi ya Mamluki huko kaskazini mwa Halab. Ushindi wao kwa kiasi kikubwa ulitokana na ubora wa mafunzo yao, lakini pia ulisaidiwa na usaliti uliofanywa na kikundi kidogo miongoni mwa Mamluki kilichokuwa upande wa Waturuki. Sultani Selim aliitwaa Damasko bila kupata upinzani mkubwa. Alitwaa pia sehemu yote ya Shamu na Palestina hadi kwenye jangwa la Sinai. Washauri wa sultani pamoja na maamiri wa Kimamluki ambao walikuwa upande wa Waturuki walimshawishi Selim akamilishe ushindi wake kwa kuitwaa Misri pia. Selim aliusogelea mji wa Kairo bila matatizo makubwa na akayafukuza majeshi ya Mamluki katika pambano la muda mfupi mnamo Januari 1517. Huo ukawa ndio mwisho wa Usultani wa Mamluki.

Ushindi wa Waturuki dhidi ya majeshi ya Mamluki haukutokana na ubora wa jeshi peke yake. Sababu kubwa ilikuwa ni tofauti za kiuchumi na kisiasa katika nchi hizo mbili. Huko Ulaya na Asia Ndogo, ufalme wa Kituruki ulitawala maeneo ya nchi yaliyokuwa yameendelea kiuchumi, yenye migodi na mali ghafi, vikiwemo vituo vya uzalishaji mali vilivyokuwa vimeshirikishwa katika biashara ya kimataifa. Kwa upande wao, nchi za Mamluki hazikuwa na raslimali za haja za madini, bali zilitegemea sana kilimo na biashara ya kimataifa ya kupitisha, ambayo mkondo wake mkuu - biashara ya viungo vya chakula kutoka mashariki - ulikuwa umeingia mikononi mwa Wareno. Uingizaji wa biashara ya metali safi kutoka Afrika ulikuwa



**6.1** *Sultan Selim I, mshindi wa Misri : (© The Hulton-Deutsch Collection, London)*

umeshuka. Kwa miaka mingi watawala Mamluki walijaribu kufidia hasara waliyoipata kwa njia mbalimbali - kuchota fedha kutoka katika akiba ya taifa, kunyang'anya ardhi na kuongeza kodi mbalimbali. Hatua hizi zilizidisha chuki ya wazawa kwa kikundi-tawala cha kigeni cha wanyonyaji wa Kimamluki.

Ushindi wa Selim ulikuwa na athari kubwa kwa nchi za Magharibi ya Asia na Kaskazini ya Afrika. Ushindi uliopatikana, hasa dhidi ya Misri, ulikuwa na maana kwamba himaya ya Kituruki ingemiliki njia kuu za bahari ya kati na kujaribu kuzishinda nchi nyingine za Kiarabu zilizoko Afrika Kaskazini.

Nchi zilizotekwa kutoka kwa Mamluki zilijumuisha majimbo yaliyokuwa na umuhimu mkubwa kiuchumi, kisiasa, kimawasiliano na kiulinzi. Misri ilikuwa ni nchi muhimu sana hasa kutokana na kilimo chake shadidi, idadi kubwa ya wakazi wake na nafasi yake kwenye Bahari ya Shamu. Aidha, hadhi ya masultani wa Kituruki iliongezeka zaidi kutokana na ukweli kwamba wao walikuwa ndio walezi wa miji mikuu miwili mitakatifu ya Kiislamu ambayo ni Maka na Medina.

Kabla Selim hajaondoka Misri mwezi Septemba 1517, alimteua msaliti wa Mamluki Khayr Bey kuwa mtawala wa jimbo la Misri. Alitawala Misri kama kibaraka wa Sultani na siyo kama msimamizi wa jimbo, hadi alipofariki mwaka 1522. Aliendelea kushikilia cheo chake cha Umamluki cha *Malik al-Umara* (Mfalme wa Maamiri), huku akiendelea kufuata taratibu za Kimamluki katika shughuli za kitala. Alizungukwa na viongozi wa zamani wa Kimamluki ambao walikuwa tayari kufanya kazi katika utawala wake mpya na kuwapa madaraka ya kiutawala, kisiasa na kijeshi. Mfumo wa mamlaka ya sharia uliendelea kuwa chini ya Majaji Wakuu wanne, kila mmoja akisimamia taaluma yake ya sharia. Selim alimwachia Khayr Bey asimamie uchumi wa jimbo. Zawadi za Khayr Bey alizokuwa akituma Istanbul mara kwa mara zilikuwa ni ishara tu ya utii wake binafsi kwa Sultani; hazikuwa kodi ya lazima kwa hazina ya dola.

Khayr alifanya kazi kwa bidii kuhakikisha kuwa anadhibiti raslimali za jimbo lake. Alifuta *ikta* (ukodishaji wa ardhi kwa utaratibu wa kikabaila), akaifanya ardhi hiyo kuwa mali ya umma chini ya dola, na wamiliki wake wa zamani akawapangia kima cha mshahara uliolipwa kutoka hazina ya jimbo. Aliamuru ardhi yote ipimwe na kusajiliwa, na akarekebisha utaratibu wa umilikaji ardhi ambao ulimwezesha kutekeleza jukumu alilokuwa nalo ya kuipelekea nafaka miji miwili mitakatifu ya Hijaz.

Mamlaka ya Khayr Bey hata hivyo yaliwekewa mipaka. Sultan Selim aliacha vikosi imara vya wanajeshi huko Misri ili kuimarisha mamlaka ya utawala wa Kituruki na ikibidi vizuie majaribio yoyote ya Mamluki ya kutaka kurejea tena kwenye madaraka. Vikosi hivi viligawanywa katika makundi mawili ya askari wa miguu (kundi la kwanza ni la Mayeniseri, na la pili ni la Waazabu), na makundi mawili ya askari wa farasi. Ili kuvidhibiti vikosi hivi ambavyo havikuwa na nidhamu ya kutosha, Khayr Bey aliunda kikosi chake maalum cha farasi ambacho kilitokana na askari Mamluki wa zamani na wapya.

Wakati Khayr Bey alipokufa mwaka 1522, maandalizi ya kuuingiza kabisa mji



*6.2 Wajanısari, kama walivyochorwa kwenye michoro ya Kituruki ya Karne ya kumi na sita*

mkuu wa Kairo (katika mfumo wa utawala wa Kituruki) yalikuwa yakiendelea, ilihali nchi ambayo Kairo ulikuwa ndio mji wake mkuu ilikuwa imeshushwa hadhi baada ya miaka mingi ya uhuru na kubakia kuwa jimbo la Uturuki.

## *Migongano miongoni mwa tabaka tawala katika utawala wa Kituruki*

Mwanzoni wa kipindi kipya kulitokea uasi dhidi ya utawala wa juu wa Kituruki. Uasi huo ulianzishwa na makamu mpya wa maliki, Ahmad Pasha, mwaka 1524. Alijitangaza mwenyewe kuwa ni Sultan wa Misri na alianza kutengeneza sarafu zake za fedha. Alifanikiwa kupata wafuasi kadhaa wa makundi ya Kiarabu, na akafikia hata hatua ya kuteka ngome inayolinda mji wa Kairo, lakini baadaye alifukuzwa nje ya mji baada ya kusalitiwa na machifu wa Kibedui ambao mwanzo walimuunga mkono.

Kwa mujibu wa matukio haya, ilionekana wazi kwamba serikali ya Istanbul ilitakiwa kufafanua hadhi halisi ya nchi ya Misri katika himaya ya Kituruki. Hii ilifanywa kwa kutoa amri - *Kanun Name*, iliyotumika kudhibiti mambo ya kisiasa, kijeshi, kiraia na kiuchumi ya Misri. Kwa mujibu wa masharti ya amri hii, makamu wa maliki, aliyeitwa *wali*, ambaye alizoea kushika cheo cha *pasha*, alipewa marupurupu kadhaa kwa mujibu wa taratibu zilizokuwa zikitumika katika ikulu ya Istanbul. Alipewa ngome ya Kairo kuwa makao yake makuu; ngome hiyo ilikuwa pia ndiyo makao makuu ya masultani waliotangulia. Pia alistahili kuwa na walinzi wake binafsi walioitwa *muteferrika*, kama wale aliokuwa nao Sultan wa Istanbul.

Amri ya *Kanun Name* ilikubali kufuata taratibu kadhaa za utawala wa Kimamluki katika fani ya usimamizi wa fedha na utawala wa kiraia. Misri iligawanywa katika wilaya kumi ua nne; kila moja ilikuwa ikiongozwa na *kashif* ambaye kazi yake ilikuwa ni kudumisha utaratibu mzuri wa umwagiliaji maji na kukusanya kodi kutoka kwa wakulima. Eneo la kusini ya mkoa wa Asyut liliachwa chini ya mamlaka ya masheikh wa Kiarabu wa kundi la Hawwara, ambao walilidhibiti eneo hilo baada ya mwaka 1517. Amri ya *Kanun Name* vilevile iliweka sheria ya kuunda ma-*ojak*, majeshi ya kifalme yaliyoanzishwa Misri na Sultani Selim I. Kwa kumsaidia Sultani kuzima uasi, Mayeniseri walifanywa kuwa mhimili wa mamlaka ya Sultani. Kamanda wao, *agha*, alikuwa mmoja wa wajumbe muhimu wa baraza la dola. Zaidi ya hayo, kiwanda cha kutengenezea sarafu ya Kimisri kilijengwa katika eneo la kambi ya jeshi hilo ndani ya ngome.

Askari wote waliopelekwa Misri walilipwa mishahara. Viongozi wa ngazi za juu, wakiwemo makamu wa maliki, Jaji Mkuu na viongozi wengine ishirini na wa nne waliokuwa na cheo cha *sanjak bey*, nao pia walilipwa mishahara, *saliyane*, kutoka hazina ya Misri.

Mishahara hii ililipwa kutokana na kodi ya ardhi, kodi nyingine mbalimbali na ushuru uliotozwa kutokana na bidhaa zilizotengenezwa mijini na katika miji mikuu pamoja na kodi ya kichwa iliyotozwa kwa raia wasiokuwa Waislamu. Kodi ya ardhi

ilikuwa ikitozwa na watawala wa kila mkoa. Katika miji, kodi zilikusanywa na watoza kodi - ma-*kashif* au ma-*emin*, ambao walikuwa wakilipwa mshahara wa kudumu wa mwaka. Kusini ya mkoa wa Asyut, Masheikh wa Kiarabu, kwa mujibu wa utaratibu wa *iltizam* utakaoelezwa hapa chini, waliweza kupandisha kodi katika maeneo yao na kuchukua kile kilichopatikana, ilimradi tu wahakikishe kwamba kazi ya kilimo inaendelea na asilimia fulani ya mapato inalipwa kwenye hazina ya Misri.


Kuanzia mwaka 1525 faida iliyopatikana kila mwaka baada ya kulipia gharama zote za matumizi ilipelekwa Istanbul badala ya Hijaz. Upelekaji wa fedha hizi (*hazine*) ulifanywa kuwa ni moja ya kazi muhimu za mamakamu wa maliki. Misri pia ilitimiza wajibu wake huko Maka na Medina.

Amri ya *Kanun Name* pia ilihalalisha kuyatoza ushuru mashamba ya binafsi yenye kulipiwa kodi yaliyoitwa ma-*iltizam*. Mwanzoni utaratibu huu ulihusu mashamba ya kilimo tu, lakini ilipofikia karne ya 16 utaratibu huu ulienea sehemu nyingi kwa kadri ma-*ojak* na maofisa wao walivyopata madaraka makubwa kuliko wawakilishi wa utawala wa Waturuki. Katika hali hiyo, watoza kodi waligeuzwa kuwa watendaji wasioweza kushauri lolote kuhusu ukusanyaji kodi au masuala mengine yahusuyo sera ya hazina.

Kufikia mwisho wa karne ya 16 viwango viwili vya utawala wa kisiasa vilibuka. Kiwango cha kwanza kilihusu watendaji walioko madarakani, walioteuliwa na utawala wa Istanbul, wakiongozwa na makamu wa maliki. Kiwango cha pili kilijumuisha ma-*ojak* na maafisa wao na ma-*bey* wa ki-*sanjak* na Mamluki wao. Ingawa utawala wa kundi hili haukuwa rasmi, bado ulikuwa na nguvu za kiuchumi na za kijeshi. Na kuanzia mwishoni mwa karne ya 16 na kuendelea, umuhimu wao katika siasa za Misri ulizidi kubainika.

## *Athari ya Waturuki Kaskazini-Mashariki ya Afrika*

Katika karne yote ya 16 Misri ilikuwa na dhima kubwa katika utekelezaji wa sera ya upanuzi ya himaya ya Kituruki. Kutokana na mazingira ya kijiografia, Misri ilikuwa kiungo asilia baina ya Bahari ya Mediteranea na Bahari ya Hindi, kwani njia ya biashara iliyosafirisha bidhaa za Mashariki kwenda Ulaya ilipitia bahari ya Shamu na Misri kwenyewe. Kufikia mwaka 1517 biashara ya Mashariki ilikuwa mikononi mwa Wareno. Baada ya kuishinda Misri, Waturuki walikabiliwa na jukumu la kuwaondoa Wareno kutoka Bahari ya Hindi au angalao kuwazuia wasiingie katika Bahari ya Shamu. Fursa ya kuingilia suala hili ilijitokeza wakati mtawala wa Gujarati alipoomba msaada wa kijeshi kwa Sultan Sulayman dhidi ya uvamizi wa Wareno waliokuwa wameikalia bandari ya Diu. Mapambano haya ya kijeshi alikabidhiwa Sulayman Pasha, makamu wa maliki huko Misri. Alipokuwa njiani kwenda Diu mwaka 1538, Sulayman Pasha aliuteka mji wa Adeni nchini Yemen na akaanzisha utawala wa Waturuki huko. Ingawa alishindwa kuwaondoa Wareno kutoka Diu, Sulayman Pasha alitia nanga Misri ya Juu, na baada ya kufika Aswan, aliendelea na safari yake kupitia mto Nili hadi Kaskazini ya Nubia.




6.3 *Misri ya Kati na ya Juu (al-Said)*

Ilikuwa vigumu kudumisha utawala katika eneo la Misri ya Juu lililotawaliwa na Masheikh wa Kihawwara. Katikati ya karne ya 16 ilibidi utawala wa Waturuki uanzishwe tena huko. Jeshi lililoongozwa na Makamu wa Maliki wa zamani wa Yemen, Ozdemir Pasha, lilipelekwa huko na kuziteka tena Ibrim, Aswan na Say. Jimbo jipya la Berberistan liliundwa na kuwekwa chini ya mamlaka ya *kashif* ambaye aliwajibika moja kwa moja kwa Makamu Maliki wa Kairo.

Katika mwaka wa 1557, Ozdemir Pasha aliteka mji wa Massawa ulioko kwenye Bahari ya Sham na pia Zayla, mkabala na Aden. Aliiteka pia sehemu ya bara iliyotawaliwa na mfalme wa Ethiopia. Mji wa Massawa ukawa kituo kikuu cha Habesh, jimbo jingine la Waturuki katika Afrika, ambalo lilifanya kazi kubwa ya kuweka ulinzi katika Bahari ya Shamu dhidi ya Wareno. Uanzishwaji wa vituo katika Bahari ya Shamu ulikuwa ni muhimu katika kuendeleza biashara ya kupitisha ambamo kahawa ilichukua nafasi ya viungo vya kijadi kutoka Mashariki. Kutokana na umaarufu huu mpya wa kahawa, Misri ilipata faida kubwa kwa biashara hii ya kupitisha.

Utawala wa Kituruki huko Misri ulifikia kilele chake kwenye kipindi cha kuanzia 1517 hadi miaka ya 1580. Hadi wakati huo hakukuwepo na dalili zozote za kudidimia kwa utawala wa Istanbul; kinyume chake, nguvu yake ilizidi kuimarika. Mwaka 1583

jimbo la Misri ya Juu lilianzishwa. Machifu wa Kihawwara waliondolewa na nafasi yao katika utawala kuchukuliwa na ofisa aliyetumwa kutoka Kairo.

Kijadi, Misri ya Juu ilishika nafasi ya pekee katika mpangilio wa kisiasa wa madola ya bonde la mto Nili. Ilitofautiana na sehemu nyingine za Misri katika jiografia yake, mifumo yake ya kijamii, siasa zake, na sifa zake maalumu za kikabila na kidini. Mara nyingi Misri ya Juu ilikuwa ndio kimbilio la wanaharakati waliopapambana dhidi ya mamlaka yalioyundwa kisheria. Ilidhibiti njia za biashara na usafirishaji kwenye mto Nili. Shauku ya Waturuki katika eneo hili ilidhihirishwa na hadhi ya pekee lililopewa eneo hii ndani ya jimbo la Misri. Hivyo, mtawala wa Misri ya Juu, kama mtawala wa Misri nzima, alikuwa na cheo cha "makamu wa maliki", na umuhimu wake kisiasa ulibainishwa na idadi kubwa ya askari waliokuwa chini yake.

## *Migongano ya ndani ya kijeshi*

Kipindi cha amani kilichofuata baada ya kuzimwa kwa maasi ya Ahmad Pasha mwaka 1524 kilidumu kwa miaka 60. Kutokana na kuendelea kuitegemea himaya ya Kituruki kijamii na kiuchumi, katika miaka ya 1580 Misri ilianza kupata matatizo ya kiuchumi kwa mara ya kwanza; matatizo hayo yalipelekea kwenye migongano mikali ndani ya kundi tawala la kijeshi.

Kati ya miaka ya 1598 na 1609 maasi kadhaa yalitokea; yaliongozwa na makundi ya askari wa farasi walioitwa *spahi*, ambao walisakamwa vibaya na mfumuko wa bei. Miaka iliyofuatia ilishuhudia kukua kwa umuhimu wa ma-*sanjak bey* 24, ambao walikuja kuunda jopo kama lile la maamiri maarufu wa usultani wa zamani wa Mamluki. Kwa kuwa walikuwa na vyeo vya juu, waliteuliwa kushika nafasi za juu katika siasa. Hadi kufikia mwaka 1620 walishika ofisi ya *Serdar*, kamanda wa majeshi yaliyofanya kazi ndani na nje ya mipaka ya Misri. Walikuwa na vikosi vilivyosindikiza *hazine* kutoka Misri kwenda Istanbul. Kadhalika, walisimamia vikosi vilivyopewa jukumu la kutoa ulinzi kwa misafara ya mahujaji iliyokwenda Maka. Kufikia karne ya 17, mmoja wao alichaguliwa kuwa *Ka'im Makam* (Kaimu wa Makamu wa Makamu wa Maliki).

Mapinduzi yao ya kwanza makubwa kisiasa yalikuwa ni yale ya mwaka 1631 yaliyomwondoa makamu wa maliki Musa Pasha na kumweka *Ka'im Makam* waliomtaka wao badala yake. Ingawa makamu wa maliki alipinga mabadiliko hayo, lakini serikali kuu ya Uturuki ilithibitisha maamuzi hayo. Kwa kufanya hivyo iliweka mfano ambao uliigwa mara nyingi kwenye miaka iliyofuata. Ma-*bey* na ma-*ojak* walimwondoa Musa Pasha madarakani kwa sababu alijaribu kufuta utaratibu uliokuwa umezoeleka wa askari kuwatoza kodi "ya ulinzi" (*himaye*) wakazi wa mijini kinyume cha sheria. Kodi hiyo mwanzoni ilitolewa kama tahadhari ya kulinda miji isivamiwe na kuporwa, lakini baadaye ikawa ni njia tu iliyotumiwa na askari kujitajirisha wenyewe kwa kuwanyonya wakazi wa mijini.

Nafasi ya Musa Pasha ilichukuliwa na Ridhwan Bey al-Fakari, ambaye alikuwa

makamu wa maliki hadi kifo chake mwaka 1656. Alikuwa kiongozi wa kikundi cha kisiasa cha *Fakariya* kilichokuwa kikipingana na kile cha *Kasimiya*. Vikundi hivi viwili viliundwa na ma-*bey* na wafuasi wao wa Kimamluki, na vilitafuta wafuasi zaidi miongoni mwa Wanomadi na wakazi wa mijini. Harakati zao zilizishirikisha pia *ojak* (ngome za kijeshi): mayeniseri wakiiunga mkono Fakariya na Waazab wakiiunga mkono Kasimiya. Matokeo ya migogoro hii yalikuwa ni kugawanyika kabisa kwa jamii ya Misri ilipofika mwishoni mwa karne ya 17. Ridhwan Bey alipata cheo chake kwa amri ya Sultan iliyomteua kuwa kamanda wa maisha wa msafara wa kwenda kuhiji, wakati mshirika wake Ali Bey aliteuliwa kuwa makamu wa maliki wa maisha wa Misri ya Juu. Hivyo utawala wa Fakariya ulikuwa umejipanga vizuri kisiasa, huku viongozi wake wakuu wawili wakishikilia nafasi za juu kabisa za utawala. Hata hivyo, Baada ya kifo cha Ridhwan Bey, mifarakano miongoni mwa Fakariya ilisababisha chama hicho kusambaratika.

Chama cha Kasimiya kilifanikiwa kwa muda kushika ofisi zilizokuwa zikishikiliwa zamani na ma-*bey* wa chama cha Fakariya, lakini ilipofika mwaka 1662 kiongozi wa Kasimiya aliuawa kwa amri ya makamu wa maliki.

Hata hivyo, mwaka 1661 serikali kuu ya Uturuki iliweza kuwasimamisha kazi wafanyakazi wasiokuwa wanajeslu katika *ojak* saba. Ilipandisha kodi ya mapato waliyoilipa ma-*multazim* kwa asilimia 20 ili kufidia deni la hazina Iililosababishwa na mfumuko wa bei. Pamoja na watu kutoridhika, ufalme wa Istanbul uliamua kuchukua hatua zaidi. Katika mwaka 1670 makamu wa maliki, Kara Ibrahim Pasha, aliagizwa afanye marekebisho ya kuimarisha hazina ya Misri kwa kushirikiana na jeshi. Baada ya marekebisho ya msingi ya bajeti na mazungumzo ya miaka minne na makundi mbalimbali yaliyohusika, alifanikiwa kuongeza fedha za hazina mara mbili. Misingi iliyotumika kufanya marekebisho hayo ikawa ndiyo msingi wa kutatua matatizo ya hazina katika kipindi chote cha kuanzia wakati huo hadi 1798. Lakini matokeo ya hatua hizi yalidumu muda mfupi kwa sababu uamuzi wa kupunguza mamlaka ya *ojak* ulichelewa kutolewa. Kudhoofishwa kwa nguvu za Pasha katika nusu ya kwanza ya karne ya 17, na kuondolewa kwa vyama vya ma-*bey* katika miaka ya 1660, kuliziwezesha *ojak* kujichukulia mapato yaliyotokana na kunyonywa kwa wakazi wa mijini. Wakati huo huo, ma-*bey* waliendelea kunyonya wakazi wa vijijini.

Kati ya mwaka 1670 na 1750 maisha ya kisiasa yalizidi kuwa magumu. Kipindi hiki kilishuhudia siyo tu kuwepo kwa mifarakano miongoni mwa *ojak* bali pia kuwepo kwa migongano iliyohusiana na vyama, baadhi ya watu wakikiunga mkono chama cha Fakariya na wengine kile cha Kasimiya. Mambo makuu mawili yaliyoleta mzozo yalihusu nguvu za kisiasa na nguvu za kiuchumi: hazina ya mapato na namna yalivyogawanywa, na pia suala la mali zilizopatikana kwa njia isiyo halali. *Ojak* iliyokuwa na mizozo zaidi ni ya mayeniseri, kwani ilidhibiti mapato makubwa zaidi.

Kwa muda wa miaka ishirini hivi, kiongozi mkuu wa mapambano ndani ya *ojak* ya Mayeniseri alikuwa Jeniseri Bashodabashi Kuchuk Mehmed. Mwaka 1680 alifukuzwa kutoka Misri na aliporejea aliungwa mkono na *Agha* ambaye alimtambulisha kwa chama cha Fakariya. Kuchuk Mehmed alifanikiwa kuwaondoa

makamanda wa Kikasimi ndani ya *ojak* ya Mayeniseri kwa msaada wa kiongozi wa Fakariya na kuitawala *ojak* hiyo mwenyewe kuanzia mwaka 1692. Muda mfupi baadaye, aliungwa mkono na viongozi wa ngazi za juu wa *ojak* zote saba kwa uamuzi wake wa kufuta baadhi ya malipo ya ulinzi na malipo haramu mengine yote yaliyodaiwa na Mayeniseri na Waazabu. Sababu kubwa ya kutaka kuzuia malipo hayo ilikuwa ni kuogopa kutokea kwa machafuko kama yake yaliyotokea mwaka 1678, ambayo yalisababishwa na mfumuko wa bei na kupanda kwa bei za nafaka.

Wakati wa kipindi cha joto cha mwaka 1694, migogoro ndani ya *ojak* ya Mayeniseri ilifikia katika hatua mbaya. Wakati huo huo, mafuriko kidogo ya mto Nili yalisababisha bei za uafaka kupanda. Kwa kuzingatia utawala wa haki, Kuchuk Mehmed aliwachukulia hatua walanguzi, akapanga bei za ngano na kuwaondoa wafanyabiashara wa kati katika usambazaji wa bidhaa hiyo. Hatua hizi ziliibua upinzani wa Mayeniseri na Waazabu, waliotawala maghala yote ya nafaka, dhidi ya Kuchuk Mehmed na kusababisha auawe. Kwa mara nyingine tena *ojak* zikawa huru kujikusanyia mapato yaliyokuwa yamezuiwa na kuamua bei za vyakula. Ongezeko kubwa la bei ya bidhaa muhimu lililofuata lilisababisha njaa ya mwaka 1695. Mafuriko makubwa ya mwaka 1697, ndiyo pekee yaliyosaidia kumaliza matatizo ya kipindi hiki kigumu.

Tangu mwaka 1688 zahama ilizidishwa na kuendelea kushuka kwa thamani ya fedha, na kufikia mwaka 1692 hali ilikuwa mbaya sana. Utawala wa jimbo ulijaribu kufidia upungufu huo katika hazina kwa kuongeza asilimia 4 kwenye kodi iliyotolewa na ma-*iltizam*, lakini Istanbul ilidai kwamba hazina iwasilishwe katika sarafu isiyoshuka thamani, sharti ambalo lilizua upinzani mkali miongoni mwa *ojak* ambazo zilikuwa zikipata faida kubwa kutokana na kushuka kwa thamani ya fedha, kama walivyokuwa wateja wao wafanyabiashara. Upinzani wao ndio uliokwamisha jitihada za kurekebisha mfumo wa fedha na utaratibu wa kodi zilizoandaliwa na mtaalamu wa masuala ya fedha, Yasif al-Yahudi, mwaka 1697.

Mwanzoni mwa miaka ya 1700 lilitokea wimbi jipya la upandaji wa bei lililosababishwa na kuingia kwa wingi kwa sarafu zisizokuwa na thamani kutoka sehemu mbalimbali za himaya ya Kituruki. Iliamuliwa kwamba sarafu zilizopungua thamani ziwe na thamani yenye kulingana na uzito wa metali yake, na kwamba sarafu za fedha zilizosanwa vizuri (*fidda diwani*) zitengenezwe ili zitumike badala ya zile zisizokuwa na thamani. Amri hii ilisaidia sana kupunguza tatizo la kushuka kwa thamani za sarafu ya Misri, lakini tatizo kubwa la malipo ya ulinzi lilibaki bila kutatuliwa, maana *ojak* hazikuwa tayari kuacha kutoza malipo hayo. Hivyo, wasiwasi uliendelea, na uhitishia kuzusha zahama mpya.

Hatimaye mgogoro ulizuka mnamo 1710, ukiwa umesababishwa na kuongezeka kwa manzo ya kahawa nje ya nchi. Biashara hii iliwapatia faida kubwa wauzaji wa jumla na walinzi wao, mayeniseri; faida ambayo haikukubalika kwa *ojak* nyingine. Mvutano huu ulisababisha mapingano makali ndani ya *ojak* ya mayeniseri, mapigano yaliyoshirikisha pia ma-*bey*.

Mtu ambaye alihusika sana na mgogoro huu ni Bashodabashi Ifranj Ahmad,

ambaye aliunga mkono kujihusisha kwa mayeniseri katika mambo ya kiuchumi. Alifukuzwa katika *ojak* mwaka 1707 lakini alipokelewa tena na kuungwa mkono na Fakariya na kurudia tena cheo chake. Lakini amri kutoka Istanbul ilisababisha pigo kubwa kwa mayeniseri: Amri hii ilikomesha vitendo vyote viovu pamoja na mahusiano ya kiulinzi kati ya askari na watumishi wa kiraia. Zaidi ya hayo, mtambo wa kutengenezea sarafu ulitakiwa uhamishwe kutoka makambi ya jeshi ya mayeniseri kwenda kwenye jengo jipya. Kufikia mwisho wa mwaka 1710 mgogoro uliongezeka zaidi kutokana na mfarakano wa ma-*bey* wawili wakuu wa Fakariya. Uwiano nyeti wa mamlaka uliokuwepo uliyumbishwa na kupelekea kwenye mapigano ya silaha ambamo ma-*bey* .walipigana waziwazi. Mnamo Juni 1711 upinzani wa mayeniseri waliokuwa ngomeni ulishindwa, hivyo ma-*bey* wa *Fakariya* wakaikimbia Misri na Ifranj Ahmad akanyongwa.

Matokeo ya matukio haya yalikuwa ni kudhoofisha uwezo wa mayeniseri na *ojak* nyingine kutokana na uchovu wa mapambano ya karibu miaka ishirini. Kipindi kipya kilianza ambamo ma-*bey* walichukua nafasi muhimu tena katika medani ya siasa ya Misri.

Licha ya migogoro ya kisiasa na kiuchumi ya miongo yake ya mwisho, kipindi cha utawala wa *ojak* kilishuhudia mabadiliko makubwa ya kiuchumi na kijamii nchini Misri. Uzalishaji katika kilimo uliongezeka sambamba na uuzaji wa bidhaa za Misri na biashara ya kupitisha, hususani ya kahawa, ilileta neema ya jumla. Hali nzuri ya uchumi ilipelekea kuongezeka kwa idadi kubwa ya watu. Ni kweli, kulikuwa na tatizo lisilokwisha la kushuka kwa thamani ya sarafu lililokuzwa na kushindwa vita kwa Uturuki huko Ulaya, lakini bado Misri haikuathirika sana na vita hivyo ambamo ushiriki wa *ojak* ulikuwa mdogo. Mazingira haya yaliibadili taratibu hulka ya kijamii ya *ojak*. Askari walianza kuchanganyika na raia wa kawaida, hasa katika kuoleana. Nidhamu yao ilianza kushuka na uwezo wao wa kijeshi haukuwa tena kama ule wa mwanzo.

Baada ya 1711 harakati za kugombania madaraka ziliendelea baina ya vikundi vya kisiasa na ndani ya kila kikundi. Mwaka 1714 viongozi wakuu katika chama tawala cha Kasimiya walimwua Kaytas Bey na wao wakachukua mamlaka ya juu (*riyasa*). Lakini mwaka 1718 Mamluki wa Abu Shanab waliunda kikundi cha upinzani kilichoitwa Shanabiya ambacho kilishirikiana na ma-*bey* wa Fakariya kuchukua tena madaraka.

Mapambano yasiyokwisha miongoni mwa ma-*bey* yalitoa nafasi kwa mamakamu wa maliki kuimarisha utawala wao baada ya mwaka 1720. Makamu wa maliki, Bakir Pasha, alitumia fursa ya ushindani miongoni mwa viongozi watatu wa Fakariya kujaribu kuhamishia hazina ya serikali kodi halali na haramu zilizokusanywa na *ojak*. Ili kuvunja upinzani, alihakikisha viongozi wote watatu wanauawa. Lakini uongozi mpya wa kijeshi wa Misri, ukiwakilishwa na Uthman Bey na Yenisari Kahya Ibrahim Kazdoghlu, uliziunga mkono *ojak*. Upinzani ulipata nguvu zaidi kutoka kwa tarika ya kidini ya maulama.

Ibrahimu Kazdoghlu aliposhika uongozi wa *ojak* ya Mayeniseri kikundi cha

Kazdughliya ndani ya chama cha Fakariya, ambacho awali kilikuwa hakijajitokeza, sasa kilijitokeza. Kuanzia mwaka 1743, alipomfukuza Uthman Bey nchini, Ibrahim Kahya akawa kiongozi pekee wa jeshi, na kikundi cha Kazdughliya kikatawala bila mshindani hadi 1798.

Ibrahim Kahya aliungana na Ridhwan, *Kahya* wa Waazabu. Utawala huu wa watu wawili (uwili) ulidumu bila kutokea ghasia zozote kwa miaka mingi baada ya mwaka 1744. Ridhwan Kahya alijitosa katika shughuli aliyoishabikia sana ya ujenzi wa majumba, wakati Ibrahim Kahya akiifanya Misri kuwa milki yake ya binafsi, akitumia kila njia kujitajirisha na kujikusanyia kundi kubwa la wafuasi wa Kimamluki. Hata hivyo, ingawa uwili huu ulionekana kuwa imara, lakini zilianza kuonekana dalili zilizoashiria kuanguka kwa miundo ya kijamii na kiuchumi ambayo utawala wa kijeshi uliitegemea.

Vurugu za chinichini zilianza kutokea wazi wazi mara baada ya kifo cha Ibrahim Kahya mwaka 1754. Ridwan Kahya aliuawa katika maasi ya Mayeniseri yaliyosababishwa na amri yake ya kuanzisha kodi mpya ya kahawa. *Ojak* zilionyesha nia yao ya kuchunga maslahi yao yaliyokuwa yakipungua; aidha, zilionyesha kuchukizwa kwao na Mamluki waliopandishwa vyeo hadi kuwa ma-*bey* na viongozi wa ma-*ojak*, na sasa walitaka kushika madaraka ya kisiasa na kiuchumi. Uhamishaji huu wa madaraka kutoka kwenye *ojak* kwenda kwa ma-*bey* wa Kimamluki uliimarishwa baada ya mwaka 1760, na *ojak* zikabakia kuwa hifadhi tu ya wafuasi wa Mamluki ambao wangeweza kuruhusiwa kushika cheo cha uofisa.

## Maendeleo ya kitamaduni

Kutoweka kwa usultani huru wa Kimamluki na kugeuzwa kwa Misri kuwa jimbo la himaya ya Kituruki kulikuwa na matokeo ya kitamaduni. Shughuli za kitamaduni zilizoendelezwa Misri zilikuwa na muhuri wa mahusiano mapya ya kijamii, kiuchumi na kitaifa. Nafasi mpya ya Misri kisiasa iliathiri pia mambo ya elimu na dhima ya Kiarabu kama lugha ya kuelezea masuala ya utamaduni.

Baada ya kuanguka kwa usultani wa Mamluki, mji wa Kairo ulikoma kuwa kituo cha kiroho cha ulimwengu wa Kisunni, hadhi ambayo Kairo ilikuwa nayo tangu mwaka 1261. Ingawa Al-Azhar ilibakia kuwa moja kati ya shule maarufu kwa wanafunzi watokao nchi za Kiarabu hata baada ya mwaka 1517, wale waliotaka kupata mafanikio katika utumishi wa umma walilazimika kuifuata elimu katika shule za Istanbul.

Kuingizwa kwa Misri na nchi nyingine za Kiarabu katika himaya ya Kituruki, ambayo ilitumia zaidi lugha ya Kituruki-Kiotomani kuendesha shughuli zake za kiutawala na kitamaduni, kuliashiria hatua muhimu katika kudidimia kwa Kiarabu kama lugha kuu ya utamaduni wa Kiarabu-Kiislamu. Nchi za Kiarabu zilipopoteza uhuru wake wa kisiasa, Kiarabu pia kilipoteza nafasi yake ya kuwa lugha ya utawala wa dola.

Kama ilivyokuwa katika majimbo yote ya Kiarabu ya himaya ya Waturuki, utamaduni wa Misri ulishinikizwa kisiasa, kijamii na kitamaduni na Waturuki. Hata

hivyo, Misri ilibakiza sifa fulani za pekee za utamaduni ambazo baadaye zilikuja kuwa kianzio na kielelezo cha mwamko wa kitaifa wa Waarabu katika karne za 19 na 20. Sifa hizi za pekee zilihifadhiwa katika fasihi ya Waarabu ya karne za 16, 17 na 18, lakini fasihi hiyo haikutoa mchango mpya kwa tanzu za kale zilizokuwepo, ingawa ilitoa mwelekeo mpya wa fasihi andishi. Maandishi ya Kiarabu yalilenga hadhira ya tabaka la kati la wakazi wa mijini, hivyo lugha na tanzu zake zilielemea sana kwenye fasihi-pendwa.

Mwelekeo huu wa fasihi ulijitokeza zaidi katika ushairi. Tarika ya Kidervi ilivyozidi kusambaa, ushairi wa kiroho wa kisufii ulipata mashabiki wengi kupitia maandishi mbalimbali yaliyoathiriwa na Ibn al-Farid, ambaye aliimba mashairi ya kumsifu Mtume Muhammad. Fasihi ya tashtiti (dhihaka) pia ilianzishwa katika kipindi hiki, na mfano unaokumbukwa ni ule wa *Hazz al-Kuhuf* (Kutikisa vichwa vya wakulima wadogo) uliotungwa na al-Shirbini (1787), ambamo mwandishi alidhihaki ujinga wa wakulima na ufinyu wa fikra wa maulama. Lugha iliyotumika katika kazi hii ni lahaja ya Kiarabu cha Misri. Mshairi mwingine maarufu alikuwa Hassan al-Badri al-Hijazi (alifariki mwaka 1719) ambaye, zaidi ya kutoa mkusanyo wa mashairi yenye dhamira za kidini, alitoa pia mkusanyo wa tungo za tashtiti kuhusu jamii ya wakati huo. Mbali na ushairi huu uliolenga jamii kwa jumla, ulitokea ushairi wa kirasmi wenye mwelekeo wa kipekee na kisodawi (wa kujiona bora), ambao mwakilishi wake nchini Misri alikuwa Abdullah al-Idkawi (alifariki 1770).

Usimulizi wa hadithi ulirutubishwa na riwaya iliyohusu kutekwa kwa Misri na Selim I, ambayo mbabe wake ni Sultani wa mwisho wa Kimamluki, Tuman Bey. Hata hivyo, uandishi wa kisayansi ulizidi kudidimia. Kipindi cha kuanzia karne ya 16 hadi ya 18 kiliendeleza hali iliyokuwepo kabla ya ukosefu wa ubunifu katika kuzalisha maarifa, na uandishi wa maelezo yasiyo na wazo jipya juu ya maandishi ya watu mashuhuri wa zamani. Uandishi wa historia ungeweza kufanyika, lakini ulikosa walezi. Mbali na kazi za Ibn Iyas ambazo, ingawa ziliishia mwaka 1522, zilionekana kuwa ni sehemu ya historiografia ya Kimamluki, kazi nyingi za historia zilikuwa ni za viwango vya chini, hususani katika mbinu zake. Ni kazi chache sana katika kipindi hiki zilizokuwa ndefu na zimeandikwa kwa mtiririko mzuri. Kwa jumla kazi nyingi ni orodha kavu tu za kitarihi za masultani, mamakamu wa maliki, na majaji wakuu, au mihtasari mifupi ya historia ya Misri. Miongo ya mwisho ya karne ya 18 inaelezwa katika tarihi muhimu iliyoandikwa katika karne ya 19 na mwandishi al-Jabarti.

Utanzu maarufu sana ulihusu njia za kwenda kuhiji Maka na Medina, pia maandishi kuhusu sehemu za hija na makaburi ya watu maarufu, hususani wanazuoni na masheikh watakatifu.

Kutukuza watakatifu kulihusishwa na maendeleo ya Tarika za Kidervi na shauku ya watu kuhusu watawa wa kisufii. Tarika iliyofahamika kuliko zote ni ile ya Ahmadiya, iliyoanzishwa na Ahmad al-Badawi (alifariki mwaka 1276), ambaye kaburi lake huko Tanta lilifanywa kuwa kituo cha madhehebu maalumu ya dini. Miongoni mwa tarika zilizokuwa na athari kubwa yafaa kuzitaja Kadiriyya, Rifaiya na Nakshbandiya. Tarika ya Dervi ilisimamiwa na mwakilishi wa dhuria wa Mtume

(*nakid al-ashraf*), ambaye alikuwa ni sheikh kutoka familia ya al-Bakri ambayo asili yake inatokana na Khalifa wa kwanza Abu Bakr. Tarika hizi zilihusishwa na vitabaka fulani katika jamii. Mfumo wao imara wa uendeshaji uliwapa viongozi wao uwezo mkubwa wa kisiasa. Pia tarika hizi zilikuwa na dhima ya kitamaduni kwa sababu zilichangia kwenye elimu ya umma kwa kuwapatia watu fasihi andishi, hasa ushairi. Ushairi wa kiroho ulikuzwa na washairi kadha, kama lile kundi tukufu la wanafamiliya ya al-Bakri, akina Abdullah al-Sha'rawi, Ahmad al Dardir, na wengine.

Kwa karne yote ya 18, Misri haikuwa na matbaa (kiwanda cha kuchapa vitabu), ingawa kuanzia mwaka 1729 vitabu vya Kiarabu na Kituruki vilikuwa vikichapwa Istanbul. Kuandika kwa mkono kuliendelea kuwa njia pekee ya kuongeza idadi ya nakala za kazi za fasihi.

Hadi leo Kairo na miji mingine ya Kiislamu ingali imepambwa na majengo ya ukumbusho yaliyojengwa wakati wa kipindi cha Waturuki. Mengi ya majengo hayo ni kwa matumizi ya dini au elimu ambayo yalijengwa kwa fedha zilizotolewa zawadi na makamu wa maliki, maofisa waandamizi wa *ojak*, ma-*bey* na hata masultani wa Kituruki au ndugu wengine wa ukoo wa kifalme. Majengo hayo yana sifa kadhaa zinazoonyesha uasili wa Misri katika mtazamo wa usanifu majengo na urembaji (utiaji nakshi). Vipengee vya kisanaa vilivyotoka nje ya Misri kwa kiasi kikubwa vinawakilishwa na minara (*manara*), fenza za ukutani, na nakshi za maua kwenye dari na kuta. Ukubwa na raha ya nyumba za binafsi zilizopo hadi leo hudhihirisha ukwasi wa wakazi wa mji mkuu. Huu ni ushahidi wa mabadiliko yaliyokuwa yakiendelea katika jamii ya Wamisri, na kukua kwa umuhimu wa wafanyabiashara, ambao walikuwa kitovu cha tabaka la mabwanyenye la baadaye.

## Kudidimia kwa uchumi na juhudi za kutafuta uhuru

Baada ya kufariki Ibrahim Bey na Ridhwan Kahya, mapigano makali yalizuka miongoni mwa wana-Kazdughliya. Kwa muda mfupi, idadi kadhaa ya ma-*bey*, wote wakiwa Mamluki wa zamani wa Ibrahim Kahya, walipokezana uongozi wa Kazdughliya. Cheo cha heshima cha *Sheikh al-Balad*, ambacho hapo nyuma kilitumiwa mara chache sana, kilianza kutolewa mwaka 1756. Mwaka 1760 Ali Bey, aliyejulikana kama al-Jinn (Jini), akawa *Sheikh al-Balad* mpya na mara akajidhihirisha kuwa mtu mwenye tamaa ya mamlaka na juhudi isiyo ya kawaida. Alifanikiwa kupata nafasi ya kuongoza Misri, na kutokana na mahusiano yake na serikali kuu, alifanikiwa kuishawishi Istanbul kuwa yeye alikuwa ndiye mtu pekee ambaye angeweza kuinyoosha hali ya Misri. Aliomba aruhusiwe kubakia na mali zilizokamatwa kutoka kwa washindani wake kwa ahadi ya kuilipa hazina ya Istanbul deni lote la *para* milioni 91 lililokuwa limelimbikizwa kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita, na alikubali kulipa jumla ya para millioni 50 zilizotokana na mauzo ya mali (za maadui zake) zilizotaifishwa.

Ukali wa hatua zilizochukuliwa dhidi ya wamiliki ardhi na watu mashuhuri kisiasa, ulisababisha kuundwa kwa upinzani ulioongozwa na Salih Bey, aliyekimbilia


Misri ya Juu mwaka 1765 ili kuungana na Sheikh Humam, kiongozi wa Waarabu wa Hawwara ambaye tayari alikuwa akiwahifadhi maadui wengi wa Ali Bey. Kwa kutambua tishio lililowakilishwa na kundi hili lililokuwa limeidhibiti vilivyo Misri ya Juu, Ali Bey alijaribu kuliteketeza kwa njia ya vita, lakini alishindwa na akalazimika kukimbilia Shamu mwaka 1766. Mwaka uliofuata Ali Bey alirudi tena Misri kwa msaada wa serikali kuu. Alifanikiwa kufanya suluhu na Salih Bey na akawafukuza wapinzani wake waliokuwa tayari wameunda utawala wa uwili wakati hayupo.

Mara tu baada ya Ali Bey kumaliza kulipa deni lililokuwa limelimbikizwa kama alivyoiahidi serikali kuu, alibadili sera yake kabisa. Mwaka 1768 alimwondoa makamu wa maliki na akajiteua mwenyewe kushika cheo hicho. Kwa kujiongezea madaraka na kuwa kiongozi rasmi wa utawala wa Misri, juu ya wadhifa wake wa kisiasa wa *Sheikh al-Balad*, Ali Bey akawa mtawala halisi wa Misri, na utii wake kwa Sultani ulibakia kuwa wa kijuujuu tu. Ali Bey hakuwahi kujitangaza mwenyewe kuwa anaongoza nchi huru inayojitegemea, lakini alijipa madaraka ya kutengeneza sarafu zake mwenyewe, na jina lake lilikuwa likitajwa wakati wa sala za Ijumaa. Alijitahidi kuimarisha utawala wake kisiasa na kiuchumi kwa kuimarisha jeshi, kukuza kilimo na biashara. Pia alianzisha mazungumzo ya kibiashara na mataifa makubwa ya Ulaya.

Katika mwaka 1770 wadhifa wake ulimhusisha katika ugomvi uliokuwa ukiendelea miongoni mwa maamiri wa Kihashima wa Maka. Kusuluhishwa kwa mgogoro huo kwa msaada wa Misri, na kubadilishwa kwa makamu wa maliki Mturuki huko Jeddah na kuwekwa Bey Mmisri mahali pake kulimpatia Ali Bey ushindi dhidi ya utawala wa juu wa Sultani wa Hijaz. Akifurahia ushindi alioupata, Ali Bey alianza kufikiria uwezekano wa kuyaunganisha chini ya utawala wake, lakini ndani ya himaya ya Uturuki, maeneo ambayo zamani yaliwahi kuunda eneo la usultani wa Mamluki, yaani Misri, Hijaz na Shamu.

Ali Bey aliamua kupanua utawala wake hadi Shamu mara tu hali ya mambo iliporuhusu mwaka 1770. Jeshi la wanamaji la Kituruki lilikuwa limekwisha angamizwa na manowari za kivita za Urusi, na makamu wa maliki wa Damasko alikuwa akikabiliwa na matatizo katika kupambana na uasi wa Sheikh Zahir Umar. Ali Bey alituma jeshi yake kumsaidia Sheikh Zahir. Majeshi haya mawili, yakisaidiwa na vikosi vilivyokuwa chini ya kamanda Muhammad Bey Abu'l Dahab, yaliyashinda majeshi ya serikali na kuitwaa Damasko. Licha ya ushindi huu wa mwanzo, ma-*bey* hawa wawili waliamua kuachana na jusura hiyo, wakakiri utii wao kwa Sultani, na kurejea Kairo na majeshi yao mwishoni mwa mwaka 1771. Mwaka 1772, baada ya washirika wake kumkimbia, utawala wa Ali Bey ulianguka, akalazimika kukabidhi madaraka yake kwa Muhammad Bey. Huku akisaidiwa na washirika wake wa Shamu na Palestina, Ali Bey alijaribu kurejea (madarakani) bila mafanikio, akafa mara tu baada ya kutekwa.

Ingawa Ali Bey alikuwa amepata msukumo kutokana na historia ya zamani ya Misri, baadhi ya matendo yake yaliashiria ushinde wake wa baadaye. Isitoshe, alikwamishwa na mfumo wa utawala wa Mamluki na ugeugeu wao katika utii.




**6.4** *'Alī Bey,* *Mtawala wa muda wa Mi...*

Wakati akiwa madarakani, dalili za kuwepo kwa hali mbaya ya uchumi zilijitokeza na kuendelea kuonekana kwa viwango tofauti hadi karne ya 19. Ili kuogeza mapato kutokana na kodi iliyotozwa kwenye ardhi ya kikabaila, Ali Bey aliamua kuanzia vijijini kutekeleza sera yake kali ya mapato. Hii ndiyo sababu mojawapo kubwa iliyowafukarisha wakulima na hatimaye wakaamua kukimbilia mijini, ambako pia hawakupata fursa za kuwawezesha kuishi vizuri, maana hata mafundi na wafanyabiashara wengi wa mijini vilevile walipandishiwa kodi. Hali hii ya ufukara wa jumla ilizidi kuwa mbaya kadiri miaka ilivyopita, na ilikuzwa zaidi na milipuko ya magonjwa.

Serikali kuu ilikuwa na matumaini kuwa kiongozi mpya (*Sheikh al-Balad*) angekuwa mtiifu kikamilifu kwake. Mwaka 1775, Muhammad Bey alipeleka (Istanbul) para zaidi ya milioni 130 zikiwa ni kodi ya mwaka. Aidha, mwaka huo huo, alipeleka jeshi kupambana na Sheikh Zahir al-Umar kwa amri ya Sultani. Lakini aliuawa wakati wa kuizingira Akka, na huo ukawa ndio mwisho wa kujihusisha kwa Misri katika masuala ya Shamu. Baada ya Muhammad Bey kufariki, waali wa Kimamluki waligombania madaraka, na hivyo kutoa fursa kwa serikali kuu kuutumia mgogoro huo kwa manufaa yake. Serikali kuu ilikuwa tayari kumuunga mkono mtu yeyote ambaye angeahidi kupeleka Istanbul sehemu kubwa zaidi ya kodi iliyotozwa kwa wenye mali, lakini haikukusudia kuingilia moja kwa moja masuala ya Misri.

Katika mapambano ya kuwania madaraka yaliyochukua kama miaka kumi, viongozi wakuu walikuwa ni ma-*bey* watatu wa Kazdughliya: Ismail Bey, Murad Bey na Ibrahim Bey. Katika awamu ya kwanza ya mapambano, viongozi wawili waliotajwa mwisho walifanikiwa kumfukuza nchini Misri Ismail Bey na wafuasi wake. Hali hii ilifuatiwa na mapigano ya muda mrefu baina ya washindi hao wawili, maana ingawa Ibrahim alitambuliwa rasmi kama *Sheikh al-Balad*, lakini alizuiwa na Murad kushika madaraka kamili. Ushindani huu ulitoa nafasi kwa serikali kuu kuingiza mizengwe yake kwa lengo la kujiongezea kipato kutokana na makusanyo ya mwaka ya kodi iliyopelekwa hazina. Lakini haikufanikiwa kutumia nafasi hiyo kikamilifu, kwani viongozi hao wawili polepole waliweza kudhibiti utawala wa jimbo lote, na kuchukua fedha na raslimali zote na kuzitumia kwa makusudio yao.

Washindani hao wawili waliposuluhishwa, serikali kuu iliona kwamba maslahi yake yalikuwa hatarini, hivyo ikaamua kurejesha utawala wa moja kwa moja nchini Misri kwa kutumia jeshi. Mwezi Julai 1786 kikosi maalumu cha kivita cha Waturuki, kikiongozwa na Hasan Pasha, kilitia nanga katika mji wa Aleksandria. Kiliyatawanya majeshi ya Mamluki, lakini Murad Bey na Ibrahim Bey walirudi nyuma hadi Misri ya Juu pamoja na mabaki ya jeshi lao. Ili kurejesha tena mamlaka ya Sultani, Hasan Pasha alilazimika kuvunjilia mbali nguvu za kijeshi za waasi hao wawili na kuwapa mwelekeo mpya Mamluki waliokuwa bado watiifu. Alikusudia kufanya hivyo kwa kuteua kundi jipya la ma-*bey* na makamanda wa vikosi kutokana na familia mbalimbali za Mamluki. Kwa kuwa madhumuni makubwa ya maingilio hayo nchini Misri yalikuwa ni kuanzisha tena utaratibu wa kupeleka kodi hazina, Hasan Pasha aliweka amri kadhaa zilizohakikisha kwamba jimbo la Misri linakubali kutekeleza

wajibu wake kwa serikali kuu na kwa miji mitakatifu. Lakini kabla hajaanza kutekeleza amri hizi, Hasan Pasha alipelekwa sehemu nyingine kwa shughuli za kijeshi.

Uvamizi wa kijeshi nchini Misri haukuwa na matokeo yaliyotazamiwa. Mgawanyo wa Misri katika ukanda wa chini uliotawaliwa na mwakilishi wa Sultani, na ukanda wa juu uliotawaliwa na waasi wawili, ulikuja kukubalika kuwa ndiyo hali ya kawaida ya mambo. Licha ya mabadiliko yaliyoletwa na Hasan Pasha miongoni mwa maofisa wa serikali, na hususani uteuzi wa Ismail Bey kuwa *Sheikh al-Balad* mpya, utawala wa Mamluki ulibakia imara, na pamoja nao mazingira ambayo yangeweza kuibua tena matatizo ya zamani.


Migogoro ya kisiasa iliongezeka sana baada ya mwaka 1783 kutokana na matatizo ya kiuchumi kama vile kupungua kwa mavuno, njaa, ongezeko la bei na kushuka kwa thamani ya sarafu. Mlipuko mkali wa maradhi ulitokea mwaka 1791 na kuua ma-bey wengi watiifu, hususani Ismail Bey. Kwa hiyo, Murad Bey na Ibrahim Bey walirejea tena Kairo kipindi cha majira ya joto katika mwaka huo huo bila kukutana na upinzani wowote na kuanzisha tena utawala wao juu ya nchi yote ya Misri.

Serikali kuu iliukubali utawala wao kwa masharti kwamba wangetimiza wajibu wao. Mwaka 1792 ma-*bey* hawa wawili walitia sahihi mkataba ulioelezea jumla ya fedha ambazo zingelipwa hazina, na utaratibu wa ulipaji, lakini waliutekeleza mkataba huo kwa shingo upande na kwa sehemu fulani tu. Kurudi kwao katika madaraka kuliashiria kurejea kwa utawala wa kikatili na wa kinyonyaji ambao Misri ilikuwa nao kabla ya safari ya Hasan Pasha, na matokeo yake katika uchumi yalikuwa mabaya zaidi. Nchi ilikuwa imeharibiwa na vurugu za kisiasa za miaka kumi iliyopita, na uporwaji usiokwisha wa raslimali na akiba zake. Hali hii mbaya ya uchumi iliakisi ukandamizaji wa jamii nzima kisiasa uliofanywa na kikundi kidogo cha ma-*bey* wa Kimamluki na wafuasi wao. Lakini serikali kuu haikuwa na uwezo wa kukiondoa kikundi hiki, na Wamisri nao walikuwa hawajawa tayari kufanya hivyo wenyewe. Msukumo wa kwanza (wa kuibadilisha hali hiyo) ulitolewa mwaka 1798 na kufika bila kutazamiwa kwa jeshi la kivita la Ufaransa katika pwani ya Misri likiongozwa na Napoleon Bonaparte.

## *Hitimisho*

Katika kipindi cha historia kilichoanza na kuanguka kwa sultani wa Kimamluki mwaka 1517 na kumalizika na maingilio ya kijeshi ya Wafaransa mwaka 1798, maendeleo ya Wamisri yaliamuliwa na nguvu za ndani. Kinyume na ilivyokuwa katika sehemu za Ulaya za himaya ya Waturuki, Misri ilibakia pembezoni mwa maendeleo ya kisiasa, na maendeleo ya kijamii na kiuchumi hayakuweza kufikia hatua ya kuchipuza tabaka jipya la kijamii la mabwanyenye. Kwa hiyo, kijamii, Misri ilibakia katika hatua ya kimaendeleo iliyojulikana kijadi kama ukabaila.

Kuunganishwa kwa Misri katika himaya ya Waturuki kulikuwa na faida kubwa kwa himaya hiyo kwa sababu kuliiongezea uwezo wa kiuchumi na nguvu za kisiasa.



6.5 Msikiti wa Muhammad Bey Abul-Dahad, 1188/1774

Lakini mahusiano baina ya serikali kuu na jimbo la Misri yalikuwa na mvutano wa mara kwa mara, na kudhoofika kwa himaya ya Waturuki kulisababisha migongano na zahama ambazo hatimaye zilizusha nguvu zilizopingana na utawala unganifu.

Kukua kwa nguvu za utengano huko Misri mwishoni mwa karne ya 18 halikuwa jambo geni katika nchi za Kiarabu zilizokuwa chini ya himaya ya Waturuki. Lakini kwa upande wa Wamisri nguvu hizo hazikuambatana na tamaa ya kuuondosha ukandamizaji wa sultani wa Kituruki.

Safari ya Hasan Pasha ya mwaka 1787 ilidhihirisha udhaifu wa kijeshi wa utawala wa Mamluki, na kwamba haungeweza kustahimili shambulio la adui mwenye nguvu zaidi kama ilivyodhibitishwa baadaye na uvamizi wa Napoleon. Isitoshe, kwa kujaribu kuangamiza nguvu zilizotishia mamlaka unganifu, na kurejesha uhusiano baina ya jimbo la Misri na serikali kuu, uvamizi wa Waturuki ulibashiri juhudi ambazo dola la Uturuki lilikuja kufanya katika karne ya kumi na tisa.

Shauku ya Misri juu ya maeneo ya nje ya mipaka yake na jitihada zake za kuwa na mahusiano huru ya kibiashara na kanda nyingine, zilidhihirisha kuwa Misri sasa ilikuwa imeachana na sera ya karne nyingi ya kujitenga na mataifa mengine. Kujitenga huko kulikoma wakati Ufaransa ilipoanza kujipanua na kutafuta makoloni mashariki mwa Mediterania. Katika muktadha uliozidi kuwa na utata wa "Tatizo la Mashariki", Misri ilikuja kuwa nchi muhimu kabisa kwenye sataranji ya siasa za ulimwengu.

# 7 Nchi ya Sudani, 1500–1800

## *Utangulizi*

Historia ya Sudani katika kipindi kinachozungumziwa iliainishwa na miguro ya watu walioingia na kuondoka Sudani. Kwa upande wa kaskazini, kujipenyeza taratibu kwa idadi kubwa ya Waarabu Waislamu ambako kulianza mwanzoni mwa kipindi hiki, kulipelekea katika kuunganishwa kwa eneo hili katika ulimwengu mpana zaidi wa Kiislamu. Mchakato wa usimilishaji wa kitamaduni na kikabila uliuma kuwili: Kwa upande mmoja uliarabisha na kusilimisha idadi kubwa ya watu wa Sudani, na kwa upande wa pili uliwajumuisha wahamiaji wa Kiarabu katika jamii ya Sudani.

Athari ya Uislamu na utamaduni wa Kiarabu kwenye maeneo ya kusini mwa Sudani haikuwa kubwa. Msukumo wa kujipanua kwa Waniloti kutoka kusini ulifanikiwa kuzuia misafara ya Waarabu kwenda kusini na ueneaji wa Uislamu. Kwa hakika Waniloti, hasa Washilluk na Wajieng, walikuwa tishio kubwa kwa majimbo ya Waislamu ya kaskazini hadi mwisho wa kipindi hiki.

Sura hii kimsingi itashughulikia uanzishaji na upanuzi wa madola mawili ya Kiislamu ya savana (yaani sultani za Funj na Fur), uhusiano baina yao, na mwingiliano wao na jamii za Kiafrika zisizokuwa za Kiislamu ambazo pia zilikuwa katika mchakato wa uundwaji kutokana na vikundi mbalimbali vya kilugha na kitamaduni. Pia sura hii itajaribu kuonyesha kuwa ueneaji wa Uislamu ulikuwa ni kipengele muhimu kwa historia ya Sudani katika kipindi hiki.

Mchakato wa uarabishaji na usilimishaji kuelekea kusini ulisitishwa pale mito inapogawanyika (Bahr al-Ghazal na Bahr al-Arab) na hivyo kuweka mpaka wa namna fulani wa kitamaduni kati ya Sudani ya kaskazini na Sudani ya kusini ambao umeathiri tafsiri ya historia ya Sudani hadi leo.

Kwa mtazamo wa Wasudani wa kusini, uhusiano kati ya maeneo hayo mawili unajidhihirisha kwa kuingiliwa na kunyonywa kiuchumi na Wafunj katika Nili ya Juu, na baadaye Wafur katika jimbo la Bahr al- Ghazal. Lakini kwa mtazamo wa kaskazini, mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na kijamii kwa ujumla yamekuwa yakihusishwa na majilio ya wahamiaji Waislamu, "wageni wenye hekima," kutoka kaskazini au mashariki. Leo, kaskazini huelezewa kuwa ni eneo la Kiarabu na

Kiislamu, na kusini kuwa ni eneo la Kiafrika (au Kinegro) na "Kipagani" (au "Kianima" - imani ya kuwa vitu vyote vina roho). Hivyo mipaka iliyowatenganisha inazidi kujibainisha katika misingi ya dini na ukabila.

Ukweli wa kihistoria kwa hakika ulikuwa changamani zaidi kuliko maelezo hayo. Kwanza, mpaka kati ya maeneo haya mawili ulikuwa unabadilika mara kwa mara, na si mara zote kuelekea kusini au magharibi.

Pili, mpaka ulikuwa ni eneo kubwa. Kwa mfano, kwenye eneo la Nili ya Juu ulitandaa kwa mamia ya kilomita. Hata kwenye eneo la upande wa magharibi hali ilikuwa vivyo hivyo. Zaidi ya hayo, ndani ya mpaka wenyewe mageuzi ya kitamaduni, kikabila na kijamii yalikuwa yanatokea wakati wote, huku watu wakijigeuza Waarabu, Wafur, Wafunj, Washilluk, Wanaath au Wajieng kufuatana na hali ya kisiasa na kiuchumi.

Tatu, ndani ya sultani za Kiislamu za kaskazini mchakato wa mabadiliko ya kikabila ulikuwa changamani pia. Kwanza, neno "Mwarabu," ambalo lilikuwa na maana dokezi za kitamaduni, taratibu lilivuliwa dhana ya ukabila, kama ilivyotokea kwa Waarabu wa Bakkara walioishi mpakani. Zaidi ya hayo, kufikia karne ya kumi na nane, kila usultani uligawanyika katika temi, nyingi kati yake zikiwa na jamii mchanganyiko. Muundo wa kijamii ndani ya sultani hizi ulitatanisha zaidi kutokana na kuwepo kwa utumwa. Watumwa wengi walioletwa kutoka kusini walikuwa ni sehemu muhimu ya jeshi la sultani, ilihali wengine walisimilishwa katika jamii zao mpya.

Mwisho, ukiachilia mbali watu waliokuja kutoka katikati na magharibi mwa *Bilad al-Sudani* (kama Watakrur na Wafulbe) na Warashayida kutoka Uarabuni, hakuna kikundi kipya cha kikabila kilichoibuka katika Sudani katika karne ya kumi na tisa na karne ya ishirini, na miguro mikubwa ya watu kimsingi ilimalizika kama mwaka 1800.

## *Dola la Abdallabi*

Katika nusu ya pili ya karne ya kumi na tano muungano wa makabila ya Waarabu ukiongozwa na chifu wao, Abdallah, aliyepewa lakabu ya Jamma (mkusanyaji), ulifanikiwa kuutiisha ufalme wa Alwa'. Kutekwa kwa Soba kulikuwa ni kielelezo cha utwazi wa Waarabu, na mwanzo wa ushawishi wa Waarabu katika *Bilad al-Sudan* ya mashariki. Abdallah Jamma na dhuria wake, Waabdallabi, walianzisha serikali yao huko Kerri kaskazini ya Soba katika mto Nili. Kerri ilikuwa inafikika kwa urahisi na Waarabu wa Butana, ambao Waabdallabi walihitaji msaaada wao. Pia Kerri iliiwezesha serikali kufuatilia nyendo zote kwenye bonde la mto Nili na pia ng'ambo ya mto kwenye ukanda wa magharibi.

Ni vigumu kufahamu ukubwa wa dola jipya. Hegemonia ya Waabdallabi yaelekea ilitanda hadi kwa Waarabu wa Jazira kaskazini, Wabutana wa mashariki ya Nili, na pia baadhi ya vikundi vya Wabeja. Uhuru wa dola la Abdallabi haukudumu muda mrefu kuweza kuanzisha asasi zake. Kufikia mwanzo wa karne ya kumi na sita

lililazimika kupambana na adui mwenye nguvu, Wafunji, ambao walikuwa wanomadi wenye kufuga ng'ombe waliokuwa wakihamia upande wa chini ya mto wa Nili ya Bluu. Majeshi hayo mawili ya wahamiaji yalipigana, pengine kwa ajili ya kumiliki ardhi ya malisho kaskazini mwa Jazira. Huko Arbaji katika mwaka 1504 Wafunji waliwashinda Waabdallabi na kumfanya mfalme wao kuwa kibaraka wao. Waabdallabi waliendelea kutawala sehemu ya kaskazini ya usultani wa Funji kama vibaraka wa makabaila wa Kifunji hadi utamalaki wa Waturuki-Wamisri mwaka 1820.

## *Usultani wa Funji*

Asili ya Wafunji imeibua nadharia tete nyingi zinazopingana. Ufalme wao unafahamika katika mapokezi ya Wasudani kama *al-Sultana al-Zarka* (Usultani wa Kibluu). David Reubeni, Myahudi mtalii aliyekwenda kule mwaka 1522-3 alimwelezea mfalme wao kuwa ni Muislamu mweusi mwenye kutawala taifa la weusi na weupe, akiwa na maana ya Waafrika wa asili na Waarabu kwa mfuatano huo. Mapokezi ya wenyeji yanaeleza kuwa Wafunji wana asili ya Kiarabu, na kuwa ni dhuria wa mkimbizi wa Kiumayya aliyeingia kupitia Ethiopia na, inavyosemekana, akamwoa binti wa mfalme mwenyeji. Inaelezwa kuwa alikuwa "mtu aliyebarikiwa" ambaye alileta desturi mpya.

Haijulikani ni lini ukoo wa Funji ulianza kudai kuwa ni uzao wa Kiumayya, lakini inaelekea Wafunji walisilimishwa haraka sana. Kama ilivyo kwa watu wengine waliosilimishwa walioishi ukingoni mwa jamii za Waislamu, Wafunji walitaka kuonekana kuwa ni Waarabu, wakitarajia kuimarisha mamlaka yao kiitikadi juu ya Waarabu wanaowatawala.

Baada ya kusimika utawala wao katika majimbo ya Waabdallabi, Wafunji waliitawala himaya yao kutokea Sennar, ambayo ilifanywa makao yao ya serikali. Sheikh wa Waabdallabi akageuzwa kibaraka wa Wafunji na akawa na cheo cha Manjil au Manjuluk ambacho wafalme wa Funji walikuwa wakiwapa vibaraka wao wakuu.

Katika juhudi ya kujikomboa kutokana na utawala wa Kifunji, Sheikh Ajib I, ambaye alingia madarakani katikati ya karne ya kumi na sita, aliwapiga Wafunji, akawashinda na kuwafukuzia Ethiopia. Wakati wa utawala wa Dakin (1568/9-1585/6), Wafunji walirudisha utawala wao wa zamani, lakini ilibidi wakubali kumwachia Ajib I haki ya kuchagua majaji katika majimbo yake.

Yaelekea sera ya Dakin ya kuupangilia upya ufalme na kuweka kanuni mpya iliharibu uhusiano nyeti ulikuwepo kati ya pande hizo mbili na kumfanya Ajib kuasi waziwazi. Mwaka 1611/12 jeshi la Wafunji liliwashinda vibaya Waabdallabi. Katika mapigano hayo Ajib I aliuawa. Makubaliano yalifanywa kati ya Waarabu na Wafunji ambayo yalirejesha hali iliyokuwepo kabla ya vita. Hivyo wazawa wa Ajib wakiwa na cheo cha *Wad Ajib* waliendelea kutawala moja kwa moja majimbo yote kuelekea kaskazini hadi Hajar al-Asal, na pia kwa kuwatumia mawakala wenyeji walitawala

makabila yote yaliyoishi katika bonde la mto Nili hadi mpaka wa Nubia ya Kituruki. Makubaliano haya yaliupa usultani kipindi kirefu cha utulivu. Hata hivyo karibu na katikati ya karne ya kumi na saba utemi wa Shaykiyya uliasi dhidi ya mamlaka ya Waabdallabi na kujichukulia uhuru wake kutoka kwa usultani wa Funji.

## Kupanuliwa kwa Usultani wa Funji

Yaelekea kupanuliwa kwa mamlaka ya Funji hadi Nubia ya chini kulitiliwa wasiwasi na Waturuki walioitiisha Misri mwaka 1517. Wakati wa utawala wa Sulayman Mtukufu (1520-1566), walipeleka msafara wa manowari, ukiongozwa na Ozdemir Pasha, katika Bahari ya Hindi dhidi ya Wareno waliokuwa wakitishia njia za Bahari ya Shamu. Alipokuwa anarejea, Ozdemir alipewa maelekezo ya kuzima "maasi" ya Wafunji huko Nubia ambako vikundi viwili vinavyopingana vilikuwa vinapigana. Ozdemir aliteka ngome muhimu kiulinzi za Ibrim na Dirr zilizokuwa mpakani, na akajenga ngome huko Say ambayo ndiyo iliyobainisha mpaka wa kusini wa Misri ya Kituruki. Jimbo hilo jipya, lililojulikana kama Berberistan, liliongozwa na Waturuki.

Ozdemir Pasha baadaye alipewa jukumu la kuipiga Habesistan (Uhabeshi). Baada ya maandalizi yaliyofanywa kwa makini sana huko Misri, msafara uliondoka ukifuata Mto Nili. Walipofika Aswan, Ozdemir alishindwa kulidhibiti jeshi hilo lisilokuwa na nidhamu, na hivyo akaamua kuliacha lengo lake la kuenda kuipiga Uhabeshi. Hapo ikafahamika kuwa msafara haukuwa umeelekezwa dhidi ya Habesistan bali dhidi ya Funjistan (nchi ya Wafunji). Hatimaye, mpaka wa Misri uliimarishwa kule Hannik mwaka 1622 baada ya mapigano madogo kati ya Waabdallabi na Wafunji.

Ozdemir pia anasifiwa kwa kuanzisha kituo huko Sawakin dhidi ya Wareno, na zaidi dhidi ya Waethiopia (Wahabeshi). Sawakin iliwekwa chini ya usultani wa Uturuki na Massawa kutekwa mwaka 1557. Ukanda wa pwani kati ya bandari hizo mbili ndio uliofanywa kuwa jimbo la Uhabeshi. Mara tishio la Wareno lilipoondolewa Sawakin kwa mara nyingine ikawa ndiyo mlango mkuu wa biashara katika usultani wa Funji. Uhusiano kati ya gavana wa Kituruki na Wafunji mwanzoni ulikuwa mbaya na uliendelea kuwa dhaifu hadi ukafikia kwenye mapambano ya silaha mwaka 1571. Hata hivyo, kutokana na mahusiano makubwa ya kibiashara ambayo yalikuwa tayari yamejengeka kati ya sehemu hizo mbili, hali ya hofu ilipungua na Sawakin ikawa maarufu na imeendelea hivyo mpaka mwanzoni mwa karne ya ishirini.

Kufikia mwanzoni mwa karne ya kumi na saba, yaelekea Wafunji walikuwa tayari wamejiimarisha huko Sennar. Eneo walilolitawala moja kwa moja lilianzia Arbaji hadi kusini mwa Fazughli. Upanuzi wa mamlaka yao upande wa magharibi hadi Kordofan ulianzishwa na Sultani Abd al-Kadir mwaka 1554. Kuongezeka kwa shinikizo la Waniloti kwenye Nili Nyeupe dhidi ya Sennar kunaonekana kulisababisha mgongano kati ya Wafunji na Washilluk. Sultani Badi II Abu Dikn (1644/5 hadi 1718) alijipenyeza kule Alays na kuweka kikosi cha Wafunji kwenye mto. Kutoka mahali hapo palipofaa kiulinzi, Wafunji waliweza kufuatilia nyendo za ng'ambo ya

mto na kuwadhibiti Washilluk, ambao yaelekea walikubali kufanya urafiki nao.

Kisha Wafunji walijipenyeza kwenye milima ya Nuba, moja ya vyanzo vikuu vya watumwa. Ufalme uliosilimishwa wa Takali ulipunguziwa hadhi yake na kuanza kulipishwa kodi na Wafunji. Kadhalika Wafunji walipanua utawala wao hadi vilima vya kaskazini vya al-Dayr na Kordofan. Idadi kubwa ya mateka wasiokuwa Waislamu waliokamatwa miongoni mwa "Wanuba wa milimani" waliwekwa kwenye vijiji karibu na Sennar. Waliunda kikosi cha watumwa cha kumlinda sultani. Kuanzishwa kwa jeshi la watumwa lililomtegemea mtawala kuliwatia wasiwasi wapigauaji wa jadi waliotokana na makabaila wa Kifunji, na hivyo wakaasi wakati wa utawala wa Badi III (aliyejulikana kama Badi Mwekundu, 1692-1716).

Mgogoro mpya ulizuka wakati wa utawala wa Badi IV Abu Shullukh (1721-1762), mfalme halisi wa mwisho wa Wafunji. Katika nusu ya kwanza ya utawala wake, Badi IV aliziacha shughuli za dola mikononi mwa waziri wake, Doka; lakini Doka alipofariki Badi alilifuta baraza la *ahl-al Usul* (wana-nasaba tawala ya asili na wenye vyeo) na kuanza kutawala bila kujali sheria. Ili kuondokana na Wafunji mashuhuri ambao walikuwa wanampinga, aliwapeleka kupigana na wa- Musabba'at ambao walikuwa wameingilia ardhi ya Funji kule Kordofan. Baada ya kurudishwa nyuma mara kadhaa, jeshi la Wafunji chini ya amri jeshi Muhammad Abu Likaylik lilipata ushindi kamili mwaka 1747. Abu Likaylik akawa gavana mkuu wa Kordofan kwa miaka kumi na minne.

Kumbukumbu za uhusiano kati ya Wafunji na Wahabeshi zinaonyesha kuwa zimejaa migogoro mingi ya mpaka, lakini hilo halikuzuia ushirikiano na kutegemeana kiuchumi kati ya nchi hizo mbili. Kwa Wakristo wa Ethiopia, Sennar ilikuwa kwa miaka mingi ndiyo njia yao pekee ya kutokea nje ya nchi na njia za biashara zilibaki wazi hata wakati uhusiano kati ya Sennar na Gondar ulipokuwa mbaya. Hata hivyo Wafunji walipigana vita mara mbili dhidi ya Ethiopia. Vita vya kwanza vilitokea mwanzoni mwa karne ya kumi na saba. Uhusiano kati ya sultani wa Funji na maliki wa Ethiopia ulizorota wakati maliki alipotoa hifadhi ya kisiasa kwa sultani Abd al-Kadir aliyeondolewa madarakani na kumfanya gavana. Matukio ya mpakani yaliongezeka kati ya mwaka 1618 na 1619, wakati idadi kubwa ya askari ilipohusishwa kwenye migongano hiyo. Watawala hao wawili hawakuviona vita hivi kuwa tishio kwao kwa kuwa vilikuwa vinapiganiwa mbali na makao yao makuu. Hatimaye vita vilimalizika kwa ushindi wa Ethiopia.

Katika karne iliyofuata, vita vya pili vilianza kwa kulivamia jimbo la Kalabat-Dindera. Mwezi Machi 1744 Iyasu II aliongoza jeshi kubwa la Ethiopia dhidi ya Sennar. Majeshi hayo mawili yalipigana vita vikali kwenye kingo za mto Dindera. Waethiopia walishindwa vibaya. Ushindi wa Wafunji ulisherehekewa na Badi IV na wafuasi wake kwa hamasa za kidini. Mwangwi wa ushindi huo ulivuma hadi Istanbul, na inasemekana khalifa wa Uturuki alifurahishwa na ushindi wa Uislamu.

## Maendeleo ya Uislamu

Usultani wa Funji-Abdallabi uliipa nchi umoja na utulivu ambao ulisaidia kueneza

Uislamu. Hii ilikuwa ni kazi ya wanazuoni Waislamu ambao watawala waliwahimiza kuja na kuishi nchini. Hapo awali Uislamu ulikuwa ukienezwa na makundi mawili, wafanyabiashara na Wanomadi wa Kiarabu. Katika kundi la kwanza, biashara na ushawishi wa kubadili dini vilienda sambamba ukingoni mwa jamii za Kiislamu. Kundi la pili, ingawa halikuwa na ujuzi mkubwa wa mafundisho ya dini, lakini lilitoa mchango mkubwa katika kueneza Uislamu, hasa kwa kuoana na wenyeji wa Sudani. Usilimishaji aghalabu uliambatana na Uarabishaji.

Kipindi cha mwanzo cha Wafunji kilishuhudia kuongezeka kwa idadi ya walimu Waislamu. Wengine walitoka Misri, Hijaz, Yemen na Maghrib. Hata hivyo wengi wao walizaliwa nchini Sudani, na wengine walisomea Kairo au sehemu nyingine takatifu. Aliporejea kutoka Kairo katikati ya karne ya kumi na sita, Mahmud al-Arak, mwanazuoni Mwislamu wa kwanza Msudani, alianzisha shule kumi na saba kwenye Nili Nyeupe. Mwaka 1570, Ibrahim al Bulad ibn Jabir alikuwa mtu wa kwanza kukita mafundisho yake katika vitabu viwili vya Kimaliki: kitabu cha *Risala* cha Ibn Abi Zayd al-Kayrawani na kitabu cha *Mukhtasar* cha Khalil ibn Ishak. Mafundisho haya yalisaidia kuifanya itikadi ya Kimaliki itawale katika eneo hilo.

Wanazuoni wa kwanza kupata mafunzo walijishughulisha zaidi na kufundisha sharia za Kiislamu na namna zinavyotumika. Juhudi zao za kueneza mafundisho ya kirasmi na kuinua kiwango cha maisha ya kidini zilikumbana na matatizo makubwa katika nchi kubwa kama hiyo, iliyojitenga na iliyo nyuma kimaendeleo. Kabla ya Uislamu wa kirasmi kuota mizizi nchini humo, Uislamu wa watu wa kawaida usiokuwa na shuruti nyingi ulikuwa umekwisha ingizwa.

Tarika (vyama vya udugu wa kidini) nyingi za kisufii zilitokea Hijaz. Ya kwanza na iliyojulikana sana ni ya Kadiriyya. Ililetwa Sudani na Taj al-Din al-Bahari wa Baghdad, aliyefika kutoka Maka mwaka 1577 na kuishi Jazira kwa miaka saba na kuwafunza Wasudani wengi mashuhuri kanuni za Kadiriyya. Tarika nyingine ni ya Shadhiliyya, ambayo ililetwa Sudani na mtu wa ukoo wa Ja'aliyyun aliyepata mafundisho yake huko Hijaz.

Usufii ulipoanza kusambaa katika Ufalme wa Funji ulikuwa tayari umepoteza umaarufu wake katika ulimwengu wa Waislamu na umetiwa doa na baadhi ya vitendo vyake visivyokubalika katika Uislamu wa kirasmi. Watu waliamini kuwa baraka hupatikaua kutoka kwa watu watakatifu ambao huwa ni kiungo kati ya binadamu na Mungu. Hivyo madhehebu ya watakatifu yalitiliwa mkazo. Walimu wa Kisufii walipewa ardhi ya bure au walisamehewa kulipa kodi, na baadhi yao walikuwa na ushawishi mkubwa kisiasa, kama ilivyokuwa kwa Idris wad al-Akbar na Majadhib. Watawala na raia waliwaheshimu masufii kuliko walivyowaheshimu wanasharia.

Wanasharia walipoona heshima waliyopewa washindani wao masufii, walijaribu kuchanganya ufundishaji wa sharia na mamlaka ya Kisufii. Maendeleo haya yalijidhihirisha katika matumizi ya wenyeji ya dhana kadha katika karne ya kumi na saba, wakati cheo cha *faki* (upotoshaji wa neno *fakih*, mwanasharia) kilipotolewa bila ubaguzi kwa wanasharia na masufii. Mafaki walianzisha vituo vingi vya dini, na walileta kiwango fulani cha utangamano katika jamii gilgili na mchanganyiko ya

Wafunji. Raghba yao ya kueneza dini haikuishia katika ufalme wa Funji, bali mwanga wake ulimulika hadi Kordofan, Darfur na Borno.

## Biashara na dola


Njia kuu za biashara zilipitia katika sultani Fur na Funji na kuziunganisha na Misri na Bahari ya Shamu. Zilikuwa na dhima muhimu ya kuimarisha uhusiano wa kitamaduni na kiuchumi na ulimwengu wa nje. Masultani wa Fur na Funji, kama watawala wengine wa ukanda wa Sudani, walihimiza biashara ya masafa marefu. Watumwa, dhahabu, manyoya ya mbuni na bidhaa nyingine za Afrika zilibadilishwa na nguo laini za pamba, silaha, mapambo ya vito, na vitu vingine vya anasa. Mbali na ushuru wa forodha waliokusanya kutokana na bidhaa zilizopitishwa katika maeneo yao, masultani walihitaji vitu vya anasa kwa ajili ya ufahari na kuwazawadia wafuasi wao waaminifu.

Biashara ya nje ilifuata njia kuu mbili: njia ya magharibi hadi mashariki, na njia ya kusini hadi kaskazini. Njia ya kwanza iliunganisha Borno-Wadai na Sennar kupitia Kobbie na Kordofan. Kutoka Sennar ilikwenda hadi Koz Rajad na Sawakin ama moja kwa moja au kupitia Shandi. Kupitia njia hii, iliyojulikana kama Barabara ya Sudani, Sudani ya Mashariki ikawekwa wazi kwa athari za utamaduni kutoka Sudani ya Magharibi na Afrika Kaskazini. Barabara ya Sudani ilitumiwa na wanazuoni Waislamu wenyeji na mahujaji ambao hawakumudu gharama za kukatisha jangwa na misafara kupitia Misri. Mahujaji wengi walisafiri kwa miguu na walinufaika kwa kupata ulinzi wa Waislamu. Waliishi kwa kupewa hisani au waliuza punda, vitabu na vitu vingine.

Njia ya pili ilianzia Sennar, ikapitia Kerri na kukatisha jangwa la Bayuda hadi Asyut katika Misri ya Juu kupitia Dunkula na Salima. Hata hivyo maasi ya Shaykiyya katika karne ya kumi na nane yaliivuruga njia hii, hivyo iliachwa na badala yake ikatumika njia iliyofuata ukingo wa mashariki wa mto, ikakatisha Atbara na ikaendelea kupitia jangwa la Nubia hadi Isna katika Misri ya Juu. Katika Oasisi ya Salima, njia ya Mto Nili iliungana na *Darb al-'Ar ban'in* (Barabara ya Siku Arobaini), ambayo ilikuwa njia kuu ya biashara kati ya Fur na Misri. Njia hiyo ilianzia Kobbie na ikaendelea hadi Asyut kupitia Oasisi za Salima na Kharja.

Kutokana na kuzungukwa na eneo kubwa la bara, na nafasi yake iliyofaa kwa ulinzi na biashara, Sennar iliweza kuwa kituo kikuu cha biashara. Wageni wengi waliofika Sennar walikuwa wafanya biashara na wachache walikuwa mafundi. Biashara kubwa zaidi ilikuwa mikononi mwa ma-*Jallaba* (wafanya biashara) wa Kisudani. Aidha Ma-*Jallaba* hao, kutokana na moyo wao wa kibiashara, walichangia sana maendeleo ya biashara ya Fur. Huko Darfur, biashara ya masafa marefu ilikuwa takriban chini ya udhibiti wa dola. Kupitia misafara hii ya biashara usultani wa Fur ulijulikana vizuri katika ulimwengu wa nje.

Maendeleo ya kibiashara ya Sennar yaliathiriwa na uadui kati ya Funji na Fur kuhusiana na Kordofan, na pia mashambulizi ya Washilluk, ambayo yaliifanya




7.1 Njia za Biashara za Sudani (kwa mujibu wa Y.F. Hasan)

barabara ya Kobbie-Sennar kutokuwa salama. Hivyo misafara iliamua kutumia njia ya kaskazini kupitia Shandi, mji ambao, katika karne ya kumi na nane, ulikuwa kituo kikuu cha biashara na ulichukua nafasi ya Sennar kama soko la biashara ya Ethiopia na Fur.

Upande wa mashariki, Wahadariba wa Sawakin walikuwa pia wakijishughulisha na biashara ya masafa marefu kati ya Bahari ya Shamu na Mto Nili. Walinunua bidhaa za Kiafrika na watumwa kutoka Shandi na walizibadilisha na bidhaa za kutoka India pale Sawakin, ambapo palikuwa soko kubwa la watumwa baada ya Kairo na Massawa.

Upelekaji wa watumwa kuelekea kaskazini hadi Mto Nili ulianza tangu kale. Waarabu waliendeleza jambo hilo walipofanya *bakt* (mkataba) na Wanubi. Watumwa mia nne kila mwaka walipelekwa kutoka Nubia na ulimwengu wa Waarabu ulipendelea kuwatumia kwa kazi za nyumbani. Walikuwa wapiga upinde wazuri na waliunda vikosi mahiri vya wapiganaji. Kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya watumwa weusi, Nubia haikuweza kukidhi mahitaji ya ulimwengu wa Waislamu na hivyo Waarabu wafanyabiasha iliwalazimu kutafuta vyanzo vingine huko kusini na kusini-magharibi mwa Nubia. Hivyo biashara ya watumwa ikapata umuhimu ambao ilibaki nao hadi miongo ya mwisho ya karne ya kumi na tisa. Mwanzoni, watumwa walikuwa Wanubi na Wabeja, lakini baadaye waliingizwa kutoka Kordofan na Darfur na hatimaye Bahr al-Ghazal, Borno-Wadai na maeneo mengine ya *Bilad al Sudan* ya kati.

Watumwa walipatikana kwa njia ya vita, utekaji au kununua, na jukumu la Waarabu waliouza na kununua watumwa lilitofautiana katika vipindi na mahali tofauti. Inaelekea kuwa Waarabu wafanyabiashara hawakutafuta watumwa wao wenyewe moja kwa moja (isipokuwa katika karne ya kumi na tisa), bali waliwategemea Waafrika au watu wa kati.

Mahitaji ya nje ya watumwa weusi kwa ajili ya majeshi yalipungua wakati wa Waayubi (1172-1251), ambao waliwatumia askari weupe badala ya weusi. Mamluki (1251-1517) walifuata sera hiyo hiyo, na kwa kipindi chote cha utawala wao karibu jeshi lote liliundwa na watumwa weupe tu. Hata hivyo mahitaji ya watumwa weusi yaliendelea katika majimbo mengine, hususan katika sultani mpya za Funji na Fur ambako watumwa weusi waliunda kiini cha jeshi. Katika karne ya kumi na tisa Muhammad Ali Pasha, Gavana Mkuu wa Misri, alianza kuwandikisha watumwa weusi katika jeshi la kisasa, na wakati wote wa karne ya kumi na tisa jeshi la Misri lilikuwa na idadi kubwa ya askari wa Kisudani.

## Kudidimia kwa Usultani wa Funji

Kuanguka kwa biashara ya Sennar kuliambatana na kurudi nyuma kisiasa. Kuongezeka kwa hatua za kikandamizi zilizochukuliwa na Badi IV kuliwafanya baadhi ya makabaila wa Kifunji ambao waliambatana na Abu Likaylik kwenda Kordofan wamshawishi jenerali huyo amwangushe sultan, jambo ambalo lilifanyika mwaka 1762. Ushindi wa uasi wa Abu Likaylik ulikuwa ni hatua muhimu katika

historia ya usultani. Sheikh Muhammad Abu Likaylik na warithi wake, mawaziri, wakawa ndio watawala halisi wa kurithi (au wasimamizi wa utawala), hadi ufalme ulipoanguka. Masultani wa Funji hawakuwa chochote bali vikaragosi wao tu.

Abu Likaylik alipofariki mwaka 1776-7, Wafalme wa Funji walikula njama na magavana wa majimbo, hususan wa Waabdallabi, kuwaondoa mamakamu wa maliki. Miaka hamsini ya mwisho ya usultani wa Funji iliambatana na mivutano, maasi na vita vya wenyewe kwa wenyewe miongoni mwa vikundi vyenye kupingana.

Upande wa kaskazini, mamlaka ya machifu wa Kiabdallabi katika bonde la Nili yalikuwa pia yanadidimia: Wasa'dab wa Shandi na Wamajadhib wa al-Damar wakawa takriban watu huru. Wapiganaji wa Shaykiyya waliolitawala jimbo la Dunkula, walikuwa wanabughudhiwa mara kwa mara na Mamluki wa Misri. Huko magharibi, Wafunji walibughudhiwa na usultani wa Fur, mwishowe walifukuzwa kutoka Kordofan. Wakati majeshi ya Kituruki-Kimisri yalipoikaribia Sennar mwaka 1821, usultani ulikuwa dhaifu mno kuweza kupinga uvamizi huo.

## *Usultani wa Fur*

Usultani wa Fur ulikuwa ni mmojawapo wa falme za Kiislamu katika ukanda wa savana wa mashariki mwa *Bilad al-Sudan*. Upande wa magharibi ulitenganishwa toka usultani wa Wadai na falme ndogo ndogo huru ambazo utii wao uligawanywa kati ya sultani hizo mbili. Upande wa mashariki kulikuwa na nyanda za Kordofan, ambazo zilijitandaza kati ya usultani wa Fur na ufalme wa Funji; nyanda hizo zilikuwa chanzo cha migogoro kati ya madola haya mawili. Jangwa la Libya kwa upande wa kaskazini na Bahr al-Arab kwa upande wa kusini ndiyo ilikuwa mipaka ya asili ya dola hili. Jimbo la kati lililomilikiwa na Jabal Marra, chimbuko la usultani wa Fur, lilikuwa ndiyo makutano ya njia kadha za biashara, ambazo zilikuwa chanzo cha ustawi wa uchumi, mihamo ya watu na athari za kitamaduni.

Chimbuko la usultani wa Fur halieleweki vizuri, lakini kutokana na mapokeo simulizi, dola la Fur lilitanguliwa na nasaba tawala mbili za wenyeji: Wadaju na Watunjur. Ufalme wa Wadaju ulistawi katika karne ya kumi na tatu na kumi na nne, lakini mwanzoni mwa karne ya kumi na tano Wadaju walipoteza udhibiti wa biashara na Watunjur wakatawala baada yao. Inawezekana ni wakati wa utawala wa Watunjur ambapo athari za Uislamu zilianza kujitokeza. Athari hizo zilitokana na uhusiano mkubwa wa kibiashara na ulimwengu wa Kiislamu na kujipenyeza taratibu kwa Waarabu wahamiaji. Hata hivyo, usilimishaji halisi wa jimbo hilo ulianza na kuasisiwa kwa usultani wa Fur mwanzoni mwa karne ya kumi na saba.

Usultani ulichukua jina lake kutoka kwa Wafur, kabila la Wasudani lililoishi karibu na Jabal Marra, na ambalo kutokana na sababu zisizozuilika liliacha makazi yake ya milimani na kwenda kuishi kwenye savana. Usultani wa Kayra ulistawi kwenye miaka ya 1640-1874. Mwaka 1898 ulifufuliwa tena, na hatimaye uliunganishwa na Sudani ya Waingereza-Wamisri. Sulayman Solongdungu pengine ndiye aliyeanzisha ukoo wa kifalme (t. 1640-1660). Anakumbukwa kuwa alikuwa

mtiishaji aliyewafukuza Watunjur na kuunganisha eneo la Jabal Marra.

Sera ya kujipanua na kujiimarisha aliyoianzisha Sulayman iliendelezwa na waliomfuata, ambao walijipanua kuelekea kaskazini na kaskazini-magharibi. Ahmad Bukr b. Musa (t. 1682-1722) aliliunganisha dola muhimu kiulinzi la Dar Kimr. Upanukaji huu uliukutanisha ukoo wa Kayra na Wazaghawa, ambao maeneo yao yalikuwa ndiyo chanzo cha migogoro kati ya sultani za Wadai na Darfur. Wadai ililazimishwa kulipa ushuru kwa usultani wa Kayra, ushuru ambao awali ulilipwa kwa wafalme wa Tunjur. Sultan Ya-kub alipogoma kulipa ushuru na kuvamia Darfur, Burk hatimaye alimshinda na kumfukuza.

Mpaka mwishoni mwa karne ya kumi nane historia ya kisiasa ya Darfur ilitawaliwa na mapambano kati ya vikundi vya ukoo tawala wa Kayra vilivyopingana: Masultani waliotaka kuweka mamlaka yote mikononi mwao na wanamfalme wengine ambao walitaka kuimarisha nguvu za ukoo kwa ujumla. Mgogoro ulilipuka wakati Sultani Bukr alipotaka kila mtoto wake arithi usultani kwa zamu. Alikuwa na watoto mia moja, watano kati ya hao walirithi usultani wa Fur. Mrithi wake wa kwanza, Muhammad Dawra alianza kwa kuwafukuza ndugu zake na kumteua mtoto wake kuwa mrithi wake. `Umar Lel alipoingia madarakani alikumbana na chuki kutoka kwa baba zake wadogo, watoto wa Bukr. Sulayman ibn Ahmad Bukr alitafuta bila mafanikio kuungwa mkono, kwanza na Wamusabbaat, baadaye na sultani wa Wadai. Hata hivyo vitendo vyake hivyo vilimchokoza Umar Lel kuivamia Wadai katikati ya karne ya kumi na nane. Baada ya mapigano makali sultani wa Wadai, Muhammad Jawda, alilishinda jeshi la Fur na kumteka sultani.

Mgogoro uliendelea wakati wa utawala wa sultani wa sita, Abu'l-Kasim ben Ahmad Bukr. Ili kuimarisha nafasi yake, aliwapiga ndugu zake na kuandikisha jeshi la watumwa badala ya askari wa jadi wa kabila, hatua mbayo iliwaudhi watu mashuhuri nchini. Kwa hakika hatua hiyo ilileta wasiwasi sawa na ule uliokuwapo katika ufalme wa Funji wakati wa utawala wa Badi IV.

Katika mapigano dhidi ya majeshi ya Wadai, Abu'l Kasim alikimbiwa na viongozi wa vita wa jadi na askari wa kikabila. Aliachwa peke yake na jeshi lake la watumwa na kushindwa katika vita hivyo. Mamwinyi wa Kifur na wapiganaji wa jadi walitangaza sultani mpya, Muhammad Tayrab ibn Ahmad Bukr, ambaye aliiga mfano wa watagulizi wake na kuunda jeshi la kudumu la watumwa lililojulikana kama *Kurkwa* (wana-mikuki). Mmoja wao, towashi aliyeitwa Muhammad Kurra, akawa kiongozi wa watumishi wa kiume wa mfalme. Baadaye alipata dhima kubwa zaidi nchini humo.

Baada ya kushindwa kupanua himaya yake kuelekea magharibi dhidi ya adui wake, sultani wa Wadai, Tayrab alifanya mkataba naye ambao uliendelea kuheshimiwa kwa miaka mia moja. Kisha aligeukia upande wa mashariki dhidi ya Wamusabba`at ambao walikuwa wanajaribu kuanzisha dola lenye nguvu huko Kordofan. Tayrab huenda pia alikuwa na malengo ya kiuchumi, kama vile kudhibiti njia za biashara na vyanzo vya watumwa na dhahabu kusini mwa Kordofan. Inawezekana lengo lake la muda mfupi lilikuwa ni kuwafukuza kaka zake na watu

mashuhuri kutoka Darfur ili kumwezesha mtoto wake kurithi ufalme hapo baadaye. Akiwa na jeshi kubwa, Tayrab alimvamia Hashim, Sultan wa Kordofan. Hashim alitorokwa na jeshi lake na kukimbilia kwenye ufalme wa Funji. Kordofan ilibakia mikononi mwa Wafur hadi Waturuki-Wamisri walipoiteka nchi hiyo.

Kifo cha Tayrab kilifuatiwa na mapambano makali kuhusu urithi wa ufalme. Hatimaye mtoto wa mwisho wa Ahmad Bukr aliyeitwa Abd al-Rahman akaibuka mshindi wa vita vya wenyewe kwa wenyewe, baada ya kupata msaada wa Muhammad Kurra. Sultani mpya alimzawadia Muhammad Kurra nafasi ya *Ab Shaykh*, cheo kilichompa madaraka makubwa. Kuanzia 1790 hadi 1804 Muhammad Kurra alikuwa ndiye mtu mwenye nguvu zaidi katika dola.

`Abd al-Rahman aliadhimisha ushindi wake kwa kujenga makao mapya ya ufalme (*fashir*) kule Khor Tandalti, mashariki ya Jabal Marra, mwaka 1741/2. Kabla ya hapo masultani wa Fur hawakuwa na makao makuu maalumu. Kukua kwa makao makuu ya kudumu kule al-Fashir ua kuimarishwa kwa nguvu za uunganifishaji wa dola na athari za usilimishaji kuliufanya utawala wa `Abd al-Rahman kuwa kilele cha usultani wa Kayra. Mahusiano na ulimwengu wa nje yaliongezeka kupitia biashara na kufika kwa walimu wa dini. `Abd al-Rahman alibadilishana zawadi na sultani wa Umruki, ambaye alimpa cheo cha heshima cha *al-Rashid* (Mtenda Haki). Pia aliwasiliana na Bonaparte mnamo mwaka 1799 wakati Ufaransa ilipoikalia Misri.

Kukubaliwa kwa Uislamu huko Darfur pengine kulitokea polepole zaidi kuliko ilivyokuwa katika ufalme wa Funji. Kasi yake iliongezeka katika karne ya kumi na nane, japo miviga na matendo ya dini za Kiafrika yaliendelea kufanywa sambamba na Uislamu katika Ikulu ya Kayra kwa kipindi fulani. Uenezaji wa Uislamu ulihimizwa na Ahmad Bukr aliyejenga misikiti na shule, ilihali Muhamad Tayrab alileta vitabu vya dini kutoka Misri na Tunisia. Abd al-Rahman al Rashid, ambaye alikuwa mwanazuoni wa Kiislamu, alihimiza wanasharia na masufii kutoka nchi nyingine kuja kuishi katika usultani wake. Kati ya hao ni Mwarabu mmoja wa Tunisia aliyeitwa `Umar al-Tunisi, ambaye baadaye alifuatiwa na mwanawe, Muhammad, ambaye maelezo yake (ya maandishi) kuhusu Darfur ni moja ya vyanzo muhimu kwa historia ya nchi hiyo. Wanazuoni wengine walitokea Misri, Hijaz, Sudani ya Kiniloti na *Bilad al-Sudan* ya magharibi. Ili kuwavutia kuja nchini mwake, sultani aliwapa ardhi walimu wa dini kupitia mfumo wa *hakura* (msamaha wa kodi) kama ilivyokuwa katika ufalme wa Funji.

Kufikia mwishoni mwa karne ya kumi na nane, sultani na washirika wake wa karibu, ambao hawakuwa na mizizi katika kabila lolote la hapo, walikuwa wamekwisha piga hatua kubwa katika kuendeleza biashara ya nje na kutumia asasi za Kiislamu kutawala nchi. Hali hii ya mambo ilisaidia kubadilisha miundo ya kikabila ya dola na kudhoofisha matendo ya kijadi ya kidini. Kuibuka kwa tabaka jipya la wafanyabiashara, wanasharia na wacha Mungu kulichangia sana katika kuleta mabadiliko hayo. Hata hivyo, nasaba tawala ya Kayra, licha ya uhusiano wake wa kiukoo na Waarabu, ilikuwa na mizizi yake miongoni mwa Wafur. Hivyo, ingawa Kiarabu kilitumika katika diplomasia na biashara, lakini Kifur kilibakia kuwa ndiyo

lugha ya baraza la sultani.

`Abd al-Rahman alipofariki mwaka 1801/2, mtoto wake Muhammad al-Fadl alirithi ufalme, akisaidiwa na Muhammad Kurra. Lakini sultani mpya punde aligombana na mtu huyu ambaye alikuwa amemteua kuwa waziri wake mkuu na hivyo akamuua. Utawala wa Muhammad al Fadl ulidumu kwa miaka arobaini; katika kipindi hicho, dola lilianza kudidimia.

## *Sudani ya Kusini*

Pamoja na kuwepo kwa kazi makini za anthropolojia zilizotolewa na wanazuoni maarufu, utafiti wa kihistoria kuhusu Sudani ya Kusini bado upo katika hatua zake za mwanzo. Hili ni kweli pia kuhusu utafiti wa akiolojia na isimu-historia. Hata hivyo, kutokana na ushahidi huu mdogo taarifa za jumla zinaanza kujitokeza. Kwa mfano, kutokaua na ushahidi wa kiisimu inazidi kudhihirika kuwa utamaduni wa Waniloti na pengine ule wa Sudani ya Kati una mizizi yake katika Sudani ya Kusini.

Eneo kubwa zaidi la Sudan ya Kusini na Uganda ya kaskazini huenda lilikaliwa na watu waliozungumza lugha za Sudani ya Kati hadi miongo ya mwisho ya milenia ya kwanza, wakati eneo hilo lilipoanza kutwaliwa na wazungumzaji wa Kiniloti cha mashariki na magharibi. Kwa hakika moja ya mada kuu za historia za kipindi chetu ni namna watu wa Sudani ya Kusini "walivyonilotishwa" taratibu. Leo eneo hilo karibu lote limekaliwa na Waniloti; Wamoru na Wamadi, wanaoishi magharibi ya mto wa Nili Nyeupe, ndio pekee waliobakia kutukumbusha kuwa hapo zamani eneo hilo lilikaliwa na wazungumzaji wa lugha za Sudani ya Kati.

Hivi karibuni, Roland Oliver alijaribu kuweka usanisi wa ushahidi wa kiakiolojia wa enzi za chuma kwa ajili ya historia ya awali ya eneo hili ambao unaelekea kuithibitisha picha ya kiisimu. Alidhani vilikuwepo vituo viwili vya utamaduni wa enzi ya chuma, kimoja kikiwa upande wa mashariki wa mabwawa ya Nili katika nchi za mpakani mwa Sudani na Ethiopia, na kituo kingine kikiwa katika uwanda wa mawe ya chuma wa bonde la mito ya Nili na Kongo. Vituo hivi viwili, kimoja cha Kiniloti na kingine cha Kibantu, vilitenganishwa na utamaduni wa Sudani ya Kati. Waniloti walisogea upande wa kusini hadi kwenye eneo la Wabantu, na matokeo ya kukutana kwao yakawa ni kwa wazungumzaji wa Kibantu kuanza ufugaji shadidi.

Kuhusiana na Sudani, Oliver alipambanua vipindi viwili vya enzi za chuma miongoni mwa Waniloti. Katika majimbo ya Equatorial Magharibi na Bahr al-Ghazal, kipindi cha kwanza kinahusianishwa na wafugaji wa enzi za chuma, Waluel, ambao walifuga ng'ombe wasiokuwa na nundu na wakajenga matuta ili kujikinga na mafuriko wakati wa masika.

Mwanzo wa Enzi ya Nyuma ya Chuma ya Waniloti inaonekana ulitokea wakati uleule wa kutokea kwa ng'ombe wenye nundu katika jimbo la Bahar al-Ghazal na kukamilika kwa utaratibu wa kuhamahama kutafuta malisho. Ng'ombe wenye nundu huenda walisambazwa upande wa kusini na Waarabu wa Bakkara baada ya kuanguka kwa ufalme wa Dunkula. Hivyo kujipenyeza kwa Waarabu katika Sudani ya

Kaskazini na ya Kati katika karne ya kumi na tatu na kumi na nne huenda hakukufanyika kwa bahati tu wakati wa uhamaji wa Waniloti wa Magharibi, bali ndiko kulikosababisha uhamaji huo.

Kwa hiyo kuenea kwa haraka kwa Waniloti wa Magharibi na Mashariki kuelekea upande wa kusini na mashariki kunaweza kuhusishwa na kuingia kwa ufugaji shadidi wa ng'ombe pamoja na kilimo cha nafaka. Mchanganyiko huo ulileta mbinu ya uzalishaji wa chakula iliyofaa kwa maeneo makavu ambayo iliwawezesha Waniloti kukalia maeneo mengi ambayo awali yalikwepwa na wazungumzaji wa lugha za Kibantu.

## Ufalme wa Shilluk

Katika Sudani Kusini, Washilluk ndio sehemu kubwa zaidi ya kundi la Waluo wa kaskazini, wengine wakiwa ni Waluo wa Bahr al-Ghazal na Waanywa, waliotagaa katika mpaka wa Sudani na Ethiopia. Awali, mwanzoni mwa karne ya kumi na sita, Washilluk walikaa karibu na Malakal, baada ya kuwafukuza Wafunji, ambao waliishi kwenye eneo la makutano ya mito ya Nili na Sobat. Eneo hili linadhibiti mafikio ya Ziwa No, na hivyo kulipa ziwa hilo umuhimu mkubwa kiulinzi. Kundi hili dogo la wazungumzaji wa Kiluo lilijumuisha Wafunji, Wanuba na vikundi vingine. Vikundi vyote hivi vyenye utamaduni na uchumi unaotofautiana viliunganishwa katika chungu kimoja cha historia kuunda kile kilichokuja kuitwa taifa la Washilluk kuanzia nusu ya pili ya karne ya kumi na saba.

Katika karne hii ya kuinukia kwao, Washilluk walianzisha uchumi mchanganyiko ulojikita kwenye ufugaji wa ng'ombe na kilimo cha nafaka. Kimsingi walikuwa wakazi wa mahali pamoja na hawakuhamahama kutafuta malisho. Waliishi katika msululu wa vijiji kando ya ukingo wa mashariki wa mto Nili, baina ya Muomo wa Tonga.

## Mipaka na kutegemeana kijamii na kiuchumi

Kufikia mwanzo wa karne ya kumi na saba, ukingo wa magharibi ya mto Nili ulikuwa tayari na idadi kubwa ya watu, na Washilluk walianza kujipanua katika maeneo mawili ya mpakani. Upande wa kaskazini walijaribu kuchukua bonde la Nili Nyeupe kati ya Muomo na Alays. Eneo hilo halikufaa kwa kilimo lakini lilikuwa na wingi wa wanyamapori, samaki na asali. Tangu enzi za utawala wa Odak Ochollo (c.1600-1635) hadi 1861, Washilluk walilitawala jimbo hili, ambalo Waislamu waliliita "Bahr Scheluk,"

Eneo la pili la mpakani lilikuwa kati ya mto Nili na milima ya Nuba. Mapokeo simulizi huzungumzia mno shughuli za Washilluk na Wanuba katika eneo hili kiasi cha kudhihirisha kwamba lazima lilikuwa muhimu kwa mataifa yote mawili kabla halijakaliwa na Waarabu wa Bakkara katika nusu ya pili ya karne ya kumi na tisa.

Tunajifunza kutokana na mapokeo ya Washilluk kuwa wakati wa utawala wa Odak Ocollo Washilluk waliiunga mkono Darfur katika mapambano yake na usultani

wa Funji kwa lengo la kudhibiti biashara ya Nili Nyeupe. Baada ya Takali kusalimu amri, Wafunji na Washilluk walibaki wakikabiliana wenyewe kwa wenyewe kwenye ukanda wa Nili Nyeupe, huku wakiwa wamechoshwa na miongo mitatu ya vita.

Kuanzia kama mwaka 1630 Wajieng, kabila jingine la wazungumzaji wa Kijii, walivamia Funji ya kusini. Katika karne zote za kumi na saba na kumi na nane walijipanua hadi kufikia Jazira ya kusini, na hivyo kubadilisha taratibu uwiano wa madaraka katika jimbo hilo. Kuwepo kwa kabila la Wajieng kulikuwa ni tishio la kutosha kiasi cha kuwafanya Washillunk wa Wafunji washirikiane kupambana nao. Walifanikiwa kuwazuia kusambaa zaidi kuelekea upande wa kaskazini na magharibi na hata kuwalazimisha kusogea upande wa mashariki kuelekea mpaka wa Ethiopia.

Ushirika huu na Wafunji ulikuwa ndiyo mwanzo wa kutegemeana kijamii na kiuchumi ambako Washilluk walianzisha na vikundi mbalimbali kwa nyakati tofauti (Wafunji, Wajallaba, Waarabu wa Bakkara, maharamia wa Kiarabu, wafanyabiashara Wazungu na Wamahdi) ili kuwanyonya Wajieng. Muungano huu wa mara kwa mara wa Washilluk na vikundi mbalimbali kwa lengo la kuwanyonya ndugu zao wenye kuzungumza lugha ya Kijii unaonyesha kuwa umoja huo wa kijamii na kiuchumi haukuwa na waa lolote la itikadi za kibaguzi au kikabila. Itikadi ya ubaguzi wa rangi ni dhana iliyoingia Sudani ya Kusini baada ya utawala wa Kimahdiyya.

## Maendeleo ya asasi za kisiasa na kijamii

Kwenye nusu ya pili ya karne ya kumi na saba, maendeleo ya kisiasa yaliyotokea yaliathiri kwa kiasi kikubwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya nchi ya Washilluk. Licha ya kuwa taifa lenye watu mchanganyiko, Washilluk walikuwa na hisia ya umoja wa kitaifa, na utawala unganifu ulianzishwa chini ya *reth* (mfalme). Ukiritimba wa kifalme wa raslimali za uchumi na pia biashara ya kijanibu na ya masafa marefu pole pole ulianzishwa.

Majina matatu yanahusishwa na maendeleo haya katika historia ya Shilluk: Abudhok, malkia na binti wa Reth Bwoc na mmoja wa wanawake wengi wenye nguvu katika historia ya Shilluk, kaka yake, Dhokoth; na Tugo, mtoto wa Dhokoth. Reth Dhokoth (t.1670-1690) ni maarufu kwa kufanya mashambulio mengi katika Nili na upande wa magharibi hadi milima ya Nuba. Baa la njaa la mwaka 1684 (*umm Laham* kwa Kiarabu) pengine ndilo lililowafanya Washilluk wengi kusogea kaskazini kupora na kukaa katika "Bahr Scheluk." Mashambulio ya Dhokoth yalifanikiwa sana na yalileta mateka wengi.

Mafanikio ya kijeshi na kiuchumi ya Reth Dhokoth kwa kiasi kikubwa yalihusika na kuunganifishwa kwa mamlaka ya ufalme ambako kulikamilishwa na mwanawe, Togo (t.1690-1710). Togo alianzisha kijiji cha Fashoda na kukifanya kuwa makao ya kudumu ya Reth. Pia alirasimisha sherehe ndefu ya kusimikwa kwa Shilluk Reth. Sifa zake zilienea haraka ndani na nje ya ufalme wake.

Kufikia mwanzoni mwa karne ya kumi na nane, himaya ya Funji ilikuwa inasambaratika. Na kadiri nguvu za Funji zilivyodidimia, ndivyo nguvu za Washilluk zilivyoongezeka. Mwishoni mwa karne, usultani wa Funji ulianguka kabisa na hii

iliwawezesha Washilluk kuimarisha udhibiti wao kwenye Nili Nyeupe. Msafiri wa Kiingereza, W.G. Browne, ambaye aliishi Darfur kwa miaka minne (1793-96), alitoa taarifa kuwa Washilluk walikuwa wakiudhibiti kikamilifu mto Nili huko Alays, ambako waliweka kivuko cha kuivusha misafara ya wafanyabiashara waliokuwa wakisafiri kati ya Sennar na al-Obeyd.

### Kuanguka kwa mamlaka ya Washilluk

Wakati wa utawala wa Reth Nyakwaa (t. 1780-1820) Wajieng walihama kwa wingi kuvuka Mto Sobat na Washilluk, ambao kwa karibu karne moja na nusu walikuwa wanadhibiti kikamilifu eneo la Nili Nyeupe kutoka Ziwa No hadi Alays, walilazimika kukubali kuwepo kwa wazungumzaji wengine wa lugha ya Kijii katika eneo hilo. Lakini mengi yalikuwa yanawajia. Mwaka mmoja baada ya kifo cha Nyakwaa, majeshi ya Muhammad Ali Pasha, Gavana Mkuu wa Misri, yaliivamia Sudani na kuumaliza kabisa utawala wa Funji na kusimika utawala wa Kituruki-Kimisri. Mgongano na Washilluk haungaliweza kuepukika. Kuanzia mwaka 1821, licha ya upinzani wa kudumu wa Washilluk, mpaka wa Shilluk ulirudishwa upande wa kusini hatua kwa hatua kadiri Waarabu na utawala wa Kituruki-Kimisri walivyoichukua nchi.

Ili kuweza kuitawala Nili Nyeupe, Washilluk walilazimika kudhibiti maeneo yenye kufaa kwa usafiri wa majini. Walihodhi idadi kubwa ya vyombo vya majini na walikuwa wapiga makasia hodari. Wakati wa safari za uporaji au za kijeshi, vikundi vya mitumbwi thelathini au arobaini vilisafiri kwa pamoja na kufanya nguvu kubwa ya kijeshi katika ukanda huo. Lakini serikali ya Kituruki-Kimisri ilianzisha kiwanda cha meli kule Manjara mnamo mwaka 1826, na hivyo kuukomesha utamalaki wa jeshi la majini la Washilluk kwenye Nili Nyeupe.

## *Mataifa ya Bahr al-Ghazal*

Nchi iliyopo kusini mwa Bahr al Ghazal na magharibi ya mstari unaotoka Meshra al-Rek hadi pale mipaka ya nchi za Sudani ya sasa, Kongo na Uganda inapokutana, ilikaliwa na mataifa yenye asili ya familia mbili kuu za lugha: Ubangi (Niger-Congo) na Sudani ya Kati (Sahara-Nili). Wazungumzaji wa lugha za Sudani ya Kati waliishi eneo hili tangu enzi za kale; waliishi kando kando ya mito na walijikimu kwa kazi za kilimo cha nafaka, ufugaji wa ng'ombe na uwindaji. Wazungumzaji wa lugha za Ubangi walifika kutoka magharibi (Jamhuri ya Afrika ya Kati), na wengi wao walistakimu, ama magharibi mwa jumuiya zenye kuongea lugha za Sudani ya Kati, au baina yao, jambo ambalo linaeleweka ukizingatia uchache wa watu wanaoishi katika eneo hilo. Wanyaubangi walikuwa wakulima ambao mwanzoni uchumi wao ulitegemea viazi vikuu, lakini baadaye walijiingiza katika uzalishaji wa mazao ya nafaka au ndizi kutegemea mazingira ya sehemu inayohusika. Hawakufuga ng'ombe: na hii inaonyesha kuwa walikuwa na mtazamo tofauti na ule ya watu wa Sudani ya Kati kuhusu utajiri, na hasa kuhusu mahari.

Tunajua kidogo sana kuhusu maisha ya watu hawa kabla ya 1800 kwa sababu maendeleo ya karne ya kumi na tisa yalisababisha kuvunjika kwa jumuiya zao. Zaidi ya hayo, hakuna mapokeo simulizi yaliyoweza kupatikana yenye kuonyesha nini kilitokea kabla ya mwaka 1800. Nasabu pekee zinazorudi nyuma zaidi (hadi kati ya 1650 na 1705) ni zile za nasaba-tawala za koo tatu za Wabongo. Na hizo zinatueleza tu kuwa watu walikuwa tayari wanaishi katika eneo la Wau-Tonj mnamo karne ya kumi na nane. Kufikia mwaka 1800 wafanyabiashara ya watumwa kutoka Darfur walikuwa tayari wapo katika Dar Fertit na Dar Banda, na Wazande walikuwa wanaanza kuyapiga maeneo ya kusini zaidi.

Tunachoweza kusema kuhusiana na kipindi kinachoshughulikiwa katika sura hii ni kwamba Darfur ilianza kuidhibiti Dar Fertit kienyeji kabla ya mwaka 1800, na ilidai ushuru kutoka kwa wakazi wa jimbo la Hofrat-en-Nahas. Wakati huohuo, familia za Waarabu au Wafur zilijipatia uongozi wa vikundi vidogovidogo (vya wenyeji) katika eneo la Raga. Utafiti zaidi unahitaji kufanywa katika eneo hili lote, ambamo bado inawezekana kupata data juu ya mitindo ya maisha, biashara na miguro ya watu kabla ya 1800.

# 8

# *Moroko*


Katika juzuu la IV ilionyeshwa kwamba karne ya 15 ilitambulishwa kwa vitendo vya uchokozi wa Wahispania na Wareno dhidi ya Afrika ya Kaskazini, hasa dhidi ya Moroko. Kuanzia 1415, mwaka ambao Ureno iliteka Sabta, walikuwa tayari wamekwisha kuteka maeneo mengi kwenye pwani ya Atlantiki na kuyafanya vituo vya mashambulizi yaliyopenya hadi ndani ya Moroko.

Masharifu kadhaa wa Dara wakiongozwa na Abu Abd Allah, aliyejulikana kama al-Kaim bi Amr Allah (yule anayenyanyuka kwa amri ya Mungu) walijiteua wenyewe ili kupigana na "makafiri" na kuwatimua kutoka kwenye ngome walizokuwa wanakalia nchini humo. Tangazo la Al-Kaim bi-Amr Allah la mwaka 1511 liliashiria mwanzo wa unasaba wa kifalme wa Saadi. Mapambano yao yalidumu kwa kiasi cha miaka 40, na kwa upande mmoja yalilengwa dhidi ya Wareno na upande mwingine kwa wafalme wa Kiwattasi.

Huko kusini mwa Moroko, baada ya kipindi kifupi wavamizi wa Kireno walikuwa salama tu ndani ya ngome zao, na kufuatia hali hiyo ukoloni wa Kireno ulianguka kwa kasi kubwa sana. Wareno pia walitishiwa huko kaskazini na wapiganaji wa Sale ambao waliendelea kuwawinda na kuwafukuza kutoka Mamura kwenye mdomo wa mto Sebu.

Katika kipindi hiki, mapambano kati ya nasaba-tawala mpya ya Saadi na ile ya zamani ya Wattasi-Wamarini yalileta maafa makubwa kwa Moroko. Kwa bahati nzuri, baada ya vita ambavyo havikutoa ufumbuzi wowote kati ya sultan wa Kiwattasi, Ahmad, na sharifu Ahmad al-Araj huko Tadla mwaka 1527, walitia sahihi mkataba ambao ulimpatia Saadi eneo la Sus na Marrakesh na kuacha sehemu nyingine za nchi hiyo mikononi mwa Sultan, huku Fez ikibaki kuwa mji mkuu. Makubaliano haya yaliipatia Moroko miaka 12 ya amani, wakati ambapo Wasaadi waliunda upya vikosi vyao na kuelekeza nguvu zao kwenye mapambano dhidi ya Wareno.

Tukio muhimu la kwanza lilikuwa lile la kuteka Agadir, mji ambao sultan wa Kisaadi, kwa msaada wa mizinga mikali, alifanikiwa kuuteka baada ya kuuzingira kwa miezi sita. Kutekwa kwa Agadir kulileteleza kuhama kwa Wareno kwenye miji ya Safi na Azemmur mwaka 1542. Ushindi huu ulimfanya Muhammad al-Shaykh shujaa wa ukombozi wa taifa na kumletea sifa kemkem nchini kote. Sasa aliweza kuanza upya mapambano yake dhidi ya Wattasi na kujaribu kuliteka tena eneo la kaskazini ya




**8.1** *Moroko kwenye karne ya kumi na sita hadi ya kumi na saba*

Moroko, ambayo Wattasi walikuwa bado wakiitawala kwa mujibu wa mkataba wa Tadla.

Baada ya kumshinda kaka yake mpinzani, Ahmad al Araj, sasa Muhammad al-Shaykh, akiwa peke yake kiongozi wa Wasaadi, aliamua kuwashughulikia Wawattasi kwa mara ya mwisho na kuwania kuteka Fez. Kuichukua Fez kungemwesha kuwa mtawala mkuu wa Moroko. Mapambano kati ya nasaba ya zamani na nasaba mpya yalidumu kwa miaka 10, na yalihitimishwa kwa Muhammad al-Shaykh kuingia Fez mnamo Septemba, tarehe 13, 1554. Lakini Sultani alikuwa akihofia tishio kwa nchi yake kutoka kwa Waturuki wa Algiers. Kwa mtazamo wake hatari ya kweli kwa Moroko ilitoka kwa himaya ya Uturuki, ambayo ilikuwa imetiisha nchi zote za Kiarabu za Mashariki na Magharibi. Ili kulinda nchi yake dhidi ya uvamizi wa Waturuki, aliamua kuwalazimisha waondoke Afrika. Watoto wawili wa kiume wa sultan wa Kisaadi, Abdallah na Abd al-Rahman, tayari walikwisha chukua Tilimsan mwaka 1550, lakini Waturuki waliuchukua tena 1552.

Ili kufanikisha azma yake hii kubwa ya kuiteka Algeria, Muhammad al-Shaykh alitafuta maafikiano na Hispania. Mazungumzo yalipangwa na gavana Mhispania wa Oran, na pande zote mbili zilikubaliana kuandaa uvamizi wa Algiers. Askari wa farasi elfu mbili wa Hispania wakiwa wanalipwa na sultan walikuwa wajiunge katika operesheni hiyo iliyoongozwa na Moroko. Waturuki walipata fununu kuhusu matayarisho hayo na Serikali Kuu ya Uturuki ikatuma askari zaidi kushambulia Oran, ambayo wakati huo ilikuwa inatawaliwa na Hispania. Hata hivyo, kikosi cha majini cha Waturuki kilichokuwa kizingire kikosi cha Wahispania baharini, kilirejeshwa kwenda kupigana na kikosi cha majini cha Kikristo cha Andrea Doria kilichokuwa kinatishia mlangobahari wa Bosforusi. Sasa Sultan aliweza kugeukia azma yake ya kujaribu kuiteka Algeria. Alianza kwa kuuzingira mji wa Tilimsan na kufanikiwa kuuteka.

Mwaka 1557 sultan Muhammad al Shaykh aliuawa na mmoja wa walinzi wake ambaye alikuwa analipwa na serikali ya Kituruki. Lakini jambo hili halikuleta hitilafu yoyote kwenye azma ya Wasaadi ya kuendelea kuisafisha Moroko kutokana na kukaliwa na wageni na kuilinda dhidi ya uvamizi wa aina yoyote ile, hata wa Kiislamu. Khalifa mpya, Abu Muhammad Abdallah, ambaye alitangazwa kuwa sultan baada ya kuuawa kwa baba yake, alifuata sera za mtangulizi wake. Alijulikana kama al Ghalib Billah (mshindi kwa nguvu za Mungu). Alianza kwa kulijenga upya jeshi lake, kupata silaha za kisasa kabisa, na kuendesha kampeni ya kisaikolojia miongoni mwa watu kwa msaada wa *zawiya* na wa viongozi wa tarika. Al Ghalib Billah alipojihisi kuwa na nguvu za kutosha aliuzingira mji wa Mazagan na kikosi imara cha mizinga. Ingawa jaribio lake lilishindwa, lakini liliwadhihirishia Wareno kwamba ni lazima wajizatiti kupambana na nguvu hii mpya na halisi.

Sultan sasa alihisi kwamba tishio la Wareno ndani ya Moroko lilikuwa limeepushwa, akageukia kwenye kujenga ustawi wa ufalme wake. Alihimiza biashara na nchi za Ulaya hasa Ufaransa. Al Ghalib Billah alikuwa mmoja wa wajenzi wakuu katika nasaba ya Kisaadi. Alijenga msikiti mkubwa huko Marrakesh na kuukarabati upya msikiti wa Kimohadi huko Agadir Kasbah. Kwa ujumla utawala wake ulikuwa mtulivu na wenye

mafanikio, na alikufa kwa amani mwaka 1574.

Urithi wake ulidhihirisha kuwa mgumu zaidi. Kwa kukiuka sheria ya muda mrefu ya kwamba mwanamume mkubwa zaidi kwa umri katika familia ndiye aliyekuwa na haki ya kurithi badala ya mtoto mkubwa zaidi wa kiongozi aliyefariki, Muhammad, mtoto wa kiume wa al-Ghalib Billah alitawazwa kuwa sultani. Huyu sultani mpya alichukua jina la Mutawakkil, lakini bado anajulikana kwa jina lake la utani la al-Maslukha. Mawlay Abd al Malik, mwanamfalme mkubwa zaidi wa Kisaadi na ami yake al Maslukha, alidhani kwamba kisheria ufalme huo alikuwa ni wake. Wakati mtoto wa al-Ghalib Billah alipotangazwa sultan wa Fez, Mawlay alikimbilia Sijilmasa, kisha Algiers na hatimaye Konstantinople. Aliingia katika jeshi la Kituruki na kushiriki katika kutiishwa tena kwa Tunis, ambako alionyesha ushujaa mwingi. Aliporejea Konstantinople, alikuta Khalifa yuko tayari kumsaidia kuupata tena ufalme wa mababu zake. Akiwa na jeshi dogo alilopewa, Mawlay Abd al-Malik aliingia Moroko ambako hakukumbana na kipingamizi chochote, kwani watu wote walikuwa upande wake. Al-Mutawakkil alitelekezwa na jeshi lake, akalazimika kutoroka. Mawlay Abd al-Malik aliingia Fez Machi tarehe 31, 1576, akapokewa kwa shauku kubwa na umma wote.

Al-Mutawakkil alitorokea kusini na kufaulu kuchukua upya mji wa Marrakesh. Alishindwa tena kwa mara nyingine, lakini akafanikiwa kutoroka kuelekea kaskazini na kumwomba gavana wa Vélez de la Gomera kumpatia hifadhi katika mji wake. Ombi lake lilikubaliwa, kwa ruhusa ya Mfalme Filipo II, kwa sharti kwamba anaruhusiwa kufuatana na idadi ndogo tu ya familia yake.

Mawlay Abd al-Malik, baada ya kuachiwa huru angalau kwa wakati huo na mpwa wake, alianza kujenga upya jeshi na kupangilia upya nchi yake. Alimfanya kaka yake, Mawlay Ahmad, Khalifa wa Fez. Na ili kutunisha tena hazina ya serikali, hakupendelea kuongeza kodi mpya kwa watu wake bali alitafuta njia nyingine. Alipanua jeshi la majini, meli mpya ziliundwa na zile za zamani zilikalafatiwa. Sera hii ilisisimua ufundi sadifu wa aina mbalimbali na kuongeza biashara na sehemu nyingine za ulimwengu, hasa Ulaya, na kuleta mafanikio katika nyanja zote.

## *Vita vya Wafalme Watatu*

Katika karne ya 16, Ureno ilikuwa na himaya yenye nguvu ambayo ilijumuisha maeneo makubwa huko Amerika, Asia na Afrika. Wakati Sultan wa Kisaadi aliyeondolewa madarakani, al-Mutawakkil, alipoomba hifadhi huko Vélez de la Gomera, himaya hii ilikuwa ikitawaliwa na mfalme kijana aliyeitwa Don Sebastian, ambaye alikuwa na njozi za kuiteka Moroko, na kutoka pale kuliteka eneo lote la Maghrib, na kuendelea Mashariki ili kulikomboa kaburi la Kristo kutoka mikononi mwa Waislamu. Katika jitihada zake za kutafuta msaada wa kuupata tena ufalme wa Kisaadi, al-Mutawakkil alikuwa amemwendea mfalme wa Hispania bila mafanikio yoyote. Sasa alimwendea Don Sebastian, ambaye alichangamkia fursa hii iliyojitokeza ya kufanya safari ya kwenda kuishambulia Moroko, ambayo kwa kipindi kirefu amekuwa akiiwazia, na ambayo iliungwa mkono na wananchi wa Ureno.

Mawlay Abd al-Malik alipopata taarifa juu ya matayarisho yaliyokuwa yanafanywa na mfalme huyo kijana, alijaribu kumshawishi aachane na jusura hiyo ya pupa. Alimwandikia Don Sebastian barua ambayo ni ya kipekee katika historia ya diplomasia, siyo tu kutokana na maudhui yake bali pia kwa udhati wake, ili kumsbawishi kuuacha mpango wa uvamizi aliokuwa nao. Hifadhi za nyaraka za Paris zina tafsiri ya Kiitaliano ya waraka huu, tafsiri ambayo ilichapishwa katika kitabu cha Count Henry de Castries cha *Sources in, édites de l'histoire du Moroc*. Katika barua hiyo Sultani Mawlay Abd al-Malik alidhihirisha pia ujuzi wake wa diplomasia, kwa kuonyesha wazi kwamba mchokozi mkubwa katika ukanda wa Mediterania kwa kweli alikuwa ni mfalme wa Ureno.

Hata hivyo, Don Sebastian aliendelea kujitayarisha kwa vita na kutia nanga Asila (Arzila). Mawlay Abd al-Malik aliyekuwa akitambua vema hisi za heshima za Wareno, alimwandikia tena, akimwomba asiwavamie watu wasioweza kujitetea na kwamba amsubiri ili naye ajiunge katika vita hivyo. Wajumbe wa msafara wa Don Sebastian, hasa Muhammad al-Maslukh, walimshauri asisikilize ushauri huo kwani ulikuwa ni mtego. Kinyume chake, alitakiwa aharakishe mashambulizi na kuteka Larache na al-Kas al-Kabir. Lakini Don Sebastian aliamua kubakia palepale Arzila, ambapo alikaa kwa siku 19 hadi mkesha wa siku ya vita.

Vikosi vya Wasaadi viliondoka Marrakesh kuelekea kaskazini huku vikikusanya na kujumuisha idadi kubwa ya wapiganaji wa kujitolea. Zaidi ya hayo, Sultani alikuwa amemwomba kaka yake, Khalifa wa Fez, kumtangulia huko al-Kasr al-Kabir akiwa na vikosi vyake vya Fez na eneo lake, akiandamana hasa na wanajeshi waali, vijana wapiga mishale (Warima). Jeshi la Wasaadi lilipowasili al- Kasr al-Kabir, Mawlay Ahmad alikuwa tayari huko na Mawlay Abd al-Malik aliwaamuru wapiga mishale mara baada ya Don Sebastian kuvuka Wadi al-Makhazin kuharibu daraja la mto ili kuzuia Wareno wasipate njia ya kurudi baharini mara baada ya kushindwa.

Vita hivi vya "wafalme watatu," vinavyojulikana miongoni mwa Waarabu kama vita vya Wadi al-Makhazin na miongoni mwa wanahistoria wa Kihispania na Kireno kama vita vya Alcazarquivir, vilipiganwa Agosti, tarehe 4, 1578.

## Siku ya Vita

Siku ya Jumatatu asubuhi, mwishoni mwa mwezi wa Jumada II mwaka wa 986 Hijriya (Agosti 4, 1578), kambi mbili zilizokuwa zinapingana ziliandaa vita. Ilikuwa ni siku ya kihistoria, kilele cha karne ndefu za migogoro kati ya Waislamu na Wakristo ambayo ilianzia huko Spain na kuenea hadi Moroko.

Vikosi vilivyopingana viliandaa shambulio, kila kikosi kikitumia mbinu zake. Jeshi la Kikristo lilijipanga kwenye uwanja wa vita kwa mraba, kikosi maalum cha askari wa kigeni likiwa mbele; jeshi la Kijerumani lilichukua nafasi upande wa kulia, Wahispania na Waitaliano upande wa kushoto. Askari wa farasi wakisonga mbele pande zote mbili. Pia kulikuwepo na idadi kubwa ya kundi lililomuunga mkono Muhammad "Mpigwaji". Jeshi la Moroko lilikuwa kwenye muundo wa mwezi mwandamo, ambamo ndani yake Sultani Mawlay Abd-Malik, aliyekuwa mgonjwa, aliongoza vita hivyo kutoka kwenye

machela. Jeshi la farasi liliongoza ncha za "mwezi mwandamo" za jeshi hilo, huku askari wa miguu na wale wa mizinga wakiwa katikati.

Baada ya sala za alfajiri, amri ilitolewa ya kuanza mapigano. Askari wa kukodiwa waliwavamia Waislamu upande wa kushoto kwa kuwashtukiza. Sultani Abd al-Malik alinyanyuka kwenye machela yake kuwahimiza watu wake waendelee mbele. Jitihada hilo zilimfanya aishiwe nguvu kabisa, lakini kabla hajakata roho, alitoa amri kwamba kifo chake kisitangazwe, kwani vita vilikuwa ndio tu vinaanza. Jinsi vita vilivyoendelea ndivyo watu wengi walivyokufa pande zote mbili. Wakristo walirudi nyuma na kutoroka kuelekea kwenye daraja, ambalo walikuta limebomolewa. Kisha wengi walijaribu kuogelea ili kuvuka mto ule, lakini walichukuliwa na mkondo mkali wa maji na kuzama.

Don Sebastian alisimama kidete, akionyesha ushujaa mkubwa, hadi alipodondoka kwenye uwanja wa vita. Muhammad (Mpigwaji) alizama mtoni alipokuwa anajaribu kutoroka. Mwili wake uliopolewa na kupelekwa kwa Ahmad al-Mansur, ambaye alijitangaza mfalme baada ya ushindi ule - (ushindi uliompatia jina lake la al-Mansur, yaani "Mshindi"). Hasara iliyopatikana kwa pande zote mbili ilikuwa kubwa na mapokeo yanaonyesha kwamha kulikuwepo na kiasi cha wafungwa 14,000 wa Kikristo. Majadiliano yalifanywa kwa lengo la kukomboa mwili wa Don Sebastian, lakini al-Mansur alikataa malipo yoyote kwa dharau, hasa kwa vile fidia ya mateka wa kivita ilikuwa imempatia fedha nyingi ambazo wanahistoria wengine wanadai kuwa ndizo chanzo cha lakabu yake ya al-Dhahabi (Wa Dhahabu). Kwa hivyo aliurudisha mwili wa mfalme yule bila malipo ya aina yoyote.

## Matokeo ya Mapigano ya Wafalme Watatu

Vita hivi vya mkataa vilikuwa na matokeo ambayo kwa karne nyingi yaliathiri, sio tu Uislamu na Moroko, bali pia nchi za Ureno na Ulaya. Ushindi huo uliupatia ufalme wa Wasaadi nguvu mpya na kuiletea Moroko amani na ustawi.

Moroko ilishuhudia ongezeko kubwa katika uchumi, hasa katika tasnia ya sukari. Katika sanaa, usanifu majenzi ulianza na kuboreshwa kwa kiwango cha juu, huku ukihimizwa na ufalme wa Wasaadi na mabwanyenye wapya waliotajirika. Utulivu mpya uliopatikana kwa watu wa Moroko, na hisia zao za heshima, zilizalisha utajiri wa sanaa, ushairi na fasihi.

Vita hivi vilikuwa na athari kubwa kimataifa. Athari za Wareno katika nchi za Waislamu zilipungua kwa kiwango kikubwa, hasa katika nchi za Ghuba. Vita hivi vilikomesha tishio la vita vya msalaba dhidi ya nchi za Mashariki. Ushindi wa Wasaadi pia uliimarisha nguvu za himaya ya Uturuki, na Wazungu wana haki ya kuchukulia ushindi huu wa Moroko kama ushindi wa Waislamu wote.

Lakini ushindi huu pia ulisababisha Waturuki kuondokana na wazo la kuishinda Moroko, ambayo ilibakia nchi pekee ya Kiarabu iliyokuwa nje ya athari za Kituruki. Kwa hali hiyo lugha ya Kiarabu nchini Moroko iliweza kubakia halisi na safi bila athari za lugha ya kigeni.

## *Upanuzi wa Wasaadi katika karne ya kumi na sita*


Al-Mansur alitawala kwa robo karne na alijitolea kuunganisha nguvu za ufalme wa Wasaadi na kuendeleza ufalme wake kwa njia zozote zile zilizowezekana. Baada ya ushindi wa Wadi al-Makhazin, aliazimia kwenda kukomboa miji ambayo ilikuwa bado chini ya mikono ya Wazungu: Asila, Tangier, Sabta na Mazagan. Alifanikiwa kuwafukuza maadui waliokalia Asila (1589), lakini Tangier haikukombolewa hadi karne iliyofuata. Sabta iliingia mikononi mwa Mfalme Filipo II wa Hispania, ambaye alikuwa amerithi ufalme wa Ureno. Mji huo pamoja na Melilla na *presidios* nyingine tatu zilibakia chini ya utawala wa Wahispania hadi hii leo.

Ushindi wa Al-Mansur ulimshawishi kuangalia mbali zaidi ya mipaka ya jadi ya Moroko, akiwa na lengo la kuirudisha hali kama ilivyokuwa wakati wa Wamoravi na kuunganisha Uislamu. Katika safari yake ya Sudan, bila shaka nia huenda ilikuwa ni ile ya kawaida kwa mataifa yenye nguvu ya kutaka kujipanua.

Kabla ya kuanza kampeni hii al-Mansur aliitisha mkutano wa baraza la kivita ambamo alielezea mipango yake. Katika kitabu cha *Histoire du Moroc*, H. Terrasse anaandika, "Karibu kila mtu alipinga jaribio hilo, kwa vile lilikuwa la hatari mno na, isitoshe, lilikuwa ni la kuwashambulia Waislamu wengine." Maulama, ambao walikuwa wawakilishi halisi wa watu, vilevile walikuwa na maoni hayohayo. Lakini al-Mansur alipuuzia ushauri huo na kuamua yeye mwenyewe kuendelea na uvamizi wa Sudan. Hakuna haja ya kuelezea uvamizi huu kwa undani hapa, kwa vile maandishi yote ya kihistoria ya Moroko huelezea tukio hili.

Kifo cha Al-Mansur mwaka 1603 kilifuatiwa na kipindi cha kuyumbayumba kwa vile kulitokea mizozo isiyokwisha ya kugombania uongozi miongoni mwa warithi wake. Mizozo hiyo iliitosa Moroko katika dimbwi la damu kwa nusu karne. Katika sehemu zote nchini, wafuasi wa tarika za kidini walizuka kwa jina la uzalendo ili kurejesha amani na kupigana dhidi ya Wareno na Wahispinia, ambao walitumia vizuri fursa iliyojitokeza ya udhaifu wa viongozi wa mwisho wa ufalme wa Wasaadi kuizingira pwani ya Moroko. Kiongozi mashuhuri wa vita hivi kwa hakika alikuwa Abu Abdallah Muhammad al-Ayyashi wa Sale, ambaye alipigana kwa ushindi mkubwa dhidi ya Wareno huko Mazagan. Aliweza kuyatuliza kwa muda maeneo yaliyokuwa chini ya udhibiti wake, na hasa mji wa Fez. Ingawa alikuwa na ushindi wote huo hakuwahi kudai kuwa kiongozi mkuu, kwani alikuwa mtakatifu wa kweli. Aliuawa kwa amri ya maadui zake, Wa-*Morisko* wa Rabat, mwaka 1641.

Mwaka 1636-7, kwa mara ya kwanza katika historia ya Atlas ya Kati, mjukuuu wa Sheikh aliyejulikana duniani kote kwa usomi na utakatifu wake ajitangaza kuwa mfalme wa Moroko yote. Jina la laghai huyu lilikuwa ni Muhammad ibn M'Hammad ibn Abu Bakr al-Dalal. Babu yake alikuwa ameanzisha *zawiya* huko Atlas ya Kati ambayo ilikuja kuwa kituo cha mafunzo ya Kiislamu chenye sifa zilizokaribia kufanana na zile za Chuo Kikuu cha Karawiyyin huko Fez. Mafanikio ya chuo hiki ambacho pia kilikuwa nyumba ya utawa, yalimtia Muhammad ibn M'Hammad hamu zaidi ya kutawala, hasa kwa vile




8.2 Himaya ya Ahmad al-Mansur "Wa Dhahabu" (1578-1603) (na M. El Fasi)

udhaifu wa watawala wa mwisho wa Kisaadi ulimwachia mwanya wa kuendeleza azma yake.

Kufuatia kifo cha al-Mansur, watu kumi kati ya madhuria wake walianza kushindania uongozi kwa zaidi ya nusu karne. Wawili kati yao waliweza kutawala kwa zaidi ya miaka ishirini, kipindi ambacho kilikatishwakatishwa wakati kaka zao au binamu zao walipochukua uongozi na kuupoteza ghafla, bila kuwataja wale waliodai madaraka miongoni mwa viongozi wa zawiya na majasuri wengine. Wote hawa waliodai kiti cha enzi cha Moroko walijifanya kuwa wahifadhi wa umoja wa nchi na watetezi wa serikali imara.

Hatuna budi kutaja maasi ya Washibana ambao walianzisha utawala huko Marakkesh uliodumu kwa muda mfupi baada ya kuuawa kwa sultani wa mwisho wa Wasaadi. Washibana walikuwa ni kikundi kidogo cha Waarabu (Wanomadi wa Kiarabu) ambao walikuwa wametimuliwa na Wafatimi kutoka Kairo na kuvamia Maghrib kwa vipindi, wakiangamiza kila kitu walichokumbana nacho. Katika karne ya 12 walikuwa wameshaletwa Moroko na Mmohadi Yakub al-Mansur. Hatimaye walilowea kwenye mabonde yenye rutuba ya pwani ya Atlantiki, na wao ndio waliohusika na kuleta Uarabu nchini Moroko. Mwaka 1658-9 kadhi wa Kishibana aliyeitwa Abd al-Karim ibn Abu Bakr al-Shbani na kujulikana kama Karrum al-Hajj aliibuka huko Marrakesh dhidi ya Sultani Ahmad, aliyejulikana kama Mawlay al-Abbas. Alimwua na kujitangaza Sultani na kuingia ikulu ya mfalme. Utawala huu uliduma kwa kiasi cha miaka 10, na uliambatana na uporaji, uonevu na ukatili wa Karrum al-Hajj. Hata wafuasi wake na wale waliomuunga mkono walianza kutafuta njia ya kumwondoa na aliuawa na mtu wa karibu sana naye. Mtoto wake wa kiume, Abu Bakr ibn Abd al-Karim alitangazwa sultani, na alitawala kwa muda hadi kifo chake, siku arobaini kabla ya kuwasili kwa sultani wa Kialawi, Mawlay al-Rashid huko Marrakesh.

## *Masultani wa mwanzo wa nasaba ya Waalawi*

Heshima ya kuunda serikali ya kudumu, yenye nguvu na yenye manufaa iliiangukia nasaba ya Masharifu wa Kialawi, ambao wameitawala Moroko kwa karne tatu na nusu. Waalawi ni familia ambayo imethibitishwa kisayansi na wanazuoni wa Moroko kuwa ilitokana na Nabii (Muhamadi).

Madhuria wa familia hii, iliyoundwa na al-Hasan ad-Dakhil, waliunda tabaka la watawala wa kidini ambao walijipatia hadhi kubwa miongoni mwa watu wote wa Tafilalet. Mjukuu wa Al-Hasan, Mawley Ali al -Sharif, alipata umashuhuri mkubwa. Alikuwa na watoto tisa wa kiume, mmoja wao akiwa Mawlay al-Sharif, ambaye alitangazwa kuwa sultani na Wafilali. Wakati huu Moroko ilikuwa imegawanywa miongoni mwa Wadilawiyya wa Atlas ya Kati walioikalia Fez; Ibn Hassun aliyetawala Sus na Atlas ya Juu, na al-Khadr Ghaylan aliyekuwa akifanya uharibifu katika eneo la kaskazini-magharibi.

Huko Tafilalet kwenyewe, familia moja ilikuwa imeikalia ngome ya Tabusamt, kwa kupinga masharifu wa Kialawi. Kulikuwepo na mapigano kati ya pande hizo mbili, na

baada ya matukio kadhaa Mawlay al-Sharif aling'atuka ili kumpa nafasi mtoto wake wa kiume, Mawlay M'hammad, ambaye alitawazwa kuwa mfalme wa Moroko mwaka 1640. Huu ndio uliokuwa mwanzo wa ufalme wa Waalawi.

Mawlay al-Rashid hakuwa tayari kumtambua kaka yake, Mawlay M'hammad, kwa hiyo aliondoka Tifilalet. Kwanza alianza kwa kuzurura kwenye miji na miongoni mwa makabila ya kusini na kaskazini; alikwenda kwenye bonde la Todgha, hadi Demnat, hadi kwenye zawiya ya Dila na Fez.

Mawlay M'hammad alikusanya jeshi na kuelekea Dara, ambayo ilikuwa imekaliwa na Abu Hassun. Alipigana na Abu Hassun na kumfukuzia nje ya eneo hilo. Kisha aliiandama zawiya ya Dila na kupigana na Wadilawiyya, lakini alishindwa. Hapo alikwenda na kuzingira Fez, mji ambao alifanikiwa kuuchukua mnamo 1650. Lakini alishindwa kujijenga kwenye mji huo na kuondoka tena kuelekea Moroko Mashariki, ambako aliukalia mji wa Ujda na kisha kusonga mbele kuelekea Tilimsan. Eneo lote la magharibi ya Algeria lilivamiwa na vikosi vyake. Baada ya kutiliana sahihi mkataba wa makubaliano na Wamruki waliotawala Algeria, Mawlay M'hammad alirejea Ujda.

Mawlay al-Rashid, aliyekuwa bado anafuatilia azma yake ya kupata ufalme wa Moroko, alifika na kujijenga huko Taza. Sasa alikuwa na fedha na wam wa kumwezesha kutekeleza mipango yake ya kutwaa madaraka. Baada ya kulishinda eneo lote la Taza, alijitangaza kuwa mfalme. Kaka yake, Mawlay M'hammad, alipopata habari za matukio hayo alifika kukutana naye ili kusitisha vitendo vyake, lakini aliuawa mwanzoni mwa vita. Hili lilitokea 1664, mwaka ambao ulishuhudia mwanzo wa kutekwa kwa Moroko.

Mawlay al-Rashid alikwenda Tafilalet, kwenye chimbuko la familia, ambako mmoja wa watoto wa marehemu kaka yake alikuwa ameanzisha vita vya kumpinga. Mtoto huyo alitoroka mara Mawlay al-Rashid alipowasili, na mfalme huyu mpya aliweza kuingia mji wake wa asili kwa amani. Baada ya majaribio mawili yasiyokuwa na mafanikio ya kuuteka Fez, hatimaye aliingia kwa ushindi mkubwa mjini humo mnamo 1666. Kutwaliwa kwa mji huu, ambao hakuna serikali yoyote inayoweza kuitawala Moroko bila kuukamata, kulidhihirisha wazi kuasisiwa kwa ufalme wa Waalawi.

Mawlay al-Rashid alianza kwa kupangilia utawala wake. Aligawa fedha kwa maulama na kuwafanya washauri wake wa karibu. Alimteua mwanazuoni Hamdun al-Mazwar kuwa kadhi wa mji huo mkuu. Vitendo vyote hivi vilimfanya apendwe na Wafasi. Alitumia miaka miwili kutuliza na kueta amani katika eneo lote la kaskazini mwa Moroko, na mwishoni mwa 1668, alijitayarisha kupunguza zawiya (tarika) ya Dila ambayo bado ilikuwa ikishikilia mamlaka makuu katika eneo la Atlas ya Kati. Alikutana na vikosi vya Muhammad al-Hajj al-Dila katika uwanda tambarare wa Fasis na kuvishinda vibaya sana. Kisha aliingia katika (makao makuu ya) zawiya akiwa na vikosi vyake, akawatendea wakazi wake kibinadamu, na hakumwaga hata tone moja la damu. Hili lilitokea mwanzoni mwa 1668.

Baada ya ushindi huu, Mawlay al-Rashid alibakiza tu kuangamiza upinzani kwenye viselemu vidogo vidogo huko Moroko ya Kusini. Kwanza aliikomboa Marrakesh kutoka kwa Washibana, na kisha aliendelea kuwashambulia Wasamlaliyun ambao

walikuwa wamesimika utawala wao huko Sus; alitwaa Tarudant na ngome ya Ighil. Kufikia mwaka 1670 Moroko yote ilikuwa imekwisha tulia na utawala wa Waalawi hatimaye ulianzishwa. Mwaka mmoja na nusu baadaye, Mawlay al-Rashid alifariki kwenye ajali ya farasi.

Hadithi ya watawala wa mwisho wa ufalme wa Wasaadi zaidi inahusu matukio, kwa vile madhara yaliyotokana na ukosefu wa serikali imara hayakuruhusu sanaa na elimu kusitawi. Ilikuwa ni wakati wa utawala wa Mawlay al-Rashid pekee ambapo Moroko ilirejelea tena jadi yake ya kitamaduni na mafaniko yake ya kijamii na kiuchumi.

Mawlay al-Rashid alijenga madrasa (chuo) kubwa kuliko yote huko Fez, na nyingine huko Marrakesh. Aidha yeye ndiye aliyejenga daraja uu ya Wadi Sebu, kilomita 15 mashariki ya Fez.

Kwa upande wa uchumi, aliwakopesha wafanyabiashara kiasi kikubwa cha fedha kuendeleza biashara zao na hivyo kuleta utajiri kwa wote. Alijihusisha sana na tatizo la maji, hasa maeneo ya jangwani, na visima vingi vilichimbwa kwenye majangwa ya mashariki, hasa huko Dara, ambako misafara ya wafanyabiashara na ya mahujaji ilipitia wakati ikielekea Maka. Kwa jumla, enzi ya Mawlay al-Rashid ilijulikana kwa maendeleo katika nyanja zote, na kwa amani na ustawi.

## *Utawala wa Mawlay Ismail*

Mawlay Ismail alikamilisha kazi iliyoanzwa na kaka zake wawili, ile ya kuleta umoja wa Moroko kwa kuiweka chini ya utawala mmoja. Aliimarisha misingi ya dola na kuhakikisha kwamba sharia ya Kiislamu inaenezwa sehemu zote za Moroko, ili kuipatia nchi umoja wa kidini na wa kisiasa.

Alivutiwa sana na mambo yaliyohusu dini na kushawishi watu kuingia dini na hata alimwandikia Louis XIV wa Ufaransa na James II wa Uingereza akiwakaribisha kuupokea Uislamu. Alifuata kikamilifu masharti yote ya sharia ya Kiislamu, na aliishi maisha ya kujinyima. Wanahistoria wa Kikristo walimwelezea kama mtu katili, mwenye kupenda kutumia nguvu, na dikteta. Sura hii potofu ya Mawlay Ismail ilitokana na hadithi zilizoelezwa na wafungwa wa Kizungu ambao kwa kawaida walikuwa wametendewa kufuatana na mtindo wa wakati ule, yaani kwa ukatili wa kulipiza kisasi.

Mabalozi wa sultani huyo walitumwa kwenye miji yote mikuu ya Ulaya. Halikadhalika, wajumbe kutoka nchi hizo za Ulaya walifika kutaka kufanya urafiki naye. Alielewa fika yale yote yaliyokuwa yanatendeka huko Ufaransa na Uingereza, kupitia kwa mawakala wake wa kijasusi, na alionyesha weledi katika siasa.

Aliingia kwenye utawala Aprili tarehe 16, 1672. Watu mashuhuri wa mijini na makabila walimwendea kufanya kiapo cha utii kwake, isipokuwa wale wa Marrakesh, mji ambao mpwa wake, Ahmad bin Muhriz, aliharakisha kujitangazia usultani. Mawlay Ismail alilazimika kwenda kupigana na Ahmad bin Muhriz pamoja na makabila ya huko Hauz ambayo yaliungana naye. Aliwashinda, akaingia Marrakesh na kuwasamehe wakazi wake kwa kuchelewa kula kiapo cha utii kwake. Mpwa wake aliyetoroka mara

baada ya kushindwa alianza kula njama dhidi yake, akiwahimiza watu wa Fez kumwasi Mawlay Ismail.

Mawlay Ismail alimwandama tena na kumlazimisha kutoroka kwa mara ya pili na kukimbilia Sahara. Aliuzingira mji wa Fez hadi ukasalimu amri, lakini baadaye aliamua kuifanya Meknes kuwa mji wake mkuu. Aliagiza kujengwe majumba ya kifalme, nyumba, kuta, mabanda ya wanyama, mabohari na majengo mengine makubwa. Alisababisha kujengwa kwa mabwawa na kutengenezwa kwa bustani nzuri kiasi kwamba Maknes ilishindana kwa nzuri na Versailles (Ikulu ya Ufaransa).

Ahmad ibn Muhriz alijaribu kwa mara ya tatu kufanya maasi dhidi ya mjomba wake. Alifanikiwa kuukalia Marrakesh mnamo 1674 na kujiwekea ngome. Mjomba wake alimzingira kwenye mji huo kwa kiasi cha miaka miwili na mwishowe ibn Muhriz alitorokea Sus. Kisha Mawlay Ismail aliingia Marrakesh na wakati huu alitoa amri ya kuadhibiwa kwa wote waliokuwa wakimuunga mkono ibn Muhriz.

Mojawapo ya matukio ya ndani ya kisiasa wakati wa enzi ya Mawlay Ismail ni maasi yaliyofanywa na kaka watatu - Mawlay al-Harran, Mawlay Hasham, na Mawlay Ahmad - kati ya kaka aliokuwa nao. Maasi hayo yaliibuka mwishoni mwa Ramadhan mwaka 1678-9. Waasi hawa waliungwa mkono na Ait Atta Kabila. Sultani alikwenda kupambana nao akiongoza jeshi kubwa, na wale kaka watatu walioshindwa walitorokea huko Sahara. Wakati huo huo baada ya kupitia vitimbi na mashaka mengi ibn Muhriz aliungana na mjomba wake al-Harran. Mawlay Ismail alipogundua kwamba walikuwa wameukalia mji wa Tarudant mwaka 1684-5, aliuzingira mji huo; ibn Muhriz aliuawa kwenye sakata hiyo. Jeshi la kifalme liliutwaa mji wa Tarudant kwa nguvu na al-Harran alikimbilia Sahara. Kuanzia mwaka huo, 1687, na kuendelea, hakukuwepo tena upinzani dhidi ya utawala wa Mawlay Ismail.

## Kampeni za Mawlay Ismail za kuikomboa miji ya Moroko iliyokuwa imekaliwa na Wazungu

Baada ya kuimarisha mafanikio ya watangulizi wake wawili, Mawlay Ismail alikamilisha kuunganishwa kwa Moroko kwa kuutokomeza ukoloni wa Kikristo.

*Kutwaliwa tena kwa al- Mahdiyya*

Al-Mahdiyya, ambayo ilikuwa ikiitwa al-Mamura wakati huo, ilikuwa ni moja ya bandari kubwa kuliko zote za Moroko. Maharamia wa mataifa mbalimbali walijaribu kuukalia. Kwa kutumia fursa ya udhaifu wa Wamoroko uliotokana na ugomvi miongoni mwa watoto wa kiume wa al-Mansur, Wahispania waliikalia al-Mahdiyya mwaka 1614 na kuushikilia hadi Mawlay Ismail alipoamua kuwatimulia mbali. Alipeleka jeshi kwenye mji huo na kuuzingira, akakata maji yake na kuutwaa mnamo 1681, na kuwashika mateka Wahispania wote waliokuwemo humo.

*Kutwaliwa tena kwa Tangier*

Tangier iliingia chini ya utawala wa Waingereza baada ya mfalme wao mmoja kumwoa



**8.3** *Sultan Mawlay Ismā'īl (Muḥammad V Mausoleum, Rabat*

mtoto wa kike wa mfalme wa Ureno. Mawlay al-Rashid alijaribu kuurudisha mji huu chini ya Moroko lakini alifariki kabla ya kutimiza azma yake. Mawlay Ismail alimtuma mmoja wa majenerali wake mashuhuri kabisa, Ali ibn Abdallah al-Rifi kuuzingira mji huo. Wanahistoria wanakubaliana kwamba Waingereza waliuhama mji wa Tangier bila kupigana baada ya kuvunja minara na ngome zake, lakini maoni yanatofautiana kuhusu sababu za kuuhama. Wanahistoria wa Moroko wanasema kwamba Waingereza walihama kutokana na makali ya kuzingirwa na Wamoroko. Wanahistoria wa Kizungu wanatoa sababu kuhusiana na siasa za ndani. Hata hivyo, wanakubali kuwa Waingereza walikabiliwa na ugumu katika kurudisha nyuma mashambulizi ya Wamoroko. Vyovyote ilivyokuwa, jeshi la Moroko liliingia Tangier Februari 1684.

*Kutwaliwa tena kwa Larache*
Mji wa Larache haukuwa umekaliwa kimabavu na jeshi la Wahispania, bali ulikuwa umekabidhiwa na Muhammad Shaykh kwa mfalme Filipo III wa Wahispania kama shukrani kwa kumsaidia kuupata utawala wa Moroko ambao kaka zake wawili walikuwa wakiugombea. Makubaliano yalifikiwa 1610 na Larache ulibakia chini ya utawala wa Wahispania kwa miaka minane. Mawlay Ismail alituma jeshi lenye nguvu kushambulia Larache na kuwazingira Wahispania mjini mle kwa zaidi ya miezi mitano. Kuchukuliwa tena kwa Larache ambako kulifanyika Novemba 1689, kuliwapatia Wamoroko furaha kubwa iliyolingana na uchungu walioupata wakati walipoupoteza mji huo.

*Kutwaliwa tena kwa Asila*
Bandari ya Asila ilikuwa imeangukia mikononi mwa Wareno mwanzoni mwa enzi ya Banu Wattas. Baada ya kutwaliwa upya na wafalme wa awali wa Wasaadi, ilitekwa tena na Wareno na hatimaye ilikuwa chini ya miliki ya Wahispania. Generali ibn Haddu alipomaliza kutwaa Larache alipokea amri ya kwenda kuuzingira mji wa Asila. Wakati wakazi waliozingirwa walipozidiwa na dhiki, waliomba kunusuriwa maisha yao, na ombi lao lilikubaliwa kwa masharti kwamba kibali cha sultani sharti kipatikane kwanza. Hata hivyo, kwa kuhofia mabaya zaidi, Wareno hao walitoroka usiku kwa meli zao. Wamoroko waliingia Asila mwaka 1691.

## Majeshi ya Mawlay Ismail

*Wanamgambo wa Kiwadaya*
Wafalme wa Moroko waliunda majeshi yao ama kutokana na makabila ya koo zao wenyewe, au kutokana na muungano wa makabila. Hali hii iliendelea kuwa hivyo hadi ulipoibuka ufalme wa Wasaadi ambao uliandikisha askari wao kutoka makabila ya Mabedui wa Kiarabu walioingizwa Moroko wakati wa kipindi cha al-Mansur, Mmohadi, ambaye alikuwa ametamakani kusini mwa nchi hiyo. Ufalme wa Wasaadi uliunda jeshi la mgambo lililojulikana kama "wanamgambo wa Wadaya" ambalo lilitawanyika wakati wa kuporomoka kwa Wasaadi. Wakati akiishi Marrakesh, Mawlay Ismail alipata wazo la kuwakusanya upya na kuwafanya askari. Makruta hawa wapya

walipelekwa huko Meknes, mji mkuu, ambako waliungana na Washibana na Wazirara. Idadi yao ilipoongezeka, Mawlay Ismail aliwagawa katika makundi mawili: moja lilitumwa Fez, na jingine lilibakia Riyad huko Meknes.

*Wanamgambo wa Bawakhir*

Mawlay Ismail alielewa fika kwamba nguvu za taifa hutegemea nguvu za kijeshi, lakini alihofia askari na viongozi wao kutwaa mamlaka mengi kupita kiasi. Ndiyo maana aliamua kuanzisha jeshi la mgambo kutokana na watumwa.

Mmoja wa makatibu wa Makhzen, aliyeitwa Muhammad ibn al-Kasim Alilish, ambaye baba yake alikuwa katibu kwa kiongozi wa Wasaadi, al-Mansur, alimwambia Mawlay Ismail kwamba mfalme huyo alikuwa na jeshi la mgambo la watumwa weusi. Aliongezea kwamba alikuwa na rejesta yenye majina yao wote. Mawlay Ismail alimwaminisha Alilish wajibu wa kuwatafuta watu hao waliko (wengi wao walikuwa bado kwenye eneo la Marrakesh), na kuwaandikisha bila kujali kama walikuwa ni watumwa au watu huru. Umma wote ulishtushwa na uamuzi huo, hasa maulama, walinzi wa sharia ya Kiislamu, ambayo inakataza utumiaji wa watu huru. Jambo hili lilisababisha mgogoro mrefu kati ya mfalme na maulama wa Fez kwa maandishi mengi na barua; mengi kati ya maandishi hayo bado yanapatikana. Hizi ndizo zile barua muhimu kutoka kwa Mawlay Ismail kwenda Sheikh al Islam al-Fasi.

Mawlay Ismail aliamini kwamba katika jambo hili alikuwa akitenda kulingana na sharia ya Kiislamu, na aliifikiria hatua hii kuwa ilikuwa ni yenye manufaa kwa Moroko na kwa Uislamu. Aliyaamini madai ya Alilish kwamba watu hawa, au labda wazazi wao, walikuwa watumwa katika enzi za Wasaadi. Barua ya kwanza ya mawasiliano kati ya Mawlay Ismail na Sidi M'hammad ibn Abd al-Kadir al-Fasi, ambayo ipo hadi leo, iliandikwa Julai 1693. Katika barua hii, mtawala huyu anamwambia Sidi M'hammad kuzitafiti hoja za Alilish na kuelezea endapo kumbadili mtu huru na kumfanya mtumwa kulikubaliana na sharia. Bila shaka mwanazuoni huyo alijibu kwamba sharia hairuhusu mtu huru kugeuzwa mtumwa, kwa vile barua za sultani zinaonyesha kukereka.

Akiwa amefanya uamuzi imara wa kupanga jeshi la Bawakhir, mtawala huyo alimwandikia Sheikh al-Islam mwezi Desemba 1698 kwamba tayari alikwisha waachia huru watumwa wote ambao walikuwa wameandikishwa kwenye mgambo, na kwamba aliendelea kuwashikilta ili awatumie kulinda nchi ya Waislamu. Hatujui jibu la Sidi M'hammad lilikuwaje alifariki 1703, na Mawlay Ismail aliendelea kuomba maulama wa Fez wakubaliane naye. Jambo hili lilikuwa na matatizo ya mara kwa mara hadi 1708-1709, wakati mfalme alipowalazimisha maulama kukubaliana na *Diwan al-Abid* (Usajili wa Watumwa).

Hivi ndivyo jeshi la mgambo la Bawakhir lilivyoundwa, na lilisaidia sana kulinda amani na usalama katika nchi ya Moroko iliyoungana. Mawlay Ismail alikuwa ameanzisha ngome (kasaba) katika sehemu zote za Moroko, na ngome hizi zililindwa na askari hawa. Kwa kuwatumia wanamgambo hawa wenye nguvu nyingi, Mawlay Ismail aliweza kurejesha nguvu na heshima ya Moroko machoni mwa mataifa makubwa ya wakati huo.

## Mawlay Ismail ateua watoto wake wa kiume kuwa wawakilishi wa mfalme kwenye maeneo kadhaa ya Moroko

Uteuzi huu ulimsababishia Mawlay Ismail matatizo makubwa kwa vile alikuwa na watoto 500 wa kiume na kiasi hicho hicho cha watoto wa kike. Hivyo hakuweza kuwaridhisha wote. Katika hali kama hii angefanya vizuri zaidi kama, tangu mwanzo, angefuata uamuzi aliokuja kuufanya mwishoni.

Mwaka 1699-1700 aligawanya majimbo yote miongoni mwa watoto wake wa kiume kama ifuatavyo: Mawlay Ahmad (jina la kupanga Al-Dhahabi) alipelekwa Tadla akifuatana na askari weusi 300; Mawlay Abd al-Malik alitumwa Dara akiongoza wapanda farasi 1,000; Muhammad al-Alem alipelekwa Sus na wapanda farasi 3,000 na Mawlay al Mamun al-Kabir alikwenda Sijilmasa. Huyu alianzisha makao yake huko Tizimi, ila alifariki baada ya miaka miwili, na baadaye nafasi yake ilijazwa na Mawlay Yusuf 1701-2. Mawlay Zaydan alitumwa mashariki ya Moroko ambapo alianzisha mapambano dhidi ya Waturuki, na hata wakati mmoja alipora jumbani mwa Amiri Uthman Bey huko Maskara. Baba yake alimwondoa madarakani kufuatia makubaliano kati yake na Khalifa wa Waturuki, na nafasi yake ikachukuliwa na Mawlay Hafid.

Wale watoto wakubwa wa Mawlay Ismail ambao hawakupewa cheo cha uwakilishi walijihisi kudharauliwa. Wengine walijaribu kujichukulia majimbo kwa nguvu, kama vile Mawlay Abu Nasr, ambaye alimvamia kaka yake Mawlay Abd al-Malik na kuteka Dara. Sultani alilazimika kumtuma mtoto wake Mawlay Sharif kulitwaa upya jimbo hilo na kisha kumkabidhi yeye kulitawala. Mawlay Muhammad al-Alem alianzisha fujo huko Sus, na kujitangazia usultani na kisha kuelekea Marrakesh, ambayo aliikalia. Mawlay Ismail alimtuma mtoto wake Mawlay Zaydam kupambana naye na alipigana na mwasi huyo kwa miaka miwili. Baada ya kuona madhara yaliyoletwa na jaribio la kuteua watoto wake kumwakilisha, na magomvi kati ya watoto wake, Mawlay Ismail aliamua kuwapeleka watoto wake wote wa kiume waliokuwa wamefikia umri wa kubalehe huko Tafilalet. Kila mmoja wao alijengewa nyumba na kukabidhiwa idadi kadhaa ya mitende, shamba, na watumwa wa kuwasaidia kufanya kazi. Lilikuwa ni wazo la busara kwa vile mtawala huyo alikuwa na watoto wengi mno wa kiume, na isingaliwezekana kwa watoto hao wote kuishi maisha ya kifalme huko Meknes au katika miji mingine ya Moroko. Mwaka 1717-8 aliwaondosha madarakani watoto wake wote isipokuwa Mawlay Ahmad al-Dhahabi, gavana wa Tadla, ambaye alikuwa ameonyesha mafanikio ya kutawala kwa kutokuwepo na machafuko katika wilaya yake kwa kipindi cha miaka ishirini.

Kufuatia hatua hii nchi ilikuwa na amani na utulivu na Wamoroko walichangia katika kuongeza utajiri wa nchi kwa kuendeleza biashara na kilimo. Mawlay Ismail alikuwa na utawala mrefu sana. Alifariki Machi, tarehe 21, 1727, baada ya kuwa kwenye enzi kwa miaka hamsini na saba.

## Warithi wa Mawlay Ismail

Baada ya kifo cha Mawlay Ismail watoto wake wengi wa kiume, ambao katika uhai

wake waliwahi kupigania madaraka huko mikoani, walijitokeza kugombania utawala mkuu. Kwa miongo kadhaa hakuna hata mmoja kati yao aliyefanikiwa kuunda serikali ya kudumu na yenye nguvu. Yule wa kwanza, Mawlay Abdallah, alipewa ukuu na kupinduliwa mara kadhaa.

Kuelekea mwishoni mwa karne ya 18 mfalme mkuu, Sidi Muhammad ibn Abdallah au Muhammad III, alitwaa utawala wa Moroko. Alirudisha amani na utaratibu, aliimarisha nguvu za ufalme na kuifanya Moroko iheshimiwe na mataifa yote. Lengo lake la msingi lilikuwa kuendeleza biashara, na alisimamia usasishaji wa bandari, hasa bandari ya Mogador, ambayo tangu wakati huo imepata jina la Essawira (Essaouira). Pia alivutiwa na Karawiyyin ya Fez, ambayo aliipangia programu kamili ya mabadiliko.

Kuhusiana na dini, aliamini juu ya usafi wa Uislamu, ambao unakataa warabiti au kuabudu watakatifu. Lakini hata hivyo, kwa vile alikuwa akielewana vizuri na sharifu wa Maka, Surur (Sourour), hakutia shinikizo kubwa mno katika kuleta mabadiliko ya kidini ambayo yangekaribiana mno na itikadi ya Wawahhabi, waliokuwa maadui wa masharifu wa Maka. Hata hivyo, nguvu za tarika za kidini zilipungua sana wakati wa utawala wake na ule wa mtoto wake, Mawlay Sulemani (Sulayman).

Kwa upande wa mahusiano na nchi za nje, alitiliana sahihi makubaliano mengi na nchi za kigeni. Alitambua uhuru wa Marekani (USA), alipendekeza kwa Louis XIV akomeshe utumwa, na aliunga mkono himaya ya Uturuki katika mgogoro wake na himaya ya Urusi. Mwaka 1767 aliwafukuza Wareno kutoka Mazagan, lakini alikufa ghafla alipokuwa akijiandaa kuuzingira mji wa Sabta.

Kwa kuhitimisha, enzi ya Muhammad III inaweza kuelezewa kuwa ilituliza na kuimarisha dola na mamlaka ya nasaba ya Waalawi. Alipenda amani, na alisuluhisha matatizo ya kisera ya ndani na nje kwa njia ya majadiliano na mazungumzo. Vita pekee alivyopigana ni vya kuikomboa Mazagan. Sera yake ya hekima na yenye kuzingatia hali halisi iliwanufaisha Wamoroko wote, ambao katika nusu ya pili ya karne ya kumi na nane, walifurahia usalama na ustawi.

# 9

# *Algeria, Tunisia na Libya: Waturuki na warithi wao*


Kipindi cha mwanzo cha karne ya kumi na sita ilijibainisha kwa zahama za hali ya juu ambazo zilisababisha kutoweka kwa miundo ya dola iliyokuwepo Maghrib pamoja na uwiano wa mahusiano ulioandamana nayo. Kutokana na uvamizi wa Waturuki katika Algiers, Tunis na Tripoli, hali hii ya matatizo iliweza kutoweka na kutoa mwanya kwa utaratibu mpya ambao hatimaye ulileta hali ya utulivu katika Maghrib hadi miaka ya mwanzo mwanzo ya karne ya kumi na tisa, ambapo palizuka zahama mpya za kimuundo zilizoashiria utawala wa kikoloni.

Je, machafuko haya yalikuwa na umuhimu gani? Waturuki walisaidia vipi, na kwa kiwango gani, kurejesha tena hali ya utulivu katika karne ya kumi na sita? Ni dhahiri kwamba hali ya Algiers ilikuwa tofauti na ile ya Tunis; na ya Tunis ilikuwa tofauti na ile ya Tripoli. Halikadhalika, karne ya kumi na saba, kipindi cha mashaka na majaribio, ilikuwa tofauti na ile ya kumi na nane, ambayo kwa kiasi fulani ilikuwa ni kipindi cha utulivu.

## *Zahama za karne ya kumi na sita na ufumbuzi wa Waturuki katika Maghrib*

Zahama zilizouathiri ulimwengu wa Waarabu katika kipindi hiki zilikuwa za aina mbalimbali. Kulikuwa na: machafuko ya kiuchumi, ambayo kwa kiasi fulani yalisababishwa na kuachwa kutumiwa kwa sehemu hii ya dunia kama njia kuu ya biashara; migogoro ya kijamii na kisiasa ambayo ilitokana na kudhoofika kwa nguvu za kujenga umoja katika jamii, na machafuko ya kiutamaduni yaliyotokana na kufungamana sana na ukale. Hali hii ilikuwa ya hatari sana, hasa kwa kuwa Ulaya ilikuwa sasa inazindukana kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni kutokana na vuvumko la Mwamko lililoleta mawazo mapya, namna mpya za kufanya mambo na tekinolojia mpya.

Waturuki wa Kiosmauli, waliokuwa pambizoni mwa ulimwengu wa Kiislamu, ndio pekee waliweza kurekebisha maisha na mienendo yao kulingana na hali ya wakati huo. Ingawa haikuwa ya mawanda mapana sana, lakini athari hiyo ya Waturuki ilikuwa ni utatuzi muafaka kwa jamii na mataifa yaliyokuwa yakididimia




9.1 *Algeria, Tunisia na Libya kuanzia karne ya kumi na sita hadi ya kumi na nane*

kasi huku yakikabiliana na vitishio kutoka nje, kama yalivyokuwa mataifa ya Maghrib mwanzoni mwa karne ya kumi na sita.

## Zahama katika Maghrib

Kufikia miaka ya mwisho mwisho ya karne ya kumi na tano, Maghrib ilikwisha kuwa katika hali ya zahama kubwa iliyobainishwa na kupungua sana kwa idadi ya watu, kuathirika vibaya kwa uchumi na jamii, na udhaifu mkubwa wa kisiasa usiorekebishika. Sababu za hali hii zilikuwa nyingi: kulikuwa na tatizo la eneo hilo kuwa karibu mno na jangwa; kuwepo sambamba kwa jamii zenye kutofautiana na ambazo mara nyingi zilikuwa hazipatani; udhaifu wa vipengele muhimu vya kujenga umoja katika jamii; na kutokuwepo kwa maendeleo ya kitekinolojia na kiutamaduni.

Mara nyingi Wanomadi wa Kihilali wamekuwa wakilaumiwa kwa kuzorotesha maendeleo ya Maghrib. Lawama hizi si rahisi kuzitolea maelezo yaliyo makini, lakini ni kweli kwamba ukizichunguza shughuli na taratibu zao, namna walivyoishi na itikadi yao ya kupenda vita, utaona kwamba ma-*kaba'il* (makundi ya Kiarabu ya Kinomadi au makundi yaliyosimilishwa katika Uarabu) yalidhihirisha namna fulani ya udhaifu kwa Maghrib nzima.

Katika karne za kumi na nne na kumi na tano, magonjwa ya mlipuko na njaa vilikwisha punguza idadi ya watu hadi kufikia kati ya milioni 3 na 6. Punguo hili la idadi ya watu lilisababisha kushuka kwa uzalishaji, ambao tayari ulikwishatishiwa na kupanuka kwa jangwa. Aidha hazina kutoka Amerika, ambazo zilikuwa zinaingia Seville kwa wingi kuanzia 1503-1505 na kuendelea, zilipunguza ?ikubwa thamani ya akiba ya fedha ya Dunia Kongwe na kusaidia kujenga uwezo wa wale waliozihodhi, kwanza Waiberia, na baadaye wale waliozipata kutokana na kazi zao katika uchumi wa Dunia Mpya, hasa Waholanzi, Waingereza na Wafaransa.

Kudhoofika taratibu kwa hali ya maisha ambako kulikuwa kunaimomonyoa miji ya Maghrib tangu karne za kumi na moja na kumi na mbili, kukaingia katika mbunguko wa haraka katika miaka ya mwisho mwisho ya karne ya kumi na tano na katika miongo ya mwanzo ya karne iliyofuata. Leo Africanus, kwa kila hali, aliihusisha hali hii ya ufukara, aliyoiona kila mahali katika miji na katika makazi ya mashambani, na utozaji kodi wa kikandamizaji na unyang'anyi wa Wanomadi.

Ama kwa hakika Wanomadi walikuwa wakijiondoa katika nira ya dola na kupanua maeneo yao na namna yao ya maisha ya ufugaji katika sehemu kubwa ya nchi. Walikuwa wakijinufaisha kutokana na ombwe iliyoletwa na kupunguka kwa idadi ya watu na kushuka kwa kiwango cha kilimo, na wakawa wanatumia mabavu ili kuweza kuishi. Maeneo yaliyokuwa yanalimwa na wakazi wa mashambani yakazidi kupungua kadri walivyozidi kuyasogelea, na kukawa na vijisehemu vidogo tu vya mashamba ya nafaka ambavyo vililindwa kwa kuzungushiwa kuta ndefu.

Kutokana na hali hiyo, madola makongwe ya Wazayyani (au Banu 'Abd al-Wadid) katika Tilimsan na Wahafsi katika Tunis yakaanza kuanguka. Rasilimali zao zikaanza kupungua kwa haraka kutokana na kupanguka kwa biashara na kupunguka kwa bidhaa za kutozwa kodi. Aidha kulikuwa na *ikta'* (misamaha) juu ya ardhi au

kodi iliyotolewa na watawala masikini kwa makundi yenye nguvu ya wapiganaji. Punde miji iliyokuwa mbali na makao makuu ya utawala ikaanza kujitegemea (Tripoli, Bougie na Konstantini, katika ufalme wa Kihafsi), na mashirikisho makuu yakawa na mamlaka juu ya maeneo yaliyokuwa chini yake. *Bilad al-Makhzen* (nchi iliyo chini ya mamlaka ya dola) taratibu ikapungua na kubakia kisehemu chembamba kuzunguka makao ya sultani na visehemu vichache vya mbali.

Utawala wa Wazayyani katika Tilimsan na Wahafsi katika Tunis ulikuwa tayari umekwisha dhoofika sana wakati Wahispania na Waturuki walipoingia na kutamalaki huko.

## Uvamizi wa Kigeni katika Maghrib ya kati na mashariki

Mipango na malengo ya watamalaki hayana budi kutazamwa kwa kuzingatia shauku za kidini za wakati huo: mwamko wa vita vya msalaba waliokuwa nao Wahispania, ambao ndio kwanza walikuwa wamemaliza kuitamalaki upya nchi yao; na utetezi wa *Dar al-Islam*, ukienda sambamba na itikadi ya *ghazi* (utamalaki) ya Waturuki. Aidha ngome za pwani ya Maghrib zilikuwa dhahiri zimejengwa kwa makusudi ya kulinda maslahi ya washindani hao wawili. Mwisho, mashambulio ya Wahispania katika Maghrib yalifanyika muda mfupi tu baada ya kuanza kufika metali za thamani kutoka Amerika, ambazo ziliwapa Wahispania uwezo wa kuitekeleza kwa nguvu sera ya upanuzi wa miliki yao.

### *Wahispania katika Maghrib ya kati na mashariki*

Kuanzia mwaka 1505 hadi 1574 wafalme wa Hispania walijaribu mara kwa mara kuzishika sehemu mbalimbali za pwani ya Maghrib. Yatosha tu kukumbuka tabaro (safari za kivita) kuu za watu kama Pedro Navarro, mnamo miaka ya 1505-1511; Charles V, mnamo miaka ya 1535-1541; na mwisho safari za John Don wa Austria, ambaye aliiteka tena Tunis kutoka kwa Waturuki, mnamo mwaka 1573. Hata hivyo matokeo yalikuwa kidogo sana, kwani utamalaki wa bara ya Maghrib na uingizaji wa wenyeji katika Ukristo ulionyesha haraka kuwa haungewezekana. Wahispania wakaridhika na kuchukua *presidio* (miji) chache tu kama vile Oran na Tripoli na kujenga ngome kadhaa kama vile Penon katika lango la Algiers au La Goulette katika bandari ya nje ya Tunis.

Sera hii ya kumiliki sehemu chache tu ilihitajia mara kwa mara kupata marafiki wenyeji. Maarufu kabisa kati ya marafiki hao walikuwa masultani wa Kihafsi ambao, kuanzia mwaka 1535 na kuendelea, walicheza mchezo wa kijanja wa kuweka urari baina ya Wahispania na Waturuki. Halikadhalika Wazayyani wa mwisho wa Tilimsan nao mara moja moja walifanya mikataba ya kirafiki na Wahispania hadi mji wao ulipotekwa na Waturuki na utawala wao kutoweka kati ya 1551-4. Kwa ujumla, hata hivyo, vizingiti vya kidini na kiutamaduni vilikuwa ni vikubwa mno kiasi cha kutoruhusu kuwepo kwa maelewano ya kudumu kati ya Wahispania na watawala wenyeji, na Waturuki Waislamu wakaitumia vizuri hali hiyo.

*Vita ya Waturuki dhidi ya Wahispania*

Waturuki wa kwanza kuanzisha vita dhidi ya Wakristo katika Maghrib walikuwa maharamia wa ki-*Ra'is*. Kwanza walijiamulia wenyewe kufanya hivyo ingawa kwa kukubaliana na watawala wenyeji na kusaidiwa na wananchi wa huko. Mfano wa watu kama hao ni wale ndugu wa Barbarossa, Arruj na Khayruddin, kati ya 1500 na 1519. Baada ya kushindwa na kufa kwa Arruj, Khayruddin akaomba msaada kwa sultan wa Waturuki ambaye yeye, Khayruddin, alikuwa akimtambna, na huo ndio ukawa mwanzo wa *iyala* (utawala kwa niaba ya mfalme) za Maghrib.

Kwa kutumia Mayeniseri na silaha alizopewa na Istanbul (Waturuki), polepole Khayruddin na warithi wake, hasa Salah Ra'is (1552-6) na *beylerbey* mbabe wa "*ojak* za magharibi", Killij au 'Ilj Ali (1568-87), walifanikiwa kuitawala Algeria. Kwa muda wa miaka arubaini (1534-74), Ifrikiya ikawa jukwaa la mapambano ya muda mrefu baina ya Wahispania na Waturuki, ambayo watawala wa Kihafsi waliingilia kati Waturuki ambamo watawala wa ki-Hafsi na viongozi wenyeji waliingilia kati mara kwa mara, ingawa wakati mwingine haikuwa kwa manufaa yao. Hatua muhimu za kutamalaki kwa Waturuki mashariki ya Maghrib zilikuwa ni kutwaliwa kwa Tripoli mwaka 1552, Kayrawan mwaka 1557, Jerba mwaka 1558 na mwisho Tunis mwaka 1569, na halafu tena 1574. Baada ya hapo hali ikawa imetulia, lakini kwa manufaa ya Waturuki ambao walibakia kuwa mabwana wa Maghrib ya kati na mashariki, kasoro Oran, ambayo ilizungukwa na eneo la Waturuki, Marsa al-Kabr na kisiwa kidogo cha Tabarka.

*Muundo wa Iyala za Waturuki*

*Ojak* za magharibi, kama majimbo mapya ya Kiafrika yalivyojulikana, hazikuingizwa kabisa kabisa katika mfumo wa Waturuki wa kisiasa na kijeshi. Hapakuwa na ushuru uliotozwa mara kwa mara wala utawala wa moja kwa moja kutoka Istanbul. Majimbo yote matatu ya Maghrib mwanzoni yalikuwa chini ya mamlaka ya mtawala mmoja wa kivita, *beylerbey* wa Algiers, lakini yalitenganishwa baada ya kifo cha mbabe Killij.

Kila jimbo liliwekwa chini ya *pasha* aliyeteuliwa kutoka Istanbul na alisaidiwa na *diwan* (halmashauri ya maofisa waandamizi wa Kituruki: madiwani). Wanamgambo wa ki-Yeniseri, ambao idadi yao ilikuwa yapata maelfu kadhaa, walikuwa na jukumu la kuilinda nchi, kuhakikisha kuwepo kwa angalau kiasi fulani cha amani, na walishiriki kikamilifu katika kukusanya kodi na kuendesha shughuli za "utawala." Tangu mwanzo kabisa wao ndio walikuwa tegemeo la utawala mpya. Maharamia waliokuja kutoka achipelago ya Ugiriki, Albania au nchi jirani za Ulaya, wote walikwishasilimu na walihesabiwa kama Waturuki: walisimilishwa katika jamii ya watamalaki na wakapata marupurupu na hadhi sawa na wengine.

Makhzen (utawala) ilitekeleza wajibati ndogo ndogo; kukusanya kodi kwa ajili ya gharama za kuanzisha au kukabiliana na vita na kulipia gharama za vikosi vya watamalaki katika nchi, kulinda usalama na kuhakikisha haki inatendeka; na kutoa huduma za posta. Idadi ndogo ya ma-*khuja* (makarani) na wahasibu, viongozi wachache wa ngazi ya juu wa siasa na dini na, zaidi ya wote, askari wa ngazi zote,

walitekeleza majukumu haya. Kadri muda ulivyopita ikawa lazima kwa Makhzen kuajiri wasaidizi wa kiraia na kijeshi kutokana na wenyeji. Katika mambo mengine asasi za kienyeji ziliendelea kutawala katika jamii, watawala wapya wakiwa wanaingilia kati mara kwa mara.

Ingawa ulikuwa mchanga na wa kijuujuu, lakini utaratibu huo mpya wa Kituruki uliipa Maghrib kitu ilichohitaji sana - njia ya kujirekebisha kulingana na ulimwengu wa kileo. Ulianzisha jeshi lenye nidhamu ambalo lilitumia silaha za bunduki, na utawala ambao kwa kiasi fulani ulikuwa unganifu. Aidha, kwa kutumia merikebu za kimamluki, utawala huo uliweza kujikusanyia baadhi ya fedha zilizokuwa katika mzunguko katika bahari ya Mediterania. Kwa ujumla, utawala mpya ulipokelewa vizuri na miji na wazee wa dini, hasa maulama ambao walipendelea zaidi uongozi mkuu wenye nguvu. Waturuki walichukiwa na wale wote waliokuwa wakinufaika na uhuru uliokuwepo mwanzoni mwa karne ya kumi na moja, yaani jamii ya vijijini ambayo ilikuwa na utaratibu wake wa kijamii na kivita, na ambayo haikupata kitu kingine kutoka kwa mabwana wao wapya isipokuwa utawala mkali na mzigo wa unyonywaji. Waturuki walilazimika kupigana vita vya muda mrefu ili kuweza kuitiisha bara yote na kuweka huko namna fulani ya sheria na utaratibu.

## *Maghrib katika karne ya kumi na saba: msako wa urari*

Katika karne ya kumi na saba jamii ya Maghrib, ikiwa imebadilishwa kidogo tu na kipindi cha Waturuki, pole pole ilianza kuondokana na zahama za karne iliyopita. Miji yake ya pwani, na pengine pia jamii zake za mashambani, ikapata kiasi fulani cha maendeleo, lakini ikabakia katika hatari ya zahama kubwa zaidi (za magonjwa ya mlipuko, njaa, vita vya wenyewe kwa wenyewe) ambazo ziliitikisa kila mara. Tabaka-tawala la Kituruki likapata mabadiliko fulani ya ndani kutokana na kuingia kwa watu wapya na pia, kwa kiasi fulani, kwa kukita mizizi yake katika Maghrib. Matatizo kadhaa yakatokea kuhusiana na uhusiano wake na Istanbul, na pia biashara ya baharini ya mamluki za Kibarbary, ambao ilifikia kilele cha ustawi wake kati ya 1600 na 1650. Yale majimbo yaliyokuwa chini ya utawala wa mfalme yakazidi kusigana kadri maendeleo yake ya kisiasa yalivyofuata mikondo tofauti.

### Jamii ya Maghrib ya Kituruki ya karne ya kumi na saba

Afrika ya Kaskazini ya Waturuki ilikuwa na makundi anuwai ya kijamii- kiuchumi. Jamii ya vijijini ilikuwa ya wakulima wenye makazi ya kudumu na wale ambao makazi yao hayakuwa ya kudumu sana, wafugaji mifugo wenye kuhamahama, Wanomadi wachunga-ngamia wa jangwani, na wakazi wa oasisi. Jamii ya mijini kimsingi ilikuwa na viongozi wa dini, wafanyabiashara, mafundi sadifu, ma-*kulughli* (vizazi vya Waturuki wahamiaji waliooana na wenyeji) na tabaka-tawala la Waturuki wa kiraia na wanajeshi.

Watu wa vijijini walikuwa wa kabila mbalimbali ambazo zilijiunga pamoja kuunda mashirikisho (*saff*, wingi *sufuf*). Hawa walifanya maamuzi, kwa kuzingatia kila suala

kipekee, iwapo ingefaa waugomee, au washirikiane na, utawala uliopo. Makundi makubwa, ambayo ama yalikuwa chini ya Makhzen au yalikuwa washirika wake, yalipingana na *siba* (makundi pinzani).

Karne ya kumi na saba ilitofautiana na karne zilizopita kwa utulivu wake katika maeneo mbalimbali, ambao ulisaidia kupunguza misukosuko, angalau katika maeneo ya Maghrib yaliyokuwa na maji ya kutosha.

Ingawa sehemu kubwa ya nchi ilitumia Kiarabu, bado paliendelea kuwapo kiasi kikubwa cha jamii zilizozungumza Kiberiberi zilizokuwa zimekimbilia milimani, kuanzia Jabal Nafusa katika Tripolitania hadi Aures na Kabylia Kuu huko Maghrib ya kati, na kuendelea hadi magharibi zaidi kwenye milima ya Atlas na Rif. Jamii hizi zilijibainisha kutoka jamii za Kiarabu kwa kuwa na mfumo safi wa ulinzi ambao uliwawezesha kupingana na Waturuki kwa mafanikio na kudumisha namna mbalimbali za utamaduni wa Kiberiberi. Kwa kila hali walihifadhi utawala wao wa ndani, wakikataa, kwa mfano, kulipa kodi.

Maeneo ya vijijini, oasisi za kusini, majimbo yaliyolima ngano yaliyokuwa chini ya mabwana wa mijini na maeneo tambarare ya miji yalikaliwa na jamii tofauti kabisa na ile ya maeneo ya milimani yaliyokuwa bara. Jamii hiyo iliyotajwa mwanzo iliishi maisha ya makazi ya kudumu ya kilimo, ikaweza kutumia soko na ikawa na *milk* (utaratibu wa kumiliki ardhi) nzuri zaidi. Iliathiriwa na uchumi na utamaduni wa miji, na maadili kama yale ya kutii mamlaka yakaenea kwa urahisi zaidi kuliko ilivyokuwa katika maeneo ya milimani. Katika jamii hizi mahusiano ya kiukoo ya kibaba yalikwenda sambamba na mahusiano ya kimsonge, kama yale yaliyomhusisha mmiliki njia za uchumi na *khamma* (mzalishaji aliyetoa kodi ya moja ya tano ya mazao yake) katika maeneo makubwa yalimayo nafaka. Sifa hizi bila shaka zilijidhihirisha zaidi katika karne ya kumi na saba kutokana na kuongezeka kwa usalama, kustawi kwa jamii za mijini na kuanzishwa kwa mahusiano na mataifa ya Ulaya yaliyofanya biashara, ambako kulichombeza upanuzi wa mazao ya kuuza nje.

Kutokana na kuwa kwake mbali na bahari na mamlaka kuu, na pia kutokana na kuendelea kuwapo kwa misafara ya biashara na Afrika ya Watu Weusi na Mashariki, oasisi zikawa ni mahali penye jamii zilizochangamana vizuri zaidi na zenye vikundi au nasaba tawala madhubuti zaidi za kienyeji, kama ile ya Wafasi katika Fezzan.

Miji nayo halikadhalika ikafanya kuwepo kwake kutambulike katika Maghrib nzima, iwe ni miji mikuu ya pwani kama Algiers, Tunis na Tripoli au vituo vya kale kama Kayrawan, Konstantini na Tilimsan. Biashara na kazi za mikono vikapata nguvu mpya kuanzia nusu ya kwanza ya karne ya kumi na saba. *'Ilm* (elimu ya dini) taratibu ikaanza kufufuka baada ya zahama ya karne iliyopita, ikiwa imechombezwa na utajiri mkubwa zaidi wa miji na ongezeko katika idadi ya *wakf* (asasi za kidini) lililotokana nao. Mamlaka za Kituruki zilitia mshawasha wa kufufuliwa kwa mambo haya, pengine kwa sababu za kidunia kuliko za kidini.

Juu kabisa ya msonge wa kisiasa na kijamii kulikuwa na tabaka-tawala ambalo kinadharia liliundwa na wanajeshi wa Kituruki, lakini kwa hakika liliingiza watu wa makundi mengine. Hawa walikuwa ni Wakristo waliosilimu na wakawa wakiitwa

Waturuki licha ya majina yao ya Kifaransa, Kiingereza, Kikorsika au Kisardinia. Hawa walianzisha tekinolojia ya kisasa ya Ulaya, hasa katika masuala ya kijeshi na kibahari, na wakashiriki kikamilifu, si katika maeneo haya tu, bali pia katika kazi za kiutawala na kisiasa. Katika Tunisia na Tripolitania Waturuki hawakuchelewa kuwapa watoto wao waliozaa na wanawake wenyeji (ma-*kulughli*) wajibati na haki za upendeleo ambazo zilikuwa maalumu kwa Waturuki wenyewe. Waturuki wa Algiers walikuwa wakijibagua zaidi na wakakataa kufanya kama wenzao wa miji hiyo miwili. Hali hiyo ikasababisha maasi makali ya ma-*kulughli* ambayo yaliishia katika kushindwa na kutengwa kabisa kwa ma-*kulughli*, walau kwenye miaka ya 1630 hadi 1680.

Kwa ufupi, katika karne ya kumi na saba tabaka-tawala lilianza kushirikiana na waali wengine katika Tunis na Tripoli, lakini lile la Algiers liliendelea kuwa la kigeni. Tofauti hii ilitokana na nguvu au udhaifu wa waali hao: walikuwa na nguvu sana katika Tunis kutokana na mapokeo yao ya kihistoria na shughuli zao, na walikuwa na nguvu Tripoli kutokana na biashara yao ya mawanda mapana, lakini katika Algiers, mji mpya ambao takribani kwa kila hali ulianzishwa na Waturuki katika karne ya kumi na sita hawakuwa na mizizi ya kutosha.

## Tawala za kisiasa katika Iyali kunako karne ya kumi na saba

Iyali tatu, ambazo kimsingi zilikuwa majimbo ya Kituruki, kwa kiasi kikubwa zilianza kuacha kuitegemea Istanbul kuanzia mwanzoni mwa karne ya kumi na saba, lakini mbali na sifa hii moja ambayo majimbo yote yalikuwa, nayo kila moja liliendelea kivyake.

Maendeleo yalikuwa ya haraka sana katika Tunis. Licha ya kunyang'anywa madaraka muhimu ya kiutawala na maafisa waandamizi wa jeshi la mgambo katika *diwan*, pasha wa Tunis, alibakia kama ishara ya utii kwa Uturuki. Lakini mnamo mwaka 1591 maafisa hawa waandamizi walilazimika kuwaachia wawakilishi wa Mayeniseri nafasi walizokuwa nazo katika *diwan*. Hata hivyo demokrasia hiyo ya kijeshi iliyoanzishwa haikudumu kwa muda mrefu: mnamo mwaka 1598 kiongozi mmoja wa Kituruki, yaani *dey*, alijichukulia mamlaka yote na kuanzisha utawala wa mtu mmoja. Karibu takribani mwaka 1630 mamlaka mpya ilijitokeza nchini, ile ya *bey* au kamanda wa majeshi ya nchi kavu. Cheo hiki, ambacho kilishikiliwa na *mamluk* (mtu aliyepewa uhuru) mwenye asili ya ki-Genoa aliyeitwa Murad, kilimwezesha mwenye kuwa nacho kuteka maeneo ya bara kwa kuyapora mashirikisho makubwa ambayo hadi wakati huo yalikuwa huru. *Bey* alijiimarisha, akaweka madaraka mengi sana mikononi mwa familia yake (ukoo-tawala wa ki-Murad), na akaamua kufuata sera ya kifalme kwa kuzingatia mila ya nchi hiyo. Alimshinda adui wake, *dey*, hasa katika mapambano ya silaha ya mwaka 1673. Lakini ushindi huo wa Wamurad ulikuwa wa muda mfupi tu. Zahama za mwishoni mwa karne ya kumi na saba, kudhoofika kwa jeshi la mgambo la Kituruki, magomvi miongoni mwa ma-*bey*, na hila na kuingilia kati kwa Algiers - yote haya yakasababisha kushindwa kwa jaribio hili la kwanza la kuunda nusu ufalme wa kitaifa

mnamo mwaka 1702.

Hali ya namna hiyo hiyo ilitokezea Tripoli, ingawa baadaye kidogo. *Dey* aliteuliwa mnamo mwaka 1603-4 na sera iliyofanana na ya Wamurad wa Tunis ikafuatwa kati ya 1630 na 1672 , huku *bey* akiwa mtawala mkuu, hasa wakati wa Murad al-Malti (1679-86) na *bey* wa *Kikulughli* Ahmad Karamanli mwaka 1711. Hata hivyo, mageuko haya yenye mwelekeo wa utawala wa kifalme uliotangamana na mapokeo ya nchi yenyewe yalikinzwa huko Tripoli na vizingiti kadhaa: kuingiliwa kati na Istanbul, ambayo ilikuwa inajaribu kuchukua tena mamlaka katika nchi, nguvu za umoja wa Mabedui, hamu ya sehemu ya mashariki ya jimbo hilo, Benghazi, na sehemu ya jimbo la kusini, Fezzan, kutaka kujitegemea, na mwisho, uchechefu wa raslimali za nchi. Mamlaka yakawa sasa yategemea urari usio thabiti baina ya Waturuki na watu mashuhuri wa mijini, maslahi ya baharini na nchi kavu, miji, makabila makuu, makao makuu na majimbo.

Utawala wa Algiers uliendelea kwa muda mrefu zaidi katika umbo lake kama jimbo la kijeshi la Kituruki. Hapo pasha aliendelea kuwa na nguvu na baadhi ya mamlaka yake hadi 1659, wakati *diwan* na *agha* (maofisa waandamizi wa jeshi la mgambo) walipotwaa madaraka. Hii nayo haikuendelea kwa muda mrefu kwani *dey*, akiwa kwanza anawakilisha makapteni wa kiharamia na kisha Mayeniseri, alinyakua madaraka hayo mnamo 1671. Lakini madaraka ya ma-*dey* yalibakia kuwa ya mashakani na wengi wao waliondolewa madarakani na kuuawa katika maasi ya Mayeniseri. Kwa hiyo utawala wa Algiers ulikuwa utawala wa kijeshi ambao ulikuwa wa kidemokrasia zaidi katika karne ya kumi na saba, lakini kwa manufaa ya tabaka-amali la Waturuki tu, kutokana na kutokuwepo kwa kundi imara la wazawa wa tabaka la juu.

Kwa ujumla, tukiachilia mbali mwelekeo wake kuhusu waali wenyeji, utawala katika majimbo yaliyokuwa chini ya mfalme uliendelea kuwa na uhusiano wa karibu na Istanbul. Sera yake kuhusu jamii za vijijini ilikuwa ya kikatili sana na ililenga katika kuwakandamiza sana raia wake. Lakini kuanzia karne ya kumi na saba, tabaka-tawala lilianza kutumia utaratibu wa kushirikiana na baadhi ya wenyeji ili kusimika utawala wake, angalau huko Tunis. Lakini mara nyingi nguvu iliendelea kutumika kuliko sera nyingine yoyote.

## Mapato kutoka nje: Uporaji wa baharini na biashara

Baadhi ya maandishi ya kihistoria ya kikoloni yameichukulia historia ya sasa ya Maghrib kuwa historia ya uporaji wa baharini ambao umenasibishwa na uharamia. Lakini uporaji wa baharini, tofauti na uharamia, ulifanywa na sehemu ndogo sana ya watu wa Maghrib, na katika miaka ya baadaye ya karne ya kumi na saba ulipambanishwa na maslahi ya biashara ya mataifa makubwa ya Ulaya na washirika wao wenyeji.

### *Uporaji wa baharini katika Maghrib kunako karne ya kumi na saba*

Ukiwa ni urithi uliotokana na harakati za mapambano ya Waturuki dhidi ya maadui

wao Wakristo katika karne ya kumi na sita, uporaji wa baharini ukawa ni haki ya Majimbo yaliyokuwa chini ya Uturuki katika Maghrib baada ya Uturuki kufanya mkataba wa amani na Wahispania katika eneo la Mediterania, na baada ya majimbo ya Kituruki yaliyokuwa magharibi kujipatia uhuru wa kujifanyia mambo yao wenyewe. Uporaji huo ulifanywa hasa na Waturuki, Waalbania na Wakristo walioongolewa, kwa maslahi yao wenyewe, na ulibakia katika ukiritimba wa kikundi kidogo cha tabaka-tawala la Kituruki. Malengo na madhumuni ya uporaji huo yalikuwa mengi: ukichukuliwa kama vita vitakatifu kwa kila hali, uporaji ulisaidia kuhalalisha utamalaki na mamlaka ya Waturuki katika majimbo ya Maghrib yaliyokuwa chini yake, na ulileta faida kubwa kubwa kutokana na fidia ya kuachiliwa watumwa na utekaji wa merikebu za Wakristo. Ilikuwa ni shughuli yenye faida sana kwa waporaji wa baharini na maharamia waliojishughulisha nayo, kwa madola ambayo yalipata sehemu kubwa ya faida za shughuli hiyo, na kwa namna isiyo ya moja kwa moja, kwa watu wote walioishi kwenye bandari za maharamia. Umuhimu wa uporaji wa baharini ulitofautiana kipindi hadi kipindi. Historia yake katika majimbo yaliyokuwa chini ya mfalme wa Uturuki ikiwa imeanzia kwenye miaka ya 1580, uporaji huo ulifikia kilele chake kutokana na vita vya nchi za Ulaya katika sehemu ya mwanzo ya karne ya kumi na sita. Majimbo hayo yaliweza kuunda makundi mengi ya manowari ambayo vituo vyake vikuu vilikuwa Algiers na Tunis. Nusu ya pili ya karne hiyo ikashuhudia kuendelea kufifia kusikozuilika kwa uporaji wa baharini kulikosababishwa na kuongezeka kwa matumizi ya silaha kali zaidi za moto katika manowari za Ulaya na maendeleo ya kibiashara katika mataifa makubwa ya Kikristo. Kuanzia miaka ya 1680 Ufaransa na Uingereza zikayalazimisha majimbo hayo ya Kituruki kuheshimu meli zao na biashara zao, na uporaji ukabakia tu dhidi ya mataifa madogo madogo ya Kikristo. Kuanzia wakati huo ikawa ni mara chache sana, kama ilivyokuwa wakati wa vita vya Ulaya (hasa vile vya mwishoni mwa karne ya kumi nane na mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa), ambapo uporaji wa Kimaghrib uliweza kufanywa pasi na kizuizi; na hata wakati huo ilikuwa ni kwa muda mfupi tu.

*Maendeleo katika biashara kati ya Ulaya na Maghrib katika karne ya kumi na saba*

Uporaji haukuondoa kabisa uendeshaji biashara kwa amani, na ulianza kufifia sana na kutoa mwanya kwa shughuli za biashara katika nusu ya pili ya karne ya kumi na saba. Badiliko hili inaelekea lilichombezwa kwanza na athari ya mataifa makubwa ya Ulaya ambayo hatimaye yalishinikiza mawazo yao kwa watawala wa Maghrib. Hawa wa mwisho waligawanyika katika makundi mawili: kundi la kijeshi na kundi la kiraia, ambalo lilipendelea zaidi biashara, na likawapiku wakinzani wao, hasa katika Tunis. Ni katika hali hiyo ambapo mahusiano ya kibiashara na Ulaya yaliimarishwa kwa misingi mipya.

Biashara ya kimapokeo ya kupitisha bidhaa ilikuwa inaanza kutoweka, isipokuwa tu katika vituo vya njia za kuvuka Sahara kupitia Tripolitania, na katika misafara ya mahujaji iliyosafiri kati ya Moroko kusini na Maka, na ambayo ilivuka oasisi za

Algeria na Tunisia, Tripolitania, na Misri. Biashara ambayo sasa ilitawala, katika ukubwa na thamani, ilikuwa ni ile ya baharini iliyolazimishwa na mataifa ya Ulaya.

Bidhaa zilizosafirishwa Ulaya zilitoka katika bara ya Maghrib. Kulikuwa na ongezeka la mahitaji ya nafaka, hasa katika majimbo ya kusini ya Ulaya magharibi. Ili kuweza kukidhi mahitaji haya na kujiongezea mapato yao, madola ya Maghrib yaliingilia kati na kujishirikisha kwa nguvu katika biashara hii ya kusafirisha nje bidhaa. Usafirishaji nje wa bidhaa za kazi za mikono haukupewa aula, na bidhaa hizo zilisafirishwa hasa katika nchi nyingine za Kiislamu, kwa mfano *checia* (kofia nyekundu za sufi) kutoka Tunis, bidhaa za nguo za fahari na ngozi iliyotengenezwa tayari.

Mbali na bidhaa za kifahari kwa matumizi ya waali wachache, bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ni pamoja na zana za kudhibitia nchi kama vile silaha, sarafu, karatasi, na bidhaa kadha wa kadha kwa matumizi ya mafundi wenyeji kama vile sufi na rangi. Bila shaka watu walionufaika zaidi na mahusiano haya ya kibiashara ni madola ya Ulaya na wafanyabiashara na wasafirishaji wao. Lengo kubwa la tabaro kuu za baharini katika miaka ya 1670 na ya 1680 lilikuwa ni kupunguza uporaji wa baharini na kuiweka biashara ya Ulaya katika misingi imara, ya kutegemewa na yenye faida. Huu ndio uliokuwa mwanzo wa sera ya mikataba isiyowiana.

Ajabu ni kwamba mara nyingi mikataba hii ilikubaliwa na Maghrib, siyo tu kwa sababu ya kuogopa uwezo wa Ulaya kisilaha, lakini pia kwa maslahi yao wenyewe, kwani walipata faida kubwa kutokana na biashara ya baharini; faida ambazo waliweza kutumia kununua bidhaa za Ulaya na silaha. Isitoshe, baadhi ya makundi ya kijamii ambayo yalijishughulisha na biashara ya Ulaya pia yalifaidika nayo, kama walivyokuwa wakulima wa mizeituni katika Sahel na wamiliki wa mashamba makubwa yaliyolimwa nafaka.


## *Karne ya kumi na nane: kipindi cha mafanikio au mpumuo?*

Kimapokeo wanahistoria huichukulia karne ya kumi na nane ya (utawala wa) Waturuki kama kipindi cha zahama na kudhoofika kwa haraka. Je, madai haya yana ukweli kiasi gani kwa upande wa iyala za magharibi *(sanjak)*?

### Jamii za Maghrib katika karne ya kumi na nane


Kinyume na hali ilivyokuwa katika karne iliyotangulia, karne hii Maghrib haikupata mabadiliko yoyote muhimu. Hata hivyo maendeleo fulani yanaweza kuonekana, kama vile kuenea kwa kilimo cha nafaka katika mashamba makubwa makubwa na kupanuliwa kwa kilimo cha mipea-miba yenye thamani sana nje ya makazi ya Andalusia ambako ilianzia kulimwa.

Lakini njia za uzalishaji hazikubadilika, na miundo ya kijamii ilibakia na sifa zake zilezile, iwe zimerithiwa kutoka zama za kale au za hivi karibuni. Mabadiliko pekee ambayo tunaweza kutaja hapa ni yale yaliyoletwa na huduma za kijamii au kukua kwa biashara na Ulaya. Kwa hiyo nguvu ya familia fulani za wenyeji maarufu katika



**9.2** *Sura ya mji wa bandari ya Tripoli, iliyochorwa na mchoraji wa Kifaransa F.A. Aveline kwenye karne ya kumi na nane*

**9.3** *Sura ya mji na bandari ya Algiers, iliyochorwa na mchoraji wa Kifaransa F.A. Aveline kwenye karne ya kumi na nane*



uongozi wa juu wa jamii za vijijini, katika baadhi ya ofisi za kidini na katika ofisi za utawala au za rushwa iliimarishwa. Kuna mifano dhahiri kabisa ya kuinukia kwa baadhi ya familia za ki-*kulughli* katika *beylik* za Algeria, na familia za Kiyahudi za Algeria ambazo zilishiriki vikubwa katika mahusiano baina ya Algiers na Ulaya mwishoni mwa karne ya kumi na nane na mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa. Katika Tunis maeneo makubwa sana ya *lizma* (majimbo ya kilimo) yaliziwezesha baadhi ya familia kupata mali na uwezo.

## Dola la Tunisia katika karne ya kumi na nane

Katika karne ya kumi na nane Tunisia ndilo lililokuwa dola imara na lililounganika zaidi kuliko madola mengine yote. Bado lilikuwa ni jimbo la himaya ya Waturuki, likitawaliwa na *veli* (gavana) ambaye aliteuliwa Istanbul; tabaka la Kituruki liliendelea kutawala kisiasa na kijamii, lakini kwa hakika utawala wa Uturuki katika sehemu hii ulianza sasa kuwa wa kidhahnia zaidi. *Bey* wa Tunis alikuwa na uhuru kamili, tabaka-tawala la Waturuki, ambalo lilikwisha waingiza ma-*kulughli*, likaanza kuingiza wenyeji wa tabaka-bora, na wanamgambo wa Kiyeniseri wakabakia na kazi ya jeshi tu. Mwisho, athari za sera ya matumizi ya nguvu zilipunguzwa na mazoea ya *bey* ya kupenda kufanya makubaliano na wenyeji mashuhuri, hasa viongozi wa dini, ambao walijiunga upande wa ufalme kutokana na marupurupu na mafao mengi waliyoyapata.

Akiitumia vizuri fursa ya uvamizi wa bara ya Tunisia uliofanywa na majeshi ya Kituruki kutoka Algiers mwaka 1705, afisa mmoja wa ki-*kulughli*, Husayn b. Ali, alijitangaza kuwa *bey*, akaongoza upinzani dhidi ya wavamizi, na akaitumia nafasi ya ushindi wake kuanzisha nasaba ya nusu-ufalme. Aliwawekea Waturuki mipaka ya kubakia tu na shughuli za kijeshi, na wawakilishi wao, *pasha* na *dey*, wakabakia kuwa na vyeo vya heshima tu, na kwa kuwatumia zaidi ma-*kulughli*, Waandalusia na wenyeji wa tabaka-bora, akaweza kwa kiasi kikubwa kuweka utawala unganifu. Lakini kukawa na mikinzano kati ya jaribio hilo la uunganifishaji na hali halisi ya jamii ya vijijini iliyokuwa imegawanyikagawanyika, kati ya kuwaondoa Waturuki katika siasa na hadhi ya utawala huo kama jimbo lililokuwa chini ya Uturuki, na kati ya uchumi wa kijungujiko na biashara kubwa iliyokuwa ikiendeshwa na *beylik*. Mwaka 1728 mpwa wa *bey*, Ali Basha, akaasi. Papo hapo nchi ikagawanyika kati ya wale waliounga mkono maasi (Wa-*bashiya* au Wapasha) na wale waliomtii *bey* aliyekuwa madarakani (Wa-*husayniya* au Wana-Hussein). Zahama hiyo iliendelea katika sura mbalimbali hadi mwaka 1762.

Baada ya hapo Jimbo likapata amani na utulivu hadi baada kidogo tu ya 1815. Huu ulikuwa wakati wa Ali Bey (1759-82) na Hammuda Pasha (1782-1814), kipindi cha kiasi fulani cha ustawi licha ya kuwapo kwa balaa la ugonjwa wa tauni mwaka 1785 na vipindi viwili vya njaa mnamo 1777-8 na 1804. Mapato kutoka vyanzo vya nje yakapanda kwa kiasi kikubwa kutokana na kuimarika kwa mahusiano ya kibiashara na Ulaya, kuongezeka kwa mahitaji ya chakula katika Ulaya wakati wa vita vya kimapinduzi na Vita vya Napoleon, na mwisho kurejewa kwa shughuli za

uharamia kwa kutumia nafasi iliyojitokeza kutokana na vita hivyo. Hali hii ililiwezesha dola kuwapunguzia wananchi mzigo wa kodi au angalau kutoongeza kodi, na hivyo kupunguza mivutano ya kisiasa.

Aidha *bey* wa Tunis alishinda katika mapambano ya vita dhidi ya wageni katika Venisi (1784-92), Tripoli (1793-4) na, muhimu kuliko sehemu zote, Algiers, ambako utawala wa kigeni ulikoma mwaka 1807.

Kipindi hiki cha utulivu na mafanikio, ambacho Tunis ilikifurahia kwa zaidi ya nusu karne, kilikwisha mara tu baada ya mwaka 1815, wakati upanuzi wa Ulaya uliporudi tena katika mazingira tofauti ukiwa unaashiria ubeberu wa kikoloni.

## Iyala ya Algiers katika karne ya kumi na nane

Kati ya majimbo matatu ya Maghrib yaliyokuwa chini ya utawala wa Uturuki jimbo la Algiers ndilo liloendelea kutawaliwa na tabaka la kigeni la kijeshi kwa muda mrefu kuliko yote. Lakini pamoja na hivyo bado likapata mabadiliko.

Ingawa uporaji wa baharini ulikuwa umepungua sana, bado ulikuwa ukifanyika kwa haadhi ya nchi za Kikristo kama vile Hispania. Ili kulinda meli zao za biashara, nchi za Skandinavia na madola kadhaa ya Kiitalia, kama vile Venisi, yalikubali kulipa ushuru kwa Algiers. Wakati huo huo biashara iliendelea kati ya Algiers na madola makubwa ya kibiashara ya Ulaya ya Ufaransa na Uingereza, ambayo zaidi yalileta nafaka.

Vita dhidi ya mataifa jirani vililinufaisha sana tabaka-tawala la Algiers. Kuingilia kati kivita kulikofanyika Tunis katika kuwatetea wale waliojifanya watawala mnamo mwaka 1735 na 1756 kuliingiza ngawira nyingi na kodi ya siri iliyolipwa na Tunis kuanzia mwaka 1756 hadi 1807.

Ndani ya nchi, kodi ziliendelea kukusanywa kwa kutumia *mah'alla* (msafara maalumu iliyokuwa na silaha) kwa manufaa ya tabaka-amali la Kituruki, ambalo liliwaondoa ma-*kulughli* katika jeshi na ofisi nyingine za ngazi za juu. Sera hii ilileta upinzani mkali: maasi mengi ya ma-*Kabyle* dhidi ya serikali, maasi maarufu ya huko Oran yaliyoongozwa na tarika za kidini, na maasi katika Konstantini mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa yaliyoongozwa na mamwinyi wenyeji.

Kuanzia mwishoni mwa karne ya kumi na saba, kulikuwa na mwelekeo wa mtawala mmoja, *dey*, kuhodhi mamlaka. Huyu aste aste alikuwa akiungwa mkono na kundi dogo la maafisa wa Kituruki wa ngazi za juu ambamo ndimo alimochaguliwa. Kutokana na hali hiyo utawala wa Algeria ukawa imara na madhubuti zaidi. Kati ya 1710 na 1798 ma-*dey* walidumu zaidi katika ofisi, Muhammad b. 'Uthman akiwa ametawala kuanzia 1766 hadi 1791.

Katika majimbo mabadiliko yalijidhihirisha zaidi, kwani ma-*bey* wa Konstantini, Titteri na magharibi, wakiwa na idadi kidogo tu ya Mayeniseri, walilazimika kuwaegemea watu mashuhuri na viongozi wenyeji. Aidha kulikuwa na ma-*bey* wa ki-*kulughli*, ambao walikuwa na uhusiano wa damu na familia maarufu za asili.

Mabadiliko haya yaliukumba mji mkuu vile vile, ingawa baadaye kidogo. Kwa msaada wa ma-*kulughli* na Wa-Zwawa, Dey 'Ali Khoja akaondosha kabisa mabaki ya

kikosi cha Mayeniseri, kama walivyofanya ma-*bey* wa Tunis na Tripoli karne moja kabla yake. Kutaifishwa kwa utawala wa Kialgeria kungeweza sasa kufanyika, lakini utamalaki wa Wafaransa ukakomesha mwelekeo huo ambao pengine ulianza ukiwa umechelewa mno.

## Iyala ya Tripoli katika karne ya kumi na nane

Kama ilivyokuwa katika Tunis mwanzoni mwa karne hiyo, mnamo mwaka 1711, afisa mmoja wa ki-*Kulughli*, Ahmad Karamanli, alitwaa madaraka katika Tripoli na akaanzisha nasaba-tawala ya ma-*bey* ambayo ilitawala hadi mwaka 1835. Mafanikio ya nasaba-tawala hii yalitokana na sababu kadhaa: Kwanza, ni urefu wa vipindi vya utawala wa Ahmad, Ali na Yusuf; pili, ni kuwepo kwa mapatano mengi ya kirafiki baina ya ma-*kulughli* na familia maarufu za Tripolitania; tatu, ni wingi wa mapato ya ma-*bey* kutoka vyanzo vya nje. Kulikuwa na mapato ya moja kwa moja na yasiyo ya moja kwa moja kutokana na uporaji wa baharini ambao ulihuishwa baada ya 1711 na kisha tena kati ya 1794 na 1805; kulikuwa pia na mapato yaliyotokana na biashara kubwa ya kuvuka Sahara kupitia Fezzan, na biashara ya Mediterania kati yake na Leghorn na nchi za Levanti.

Hata hivyo utawala huo wa Tripoli ulipata matatizo makubwa. Kwanza kulikuwa na maafa asilia kama ile njaa ya 1767-8 na baa la tauni la 1785. Pili, ni lile tatizo lililotokana na kugawanyika kwa watu wa nchi hiyo katika mashirikisho makubwa mawili ambayo ushindani wake ulikuwa chanzo cha maasi na vita vya wenyewe kwa wenyewe, kama vile vya 1791-3 vilivyofumuka miongoni mwa wanafamilia ya Karamanli. Mwisho, Istanbul haikukata tamaa katika jitihada zake za kutwaa tena madaraka katika Tripoli. Mwaka 1793 afisa mmoja wa Kituruki, Ali Burghul, aliingia Tripoli na kuwafukuza Wakaramanli. Lakini alipojaribu kufanya hivyo katika Jerba, katika ardhi ya Tunisia, alifukuzwa na *bey* wa Tunis, ambaye alimrudisha madarakani Yusuf Karamanli. Hata hivyo mnamo mwaka 1835 Waturuki waliingia Tripoli na serikali kuu ya Uturuki ikachukua madaraka ya moja kwa moja juu ya Libya.

Chanzo cha mwisho cha matatizo ya utawala huu, ingawa si cha mwisho katika umuhimu, ni yale majaribio ya Wakristo ya kupunguza uporaji wa baharini. Ikiwa ndiyo kwanza inaingia katika medani ya kimataifa, Marekani ilipigana vita na Tripoli kuanzia 1801 hadi 1805. Vita hivyo viliisha kwa makubaliano ya amani. Baada ya mwaka 1815 Wazungu ndio walioondoa uporaji wa baharini na kuiingiza nchi hiyo katika biashara yao na kwa masharti yaliyowafaa wao. Mara kwa mara walidai fidia kutoka utawala wa Tripoli kwa kitu chochote kile, na kwa hakika kwa kila kitu. Likiwa limetindikiwa na vyanzo vya kifedha, dola la Tripoli likajikuta katika hali ngumu, na zaidi ya yote, likawa linamomonyolewa na maasi mbalimbali ambayo lilishindwa kabisa kuyazima. Tripoli likawa mboga kwa himaya ya Uturuki ambayo ilirejesha utawala wake tena mnamo mwaka 1835 na ikaendelea kutawala kwa muda mrefu.

## Hitimisho

Katika karne ya kumi na sita Maghrib ilishuhudia zahama kubwa, ambayo kimsingi ilisababishwa na kushindwa kwake kujirekebisha ili kukabiliana na ulimwengu wa silaha za moto (bunduki), falme unganifishaji, na hazina za Amerika. Waturuki wakazipa nchi za Magrib kati na mashariki ufumbuzi kwa kuanzisha, katika sehemu hizo, mfumo wa kisasa wa jeshi na utawala ambao ulikuwa na uwezo wa kuweka ulinzi dhidi ya shambulio lolote kutoka nje, na utulivu ambao angalau ulitakikana katika kuhakikisha usalama wa maisha kwa watu wote. Lakini wakati huo huo wakasimika utawala mkali ulioandamana na unyonyaji mbaya wa raslimali za nchi ambao ulichangia katika kudumaa kwa maendeleo ya jamii za asili za hapo.

Zikiwa katika kasi ya kuachana na kuitegemea Istanbul (bila kukataa wazi kutii mji-mama) *ojak* za magharibi polepole zilijitenga na kuwa madola peke na ambayo yalikuwa na mwelekeo wa kuhasimiana. Vita vilivyopiganwa baina ya tawala za Tunis na Algeria kati ya 1600 na 1800 vilikuwa havipungui kumi. Mataifa haya yaliinukia kwa namna tofauti kabisa: wakati tabaka-tawala la Kituruki katika Tunis na Tripoli taratibu liliwaingiza ma-*kulughli* na wenyeji mashuhuri, huko Algiers matabaka hayo yalitengwa kabisa. Matokeo yake yakawa ni kuzaliwa kwa dola ambazo zilikuwa za nusu-kitaifa katika karne ya kumi na nane katika Tunis na Tripoli na kuendelea kuwepo, katika Algiers, kwa utawala ambao kwa kiasi kikubwa ulikuwa umeathiriwa na asili yake ya utamalaki wa kigeni. Maendeleo haya tofauti na ya kipekepeke ya iyala (ambazo tofauti zao baadaye zilizidishwa na uanuwai wa hali zao za ukoloni) yaliukilia kugawanyika kwa Maghrib katika mataifa yaliyojitenga hadi hii leo.

Historia ya Maghrib ya Waturuki pia iliukiliwa na uhusiano wake na Ulaya ya Kikristo. Ulaya ilileta zana na vifaa vingi vya kisasa ambavyo viliyawezesha madola hayo na matabaka-tawala yake ya kigeni kuwatawala wenyeji. Walileta pia watu ambao walikuja na tekinolojia mpya na mawazo mapya. Kwa hiyo mahusiano baina ya Maghrib na Ulaya yalikuwa muhimu sana kwa matabaka-tawala ya Maghrib. Kwanza kukawa na mahusiano ya vita, yakiandamana na uporaji wa baharini, kisha mahusiano ya amani, hasa ya kibiashara. Ubepari wa Ulaya ndio ulionufaika zaidi na mahusiano haya ya kibiashara, lakini watawala wa Maghrib na washirika wao wenyeji pia walinufaika, angalao kwa muda walioweza kulinda maslahi yao dhidi ya washindani wao wa Kizungu hadi kwenye miaka ya 1815. Tarehe hiyo inaonyesha wazi mwisho wa kipindi kimoja na mwanzo wa kingine - kile cha kutawaliwa moja kwa moja na Wazungu.

# 10 Senegambia kuanzia karne ya kumi na sita hadi karne ya kumi na nane: kuinukia kwa Wawolof, Wasereer na Watukuloor

## *Utangulizi*

Senegambia ambayo inaundwa na mabonde ya mito Senegal na Gambia iko katikati ya Sahara na msitu. Hadi kufikia karne ya kumi na tano ilikuwa chini ya utegemezi wa nchi za Sudani na Sahara, lakini kufunguka kwa mipaka yake ya upande wa Atlantiki kutokana na kufika kwa Wareno kuliipa umuhimu mkubwa wa kijiografia-kisiasa kama mahali mwafaka pa kuingilia kwa utawala wa Ulaya wa kiuchumi na kisiasa na kama njia ya kupitia bidhaa za Sudani Magharibi.

Kuanzia karne ya kumi na tano biashara ya Wareno ya dhahabu, pembe za ndovu, ngozi na watumwa ilibadilisha njia za biashara kutoka bara kuelekea pwani, na kadri karne ya kumi na sita ilivyokuwa ikiendelea, biashara hiyo ikachochea kuvunjika kwa haraka kwa shirikisho la Jolof na kuinukia kwa ufalme wa Denyanke katika bonde la Senegal na ufalme wa Kaabu katika Mito ya Kusini.

Katika karne ya kumi na saba, kugawanywa kwa Pwani katika miliki za Kiholanzi, Kifaransa, Kiingereza na Kireno kulitokea sawia na vuvumko la biashara ya watumwa ambayo iliendelea kuwapo katika kipindi chote cha karne ya kumi na nane na ambayo ilikuwa sifa kuu ya biashara ya Atlantiki. Biashara ya watumwa ya Atlantiki ikaleta machafuko na ikaimarisha tabia ya kishari na isiyo na kanuni ya utawala wa masedo (*cedo* = malodi wa kivita), kama ilivyokuwa katika utawala wa *damel-teen* wa Kayor na Bawol, na *satigi* wa Futa Toro. Katika hali ya kukabiliwa na machafuko ya masedo, Uislamu ukawa ndio kinga pekee iliyotumiwa na utawala wa ukoo-bora. Mwishoni mwa karne ya kumi na saba waumini wa Kiislamu wakaingia vitani katika Vita ya Murabiti. Kushindwa kwao kukafuatiwa na mafanikio makubwa sana ya mapinduzi katika Bundu, Futa Jallon na Futa Toro katika karne ya kumi na nane. Katika hali hii ukinzano kati ya utawala wa Kiislamu (wa kidini) na utawala wa masedo unakuwa ndio usuli wa historia ya Senegambia ambayo iliathirika vibaya kutokana na matokeo ya biashara ya Atlantiki.




**10.1** *Senegambia kuanzia karne ya kumi na sita hadi ya kumi na nane*

## *Ukiritimba wa Wareno na kuchorwa upya kwa ramani ya mipaka ya kisiasa katika karne ya kumi na sita*

Senegambia ndio sehemu ya upwa wa Afrika ambayo imetokeza sana magharibi. Baada ya kuwa chini ya utegemezi wa Sudani na Sahara kwa muda mrefu, katika karne ya kumi na sita nchi hii iliingia katika athari za Atlantiki kutokana na majilio ya Wareno, ambao biashara yao ilileta mabadiliko makubwa sana, hasa kule kuchorwa upya kwa ramani ya mipaka ya kisiasa ya Senegambia katika miaka ya katikati ya karne ya kumi na sita.

### Biashara ya Wareno

Senegambia, ambayo ilikuwa chini ya Mali, baada ya muda mfupi ilitawaliwa na Wamande Juula (Dyula), ambao walikuwa pambizoni mwa Mto Gambia na ambao, kupitia mfuatano wa hatua kadhaa, waliingiza pindi la ya mto Niger (Niger Bend) katika biashara ya kola, chuma na nili (indigo) kutoka maeneo ya msituni. Kutokana na hali hiyo, watamalaki wa Mande wakaanzisha ufalme wa Kaabu, kusini mwa mto Gambia, ambao, kwa kutumia mamlaka ya Mali, ulikuja kutawala sehemu yote ya kusini ya Senegambia na baadhi ya sehemu zake za kaskazini.

Mgogoro wa urithi uliofuatia kifo cha Mansa Sulayman mnamo mwaka 1630 ulisababisha kuanzishwa kwa shirikisho la Jolof ambalo mtawala wake, Njaajan Njaay, alipanua utawala wake na kuitwaa sehemu yote ya Senegambia kaskazini kati ya Mto Senegal na mto Gambia. Hata hivyo baada ya muda mfupi utawala wa Jolof uliteteresliwa na hatimaye kuanguka, katikati ya Karne ya kumi na sita, kutokana na uvamizi ulioongozwa na Koly Tengella ambaye alitoka Pwani ya Mali na Wafulbe wengi akaenda kuishi katika nyanda za juu za Futa Jallon. Baada ya 1490 rafiki za Koly wengi, au pengine mwanaye wa kiume, walielekea kaskazini na kuanzisha ufalme wa Denyanke huko Futa Toro, katika bonde la Senegal.

Kuanzishwa kwa ufalme wa Denyanke kulitokea sawia na tuajilio ya Wareno ambao ndio waliokuwa Wazungu wa kwanza kufanya safari za upelelezi katika upwa wa Afrika. Walianzisha makazi Arguin kwenye miaka ya 1445 wakiwa na nia ya kuikengeushia Atlantiki biashara ya Sudani na Senegambia; biashara ambayo hapo awali ilikuwa ikielekezwa kaskazini kuvuka Sahara.

Wareno wakiwa wameweka makao yao katika Visiwa vya Rasi ya Verde (Cape Verde Islands), walishiriki katika biashara iliyokuwa pambizoni mwa upwa na katika malango ya mito Senegal na Gambia kwa kuvinjari pwani pwani. Walijiimarisha vikubwa katika Mito ya Kusini na huko Gambia kutokana na umuhimu wa kibiashara wa ukanda huu. Biashara ya Wareno katika dhahabu, pembe za ndovu, ngozi, na watumwa pia ikapandikizwa kwenye biashara ya zamani ya kikanda katika bidhaa za kola (*kola nuts*), chumvi, bidhaa za pamba, chuma na nili. Haukupita muda mrefu Wareno wakawa pia wamejishughulisha sana katika kituo muhimu sana cha biashara cha Wuli, ambapo ndipo ilianzia misafara iliyounganisha Gambia katika uelekeo wa

kaskazini kwenda Senegal ya juu na uelekeo wa mashariki kwenda pindi ya Mto Niger; na kutokana na hali hiyo Mali, ambayo sasa ilikuwa inaanza kudhoofika, ikalazimika kuelekea zaidi na zaidi Atlantiki kuuza dhahabu yake huko.

Biashara ya Sudani ya dhahabu, ambayo sasa ilizagaa katika masoko ya Wuli na Kantora, ilichukuwa nafasi kubwa sana katika kuyaondoa maeneo ya Bambuk na Bure katika mahusiano yake na pindi ya Niger na Sahara, na kuyafanya sehemu ya Senegambia. Ngozi lilikuwa zao la Senegambia la pili, ukiacha dhahabu, lililosafirishwa nje. Aidha kulikuwa pia na pembe za ndovu, nta na, zaidi ya yote, watumwa, bidhaa ambayo kwayo Senegambia haikuwa na mshindani, na ndiyo pia iliyokuwa chanzo kikuu cha watumwa walizosafirishwa kwenda Ulaya, katika Karne ya kumi na sita, na baadaye kupelekwa katika Dunia Mpya.

Isitoshe, tangu mwanzo, kutokana na msingi wa biashara ya watumwa, Wareno walianzisha uchumi wa mashamba makubwa katika Visiwa vya Rasi ya Verde, ambayo yaliwawezesha kuzalisha sukari, pamba na nili. *Lançados* au *tangomãos* (machotara wa Kireno-Kiafrika) pole pole wakajidhihirisha kuwa madalali muhimu kabisa kati ya biashara ya Ulaya na Senegambia, ambayo kufikia sehemu ya pili ya karne ya kumi na sita ilikuwa imepata mabadiliko makubwa.

## Uchoraji upya wa ramani ya mipaka ya kisiasa ya nchi za Senegambia katika nusu ya pili ya karne ya kumi na sita

Licha ya kutokuwa muhimu sana, biashara ya Ureno, katika karne ya kumi na sita, ilizusha hali ya hatari kiuchumi na kisiasa katika Mito ya Kusini na ikachapuza kuvunjika kwa shirikisho la Jolof kaskazini mwa Senegambia.

Hali hiyo ya hatari ilitokea mapema zaidi katika eneo lililo katikati ya Mto Kasamansi na Rio Kacheu ambako wafanyabiashara wengi wa Rasi ya Verde walikuwa wakiendesha shughuli zao. Hapo Wabainuki na Wakasanga, ambao walikuwa na ufundi wa hali ya juu wa kufuma na kutia nguo rangi, walinunua pamba kutoka Visiwa vya Rasi ya Verde. Wabainuki pia walisitawi kutokana na mazao yao ya kilimo ambayo yalihitajika kwa Wazungu wakazi na kwa ajili ya chakula cha shehena za watumwa. Hali bora ya Wabainuki ilichombeza mgongano kati yao na machotara, ambao mnamo mwaka 1570, wakiutumia vema utesi baina ya Wabainuki na Wakasanga, waliomba msaada kutoka kwa Mansa Tamba, mfalme wa Wakasanga. Utesi huo uliisha tu mwaka 1590 alipokufa Mansa Tamba.

Tokea mwanzo kabisa biashara ya watumwa ilianza kuitibua hali katika Mito ya Kusini kwa namna ya kudumu. Wamande, ambao walikuwa maarufu sana kwa kuwinda watumwa, waliimarisha nguvu za Kaabu, ambayo kutokana na hali hiyo ikawa na mamlaka juu ya ardhi yote kati ya mto Gambia na Futa Jallon. Halikadhalika wakazi wa visiwa vya Bijago nao wakaanzisha utaratibu wa kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika uwindaji wa watumwa kutoka bara. Wakati wanawake walijishughulisha na kilimo, uvuvi na ujenzi wa nyumba, wanaume walijishughulisha na utengenezaji wa almadi, zile mashua maarufu ambazo ziliunda

kundi kubwa la mashua za kivita ambazo ziliwawezesha kuwatia woga watu wa Mito ya Kusini. Kwa hiyo watu wa aina mbalimbali katika eneo hili wakawa ndio maathura wa kwanza wa biashara ya watumwa ya ng'ambo. Hata hivyo, makundi madogo zaidi ya eneo la Tenda - Wabassari, Wakoniagui na Wabadyaranke, waliokuwa wakiishi kati ya nyanda za juu za Futa Jallon na Mito ya Kusini, ndio hasa waliokuwa maathura wa biashara ya watumwa.

Maendeleo ya kisiasa ya nchi zenye nasaba za kitawala za Mito ya Kusini yalizuiwa na shinikizo kutoka majirani zao na ghasia zilizoletwa na uwindaji wa watumwa ulichombeza hali za kujihami na kujitenga. Kikwazo hiki kilidumu hadi karne ya kumi na tisa na utamalaki wa wakoloni.

Baada ya kusambaratika kabisa kwa dola la Mali, Kaabu ikawa ndiyo yenye nguvu kuliko sehemu nyingine yoyote. Ikadhibiti mtandao wa biashara ya Wabainuki na Wabafada kwa manufaa yake, na pia ikaziteka nchi zilizokuwa chini ya Mande kandoni mwa mto Gambia. Wamaane na Wasaana, ambao ndio waliokuwa koo-tawala za ufalme wa Naanko katika Kansala, wakaimarisha tabia yao ya kishari, na tokea mwanzo walikuwa ni ishara ya masedo, ambao walimiliki maisha ya kisiasa katika Senegambia wakati wa enzi za biashara ya watumwa ya ng'ambo.

Karne za kumi na sita na kumi na saba zikawa ndio kilele cha ufalme wa Kaabu ambao ulichukua nafasi ya Mali katika maeneo yote ya Mito ya Kusini mpaka ulipotokea ushindi wa mapinduzi ya uongozi wa kidini katika Futa Jallon mwanzoni mwa karne ya kumi na nane. Kupanuka kwa Kaabu kulitokea wakati sawia na maendeleo ya biashara ya watumwa ya ng'ambo na pia kuchukuliwa kwa biashara katika Mito ya Kusini na Wazungu. Hamasa katika biashara hii ya kikanda, ambayo ilikuwa muhimu sana kwa Senegambia yote, ilitoka kwa wananchi wazawa ikaenda kwa Wareno ambao walizigeuza Beafada, Bainuk, na zaidi ya yote, Mande na Bijago kuwa maeneo ya wawinda watumwa tu au watu wake kuwa madalali katika biashara ya Atlantiki kuelekea bara.

Mwishoni mwishoni mwa nusu ya pili ya karne ya kumi na sita Senegambia ya kaskazini, kati ya mto Gambia na mto Senegal, pia ikaingia katika mkumbo wa kuchorwa upya kwa ramani ya mipaka yake ya kisiasa; mipaka ambayo ilikuwa na athari kubwa na za kudumu.

Shirikisho la Jolof, likiwa sasa limekwishakuwa legelege kutokana na uvamizi wa kila mara ulioongozwa na Koly Tengella, likasambaratika kabisa kutokana na athari ya biashara ya Wareno ambayo ilipendelea sana majimbo ya pwani. Hivyo basi, Amari Ngoone, *damel* (mtawala) wa Kayor, baada ya ushindi wake dhidi ya Jolof wa Buurba, akatangaza kujitegemea kwa jimbo la pwani la Kayor, naye akawa *damel* wa kwanza. Mfano wake ukafuatiwa na majimbo ya Waalo, mwanzoni mwa mto Senegal, na Bawol, kusini magharibi. Kwa hiyo Jolof ikawa imepunguzwa sana kieneo, ikanyimwa mahusiano ya moja kwa moja na biashara ya Atlantiki na ikawa pia imeondolewa katika biashara ya kuvuka Sahara na ufalme wa Denyanke wa Futa Toro, ambao ulikuwa na nguvu kubwa.

Wafalme wa kisedo ambao walitokea baada ya kusambaratika kwa Jolof walileta zahama si tu katika mahusiano miongoni mwa nchi za Senegambia, bali pia katika mahusiano ya kisiasa na kijamii ndani ya kila nchi. Mchakato huo huo pia ukasababisha kuzaliwa kwa falme za Siin na Salum, ambazo hatimaye zilijiondoa kabisa katika dola la Jolof katika karne ya kumi na sita.

Katika kipindi fulani *damel* wa Kayor, Amari Ngoone, alijaribu kuingiza utawala wake kwa nguvu kwa kuzitwaa Bawol na sehemu ya Waalo. Akajipa cheo cha *damel-teen*, na hivyo basi akaanzisha msururu mrefu wa miungano iliyodumu kwa muda mfupi baina ya Kayor na ufalme wa Bawol. Lakini haikupita muda mrefu pambano baina ya Kayor na Bawol likamzuia *damel* kutimiza lengo lake la kuyaunganisha, chini ya utawala wake, majimbo ya zamani ya shirikisho la Jolof.

Hata hivyo kushindwa huko kwa *damel* kulitoa mwanya mwafaka wa kuinukia na kupata nguvu kwa ufalme wa Denyanke huko Futa Toro. Satigi akakutumia vizuri kusambaratika kwa Jolof kupanua utawala wake katika sehemu kubwa ya Senegambia kaskazini. Kutokana na hali hiyo, basi, ukoo-tawala wa Denyanke ukawa umefikia kilele cha ustawi wake mwanzoni mwa karne ya kumi na saba wakati wa utawala wa Samba Lamu. Futa Toro ikawa sasa imedhibiti biashara kati ya Sudani na Sahara, na pia biashara ya baharini, ya Ulaya.

## Kugawanywa wa pwani ya Senegambia na jinsi kulivyopokewa na Waislamu

Mwanzoni mwa karne ya kumi na saba ukiritimba wa Wareno katika upwa wa Afrika ulisaiwa kwa mafanikio makubwa kwa kufika, mmoja baada ya mwingine, kwa Waholanzi, Waingereza na Wafaransa. Nchi hizo za Ulaya zilijiingiza katika ushindani mkali, zikajijengea maeneo ya kumiliki katika Senegambia, ambayo yalilindwa kwa wivu kwa kujengewa ngome za vituo vya kufanyia biashara huko pwani.

Vituo hivi vya biashara kwanza kabisa vilitumika kama mahala pa kufanyia biashara ya watumwa, ambayo kufikia nusu ya pili ya karne ya kumi na saba ilikwishakuwa ndiyo shughuli muhimu ya nchi za Ulaya. Biashara ya watumwa, ikiandamana na mwenzi wake, uwindaji wa watu, ikazaa mahusiano kati ya nchi, kuanzishwa kwa nguvu za kijeshi, na kuinukia kwa Uislamu wa matumizi ya nguvu. Kwa hiyo kufikia mwisho wa karne ya kumi na saba chama kilichokuwa kikiongozwa na warabiti kilikwishaanzishwa kikiwa na lengo la kuziunganisha nchi za bonde la Senegal ili zipigane dhidi ya athari mbaya zilizotokana na biashara ya watumwa ya ng'ambo.

### Vituo vya biashara na kugawanywa kwa pwani

Kuchorwa upya kwa ramani ya mipaka ya kisiasa kulikwenda sambamba na kutokea tena kwa ghasia baina ya nchi na nchi na maendeleo ya biashara ya watumwa. Zoezi

hilo pia lilitokea sawia na majilio ya Waholanzi, Wafaransa na Waingereza, watu ambao kuwepo kwao katika upwa wa Senegambia kuliimarika wakati wa nusu ya pili ya karne ya kumi na saba.

Mnamo mwaka 1621 Waholanzi wakatamakani Goree, wakifuatiwa na Wafaransa mnamo mwaka 1659, ambao walitamakani Saint-Louis kwenye lango la mto Senegal, nao Waingereza wakajenga ngome ya Fort St. James kwenye lango la mto Gambia mnamo mwaka 1651. Kwa hiyo, taratibu Wareno wakawa wanaondolewa katika sehemu za kaskazini za Senegambia, lakini wakabakiwa na vituo vya biashara vya Kacheu na Bissau, mbali na maskani yao makuu ya Visiwa vya Rasi ya Verde. Lakini wakati huo tayari walikuwa wakishiriki pamoja na nchi za Ulaya katika soko kubwa la Mito ya Kusini.

Ngome ya Saint-Louis iliwawezesha Wafaransa kudhibiti biashara yote iliyokuwa pambizoni mwa mto Senegal kati ya Februari na Mei. Aidha kujengwa upya kwa ngome ya Fort St. Joseph katika Gajaaga, mwishoni mwa karne ya kumi na saba, kuliwahakikishia Wafaransa ukiritimba wa eneo lote hadi kufikia Senegal ya juu kwenye lango la kuingilia katika biashara ya Sudani.

Kisiwa cha Goree, ambacho kilikuwa na ukiritimba wa biashara kwenye *petite cote*, kwanza kilimilikiwa na Waholanzi, kisha kikachukuliwa na Wareno katika mwaka 1629 na 1645, kikachukuliwa tena na Waingereza mnamo mwaka 1667 na hatimaye kikachukuliwa na Wafaransa mnamo mwaka 1677. Kwa hiyo, wakiwa Goree, Wafaransa walifanya biashara na Kayor, katika kiwanda cha Rufisque; Bawol, katika kiwanda cha Portudal; na Siin, katika kiwanda cha Joal. Kusini zaidi walipata ushindani kutoka kwa Wareno, na zaidi ya wote Waingereza. Fort St. James ilidhibiti biashara zote zilizokuwa pambizoni mwa mto Gambia hadi kufikia Maporomoko ya Barakunda. Kila mji wa Mande katika mto huu, ambao unaabirika kipindi chote cha mwaka, ulikuwa na uweza wa kuwa bandari kwa biashara ya Waingereza, ambayo ilikuwa imeshanuri sana katika maeneo haya.

Katika hali hiyo Senegambia ikawa imezingirwa katika upwa wake wote na vituo vya biashara vilivyokuwa vimejengewa ngome na ambavyo kazi yake kubwa ilikuwa ni kuielekeza biashara ya eneo hili katika uelekeo wa pwani. Majengo haya ya kudumu yalikusudiwa kulinda kila eneo lililomilikiwa dhidi ya ushindani kutoka kwa nchi nyingine za Ulaya na kuzizuia nchi za Senegambia kuungana dhidi ya ukiritimba wa biashara ya Wazungu.

Kuwepo kwa wingi kwa Waholanzi, Wafaransa na Waingereza, ambako kulifuatia kuwapo kwa Wareno, katika Senegambia, kulihusiana sana na kuinukia kwa ufanyaji biashara wa kikoloni. Katika hamu yao kubwa ya kutaka kulimbikiza mali, nchi za Atlantiki zikajitumbukiza katika utamalaki wa masoko ya Afrika, Asia na Dunia Mpya.

Kila moja ya nchi za Ulaya ilikuwa na makampuni ambayo yalikuwa yamepewa ukiritimba wa biashara ya bahari: Kampuni ya Waholanzi ya India Magharibi (*Dutch West India Company),* iliyoanzishwa mwaka 1625; Kampuni ya Wafaransa ya India

Magharibi (*French West India Company*), iliyoanzishwa mwaka 1664; na Kampuni ya Kifalme ya Afrika (*Royal Africa Company*), iliyoanzishwa na Waingereza mnamo mwaka 1672. Makampuni haya yaliashiria kuinukia kwa nchi zenye utaifa katika Ulaya na yakaakisi ushindani kati ya nchi hizi katika utamalaki wa masoko.

Waholanzi, ambao ndio waliokuwa wa kwanza kuutibua ukiritunba wa Wareno, walitolewa katika upwa wa Senegambia na Waingereza na Wafaransa mnamo mwaka 1677, tukiacha Arguin na Portendick, ambako walibakia hadi nusu ya kwanza ya karne ya kumi na nane. Kwa hiyo Senegambia ikabakia imegawika katika eneo la Wafaransa, kuanzia Saint Louis hadi Goree, na eneo la Waingereza katika Gambia; na wakati huo huo Wafaransa na Waingereza walishindania Mito ya Kusini pamoja na Wareno. Kumilikiwa kwa Gambia kulikuwa muhimu sana kwa sababu ya ukaribu wake na Ulaya katika wakati ambapo maendeleo ya mashamba yalikuwa yakichapuka na yakiwa yanahitaji watumwa mara tatu zaidi ya wale waliotakiwa katika India ya Magharibi kati ya 1651 na 1700.

Saint-Louis, Goree, St. James, Kacheu na Bissau zikageuzwa kuwa vituo vikuu vya watumwa ambako watumwa walionunuliwa bara walingojea meli za kuwachukua kwenda Dunia Mpya. Senegambia ilikuwa muhimu sana katika siku za mwanzo za biashara ya watumwa, katika karne za kumi na sita na kumi na saba, kwani masoko makuu ya pindi la Guinea na Angola yalianzishwa baadaye.

Haiwezekani kutoa makadirio ya kiwango cha watumwa waliosafirishwa nje kutoka Senegambia, lakini ni dhahiri kwamba biashara ya watumwa ya Atlantiki ilisababisha msukosuko mkubwa wa kisiasa na kijamii. Msukosuko huu nao ukasababisha kuanzishwa kwa chama kilichoongozwa na Warabiti na kilichozagaa sana katika bonde la Senegal miaka michache baada ya kujengwa kwa ngome ya Saint-Louis.

## *Vita vya* Warabiti

Baada ya kuundwa upya kwa nchi katika karne ya kumi na sita kutokana na athari za biashara ya Wareno, Senegambia ikapata msukosuko mkubwa katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na saba; msukosuko ambao ulijidhihirisha sana kaskazini mwa Senegambia.

Chama cha Warabiti, kikiendeshwa kwa kutumia jina la Uislamu na Murabiti wa ki-Moori Nasir al-Din, kilikuwa kikijua athari za kuwepo kwa Wazungu katika Senegambia, kwani chama hicho kilianzia kusini mwa Mauritania ya leo ambako jamii ya Waberiberi ilikuwa katika hali mbaya sana kiuchumi kutokana na kudidimia kwa biashara ya kuvuka Sahara, hali ambayo ilikuwa imezidi kuwa mbaya tangu kuanza kuwepo kwa Wafaransa katika Saint-Louis mnamo mwaka 1659.

Kisiwa cha Saint-Louis, kutokana na kuwa kwake katika nafasi nzuri kwenye lango la Senegal, kilikuwa kikivuta biashara ya bonde hilo kuelekea Atlantiki, na hivyo, basi, kuvunja uhusiano wa kukamilishana uliokuwepo kwa miaka mingi baina ya Waberiberi wa Chamama na wakulima wakazi waliokuwa wakiishi kando kando ya

mto. Kwa hiyo, ukiritimba wa biashara wa Saint-Louis ukawanyima Wamoori siyo tu watumwa ambao walikuwa wakitumiwa kwa karne nyingi, lakini pia nafaka kutoka katika bonde ambalo lilikuwa likitumika kama ghala kuu ya kulishia nchi za Saheli kaskazini ya mto Senegal. Msukosuko huu wa uchumi ukazidisha uhasama wa kisiasa na kijamii baina ya wapiganaji wa Hasaniyya wenye asili ya Kiarabu, waliojulikana kama Banu Maghfar, na Warabiti wa Sanhaja, wenye asili ya Kiberiberi.

Jamii ya Kiberiberi ilijikuta imebanwa katikati kati ya vuguvugu la mapambano ya wapiganaji wa Kiarabu wa Hasaniyya yaliyokuwa yakielekea kusini na ukiritimba wa Saint-Louis ambao ulikuwa ukiikengeusha biashara ya bonde kwa manufaa yake. Nasir al-Din akaanzisha chama cha kidini kilichojengwa kwenye misingi ya Uislamu wa kisufii ili kuinusuru jamii ya Kiberiberi isisambaratike. Chama hiki kilijaribu kuweka sawa maisha ya kisiasa na kijamii kwa mujibu wa mafundisho ya sharia (sheria ya Kiislamu) katika ukamilifu wake wa tangu awali, kwa kukomesha mamlaka ya kujichukulia ya wapiganaji wa ki-Hasaniyya na kuanzisha serikali inayoongozwa na sharia za Kiislamu.

Kutangazwa kwa jihadi katika falme za bonde la mto kulichombezwa na sababu za kiuchumi na kidini, kutamalaki biashara ya nafaka na watumwa, kuwasilimisha watu na kutakasa uumini wa dini ya Kiislamu. Ushindi wa vita vitakatifu mwaka 1677 katika Waalo, Futa Toro, Kayor na Jolof ulisaidiwa sana na hali ya msukosuko iliyokuwako Senegambia kaskazini kutokana na biashara ya watumwa.

Mwanzoni kabisa chama cha Nasir al-Din kilipinga kuendelezwa kwa biashara ya watumwa na kikalaani vikali udhalimu wa wafalme walioshiriki katika uwindaji wa watumwa. Lakini upingaji huu haukuwa na maana ya kutaka kuzima utumwa uliokuwemo katika nchi hizo au biashara ya watumwa ya kiwango kidogo, zoezi ambalo lilikuwa likifanyika karne na karne na ambalo, likiwa katika kimia cha biashara ya kuvuka Sahara, lilikuwa halijawahi kuleta msukosuko mkubwa kama ilivyofanya biashara ya watumwa ya Atlantiki.

Uislamu, ambao ulitumika kama kisingizio cha vuguvugu la Warabiti, ulikuwa sasa unabadili sura yake. Badala ya kuwa dini ya tabaka la watu wachache wafanyabiashara na wafanyakazi katika majumba ya wafalme, ukaanza sasa kuwa chama cha upinzani kilichopendwa na wengi kilichokuwa kikipinga mamlaka ya kujitwalia ya koo-tawala na athari mbaya za biashara ya Atlantiki. Kikiwa hakikupingwa na Waislamu wenyeji, na kikiwa kinaungwa mkono na watu wengi, chama hiki kikaziondolea mbali, moja baada ya nyingine, koo-tawala za Futa Toro, Waalo, Kayor, na Jolof pasi na vipingamizi vikubwa. Baada ya kuzishinda falme hizo nne, Nasir al-Din akawaweka viongozi wa kidini kutawala badala ya koo-tawala zilizoangushwa, viongozi ambao waliendeleza azma yake. Huu ukawa ndio mwanzo wa ushindi wa tawala za Kiislamu katika eneo lote la kaskazini mwa Senegambia, kila utawala ukiwa na sifa zake maalumu.

Katika Futa Toro ushindi wa Warabiti ulipatikana kwa haraka na ulishirikisha umma katika mapambano ya kuangusha utawala wa *satiagi*. Katika Waalo, mtawala

(*brak*), Fara Kumba Mboji, alisimama imara kutetea ufalme wake, lakini alikufa vitani na Warabiti wakaweka *brak* kibaraka, Yerim Kode, aliyetokana na ukoo-tawala lakini ambaye alikubali masharti ya mfumo wa kidini uliowekwa na Nasir al-Din.

Katika Kayor chama cha Warabiti kilisaidiwa sana na machafuko ya kisiasa katika ukoo-tawala wenyewe. Mapokeo simulizi yanaelezea kwa undani jinsi chama, ilichokuwa kikiongozwa na *xaadi,* kilivyokuwa kikitetea na kuendeleza azma ya *linger*, Yaasin Bubu, ambaye alikuwa ameachishwa kazi na *damel* mpya. Yaasin Bubu akasilimu na kuwaingiza katika Uislamu pamoja naye baadhi ya *garmi* (tabaka la watawala) na wateja wake. Kisha akaolewa na Murabiti Njaay Sall ambaye, baada ya misukosuko, alijitangaza kuwa gavana wa jimbo hilo.

Lakini kifo cha Nasir al-Din katika mwaka 1674, katika vita dhidi ya wapiganaji wa Hasaniyya huko Mauritania, kilichochea kufifia kwa chama cha Warabiti. Kufifia huko kukawapa nafasi Wafaransa katika Saint-Louis kuingilia kati moja kwa moja na kuziunga mkono koo-tawala zilizokuwa zimeangushwa huko Futa Toro, Waalo, Kayor na Jolof. Wafaransa katika Saint-Louis walitaka kuzuia muungano wa kundi kubwa la kisiasa ambalo, chini ya mwavuli wa Uislamu, lingeweza kuwapa masharti ya ufanyaji biashara. Walitaka pia kurejea biashara ya watumwa ambayo ilikuwa muhimu sana katika mashamba ya Dunia Mpya.

Katika kiunzi cha maslahi yao wenyewe, Wafaransa wakamwunga mkono *brak* wa Waalo, Yerim Kode, ambaye aliachana mara moja na chama cha Warabiti, na ambaye alifanya kazi kubwa sana katika kukiangamiza chama hicho huko Futa Toro, Jolof na Kayor. Kutokana na hali hiyo, kufikia mwaka 1677 chama cha Warabiti kilikuwa takribani kimekwisha kusambaratika kabisa, na koo-tawala za zamani zikawa zimechukua tena mamlaka zake. Kushindwa kwa ukinzani huu wa kwanza wa umma dhidi ya biashara ya watumwa ya ng'ambo na mamlaka yasiyo na kanuni ya tawala zilizokuwepo kulikuwa na athari za muda mrefu katika maendeleo ya falme za Senegambia.

Katika Mauritania, mahali ambapo chama kilizaliwa, kushindwa kwa Warabiti kuliimarisha nguvu ya kisiasa ya wapiganaji wa Hasaniyya, ambao walianzisha utawala wa maamiri katika Trarza na Brakna. Katika karne ya kumi na nane, wakati maendeleo ya biashara ya sandarusi yalipoziwezesha kushiriki kwa manufaa katika biashara ya Atlantiki, nchi hizi za maamiri kila mara ziliweka shinikizo la kijeshi katika nchi zilizokuwa ukingo wa kushoto wa mto Senegal. Vita vya Warabiti – ambavyo vinajulikana kama vuguvugu la Tuben katika vyanzo vya Kizungu, na ambavyo pia vinajulikana kama Shurbuba katika tarihi za ki-Beriberi – vilikuwa na athari za kudumu zaidi kuliko zile za chama cha Wa-moravi ambacho kilianzia katika eneo hilo hilo mnamo karne ya kumi na moja.

Waberiberi wa Chamama, wakiwa wamevutiwa sana na biashara ya Atlantiki kuelekea bonde la Senegal, walishiriki kwa wingi katika siasa, uchumi na historia ya dini katika Senegambia. Wakati nchi za kiamiri za Trarza na Brakna zikijishughulisha na mahusiano yenye vurugu yaliyokuwa yamesambaa sana katika nchi za bonde la

Senegal, Warabiti wa ki-*zwauiya,* waliendelea kukuza mahusiano ya karibu zaidi na makundi ya Kirabiti yaliyokuwa yameanzishwa katika falme za Senegambia, na katika kufanya hivyo wakawa wanashiriki katika ukinzani wa Kiislamu dhidi ya tawala za kijeshi.

Vita hivi vya muda mrefu vya Warabiti vilisababisha mlolongo wa njaa katika eneo lote lililohusika, na zaidi ya yote, vilisababisha kunyamazishwa kwa Waislamu. Kushindwa kwao, kulikochangiwa na ushirikiano uliotolewa na koo-tawala - ambao ndio Waafrika pekee walionufaika na biashara ya Atlantiki - kwa maadui, kuliihakikishia Saint-Louis upanuzi zaidi wa shughuli zake za kibiashara. Kusambaratika kisiasa kulitokea kwa haraka sana katika maeneo haya kutokana na matatizo ya ndani na vita vilivyopiganwa baina ya falme mbalimbali kuhusu nani ahusike na biashara ya watumwa. Matumizi ya silaha (za moto) yakaenea na serikali za wachache zisizo na kanuni na zile za kijeshi zikashika hatamu katika falme zote. Uislamu sasa ukawa ndio kiini cha upinzani kwa tawala zote katika Senegambia.

Kuanzia kipindi hiki familia nyingi za Kirabiti zikaanza kuondoka katika maeneo ya pwani na bonde la Senegal na kukimbilia bara, hasa katika Bundu na Futa Jallon, ambako walifanya jitihada za kujenga umoja wa jamii za Kiisalmu zilizojitegemea. Mapinduzi ya Kiislamu mwanzoni mwa karne ya kumi na nane yakawa ndio mwanzo wa ushindi wa Uislamu wenye kutumia nguvu.

## *Athari za biashara ya watumwa ya ng'ambo: utawala wa* masedo *na mapinduzi ya Kiislamu katika karne ya kumi na nane*

Biashara ya Atlantiki, na hasa biashara ya watumwa, iliiongezea makali hali ya msukosuko iliyokuwemo katika nchi za Senegambia katika kipindi chote cha karne ya kumi na nane. Katika hali ya vurumai zilizokuwa zimeenea kote, koo-tawala za ki-sedo ziliimarisha tabia yake ya kishari na kulazimisha kuwepo kwa serikali unganifu za kifalme. Jamii za Kiislamu zilijibiza ukandamizaji huu wa utawala wa kifalme usiofuata kanuni wala sheria kwa kuanzisha vijisehemu vyao katika kila nchi, au kwa kupanga mapinduzi kama ilivyotokea huko Bundu, Futa Jallon na Futa Toro.

### Kuimarishwa kwa utawala wa *ki-sedo* na zahama za kisiasa

Falme za ki-Wolof za Kayor, Bawol na Waalo, na falme za ki-Sereer za Siin na Salum zilikumbwa na wimbi lile lile la kuimarishwa kwa utawala wa kifalme. Kayor, wakati wa utawala wa Lat Sukaabe Fall (1695-1720), ndiyo iliyokuwa mfano mzuri sana wa mageuzi ya utawala wa *ki-sedo* kuelekea utawala wa mtu mmoja. Lat Sukaabe Fall akaitumia vizuri nafasi ya hali ya wasi wasi iliyokuwapo Kayor na kuziunganisha falme za Bawol na Kayor chini ya cheo cha *damel-teen.* Akaanzisha ukiritimba wa kifalme juu ya unzaji wa watumwa na ununuzi wa bunduki, na akaimarisha utawala wa kifalme kwa kuyaondoa matawi ya kifalme ya Dorobe na

Gelowar kwa manufaa ya familia yake mwenyewe ya *meen* (ndugu wa kukeni), iliyojulikana kama Geej.

Akihofia hatari ya chama cha Warabiti, alianzisha mabadiliko ya kiasasi ili kuhakikisha kwamba Warabiti nao wanashirikishwa katika mfumo wa siasa. Akateua ma-*serin lamb* (watu waliopewa vyeo vipya) ambao aliwafanya mawakala wa serikali kuu waliokuwa na wajibu wa kulinda mipaka ya nchi na punde wakaanza kufuata taratibu za kijeshi zilizokuwa zikitumiwa na watawala wa ki-*sedo*. Walakini ma-*serin jakk* walikataa mapatano ya aina yoyote na watawala, na, wakiwa wameelekeza nguvu zao zote katika shughuli na mafundisho ya kidini, waliendelea kuwa kitovu cha malalamiko ya umma wa wakulima wadogo wadogo.

Utawala wa Lat Sukaabe Fall ndio unaohitimisha kujitokeza kwa malodi wa kivita katika falme za ki-Sereer. Lat Sukaabe Fall alijiweka mwenyewe, kwa kutumia ufundi wake wa kutatua mitafaruku ya siasa za ndani, kwa ajili ya manufaa yake, na pia kwa sababu ya ukiritimba wa kifalme juu ya uingizaji nchini wa bunduki. Akiwa sasa ni mtawala wa Kayor na Bawol, aliweza kutoa masharti katika vituo vya biashara vya Goree na katika viwanda vya Rufisque na Portudal, jambo ambalo liliathiri vibaya sana biashara ya Wafaransa. Lat Sukaabe Fall alipokufa Wafaransa wakaitumia nafasi ya mgogoro wa urithi wa ufalme kuhakikisha kwamba wanazuia kuungana tena kwa Kayor na Bawol chini ya mtawala mmoja.

Katika Waalo pia Wafaransa waliingilia kati mgogoro wa urithi kati ya familia za kifalme tatu - familia ya Tejek, familia ya Loggar na familia ya Joos. Hali hii ya kuingilia kati ilitokea wakati hali ya kiuchumi ilikuwa inabadilika kutokana na biashara ya gundi kuongezeka umuhimu. Wafaransa walikusudia kuivutia biashara hii katika viwanda vilivyokuwa ukingoni mwa mto Senegal, kwani vilikuwa vinapata ushindani mkubwa kutoka kwa viwanda vya Waholanzi na Waingereza vya Arguin na Portendick kwenye pwani ya Mauritania. Vita vya kwanza vya sandarusi kati ya 1717 na 1727 vilileta athari za kudumu, hasa juu ya maendeleo ya ufalme wa Waalo.

Baada ya safari ya kivita ya de la Rigaudiere ya mwaka 1723 kushindwa kuviteka tena viwanda vya Mauritania kutoka kwa Waholanzi, Brue, aliyekuwa afisa mwenye mamlaka Saint-Louis, akajaribu kufanya mapatano na *beecio* Malixuri, *kangam* (chifu wa jimbo) wa Roos beecio. Lengo la mapatano haya lilikuwa kumshawishi Alichandora, amiri wa Trarza, kuwapa tena Wafaransa ngome ya Arguin na pia kuwa msuluhishi katika uhasama ulioonyeshwa na *brak* wa Waalo na *damel* wa Kayor. Katika 1724 Malixuri, akiwa anaungwa mkono na Saint-Louis, akamuasi Yerim Mbanik, *brak* wa Waalo. Lakini baada ya usuluhishi kati ya Saint-Louis na Alichandora kutofanikiwa, hakupata kuungwa mkono na kampuni na akashindwa na *brak* Yerim Mbanik. Kufikia mwaka 1734, huyo aliyetajwa mwisho, ambaye alikuwa na jeshi zuri, alikwishakuwa mmoja kati ya wafalme wenye nguvu sana katika ukanda huo. Hali hii iliwawezesha warithi wake, ndugu zake wawili, Njaag Aram Bakar (1733-57) na hasa Naatago (1756-66), kueneza himaya yao juu ya falme nyingine za jirani, hasa Kayor, ufalme ambao ulikwishadhoofishwa na njaa na vita vya wenyewe

kwa wenyewe vya miaka saba.

Sera hii ya kutawala falme nyingine iliyokuwa ikifuatwa na Waalo ilikomeshwa na Waingereza, ambao walitamalaki Saint-Louis kuanzia mwaka 1758. Brak Naatago Aram, ambaye sasa alikuwa akidhibiti ushiriki katika biashara ya mto Senegal, kila mara alidai ongezeko la ushuru na la bei ya watumwa. Mnamo mwaka 1764 aliizuia mara mbili biashara ya Saint-Louis. Waingereza wakajibu mapigo kwa kumpa msaada *damel* wa Kayor, Makoddu Kumba Jaaring, ambaye alifanikiwa kurudisha sehemu kubwa ya nchi aliyokuwa amenyang'anywa na Waalo.

Gavana wa Kiingereza, O'Hara, akaitumia nafasi ya kifo cha Naago Aram hatimaye kuivunja kabisa nguvu ya Waalo. Nia yake kubwa ilikuwa ni kupata watumwa wengi kadri ilivyowezekana kutoka ukanda huu kwa ajili ya mashamba yake mwenyewe huko West Indies, na akatoa silaha kwa Wamoori ambao walienea eneo lote la mto Senegal. Katika mwaka 1775, katika ufalme wa Waalo peke yake, Waingereza walichukua zaidi ya watumwa 8000 katika kipindi cha chini ya miezi sita. Watumwa walipatikana kwa wingi kiasi cha mtumwa mmoja kuuzwa kwa kipande kimoja cha nguo katika mitaa ya Saint-Louis.

Unyonyaji huu wa nguvukazi ulitokea sawia na kuanza kwa vita vya wenyewe kwa wenyewe ambavyo vilidumu kwa takribani miaka ishirini na tisa, wakati ambapo koo mbili za kifalme, Loggar na Joos, zilijaribu kurejesha tena utawala wao uliokuwa chini ya ukiritimba wa ukoo wa Tejek tangu mwanzoni mwa karne ya kumi na nane. Lakini Waalo ilikuwa inapata shinikizo kutoka kwa Wamoori wa Trarza, ambao kila mara walikuwa wakiingilia kati katika migogoro ya kurithi na kusambaratisha kabisa nguvu ya ufalme ambao, kuanzia kipindi hicho, haukuweza tena kuwa na sera yake wenyewe.

Falme za Sereer za Siin na Salum zilipitia hatua zilezile zilizopitiwa na falme za Wolof. Hata hivyo, wakati Siin, ikiwa na eneo dogo tu, ilijaribu kujiondoa katika athari za nje, Salum, ikiwa na eneo kubwa zaidi na wakazi wa mjini, na ikiwa katika hali nzuri ya kibiashara kwenye mto Salum, ilishiriki katika biashara ya watumwa na ikapanuka kuelekea Gambia.

Futa Toro, chini ya utawala wa Kidenyanke tangu (enzi za) Koly Tengella, ilipitia katika hali sawa na ile ya falme za Kiwolof. Kutokuwepo kwa sheria makini zilizoelezea taratibu za kurithi ofisi ya *satiagi* kulishawishi kuanzishwa kwa vita kati ya watu mbalimbali waliodai kuwa walistahili kutawala. Mnamo mwaka 1716 Bubakar Sire aliomba msaada kutoka kwa Wamoroko, na hivyo kuwapa nafasi kuingilia mambo ya Futa Toro, ambayo kuanzia wakati huo ililazimika kulipa *muudal horma* (kodi iliyolipwa kwa nafaka). Aidha, Futa Toro ilishiriki katika mapambano baina ya Alichandora, amiri wa Trarza, na Brakua.

Katika mwaka 1720 Alichandora, akiwa amefukuzwa na jirani zake Waulad Bellum, ambao walimzidi nguvu, alitafuta msaada kutoka kwa sultani wa Moroko. Lakini majeshi ya Moroko (Waormani), baadaye yalijichukulia madaraka, yakazisakama nchi zote zilizokuwa kwenye ukingo wa mto Senegal kwa moto na

upanga. Majeshi hayo yakaishia kugawanyika katika makundi mawili, moja kati ya makundi hayo likaungana na Trarza na jingine likaungana na Brakna. Alichandora, akiwa ameshindwa mnamo mwaka 1722 katika mapambano baina yake na kundi lililoungana na Brakna, akakimbilia kwa *beecio* Malixuri huko Waalo. Kuanzia wakati huo na kuendelea, Waormani wakawa wanaingilia kati, mara kwa mara, katika migogoro ya kurithi ufalme katika Futa Toro wakati wa nusu ya kwanza ya karne ya kumi na nane. Kuanzia mwaka 1721 hadi 1724, kulikuwa na mkanganyiko mkubwa katika nchi hadi mtawala maarufu Samba Gelaajo Jeegi alipochukua mamlaka mnamo mwaka 1725, akisaidiwa na Waormani wa Gaidy na kamanda wa ngome ya St Joseph.

Samba Gelaajo Jeegi (1725-31) ndiye mfano asilia wa malodi wa kivita ambaye vitendo vyake vya kishujaa bado vinasheheni hekaya maarufu za mayeli wa Futa Toro. Alikuwa kiongozi wa *ki-sedo* wa kweli kweli ambaye, akiwa na jeshi la *sebbe* lililokuwa na silaha za moto, alipigana vita arobaini na tano katika kipindi cha utawala wake; vita ambavyo vilipambwa na sauti za *bawdi peyya yiyan* (ngoma za damu) na *dadde yiyan* (nyimbo za vita/nyimbo za damu).

Hekaya ya Samba Gelaajo Jeegi imejitokeza vizuri sana katika fasili mbili zilizochapishwa na Amadou Abel Sy. Utenzi wa *sedo* bado unatongolewa vizuri sana na ma-*sebbe* katika nyimbo zao za kivita, *gumbala* na *lenngi*. *Gumbala*, wimbo wa hamaki na ujasiri, ni utendi wa kifo ambamo *sedo* anaikubali takdiri yake kama mpiganaji shujaa, na kukiri uaminifu wake kwa mababu wake wa zamani waliokwisha kufa na kwa maadili ya tabaka lake. Nyimbo ziitwazo *Lenngi*, ambazo huimbwa na wanawake peke yao katika harusi au wakati wa kutahiri watoto, ni nyimbo za kishujaa ambazo huonyesha dharau juu ya kifo na kulinda heshima ya mtu. Lakini, kwa bahati mbaya, hekaya ya Samba Gelaajo Jeegi hurejelewa nje ya muktadha wake halisi wa kihistoria ambao ulijaa mapigano na biashara ya watumwa ya ng'ambo.

Mambo mawili yalisababisha hali hii ya vurugu za kudumu. Kwanza, Moroko, ikiwa na jeshi lake la Waormani, ilikusudia kuchukua mamlaka juu ya nchi za Kimoori zilizokuwa zikitawaliwa na maamiri na ambazo zilikuwa katika mzunguko wa biashara ya Atlantiki. Pili, kituo cha biashara cha Wafaransa cha Saint-Louis kilikuwa kikijishughulisha sana katika bonde lote la Senegal, nia ikiwa ni kujaribu kupata watumwa wengi katika eneo hilo kadri ilivyowezekana. Kwanza Samba Gelaajo Jeegi aliungana na Wamoori, lakini baadaye akatafuta mapatano na maadui zake wa zamani, Wafaransa, huko Saint-Louis, ili ajitoe katika nira ya Moroko. Katika mwaka 1725 akaiomba kampuni hiyo kumpa silaha na pia kumjengea bandari katika makao yake makuu, Jowol. Alidiriki hata kutetea maslahi ya Wafaransa yasitekwe nyara na Wamoori. Pengine urafiki huu ndio uliomwezesha kutawala bila kuingiliwa kati kuanzia mwaka 1725 hadi 1731, licha ya madai ya maadui wake wawili: Bubu Musa na Konko Bubu Musa.

Hata hivyo, kwa msaada wa *tunka* wa Gajaaga, Konko Bubu Musa aliweza kutwaa madaraka ya nchi hiyo. Baada ya kukaa ukimbizini Bundu, Samba

akaitamalaki nchi hiyo tena kati ya mwaka 1738 na 1741, lakini akabakia kuwa mfungwa wa marafiki zake Waormani na Wamoori, na akafa katika mazingira ya kutatanisha. Kwa mujibu wa mapokeo yaliyopo, alikufa kutokana na kusalitiwa na mke wake aliyehongwa na maadui zake wakati wa kipindi chake cha pili cha ukimbizi huko Bundu.

Mnamo mwaka 1752, *satiagi* mpya, Sube Njaay, naye aliondolewa madarakani na Yaye Hoola na wapiganaji wake shujaa ambao, wakisaidiwa na Xaaso na Waormani, waliishambulia na kuiteketeza Bundu. Futa Toro ikaonekana kudhoofu kupindukia, kwani ma-*satiagi* waliokuwa wakiondoana katika kinyang'anyiro cha urithi walijikuta wakiwanufaisha Wamoori pekee, ambao ndio waliomiliki uchumi. Hali sasa ilikuwa muafaka kwa mapinduzi ya Kiislamu, yaliyotokea mwaka 1776, kuweza kufanikiwa.

Upande wa juu wa mto, Gajaaga nayo pia ilikwishaingia katika mzunguko wa biashara ya Atlantiki tangu mwisho wa karne ya kumi na saba. Lakini pamoja na nguvu ya wafanyabiashara wa ki-Soninke, ambao ndio waliokuwa wakipelekea pindi la Niger chumvi na bidhaa kutoka Ulaya, na wakiipelekea Senegambia mashariki bidhaa za pamba, Gajaaga ilipata matatizo yaleyale ya kisiasa na kijamii yaliyohusiana na biashara ya watumwa na uvamizi wa Waormani. Msukosuko wa kisiasa ulianza kwenye miaka ya 1700 kwa mapambano baina ya *tunka* Naame wa Maxanna na binamu yake, Maxan wa Tambukane, na ukaendelezwa katika 1730 kwa vita baina ya Gey na Kammera. Mvutano ukazidi sana na kusababisha vita vya wenyewe kwa wenyewe kati ya mwaka 1744 na 1745; vita mbavyo hatimaye vilivunja umoja wa shirikisho la Soninke.

Hakuna mengi yanayojulikana kuhusu maendeleo ya ufalme wa Kaabu ambao ulimiliki Senegambia ya kusini hadi ulipopatikana ushindi wa mapinduzi ya Kiislamu katika Futa Jallon. Lakini nguvu ya Kaabu iliegemea sana kwenye biashara ya watumwa. Kwenye mwaka 1738 *mansa* wa Kaabu alikuwa akitoa watumwa 600 kwa mwaka kwa Wareno peke yao, wakati ambapo Mito ya Kusini iliyokuwa chini ya himaya ya Kaabunke ilikuwa ikisafirisha nje maelfu ya watumwa. Kaabu ikaimarisha nguvu yake juu ya majimbo ya pwani na wakati huo huo ikavamia na kushambulia jirani zake wa bara - Wabajaranke, Wafulakunda, Wakoniagui na Wabassari. Chini ya uongozi wa Biram Mansa, ambaye alifariki kama mwaka 1705, Kaabu ilionekana kuwa katika kilele cha nguvu yake, huku ikiongozwa na ufalme wa Kinanko. Lakini hapa napo mfarakano kati ya koo-tawala tatu, yaani Sama, Pakana na Jimara, ulikuwa chanzo cha vita kadhaa vya wenyewe kwa wenyewe. Hali hii ndiyo iliyosababisha kufanikiwa kwa vita vitakatifu ambavyo vilipiganwa baadaye kuanzia Futa Jallon na Bundu, na mapinduzi ya ndani kwa ndani ya Waislamu dhidi ya taifa la Kisoninke la Kaabu.

## Mapinduzi ya Kiislamu katika karne ya kumi na nane

Kushindwa kivita kwa harakati za Warabiti zilizoongozwa na Nasir al-Din katika nusu ya pili ya karne ya kumi na saba kulifuatiwa na kuenea kwa vitendo vya kichini

chini vya Kiislamu dhidi ya utawala wa ma-sedo na athari angamizi za biashara ya watumwa ya ng'ambo.

Katika nchi zilizokuwa chini ya mamlaka ya falme zenye nguvu kubwa za kijeshi, jamii za Kiislamu zilijiimarisha chini ya uongozi wa familia maarufu za Kirabiti. Zikiwa zimeunganishwa kupitia uhusiano wa kidini, kisiasa na kiuchumi, jamii hizo zikaanzisha harakati za ama kuanzisha mataifa mapya au kunyang'anya mamlaka ya utawala pale zilipokuwa kwa kutumia nguvu na kutangaza vita vitakatifu.

Hivyo basi, mwishoni mwa karne ya kumi na saba, Maalik Sy akaanzisha utawala wa Kiislamu wa Bundu, ambao ulifuatiwa, mwanzoni mwa karne ya kumi na nane, na mapinduzi ya Kiislamu katika Futa Jallon chini ya uongozi wa Karamokho Alfa. Sehemu ya pili ya karne ya kumi na nane ikashuhudia ushindi wa chama cha Warabiti wa Torodo kilichoongozwa na Sulayman Baal, huko Futa Toro, ambapo ndipo palipokuwa kiini cha utawala wa Denyanke. Mafanikio haya matatu yanaonyesha mwendelezo na mshikamano wa chama cha Warabiti katika Senegambia yote.

*Mapinduzi ya Kiislamu katika Bundu*

Kukandamizwa kwa Warabiti baada ya kifo cha Nasir al-Din kulisababisha uhamaji kwa wingi sana wa Waislamu kutoka Futa Toro kwenda Bundu, ambako Maalik Sy alianzisha utawala wa kwanza wa kidini kwenye mipaka ya Senegambia kwenye mwaka 1690.

Maalik Sy alikuwa mmojawapo wa kundi la watu waliopata mafunzo yao ya dini katika Pir au Kokki huko Kayor, nchi ambayo ilikuwa na uhusiano wa karibu na *zawiya* za Kiberiberi. Baada ya kusafiri kupitia Senegambia, hatimaye aliweka mastakimu katika mipaka ya Gajaaga kwa ruksa ya *tunka* wa Siaabu ambaye alimpa kipande cha ardhi. Maalik Sy akakaa katika eneo hili la kimji, akautumia vema udhaifu wa Gajaaga kutangaza vita vitakatifu. Kwa kutumia umaarufu wake wa kidini, na uwezo wake wa mipango ya kijeshi, akisaidiwa na Waislamu, wengi wao wakiwa ni wale waliokimbia kutoka Futa Toro, aliweza kuanzisha utawala wa kidini katika Bundu.

Maalik Sy aliwaunga mkono Warabiti wa Jaksanke, ambao maslahi yao ya kibiashara kila mara yalikuwa yakitishiwa na uporaji wa ukoo-tawala wa Gajaaga. Akajipa cheo cha *almamy*, ambayo ni fasuli ya Kifulfulde ya *al-Imam*, cheo ambacho hapo mwanzo kilikuwa kimechukuliwa na Nasir al-Din. Ingawa hakushiriki moja kwa moja katika vita vya Murabiti, lakini bado alifanikiwa kutekeleza baadhi ya malengo ya kisiasa na kidini ya chama cha Warabiti.

*Mapinduzi ya Kiislamu katika Futa Jallon*

Mafanikio ya mapinduzi ya Kiislamu katika Bundu yalifuatiwa, miaka michache baadaye, na mapinduzi ya aina hiyohiyo katika Futa Jallon. Majaaliwa ya milima mingi ya Futa Jallon, ambayo kwa muda wa karne kadhaa ilikuwa ni makimbilio ya Wajallonke, Wa-soso na Wafulbe, yakabadilishwa na uvamizi wa Koly Tengella, na zaidi ya yote, maendeleo ya biashara ya Atlantiki. Sehemu hii muhimu ya njia panda

ilihuishwa kiuchumi na kuwepo kwa makundi makubwa sana ya ng'ombe ambayo yalikuwa mali ya wachungaji wa Kifulbe waliokuwa wakimiminika katika eneo hili tangu karne ya kumi na tano kutokana na kuvutiwa na maeneo makubwa ya malisho ya mifugo yao katika nyanda za juu, na hatimaye wakawa kundi tajiri na lenye nguvu kuliko yote.

Mapinduzi ya Kiislamu hayakuwa kamwe vita vya kimbari baina ya wachungaji wa Kifulbe na wakulima wakazi wa Kijallonke kama ambavyo baadhi ya watu wamewahi kusema. Mapokeo yanaonyesha wazi kwamba mapinduzi haya yalikuwa yamejumuisha watu wa sehemu mbalimbali, mwanzoni wakiongozwa na Warabiti kumi na wawili wa Kifulbe na kumi wa Kimande, ambao bila shaka walikuwa wenye asili ya Kijaksanke. Kinyume chake, chama hicho kilipata upinzani kutoka kwa viongozi wa Kafu, ambao walikuwa Wajallonke, na pia kutoka kwa Wafulbe wasiokuwa Waislamu, ambao waliishi porini na ng'ombe wao. Wafulbe Waislamu, ambao walitaka kukomeshwa kwa kodi za ng'ombe, waliungana na Wamande wa Kijuula au Kijaksanke, ambao maisha yao ya biashara siku zote yalikuwa yakinasibishwa na Uislamu, kuunda kundi kubwa la kisiasa lililokuwa na uwezo wa kulinda usalama wa raia uliokuwa ukitiwa msukosuko na biashara ya watumwa ya ng'ambo. Ama kwa hakika chama cha Warabiti kiliimarishwa na kushiriki kwa Wafulbe wengi kiasi, ambao waliutumia utajiri wao wa ng'ombe kwa manufaa katika mazingira ya mabadiliko ya polepole kuelekea kwenye maisha ya makazi ya kudumu. Biashara katika ng'ombe na ngozi ikawapa nguvu ya kiuchumi wakati Uislamu uliwapa itikadi iliyohitajika katika kujenga utaratibu mpya wa kisiasa na kijamii.

Kwa hiyo basi, baada ya ushindi wa chama cha Warabiti katika vita vitakatifu dhidi ya koo-tawala kadhaa za Kijallonke, viongozi wa Kiislamu wakaanzisha Shirikisho la Futa Jallon, chini ya uongozi wa Ibrahima Sambegu, ambaye alijulikana kama Karamokho Alfa, mkuu wa nasaba ya Sediyanke ya familia ya Bari iliyokuwa huko Timbo, na ambaye alichukua cheo cha *almamy*. Shirikisho hilo liligawanywa katika *diwe* (umoja: *diwal* = jimbo) saba ambazo wakuu wake walijulikana kama *alfa* na walichaguliwa kutoka miongoni mwa wale walioshiriki katika ukombozi wa nchi. Tangu mwanzo mamlaka ya *almamy*, makao yake makuu yakiwa Timbo, yalipunguzwa kutokana na uhuru waliopewa wakuu wa majimbo, na pia kutokana na kuwepo baraza la wazee lililofanya kazi kama bunge huko Fugumba, makao makuu ya kidini.

Kwa hiyo utawala wa Kiislamu katika Futa Jallon ulikuwa ni matokeo ya mfululizo wa kampeni za kijeshi baina ya chama cha Warabiti na viongozi wa Jallonke Kafu. Baada ya vita maarufu vya Talansan, ambavyo vilikamilisha kabisa ushindi wa chama cha Wararabiti, vita vitakatifu viliendelezwa kwa kujaribu kuwasilimisha watu wote katika milima ya Futa Jallon ambao walikuwa hawajasilimu. Waislamu wakakabiliwa na upinzani kutoka kwa wachungaji wa Kifulbe, ambao walikuwa wakiishi maisha ya kinomadi karne na karne na hawakuipenda dini ya Kislamu, ambayo waliichukulia kuwa sawa na utamakani wa

mahali pamoja na njia ya kudhibitiwa kisiasa na kiuchumi. Hii yote inatuonyesha ni kwa nini chuki ilidumu kwa muda mrefu, na kwa nini utawala wa Kiislamu ulichukua muda mrefu kujiimarisha katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na nane.

Baada ya kifo cha Karamokho Alfa, mnamo mwaka 1751, *u-alimamy* ukachukuliwa na Ibrahima Sory, ambaye alijulikana kama Sory Mawdo (Sory Mkuu). Kwa hiyo kiongozi wa dini wa jihadi akafuatiwa na kamanda wa jeshi ambaye aliingiza Futa Jallon katika sera ya uchokozi dhidi ya nchi jirani. Kama ilivyo kuhusu ufalme wa Dahomey au shirikisho la Asante, kuinukia kwa Futa Jallon hakueleweki vizuri kukitazamwa nje ya muktadha wa biashara ya watumwa ya ng'ambo. Falme hizi ambazo mwanzoni zilianzishwa kama mbinu ya kujibu mapigo dhidi ya madhara yaliyotokana na uwindaji wa watumwa, nazo zikaishia kujiingiza katika biashara hiyo hiyo. Uislamu ukawa, basi, mojawapo kati ya itikadi nyingi zenye kulinda na kuimarisha mamlaka ya koo-tawala.

Kwa hiyo Ibrahima Sory Mawdo, akisaidiwa na kiongozi wa ufalme wa Jallonke wa Solimana, akajiingiza katika mfululizo wa vita dhidi ya majirani zake ili kuteka mali na watumwa. Lakini ushirika wao huo ulishindwa na Konde Burama, mfalme wa Sankaran, ambaye aliichukua Timbo, mnamo mwaka 1762. Ilibidi nguvu za nchi nzima zitumike kulizuia jeshi la Konde Burama kuingia katika malango ya Fugumba, na Ibrahima Sory hakuweza kumshinda mfalme wa Sankaran hadi mwaka 1776. Ushindi huo wa Ibrahima Sory ulimwezesha kuimarisha nguvu zake za utawala, na akaweka mamlaka ya kijeshi juu ya mamlaka ya kidini hadi kufa kwake mnamo mwaka 1791.

Kifo cha Sory Mawdo kilileta mkanganyiko mkubwa wa kisiasa. Ni kuanzia wakati huu ambapo mfumo wa kubadilishana utawala baina ya familia mbili ulipoanza; yaani baina ya familia ya Alfaya, nzao wa Karamokho Alfa, na familia ya Soriya, nzao wa Ibrahima Sory Mawdo. Utartibu huu wa kubadilishana utawala ulidhoofisha kwa kiasi kikubwa sana serikali kuu. Hata hivyo pamoja na udhaifu uliokuwemo katika mfumo wake wa siasa, ufalme wa Futa Jallon uliweza kuulinda uhuru wake hadi utamalaki wa wakoloni, na hata kuweza kupanua mipaka yake. Lakini utawala huo mpya ukapoteza tabia yake ya kimapinduzi iliyokuwepo hapo awali, kwani chama cha Warabiti kilijigeuza kuwa ukoo-tawala wa kijeshi na kidini na kushiriki kikamilifu katika biashara ya watumwa ya ng'ambo. Kama ilivyokuwa kwingineko, biashara ya watumwa ikawa ni ukiritimba wa serikali, ambayo sasa ilisimamia njia za biashara na kupanga misafara ya kwenda pwani. Uislamu sasa ukawa ni kisingizio tu cha kukamatia watumwa miongoni mwa wale wasiosilimu katika mipaka ya Futa Jallon. Wasiokuwa Waislamu, ambao walikamatwa kwa wingi sana, ama waliuzwa pwani au waliwekwa katika *runde* (vijiji vya watumwa). Ikiwa katikati ya mataifa ya Bambara na pwani, Futa Jallon ilishiriki katika kuvamia na kukamata watumwa au ilinunua watumwa kwa matumizi yake ya ndani, na ikauza waliosalia ili kupata bidhaa za kutoka Ulaya na chumvi iliyokuwa ikihitajika kwa ajili ya uchumi wake wa kichungaji. Katika karne za kumi na nane na kumi na tisa

biashara hii ikaleta, kutoka sehemu mbalimbali, watumwa wengi sana katika Futa Jallon: kutoka Bambara, kutoka Kisi, kutoka Jallonke, kutoka Fulbe, kutoka Bassari na kutoka Koniagui.

Historia ya ndani ya Futa Jallon ilijibainisha kwa kuunda jamii ya matabaka-msonge ikiwa imeegemea kwenye Uislamu kama itikadi ya mamlaka. Waislamu walikuwa na haki zote za watu huru wakati wale wasio Waislamu walikuwa katika tabaka la kitumwa katika jamii mpya iliyotawaliwa kwa kutumia sharia. Kutumiwa sana kwa lugha na utamaduni wa Kifulfulde kusigubike hali halisi ya mageuko ya ndani na maendeleo ambayo yalijidhihirisha katika kuwepo kwa matabaka bayana ya kijamii.

Mbali na tofauti ya msingi baina ya watu huru (*rimbe:* umoja: *dimo*), na watumwa (*maccube*), katika jamii kuu ya watu huru kulikuwa na utaratibu msonge wa daraja ambazo ziliakisi unyonyaji na kutokuwepo kwa usawa. Katika *rimbe*, juu kabisa kulikuwa na *las li* (makabaila wa upanga na mkuki, na makabaila wa kitabu na kalamu); hawa walikuwa ni vizazi vya familia za Warabiti maarufu waliopigana vita vitakatifu na kisha kuhodhi madaraka ya utawala. Kisha kulikuwa na idadi kubwa sana ya watu huru ambao hali zao ziliitegemea namna walivyohusiana na tabaka-tawala. Wakiwa kati ya watu huru waliokuwa katika tabaka la chini kabisa, Wafulbe, ambao walifanya ajizi sana katika kusilimu, walitegemea ng'ombe kama utajiri wao pekee na walilazimika kulipa kodi zisizokuwa na mwisho na ushuru wa kazi. Lakini maendeleo ya utumwa wa ndani, ambao uliwiana sana na biashara ya watumwa ya Atlantiki, ndiyo iliyokuwa sifa kuu na muhimu ya mageuzi yaliyotokea katika jamii za Senegambia katika karne ya kumi na nane.

Desturi ya utumwa wa nyumbani bila shaka ndiyo iliyokuwa kiini cha mapinduzi ya kitamaduni katika Futa Jallon ambapo Warabiti na tabaka la siasa, ambalo halikuhusishwa na kazi za kilimo, liliweza kujishughulisha na kufundisha elimu tu. Utawala mpya ulianzisha shule nyingi za Kurani nchini kote. Kuwepo kwa chama imara cha kisiasa na kijamii kilichofuata taratibu za sharia na kupiga marufuku kuuzwa kwa Waislamu kuliiwezesha Futa Jallon kuepaka utawala usiokuwa na serikali na kupunguka kwa watu. Kwa hiyo taifa hilo, ambalo liliongozwa kwa misingi ya kidini, likawa na kiwango fulani cha utulivu.

Haikuchukua muda mrefu Warabiti wakatafsiri Kurani katika Kifulfulde ili kurahisisha mafunzo ya kidini kwa umma. Matokeo yake hayakuwa tu wingi na utajiri mkubwa wa fasihi katika Kifulfulde, lakini pia kuoteshwa kwa mizizi ya Uislamu katika umma. Kutokana na hali hiyo, Uislamu wa miji kama Timbuktu na Jenne, kupitia mapinduzi ya Kiislamu katika Futa Jallon, ukawa ni Uislamu wa umma ambao ulichombeza kuanzishwa kwa msururu wa madola ya Kiislamu Afrika Magharibi kote.

*Mapinduzi ya Kiislamu katika Futa Toro*

Uislamu ulipata ushindi mkubwa sana katika Futa Toro katika nusu ya pili ya karne ya kumi na nane chini ya uongozi wa chama cha Warabiti wa Torodo kilichoongozwa

na Sulayman Baal na Abd al-Kadir. Hapa, pengine hata zaidi kuliko ilivyokuwa katika Bundu na Futa Jallon, kuna uhusiano wa wazi kati ya chama cha Torodo na chama cha Nasir al-Din katika karne ya kumi na saba. Hata hivyo, wakati huo huo chama cha Torodo, kikiwa kinafanya mambo yake kwa karibu sana na *zawiya* za Kimoori, kilitiwa moyo na nguvu kutokana na mafanikio ya jihadi katika Bundu na Futa Jallon.

Mgogoro wa urithi ulioanzishwa kwenye miaka ya 1716 na Bubakar Sire uliendelea katika kipindi chote cha karne ya kumi na nane, ukaiingiza Futa Toro katika misukosuko na vita vya wenyewe kwa wenyewe. Hali ilikuwa mbaya zaidi wakati gavana wa Kiingereza, O'Hara, aliposaidia jitihada za kuchukuliwa kwa Futa Toro na Wamoori wa ki-Brakna na ki-Trarza. Katika mazingira haya, mapinduzi ya Kitorodo hayakuelekezwa tu dhidi ya utawala wa Denyanke, lakini pia dhidi ya kutawaliwa na Brakna na kuuzwa kwa Waislamu kama watumwa. Chama cha Torodo, kikiongozwa na Sulayman Baal, kiliweza mara moja kushinda mapambano ya kijeshi dhidi ya Ulad Abdallah huko Mboya, na hivyo kuikomesha *muudul horma*. Baada ya kuanzisha madaraka yake katika Futa Toro kati, chama cha Torodo kikakomesha utawala wa karne nyingi wa Kidenyanke, na katika Julai 1776, kikapiga marufuku biashara yote ya Waingereza na Galanı, ikiwa ni kujibu mapigo ya madhara yaliyosababishwa na O'Hara katika kusaka watumwa.

Ushindi wa Torodo ulitokea wakati sawia na kifo cha kiongozi wake maarufu, Sulayman Baal. Mrithi wake, Abd al-Kadir, ambaye aliwahi kuchaguliwa kuwa *almamy*, akachukna taratibu nyingi za kisherehe kutoka Futa Jallon na wakati huo huo akishikilia baadhi ya mapokeo ya utawala wa Denyanke. Akagawa upya bayti (ardhi iliyokuwa haitumiki), wakati huo huo akithibitisha haki za familia maarufu za Kitorodo kwenye maeneo mengi ya Futa Toro ya kati. Familia tatu za 'Abe' - Bosseyabe, Yirlabe na Hebbyabe - ndizo zilizotoa wajumbe wengi wa *jaggorde* (Baraza la Wachaguzi). Juu ya hivyo, Abd al-Kadir aliimarisha utawala mpya na akapanua taathira zake za kidini nje ya mipaka ya Futa Toro. Mafanikio yake yakaleta matumaini makubwa ya mabadiliko na yakazidisha hali ya mvutano baina ya wanamapinduzi wa Kiislamu na matabaka-tawala ya ki-*sedo* ya Waalo, Jolof, Kayor na Bawol.

Mnamo mwaka 1786 utawala wa Kitorodo ukaanzisha mashambulizi ya kutamalaki Trarza, ambako Abd al-Kadir alikusudia kuingiza utawala wake na kutoza watu ushuru kama alivyokuwa amefanya katika Brakna. Aliishinda Trarza, ambayo amiri wake, Ely Kowri, aliuawa katika vita. Baada ya ushindi huu, Abd al-Kadir bila shaka akajitangaza kuwa Kamanda wa Waumini waaminifu, mrithi halali wa Nasir al-Din. Kwa hiyo azma yake ikawa ni kulazimisha sharia ya Kiislamu kwa watawala wa Waalo, Jolof na Kayor, na kupanua utawala wake hadi mto wa juu.

Lakini katika mwaka 1790 *damel* mpya wa Kayor, Amari Ngoone Ndeela, akaukana utii ambao mtangulizi wake alikuwa ameukubali kwa Abd al-Kadir, na akayazima kwa ukatili majaribio yote ya kutaka uhuru yaliyokuwa yamefanywa na

vikundi mbalimbali vya waongofu wa Kiislamu katika jimbo la Njambur. Kwa hiyo Abd al-Kadir akatayarisha safari kubwa ya kijeshi akikusudia kwenda kuiteka na kuitawala Kayor. Jaribio hili liliishia katika maangamizi makubwa katika Bungoy ambapo jeshi hilo kubwa lilishindwa vibaya kutokana na kutumiwa kwa mbinu ya "kuteketeza kila kitu kinachoweza kumsaidia adui" aliyoiandaa Amari Ngoone Ndeela. Wafutanke wengi waliuzwa kama watumwa na Abd al-Kadir akapelekwa Kayor ambako alifungiwa na baadaye kurudishwa Futa Toro.

Baada ya kushindwa Bungoy, mamlaka ya Abd al-Kadir yakaanza kufifia. Sasa akawa anashindana katika Futa Toro na wajumbe wawili maarufu wa *jaggorde.* Familia ya Kitorode maarufu na yenye nguvu ya Thierno Molle, ambayo ilichukia sana kung'ang'ania sana dini kwa kiongozi wa Kiislamu ilimlazimisha *almamy* kuondoka katika mji wake na kwenda Kobbilo, kwenye ardhi yake, na wakati huo huo watoto wawili mbumbumbu wa mfalme, Ali Sidi na Ali Dundu, wakajiweka kuwa ndio kiungo baina ya serikali kuu na majimbo ya Toro ya magharibi na mashariki.

Mvutano wa ndani wa madaraka ulitokea sawia na kutokea kwa uhasama baina ya Futa Toro na kituo cha biashara cha Saint-Louis; kituo ambacho biashara yake katika mto ilisimamishwa kati ya 1801 na 1803. Lakini mnamo mwaka 1806 mkataba uliokuwa ukiuthibitisha ule wa 1785 ulitiwa sahihi na pande zote mbili, kwani kusimamisha biashara kulikuwa kunaathiri vibaya pande zote.

Kisha Abd al-Kadir akafunga safari ya kwenda katika mto wa juu kukomesha uharibifu uliokuwa ukifanywa na *almamy* Sega na ambao uliwaathiri vibaya Warabiti wa Bundu. Akaamrisha Sega anyongwe na badala yake akamweka mtu wake Hammadi Pate, na hivyo kuchochea mapatano ya kirafiki baina ya Hammadi Aissata, mdai maarufu wa Bundu lakini ambaye hakufanikiwa, na mfalme wa Kaarta. Akiwa ameondolewa madarakani na *jaggorde,* Abd al-Kadir akaungana na Gajaaga na Xaaso, lakini aliuawa na makundi ya pamoja ya Bundu na Kaarta katika mwaka 1807, baada ya kusalitiwa na kizazi cha pili cha chama cha Torodo. Kifo chake kikatoa mwanya kwa ushindi wa *jaggorde*, ambao kuanzia wakati huo waliweka *almamy* ambaye alitetea azma zao na wakapata kiasi kikubwa cha uhuru katika maeneo yao ya uchifu. Kama ilivyokuwa katika Bundu na Futa Jallon, chama cha Warabiti, ambacho mwanzoni kilikuwa cha wasomi, kikauacha mfumo wote wa siasa mikononi mwa watawala wapiganaji ambao hawakuwa na elimu yoyote ya dini.

Kushindwa kwa Abd al-Kadir kulazimisha matumizi ya Uislamu kama itikadi ya dola katika ufalme wa Wolof kulifidiwa kwa kiasi kikubwa na maendeleo ya kutosha yaliyotokea katika vyama vya ndani vya Warabiti. Waislamu wengi walijaribu kuzisai vurumai za ki-*sedo* zilizokuwemo ndani ya nchi. Hasa huko Kayor, kushindwa kulikotokea Bungoy kulisababisha kuhama kwa makundi makubwa ya Waislamu kutoka Njambur na kukimbilia ghuba ya Rasi ya Verde ambako walisaidia kuanzishwa kwa utawala wa kidini ulioongozwa na Jal Joop. Kutoka pale wakachochea upinzani wa Lebu na kuunga mkono vuguvugu la kujitenga la Kayor.

Baada ya miaka kadhaa ya upinzani, chama cha Warabiti kikapata uhuru wake – tukio la kwanza la kumeguka kwa ufalme wa Kayor.

## *Hitimisho*

Mageuzi ya Senegambia kuanzia karne ya kumi na sita hadi karne ya kumi na nane yaliathiriwa, kwa kiasi kikubwa, na nguvu iliyotokana na biashara ya Atlantiki ambayo iliifanya Afrika ya watu weusi kuwa katika utegemezi wa mataifa ya Ulaya yaliyokuwa na nguvu za kiuchumi. Katika kipindi hiki shirikisho la Jolof lilisamabaratika na likatoa mwanya wa kujengwa falme za Waalo, Kayor, Bawol, Siin na Salum, na wakati huo huo ufalme wa Denyanke ukawa ndio utawala wenye nguvu katika bonde la Senegal. Katika Mito ya Kusini, biashara ya Wareno iliharibu biashara ya kikanda na kusababisha kuanzishwa kwa utawala wa kijeshi katika Kaabu, ambao ulichukua nafasi ya dola la Mali ambalo lililokuwa linaporomoka.

Katika karne ya kumi na saba, kushamiri kwa biashara ya watumwa katika mabadilishano ya biashara ya nje kulisababisha kugawanywa kwa pwani katika maeneo ya miliki, na kujengwa kwa ngome katika vituo vya kufanyia biashara. Biashara ya watumwa iliimarisha tabia ya ukali ya utawala wa ki-*sedo* ambayo nayo ilisababisha kuenea kwa vyama vya Kirabiti ambavyo vilipingana sana na koo-tawala za kijeshi. Baada ya kushindwa kwa chama cha Nasir al-Din (1673-7), wale walioshikilia Uislamu wa kimapambano walijiunga pamoja katika Bundu, Futa Jallon na Futa Toro.

Hata hivyo, mwishoni mwa karne ya kumi na nane mataifa ya Kiislamu taratibu yalianza kupoteza ari yake ya kimapinduzi wakati tu Ulaya ilikuwa imeanza kufikiria kupiga marufuku biashara ya watumwa ambayo nafasi yake katika kulimbikiza mtaji wa fedha ilikuwa inaanza kupotea. Kisha Ulaya ikaanza kuiingiza Senegambia katika mfumo wa kibepari na kuitumia kama kituo cha moja kwa moja cha pambizoni cha kupatia mali ghafi kwa ajili ya viwanda vyake. Senegambia, ikiwa tayari imeathirika vibaya sana kutokana na misukosuko mikubwa ya enzi za wasaka watumwa, haikuwa na uwezo wa kuzuia utamalaki wa kijeshi ulioanzishwa na Ulaya katika nusu ya pili ya karne ya kumi na tisa.

# 11 Mwisho wa himaya ya Songhai

## *Kuanguka kwa dola la Songhai*

### Sababu za uvamizi wa Moroko

Mawlay Ahmad al-Mansur aliporithi kiti cha enzi cha Sa'adi baada ya vita vya Wadi al-Makhazin, ushindi wake dhidi ya Ureno ulimweka miongoni mwa watetezi wakuu wa Uislamu; aidha fedha aliyolipwa kufidia mateka wake wa Kikristo ilimfanya awe mmojawapo wa watu mashuhuri sana katika ulimwenguni.

Akiwa sasa ni Khalifa, Imam na Mtawala wa Waumini, azma yake ikawa ni kuwaunganisha Waislamu wote katika namna moja ya kuutazama ulimwengu na kuyahuisha mapokeo ya jihadi. Kwa sababu hiyo, faida aliyopanga kuipata kutokana na mashapo ya chumvi katika Taghaza huko Sahara ilikuwa itumike kuutunisha tena mfuko wa Bayt al-Mal (Hazina); aidha watumwa ambao wangepatikana katika utamalaki wa Songhai wangetumikia jeshi la majini ambalo ndilo lingetumika kwenda kuwashambulia wasioamini.

Lakini azma hizi za juu sana na za kufikirika hazikuacha kando zile zilizokuwa za dhahiri na yakini zaidi - zile za kupata dhahabu na watumwa huko Sudani. Watumwa walihitajika katika kiwanda cha sukari huko Moroko kusini. Ama kuhusu dhahabu ya Sudani, kiwango cha upatikanaji wake kilikuwa kimeshuka kwa haraka sana tangu kuinukia kwa dola la Songhai katika Pindi la Niger

Isitoshe, biashara kati ya Moroko na Sudani bado ilikuwa ikitishiwa na Wareno, ambao mnamo mwaka 1565 walijaribu kufika Timbuktu kupitia Senegal, na Waturuki, ambao baadhi yao nyendo zao ziliashiria kwamba walikuwa wakijaribu kupanua maeneo yao ya kufanyia biashara kuelekea Maghrib kusini. Mwisho, mategemeo ya Sa'adi yaliyokuwa yameelekezwa Taghaz yalififia, kwani Wasonghai walianzisha mashapo mengine ya chumvi huko Taghaza al-Ghizlan (Taudeni).

Mnamo mwaka 1582 al-Mansur alizitwaa oasisi za Tuwat na Gurara. Kutekwa huku rasmi kwa oasisi kulielezwa kuwa ni hatua ya kujaribu kurejesha amani na utulivu, lakini kwa kweli ulikuwa ndio mwanzo wa kuitamalaki Sudani.

Katika mwaka 1583 mfalme wa Borno, May Idris Alaoma, akampa al-Mansur mwanya, ambao hakuwa ameutegemea, wa kutekelezea azma zake. Akiwa anaogopa

kuingia kwa Waturuki katika miliki yake, kutokea Fezzan, May Idris Alaoma alimwomba al-Mansur amsaidie kupigana na makundi ya watu wasiokuwa Waislamu "katika mipaka ya Sudani." Mtawala huyo wa Moroko akakubali baada ya kupata *bay'a* (hati ya utii) kama sharti la msaada wake. Mwaka uliofuata kikundi cha msafara wa uchunguzi cha Moroko kiliingia Saheli ya Atlantiki katika uelekeo wa Senegal, lakini kililazimika kurudi nyuma katika mazingira ambayo hayaeleweki.

Amri ya kulishambulia dola la Songhai ilikuwa karibu itolewe mnamo mwaka 1586, lakini kutokana na matatizo ya utekelezaji wa amri hiyo yaliyojiri, al-Mansur akajipa miaka mingine michache ili aweze kuimarisha jeshi lake, kupata habari zote ambazo zingeweza kupatikana juu ya dola la Askiya, na mwishowe kuweza kuwashawishi wananchi wake muhimu juu ya uthabiti wa mpango huo.

## Tondibi na sababu za kuanguka kwa Songhai


Tarehe 30 Oktoba, 1590 kundi kubwa la jeshi la Moroko liliondoka Marrakesh chini ya uongozi wa Judar Pasha. Likavuka Atlas ya Juu (High Atlas), likaeuda kupitia bonde la Da'ra, hadi Ktawa ambako liliingia Sahara. Tarehe 1 Machi, 1591, baada ya kulazimika kutembea kwa miguu kwa muda wa siku sitini, jeshi hilo la Moroko likafika kwenye kingo za Mto Niger; na siku kumi na moja baadaye likafika Tondibi, kiasi kama kilometa hamsini hivi toka Gao, mji mkuu wa Songhai.

Askiya Ishak II akakusanya na kutayarisha askari wake, ingawa kwa kuchelewa. Pamoja na hivyo, aliwakabili wavamizi kwa nguvu kubwa, lakini kutokana na nguvu za bunduki za Moroko, majeshi ya Songhai yalivunjiliwa mbali baada ya upinzani wa kishujaa wa siku moja. Na hivyo, basi, likaanguka dola kuu la mwisho la Saheli, ambalo watawala wake, wakiwa wamezamia katika magomvi yao ya ndani, hawakuweza kutambua ukubwa wa tishio la Moroko

Tangu kuanguka kwa askiya mkuu, Muhammad al-Haji, mnamo mwaka 1529, ikulu ya mfalme katika Gao ilikuwa imebakia kuwa jukwaa la mapambano makali kati ya watu mbalimbali waliodai kuwa na haki ya kutawala. Miaka miwili kabla ya kuvamiwa na Moroko kimsingi dola la Songhai ilikwishagawanyika katika madola mawili kutokana na maasi ya *balama* al-Sadduk, ambaye makao yake makuu yalikuwa Timbuktu. Ishak II aliweza kuyazima maasi hayo lakini hakupata muda wa kutosha wa kuiunganisha tena nchi.

Kiuchumi, kwa miongo kadhaa Songhai ilikuwa katika matatizo makubwa kutokana na athari mbaya za biashara ya Wareno huko pwani. Aidha matatizo ya kivita katika Dendi, Borgu na nchi ya Mossi, pamoja na kuipoteza Taghaza kalika mwaka 1585, viliyaongezea makali matatizo ya kiuchumi na kijamii.

Mwisho, dola hilo, ambalo lilijengwa na Sonni Ali na *askiya* Muhammad, ilikuwa limetanda katika eneo kubwa sana lakini lilikosa kiunzi cha kitaifa na kijamii-kitamaduni ambacho kingeweza kulipa umoja wa kweli. Ajabu ni kwamba kiini cha mvutano katika dola hilo hakikuwa Gao, mji mkuu wa kisiasa, wala hakikuwa katika bara ya Songhai, bali kilikuwa katika sehemu iliyotamalakiwa ya Timbuktu na Jenne.



**11.1** *Kijiji cha Songhany*

## Kuanzishwa kwa utawala wa Moroko wa ki-pasha

Katika kufuatilia mabaki ya jeshi la Songai, Judar Pasha alikwenda hadi Gao, mji ambao ulikwishakimbiwa na wakazi wake. Ishak II hakufanya jaribio lolote la kujibu mapigo na badala yake akapendelea kufanya makubaliano na Judar juu ya masharti yake ya kurudi Moroko. Pasha huyo wa Moroko akiwa amekatishwa tamaa na hali ya kusikitisha ya Gao, na akiwa anajua wazi kwamba watu wake mwenyewe walikuwa katika hali mbaya, alikuwa tayari kukubali mapendekezo ya *askiya,* lakini al-Mansur hakukubaliana na mapendekezo hayo. Alimwita nyumbani Judar na badala yake akampeleka afisa wa pili wa juu katika jeshi la Moroko, Mahmud b. Zarkun, ambaye alipewa kazi ya kuitamalaki Sudani yote.

Mahmud Pasha akaazimia kuivunjavunja nguvu ya kisiasa ya Songhai. Akauteka mji mkuu wa zamani wa Kukya, akamfukuza Ishak II nchini, na akamwekea mtego wa kumwangamiza kabisa Muhammad-Gao, ambaye aliteuliwa kuchukua nafasi ya Ishak II, na kisha akafanya mipango ya kuondoa kabisa mabaki ya mwisho ya upinzani wa Kisonghai katika Dendi (1592-94). Baada ya hapo Zarkun akarudi Timbuktu kuyavunja kabisa matabaka ya wasomi ambao ndio waliokuwa nguvu ya kisiasa: makumi kadhaa ya ma-ulama ama wakachinjwa au wakapelekwa ukimbizini Moroko.

Mahmud Zarkun aliuawa mwaka 1594 katika uvamizi uliofanywa na upinzani wa ki-Songhai, na kazi ya kuendeleza utamalaki wa eneo hilo ukawekwa tena mikononi mwa Judar. Hii ikaonekana wazi kuwa kazi ngumu na isiyowezekana mbele ya upinzani mkubwa kutoka kwa Wafulbe, Wabambara, Wamande, wote ambao walimzunguka *mansa* Mahmud. Yakafanywa makubaliano ya kusitisha mapambano kwa muda kungojea maamuzi baina ya Wamoroko waliopandikizwa katika Jenne na wenyeji wa eneo hilo, ambao walikubali, ingawa "kwa maneno tu" kukaliwa kwa sehemu yao na watu wa Moroko.

Askari wa al-Mansur walilazimika kubakia katika bandari za mto ili kuzimiliki kikamilifu, na huko waliweka *kasaba* (ngome za majeshi). Wengi wao walikuwa katika mwambao wa mto kuanzia Jenne hadi Timbuktu, na wakati huo huo kwenye kingo zote mbili za Niger kulikwa na maeneo makubwa sana ambayo takriban hayakuguswa na athari za Moroko.

Ma-pasha hawakujaribu kubadilisha utawala wa kienyeji. Hata hivyo kila chifu wa wenyeji alipochaguliwa ilibidi athibitishwe na *pasha*, ambaye pia ndiye aliyewatawaza ma-*kadii* (makadhi) na ma-*imam* (maimamu) katika miji mikubwa na katika *ardo* za Fulbe na *amenokal* za Tuareg. Wawakilishi wa Moroko, kama walivyokuwa ma-*askiya* kabla yao, mara chache sana waliingilia kati uchaguzi wa wagombea.

Ngome za kijeshi za Kimoroko hazikuwa zimejitenga peke yake tu: hawakuwa wakiishi katika kambi za upeke au katika kambi zilizozungushiwa ngome. Al-Mansur aliamini kabisa kwamba utamalaki wa eneo hilo ungekuwa wa muda mfupi kama usuluhishi usingefuatiwa na kulifanya eneo hilo kuwa koloni na kukaliwa na watu kutoka Maghrib ambao wangeweza kufanya makazi ya kudumu pale. Kwa hiyo basi, Sudani ikashuhudia majilio ya watu wa Guish kutoka Sus na wa Haha pamoja na makundi madogo ya Ma'kil na Jusham ambao al-Mansur alitaka sana kuwaondoa. Kuanzia 1599

na kuendelea wanajeshi wenye asili ya Kikristo ambao walikuwa wamekuja na Judar walirudishwa Moroko.

## *Siasa za Sudani kufikia mwisho wa karne ya kumi na nane*

### Uzoefu wa watu wa Pindi la Niger baada ya ubeberu: sifa za jumla

Katika hali ya kutokuwa na hakika na kutokuwa salama iliyotokana na kuanguka kwa dola la Songhai, nguvu za kisiasa zilikuwa mikononi mwa wale tu walioweza kuwatetea na kuwalinda watu wao. Mataifa katili ya zamani yalichukuliwa nafasi yake na msururu wa falme ndogondogo na tawala ndogondogo za viwango vya kabila, ukoo, mji au hata vijiji kadhaa.

Kiongozi wa siasa alikuwa, kwanza kabisa, mpiganaji shujaa ambaye alifuata zaidi mapokeo ya jadi na siyo maadili ya kilimwengu yaliyoenezwa na wasomi wa Kiislamu. Uislamu, ambao ulikuwa umetoa mchango mkubwa sana katika ujenzi wa madola ya Kisudani, sasa kwa muda, ukawa hauna umuhimu mkubwa kisiasa, ila uliendelea kuenezwa mbali zaidi na wafanyabiashara wa Jula ambao walipita njia za biashara kuanzia Saheli hadi kwenye msitu.

### Timbuktu, Jenne na Arma

Baada ya mwaka 1618 Moroko ikaacha kuteua maafisa wa ngazi za juu wa tawala za ki-pasha au kupeleka askari zaidi wa kivita, na watu wa mwisho mwisho wa jeshi la al-Mansur, na vizazi vyao, Waarma, waliachiwa waangalie mustakabali wao wenyewe. Wakabakia kuwa mabwana halali wa eneo la Timbuktu hadi mwanzo wa karne ya kumi na tisa.

Ingawa nguvu zake za kijeshi zilipunguzwa sana, taifa hilo la ki-pasha lilithibitika kuwa madhubuti sana na lilibakia na takribani miundo yake yote hadi majilio ya Shykhu Ahmadu. Ambavyo, kabla ya kuanzishwa kwa dola la Kifulbe la Masina, kulikuwa na majeshi katika Pindi la Niger ambayo yalikuwa na uwezo wa kuondoa kabisa mabaki yote ya koloni la zamani la Moroko. Kulikuwa na Wabambara wa Segu, mashirikisho yenye nguvu ya Watuareg ya Kel-Awllimiden, na zaidi ya yote Kel-Tadmekket, ambao, pamoja na ushindi wao mkubwa sana juu ya Waarma katika mwaka 1737, hawakufikiria kamwe kuchukua madaraka katika Timbuktu. Halikadhalika Wakunta waliingia tu Timbuktu katika mkesha wa kutamalakiwa kwake na Wafulbe katika 1825-6.

Inaelekea mwanzoni hapakuwa na kanuni zozote maalumu zilizofuatwa katika kuwateua viongozi wa ofisi mbalimbali katika utawala wa pasha, ikiwa ni pamoja na cheo cha pasha chenyewe. Lakini kuanzia katikati ya karne ya kumi na saba, wakati kizazi cha kwanza cha Waarma waliozaliwa humo humo nchini kiliposhika madaraka, kanuni za kurithishana mamlaka zikaanza kujitokeza, zikiwa zimeegemezwa katika mzunguko wa kubadilishana ofisi muhimu kati ya Divisheni kuu tatu ambazo Waarma wote walikuwa sehemu yake.

Mfumo huu ukasababisha kuwepo kwa vipindi fulani fulani ambapo hapakuwa na mtawala kwa sababu alikuwa hajachaguliwa au kukawa na vipindi vya utawala vifupi

vifupi. Isitoshe, kwa kuwa watu wale wale walichaguliwa kuongoza zaidi ya mara moja, idadi kubwa ya familia au nasaha kuu ikaanza kujitokeza, ikijihainisha kutoka kwa jamii nyingine ya Arma kwa sababu ya nguvu zao za kisiasa na uwezo wao wa kiuchumi. Kutokana na hali hiyo, kukaibuka "ıahaka-ıawala" ambalo limeelezwa katika tarihi kama "tabaka la machifu."

Kati ya 1646 na 1825 ma-pasha 145 walichaguliwa katika Timbuktu. Wengi wao walitokana na zile nasaba tatu za Tazarkini, Mubarak al-Dar'i na al-Za'ri. Pasha Mansur b. Mas'ud al-Za'ri alitokana na nasaba iliyotajwa mwisho. Alichukua utawala kwa nguvu mnamo mwaka 1716 na akaiingiza Timbuktu katika utawala wa kutisha. Mnamo mwaka 1719 wananchi wakasimama kidete dhidi yake na wakamfukuza na *legha* (vibaraka) wake kutoka mjini na wakarejesha mfumo wa kisiasa wa Kiarma wa zamani na misukosuko yake isiyokwisha.

Katika mwaka 1766 Waarma walimchagua Ba-Haddu b. Abu-Bakr al-Dar'i kuwa pasha; naye akafanya maajabu kwa kukaa katika kiti kwa miaka minane, lakini baada ya kifo chake mji ukakaa bila pasha kwa miaka kumi na minane. Katika mwaka 1794, baada ya Divisheni kuu kukubaliana kuhusu mtu wa kumteua, al-Mustafa al-Tazarkini alichaguliwa kuwa pasha, naye akarejesha vyeo vyote vya utawala wa ki-pasha vilivyokuwepo hapo awali. Katika utawala wa mrithi wake, Abu Bakri b. Ahmad al-Dar'i, ofisi ya pasha ikawa ya kurithiwa, na wanaye wawili, Muhammad na Uthman wakamrithi. Ka'id Uthman ndiye aliyekuwa pasha wa mwisho wa Timbuktu.

Hadi kufikia mwisho wa karne ya kumi na saba utawala wa ki-pasha ulikwishaanza kugawanyika katika makundi ambayo kwa kiasi fulani yalikuwa yakijitegemea chini ya *kasaba* kuu za Gao, Bamba, Timbuktu na Jenne. Wakati wakiendelea kuitambua serikali kuu ya Timbuktu, kila boma lilichagua viongozi wake kama walivyopenda wenyewe.

Boma la Jenne nalo lilikuwa na uhuru kama *kasaba* nyingine, kasoro tu wakati ambapo pasha fulani aliyekuwa jasiri na hodari alipochukua madaraka katika Timbuktu, kama ilivyotokea katika mwaka 1767, wakati pasha Ba-Haddu mwenyewe alipomchagua gavana mpya wa Jenne. Mahusiano ya kibiashara na kisiasa kati ya Timbuktu na Jenne kamwe hayakuingiliwa kati, na *kasaba* hizo mbili kila mara zilisaidiana.

Lakini mnamo mwaka 1796 Mskoti Mungo Park, akiwa Segu, aliambiwa rasmi kwamba Jenne ilistahili kuwa chini ya ufalme wa Bambara, ingawa ilikuwa ikitawaliwa na Wamoori. Je, tuseme kwamba Jenne ilikuwa "chini ya ulinzi" wa Bambara?. Vyanzo vya humo humo nchini vinaelekea kuunga mkono maoni ya Rene Caillie kwamba Jenne iliishi peke yake na ikiwa huru hadi hapo ilipotamalakiwa na Wafulbe wa Masina katika mwaka 1818-9.

## Wasonghai wa Dendi

Baada ya kufukuzwa Gao na kupoteza wafalme wawili na makumi kadhaa ya familia ya kifalme katika miezi michache tu, Wasonghai, wakiongozwa na *askiya* Nuh, waliweza kuwazuia Wamoroko wasiingie Dendi. Wakitumia mbinu ya kuvizia, waliyafukuza majeshi ya Zarkun, na yeye mwenyewe akauawa huko Bandiagara. Mrithi wake Mansur b. Abd al-Rahman (1595-6) akawafanya Wasonghai wajutie ushindi wao. Akiwa

ameshindwa na amelazimika kuwaacha baadhi ya watu wake mikononi mwa Wamoroko, Nuh akakimbilia Dendi; wakati huo huo Wamoroko wakamteua *askiya* mwingine kuwaongoza Wasonghai, naye akabakia chini ya utawala wao.

Wasonghai wa Dendi wakagawanyika katika falme ndogo ndogo nyingi, ingawa walifanikiwa kuudumisha umoja wao hadi katikati ya karne ya kumi na saba. Katika mwaka 1630 wakawekeana mkataba wa amani na Wamoroko, ambao kuanzia wakati huo walianza kuingilia mambo yao ya ndani na kuwa waamuzi katika migogoro ya urithi. Hata hivyo walikuwa na uhuru wao hadi kufikia mwanzo wa karne ya kumi na tisa, pamoja na shinikizo kubwa walilopata kutoka kwa Wafulbe, Watuareg Wanomadi, Waliptako na Waair.

## Falme za Wabambara za Segu na Kaarta

Baada ya kusambaratika kwa mipaka ya magharibi ya Songhai, wakulima wa Kibambara kwenye mto Niger wakawa sasa wamebaki wazi na katika hatari ya kuweza kushambuliwa na uvamizi wa Wafulbe na Waarma. Wakiwa wamegawanyika katika kufu kadhaa ambazo viongozi wake wa Kimarka na Kiislamu walikuwa na mahusiano mazuri na Jenne na Timbuktu, wakaomba ulinzi kutoka kwa vyama vya wawindaji wa jadi au koo ambazo zilikuwa na utaalamu wa kivita.

Katikati ya karne ya kumi na saba Wabambara wakafanya maasi dhidi ya viongozi wao wa Kimarka, na yawezekana ni katika wakati huu huu ambapo ukoo wa Kulibali ulipojidhihirisha; baadaye ukoo huo ulikuja kuanzisha falme za Segu na Kaarta.

Katika Segu, Biton Kulibali (t.1710 - t.1755), akisaidiwa na ma-*ton-dyon* (mateka au mateka wa zamani) wake, kwenye mwaka wa 1739 akaingiza kwa nguvu mamlaka yake, lakini kabla hata hajaweza kujiimarisha vizuri ufalme wake ukashambuliwa na Wajuula wa Kong, ambao walikaa nchini hadi mwaka 1745. Akiwa sasa amedhoofishwa, Biton Kulibali akatumia sehemu ya maisha yake iliyobaki akijaribu kuimarisha ufalme wake kwa kuondoa ushindani kutoka kwa watoto wa ndugu yake, Wa-Masa-si, ambao waliishi kaskazini mashariki ya Segu katika jimbo la Murdia. Mwaka 1753-4 aliwavamia kwa vita katika nchi yao, akawashinda na kumteka kiongozi wao. Kutokana na kushindwa huku wa Wa-Masa-si, wakiongozwa na Sebamana, wakaondoka kwenda Kaarta ambako walianzisha utawala wao.

Baada ya kifo cha Biton, ufalme wa Segu ukapitia kipindi kirefu pasipo utawala, kipindi ambacho kiliisha tu mwaka 1766 wakati ilipoibuka nasaba-tawala mpya iliyoanzishwa na Ngolo Diarra. Yaelekea mahusiano mazuri sana yaliyokuwepo kati yake na Wa-Azawad Kunta na kiongozi wao shaykh al-Mukhtar, yalimfanya awe na hadhari kubwa sana na Timbuktu.

Ngolo alirithiwa na mwanae Monzon (t.1789-1808), ambaye hasa ndiye aliyeujenga sawa sawa ufalme wa Segu. Kama Biton Kulibali, alilazimika kukabiliana na uadui kutoka kwa Wa-Masa-si, ambao waliteka Nyamina kwenye mto Niger, na hivyo basi, kuinyang'anya Segu mojawapo ya njia muhimu sana za kupitishia bidhaa. Jibu la Monzon lilikuwa balaa kubwa: baada ya kuikomboa Nyamina, aliendelea hadi Kaarta, akauteka mji wake mkuu, Guemu, na akamlazimisha mfalme wa Wa-Masa-si

kukimbilia Guidimakha. Kisha Monzon akashambulia Wamoori wa Awlad M'Bark, katika jimbo la Nyoro, ambao walikuwa wamekataa kumsaidia katika vita vyake dhidi ya Kaarta.

Monzon alikufa katika mwaka 1808, akafuatiwa, miaka mitatu baadaye, na Shaykh al-Mukhtar. Baada ya vifo vya viongozi hawa wawili, Pindi la Niger likapitia kipindi cha matatizo hadi majilio ya Shaykhu Ahmadu; matatizo ambayo kusema kweli yalisababishwa na majeshi ya Wafulbe na Watuareg.

## Wafulbe na Watuareg

Mojawapo ya athari kubwa zilizotokana na kuanguka kwa dola la Songhai ilikuwa ni mparaganyiko wa kijamii.

Kuanzia mwanzoni mwa karne ya kumi na saba Wanomadi wa sahara walikuwa wakisonga mbele kuelekea bonde la Niger na eneo la ziwa kusini mwa Timbuktu. Katika Masina Wafulbe walikuwa wengi zaidi. Wafulbe wakahimili mashambulio ya Wamoroko kutoka Timbuktu na Jenne, wakadumisha uhuru wao na wakaongeza uhamiaji wao kuelekea Futa Jallon, upande wa magharibi na katika Liptako na nchi ya Hausa upande wa mashariki.

Katika kipindi hicho hicho cha utamalaki wa Moroko kulikuwa pia na upanuzi wa Watuareg wa Adrar - Wa-Kel-Tadmekket na Wa-Kel-Awllimiden. Wakati Wa-Kel-Tadmekket. Hawakujitokeza hadi mwisho wa karne ya kumi na saba, Wa-Kel-Awllimiden hawakuchelewa kuonyesha nguvu zao katika upande wa mashariki wa bonde la Niger, hasa kati ya Gao na Dendi. Waliingilia migongano baina ya machifu wa Kiarma, wakiviteka vijiji vya wakulima kando ya mto na kuwa baa kubwa kwa Timbuktu. Karne ya kumi na nane ilijaa mapigano baina ya Watuareg na Waarma.

Mnamo Mei 1737, *amenokal* Oghmor ag Ald akayazidi nguvu majeshi ya Waarma huko Toya na kuyatia hasara kubwa sana. Mnamo mwaka 1770, Watadmekket wakaizingira na kuishambulia vibaya Timbuktu na kulacha katika njaa kali, baada ya kundi la Waarma kumwua *amenokal* wao, Habatit. Nchi ilinusuriwa tu na kuingilia kati kwa shaykh wa Kunta, ambaye alifanikiwa kuwasuluhisha pasha Ba-Haddu na *amenokal* Hammiyuk, mrithi wa Habatit. Makubaliano yakafanywa kati ya pande zote mbili mnamo mwezi Agosti, 1771, lakini Watuareg wakayavunja na shaykh akajiondoa katika kutoa msaada wowote wa hali kwa Hammiyuk na akamtawaza mpinzani wa Hammiyuk. Hali hiyo ikasababisha kugawanyika kwa Tadmekket katika matawi mawili. Wakati huo huo, akavuta itibari ya Wa-Awllimiden, ambao waliutumia ule utengano kati ya Watadmekket kujaribu kupanua utawala wao kwa Wanomadi wa Sahara katika jimbo la Timbuktu.

Kwa hiyo Wa-Awllimiden wakawa ndio wasaidizi wakubwa wa watu wa Kunta ambao, kadri Waarma walivyozidi kudhoofika, walifanikiwa kujaza ombwe la kisiasa lililokuwa limetokea na kupunguza athari za hali ya kutokuwepo na uongozi madhubuti. Lakini hadi lilipoanzishwa dola la Wafulbe, walikuwa waangalifu sana kuhakikisha kwamba hawajijengei haki zozote za kisiasa katika Timbuktu au kuondoa mabaki ya

mwisho ya utawala wa Waarma. Hivyo Kawa ag Amma, yule *amenokal* mwenye nguvu wa Wa-Kel-Awllimiden, akafuata desturi za zamani na ilipofika Julai, 1796, akaenda Timbuktu kutawazwa na pasha Abu Bakr.

### Sudani Magharibi na ulimwengu

Pamoja na kujitoa taratibu kwa Moroko baada ya kifo cha al-Mansur, mapasha wa Timbuktu bado walibakia watiifu kwa masultani wa mwisho wa ukoo-tawala wa Sa'adi. *Khutba* (Hutuba) ya Ijumaa ilitolewa kila juma kwa jina la watawala wa Marrakesh ambao walihakikisha kuwa wanatangaza kurithi kwao utawala kwa mapasha wa Timbuktu na wakuu wa maboma ya majeshi katika Gao na Jenne. Wakati ukoo-tawala wa Waalawi ulipochukua mamlaka, Waarma wakaanzisha tena utii wao kwa utawala wa Moroko, kwanza kwa Mawlay al-Rashid na kisha kwa Mawlay Isma'il.

Lakini, tofauti na Wa-Sa'adi, Waalawi hawakutilia sana maanani maeneo ya Saheli pambizoni mwa Mto Niger. Sera yao ilitilia mkazo zaidi Mauritania kuliko Sudani. Mawlay Isma'il alimsaidia sana *amir* wa Trarza na mara kadhaa alipeleka, takribani majeshi ya kudumu, Waormani, katika bonde la Senegal, ambako walitiisha kwa ukatili wakazi wa huko hadi kwenye miaka ya 1720. Wakiwa wamewahi kuwa watawala wa Futa Toro huko nyuma, wakawataabisha sana wakazi wa bonde la Senegal ya juu, na mateka waliochukua huko waliwapeleka wakajiunge na askari wengine maarufu weusi wa jeshi lilioundwa na sulutani wa Moroko.

Sultani Sidi Muhammad (1757-90) alipochukua utawala Sera ya Moroko kuhusu Sudani ikaanza upya kwa kurejesha tena biashara ya kuvuka Sahara. Kama ilivyokuwa kwa watawala wa ukoo-tawala wa Sa'adi, sultani wa Waalawi, katika mawasiliano yake na serikali za Ulaya, alijiita "mfahme wa Gao na Guinea." Kwa mujibu wa ushahidi tulionao, hii haikuwa ni kupiga makuu bure. Ukweli ni kwamba mageuzi ya kisiasa ya Timbuktu kuhusiana na Moroko, yanalingana kwa namna nyingi na mageuzi ya nchi za Barbary zilizotawaliwa kwa niaba ya mfalme katika karne za kumi na saba na kumi na nane, wakati ambapo utawala wa Konstantinople, ingawa sasa ulikuwa zaidi kwa jina tu, ulieudelea kuwa muhimu.

## *Mabadiliko ya kiuchumi na kijamii*

### Maafa ya kimaumbile na mazingira ya binadamu

Kufikia mwisho wa karne ya kumi na nane Sudani Magharibi haikuwa tena ile nchi nzuri na yenye maendeleo makubwa aliyokuwa ameyazungumzia al-Mansur mnamo 1591.

Mwanzo wa karne ya kumi na saba uliandamana na msururu wa maafa (ukame, ukosefu wa chakula, maradhi ya mlipuko, na njaa) ambayo yaliteketeza mavuno na kupunguza sana idadi ya watu, yakaongeza mvutano kati ya watu wenye makazi yao maalumu na Wanomadi. Mwaka 1639 kulikuwa na njaa katika jimbo la Jenne, ambalo ndilo lililokuwa ghala ya Pindi la Niger. Kuanzia delta ya kati, njaa ikaenea sehemu zote za kuruba kwa muda wa miaka minne mfululizo. Dhiki iliyotokana na hali hiyo

pengine ndiyo iliyokuwa chanzo cha chama cha kijamii ambacho kilitangulia kuinukia kwa ufalme wa Bambara huko Segu.

Kulikuwa na miaka michache ambayo haikuwa na vurugu katika karne ya kumi na nane. Baada ya upungufu wa chakula uliodumu kwa miaka saba, kuanzia 1711 hadi 1718, kuanzia mwaka 1738 Sudani Magharibi ikapata njaa kali kuliko yoyote iliyowahi kutokea. Ikaiathiri Saheli yote na sehemu kubwa ya Maghrib. Katika mwaka 1741 balaa hilo likaandamana na mlipuko wa ugonjwa wa tauni. Athari za njaa zikaanza kufifia katika mwaka 1744, lakini tauni ikaendelea kuwa ugonjwa wa kudumu ambao ulilipuka mara kwa mara hadi mwaka 1796.

Nchi ya kati ya Timbuktu, Maziwa Makubwa na Niger ilikuwa ndio makutano ya watu kutoka mataifa mbalimbali, na kwa sehemu kubwa ya mwaka ikawa ni mahala palipovuta watu wengi na pakawa pia mahali palipokutanisha namna mbili za maisha - yale ya makazi ya vijijini yaliyotegemea kilimo na yale ya kinomadi yaliyotegemea ufugaji mifugo. Lakini kwa kuwa ardhi iliyokuwa bora kwa malisho ya mifugo ilikuwa pia ndiyo bora kwa kilimo, makutano haya mara nyingi yalizua migongano. Hali hii ilikuwa mbaya zaidi kwa sababu hapakuwa na nguvu yoyote ya kisiasa katika eneo hilo ambayo ilikuwa na uwezo wa kuzuia uvamiwaji wa mashamba ya wakulima na wafugaji au kinyume chake. Hali ilikuwa inakuwa mbaya zaidi mwishoni mwa majira ya kiangazi, wakati ambapo mvua za mwanzo ziliwalazimisha wakulima kwenda mashambani: kuchelewa kidogo tu kwa wakulima, au Wanomadi kuchelewa kuondoa mifugo yao katika maeneo hayo, kulitosha kuleta athari mbaya kwa mavuno ya mwaka huo.


## Uzalishaji nchini na biashara ya kikanda

Kwa ujumla, katika maeneo yaliyopakana na jangwa kilimo kilififia sana. Lakini katika baadhi ya sehemu umilikaji wa ardhi kwa ajili ya kilimo uliongezeka, kama inavyodhihirishwa na uhamiaji wa Wabambara katika Bara, kuanzishwa kwa maisha ya kustakimu miongoni mwa Wafulbe wa Masina, na makazi ya kudumu kwa baadhi ya makundi ya Watuareg katika maeneo yaliyozunguka Timbuktu.

Aidha, kutokana na faida zisizo kifani za kutumika kwa Mto Niger kama njia ya mawasiliano na kupanuka kwa kimia cha biashara ya kimapokeo, biashara ya kikanda ilistawi sana.

Katika Jenne uzalishaji wa chakula ulijaliziwa na mchango kutoka jimbo la San linaloizunguka: karanga, unga wa mbuyu, ushea, asali, vitunguu vilivyokaushwa, pilipili hoho, maharage na fonio. Kulikuwa pia na pamba, nili, sanamaki kwa ajili ya kutengenezea sabuni, sufi, nta, chuma kutoka Bendugu na, bila shaka, mazao mawili muhimu yaliyoagizwa kutoka katika maeneo ya msitu, yaani kola na dhahabu.

Katika jimbo la Timbuktu maeneo ya kilimo yalikuwa karibu na maziwa ya Tele, Oro na Fati, na pambizoni mwa maeneo yenye maji mtuamo. Baada ya kufika kwa Wamoroko Sudani kilimo cha ngano kikaenea, lakini ni Waarma na wafanyabiashara wa Maghrib tu ndio waliokula mkate. Kati ya mazao ya viwanda yaliyozalishwa ni pamoja Na tumbaku na sandarusi, ambayo ilikusanywa kwa wingi sana katika maeneo ya




**11.2** *Njia za kuvuka Sahara kwenye karne ya kumi na sita hadi ya kumi na nane (M. Abitbol)*

Gundam na Ziwa Faguiban.

Maisha ya kibiashara ya Timbuktu yalitegemea sana mafundistadi wa aina mbalimbali: watengeneza chumvi, wafumi, mafundi cherehani, watengeneza ngozi, masonara na watengenezaji wa zana za kilimo na silaha. Kila ufundi ulikuwa chini ya ukiritimba wa ushirika wa kimbari-kitaalamu: watiaji rangi wote, kwa mfano, walitoka Sansanding, ambavyo Waarma ndio pekee waliokuwa wakitengeneza viatu.

Sehemu ya mashariki ya bonde la Niger, ambayo tabia yake ya nchi ilikuwa mbaya na ambayo ilikuwa imetengwa na vimia vya biashara kutokana na kuanguka kwa Gao, ndilo eneo lilikuwa limeathirika zaidi tangu enzi za Songhai.

## Biashara ya kuvuka Sahara na biashara ya Atlantiki

Pamoja na mabadiliko ya kisiasa, mpangilio wa kibiashara katika pindi la Niger uliendelea kuwa imara, ukiwa umeegemezwa kwenye mipaka ya kijiografia na misingi ya kiuchumi na kijamii ambayo iliendelea kuwepo hata katika enzi za utamalaki wa Moroko, na hata wakati wa kuimarishwa kwa biashara ya Ulaya pwani. Ikiwa imeweza kuhimili matatizo anuwai ya kisiasa na kijeshi, biashara ya kuvuka Sahara ikabakia ndiyo shughuli kuu ya kiuchumi katika eneo kubwa la Maghrib na Saheli. Kilichobadilika baada ya karne ya kumi na tano si ukubwa wa biashara bali umuhimu wake kiuchumi katika matarajio ya maendeleo ya nchi zilizohusika.

### *Njia*

Baada ya 1591 njia ya kutoka Dar'a hadi Taghaza ikawa ndiyo njia rahisi ya biashara kati ya Sa'adi na Moroko na Sudani Magharibi. Lakini njia hii ndiyo iliyokuwa ya kwanza kuathirika na misukosuko ambayo ilifuatia baada ya kifo cha al-Mansur. Pole pole wafanyabiashara wakaanza kuiacha njia ya Da'ra na Taghaza, wakaanza kuitumia ile ya Sus na Tafilalet, ambako viongozi wa kidini wenyeji wa pale walikuwa na uwezo wenye manufaa kwao. Kwa hiyo haikufika hata nusu karne baada ya utamalaki wa Moroko kimia cha njia za biashara kikawa takribani kimerudia kuwa vile kilivyokuwa hapo awali. Mabadiliko ya kudumu zaidi ni yale yaliyokuwa yakiathiri sehemu ya kimia ya Saheli na Sudani.

*Njia ya Atlantiki:* Kufufuliwa kwa njia hii kulianza kwenye miaka ya 1620 na kukaendelezwa na Waalawi. Watajukant walikuwa ndio wakuu wa njia za misafara kati ya Moroko kusini na Adrar ya Mauritania. Aidha uenezaji wa mafundisho ya dini katika Sahara magharibi, kama yale ya udugu wa Kadiriyya na Tijaniyya, ulisababisha kwa kiasi kikubwa msambao wa watu na mawazo kati ya vituo vya dini vya Moroko kusini na vile vya Sahara kusini.

Misafara kutoka Shinguetti au Waddan ilisafiri kwenda Saint-Louis katika Senegal kupitia Trarza, Galam kupitia nchi ya Brakna na Hodh kwenye kijia cha Dhar. Kutoka Hodh kuna vijia kadhaa vinavyoelekea katika falme za Bambara za Kaarta na Segu.

Misafara ya Wamoori ilisafiri hadi Segu, Banamba na hata Nanyima, lakini biashara nyingi ya Bambara ilifanyikia Sansanding, kituo kikuu cha biashara cha ufalme wa Segu

*Njia ya Mashariki:* Kundi hili la barabara lilianzia Tafilalet na kuvuka Tuwat, ambako ndiko misafara mikuu ya mahujaji wa Moroko ilikopitia. Pale Timimun, barabara kutoka Tuwat kwenda Sudani ilikutana na vijia kutoka Maghrib kati. Kuelekea kusini zaidi, katika In-Salah, barabara ilikutana na kijia kutoka Ghadames, ambacho kiligombewa na Tunis na Tripoli katika karne yote ya kumi na nane na ambacho ndicho kilichopitishiwa bidhaa za Sudani kwenda katika miji hiyo miwili.

Baada ya Tidikelt, misafara iliambaa mpaka wa magharibi wa Ahnet na kisha, baada ya uvukaji wa shida wa Tanezruft, ikafika Azwad ambako kulikuwa na kambi za Kunta. Wakunta walitoa huduma, maarifa na baraka; kadhalika, walikuwa ndio walinzi wakuu wa barabara za kwenda Timbuktu.

Kila walipofika Timbuktu, wafanyabiashara wa Maghrib walihudumiwa na ma-*diatigui*, ambao waliwakirimu, wakawapa usafiri na kuwapa ulinzi wa silaha, pale ambapo ilikuwa lazima. Kwa wengi wao, safari haikuishia hapo, kwani bidhaa kutoka Afrika Kaskazini ilibidi zipelekwe Jenne.

*Kimia cha Jula* Jenne iliunganishwa na majimbo ya msitu na nchi zilizozalisha dhahabu na njugu za kola kwa njia mbili. Njia ya kwanza, ambayo ilikuwa kusini-magharibi, ilikwenda Bure au Wurodugu; ya pili, ambayo ilikuwa kusini-mashariki, ilikwenda Kong na Asante.

Kong iliipelekea Jenne kola na dhahabu kutoka Lobi na Gold Coast. Bidhaa zote hizo mbili zilichukuliwa na wafanyabiashara wale wale wa Jula ambao waliuza mabamba ya chumvi kutoka Taudeni hadi Buna. Mizigo yao mingine ilikuwa ni ya bidhaa za pamba na bidhaa za Ulaya ambazo zilikuwa zikiuzwa katika maeneo ya Kumasi.

Sambamba na njia hii kulikuwa na njia ya Mossi Yarse ambayo ilikwishaanzisha mahusiano ya moja kwa moja kati ya Timbuktu na nchi ya Asante, pambizoni mwa Jenne, na delta ya ndani.

## Bidhaa za biashara

Chumvi ilikuwa sehemu ndogo sana ya biashara kati ya watu wa Maghrib na wale wa Saheli na Sudani. Tangu mwanzo wa karne ya kumi na saba, wakazi wa miji iliyokuwa ukingoni mwa Mto Niger waliyafikia mashapo ya chumvi ya Sahara kupitia njia tofauti na zilizojitegemea zilizotumiwa na *azalai* (misafara mikubwa) za Wamoori na Watuareg.

Tangu zamani Sudani ilikuwa ikisafirisha nje dhahabu, watumwa na pembe za ndovu. Lakini Sudani ilihitaji pia kuuza bidha nyingine zilizotengenezwa humo nchini, kama vile vitambaa na vito vya thamani, bidhaa ambazo uwiano wake ulizidi kuongezeka kadri usafirishaji nje wa dhahabu na watumwa ulivyozidi kushuka.

Ingawa kiasi cha dhahabu iliyosafirishwa nje kamwe hakikuweza tena kulingana na kiasi kikubwa sana kilichotolewa nchini mara tu baada ya utamalaki wa Moroko, dhahabu ya Sudani ilikuwa sehemu ya mizigo ya misafara iliyokuwa inarudi kutoka Sudani. Mwishoni mwa karne ya kumi na saba kulikuwa na kiasi kikubwa cha ongezeko

la usafirishaji nje wa watumwa baada ya Mawlay Isma'il kuunda jeshi lake la Abid, na katika nusu ya pili ya karne ya kumi na nane, sandarusi ikachukua nafasi muhimu sana katika bidhaa zilizopelekwa Moroko. Kufunguliwa kwa bandari ya Mogador kuliipa misafara ya Kisudani upenyu mpya wa bahari ambapo, mbali na bidhaa zilizokwishatajwa, waliuza pia kiasi kikubwa cha pembe za ndovu na manyoya ya mbuni.

Bidhaa za Moroko zilizosafirishwa Sudani magharibi zilikuwa anuwai, zikiwa ama ni za palepale Moroko (nafaka, tumbaku ya Meknes, nguo za hariri na vitabu vya kidini), au bidhaa kutoka Mediterania mashariki (viungo na hariri), au bidhaa kutoka Ulaya (nguo, sukari, kahawa, vyombo vya kioo na bunduki).

Katika Maghrib ya kati, biashara ya Kisudani ndiyo iliyokuwa chanzo kikubwa cha shughuli katika majimbo ya Tuwat, Mzab, Suf na Jarid. Biashara hiyo ilikuwa ni ya bidhaa anuwai, kuanzia nili, nguo na Turkedi kutoka Kano hadi kola kutoka Asante.

Biashara hii ambayo ilikuwa ya aina aina na iliyokuwa ya kuendelea ilikuwa yenye faida kubwa. Isitoshe, biashara ya kuvuka Sahara haikuwa ikisafirisha bidhaa tu bali pia ilisafirisha mawazo na amali za utamaduni mzima.

## *Maendeleo ya kiutamaduni na kidini*

### Uislamu katika Sudani katika mkesha wa vita vya jihadi vya karne ya kumi na tisa

Kipindi kinachochunguzwa sasa mara nyingi kimeelezwa kama kipindi cha kufifia (kwa maendeleo) na kudumaa kwa utamaduni, kitu ambacho si kweli kama maana yake ni kufifia kwa utamaduni wa Kiislamu.

Kupitia katika maingiliano yasiyosita ya kuvuka Sahara, katika *zawiya* (sehemu takatifu za ibada), katika tarika na makundi ya Warabiti, na kupitia katika vimia vilivyopangiliwa vizuri vya wafanyabiashara wa Jula, athari ya Uislamu iliendelea kuenea kwa viwango mbalimbali miongoni mwa watu wote wa bonde la Niger.

Mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa Rene Caillie aligundua kwamba wakazi wote wa Timbuktu na Jenne waliweza kusoma na kuandika katika Kiarabu. Aidha *Ta'rikh* (tarihi maarufu za Timbuktu) zote ziliandikwa kati ya karne ya kumi na saba na karne ya kumi na tisa.

Uislamu haukuwa tena jambo la mijini tu kama ilivyokuwa katika karne za nyuma. Ukiwa unaenezwa na makundi ya Warabiti wa Kiberiberi au Kisudani, ulikuwa sasa umeenea vijijini na kuwaathiri wakulima wa Kibambara na wafugaji wa Kifulbe.

Kutokea kwa makundi ya Warabiti (*zuwaya* au *insilimen*) ni mojawapo ya vipengee vya kipekee sana katika utabakishaji wa kiethnolojia-kijamii ambao ulitokea katika ukingo wa kusini wa Sahara katika nusu ya pili ya karne ya kumi na saba. Jamii ya kinomadi, kuanzia Senegal hadi Air, ikagawanyika katika matabaka mawili bainifu: makundi ya wapiganaji na makundi ya makarani. Hili la pili lilikuwa na ufahari mkuu wa kidini na *zawiya* zao ziliwavutia wanafunzi na wafanyabiashara wasafiri waliokuwa

wakitafuta ulinzi. Nyingi kati ya zawiya hizi, ambazo zilijengwa kwenye njia za biashara, baadaye zikawa vituo vya misafara. Ma-shaikh wa jangwani wakachukua nafasi za maulama wa mijini, na wakawa wakuu wa kiroho wa wachochezi wengi wa jihadi za karne ya kumi na nane na kumi na tisa.

Uislamu wa Warabiti, kwa kiasi fulani, ulikuwa ni mwendelezo wa jadi ya Kimoravi, na mwelekeo wake wa kimapambano ulitofautiana sana na Uislamu changamani na wenye kuvumiliana "wa Weusi" ambao ulijitokeza katika miji ya Kisudani na vituo vya Jula. Aidha kwa kujihusisha haraka na tarika na vikundi vya kidini kama vile vya Kadiriyya, Uislamu wa Warabiti uliwapa wafuasi wake kiunzi kilichokwenda mbali zaidi ya kategoria za kimapokeo za utambulisho kama vile koo au mbari.

Uislamu ukawa ni kiungo, nguvu ya ukombozi wa kisiasa na kijamii, na kwa hiyo ukawavutia Watukuloor wote wa Futa Toro ambao walikuwa hawapendelei nasaba-tawala ya Denyanke; ukawavutia pia Wafulbe wa Masina, ambao walikuwa wanajaribu kuachana na nira ya Wabambara, na Wafulbe na wakulima wa nchi ya Hausa, ambao walikuwa wakipambana dhidi ya ukandamizwaji waliokuwa wakifanyiwa na madola ya wafalme mbalimbali.

# 12 Kutoka (mto) Niger hadi (mto) Volta

Kuanguka kwa himaya ya Gao katika mwaka 1591 kutokana na uvamizi wa Moroko kulileta ombwe la kisiasa ambalo lilianza kujazwa polepole na himaya nyinginezo.

Falme nne ziliibuka kati ya pindi la Niger na maeneo ya juu ya mto Volta mnamo karne ya kumi na saba na kumi na nane: falme za Bambara za Segu na Kaarta, falme za Mossi, falme za Kong na Gwiriko na falme za Gulmanseba. Hili lilitukia katika mazingira ya makundi mengi ya mbari yasiyo na mamlaka unganifu. Inasemekana kuwa katika kipindi hiki madaraka yalidhibitiwa na makabila. Lakini hii si sahihi, kwani maisha ya Mali na Gao yaliendelea katika mazingira yaliyotawaliwa na mambo ya nje zaidi na zaidi na magomvi ya wenyewe kwa wenyewe yaliyozaa miundo mipya ya kisiasa. Zaidi ya hayo, baadhi ya matukio ya kijamii, kiuchumi na kidini, ambayo katu hayakuwa ya kikabila, yaliathiri mabadiliko ya miundo na, mwisho wa karne ya kumi na nane, kuzusha nyufa za kwanza zilizotangaza mageuzi ya karne ya kumi na tisa.


## *Watu, temi na falme*

### Falme za Kibambara za Segu na Kaarta tangu karne ya kumi na sita hadi karne ya kumi na tisa

*Mabadiliko ya kisiasa*

Chimbuko la falme za Kibambara, japo si la kale, linavurugwa na kusigana kwa masimulizi na tarihi. Mpangilio wa watawala kurithishana madaraka, na urefu wa vipindi vya utawala haukupatana. Uchunguzi huu, hata hivyo, unajishughulisha zaidi na mpangilio na mahusiano ya nguvu yaliyowaendesha watu hawa tangu karne ya kumi na sita hadi karne ya kumi na tisa kuliko matukio.

Suala linalobishaniwa sana linahusu watu waliohusika na uanzishaji wa matukio ya kihistoria katika falme za Kibambara. Tauxier analisemea wazi hili; anaandika: "Ala kulihali, Wabambara wenyewe hawakuwahi kuanzisha falme: wafalme wa Segu na Kaarta walitokana na Wafulbe na wale wa Sikasso na Kong walikuwa wa asili ya




**12.1** *Eneo la Niger-Volta kuanzia karne ya kumi na sita hadi ya kumi na nane*

Kimande - Jula." Ingawa asili za Wabambara zimepotea kwa hakika, nyendo za kisasa zinaakisiwa katika mapokezi yanayowezesha kusema kwa dhati kwamba wamekuwa wenyeji wa pindi la Niger kwa muda mrefu. Wabozo wanaelekea mno kuwa walikuwako kabla yao, na kwamba walichanganyika na Wasoninke, Wasoso, Wamalinke, Wafulbe na wengineo.

Hadithi ya hajira ya wahenga waliotoa majina kwa nasaba tawala za Kibambara ina dhamira ya "kuvuka mto" inayotokea ndani ya visakale vingi vya asili katika Afrika. Ndugu wawili, Baramangolo na Nyangolo, wakiandamwa na adui na kwa kutokuwa na mtumbwi, walivuka mto kwa msaada wa samaki kubwa lililoitwa *m'polio* (kambare) lililowaokoa dakika ya mwisho.

Kipengee cha kipekee cha hadithi hii ya asili ni uhusiano wa haraka uliojitokeza miongoni mwao na Wasoninke. Wasoninke walikuwa wafanyabiashara waliokwisha kulowea kwa karne nyingi, wakati mwingine wakiuza watumwa, na hawakuwa na hamu ya haja ya uaskari, ingawa wageni wa Kibambara karibu waliufanya uaskari kuwa ndiyo kazi. Mmoja wa ndugu wawili, Baramangolo, aliomba hifadhi ya kisiasa kwenye ukingo wa kulia wa mto Niger kwa Wabuare wa Segu. Wabuare, ambao walikuwa Wasoninke, walimpa wilaya ambayo, pamoja na kujitenga, iliwapa nafasi Wabambara wageni kuulinda ufalme wote wa Segu. Wakati huo huo ndugu wa pili, Nyangolo, akajenga *tata* (ngome) huko Baiko. Baada ya kushindwa kuivamia ngome, Wamarka hatimaye walitulia na kuishi kwa amani na wageni. Hivyo Wabambara (hatua kwa hatua) wakabadilika kutoka hadhi ya wakimbizi hadi kuwa walinzi wa wenyeji wao na hatimaye kuwa mabwana. Mchakato huu unadhihirika katika kila maelezo ya chimbuko la nguvu ya Wabambara.

Kipengee kikuu kingine cha historia hii kilikuwa umuhimu wa mto Niger kimkakati pale pindi la mto lilipopinda kabisa hadi ndani ya jangwa na kuelekea njia za kuendea Afrika Kaskazini. Kwa kuunganisha kingo mbili, Niger ya kati ilikwishatenga nguvu za kisiasa kwa karne nne. Ilikuwa vigumu kushirikiana madaraka, na ndiyo maana falme mbili za Segu na Kaarta ziliendelea kushambuliana.

Ni vigumu kuhusisha wahenga wa visakale wa nasaba-tawala za Kibambara na viongozi wa kwanza wajulikanao kihistoria. Kuhusu Segu, tunaambiwa kuwa mmoja wa madhuria wa Baramangolo alikuwa Kaladian Kulibali. Kaladian ambaye hatokei katika mapokezi simulizi, anasifika kuwa alikaribia kurejesha utukufu wa Mali katika karne ya kumi na saba, hususa kwa kuiteka tena Timbuktu kutoka kwa Wamoroko. Wakati huo huo huko Kaarta, kwenye ukingo wa kushoto wa Mto Niger, kufuatana na hekaya ya Wanyoro, Sunsan (t. 1635), mtoto wa kiume wa Nyangolo, anasemekana kuwa alianzisha Sunsana, karibu na Murdia. Mwanae wa kiume, Massa (t. 1666), alikuwa mkulima mashuhuri na baba aliyezaa sana, na aliyewaoza binti zake hatua kwa hatua, si kwa wanamfalme ambao hakuweza kuwatawala, bali kwa watu maskini kwa sharti kwamba wangekuja kuishi naye na kuunga mkono mambo yake. Mtoto wa kiume wa Massa, Benefali (t.1710-45) alipanua sana madaraka ya Wamassasi akitumia njia zilizounganisha maisha ya kilimo cha ubaba na ukatili wa

mavamizi ya kijeshi.

Fulakoro, aliyemrithi kaka yake Benefali, hakuweza kukwepa pambano zito la kwanza kati ya Wamassasi na wafalme wa Segu, ambao walikuwa na nguvu zaidi kwa sababu nchi yao ilikuwa tajiri zaidi na watu wake wa mbari mbalimbali wachangiaji zaidi. Mtu wa kukabiliana naye alikuwa Mamari Kulibali (1712-55), kitukuu wa Baramangolo, mwanzilishi wa ufalme. Mamari, aliyekuwa amejaaliwa nguvu za ajabu, mara akawa kiongozi wa *ton* (umoja wa vijana waliotahiriwa wakati mmoja), iliyompatia jina lake la Biton au Tiguiton; halafu akawa kiongozi wa kijamii na kisiasa nje ya mipaka ya asasi za kizee na za kidini nchini. Alitumia nafasi hiyo kuimarisha mafanikio yake ya nyumbani kwa kujipatia ushindi wa nje, mmoja dhidi ya Kong na mwingine dhidi ya Wamassasi.

Mamari aliweza tu kufukuza vamizi la kwanza la Kong kutokana na kushirikiana na Wamasina Fulbe. Shambulio la pili lilitimuliwa kwa msaada wa Watyero Somono wakitumia makundi ya nyuki dhidi ya majeshi ya farasi ya Kong.

Fulakoro alikuwa akiizingira Murdia, jambo ambalo liliwafanya waombe msaada kwa Mamari. Mamari, aliyekuwa akisubiri ishara hiyo ili aingilie kati, alimshinda Fulakoro na kumweka mahabusu, na kwa mara nyingine tena Wamassasi ilibidi wahamie upande wa magharibi. Mamari Kulibali aliiteka nchi yote ya Bambara, pamoja na Beledugu. Masina na Jenne ziliwekwa chini ya mamlaka yake, naye akajengesha makasri kwa kutumia msanifu majengo wa Kijenne. Mwisho, mwaka 1751, Mamari aliiteka Nyani, mji mkuu wa Mali yenye kusambaratika, kwa urahisi, na mtawala wake, Massa Maghan Keita, akamlipa ushuru. *Mapasha* wa Timbuktu walipaswa kutenda vivyo hivyo baada ya majeshi ya miguu na ya farasi ya wa Biton kuliondoshea pindi la Niger kodi za Watuareg.

Warithi wa Biton hawakuwa watawala wa hadhi kubwa. Mwanawe, Denkoro (1755-57) katili fidhuli aliyepokonya shoka la dhahabu (nembo ya mamlaka ya ufalme), aliuawa na machifu wa vita. Wastani wa urefu wa tawala zao ulikuwa chini ya miaka mitatu. Ngolo Diarro (1766-90) pekee ndiye aliyetawala muda mrefu wa kutosha kutayarisha sera ya maana. Alikomesha vitisho vya machifu wa *ton-dyon* waliokwisha kuwa mamuluki, na kurudisha ufalme wa kweli. Alitelekeza Segu-Koro na kuhamia juu mtoni katika Segu-Si-Koro. Aliimarisha mamlaka ya Bambara kote, Masina na Timbuktu, ambako maofisa wa kiraia kutoka Moroko na Waarma sasa walikuwa chini ya usimamizi wa machifu wa vita wa Kibambara. Kampeni yake dhidi ya Sila Makan Yero, chifu wa Kifulbe, ilimpeleka hadi nchi ya Dogon. Alipokuwa mzee aliandama msafara dhidi ya Yatenga na kushindwa, na akafa njiani akirudi nyumbani, baada ya kuunda nasaba mpya katika Segu.

Baada ya Ngolo, magomvi ya wenyewe kwa wenyewe yalifumuka tena; hali hii iliendelea hadi Monson Diarra (1792 - 1808) alipofanikiwa kuufanya utawala wake utambuliwe tangu San hadi Timbuktu, na kutoka nchi ya Wadogon hadi Kaarta.

Lakini Kaarta ilikuwa haijaisha. Baada ya kifo cha Falakoro kifungoni, Kaarta iliibuka kutokana na mashambulizi dhidi ya Beledugu, Bambuk na nchi ya

Wakhassonke. Baada ya utawala wa Deniba Bo (1758-61), shujaa mkuu Sira bo Kulibali (1761-80) alijenga makazi ya kifalme Guemu. Alikwisha twaa nusu ya Bakhunu wakati Ngolo Diarra akishughulishwa huko kaskazini na mashariki. Aliiteka nyara Kita, mji mkubwa wa Malinke katika Fuladugu, na kwa kutumia magomvi kati ya koo mbili za Kidiawara, Wasagone na Wadabora, aliwatimua Wadabora na kuwasamehe ushuru Wasagone kwa sharti la kutoa kikosi cha wapiganaji pindi vita vikitokea.

*Muundo wa kijamii - kisiasa wa falme za Kibambara*

Jambo la kuvutia kabisa katika harakati za Wabambara za kuelekea kuwa dola ni fomula waliyobuni ya kusuluhisha taratibu za Kibambara na hali ya maisha katika falme kubwa zenye mbari mchanganyiko. Kuanzia na utaratibu wa kawaida wa ushirika wa *waton*, polepole waliunda chombo cha dola cha kuwageuza toka koo hadi himaya katika muda wa miongo michache.

*Ndani ya ufalme wa Segu* Mahali pa kuanzia ni *fla-n-ton* (umoja wa rika) ulioongozwa na Mamari Kulibali. *Fla-n-ton* ilikuwa ni ushirika wa vijana wa kiume waliotahiriwa pamoja. *Ton-den* (wanachama wa ushirika) walimchagua *ton-tigui* (chifu) ambaye angeweza kuwa mateka ama mwana wa mtu mashuhuri. Tabia kuu ya *fla-n-ton* ilikuwa ni ujamaa kamili miongoni mwa watu wa aina zote za kijamii, ambao ulikingama na utaratibu uliokuwepo wa kikabila au wa utawalamsonge wa wazee. Madhumuni ya *ton* yalikuwa kusaidiana na kugawana rasilimali ili kuweza kushiriki katika maisha ya kijamii.

Mamari Kulibali alipaswa kuimarisha kikosi chake dhidi ya wazee ambao walipinga mpango wake wa *ton,* kwanza kwa kutumia dhima yao kama *faaya* (mababa) na pia kwa madai ya kazi za shamba. Kwa kuwaua wazee wa Donkuna na Banankoro, Mamari alivunja mara moja mamlaka ya utawala wa wazee na kujiweka badala yake kama *faa* (baba) wa *ton-den.* Lakini, kadiri mafanikio ya kiongozi yalivyoongezeka, ndivyo wanachama wa mashirika mengine walivyozidi kujiunga na kundi la asili - wadaiwa muflisi, wahalifu waliosamehewa, wafungwa waliotoroka, na vijana majasura. Wanachama hawa wapya waliingizwa na hadhi ya *ton-dyon* (mateka wa *ton*).

Wanachama wa ushirika - ambao kimsingi ndio uliokuwa jeshi la dola la Bambara - walipomiminika, haikuwa tena suala la *fla-n-ton* bali la *foroba-dyon* (mateka wa uwanja mpana wa pamoja) au *furaba-dyon* (mateka wa Muungano Mkuu). Hii ni *ton-dyon* ya kwanza iliyounda utawala wa kikabaila. Muundo huu uliimarishwa kwa kuhusisha *ton-dyon* na madhehebu mbalimbani aliyoyadhibiti Mamari .

Hatima ya mchakato huu wa kunafsisha na kuhodhi madaraka ilikuwa ni kumbatiza cheo cha *faama* (lodi mhodhi mamlaka kuu) kiongozi wa chombo hiki cha kisiasa-kijeshi. Uchanganyaji wa hadhi hii na ile ya mzee wa kiukoo ulikuwa ni moja ya mikingamo mikuu ya mfumo huu. Mwanzoni, mali iliyopatikana kutokana na

michango, uvamizi na ngawira za vita ilibakia katika *foroba* (hazina ya umma) na kunufaisha jamii yote. Lakini hatimaye *faama* alikuwa na udhibiti wa hiari wa mali ya dola. Mtawala, kwa hakika, alisaidiwa na seneti ya ushauri ya wajumbe arobaini, wakiwemo wanajeshi na wacha Mungu, lakini waheshimiwa hawa walikwisha kula kiapo cha uaminifu kwake katika miviga ya siri kwenye kisiwa ndani ya Mto Niger, na kisha kula kiapo cha utii baada ya kukabidhiwa madaraka.

Mkingamo mwingine hatari ulikuwa jaribio la warithi wa Mamari kuwafanya *foroba-dyon* watwana wa dola ambao kazi yao ni kulima, jambo ambalo lilizusha mgogoro mkuu wa ukinzani miongoni mwa wapiganaji.

Moyo wa ujamaa na uhuriahuria wa *fla-n-ton* haukupotea kabisa kabisa isipokuwa wakati wa enzi za watawala imara kama Mamari Kulibali na Ngolo Diarra. Moyo huu ndio uliochochea mkutano wa *ton-dyon* kumwondosha Denkoro, mtoto wa Mamari, ili "kubadili mbegu." Hata hivyo, baraza la viongozi wa kijeshi polepole waliung'oa mkutano mkuu. Baraza lenyewe liliendelea kudhoofishwa na kuhama Segu kwa baadhi ya wajumbe kadiri ufalme ulivyopanuka. Ili kuvuvumua imani ya vikosi vyake kwake, *faama* aliendelea kuitisha mkutano mkuu angalau mara moja kwa mwaka kuwaapisha upya viapo vya utii, kutambika na kuwaingiza vijana wadogo kikosini.

JESHI LA SEGU Wakati wa uchaguzi, nembo ya ufalme ilikuwa ni pamoja na upinde, podo na shoka la dhahabu - ishara bayana za shughuli kuu za dola. Mapokeo simulizi yanatamba juu ya matendo ya ujasiri ya *faama* wa jeshi la Segu, hasa uzingiraji wa miji. Jeshi lilipopangwa kwa vita, kiini cha kikosi - *sofa* (masaisi) kilikuwa katikati, kiliitwa *disi* (kifua). Kifua hiki kilikingwa kulia na kushoto na *bolo* (mikono); hawa walikuwa ni *foroba-dyon* walioongozwa na *ton-dyon*. Nyuma ya *disi* kilikaa kikosi cha akiba cha *ton-don* wazoefu walioitwa *ton-koro-bolo*.

Silaha zilikuwa ni pamoja na mashoka, mishale, mikuki na bunduki. Bunduki za kwanza za mitutu mifupi na myanzi mipana inaelekea zilitoka Kong. Ngoma zilikuwa na kazi muhimu; hizi zilikuwa ni *tabala* (ngoma kuu) iliyonasibishwa na kila mtawala, na kutangaza vita; au *dunuba* - ngoma iliyopeleka ujumbe wa masafa ya mbali. Mtu aliyehusika na uhamasishaji wa kikosi chote alikuwa ni *yeli* ambaye kazi yake ilikuwa ni kuhakikisha kuwa watu walikuwa na ari ya vita.

Jeshi lilikuwa medani kuu ya watu wa mataifa mbalimbali kukutana. Lilikuwa na watu toka jamii, mbari na mazingira ya kila aina. Hivyo vijana walivutiwa kujiunga, wakiwa na hakika - kama walivuka salama - ya kutajirika haraka.

Mpangilio wa jumla wa nchi, kama ilivyo katika takriban falme zote za Kiafrika, ulikuwa wa kitovu kimoja kutoka chimbukoni kwenye Mto Niger, na kutoka Makao Makuu, Segu-Koro hadi Kirango, hadi maeneo yaliyotekwa miaka mingi iliyopita, ambayo yaliambaa mto toka Kanbaga hadi Timbuktu. Eneo hili kuu la harakati za kidola za Wafalme wa Segu lilipewa jina la kihisia *too-daga* (chungu cha ugali wa mtama). Kutokana na kuendelea kuchanganya mali ya dola na utajiri wa watu binafsi,

watoto (wa kiume) wakubwa wa wafalme walipewa fadhila maridhawa, na makazi yao yalipamba mkondo wa Niger. Katika maeneo ya pembezoni, mamlaka kuu takriban iliwakilishwa na ama machifu wenyeji au magavana walioteuliwa na Segu.

Jumuiya mbili – Somono na Fulbe - zilikuwa na dhima maalum katika mpangilio wa jeshi na ufalme. Mto Niger ulikuwa ndio mshipa mkuu ulioupatia ufalme samaki, usafiri wa umma na mahitaji ya kijeshi. Wavuvi wa *Kisomono* walitakiwa kutoa usafiri na samaki, ambapo Wafulbe walitarajiwa kutunza mifugo ya umma. Vikundi viwili hivi viliungwa mkono na *foroba-dyon*, lakini pia zilikuwepo *foroba-dyon* zilizoanzishwa kama jumuia za wakulima kwenye ardhi ya kilimo kwa mahitaji ya watawala wa Segu.

*Ndani ya ufalme wa Kaarta* Utaratibu wa kijamii-kisiasa wa ufalme wa Massasi wa Kaarta ulifanana na ule wa ufalme wa Segu. Urithishaji wa ufalme haukuleta matatizo kati ya Wamassasi, kwani walikuwa na udhibiti imara wa nchi kupitia magavana wa majimbo na wakuu wa vikosi vya kijeshi. Zaidi ya hayo, watumishi wote wa *sofa*, iliyoambatana moja kwa moja na mfalme, waliandaliwa vizuri sana na watu wote wenye mamlaka, wanajeshi wote wa vikosi, na marafiki wa ukoo walikuwa wajumbe wa udugu huu uliotukuza pepo mlezi wa ukoo.

Kwa kifupi, ukoo wa Wamassasi yaelekea ulifungamana zaidi kuliko ule wa Wasegu, kwani haukubanwa tangu mwanzo na asasi za kienyeji zilizoutangulia. Utawala wao uliundwa na kuendelezwa kwa uhuru chini ya ubunifu wa familia ya Massasi ambayo siku zote ilihakikisha uongozi wake unabakia mikononi mwake.

## Kwenye Uwanda wa Juu wa Volta ya Kati: Falme za Kimossi tangu karne ya kumi na sita hadi karne ya kumi na tisa

*Asili*

Maendeleo muhimu kabisa katika uwanda wa juu wa Volta kipindi hiki bila shaka yalikuwa ni kuundwa kwa falme za Kimossi, ufalme wa mapema kabisa ukiwa katika karne ya kumi na mbili. Tukichukulia, kama waandishi wengi wafanyavyo, kuwa Na Gbewa na Nadega wa simulizi za Mossi ni mtu yule yule, kupitia Naaba Rawa na Naaba Zungrana, watoto wa kiume wa Naaba Wedraogo, basi nasaba za Wamossi zinaunganishwa na falme za Mamprusi, Nanumba na Dagomba. Mchakato wa kuandaa miundo ya kisiasa ya falme za Kimossi ulianza na Naaba Wabri, ambaye majilio yake katika ukuu wa ufalme wa baadaye wa Wagadugu yanakadiriwa kujiri mwaka 1495, na Naaba Yadega, mjukuu wa kuumeni wa Naaba Wubri aliyeanzisha ufalme wa Yatenga mnamo 1540.

Kati ya falme tatu (Mamprusi, Nanumbe, Dagomba) zilizoanzishwa na vizalia vya Na Gbewa, Dagomba pekee ndio uliochukua dhima kubwa, tangu wakati wa Na Nyanghse (1460-1500). Hatujui sana kuhusu tawala zilizofuata kuanzia mwanzoni mwa karne ya kumi na sita hadi katikati ya karne ya kumi na saba. Magomvi ya

kinasaba yaelekea kuwa ndiyo yalikuwa mambo makuu. Lakini katika nusu ya pili ya karne ya kumi na sita chifu wa Kimande (Naaba) alianzisha ufalme wa Gonja.

Katika nusu ya pili ya karne ya kumi na saba wafalme wa Gonja walianzisha misafara ya vita toka makao makuu yao, Yagbum. Moja ya vita hivi, dhidi ya Dagomba, vilifanikiwa, na Gonja ikaiteka Daboya, kitovu cha uzalishaji wa chumvi.

Lakini katika mwaka wa 1713, wakati wa utawala wa Na Zangina, aliyekuwa amesilimu Dagomba ilizima uvamizi mpya toka Gonja. Amani iliyofuata ilikomesha matendo ya uchokozi ya Gonja na pia uvamizi wa mara kwa mara wa ufalme wa Nanumba.

Hata hivyo mnamo 1740 vita vya urithi vilitokea kati ya mteuliwa mpya, Na Garba, na mwana wa mfalme ambaye hakufanikiwa kutawazwa kiti cha ufalme. Kuona hali hiyo, katika mwaka 1744, mtawala wa Asante, Opoku Ware, aliandama msafara dhidi ya Yendi, akiunga mkono kikundi kilichompinga mfalme mpya. Na Garba alitekwa na kufungwa na kuachiwa baada ya kukubali kupeleka Kumasi (kodi ya) wafungwa 2000 kila mwaka. Maisha ya baadaye ya Dagomba yakakwamishwa na matokeo ya mkataba huu, ulioilazimisha kujiingiza katika usakaji watu na muda wote kuendelea kutafuta vyanzo vipya vya wafungwa. Hadi mwisho wa karne ya kumi na nane, Dagomba haikuwa chochote zaidi ya njia ya kupitishia athari za Waasante ambazo zilienea hadi mipakani mwa Mogho (jina la nchi ya Mossi).

*Ufalme wa Wagadugu*

Warithi ishirini na watatu wa Naaba Wubri wanafahamika kutawala (katika) Mogho ya kati na kusini kati ya 1500 na 1800. Naaba Kumdumye, mtoto wa kiume wa Naaba Nyingnemdo, aliyeanzisha serikali ya Mossi katika makazi ya kale ya Wagadugu, alianza utawala wake na mzozo wa kinasaba ambao ulikuwa na matokeo mabaya.

Naaba Kumdumye alishindania ufalme na Naaba Yadega, ambaye baada ya kukataliwa, aliiba nembo ya Naaba Wubri. Akiwa na nembo ya kuhalalisha ufalme wake, Naaba Yadega alielekea Gursi na kuliteka jimbo ambalo hatimaye lilitwaa jina lake, Yatenga (tokana na *Yatega-tenga*: nchi ya Yadega).

Naaba Kumdumye aliwatawaza wanawe wa kiume huko Yako na Tema, sehemu ambazo zilitokea kuwa tawala mbili huru za machifu. Kwa kuwapa nafasi wana wa mfalme ambao uaminifu wao ulikuwa na walakini, mfalme alikuwa anaua ndege wawili kwa jiwe moja: alikuwa anamiliki maeneo kisiasa, na huku akiendelea kuwafurahisha warithi watarajiwa wa kiti cha enzi. Lakini ilikuwa kupitia mchakato huu ndipo tawala kadha za upenuni zikageuzwa kuwa falme au nchi huru za wana mfalme. Zilianza zikiwa nasaba tiifu, kisha zikaendelea kupoteza utii kadiri zilivyozidi kuwa mbali na ufalme kinasaba na kimaskani.

Mwishoni mwa karne ya kumi na sita, Naaba Kuda alihamisha makazi ya ufalme hadi Sapone, jambo ambalo linaonyesha kuwa chombo cha dola kilikuwa bado dhaifu. Pia aliwaweka wanawe katika maeneo kama Laale, Zorgo na Riziam.

Hakuna cha haja kilichojulikana kuhusu Wagadugu hadi utawala wa mporaji wa ufalme wa Kifulbe, Naaba Moatiba (1729-37), mpenda vita ambaye inasemekana alikufa kwa sumu. Jina lake lilifutwa toka shajara ya (nasaba ya) ufalme.

Utawala wa Naaba Warga (1737-44) ulikuwa wa muda mfupi lakini uliojaa mikakati mipya ya kuimarisha ufalme. Alikuwa mwanasheria mkubwa. Kufuatana na Yamba Tiendrebeogo, Warga alianzisha utangazaji wa kimiviga wa *zabyuya* katika sherehe ya kuwasimika machifu. Akaunda baraza la kifalme, lenye watumishi wa makundi mawili, kundi moja la Wamossi na jingine la Wafungwa. Pia aliasisi mfumo wa *pogsyure (napogsyure),* ambao ulikuwa ni utaratibu wa kifalme wa kukusanya na kugawa wanawake ili kuwawezesha watumishi wa mfalme kuzaa watoto. Inasemekana kuwa aliziingiza sheria za mila katika mfumo wa sheria uliokuwa ukitumika kabla ya ukoloni.

Kwa muhtasari, mwisho wa karne ya kumi na saba na nusu ya kwanza ya karne ya kumi na nane ulishuhudia kuasisiwa kwa mfumo wa siasa wa Mossi katika Yatenga na katikati na kusini mwa Mogho. Hata hivyo, baada ya utawala mrefu na wa amani wa Naaba Zombre (t.1744-84) na ule wa Naaba Koom (t.1784-91), aliyekuwa wa kwanza kueneza athari za Uislamu, utawala wa Naaba Saaga (1791-6) ulichafuliwa na magomvi ya ndani ambayo yalitangulia machafuko ya karne ya kumi na tisa.

*Falme ndogo za Mogho*

Falme ndogo na temi za Mogho ya kusini hazijulikani sana. Upande wa kaskazini na mashariki ya kaskazini, hata hivyo, falme tatu zinajitokeza: Bulsa, Busuma na Tatenga.

Ufalme mdogo (wa mwanamfalme) wa Bulsa unakadiriwa kuanza mwazoni mwa karne ya kumi na sita kwa kusimikwa Naaba Namende, mwana na *kurita* wa Naaba Wubri. Ufalme wa Busuma ulimeza temi moja moja ambazo zilikuwa bado zimetawanyika katika eneo hilo: Naamtenga (katika jimbo la Luda) mwanzoni mwa karne ya kumi na nane, halafu utemi wa Pisila, na hatimaye Salmatenga (katika jimbo la Kaya). Dola la jirani la Tatenga, lililoanzishwa na mmoja wa wana wa Naaba Kuda, lilitamalaki eneo hili katika karne ya kumi na nane wakati Naaba Manzi, shujaa wa kitisho na mwingi wa tamaa, alipoingia madarakani. Hata hivyo, Naaba Ruubo wa Busuma alifanikiwa kumwondosha katili Manzi vitani. Mwanawe Wema alilazimika kujisalimishia sehemu za mbali kabisa za safu ya milima ya Riziam, ambayo baadaye, katika karne ya kumi na tisa, ilipoteza ardhi kubwa kwa dola la Yatenga.

*Yatenga*

Warithi wa Naaba Yadega, mwasisi wa ufalme, walitawala eneo la kiasi, pole pole wakihamishia maskani yao ya kifalme upande wa kaskazini. Kaskazini, hata hivyo, ilitawaliwa na ufalme wa Zandoma chini ya enzi ya madhuria wa Naaba Rawa. Shughuli za kisiasa na za kijeshi za Naaba Lambwega zilikuwa hasa ni kuvunja urithi wa Naaba Rawa, ambapo upande wa mashariki alishirikisha temi za zamani za

Kikurumba za Lurum.

Katika karne ya kumi na saba na mwanzoni mwa karne ya kumi na nane, madhuria wa Naaba Lambwega walijaribu kuimarisha eneo la ufalme lililopanuka mno kwa kusimika temi za Mossi huko, zenye Wamasina na Wajelgoji Fulbe, na pia kwa kudumisha maeneo ya tawala za ndani katika Mogho.

*Naaba Kango*

Mara tu baada ya Naaba Kango kuingia madarakani mwaka 1754, alikabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa wanamfalme wakiongozwa na Naaba Wobgo, akalazimika kuacha ufalme na kuikimbia nchi pamoja na wafuasi wake wachache waaminifu. Alifika Kong halafu akahamia Segu, ambako alipata msaada wa Wakulibali kutwaa tena kiti chake cha enzi. Mwaka 1757 alirudi Yatenga akiongoza jeshi la mamluki na kumshinda Naaba Wobgo, ambaye aliikimbia nchi.

Naaba Kango alianza utawala wake na maajabu yaliyoashiria kuachana moja kwa moja na ukale: alikataa kutekeleza safari ya *ringu* (kutawazwa) ambayo pekee iliwapa watawala wa Yatenga hadhi ya *rima* (mfalme). Mnamo 1780 alizindua makao makuu Waiguyo, si mbali na makazi ya ufalme uliopita huko Biisigi. Ulikuwa ni mji mpya kuzunguka ikulu kubwa iliyojengwa kwa mtindo wa Kimali na kuwajumuisha pamoja rafiki zake wa zamani ukimbizini. Kwa mara ya kwanza, wakazi wa makao makuu walikuwa ni wawakilishi wa chombo cha dola tu (serikali), wanasiasa anuwai na ahalulbaiti - jamaa za mfalme wote, wafungwa na walio huru. Jina la makao makuu mapya, Waiguyo, lenyewe liliashiria programu yote: "njoo usujudu na kujisalimisha." Sharti hili lililengwa kwanza kabisa kwa wale wote wa nasaba ya mfalme, waheshimiwa *nakombse* (wana mfalme wa damu) waliomuunga mkono Wogbo mnyang'anyi na ambao sasa ilibidi watiishwe. Lakini, hadi ukoloni ulipoingia, wanamfalme walikataa kukiri ushinde.

Ili kurudisha amani iliyokwisha vurugwa sana katika miaka ya ukosefu wa utulivu, Naaba Kango aliudhibiti ugaidi bila huruma. Ukosefu wa nidhamu wa machifu uliadhibiwa vikali, kama yalivyokuwa matendo yao yote ya ubadhirifu.

Je mauaji ya kinyama ya mashujaa wa Kibambara yalisababisha kupelekwa kikosi cha jeshi na Segu dhidi ya Yatenga? Hakuna kumbukumbu ya msafara huo katika mapokezi ya Mossi, ingawa kumbukumbu hiyo imo ndani ya mapokezi ya Bambara. Kwa kila hali, Naaba Kango, aliyekusudia kuwapatia wafungwa wa damu ya mfalme nafasi maalum katika mfumo wa serikali aliwahitaji wengi zaidi. Baadhi walichukuliwa kutokana na mateka, lakini karibu wote walitekwa wakati wa uvamizi.

Naaba Kango alipokufa 1787, alizikwa katika makao makuu yake wala si katika makaburi ya kifalme. Kifo chake bila shaka kilikuwa faraja kwa wengi, kwani alitawala bila huruma. Chuki ya wanamfalme ilikuwa kubwa kiasi kwamba walimkaba hadi kufa binti pekee wa marehemu mfalme; lakini makabaila wa kitala walioendelea na utii waliweza kumteua mmoja wa marafiki wa muda mrefu wa mfalme, Naaba Saagha (1797-1803) kumrithi.

*Miundo ya kijamii - kisiasa ya Mogho*

Falme za Mossi si madola yenye jamii za aina moja - kikundi mbari cha Mossi - bali ni mchanganano wa vikundi vya kijamii-kisiasa vitokanavyo na ushindi wa mashujaa waitwao Mossi, wa bonde la Volta Nyeupe. Hata hivyo, mchakato wa kuoana kati ya makabila na kujipenyeza polepole kwa kusakini ulioendelezwa na wakulima wa Mossi bila shaka ulileta athari zaidi kuliko ushindi wa kivita. Kila mara eneo lilipotwaliwa liliundwa kufuatia modeli ya kijamii-kisiasa ya Mossi.

Kwa upande wa Yatenga, mwisho wa karne ya kumi na tisa, umma wa Yatenga ulikuwa na jamii tatu tofauti: Jamii ya Mossi, jamii ya Silmiga (Fulbe), na jamii ya Silmi-Mossi. Jamii ya kwanza iliwajibika kwa mfalme, Yatenga-Naaba. Wafulbe au Wasilmiise walikuwa na hadhi ya wageni, kwa misingi ya mikataba ya ukazi ambayo kwayo kipande kipana cha ardhi kaskazini mwa nchi kilitengwa kwa ajili yao. Wafulbe walikwisha sakini ndani ya Yatenga tangu karne ya kumi na saba, na walikwisha jenga vijiji vya kudumu huko ambako utaratibu wa kuhamisha hamisha ng'ombe kufuata misimu ulifanywa. Labda inapotosha kuzungumzia jamii ya Silmi-Mossi, lakini wafugaji wachache walioishi mahali pamoja, wengi wakitokea kusini mashariki mwa Yatenga, kwa kila hali wanaingia katika kategoria tofauti. Jina lao mrakabu linakumbusha kuwa walizaliwa kutokana na ndoa mchanganyiko (ambazo ziliharamishwa hata hivyo) kati ya wanaume wa Kifulbe na wanawake wa Kimossi. Walifika kutoka utemi wa Tema katika karne ya kumi na nane, na hawakuingia chini ya mamlaka ya Mossi, bali hatimaye waliishi chini ya hifadhi ya mbali ya kituo cha kisiasa- kidini cha Wafulbe huko Todiam, mashariki mwa ufalme.

Lakini vipi jamii ya Wamossi yenyewe? Migawanyiko yake ya ndani ilihusishwa na tofauti zilizowekwa na Wamossi kati ya *naaba* (chifu), *naabise* (watoto wa kiume wa machifu) na *nakombse* (watoto au madhuria wa watoto wa kiume wa wana wafalme ambao walikuwa hawajawa machifu). Watoto wa machifu tu ndio waliweza kuwa machifu, na kwa hivyo, kusema kweli, Wamossi wengine wote waliodai kuwa madhuria wa Wedraogo walistahili kuitwa *nakombse*, isipokuwa kikundi kidogo cha machifu na watoto wa machifu. Nakombse wa nasaba ya ufalme wenyewe waligawanyika katika matawi matano, kila tawi likiwa ni kizazi kimoja cha wana mfalme. Nasaba ya kifalme ilionekana waziwazi tangu mapema kabisa kuwa ya kina cha kizazi kisichobadilika (vizazi vitano), uingiaji wa kizazi kipya katika nasaba ya kifalme ulikuwa na maana ya kuondoshwa kwa kizazi kizee kabisa na kukihamishia kwenye kikundi cha *talse* (watu wa kawaida).

Kwa kuwa walitwaa uchifu wa vijiji, *nakombse* walifanya kategoria ya washika madaraka chini ya machifu. Walikuweko wawili wengine: *tasobnamba* (machifu wa vita), wenyeji mashuhuri wa ukoo wa kale, na jamaa wa kaya ya mfalme. Kwa upande wa baraza, muundo uliotawala katika ngazi ya juu ya kisiasa chini ya mfalme ulikuwa ni uleule uliokuwa chini ya chifu mwenyeji. Waheshimiwa watatu walimsaidia chifu, baraza la kifalme liliongeza wa nne, *Bin-Naaba* au *Rasam Naaba*, chifu wa wafungwa wa kifalme.



12.2 *Sanamu ya Mossi inayoonyesha mhenga wa kike, imetengenezwa kwa mti wenye rang'ao asilia (urefu wa cm 47 (H. Dubois, Brussels)*

Hivyo jamaa wa damu ya kifalme waliozama katika mapambano ya kutwaa kiti cha ufalme hawangeweza kumtumikia mfalme. Mwisho, washikilia madaraka ya asasi waligawanywa vyema katika makundi madogo wawili yenye nia kinzani: Machifu wa vita na watumishi wa mfalme, ambao mfalme aliwategemea ili kutawala, na *nakombse,* ambao alitawala dhidi yao. Mgawano huu ulizama sana miongoni mwa Wamossi, kwani watu hawa wenye asili ya chini walioshikilia ofisi kubwa za dola walikuwa ndio wachaguzi wakubwa waliomchagua *Mogho-Naaba* mpya. Migogoro ya ndani siku zote iliambatana na historia ya falme zote za Mossi, nayo siku zote ilihusu kurithisha madaraka. Kwa jumla, palikuwa na ushindani kati ya ndugu wa kiume wadogo wa mfalme na watoto wake wa kiume.

Tofauti na ulimwengu wa serikali uliokuwa maskani ya wafungwa wa kifalme, ulikuwepo ulimwengu wa nchi. Kinadharia watu au wana wa nchi walikuwa madhuria wa wenyeji, isipokuwa wafua chuma. Baada ya kunyimwa madaraka yote ya kisiasa, wananchi hawa walihusika na matambiko ya ardhi yaliyohusu mavuno na amani ya jamii na kuendeleza makundi ya wenyeji. *Naaba* alitofautishwa na *tengsoba* (kuhani wa ardhi), mdhibiti wa nguvu takatifu. Uwili huu uliakisiwa katika nadharia ya asili ya ulimwengu katika ndoa takatifu ya Naaba Wende, Mfalme-Mungu, na Napanga Tenga, Malkia-Ardhi.

Dhana ya "wana wa nchi" ilibadilika maana kwa kadiri karne zilivyopita. Hii ni kwa kuwa Wamossi halisi pia waliingizwa katika kundi la wenyeji na kuitumia hadhi yao hiyo kuwa makuhani wa ardhi. Sambamba na kuhani wa ardhi alikuwepo *bugo* (kuhani wa uzazi), ofisi ambayo inaelekea ilikuwa ya asili ya Dogon.

Ulimwengu wa kisiasa na ulimwengu wa nchi vilichanganywa katika mfumo ambamo mfalme alikuwa ndiye kitovu kupitia miviga mikubwa ya kila mwaka. Wamossi wa Yatenga, kama Wakurumba, walikuwa na kalenda ya jua ya mwaka iliyogawanywa katika miezi ya mwezi, tofauti kati ya mwaka wa mwezi na mwaka wa jua ikifidiwa na mwezi ulioongezwa kila baada ya miaka mitatu. Baada ya *filiiga* (sherehe ya kushukuru) ya mwaka mpya, zilifuata sherehe za *napusum* (kusalimia mfalme) ambapo, katika sherehe tatu tofauti, watumishi wa mfalme, machifu wa vita na *nakombse* walitoa heshima kwa mfalme. Kipindi kilichofuata, tangu mwezi wa pili hadi wa sita, kilichukuliwa na duru ya sherehe iitwayo *bega,* iliyomshirikisha mfalme na waheshimiwa wote wa nchi katika kafara zilizokusudiwa kuomba mavuno mazuri. Sherehe za *bega* zilimalizika mwanzoni mwa msimu wa mvua. Shughuli ya sherehe ilirudiwa wakati wa msimu wa mavuno, na ilijumuisha matamasha mawili ya mavuno ya kwanza.

Mfumo huu changamano sana wa kidini na kisiasa ulileta mshikamano ndani ya jamii ya dola iliyoundwa na makundi yenye asili anuwai ambayo kwa kawaida yalibakiza ndumi za kitamaduni kutoka zama za kabla ya dola tangu yalipojigawa katika tabaka za kijamii-kisiasa. Hivyo mgawanyo huu wa jumuiya kwa jumla katika makundi manne makubwa ya kikazi - washika madaraka, watu wa ardhi, wafuavyuma na wasanii, na wafanya biashara - unajitokeza pia, na tofauti kadha, miongoni mwa

Wakurumba au Wafulse.

Vikundi vyote vya kimbari viligawanywa matawi mawili: vikundi vya madhuria na vikundi vya wenyeji.

Katika jumuiya hii fungamano, jamii ya nasaba na makazi ya kuumeni, neno la Kimossi *bubu* linamaanisha kikundi chochote cha kidhuria ambacho wanajamii wake hawawezi kuoana. Kikiwa na historia yake iliyotambulishwa na jina la mwanzilishi na mahali kilipoanzia, *bubu* ilijitambulisha kwa kuwako *budkamsa* (kiongozi) na *kiims'rogo* (hekalu la jadi) pamoja na kuwa na jina la jumla au motto tambulishi moja au zaidi (*sonda).*

Urithi wa kuumeni ulidumu nchini katika ngazi ya kwanza tu ya jamii, iliyoitwa *zaka* (sehemu). Sehemu iligawanywa katika *yiiya* (kaya), ambazo zilikuwa vitengo vya uzalishaji na ulaji. Sehemu za nasaba moja kwa kawaida zikitawanyika na hivyo zilikutwa ndani ya vijiji kadhaa. Kwa maana nyingine, kijiji cha Kimossi kilikuwa na sehemu za nasaba anuwai, na nasaba ilisambazwa katika vijiji kadhaa.

*Gulma na Borgu*

Kwa muda mrefu, historia ya ukingo wa Gulma (au Gurm) wa Niger haikujulikana sana - Gulma ulikuwa ukingo wa kulia kuelekea mtiririko wa mto kutoka kwenye Pindi. Kufuatana na uchunguzi uliofanywa na mwanahistoria Georges Madiega, sasa tuna taarifa isiyokamilika lakini thabiti kisayansi juu ya Gulma ya kaskazini.

Wadogoni ni miongoni mwa watu wa zamani sana katika Gulma ya kaskazini. Baada yao lilifuata kundi liitwalo Watindamba (watu wa ardhi) na Wawoba kutoka kusini. Gulma ya kaskazini ilikaliwa na Wakurumba pia. Katika Gulma ya kusini wakazi wa zamani kabisa walikuwa ni pamoja na Watankamba, Waberba na, kama kaskazini, Watindamba na Wawoba. Hawa wa mwisho kwa hakika walishika eneo kubwa kabla ya kumezwa kwa kiasi fulani na Wagulmanseba na watu wengine walioanzisha madola huko.

Juu ya muundo huu wa wenyeji wa zamani ulijiingiza utawala wa kigeni wa Wabemba au Waburisimba, ambao baadaye ulizaa madola ya Wagulmanseba. Georges Madiega ana nadharia tete mbili: ya kwanza ni kwamba wahenga wa Mamprusi walipitia Gulma kabla ya kuwasili kwa Waburisimba; (nadharia) ya pili inadai kuwa nasaba za Wagulmanseba za kwanza ziliishi wakati mmoja na nasaba za Wamossi za kwanza. Hii inadokeza kuwa mwanzo wa historia ya Gulma kama dola ulikuwa labda katika karne ya kumi na tano. Mhenga wa kisasili-kihistoria aitwaye Jaba huhusishwa na kuzaliwa kwa madola ya Wagulmanseba. Haelekei kuwa alikuwa shujaa sana, kama Naaba Wedraogo katika historia ya Mossi, kwani nguvu alizosifiwa nazo zilihusu zaidi ujusi (sihiri) kuliko ujenerali. Jambo linaloelekea kuwa la uhakika ni kwamba muungano unaodokezwa na Wamossi kati ya madhuria wa Na Bawa na Jaba si chochote ila maelezo ya baadaye yaliyobuniwa katika baraza la *Mogho-naaba* kutetea mchanganyiko usio dhahiri wa utawala wa Wagulmanse na utawala wa Wamossi wakati wa kipindi cha ukoloni. Ushahidi wote unaonyesha

kuwa, kufuatana na asili za nasaba, himaya za Mossi na Gulmanseba sharti zishughulikiwe kila moja peke yake.

Waburisimba walitoka wapi? Kwa sasa hakuna namna ya kujua ni hajira gani za kivita zilizozaa himaya ya Gulmanseba. Tunajua kuwa makao makuu ya kisiasa ya Wagulmanseba wa mwanzo kabisa yalikuwa Lompotangu au Sangbantangu, kusini mashariki ya Nungu. Waburisimba baadaye walihamia Kujuabongu kusini mwa Pama. Hawakuwa waanzilishi pekee wa falme katika eneo hili. Nasaba ya Jakpangu ni ya asili ya Berba, na nasaba ya Gobnangu ni ya asili ya Uhausa. Pia kuna nasaba ambazo waanzilishi wake walitoka Yanga.

Upanuzi wa Waburisimba uliendelea kipindi chote cha karne ya kumi na sita na kumi na saba, na upeo wa utawala wa Gulmanseba unakadiriwa kuwa karibu na katikati ya karne ya kumi na nane. Wakati huo Gulmanseba ilikuwa na mamlaka juu ya eneo kubwa sana, ingawa kwa hakika lilikuwa na watu wachache sana. Upande wa kusini ilikingamwa na ufalme wa Mamprusi na Borgu, upande wa mashariki na Torodi na mabaki ya himaya ya Songhai, kaskazini na maeneo ya Saheli yaliyokaliwa na Wakurumba, Wasonghai na Wafulbe, na upande wa magharibi na temi za Tuguri, Bulsa, Kupela na Tankudgo. Katikati ya karne ya kumi na nane falme mbili kubwa, Bilanga na Kuala, ziligawana takriban nchi yote ya Gulma ya kaskazini kati yao, pamoja na madola madogo matatu: Piala, Bongandini na Kon.

Historia ya Gulma ya kati na kusini bado haijawa wazi. Kati ya falme kumi na moja za kusini, ufalme wa Nungu ulianzishwa na Yendabri, dhuria wa Jaba, katikati ya karne ya kumi na nane. Huo ulikuwa wakati ambapo Gulma ya kusini ilitwaliwa na Watyokosi, mamluki wa Kimande wa kundi la Wattara ambao awali waliwatumikia wafalme wa Mamprusi. Yendabri, mtawala wa Nungu, alitwaa uongozi wa muungano wa falme ili kuwatimua Watyokosi kutoka Gulma. Baada ya kuzidiwa nguvu na maadui zao, Watyokosi walikimbilia makao makuu yao, Sansane-Mango, ambayo yalizingirwa na majeshi ya muungano. Kuna shaka kama Yendabri mshindi alichukua fursa ya mafanikio yake kuimarisha mamlaka yake juu ya umoja aliouunda. La hakika ni kwamba, katika karne ya kumi na nane, Nunbado (mtawala wa Nungu) alikuwa mtawala kiongozi katika Gulma. Makao yake ya kifalme yakawa mji mkuu wa nchi, sana sana kwa sababu ya nafasi ya uchumi ya wafanya biashara wa Kihausa hapo. Ni vigumu kufasiri mahusiano aliyokuwa nayo Nunbado na watawala wa Gulmanseba. Haielekei kuwa kulikuwa na muungano wa Gulmanseba, na mamlaka hasa ya Nunbado bila shaka yalikuwa na mipaka kinchi kama yalivyokuwa ya wafalme wengine, lakini alipata hadhi kubwa ya kiadilifu na kimiviga kiasi cha kuja kutambuliwa hapo baadaye kama mrithi wa moja kwa moja wa Lumpo, na hivyo wa "baba" yake, Jaba.

Borgu, kusini mashariki ya Gulma, ina historia yenye kukanganya, ikiwa na tawala kadha za kidola, wa mwanzo kabisa ukiwa Busa uliofikia upeo wake katika karne ya kumi na sita, na halafu kuporomoka. Falme nyinginezo, kama Nikki, kwa kiasi zimetokana na Busa.

*Jamii zisizokuwa na mamlaka unganifu*

Watu hawa wanaelezwa hivi kwa kukosa jina bora. Walitokea mapema sana na walisakini katika bonde la Volta ya juu. Ingawa watu hawa hawakutawala jukwaa la siasa, mchango wao katika historia ya Afrika lazima utiliwe maanani, kwani wanaunda umma wa msingi ambao ndani yake michango ya nje ilipandikizwa kibiolojia.

Neno lenyewe Moaga (wg. Mossi) lina maana ya "mchanganyiko." Hatuwezi kusisitiza sana juu ya nafasi ya Wanyonyosse, ambao waliishi zamani za kale. Watu wa Yatenga wenyewe hawakupitwa salama na michango ya kibiolojia kutoka kwa watu wa Mande wa pindi la Niger. Mchango wa wenyeji kwenye medani ya utamaduni na uchumi ulikuwa mkubwa sana. Tumeona mchango wa Wadogoni katika maeneo ya uongozi wa kidini na kisiasa na wa Wakurumba kwenye mfumo wa utawala wa kinasaba katika Yatenga.

Wenyeji wote, wawe wa utamaduni wa Kimande au wa Kivolta, walikuwa tayari kwa mabadilishano, lakini walikataa katakata kukubali kutawaliwa - mkakati ambao ulifanikiwa sana hadi kufikia wakati wa ukoloni.

Licha ya kukosekana kwa dola unganifu, Wagurunsi na Wabwaba walichipuza haiba yao ya kipekee. Wagurunsi, walioishi kama vikundi vya kifamilia katika vibanda vilivyojengwa kwa namna yake, walipinga vikali aina yoyote ya utawalamsonge changamano wa kisiasa. Hata hivyo, upande wa mashariki ulikuweko muundo uliopangwa vizuri zaidi chini ya chifu wa jimbo, wenye baraza na mshauri wa kidini aliyehusika na madhehebu ya *kwara* (alama ya sihiri) yake. Wabwaba wanaonekana kuibuka kama kikundi maalumu kati ya karne ya kumi na ya kumi na tano. Hawakutambua mamlaka yoyote ya kisiasa nje ya ngazi ya kijiji. Dini ya *Do* iliwaunganisha waliotiwa kumbini katika kijiji kimoja na wale wa vijini vya jirani.

Karibu na Yatenga waliishi Wasamo wa kaskazini, ambao makazi yao ya msongamano yanasifika kwa maghala makubwa ya nafaka. Mpangilio wao wa kisiasa ulikuwa wa muungano imara kiasi wa dazeni kadha za vijiji vilivyozunguka vituo vichache vya kisiasa, mfano wa *kafu* (jimbo) ya Wamande. Mfumo wao uliegemea udugu wa koo na miungano ya maeneo. Wasana (*Samo* ndilo jina lao la Kimande), mashujaa na wakulima sugu waliokuwa tayari kufia uhuru wao, hawakusalimu amri kwa shinikizo la Yatenga, iliyojaribu mara kadha kuwashinda.

Kuhusu Wabisa, waliohusiana na Wasana na waliotengana nao baada ya magomvi ya kiukoo, waliishi kusini mashariki ya Mogho. Wao pia walipinga kweli kweli kutawaliwa, licha ya mabadilishano muwafaka kati ya wahusika na kulipa kodi ya mateka mwishoni mwa karne ya kumi na nane.

*Kong na Gwiriko*

Tangu wakati wa himaya za Kisudani kuanzia karne ya kumi hadi karne ya kumi na tano, wafanyabiashara wa Jula, waitwao Wangara, walikuwa wakiandama njia za kuelekea msituni ambako dhahabu na pembe vilipatikana. Lakini, kuanzia karne ya kumi na sita, jambo jipya lilizuka kwenye Ghuba ya Guinea: biashara ya watumwa na

bunduki. Tukio moja hili linatosheleza kueleza kwa nini makundi ya Wajula - mara wafanyabiashara, mara wanajeshi, mara Wamisionari wa Kiislamu - walikwenda zaidi na zaidi kusini ndani ya maeneo ya savana ambako bidhaa zenye kutakiwa sana na wateja wapya ziliuzwa kwa wingi. Ni Wajula ambao walisaidia kuanzisha kituo kikuu cha biashara cha Begho. Njia ya Begho ikaunganishwa na ile inayovuka Cote d'Ivoire ya leo kutoka Assimie hadi Bobo na Bamako kupitia Yakasso. Mwishoni mwa karne ya kumi na sita ufalme wa Gonja ulitokea, na mwishoni mwa karne ya kumi na saba, baada ya Begho kuteketezwa, Wajula walikimbilia katika ufalme wa Abron na kuanzisha Bonduku.

Idadi kadha ya mambo muhimu yalizipa msukumo mkali shughuli za Wajula kuanzia karne ya kumi na saba na kuendelea. Kwanza ilikuwa ni kuanguka kwa himaya ya Gao na pili, kuundwa kwa himaya ya Asante ambayo ilikuwa kituo kikuu cha ugavi wa dhahabu, silaha, chumvi na bidhaa za viwandani. Tatu, zilikuweko jamii katika savana ya Volta, ambazo zilijaa watu wengi na nyingi hazikuwa na mamlaka unganifu ya kisiasa, na kwa hivyo ziliweza kutoa watumwa, na pia ngo'mbe na dhahabu - bidhaa zilizotakiwa na maeneo ya pwani. Kwa hivyo ni rahisi kuelewa kwa nini Wadagomba walilazimika kuunda ufalme wa Kulango wa Buna katika nchi ya Larhon kwa kuiga mfano wa kwao.

Ilikuwa katika muktadha huu ndipo diaspora (msambao) mpya ya makazi yaliyoanza yakiwa ya kibiashara, kisiasa, kijeshi na kidini, ilistawi kwa msukumo wa Wajula. Katikati ya karne ya kumi na nane, magenge yenye silaha yaliyoingia kutoka Segu - Madiarrasuba - yaliwaswagia kando Wasenufo na kusimika ufalme wa Kimande katika Odienne.

Wasenufo ni miongoni mwa kundi la wasemaji wa lugha za Kivolta. Waliishi kiukoo katika Korogho, Seguela, Odienne na Kong. Kuanguka kwa Mali kunaelekea kuliwafungulia uwezekano wa kupanuka kuelekea kaskazini hadi Sikasso na Bunguni, na kusini hadi ndani ya jimbo la Bwake ambako wangemezwa ndani ya kundi la Baule. Upande wa mashariki waliishi katika vikundi mbalimbali vilivyotengana kabla ya kudhibitiwa na Abron. Pamoja na yote Wasenufo walikuwa wakulima waali. Walikuwa wajamaa na wenye kujitegemea kimawazo, na walikuwa na asasi moja tu kubwa ya kijamii, Poron, iliyokuwa na sifa ya kidini, na ambayo ilisaidia kurekebisha tabaka msonge za kijamii. Walikuwa na wasanii stadi ambao, tangu zama za kale, walikuwa wakisanifu baadhi ya sanaa teule za mtindo ashirifu wa Afrika ya Kinegro. Ni karibu katika karne ya kumi na tisa tu Wasenufo walipojiandaa kujenga falme chache unganifu.

Mwanzoni mwa karne ya kumi na nane Wamande waliongeza kituo mashuhuri cha Kong kwenye msururu wa makazi ya Wajula. Ni hapa ambapo Keita na Kulibali Mande, waliokwisha kuwa Wattara, waliwashinda nguvu wenyeji. Kwa msaada wa jeshi lenye nguvu, mmoja wao, Seku Wattara, aliyaondosha makundi mengine ya Wajula na kutawala Nafana na Kong. Jeshi hilo vilevile lilimwezesha kuteka sehemu ya magharibi ya Volta ya juu hadi kufika Dafina.

Baada ya hapo, majeshi ya Kong yalishinda nchi ya Turka na Folona, yakateketeza jimbo la Sikasso na sehemu ya Minyanka na Masina, na hata kwenda hadi Sofara, mkabala na Jenne kwenye Mto Bani. Tumekwisha ona jinsi msafara huu ulivyotimuliwa na Biton Kulibali, hatimaye. Baada ya kifo cha Seku Wattara mwaka wa 1740, himaya ilivurugwa vibaya. Kulikuwa na mgawanyiko kati ya tabaka-amali la wapiganaji wasio Waislamu wa Kijoola na Kisenufo, Wasohonji, na Wajula wa Salama, ambao walikuwa wafanyabiashara na Waislamu. Kong, kwa hakika, ilikwisha kuwa kituo kikubwa cha mafunzo ya Kiislamu, lakini jaribio lake la kudhibiti Jenne linaonyesha kuwa mpango mkuu wa Wattara zaidi ya yote ulikuwa wa kiuchumi: kudhibiti njia za biashara zenye kuunganisha msitu na pindi la Niger kwa masafa marefu kadiri iwezekanavyo. Baada ya mradi huu wa makuu kushindikana, makundi ya Wajula yalirudi na kujishughulisha na miradi ya wastani.

Mradi mmojawapo wa kijasiri ulikuwa ni kuunda ufalme wa Wiriko, ulioanzishwa na Famaghan Wattara, katika eneo tajiri la dhahabu kwenye miinuko ya kati ya mito ya Banafin (kijito cha Niger), Komoe na Volta Nyeusi. Famaghan Wattara alitwaa, takriban moja kwa moja, Tiefo, Dafin na Bwamu (nchi ya Wabwaba). Warithi wake waliweza tu kuzima maasi ya watu waliotawaliwa na kukandamizwa na Wajula. Kutawaliwa huku, baada ya yote, kulikuwa kwa kiuchumi, hata pale ilipofanywa ionekane kama ni kwa lengo la kueneza dini.

## *Maisha ya kiuchumi kutoka Niger hadi kwenye bonde la mito ya Volta*

J.B. Kietegha anakadiria kipindi cha uzalishaji wa juu kabisa wa dhahabu toka Volta Nyeusi kuwa katikati ya karne ya kumi na nane, ambapo wageni walihodhi uchimbaji wa dhahabu ya Pura na kuingiza maendeleo ya kiteknolojia.

Biashara ilitia fora katika magharibi na nusu ya kaskazini ya eneo la kati ya Mto Niger na bonde la mito ya Volta. Lakini wakati wa karne za kumi na saba na kumi na nane - hata katika falme za Mossi na miongoni mwa watu wasiokuwa na mamlaka unganifu, lakini waliovuka kiwango cha uchumi wa kijungu-jiko - pole pole kukaibuka mtandao wa biashara uliokuja kuwashirikisha wafanyabiashara weledi zaidi na zaidi.

Katika nchi ya Wamossi, eneo la kilimo cha takriban zao moja la mtama kwenye ardhi iliyochakaa na mvua isiyotabirika, upungufu, hata njaa, vilikuwa vitu vya kawaida. Zaidi ya mtama, uliokuwa chakula cha kawaida, mazao mengine yalikuwa ni pamoja na mahindi, karanga, kunde, maharage, ufuta na baadhi ya mboga za majani. Pamba, mmea mkuu uliotumika katika sanaa za ufundi, unaelekea ulikuwa ukipandwa kwa muda mrefu. Wayarsa Waislamu wamehusishwa na ufumaji tangu mwanzo wa historia ya Wamossi na majora ya vitambaa vya pamba yalikuwa ndiyo mizigo yao katika misafara ya biashara ya kaskazini - kusini. Wamarase (Songhai), waliokuwa mabingwa wa kutia rangi, walitumia buluu iliyokoza. Mimeapori iliyokusanywa ilikuwa ni *nere* na njugu za *mshea.*

Huko Lurum, kabla ya enzi ya Wamossi (hadi karne ya kumi na tano na kumi na

sita), Wakurumba walikuwa na Wamarase miongoni mwao walioshughulika na biashara ya chumvi ya jangwa la sahara. Baada ya kuundwa kwa madola ya Mossi ya kaskazini, pamoja na Yatenga, Wamarase waling'olewa na Wayarse, ambao, pamoja na biashara ya chumvi, waliingia biashara ya kola walizozinunua katika mipaka ya kaskazini ya Asante. Masoko makubwa ya ufalme huo, kama vile Yuba na Gursi, yalikuwa ndiyo vituo vya mwisho vya misafara ya chumvi na kola. Wayarse wa Yatenga walikuwa kundi la wafanyabiashara chapuchapu waliopatikana Timbuktu, hali kadhalika katika bonde la mto Bani na Masina nzima. Katika nchi ya Wamossi waliishi kwa mwafaka na kutegemeana na viongozi: walikubali kupokea fadhila fulani fulani kwa ahadi ya kutochochea mapinduzi ya aina yoyote, kuuza mali kwa *Naaba* kwa upendeleo maalumu, kumuunga mkono kupitia matambiko muwafaka na hata, kwa nyakati fulani fulani, kumfanyia kazi za ujasusi.

Ingawa fedha ya kuhesabia ilikuwa kauri kwa wafanyabiashara, vipimo vingine vilitumika katika biashara ya misafara, na ilikuwepo mifumo mbali mbali ya kulinganisha thamani za kauri, dhiraa ya upande wa kitambaa cha pamba, pande la chumvi, watumwa na farasi.

Yatenga ilikuwa moja ya maeneo makuu ya ufuaji metali ya Afrika Magharibi, na wafuachuma walichanganya bidhaa za metali na biashara ya usafirishaji nje kuelekea Mogho ya kati, ambayo haikuwa na mbale (mtapo) za chuma.

Biashara ya watumwa, iliyokiendelea katika kila sehemu ya pwani ya Afrika ya Weusi kipindi hiki, iliingiza ndani ya utaratibu wa biashara na mahusiano ya kijamii-kisiasa mantiki ya kutisha tangu bunduki, watumwa na madaraka ya kisiasa yalipofanywa sehemu ya mlinganyo mmoja. Wafalme wakubwa kabisa wa wakati huo walishiriki katika shughuli hii ya utumwa, wakichochewa na msururu wa machifu wa kienyeji ambao, watake wasitake, waliandama biashara hii ili kuingia katika mchezo wa kisiasa.

Tumeona ni jinsi gani, katika mfumo wa Wabambara, hadhi ya watekwa ilirasimishwa kijanja kwa kuitumia vizuri asasi iliyokwisha jijenga ya *ton-den* (mwanachama) kuunda *ton-dyon* (watekwa wa jamii). Hatua nyingine ilichukuliwa kuhusiana na *foroba-dyon* (watumwa wa mfalme). Hawa walikuwa mateka wa vita waliokusanywa katika vikosi visaidizi, kila kimoja kikinasibishwa na *faama* aliyekiunda. Baada ya kupata adha ya kila bidhaa ya biashara iuzwayo sokoni, waliona hali yao inakuwa bora waliponunuliwa na jumuiya. Mwanamke alipata hadhi ya *woloso* (kizalia) mara baada ya kuzaa mtoto, na mwanamume angeweza kupata hadhi hiyo hiyo mara baada ya bwana wake kuwa na imani ya kutosha naye. Mara baada ya kufikia hadhi ya *woloso*, alijiunga katika tabaka-amali. Hakuweza kuuzwa tena, na alikuwa na haki ya kumiliki mali na kurithisha wanawe mali yake.

Ni kweli hadhi ya *woloso* iliwapata madhuria wake, hata kama, kama ilivyotokea katika mabaraza ya mfalme, baadhi ya wana tabaka-amali waliweza kupanda hadi vyeo vya juu kabisa. Alama hii ilidumu daima katika kumbukumbu ya jamii. Hivyo, familia ya mfalme mkuu Ngolo Diarra ilishindwa kufuta kumbukumbu ya hadhi ya

utumwa ya mababu zao, jambo ambalo liliwafanya wadhihakiwe na Wamassasi wa Kaarta.

## *Uislamu na dini za jadi za Kiafrika*

Lilikwisha kuwa jambo la kawaida kusema kuwa Wabambara na Wamossi walikuwa ni kikwazo kikubwa cha kuenea kwa Uislamu katika Afrika Magharibi. Hii ni kauli sahili mno yenye kudai marekebisho. Uislamu uliokuwa kazini tangu karne ya nane kama si kabla, uliongeza athari yake ndani ya himaya kuu toka himaya ya Ghana hadi himaya ya Gao. Bila shaka, kulikuwa na vikwazo na pingamizi. Hata hivi karibuni katika karne ya kumi na nane Wajelgoobe na Waferoobe Fulbe aghlabu walikuwa wafuasi wa dini za jadi. Kwa kipindi cha miaka elfu moja, tangu karne ya nane hadi karne ya kumi na tisa, Uislamu uliendelea kupenya jimbo lote hili kupitia mikondo mingi, ikiwemo wafanyabiashara, viongozi wa sala (maimamu) na hata matumizi ya mabavu.

Awali Wabambara waliuangalia Uislamu kiuchangamani: kuwako kwake kuliwalazimisha kusisitiza tena Mungu Mkuu, Maa Ngala. Baada ya kuupokea Uislamu kwa njia hii, wafalme wa Segu na Kaarta hawakuona kipingamizi cha kuwataka ushauri watumishi wa Mungu huyu Mkuu kupitia kwa *Warabiti,* na huku wakiendelea kuwa waaminifu kwa madhehebu yao, ambayo kiutendaji walikuwa ni makasisi wake wakuu kutokana na nyadhifa zao, na kwa majusi.

Ingawa waliendesha viviga vya jadi, Wakulibali walishiriki katika sherehe za kidini za Waislamu, angalau kwa kuhudhuria, na kutoa zawadi aliali kwa Warabiti wa Sarakolle. Uchangamani huu, ambao wakati huohuo ulikuwa ukitokea kuhusiana na Ukristo katika ibada ya Waafrika-Wamarekani huko Brazil, Haiti na Kuba, ulikuwa ni moja ya sifa za mtazamo wa kidini wa Mwafrika-Mnegro. Hivyo kama maombi kwa mizimu yalishindwa kutoa jibu la wazi na la kutosheleza, msaada wa Warabiti ulitafutwa na kukaribishwa kwa unyenyekevu na wafalme mbalimbali wa Kibambara.

Lililokuwa la uhakika ni kwamba Uislamu ulijiingiza kwa Wabambara na asasi kama mitala, talaka, kukana na utumwa, ambazo hazikutishia asasi za kwao kimfumo. Zaidi ya hayo, Warabiti hawakufanya lolote la kuwatisha waumini wapya wa Kibambara. Hivyo huko Dia, pengine moja ya vituo vya zamani kabisa vya Kiislamu katika Sudani ya Magharibi, ufundishaji (wa Uislamu) kwa jumla ulijirekebisha ili kuchukuana na mila za wenyeji, na ulizingatia sana masuala ya ujusi. Warabiti wengi zaidi miongoni mwa Wabambara walikuwa Wamarka, Wabozo na Wasomono, waliodai kuwa ndani ya mkondo wa Uislamu wa Kimoori au Kifulbe. Baadhi ya vikundi vya mbari, kama Wasoninke, Wamarka, Wafulbe na Watorobe, waliosilimu mapema zaidi na kufurahia mavumiliano ya kidini, walitumiwa kama mifano na vichocheo.

Kwa kifupi, kuvumiliana huku kulikuwa kwa manufaa sana kwa pande zote mbili: kuliwashirikisha viongozi wa Kiislamu na serikali, na kutumia njia za kienyeji kuwateka watu katika imani ya Kurani. Aidha, kulichangia pia kuimarisha madaraka

ya wafalme ambao, baada ya kukabiliwa na mtengano wa kimbari na kijamii wa madola yao, wasingehimili anasa ya mfarakano wa kidini. Hii angalau ndiyo iliyokuwa hali ya mambo kabla ya jihadi zenye kuhitilafiana za Seku Ahmadu Barry na Al-Haji Umar.

Katika nchi ya Wamossi, mwanzo wa athari ya Waislamu kwenye baraza la Wagadugu labda ni kwenye utawala wa Naaba Kom, mtoto wa kiume wa Naaba Zombre (t. 1744-84). Uislamu ulienea katika bonde la Volta kufuatia misafara ya wafanyabiashara na wapiganaji wa Kijula, kwa kufuata mstari wa kaskazini hadi kusini, magharibi ya eneo la Volta, kwenye bonde la Volta Nyeusi. Mji wa Bobo-Diulasso ukawa kituo kikuu kimojawapo cha kueneza Uislamu.

Waasisi wa Gonja walikuwa Waislamu wa Kimande. Kutoka Gonja Uislamu ukaingia nchi ya Dagomba. Vituo vya biashara katika maeneo haya mara vikawa vituo vya dini, vikibainishwa kwa kuwako ma-*malam* (wanazuoni wa Kiislamu). Mfalme wa kwanza wa Dagomba kusilimishwa alikuwa Na Zangina, aliyetawala mwanzoni kabisa mwa karne ya kumi na nane.

Uislamu ukaingia nchi ya Mamprusi takriban wakati ule ule. Gambaga, soko kuu, haraka likawa kituo cha Uislamu. Kwa hiyo, Uislamu ulikuja Mogho kutoka kusini mwishoni mwa karne ya kumi na nane, wakati wa utawala wa Mogho-Naaba Zombre, aliyejionyesha kuwa mwenye huruma kwa Waislamu. Ilikuwa katika utawala wa Naaba Dulugu (t.1796-1825), ambapo hatua mkataa ilichukuliwa. Alibadili dini rasmi na kujenga msikiti wa kwanza katika Wagadugu. Uislamu huu wa awali wa Mossi, kama ule uliokuja kutawala katika falme za Mamprusi na Dagomba, ulikuwa Uislamu wa kikabaila, na kwa Mogho-Naaba na machifu wengine na waheshimiwa, taratibu zake hazikugongana kamwe na ibada za dini za jadi. Mbali na kujaribu kupandikiza dini mpya kwa watu wake, Naaba Dulugu anaelekea alichelea Uislamu usienee kwa kasi sana ndani ya ufalme wake.

Hivyo, katika falme za Bambara na Mogho, ingawa palikuwa na uvumilivu usiosailika juu ya Uislamu, dini ya jadi iliendelea kuchukua tahadhari na kutafuta fomula mwafaka. Kwa vituo vingine viwili vya kisiasa, himaya ya Kong na Gwiriko kwa upande mmoja, na falme za Gulmanseba kwa upande mwingine, mkabala wa jumla ulikuwa tofauti kabisa kabisa: Huko Kong, kama ilivyokuwa miongoni mwa Wa Bobo-Jula, dini ya Kiislamu ilikuwa ndiyo sababu ya kuishi na njia ya maisha, kiasi kuwa sera yao, iliyosharabu imani kali, iliashiria jihadi za karne ya kumi na tisa. Kinyume chake, Wagulmanseba walikuwa wang'ang'anizi sugu wa dini ya jadi.

## *Hitimisho*

Kwa nchi za pindi la Niger na bonde la Volta ya juu, kipindi cha tangu karne ya kumi na sita hadi karne ya kumi na nane bila ya shaka kilikuwa ni awamu ya kujenga dola.

Kufuatana na ada za kale ndani ya ukanda huu, madola yote ya Jula, Mossi,

Gulmanseba na Bambara yalikuwa makundi ya mbari nyingi. Hata kama kundi kuu la mbari lilidai fadhila fulani, lenyewe lilikuwa ni matokeo na chanzo cha mchanganyiko wa mbari. Utaratibu wa kisiasa ambao pengine ulionekana kuwa wa kisasa na wa kistaarabu, bado ulikuwa dhaifu, hasa kutokana na kutokutumika kwa maandishi katika utawala.

Zaidi ya hayo, madola yalichimbwa na mikinganio ya ndani. Kwanza, kurithisha madaraka aghlabu kulileta matatizo makubwa. Naaba Kundumye wa Wagadugu alipowapatia nyadhifa wagombea walioshindwa kupata uchifu, hakushuku kuwa mrithi wake, Naaba Warga, ingebidi apigane vita na madhuria wa machifu hao. Tatizo hili la kisiasa lilifanywa gumu na tatizo la kijamii, kwani wana wa wafalme walipotengwa na madaraka walielekeza chuki zao dhidi ya wakulima, ambao walinyonywa bila huruma. Pili, palikuwa na ukinzano mkali kati ya msafara wa kifalme, uliokuwa na watu wa kawaida, na jamaa za mfalme, ambao walidhibitiwa kwa msururu wa hatua, mfano mzuri kabisa wa hatua za aina hiyo ukiwa ni sera ya Naaba Kango wa Waiguyo.

Zaidi ya hayo, suala la dini lisipuuzwe. Ni kweli kuwa, hadi mwisho wa karne ya kumi na nane, madola ya Mossi na Bambara yalifanikiwa kuweka utaratibu wa kuishi uliojengwa juu ya kuvumiliana, mseto wa imani na kubadilishana huduma. Lakini palikuwa na tofauti ya msingi kati ya madola ya Mossi na Bambara, kwa upande mmoja, na himaya ya Kong na falme za Gulmanseba kwa upande mwingine.

Ujeuzi wa dola katika ukanda huu, hata hivyo, ulikubaliana na muktadha mzima wa uchumi ambao ulitangaza hatima ya majaribio ya aina hiyo ya kisiasa. Nchi zote hizi zilikuwa kati ya ukingo wa kusini wa Sahara na pwani ya Atlantiki, ambayo iliendelea kudhibitiwa zaidi na zaidi na Wazungu, ambao sera yao ya biashara ilirekebisha mizunguko ya biashara na miundo na masharti ya biashara kwa manufaa yao. Polepole ugavi na mahitaji vikavurugwa. Katika mkufu wa uchumi ambao kila mtawala alijaribu kuudhibiti, umuhimu wa bidhaa zilizotumiwa kushinda na kushikilia madaraka (farasi, silaha, na mateka) uliendelea kuongezeka, na pamoja nao jinamizi la biashara ya watumwa.

Kwa kulinganisha na watawala wa Kiafrika . wa mwambao - ambao walipambanishwa moja kwa moja na Wazungu na hawakuwa na uchaguzi mwingine zaidi ya kusalimu amri au vita - nchi hizi za bara kwa hakika zilikuwa na nafasi ya kupumua na zilielekea kudhibiti majaaliwa yake. Lakini hatima hiyo kwa kweli ilikumbwa ndani ya mchakato uliokuwa unaendelea kutegemea ulimwengu wa nje zaidi na zaidi. Mamlaka za ukanda huu hazikuwa na muda wa kutosha kujenga dola la kisheria (*de jure*) ambalo lingeleta utulivu na amani iliyotajwa na waandishi wa tarihi kuhusu himaya zilizotangulia. Hata hivyo, imeonyeshwa kuwa, katika hali ngumu, watu walithibitisha kuwa wanaweza kujenga dola kwa kutumia njia zao za Kiafrika.

# 13 Madola na tamaduni za pwani ya Guinea ya Juu

## *Utangulizi*

Kuanzia Mto Kasamansi hadi Cote d'Ivoire(Pwani ya Pembe za Ndovu) kote, kumefululiza eneo kubwa sana la pwani na misitu, lililokaliwa na jamii nyingie za aina nyingi. Eneo hili ni kubwa zaidi kuliko lile wanahistoria walilozoea kuliita Guinea ya Juu. Sura hii inakusudia kusawidi muhtasari wa maendeleo yake kati ya mwaka 1500 na 1800.

### Jamii

Kwa kulinganisha na makundi makubwa ya kimbari ya Sudani, ambako jamii za aina ya madola zimetapakaa, eneo hili linasifika kwa kuwa na vitengo vingi vidogo vya kijamii-kitamaduni vilivyojengwa kwa misingi ya nasaba, koo na vijiji. Kutoka Mto Kasamansi hadi Tanoe kati ya Savana ya kaskazini na mwambao wa kusini kwa upande mmoja, na kati ya safu za milima ya Futa Jallon na "Uti wa Guinea" (Guinea Spine), na mwambao wa magharibi na kusini-mashariki kwa upande mwingine, kuna makundi na vikundi vya mbari zaidi ya mia moja.

Utitiri huu wa makundi ya watu unaeleza wazi tofauti nyingi za kiisimu zinazopatikana katika mandhari hii ya kitamaduni. Wakati mwingine kuna tofauti za kilahaja ndani ya lugha moja, ambazo zinazuia kuelewana kati ya watu ndani ya kundi moja la mbari.

Licha ya tofauti hizi, kuna makundi mapana zaidi ya kiisimu. Familia tatu kubwa za lugha zinachangia eneo kati ya Kasamansi na Tanoe. Ndani ya familia ya lugha za Kimande, kikundi cha Kimande cha Kusini kinatawala - Kimande cha Kaskazini kinajitokeza tu kama Kimande kinachozungumzwa katika Gambia, Kasamansi, Guinea-Bissau, Sierra Leone na Liberia. Kusini mwa lugha za Kimande, kufuata mwambao toka Kasamansi hadi Liberia, lugha ziitwazo "Atlantiki-Magharibi" nazo zimegawanyika kati ya zile za makundi ya kaskazini na makundi ya kusini, na zinatofautiana sana. Mwisho, mashariki na kusini mashariki zile lugha zinazoitwa Kwa zinajumuisha lugha za Kru-Bete na za Akan, ambazo zinaonyesha tofauti zile zile kama lugha ziitwazo "Atlantiki Magharibi."

## Ugumu wa kutayarisha sanisi ya kihistoria

Kufuatilia maendeleo ya nchi za mwambao wa Afrika Magharibi toka Mto Kasamansi hadi Cote d'Ivoire kati ya karne za kumi na tano na kumi na tisa ni kazi ngumu kwa mwanahistoria.

Ugumu kwanza unahusiana na vyanzo vya taarifa vyenyewe. Baada ya karne ya kumi na tano, vyanzo vya Ulaya vya maandishi, vinaendelea kuwa vingi na sahihi kadiri biashara inavyokolea, lakini havipatikani sawa sawa kwa vipindi na kanda zote: vinapatikana kwa wingi katika Senegambia, Pwani ya Mito *(Rivers Coast)* na sehemu ya kutoka Pwani ya Dhahabu *(Gold Coast)* hadi delta ya Niger, lakini vinapungua kwa Liberia na Cote d'Ivoire. Ingawa vinaakisi upendeleo wa Wazungu, hata hivyo, vinatoa picha nzuri ya eneo la mwambao, pamoja na mandhari ya kijiografia, shughuli za kiuchumi, mifumo ya serikali na tabia na mila.

Iwapo vyanzo hivi havitoshi au havipo kabisa, havina budi kuongezewa na vya akiolojia, mapokeo simulizi na vyanzo vinginevyo. Ingawa akiolojia ya eneo kavu la Sudani-Saheli inazidi kukua, ile ya eneo nyevu-nyevu la Guinea ndiyo kwanza inaanza, licha ya uchimbuzi katika Kasamansi, Guinea-Konakri, Sierra Leone na Cote d'Ivoire. Uchunguzi katika mapokeo-simulizi umepiga hatua muhimu ya maendeleo katika sehemu za Mande na Fulbe, lakini haujachanua sana mahali pengine. Zaidi ya hayo mapokeo simulizi hurudi nyuma kuvuka karne ya kumi na saba kwa nadra sana. Mwisho, tukitenga kundi la wasema Kimande ambao kwa kiasi kikubwa wanapatana, isimu-historia katika eneo hili la mchangamano wa ajabu wa lugha bado ipo katika hatua ya maandalizi.

Pia kuna magumu yanayohusiana na mgawanyiko wa kijamii -kisiasa ambao ni wa kawaida kwa jimbo hili. Wanahistoria wa madola yaliyozaliwa kutokana na kugawana makoloni aghalabu hutoa nafasi zaidi kwa watu wa sehemu za Sudani kuliko wale wa sehemu za pwani. Zaidi ya hayo, hakuna uwezekano wa uchunguzi wa jumla wa kihistoria wa watu hawa wa pwani na misituni bila kuwa na maarifa kamili ya historia ya kila kundi.

Uchunguzi wetu utajikita kwenye uhalisi wa historia kama ilivyowasibu watu wenyewe, bila ya kuachana na mtiririko wa historia ya dunia. Mwambao wa Afrika Magharibi ulikuwa kiungo kikuu kati ya shinikizo za kihistoria za Sudani na zile za biashara ya Ulaya; na kadiri karne zilivyopita sehemu mbalimbali za mwambao huu zilichangamka, zikafufuka tena na kutulia.

*Miguro ya Watu*

## *Miguro ya Wamande*

Katika eneo kati ya Gambia na mito ya Guinea na Sierra Leone, alama za uhamaji wa mwanzo wa Wamande (Malinke) kuelekea bahari ya Atlantiki zinaturudisha hadi karne ya kumi na mbili. Mapokeo simulizi yaliyokusanywa Gambia, Kasamansi na Guinea-Bissau yanataja makazi ya kilimo ya Wamande katika kipindi cha mwisho cha

karne ya kumi na mbili. Uhamaji huu wa amani wa wakulima ulifuatwa na uhamaji wa kuteka nchi wa wanajeshi wa Tirmaghan Traore, mmoja wa majenerali wa Sundiata. Kufikia mwisho wa karne ya kumi na tano, utekaji wa maeneo ya pwani ya Atlantiki uliipatia Mali njia pana ya kuifikia bahari, ikaweza kutawala eneo la kati ya Gambia na Sierra Leone.

Hata hivyo itakuwa ni upotoshaji kuona harakati hizi kama ushindi wa kijeshi tu. Uchanganuzi wa kina wa upanuzi huu kuelekea magharibi unaashiria kuwa huenda ulikuwa ni matokeo ya mambo fulani ya ndani ya jamii ya Wamande. Utaratibu wa kurithishana wanandugu ulifanya iwe vigumu kwa wana wa watawala kuwarithi baba zao. Kwa hivyo wengi wao waliandama magharibi na familia zao kuanzisha madola yao. Wananchi wengine wa jamii ya Kimande waliotaka kunufaika na biashara na nchi za Magharibi, na kutafuta maeneo ya makazi, walishiriki vilivyo katika upanuzi huu wa kuelekea magharibi.

## Watu wa ukanda wa Pwani na Bara katika 1500

Kuingia kwa watu katika pwani na misitu kabla ya safari za Wazungu za karne za kumi na tano na kumi na sita ni moja ya maeneo ya giza kabisa katika historia ya Afrika Magharibi. Ni nyaraka chache tu zinazohusu himaya za Sudani na biashara ya dhahabu zinaweza kutupa taarifa kidogo juu ya watu wa Senegambia, Mito ya Kusini na Gold Coast. Kwa maeneo yaliyo kati ya haya, tunaweza tu kubuni historia ya hapa kutokana na kumbukumbu za haraka za wasafiri wa Kireno na mapokeo simulizi ya baadhi ya watu wa bara wanaodai kuwa walikuwa hapo siku zote.

### *Mito ya Kusini kati ya Gambia na Cape Mount*

*Senegambia ya Kusini – Kasamansi na Guinea-Bissau* Makundi matatu makuu yalisakini kwenye milango ya mito na mito ya chini Wareno walipowasili: Wabainuk au Wabanhun, watu wa asili ya Mande waliokuja kutoka mashariki katika karne ya kumi na nne; Wajuula, waliokuja kutoka kusini kabla ya karne ya kumi na tano, na Wabalante kutoka mashariki, waliojitweza juu ya Wabainuk kabla ya karne ya kumi na tano. Nyuma ya makundi haya ya mwambao walikuwepo Wamande waliokwisha fika kutoka mashariki katika karne ya kumi na mbili na kumi na tatu, wakifukuzia watu wengine magharibi kuelekea baharini. Baada ya Wamande, Wafulbe kutoka Masina waliingia katika karne ya kumi na tano.

*Guinea-Konakri na Sierra Leone* Ugunduzi wa kiakiolojia huko Yengema katika nchin ya Kono, uliothibitishwa na uchunguzi wa kiisimu, umemshawishi C. Fyfe kutoa rai kuwa "Pwani ya Upande wa Upepo" *(Windward Coast)* ilikwishakaliwa kwa muda mrefu, tangu milenia ya tatu kabla ya enzi ya Ukristo. Wakazi wa mwanzo kabisa huenda walikuwa Walimba wa Sierra Leone. Halafu wakafuata Watemne na Wabaga, na lugha zao zenye kufanana. Mwishowe walikuja Wakisi na Wabullom, makundi mawili yaliyohusiana ambayo yalitengana, la kwanza likabakia

bara na la pili kuendelea hadi baharini.

Mwisho wa karne ya kumi na mbili, miguro iliyofuatia kuanguka kwa Ghana na Sosso iliwaleta Wasosso katika Futa Jallon, ambako makundi ya Wadyallonke, Wabaga, Wanalu, Walanduma na Watyapi yalikwisha sakini. Kulifuata mchanganyiko wa watu ulioishia kwa baadhi yao kuhamia magharibi. Wanalu, Wabaga na Wa-Landuma-Tyapi walijenga makazi yao pwani na mrima. Mwishoni mwa karne ya kumi na tano, shinikizo la Wafulbe kwa Wasosso, Wadyallonke, Wabaga na Watimne likaazisha harakati mpya za uhamaji zilizowawezesha Wabaga kusambaa kusini kwa kuambaa pwani, na hivyo kuwakutanisha na Wabullom.

*Cape Mount hadi Mto Bandama: Liberia na Cote d'Ivoire magharibi*

Eneo hili lilikaliwa na Wakru, wasemaji wa Kikwa, na sehemu hii ya pwani ilikuwa eneo la biashara ya *malaguetta* au "pilipili jinga." Bara ilitawaliwa na misitu mirefu na milima ya mashariki ya Uti wa Guinea, iliyoruhusu mahusiano finyu na ulimwengu wa savana ya Sudani.

Wasafiri wa Kizungu wa mwishoni mwa karne ya kumi na tano walikutana na watu kwenye mwambao huu kuanzia Rasi Mesurado hadi Rasi Lahou. Wanahistoria wanadhani kuwa haya yalikuwa sehemu ya makazi ya muda mrefu ya Wakru. Akiolojia na uchunguzi katika mapokeo simulizi pia vinaonyesha kuwa jimbo hili lilikwisha kaliwa kwa muda mrefu sana. Kwa hiyo hatuna budi kuchukulia kuwa sehemu ya savana kaskazini mwa msitu ilikaliwa na makundi ya Wamande wa Kusini. Katika karne ya kumi na tano, bila shaka, walikwisha anza kujiingiza kusini hadi msituni kutokana na shinikizo la Wamande wa Kaskazini kutoka Niger ya juu. Msukumo huu wa kaskazini-kusini lazima ulileta vikundi vingi vidogo vidogo vya Wakru kwenye ukingo wa msitu mkabala na bahari.

*Miguro ya watu kutoka Sierra Leone hadi Cote d'Ivoire*

Katika karne ya kumi na sita watu wapya waliingia kutoka bara kuungana na wale waliokwisha kaa hapo. Wengi wao walikuwa ni Wamande waliokimbiziwa kusini na matatizo ya kiuchumi na ya kisiasa ya Mali. Msambao huu kuelekea kwenye kingo za msitu haukufanywa na wapiganaji tu, bali na wafanya biashara pia. Wamande wa kwanza kuhama walikuwa Wakono-Vai, waliokuja kutoka Niger ya juu na kuelekea pwani kati ya 1500 na 1550. Hadi mwanzo wa karne ya kumi na saba, Wavai walikwisha twaa midomo ya mito Mano na Moa, ambapo ndugu zao Wakono walikuwa katika maeneo ya mrima.

Katikati ya karne ya kumi na sita, Wamane-Sumba, kikundi cha wavamizi wa Kimande kutoka Niger ya juu, pia waliwasili kwenye pwani za Sierra Leone na Liberia. Wamane waliwasili Cape Mount mnamo 1545, halafu wakaelekea kaskazini wakiwatiisha wenyeji na kujipenyeza ndani ya Futa Jallon kupitia Scarcies. Walirudishwa nyuma na Wasoso, marafiki wa Wafulbe, hivyo ikabidi warudi pwani, na kuitwaa toka Liberia hadi visiwa vya Los, wakiungana na wenyeji wa asili.

Muundo hasa wa vikundi vilivyohusika katika uhamaji huu haujawa wazi. Lililo

hakika ni kwamba uvamizi huu ulikuwa na matokeo muhimu kwa watu wote katika eneo hili - Wamande wa Kusini, Wakru na Wa-Atlantiki Magharibi - kuanzia uangamizaji wa ufalme mashuhuri wa Wasape hadi ujenzi wa jamii mpya ya kisiasa chini ya utawala wa Wamande. Watu wa mwambao huu walitengwa katika falme nne: Bullom, Loko, Bure na Sherbro. Halafu watu hawa wakachanganyika kijamii-kitamaduni. Katika harakati za utamalaki, Wamane wakaandama mchakato wa maingiliano na wenyeji ulioishia katika kuingiza athari za Kimande ndani ya jimbo hili. Hatimaye, Wamane waliingiza maarifa mapya ya kijeshi yaliyokuza uwezo wa kupigana wa watu wa pwani. Hadi mwisho wa karne ya kumi na sita, wavamizi wanaelekea walikwisha kuwa raia, na kufikia mwanzo wa karne ya kumi na saba, Wamane asili walikwishamezwa kabisa.

Katika karne ya kumi na sita, kundi la Wamande wa Kusini, Wamande (Malinke) wa ukoo wa Kamara kutoka Niger ya juu, walisakini katika Liberia na magharibi ya Cote d'Ivoire, na kusababisha uhamaji wa Wakono na Wavai kuelekea pwani ya Sierra Leone na Liberia, na pia Watoma, Waguerze na makundi yanayohusiana nao kuhamia katika misitu ambayo sasa ni jamhuri za Guinea na Liberia. Wakati huohuo Wadiomande, ndugu za Wakamara, walikuwa wanaelekea mashariki, wakisakini Tuba (Cote d'Ivoire) na kuwatimua Wa-Dan-Tura. Wakijongea zaidi mashariki. Wamande (Malinke) waliingia Worodugu na kuwasukumia Waguro kusini-mashariki kuelekea msituni.

Kishindo cha Wamande kilishinikiza Wakru, ambao waliingia ndani zaidi msituni kuelekea mwambao. Hadi katikati ya karne ya kumi na sita miguro ya kaskazini-kusini ya Wakru huenda ilikuwa imekamilika. Katika sehemu ya Cote d'Ivoire inaelekea miguro hii ilifanyika baadaye.

## Miguro ya watu katika karne ya kumi na saba na ya kumi na nane

Uhamaji wa watu katika karne za kumi na saba na kumi na nane uliathiri eneo lote la mwambao na mrima, na ulikuwa wa kuelekea pande zote. Sekta iliyoathirika sana ilikuwa ni eneo kati ya Liberia na Mto Tanoe. Warren L. d'Azevedo ametoa rai kuwa miguro hii ilichochewa zaidi na hamu ya kudhibiti biashara ya watumwa ambayo nayo iliingiza migogoro na kusababisha kuunda ushirika wa kijeshi na wa kibiashara kati ya, na ndani ya, vikundi vya mbari.

### *Kutoka Gambia hadi Sierra Leone*

*Kasamansi na Guinea-Bissau* Katika karne za kumi na saba na kumi na nane hakukuingia watu katika eneo hili; lakini kutokana na kustawi kwa biashara ya watumwa palikuweko na mchanganyiko wa watu uliosababishwa kwa kiasi fulani na mashambulizi ya Wamande, ambayo yalileta maafa makubwa, yakiongezewa na upanuzi wa Kaabu, iliyokuwa katika upeo wa ustawi wake. Wamande na vibaraka wao wa Kasanga waliendelea kuwasumbua Wabijago, Wajuula, Wabalante na Wabainuk. Ili kukwepa shinikizo la wafanya biashara ya watumwa, watu wengi

walikimbilia kwenye maeneo ya kinamasi ya pwani, wakiwaachia Wamande udhibiti wa mito yenye kuelekea bara.

*Guinea-Konakri na Sierra Leone* Athari yenye kukua ya biashara ya Atlantiki kwa watu wa zoni ya Sudani na ueneaji wa Uislamu ulioonyeshwa na mapinduzi ya Wafulbe katika Futa Jallon kwenye karne ya kumi na nane ndiyo mandhari yaliyoleteleza miguro ya watu katika eneo hili kwenye karne ya kumi na saba na ya kumi na nane.

Katika thuluthi ya kwanza ya karne ya kumi na nane, Wafulbe wa vita vya jihadi walianzisha hajira ya watu wa kundi la Tyapi kuelekea kwenye pwani za nchi ambayo sasa ni jamhuri ya Guinea. Wakikataa mamlaka ya watawala wa dini mpya, na baada ya kushindwa vita kadhaa walivyopigana kwa ujasiri mkubwa, kama vile vya Talansam viliyopiganwa na Wabaga, makundi ya mwisho yaliihama Futa Jallon kuelekea pwani.

Uhamaji mwingine mkubwa ni ule ulioyaleta pwani makundi kwa makundi yenye nguvu ya Wasoso-Dyallonke. Baada ya kufukuzwa kutoka Futa Jallon, Wasoso walijongea polepole kuelekea pwani ambako tayari kulikwisha kaliwa na Wanulu na Wabaga. Lakini wimbi kubwa la uhamaji lilianza 1760 wakati Wasoso, chini ya uongozi wa Suba Tumane, walipowavamia Wabaga na kuanzisha utemi wa Tumania katika mrima wa musoma wa Kalum. Waliwakaribisha jamaa zao, Wadyallonke, ambao pia walifukuzwa kutoka milimani na Wafulbe, na ufikia mwisho wa karne ya kumi na nane walikwisha tawala pwani yote kati ya Rio Pongo na Sierra Leone.

Hata hivyo, watu wa kundi la Tenda, kwenye viduta vya kaskazini-magharibi vya milima ya Futa Jallon, waliwapinga Waislamu wa Fulbe. Na ndivyo ilivyokuwa kwa Wakonyagwi na Wabassari walioepuka kutawaliwa na wavamizi tangu karne ya kumi na tano.

Wahamishaji wengine wakuu wa umati wa watu kuingia Guinea na Sierra Leone walikuwa Wamande wa Kaskazini, waliosababisha Watoma, Waguerze na Wamanon kuhamia kwenye zoni za misitu ya Guinea, Wamande kuhamia Sierra Leone na Wakwoja kuhamia Sierra Leone na Liberia. Hatuna budi kutofautisha hapa kati ya miguro ya kawaida ya Wamande kuelekea kusini hadi baharini, na uhamaji uliotokana na kuenea kwa Uislamu.

Majilio ya mapinduzi ya Kiislamu katika Futa Jallon yaliwafanya Wamande waungane na Wafulbe kuwasilimisha au kuwatiisha Wasoso, Wabaga, Wabullon na Watemne. Hivyo walitwaa Mellakori katika karne ya kumi na nane, wakawekea utaratibu temi za Kiislamu za Mande, na kuwakilishwa katika mwambao wote kutoka kisiwa cha Matakong hadi mto wa Saint Paul. Mwisho wa karne ya kumi na nane upinzani dhidi ya Uislamu ulianza miongoni mwa Wasoso na watu wa Atlantiki Magharibi wakati *Almamy* (Imam) wa Futa Jallon alipojaribu kueneza mamlaka yake kwenye eneo lote. Hata hivyo, jamii ya mito ya Guinea na Sierra Leone haikubahatika kuepuka athari za Futa Jallon, wala athari za kisiasa na za kitamaduni za mawalii-wafanya biashara wa Kimande.

*Liberia hadi Mto Bandama*
Hajira zilizosaidia kuanzisha jamii za eneo hili katika karne ya kumi na saba na kumi na nane kimsingi zilikuwa ni maendelezo ya miguro ya kaskazini-kusini iliyotokea katika karne ya kumi na tano na kumi na sita. Zilisababishwa pia na misukosuko mikubwa iliyotokea katika ulimwengu wa Waakan katika karne za kumi na saba na kumi na nane, na vivutio na hitilafu za hali halisi ya pwani wakati ule. Matokeo yake yakawa ni misafara ya uhamaji kuelekea kila upande, uhamiaji ambao, huko msituni, wakati mwingine ulikuwa ni wa mzunguko tu.

*Wamande na Wawe* Uvamizi wa pwani za Sierra Leone na Liberia unaonyesha kuwa msukumo wa Wamande bado ulikuwa unawashinikiza wakazi wa pwani na wa msituni katika karne ya kumi na nane. Wamande wa kaskazini waliendeleza mjongeo wao kuelekea kusini na kusini-mashariki na kufika Mto Bandama. Miguro yao ilishadidisha ile ya Wamande wa Kusini: Wadan waliendelea kuhamia kusini-mashariki na kusini-magharibi, ambapo Waguro na Wagagu walikuwa wakielekea mto Bandama na kuupita. Msukumo huu wa Wamande wa kusini uliwaathiri Wawe, hasa wale wa Tuleplu katika Cote d'Ivoire, walioufikia msitu katikati ya karne ya kumi na saba na Mto Cavally baadaye.

*Wamagwe-Kru* C. Behrens anafikiri kuwa Wakru waliingia mwambao wa Liberia kutoka mashariki kuelekea magharibi katika karne ya kumi na sita. Baada ya kugawanyika katika makundi mbalimbali, walitamalaki eneo ambalo sasa linaitwa Grand-Bassa County (Wilaya ya Bassa Kuu) katikati ya karne ya kumi na saba. Kuhusu makazi ya Wakru ya Cote d'Ivoire, inaelekea kuwa uhamaji wa magharibi-mashariki ulifuata ule wa kaskazini-kusini. Hivyo Wakru wa Grand-Bereby (Bereby-Kuu) walikuja Cote d'Ivoire kutoka Liberia kufuatia kumegukameguka kwa makundi ya Wagwerre (Wawe) kutoka kaskazini.

Wimbi kubwa hili la uhamaji liliyaondoa makundi makubwa ya Wamagwe kutoka bonde la Cavally huko magharibi kwenda katika bonde la Sassandra na kulipita hadi Mto Bandama. Wimbi hilo lililipatia wakazi eneo la kati ya mito Sassandra na Bandama hadi mwisho wa karne ya kumi na nane.

## *Mitantiko (mabadiliko ya maumbile) ya kisiasa na mabadiliko ya kijamii-kiuchumi*

### Kuanzishwa kwa njia za bahari: mwishoni mwa karne ya kumi na tano hadi mwanzoni mwa karne ya kumi na saba

Mara baada ya kuruhusu kuingia na kutoka kwa misafara na biashara, kati ya mwisho wa karne ya kumi na tano na mwanzo wa karne ya kumi na saba, eneo la pwani lilikuwa kivutio kwa wakazi wa pwani na sehemu za karibu za bara na wafanyabiashara wa Sudani kutoka bara. Uanzishwaji wa njia za bahari ulikwisha anza kabla ya kufika kwa majahazi ya Wareno, wakati upanuzi wa Wamande

ulipounganisha Sudani ya kati na pwani ya Atlantiki, kutoka Senegambia hadi Gold Coast.

*Wahusika wa ndani waliowezesha kuanzishwa njia za baharini*

Katika karne za kumi na nne na kumi na tano, Mali, kutokana na harakati zake za kupanuka kuelekea magharibi, ilikwisha andaa mazingira ya ukuaji wa biashara ya Wamande ndani ya eneo la pwani. Gambia na Kasamansi baada ya kuwa majimbo ya Mali walibadilishana mazao yao ya kilimo na bidhaa za ufundi kwa chuma na metali nyingine kutoka bara. Miji ya biashara ya Kantor iliendesha biashara hii ambayo ilitumia njia za maji, hasa mito Gambia na Kasamansi, ambayo milango yake iliunganishwa na biashara motomoto ya pwani. Biashara tofauti iliendeshwa toka Mto Niger hadi msituni, ambako Wajuula walibadilishana chumvi, shaba, bidhaa za pamba na samaki kwa kola na, wakati mwingine, mafuta ya mawese. Wajuula walileta bidhaa kutoka pindi la Niger hadi El Mina, kama ilivyoripotiwa (katika) Begho katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na tano.

Eneo la biashara la Wamande lilitegemea mtandao wa njia na vituo vya masoko vilivyoenezwa tele kwenye mipaka ya msitu na kuendelezwa na mabonde ya mito hadi pwani.


*Sababu za nje: msafara ya upelelezi ya Wareno*

Wareno walikuwa Wazungu wa kwanza kuipeleleza pwani ya Afrika Magharibi katika karne ya kumi na tano, mara baada ya uundaji wa jahazi la kuwawezesha kuzunguka Rasi Bojador mwaka 1434. Walitia nanga kwenye kisiwa cha Arguin mwaka wa 1448 na kujenga vituo vya biashara katika sehemu mbalimbali za mwambao, kutoka Senegal hadi Gold Coast, na kuvinjari eneo lote la Ghuba ya Guinea. Katika harakati za kutafuta dhahabu na viungo, waliunganisha himaya yao ya kuvuka bahari iliyokuwa inainukia na eneo la biashara la Wamande, lililostawishwa na upanuzi wa Mali.

Nyaraka za Wareno za wakati ule zinaonyesha orodha ya bidhaa za shehena ya majahazi yanayorudi. Bidhaa hizo ni pamoja na mchele, sandarusi, ngawa, majamvi na mifuko ya ukindu, na vifaa vya pembe za ndovu hasa vijiko, mabakuli yenye viweko, na baragumu za kuwindia. Baadhi ya bidhaa hizi zimehifadhiwa na zinapatikana katika makumbusho makuu ya makontinenti matatu. Kazi bora kuliko zote, zile za Wabullom wa Kisiwa cha Sherbro, zinathibisha kiwango cha juu cha usanii kilichokwisha fikiwa na watu wa pwani kabla ya kufika kwa Wazungu.

Muda wote wa karne ya kumi na sita, Wareno walishika hatamu ya shughuli za baharini na za biashara kwenye pwani ya Afrika Magharibi kuanzia Arguin hadi Angola. Katika Guinea ya Juu walisafiri kwa mto wakitafuta dhahabu ya Sudani. Katika eneo hili, lililokuwa njia ya Mali ya kutokea baharini, walisaidia kuboresha mahusiano kati ya Pwani ya Mito kwa upande mmoja na Gambia ya Juu, Senegal ya Juu na Niger ya Juu kwa upande mwingine.

Katika karne ya kumi na sita njia za ndani za biashara za Wajuula zilielekea



13.1 *Pembe ya kuwindia ya karne ya kumi na sita kutoka Kisiwa cha Sherbro (Bullom), Siera Leone. Urefu cm 43.*

kwenye sehemu za pwani zilizotwaliwa na Wareno. Dhahabu ya Sudani, kwa hivyo, ilifika Lisbon pamoja na pilipili jinga (malaguetta). Kwa njia hii maeneo ya biashara ya Wazungu na Wamande yakafumana, na na huo ukawa ndio mwanzo wa kuchukuliwa kiuchumi kwa biashara ya Sahara.

*Safari za Wazungu na biashara za mwanzo*

Ubabe wa Wareno, hata hivyo, ilibidi upambane na maharamia wa Kifaransa na wa Kiingereza waliovinjari pwani ya Guinea tangu 1530 na kuendelea. Baadaye matatizo yao yalikolezwa na ushindani wa Waholanzi. Merikebu za Waholanzi zilianza kuambaa Afrika Magharibi miaka ya 1590, na muongo mmoja baadaye Uholanzi ilikuwa ikifanya biashara zaidi na Afrika Magharibi karibu kuliko mataifa ya Ulaya yote pamoja. Ubabe wa Waholanzi ukaupiku ule wa Wareno.

Hata hivyo, kufikia mwisho wa karne ya kumi na sita Wareno walikwisha kamilisha kuifungua pwani ya Atlantiki ya Afrika ya Magharibi kwa ajili ya biashara, na kuweka mkakati uliokuja kutawala karne za baadaye.

*Miundo ya awali ya kijamii na "Ufalme wa Wasape"*

Ustaarabu wa Atlantiki ya Magharibi, uliosambaa kutoka kwa Wajuula wa Kasamansi hadi Watemne wa Sierra Leone, ulisifika kwa kumudu kuishi katika mazingira ya kiekolojia ya nyanda za chini na maji yaliyotuwama. Ustaarabu huu ulisheheni kilimo cha kwenye vinamasi, utoaji chumvi, kilimo cha mpunga na matumizi ya mikondo ya maji kwa usafirishaji na mawasiliano.

Wakiishi kama jamii za vijijini bila watumwa wala tabaka amali (caste), lakini wakiwa na makundi ya rika na vikosi vya kazi, Wajuula walikwisha fikia enzi ya chuma walipokutana na Wamande. Hawakuwa na muundo wowote wa kidola lakini walikuwa na ustaarabu na utamaduni uliofungamana. Waandishi wote wanakubali kuwa mfumo wa tabaka amali, urithi wa kuumeni na miundo ya kidola ni asasi zenye asili ya kigeni. Hivyo basi, kutokana na athari ya Wamande iliyoingizwa na upanuzi wa himaya ya Mali, jamii mbalimbali za pwani zilipangwa katika temi na tawala za wana mfalme, chini ya ufalme wa *Mandi-Mansa*, maliki wa Mali.

Katika karne ya kumi na tano Wareno waliona kuwako kwa majimbo haya ya magharibi, lakini wakaripoti pia kuwako kwa ufalme wa Wasape upande wa kusini. Je, hili lilikuwa shirikisho kubwa lenye kujumuisha Wabaga, Wanalu, Walanduma, Walimba na Watemne, au lilikuwa ni ufalme ulioundwa kati ya Rasi Verga na Rasi Saint-Anne kufuatia kujipenyeza kusini kwa Wa-Tyapi-Landuma-Baga-Nalu chini ya uongozi wa machifu wa Kimande? Wanahistoria wana nadharia tete zenye kusigana kuhusu suala hili.

*Kaabu: kutoka ukombozi hadi kutawala wengine*

Kupanuka kwa Mali kuelekea Atlantiki kufuata bonde la Gambia kulisababisha kuanzishwa, katika karne ya kumi na tano, kwa tawala za kisiasa-kijeshi kama vile

falme ndogo ndogo za Gambia, Kasamansi na Guinea-Bissau zilizofanya mipaka ya magharibi ya dola la Wamande. Watawala wake walilipa kodi kwa *Mansa* kupitia kwa ma-*farin* (magavana) wake. Lakini kufikia karne ya kumi na sita ilikuwa ni *farin* wa Kaabu aliyekuwa akipokea kodi kutoka kwa machifu wa Kimande katika Gambia yote.

Likiwa baina ya Gambia ya kati, Rio Grande na Futa Jallon, jimbo la Mali la Kaabu lilidhibiti biashara ya Kantor. Katika karne ya kumi na sita Kaabu ilimega jimbo la Sankola, kusini mwa Kasamansi ya juu, na kuwa jimbo lenye nguvu, ingawa bado tegemezi kwa Mali. Lakini himaya kongwe ya Mali, ilikuwa ikidhoofishwa na mashambulizi kutoka Songhai, na takriban majimbo yote ya magharibi yalikwishajipa uhuru kutokana na utawala wake, na ma-*farin* wakijiita wenyewe wafalme huru; Kaabu ilifanya hivyo mwaka 1537.

Baada ya kujikomboa, Kaabu iliunganisha nchi zote kati ya Gambia, Kasamansi ya juu na Geba ya juu, na kumng'oa *Mansa* wa Mali katika jimbo hili. Iliendelea kupanua utawala wake juu ya Wakasanga, Wabalante, Wajuula na Wabeafada. *Farin* wake aliimarisha mamlaka juu ya kusini mwa Senegambia yote na kudhibiti biashara ya jimbo hilo.


### *Biashara ya Atlantiki na jamii za Mito ya Kusini*

Katika Sierra Leone Wabullom, Watemne na makundi ya jirani walijishughulisha sana na biashara na Ureno. Wabullom waliochuuza chumvi ya baharini kwa dhahabu kutoka Mali, sasa wakauza dhahabu hii kwa Wareno kwa bidhaa za pamba, kengele za shaba na vyombo aina aina. Mwishoni mwa karne ya kumi na sita Watemne, wakidhamiria kunufaika na biashara ya baharini, walifika mdomo wa Sierra Leone, hivyo kuwagawa Wabullom sehemu mbili.

Hadi wakati huu, Wareno hawakuwa tu wameandaa makazi mengi ya biashara kwenye mwambao wa mito ya kusini, bali pia walikwisha andaa vituo vingi vya kukutana na Wamande katika mabonde ya kati na ya juu ya mito. Mahusiano na bara yalikolezwa, kama yalivyokuwa ya kaskazini-kusini. Wenyeji wa Cape-Verde walifanya biashara moja kwa moja na jimbo la mito la Sierra Leone, wakiuza pamba yao kwenye njia ya kuelekea Bainuk na Kasanga, na vifaa vya kazi za mikono kutoka pwani vilisambazwa hadi Scarcies.

## Maeneo ya pwani kama uwanja mpya wa biashara wa Afrika Magharibi katika karne za kumi na saba na kumi na nane

Kwa kuiingiza pwani ya Afrika Magharibi kwenye biashara ya dunia, misafara mikuu ya upelelezi ya Ulaya iliziingiza nchi za Guinea kwenye mchakato wa maendeleo ya kihistoria usio kifani, yaliyoambatana na upanuzi wa biashara, uhamaji wa watu kutoka bara hadi pwani, na kuibuka kwa jamii mpya. Mabadiliko haya polepole yalisababisha kutengwa kwa zoni ya Sudani ambayo, ili iweze kuishi, ililazimika kuzifufua njia zilizoelekea msituni na baharini.




**13.2** *The main states of West Africa, pre-sixteenth century (after C. Wondji)*

*Kujengwa na kuimarishwa kwa biashara ya Wazungu*

Maendeleo ya biashara ya Ulaya kwenye upwa wa Afrika Magharibi yalikuwa na sifa tatu: Uimarishaji wa biashara hii kwa kuiwekea mfumo wa mabadilishano ya kibiashara, kuongezeka kwa umuhimu wa biashara ya watumwa, na ushindani mkali miongoni mwa mataifa ya Ulaya.


Katika karne ya kumi na saba, Waholanzi walikamilisha mpango wa mfumo wa biashara ya dunia kwa kuunda kampuni zilizosajiliwa. Kampuni ya India ya Magharibi, iliyoanzishwa mwaka 1621 na kupewa ukiritimba wa miaka ishirini na nne juu ya biashara na Amerika na Afrika, ilikuwa na dhamana ya kijeshi na ya kibaharia kutoka dola, na iliweza kuandama upanuzi wa biashara na makoloni kwa usalama kabisa. Waholanzi walisambaza Ulaya bidhaa walizoingiza kutoka Asia, Afrika na Amerika, hasa hasa shehena kubwa ya dhahabu na pembe za ndovu, na hivyo kupata faida tele. Waligawa watumwa katika makoloni ya Amerika ya mataifa mengine ya Ulaya (Hispania, Ureno, Ufaransa na Uingereza) ambayo, mnamo 1641, yalikiri ukiritimba wa Waholanzi wa biashara kwenye mwambao wote wa Guinea.

Hata hivyo, baada ya 1660, Ufaransa na Uingereza waliauza mapambano yasiyo na huruma dhidi ya ukiritimba wa Waholanzi, wakiwa na silaha zile zile kama za mpinzani wao. Waingereza waliunda Kampuni ya Majasuri wa Kifalme *(Company of Royal Adventurers)* (1660) na baadaye Kampuni ya Kifalme ya Afrika *(Royal African Company)* (1664), na Wafaransa wakaunda Kampuni ya Kifaransa ya Uhindi ya Magharibi *(Compagnie francaise des Indes occidentales)* (1664) na baadaye Kampuni ya Guinea *(Compagnie de Guinee)* (1685). Kati ya 1640 na 1750, ngome nyingi na vituo vya biashara vilijengwa mwambao wa Afrika, lakini wamiliki walibadilika kufuatana na majaliwa ya vita miongoni mwa mataifa yaliyokuwa yakiendesha biashara ya watumwa.

Kutoka katika sitara ya ngome hizi, na kwenye vituo vya biashara, Wazungu waliendeleza unyonyaji wa kibiashara wa eneo la pwani ya Atlantiki. Kutoka Goree hadi kisiwa cha Sherbro, katika Sierra Leone, biashara ilistawi lakini hakuna kampuni ya Kifaransa au ya Kiingereza iliyoweza kuhodhi biashara yote kutokana na wingi wa vijisiwa vya pwani na visiwa vilivyo nje ya bandari ambako merikebu yoyote iliyopenda ingeweza kutia nanga. Sehemu hii ya pwani hivyo ikawa mahala mwanana pa wawindaji watumwa wa mataifa yote ambayo hayakuhusishwa na makampuni makubwa. Makampuni yaliyosajiliwa hayakujihangaisha na Grain Coast (Pwani ya Nafaka) au Cote d'Ivoire katika karne za kumi na saba na kumi na nane kwa kuwa pilipili jinga *(malaguetta)* haikuwa na thamani tena katika soko la dunia, pembe za ndovu zilikuwa zimepungua, na matatizo ya maegesho mazuri ya kutia nanga yalizifanya merikebu ziikwepe pwani hii. Lakini mwanzoni mwa karne ya kumi na nane, ongezeko la mahitaji ya watumwa katika Amerika liliwashawishi wafanya biashara binafsi kujishughulisha na eneo hii.

*Mabadiliko katika Sudani*

Katika Sudani, hususan katika ulimwengu wa Wamande, matokeo ya biasbara ya




**13.3** *Dola kuu za Afrika Magharibi, kabla ya karne ya kumi na sita*

Atlantiki, iliyotawaliwa na watumwa kama bidhaa, yalikuwa ni ya aina nyingi. Katika darajia ya kijamii-kiuchumi, uhusiano na pwani ulikuwa muhimu zaidi, na biashara ya watumwa iliambatana na kuenezwa kwa silaha za moto na wafanya biashara wa Kijuula. Katika darajia ya kijamii-kitamaduni, baada ya Uislamu kupoteza utawala wake kufuatana na kuanguka kwa himaya kubwa, tabaka la watawala liligawanyika katika pande mbili zenye kuhasimiana. Upande mmoja, wa kiasili na kisiasa, ulijikita kama makabaila wa kijeshi, na upande mwingine, uliokusanya mawalii (Warabiti) na wafanya biashara, uliendeleza Uislamu na kuchochea mapinduzi ya kisiasa-kidini. Pande zote mbili zilidhamiria kumaliza mgogoro wa kijamii uliozalika kutokana na kusambaratika kwa himaya na kuenea kwa biashara ya watumwa.

Baada ya kusambaratika kwa kisiasa kulikofuata kuanguka kwa himaya kubwa, tawala za kushikiza zilijaribu kujenga upya sehemu mbalimbali za bara. Upande wa kaskazini na kaskazini-magharibi himaya kuu ya Foul iliibuka katika karne ya kumi na saba kwenye magofu ya Songhai lakini baadaye, katika nusu ya pili ya karne ya kumi na nane, ikasalimu amri kwa himaya ya Kaarta. Upande wa Atlantiki, nchi zilizoibuka kutokana na kugawanyika kwa Mali ziliunganishwa na Kaabu katika karne za kumi na saba na kumi na nane, na baadaye na Futa Jallon katika karne za kumi na nane na kumi na tisa. Kwenye Niger, kuibuka kulitukia mwanzoni mwa karne ya kumi na nane chini ya mamlaka ya Wabambara wa Segu, chini ya uongozi wa Biton Kulibali. Lakini kusini, kuanzia Niger ya juu hadi Bandama na kuelekea mashariki hadi kwenye eneo la Volta-Senufo, Wajuula waliongeza athari yao. Katika karne ya kumi na nane waliiandaa himaya ya Kong kuhakikisha (usalama wa) njia ya biashara inayoanzia Niger ya kati hadi msituni na Gold Coast, na pia walianzisha miji ya masoko.

Kama biashara ya kuvuka Sahara ilivyosaidia kuleta mamlaka za kisiasa za Sudani kwenye ukanda wa Saheli kati ya karne ya saba na karn e ya kumi na sita, ndivyo shadidisho la biashara ya Wazungu lilivyohimiza kuibuka kwa mamlaka za kisiasa katika mwambao na bara katika karne za kumi na saba na kumi na nane.

*Hegemonia za Mrima za kaskazini-magharibi:ku toka Kaabu hadi Futa Jallon*

Katika karne ya kumi na saba Kaabu ilijijenga na kuwa himaya ya nguvu katika sekta ya Mito ya Kusini. Iliundwa katika shirikisho la majimbo kumi na mawili ya Kimande na kuongozwa na *mansa* mkuu akisaidiwa na askari-maofisa wa kimwinyi na jeshi la kudumu la wapanda farasi. Ufalme huu, uliogeuka kuwa himaya, ulidhibiti biashara ya bonde la Gambia na mito ya Guinea ambamo vituo vya biashara na Ulaya vilijengwa.

Katika nusu ya pili ya karne ya kumi na nane shirikisho la Waislamu Wafulbe lilijisimika; lilitokana na mapinduzi ya Kiislamu yaliyotikisa mkusanyiko wa milima ya Guinea-Sudani mnamo 1725-30. Ikiwa kwenye ndagano ya mito inayotiririkia

baharini kutoka eneo la Niger ya juu, Futa Jallon ilijizatiti kama mshindani wa Wamande wa Kaabu na kupigana nao hadi waliposambaratika katika karne ya kumi na tisa.

*Hegemonia ya pwani ya Wakaru katika Sierra Leone na Liberia*

Historia ya Wakaru imeandikwa na O. Dapper. Kwanza ulikuweko ufalme wa Kwoja, kuzunguka Rasi Mount, uliotekwa na Wakaru na Wafolgia, makabila yaliyotoka bara. Viongozi wa Wakaru walikuwa kimsingi ni malodi wa vita. Wafalme wasiotetereka, watetezi wa ufalme, walirithiana mmoja baada ya mwingine toka baba hadi mwana. Walizima maasi ndani ya majimbo yaliyotekwa, wakafukuza mashambulizi ya mbari za jirani na kutetea mara kwa mara umoja wa himaya yao. Pamoja na hayo, waliendelea kusuhubiana na Wafolgia na Wamanu wa bara, ambao walikuwa na uhusiano wa kitwana nao. Msururu wa ngazi za utwana ulipanda kutoka pwani ya ndani hadi kufikia *Mande-Mani* (Lodi wa Wamanu), Mfalme Mkuu katika jimbo lote.

Kazi ya hegemonia ya Karu ilikuwa kurekebisha biashara kati ya pwani na bara. Msingi wao mkuu wa uchumi ulikuwa biashara na Wazungu, ambayo kwayo walipata faida nyingi kama walanguzi. Eneo la biashara walilolitawala yaelekea lilikuwa lile la lazima kwa shughuli za mfumo wa biashara ya uchuuzi wa watumwa katika ukanda huo katika karne za kumi na saba na kumi na nane.

*Biashara ya Wazungu na Mawakala* (comprador peoples) *wa pwani*

Maendeleo ya biashara katika karne ya kumi na nane na karne ya kumi na tisa yalisababisha kuundwa kwa vikundi vya wafanya biashara miongoni mwa watu wa pwani vilivyofanya kazi ya mtu wa kati au walanguzi kati ya merikebu za Ulaya na jamii za Kiafrika za bara. Watu hao walikuwa *mestizos* (machotara) na Wakrioli wa mito ya Kasamansi, Guinea na Sierra Leone.

*Kutoka* lancados *wa Kireno hadi* mestizos *na* Wakrioli *wa mito ya Guinea na Sierra Leone*

Makundi ya machotara, yawe ya Waafrika-Wareno waliotokana na walowezi wa Kireno wa karne za kumi na tano na kumi na sita, au ya Waafrika-Waingereza walitokana na wafanya biashara wa Kiingereza katika karne za kumi na saba na kumi na nane, yaliunda jamii maalumu kabisa ambayo athari yake juu ya maendeleo ya kihistoria ya pwani ya kati ya Gambia na Sierra Leone ilikuwa ya mkataa.

Lancados *na Waafrika-Wareno:* Wageni wengi wa Kireno walimiminika kwenye Mito ya Kusini na visiwa vya Atlantiki (hasa Rasi Verde) kuanzia karne ya kumi na tano na kuendelea. Miongoni mwao walikuwa wafanya biashara majasuri, mawakala wa kampuni za biashara, na waliitwa *lancados*. Karibu wote walikuwa Wareno, japo katika kundi hilo walikuwemo pia Wagiriki, Wahispania na hata Wahindi wa kuhesabu. Waliajiri *grumetes* (wahudumu wa Kiafrika) na kuvinjari mabonde ya

mito ya Senegal, Gambia, Kasamansi na mito midogo ya Guinea. Wengi wao walilowea katika sekta za Kacheu na Geba ndani ya Guinea-Bissau ya leo.

*Lancados* mara wakajenga misingi ya jumuiya ya Waafrika-Wareno: wakaishi vijijini, na kwa kuwa waliishi karibu sana na watu weusi, wakajipatia wake wa Kiafrika au vimada. Lakini mtiritiko wa wahamiaji ukapungua katika karne ya kumi na saba na idadi ya Wareno menyu ikashuka chini ya ile ya machotara. Hawa *mestizos* wakaendelea kuwa weusi zaidi na zaidi kiasi cha kutoweza tena kutofautishwa na Waafrika menyu. Kufikia mwisho wa karne ya kumi na saba jumuiya ya Waafrika-Wareno ikawa na watu weupe wachache na weusi wengi, lakini iliongozwa na *mestizos* ambao waliipatia nduni kuu za kijamii-kitamaduni.

*Lancados* walikwishaunda kundi jipya la kijamii-kitamaduni kwenye pwani ya Afrika. Wakizungumza Kireno, wakivaa nguo za mitindo ya Kizungu, na wakiishi ndani ya nyumba zilizopakwa chokaa nyeupe; hata hivyo, walichukua baadhi ya desturi za Kiafrika kama vile kunakshi mwili kwa rangi na kuweka alama za kimbari. Walitekeleza ibada ya kipekee ya Kikatoliki ambapo sherehe za watakatifu wa Kikristo hazikuzuia kuabudu mizimu ya wahenga.

Awali *lancados* walijenga urafiki na watu wa pwani. Baadaye, baadhi yao walifungwa na mahusiano ya kidugu yaliyowaingiza katika maisha ya kijamii kisiasa na ya kitamaduni ya Waafrika. Hivyo Jose Lopez de Moura, mjukuu wa mfalme wa Kimane wa Sierra Leone, aghlabu alishiriki katika maisha ya kisiasa ya eneo hii. Wengine walikuwa Waafrika walioonjeshwa uzungu tu.

Kundi hili la Waafrika-Wareno lililipata nguvu zake kutokana na kazi yake kama tabaka la mawakala. Wanachama wake hawakufanya kazi yoyote ya kuzalisha bali walizipatia meli za Wazungu bidhaa na kuendelea na biashara ya msimu iliyohusiana na shughuli za kilimo za wenyeji Waafrika. Baadhi walikuwa matajiri wa kutosha kiasi cha kutojishughulisha na meli za Wazungu. Miongoni mwa familia za machotara, familia ya Bibiana Vaz ilitokeza kuwa mashuhuri ndani ya eneo la Kacheu katika karne ya kumi na saba. Jose Lopez de Moura alikuwa mtu tajiri kuliko wote katika Sierra Leone katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na nane.

Palikuwa na kutoelewana kati ya wafanya biashasha matajiri wa kichotara, wenye kuunga mkono biashara huria, na makampuni ya biashara yaliyopania kuhifadhi ukiritimba wao. Wafanya biashara Waafrika-Wareno walipigana kufakupona kutetea uhuru wao wa kufanya biashara mwambao. Hivyo, Kampuni ya Kifalme ya Kiafrika ilipojaribu kuvunja uhusiano kati ya watawala wa Kiafrika na machotara na kufutilia mbali dhima ya machotara ya ulanguzi, palitokea upinzani mkali. Machotara wakiongozwa na Lopez de Moura waliteketeza karakana ya kampuni ya Kiingereza na wala haikuweza tena kuanzisha upya shughuli zake katika Sierra Leone.

*Toka wafanyabiashara majasuri wa Kiingereza hadi Waafrika-Wangereza katika Sierra Leone*

Kundi jingine na machotara lilikuwa la Waafrika-Waingereza wa Sierra Leone. Mwishoni mwa karne ya kumi na nane waliunda kundi la karibu watu 12,000,

wakiwemo miongoni mwao akina Tucker Rogers, Corker na Cleveland, ambao walikuwa familia zenye kuongoza. Akina Tucker, Roger na Caulker (baadaye Corker) walikuja kutoka Uingereza katika karne ya kumi na saba na mwanzoni walijishughulisha na biashara ya makampuni ya Kiingereza. Walioa wake wa Kiafrika na kujipenyeza katika jamii ya wenyeji, ambako walihusishwa na tabaka tawala. Kama ilivyokuwa kwa Waafrika-Wareno, kundi la kijamii la mseto wa kitamaduni lilijitokeza ambamo mtu kama James Cleveland, ambaye mama yake alikuwa Mkisi, aliweza kutwaa nafasi muhimu katika jamii ya siri ya Waporo.

Kwa hivyo katika karne za kumi na saba na kumi na nane Waafrika-Wareno na Waafrika-Waingereza waliunda kundi la kijamii lenye kazi mahususi kiuchumi na kuandaa mazingira ya kitamaduni ambamo Wazungu na Waafrika walikutania. Lakini, wakiwa mahiri juu ya matilaba yao, waliwanyonya Waafrika na kuzoa faida ya juu kabisa, na ingawa waliasi dhidi ya ukiritimba wa makampuni ya biashara, walikuwa hata hivyo, mawakala katika huduma za ubepari wa biashara wa Ulaya.

*Biashara na watu kutoka* Grain Coast *(Pwani ya Nafaka) hadi* Tooth Coast *(Pwani ya Meno)*

Kuanzia Rasi ya Mesurado hadi Rasi Lahu, maendeleo ya biashara ya Wazungu katika karne za kumi na saba na kumi na nane hayakuzaa makundi ya biashara yoyote motomoto miongoni mwa watu wa Kru. Ingawa lilikuwa na uhusiano mdogo na Sudani ya bara, eneo hili la pwani hata hivyo lilijivunia vijiji vingi vilivyojengwa kwenye milango ya mito na kujaa mazao aina aina. Merikebu za Waholanzi na za Waingereza zilishughulikia pilipilli jinga katika Mto Sestos, Rasi Palmas na Cavally, na watumwa katika Bassa, Drewin na Saint Andrew; pembe za ndovu walizinunua kila mahala.

## *Hitimisho*

Licha ya matatizo ya asili katika kuandaa usanisi wa kihistoria, inaweza kuonekana kuwa kati ya miaka 1500 na 1800 watu na nchi za jimbo hili kwa jumla walipitia maendeleo ya aina moja. Kutoka kwenye hali ya kujitenga, polepole walichanganywa katika mitandao ya biashara ya dunia iliyojengwa na safari za Wazungu za Atlantiki, tangu safari kuu za upelelezi. Uchanganyikaji huu uliambatana na miguro ya watu kutoka bara hadi pwani, na mabadiliko makali ya kijamii na ya kisiasa kila mara watu walipojaribu kunufaika na fursa zilizotolewa na biashara ya Wazungu.

# 14


# *Madola na tamaduni za pwani ya Guinea ya Chini*

Kwa watu wa pwani ya Guinea ya Chini walioishi katika eneo kati ya Cote d'Ivoire na Benin ya leo, au kati ya mito Bandama na Mono, kipindi kati ya 1500 na 1800 yawezekana kilikuwa cha kimapinduzi kuliko vipindi vyote katika historia yao. Kilishuhudia, awali kabisa, kukamilika kwa hajira za watu hawa na uundaji wa karibu makundi yote ya kimbari-kiisimu yaliyopo leo. Pili, kiliona ushadidishaji wa mahusiano ya kibiashara na ya kitamaduni kati ya watu hawa na wale wa Sudani ya Magharibi, Sahara na Maghrib, na uwezekano mpya wa kuwa na mahusiano ya kuvuka Atlantiki - kwanza na Ulaya na baadaye na makontinenti ya Amerika. Tatu kiliona ugatizaji (uunganifishaji) polepole wa madola na uzukaji wa makundi makubwa zaidi ya kisiasa. Mwisho, kipindi hiki kilikuwa ni cha mageuzi ya kijamii na kitamaduni.

## *Hajira na uundaji wa makundi mapya ya kimbari-kiisimu*

Mwaka 1500, karibu watu wote walikuwa bado wanaishi katika sehemu zao mbalimbali za asili na wachache tu walikwisha jipenyeza katika baadhi ya maeneo ambamo wanaishi leo. Nyendo zao za kuhama zilitokea kati ya 1500 na 1800, hasa katika karne ya kumi na saba na miongo ya mwanzo ya karne ya kumi na nane. Kutokana na sababu za kiuchumi, za kijamii na zaidi ya yote za kisiasa, Waakan, Wa Ga-Adangbe na Waewe walianza kusambaa katika koo ndogondogo na makundi ya nasaba.

Katika karne ya kumi na sita, Waakan walihamia kwanza kaskazini na mashariki hadi katika maeneo ya Kumasi ya leo, Mampong na Akyem, na baadaye kusini na kusini-magharibi hadi katika maeneo ya Wassa, Igwira, Sanwi na Assini. Katika karne ya kumi na saba, Waakan wengine walihama kwa makundi mbalimbali ya koo za umama na kwenda kaskazini na kaskazini magharibi, na pia kusini magharibi hadi Wassa na Sefwi na maeneo ya Wangwa ya Cote d'Ivoire. Kati ya 1680 na 1730 palikuwa na uhamaji mkubwa, hususa wa Waakan kuingia Nzima, Aowin, Sefwi, Ahafo na maeneo ya Bono kaskazini na maeneo ya Anyi na Baule ya Cote d'Ivoire. Hadi katikati ya karne ya kumi na nane, mmiminiko wa Waakan yaelekea ulikuwa umekauka.




14.1 *Waakan, Waga na Waewe*

Waga waliendelea kusambaa kuelekea pwani, wakivutwa na kuwepo kwa Wazungu na fursa za kiuchumi zilizojitokeza hatimaye. Waga-Mashi, Wanungua na Watema walikuwa watu wa kwanza kuhama katika karne ya kumi na sita, wakifuatwa katika karne ya kumi na saba na Waosu na Wateshi. Jamaa zao, Waadangbe, pia walianza kutawanyika kusini na kaskazini kwenye uwanda wa Akkra wakati wa karne za kumi na sita na kumi na saba.

Hajira zilizotia fora, hata hivyo, zilikuwa ni zile zilizowahusu Waewe. Mwishoni mwa karne ya kumi na sita au mapema katika karne ya kumi na saba, ili kuepuka utawala katili wa mfalme wao, Agokoli, Waewe waliondoka Notsie katika makundi mawili makuu, Waewe wa kusini na Waewe wa kaskazini au bara. Kundi la kusini lilielekea pwani na makundi ya kaskazini kutwaa sehemu ya kati na ya kaskazini ya Jimbo la Volta ya Kusini ya sasa. Vijikundi kadha vilijiengua mara na kuanzisha makazi mengine, na mchakato huu wa kujitenga na kuungana uliendelea muda wote wa karne za kumi na saba na kumi na nane.

Watu hawa hawakutawanyika na kuhama tu; bali pia walikumbwa na mabadiliko ya kimbari-kiisimu. Waewe na Waga-Adangbe, waliohamia katika maeneo yenye watu wachache sana waliweza kuendeleza umenyu wa mbari na lugha zao. Wengi wa Waakan, hata hivyo, walihamia katika maeneo yenye wakazi wengi sana wenye kusema lugha tofauti tofauti. Mchanganyiko wa watu hawa na Waakan wahamiaji ulichipuza, miongoni mwa mengine, makundi ya Wambalo, Waalladian, Waebrie, Waeotile na Wavikam - wote hawa wanajulikana kwa jina la jumla la Walagunaire. Halikadhalika, mchanganyiko wa wahamiaji wa baadaye wa Kiakan na baadhi ya watu walioishi kabla ndio uliozaa Waanyi, Wabaule na Wasefwi. Kwa hiyo, Waakan wakagawanyika katika makundi mawili mapana ya leo, Waakan wa Mashariki na Waakan wa Magharibi. Kila moja ya makundi haya likagawanyika zaidi: Kundi la Akan Mashariki, likagawanyika katika Waasante, Waakuapen, Waakyem Waakwamu, Wabron, Wawassa, Wakwahu, Wafante, Waassin, Wadenkyira na Wagomua, wote wanasema lugha moja, Kitwi. Waakan wa Magharibi waligawanyika katika Waanyi, Wabaule, Wanzima, Waahanta, Wasanwi, Waaowin na Wasefwi – makundi haya yanasema lahaja za Kiakan zinazoeleweka na wote.

Katika karne ya kumi na sita, asasi za kijamii kisiasa za makundi haya katika makazi yao mapya zilionyesha mifanano na mifarakano pia. Waga-Adangbe na Waewe waliishi katika makazi huru yaliyotawanyika, katika makundi ya koo za kuumeni. Katika kila kundi, kila nasaba ilikuwa na mungu wake mwandamizi ambaye makuhani wake walikuwa viongozi. Hata hivyo, kufikia mwisho wa karne ya kumi na tano Waga-Mashi walikwisha jipatia mfalme, aliyekuwa na baraza lake huko Ayawaso.

Waakan waliishi katika miji iliyotawaliwa na wafalme na malkia na vijiji vilivyotawaliwa na machifu. Kila mji au kijiji kilikaliwa na familia zilizogawanyika katika koo nane za umama. Kila familia ilikuwa na *abusuapanin* (mkuu), hali kadhalika kila ukoo. Inaelekea kila familia au ukoo ulikuwa na mungu au miungu

yake, kama ilivyokuwa kwa kila kijiji, na kwamba makuhani wao walihodhi madaraka mengi. Kwa maana nyingine, jamii ilikwisha gawanyika katika matabaka mapana matatu: tabaka la watawala wa kikabaila la makuhani na wafalme, tabaka la raia wa kawaida, na tabaka la watumwa wachache wa nyumbani. Muundo huu wa kijamii ulibadilishwa sana na maendeleo ya kisiasa na ya kiuchumi ya kipindi cha kati ya 1500 na 1800.

## *Mabadiliko ya kiuchumi katika Guinea ya Chini*

Mabadiliko makubwa sana, ya ndani na ya nje, yalitokea ndani ya Guinea ya Chini katika kipindi hiki. Ndani, shughuli za uchumi zilizokwisha anzishwa ziliendelezwa na kupanuliwa. Hizi zilikuwa ni pamoja na ukusanyaji, ukulima, ufugaji, uwindaji, uvuvi utengenezaji chumvi na uchimbaji dhahabu. Zao kuu lililokusanywa lilikuwa kola katika eneo la msitu la Gold Coast. Kola hizi zilikuwa uti wa mgongo wa biashara kati ya Waakan na kaskazini na magharibu ya Sudani.

Mazao makuu yalikuwa ndizi, viazi vikuu na mchele. Katika karne za kumi na saba mazao mapya yaliyoingizwa kutoka Asia na Amerika na Wazungu, yaliongezwa kwenye yale ya asili, yakiwemo mahindi, mihogo, aina mbalimbali za viazi vikuu, nyanya, vitunguu, biringani, maparachichi, viazi vitamu, matunda ya jamii ya machungwa na karanga. Upokeaji wa haraka wa mazao haya uliufanya uchumi wa kilimo wa pwani ya Guinea uwe anuwai, na hivyo kuharakisha ongezeko la watu.

Ufugaji wanyama ulihusu kuku, kondoo, mbuzi na nguruwe. Uvuvi ulikuwa shughuli kuu ya uchumi ya Waewe, Waga na watu wengine wa pwani. Uwindaji ulikuwa shughuli ya watu wote.

Utengenezaji chumvi na uchimbaji dhahabu uliongezeka umuhimu wake kati ya 1500 na 1800. Karibu chumvi yote ilizalishwa na wakazi wa pwani, ambapo uchimbaji dhahabu ulikuwa mradi teule wa watu wa msituni bara, hasa Waakan. Ilipatikana kwa kuchekecha madongo ya kitope au kwa uchimbaji wa kina (*nkoron*). Uchimbaji dhahabu ulidhibitiwa vikali na dola na ulikuwa chanzo kikuu cha mapato ya watawala. Uchimbaji ulifikia kilele chake katika karne ya kumi na saba na kubakia mradi kiritimbi wa Waakan, licha ya juhudi za Wazungu - hasa Waholanzi, za kushiriki ndani yake moja kwa moja.

Sambamba na shughuli hizi, biashara iliendelea, na dhima ya watumwa katika biashara hiyo iliongezeka. Ni muhimu kutofautiasha biashara ya ndani na biashara ya nje. Waewe, Waga na Waakan walikwisha fanya biashara miongoni mwao kwa muda mrefu. Samaki na chumvi ilizalishwa na Waewe, Waga na Wafante, na vyombo vya ufinyanzi vilibadilishwa na dhahabu na vijiti vya mswaki (*tweopea*), pembe za ndovu na chuma na bidhaa nyingine za metali zilizotengenezwa na Waakan wa bara. Matawi mawili ya biashara ya nje yalianzishwa: moja, la tangu zamani, la biashara ya savana na Sudani magharibi, na jingine, la kuvuka Atlantiki, la biashara ya Ulaya na Amerika. Waewe, Waga na Waakan walikwisha jenga mahusiano ya kibiashara na Waguan na Wagur upande wa kaskazini, Wahausa wa Nigeria ya kaskazini upande

wa kaskazini-mashariki, na Wamande wa pindi la Niger upande wa kaskazini magharibi; waliuziana dhahabu, kola, vitambaa, watumwa na chumvi. Kuinukia na kupanuka kwa Songhai katika karne za kumi na tano na kumi na sita kulistawisha biashara kati ya Waakan na Wamande. Ili kuidhibiti biashara hii vyema, Wajuula walijenga vituo kadha vya biashara au vya kuondokea kama Bobo-Diulasso, Kong, Bonduku, Buna na Begho kati ya pindi la Niger na nchi zenye kuzalisha dhahabu za kusini. Miji ya Jenne na Begho, mapitio makuu ya biashara ya kaskazini-magharibi, ilitajirika sana katika karne ya kumi na sita, kama inavyothibitishwa na vyanzo vya maandishi na vya akiolojia. Katika masoko ya kaskazini magharibi, Waakan walibadilisha zaidi dhahabu, kola na, baadaye, bidhaa zilizoingizwa na Wazungu kwa nguo, mablangeti, mazulia ya Kituruki, vitambaa vya hariri ya milia na buluu, bidhaa za ngozi, vyombo vya chuma, vifaa vya sufuri (shaba nyeupe) na chumvi.

Kupinduliwa kwa Songhai mwishoni mwa karne ya kumi na sita, na ukosefu wa usalama uliofuata, kwanza ulifikiriwa kuwa uliharibu biashara kwenye njia za kaskazini-magharibi. Lakini sasa imekwisha onyeshwa wazi wazi kuwa biashara hiyo haikushuka, na hasa iliongezeka, katika karne ya kumi na nane.

Biashara kati ya Waakan na nchi ya Hausa na Borno pia iliendelea. Ilikwisha kuwa na umuhimu wa kiasi mwanzoni mwa karne ya kumi na sita, kama ilivyoshuhudiwa na maelezo ya Leo Africanus, aliyetembelea Songhai na nchi ya Wahausa wakati huo. Kasi yake iliongezeka katika karne za kumi na saba na kumi na nane, sambamba na kukua kwa madola ya Wamole-Dagbane ya Mamprusi, Dagomba, Nanumba na Mossi na madola ya Wahausa. Miji kama Kano na Katsina, ya Uhausa, na zaidi ya yote Salaga, ulioko kaskazini mwa Gold Coast, ilitajirika sana. Usafirishaji wa dhahabu wa Waakan kwenda Uhausa yaelekea ulisimama katika karne ya kumi na nane, labda kutokana na ushindani mkali wa Wazungu, lakini kola za Akan ziliendelea kuwa uti wa mgongo wa biashara na kaskazini-mashariki. Kola zilisafirishwa toka Uhausa na Borno hadi Sahara na katika madola ya Wabarbari.

Uhusiano muhimu zaidi wa biashara, hata hivyo, ulikuwa unaendelezwa pia mahali pengine: biashara ya kuvuka Atlantiki kati ya pwani ya Guinea ya chini na Ulaya na makontinenti ya Amerika. Ulianza Wareno walipotia nanga nje ya pwani ya Ghana ya leo mwaka 1471. Walifuatwa katika karne ya kumi na sita na Wafaransa, Waingereza na Waholanzi, na katika karne ya kumi na nane na Wadeni. Biashara ya moja kwa moja na West Indies ilianza mwaka 1518, shehena ya kwanza ya watumwa ilipopelekwa huko katika merikebu ya Wahispania. Biashara na bara la Amerika ya Kaskazini ilianza mwaka wa 1619 manowari ya Kiholanzi iliposhusha shehena ya kwanza ya watumwa wa Afrika Magharibi huko Jamestown katika jimbo la Virginia. Hivyo kufikia katikati ya karne ya kumi na saba, biashara ya pembe tatu yenye kuunganisha pwani ya Guinea, Ulaya na Amerika ilikwisha stawishwa kabisa.

Bidhaa walizouziwa Wazungu zilitofautiana toka ukanda hadi ukanda, na toka karne hadi karne. Mpaka mwishoni mwa karne ya kumi na saba Waakan wa kati ya mito Bandama na Ankobra waliuza zaidi pembe za ndovu kwa Wazungu, ambapo

Waakan na Waga walioishi baina ya Ankobra na Volta waliuza dhahabu zaidi. Kwa karne nzima ya kumi na sita, inaeleka kulikuwa na biashara haba kati ya Waewe na Wazungu kwenye eneo kati ya mito ya Volta na Mono. Waholanzi na Wadeni hawakuanza kufanya biashara huko hadi katikati ya karne ya kumi na saba, na bidhaa kuu ilikuwa watumwa. Kutokana na ubobezi huu, wafanyabiashara wa Kizungu wakaingia pwani ya Guinea ya Chini katika Ivory Coast, Gold Coast na Slave Coast (Pwani ya Watumwa).

Hadi mwisho wa karne ya kumi na saba, biashara ya dhahabu ilikuwa ndiyo muhimu kabisa. Ilishinikiza kila taifa la Ulaya kuweka mizizi kwenye pwani hii, na matokeo yake idadi kubwa ya ngome na kasri kubwa zilijengwa pwani pwani kati ya mito ya Ankobra na Volta.

Hata hivyo, kati ya 1650 na 1800 biashara ya nje kati ya Waga na Waakan wa Mashariki na Ulaya ilikumbwa na mabadiliko ya kimapinduzi. Kuanzia katikati ya karne ya kumi na saba, Waga na Waakan walianza kusafirisha watumwa kwa idadi yenye kuongezeka kiasi kwamba kufikia 1710 biashara ya watumwa ilizidi ile ya dhahabu. Idadi ya watumwa iliyosafirishwa kutoka Gold Coast iliendelea kuongezeka kwa kipindi chote cha nusu ya kwanza ya karne ya kumi na nane. Kwa mujibu wa K.Y. Daaku, watumwa 5000 - 6000 walikuwa wakisafirishwa kila mwaka kufikia mwisho wa karne ya kumi na saba, na idadi hii ikapanda hadi 6000 - 7000 katika karne ya kumi na nane. Kwa mujibu wa P.D. Curtin, jumla ya watumwa 474,000 walisafirishwa kutoka Gold Coast katika karne ya kumi na nane, lakini inaaminika na wengi kuwa makadirio ya Curtin ya idadi ya watumwa kutoka Afrika Magharibi yalikuwa pungufu kwa asilimia kati ya 7.3 na 18.4. Eneo la Waewe nalo lilisafirisha idadi kubwa ya watumwa, hasa baada ya mwaka 1730, Waakwamu walipovamia jimbo hilo.

Kwa nini biashara ya watumwa iliizidi biashara ya dhahabu huko Gold Coast? Swali hili lina majibu matatu makuu. La kwanza ni ongezeko kubwa la mahitaji ya watumwa kufuatia na kuanzishwa kwa mashamba ya miwa huko West Indies na bara ya Amerika kuanzia miaka ya 1640 na kuendelea. Jibu la pili ni kuongezeka sana kwa idadi ya mateka wa vita. Sababu ya tatu ni kwamba baada ya kuimarika kwa himaya za Denkyira, Akwamu na Asante, madola ya vibaraka yalilipa kodi kwa njia ya kuwasilisha watumwa. Yafaa kuongezea kuwa kutoa watumwa kwa Wazungu katika Gold Coast ulikuwa ni mradi waliojitengea Waafrika wenyewe.

Maduhuli katika Guinea ya Chini pia yalipata mabadiliko ya kimapinduzi katika wingi na ubora wake. Mwishoni mwa karne ya kumi na tano na kwa karne nzima ya kumi na sita, bidhaa kuu zilizoingizwa zilikuwa ni nguo, nyingi zikiwa zimetengenezwa si Ulaya bali katika madola ya Barbari, Benin na Cote d'Ivoire. Vitambaa kutoka Benin na nguo za *Quaqua* kutoka Cote d'Ivoire zilipendwa sana, na kwa hakika ziliendelea kuagiziwa katika karne ya kumi na saba, lakini wakati huu orodha ya bidhaa zinazoingizwa ilikwisha refushwa sana. Pieter de Marees, akiandika mwanzoni mwa karne ya kumi na saba, anatoa orodha iliyojaa ya bidhaa

zilizoletwa na Waholanzi na kuhitimisha kuwa vifaa vilivyokuwa vinatafutwa sana vilikuwa ni nguo za kitani, vifaa vya sufuri na kupri (shaba nyekundu), mabeseni, vyungu, visu na marijani.

Orodha hii haitaji bunduki, kwani uingizaji bunduki na baruti ulianza kwa dhati katika miaka ya 1640 tu, Waingereza na wadukizi walipoanza kuuza silaha pwani. Mwaka 1660 Waholanzi waliondoa amri ya kuzuia usafirishaji wa silaha nje ya nchi na kuanza kuzisafirisha kwa wingi. Shehena ya silaha zilizosafirishwa iliendelea kuongezeka kipindi chote cha karne ya kumi na nane. Silaha ziliendelea kuwa bidhaa yenye kutafutwa sana katika Gold Coast na kuishia kuwa mhimili wa biashara ya Waingereza na Afrika Magharibi.

## *Athari za maendeleo ya kiuchumi*

Moja ya athari za kwanza za mabadiliko ya kiuchumi ilikuwa ni kutokea kwa mtandao changamano wa njia kuu na ndogo. Njia hizi kwanza ziliwaunganisha watu wa eneo hilo wenyewe kwa wenyewe, halafu zikawaunganisha na Wamole-Dagbane na Wahausa upande wa kaskazini-mashariki, Wamande kaskazini-magharibi na madola ya Wabarbari na ulimwengu wa Waislamu kuvuka Sahara. Hatimaye mtandao ulienea kwenye Atlantiki, kwanza kuelekea Ulaya halafu Amerika. Mji wa Kumasi ulikuwa kitovu cha mtandao huu.

Idadi kadhaa ya vituo vya mjini vilistawi kwenye njia hizi. Hivi vilikuwa ni pamoja na Kong, Bono-Diulasso, Buna Begho na Bonduku upande wa kaskazini-magharibi, Salaga, Yendi na Sansanne-Mango katika kaskazini-Mashariki na Tiassale, Sakasso, Krinjabo, Kumasi, Kete-Krachi na Akwamufie upande wa kusini. Vituo hivi vilitumiwa kama mapitio, magulio, na mafikio. Zaidi ya hayo, kuwapo kwa Wazungu kuliharakisha kukua kwa miji ya pwani dhidi ya miji ya zamani ya mrima.

Athari ya mtandao mpya ulioanzishwa na Ulaya ilikuwa ni kuiingiza pwani ya Guinea ya Chini katika eneo kubwa zaidi la uchumi lililoundwa na nchi za Ulaya ya magharibi na Amerika kwa upande mmoja na ulimwengu wa Wamande-Wahausa-Waislamu kwa upande mwingine. Hata hivyo, uhusiano huu wa mwisho ulidhoofika polepole wakati uhusiano na Ulaya na Amerika uliendelea kuwa na nguvu zaidi na zaidi.

Athari ya kuingizwa katika mtandao huu ilikuwa ni uvunjaji au udhoofishaji wa maendeleo ya uchumi na ya viwanda katika Guinea ya Chini. Biashara ya watumwa – biashara ya kinyama kuliko zote – bila kutaharaki ilichukua nafasi ya biashara ya mazao ya asili, ikiliondoshea jimbo wafanyakazi wa msingi pamoja na wengi wa wasanii na wasani wake. Zaidi ya hayo, Ulaya ilisafirisha bidhaa rahisi kwa matumizi y a wengi, hivyo kuua karibu viwanda vyote vilivyokuwepo au kuviza sana ukuaji wake. Kwa muhtasari, kati ya 1500 na 1800 kulikuwa na ukuaji wa uchumi katika Guinea ya Chini lakini bila maendeleo ya kiuchumi. Zaidi, kwa kuwa Ulaya

ilidhibiti maduhuli na mahuruji ilijilimbikizia karibu faida yote. Humu ndimo ilimosimikwa mizizi ya mchakato wa kuvia, uliokuzwa katika karne ya kumi na tisa na ukomeshaji wa biashara ya watumwa na kuanzishwa kwa ukoloni katika Afrika.

## *Mabadiliko ya kisiasa kwenye upwa wa Guinea ya Chini*

Mabadiliko ya kisiasa yalikuwa makali zaidi kuliko mabadiliko ya kiuchumi kati ya 1500 na 1800. Hadi 1500 mchakato wa kuunda dola ulikwishaanza na madola kadhaa yalikwisha ibuka pwani na katika jimbo la savana. Wareno walifika (na) kukuta madola ya Ahanta, Shama, Aguafo, Fetu, Asebu, Agona na Akkra, pia yalikuweko madola ya Mole-Dagbane na dola la Akan la Bono ndani ya ukanda wa savana. Mchakato uliendelea kupata nguvu wakati ufalme wa kwanza wa Akan, Bono, ulipoibuka katika nusu ya pili ya karne ya kumi na tano na kufikia upeo wake kupitia biashara yenye faida kubwa kati ya Wamande na Waakan. Katika karne ya kumi na sita, Waga-Mashi, Wanungua na Watema waliungana na Walabadi na Waosu kwenye uwanda wa Akkra, na kuanzisha makazi mengi. Hadi karne ya kumi na nne, Waga waliwatumia makuhani kama machifu, lakini mwishoni mwa karne iliyofuata ufalme usiokuwa wa kidini ulikwishaanza, pengine kutokana na kuwaiga majirani zao wa Akan na Adangbe. Mwanzoni mwa karne ya kumi na saba baadhi ya Waga walihamia Pwani, wakivutiwa na kuwapo kwa Wazungu, nao walifuatwa na Wala na Waosu. Miji yote ya pwani waliyoanzisha ilitambua utawala wa *mantse* (mfalme) wa Waga, na Ayawaso ulibakia mji mkuu wa ufalme hadi 1680, ulipohamishiwa pwani.

Kinachoelekea kuwa kilitokea miongoni mwa Waakan katika karne ya kumi na sita ni kuundwa, katika bonde la Pra-Ofin, kwa idadi kadha ya jumuiya ndogondogo na madola ya miji au temi ambazo hazikuunganishwa na utii kwa ufalme mmoja, bali na pingu za udugu, ubaba na ukoo. Hata hivyo, inadhihirika kutokana na mapokezi simulizi ya Adansi kuwa, mnamo 1550, palikuwa na jaribio la ugatizaji mamlaka lililosababisha kuundwa kwa shirikisho la madola na pia kuanzisha hajira ya baadhi ya Waakan kuelekea kaskazini na kusini walikoanzisha temi, madola ya miji na tawala za wanamfalme.

Mchakato huu wa kuunda madola unaelekea ulichapuka kati ya 1580 na 1630, kama inavyoonyeshwa na ramani ya madola ya Gold Coast ya kusini kati ya mito ya Tano na Volta iliyochorwa na mchoraji wa Kiholanzi mwaka 1629. Ramani hii inaelezea madola thelathini na nane na falme. Yote isipokuwa Inkassa Kuu na Iakassa Ingwira yamekwisha tambuliwa na bado yamo katika maeneo yale yale.

Madola yaliyoanzishwa na Waga na Waakan waliohama yawezekana yalikuwa madogo lakini yalikuwa na muundo mmoja, na kiongozi mmoja, chifu au mfalme, na malkia wake. Katika shirikisho la Adansi madaraka yalizunguka miongoni mwa familia za kifalme za madola mbalimbali. Ndani ya kila dola, mfalme alichaguliwa kutoka familia au ukoo wa kwanza kufika katika eneo hilo. Alishauriwa na baraza la wakuu wa familia na wa koo. Kila dola lilikuwa na miungu yake, kwa mfano mito,

maziwa au majabali, na makuhani wao walikuwa na athari kubwa sana katika jamii.

Kati ya 1630 na takriban 1670, matukio makubwa mawili yalitokea katika maeneo ya Ga na Adangbe: kuimarika kwa madola yanayoonyeshwa kwenye ramani ya 1629, na kutokeza kwa madola mapya. Vyanzo simulizi vinaonyesha kuwa falme kama Akwamu, Denkyira, Akkra au Ga, Fante, Wassa na Adom zilipanua sana mipaka yao, zaidi kwa njia za amani. Ufalme wa Ga ulifikia upeo wa upanuzi wake na kilele cha mamlaka yake chini ya mfalme Okai Akwei (1640 -77).

Katika kipindi hiki dola la Aduana la Akwamu pia lilikuwa ufalme imara ambapo Denkyira ilijitenga na Shirikisho la Adansi baada ya msururu wa vita na kujisimika imara kwenye ndagano ya mto Ofin na mto Pra. Huko pwani Wafante pia walipanua nchi yao, na kumbukumbu za Ulaya zinagusia mara kwa mara vita kati ya Wafante na Waetsi upande wa kaskazini.

Vita vya Wadenkyira-Waadansi (1650-70) na vya Wabono vilichapusha uhamiaji kusini na magharibi hadi msituni ambako watu wa zamani kama Waadisi, Waewotre, Waagwa, Wakompa na Walagunaire waliishi. Makundi haya mapya hayakuanzisha Aowin tu, karibu na Wassa Amanfi, bali walianzisha pia madola matatu ya Sefwi kusini, madola kama Assini, Abripikwem na Ankobra, na idadi kubwa ya miji ya pwani. Ikiwa katika moja ya maeneo tajiri sana ya dhahabu, na kwenye njia kuu ya biashara yenye kukutanisha masoko ya kaskazini na pwani, Aowin, kufikia miaka ya 1670, ilikwisha kukua na kuwa ufalme tajiri na wenye nguvu sana.

Wahamaji wa Denkyira-Adansi waliohamia upande wa kaskazini walianzisha madola ya Oyoko yakiwemo Kumasi, Kokofu, Dwaben, Nsuta na, baadaye, Bekwai, na madola ya Bretuo ya Mampong na Afigyaase, yote yakiwa ndani ya kipenyo cha kilomita hamsini cha Kumasi. Kaskazini zaidi, wengine walianzisha dola la Aduana la Gyaaman au Abron.

Madola mapya yaelekea yaliundwa kwa misingi ileile ya madola ya zamani. Madola ya Sefwi na Aowin, kwa mfano, yaliingiza mfumo mpevu wa ukoo wa Akan, na asasi za kifalme ambazo wafalme wake walichaguliwa kupitia kukeni, kwenye muundo wa kijamii-kisiasa uliotegemea *asago* (wapiganaji) waliounda vikosi cha kimaskani.

Hata hivyo, katika miaka thelathini ya mwisho ya karne ya kumi na saba, mapinduzi ya kisiasa yalitokea, yakiashiriwa siyo na uibukaji wa madola mapya bali na ongezeko la ugatizaji wa yale yaliyopo. Aowin na Denkyira yaelekea ziliongoza katika mabadiliko haya. Aowin iliyateka madola ya Sefwi yaliyo kaskazini na magharibi, na kupanukia magharibi ya mbali kutwaa miji kama Keteso, Yawu, Brako na Sikasso ndani ya Cote d'Ivoire ya sasa.

Katika miaka ya 1670 na 1680, watawala wa Agona na Denkyira waliteka madola yote ya Waadensi pamoja na madola ya kabla ya Asante yaliyopo karibu na Kumasi upande wa kaskazini, na karibu na Assin na Twifo upande wa kusini. Kati ya 1686 na 1690, Demkyira iliishinda Aowin, madola ya Sefwi na Wassa upande wa kusini magharibi, na falme za pwani za Adom na Fetu. Kufikia 1690, Denkyira iliitawala

kusini magharibi ya Gold Coast, na sehemu za Cote d'Ivoire.

Katika majimbo ya kusini-mashariki viongozi wa Akwamu pia walikuwa wanaandama vita vya upanuzi. Kwanza waliushambulia ufalme wa Ga, na kuuteka mwaka 1681. Halafu waliuteka ufalme wa pwani wa Agona upande wa magharibi mwaka 1689. Katika kampeni zao za mwisho (1702-10), waliyateka madola ya Adagbe upande wa mashariki na Kwahu kaskazini na, baada ya kuvuka mto Volta, wakayashinda madola ya Waewe ya Peki, Ho na Kpandu.

Wadenkyira na Waakwamu walitumia utaratibu uleule kutawala himaya zao. Kila nchi iligawiwa sehemu mbili, eneo la mjini na eneo la mashambani. Eneo la mjini lilizunguka makao makuu, makazi ya *omanhene* (mfalme), aliyetawala himaya yote. Chini yake kulikuwa na msururu wa maofisa au wafalme waliotekeleza shughuli fulani barazani. Kwa madhumuni ya kisiasa - kijeshi, kila dola liligawanywa katika vikosi, vikosi vitatu katika Denkyira na vitano katika Akwamu. Kila kikosi kiliongozwa na mfalme wa mji au dola katika eneo la mjini au katika makao makuu yenyewe. Alikuwa na mamlaka ya kisiasa juu ya kikosi hiki wakati wa amani, na alikuwa *asafohene* (kiongozi wa jeshi) wakati wa vita. Viongozi wote wa vikosi walikuwa wajumbe wa baraza lililomshauri *omanhene*. Maeneo ya mashambani yalikuwa ni pamoja na madola yote yaliyotekwa ambayo sasa yalikuwa sehemu ya himaya. Kila dola liliendelea kutawaliwa na mfalme wake lakini lilidhibitiwa moja kwa moja na *omanhene* au mkuu wa kikosi. Kila dola lilitarajiwa kulipa kodi ya mwaka na kupigana vitani chini ya mkuu wa kikosi.

Wanahistoria wengi wameitazama historia ya kisiasa ya Gold Coast katika karne ya kumi na nane zaidi kwa kuzingatia kuibuka kwa himaya ya Asante tu, lakini mkondo wa maendeleo ya kisiasa ulikuwa changamani zaidi. Kwanza, madola mengine yalianzishwa nje ya himaya ya Asante. Pili, kulikuwa na kufufuka, ingawa kwa muda mfupi, kwa Aowin, na matukio ya Akyem kuipindua Denkyira na Asante kuipindua Akwamu. Tatu, kulikuwa na upanuzi wa ufalme wa Fante katika mapana yake yote na, mwisho, uibukaji wa kushangaza wa himaya ya Asante.

Madola mapya kabisa yaliyozuka katika karne ya kumi na nane yalikuwa Nzima, madola ya Kiaowin au Kianyi ya Sanwi, Ndenye, Diabe, Maronou na Bettie, na temi nyingi za Kibaule za wana mfalme. Baada ya kushindwa na Wadenkyira katika miaka ya 1680, Waaowin, au Waanyi, waliondoka Anwianwia na, baada ya kuvuka mto Tano, wakaunda upya ufalme wao eneo la Enchi. Walikuwa bado wanajizatiti Waasante walipowashambulia mnamo 1715. Baadhi yao walihamia magharibi walikoanzisha ufalme wa Sanwi. Baada ya kujenga makao makuu yao hapo Krinjabo mara waliishika Assini, hivyo wakadhibiti biashara kati ya bara na wangwa ya Abi.

Kaskazini mwa Sanwi yaliibuka madola mengine ya Kianyi: Ndenye na Diabe, yaliyoanzishwa na kundi la wakimbizi kutoka Anwianwia lililohamia kaskazini-magharibi. Hadi karibu na 1715, Waanyi wa Ndenye walikula kiapo cha utii kwa Aowin, lakini sehemu yao walikataa kukubaliana na hili na wakaondoka kwenda kuanzisha ufalme wa Bettie. Baadhi ya Waanyi, Wamonfwe, walivuka Mto Komoe

na kuanzisha ufalme wa Moronou.

Kaskazini-magharibi ya Anyi, kati ya mito Komoe na Bandama, kulizuka pia, katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na nane, utitiri wa nchi za wanamfalme au temi. Mapokeo simulizi ya waanzilishi yanaonyesha kuwa walifika kutoka Gold Coast katika mawimbi mawili tofauti. Wimbi la kwanza liliwaleta Waalanguira Baule karibu na mwaka 1700. Walikuja kutoka Denkyira baada ya nchi hiyo kushindwa na Waasante, wakasakini katika eneo la mkoa wa Agba ya leo. Kutoka hapo wengine waliendelea magharibi ili kuishi miongioni mwa Waguro na Wakoro.

Wimbi la pili, kubwa zaidi, la Waasabu, lilitoka Kumasi kufuatia urithi uliobishaniwa baada ya kifo cha Osei Tutu mwaka 1717. Kufuatana na mapokeo simulizi yao, waliongozwa na malkia wao Abla Poku, aliyemtoa mhanga mwanae kwa mzimu wa Mto Komoe kabla ya kuvuka, ndipo lilipotokea jina lao la *Baule* (mtoto mchanga amekufa). Kundi liligawanyika, lakini walio wengi, wakiwa bado wanaongozwa na Abla Poku, walivuka mto Bandama na kwenda kuishi karibu na Bwake. Akwa Boni, aliyemrithi Abla Poku, aliweza kusimika mamlaka yake juu ya Wabaule, Wamalinke, na Wamande waliokuwa wanakalia jimbo la Warebo. Hata hivyo, baada ya kifo chake ufalme uligawanyika katika temi huru. Makundi yote mawili ya wavamizi mara walichanganyika na Waguro, Wamalinke, Wasenufo na Wagoli kuunda taifa la Wabaule wa leo.

Ufalme wa Nzima ulioibuka pia kipindi hiki, ulianzishwa na ndugu watatu ambao waliunganisha chini ya utawala wao madola matatu ya zamani ya Jomoro, Abripikwem na Ankobra kwa kutumia utajiri walioupata kutokana na kufanya biashara na Wazungu. Likijulikana katika rekodi za Wazungu kama Apollonia, dola hili jipya lilitawala kona ya kusini-magharibi ya Gold Coast kipindi chote cha karne ya kumi na nane.

Wakati huohuo, baadhi ya madola ya zamani, kama Bron, Sefwi-Wiawso, Aowin na Fante yalikuwa yanatanua mamlaka na athari zao. Aowin, kwa mfano, laonekana kujirudishia uhuru wake toka Denkyira katika miaka ya 1690. Likisaidiwa sana na wakimbizi wenye kukimbia vita vya Asante-Denkyira, lilikuja kutawala madola ya Sefwi na kuandama kuteka maeneo yenye kuzalisha dhahabu na kutoa pembe za ndovu upande wa kaskazini. Aowin ilipata nguvu nyingi kiasi kwamba mashujaa wake walivamia Asante kunako 1718-19, wakachakaza makao makuu, Kumasi, na kurudi nyumbani na ngawira na mateka, pamoja na baadhi ya jamaa wa familia ya kifalme ya Asante.

Pia mwanzoni mwa karne ya kumi na nane, dola la Bron lilipanua sana nchi yake kwa njia ya kuteka. Taifa jipya la Bron lilikuwa la aina yake, likiwa limeundwa kutokana na mchanganyiko wa watu wa makabila ya Waakan, Wakulango, Wanafana na Wamande. Wavamizi wa Kiakan, waliotawalia dola kisiasa, walihifadhi koo zao, mfumo wao wa kurithisha kwa umama, mfumo wao wa sheria na vipengele vya dini yao ya jadi. Lakini hawakugusa kabisa miundo ya kijamii na maongozi ya kisiasa ya Kikulango na Kinafana katika ngazi ya shamba na kijiji. Mwisho, baadhi walipokea

Uislamu, ulioingizwa na Wamande-Jula, ambao pia waliathiri sana mfumo wa uchumi wa ufalme.'

Ilikuwa pia kati ya 1700 na 1710 Waakwamu walipopanua himaya yao kieneo kuvuka mto Volta. Kwa kiasi fulani, katika kujibu upanuzi huu wa Waakwamu na baadaye ule wa Waasante na Waakyem, Wafante waliyateka madola ya jirani ya pwani, na kutwaa udhibiti wa pwani kuanzia mlango wa mto Pra hadi ufalme wa Ga.

Mabadiliko ya kisiasa yaliyotokea katika majimbo ya katikati ya msitu baina ya mito Komoe na Volta yalikuwa ya kuvutia zaidi. Kwanza palikuwa na kuporomoka kwa himaya ya Denkyira katika msururu wa vita kati ya 1699 na 1701, vilivyopiganwa na madola machanga ya shirikisho la Asante. Ushinde huu ulifuatiwa na utekaji wa madola yote vibaraka yaliyokimilikiwa na Denkyira: madola ya Kisefwi ya Twifo na Wassa, halafu Aowin, Nzima, dola la Waanyi la Ndenye, Wenchi na Bono, na mwisho dola la Bron na Gonja. Kufikia 1730 eneo lote kati ya mito Komoe na Volta lilikuwa chini ya udhibiti wa Waasante.

Halafu kulikuwa na ushinde wa Waakwamu dhidi ya Waakyem Abuakwa na washirika wao, Waga, Wakotoku na Waagona. Watawala wa Waakwamu walifukuzwa nchini mwao na kuvuka mto Volta ambako walianzisha jiji lao la sasa, Akwamufie. Hivyo hadi 1733, eneo lote kati ya mito Komoe na Volta liligawanywa miongoni mwa Waasante, Waakyem na Wafante.

Mchakato wa ugatizaji ulikamilika kati ya 1731 na 1750, Waasante walipoteka Akyem Kotoku na Akyem Abuakwa na dola la Waga kusini, pia Gonja ya mashariki na dola la Dagomba kaskazini mwa mto Volta, na madola ya Krakye na Bassa upande wa kaskazini-mashariki. Wafante pekee ndio waliendeleza mamlaka yao kwa kipindi chote cha karne ya kumi na nane, kiasi kwa kutumia ufundi wao wa kidiplomasia, na kwa kiasi fulani kwa kusaidiwa na Waingereza, ambao walitaka kuwazuia Waasante kudhibiti pwani yote.

Muundo na serikali ya himaya ya Asante vilifanana na vile vya himaya za Akwamu na Denkyira. Iligawanywa katika sehemu mbili: Asante ya Mjini na Asante ya Shamba. Asante ya Mjini ilikuwa na madola yote ya zamani ndani ya kipenyo cha kilomita hamsini cha Kumasi. Wote walimtambua *ohene* wa Kumasi kama *asantehene* (mfalme mkuu) wao. Waliwakilishwa na mfalme wao kwenye Baraza la *Asanteman*, chombo kilichotawala shirikisho na himaya yote. Kwa sababu za kisiasa-kijeshi, Asante ya Mjini iligawanywa, kama Akwamu, katika vikosi vitano.

Asante ya Shamba au Asante Kuu ilikusanya madola yote yaliyotekwa na kugeuzwa madola vibaraka. Madola haya hayakuwa na mwakilishi wa moja kwa moja kwenye Baraza la *Asanteman* wala namna yoyote ya kuweza kuwasiliana moja kwa moja na *asantehene*. Badala yake, kila dola lilimtumikia *Asantehene* kupitia mtu wa kati, aliyekuwa mmoja wa wafalme, au moja ya madola ya shirikisho, au mmoja wa machifu wa vikosi wa dola la Kumasi. Mfumo huu wa utawala wa majimbo (*adamfo*) ulitoa uhuru mkubwa, na madola mara nyingi yaliachiwa huru kufanya

yatakavyo, madhali yalilipa kodi yao ya mwaka na kushiriki katika vita vyovyote iliyopiganwa na Waasante.

Hivyo mapinduzi ya kisiasa yalitokea msituni na katika majimbo ya Pwani ya Guinea ya Chini kati ya 1670 na 1750. Kutoka madola thelathini na nane ya ramani ya 1629 ziliibuka himaya tatu za Aowin, Denkyira na Akwamu, ambazo kufikia 1750 zilikwisha changanyika kuwa himaya moja ya Asante.


Himaya hizi ziliweza kuundwa, ilikuwa ni kwa kuwa zilikuwa na uwezo wa kununua silaha na risasi, na pia motisha iliyohitajika ili kujipanua. Aowin, Denkyira, Akwamu na Asante yalikuwa madola makuu ya kuzalisha dhahabu na yalifanya kazi ya ulanguzi kati ya savana na majimbo ya pwani. Kwa kupanuka kuelekea kaskazini na kusini madola haya yangeweza kudhibiti njia kuu za biashara. Zaidi ya hayo, kuwako kwa Wazungu pwani kulitoa motisha kubwa, ilivyokuwa biashara na Wazungu ilikuwa na manufaa zaidi kuliko biashara na savana. Kwa hiyo haistaajabishi kuona kuwa watu wengi walijaribu kupigana ili wafike pwani.

Madola yaliyounda Asante Mjini pia yalikuwa na sababu za kisiasa. Walikuwa na nia ya kuwang'oa watekaji wao dhalimu Wadenkyira, na walikuwa wakisubiri watemi wanaofaa tu kuwaongoza. Watemi hao walitokea kuwa ni Osei Tutu na Opoku Ware, waanzilishi wa himaya ya Asante.

Sababu ya ziada ya kuibuka kwa himaya hizi ni kwamba, zilipoanza kupanuka, hazikuingiliwa katika mambo yake ya ndani. Madola ya Akyem, ingawa yalikuwa na nyenzo na motisha, hayakuweza kuendelea kuwa himaya kubwa kwa sababu hayakuwa na uhuru huo. Yakibanwa kati ya Denkyira yenye kupanuka na, baadaye, Asante na Akwamu, muda wote yalikuwa yakijihami. Hali kadhalika, madola ya pwani yalizimwa kwa kuingiliwa mara zote na mataifa pinzani ya Ulaya. Madola ya bara ya Aowin, Denkyira, Akwamu na Asante tangu mwanzo yaliepuka kuingiliwa, hivyo yakaweza kuimarisha vya kutosha nguvu zao kabla ya kukutana na Wazungu.

Kuna mambo mawili ambayo sharti yazingatiwe katika kuelezea kuibuka kwa himaya hizi: matumizi ya teknolojia mpya na ubora wa uongozi wao. Watawala wa madola haya walikuwa na nyenzo za kununulia silaha na risasi kutoka kwa Wazungu, na hiyo iliwawezesha kuwazidi wenzao ambao hawakuwa navyo. Njia za kizamani za kupigana zilibadilishwa kwa kulipanga jeshi katika vikosi vya wapiganaji, na mpangilio huu mpya ulisimikwa juu ya muundo wa kisiasa wa mapokeo. Hivyo, uwezo wa watawala wa kubadilika kulingana na hali mpya ukawa muhimu sana.

Katika hatua hii machache sana yanajulikana kuhusu wafalme wa Aowin, lakini vyanzo simulizi na vyanzo vya maandishi vya Kizungu vinakiri ujasiri na uwezo wa watawala wa Denkyira, Akwamu na Asante. Wafalme wa Denkyira walikuwa ni pamoja na Werempe Ampem, Boadu Akafu Brempon na, aliyetia fora, Boa Amponsem. Wafalme wa Akwamu walikuwa ni pamoja na Ansa Sasraku, Basua na Akwono, na wa Asante walikuwa ni Osei Tutu na Opoku. Wanahistoria wengi wanaamini kuwa himaya hizi zilitokana na biashara ya watumwa. Lile linaloweza kuwa la kweli katika sehemu nyingine za Afrika Magharibi si la kweli kwa eneo hili.




14.2 Uchoraji mpya wa *1629* wa ramani ya Gold Coast

Katika pwani ya Ghana, biashara ya watumwa ilikuwa muhimu kiuchumi kuanzia 1700-1710, ambapo shughuli za mapanuzi zilikwishaanza miaka ya 1670 na ya 1680. Katika Gold Coast, biashara ya watumwa ilikuwa ni matokeo, wala si sababu, ya mchakato wa ujenzi wa madola.

Katika maeneo ya Akan magharibi ya Mto Tano na maeneo ya Ewe mashariki ya Mto Volta, makazi ya asili ya Walagunaire, Waanyi na Wabaule, hapakuwa na mabadiliko ya kisiasa ya kusisimua ya aina hiyo wakati huo. Mwaka 1800 waliongozana kama walivyoishi miaka mia moja na hamsini iliyopita au kabla, wakiwa na falme ndogo au temi, kila mmoja ukiwa ni mkusanyiko dhaifu wa makundi ya familia yaliyotokana na koo zenye asili moja.

Mwaka 1800, nchi ya Ewe ilikuwa bado imegawanyika katika tawala huru (*dukowo)* za akubwa mbalimbali. Kila *dukowo* ilitawaliwa na *fia* (mfalme) aliyechaguliwa kwa utaratibu wa ubaba kutokana na nasaba moja au mbili za familia anzilishi na kusaidiwa na Baraza la Wazee.

Kuna sababu kadha zenye kueleza kwa nini Waakan wa Magharibi walioishi kwenye bonde la mito Tano-Bandama, na Waewe wa bonde la mito Volta-Mono, hawakufanya mabadiliko ya kisiasa. Kwanza uhamiaji katika maeneo yote mawili uliendelea muda wote wa karne za kumi na saba na kumi na nane. Matokeo yake, kufikia 1800, Waewe na Waakan wa Magharibi hawakuwa wametulia vya kutosha kuandama vita vya upanuzi. Pili, ilivyokuwa hawa wahamiaji wenyewe walikuwa wanakwepa shughuli za ugatizaji na tabia za kikatili za watawala wao wa awali, hawakuwa na hamu ya kuunda upya miundo ileile ya kijamii - kisiasa katika makazi yao mapya. Tatu, kwa upande wa Waewe, motisha ya kiuchumi ya kujenga dola haikuwapo. Bila dhahabu, pembe au kola, Waewe hawangeweza kushiriki katika biashara yenye faida ya Atlantiki ya kaskazini-kusini. Wakati wa karne za kumi na saba na kumi na nane, mahuruji makuu ya jimbo yalikuwa ni watumwa, shughuli iliyohatarisha amani na utulivu, na hivyo haikuweza kuchochea mapanuzi ya kisiasa.

Waakan wa Magharibi walikuwa na dhahabu, pembe na kola, lakini kwa kuwa hawakuwa wanadhibiti njia za biashara kuelekea kaskazini, hawakuwa na uwezo hasa wa kuandama zoezi la upanuzi la haja. Aidha, wao, kama Waewe, walikabiliwa na kikwazo cha kiekolojia katika umbo la wangwa zilizotenganisha pwani na bara na kukwaza mawasiliano ya kibiashara.

Hatimaye, maingilio ya mara kwa mara ya jirani zao wa kaskazini wenye mabavu zaidi yaliwafanya wawe kwenye hali ya kujihami muda wote, na kujali zaidi kudumisha uhuru wao.

## *Mabadiliko ya kijamii na kitamaduni katika Guinea ya Chini*

Badiliko la wazi kabisa la kijamii-kitamaduni katika Guinea ya Chini kati ya 1500 na 1800 lilikuwa la kidemografia. Kwa kuingiza nafaka na mazao mengi sana ya vyakula kutoka Dunia Mpya na Asia, idadi ya wakazi iliongezeka sana. Katika karne

ya kumi na nane, hata hivyo, zaidi kutokana na biashara ya watumwa, idadi ya watu ilituama au hata kupungua.

Pili, jamii ilistaarabika zaidi. Mwaka 1500 ilikwisha kuwa na watawala wa kikabaila, wakiwemo waali wa kidini na waali wa kisiasa, raia wa kawaida na watumwa wa majumbani. Kufikia 1800, waali wa kisiasa walikwisha wazidi wa kidini, isipokuwa miongoni mwa Waga-Adangbe na Waewe. Ongezeko la kupindukia la shughuli za uchumi na vita vya upanuzi viliongeza idadi ya watumwa wa nyumbani. Hadi 1800 karibu watumwa wote walikwisha ingizwa katika jamii walimoishi na ilikuwa sheria takatifu, hasa miongoni mwa Waakan, kutotangaza asili zao.

Zaidi ya hayo, kutokana na shughuli za biashara na kuwako kwa Wazungu, matabaka mapya matatu yasiyojulikana na jamii ya asili yaliibuka - tabaka la wapokea mshahara, takaba huru la wafanyabiashara matajiri na wanamfalme wafanyabiashara, na kundi la machotara. Tabaka la kwanza lilikuwa la watu walioajiriwa na Wazungu kama waashi, maseremala, wakalimani, waandishi au makatibu, wachuuza dhahabu, watumishi wa serikali, mabalozi na maofisa uhusiano mwema.


Kundi la pili lilikuwa la Waafrika ambao, kutokana na juhudi zao katika kilimo au biashara walitokea kutajirika sana na kuwa wenye nguvu zaidi ya watawala wenyeji. Katika pwani ya Cote d'lvoire ya leo, kwa mfano, Wakosehirange walipata nguvu sana na walikuwa na dhima kuu katika uteuzi wa wakuu wa nasaba.

Kundi la machotara lilikuwa ni mazao ya maingiliano baina ya wafanyabiashara wa Ulaya na wanawake wa Kiafrika. Watu kama hao wanaweza kupatikana sehemu zote za pwani ya Guinea ya Chini. Baadhi, kama madhuria wa Richard Brew, walifanya kazi muhimu katika uga wa biashara na siasa ya jimbo.

Badiliko jingine muhimu lilikuwa kuingizwa kwa Ukristo na elimu ya magharibi na Wazungu, na Uislamu na wafanyabiashara Waislamu wa Kimande na Kihausa. Waholanzi na Waingereza walianzisha shule za msingi katika Cape Coast, Elmina na Akkra, na katika miaka ya 1750 chama cha kueneza Biblia kilituma wamisionari Cape Coast. Zaidi ya hayo, baadhi ya watoto wa machotara na watawala wa jadi walipelekwa ng'ambo kusomeshwa, wakarudi nyumbani wakiwa walimu na wamisionari. Hivyo, kufikia 1800 wasomi wachache na waumini kadha wa Ukristo waliweza kupatikana katika baadhi ya miji ya pwani.

Hata mapema zaidi ya Ukristo, Uislamu na utamaduni wa Kiislamu vilienea kufuata njia za kaskazini za biashara, kwanza katika Ghana ya kaskazini kufikia karne ya kumi na nne, halafu katika maeneo ya Asante na Baule kufikia katikati ya karne ya kumi na nane. Kufikia 1800, Kumasi ilikuwa na makazi ya Kiislamu yaliyostawi na chuo cha Kurani. Hata hivyo, si Ukristo wala Uislamu uliokuwa na athari ya haja juu ya watu wa Guinea ya Chini, ingawa kusoma na kuandika kwa lugha za Ulaya na Kiarabu vilikwisha jengeka imara.

Kuhusu sanaa na kazi za mikono, watu wa Pwani ya Guinea, kufikia 1800,



**14.3** *Mizani za Kiakan ya kupimia dhahabu. Aina za kijiometria (kushoto) zilitumika kuanzia karne ya kumi na tano na kuendelea: Picha (kulia) za ishara zilizotumika kuanzia karne ya kumi na saba; pia hutumika kuonyesha methali na misemo maarufu.*

walikwisha kuwa na ufundi wa juu katika ufinyanzi vyungu, uchongaji, ufumaji, uunzi na kukalibu vyombo vya shaba nyeupe na vya dhahabu.

Ufinyanzi katika Ghana unafahamika tangu Enzi ya Mawe ya Baadaye (baada ya mwaka 3000 KK) na ulikwisha endelea sana kufika mwanzo wa karne ya kumi na nane, hususa miongoni mwa Waadangbe. Kwa mujibu wa J. Anquandah, Waasante walifinyanga baadhi ya vyombo bora vyenye maumbile anuwai, kwa mfano *abusua kuruwa,* chungu cha ukoo, na *mogyemogye*, jagi la mvinyo lililotumika kumininia matambiko kwenye Kigoda cha Dhahabu.

Uchongaji na utengenezaji wa sanamu za miti, pembe na udongo wa mfinyanzi uliendelezwa katika kipindi hiki pia, hasa miongoni mwa Waakan. Watalii wa karne za kumi na saba na kumi na nane katika pwani ya Ghana, kama vile W. Bosman, walivutiwa na uzuri wa matarumbeta ya pembe yanayopuliziwa pembeni. Miongoni mwa kazi zenye kuwakilisha sanaa hii, mashuhuri kabisa ni *akuaba* (sanamu za uzazi) za mti na udongo wa mfinyanzi, na picha zilizofinyangwa za wafalme na malkia marehemu.

Ufumaji ulienea sana katika jimbo lote karne za kumi na sita na kumi na saba na, kufuatana na ramani ya 1629, Nsoko ("Insoco" katika ramani), yaani Begho ya leo, ilikuwa kituo muhimu cha ufumaji. Lakini ilikuwa katika karne ya kumi na nane ufumaji miongoni mwa Waakan na Waewe ulipokomaa, kama inavyoonyeshwa na vitambaa mashuhuri vya rangi, *kente*, vya Waakan, na vitambaa teule vya *adanudo* vya Waewe. Kitambaa cha *adinkra*, na motifu na ishara za jadi ya Akan zilizochapwa juu yake, kilikuwa mashuhuri katika jimbo la Brong na baadaye kiliigwa na Waasante.

Hata hivyo, watu wa Guinea ya Chini, hususan Waakan, walitia fora hasa katika ufuaji wa metali na ukalibaji., hasa wa dhahabu na shaba nyeupe. Wakitumia zaidi mchakato wa *cire-perdue* (nta-potevu), wafuaji walifua vyombo bora vya dhahabu na fedha, pamoja na mipini ya panga, pete, bangili, mikufu na kofia. Wafuaji wa Akan pia walifua mawe ya uzani elfu nyingi, ya dhahabu au sufuri, yenye maumbo ya kijiometri au ya kisanamu, ambayo sasa yanapatikana katika makumbusho makuu ya sanaa duniani kote.

Sanaa na kazi za mkono za Guinea ya Chini zilifikia upeo wake ilipoibuka himaya ya Asante kwenye karne ya kumi na nane. Wafalme wa Asante walifanya kila kilichowezekana katika mamlaka yao kukuza shughuli hizi. Baada ya ushinde wa Denkyira, Tekyiman na Akyem, walikusanya wasanii na wafua dhahabu bora wa madola haya na kuwapeleka Kumasi. Idadi kadha ya vituo vya ubobezi vilianzishwa kando kando ya jiji. *Asantehene* alianzisha *Apagyafie*, kikundi cha wafua dhahabu na wasani kutoka Denkyira ambao kazi yao ilikuwa ni kutengeneza regalia (nembo) ya mfalme. Pia aliingiza kigoda cha dhahabu, *Asomfo*, ambacho mtu aliyekikalia kwanza, Nana Tabiri, alikuwa mwana wa chifu wa Denkyira.

Mchanganyiko huu wa tajriba anuwai za kisanii, ubingwa na jadi, uliwawezesha wafalme wa Asante katika karne ya kumi na nane kupandisha maendeleo ya

kitamaduni ya watu wa Akan hadi kilele cha juu kabisa cha ubora, na kuhakikisha kuwa mamlaka yao yanaakisiwa ndani ya kazi za sanaa bora kabisa.

## *Hitimisho*

Kipindi cha kati ya 1500 na 1800 hakika kilikuwa ni cha mabadiliko makubwa kwa madola na watu wa Guinea ya Chini. Kisiasa mchakato wa kuelekea ugatizaji ulikamilishwa. Kiuchumi biashara ya dhahabu na pembe iligubikwa na biashara ya watumwa; vituo vya biashara na vya uchumi vilihama kutoka bara hadi pwani; mahusiano imara ya kibiashara yalijengwa na Amerika na Ulaya, na hivyo kuchanganya uchumi wa ukanda na uchumi wa ulimwengu. Zaidi ya yote, hiki kilikuwa kipindi cha mabadiliko ya kijamii, yaliyoashiriwa na kuibuka kwa tabaka mpya za jamii japo kwa kiwango kidogo na zaidi kwenye maeneo ya pwani; kuanza kwa kisomo, kuingizwa kwa elimu ya Magharibi na Ukristo, kuenea kwa Uislamu na kuchanua kwa tamaduni za wenyeji, kulikojitokeza katika ufumaji na ufuaji metali. Kwa hakika hizi zilikuwa karne zenye vuguvugu kwa watu wa Pwani ya Guinea ya Chini, na kwa kweli ilibidi iwe hivyo, kwani hadi mwishoni mwa kipindi hiki walikuwa bado wanadhibiti kabisa majaliwa yao.

# 15


# *Wafon na Wayoruba: Delta ya na Kameruni*

Sura hii inahusu eneo linaloanzia kwenye bonde la Mto Volta upande wa magharibi hadi Mto Kameruni upande wa mashariki. Sehemu kubwa ya eneo hili ni msitu wa tropiki uliopakana na savana yenye vichaka upande wa kaskazini. Sehemu ya magharibi, kutoka mpaka wa Nigeria hadi Mto Volta, ni savana pia. Jamii zinazoishi katika eneo hili la msitu wa Guinea na savana ya jirani ni pamoja na Wafon au Waaja wa Jamhuri ya Benin ya sasa, Wayoruba, Waijo wa delta ya Niger, Waigbo wa kaskazini-mashariki mwa delta, Waibibio na makabila mengine mbalimbali huko kusini mwa Kameruni.

Lugha zote za eneo hili ni za familia ya Kiniger-Kikongo, idadi kubwa zaidi ya lugha hizo zikiwa ni za familia ndogo ya Kikwa. Kiefik/Kiibibio na lugha nyingine za eneo la Nigeria lililoko kwenye mpaka wa Nigeria na Kameruni, na lugha za Kameruni yenyewe, zina uhusiano wa karibu na lugha za Kibantu za Afrika ya kati, ya mashariki na ya kusini. Watu na tamaduni za eneo hili la mpakani ndio kiungo kati ya Afrika Magharibi na Afrika ya Kibantu. Miongoni mwa lugha za Kikwa, Kiyoruba na Kiigbo ndizo zilizo kubwa zaidi kwa upande wa idadi ya wazungumzaji (milioni 8-12) na mtandao wa kijiografia. Kundi la Kiedo nalo ni kubwa, maana linajumuisha jamii kama zile za Waisoko na Waurhobo, Waishan (Waesan) na wengineo. Miongoni mwa lugha za Kikwa, Kiijo cha delta ya Niger ndicho kilicho tofauti sana na lugha jirani zake, yaani Kiigbo, Kiedo na Kiyoruba.

Mwendeleo wa muda mrefu katika historia ya eneo hili hauna budi kuzingatiwa wakati wa kutathmini mabadiliko yanayodhaniwa kuwa yaliletwa na ujio wa Wazungu kwenye pwani ya nchi hii mwishoni mwa karne ya kumi na tano. Wareno waliwasili Benin mwaka 1486 na wakaanzisha mahusiano na Oba wa Benin. Walianzisha mahusiano ya kibiashara katika vituo mbalimbali kandokando ya pwani ambavyo ndivyo vilikuwa chachu kuu za mabadiliko.

Ni dhahiri kwamba biashara ya watumwa ndiyo iliyokuwa shughuli kubwa ya Wazungu kati ya karne za kumi na sita na kumi na nane. Eneo linalozingatiwa katika sura hii lilikuwa mojawapo ya masoko makuu ya watumwa kwenye pwani ya Afrika Magharibi. Baadhi ya madola, kama vile himaya ya Dahomey, yalianzishwa na kukua kwa kusukumwa na biashara hii. Maendeleo ya mataifa mengine, kutoka delta ya




**15.1** *Maeneo ya delta ya Niger na Cameroon kuanzia karne ya kumi na sita hadi ya kumi na nane.*

Niger hadi Mto Kameruni, yaliathiriwa na faida zilizotokana na biashara hii. Jumuia nyingine, hasa zile ambazo hazikujiunga katika mfumo wa dola, zilikuwa waathirika wa biashara ya watumwa ya kuvuka bahari.

Kuongezeka kwa biashara ya watumwa ya ndani pia kulileta mabadiliko ya kijamii na kisiasa katika jumuiya. Mapokeo simulizi yanaonyesha athari za biashara hii kwa ustawi wa koo, vikundi au nasaba-tawala.

## *Ufalme wa Wafon wa Dahomey*

Maendeleo ya kisiasa ya himaya ya Dahomey na madola jirani ya Allada, Whydah, Popo, na Jakin kwa kiwango kikubwa yalihusiana na shughuli za wafanyabiashara ya watumwa wa Kizungu kwenye ukanda wa pwani, na athari za ufalme wa Kiyoruba wa Oyo uliokuwa kaskazini-mashariki.

Asasi za kimapokeo za jumuiya ndogondogo na madola ya eneo hili yalidhoofishwa na kuingizwa kwa biashara ya watumwa, na ilipofikia mwishoni mwa karne ya kumi na saba ombwe la kisiasa lilikuwa limejitokeza. Ni katika kipindi hiki ambapo waasisi wa ufalme wa Dahomey walirejesha utulivu kwa kubuni mpangilio mpya wa kisiasa kutokana na vikundi mbalimbali vya Waaja, vikijumuisha Wagun, Wafon, Waarada na watu wengine kutoka sehemu ya kusini ya Jamhuri ya Benin ya sasa. Ilipofikia 1700, Dahomey ilikuwa taifa kubwa katika eneo hili. Kati ya 1724 na 1726, mtawala wake, Agaja, alianza kuyashambulia mataifa madogomadogo lakini ya kale yaliyokuwa jirani na Abomey. Hii ilisababisha Oyo kuingilia kati, lakini si kwa kutaka kuweka mfumo wake yenyewe nchini humo. Baada ya 1730 Dahomey ilikubali mamlaka ya kisiasa ya Oyo na ikaafiki kufuata uchumi wa biashara ya watumwa.

Zahama iliyoanza takriban 1767 iliishia katika kuanguka kwa nasaba ya Agaja mnamo 1818 na kuinukia kwa nasaba mpya ya Gezo. Nasaba mpya ilifuata kikamilifu uchumi wa biashara ya watumwa na kuufanya kuwa msingi wa nguvu zake. Hivyo ilifaidika na kusambaratika kwa ufalme wa Oyo na vita vya Wayoruba katika karne ya kumi na tisa.

Mahusiano kati ya jumuiya za Waaja na Wayoruba upande wa mashariki na kaskazini-mashariki yalikuwa makubwa na ya muda mrefu. Kwa hakika kuna madola kwenye eneo hili yenye asili na utamaduni wa Kiyoruba, hasa Waketu, jumuiya ya wahamiaji wa Kiyoruba kutoka Ile-Ife.

Madola katika eneo hili kwa kiwango kikubwa yalifuata mifumo ya utawala ya Wayoruba; himaya "baba" ikiwa Allada, iliyoasisiwa kunako takriban 1575. Kuingilia kati kwa Oyo, ambako kulidhibiti nguvu za kijeshi za Dahomey, kuliliwezesha dola hili changa kuimarisha utawala wake wa ndani. Baadhi ya mifumo ya utawala ya Oyo ilichukuliwa, kwa mfano mfumo wa *ilari* ulioanzishwa na Tegbesu, mtawala wa mwisho wa nasaba anzilishi.

Athari za biashara ya watumwa zilikuwa muhimu kiasi hicho kwa kuwa wakati biashara hiyo ilipoanzishwa kunako karne ya kumi na sita madola haya yalikuwa bado

dhaifu. Shughuli za kiuchumi zilidhoofishwa na kanuni za jamii ziliharibiwa. Isitoshe, ushindani uliozuka kutokana na kugombania vituo vya biashara uliharibu mahusiano ya kijadi miongoni mwa madola. Mapema kwenye karne ya kumi na saba, Waholanzi waliweka mawakala wao Assim, mji mkuu wa Allada. Wafaransa walianzisha kituo kinzani cha biashara huko Whydah mnamo 1671. Jambo hilo liliharibu uhusiano uliokuwa tayari umedhoofika kati ya madola haya mawili. Ni katika hali hii ya mashindano ya kisiasa na kibiashara ambapo wahamiaji kutoka Allada walianzisha ufalme wa Dahomey.

Walianzisha makazi Abomey, mbali na eneo lililodhibitiwa na Wazungu, kunako takribani mwaka 1625, na wakajaribu kutengeneza mfumo mpya wa kisiasa. Walilifananisha dola na chungu kilichotobolewa, likiwakilishwa kiishara na mfalme. Ili chungu kilichotobolewa kiweze kuhifadhi maji, kila mwananchi alipashwa kutia kidole chake kwenye tundu moja, na kwa hivyo kutumbukiza utambulisho wake katika dola lenye mamlaka kamili. Maendelezo thabiti ya wazo hili la kuwa na dola imara unganifu lenye mfalme aliyedai utii kamili ndiyo yaliyoitofautisha Dahomey na madola mengine. Kutokana na sifa hii, Dahomey polepole iliweza kuyaleta madola ya jirani katika udhibiti wake.

Madai ya kuwa biashara ya watumwa ya Atlantiki ilikuwa na dhima muhimu katika historia ya Dahomey sasa yameanza kudurusiwa na utafiti wa hivi karibuni. W. Peukert anapinga moja kwa moja dhana mbili muhimu: kwamba historia ya Dahomey ilitegemea biashara ya watumwa na kwamba uchumi wake ulikuwa wa kikale. Nadhariatete mpya za wanahistoria zinadai udurusu wa mawazo ya kizamani na utafiti zaidi.

## *Falme za Kiyoruba*

Historia ya jumuiya za Kiyoruba za Nigeria ya kusini-magharibi inaweza kuelezwa kwa ufupi kwa kuzingatia mambo makuu matatu. La kwanza linahusu mapokeo yanayoifanya Ile-Ife kuwa kitovu cha chimbuko la falme za Kiyoruba, dai ambalo linahitaji kuoanishwa na ushahidi wa kiakiolojia. La pili ni kuinukia kwa nguvu za kivita na kisiasa za Oyo, kulikofikiriwa kwenda sambamba na mamlaka ya kiroho ya *oni* wa Ife juu ya nchi nzima ya Wayoruba. Jambo la tatu ni hali ya maendeleo ya kisiasa, kiutamaduni na kijamii katika jumuiya na falme za Wayoruba.

Umaarufu wa Ife katika historia ya Uyoruba umesababishwa na mambo mengi. Kulingana na mapokeo, mwasisi wake, Oduduwa, alifikiriwa kuwa alitoka mbinguni au Maka, na watoto au wajukuu wake ndio walioasisi mataifa mengine yote ya Kiyoruba. Ufafanuzi wa hivi karibuni wa mapokeo haya unaonyesha kwamba Oduduwa, au kikundi cha wahamiaji, walikuja kwenye eneo hili takribani miaka 1,000 iliyopita, lakini eneo tayari lilikuwa limekwisha kaliwa, pengine na Waigbo wa mapokeo ya Ife.

Sanamu maarufu za shaba nyeusi za Ife zimechangia kuthibitisha mapokeo juu ya uhusiano baina ya Ife au nchi ya Wayoruba na ufalme wa Edo wa Benin. Lakini



**15.2** *Fifteenth- or sixteenth-century commemorative head from Benin, Nigeria, cast in bronze and inlaid with iron. Height 22 cm (National Museum of African Art, Eliot Elisofon Archives, Smithsonian Institution, Washington DC, photo: B. Fleischer)*

sanamu hizo pia zinaihusisha Ife na Nupe na Benin, na maeneo yanayopakana na mto Niger, kwani ushabihiano dhahiri umekwisha onekana kati ya sanamu kubwa za shaba nyeusi zilizopo Nupe na zile za Ife.

Hali kadhalika imedhihirika kuwa "Maka" ya mapokeo simulizi haikuwa ikitaja eneo lolote la Mashariki ya Kati, Misri au Meroe, bali maeneo ya ng'ambo tu ya Mto Niger kaskazini mwa nchi ya Wayoruba ya sasa. Zaidi ya hayo, sanaa ya Ife imelinganishwa na sanaa ya terakota (udongo mwekundu) ya Nok ya Nigeria ya kati, licha ya tamaduni hizi mbili kuwa za nyakati tofauti.

Siyo tu kwamba Oyo ilikuwa mashuhuri miongoni mwa falme za Kiyoruba, bali pia ilipata sifa bainifu za kipekee. Baadhi ya sifa hizo zilitokana na kuwepo kwake karibu na Nupe na Borgu. Kwa mfano, Oyo ilitegemea mno maofisa wenye asili ya watumwa katika uendeshaji wake wa mambo ya kijeshi na kijamii kuliko yalivyofanya madola mengine ya Kiyoruba. Kwa upande wa majeshi, kuongoza kwa Oyo bila shaka kulitokana na matumizi ya askari farasi na wapiga mishale, mbinu ziliyotokana na mahusiano ya awali ya Oyo na biashara ya kuvuka Sahara na mataifa ya kaskazini. Mahusiano haya na nchi za nje pamoja na kuwemo ndani ya savana kuliiwezesha Oyo kufanya bidaa katika dhana za Kiyoruba ilizochangia na falme nyingine.

Kuasisiwa kwa Oyo kunahusishwa na Ife na Benin kupitia kwa mwasisi wake wa kwenye visakale, Oranyan (*Oranmiyan*), ambaye anadaiwa kuwa alitawala Ife na Benin kabla ya kuhamia Oyo. Lakini madola mengine tayari yalikuwemo katika eneo hili, na Oyo iliyafanya baadhi yake kuwa madola ya kitwana, zikiwemo Owu upande wa kusini na Ede upande wa kusini-mashariki. Kupanuka kwa Oyo hatimaye kulisimamishwa na Waijesha, kwa vile askari farasi wa Oyo walishindwa kupigana kwenye maeneo ya misitu. Waijebu, na nchi ya milima ya Waekiti, pia waliepuka udhibiti wa moja kwa moja wa Oyo. Ufalme wa Benin upande wa mashariki vilevile ulikuwa kikwazo kingine kwa upanuzi wa Oyo. Oyo ilifungua njia ya biashara kuelekea pwani kupitia nchi ya Waegba na Waegbado, na kupitia njia hii mamlaka ya Oyo yakapanuliwa hadi Dahomey.

Nguvu za Oyo zilitokana na shida. Katika karne ya kumi na tano watawala wake walikuwa wamefukuzwa kutoka Oyo ya Kale (Oyo Ile au Katunga) na kukimbilia Kusu miongoni mwa Waborgu, na baadaye Igboho. Oyo iliunda upya jeshi lake na kuanza sera mpya ya kupenda kutumia nguvu za kijeshi katika siasa. Ilipofikia mwanzoni mwa karne ya kumi na sita Oyo ilikuwa tayari imeshaliteka tena eneo lake na kuwasukuma Wanupe nyuma.

Oyo ilibakia nje ya eneo lililoathiriwa moja kwa moja na Ulaya hadi karne ya kumi na tisa, ikiendeleza asasi zake na kuanzisha upanuzi kwa kujitegemea. Kujiingiza kwake Dahomey kwaweza kuwa kulisababishwa na ushiriki wake kwenye biashara ya pwani, lakini mapokeo simulizi mengine yanadai kwamba Oyo haikujihusisha na biashara ya watumwa na iliepuka kabisa mahusiano na Wazungu.

Maeneo ya Uyoruba yaliyoko ng'ambo ya eneo la upanuzi wa Oyo, upande wa

mashariki na kaskazini, yalijumuisha madola madogomadogo kwenye eneo la Ekiti na maeneo mengine, kama vile dola la Igala, ambayo yalielekea zaidi upande wa bonde la Niger-Benue. Madola mengine, kama vile Owo na Ijebu, yaelekea yalikuwa na uhusiano zaidi na ufalme wa Edo huko Benin kuliko Oyo. Kazi za kisanaa zilizochimbuliwa Owo zinaonyesha kuwa ilipofika karne ya kumi na tano maumbo ya sanamu za eneo hili tayari yalikuwa na uhusiano na mitindo ya Ife na Benin.

## *Delta ya Niger*

Historia ya delta ya Niger imefungamana na historia ya sehemu za eneo la pwani mashariki hadi Kameruni na magharibi hadi kwenye nyangwa za Lagos na ng'ambo yake. Hadi karne ya kumi na tisa, njia za biashara zilikatisha eneo hili kutoka mashariki hadi magharibi, na kutoka kaskazini hadi kusini. Nguo zilizotengenezwa katika eneo la Ijebu la nchi ya Wayoruba ziliuzwa kwenye delta ya magharibi na yaelekea ziliuzwa tena upande wa mashariki hadi Nembe kwenye delta ya mashariki. Waitsekiri (wa delta ya magharibi) walihusiana na Waijebu, kama inavyoonyeshwa na kufanana kwa lugha yao, lakini walikopa baadhi ya amali za kiutamaduni kutoka kwa Waijo, na walifanya biashara ya vifinyange, chumvi na nguo na madola ya delta ya mashariki, hasa Nembe.

Kwenye delta ya magharibi ya Niger, Ode Itsekiri, mji mkuu wa ufalme, ulikuwa kitovu cha nguvu za kisiasa. Wareno walipokuja kwenye eneo hili, Waitsekiri wakawa washirika wao wakuu katika delta. Kunako karne ya kumi na nane baadhi ya Waitsekiri waliondoka makao makuu na kuanzisha makazi kwenye mlango wa mto Benin, mahali palipofaa zaidi kwa biashara ya kuvuka Atlantiki. Kutoka kwenye maeneo haya mapya, Waitsekiri walihudumu kama mawakala wa ufalme wa Benin na kama walanguzi wa kujitegemea wa kuuza nje mazao ya watu wa bara.

Waijo wa delta ya Niger ya magharibi waliishi katika jumuiya zilizogawanyikagawanyika zisizokuwa na mfumo wa dola, na walishiriki kwenye biashara ya ng'ambo ya bahari kwa kupora kama maharamia. Sanamu za shaba nyeusi zilizopatikana miongoni mwa vikundi hivi vya Waijo, na pia miongoni mwa Wamein na Wakobewei, huweza kuashiria utajiri uliopatikana kutokana na kushiriki kwenye biashara ya ndani na nje, na hali kadhalika kutokana na muingiliano na Benin na vituo vingine vya bara.

Waijo wa delta ya kati ndio waliokuwa kitovu cha kundi hili. Mapokeo simulizi yanaelekea kudokeza uhamaji kutoka eneo hili kwenda kwenye delta ya mashariki na ya magharibi na hadi pembezoni mwa delta. Jumuiya za sasa za delta ya mashariki zinakadiriwa kuhamia hapo miaka elfu moja iliyopita. Ukadiriaji tarehe wa radio-kaboni wa vyombo vilivyopatikana huko Ke na Saikiripogu (Ewoama) unathibitisha kuwa watu walikuwa wakiishi hapo kabla ya karne ya tisa.

Uchimbuzi katika delta ya Niger ya mashariki umeleta mtazamo mpya kuhusu historia ya delta ya Niger. Unaonyesha kuwa wakazi wa mwanzo kabisa walifahamu jinsi ya kutumia chaza (samaki kombe) wa delta na kadhalika walifuga wanyama.

Wingi wa vifinyange katika maeneo kama vile Onyoma unaashiria kuwepo kwa uchumi changamani, ambao kiasi ulikitwa kwenye kilimo, na kiasi kwenye biashara. Uchimbuzi umeonyesha pia ushahidi wa ufuaji chuma. Na hili linaashiria kuwepo kwa mwingiliano na bara kwa ajili ya malighafi na bidhaa zilizokwishatengenezwa tayari.

Sanaa katika delta ya Niger ilijumuisha hasa michongo ya miti ikionyesha mizimu ya maji, wahenga au vinyago vya kuchezea ngoma. Uchimbuzi umetoa idadi ndogo ya majuso ya udongo mwekundu kutoka Ke na sanamu za binadamu kutoka Onyoma, ambazo ni za kipekee, miongoni mwa terakota za Nigeria, lakini zinakumbusha terakota za Nok na Ife.

Biashara ya watumwa ya Atlantiki na, kabla yake, biashara ya ndani ya masafa marefu, ilitoa mchango mkubwa katika uanzishaji wa mataifa ya delta ya Niger ya mashariki - Bonny, Elem Kalabari (Kalabari Mpya), Okrika na Nembe. Kutokana na mapokeo simulizi yaonekana kana kwamba waasisi wake walitoka kwenye delta ya kati ya maji baridi na wakazoea maisha katika delta ya mashariki ya maji chumvi. Marekebisho ya kijamii na kisiasa yalifanyika na asasi za kifalme zilianzishwa kuanzia takriban karne ya kumi na tatu. Biashara ya watumwa ya Atlantiki ilichapusha mabadiliko, na aina ya dola lililoanzishwa ilipofika karne ya kumi na saba imeitwa dola-jiji au dola la biashara. Biashara ya watumwa ilitoa utajiri ambao ulikuwa msingi wa mamlaka wa *amanyamabo* (mfalme) na tabaka la watawala.

## *Nchi ya Waigbo*

Maeneo kadhaa ya zama za mawe katikati ya nchi ya Waigbo yanaashiria historia ndefu ya makazi ya watu. Pango moja huko Afikpo lilitoa zana za mawe na vyombo vya udongo vya umri wa miaka 5,000, na maeneo yenye ushahidi unaofanana na huu yamepatikana huko Nsukka. Inaonekana dhahiri kuwa watu walilima hapo walau miaka 3,000 iliyopita, na viazi vikuu ndilo lilikuwa zao lao kuu. Mazao mengine asilia yanajumuisha michikichi, *okro*, *egusi* na aina kadhaa za mkola. Mihogo, mpunga, ndizi, na mazao mengineyo yaliingizwa kutoka Amerika.

Ufuaji chuma ulianza mapema na sanaa ya shaba nyeusi ya eneo hili imekuwa maarufu duniani kutokana na machimbo ya Igbo-Ukwu. Sanamu za shaba nyeusi za eneo hili zinatokana na jadi tofauti na zile za Ife na Benin, lakini uzuri na ubora wao unalingana. Zina uhusiano na ufalme mtukufu na kituo cha miviga ya kimila cha Nri. Makuhani wa Nri walikuwa na mamlaka katika eneo kubwa la nchi ya Waigbo, yakijumuisha kutunuku vyeo vya *ozo* na *eze* na kuondosha mabalaa. Yawezekana kuwa mapato yaliyokusanywa na makuhani katika ziara zao ndiyo yalitoa utajiri ulioendeleza sanaa hii ya shaba nyeusi.

Jumuiya ya makasisi wa Nri ilikuwa na dhima kubwa katika nchi ya Waigbo ambako jumuiya zilipangiliwa kwa kufuata mfumo wa vyeo. Lakini baadhi ya vikundi vya Waigbo magharibi mwa mto Niger na kwenye ukingo wake wa



*15.3 Sanamu ya mwanamke wa Kiyoruba, iliyotengenezwa kwa ajili ya kumbukumbu ya Usanii wa Orisha, Obatala. Amevishwa nguo nyeupe kama Mchungaji na Mtumikia Mungu, kidani na mkufu mweupe. Bakuli aliloshikilia ni la kupokelea sadaka ya damu nyeupe ya konokono, ishara ya amani na utulivu. Ni alama ya mwanamke wa Orisha, wakati mwanamume anawakilishwa na sanamu iliyoshika kipungia upepo na Unyoya. Mshika bakuli huyu asichanganywe na Olumeye, au chombo cha kola, ambaye huwakilishwa na picha kubwa zaidi iliyopiga magoti na kushikilia bakuli lenye mfuniko. Urefu cm 49.*

mashariki viliiga asasi za kifalme za jumuiya vilizoshirikiana nazo. Hivyo yaelekea falme za Waaboh, Waonitsha na Waoguta zilipata *obi* wao kutokana na *oba* (mfalme) wa Benin. Mataifa haya yaliundwa na wahamiaji kutoka maeneo yaliyoathiriwa na utawala wa Benin kwenye karne za kumi na sita na kumi na saba.

Madola mengine katika Mto Niger, kama vile Osomari, yanadai kuwa wahenga wao walitokea katika ufalme wa Waigala wa Idah upande wa kaskazini. Lakini athari ya Igala ilielekea kuwa kubwa zaidi miongoni mwa Waigbo wa kaskazini kwenye bonde la Anambra na katika eneo la Nsukka. Madola ya Waigbo kandokando mwa mto Niger yalikuwa washiriki wa kwanza kwenye biashara ya watumwa ya kuvuka bahari na baadaye kwenye biashara ya mawese kunako karne ya kumi na tisa kwa kushirikiana na mataifa ya delta ya Niger.

Mfumo wa kisiasa na kijamii wa Waigbo ulikuwa na nyenzo za udhibiti mpana kuliko kijiji au mji. Moja ya nyenzo hizo ilikuwa idhini ya kidini iliyotolewa na kahini (mwaguzi). Makahini wamefanya kazi katika nchi ya Waigbo nyakati na mahali tofauti, lakini wanaojulikana sana ni Agbala wa Akwa na Ibini Okpube (Juju Ndefu) wa Arochukwu. Hivyo, wahunzi wa Kiakwa, waliofanya kazi sokoni na kuishi sehemu zote za Uigbo na delta ya Niger, walieneza athari ya kahini wa Agbala. Lakini kahini wa Aro Chukwu alifaulu zaidi kutokana na wafanyabiashara wa Aro, ambao ni wafanyabiashara ya watumwa waliomtangaza kila mahali. Mtandao wa biashara wa Aro ulianzia kwenye bandari ya Kalabari na baadaye ukaenea hadi kwenye madola ya delta. Wafanyabiashara wa Aro walitumia matamshi ya kahini kupata watumwa, lakini waliweza pia kutumia nguvu kwa kusaidiwa na wapiganaji wa Abam, Edda, Ohofia, Abiriba na wengineo waliogawana nao nyara.

Maeneo ya Uigbo yasiyo na serikali unganifu imara bila shaka yaliathirika zaidi na mashambulio ya kutafuta watumwa. Kunako karne ya kumi na nane, bandari za delta ya Niger ya mashariki zilikuwa vituo vikuu vya kuuza nchi za nje watumwa kutoka Afrika Magharibi, na wengi wao walitoka bara ya Uigbo.

## *Bonde la Mto Cross na Kameruni*

Watu wa eneo hili wanaonyesha uhusiano wa lugha na pia asili moja kihistoria. Nyingi ya lugha ni za familia ya lugha za Kibantu. Mbari kubwa zaidi katika bonde la mto Cross, Waibibio, imeishi kwenye eneo hili tangu zamani sana. Kwenye maeneo ya kaskazini ya bonde, eneo la Ogoja limekaliwa na watu mbalimbali wenye mapokeo simulizi ya uhamiaji kutoka bonde la Benue, kaskazini zaidi, au kutoka Kameruni. Baadhi ya jumuiya za kikundi cha Waibibio au vikundi vya karibu nacho, kama vile Waendoni na Waibeno, pia zinadai kuwa zilitoka Kameruni. Halikadhalika, baadhi ya jumuiya za Kameruni, kama vile Waisangele, asili yao ni Ibibio.

Jumuiya katika eneo hili kimsingi zilikuwa na mifumo changamani sana isiyo unganifu. Utaratibu wa marika na pia vyama vya kisiri kama vile vya *Ekpo* na *Mgbe*

(jamii ya Chui) vilitoa udhibiti imara wa kijamii na kisiasa.

Waefik wana uhusiano wa karibu sana na Waibibio, makazi yao ya karibuni yakiwa ni Uruan Ibibio kwenye ukingo wa magharibi wa mto Cross. Baadhi ya mapokeo simulizi yanaonyesha kuwa awali waliishi huko Ibom, karibu na Arochukwu katika nchi ya Waigbo. Kukukaa kwao, mwishoni, huko Ikot Etunko (Mji Kijito), Obutong (Mji Mkongwe) na Atakpa (Mji Mwinyi) kuliyafanya maeneo haya, ilipofikia karne ya kumi na saba, yawe vituo vikuu vya biashara ya kuuza watumwa ng'ambo ya bahari katika ukanda huu. Dola lililoanzishwa na Waefik kwenye mto Cross wa chini - sasa wajulikana kama Kalabari - liliuza nchi za nje watumwa toka bara ya Uigbo kutokea kwenye kituo cha Arochukwu.

Biashara ya watumwa kwa kiasi fulani ilichangia kubadilisha vyama vya kisiri vya *Ekpo* ya Ibibio na *Mgbe* ya Ekoi kuwa *Ekpe* ya Kalabari. *Ekpe* ikawa ni jamii ya kitabaka iliyowaunganisha makabaila na kuwadhibiti watumwa na maskini. Aidha ilihakikisha utekelezaji wa kanuni za kisiasa na kijamii, ilikusanya madeni na kulinda amani. Kutokana na athari za shirika za biashara ya watumwa na mahusiano ya kuvuka Atlantiki, Kalabari ilichipuza taratibu za kiukoo zenye kufanana na Nasaba Tawala za madola ya delta ya mashariki.

Vikundi muhimu zaidi kwenye pwani ya Kameruni vilikuwa vikundi vya Kibantu vya kaskazini-magharibi vya Wakpe-Mboko, Waduala, Walimba na Watanga-Yasa. Kulikuwa na vikundi vingi vya wavuvi, wakulima na wawindaji. Wengi wao waliishi katika jamii ndogo ndogo za vijijini, lakini ilipofikia karne ya kumi na nane Wabubi, Waduala na Waisubu walikuwa wakiishi katika vikundi vikubwa zaidi vya kisiasa. Ama walihusika na biashara ya watumwa ama walifaidika nayo. Chama cha kisiri cha *Jengu*, ambacho kilikuwa kitovu muhimu cha udhibiti wa kijamii na kisiasa, kikawa na hadhi ya juu kabisa katika eneo la pwani la Kameruni.

## *Hitimisho*

Athari kuu ya nje katika historia ya eneo hili la kinamasi na misitu mikubwa ya pwani kuanzia karne ya kumi na tano hadi ya kumi na nane ilikuwa ni biashara ya watumwa. Iliwaathiri sana watu wa eneo hili, lakini ni vigumu kutathmini nafasi yake halisi kuhusiana na mambo ya ndani yaliyoleta mabadiliko mapema kabisa kabla ya ujio wa biashara hiyo.

Katika mapokeo simulizi mengi, biashara ya watumwa inaonekana kama shughuli iliyowatajirisha watu na kuongeza idadi ya watu. Hii hasa ilizihusu jumuiya za pwani zilizoshiriki kama walanguzi, bila kwenda kusaka watumwa zenyewe, bali zikiwanunua na kuwauza upya kwa wafanyabiashara ya watumwa. Madola ya delta ya Niger na dola la Efik yanaingia kwenye mkumbo huu.

Ufalme wa Wafon wa Dahomey ni mfano wa aina ya pili ya ushiriki katika biashara ya watumwa - ule wa kushika hasa watumwa kwa ajili ya wafanyabiashara ya watumwa. Katika Uigbo, Waaro na washirika wao mamluki walikuwa na dhima kama hiyo ya kuwinda watumwa.

Kumbo la tatu la jumuiya zlizoathiriwa na biashara hii ni zile za maathura wa janga hili. Hizi ni jumuiya ambamo watumwa wengi walitoka kwa ajili ya kuuzwa pwani, na zilijumuisha sehemu za Uyoruba, Uigbo na Uibibio. Mashambulio, utekaji nyara, vita na kupungua thamani kwa maisha ya watu viliharakisha kuvunjika kwa mifumo ya kiuchumi na kijamii ya jumuiya hizi. Vijiji viliharibiwa na kutawanywa, mashamba yalitelekezwa na watu waliishi katika hofu kuu.

Wakati mwingine husemwa kuwa biashara ya watumwa iliyatoa maeneo haya ya kitropiki katika hali ya kujitanibu na kuyaingiza kwenye uchumi wa kimataifa. Zaidi ya hayo, uanzishwaji wa mazao kama vile mahindi, muhogo na mpunga waweza kuonekana kama ulisawazisha urari wa kidemografia kwa kuongeza idadi ya watu. Hizi ni nadhariatete za kufikirika. Kwa Waafrika wa eneo hili, zama za biashara ya watumwa huonekana kama ndoto mbaya inayopaswa kusahaulika.

# 16 Madola ya Kihausa

Ni rahisi kulihusisha eneo linalojadiliwa katika sura hii na dhana ya utajiri. Utajiri huu unatokana na ujalizano kati ya maeneo ya jirani na Uhausa kama mzalishaji na mlaji, na pia kutokana na muunganiko wa uchumi wa Afrika Magharibi, (unaohusisha) Wawangara, Wahausa na Wakanuri katika savana, na Wafante, Wabini, Waijaw na Waarochukwu kwenye msitu.


Nyaraka zilizopo kuhusu maendeleo ya eneo hili kati ya 1500 na 1800 ni za ubora usiolingana. Nyaraka juu ya mataifa ya Kihausa zinatofautiana sana. Zinajumuisha ripoti za mashahidi wa matukio na marejeo mbalimbali, ambayo yote ni machapisho yanayopatikana kwa urahisi, tasnifu - hasa zilizoandikwa na watafiti kutoka eneo hili - na kumbukumbu za semina za fani za historia na akiolojia. Mwisho, mawazo na msimamo wa watu wanaohusika moja kwa moja umeelezwa kwenye nyaraka kadhaa zilizochapishwa katika Kiingereza na Kihausa, mathalani *Tarihi ya Kano.*

Ruwaza hii ya utafiti usio linganifu inamaanisha kuwa jumuiya mbalimbali za kisiasa haziwezi kushughulikiwa kwa kina kilekile. Kuwepo kwenye nafasi ya pembezoni kwa Borgu, Kwararafa na Nupe katika kipindi tunachokishughulikia vilevile, kwa kiasi fulani, kumechangia kutokea kwa hali hii.

## *Madola ya Kihausa*

## Maendeleo ya Kisiasa

Kila Sudani ya kati ya baada ya mwaka 1500 inapojadiliwa, imekuwa ni kawaida kuangalia athari maalum ya Sudani ya magharibi - Mali na Songhai - na Kanem-Borno. Karne ilianza na kampeni ya *askiya* Muhammad huko Azbin. Aidha, watu walikuwa bado wanakumbuka kwa shauku tawala za zamani za maliki walioitwa *sarakunan noma* (wakuu wa mazao), *mai* (mfalme) wa Kanem na *mansa* (maliki) wa Mali. Kwa vile Sudani ya magharibi na mashariki zilijulikana zaidi, mkazo mdogo uliwekwa wakati huo kwa mabadiliko yaliyokuwa yakitokea Sudani ya kati. Hata hivyo, punde ilijumuishwa kwenye mfumo wa kibiashara na kiitikadi ulioziunganisha jamii za Sudani ya magharibi na ulimwengu wa Kiislamu. Maendeleo yake ya kisiasa




**16.1** *Nchi ya Hausa, kabla ya 1800*

yalitazamwa kwa kuyahusisha na mataifa jirani, migogoro kati ya Kano na Katsina na vipindi vya amani vilivyohusisha Kebbi, Zamfara na Gobir.

Kiunzi cha kikronolojia kilichotumika hapa kinabainisha vipindi vitatu:

(1) Miaka ya 1500 hadi 1620, wakati madola yalipopata nguvu lakini kulikuwa na ugomvi mkubwa kati ya Kano na Katsina, na Kebbi ilikuwa ndiyo dola lenye nguvu zaidi katika Uhausa ya magharibi.

(2) Miaka ya 1620 hadi 1730, wakati Kano ilikuwa ikielekea kuwa ukhalifa, Zamfara na Gobir ziliimarisha nafasi zao kufuatia kufifia kwa Kebbi, na Kwararafa ilikuwa ikiongeza zaidi uwezo wake wa kushambulia.

(3) Miaka ya 1730 hadi 1808, kipindi ambapo Zamfara iliporomoka na Gobir kufikia kilele cha nguvu zake.

## Mahusiano na maeneo jirani

Ingawa mahusiano ya Uhausa na majirani zake yanachuguzwa kwa kina zaidi, bado kuna maeneo yenye ubishani.

Kwa upande wa Songhai, umuhimu usiostahili umewekwa kwenye mamlaka ya *askiya* Muhammad. Matokeo makuu ya kampeni yake huko Azbin yalikuwa ni kujitokeza kwa Kebbi kama dola huru mwaka 1516. Kwa hali hiyo Songhai ilijaribu kuidhibiti tena Kebbi. *Askiya* Muhammad II Benkan Kiriai (1531-7) aliongoza mashambulizi kunako takribani 1533 lakini akashindwa. Mashambulizi mengine yalifanywa 1552 wakati wa utawala wa *askiya* Dawud, ugomvi ambao ulimalizwa kwa mkataba wa amani wa 1553.

Azbin ilifanywa kisingizio cha mapigano kati ya Kebbi na Borno. Kwa vile Kebbi iliendeleza uvamizi wake, Azbin iliomba msaada wa Borno kunako 1561. Baada ya ushindi wa awali kule Surame, jeshi la Borno lenye wapiganaji 100,000 lilipigwa na Wakanta huko Nguru. Kisha, mwishoni mwa karne, mgogoro wa koo tawala ulizuka Azbin. Yusuf, baada ya kupokonywa madaraka na Muhammad ben al-Mubarak (t.1601), aliomba msaada wa Kanta Dawud. Kanta Dawud, aliyetaka kuendeleza uwezo wake, alimsaidia Yusuf kumshinda adui yake aliyeungwa mkono na Borno. Ushindi huu ulizuia hila za *mai* dhidi ya Azbin, iliyokuwa kwenye kilele chake cha usitawi chini ya utawala wa Muhammad al-Mubarak (t. 1653-87). Kunako 1674, akitumia nafasi ya ugomvi ulioendelea kati ya Gobir na sehemu ya mashariki ya Uhausa na kati ya Zamfara na Kebbi, Muhammad alituma kikosi kilichoongozwa na mwanae Agabba, ambaye aliishinda Adar na hivyo kuchapusha kuporomoka kwa Kebbi. Kuanzia hapo na kuendelea, ni Zamfara na Gobir ndizo zilizojaribu kupunguza nguvu za Azbin katika maeneo ya Kwanni. Mwaka 1675, ugomvi kati ya Azbin na Zamfara ulipelekea kwenye mauaji ya kinyama na vita. Gobir, iliyokuwa ikipora katika eneo hilihili, ilishambuliwa na kushindwa na Azbin kunako takribani 1689. Mwisho, Agabba, ambaye alikwisha kuwa Sultani, aliivamia Surame na kumuua Kanta Ahmadu. Mwaka 1722, kitala cha Kebbi kilirudi nyuma kuelekea maeneo ya magharibi. Hata hivyo, Azbin ilianza kuingia katika kipindi cha migogoro

ya kinasaba na majanga, na hali hii iliziacha Zamfara na Gobir kushika nafasi ya uongozi katika eneo hili.

Kabla ya mwaka 1561, Borno ilikuwa na nguvu. *Sarkin* Kano Abdullahi (1499-1509) alishambuliwa na *mai* na kuchukua mwelekeo wa utiifu mkubwa, jambo lililomfanya mchokozi aondoke. Hata hivyo, mrithi wake, Muhammad Kisoki (1509-65), alivamia jiji la Nguru huko Borno, ambako alitoa amri ya kupora farasi na nguo tu. Akiwa kashitukizwa, *mai* alichukua hatua mwaka uliofuata na kushambulia Kano, lakini alilazimika tena kujitoa. Aibu aliyopata *mai* toka kwa Kisoki ilikuwa ishara ya uwezo wa Kano wakati Borno ilipokuwa imekumbwa na misukosuko ya ndani na njaa kwa miaka kadha.

Muda mfupi tu baadaye Kano ilianza kushambuliwa mara kwa mara na Kwararafa: kati ya 1582 na 1618 wananchi wake walilazimika kutafuta hifadhi Daura. Utawala wa Kano ulifukuzwa tena 1653, na wananchi wake kwa mara nyingine wakatafuta hifadhi Daura kunako 1671. Kwa mujibu wa C.A. Palmer, mkataba wa amani uliosainiwa kati ya Kano na Katsina (t.1649-51) ulichochewa na hofu kwa Kwararafa, ambayo hatimaye ilishindwa na Borno kunako 1680.

Ugomvi huu unaonyesha ulinganifu usio thabiti kati ya majirani wenye nguvu.

## Harakati kwa ajili ya hegemonia

Njia ya Gwanja-Kano-Borno ilikuwa imekwisha funguliwa kati ya 1438 na 1452. Zaidi ya hayo, kunako karne ya kumi na tano, Agades ilikuwa imekwisha chukua nafasi ya Takedda kama kituo cha misafara, hivyo kuifanya Katsina kuwa kituo cha mwisho.cha njia ya misafara ya kuvuka Sahara, na kituo cha biashara kwa Uhausa yote. Migogoro ya kijeshi kati ya Kano na Katsina huenda ilisababishwa na mashindano kati ya mataifa haya mawili ya kudhibiti kituo cha mwisho cha misafara ya kuvuka Sahara, lakini hakuna kinachofahamika mintarafu hali na ukubwa wa vita hivi.

Ugomvi wa kwanza ulizuka wakati wa utawala wa Rumfa (t. 1463-99), mtawala mkwasi sana na wa kwanza kusindikizwa na jeshi la farasi wenye vifaa vyote kwenye vita dhidi ya Katsina. Vita hivyo vilichukua miaka kumi na mmoja, bila mshindi kamili kupatikana.

Ugomvi wa pili ulitokea wakati wa Abu Bakr Kado (t. 1565-73), wakati Ibrahim Badankari akitawala Katsina. Wakatsinawa walifika hadi kwenye malango ya Kano, wakashinda na kurejea nyumbani.

Ili kulipiza kisasi ushinde huu, Muhammad Shashiri (t. 1573-82) aliandaa mashambulizi dhidi ya Katsina, ambako Muhammad Wari (t. 1575-87) alikuwa akitawala. Pambano lilifanyika Kankiya, Kano ilishindwa na mtawala wake kuondoshwa madarakani.

Mapambano yaliyofuatia yalitokea wakati wa utawala wa Muhammad Zaki (t. 1582-1618) wa Kano. Huko Katsina Muhammad Wari alirithiwa na Sulayman (t. 1587-1600) na Uthman Nayinawa (t. 1600-18). Kuna mkanganyiko kuhusu nini

kilitokea baadaye, na huenda kulikuwepo na mabadiliko ya nasaba tawala. Katsina ilikuwa na nguvu mno kiasi kwamba Kano ilihofia kushambuliwa nayo. Hata hivyo, Kwararafa iliivamia Kano, ikaishinda na kuidhoofisha. Muda mfupi baadaye, Muhammad Zaki wa Kano alimwona *ulama* na kupata zindiko kwa bei kubwa. Ikiwa na ulinzi huu imara, Kano ilishambulia majeshi ya Katsina na kuibuka mshindi.

Mara tu baada ya kutwaa madaraka huko Kano, Muhammad Nazaki (t. 1618-23) alitoa mapendekezo ya amani yaliyopuuzwa na Katsina, ambayo ilishindwa vita tena. Wakati wa utawala wa Kutumbi (t. 1623-48) Kano iliibana Katsina na kulikuwepo na mfululizo wa visa. Katika moja ya mashambulizi, jeshi la Kutumbi lilifurushwa na Muhammad Nazaki akanawa. Mmoja wa warithi wake, Shekarau (t. 1649-51), alifaulu kupata makubaliano ya amani baada ya mazungumzo yaliyoendeshwa na *ulama*. Nguvu za Katsina ziliimarishwa zaidi bila mkataba wa amani na Kano kuvunjwa.

Hivyo kulikuwepo na mapambano ya muda mrefu kwa ajili ya udhibiti wa Uhausa ya mashariki.

## Vipumziko

Hadi mwishoni mwa karne ya kumi na sita, Kebbi haikumwogopa adui yake yeyote, hata Moroko. Miongoni mwa sababu zilizochangia kuimarika kwa dola hili, kama alivyorai mwandishi mmoja, ni mchanganyiko wa asili za wananchi wake, kugawanyika kwa upinzani dhidi ya utawala wa Songhai, na dhamiri ya viongozi wake wa kijeshi kulinda uhuru wa nchi. Baada ya mapigano na Zamfara, Kebbi iliishinda Borno kunako 1561 na ikapanda na kushika nafasi ya uongozi katika maisha ya kisiasa ya Uhausa.

Mji mkuu wa Gobir ulikuwa umekwisha hamishwa kutoka Azbin hadi Uhausa, pale Birnin Lalle, katikati ya eneo lenye watu wengi na maji mengi la Gulbin Tarka, kunako takribani 1450. Watawala walibakia hapo hadi takribani 1600, wakati Watuareg walipofanya shambulio. Wagobirawa walilazimishwa kutangatanga tena na wakaelekea kusini. Ndipo walipoelekea kaskazini-magharibi na kuanzisha Gwaran Rama mpya mnamo takribani 1685-90. Kutoka jiji hili, Uhan Doro alifanya mashambulizi dhidi ya Kebbi na hata dhidi ya Uyoruba na Gurma. Mrithi wake, Soba, alishambulia Adar, Kebbi na Maradi. Hata hivyo, alianzisha mahusiano ya kirafiki na Zamfara, yaliyoifungua Alkalawa kwa wakulima na wafanyabiashara wa Gobir. Umwinyi wa kijeshi wa zamani polepole ulibadiliwa na umwinyi mpya ambao msingi wake ulikuwa fedha. Kuporomoka kwa Gobir kulianza mara tu Zamfara ilipoanza dhahiri kupata nguvu.

Kunako katikati ya karne ya kumi na saba, Zamfara iliongozwa na watawala imara waliosaidiwa na Uislamu. Aliyu, mtawala wa Kiislamu wa kwanza wa Zamfara, alianzisha mahusiano mazuri na Katsina na akajenga misikiti huko. Zamfara ilisitisha mashambulizi yake ya hapa na pale na badala yake ikaimarisha mashambulizi yake kwenye miji mikubwa ya Kebbi. Mwaka 1674, Sulayman alilifurusha jeshi la Kebbi.

Katika mwaka huohuo, Kebbi ilipoteza Adar, iliyopokonywa na mwanamfalme Agabba, kama tulivyoonyesha hapo juu. Ulikuwa ni mfululizo wa ushinde tofautitofauti na sio shughuli ya pamoja ya Azbin, Gobir na Zamfara. Baada ya ushindi huu, Zamfara likawa taifa lenye nguvu zaidi katika eneo hili, kama ilivyodhihirishwa na ushindi wake dhidi ya jeshi la Kano wakati wa utawala wa Muhammad Sharif (t. 1703-31).

Hivyo Zamfara ilikuwa imetengemaa baada ya athari ya kushindwa na Azbin, lakini nguvu za kijeshi za Gobir zilikuwa pia zikiongezeka. Wakati wa utawala wa Kumbari (t. 1731-43), kulikuwa na vita vikali kati ya Kano na Gobir, ambayo *sarkin* wake aliitwa Soba. Kushindwa na kulipizana kisasi kulifuatana mwaka baada ya mwaka, na mauaji ya kikatili yalikoma tu baada ya kifo cha Kabi. Punde Gobir ilianza kuhisi athari ya vikwazo ilivyowekewa na *sarkin* (wa) Zamfara, aliyekuwa na wasiwasi na jirani yake asiyetulia. Mwanzoni Gobir iliridhika kuwashambulia mara kwa mara adui zake, lakini sasa ilitumia fursa ya mgogoro wa kinasaba kuiteketeza Birnin Zamfara kunako takriban 1762.

Jambo hili liliathiri hali ya kisiasa katika maeneo ya pembezoni. Upande wa mashariki, usultani wa Damagaram ulianzishwa mwanzoni mwa karne ya kumi na nane, wakati ambapo mataifa ya Tsotsebaki yalikuwa yakiimarisha mshikamano wao kabla hayajatenganika baadaye. Eneo hili, lililokuwa la mpito kati ya Borno na Uhausa, lilikuwa nyeti sana kwa maendeleo ya kisiasa na kiutamaduni.

Upande wa kaskazini-magharibi, historia ya Adar inajulikana vizuri, lakini bado haijafahamika wazi uhusiano wake na Kurfai ulikuwaje. Kurfai pengine huhusishwa na Adar, ilhali pengine huhusishwa na Borno.

Zarma, sehemu ya mashariki kabisa ya himaya ya Songhai, ilianzisha kwa mara ya kwanza ushirikiano na Uhausa wakati Gobir ilipokuwa sehemu ya Azbin. Wakati huo Kebbi, Zamfara na Gobir zote zilikuwa zinapigania eneo hili. Kabla haijateketezwa kunako 1722, Kebbi ilikuwa na nafasi muhimu ya kisiasa katika Zarmatarey, ambako jina lake lilihusishwa na askari farasi waliokingwa na *lifidi* (deraya-mfarishi) ambao walieneza hofu kuu.

Mwisho, upande wa magharibi, kwenye *gurma* (ukingo wa kulia) ya mto Niger, baadhi ya kootawala za Gulmanseba zilidai kutokea Sudani ya kati, Borno na Uhausa – dai ambalo laekekea kuthibitishwa na machimbo ya kiakiolojia, hasa kwa maeneo ya *hausa* au ukingo wa kushoto.

Hata hivyo, hali iliimarika zaidi baada ya ushinde wa Zamfara kunako 1762. Katsina, pamoja na matatizo yake ya ndani, iliweza kuishinda Gobir, wakati ambapo huko Kano, Babba Zaki (t. 1768-76) aliwatisha sana washirika wake.

## *Utaratibu wa kisiasa na kiutawala*

Hivyo, licha ya migogoro ya kijeshi, mataifa haya yaliendelea kuwepo. Baada ya kushindwa vibaya, watawala wa Kebbi na Zamfara walikimbilia kwenye eneo dogo

zaidi ili kulinda mamlaka yao. Hali hii inaweza kuwa ndiyo iliyopelekea kuanzishwa na kuendelezwa kwa mfumo wa *sarauta* (ufalme) katika Sudani ya kati.

*Sarki*

Juu kabisa ya taifa, ambalo awali ya yote lilikuwa *kasa* (eneo), alikuwepo *sarki*, ambaye mhenga wake alikuwa kashika madaraka ya kisiasa. Huko Kano, Katsina na Zamfara, madaraka yalipokonywa toka kwa kuhani mkuu, ambapo huko Kebbi ni *magaji* (askari) aliyepanda cheo na kuwa *sarki*.

Uteuzi wa mrithi wa ufalme lilikuwa jukumu la jopo maalum la uchaguzi. Huko Katsina jopo lilijumuisha wajumbe wanne. Ni vigumu kusema kama jopo la aina hii lilikuwepo Kebbi wakati huu, lakini bila shaka lilijitokeza baadaye. Huko Zamfara, Gobir na Kano, jopo hili liliitwa *tara* (tisa), likifuatiwa na jina la dola. Majina na kazi za majopo mbalimbali ya uchaguzi yanatofautiana, lakini mjumbe mmoja anatambuliwa kuhifadhi cheo cha zamani sana, cha *basase,* huko Zamfara, na, licha ya huyo, walikuwepo magavana wa majiji na mikoa muhimu na watumishi wa umma wa ngazi za juu. Walijumuisha pia wawakilishi wa nasaba tawala zilizopinduliwa na zinazoendelea kutawala.

Mrithi alitakiwa kuchaguliwa kwa kauli moja na wachaguzi wakuu. Mara baada ya kuteuliwa, taratibu za kumsimika zilifanyika. Jopo la uchaguzi vilevile liliunda baraza la *sarki,* na lilikuwa jambo la kawaida kwa baraza kukwaruzana na *sarki* au kwa *sarki* kumzuia mmojawapo wa wajumbe wa baraza.

## Serikali

*Sarki* alitekeleza mamlaka yake kupitia vikundi vitatu vya maofisa: wana-nasaba tawala, watumishi wa umma, magavana wa miji na mikoa.

Wana-nasaba tawala walipangiwa majukumu muhimu. Dada wa mtawala alikuwa na nafasi kubwa sana ya kisiasa, ingawa aliitekeleza kupitia ibada ya kimila. Historia ya Kano ina majina mengi ya dada mashuhuri wa watawala waliopita. Kama *madaki* (mama malkia) Auwa asingekuwa ameingilia kati, bila shaka Abdulahi (1499-1509) angefukuzwa na maasi. Mwanaye, Kisoki, alitawala jiji akiungwa mkono na *madaki* Auwa yuleyule, nyanya yake, Iya Lamis, mama yake, na Gulli, kakaye Auwa.

Katika kinachoweza kuitwa serikali kuu, kulikuwepo na kategoria kadha za maofisa:

(1) Waadhama wa kitala waliendesha shughuli za ikulu (kasri) na jiji. Walikuwa ndiyo kiungo kati ya *sarki* na serikali za mikoa.

(2) Wawakilishi wa vyama vya kifani (guilds) waliteuliwa kutoka miongoni mwa mafundistadi, kama vile wahunzi, wafumaji, watia rangi, watengeneza ngozi, waashi, wachinja nyama na wawindaji. Waliwajibika kuchunga uhusiano na vikundi mbalimbali vya kiufundi na kikazi, hususani kukusanya ushuru wa serikali.

(3) Wakazi wenyeji walikuwa na wawakilishi wao. Kijiji cha Sarkin Naya na mkoa wa Sarkin Mazum, kwa mfano, vilihifadhi vyeo vyao hata baada ya Gobir kuanzisha makao yake makuu kule Hisatau.
(4) Wahamiaji, ambao walikuwa wengi, pia waliruhusiwa kuwa na wawakilishi wao. Huko Gobir, *sarkin* Azbin alishughulikia ushirikiano na Watuareg walioishi nchini, na *sarkin* Fullani alifanya vivyo hivyo kwa Wafulbe.
(5) Jumuiya ya Waislamu ilikuwepo kila mahali na *mallamai* (wanazuoni) wake.

Kwa upande wa serikali ya mkoa, au kwa usahihi zaidi, udhibiti wa kieneo, tofauti lazima ibainishwe kati ya kategoria kadha:

(1) Mamlaka ya magavana wa baadhi ya majiji yalikuwa na uhuru kamili, hayakutegemea nasaba tawala. Pengine mahusiano ya magavana hawa na mtawala yalikuwa magumu, kwa vile hatimaye walichukuliwa kuwa kama vibaraka tu.
(2) Magavana wa majiji na mikoa mingine walikuwa ama malodi ambao wahenga wao walishakuwa marafiki wa nasaba tawala huku wakihifadhi mamlaka yao, au watumishi wa umma. Zamfara ni kielelezo cha kategoria ya kwanza, ikiwa na *danau* aliyepata cheo chake kutokana na mji alimokuwa akiishi, kituo muhimu cha kibiashara alichokitumia kusimamia barabara zilizoelekea kusini na magharibi mwa Kebbi. Huko Kebbi, *innamme* alisimamia mpaka wa magharibi. Kule Katsina, *marisa* (mwangamizi) aliishi Gwiwa na kusimamia mpaka wa mashariki, ilihali *gatari* (shoka) wa Ruma alisimamia mpaka wa kaskazini-magharibi.
(3) Magavana wengine walikuwa ni nyenzo tu ya shughuli za kiserikali. Wahamiaji waliendeleza mfumo wao wa utawala msonge.
(4) Mwisho, baadhi ya vyeo vilitokana na maendeleo ya kihistoria. Huko Kebbi, *kokani* alishughulikia uhusiano na wakazi wa Kwanni baada ya eneo hilo kutekwa; Ofisi ya *saburu* ilianzishwa takriban 1650 ili kulinda barabara zilizoelekea Kwanni na Azbin.

Waadhama, malodi, wananchi wa kawaida au watumwa - wote hawa walifanya kazi zisizokuwa za kijeshi isipokuwa, mahitaji yalipotokea, walikuwa wapiganaji hodari wakiwa na vikundi vyao vya askari.

## Mpangilio wa kijeshi

Kuanzishwa kwa dola la Kebbi kulidhihirisha kungezeka kwa umuhimu wa viongozi wa kijeshi katika masuala ya kiserikali. Marafiki wa kwanza wa *kanta* walitoka kwenye familia maarufu nchini, lakini, baadaye, vikundi vilivyoshiriki katika mapambano ya uhuru vilipatiwa wawakilishi wawili, mmojawapo, *kunduda*, ndiye baadaye alikuwa kiongozi wa kijeshi wa Kebbi.

Kutokana na mahitaji ya kujilinda dhidi ya majirani na kulinda mipaka na barabara, idadi ya viongozi wa kijeshi iliongezeka, na ngazi za vyeo zikaanzishwa. Cheo cha juu kabisa kilitofautiana kutoka taifa hadi taifa: kilikuwa *kunduda* huko Kebbi, *kaura* kule Katsina, *ubandawaki* katika Zamfara na Gobir, ilihali Kano kilijulikana kama *galadima*.

Kadiri silaha zilivyoboreshwa, ndivyo mikakati na mbinu zilivyobadilika. Wakati wa kukusanya wapiganaji, huduma za stadi mbalimbali, kama vile wawindaji na wahunzi, zilihitajika. Jeshi lilijumuisha vikundi vikuu viwili - askari wa miguu, waliogawanyika katika wapiga mishale na wapiga mikuki, na askari wa farasi. Kebbi ilikuwa pia na msafara wa manowari ndogo za mtoni.

Idadi kubwa zaidi ya farasi ilitoka Azbin na Borno na walipatiwa matunzo maalum. Mtawala aliwanunua farasi hao kutoka nje na akaanzisha mazizi: *kanta* wa Kebbi, mathalani, alikuwa na mazizi katika maeneo matatu. Nafasi kubwa iliyochukuliwa na farasi inaweza kuelezeka kwa uvumbuzi kama vile matumizi ya *sulke* (deraya) na utengenezaji wa *lifidi* (deraya-farishi). *Sarkin lifidi* (jenerali wa divisheni ya askari wa farasi wa deraya) na *lifidi* (amiri jeshi mkuu wa divisheni ya askari farasi wa deraya) walikuwa miongoni mwa maofisa wa ngazi za juu kabisa.

Magobori yalikuwa yamekwisha ingizwa Kano na mwanamfalme wa Borno wakati wa utawala wa Dauda (1421-38), lakini ilikuwa baada ya karne tatu ndipo yalipoagizwa kutoka Nupe. Babba Zaki (t. 1768-76) ndiye aliyekuwa mtawala wa kwanza kuanzisha kikosi cha watumia magobori kilichomlinda yeye. Songhai, iliyopata fursa ya kutathmini uwezo wa kuangamiza wa magobori kutokana na madhara iliyokuswa nayo, haikujisumbna kuchukua magobori yaliyoachwa na askari wa Moroko nusu karne baadaye (1591 hadi 1640). Uhausa yaonekana iliisusa kwa makusudi silaha ambayo ingeweza kujinunulia kutokana na utajiri wake.

Mbinu za kivita zilizotumika zilijumuisha mashambulizi ya kushitukiza, uvamizi, mapigano ya majeshi yaliyoandaliwa rasmi na kuzingira. Ongezeko la ujenzi wa ngome kuzunguka majiji lilitokana na kuzingirwa na kuteketezwa mara kwa mara. Katika eneo hili, ambamo maendeleo ya kiuchumi yalikuwa yameongezeka, kuboreshwa kwa ufundi wa kupigana vita kuliongeza uporaji. Sio rahisi kutofautisha kati ya vita vilivyopiganwa kwa ajili ya kutamalaki au kujiimarisha, vita vya kukomesha maasi, vita vya kuwatisha maadui, na mashambulio ya kawaida. Gobir daima ililazimika kupigana ili kudumisha dola lake. Waungwana wa kisiasa, kiutawala na kijeshi walihusudu uporaji, kama *Tarihi ya Kano* inavyoonyesha: walizidi kujitajirisha na wakawapatia zawadi watawala na wanazuoni. Huko Kano, kwa muda wa karne mbili - kati ya 1573 na 1768 - walikuwa na nguvu kiasi cha kulihimiza dola kupigana vita, wakashiriki katika njama na kumtia wasiwasi mkubwa mtawala. Idadi kamili ya waadhama ilitofautiana kutoka taifa moja hadi jingine; Gobir ilikuwa na ishirini na wawili (malodi kumi na watatu na wananchi wa kawaida tisa) na Katsina arobaini na sita (malodi kumi na sita na wananchi wa kawaida thelathini).

## Rasilimali

Taifa la Kihausa lilikuwa na mfumo mzuri sana wa kudhibiti nchi na kutoza kodi. Kulikuwepo na vyanzo vikuu vya mapato vitatu:

*Kodi na ushuru*

Kodi na ushuru ndivyo vilikuwa vyanzo vikuu vya mapato. Navyo vilijumuisha:

*kudin kasa* (kodi ya ardhi), ililipwa na wakulima. Yaelekea kizio kilichotumika ni *gandum gida* (shamba la familia).

*kudin sana'a* (kodi ya weledi), ililipwa na mafundistadi na wafanyabiashara.

*kudin hito* (ushuru wa forodha), ulilipwa kwa baadhi ya bidhaa zilizoingizwa nchini toka nje. Zaidi ya hapo, chumvi iliyosafirishwa kwa meli hadi Zarmaterey na Arewa ililipiwa kodi.

*jangali* (kodi ya mifugo), ililipwa na wafugaji hasa Wafulbe. Huko Kano, ilitozwa kwa mara ya kwanza na Kutumbi (t. 1623-48). Nchini Kebbi, Wafulbe wa kinomadi walilipa *kudin haki* (kodi ya malisho), wakati ambapo mwadhamu mwenye cheo cha *nono* alikusanya maziwa na siagi kwa ajili ya mtawala.

*Zawadi*

Magavana, waadhamu na watu wengine mashuhuri walimpelekea mtawala *gaisuwa* (zawadi iliyoandaliwa kwa ajili ya mkuu). Hili lilikuwa suala la kisiasa ambapo mhusika alimzawadia *sarki,* kwa matarajio kuwa naye angepatiwa upendeleo fulani na huyo *sarki*. Wale walioteuliwa kwenye nyadhifa za kiandamizi pia walitoa zawadi kwa *sarki*. Mbinu ya kawaida ya kupata mali ya kutolea *gaisuwa* ilikuwa ni uporaji.

*Ngawira*

Utekaji nyara ulileta watumwa, farasi, ng'ombe na bidhaa nyinginezo. *Tarihi ya Kano* inasisitiza umuhimu wa farasi kati ya 1582 na 1623. Watumwa waliuzwa au waligawiwa miongoni mwa milki kuu za kifalme.

*Rasilimali nyinginezo*

Zilikuwepo njia nyingine chungu nzima ambazo *sarki* angeweza kuzitumia kujaza hazina ya serikali. Kwa mfano, endapo mtawala alimsamehe mkosaji, basi mkosaji alipaswa kulipa *kudini laifi* (kodi ya msamaha). Kwa kutumia *Tarihi ya Kano*, inawezekana kubaini jinsi kodi na ushuru mwingine ulivyoanzishwa kwa faida ya taifa. Sharif (t. 1703-31) alianzisha kodi saba zilizochukuliwa kuwa za kikandamizaji, ukiwemo ushuru uliolipwa na wasichana walipokuwa wakiolewa. Mrithi wake, Kumbari (t. 1731-43), aliwalazimisha wanazuoni kulipa ushuru, jambo lililowafanya Waarabu kuondoka na kuhamia Katsina.

## Muhtasari

Mfumo wa *sarauta* uliendelea kwa namna ambayo iliwawezesha wananchi wa

kawaida na watumwa kupatiwa nyadhifa za juu kabisa iwapo walionekana kuwa ni waaminifu. Kwa hiyo watumwa wa mfalme, hususani matowashi, walikuwa na nafasi muhimu serikalini katika eneo lote.

Hali hii ilipelekea katika upinzani kati ya *mai sarauta* (mtawala) na *talakawa* (watawaliwa). Kwa kiwango kidogo, magavana wa majiji na mikoa wangeweza kuwa wapinzani. Maasi ya mara kwa mara ya magavana wa Gaya na Dutse yanaonyesha kuwepo kwa misuguano kati ya mtawala na vibaraka katika historia ya Kano.

Waungwana wa kisiasa, kiutawala na kijeshi waliunda kikundi kilichofanana ambacho kilijilimbikizia utajiri kutokana na mbinu mbalimbali za unyonyaji. Waliendesha maisha kulingana na utajiri wao, na wakajipamba vilivyo kuonyesha ufahari wao, huku wakiwa wagumu kudhibitiwa kwa sababu ya ufisadi na utoaji rushwa.

## Mahusiano ya kiuchumi

### *Kilimo na ufugaji*

Kutoka 1500 hadi 1800, Uhausa ilibaki kimsingi kuwa ni eneo la wakulima. *Manoma* (wakulima wadogo) walilima kwa kutumia mbinu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na mbolea na kubadilisha na kuchanganya mimea. Zana zao zilikuwa za aina nyingi kama ilivyo sehemu nyingine za Afrika, yakiwemo majembe ya aina mbalimbali kulingana na hali ya udongo. Kiwango kikubwa cha nguvu-kazi kilitokana na *gida* (familia pana) na *gayya* (mfumo wa kusaidiana kazi).

Licha ya mtama, serena, mpunga, mahindi, karanga na maharage, wakulima walipanda pamba, nili, mihina, tumbaku na vitunguu. Mishea, mikwaju na *nere* pia ililimwa na asali ilirinwa. Aidha walijishughulisha na uvuvi na uwindaji. *Jibda* (maski) ilitolewa katika ngawa na kutumika kutengenezea zabadi (aina ya manukato).

Kulikuwepo na kiwango kikubwa cha ufugaji kwa matumizi ya ndani. Mbuzi walitolewa kafara kwa kuwakata shingo zao katika baadhi ya sherehe, ilihali punda walitumika kwa usafirishaji, hasa na wafanyabiashara. Wafulbe, wakiwa na kondoo na ng'ombe wao, walifanya makazi katika maeneo kadhaa ya Katsina, Kebbi na Zamfara. Kilimo na ufugaji vilifungamana sana, na yalizuka maisha ya kiuchumi yaliyokitwa katika shughuli hizi mbili, kama vile katika eneo la Ingawa huko Katsina.

### *Ufundistadi*

Uanuwai na viwango vya juu vya kiufundi vilivyofikiwa na mafundistadi vilikuwa tayari vikisifika wakati wa Leo Africanus: watu walifanya kazi wakitumia chuma, mbao na ngozi, na pia walijishughulisha na utengenezaji vikapu na ufinyanzi huku kukiwepo na maendeleo makubwa katika ufumaji na utiaji rangi. Zaidi ya hayo, mahitaji makubwa ya bidhaa yalisisimua utengenezaji wa bidhaa bora zaidi.

Mwelekeo wa vikundi kubobea katika fani fulani waweza pia kuonekana. Huko Kebbi, ufumaji na utiaji rangi ulifanywa na Wakebbawa; Zamfara iliwavutia wafumaji na watia rangi toka Kano. Nchini Kebbi na Zamfara, Wazoromawa

walibobea katika usonara wa fedha na ufinyanzi; huko Kano, ufinyanzi ulifanywa na Wabambadawa.

Vitu mbalimbali vilitengenezwa. Ngozi, makubadhi, hatamu na matandiko (ya farasi) vilinzwa nje ya nchi. Johari zilinunuliwa na matajiri. Nguo, mathalan kanzu , zilisifika kwa ubora wake. Uhausa ilikuwa pia miongoni mwa maeneo yenye kutoa bidhaa bora zilizofumwa na kutiwa rangi.

*Biashara*

*Bahausha* (mfanyabiashara) ni mtu aliyejulikana sana, akajipenyeza kwenye mtandao wa wafanyabiashara wa Afrika magharibi na tabaka la wafanyabiashara wa kimataifa katika savana.

Maeneo yaliyoat hiriwa na masoko yalitofautiana sana. Baadhi ya masoko yalikuwa muhimu palepale yalipokuwa, na yalihifadhi sifa zake za kijamii na kiuchumi: bidhaa ziliuzwa, lakini maisha ya kijamii yalichangamka sana siku ya soko. Katika ngazi ya juu, soko la ukanda kilikuwa kituo ambapo bidhaa kutoka maeneo mbalimbali zililetwa na ambapo bidhaa za matumizi ya kila siku zilizoingizwa kutoka nje ziligawanywa. Katika Zamfara yenyewe, masoko ya kaskazini na kaskazini mashariki yalitoa pamba, nili, tumbaku, vitunguu na ng'ombe, ilihali masoko ya kusini yalipatiwa nafaka za kutosha. Kebbi ya Juu ilipeleka kitani, vitambaa na watumwa huko Kebbi ya Chini, ambayo nayo ilitoa nyavu, chusa, ngozi na *abara* (mitumbwi mikubwa iliyochimbwa).

Biashara ya nje ilibakia mikononi mwa Wahausa, ingawa Waazbinawa, Waarabu, Wakanuri na Wawangara wachache walishiriki pia. Misafara iliiunganisha Kawar na Gao, Azbin na Uhausa, na Kano na Gwanja. Kila mtawala alichukua hadhari ya kulinda misafara katika eneo lake kwa vile misafara hiyo ililipa kodi kwa nchi ilimopita.

Kulikuwepo na masoko kadhaa ya kimataifa ndani ya ukanda na pembezoni mwake. Upande wa kaskazini, Agades na Bilma zilikuwa kiungo na Afrika ya kaskazini; upande wa katikati Katsina na Kano vilikuwa vituo vya mahusiano kati ya kaskazini na kusini na mashariki na magharibi; upande wa kusini, Zaria, Birnin Gwari na Birnin Yawusi ziliwezesha mtandao kupanuliwa kuelekea Yoruba, Nupe, Borgu na Gwanja. Idadi ya kutosha ya Bidhaa ilizunguka ndani ya Uhausa.

Sahara na Azbin zilipeleka bidhaa za Kiarabu na Kizungu kwenye masoko haya, vikiwemo vioo na karatasi, lakini hasa farasi, ngamia, tende, hina, chumvi, mapanga na bidhaa nyinginezo. Kiasi fulani cha chumvi na mapanga kilikuwa kingali kinasafirishwa kuelekea kusini. Kwa upande wake, Uhausa iliyapatia masoko haya watumwa, nguo, vitambaa, mtama, ngozi, vumbi la dhahabu na kola kutoka Gwanja.

Borno ilitoa farasi, natroni na chumvi ikibadilishana na bidhaa za metali, vumbi la dhahabu na kola. Uhausa iliziuzia Gwanja, Borgu, Nupe na Uyoruba chumvi, mapanga, viungo, ngozi, nguo na vitambaa, watumwa na farasi, na yenyewe ikanunua bidhaa mbalimbali za Ulaya, chuma cha kienyeji, wanja wa manga (antimoni), watumwa na matowashi, magobori kutoka Nupe (kwa ajili ya Kano) na

kola kutoka Gwanja kwa matumizi ya ndani.

## Mahusiano ya kijamii

Vikundi vikuu vitatu vinaweza kuainishwa katika jamii:

*Wazalishaji wa mali*

Wakulima ndio waliounda kikundi kikubwa kuliko vyote. Matumizi shadidi ya ardhi na uboreshaji wa kilimo ulikuja kuleta mabadiliko makubwa. Hadi wakati huo, chanzo kikuu cha nguvu-kazi kilikuwa familia pana. Ni dhahiri kwamba baadhi ya vikundi vya watu vilichukuliwa kama watumwa: Wamezumawa, kwa mfano, walipoteza uhuru wao mara tu Gobir ilipofika eneo la Birnin Lalle. Wamaguzawa wa Fanfui walikuwa watu wa hadhi ya chini na, hivyo, walipa kodi tu kwa nchi nyingine. Chanzo cha mwisho cha nguvu-kazi kilikuwa watumwa.

Miongoni mwa mafundistadi kulikuwepo na ubobezi mkubwa katika fani tofautitofauti, na watumwa wengi walifanya shughuli walizoamriwa na waajiri wao, na kwa faida ya waajiri hao, hasa mwanzoni mwa shughuli. Idadi kubwa ya wafugaji walianza kuishi maisha ya kustakimu (kukaa mahali pamoja). Waliwaajiri watumwa, ambao haraka walijumuishwa katika jumuiya ya kisiasa.

Hata kama wazalishaji walikuwa watu huru, walipa kodi au watumwa, wote walikuwa wanajumuiya ya kisiasa na mahusiano yao na dola yaliwekwa katika mpango ulio wazi. Tofauti zilizotokana na utajiri na ukaribiano na vyombo vya dola polepole zilianza kujitokeza.

*Wafanyabiashara*

Wafanyabiashara waligawanyika katika vikundi kadhaa, kutoka wauzaji wa jumla waliojihusisha na *fatauci* (biashara ya masafa ya kati na marefu) hadi wauzaji wa rejareja walioandaa *kasuwanci* (biashara ya rejareja). Kikundi cha *attajirai* (wafanyabiashara matajiri) kilichipuka na kilijumuisha wafanyabiashara waliojihusisha na watumwa, farasi, kola na nguo. Wafanyabiashara na wasomi yaonekana daima walikuwa na ushirikiano wa karibu. Wafanyabiashara waliunganishwa na biashara yao na hawakusita kuhama walipoona kuwa walikuwa wakilipishwa kodi kubwa mno.

Kati ya mwaka 1500 na 1800, vikundi mbalimbali vya Wawangara na Wahausa vilifaulu kuunganisha mitandao ya kibiashara katika Afrika ya magharibi yote na kuunda tabaka la kati katika miji mikubwa. Waliendelea kuimarisha nafasi yao kama tabaka na wakaeneza imani ya Kiislamu kwa manufaa yao.

*Makabaila*

Tabaka la watawala lilijumuisha *masu sarauta* (watu wote wenye mamlaka yoyote ya kisiasa). Liligawanyika katika ngazi kadhaa.

*Sarki* alikuwa mkuu wa tabaka la malodi, ambalo lilijumuisha familia za wafalme,

familia zilizotawala majiji yaliyokuwa nusu-huru na majimbo vibaraka, na wawakilishi wa mataifa mbalimbali, hususani Waazbinawa, Waarabu wa Shuwa na Wafulbe. Malodi walitekeleza majukumu mbalimbali ya kiserikali, na walielekea kuwa ni kikundi kilichofanana ambacho ushikamano wake uliimarishwa kwa kuoana miongoni mwao.

Waadhamu wote walioteuliwa na *sarki* kuendesha serikali waliunda ngazi ya pili. Walitokana na wananchi wa kawaida au watwana lakini nafasi yao ya uongozi iliwawezesha kupata utajiri na heshima kutokana na zawadi walizopewa, lakini hasa kutokana na uporaji. Pengine walikuwa na nyadhifa muhimu za kijeshi. Ni wao waliomhimiza Muhammad Nazaki kuyakataa mamlaka ya Katsina na waliopinga mashambulizi dhidi ya Katsina yaliyoandaliwa na Zaudai. Kuporomoka kwa Kebbi kulianza wakati waadhamu walioshikilia nyadhifa za kijeshi walipokuwa matajiri mno kiasi cha kutojali tena masuala ya kitaifa.

Makabaila, hususani wanamfalme na watumwa wa kifalme, walinyang'anya mali ya *talakawa* (watawaliwa) hasa pale mtawala alipoonyesha dalili za kuwa dhaifu.

Suala la mahusiano ya kijamii yaelekea lilitawaliwa na mambo mawili: uuzwaji wa Waafrika uliofanywa na baadhi ya watawala na ushiriki wa Kawar na Zawila katika biashara ya watumwa. Huko Kanem, ishara za kwanza za uuzaji nje watumwa na matumizi yao ndani ya nchi zilionekana tangu mapema kunako karne ya kumi na moja. Katikati ya karne ya kumi na tano *galadima* Dawuda alikwenda na kupigana vita na kumpelekea *sarkin* Kano watumwa thelathini kila miezi miwili. Ilipofikia mwisho wa kampeni, alikuwa amekusanya watumwa 21,000 waliosambazwa miongoni mwa vijiji ishirini na moja, vyote vikiitwa *indabo*. Neno *indabo* (kijiji cha watumwa) linakumbushia neno *debe* la Kisoninke, *debeere* la Kifulfude na *dabey* la Kisonghai. Katika vijiji hivi shughuli za uzalishaji zilikuwa ufundistadi na hasa kilimo. Huko Katsina, jiji la Tsagero lilikuwa mali ya kifalme ambako watumwa wengi walihifadhiwa, na ambako hata wanamfalme walipelekwa. Katika mashamba makubwa ya eneo la Gozaki, kilimo cha pamba hatimaye kilitegemea watumwa walionunuliwa kutoka Zazzau, na sehemu ya zao hilo iliuzwa Kano.

Bila kujali kama mtumwa alikuwa bidhaa, mtumishi, ofisa wa ngazi ya juu au mzalishaji huru wa chini, alikuwa na nafasi muhimu katika maendeleo ya uchumi na taifa. Hata hivyo, uuzaji nje watumwa hauna budi kuangaliwa kwa kuuhusisha na vyauzo vya upatikanaji wa watumwa huko Ulaya na Mashariki, hata kabla biashara ya Atlantiki haijaanza kudai sehemu yake. Mchango wa utumwa katika usitawi wa eneo hili utakuwa wazi zaidi utumwa utakapotazamwa kipekee miongoni mwa aina nyingine za ukandamizaji.

*Masu sarauta* (makabaila) waweza kuchukuliwa kama wapinzani wa *talakawa,* ambao walikuwa wazalishaji huru lakini hawakuwa na mamlaka ya kisiasa. Kadiri makabaila, wanazuoni na wafanyabiashara walivyozidi kutajirika, tofauti za kijamii zilihamia kwenye ngazi ya kiuchumi na kuwa kati ya *attajirai*, matajiri, na *talakawa,* masikini. *Bawan sarki* (mtumwa wa kifalme) alikoma kuwa *talaka,* kisiasa na

kiuchumi. Kwa namna hii hali ikawa wazi, kwa sababu tofauti za kimbari na kidini zilifutikwa, na hivyo kuwaacha walio madarakani na wananchi wa daraja la pili wakipambana.

## Utamaduni na dini

Maendeleo ya kisiasa na kiuchumi yalisababisha mabadiliko mengi ya kiutamaduni. Kwa upande wa vitu vya kuonekana, mathalani, usanifu majengo uliboreshwa na hata leo, miji bado inashindana miongoni mwao katika mitindo yake. Katika medani ya muziki, baadhi ya ala, kama vile *kakaki* na *algaita,* zilienea kote na okestra zikatumika kwenye sherehe za kifalme. Sifa kuu ya Uhausa katika snala hili ilikuwa utajiri wake na umoja wa kiutamaduni - matokeo ya msawazisho uliokifanya Kiguber kuwa mojawapo ya lugha kuu za mawasiliano ya kimataifa Afrika, ikitumia jina la *Kihausa.*

Mwanzoni mwa karne ya kumi na sita usilimishwaji uliwahusu wafanyabiashara na wanasiasa tu. Hata hivyo, mwisho wa kipindi hiki ulitawaliwa na ongezeko la mapambano ya wazi kati ya makabaila na wanazuoni. *Tarihi ya Kano* na *Tarihi ya Wangara* huonyesha maendeleo ya mahusiano yao kutoka ndani.

Kano ilishuhudia kuingia kwa wanazuoni kwa wingi na mara nyingi. Wakati wa utawala wa Kisoki (1500-65), wanazuoni kadhaa waliwasili. Wa kwanza Shaihu Ba-Tunashe, alileta kitabu cha *ashafa;* wa pili, Dan Gwarandume, ndiye aliyekisoma kitabu hiki; na wa tatu, Shaihu Abdussalami, aliingiza vitabu vitatu. Kisha kikundi cha ndugu watatu kutoka Borno kiliwasili, mmoja wao alikubali wadhifa wa kadhi. Wakati wa utawala wa Abu Bakr Kado (t. 1565-73), kikundi cha pili cha wanazuoni, kutoka Bagirmi, kilihamia Kano. Walikuwa wamekaa kwa muda huko Katsina, ambako Muhammad Zaki (t. 1582-1618) alimwoa mmoja wa mabinti wa Tama, kiongozi wa kikundi hiki. Kutokana na ushawishi wa wanazuoni hawa Katsinawa iliacha kuipora Kano, na ni wanazuoni waliofanya mapatano ya amani kati ya Kano na Katsina kwenye kipindi cha kati ya mwaka 1648 na 1651.

Huko Birnin Katsina, iliwezekana kutofautisha kati ya vikundi kadhaa vilivyotokana na koo za Wali Abu Abdullahi B. Masani, Malam Buhari na Malam Uthman. Wasomi wengi wa usuli, mbari na asili mbalimbali waliishi kwenye miji mingine. Wasomi hawa, waliotapakaa kwenye eneo ambamo wakazi na viongozi walijichukulia kuwa wamesilimishwa, walijitenga na tabaka tawala.

Zamfara ilikuwa tofauti kwa vile Uislamu haukuwa na mashiko huko hadi baadaye kabisa, pengine kwa sababu miji yake mingi ilikuwa mbali na njia za misafara za Sudani ya Kati. Hata hivyo, wanazuoni wa Kikanuri huenda walishiriki katika kumsilimisha mtawala wake. *Imam* wa Anka alikuwa na miliki ya kinyarubanja, na makazi yake yalikuwa kimbilio kwa wale wote walioghadhabikiwa na watawala wao. Baadhi ya nyadhifa zilihifadhiwa kwa ajili ya wanazuoni: *limanin ciki* alishughulikia elimu ya familia ya kifalme, ambapo *dan kodo* na *dan dubal* walikuwa washauri wa mambo ya kidini, wahifadhi wa historia ya Zamfara na wenye

jukumu la kuliombea jeshi ushindi vitani.

Kipato cha wanazuoni kilitegemea ukarimu wa makabaila. Hata hivyo, ni vigumu kudai kuwa wanazuoni hao walipendelea upande fulani, hata kama (mathalani huko Kano) walipewa miliki za nyarubanja na mashamba makubwa. Mtazamo wao wa kukosoa uliakisiwa kwenye *Tarihi ya Kano*.

Kusafiri mara kwa mara kwa wanazuoni na uingizwaji wa vitabu kwa kiasi fulani kulichangia kuleta mzinduko wa kitaaluma wa eneo hili. Hata hivyo, licha ya sababu hizi lazima kuongeza kuwepo kwa vituo vya elimu na, hasa, matumizi ya hati ya *ajami* (maandishi yaliyotokana na hati ya Kiarabu) huko Kano na Katsina kwenye karne ya kumi na sita. Wasomi waliandika kwa Kiarabu, Kifulfulde na Kihausa.

Wakiombea ushindi katika vita na kutoa ushauri katika masuala ya kisharia, wanazuoni walikuwa na athari kubwa kwenye maisha ya kijamii, hasa kupitia *wa'azi* (hutuba). Huko Zamfara, miongoni mwa wasomi maarufu wanaotajwa ni pamoja na Ramadan b. Ahmadu (kutoka Fezzan), Hashimu Bazanfane, Maman Tukur dan Binta na al-Mustafa Gwani, Mkanuri aliyemkabili Utham alipokuwa akizuru Zamfara kuhusu ujumuishaji wa wanaume na wanawake katika hadhira moja wakati wa hutuba.

Majina mawili yamejitokeza zaidi huko Katsina. Abu Abullahi b. Masani b. Muhammad al-Barnawi al-Kashinawi (t. 1595 - 1667) na Muhammad al-Sabbagh al-Kashinawi, aliyejulikana zaidi kama Dan Marina, aliyeshamiri zaidi katika takriban 1650 na kutunga shairi la kumsifia *mai* Ali, aliyeishinda Kwararafa kunako takriban 1680.

Hata hivyo, hapana shaka kuwa Malam Jibril dan Umaru ndiye aliyekuwa maarufu zaidi katika kundi. Mwanazuoni huyu, mwenye maarifa mengi, alizaliwa Adar na kufia hukohuko Adar, baada ya kufanya safari kadhaa za kuhiji. Suala kuu alilolishughulikia lilihusu mageuzi ya Uislamu katika Sudani. Baada ya kushindwa kuwashawishi Watuareg huko Adar, aliwaendea wanamfalme wa Kihausa, na kuibusha uhasama wao. Uthman alikuwa mfuasi wake. Nusu ya pili ya karne ya kumi na nane ilijawa na shughuli nyingi za kitaaluma na majadiliano makali miongoni mwa wanazuoni, hii ikiwa ni namna sahili ya upinzani dhidi ya utaratibu uliokuwepo uliowakilishwa na *masu sarauta*.

## *Hitimisho*

Muda mfupi kabla ya jihadi, mahusiano yenye ghasia kati ya madola yalipungua sana. Kebbi na Zamfara zilikuwa zimeshindwa vitani, lakini mataifa mengine yalikumbwa na matatizo magumu. Huko Kano, amani na utulivu viliingiliwa na kutofautiana kukubwa kulikojitokeza mara mbili kati ya *sarki* na waadhamu. Nchini Gobir, Bawa (t. 1777-89) kwa mara ya kwanza alianzisha kodi kwa aina fulani ya mahindi na wafugaji walilipishwa *jangali* mara kadhaa katika mwaka uleule mmoja. Migogoro miwili ya nasaba tawala iliitikisa Katsina mnamo 1767 na 1796. Hatari ya

kukosekana kwa utulivu ilionekana karibu katika eneo lote, kutokana na upinzani wa waadhamu, ongezeko la udhalimu, na upinzani fiche wa *talakawa*. Mamlaka ya kisiasa yalikuwa yamefikia kiwango cha juu cha ukandamizaji ambao haukuwaacha kando wanazuoni, lakini wao ndio pekee waliothubutu kupambana waziwazi na utaratibu uliokuwepo.

Kiuchumi, upinzani dhidi ya maendeleo ulioonekana kujitokeza zaidi kwenye miaka ya kati ya 1600 na 1790 umekuwa ukisisitizwa kupita kiasi. Ni kweli kwamba si gurudumu wala kinu cha upepo kilitumika, na hata gobori lilidharauliwa. Hata hivyo, licha ya majanga mengi ya asili, eneo hili liliendelea vema, sio tu kutokana na kukua kwa biashara kulikosaidiwa na dola kwa njia mbalimbali, bali pia kutokana na maendeleo katika uzalishaji na usindikaji.

Kisiasa, pamoja na kupiganwa vita, hakuna taifa lililotoweka katika kipindi kinachojadiliwa. Kwingineko, Ghana, Mali na Songhai zilisambaratika, ilhali Kanem-Borno ilikuwa na maisha marefu. Mafanikio ya kiuchumi ya Uhausa yameugubika uimara mkubwa wa dola kama asasi. Hulka yake ya kirasimu na kikandamizaji ilisisitizwa na hatua zilizoanzishwa na Sharif huko Kano. Kusema kweli, vyombo vya dola vilikuwa madhubuti na vilifanyiwa mabadiliko machache tu na tawala zilizofuata.

# 17 Kanem-Borno: uhusiano wake na bahari ya Mediterania, Bagirmi na mataifa mengine katika bonde la Chad

Kwenye karne ya kumi na tatu taifa la Kiislamu la Kanem lilikuwa mojawapo ya mataifa makubwa katika *Bilad al-Sudani*. *Mais* (wafalme) wa Kisefuwa walidhibiti eneo kubwa kutoka pwani ya mashariki ya Ziwa Chad upande wa kusini hadi kwenye Oasisi za Fezzan upande wa kaskazini, lakini upanuzi wao haukuambatana na maendeleo mwafaka ya kisiasa na kiuchumi. Kuibuka kwa vikundi takriban huru vya kimbari vilivyo tofauti na nasaba tawala ya Kisefuwa kulizuia uanzishwaji wa mfumo unganifu wa kisiasa. Zaidi ya hapo, Kanem, ambayo eneo lake kubwa lilikuwa jangwa au nusu-jangwa, haikuwa na rasilimali za msingi zinazohitajika kugharamia mfumo mpana kama huo.

Mgogoro mkubwa hatima ye ulipelekea katika kuanguka kwa dola la Kanem mwishoni mwa karne ya kumi na nne. *Mai* Umar B. Idris (1382-87) akiwa kiongozi wa kikundi cha Wamgumi na watu walio kiunga mkono,, alielekea Borno, magharibi mwa Ziwa Chad, ambako rasilimali zilizohitajika zilikuweko, na ambako Wasefuwa tayari walishawapeleka vibaraka wao. Idadi kubwa ya wahamiaji wengine kutoka Kanem ilikuwa pia imekwisha tamakani huko.

Lengo kuu la Wasefuwa walipowasili huko Borno yaelekea lilikuwa kujenga uchumi imara wa kikanda ambao ungehimili mfumo wa kisiasa ulioandaliwa vizuri na kudhibitiwa na Wasefuwa. Hata hivyo, katika karne yao ya kwanza huko Borno, walikumbana na matatizo mengi ambayo wakati mwingine yalitishia hata uhai wao: misukosuko ya kijamii ya mara kwa mara, migogoro ya nasaba tawala, mashambulizi ya mara kwa mara kutoka kwa Wabulala na wakuu wengine wenye nguvu.

## Mai Ali Gaji na kuanzishwa kwa ukhalifa wa Borno t. 1465 - 1497

Ali b. Dunama, aliyejulikana zaidi kama Ali Gaji, aliweza kuimarisha mamlaka katika nasaba yake tawala. Mnamo takribani 1471, wakati Wabulala walipoishambulia Borno, aliwashinda, lakini hakuwafuatilia zaidi. Kunako takribani 1472, alijenga ngome ya Birnin Gazargamu ambayo hatimaye ilikuwa mji mkuu wa

Wasefuwa na kubakia hivyo kwa kipindi chote cha utawala wao huko Borno.

Ali Gaji anakumbukwa kama mfufuaji wa Uislamu. Alijaribu kuanzisha serikali ya Kiislamu halisi, akiwatumia *maulama* kama washauri wake. Wengi wa viongozi waliokuwa na madaraka makubwa sana walipunguziwa madaraka hayo, hasa *wakaigama* na *wayerima* (magavana wa majimbo ya kaskazini).

Wakati wa hija yake huko Maka mnamo takrihani 1484, yasemekana Ali Gaji alipatiwa madaraka ya *ukhalifa* wa Takrur. Kuanzia kipindi hiki na kuendelea, watawala wa Borno walijichukulia kuwa ni *makhalifa* - dai lililokubaliwa na wasomi na watawala wengi katika *Bilad al-Sudani.*

## *Matatizo na fursa katika upanuzi wa ukhalifa wa Borno: t. 1497 - 1564*

Sera za Ali Gaji ziliendelezwa na mwanaye aliyemrithi, Idris b. Ali, aliyetumia ubini wa Katakarmabe (t. 1497-1519), ambaye aliyadhibiti mafanikio ya Ali Gaji na kujaribu kulipanua taifa. Lakini kwa miaka hamsini ama zaidi iliyofuata Katakarmabe na warithi wake walipambana na changamoto nyingi zilizowafanya wasitimize malengo yao.

Tatizo la kwanza la Wasefuwa lilikuwa ni kuanza tena kwa mashambulizi ya Wabulala. Katakarmabe alishambuliwa na Wabulala mara tu alipokuwa *mai*. Sio tu kwamba aliwashinda bali pia aliingia tena kwa ushindi Njimi, mji mkuu wa awali wa Wasefuwa ambao, hata hivyo, kamwe haukutekwa tena. Baada ya kuwekeana mkataba na Wabulala, Idris alirejea Borno, lakini makubaliano hayo ya kusitisha vita yalidumu muda mfupi tu na uhasama wa mara kwa mara ukaendelea hadi kipindi cha utawala cha Idris Alawoma (1564-96).

Tatizo jingine la wafalme wa Kisefuwa lilikuwa ni kuibuka kwa mataifa mengi katika bonde la Chad na sehemu nyingine za Sudani, kulikowalazimisha Wasefuwa kutatua matatizo yao na kila dola.

Ilipofika mwanzoni mwa miaka ya 1500 falme nyingi ndogondogo zilikuwa zimekwisha ibuka kwenye mpaka wa kusini wa Borno. Hizi zilijumuisha Bagirmi, Mandara, madola ya Kotoko, Bolewa ya Kaskazini ya Daniski, Yamta na Margi. Baadhi ya mataifa haya yalilazimishwa kutambua namna fulani ya utawala wa Wasefuwa. Lakini mara nyingi Wasefuwa walifanya makubaliano ya amani na mataifa haya machanga, wakiyatia moyo kuendeleza uchumi wao na kuanzisha biashara na Borno. Kutokana na mahusiano haya mataifa haya machanga yaliiga sana utamaduni wa Borno, jambo ambalo huenda lilichangia kuchapusha maendeleo yao.

Katika kipindi hichohicho, mataifa mengi yalikuwa yakiibuka katika nchi ya Uhausa. Punde Katsina na Kano vikawa vituo vya njia ya kuvuka Sahara na pia vituo vikuu vya kuhifadhia na kusambaza bidhaa vya njia ya mashariki-magharibi. Kutoka vituo hivi dhahabu ya Akan na kola zilichukuliwa hadi Borno. Kaskazini zaidi, kulitokea mabadiliko kidogo ya njia ya kuvuka Sahara wakati Agades ilipochukua

nafasi ya Takedda kama kituo kikuu cha hifadhi na usambazaji wa bidhaa.

Borno ilibidi kuwa na hadhari na maendeleo haya. Njia mpya ya biashara kati ya Borno na nchi ya Uhausa punde ilikuwa si salama na juhudi ilibidi zifanyike kuilinda. Matatizo kuhusu njia hii ya biashara na harakati za kudhibiti makazi yaliyoibuka kwenye hiyo njia huenda yalichangia katika mgogoro kati ya *mai* Idris Katakarmabe na wafalme wawili wa Kano, Abdullahi (t. 1499-1509) na Muhammad Kisoki (t. 1509-65).

Vilevile Borno lazima ilitaka kukidhibiti kituo kipya cha hifadhi na usambazaji wa bidhaa cha Agades ambacho taifa lenye nguvu nyingi la Songhai lilitaka kukimiliki mnamo 1501 na 1515. Hata hivyo, kuibuka kwa Kebbi wakati wa utawala wa Muhammadu Kanta (t. 1516-54) kulikwamisha juhudi za Songhai na Borno. Matatizo ya Agades yaliendelea kuwasumbua wafalme wa Kisefuwa karibu kwa kipindi chote cha utawala wao.

Kipindi cha kuanzia takribani 1480 hadi 1520 kilikuwa cha uimarishaji wa Uislamu katika *Bilad al-Sudani*. Upande wa mashariki, Usultani wa Funj, ulioanzishwa takribani 1504, punde ulikubali Uislamu. Upande wa magharibi, wanazuoni wengi kutoka Mali, Afrika Kaskazini, Misri na oasisi za Sahara walizuru Uhausa na kuchangia katika kuisilimisha. Magharibi zaidi, ufalme wa Songhai ulifikia kilele cha ustawi enzi za *askiya* Muhammad (t. 1493–1528), ambaye utawala wake ulisadifu mlipuko wa ari ya Uislamu. Wakati wa hija yake Maka (t. 1496-8), mtawala huyu alipatiwa *ukhalifa* wa Takrur, kama ilivyokuwa kwa *mai* Ali Gaji miaka kumi iliyopita.

Ma-*mai* wa Kisefuwa walikwisha kuwa Waislamu tangu karne ya kumi na moja, na kwa desturi walizungukwa na *maulama*, jambo ambalo liliwaongezea nguvu dhidi ya watawala wengine. Kufifia na kuanguka kwa ufalme wa Songhai mwishoni mwa karne ya kumi na sita kuliwahakikishia hegemonia juu ya mataifa mengine.

Borno kikawa kituo kikuu cha taaluma kikitembelewa na wasomi kutoka *Bilad al-Sudani* na sehemu nyingine za ulimwengu wa Kiislamu na athari za utamaduni wake zilienea katika mataifa mengi.

Tangu wakati wa utawala wa Idris Katakarmabe, zipo rekodi zenye kuonyesha kuwepo kwa uhusiano wa kidiplomasia na kibiashara kati ya Wasefuwa na mamlaka mbalimbali zilizodhibiti pwani ya Afrika Kaskazini. Kunako takribani 1512, Katakarmabe alipeleka ujumbe wa kidiplomasia na kibiashara kwa Wahispania, ambao ndio tu walikuwa wameiteka Tripoli, ili kurejesha tena uhusiano wa kibiashara na eneo hilo. Wakati Waotomani (Waturuki) walipojijenga huko Maghrib, Dunama b. Muhammad kunako takribani 1555, alituma ujumbe uliofanya mkataba wa "urafiki na biashara" na Tighurt Pasha. Mkataba huu uliendelezwa na warithi wao. Bila shaka uhusiano imara na Misri pia ulianzishwa.

Dhuria wa Katakarmabe waliendeleza sera yake katika kukabili mashambulizi ya Wabulala na uibukaji wa mataifa mapya. Kunako takribani 1561, kulizuka vita vya

kugombea udhibiti wa Agades kati ya Kebbi na Borno, ambavyo Borno yaelekea ilishindwa.

## *Kuanzishwa kwa uchumi imara wa kikanda na mfumo unganifu wa kisiasa, na kuibuka kwa Wakanuri, t. 1564 - 1577*

Wanazuoni wengi zaidi wanakubaliana kuwa Borno ilifikia upeo wa usitawi wakati wa utawala wa Idris b. Ali, aliyepewa ubini wa Alawoma baada ya kifo chake (1564-96). Alionekana kuwa ni mbunifu wa kijeshi na kiutawala na kadhalika mwenezaji wa Uislamu na mwanadiplomasia stadi.

Lengo lake kuu baada ya kushika madaraka lilikuwa kuipatia nchi yake mfumo imara wa kiuchumi na kisiasa. Alikuwa *mai* wa kwanza kujaribu kuliweka jimbo lote la mji mkuu chini ya udhibiti imara. Jeshi la farasi liliundwa upya. Aidha kulikuwepo na kikosi cha bunduki cha Waturuki kilichokuwa kikiimarishwa na watawala waliomtangulia. Boti kubwa zaidi zilijengwa ili kurahisisha uvukaji wa mito. Ni baada ya kuwa na jeshi hili ndi po Alawoma alipoanza mashambulizi dhidi ya mataifa mengine na kuyashinda.

Makundi mengi ya kiadui yaliyokataa kushawishiwa au kushurutishwa kukubali utawala wa *mai* yalishambuliwa mfululizo. Haya yalijumuisha Wangafata, Watalata, Wadugurti, Wamaya, Wangizim na Wabedde. Baadhi yao, mathalani Wamukhulum, waliruhusiwa kubakia na kaya zao kwa ahadi ya kulipa ngano kama kodi. Wengine, waliochukuliwa kuwa sugu, walifukuzwa kutoka jimbo la makao makuu.

Badala ya makundi haya yaliyofukuzwa nchini, makundi mengine, hasa kutoka Kanem, yalikuja na kuishi Borno. Mabadiliko haya makubwa ya kidemografia, pamoja na uoaji kwa wingi wa watumwa wa kike waliotekwa wakati wa mapigano au waliobadilishwa na mataifa ya pambizoni, yalichangia kuibua kikundi cha Wakanuri ndani ya jimbo la makao makuu.

Katika Borno ya kusini *ribat* (ngome za mpakani) zilijengwa ili kudhibiti vikundi vya wapinzani kama vile Wagamergu, na makubaliano yalifanywa na watawala wa mataifa ya pambizoni kuendesha mashambulizi ya kijeshi ya pamoja dhidi ya wapinzani.

### Suluhisho la mwisho kwa matatizo ya Kanem

Baada ya kulipatanisha na kuliunganisha jimbo la makao makuu, Idris Alawoma alielekeza nguvu zake zote Kanem ili kulimaliza kabisa tishio la Kanem dhidi ya Borno. Alikuwa na malengo matatu: kuharibu kabisa uwezo wa kijeshi na msingi wa nguvu wa Wabulala; kuharibu msingi wa uchumi wa taifa la Kanem; na kuvihamishia Borno vikundi vingi iwezekanavyo.

Alawoma alifanya mashambulizi kadhaa dhidi ya Wabulala na vikundi vingine vilivyowaunga mkono. Mabonde matatu kati ya mabonde yenye rutuba nyingi ya

Kanem yaliteketezwa, na baadhi ya miji mashuhuri, kama vile Ikima, Aghafi na Ago, iliharibiwa, na wakazi wake wakahamishiwa Borno. Vikundi vilivyolazimishwa kuishi Borno vilijumuisha Watubu, Wakoyam, Wakulu na Waarabu wa Shuwa. Vikundi viwili vya mwisho, ambavyo vilikuwa vya wafugaji wa ng'ombe, vilipelekwa kuishi kwenye fukwe za kusini za Ziwa Chad na magharibi mwa jimbo la makao makuu. Watubu walipelekwa kuishi kwenye ukingo wa jangwa, kwa sababu za kimkakati na ili washiriki katika uzalishaji chumvi.

Ilipofikia miaka ya 1580, Alawoma alikuwa amekwisha tekeleza mengi ya malengo yake, na nchi ya Kanem, kwa mkataba maalum, iligawanywa kati ya Borno na Wabulala, huku Wabulala wakikubali namna fulani ya udhibiti mdogo kutoka Borno.

## Mageuzi ya ndani

Yaelekea Alawoma alikwenda kuhiji Maka kunako takribani 1571. Aliporejea alijaribu kuleta mabadiliko kadhaa kuifanya nchi yake iendane na mataifa mengine ya Kiislamu. Alijaribu, bila mafanikio, kutenganisha kazi za idara ya mahakama na zile za serikali. Hata hivyo, alifaulu kuanzisha mahakama ya rufaa ambamo "Wasomi na Maimamu walijadili mbele ya Amir Ali masuala yenye utata ya sharia na imani." Mahakama hii iliwavutia wanazuoni wengi wa Afrika Kaskazini na wengineo, jambo lililoifanya ionekane kuwa ya kimataifa.

## Kuibuka kwa uchumi imara wa ukanda

Ushindi na mabadiliko ya kidemografia chini ya Idris Alawoma, na kadhalika mabadiliko yake mengine, yalipelekea kuibuka kwa uchumi imara wa ukanda, uliokuwa na msingi wake katika jimbo la makao makuu, eneo la takriban kilomita za mraba 20,000.

Upande wa mashariki ulishamiri uvuvi kwenye fukwe za Ziwa Chad uliofanywa na Wabuduma na Wakanembu, ilihali maeneo mazuri ya malisho yaliwavutia wengi wa wafugaji ng'ombe wa Kinomadi - yaani Wakanembu, Washuwa na Wafulbe. Natroni na chumvi zilizalishwa na Wakanembu na Wabuduma, jamii ya watu ambao walikuwa hawahamihami. Vituo mashuhuri vya kimji viliibuka, ikiwa ni pamoja na Mungono, Kauwa, Burwa na Ngurno.

Magharibi mwa nchi pia kulikuwepo na natroni nyingi, iliyochimbwa na Wamanga na Watubu. Kusini walikuwepo wakulima wengi, wakiwemo Wangizim na Wabedde. Eneo hili lilipata aina nyingi za wahamiaji, na vituo vingi vya kimji vilivyoibuka hapa, ikiwa ni pamoja na Nguru Ngilewa, Mashina Kabshari na Maja Kawuri, vilionekana kuwa vya kimataifa zaidi kuliko vile vya upande wa mashariki.

Mji wa Birnin Gazargamu na maeneo yanayouzunguka yaliunda kituo cha tatu cha kiuchumi. Ukiwa kwenye njia ya biashara iliyokatisha nchi toka mashariki hadi magharibi, Birnin Gazargamu ulikuwa pia kituo cha mwisho kwa njia ya misafara ya Borno-Kawar-Tripoli na pia kwa njia kuu iliyoliunganisha eneo hili na Uhausa. Kwa

hiyo jiji hili lilikuwa kitovu cha uchumi wa nchi na soko lake kubwa liliwavutia wafanyabiashara wengi wa kigeni. Kwenye bonde lenye rutuba na lililomwagiliwa la Yobe kulikuwa na mkusanyiko mkubwa wa kundi la Wakanuri lililokuwa linaanza kujitokeza; Wakanuri hao walikuwa tayari wanaishi katika maeneo mengi ya mijini, licha ya Birnin Gazargamu.

Maendeleo ya viwanda vya msingi yalipelekea kwenye uanzishaji wa viwanda saidizi kama vile vya ufinyanzi, ufumaji, uzalishaji bidhaa za ngozi, utiaji rangi na uchukuzi.

Biashara ya natroni na chumvi ilienea hadi pwani ya Atlantiki, Uhausa, bonde la Volta na kuelekea kaskazini hadi Azbin na Adrar. Samaki wakavu waliuzwa nchini na pia huko Mandara, Uhausa na oasisi za Sahara. Watumwa, matowashi, ngozi, meno ya ndovu, manukato, bidhaa za ngozi na dhahabu zilipelekwa kuvuka Sahara hadi Afrika Kaskazini na Misri. Bidhaa hizo zilibadilishanwa na farasi, matandiko na mapambo ya farasi, deraya, kupri, shaba nyeusi na bidhaa nyingine zilizotoka Ulaya na Afrika Kaskazini na kusambazwa Borno na sehemu nyingine za *Bilad al-Sudani.*

Kuanzia wakati wa utawala wa Alawoma, jamii mbalimbali zilizoishi kuzunguka bonde la Chad zilitiwa moyo na Wasefuwa kujishughulisha na biashara. Watu hawa wote walijulikana kama Waborno na lazima walisaidia kueneza utamaduni wa Kiborno ulioibuka huko Uhausa na sehemu nyingine. Borno iliweza kutawala shughuli zote za *Bilad al-Sudani* wakati wa kipindi hiki kutokana na uchumi wake wa kikanda, udhibiti wake wa biashara na uongozi wake katika Uislamu.

Ma-*mai* hawakuingilia sana biashara yenyewe, isipokuwa walizilinda njia za biashara na kuingia mikataba na serikali za Sahara na Afrika Kaskazini kuhakikisha kuna mtiririko huru wa biashara. Kwa upande mwingine, walijitahidi huandaa masoko – kuwatia moyo wafanyabiashara na kupata kodi. Kwenye mji mkuu na miji mingine mashuhuri, ma-*wasili* (wafanyabiashara wa Afrika Kaskazini) walitambuliwa kama wageni wa serikali. Walipatiwa malazi, na ofisa wa serikali, *zanna arjinama*, alishughulikia masuala yao. Kwenye masoko, *mala kasuube* alisimamia mauzo na kuhakikisha kwamba haki inatendeka katika uendeshaji wa biashara kubwa.

## Uhusiano wa kidiplomasia wa Idris Alawoma na masultani wa Uturuki na Moroko

Uhusiano wa Waturuki (Waotoman) na Borno ulianza mara baada ya Waturuki kuwasili Maghrib. Kuanzia takribani 1549 – wakati Waturuki walipodhibiti Fezzan – hadi takribani 1570, uhusiano huu ulikuwa mzuri. Mambo yalibadilika kunako takribani 1571, wakati uongozi wa Waturuki ulipopandisha ghafla kodi ya mwaka ya Fezzan. Uamuzi huu ulitolewa wakati Fezzan ikikabiliwa na njaa, na watu wengi walilazimika kuhamia Uhausa na Borno. Maofisa wa Kituruki huko Fezzan waliwalazimisha wananchi waliobakia, wengi wao wakiwa wazee, kufidia pengo la kodi lililojitokeza. Hata mahujaji kutoka Uhausa na Borno walisimamishwa na kulazimishwa kulipa kodi.

Alawoma aliweza kupata habari za uhakika kuhusu hali hii alipokwenda hija Maka mnamo takribani 1571. Kunako takribani 1574, akiwa na shauku ya kuhakikisha usalama wa njia kwa hija na biashara, Alawoma alituma ujumbe Istanbul ukiwa na maombi mahsusi matatu: kuhakikishiwa usalama wa njia na mali kwa wasafiri wote kutoka Borno wanaovuka nchi yenye kutawaliwa na Waturuki; usimamizi mzuri au, ikishindikana kufanya hivyo, kurejeshwa Borno kwa ngome zote zilizotekwa karibuni kusini mwa Fezzan, ikiwa ni pamoja na Guran; na ushirikiano baina ya tawala hizi mbili katika kuwashughulikia wakorofi wa Kituareg na watu wengine wowote waliohatarisha usalama wa eneo hilo. Yaelekea hapakuwepo na maombi ya silaha.

Mnamo Mei 1577, sultani Murad III aliyakubali maombi yote haya matatu isipokuwa lile la kurejesha ngome ya Guran, ambayo mfalme aliahidi ingesimamiwa vizuri kuanzia wakati huo na kuendelea. Kuanzia kipindi hiki na kuendelea uhusiano mzuri wa kibiashara na kidiplomasia ulidumishwa kati ya nchi hizi mbili.

Ushindi wa Moroko kule Kasr al-Kabir mnamo 1578 kimsingi ulichukuliwa kama ushindi wa itikadi ya Kiislamu dhidi ya ile ya Kikristo. Borno, kama ilivyokuwa kwa mataifa makubwa ya Kiislamu, ilituma ujumbe kumpongeza sultani wa Moroko. Hata hivyo, Alawoma aliogopa mashambulizi yaliyopendekezwa ya mwungano wa Waturuki na Wasaadi dhidi ya oasisi za Sahara na hata Sudani, na akajaribu kukwamisha mpango huo kwa kupendekeza kufanywa kwa mashambulio ya pamoja ya Borno na Moroko dhidi ya oasisi za Sahara, ambazo wakati huo hazikuwa na usalama wa kutosha. Matokeo ya ujumbe huu, kulingana na vyanzo vya Moroko, yalikuwa ni kukubaliwa kwa mapendekezo ya Borno kwa masharti kwamba Alawoma amtambue al-Mansur kama *khalifa* wa zama hizo. Kwa Moroko, kutambuliwa kwa ukhalifa wake na mojawapo ya mataifa mashuhuri ya Sudani kungeleta ushindi wa kiitikadi na kuimarisha nafasi yake dhidi ya Songhai. Kwa Alawoma, gharama hiyo ilifaa kulipwa, kwani iliondosha tishio la uvamizi wa Wamoroko-Waturuki dhidi ya Borno au eneo jingine lolote lililokuwa na masilahi kwa Borno.

Kuelekea mwishoni mwa utawala wake, Alawoma yamkini alijishughulisha kudhibiti maendeleo ya haraka ya madola ya Mandara na Bagirmi. Alilazimika kufanya mashambulizi kadhaa dhidi ya Mandara, na hakushinda katika mengi ya mashambulizi hayo. Huko Bagirmi, Abdullah b. Lubekto (t. 1561-1602), pamoja na kwamba huenda aliupata ufalme kwa msaada wa Borno, alianza kuleta matatizo. Inasemekana kwamba Alawoma aliuawa na Mgamergu wakati wa mapigano dhidi ya Abdullah.

Kifo cha Idris Alawoma, kinyume na maoni ya baadhi ya waandishi, hakikupelekea kwenye kuanguka kwa ufalme wa Borno. Kwa hakika ni wakati wa utawala wa warithi wake wanne waliofuatia (t. 1596-1677) ndipo nchi alizoziteka zilipoimarika na mfumo wa uongozi kutengemaa. Aidha ni katika kipindi hiki ndipo Wakanuri hatimaye waliibuka kama mbari yenye utamaduni wa kipekee.

## Utamaduni wa kijamii na yakinifu wa Wakanuri

Jina "Kanuri" yaelekea lilianza kutumika mwanzoni mwa karne ya kumi na saba.

Linataja mbari kuu ya Borno ambayo ilikuwa msingi wa nguvu za ma-*mai* wa Kisefuwa. Wakanuri walikuwa ni matokeo ya kuoana kwa Wamagumi kutoka Kanem na wazawa wa Borno waliozungumza Kichadi. Mchakato huu ulitiwa msukumo zaidi na sera ya kidemografia ya Idris Alawoma.

Wengi wa Wakanuri waliishi vijijini katika viunga vya vibanda kadhaa vya mduara vyenye mapaa ya umbo la pia yaliyoezekwa kwa nyasi. Viunga vingi vilizungushiwa *sugedi* (mikeka ya manyasi). Katika miji mikubwa, vibanda na misikiti mingi ilijengwa kwa udongo, na nyumba za matajiri zililindwa kwa kuta ndefu za udongo. Miji na vijiji vingi vilijengwa kwa umbo la U, kati pakiwa na mtaa mkuu *(dandal)*, ukitoka mashariki hadi magharibi kuelekea kwenye kasri ya gavana wa eneo hilo, iliyopakana na msikiti mkuu.

Huko Birnin Gazargamu na katika baadhi ya miji mikubwa zaidi, nyumba kwa kawaida zilijengwa katika umbo la mstatili zikiwa na kuta nene za udongo na mapaa bapa. Kasri za kifalme huko Birnin na Gambaru, misikiti yake mikuu na majumba ya kuishi watu mashuhuri yalizungushiwa kuta nzuri za matofali ya kuchoma, mojawapo ya sifa bainishi za utamaduni wa Kikanuri kutoka katikati ya karne ya kumi na sita hadi mwanzoni mwa karne ya kumi na nane.

Mkanuri wa kawaida aliweza kutambulika kwa lugha na sura yake. Wanaume kwa wanawake walikuwa na alama za wima katika kila shavu. Msichana asiyeolewa alitengeneza nywele zake kwa mtindo maalumu ulioitwa *kela yasku,* na mwanamke aliyeolewa nywele zake zilikuwa katika mtindo wa *jurungul* (taji). Wanawake walikula kola na kutia meno rangi kwa maua ya tumbaku. Kwa kawaida walivaa *gimaje* (magauni marefu ya pamba yaliyotiwa rangi) na wanawake wa hadhi ya juu walivaa *kalaram* (kilemba). Wanaume walivaa *tobe* (kanzu pana za pamba zisizotiwa rangi au zilizotiwa rangi ya bluu). Wanaume wa daraja la juu walivaa kanzu za aina mbalimbali za vitambaa ghali kutoka nje ya nchi, na mwishoni mwa karne ya kumi na nane walianza kuvaa vilemba vikubwa sana, desturi ambayo yaonekana iliigwa kutoka kwa uvaaji wa Waturuki wa karne ya kumi na saba.

Ndoa katika utamaduni wa Wakanuri ilikuwa na sifa zake bainifu zikijumuisha mchanganyiko wa kaida za Kiislamu na zile za Wamagumi na nyinginezo za kabla ya kuingia kwa Uislamu.

Jamii ya Wakanuri ilikuwa na mgawanyiko mkali wa kitabaka. Iligawanyika katika matabaka mawili makubwa, *wakontuowa* (tabaka la watawala au waadhamu) na wa-*talaa* (makabwela), na matabaka haya yalikuwa na vijitabaka vyake kadhaa. Tofauti za uzungumzaji, nguo na nyumba za kuishi ziliyabainisha matabaka haya na vijitabaka vyake. Mtu aliweza kupanda ngazi ya kijamii kwa kulimbikiza utajiri, kuingia udugu au ushirikiano wa karibu na tabaka tawala, au kuteuliwa kushika wadhifa mkubwa serikalini.

Utamaduni wa kijamii na kisiasa wa Wakanuri ulihimiza sana juu ya uhusiano wa tabaka la chini na la juu. Mtu wa tabaka la chini alipaswa daima kuonyesha hadharani utii wake kwa yule aliyempita daraja. Zaidi ya hapo, alihitajika pia kumtembelea

nyumbani "baba yake wa kijamii," ambaye angeweza kumtaka amfanyie upendeleo wowote. Kwa upande wake, mtu wa tabaka la juu alishughulikia mahitaji muhimu ya mtu wake wa tabaka la chini na kupigania masilahi yake katika jamii.

Wakati huu Borno kilikuwa kituo cha usomi kilichowavutia wanafunzi wengi na kutembelewa na idadi kubwa ya wanazuoni kutoka *Bilad al-Sudan,* Afrika Kaskazini na Mashariki ya Kati. Borno ilijikita katika *tafsir* (maelezo juu ya Kurani) kwa lugha ya Kanembu, na utaratibu wa kuandika lugha ya Borno kwa herufi za Kiarabu yaelekea ulianza katika karne ya kumi na saba.

Kulikuwepo na wasomi wa aina mbili. Wa kwanza walishika nyadhifa rasmi za kidini. Maimamu, makadhi, *mainin kinendi* (mshauri wa Kiislamu na sharia wa *mai*), *talba* (mkuu wa polisi na mahakimu), *khazin* (mweka hazina) na *wazir* (waziri) walikuwa maulama wakubwa waliomsaidia *mai* kutawala kulingana na maelekezo ya Uislamu. Nafasi zao zilirithishwa na kushikiliwa na familia chache tu za wasomi mashuhuri. Urasimi wa ofisi walizozishikilia uliwahusisha mno na watawala wa wakati wao na hivyo kuzidi kuwatenga na wanazuoni wasio wa kitalani.

Wanazuoni wa kawaida zaidi waliishi vijijini na kueneza dini yao. Wakati wa kipindi cha Wasefuwa, wengi wao walilindwa na wafalme, ambao waliwapatia *mahram* (upendeleo). Hata hivyo, ni wanazuoni hawahawa walioanza kuukosoa vikali utawala wa Wasefuwa.

## Mfumo wa kisiasa

*Mai* alikuwa mkuu wa familia ya kifalme, kiongozi mkuu wa taifa na *larde kangema* (mmiliki wa heshima wa ardhi). Alikuwa ishara ya umoja na uendelevu wa taifa. Kama *amir al-muminim* (amiri wa waumini) alikuwa kiongozi wa Waislamu wote na msuluhishi wa mwisho wa masuala yanayohusu haki ya umma au ya binafsi.

Sifa nyingi za utukufu wa wafalme waliotawala kabla ya Uislamu kuingia yaonekana ziliendelezwa wakati wa kipindi cha Uislamu. Kwa kiwango kikubwa *mai* alitengwa, alionekana hadharani akiwa tu katika *fanadir* (kizimba), na watu hawakuruhusiwa kuzungumza naye moja kwa moja. Wanazuoni wa Kiislamu yaelekea ndio walioukuza utukufu huu wa mfalme.

*Mai* alichaguliwa kutoka miongoni mwa wa-*maina* (wana wa mfalme wenye sifa za kurithi kiti cha enzi), lakini urithishaji haukuwa wenye utulivu. Kuanzia kipindi cha *mai* Idris b. Ali (t. 1677-96), au mapema kabla ya hapo, yaelekea wafalme walitumia mbinu za kuwaua wapinzani wao - desturi ambayo huenda walijifunza kutoka kwa Waturuki.

Wengine waliojumuishwa katika familia ya kifalme walikuwa wake wanne rasmi wa mfalme, masuria, wana na mabinti mfalme, *magira* (mama mzazi wa mfalme) na *magram* (dada rasmi wa mfalme). *Gumsu* (mke mkubwa wa mfalme) alihusika na usimamizi wa kasri; *magira* alikuwa kabaila mkuu katika ufalme na alikuwa na haki ya kutoa kimbilio; *magram* kwa kawaida alisimamia upishi wa chakula cha mfalme.

Wengi wa wanamfalme waliishi nje ya kasri na shughuli zao zilidhibitiwa sana,

ingawa baadhi yao walipatiwa milki za kikabaila. Waliokuwa mashuhuri kabisa miongoni mwao ni *chiroma* (mrithi mstahiki) na *yerima* (gavana wa majimbo ya kaskazini) ambaye daima alikuwa *maidugu* (mjukuu wa mfalme aliyetangulia). Hii ilimaanisha kwamba *maidugu* asingeweza kudai ufalme.

Baraza la juu kabisa la nchi lilikuwa *majlis*, ambalo kwa kawaida liliongozwa na mfalme na lilijumuisha viongozi mashuhuri wa kijeshi na kidini. Wengi wa viongozi wa Kiislamu ambao tayari wamekwisha tajwa awali na hali kadhalika makamanda wa kijeshi walikuwa wajumbe wa baraza hili. Baraza pia liliwajumuisha watumwa mashuhuri wa *mai*, ambao baadhi yao walikuwa matowashi. *Majlis* ilichunguza masuala yote muhimu ya nchi. *Noguna* (baraza la *mai*), iliyojumuisha watu mashuhuri wote katika mji mkuu ilikutana kila siku.

Miji, vijiji na vitongoji vya kimbari viligawanywa katika *chidi* (miliki za nyarubanja) na maofisa wakuu wote wa taifa walikuwa ma-*chima* (wamiliki wa nyarubanja). Ma-*chima* walidumisha amani na utulivu katika miliki zao, wakakusanya kodi na kuunda majeshi ya wapiganaji. *Mai* aliweza kunyang'anya, kupunguza au kugawanya upya miliki za nyarubanja kulingana na mapenzi yake. Katika ngazi ya chini kabisa watu walitawaliwa na *mbarma* au *bulala*.


Pato la Wasefuwa lilijumuisha *zakat* (zaka) *dibalram* (kodi ya barabara), *kultingo* (ushuru) na nyara za vita.

## Kipindi cha upeo wa ustawi katika Borno

Karne ya kumi na saba - sio ya kumi na sita kama inavyodaiwa kwa kawaida - inapaswa kuchukuliwa kuwa ndicho kipindi cha upeo wa ustawi wa Borno. Ilikuwa wakati wa utawala wa Umar b. Idris (t. 1619-39) ndipo ofisi za *galadima* wa Nguru na *alifa* wa Mao huko Kanem zilipoanzishswa kama tawala za vibaraka zenye uhuru kidogo ili kuongoza maeneo ya mipaka ya magharibi na mashariki ya nchi, kwa mpangilio huo. Madola kinga yalianzishwa pembezoni mwa jangwa kule Muniyo na Mashina kama kinga dhidi ya mashambulizi ya Watuareg katika jimbo la mji mkuu. Hiki ndicho kipindi ambapo Abd al-Karim ben Jame (t. 1611-55) alianzisha Wadai - bila shaka kwa baraka za Borno, kwa vile Wadai ilizuia kwa muda upanukaji wa Bagirmi. Kama ilivyokuwa kwa mataifa mengine ya jirani, Wadai iliangukia katika mzingo wa kisiasa, kiutamaduni na kibiashara wa Borno.

Uhusiano wa kidiplomasia na kibiashara na pwani ya Mediterania ulikuwa wa juu kabisa katika kipindi hiki. Hapana shaka kwamba uhusiano na Misri pia ulikuwa mzuri, kupitia biashara, na pia kwa vile Misri ilikuwa kwenye njia ya hija kuelekea Maka.

Ilipofikia karne ya kumi na saba, hususani wakati wa utawala wa Ali b. Umar (t. 1639-77), Borno ilishakuwa taifa lenye nguvu kushinda mataifa yote katika *Bilad al-Sudani*. Sio tu ilikuwa kituo kikuu cha taaluma na utamaduni, bali pia ilidhibiti vyanzo vyote vilivyofikika kirahisi vya chumvi za madini - huko Muniyo, Bilma na maeneo ya kuzunguka Ziwa Chad. Uhusiano wake wa karibu wa kibiashara na pwani




**17.1** *Borno, Kānem na majirani zake kwenye karne ya kumi na nane*

ya Mediterania uliipelekea kuongoza katika usambazaji wa bidhaa za nje kwenye mataifa ya Sudani ya Kati. Ma-*mai* walitambuliwa kama viongozi halali wa mataifa ya Kiislamu ya kanda hii. Mengi ya mataifa haya yaelekea yalijiweka kwa hiari yake yenyewe chini ya ulinzi wa *khalif* ili kufaidika na baraka zake na kupata bidhaa walizohitaji. Ulikuwa ni mmomonyoko wa mfumo huu ambao ulipelekea kwenye kudhoofika na hatimaye kuanguka kabisa kwa Wasefuwa.

## Zahama za mwishoni mwa karne ya kumi na nane

Wakati wa utawala wa Ali b. Dunama (.1742-92), Borno iliingia kipindi cha zahama ambacho kilifikia kilele chake katika jihadi ya karne ya kumi na tisa.

Katika Borno ya magharibi, Wabedde walikuwa wakizidisha mashambulizi yao ya njia za biashara kuelekea Uhausa, ilihali upande wa kaskazini Watuareg wa Agades walikuwa wakiimarisha uvamizi wao. Matukio yote haya yalichapusha mwelekeo wa kusini wa vikundi vya Wamanga.

Huko Bagirmi, Muhammad al-Amin (t. 1751-85) alijitoa katika mamlaka ya Borno na kufanya mashambulizi kadhaa kwenye mipaka ya mashariki ya Borno, ilihali Wadai chini ya Jawda (t. 1747-95) iliendeleza sera yake ya upanuzi kuelekea Bahr al-Ghazal. Mashambulizi haya yalipelekea kwenye uhamiaji Kanem na jimbo la makao makuu wa Watubu, Wakanembu na Waarabu wa Shuwa, na hivyo kuleta mgogoro wa kugombea maeneo ya malisho.

Kunako takribani 1791, Mandara iliasi, punde ikafuatiwa na madola ya Wasosebalki na, kunako takribani 1795, na Gobir.

Wakikabiliwa na hali isio salama, njaa na malisho duni ya wanyama, Wanomadi wengi wa Kifulbe waliikimbia Borno na kuhamia Uhausa, Mandara na Fombina. Hata hivyo, hawakupata mahali popote amani na usalama waliokuwa wakiutafuta, na hii inaeleza kwa kiasi fulani kwa nini walishiriki kwa nguvu sana katika jihadi.

Wanazuoni wasio wa kitalani na Waislamu wa kawaida walidai kuwa zahama hii ilisababishwa na ongezeko la rushwa miongoni mwa watawala wa Kisefuwa na kushindwa kwa ma-*mai* kuzuia ukuaji wa tofauti za kiimani miongoni mwa wananchi. Jihadi ilipoanza, watawala-wateja wa Uhausa walimwita *mai* aende kutekeleza wajibu wake kama *khalif* na kuwasaidia katika vita hivyo. Kwamba hakuweza kufanya hivyo na kwamba hakuweza hata kuzuia kufukuzwa kwake kutoka katika makao yake makuu kulimaanisha kuwa *khalif* alikuwa amekwisha poteza mamlaka yake.

Hata hivyo, ingawa *jihadi* ilichangia katika kuyapoteza madola ya vibaraka na kumaliza utawala wa Wasefuwa, mfumo uliojengwa na ma-*mai*, hususani katika Borno, uliendelea, japo kwa kufanyiwa marekebisho, hadi kwenye karne ya ishirini.

# 18

# Kuanzia mbuga za Kameruni hadi Nili ya juu

Katika sehemu hii ya Afrika, taarifa za kihistoria za kipindi cha kati ya 1500-1800 ni kidogo, hazieleweki vizuri na wala siyo za kuegemewa sana kama ilivyo katika kanda nyingine. Katika maeneo ambako mipangilio ya kisiasa ilichukua muundo wa dola, kuanzishwa kwa madola hayo kulifanyika baadaye kabisa katika karne za kumi na nane na kumi na tisa. Mapokeo simulizi yaliyopo hayatoi taarifa nyingi na wala hayaturejeshi nyuma zaidi ya vizazi kadhaa. Yale yaliyopo mara nyingi husimulia historia za nasaba fulani tu, na huzua matatizo ya tafsili ambayo mara kwa mara hujitokeza katika taarifa za namna hiyo. Vyanzo vingine ni vichache na vya hapa na pale tu. Katika sehemu zilizokuwa na muwasala na wageni kuna maelezo machache ya wasafiri ya kuanzia karne ya kumi na sita na kuendelea. Mwisho, katika eneo hili uchunguzi wa kiakiolojia, kihistoria, kiisimu na kiisimujamii ndiyo kwanza unaanza.

Isitoshe, hakuna hata jambo moja linaloziunganisha sehemu mbalimbali za eneo hili. Hapana shaka kwamba msitu ndiyo sifa kuu ya kimaumbile ya eneo hili, lakini sehemu zake nyingi zimebakia kuwa mbuga za savana tu. Idadi kidogo ya watu yaelekea pia kuwa sifa mojawapo inayojitokeza katika eneo hili, lakini kulikuwa pia na sehemu zilizokuwa na watu wengi kiasi, hasa katika mbuga za savana na katika maeneo yaliyoko kwenye njia za misafara ya majini. Ama kuhusu watu, kulikuwa na tofauti za wazi katika lugha zao, maisha yao na miundo yao mbalimbali. Tofauti hizo na hali ambayo isingeweza kuzuilika ya upatikanaji taarifa usio linganifu vinafanya iwe lazima kuitazama kila sehemu ya eneo hili kwa upeke wake.

## Eneo la mpaka wa kaskazini

Sehemu ya kaskazini ya eneo hili, kuanzia nyanda za juu za Kameruni ya kati kwa upande wa magharibi hadi Mto Nili kwa upande wa mashariki, ndilo eneo ambalo habari zake za kihistoria ni haba sana. Isitoshe ule mwelekeo wa kazi za ethnolojia na historia kujibana katika mipaka ya kimbari, na hivi karibuni, kujibana katika mipaka ya madola yaliyopo hii leo, hufanya iwe vigumu kuzisanisi taarifa za eneo zima. Kwa hiyo yaelekea kuwa busara zaidi kujaribu kuyaelezea kwa pamoja maeneo

madogo madogo ambayo kwa kiasi fulani yanakubaliana kiutamaduni; au kwa kiasi fulani yana takdri moja.

## Nyanda za juu za Kameruni ya kati

Yaelekea mbuga hizi zenye rutuba kiasi zilikaliwa na watu mapema sana. Kuna walau vidokezo viwili vinavyoashiria kuwepo kwa makazi ya mapema sana katika eneo hili. Kidokezo cha kwanza ni uoto ambao hii leo ni mbuga zenye vichaka, lakini ambazo hapo zamani zilikuwa msitu mnene. Kugeuzwa huku (ambako kronolojia yake bado haijaelezewa) kwa eneo hili kuwa mbuga za savana, kunaweza kusemwa kuwa kulisababishwa na vitendo vya taratibu vya jamii za watu zilizosongamana mahali pamoja, mwingilio wa ghafla na wa kikatili wa kiasi kidogo cha wahamiaji, au athari za hali ya hewa. Pili, kuwepo kwa zana za mawe nyingi kunaashiria kuwepo kwa makazi ya watu, ambayo pengine yalitokea katika nusu ya pili ya milenia ya kwanza. Lakini haijawezekana kutambua hawa wakazi wa kwanza walikuwa watu gani. Inawezekana walikuwa Mbilikimo wawindaji, ambao vizazi vyao vichache bado vingaliko leo katika kingo za Mbam, au wasemaji wa lugha ya mame-Bantu ambao walikuwa bado hawajagundua utengenezaji chuma; au mchanganyiko huru wa watu wa mbari kadhaa zenye kutofautiana.

Ni kuanzia tu katika karne ya kumi na sita na kuendelea ambapo taarifa kadhaa za uhakika zinaanza kudhihirika. Miguro ya watu inayoelezwa katika mapokeo ilihusisha aina mbalimbali nyingi za watu. Kila ushahidi uliopo unaelekea kutuambia kwamba idadi ya wahamiaji ilikuwa ndogo, kwani, ingawa waliwatawala watu waliowakuta wakiwa na makazi ya kudumu huko walikokwenda, kila walipofika huko waliacha lugha zao wakachukua lugha za nchi walimohamia. Mapokeo pia yanaeleza sababu nyingi za mijongeo hii, ikiwa ni pamoja na magomvi ya wenyewe kwa wenyewe, kutafuta mtapo wa chuma na miti ya kuuyeyushia, kutafuta ardhi mpya, biashara ya chumvi, na shinikizo la wavamizi kutoka kaskazini. Tatizo la kaskazini, hasa mashambulizi ya Wafulde, ambalo linajulikana sana katika kipindi cha karne ya kumi na tisa lilijitokeza mapema zaidi, kuanzia katikati ya karne ya kumi na nane, au hata kabla. Katika msamiati na sarufimiundo ya lugha ya Kimbum, ambayo inazungumzwa katika nyanda za juu za Kameruni ya kati, kuna maneno na miundo ya mikopo kutoka Kifulfulde. Kutokana na hali hiyo inaelekea kwamba Wafulfulde waliwafukuzia kusini Wambum, na kwamba hawa wa pili nao wakawasukuma Wavute kuelekea kusini zaidi; hali ambayo ilisababisha uhamaji wa Wafang na Wabeti.

Kuchanganyika huku kwa watu, kwa mara kwa mara, ambako kulitokea katika karne kadhaa, ndiko kulikokuwa cheche muhimu iliyochombeza mlandano mkubwa wa utamaduni uliopo kati ya watu wa Kameruni ya kati. Katika eneo hili watu wote huzungumza lugha ambazo ama ni Kibantu au nusu-Kibantu. Kuna mishabaha kadhaa katika namna mgawanyo wa madaraka unavyofanywa katika asasi zao za kisiasa na kijamii. Wanaume walikuwa katika vyama vingi vilivyojishughulisha na miviga na ulinzi wa amani. Teknolojia zao pia zilifanana, hasa katika utengenezaji wa chuma na

shaba nyekundu. Katika jamii zote hizi mhunzi aliaminika kuwa mtu mwenye nguvu za ajabu, na hii inajitokeza sana katika visasili na mapokeo ya kihistoria. Mlandano huu, ambao ulikwishajibainisha kwenye miaka ya 1800, ulikuwa umeanza kujengeka taratibu katika karne zilizotangulia.

Makundi matatu kati ya makundi mengi ya watu hawa yanastahili kupewa nafasi muhimu. Kundi la kwanza ni la Watikar, ambao ni muhimu sana kwa sababu watu wengi kutoka katika nyanda za juu za Kameruni wanadai kwamba ama ni vizazi vyao au wameathiriwa sana nao. Yasemekana kwamba Watikar ni watu watokanao na mfanya biashara mmoja kutoka Borno ambaye aliishi na kupata watoto miongoni mwa Wambum. Mapokeo yao mbalimbali yaonyesha kwamba asili yao ni kaskazini-mashariki mwa Kameruni. Hapo mwanzo kabisa *Tikar* lilikuwa jina la kupangwa ambalo lilipewa kundi la kwanza la Wambum ambao walihama kwao na kwenda katika nyanda za juu, lakini baadaye likawa ndilo jina la wahamaji wote kutoka Mbum na watu ambao wao waliwatamalaki. Sehemu kubwa ya uhamaji huu pengine ilifanyika katika karne ya kumi na saba. Walipofika eneo la Bamenda, Watikar waliwakuta Watumu, ambao kwanza walifanya usuhuba nao lakini baadaye wakawatawala. Lakini ushindi wao uliwagharimu lugha yao ambayo ilibidi waiache na kuchukua lugha ya watamalakiwa wao, na asasi zao, hasa vyeo vyao vya kisiasa na vyama vya siri.

Msingi wa ufalme wa Bamum ulitokana na kundi la wahamiaji waliokuwa na mnasaba na utawala wa kifalme wa Watikar wa Nsaw. Katika kitabu cha *Historia na Mila za Wabamum* mmeorodheshwa wafalme kumi baina ya mfalme mwanzilishi Nchare na mfalme Kwotu, aliyefuatiwa na Mbwembwe, mfalme ambaye utawala wake umekadiriwa kuwa katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na tisa. Nchare alikuwa mtamalaki ambaye aliwashinda watawala kama kumi na wanane. Alianzisha mji mkuu wa Wabamum, Fumban, wakati huo ukijulikana kama Mfomben. Nchare akaingiza katika ufalme huo asasi za kisiasa ambazo nyingi ziliigwa kutoka kwa Watikar. Akaanzisha utaratibu wa vyeo kadhaa, wakiwemo ma-*kom ngu* (wajumbe wa baraza la ufalme) ambao aliwatumia katika kuigawa ardhi iliyokuwepo. Akaanzisha vyama vya siri; kimojawapo ni kile cha wanamfalme peke yao, ambacho kilijulikana kama *ngiri*; na kingine ni kile cha *mitngu*, ambacho kilikuwa wazi kwa watu wote bila kujali hadhi zao za kijamii. Hata hivyo Wambum waliiacha lugha ya Kitikar na kuchukua Kimben, lugha ya watamalakiwa. Wafalme tisa ambao walikuja baada ya Nchare wamepewa maelezo mafupi sana katika mapokeo. Wao hawakuwa watamalaki, kwani upanuzi wa himaya ulianza mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, wakati wa utawala wa Mbwembwe. Aidha ufalme huo ulifikia hata kukabiliwa na tishio kubwa la kuvamiwa na Wachamba na Wafulfulbe, kutoka kaskazini, hasa katika karne ya kumi na nane. Hata hivyo, kulikuwa pia na maendeleo muhimu yaliyojitokeza katika kipindi hiki. Kuongezeka kwa kiasi kikubwa kwa ndoa za mitala za wanamfalme kulisababisha ongezeko kubwa la nasaba za wanamfalme; watukufu pia wakaongezeka sana katika ikulu. Mfalme alichukua watumishi wake wengi

kutokana na mapacha na wana wa mabintimfalme. Hakuna taarifa za kutosha kuhusu maendeleo ya vitu na ya kijamii katika ufalme huo. Mwishoni mwa karne ya kumi na nane ufalme ulikuwa na watu kama 10,000-12,000, kati yao ikiwemo idadi ndogo ya watumwa. Uchumi, ambao kwa kiasi kikubwa ulitegemea kilimo, ulishiriki katika biashara ya nje. Wabamum walikuwa wakiingiza nchini chumvi, chuma, shanga, bidhaa za pamba na vifaa vya shaba nyekundu tokea zama za zama.

Ama kuhusu Wabamileke, historia yao ya kale inahusiana sana na ile ya makundi hayo mawili ya nyuma. Wote walitoka kaskazini, katika eneo ambalo hii leo limekaliwa na Watikar. Uhamaji wao pengine ulianza katika karne ya kumi na saba na ulifanyika katika mawimbi kadhaa yaliyofuatana. Wahamaji walilichukua eneo la nchi ambayo hii leo hujulikana kama Bamum, ambako walianzisha vijiji kadhaa kabla ya kufukuzwa katika vijiji vingi na Wabamum: wale waliobakia walisimilishwa. Miongoni mwa makundi kadhaa ya Wabamileke, Wabaleng walikuwa wa kwanza kuvuka mto Nun, bila shaka karibu na mwanzo wa karne ya kumi na nane; na baadaye kidogo wakafuatiwa na Wabandeng, Wabapi na Wabafusam. Temi mbalimbali zilikuwa na sifa zilizofanana sana na zile za jamii za kisiasa za nyanda za juu za Kameruni. Watu walikuwa na miguro mingi, sifa ambayo yaelekea kuhusiana na ongezeko kubwa la idadi ya watu na mfumo wa kurithi ambao ulimrithisha ardhi mrithi mmoja, na hivyo basi watoto wengine wa kiume wakalazimika kupata ardhi kutoka kwa mtemi au kwenda kuishi kwingineko.

## Maeneo yanayopakana na mito ya Uele na Ubangi

Hapajawa na maendeleo makubwa sana katika kupata taarifa zaidi kuhusu maeneo yanayopakana na mito ya Uele na Ubangi tokea kazi za wanaanthropolojia wa mwanzo. Swali linalotanza zaidi ni lile linalohusu kukaliwa kwa maeneo haya. Utafiti wote unaainisha aina tatu za wakazi: wale wa ki-Niolithi, wa ki-Bantu na wa ki-Sudani. Matatizo yanaonekana kuwa katika kuyaelezea mabadilikobadiliko na ruwaza za makazi na mfuatano wa aina za mahusiano miongoni mwa watu hawa.

Kimapokeo, maeneo madogo mawili yalikuwa yakibainishwa, eneo la Uele na eneo la Ubangi. Eneo la Ubangi, ambalo hii leo limekaliwa zaidi na watu wa ki-Sudani, pengine, hadi kufikia karne ya kumi na saba, lilikuwa limekaliwa na Wabantu, ambao walikuwa wamelichukua eneo hilo kutoka kwa watu wasiojulikana sana, na ambao zana zao za ki-Niolithi zimedumu hadi hii leo. Watu wa ki-Sudani pengine walianza kuingia katika eneo hili wakitokea Darfur na Kordofan katika karne ya kumi na saba au mwanzoni mwa karne ya kumi na nane. Wale ambao baadaye waliunda kundi la Wangbandi (*Ngbandi*) pengine ndio waliofika mwanzo, wakifuatiwa na Wabanda (*Banda)* na Wangbaka (*Ngbaka*).

Yaelekea mfuatano wa makundi ya jamii katika eneo la Uele, ambalo hii leo linakaliwa zaidi na Wazande (*Zande)*, watu waliomezwa na Wazande na Wamangbetu (*Mangbetu*) ulikuwa tofauti. Hadi kufikia karne ya kumi na sita au mwanzoni mwa karne ya kumi na saba mabonde ya Uele, Mbomu na Aruwimi pengine yalikuwa

yanakaliwa na watu wa ki-Niolithi, watu ambao vizazi vyao vilivyobakia vyasemekana kuwa ni Wamomvu, Walogo, na Wamakere. Makundi mawili ya watu ambayo katika mapokeo huelezwa kama wavamizi yalijipandikiza katika makundi hayo tuliyoyataja mwanzo. Kwanza kulikuwa na watu wa Kisudani ambao kutokana nao wakapatikana Wamangbetu, Wangbandi na Wazande; kisha Wabantu ambao waliifuata mito kuelekea kaskazini. Ilikuwa katika kipindi hiki - katika karne ya kumi na saba na mwanzoni mwa karne ya kumi na nane - ambapo makundi ya kisiasa-kijamii yaliundwa.

Baadhi ya watafiti wamependekeza usanisi wenye kujumuisha maeneo yote ya Ubangi na Uele. Madai yao yameegemezwa kwenye data za kiisimu na kiisimujamii, na wanatofautisha hatua tatu kubwa za maendeleo ya makazi. Kwanza, katika milenia ya kwanza kabla ya Enzi ya Kikristo kulikuwa na mguro mkubwa wa magharibi-mashariki ambao uliwaleta wa-mame-Ubangi hadi kwenye mto wa Nili. Katika karne ya kumi na moja kulikuwa na msukumo wa Kiniloti ambao ulilisambaratisha kundi la Wa-ngbaka-Sere-Ngbandi na kuwasukuma Wangbandi kusini hadi kufikia eneo lililo katikati ya mito ya Ubangi na Zaire (Kongo), ambako walikutana na Mbilikimo na Wabantu. Msukumo huo wa Kiniloti pia uliwasukuma watu wa Zande-Nzakara mashariki hadi kwenye eneo lililokuwa likipata maji kutoka mito ya Uele na Mbomu. Hatua ya tatu, ambayo ilianza katika karne ya kumi na nane, inaoana na msukumo wa Wabantu kutokea kusini, wakikimbia harubu za biashara ya watumwa.

Usanisi huu unavutia, lakini unaleta wasiwasi wa namna mbili. Kwanza yaelekea kuwa vigumu kuzungumzia uhamaji katika hali hii ambapo, katika mifano inayojulikana vema ya Wazande na Wamangbetu, wavamizi walikuwa waali walioridhika na kuwagawanya wenyeji katika temi na falme mbalimbali. Pili, mapokeo yote, hasa shajara za koo muhimu, yanaonyesha kwamba ilikuwa katika karne ya kumi na saba tu ambapo "mikusanyiko ya watu" (rejea E.de Dampierre) ilitokea kutokana na mawimbi mbalimbali ya uhamaji. Maendeleo ya baadaye, pengine kuanzia karne ya kumi na saba, yaliziwezesha koo mbili, Wavungara na Wabandia, kuimarisha nguvu zao kwa kuzidhoofisha koo nyingine. Wavungara walikwenda wakatamalaki, kumeza au kufanya urafiki na watu wa makundi mbalimbali. Ustadi wao mkubwa katika kuwapangilia watu hawa katika miundo ya kisiasa ndio ulioijenga na kuiimarisha jamii ya Wazande. Ama kuhusu Wabandia, kilele cha upanuzi wao kilifikiwa katika karne ya kumi na nane kutokana na nguvu za Wangubenge, ambao waliendeleza utamalaki katika nchi ya Nzakara na kusaidia katika kuwasukuma Wavungara kuelekea mashariki.

Tunajua kidogo sana kuhusu ustaarabu halisi na yakinifu wa jamii hizi mbalimbali. Hata hivyo, yaelekea kwamba tabaka tawala lilikuwa likijishughulisha na uwindaji kwa kipindi kirefu, shughuli ambayo iliendelea kuthaminiwa sana. Wazande walijifunza mbinu za kilimo kutoka kwa jamii walizozitiisha. Ufuaji chuma uliheshimiwa sana, na katika baadhi ya makundi, kama vile Wangbandi, wahunzi waliunda vyama vya kipekee vya weledi. Mtandao mkuu ulioundwa na mito ya

Ubangi, Uele, Mbomu, Aruwini na matawi yake mengi ndio uliokuwa kitovu cha biashara. Katika masoko bidhaa za ufundi, chakula na wanyama, pamoja na watumwa, ndizo zilizouzwa. Biashara hii ilikua haraka kadri biashara iliyokuwa inaendeshwa na Wazungu kwenye pwani ya Atlantiki ilivyojipenyeza bara.

## *Jamii za pwani na biashara ya Atlantiki*

Kwa nchi za msitu za Afrika ya kati kipindi cha kuanzia mwaka 1500 hadi 1800 kilishuhudia kuanzishwa na kuendelezwa kwa biashara ya pwani; biashara ambayo baada ya muda mfupi ilibakia kuwa biashara ya watumwa. Ukingo wa pwani ulikuwa ndio kiungo cha mwisho cha mlolongo mrefu wa biashara ambao ulijipenyeza bara kwa kiwango ambacho kilikuwa hakijawahi kufikiwa. Hadi kufikia 1800, mlolongo huu ulikwishafikia Mungo ya juu, mbuga za Kameruni, Ogowe ya juu, hadi mto Kongo na mto Ubangi.

### Jamii za watu

Hali ya wakazi na jamii zenyewe katika ukanda wa pwani mnamo miaka ya 1500 bado haifahamiki vizuri. Maandishi ya mabaharia na wafanyabiashara wa Kizungu yanaonyesha kwamba eneo lote hili lilikuwa na watu, lakini hatujui watu hao walikuwa akina nani.

Kwa upande wa pwani yenyewe, kitabu cha O. Dapper cha *Description de l'Afrique*, ambacho kina orodha ya (majina ya) namba zilizokuwa zikitumiwa na watu wa pwani, kinatuwezesha kusema kwamba kwenye mwaka wa 1660 bila shaka watu hao walikuwa Wabantu. Vyanzo hivyo hivyo vya kimaandishi pia vinatuwezesha kukadiria tarehe za vipindi vya tawala kadhaa ambazo zimetajwa katika taarifa za kimapokeo. Kutokana na taarifa hizo tunaweza kukadiria kwamba kilele cha utawala wa Mulobe, mfalme wa kihistoria wa tatu wa Duala, kilikuwa mnamo mwaka 1650. Na hii inatuwezesha kukadiria kwamba matendo ya ushujaa ya babu yake, Mbedi, yalitukia katika karne ya kumi na sita, na yale ya shujaa maarufu Mbongo, ambaye anatajwa sana na Waduala na watu wengine walio na mnasaba nao, yalitukia baada ya karne ya kumi na sita.

Kwa hiyo, ingawa yawezekana kukubali kwamba hadi kufikia mwanzo wa karne ya kumi na sita pwani tunayoiongelea ilikuwa ikikaliwa na Wabantu, kwa upande wa maeneo ya nyrima bado haijawezekana kusema kwa yakini kulikuwa na watu gani. Kwa upande wa eneo la Miulaaba na nchi ya Beti, darajia sita za wakazi zimeonyeshwa, ingawa bila kutumia data mahsusi za kikronolojia; darajia ya kale kabisa ni ile ya Mbilikimo, ikafuatiwa na ya wawindaji-wakusanyaji, kisha yakafuata makundi mbalimbali ya Kibantu ambayo uhamaji wao uliendelea hadi katika karne ya kumi na tisa. Kusini zaidi, katika Gabon ya leo, picha ni wazi zaidi. Mwishoni mwa karne ya kumi na tano, Wareno waliwakuta Wampongwe katika eneo la mlango wa

mto. Eneo lililopakana na Ogowe ya chini (Rasi López na Fernán-Vaz) bado halikuwa na Wabantu; pengine waliokuwa katika eneo hili walikuwa zaidi ni Waafrika vibete (*negrillos*). Taifa pekee lenye mpangilio wa kidola katika eneo hili lilikuwa katika mlango wa mto Gabon. Kwa mujibu wa maelezo ya baadaye yaliyoandikwa na Dapper katika karne ya kumi na saba, mfalme wake alikuwa na cheo cha *mani pongo*.

Kusini zaidi ufalme wa Luango ulikwishaimarika hadi kufikia 1500, kwani taarifa zote za mabaharia-wapelelezi wa mwanzoni mwanzoni mwa karne ya kumi na sita hutaja Mani Luango na Mbanza Luango kwa majina. Baadhi ya mapokeo huieleza Luango kuwa dola lililotokana na ufalme wa Kongo; kwa mujibu wa mapokeo mengine ufalme wa Luango ulitokana na mchakato wa ndani katika jamii ya Wavili. Yawezekana kwamba Luango ilikuwa na mahusiano ya karibu, pengine ya kitwana, na Kongo hadi mwishoni mwa karne ya kumi na tano. Kama ilivyokuwa katika sehemu nyingi za Afrika ya Kati, kazi muhimu za mfalme zilikuwa kulinda miviga na ibada za kimila. Asasi ya kifalme, ambayo ilianzishwa na familia za wahunzi, ilihusishwa na madhehebu ya moto. Wakati wa sherehe ya kutawazwa mfalme kila *maluango* aliwasha *ntufia* (moto mtakatifu) ambao ulipaswa kuwaka hadi kifo chake. Mviga mwingine ulihusu mvua, ambayo ilikuwa wajibu wa mfalme. Sifa kuu ya jamii hii ilikuwa ni uchangamani wa uchumi wake. Kilimo cha mazao ya chakula ambacho kilikuwa kikikua na kubadilika kiliingiana vizuri na uzalishaji wa bidhaa za ufundi, ambazo zilikuwa ni pamoja na utengenezaji nguo kutokana na magome ya michikichi kwa ajili ya ufumaji, utengenezaji wa bidhaa za pembe za ndovu, shaba nyekundu na miti myekundu, na chumvi. Bidhaa hizi ziliuzwa katika soko la ndani, hasa lile lililokuwa Buali, ambao ndio uliokuwa mji mkuu, na pia ziliyafikia masoko ya nje ya ufalme huo. Kwa hiyo biashara ya Atlantiki haikuanzisha biashara katika eneo hili, bali iliipa tu msukumo na mwelekeo mpya.

## Biashara ya Atlantiki

Historia ya kijanibu ya biashara ya Atlantiki katika sehemu hii ya Afrika haifahamiki sana. Vitabu vya masimulizi ya wafanyabiashara wa Kizungu, ambavyo vingi vimetoweka, vinatoa maelezo kidogo tu ya hapa na pale. Lakini baadhi ya mambo yamejidhihirisha.

Mwanzoni biashara ilikuwa katika ukiritimba wa Ureno, ambayo mabaharia-wapelelezi wake Fernao do Po na Lope Gonçalves walifika katika kisiwa cha Formosa na Gabon mwaka 1472 na 1473, kwa mfuatano huo. Biashara ilianza kuongezeka tu baada ya mwaka 1500 wakati Wareno walipoanza kuishi katika kisiwa cha Sao Tomé, ambacho kilihitaji watumwa kwa ajili ya mashamba yake, na wakati huo huo kikitumika pia kama bandari ya mizigo iliyokuwa ikipelekwa Marekani. Mwishoni mwa karne ya kumi na sita maasi ya watumwa, muhimu kabisa yakiwa yale yaliyotokea huko Sao Tomé katika mwaka 1574 na mwaka 1586, yaliharibu kabisa biashara ya Wareno katika eneo hilo. Waholanzi walifika baada ya mwaka

1598 na kuanzishwa vituo vipya vya biashara vya Duala na Rasi López, na wakawaondoa Wareno katika Luango. Baada ya mwaka 1660, biashara ya watumwa ikapanuliwa sana na ikaendelea kupanuka hadi kwenye miaka ya 1850. Ufaransa na Uingereza yakawa ndiyo mataifa makubwa ya biashara katika eneo hili, lakini shughuli za Wareno, Waholanzi na Wadeni zikafanikiwa kuleta hali ya ushindani.

Si rahisi kusema kwa yakini kiwango halisi cha biashara hii, ambayo ilitofautiana toka sehemu hadi sehemu huko pwani. Kuwepo kwa nchi hizi chini ya Ghuba ya Guinea, kulikuwa kipingamizi. Vyombo vya kubebea watumwa mara nyingi vilifuata "njia ndogo" vikitia nanga katika vituo kadhaa vya watumwa huko pwani kuanzia Senegambia hadi Kalabari, na hata vilipofikia Kameruni, Gabon na Luango vilikuwa vimekwishafikisha sehemu kubwa ya mizigo yake. "Njia Kuu" iliruhusu mashua kuepuka vituo hivi vidogo na kwenda moja kwa moja hadi Rasi López na kuanza kufanya biashara katika Luango au katika bandari za jirani.

Kwenye upwa wa Kameruni, biashara ilishamiri kwenye miaka ya 1750, ikitumia bandari za mlango wa mto Wuri, na hasa Duala, kama vituo vyake vikuu, hasa kwa meli za Waholanzi. Duala ilipata watumwa wake wengi kutoka kaskazini na kaskazini-mashariki. Kwenye mto Gabon eneo la mlango wa mto lilikuwa ndilo kituo kikuu cha biashara. Rasi López ilianza tu kujishughulisha kikamilifu katika biashara ya Atlantiki wakati wa utawala wa Reombi-Mpolo (c. 1790-1810). Makadirio yoyote kuhusu idadi ya watu waliohusika katika biashara hii hayangeweza kuwa sahihi kwa namna yoyote ile. Lakini biashara ya watumwa ilikuwa imepanuka sana, hasa tukizingatia ukali wa mgongano kati ya Wareno na Waholanzi uliojitokeza mwanzoni mwa karne ya kumi na nane kuhusu nani aichukue Gabon; na pia tukizingatia idadi ya meli zilizopelekwa katika eneo hili kutoka bandari ya Ufaransa ya Honfleur. Zaidi ya watumwa kulikuwa pia na pembe za ndovu kwa wingi, nta na misandali, vilivyopatikana kutoka kwa wawindaji-wakusanyaji wa Kele na Fang kutoka eneo jirani.

Biashara ya Luango ndiyo ijulikanayo sana. Biashara yake ya watumwa haikudumu kwa muda mrefu ikilinganishwa na ile ya Slave Coast (Pwani ya Watumwa) au Angola. Ilianza kwa wingi sana kwenye miaka ya 1670 lakini hadi kufikia mwaka 1780 ilikuwa takribani imetoweka. Hadi kufikia miaka ya kati ya karne ya kumi na saba biashara ya Luango ilikuwa zaidi ni pembe za ndovu. mitirangi na viramba (nguo za ukindu), ambavyo vilikuwa vikitafutwa sana na kutumiwa katika Afrika ya Kati kama sarafu. Idadi ya watumwa waliosafirishwa kutoka pwani ya Luango - watumwa mia moja kwa mwaka kwenye miaka ya 1639 - iliongezeka na kufikia watumwa 12,500 kwa mwaka katika kipindi kati ya mwaka 1762 hadi 1778, na kufikia watumwa kati ya 13-14,000 kwa mwaka kati ya 1780 na 1790. Vitabu vya kumbukumbu za manahodha wa meli zilizokuwa zikibeba watumwa vimetoa madokezo muhimu sana juu ya asili za watumwa walionunuliwa na Wazungu huko Luango. Kuwepo kwa *Quibangues* (Wabubangi na "watu wa mto" kutoka katika mito ya Kongo na Ubngi) kunaonyesha kwamba wakati wa kilele chake, biashara ya

Atlantiki ilikuwa imefika katika kitovu cha kontinenti hili.

## Harakati changamani

Katika eneo dogo kama hili uchanganuzi wa athari za mfumo huu wa biashara shadidi na ya muda mrefu hauna budi kufanywa kwa makini na uangalifu. Hatutajiingiza katika mjadala juu ya uharibifu au athari chanya za biashara ya Atlantiki, mjadala ambao bado unaendelea. Badala yake tutajibana katika kusisitiza, kuhusiana na mabadilishano hayo, michakato ya mikikimikiki ya kila aina ambayo ilikuwa ikitokea na kuleta mabadiliko ya muda mrefu yaliyoathiri taratibu za kijamii, miundo ya kisiasa, idadi ya watu na mielekeo yao.

Mojawapo ya mabadiliko ya mwanzo mwanzo kabisa yaliyotokea mwanzoni mwa karne ya kumi na saba ni kuingizwa nchini kwa mazao kutoka Amerika: mahindi, muhogo, karanga, maharage, na tumbaku. Mazao haya hayakuenea pwani tu bali pia yaliingia haraka bara, wakati mwingine yakipitia katika njia za biashara. Muhogo ulikuwa na mafanikio makubwa sana, kwani zao lake lilijibainisha kuwa kubwa kuliko lile la viazi vikuu. Muhogo ulikuwa na matumizi mengi: majani yake yaliweza kuliwa, ilihali mizizi yake iliweza kusindikwa na kuhifadhiwa kwa kutumia mbinu mbalimbali. Hapana shaka kwamba zao la mahindi, ambalo kumbukumbu za kuwepo kwake zinaturejesha nyuma hadi kwenye 1600, polepole lilianza kuchukua nafasi ya ulezi. Mazao mengine nayo polepole yalianza kuingizwa katika utaratibu wa kilimo cha kubadilisha mazao mashambani. Mabadiliko haya yanadhihirisha uwezo mkubwa wa uvumbuzi wa kiteknolojia wa jamii ya wakulima wadogo katika Afrika ya Kati. Je mabadiliko haya yalichangia katika kukuza uwezo wa kujenga na kulinda miili na ongezeko la idadi ya watu, kutokana na uzalishaji wa mazao ya aina mbalimbali za vyakula uliokuwa imara? Hakuna hakika juu ya hili, kwani muhogo una kiasi kidogo cha lishe. Kijamii, mageuzi haya ya kilimo si tu kwamba yalikuwa na mchango mkubwa katika biashara yake bali pia katika kuanzishwa kwa mgawanyo mpya wa kazi. Polepole wanaume wengi, ambao sasa walipendelea zaidi kujishughulisha na biashara, ambayo ilielekea kuwa na faida zaidi, wakaziacha kazi kadhaa za kilimo zifanywe na wanawake na watumwa. Kuzuka kwa utumwa wa majumbani na aina nyingine za utegemezi yalikuwa matokeo ya moja kwa moja ya mabadiliko haya ya kilimo.

Katika maeneo ya mwambao wa pwani ambayo yalihusika moja kwa moja na biashara ya ng'ambo mageuzi yalikuwa changamani sana. Katika karne za kumi na saba na kumi na nane idadi ya watu ikawa haina mabadiliko makubwa na mchakato wa watu kujigawa tena katika maeneo mbalimbali ukaanza; mchakato ambao uliendelea hadi karne ya kumi na tisa. Karne ya kumi na saba ilishuhudia kutwaliwa kwa mlango wa mto Gabon na koo mpya za Wampongwe. Halikadhalika karne ya kumi nane ikashuhudia kufika kwa Waorungu katika Rasi Lopéz na Wankomi katika Fernán-Vaz. Ama kuhusu miundo ya kisiasa, biashara ya pwani ilikuwa na athari zilizopingana. Ni katika wakati mmoja tu, kati ya Waorungu wa Rasi Lopéz, ambapo

biashara hiyo ilisababisha kuanzishwa dola imara na unganifu ambalo ukoo wake wa kifalme - Waabolia au Waalombe - ulikuwa na ukiritimba wa kuendesha biashara na Wazungu wakati wa kilele cha biashara ya watumwa. Kwingineko kote pwani hali ilikuwa kinyume - kulikuwa na kuvunjika kwa vituo vikuu vya mamlaka na kugawanyika kwa nguvu za kisiasa. Katika upande huu mpangilio wa biashara, kwa upande wa Afrika, haukuwa wa ukiritimba wa dola. Ushindani uliwanufaisha watu kadhaa wachache, wanamfalme, watu wa kawaida na hata baadhi ya watumwa-huru; wote ambao sasa waliunda tabaka tawala jipya lililowania kupata nguvu za kisiasa. Huko Duala uadui ulijengeka kati ya familia ya Bela ("Mfalme Bell") na familia ya Ngando ("Mfalme Akwa") na ukaishia katika kutengana mnamo karne ya kumi na tisa. Huko Luango watu wageni - madalali, wafanyabiashara, viongozi wa misafara na watu wengine wa kati au walanguzi - ndio walinufaika zaidi kwani walikuwa na uwezo wa kununua ardhi kutoka kwa mfalme na kuwa na mlolongo wa wategemezi wengi, watumwa huru au watumishi wa nyumbani. *Maluango* walilazimika kuchuuza vyeo vya juu kwa matajiri hawa wapya.

Wakati huo huo hali za wananchi wa kawaida zikawa zinazidi kuwa mbaya. Karne ya kumi na nane ikashuhudia kutokea kwa aina mpya za shughuli za kiuganga na magonjwa ambazo zilikuwa zimekitwa kwa mtu binafsi badala ya kukitwa katika kundi zima la familia; lengo kubwa likiwa ni kujilinda na mashambulizi kutoka kila sehemu. Hapana shaka kwamba hali hii inahusiana na kutokuwepo kwa usalama katika jamii.

## *Kikoa cha Mto Kongo na biashara kubwa ya Kongo*

Hadi kufikia wakati wa ukoloni, mto Kongo ulikuwa ndio kiungo kikubwa cha kuwaleta pamoja watu mbalimbali wa bonde la Kongo. Hii haikutokea tu katika mto wenyewe kupitia sehemu yake inayoabirika juu ya Bwawa la Malebo (Malebo Pool), bali pia katika matawi yake, hasa Alima, Likwala, Sangha, na Ubangi katika ukingo wa kulia; na Kwa, Ruka, Ikelemba na Lulonga katika ukingo wa kushoto. Tangu zama za zama kulikuwa na mtandao wa biashara ambao uliziunganisha jamii za watu zilizokuwa zikiishi kando kando ya mto na matawi yake.

### Uchumi wa kale wa ubadilishanaji

Kuna ushahidi mwingi wa uchumi huu wa kale. Bado ni vigumu kuunda upya hatua mbalimbali za kikronolojia na sehemu mahsusi za makazi katika eneo hili, lakini tunaweza kubainisha miguro mikuu miwili. Mguro wa kwanza uliwaleta watu hawa wazungumzao lugha za Kibantu kutoka katika eneo lao la asili. Mlandano mkubwa uliopo baina ya lugha hizi na baadhi ya lugha za Kiniger-Kameruni unaashiria uhamaji wa moja kwa moja kutoka eneo lao la asili la Niger-Kameruni kuja katika sehemu wanazotamakani hii leo, wakiabiri majini, ambayo ndiyo njia rahisi kupitia katika eneo hili lenye kinamasi na misitu mikubwa. Mbali na mguro huu wa kwanza,



18.2 Kinyago cha kufunika uso kinachovaliwa na mwanajamii ya Ngil kikundi cha wanaume ambao kazi yao ni kutunza amani kwenye jamii na kulinda jamii dhidi ya mabaya.

kulikuwa pia na miguro mingine midogo midogo ambayo pengine ilitokea baadaye ikiwa na uelekeo wa mashariki-magharibi, na ambayo taratibu iliyatengemeza na kuyatenganisha baadhi ya makundi.

Miguro hii ya baadaye ilisaidia kujenga mazingira ya uchumi wa ubadilishanaji kwa kuwatawanya watu katika kanda za kiekolojia ikiwa ni pamoja na mwambao, maeneo ya mafuriko na maeneo makavu. Jamii za wavuvi ziliweza kuuza samaki, ambao walithaminiwa sana, bila tatizo, na kupata chakula au bidhaa za ufundi. Maki zote za akiolojia ya Zaire-Kongo zinapatikana kwenye maeneo ya Bwawa la Malebo, huu ukiwa ni ushahidi wa kuwepo kwa kiwango kikubwa kisicho cha kawaida cha mwendelezo katika wingi wa makazi na shughuli anuwai za binadamu. Kuna maeneo mawili ambayo yanatueleza mengi kuhusu biashara. Kwauza, huko Kingabwa katika ukingo wa kulia wa Bwawa la Malebo, kumechimbuliwa vifinyange kadhaa, na aina moja ya vifinyange hivyo imepatikana pia katika maeneo mengine madogo huko Kinshasa na kando kando ya mto. Vifinyange hivi ambavyo vimekadiriwa tarehe ya kati ya mwaka 1450 na 1640 ni ushahidi wa mahusiano ya kibiashara ya zamani sana kando kando ya mto Kongo na matawi yake. Katika eneo jingine huko Mafamba paipu (labda "viko") nyingi za udongo wa mfinyanzi zimegunduliwa, nyingi yake zikiwa hazijatumiwa; jambo ambalo linaashiria kwamba Mafamba lilikuwa eneo ambako paipu hizo zilikuwa zikitengenezwa au kituo cha kuhifadhia na kusambazia bidhaa hiyo katika sehemu mbalimbali.

Kuna bidhaa mbili ambazo yaelekea ndizo zilizokuwa zimeshamiri sana katika biashara ya masafa marefu: miti ya kemu, kwa ajili ya matumizi ya vipodozi, na shaba nyekundu ambayo ilikuwa ikichimbwa katika mashapo yaliyokuwa katika Kongo ya chini. Biashara ya kijanibu ilihusu bidhaa kama chumvi, nguo, mikeka au majamvi na vikapu.

## Kupandikizwa kwa biashara ya Atlantiki na matokeo yake

Kupandikizwa huku kulifanyika katika hatua kadhaa. Kwanza, kuanzia mwishoni mwa karne ya kumi na tano hadi takriban mwaka 1560, ufalme wa Kongo ndio uliokuwa katika mstari wa mbele. Hati zenye asili ya Kireno za kuanzia mwaka 1529 zinaonyesha kwamba eneo la Bwawa la Malebo lilikuwa ni eneo mojawapo ambako watumwa walikuwa wakipatikana kwa wingi kupitia njia zilizoliunganisha na Mbaza Kongo (São Salvador) na Mpinda. Kipindi cha kati ya 1560 na 1750 kilishuhudia kufifia kwa biashara ya Kongo kutokana na kuongezeka kwa ushindani Angola na matatizo ya ndani yaliyoletwa na Wajaga. Wakati wa hatua ya tatu kuanzia kwenye mwaka 1750 hadi 1850, bonde la mto Kongo na matawi yake pakawa ndio mahali ambapo watumwa waliopelekwa Amerika walipatikana kwa wingi. Mtandao mzito wa njia za misafara uliiunganisha sehemu hiyo na mlolongo mrefu wa bandari katika pande zote za lango lake - Luango, Kabinda, Boma, Ambrizette, Ambriz na Luanda.

Katika hatua zote hizi tatu Bwawa la Malebo ndilo lililokuwa makutano ya biashara za masafa marefu za Kongo na Atlantiki. Athari kubwa ya biashara hiyo ya

pili katika kusisimua uchumi wa eneo hili ilikuwa imekitwa katika taratibu ambazo ni rahisi kuelewa. Biashara ya bidhaanje ilihusu bidhaa za thamani kubwa, na hii ikafanya usafirishaji wa masafa marefu katika mto Kongo na matawi yake kuwa wenye faida kubwa. Kwa hiyo, biashara ya bidhaa zilizotumiwa ndani ya nchi, hata kama ilisafirishwa masafa marefu, nayo ikawa na faida, na hali hii ikayachombeza maeneo mbalimbali kujishughulisha na bidhaa za aina fulani tu.

Eneo la kijiografia lililozungukwa na viwango hivi mbalimbali vya biashara likaendelea kupanuka kuanzia kama mwaka 1500. Hadi kufikia 1690 Bwawa la Malebo lilikwisha ingia katika mahusiano ya kudumu na Kasai ya chini na maeneo yaliyozunguka Mto Alima. Karne moja baadaye Mto Ubangi ulikwisha kuwa sehemu kamili ya ruwaza hii ya biashara, kama ilivyokuwa mito yote iliyo ndani ya eneo hilo na matawi yake. Ni katika karne ya kumi na tisa tu ndipo upeo wa biashara unapoonekana kufikia makutano ya mito Ubangi na Uele. Masoko anuwai yalikuwepo katika maeneo haya ya njia za maji, bila shaka kubwa kabisa likiwa katika makutano makuu ya Bwawa la Malebo. Kila moja ya masoko manne ya Ntamo na Kinshasa katika ukingo wa kushoto, na Mpila na Mfwa katika ukingo wa kulia, lilikuwa na wakazi wa kudumu kati ya 3,000 na 5,000; kwenye idadi hiyo lazima tuongeze watu wengine waliokuwa wapita njia, ambao walikuwa wengi sana wakati wa majira ya biashara, ambayo yalitokea sadfa na majira ya kiangazi kuanzia Aprili au Mei hadi Septemba.

Mfumo wa biashara iliyoelekezwa nje uliegemezwa kwenye bidhaa mbili – watumwa na pembe za ndovu. Watumwa, ambao biashara yao ilishamiri hasa baada ya 1750, walitoka zaidi katika maeneo manne: bonde la Lulonga; maeneo yanayozunguka Mto Alima; nchi ya Boma kati ya makutano ya mto Kongo na mto Kwa na Ziwa Mai-Ndombe; na bonde la Ubangi. Kuzunguka soko kuu la Basankusu, katika bonde la Lulonga, kulikuwa na vijiji vingi ambako watumwa walilima mashamba wakati wakisubiri kuuzwa. Baadhi ya watumwa waliouzwa walifuata mkondo wa mto kwenda kusafirishwa nje; wengine walikwenda hadi Mto Ubangi kuuzwa kwa Waloin kwa kubadilishana na pembe za ndovu ambazo zilikusudiwa kupelekwa katika masoko huko Bwawani na pwani ya Atlantiki.

Miongoni mwa Watio, utumwa wa nyumbani ulikwisha endelea kiasi kwamba neno *mboma* (mwanaume wa kabila la Waboma) lilibadilika maana na kuwa "mtu mjinga" au "mtu wa kazi ya daraja ya chini." Kutokana na kukua kwa biashara ya watumwa, mbinu mbalimbali za kuwapata watumwa zikaongezeka. Miongoni mwa Wabobangi, ambao ndio waliokuwa maarufu kwa biashara katika bonde la Kongo, kulikuwa na tofauti ya wazi kati ya *montonge* (mtumwa aliyekamatwa) na *montamba* (mtumwa aliyeuzwa na jamaa zake), hali ambayo inaonyesha ni kwa kiwango gani maadili ya kijamii yalikwisha haribiwa na biashara ya watumwa.

Bidhaanje ya pili muhimu, pembe za ndovu, inajitokeza katika matini za Wareno za karne ya kumi na sita kama mmojawapo wa mikondo ya biashara iliyoleta faida kubwa. Tangu zamani za kale pembe za ndovu zilikuwa zikitumiwa humo humo

nchini kwa kutengenezea bangili na chupio za nywele, lakini thamani yake kibiashara katika eneo hili ilikuwa ndogo. Kulikuwa na makundi mengi ya tembo katika ukanda wa msitu, na Mbilikimo takribani walikuwa na ukiritimba wa uwindaji wa wanyama hao; lakini mtandao wa haki juu ya wanyama waliouawa ulikuwa changamani kiasi kwamba baada ya watemi kuchukua sehemu yao faida iliyobakia kwa ajili ya mwindaji ilikuwa kidogo tu. Hadi kufikia mwishoni mwa miaka ya 1700 pembe za ndovu zilisafirishwa kwa kutumia njia zilezile za kusafirishia watumwa, ambao kwa thamani walichukua sehemu kubwa ya biashara, na zikapitia katika mikono ya watu wale wale. Uhusiano wa kithamani kati ya bidhaa hizo mbili uligeuka tu baada ya 1830.

Bidhaa zilizopatikana katika ubadilishanaji kutoka pwani, ambazo mwanzoni zilikuwa ni chumvi, *nzimbu* (samakigamba) kutoka Luanda, nguo na shanga tu, zilipanuliwa katikati ya miaka ya 1600 kwa kuingizwa bidhaa za metali, hasa visu na vioo. Karne ya kumi na nane ilishuhudia ongezeko kubwa la magobore na baruti, vifaa vya bati na shaba nyekundu na vileo. Haieleweki vizuri ni vipi bidhaa hizi zilikuwa katika mzunguko katika bonde la Kongo; wepesi wa mzunguko huo umebakia jambo la kukisia tangu Stanley alipokadiria, mnamo mwaka 1880, kwamba ilichukua wastani wa miaka mitano kwa bidhaa kutoka Ulaya kusafirisha kutoka pwani hadi Ubangi.

Biashara ya bidhaandani ilichukua eneo lile lile, au pengine kubwa kidogo kuliko lile la bidhaanje. Mara nyingi watu walijishughulisha katika biashara zote kwa pamoja. Biashara hii ya ndani ilihusu hasa bidhaa za chakula na chumvi. Bidhaa ya chakula ilikuwa na faida ya kuwa na soko kubwa kwa sababu kuanzia karne ya kumi na nane na kuendelea, kiu ya mahitaji yake makubwa ambayo yalikuwa yakiongezeka kila leo ilikuwa haina budi kuzimwa. Muhogo, uliolimwa na kutayarishwa na wanawake, ulikuwa bidhaa mojawapo iliyokuwa ikitafutwa sana. Michikichi ilitoa mafuta kwa matumizi ya nyumbani na tembo. Chumvi ilikuwa bidhaa nyingine iliyokuwa muhimu sana, iwe ni chumvi ya mawe kutoka Mbosi, au chumvi ya mboga ambayo ilizalishwa zaidi na watu walioishi karibu na maji. Jamii hizi pia ziliuza aina maridhawa za samaki wabichi au waliokanzwa kwa moshi kwa kutumia mbinu bora. Tumbaku na pombe ya kienyeji viliuzwa pia .

Kazi za mikono pia zilichangia katika biashara. Hizi zilikuwa kazi za wataalamu maalumu: katika jamii za wakulima, wanawake walilima, wakiacha kazi za ufundi zifanywe na wanaume; hata hivyo katika jamii za wavuvi, kuvua ilikuwa kazi ya wanaume, na kazi za mikono zikifanywa na wanawake. Bidhaa zilizokuwa zikitafutwa sana zilikuwa ni: mikeka/ majamvi na unga wa miti ya kemu, bidhaa zilizotengenezwa na wanawake; viramba, ambavyo vilitengenezwa sana na Watio; zana za chuma; vyombo vya mfinyanzi; na mwisho, mitumbwi ya ukubwa mbalimbali, kuanzia mita tatu hadi mita ishirini, na pengine zaidi ya hapo.

Kwa hiyo kulikuwa na tofauti kubwa kati ya aina hizi mbili za biashara. Biashara ya kusafirisha bidhaa nje iliegemezwa kwenye uchumi wa uharibifu na iliwanufaisha

watu wachache sana. Biashara ya bidhaa za ndani iliegemezwa kwenye uchumi wa uzalishaji na iliwanufaisha watu wa kawaida, wanaume na wanawake, kila mmoja akipata kulingana na alivyozalisha.

## Jamii anuwai

Uchumi huu wa ndani uliendeleza muungano wa hatua kwa hatua wa jamii mbalimbali za bonde la Kongo, japo kulikuwa na vikwazo vilivyoshawishi kuwepo kwa tofauti. Kikwazo kimojawapo ni namna biashara ilivyokuwa ikiendeshwa. Ilikuwa ni biashara iliyogawanyikagawanyika, na ilibakia hivyo hadi karne ya kumi na tisa. Mto na matawi yake yaligawanywa katika maeneo ya udhibiti, kila moja likiwa linadhibitiwa na mbari moja. Ni katikati ya karne ya kumi na nane tu ambapo Wabobangi walianza kukidhibiti kikoa chote cha Kongo-Ubangi. Kwa kipindi kirefu sana kutoaminiana kulitawala mahusiano yaliyokuwepo kati ya wabia mbalimbali, na uporaji Ililikuwa jambo la kawaida. Mgongano wa kimaslahi aghalabu uliishia katika vita kamili, kama vile vilivyotokea kati ya Wabobangi na Watio, ambao walifikia makubaliano ya kudumu mwanzoni mwa miaka ya 1800 tu.

Kati ya mambo mengi yaliyoleta muungano, muhimu kabisa zilikuwa ni zile mbinu zenyewe za biashara. Kutokana na hali hiyo, kuanzia karne ya kumi na nane, eneo lote likaanza kutumia sarafu katika kubadilishana bidhaa - viramba, *nzimbu*, kauri na fito za shaba. Utaratibu wa kukopeshana ulioenea sana ukaleta mlolongo ya mshikamano katika eneo lote la biashara. Maadili mema ya biashara pia yakapelekea kutafuta mbinu za kupanua umoja kwa njia ya kuoana; na, zaidi ya yote, udugu wa kuchanjiana ambao ulileta uwajibikaji wa aina mbalimbali kati ya wahusika. Kwa hiyo, biashara ya mto ikawa kalibu iliyowakutanisha watu kutoka sehemu tofauti tofauti, wakieneza mila na imani zile zile na kuifanya lugha ya Kibobangi kuinukia haraka kama lugha ya biashara. Ustaarabu huu wa pamoja, uliojengeka haraka katika karne ya kumi na nane, ulifikia kilele chake kati ya 1850 na 1880.

Hata hivyo, kukua huku kwa umoja kulikwenda bega kwa bega na kiasi fulani cha kutofautiana, kulikotokana na namna anuwai ambazo jamii mbalimbali zilifuata katika kuendesha biashara pana ya Kongo. Si kila mtu alijishughulisha na biashara. Katika eneo hili, ambako kulikuwa na maji mengi, uvuvi, kazi mojawapo iliyofanywa tangu zama za zama na Wabantu wa bonde la Kongo, uliendelea kuwa ndiyo shughuli kubwa ya makundi mengi. Jamii za wavuvi zilijibainisha kwa miguro yao ya mara kwa mara, ambayo ilitegemea tofauti za kiwango cha maji na kubadilikabadilika kwa mafungu ya kuvulia samaki. Kutegemeana na majira, watu waliishi katika vijiji vya kudumu au katika kambi za wavuvi zilizojengwa wakati kiwango cha maji kiliposhuka na ambazo zilihamwa wakati kiwango kilipoongezeka. Kijamii na kisiasa kulikuwa na kusigana dhahiri kati ya vitengo vya kisiasa na kiuchumi. Kitengo cha msingi cha kisiasa bado kilikuwa ni kijiji: Mamlaka ya chifu, ambayo kimsingi yalikuwa ya kimiviga na kidini, yalitekelezwa katika kiunzi hiki peke yake. Kwa hiyo shughuli za vikosi mbalimbali vya wavuvi hazikuwa chini ya udhibiti wake. Lakini

kitengo cha msingi cha uchumi kilikuwa ni kile cha kikosi cha wavuvi ambacho muundo wake haukuwa imara sana na ambacho kilitokana na jitihada za mvuvi mmoja maarufu pamoja na baadhi ya ndugu zake na watu wengine waliojitolea. Kwa njia hii, kaya za kifamilia ambazo zilikuwa ndizo msingi wa vijiji zilivurugwa ili kukidhi mahitaji ya uvuvi.

Wale waliofanya shughuli za biashara peke yake walipitia mageuko ya namna tofauti, kama inavyojionyesha katika namna tofauti za mageuko ya Wabobangi na Watio. Ni vigumu kupata maelezo ya kina ya uhamaji wa Wabobangi kutoka Ubangi ya kati au ya chini kwenda Bwawa la Malebo. Kinachofahamika sasa ni kwamba ile jamii ambayo hapo awali ilikuwa ya wavuvi iligeuka kwa kasi kuwa jamii ya wafanyabiashara, kazi ambayo ilitokea kuwa msingi pekee wa maisha ya jamii hiyo. Kuanzia wakati huo kukawa na mwingiano kamili wa kitengo cha siasa na kile cha uchumi. Jamii ya Wabobangi ilikuwa imekitwa kwenye makampuni ya wafanyabiashara matajiri. Ilikuwa jamii iliyoacha milango yake wazi na yenye kutoa fursa kwa mtu kujiinua: Yeyote aliyejishughulisha sana na biashara na kufanikiwa aliweza kujilimbikizia mali, ambayo ndiyo iliyokuwa njia ya kujiongeza idadi ya watu waliomtegemea, kupata nguvu na kudai vyeo vya kisiasa.

Watio walikuwa na bahati nzuri ya kuishi kwenye njia panda na kituo kikuu cha kutawanyia shehena katika mtandao wa biashara ya Kongo. Yaelekea kwamba biashara haikuidhoofisha miundo ya kisiasa ya ufalme huo. Miundo hiyo ilikuwa imeunganifuliwa (imesambaza madaraka) kwa mapana. Muundo kiini ulikuwa ni wa temi ambazo kwa kiasi fulani zilikuwa zikijitegemea. Mtemi alikuwa na madaraka makubwa ya kimiviga na kidini, lakini mamlaka yake ya kisiasa yalikuwa kidogo. Hali ya namna hiyo hiyo ilijitokeza katika ngazi za juu. Mfalme, ambaye alijulikana kama *Ôkoo* (neno ambalo lilitamkwa vibaya na Wazungu kama *makoko*), zaidi alikuwa na madaraka ya kiroho. Mamlaka ya kutawala yalikuwa mikononi mwa watu maarufu wachache kama *ngaailiino,* ambaye alishughulika na ukusanyaji ushuru na kusimamia utawala, na *muidzu*, jaji kiongozi wa nchi. Kinyume na utemi, cheo cha *Ôkoo* hakikuwa cha kurithi; mfalme alichaguliwa na machifu wenzake kutokana na watemi mashuhuri katika ufalme huo. Muundo huu wa zamani uliendelea kuwa na sifa zake muhimu hadi majilio ya ukoloni. Mabadiliko ya kudumu yalitokea katika kiwango cha kijamii. Kwanza kulikuwa na kuongezeka kwa utengano baina ya watu walioishi kando kando ya mito, ambao walikuwa na ukiritimba wa shughuli za biashara, na Watio wa bara ambao walijishughulisha zaidi na kilimo (cha muhogo na tumbaku) kwa ajili ya soko la maeneo ya mto. Kati ya watu walioishi kando kando ya mto, wale ambao walifaidika zaidi na biashara walikuwa machifu, ambao waliitumia kikamilifu haki yao ya kuuza binadamu na pembe za ndovu. Kinyume chake, machifu ambao waliishi mbali na mito na watu wengine wenye vyeo ambao walikuwa mbali na Bwawa, kwa mfano, mfalme, ambaye aliishi Mbe, walishiriki mara chache tu katika biashara hiyo kwa kutuma wawakilishi wao huko. Walikuwa na mamlaka ya

kisiasa lakini mamlaka yao ya kiuchumi yalikuwa kidogo kuliko ya wale walioishi kando kando ya mto.

Uchumi huu wa biashara wa Wabobangi na Watio haukupata kuwa wa kibepari, ingawa ulileta faida kubwa sana. Ilikuwa haiwezekani kununua ardhi au nguvukazi, isipokuwa ile ya watumwa. Fedha, ambayo ilikubaliwa katika baadhi ya biashara, haikuweza kutumiwa kwa kununulia kila bidhaa. Baadhi ya bidhaa na huduma nyingine za kijamii na kidini, kama vile faini na mahari, havikuingizwa kabisa katika uchumi wa kifedha.

Kwa hiyo picha inayopatikana kutoka kwa jamii za Afrika ya Kati inaonyesha wazi tofauti zao za kimaisha na welekeo wao wa ubunifu, hata katika mazingira magumu. Inaonyesha pia, kwa kuzingatia mapengo katika taarifa zilizopo, ni uelekeo gani watafiti wafuate: utafiti mpana wenye nyenzo za kutosha, ukiwa umeelekezwa hasa katika kukusanya mambo mapya kwa njia ya akiolojia na mapokeo simulizi, na kuunda viunzi makini vya kinadharia katika uchunguzi wa miundo ya kijamii, mageuko ya kiutamaduni na historia ya tabia na mitazamo ya watu.

# 19 Ufalme wa Kongo na majirani zake

Upande wa Magharibi wa Afrika ya Kati kuelekea kusini mwa Misitu ya Ikweta, wanaishi watu wanaosema lahaja za lugha ya Kikongo na lugha nyinginezo zinazokaribiana nayo. Umoja huu unaimarishwa na umoja mzito wa kitamaduni. Kundi hili lililoshikamana kiethnografia na kiisimu linakalia eneo linalotanda kutoka Gabon ya kusini hadi uwanda wa juu wa Benguela na kutoka Bahari ya Atlantiki hadi kuvuka Mto Kwango.

Historia ya jimbo hili imeandikwa vyema tangu mwaka 1500 na kuendelea. Kwa zaidi ya miaka mia moja, matini na vitabu vya miongozo vimekuwa vikichapishwa chapa nyingi, na tapo la historiografia (ya eneo hili) limeendelea kukua tangu karne ya kumi na saba.

Mwelekeo wa kihistoria katika maeneo haya katika karne za kumi na sita na kumi na saba ulikuwa tofauti na ule wa nyakati za baadaye. Nchi kubwa kubwa ziliunganishwa, kwa kutumia miundo ya kisiasa, kuunda madola. Hata hivyo baada ya takriban 1665 nchi hizi zilipangiliwa upya katika maeneo makubwa zaidi, kigezo cha kuziunganisha sasa kikitokana na matakwa ya muundo wa kiuchumi uliotokana na biashara shadidi ya watumwa. Kwa hiyo tutazikabili karne za awali kwa kutanguliza historia ya falme hizo, na kisha, kwa kuwa harakati za biashara zilishusha hadhi ya falme, biashara itakuwa ndiyo lengo la uchunguzi wetu.

Mandhari ya majimbo haya yanatawaliwa na umbile la nchi na mvua. Hali ya nchi kuwa ya milima milima inaeleza kwa nini idadi ya watu wenye kutafuta makazi bora haikulingana sehemu zote. Eneo lililofaa zaidi lilikuwa upande wa kaskazini mwa mto Zaire/Kongo, kuanzia pwani hadi eneo lililoitwa Mayombe. Hapa, pia, palikuwa na migodi ya haja ya madini. Hapa ndipo madola mawili makubwa kabisa ya pwani, ya Kongo na Luango, yalipozaliwa.

Tangu angalau mwaka 400 kabla ya zama za Ukristo angalau, wakulima wenye kusema lugha za Kibantu za magharibi walikwisha sakini kaskazini na kusini mwa sehemu ya chini ya Mto Kongo, ambako walilima viazi vikuu, mboga na michikichi. Kuanzia karne ya pili hadi ya tano, watu hawa waliongezeka kutokana na kuwasili kwa watu wanaosema lugha za Kibantu za mashariki kutoka upande wa mashariki. Watu hawa walilima nafaka na, pale mbung'o waliporuhusu, waliweka mifugo.

Mwisho, labda katika karne ya sita, kilimo cha migomba kiliingizwa kukamilisha utaratibu wa uzalishaji.

Baada ya hapo, miundo ya kisiasa-kijamii ikawa changamani zaidi, na temi zikaundwa baina ya bahari na upande wa juu wa mto Kongo toka Bwawa la Malebo. Ilikuwa katika jimbo liitwalo Mayombe ambako mgawano wa kikanda wa kazi uliendelezwa vyema kabisa. Hadi karibu na mwaka 1500, wakazi wa pwani walikuwa tayari wanauza chumvi na samaki na walikwisha geuza uwanda wa pwani wa Luango, kuelekea mlango wa Mto Kongo, kuwa msitu mkubwa wa michikichi wenye kuzalisha mafuta ya mawese. Kaskazini zaidi, karibu na kingo za msitu mkuu, mikindu ililimwa na kutumiwa kutengeneza nguo. Mwisho, ndani ya eneo hilo hilo na kuingia zaidi msituni, miti ya rangi nyekundu ilibadilishwa na bidhaa za savana. Hapa ndipo ulipozaliwa ustaarabu wa Kongo.


Ufalme wa Kongo ulianzia kwenye utemi wa Vungu Kaskazini mwa Mto Kongo. Nimi Lukeni, mwasisi wa ufalme wa Kongo, alianzisha mji wa Mbanza Kongo mahali ilipo San Salvador sasa. Ufalme wake uliundwa kiasi kwa kufanya ushirika na chifu mwenyeji, *Kabunga,* na mfalme aliyetawala Mbata katika bonde la Inkisi, na kiasi kwa kuteka nchi nyingine kuelekea baharini na sehemu ya chini ya bonde la Inkisi. Tarehe ya uasisi wa ufalme huu haijulikani, lakini inawezekana ilikuwa kati ya miaka ya 1300 na 1400.

Ufalme wa Tio huenda ulianzishwa mapema zaidi. Ufalme wa Luango, ulioanzishwa karibu na Vungu upande wa kaskazini mwa mto, unafikiriwa na baadhi ya wanazuoni kuwa ulifikia kilele cha ustawi wake katika karne ya kumi na sita, lakini nadharia hii tete inabishaniwa. Upande wa kusini wa Kongo, dola la Ndongo, ambalo mfalme wake alikuwa na cheo cha *Ngola* neno lililogeuzwa kuwa "Angola," lilikuwa linaanza kujengeka mnamo miaka ya 1500.

## *Hegemonia: Kongo*

Katika karne za kumi na sita na kumi na saba dola moja, Kongo, lilitawala eneo lote baina ya uwanda wa juu wa Benguela na nyanda za Bateke na kutoka baharini hadi kuvuka Mto Kwango. Mnamo 1500, mipaka halisi ya dola ilifuata Mto Kongo toka mlango wake kuelekea juu hadi ndagano na Mto Inkisi, ikivuka hadi ng'ambo ya mto kuelekea kaskazini katika baadhi ya sehemu. Nchi hiyo ilijumuisha bonde la Inkisi na nchi zote za kusini hadi Loje. Eneo hilo lilikuwa na watu kati ya milioni mbili na tano, ingawa hatujui idadi hasa. Eneo lililokuwa chini ya twaa ya Kongo lililingana na ufalme huo, angalau kwa idadi ya watu. Idadi ya watu katika ufalme wa Tio bila shaka ilikuwa ndogo sana, isipokuwa katika maeneo ya Bwawa la Malebo.

Ufalme uligawanywa kati ya sehemu ya mji mkubwa, yaani makao makuu Mbanza Kongo, na sehemu ya shamba. Tabaka tatu za kijamii zilizojibainisha vizuri ziliishi pamoja: Malodi, Washamba na Watumwa. Malodi walikuwa ndio kiunzi cha ufalme, na waliishi mijini isipokuwa pale walipotakiwa kufanya kazi kama magavana




**19.1** *Kongo na majirani zake kwenye karne ya kumi na sita.*

wa majimboni. Tabaka la juu ya malodi lilijumuisha jamaa wa mfalme au mmoja wa watangulizi wake. Kwa mtazamo wa vijiji, malodi waliunda kikundi pekee. Utaratibu wa umama uliamua upatikanaji wa ardhi, makazi, na urithi wa uongozi wa kijiji. Mfalme aliwateua jamaa zake wa karibu kwenye nafasi muhimu. Ufalme ulikuwa wa kuchaguliwa; baraza tukufu liliundwa na wajumbe kumi na wawili, wakiwemo wanawake wanne ambao, kufuatana na A. Hilton, waliwakilisha koo za mababu wa mfalme. Mapambano ya kurithi ufalme yalikuwa mambo ya kawaida. Baada ya mapambano baina ya malodi wa kaskazini na wale wa makao makuu na kusini, Nzinga Mbemba, ambaye alijulikana pia kama Afonso I, alimrithi baba yake Nzinga Nkuwa mwaka 1506.

Wafalme, ambao walishiriki ndoa za mitala, walikuwa na watoto wengi, na koo zao zilikua kupindukia. Kongo iligatizwa mno. Mfalme aliteua magavana wa majimbo isipokuwa gavana wa Mbata na, baada ya 1491, gavana wa Soyo. Aliwafukuza magavana na maofisa wengine kadiri alivyoona inafaa. Malodi hawakuwa na dhima za urithi na katika kila kizazi hadhi yao ilifasiliwa upya kuhusiana na mfalme mpya. Ugatizaji ulipaliliwa na kuwako kwa sarafu iliyodhibitiwa na mfalme. Sarafu hii ilikuwa ni kombe zilizoitwa *nzimbu* zilizopatikana kutoka mavulio ya samaki ya kisiwa cha Luanda, ambacho kilikuwa sehemu ya ufalme. Pia lilikuwepo jeshi unganifu. Mwishoni mwa karne ya kumi na sita, kikosi cha walinzi wa mfalme kilichoundwa na watumwa kilikuwa na askari kati ya 16,000 na 20,000, na ndicho kilichokuwa jeshi pekee la kudumu la ufalme. Wakati wa vita vya nje, wakulima walishirikishwa kama vikosi vya majimbo.

Itikadi ya ufalme, iliyoitwa *nkisi,* ilitokana na dhana za kidini ambamo madhehebu matatu yalihusika. Haya yalikuwa ni kuabudu wahenga, ambako mahali pake patakatifu palikuwa ni msitu wa maziara matakatifu, kuabudu mizimu ya ardhi na kuabudu hirizi za kifalme. Dhana ya *nkisi* ilikuwa ya msingi, na hata Wakristo walitwaa kutwaa neno hilo, wakilitumia kumaanisha "hicho kilicho kitakatifu," kwa mfano kuliita kanisa nyumba ya *nkisi.* Maradhi na mikosi vilisingiziwa *ndoki* (mchawi) aliyeweza kutambuliwa na *nganga ngombo* (waaguzi), wakati mwingine kwa majaribu. Ufalme ulikuwa mtakatifu. Mfalme aliitwa *Nzambi Mpungu* (Muumba Mkuu). Kwa *tumba* (baraka) zake mfalme aliwapa ulinzi watumishi wake watiifu, na kwa jumla aliwahakikishia watu neema, hasa kwa kudhibiti mvua. Mfalme mwenyewe kwa hakika na kwa dhati, alikuwa *nkisi* wa nchi .

Miundo katika falme za jirani ilikuwa tofauti, lakini itikadi ilikuwa karibu ni ile ile. Falme hizi hazikugatizwa sana. Katika Luango, nasaba za malodi hazikuyang'oa makundi ya umama, na tabaka hili lilikuwa na mshikamano mdogo wa ndani kuliko katika Kongo. Ndongo haikuwa na muundo wa kincli zaidi ya kiwango cha utemi, na mfumo wa kijeshi ulikusudiwa kuziba pengo la kasoro hii.

Ushindi wa Afonso I uliingiza utawala mrefu kabisa katika historia ya Kongo, tangu 1506 hadi 1543. Kazi iliyotendwa na mfalme huyu ilikuwa muhimu. Alifungua milango ya nchi kwa Wareno, hivyo akaanzisha msururu wa mageuzi

makubwa ya kiuchumi na ya kisiasa, na usimilisho wa makusudi wa nduni za Kikristo ambazo zilitokea kuwa za kudumu. Alipokuwa mfalme, chifu huyu wa kikundi kidogo haraka akalifanya Kanisa Katoliki dini ya dola. Kanisa hilo, kuanzia 1518 hadi 1536, liliongozwa na mwanawe, Henrique, ambaye alisimikwa kuwa askofu huko Roma. Uaskofu baadaye ulidhibitiwa na Ureno. Biashara ya watumwa ilianza tangu 1514 na kuendelea. Mwanzoni mfalme alijaribu kuidhibiti kwa kujenga ukiritimba wa kifalme na halafu, mwaka 1526, kuikomesha. Jaribio hili lilishindikana, na hata ukiritimba wa kifalme ulivunjwa mara kwa mara na Wareno wa Kiafrika wa São Tomé na majirani wa ufalme, hata katika Luanda, ambayo ilikuwa sehemu ya ufalme. Mfalme alitumia mapato yake kutokana na biashara ya watumwa, biashara ya pembe za ndovu na biashara ya nguo za kindu kuwavutia mafundi wa Kireno na zaidi ya wote, wamisionari. Katika utawala wake, maisha ya kijamii na ya kisiasa yalibadilishwa. Pengo kati ya mamwinyi na watu wa kawaida lilipanuka: mamwinyi walisoma, wakaupokea Ukiristo na kushiriki katika biashara ya watumwa, ilihali watu wa kawaida walinyonywa vikali.

Wafalme wote waliofuata walikuwa ni wajukuu wa Afonso kupitia mabinti zake wakuu watatu. Ongezeko lisiloisha la wadai wa kiti cha enzi lilileta mgawanyiko wa nyumba ya mfalme katika makundi na, baada ya 1665, kuzusha vita vya wenyewe kwa wenyewe. Kuwako kwa Wareno mjini kuliingiza sura mpya ya kisiasa. Kutokana na mahusiano yao ya kindoa na familia za malodi, Wareno waligawanyika katika makundi ya machotara wa Kireno-Kiafrika na wenyeji wa Ureno, na waliongoza vikundi vya upinzani barazani hadi 1665, na kushiriki katika mapambano yote ya kuwania kiti cha enzi.

Biashara ya kimataifa, iliyokuwa ndogo sana kabla ya 1506, ilikua baada ya kuanza kushughulikia watumwa. Mahuruji yalifikia watumwa 4000 hadi 5000 kila mwaka mpaka karibu mwaka 1540, na watumwa 6000 hadi 7000 baada ya hapo. Maduhuli kutoka Bwawa la Malebo bila shaka yalikuwa makubwa mno, kwani watumwa wengi waliingizwa Mbanza Kongo siyo tu kwa ulinzi wa mfalme bali pia kwa ajili ya mashamba ya chakula kilicholisha makao makuu, na watumwa wengine walipangiwa bandari ya Mpinda na misafara ya aila ya mfalme. Pamoja na biashara hii iliyosimamiwa, biashara ya sirisiri ya watumwa iliyoendeshwa na wakazi wa São Tomé ilistawishwa katika mipaka ya kaskazini na kusini ya ufalme, hasahasa baada ya mwaka 1526, wakati mahuruji kutoka ufalme wa Benin yaliposita.

Ureno ilishabikia sana mazao ya madini ya nchi na kutaka kuyadhibiti. Hata hivyo mfalme wa Kongo alidhamiria kudhibiti vikali uchimbaji wa shaba ya Bembe na ufuaji chuma wa Mbanza Kongo. Mfalme wa Ureno kwa upande wake hakuruhusu kabisa kuuzia Kongo meli na alipinga majaribio ya Kongo ya kuandaa vyombo vyake yenyewe vya usafiri kwenda São Tomé au Ulaya. Wareno walidhibiti biashara na kuigeuza kuwa mabadilishano yasiyolingana. Kitala cha Kongo kilitumia sehemu kubwa ya mapato yake kuagiza nguo, mvinyo na bidhaa za anasa ambazo punde zilligeuka kuwa mahitaji ya lazima japo ya kifahari.

Wakati wa uongozi wa warithi wa Afonso I, nguvu ya Kongo ilipungua, hasa kwa kulinganishwa na Ndogo, ambayo ilikuwa ikiongezeka nguvu hasa kupitia biashara ya sirisiri na São Tomé. Mwaka 1561 Kongo ilijitenga na Ureno takriban moja kwa moja, lakini mfululizo wa vifo vya wafalme wawili wakati wa vita na Watio wa Bwawa la Malebo katika 1566 na 1567 ulileta mtafaruku ambao, pamoja na uvamizi wa wapiganaji waitwao Wajaga kutoka Mashariki ya Kongo, uligeuka kuwa maangamizi.

## *Madola matatu: 1575 -1640*

Wajaga walitimua majeshi ya mfalme, naye akalazimika kukimbilia kisiwani sehemu ya chini ya Mto Kongo. Wakimbizi wengi waliuzwa utumwani na Wajaga kwa watu wa São Tomé. Mfalme alilazimika kuililia Ureno, ambayo ilituma jeshi la tabaro, na nchi ikatwaliwa tena kati ya 1571 na 1573, ingawa majeshi yalikuwa hayakuondoshwa kabla ya 1575 au 1576.Hegemonia (mamlaka) ya Kongo juu ya ukanda huu ilivurugwa, kwani koloni la Angola lilianzishwa mwaka 1575, na Wareno walikuja Luango kwa idadi kubwa kufanya biashara tangu mwaka huo na kuendelea.

Haijapata kujulikana ni watu gani waliivamia Kongo. Jina "Wajaga" linatumiwa ndani ya kumbukumbu kumaanisha "washenzi." Uvamizi huu hauna budi kuhusishwa na vita vya Kongo na Tio, na pengine ulihusiana na ukomeshaji wa biashara ya watumwa mwaka 1561. Inadhaniwa kuwa safu za wavamizi zilijazwa na idadi kubwa ya wanavijiji waliokuwa wamechoshwa na dhuluma za malodi.

Paulo Dias de Novaes, baada ya kuishi kwenye kitala cha Ndongo, alijijenga kiasi cha kupata mkataba kutoka kwa Mfalme wa Ureno uliomruhusu kuiteka Ndongo na kuigeuza koloni. Koloni lingeitwa Angola, kutokana na jina la cheo cha mfalme wa Ndongo. Dias alizindua Luanda mwaka 1576 na kuanza kufanya biashara ya watumwa, akijaribu kuing'oa jumuiya ya machotara wa Kireno (Wareno-Waafrika) kutoka São Tomé waliokuwa wakivinjaria biashara katika maeneo hayo. Jumuiya hii ilimwachia soko na kuhamia kwenye kitala cha *ngola*. Mwaka 1579, hata hivyo. shinikizo toka Ureno lilimlazimisha Dias kusitisha mkataba wake. Mfalme wa Ndongo alipoambiwa haya, aliamrisha Wareno wote kwenye kitala chake wachinjwe kama kinga, hivyo akatoa kisingizio cha vita viliyodumu kwa karibu karne nzima, hadi 1671. Mwanzoni, mafanikio ya vita yaliyumba, na Wareno walifanikiwa kwa shida kujenga ngome chache bara. Mwaka 1612 Wareno walifanya urafiki na Wambangala (waitwao Wajaga) na kwa msaada wao, na hasa ule wa Jaga Kasanje, Wareno walitwaa sehemu kubwa ya ufalme tangu 1617 hadi 1621. Mfalme alikimbilia mashariki ya nchi na washirika wakafanya uporaji jimboni kote. Mkataba wa amani uliandaliwa mwaka 1622-1623, *ngola* akiwakilishwa na Nzinga Mbande, dada yake, aliyebatizwa na kuitwa Anna huko Luanda. Nzinga akawa kiongozi wa kikundi kilichopiuga Wareno; mwanzoni mwa 1624 mfalme alifariki na Nzinga



19.2 *Mahakama ya Mfalme wa Waloango, 1668*

akawa Naibu Mtawala, halafu Malkia mwaka 1626. Vita vikazuka tena dhidi yake, lakini pia dhidi ya Kasanje, ambaye alikuwa bado anakalia sehemu bora kabisa ya Ndongo. Wakati mapambano yanaendelea Kasanje alijenga kituo katika bonde la Kwango, ambako alijenga dola la Imbangala mnamo 1630. Wakati huohuo, Nzinga aliteka ufalme wa Matamba, ambako alisimika kituo imara cha upinzani kwa utawala wa Wareno. Waholanzi walipotwaa Luanda, alikuwa bado kwenye kampeni yake, na akafanya urafiki nao.

Koloni la Angola lililotawaliwa na gavana aliyeteuliwa na Lisbon, liligawanywa katika mji wa Luanda na *presidos* chache. Muundo wa utawala ulikuwa wa kimwinyi, misingi yake ya kisheria ikiwa mikataba ya kitwana iliyowaunganisha *soba* (machifu uchwara) na kitala cha Wareno. Mapato ya dola na ya wawakilishi wake yalitokana na ushuru wa kimwinyi, na yote, yawe ya kutokana na bidhaa au nguvukazi, yalilipwa kwa (njia ya) watumwa. Mfumo huu haukubadilishwa hadi karne ya kumi na nane, ilipoanzishwa kodi ya kichwa na mikataba ya kitwana kubadilishwa na hati ya kisheria yenye kuhalalisha haki za ufalme wa Ureno.

Wakati huo huo Kongo ikafufuka. Licha ya kupoteza hegemonia yake na mabadiliko yaliyokuwa yakitokea polepole katika muundo wa tabaka la malodi, ufalme ulibakia imara na hata kuenea kuelekea mashariki. Kongo ilifanikiwa kuzuia majaribio mengine ya Ureno ya kuidhibiti kwa kufanya urafiki wa kibalozi na Vatikani, na kwa kuigonganisha Ureno na Hispania, na hata kuzigonganisha nchi zote mbili na Uholanzi. Hasara kubwa iliyotokea ilikuwa ni kupoteza jimbo la majini la Soyo, pamoja na bandari ya Mpinda. Baada ya 1636, jimbo hili lilikuwa huru.

Luango lilikwishakuwa dola kubwa hata kabla ya 1600. Eneo lake lilienea kutoka wangwa wa Fernán Vaz hadi kusini mwa Pointe-Noire. Athari yake ya kitamaduni, iliyoenezwa na biashara, iliendelea hadi mbali zaidi; lakini karibu hatujui chochote kuhusu maendeleo yake ya kisiasa kabla ya 1700.

Luango ilifanya biashara ya pembe za ndovu, ngozi, miti yenye kutoa rangi nyekundu, na viramba (nguo za kindu), lakini ilisafirisha watumwa wachache sana. Kuanzia 1600 Waholanzi walitembelea Luango na Soyo mara kwa mara. Meli za Waholanzi zilikuwa na bidhaa bora kwa bei nafuu. Walinunua shaba na, zaidi ya yote, waliuza bunduki na baruti. Matokeo yake yakawa kwamba Wavili, wafanya biashara katika pwani ya Luango walioandaa misafara ya kwenda bara, walipanua mitandao yao kwa kasi kubwa ajabu.

Kipindi hiki mtandao wa Wavili ulikuwa katika mashindano na mitandao mingine iliyopo, si kwa kuuza pembe au nguo tu bali pia kwa biashara ya watumwa. Mtandao wa Kongo na Angola ulivurugwa kwa kuanzishwa kwa mji wa Luanda, ambao, tangu awali, ulisafirisha watumwa wengi kuliko Mpinda; shehena za kwanza zilikuwa kati ya watumwa 12,000 na 13,000 kwa mwaka, wengi wao wakiwa mateka wa vita. Baada ya miaka michache ya mwanzo, watumwa wengi zaidi na zaidi walitokana na manunuzi bara, ama katika Bwawa la Malebo au katika soko la Ocanga kwenye Mto Kwango. Katika miaka ya 1630 watumwa walianza kuwasili Luanda kutoka Matamba na Kassange, makao makuu ya Kasanje.

Maendeleo haya yaliathiri Kongo vibaya sana, kwani makao makuu yake hayakuwa kituo cha lazima cha kupitishia bidhaa na watumwa. Zaidi ya hayo, sarafu yake ilipoteza thamani sana, baada ya Wareno kuingiza simbi nyingine. Hadi 1619 *nzimbu* ilikwisha poteza thuluthi mbili ya thamani yake - na mfalme kupoteza thuluthi mbili ya mapato yake. Mfalme hata hivyo, aliweza kukabiliana na hali halisi na sarafu taratibu ikarejea thamani yake ya awali. Mapato ya mfalme na malodi bila shaka yaliathirika kwa kuielekeza biashara Luanda na Luango.

Kipindi hiki kilishuhudia kuingizwa kwanza kilimo cha mahindi (baina ya 1548 na 1583) na mara baada ya 1600, kilimo cha mihogo, tumbaku na labda maharage, karanga na mimea mingine ya Dunia Mpya (Amerika). Nguruwe wanatajwa tangu

1583 na kuendelea, na hawa huenda ni wanyama walioingizwa kutoka nje. Walienezwa zaidi ndani ya Kongo na Angola ya Kati. Mazao mapya yaligeuza kilimo katika karne ya kumi na saba, hasa baada ya 1650, yakiongeza mavuno na kutoa, pamoja na muhogo, chakula kilichofaa mno kwa ukame wa mara kwa mara na hali ya kivita. Hata hivyo, tangu zama za 1560 ugonjwa wa ndui unagusiwa; huu ni ugonjwa wa mlipuko ulioingizwa kutoka Ulaya na kuwa kero ya kudumu.

Hivyo, nusu ya kwanza ya karne ya kumi na saba ilishuhudia mabadiliko ya hali ya lishe na siha - na kuingia kwa biashara ya watumwa. Kwa vyovyote vile haya yote yalianzisha taratibu mpya za maendeleo ya watu, ingawa undani wa mabadiliko haya haujulikani. Hata hivyo, hasa katika Angola, idadi ya watu lazima ilishuka.

## *Kuelekea utaratibu mpya: 1641 - 1700*

Mwaka 1641, Waholanzi waliiteka Luanda na kutwaa sehemu kubwa ya Angola kabla ya kikosi kilichoandaliwa toka Brazil kuwatimua mwaka 1648. Tangu wakati huo na kuendelea, Wabrazil walitawala kikamilifu biashara ya Angola hadi 1730, na kwa kiasi fulani baadaye. Pia mwaka 1641, Garsia II alikuwa Mfalme wa Kongo, na kama Nzinga, alijenga urafiki na Waholanzi. Kurejeshwa kwa utawala wa Kireno kuliwakutanisha uso kwa uso na jeshi kuu la Kireno ambalo walipaswa kuafikiana nalo. Kasanje, iliyokuwa imeepukana na vita, ilitia sahihi mkataba wa urafiki na kuwa rafiki wa Ureno kwa zaidi ya karne moja. Kutoafikiana juu ya mkataba hatimaye kuliifanya Angola iivamie Kongo. Antonio I wa Kongo aliwakusanya malodi wake wote na kushindwa mwaka 1665 kwenye vita vya Mbwila. Alifariki vitani pamoja na mamwinyi wengi. Lakini jeshi la pili la Kireno liliangamizwa vibaya huko Soyo mwaka 1670 kiasi kwamba Angola iliacha majaribio yake ya kuiteka Kongo. Mwaka 1671, mabaki ya Ndongo yalitekwa, na kufikia 1680, amani ilikwishawekwa kwa lazima katika Matamba (Nzinga) na Kasanje, na miongoni mwa machifu wa upande wa kusini wa Kwanza ya Kati. Utekaji ulikuwa umekamilika.

Ufalme wa Kongo haukuinuka tena baada ya vita vya Mbwila. Mgogoro wa kuwania urithi wa ufalme uliishia katika vita vya wenyewe kwa wenyewe kati ya malodi, na kufanya Mbanza Kongo kuangamizwa mwaka 1666 na kuhamwa kabisa mwaka 1678. Kwa kuwa mji ulikuwa ndio egemeo la mfumo wa siasa, kila kitu kilivurugika. Hatimaye mfalme mmoja aliporudi Mbanza Kongo mwaka 1709, ufalme wake haukuwa zaidi ya mkusanyiko wa tawala za wanamfalme ambazo aghlabu zilikuwa bado zikisumbuliwa na vurugu za ndani baina ya wadai wa ufalme. Kila kitu kilikwisha sambaratika isipokuwa Soyo, na hata Soyo ilipata shida sana kubaki imeungana. Baada ya kuikimbia Mbanza Kongo malodi hawakuwa na budi kujizoeza maisha ya shamba na kugombea nafasi za uongozi huko. Idadi kubwa kiasi ya malodi walivuka mto upande wa kaskazini na kuanzisha temi ndogo ndogo katika Mayombe na kati ya mito ya Kongo na Niari.

Mageuzi yalikuwa kamili, na yalivunja misingi ya jamii yenyewe kiasi cha kusababisha kutokea kwa mitume wa kike. Mwaka 1704, Dona Beatrice Kimpa Vita

alianza kuhubiri Ukiristo mpya ulioitwa Uantonia. Aliwakana wamisionari na Wazungu, lakini zaidi ya yote aliwasihi wawaniaji wa kiti cha ufalme kuachana na mapambano, kurudisha mfalme na kuijaza watu tena Mbanza Kongo. Alikuwa na wafuasi wapenzi wengi, na alimshawishi mdai wa kiti cha ufalme kukaa katika Mbanza Kongo, ambako alimvisha taji jeusi la Antonia. Lakini mwaka 1706 alikamatwa na kuchomwa kama mwasi wa dini. Pedro II alirejesha ufalme na kufanya watu warudi Mbanza Kongo, lakini wimbi la miaka arobaini ya mabadiliko ya kisiasa halikuweza kurudishwa nyuma.

Nchini Kongo, mfumo wa uongozi wa eneo hilo pana ulitoweka. Kuanzia wakati huo kiunzi cha muundo cha eneo hili, kama kile cha Angola, kingekuwa cha kiuchumi, chenye mtandazo wa njia za biashara zilizounganishwa na vituo vya kupokea na kupakia bidhaa. Angola, ambayo kuelekea mwaka 1680 ilikuwa imepanuka, pia ilidhoofishwa. Magavana na *Camara* wa Luanda hawakuweza kudumisha ukuu wao juu ya ma-*quimbare* na ma-*ovimbali* (machotara wa Kiafrika-Kireno), au juu ya wafanyabiashara wa Kibrazil. Katika Luango, dola lilielekea kuwa bado imara, lakini mfalme alipokufa mwaka 1701, ilichukua zaidi ya mwaka mmoja kuchagua mfalme mpya. Licha ya heshima yake ya kidini, hadhi ya kifalme ilianza kufasiriwa upya kulingana na mamlaka ya mfalme juu ya biashara.

Pembezoni mwa eneo la biashara ya watumwa, madola yalijiimarisha kupitia biashara yenye kukua ambayo waliidhibiti, au angalau yalibakia imara kwa muda wote ambao yalidhibiti biashara hiyo. Kasanje ikawa dola lenye nguvu kwenye mto Kwango kwa sababu ilidhibiti mtiririko wa watumwa wenye kuongezeka muda wote baada ya 1648. Kaskazini, ufalme wa Tio ulisimama kidete, yaelekea bila mabadiliko yoyote makubwa.

Utamalaki wa Waholanzi na kurejeshwa kwa utawala wa Kireno kulikuwa na matokeo makubwa ya kiuchumi. Sarafu - viramba na *nzimbu* - ilishuka thamani. Katika Angola, biashara ya watumwa ilipangwa upya na Wabrazil, waliotoa mtaji, meli na bidhaa za Ulaya na kutenda mambo kwa masikilizano na waandazi wa misafara na washika watumwa wa Kiafrika-Kireno.

Katika Pwani ya Luango, Wafaransa na Waingereza, wakisukumwa na njaa isiyoshibishwa ya watumwa iliyojitokeza katika makoloni yao ya West Indies, waliingia katika mashindano makali na Waholanzi baada ya 1660-1665. Hapa makampuni yaliyogharimiwa Ulaya yaliendesha biashara ya pembe tatu. Hivyo ikaanza biashara ya watumwa kwa mapana iliyokuja kufikia upeo wa maendeleo yake katika karne ya kumi na nane.

## Mageuzi ya kijamii na ya kitamaduni: karne za kumi na sita na kumi na saba

Tunazo taarifa nzuri zaidi kuhusu Kongo. Mgawanyo wa jamii katika tabaka tatu za kijamii, *mwisikongo (malodi), babuta* (u. *mubuta)* (washamba) na *babika* (u. *mubika) (watumwa)* uliendelea hadi wakati fulani baina ya 1666 na 1678, mabadiliko

yakitokea kwanza miongoni mwa malodi na baadaye mashambani.

Istalahi *ekanda* (mzizi wake: *kanda*) leo ina maana ya "ukoo wa kukeni" au "nasaba ya kukeni." Wakati huo ilikuwa na maana ya "familia" - familia ya nasaba kukeni kwa hakika, lakini pia jamii yoyote. Watu wa kijiji waliunda *ekanda,* na jamii ya Kikristo halikadhalika. Kijiji kilidhaniwa kuwa ni mali ya ukoo fulani wa kukeni, uliotokana na mwasisi wake, na kuwakilishwa na kiongozi wa kijiji, *nkuluntu* (mzee). Kwa kweli, kwa kuwa wanawake walifuata waume zao, na watoto wao wa kiume kwa kawaida hawakuenda kuishi katika kijiji cha mjomba wao, kundi la kijiji liliunganishwa pamoja kieneo. Kijiji kilikuwa na haki za ardhi, na mzimu ulioishi ndani yake uliendelezwa na *kitomi* (mwinyi wa kale wa ardhi). Kiitikadi, haki hizi zilihodhiwa na ukoo wa kukeni wa muasisi, lakini kimatendo kijiji kilitenda kama asasi. Hili linaweza kuonekana hasa kwa kuwako kwa vyama kama *khimba, nzo longo* au *kimpasi*, vyote vikiwa ni asasi za jando kwa vijana wa kiume, au asasi za tiba ambazo zilitofautiana kati ya eneo moja na jingine.

Kadiri muda ulivyopita, nguvu za ukoo wa kimama na za kijiji zilipungua. Wanavijiji walikwisha nyonywa vibaya kufikia mwaka 1525. Inawezekana waliasi pamoja na Wajaga mwaka 1568, na maasi zaidi yalitokea wakati wa utawala wa Garsia II. Wakati huo *kimpasi,* madhehebu ambayo madhumuni yake yalikuwa kuondoa *mpasi* (mateso, umaskini, maafa au adha) ilijishughulisha sana wakati wa maonevu au maafa ya kawaida. Maisha ya wanavijiji yaliendelea kuwa ya wasiwasi, hasa malodi walivyozidi kuwaingilia na kudai vimada na kisha kuwatumia watoto wa kiume waliozaa nao kuchunga vijiji.

Nyumba za malodi, zikiiga mjengo wa ikulu, ziliongezeka ukubwa na umashuhuri. Ziliweka watumwa wengi kupindukia. Viongozi wake walikuwa na harimu za wake waliotokana na familia nyingine za malodi au za vijijini. Walilipa mahari kubwa kwa wake zao wakuu, hivyo wakajihakikishia miliki ya watoto wao baadaye. Mahari alipewa mke; kwa njia hii wake wa malodi walijiimarisha kiuchumi na kisiasa. Mwanamke mwandamizi wa nyumba kwa koo zote mbili alikuwa ndiye mfano wa kuiga. Hata hivyo hadhi ya wazawa wa kuumeni - wavulana - pia iliongezeka. Mali yenye kuhamishika iliyopatikana kwa biashara ilimilikiwa na wavulana, ambao, baada ya takriban 1550, hawakuchukua majina ya baba yao bali jina la ukoo la Kireno likiashiria nyumba yao. Urithi, hata hivyo, haukuwa mkubwa kama ambavyo ingetarajiwa, kwani kila kilichopatikana kutokana na wadhifa wa mtu katika huduma ya kiserikali kilimrudia mfalme baada ya mhusika kufariki au kufukuzwa kazi.

Baada ya 1666, nasaba tawala zilifanya mfululizo wa mabadiliko tofauti ya aina mbili. Katika Soyo nyumba ya watawala iliendelea kuchukua nasaba ya kuumeni, ikiwapuuza wapwa na kuwapendelea watoto wa kiume, hata wale waliozaliwa na wajakazi. Hatimaye, katika karne ya kumi na tisa, Soyo yote ilitwaa itikadi ya ubaba. Katika Kongo, nako, baada ya kupoteza mji wao, malodi ilibidi watengeneze makazi yao mapya mashambani. Nyumba kuu ziliyeyuka kama theluji juani, na

nafasi yao kutwaliwa na makundi makubwa au *mvila* (koo) za kimama mnamo 1700. Serikali ilikwisha gatuliwa na kupelekwa shamba.

Watumwa - awali mateka wa vita - hawakubakia kama kijitabaka cha pekee kwa muda mrefu. Kulijitokeza tofauti kati ya watumwa wanaouzika na watumwa wa nyumbani ambao walikuwa hawawezi kuuzwa tena. Wasiouzika walitumika kwenye nyumba za malodi, na baadhi ya makundi - mathalan watumwa wa mfalme na watumwa wa vituo vya misioni - yalianza kujitegemea na kuwa na nguvu ujanibuni, na kuendelea hivyo hadi karne ya kumi na tisa. Kwa kuwa watumwa wanaouzika walisafirishwa nje, hawakupata kuunda makundi yaliyoshikamana. Kadiri muda ulivyopita, vijitabaka vitatu vya jamii vikashindiliwa katika matabaka mawili - malodi na raia wao wenye kudhulumiwa

Katika Angola muundo wa kijamii wa wenyeji ulikuwa na matabaka ya kijamii sawa na ule wa Kongo, na kijitabaka cha Wareno kilikuwa juu. Lakini hali ilifanywa ngumu zaidi kwa kuzuka kijitabaka cha Wareno-Waafrika kutokana na machotara wafanya biashara, ambao kiutamaduni walikuwa Waangola au Wakongo, na pia walikuwa Wareno. Kundi hili la machotara lililotokana na maingiliano (ya Wareno) na malodi wa Kongo. Kwanza lilitokea katika São Tomé, halafu likahamia makao makuu ya Kongo na kisha Luanda. Hadi 1680 yalikuwapo makundi mawili makubwa, moja lilisakini kando kando ya ngome ya Ambaka, jingine lilianzisha mji wa Cacunda Velha. Katika karne ya kumi na nane, Waafrika-Wareno hawa walienea kwa mapana na marefu katika uwanda wa juu wa Benguela. Waliwakilisha jamii inayoelea ya wanamisafara na wafanya biashara, ambao walifanya kazi kwa ushirikiano na machifu wa Kiafrika na kuoa katika familia za malodi wenyeji.

Historia ya dini na itikadi imepambwa kwa nje na kuingia kwa Ukatoliki, ambao, katika Kongo, ulienea kwanza miongoni mwa malodi wa mjini na katika miji mikuu ya majiunbo. Utawala wa kanisa ulibakia zaidi mikononi mwa Wareno hadi 1645, wakati wamisionari wa Ki-Capuchini wa Kitalia walipoanza kampeni kabambe ya kuingiza watu katika Ukiristo na kuendelea hadi karibu mwaka 1700 katika Kongo. Katika Angola, Ukatoliki uliolazimishwa na watekaji haukuendelea nje ya koloni isipokuwa katika Matamba. Haukuenea katika Luango, licha ya kumgeuza mfalme mwaka 1663.

Maendeleo ya mawazo na matendo ya kidini katika Kongo yanaonyesha kuwa mafunzo ya Kikristo yaliathiri dini ya zamani na kuendana nayo. Istilahi ya Kikristo inatokana na kikoa cha *nkisi, ndoki* na *nganga; nkisi* ikiwa "hicho kilicho kitakatifu" au "neema." Wamisionari walipambana na ada za *kitomi* na uchawi, matambiko na vyama vya uganga, lakini walivumilia tiba iliyotolewa na *nganga*. Wa-Capuchini walitumia maandamo na sala kufuta ada za urutubisho, na walipunga pepo.

Kuanzia karne ya kumi na sita na kuendelea inaweza kudaiwa kuwa kulikuwa na dini moja ambamo, angalau miongoni mwa malodi, nduni za Ukiristo na za dini ya kijadi ziliungana. Msambao mkuu wa dini hii ulitokea katika karne ya kumi na saba. Garsia II alikuwa mtetezi wa vyote - Ukatoliki na *Kitomi*. Hata alipewa jina la utani

la "Mchawi." Dini hii mpya ilikuwa chanzo cha *voodoo* ya Haiti.

Matapo mengi ya kidini yamerekodiwa tangu miaka ya 1630, jaribio la kwanza la kuanzisha kanisa la kienyeji lilipofanywa. Mwaka 1704, Dona Beatrice alihubiri mabadiliko ya kina ambayo hayawezi kuelezwa kwa kuangalia hali ya kisiasa tu. Alidai kuwa alikuwa na mawasiliano ya moja kwa moja na mbinguni na alichukuliwa kama *munaki* (mtume). Alitoa hoja ya "Kuafrikisha" Ukristo barabara. Familia Takatifu ilikuwa ni ya weusi na ilizaliwa Mbanza Kongo, na ishara alizotumia zilikuwa za pepo wa kienyeji zilizohusishwa na maji, ardhi na uoto (mimea). Lakini alimtambua Papa, licha ya matamanio yake ya kuwatimua Wamisionari weupe ambao walioupotosha wahyi (ufunuo). Kwa muhtasari, maono yake yalikuwa sanisi zaidi kuliko dini iliyoabudiwa wakati wa uhai wake.

Imetolewa tetesi kuwa baada ya 1700 Kongo ilipoteza Ukatoliki wake. Huu ni uongo, lakini Wamisionari wa Kikristo wa mwisho wa karne ya kumi na tisa, waliosharabu mazingira ya kikoloni, walishindwa kutambua Ukatoliki wa kienyeji ambao ulikwisha kuwa sehemu changamani ya dini ya Kongo.

Sanaa huelezea utamaduni. Ingawa hakuna kinachodumu katika Kongo kwa upande wa sanaa tendwa, mfano muziki, ngoma na masimulizi, sanaa ya vitu vya kuona imedumu, pamoja na matini nyingi juu ya mada hiyo. Vifaa hivi vilivyosanifiwa kuashiria tofauti za kitabaka (sanaa ya mavazi kwa mfano), dhana za kisiasa (nembo na vifaa vya sherehe) na dhana za kidini (sanaa ya Kikristo, vifaa vilivyotumika kuagulia, masanamu ya wahenga na mizimu na barakoa au majuso) viliagizwa kutengenezwa na baraza, Kanisa Katoliki, viongozi wa vijiji na wa madhehebu ya vijiji na hata wakuu wa kaya.

Kinachovutia katika sanaa ya Kongo ni maendelezo ya vipengele vya mtindo, yanayochukuana na uhai wa fani hiyo inayosimilisha athari nyinginyingi za Ulaya. Mifano ni pamoja na nakshi za kijiometri zenye kupishana katika pembe kali kwenye nembo ya kifalme (pembe ya ndovu) tangu kabla ya 1533, nguo tangu mnamo 1650 hadi 1800 na kazi za vikapu, chanjo za mwili na mikeka kutoka karne ya kumi na tisa na hata karne ya ishirini. Athari ya Kizungu ilikuwa kubwa na ilionekana katika uingizaji wa usanifu mawe wa Kizungu (makanisa na makasri), alama za mamlaka (panga, mataji, bendera na mavazi rasmi) na, zaidi ya yote, vifaa vya kidini. Karibu tabia zote za sanaa ya Kongo, hasa ya michongo na ya michoro, zimenasibishwa na athari za Kikristo. Lakini ushahidi wa sanaa ya michoro ya kale - michoro juu ya miamba iliyobakia toka vipindi mbalimbali - umeendelea kutelekezwa. Katika karne ya kumi na saba, tunakuta sambamba na michoro mwigo msururu wa taswira ambazo dhahiri zimetokana na hati za maandishi na zinaelezea utamaduni wa watu wa kawaida. Matumizi haya ya maandishi ya michoro yaliendelea na kuchanganyika na utengenezaji wa nakshi za kijiometri. Sambamba na michoro hii, utaratibu tofauti wa sanaa za maumbo uliendelezwa: Shuhudia michongo simulizi na picha za ukutani za karne za kumi na nane na kumi na tisa.

Michongo inawakilishwa kwanza na vifaa vya Kikristo. Ina elementi za kanuni za

mlinganyo za Kizungu lakini mtindo ulioelemea uhalisia wa Kongo ulikuwepo tangu awali. Wasanii walitumia vifaa aina aina - shaba nyekundu, pembe za ndovu, mbao, mawe, vyombo vya ufinyanzi, nyuzi na vitambaa - na kuchora juu ya vitu anuwai, vikiwemo hata vyungu vya kupikia. Tarihi za kwanza zinatukuza ubora wa viramba vya Kongo, vilivyofumwa au kuwekewa mahameli. Hata mapadri walivitumia kushona mavazi ya makasisi kuchangia yale waliyoingiza kutoka ng'ambo, hususan Italia. Uchongaji wa sanaa za madhehebu zilizotumika katika dini za kale ulipigwa marufuku na sanaa ziliharibiwa katika nyakati mbalimbali, hasa chini ya Afonso I na Garsia II, na pia Kimpa Vita. Hata hivyo mahitaji ya vitu hivi yalirudiwa mara kwa mara.

Athari ya sanaa ya Kongo ilienea kaskazini na mashariki kipindi chote hiki. Kuenea kwa kile kinachoitwa barakoa nyeupe toka Gabon kunatokana na majuso ya Kongo ya kaskazini na kuliambatana na upanuzi wa Luango, hasa katika karne ya kumi na saba. Ufundi wa kutengeneza mahameli za kindu ulienea kufuatia njia ya Okango kuelekea mashariki na ndio uliotangulia "mahameli za Kasai" na hasa za Kuba.

## *Karne ya kumi na nane: Maeneo ya kaskazini*

Katika karne ya kumi na nane Afrika ya Kati yote ilipangwa upya. Mtandao wa biashara - siyo madola - ukawa jambo kuu. Tabaka la wafanya biashara lilichukua nafasi ya, au kuchangia, matabaka tawala ya kale. Kulikuwa na mitandao miwili ya biashara ya watumwa: mmoja, wa Wareno, uliendesha biashara kutoka Angola hadi Brazil, na mwingine, upande wa kaskazini, ulifungamana na mataifa mengine ya Ulaya; lakini biashara ya bara ilibakia kabisa mikononi mwa Waafrika.

Biashara hii katika eneo la kaskazini, eneo la pwani ya Luango, ilipaliliwa na makampuni yaliyogharimia biashara yote ya pembe tatu. Mashindano miongoni mwa makampuni mbalimbali ya Ulaya yalikuwa ni sababu kubwa zaidi ya kupanda kwa bei kuliko ongezeko la mahitaji ya watumwa katika West Indies na Amerika ya Kaskazini. Mahitaji ya watumwa yaliendelea kuongezeka tangu karibu 1665 hadi 1755, yakifikia upeo wake kati ya 1755 na takriban 1797, ambapo vita vikuu vya Ulaya vilisitisha biashara kwa muda.

Bandari zilizotumika kwanza zilikuwa Luango halafu Malemba, Kabinda na, baada ya 1800, Boma. Wafanyabiashara wa Kizungu walikodi mabohari bandarini, walikobadilishana bidhaa zao kwa watumwa kupitia mawakala walioitwa *mercadores*. Mawakala walikuwa watu wa lazima, kwani mifumo ya fedha ilitofautiana na hapakuwa na budi kuafikiana juu ya thamani za kubadilishania. Kwa madhumuni hayo, fungu la bidhaa - furushi - liliwekwa, kulingana na thamani ya kiasi cha watumwa. Furushi lilikuwa na vitu aina tatu: bunduki na baruti, nguo na bidhaa anuwai, hasa bidhaa za metali. Pamoja na bei za kununulia, mfanyabiashara wa Ulaya alipaswa kulipa ushuru wa biashara na kutoa zawadi kwa mfalme wa mahala hapo na kwa mwadhama mwenye kusimamia biashara ya Wazungu. Wakala, kwa

upande wake, alilipwa ada kubwa kutokana na bei ya kuuzia watumwa.

Karibu watumwa milioni moja na kiasi kidogo cha pembe, shaba na nta vilisafirishwa nje katika karne ya kumi na nane. Maduhuli yalikuwa zaidi ni nguo na silaha. Inakadiriwa kuwa bunduki 50,000 ziliingizwa kila mwaka katika nusu ya pili ya karne.

Misafara iliongozwa na waelekezaji ambao walikuwa mahiri katika kutafuta ruhusa za njia na walikuwa na ubingwa wa masoko makubwa ya bara. Wakati mwingine walisafiri masafa marefu sana, wakichukua si tu bidhaa za Ulaya bali pia chumvi, samaki wakavu waliotiwa chumvi na bidhaa zilizotengenezwa na wenyeji, hasa mapambo ya vito kutoka Luango. Njiani waliweza kununua bidhaa nyingine za wenyeji na kuziuza mahali pengine.

Njia kuu iliunganisha bandari na Bwawa la Malebo, ambapo watumwa waliosafirishwa kwa mto na vijito vyake waliwasili kwa idadi kubwa. Wabobangi waliacha uvuvi ili kushiriki katika biashara hii, na mtandao wa biashara yao ulitanda kutoka mto Ubangi hadi mto Kwa. Wasafirishaji hawa wa majini pia waliendesha biashara pana ya bidhaa nyingine - vyungu, samaki, mikeka, chakula, pombe, miti ya rangi nyekundu na bidhaa nyingine zilizonunuliwa mahali pamoja na kuuzwa mahali pengine; biashara hii ilihimiza sehemu mbalimbali kubobea katika biashara ya bidhaa fulani maalumu tu. Zoni ya biashara ya watumwa ilikwishafika Ubangi, Tshuapa ya chini na maeneo ya kando ya Ziwa Mayi Ndombe mapema kabla ya 1800, na kuendelea kupanuka kadiri mahitaji ya watumwa yalivyoongezeka. Njia nyingine za misafara ziliivuka Kongo, na kufikia Matamba na Kassange. Baada ya 1750, makao makuu ya dola jipya la Yaka kwenye Mto Kwango yakawa kituo kikuu cha biashara ya watumwa walimomiminika watumwa waliotekwa katika kampeni za kijeshi zisizokwisha zilizoendeshwa na Wayaka kuvuka mto Kwango.

Biashara ya watumwa ya kaskazini ilikuwa ya faida mno ikilinganishwa na ile ya Angola kiasi cha kuusogeza uwanja wa biashara wa Angola kuelekea Luanda na Kassange. Jambo hili lilisababisha Wareno kuchukua hatua za kijeshi dhidi ya bandari ya Mosul (baadaye Ambriz) na kutwaa Enkoje katikati ya Kongo mwaka 1759, na baadaye Kabinda, mwaka 1783. Wareno walitimuliwa na kikosi cha Wafaransa kikisaidiwa na majeshi ya wenyeji.

Athari za kidemografia za biashara ya watumwa hadi sasa hazijajulikana kwa yakini. Idadi ya watu ilishuka katika Kongo na Mayombe, ingawa hatujui kwa kiasi gani. Kwingineko, matokeo makuu yalikuwa kupunguza kasi ya ukuaji wa idadi ya watu.

Tunajua zaidi juu ya athari za uchumi. Upande wa kaskazini wa mto Kongo eneo kubwa lilijigawa katika mkusanyiko wa majimbo, kila moja na ubobezi wake: kindu, tumbaku, mvinyo wa miwa, pembe, vyakula, vifaa vya chuma, ufinyanzi, mashua na kadhalika. Hali hii ilididimiza maendeleo ya kiteknolojia katika kila jimbo, kadiri baadhi ya shughuli zilivyoachwa, lakini nguvu ya uchumi wa majimbo yote kwa pamoja iliongezeka bila kutetereka, kutokana zaidi na maendeleo ya usafiri wa majini.

Athari za kijamii na za kisiasa zilikuwa kubwa sana. Mawakala na waadhama waliosimamia biashara ya watumwa polepole waliendelea kupata umashuhuri katika baraza la Luango, Ngoyo na Kakongo, dhidi ya malodi wa zamani waliokuwa na uhusiano na ufalme. Mamlaka ya kifalme nayo pia yaliathirika vibaya. Katika Luango, baraza la mfalme lilishuhudia kubadilishwa kwa malodi wa majimbo wa nasaba ya kifalme na hawa malodi wapya, baada ya nyadhifa hizi kunadiwa na mfalme kwa wenye fedha zaidi. Mwaka 1750 au kabla, aila ya mfalme ilitoweka na makundi sita yakapigania kiti cha ufalme, lakini *kitomi* (baraza la kifalme) hatimaye kilifanikiwa kusimika mfalme asiyehusiana na kundi lolote, japo kwa gharama kubwa ya kudhoofisha mno madaraka yake. Zaidi ya hayo, majimbo ya mbali kama vile Mayumba yalianza kujitenga na Luango tangu 1750 na kuendelea.

Ufalme wa Tio nao ulikuwa mashakani. Malodi wakubwa wa eneo hilo walioendesha biashara yao wenyewe walitajirika na kuzua itikadi mpya iliyohalalisha kujitenga kwao. Itikadi hii ilikuwa ya kiroho, ikitegemea hirizi, *nkobi*, na iliweza kuachana na misaada ya mizimu ya nchi. Kuanzia karibu mwaka 1780 na kuendelea dola la Tio lilikuwa katika msukosuko wa vita vya wenyewe kwa wenyewe, na hali ya kawaida haikurejea hadi karibu na 1830.

Katika bonde la kati la Kongo, kupanuka kwa biashara ya watumwa kulisababisha miguro mipya ya watu wachache wachache pamoja na uhasama, katika eneo la Mayi Ndombe na kaskazini zaidi. Wakati huohuo, makazi makubwa ya watu yalianza kujitokeza karibu na mto, kwenye sehemu za vivuko. Vituo hivi vilikuwa miji ya masoko katika karne ya kumi na tisa.

Huko Kongo kwenyewe, itikadi ya Kikristo, na hususani ile ya "Tarika ya Yesu" ambayo watawala walikuwa wanachama wake, iliendelea kuwa msingi wa itikadi tawala. Kitovu cha itikadi hiyo kilikuwa ni mfalme mwenyewe, ambaye hakuwa zaidi ya *nkisi* mkuu, na vituo vya zamani vya misioni, vilivyoendeshwa na watumwa wa zamani wa misioni hizo. Vitengo vya kiutawala vya nchi vilivunjika mara kwa mara, wakati mwingine hata katika ngazi ya kijiji. Wakati huo huo, hata hivyo, *mvila* (koo) kubwa zilijitokeza, zenye mifumo ya kinasaba iliyokwisha simika mizizi yake nchini. Mtandao huu wa koo ukawa ndio kiungo kilichounganisha vijiji huru pamoja.

Mageuzi haya yaliambatana na mabadiliko muhimu ya kiutamaduni. Dhima ya wahenga wakuu, waliohusishwa na koo, iliongezeka. Maziara na makanisa, hasa yale ya Mbanza Kongo, yaliongezeka ukubwa. Dhana ya *zombi,* aina ya mtumwa-mfu, iliingia, halikadhalika tatizo la kuchanganya dhana za "watakatifu" na "wahenga wakuu." Baada ya karibu 1700 watu mashuhuri walianza kuzikwa kwa ufahari mwingi zaidi. Utaratibu wa kuvisha sanda maiti sasa ukabadilishwa na mtumba mkubwa wa kuzikia. Sanamu ya kichwa au busto (sanamu ya kichwa na kifua) iliyowekwa juu ya mtumba katika karne ya kumi na nane iligeuka kuwa sanamu ya mawe au ya ufinyanzi ya kupamba kaburi, ambapo idadi kubwa ya magae iliwekwa. Maeneo ya Boma na Mayombe ndiyo yalikuwa kitovu cha mabadiliko haya.

Madhehebu ya tiba-jumui yalitapakaa kila mahala. *Lemba*, iliyokuwa mfano wa kale wa *nkisi* hizi katika Luango, ilibadili hulka yake na kuwa *nkisi* ya kinga ya waali walioweza kulipia kiingilio cha juu. Mtu mashuhuri alipougua kasisi wa *lemba* alikuja kumtibu

Ukristo ulidumu lakini ulibadilika. Uhaba wa makasisi wa nje au wenyeji ulifidiwa na wasaidizi wa zamani wa wamisionari, na katika kitala, wapambe wa mfalme. Sanamu za Ambriz zinaonyesha mandhari za kusulubiwa ambamo mkuki umekuwa chatu, zikikumbusha Mbumba au Bomba, iliyohusishwa na biashara ya watumwa na utajiri; wakati huohuo mandhari hayo yameambatana na wapiga ngoma. Misalaba yenye sanamu ya Yesu ilibakizwa kama nembo za mamlaka na, katika muktadha wa dhima ya sheria, kama nembo za *nkangi* (mkombozi). Misalaba mingine ilizuka, kwa mfano *santu,* au hirizi zilizohusishwa na uaguzi kwa kuwinda, na ambazo zilitumiwa kugundua sababu ya maafa ya pamoja. Hizi zilikuwa pande mbili za dini rasmi ile ile.

## *Angola katika karne ya kumi na nane*

Biashara ya watumwa ya Angola iliendeshwa katika kiwango kikubwa mapema kabla ya kuanza kwa ile ya kaskazini. Mfumo huu, ambao hasa uliilenga Brazil, haukuwa umeunganika vizuri ukilinganishwa na ule wa kaskazini. Kabla ya 1730, mfumo huu ulikuwa na wahusika wafuatao: wasafirishaji katika Ureno; mawakala katika Brazil; wenye meli; wachuuza watumwa katika Luanda au Benguela; waendesha misafara wa Kiafrika-Kireno; na malodi na wafanyabiashara wa Kiafrika waliotoa watumwa wa kuuza sokoni. Kampuni moja ingeweza kufanya baadhi ya shughuli hizo, lakini ilikuwa ni mara chache sana kwa kampuni moja kuzifanya zote. Kila mmoja alijitahidi kuepuka hasara ili kupata faida kubwa iwezekanavyo. Hatari kubwa kabisa ilikuwa kwamba watumwa wangeweza kufa kwa lishe mbaya, magonjwa yasiyotibiwa na kutendewa vibaya. J.C. Miller anadondoa makadirio yaliyoonyesha kwamba nusu ya watumwa walionunuliwa walikufa baina ya soko la kununua na bandari ya kuondokea, na asilimia 40 nyingine katika Luanda wakingoja kuondoka. Hasara baharini ilitofautiana kufuatana na hali ya afya ya watumwa waliosafirishwa na kiasi cha msongamano melini. Ilikadiriwa kuwa asilimia kumi ya wale wote walioabiri meli walikufa baharini.

Furushi (la bidhaa), lililoitwa *hanzo* nchini Angola, lilitolewa kwa mkopo kwa mwendesha msafara, na hivyo kumfanya mdeni wa mdhamini wake. Furushi lilikuwa na nguo kutoka Goa au Ulaya, brandi kutoka Brazil, chumvi ya kienyeji, shanga na wakati mwingine silaha chache. Gharama za waendesha misafara zilikuwa kubwa, kama shughuli yenyewe, ilivyokuwa hatari, na hawakuchelewa kuingia madeni na kuwategemea kabisa kabisa wakopeshaji wao. Lakini kuanzia takriban 1760 na kuendelea wenye misafara walianza kuuza watumwa wao kwa mfanyabiashara yeyote katika Luanda au Benguela katika jitihada ya kurekebisha hali hiyo. Mbia-mkopeshaji aliachiwa karatasi isiyokuwa na thamani.

Baada ya 1730 makampuni ya Ureno yalirudi tena Luanda kuuza bidhaa za Ulaya, na wafanya biashara wa Brazil wakahamia Benguela. Meli pia zilileta idadi kubwa ya wahamiaji fukara, wahalifu na majasuri wenye kutaka kutajirika kwa biashara ya watumwa, hasa kama waendesha misafara. Mapambano yasiyokoma yalianza baina ya *quimbares* na wageni wapya.

Wageni, wakiwa ni wafanyabiashara, waliungwa mkono kabisa na mamlaka ya juu ya Luanda, lakini *quimbares* waliungwa mkono na viongozi wa majimbo na, kwa jumla, na machifu wa Kiafrika katika masoko ya bara. Wabrazil na *quimbares* hawakufanikiwa tu kujizatiti katika nafasi zao huko Benguela bali pia waliongeza mahuruji yao ya watumwa. Lakini makampuni ya Wareno, kutokana na mitaji yao na msaada wa kiutawala walioupata, yalifanikiwa kuhamisha "hasara ya watumwa" ambayo wangeweza kuipata: badala ya kununua watumwa, walinunua pembe za ndovu au hati za malipo ambayo wangeyapokea Brazil. Mwishoni mwa karne, magavana waliwaunga mkono Wabrazil. Baadaye, walielekea kupendelea makampuni makubwa ya Lisbon. Wayesuti, marafiki wa Wabrazil, walifukuzwa mwaka wa 1660. Fransisco Innocencio de Sousa Coutinho (1664-72) alifanya jitihada kali kurejesha udhibiti wa Ureno ndani ya Angola, lakini si yeye wala viongozi waliomfuata waliofanikiwa katika hili. Waafrika-Wareno walihama mara nyingine tena, wakielekea hasa uwanda wa juu wa Benguela ambako penyezi jipya la biashara na bara lilifunguliwa. Watumwa walipelekwa Benguela kuepuka Luanda. Lakini Luanda iliendelea kuvutia biashara ya watumwa kupitia ufalme wa Kasanje. Misafara iliandama njia iliyotoka Kassange hadi Mussumba, makao makuu ya himaya ya Walunda.

Himaya ya Walunda ilitengenea katika karne ya kumi na nane. Kampeni za kudumu za kijeshi zilizaa idadi kubwa ya watumwa, ambapo ushuru kwa njia ya watumwa ulimiminika makao makuu kutoka mikoa ya himaya. Baada ya 1750, himaya ilifanikiwa kuanzisha ufalme wa Kazembe kwenye mto Luapula na kuanzisha mawasiliano na Tete na Zumbo katika Msumbiji. Kabla ya hapo upanuzi kuelekea magharibi ulikwishafikia Mto Kwango. Ufalme wa Yaka, ulioanzishwa baina ya 1740 na 1760, ulitamalaki sehemu kubwa ya bonde la Kwango upande wa chini wa Kasanje na kupanua utamalaki wake kuelekea mashariki upande wa Kwilu. Idadi kubwa ya mateka ililetwa kutoka huko na kuuzwa kwa Wazombo, Wasoso na Wavili, lakini pia kwa Waimbangala na kwa misafara iliyopita Nkonje.

Katika Angola, biashara ya watumwa ilikuwa na nguvu kiasi kwamba, licha ya juhudi za De Sousa Coutinho na wengine, nchi ilishindwa kuanzisha uchumi anuwai. Koloni liliendelea kutegemea Brazil kiuchumi: Mnamo 1800, asilimia 88 ya mapato yake bado ilitokana na biashara ya watumwa na Brazil, na kiasi kidogo, chini ya silimia 5, kilitokana na pembe za ndovu zilizopelekwa Ureno.

# 20 Mfumo wa kisiasa wa Waluba na Walunda: kuibuka na kupanuka kwake


Historia ya Waluba ni hadithi ya maendeleo ya mfumo wa kisiasa ambao kwanza uliibuka huko Shaba, katika Jamuhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, na kisha kuenea katika sehemu kubwa ya uwanda wa nyasi wa kusini, eneo linaloanzia karibu na Mto Kwango na kuenea hadi Mto Zambezi.

Mahusiano na tofauti baina ya madola ya Waluba na Walunda zinajitokeza katika majina yao mawili ambayo hayaakisi sana tofauti za kimbari kama yanavyoakisi mifumo ya kisiasa na kitamaduni ambamo ndani yake vipengele vingi vilivyorejelea mbari vilizuka. Historia ya Waluba inahusu mambo yanayoathiri Waluba wa sasa wa Shaba na wa Kasai, na vilevile mambo yanayowahusu Wasongye, Wakanyok, Wakete, Wasala Mpasu, Wabinji na Walulua. Historia ya Walunda inashughulikia makundi ya Warund (Walunda katika fahiwa finyu) na Walozi, Wandembo, Walwena, Waimbangala na makundi mengine (yaani Walunda katika fahiwa pana). Uainishaji wa kiisimu uliofanywa kwenye lugha za Kiluba na Kilunda unaashiria mahusiano haya yaliyoingiliana.

Kuna kukubaliana kwa jumla kwamba magunduzi ya kiakiolojia katika Bonde la Upemba huko Sanga na kwingineko yanapaswa kuhusishwa na wahenga wa Waluba. Nembo za utawala, ambazo baadaye zilikuwa za kawaida miongoni mwa Waluba, zinajitokeza kabla ya karne ya kumi na tatu, pamoja na ushahidi, huko Katota na Sanga, wa kuundwa kwa temi mbili. Hata hivyo, Katota na Sanga hazikuwa chimbuko la moja kwa moja la ufalme wa Waluba. Tunachojua tu ni kwamba ufalme wa Waluba uliibuka na kuanza kupanuka kabla ya kuundwa kwa dola la Warund, ambalo ndilo asili ya Walunda. Mapokeo simulizi yanataja dola la Warund kuanzia mwaka 1680 lakini hayatuwezeshi kukadiria tarehe ya kuanzishwa kwake.

## Kuibuka kwa Madola ya Waluba na Walunda

Shaba na sehemu jirani za Zambia na Angola zimefunikwa na misitu, udongo hauna rutuba na kipindi cha ukame ni kirefu sana. Ardhi nzuri hasa ipo katika mabonde ya mito na ardhi mbaya kabisa iko mashariki mwa Angola. Lakini eneo la kusini ambalo




**20.1** *Nchi za Shaba kabla ya 1700*

ni nusu kame, hususani kusini mashariki, lina hazina ya madini kama shaba, chuma na chumvi.

Kwa hiyo, haishangazi kuona kwamba watu waliishi katika maeneo madogo ya ardhi yenye rutuba, hali kukiwa na maeneo makubwa yasiyokaliwa baina yake ambayo yalitumika zaidi kwa kuwindia. Msambao huu wa watu unasaidia kuelezea mpangilio wa maeneo ya kiutawala ya kale kabisa, ambayo yalikuwa ni temi, kila utemi ukilingana na sehemu moja ya makazi. Hivyo msururu wa makazi ya Wasanga ukawa uchifu wa baadaye wa Wakikonja, na Katoka, iliyokuwa sehemu ya juu ya mto, upande mwingine wa mfumo wa ziwa Lualaba, nayo iliunda utemi mwingine. Watu wa maeneo haya mawili walikuwa wavuvi na wakulima. Kulikuwa na temi nyingine nyingi, zote zikiwa katika mabonde makubwa ya mito.

Maeneo haya ya mikusanyiko ya watu yaliunganishwa kwa biashara na pengine kwa ndoa. Kaskazini kulitoka ukindu na mawese, huko Lualaba kulitoka samaki, kusini kulitoka shaba nyekundu na chumvi, na eneo la katikati kulitoka mafuta ya *mbafu*. Biashara ilikuwa muhimu kiasi cha kusababisha kuanzishwa kwa sarafu tangu walau mwaka 1000 na kuendelea. Katika Bonde la Upemba mnamo mwaka 1300,

msalaba wa Shaba ulifanywa kuwa sarafu. Baada ya mwaka 1700 misalaba ilipotea; kufikia karne ya kumi na tisa, shanga zilizoagizwa kutoka nje zilianza kuwa sarafu mpya.

Katika muktadha huu kuliibuka itikadi ya kisiasa ambayo baadaye ilitokea kuwa msingi wa ufalme wa Waluba. Hii ilikuwa na kanuni mbili zilizofungamana, yaani ile ya hulka ya kiwakfu ya ufalme (*bulopwe*) na ile ya utawala kupitia ushirika wa siri.

Kulingana na baadhi ya mapokeo, ufalme uliotangulia ufalme wa Waluba ni ufalme mdogo wa Wakalundwe. Makao yake makuu yalikuwa huko Chifinda. Mmoja wa wafalme wake aliyejulikana kwa jina la Kongolo (Upinde wa Mvua) alihama kwenda kuanzisha makao makuu katika tambarare huko Mwibele, ambapo palikuwa si mbali kutoka Ziwa Boya na ambapo ndipo palitokea kuwa katikati ya dola la baadaye la Waluba. Hata hivyo, maelezo mengine yanaonyesha kuwa Kongolo alikuja kutokea kwingine. Masimulizi ya utendi kuhusu uanzishwaji wake yanaeleza jinsi Kongolo alivyoshindwa na kuchinjwa na Kalala Ilunga (Ilunga mwindaji), mgeni kutoka mashariki aliyehamisha makao makuu kwenda Munza. Kongolo pengine si mtu halisi, lakini Kalala, kama *mwine Munza* (mwinyi wa Munza), anawakilisha mzee-muasisi anayesawiri sifa bora ambazo mfalme wa Waluba anapaswa kuwa nao. Ufalme wa Waluba ulitawala, pengine toka mwanzo, Wakalundwe upande wa Magharibi na Wakikonja upande wa kusini na ulidhibiti njia kuu za biashara za kaskazini-kusini. Hata hivyo, hadi kuingia kwa karne ya kumi na nane uliendelea kuwa ufalme mdogo kiasi.

Wakati huohuo, huko magharibi zaidi tawala nyingine za kisiasa zilikuwa zikiundwa. Utawala wa kwanza kabisa miongoni mwao ni ule wa Nkalany, ulioundwa huko katika bonde la Mbuji Mayi kutokana na kuunganika kwa maeneo madogo kadha yaliyoongozwa na *tubung* (mamwinyi wa ardhi). Kwa hakika hakuna chochote kilichoashiria kuwa nchi za Warund zingekuwa himaya. Lakini katika hatua fulani *tubung* za kaskazini ziliungana chini ya nchi mojawapo ya Kirund. Mapokezi ya *tubung* za kaskazini yanaeleza ni kwa nini chifu wa Wankund alimkabidhi utawala binti yake aliyeitwa Rweej au Rueji, ambaye aliolewa na Chibinda Ilunga, mwindaji kutoka kitala cha Waluba, na kisha kumwachia utemi.

Kulingana na Carvalho Dias, baada ya hatua ya kutekwa kwa nchi, mamlaka yalikwenda kwa mtoto wa kwanza wa Rueji aliyeitwa Yav, ambaye alipata cheo cha *mwant Yav* (Mwinyi Yav). Hata hivyo, maelezo mbalimbali yaliyokusanywa hivi karibuni yanadai kwamba Rueji alikuwa tasa. Ili kutohatarisha urithi, alimpa mumewe mke wa pili, aliyeitwa Kamonga, ambaye ndiye aliyezaa warithi wa mfalme. Hali hii inaelezea kuwepo katika mfumo wa utawala wa kifalme wa *mwant yav* kwa wanawake wawili wenye heshima: yaani *swan murund* au *swana mulunda*, mama wa kiishara wa jamii aliyeashiria kuendelezwa kwa dhima ya Rueji, na *rukonkesh* au *lukonkeshia*, mama malkia aliyeshika dhima ya Kamonga.

Ushahidi huu unaelezea asasi tofauti zilizoibuka baada ya kujitokeza kwa mwindaji wa Kiluba. Kwanza makundi tawala mawili ya kike, moja likiashiria uzazi



**20.2** *Hemba, Zaire: kigoda ambacho chini yake kimelika: Ingalia nutai iliychongwa na uzuri wa bangili:*



**20.3** *Luba, Kusini mwa Zaire: Kishikio cha fimbo ya sherehe maalumu, ikiwa na umbo la kichwa cha binadamu kilichopambwa na kofia ndefu sana yenye picha za watu wawili juu walioshikana viuno. Urefu: cm 165*

wa kijamii na jingine uzazi wa kibiolojia; na pili, cheo cha kifalme kilichokitwa katika cheo cha kichifu cha *mwant*, ambacho kiliongezewa jina la mfalme wa kwanza.

## *Waluba: muundo wa ndani na maendeleo hadi mwaka 1800*


Wakati wa utawala wa *Mwine Munza* Kalala, dola lilijitokeza katika sehemu za tambarare likijumuisha ufalme wa Wakikonja kwa upande wa kusini na ufalme wa Kalundwe kwa upande wa magharibi. Lilipanuka zaidi kuelekea kusini mashariki hadi kufikia sehemu za chini za mto Luvua.

Uanzishwaji na uimarishwaji wa mwanzo wa ufalme ulisababisha vurugu fulani katika eneo hilo, na idadi fulani ya wahamaji waliondoka kutoka sehemu za chini za Luvua na kuanzisha dola la Washila katika ufuko wa magharibi wa Ziwa Mweru na katika Luapula ya chini. Uhamaji muhimu kabisa ulikuwa ni ule wa kuelekea kaskazini. Makundi ya Waluba wa Kasai yaliondoka Shaba na kuenea kuelekea kaskazini kufuata mto Lubilash ambako yalikuta nchi zenye maji ya kutosha. Njaa ndiyo inaelezwa kuwa sababu kuu ya miguro katika mapokeo ya makundi mengi yanayohusiana ya huko Kasai.

Ingawa kwa upande wa kusini, katika nchi ya Washila na Wakanyok, kulianzishwa muundo wa kisiasa wenye kufananafanana na ule wa Waluba wa Shaba, kitu kama hicho hakikutokea huko Kasai. Hapa muundo wa kisiasa ama ulikomea tu katika kijiji na ardhi yake, au cheo cha juu kilitolewa kwa maisha yote au kwa muda maalumu kwa mgombea aliyeongoza, mfumo ambao unapatikana pia miongoni mwa baadhi ya Wasongye. Waluba wa Kasai pia walianza kutumia nembo na baadhi ya mazoea ya kisiasa kutoka kwa Wakanyok. Hata hivyo, Wasongye wengi walitawaliwa kwa namna tofauti. Kufikia miaka ya 1880 na pengine kwa karne chache kabla, Wasongye walikuwa wakiishi katika makazi makubwa ya kilimo ambayo takribani yalikuwa miji, yaliyotawaliwa na vyama vya Wabakishi na kudhibitiwa na machifu na waadhama wachache wenye vyeo vya juu.

Muundo wa dola la Waluba ulifanana na piramidi la mapiramidi. Katika ngazi ya kijiji, kaya ziliunganishwa kwa kufuata ukoo wa kuumeni. Uhusiano baina ya vijiji pia ulichukuliwa kama uhusiano baina ya koo, ingawa kila kijiji kilikuwa na chifu mwenye cheo. Juu ya ngazi hii, ufalme wenyewe ulitawaliwa kutoka makao makuu ambayo mpangilio wake uliakisi muundo huu, makao makuu ya kifalme yakiwa katikati na makazi ya maafisa wenye vyeo wa jinsi zote, yakiwa yametengwa kulingana na kazi zao za kijeshi au za kiraia. Chama cha siri kilichojulikana kama *bambudye* kilimsaidia mfalme kutawala. Mfalme hakupaswa kuwa na nasaba au ukoo ingawa cheo hicho kwa kawaida kilirithishwa kutoka kwa baba kwenda kwa kaka yake au mwanaye. Mfalme pia alikuwa hahusishwi na mivutano ya kisiasa, japo alihusiana kidugu na viongozi wengi wa wilaya. Alikuwa kweye kilele cha piramidi ya mapiramdi ya kiukoo. Cheo cha *mulopwe* kinaashiria hali ya kutogawanyika kwa mamlaka ambayo yalikuwa si ya kushirikisha watu wengine.

*Mulopwe* alizungukwa na wanakaya yake na maafisa wenye vyeo. Kwanza kabisa




20.4 *Falme ya Luba kwenye karne ya kumi na nane na kumi na tisa*

ilikuwepo harimu wake, ikiakisi muungano halisi wa kisiasa ulioungunisha ufalme pamoja. Maafisa wake walihakikisha kwamba ushuru ulilipwa kwa njia ya *mingilu* (kazi isiyolipiwa), kwa *milambu* (kodi inayolipwa kwa chakula au kwa mazao ya mahali hapo) na kwa zawadi zinazotolewa wakati wa usimikaji wa waheshimiwa. Utawala wa nchi ulikuwa mikononi mwa *bilolo* (umoja: *kilolo*) ambao kila mmoja alisimamia mkoa. Utawala mkuu ulisimamia ukusanyaji wa ushuru, uliandaa jeshi na kumshauri mfalme kupitia kwa *tshidie* (baraza la jumla) na kwa *tshilanga* (baraza la mfalme).

Hatujui hasahasa jinsi chama cha *bambudye* kilivyofanya kazi kwa kuwa siri zake hazijawahi kufichuliwa. Lakini kilikuwa na nyumba nyingi za kupanga na kilikuwa na udhibiti wa kidini na wa kilimwengu juu ya nchi na hata juu ya mfalme.

Mabaraza ya watawala wa kijanibu yaliundwa kufuata mfano wa makao makuu, na machifu wa mabaraza hayo walikuwa na vikorokoro vitakatifu na mahusiano na madhehebu ya mizimu ya mahali hapo, aghalabu kwa ajili ya wahenga wao. Mamlaka ya mabavu ya wapiganaji wa mfalme ndiyo nguvu halisi iliyochunga umoja wa nchi. Lakini hakukuwa na jeshi la kudumu, hivyo nguvu ya kiitikadi iliyotokana na *bambudye* ilikuwa na umuhimu mkubwa. Ushuru mkubwa ulikuwa unaweza kushurutishwa tu pale wilaya kuu zilipokubali kumsaidia mfalme dhidi ya maadui wa ndani na nje. Kwa hiyo, haikuwa ajabu kwamba ufalme haukupanuka kwa haraka.

Kuna taarifa kidogo sana kuhusu historia ya nchi hadi yapata mwaka 1700, wakati wa utawala wa mfalme Kadilo. Mfalme huyu alianzisha mashambulio ambayo hayakufaulu huko kaskazini dhidi ya miji jirani ya Wasongye, lakini upanuzi halisi wa ufalme ulitokea katika bonde la Lualaba kufuata moto Luvua (Kiambi) na kusini mwa Bonde la Upemba. Upanuzi huo uliteterekea wakati ulipotokea mgogoro mkubwa wa urithi wa ufalme kuanzia mwaka 1780 hadi mwaka 1810. Wakati wa mgogoro huo, Wakanyok walijikomboa kutoka utawala wa Waluba na athari ya kisiasa na kiutamaduni ya Wasongye ilifikia upeo wa juu. Baadaye upanuzi uliendelea kuelekea mashariki kwa kuteka nchi zilizokuwa kati ya Mto Lualaba na Ziwa Tanganyika, na kuelekea kaskazini kufuata mto Lualaba hadi kufika Buli.

## *Walunda: muundo wa ndani na maendeleo hadi mwaka 1800*

Ufalme wa Warund uligeuka kuwa himaya ya Walunda katika karne ya kumi na nane. Muundo wake wa awali haujulikani kikamilifu isipokuwa tu kwamba hali yake ya kijeshi ilikuwa imeendelea kuliko ile ya ufalme wa Waluba. Hata hivyo, habari kidogo tu hujulikana kuhusu kanuni za miundo (yake) ya kijamii na ya kisiasa.

Urithishaji wa *tubung* ulikuwa wa kukeni, lakini urithishaji wa cheo cha kifalme na katika baraza la kifalme ulikuwa na kuwili: Msuko wa msingi wa kijamii ulikitwa katika urithishaji wa vyeo na udugu wa kudumu. Hii ilikuwa na maana kwamba kila aliyekuwa kwenye nafasi au cheo alipaswa kuchukua nafsi ya mtangulizi wake. Mwenye kushika nafasi fulani alichukua jina la aliyemtangulia, na wake, watoto na jamaa zake wengine. Matokeo yake yakawa ni udugu wa kudumu. Ikiwa, mathalani, aliyeshika cheo kwa mara ya kwanza alikuwa mjukuu wa mfalme, basi kwa vizazi vitano vilivyofuata yule aliyeshika cheo hicho alikuwa bado ni mjukuu wa mfalme.

Kwa hiyo ilikuwa inawezekana kulifikiria dola kama shirika linaloendeshwa na familia moja, likiongozwa na *mwant yav* (maliki). Machifu wapya wangeweza kujumuishwa kwa kupewa mahusiano ya kidugu (kama vile kuwa mkwe, baada ya muungano wa ndoa) na vilevile kupewa nafasi nzuri katika himaya. Muundo wa himaya katika mfano wa kifamilia ulidhibiti mahusiano baina ya maafisa yaliyokitwa katika dhana kali ya vizazi.

Hivyo, kwa Warund, dola lilikuwa familia pana—pana sana, kwa hakika, kwani himaya hatimaye ilienea kutoka Mto Kwango hadi kuvuka Mto Luapula. Lakini ilikuwa familia ya wapiganaji, na familia ambayo baadaye ingesitawi kwa kutegemea utumwa. Kufikia karibu mwaka 1700, wapiganaji wa Lunda waliwashinda nguvu watu walioishi pembezoni mwa himaya, wakawajumuisha na kisha wakasonga mbele. Kutoka mwaka 1750 hadi mwaka 1760, falme ndogondogo zenye nguvu ziliibuka kutoka nchi ya Wayaka katika mto Kwango hadi Kazembe katika mto Luapula kufuata mhimili wa mashariki-magharibi uliojumuisha rasilimali ya madini ya eneo la Shaba na njia ya kwenda kwenye himaya ya Wareno katika Mto Zambezi, na vilevile njia za biashara kutoka nchi ya Warund hadi nchi ya Waimbangala kwenye mto Kwango.

Utawala wa kifalme ulikuwa umepwaya. Himaya ilikuwa ni ufalme wa kiini na falme nyingine za pembezoni ambazo watawala wake walilipa tu ushuru kwa mfalme. Mfalme alikuwa ameweka maafisa maalum waliozurura nchini wakiwa na kikosi cha jeshi ili kushurutisha *bilolo* kulipa ushuru. Mbali na vikosi hivi, kulikuwako na jeshi kubwa lililoongozwa na *kazembe* (amirijeshi). *Kazembe* alikuwa na mamlaka yote katika eneo lake, lakini mara eneo lake lilipojumuishwa, ama alipoteza hadhi yake au aliamua kuwa mtawala wa kujitegemea, yaani *kilolo* wa maliki.

Makao makuu yalipangiliwa kama kambi ya jeshi, kukiwa na upande wa mbele na kikosi cha mbele, mirengu na katikati. Kitovu chake kilikuwa ni jumba la mfalme, ambako maliki (*swan murund), rukonkesh* na waheshimiwa wengine waliishi. Mamlaka yote alikabidhiwa maliki, cheo chake *mvant yav* (bwana wa kipiribao), kilidokeza umbali uliopo baina ya mfalme na binadamu wengine, lakini pia utata wake, kwa kuwa alikuwa akitetea amani na vita, ufanisi na uharibifu.

Utafiti wa karibuni umeonyesha kuwa upanuzi wa himaya ya Walunda ulianza kabla ya mwaka 1700. Utamalaki ulikuwa ukielekea kusini-mashariki, kwenye mashimo ya chumvi ya mto Lualaba, karibu na mji wa sasa wa Kolwezi. Kutoka pale mnamo karibu mwaka 1700, kikundi kilichojitenga kilikwenda kusini katika Zambia ya leo na kikaunda dola katika eneo la Nembu baada ya kuwasimilisha kiasi fulani wenyeji Wambwela na kuwasukuma wengine kuelekea kusini.

Kutoka kwenye mashimo ya chumvi ya mto Lualaba, maamirijeshi wa Kilunda walijongea kuelekea mashariki katika mashambulizi mapya na kufika katika bonde lenye rutuba la Luapula. Jeshi la Walunda lilishinda mashambulizi ya Waluba dhidi yao na kuwatiisha machifu wa Shaba na dola la Washila huko Luapula. Dola lilikua, na kufikia nusu ya pili ya karne ya kumi na nane, Kazembe wa Lulapula alikuwa mkuu wa ufalme mkubwa ulioshikamana vizuri. Punde tu baada ya kuweka makazi, Walunda wa Kazembe waliwasiliana na Wareno wa Sena na Tete. Ujumbe ulioongozwa na F. de Lacerda e Almeida ulitembelea ufalme mpya mwaka 1798 hadi 1799. Ujumbe huo ulivutiwa na uwezo wa kijeshi wa Kazembe na hatua kali zilizochukuliwa dhidi ya wakazi. Ugeni huu wa Wareno ulizindua kipindi cha mahusiano mazito ya kibiashara kati ya Kazembe na Zambezi ya chini. Hali hii iliimarisha uhuru wa Kazembe kutoka makao makuu kiasi cha kuyageuza malipo ya ushuru ya miaka ya 1790 kuwa mabadilishano sawa ya zawadi kufikia miaka ya 1830.

Kuelekea kaskazini na magharibi, upanuzi mwingine wa Walunda ulikuwa ukihusiana kwa karibu na maendeleo ya biashara ya watumwa huko Angola. Muwasala na mfumo wa biashara ya watumwa wa Angola ulianza kabla ya mwaka 1670, na baadaye kukua. Waimbangala waliendeleza mfumo wa kufanya biashara kwa misafara ambayo ilileta bidhaa za Kizungu kama vile nguo, shanga na vyombo vya nyumbani, katika makao makuu ya Walunda, ambako zilikuwa bidhaa za anasa kwa watawala. Walunda hawakukubali kupokea bunduki, wakipendelea zaidi kubakia waaminifu kwa upanga wao uliojulikana kama *mpok*. Kwa kubadilishana na bidhaa hizo, walisafirisha nje watumwa ambao mwanzoni walitekwa kutoka maeneo ya

kaskazini na mashariki mwa kitovu cha Warund. Baadaye, mateka wa Kimbwela kutoka kaskazini mwa Zambia na mashariki mwa Angola waliongezwa katika orodha ya kusafirishwa nje. Wakati huohuo mahitaji ya watumwa yalikua ndani ya himaya ya Walunda yenyewe. Walitumiwa kulima mashamba makubwa ya mihogo, na walifanya kazi pia kama wavushaji na wachukuzi katika misafara.

Muda mfupi baada ya mwaka 1700, tabaro za kijeshi zilielekezwa magharibi, na kufikia karibu mwaka 1750 machifu wa Kilunda walikuwa wamefika kwenye mto Kwango. Mashariki mwa Angola, katika nchi ya Walwena, palikuwa lengo lao la kwanza. Viongozi wa Walunda walijifanya watawala juu ya jamii kubwa kiasi zenye mifumo mikongwe ya urithishaji wa kukeni. Magharibi mwa nchi ya Walwena temi mbalimbali ziliundwa pia na Walunda kwa kujitawaza kwa nguvu juu ya jamii zilizokuwepo. Miongoni mwa jamii hizi, Wachokwe ndio baadaye walitokea kuwa muhimu sana. Hata katika karne ya kumi na nane, walikuwa na thamani kwa himaya kama wafua vyuma, wachongaji na wawindaji.

Katika bonde la Kwango, wavamizi wa Kilunda waliwakuta Wayaka, Wasuku na pengine, huko Okango, tawala nyingine za machifu zilizoundwa katika ruwaza ya Kikongo. Waliwateka watu hawa. Wakazi wengi walikimbia, lakini miundo haikuharibiwa. Matokeo yake, mfumo changamani uliibuka ambamo hata itikadi ya dola ilikiri kuwepo kwa wenyeji na wavamizi wa Kilunda. Lakini kiongozi wa Wayaka, aliyejulikikana kama *kiamfu*, hakuweza kuwadhibiti watu wake wote. Huko kaskazini, dola lenye uhuru kiasi liliibuka; wakati huohuo, kundi lililoitwa Wasonde-Waluwa lilihamia mashariki mwa Kwango ya kati na kuanzisha temi zao.

Mara tu walipoanzisha ufalme wao, wafalme wa Wayaka walianza kushambulia nchi zilizoelekea upande wa Kwilu ili kukusanya watumwa wa kuuza kwa wafanyabiashara wa Angola, Kongo na Vili. Hii ilichochea machafuko makubwa katika eneo hili. Ufalme wa Wasuku ulifaulu kuzuia mashambulizi haya, lakini kwingineko watu walikimbia kuelekea kaskazini mashariki na kusababisha misongamano mikubwa ya watu.

Tabaro ya mwisho ilifanywa magharibi mwa mto Kasai kuelekea kaskazini, pengine kufuata bonde la Tshikapa. Walunda waliunda madola mawili madogo: moja kwenye maporomoko makuu ya Kasai likiwa na makao makuu yake huko Mai Munene, ambalo punde tu lilitokea kuwa soko kubwa kwa misafara kutoka Mto Kwango; na jingine, lililoitwa Mwaka Kumbana, kwenye Mto Lwange. Katika sehemu hizi mbili Walunda walichanganyika na wahamiaji wengine wa karibuni waliojulikana kama Wapende. Mifumo ya kisiasa iliyotokea ilikuwa na athari za Wapende.

# *Hitimisho*

Kufikia mwaka 1800 upanuzi wa Waluba na Walunda ulikuwa umeweka miundo yake katika maeneo yote ya mbuga ya Afrika ya kati mashariki mwa Mto Kwango. Watu

wa eneo hili walikuwa na utamaduni unaofanana, matambiko yanayofanana na nembo na alama zinazofanana. Kuenea kwa utamaduni huu kuliwezeshwa na kuwepo kwa njia za biashara au hata mashambulizi. Mjongeo wa watu, hasa kupitia miungano ya ndoa, ulikuwa mkubwa ajabu, kama inavyothibitishwa na kuenea kwa majina ya ukoo yaliyorithishwa kupitia kwa mama. Majina hayo hayo yanapatikana kutoka mito ya Kwango hadi Kasai, na kutoka Kasai hadi Luapula.


Hata hivyo upanuzi wa Walunda pia ulisababisha uharibifu mkubwa. Hulka ya kijeshi ya madola ya Walunda isipuuzwe, wala ukubwa wa mashambulizi yao ya kuteka watumwa na matokeo yake kwa idadi ya watu. Jambo hili, na kuwepo kwa utamaduni wa kisiasa unaofanana kutoka Kwango hadi Luapula, bado ndio mambo yanayounda urithi wa karne hizo kwa wakazi wa eneo hili kubwa.

# 21

# *Zambezia ya kaskazini — Eneo la Ziwa Malawi*

Eneo linalojadiliwa hapa linapakana kwa upande wa kusini na mto Zambezi, mito Songwe na Ruvuma kwa upande wa kaskazini, kwa upande wa magharibi linapakana na Luangwa na upande wa mashariki linapakana na Bahari ya Hindi. Sehemu ya kusini ya eneo hili ilitawaliwa na wazungumzaji wa Kichewa na matawi yao. Magharibi mwa Wachewa kulikuwa na Wansenga, na mashariki kulikuwa na wazungumzaji wa Kilolo-Kimakua-Kilomwe na Wayao. Ukanda wa kaskazini ulienea upande wa magharibi mwa Ziwa Malawi kutoka ukanda wa pembezoni mwa Wachewa-Watumbuka huko kusini hadi kwenye mto Songwe huko kaskazini. Lugha za makundi matatu zinazungumzwa katika ukanda huo: Kitumbuka, Kingonde-Kinyakyusa na Kisukwa-Kilambya-Kinyiha. Kwenye mwaka wa 1500 watu wote wa ukanda wa kusini na Watumbuka wa kaskazini walikuwa kwenye kundi lililofuata nasaba ya kukeni la wazungumzaji wa Kibantu cha Kati ambacho kilienea kutoka Kongo ya kusini kwa upande wa magharibi hadi Bahari ya Hindi huko mashariki. Katika karne zilizofuatia, Watumbuka walibadilika na kufuata nasaba ya kuumeni. Wakati wote Wangonde-Wanyakyusa na Wasukwa-Walambya-Wanyiha tayari walikuwa wakifuata nasaba ya kuumeni tangu mwanzoni mwa mapokeo ya kihistoria. Eneo hilo sasa linajumuisha Zambia ya mashariki, Malawi nzima na Msumbiji ya kaskazini.

Katika kipindi kinachojadiliwa, ukanda wa kusini katika karne ya kumi na tano ulitawaliwa na kuwasili kwa Wamaravi na kuibuka kwa madola yao ambayo yaliendelea kupanuka katika karne za kumi na sita na kumi na saba. Huko kaskazini, katika karne ya kumi na sita, watu walikuwa wamejiunga katika vikundi vya koo zilizojitawala. Hata hivyo, baadaye katika karne hiyo kikundi cha wahamiaji - Wangulube - kilianzisha madola ya Lumbya, Ngonde, Chifungwe, Sukwa na idadi kadhaa ya temi za Kinyakyusa. Katika kipindi hicho hicho, upanuzi wa Wamaravi katika ukanda wa pembezoni wa Watumbaka-Wachewa ulisababisha kuanzishwa kwa temi mpya za Wachewa ambazo ziliweka utawala wao juu ya jamii za Kitumbuka, na hivyo kuanzisha kabila la Watonga na lugha yao. Katika kanda zote mbili biashara ya pembe za ndovu ndiyo iliyoshamiri katika karne ya kumi na nane. Wakati huo, ukanda wa kusini ulibainishwa na kuporomoka kwa mfumo wa dola wa Wamaravi,




21.1 *Iamii za Zambezia ya kaskazini katika karne ya kumi na nane.* (*Chanzo: Kutoka A.D. Roberts,* Historia ya Wabemba kabla ya 1900, *London, Longman, 1973, uk.xxv. Ramani ilinukuliwa na kurekebisiwa kwa kibali cha Longman Group UK Ltd)*

kuibuka kwa madola yaliyolirithi dola hilo, na kusambaa nje kwa Wayao, mwanzoni wakiwa wafanyabishara na hatimaye wakiwa waanzilishi wa dola. Kikundi cha wahamiaji kutoka nchi ya Unyamwezi - Wabalowoka - walilowea miongoni mwa Watumbuka na kuanzisha twaa za kiuchumi ambazo hatimaye ziliibuka kama tawala za kisiasa. Hata hivyo dola zilizokuwa zimeanzishwa mapema huko kusini mwa mto Songwe zilijitenga na maendeleo haya mapya ya kibiashara hadi hapo baadaye kabisa katika karne ya kumi na tisa.

Kabla ya karne ya kumi na sita eneo hili lilishuhudia mfululizo wa uhamiaji wa Enzi ya Mawe, ukiwemo ule ulioleta wahenga wa kwanza wa wakazi wenye kuzungumza Kibantu cha kisasa. Yaelekea hawa wahamiaji wapya waliwasili kutoka kaskazini baada ya mwaka 1200 na kuwaondoa au kuwasimilisha Wabantu na wenyeji wakulima na wasasi-wahemeaji waliokuwepo tayari kwenye eneo hilo.

Huko Malawi ya kaskazini, wahenga wa wakazi wa sasa wenye kuzungumza lugha za Kibantu walikuwa ni watu wasiokuwa na dola wala nasaba-tawala. Huko Zambia ya mashariki, mashariki mwa mto Luangwa, wenyeji wa kwanza kati ya wazungumzaji wa sasa wa lugha za Kibantu, wanasadikiwa kuwa walikuwa Wakatanga. Huko Mashariki zaidi, Malawi ya kati, wazungumzaji wa awali wa Kibantu walijumuisha koo kadhaa ambazo zimepewa jina la "Wa-Mame-Chewa" (Wachewa wa asili). Katika mapokeo simulizi wakati mwingine hawa "Wa-Mame-Chewa" walijulikana kama *Wakalimanjira* (watengenezaji-njia), ambao waliisafisha nchi kwa kuiondoshea wenyeji wake wa asili waliokuwa wahamahamaji - yaani Watwa na Wakafula.

Tunajua kidogo sana kuhusu jamii za awali zilizounda kundi la Walolo-Wamakua-Walomwe na jumuiya za Kiyao huko Msumbiji ya mashariki. Hakuna mapokeo yenye kuonyesha jinsi walivyokuja kukalia makazi yao ya sasa. Labda hii ni kwa kuwa walikalia nchi yao tangu karne nyingi zilizopita, na hivyo wamepoteza kabisa kumbukumbu ya chanzo chao halisi.

Katika ukanda wa kaskazini, wakazi wa kwanza kati ya jamii za kisasa zenye kuzungumza Kibantu ambao rekodi zao zipo, waliselelea kwenye eneo la katikati ya Songwe na Rukuru ya kusini. Mapokeo yao yanadai kuwa waliwasili kutoka upande wa kaskazini-mashariki mwa Ziwa Malawi na huenda walikuwa na uhusiano na *abilema*. Muda mfupi baadaye, vikundi vingine vya wahamiaji vyenye nguvu zaidi vilianza kujipenyeza kwenye eneo hilo. Vikundi hivi vinajumuisha Wasimbowe, ambao walikalia uwanda wa Karonga, na Wambale, ambao walivamia eneo la Phoka. Huenda kuhamia kwa Wambale katika nyanda za juu za Phoka kulitokea katika karne ya kumi na nne. Hawa wahamiaji wapya walifahamika kwa ufuaji vyuma na walianzisha kwa urahisi mahusiano mazuri na wenyeji asili ambao ni Wamzembe na Wachiluba, ambao waliwapatia mazao ya kilimo na mkaa na badala yake kupokea zana za kilimo pamoja na silaha. Kwa hiyo yaonekana kwamba kulikuwepo na uhamaji wa jumla wa watu kuelekea kusini kwa kutumia ushoroba kati ya Ziwa Tanganyika na Ziwa Malawi kama njia yao kuu.


Baina ya maeneo ya Waphoka na Wachewa huko kaskazini na kusini kwa mpangilio huo, ziliishi koo kadhaa zilizozungumza Kitumbuka. Vikundi kadhaa kati ya hivi huenda vilisambaa sana mashariki hadi pwani ya ziwa na hata magharibi zaidi kufikia bonde la mto Luangwa katika wilaya ya sasa ya Lundazi huko Zambia. Wansenga, wenyeji wa siku hizi wa mkoa huu, wanazungumza lugha inayofanana na Kitumbuka na wanatumia majina yale yale ya kiukoo kama wenyeji wa nchi ya Watumbuka.

Kwa hiyo, kabla ya mwaka 1500, muundo wa kisiasa wa eneo zima kuanzia mto Songwe huko kaskazini hadi mto Zambezi huko kusini, isipokuwa kwa sehemu chache chache, ulibainishwa kwa kutapakaa kwa nchi ndogondogo zisizokuwa na mfumo wa kidola. Vikundi mbalimbali vya kimbari viliunda temi za kieneo. Mtemi wa eneo alitawala kikundi cha vijiji vya kiukoo vilivyohusiana kwa karibu sana kinasaba, ambapo ukoo wa mtemi huyo ndio uliokuwa na ukuu kinasaba. Mtemi alizipatia jumuiya za vijiji vilivyomzunguka huduma za kidini, za kimahakama na za kijeshi, na kwa upande wao wote walitakiwa kuonyesha utii.

Ijapokuwa kisiasa na kimaumbile eneo la Ziwa Malawi liligawanyika katika twaa za kikabila na kiukoo, lakini lilikuwa na kiwango fulani cha mshikamano wa kidini na wa kijamii. Kwenye ngazi ya kijanibu, dini ilichukua jukumu la kuhakikisha kuwapo kwa ustawi wa umma mzima kwenye masuala ya maadili na mali; ambapo kwenye ngazi ya nchi dini ilikuza ushirikiano wa kiutamaduni na wa kiekolojia. Kwa watu wengi matendo ya kidini yalihusisha kuheshimu wahenga, kupagawa na mizimu, kutengeneza mvua na kudhibiti uchawi. Alama kuu ya tajriba ya kidini katika eneo fulani ilikuwa madhehebu ya kuleta mvua, yaliyowekwa wakfu kwa mungu au mzimu uliotambuliwa katika eneo kubwa.

Imedhihirishwa kwamba angalau ndani ya ukanda unaofuata nasaba ya kukeni kuanzia eneo la pembezoni la Watumbuka-Wachewa huko kaskazini hadi kwenye bonde la Zambezi huko kusini, kulikuwa na mwingiliano wa kutosha miongoni mwa madhehebu mbalimbali ya kidini yaliyotambulika kinchi. Mungu aliwakilishwa kwa namna moja katika eneo lote hilo. Kwa mfano miongoni mwa Watumbuka na Wachewa mungu alichukua umbile la nyoka, alisadikiwa kuwa "nguvu ya kiume," huku akiwa na wake kadhaa wa kimzimu waliojitoa kwa huduma zake. Watendaji waliojitoa kwa mungu walikuwa wamepagawa na kutengwa kwa ajili ya jukumu lao maalumu. Kwa hali hiyo dini ilitoa njia muhimu ya mawasiliano miongoni mwa watu ambapo vinginevyo walikuwa wametengana kisiasa.

Miongoni mwa Wachewa na watu wa ukanda wa kusini waliohusiana nao, ule muundo hafifu wa kisiasa uliokuwepo kabla ya mwaka 1500 ulibadilika kwa kiasi kikubwa kutokana na kuibuka kwa mfumo wa dola wa Wamaravi mwanzoni mwa karne ya kumi na sita, na upanuzi wake uliofuata. Hivyo Wamaravi walitawala historia ya kisiasa ya karne ya kumi na sita na ya kumi na saba katika ukanda wa Zambezia ya kaskazini kama wajenzi wa dola la Mutapa walivyotawala ukanda wa Zambezia ya kusini katika karne ya kumi na tano na ya kumi na sita.




21.2 *Mbari za kipindi cha kabla ya kuanzishwa kwa tawala za kitemi kaskazini mwa Zimbabwe (K.W. Phiri na O.J.M Kalinga)*

Kwa kawaida sasa inakubalika kwamba Wamaravi walikuwa wahamiaji waliotoka eneo la Luba kusini-mashariki mwa Kongo, na kwamba waliingia Malawi ya kati kutokea magharibi. Walipofika kusini na mwishoni mwa Ziwa Malawi mara moja walijijenga kama watawala juu ya Wachewa-asili waliokuwa wakazi wa awali wa eneo hilo, wakaimarisha utawala wao, na kisha wakaanza kampeni ya upanuzi wa nchi uliowafikisha maeneo ya mbali kupita Malawi ya kati na ya kusini. Ilipofikia mwanzoni mwa karne ya kumi na saba muungano wa madola yao ulihusisha sehemu kubwa ya Zambia ya mashariki, Malawi ya kati na ya kusini na Msumbiji ya kaskazini. Kwa njia hii mfumo wa dola wa Wamaravi ulikuja kuwa na athari za kisiasa, kiuchumi na kijeshi katika eneo kubwa.

Hata hivyo mchakato uliopelekea kuibuka kwa mfumo wa dola wa Wamaravi bado haueleweki waziwazi kwa wanahistoria. Wanahistoria wengine wanashikilia kwamba Wamaravi waliingia nchini wakiwa wamesheheni kikamilifu alama za mamlaka ya utemi, ambazo ziliwasaidia katika kujijenga kama tabaka la watawala juu ya umma wa wazawa ambao bila shaka hawakuwa na dola. Wengine wanasisitiza umuhimu wa mambo ya kidemografia na kutoa hoja ya kwamba ongezeko la watu linalojihusisha na uzalishaji wa ziada, japo wa wastani, bado lingeweza kuwa msingi wa kutosha kuleta limbikizo la mamlaka ya kinasaba. Nadharia tete nyingine inahusisha suala la kibiashara, kwa kudai kwamba kuundwa kwa dola kwenye ncha ya kusini ya Ziwa Malawi katika karne za kumi na tano na kumi na sita kumezuka kutokana na haja ya kuwepo kwa mamlaka ya kudhibiti maendeleo ya biashara ya pembe za ndovu kati ya pwani ya kusini ya ziwa, na pwani ya mashariki ya Afrika, kupitia mfumo wa maji wa Shire-Zambezi.

Mapokeo simulizi yamerekodi kidogo sana kuhusu historia ya awali ya eneo hilo ama hata jinsi dola ya Wamaravi ilivyoanzishwa. Yanashikilia tu kwamba chini ya uongozi wa *kalonga* (cheo cha mtawala) Chidzonzi, ambaye ndiye aliyekuwa akiongoza nasaba kuu zaidi ya kifalme miongoni mwa Waphiri, Wamaravi walianzisha miliki yao ya kwanza kuzunguka Mankhamba na Manthimba upande wa kusini-magharibi ya Ziwa Malawi. Kwa mujibu wa nyaraka za Wareno, ilipofikia 1624 Manthimba ilikuwa kituo muhimu cha kibiashara, na wakazi wake walikuwa wakifanya biashara na wafanyabiashara wa Kirèno kutoka Tete kwenye mto Zambezi.

Hata hivyo mapokeo simulizi ndiyo pekee yanayoonyesha utaratibu wa kiasasi ambao ulishikilia pamoja dola la *kalonga*. Moja kati ya asasi hizi ni madhehebu ya *mlira*. Mara moja kwa mwaka viongozi wa nasaba mbalimbali za kifalme za Kiphiri walikaribishwa Manthamba kwa ajili ya kufanya tambiko kwa heshima ya Mlira, mzimu wa *kalonga* mkuu Chinkhole, aliyewaongoza wahenga wao kuja nchini humo wakati wa uhamiaji wao. Tunaamini kuwa mviga huu ulikuwa dhihirisho la wazi la madhehebu ya kifalme ambayo yalikuwa na dhima muhimu ya kuwaunganisha watu katika dola la Wamaravi. Jambo jingine lililokuwa muhimu sawa na hili katika kuunganisha miliki hiyo ni jinsi nyadhifa za kuteuliwa zilivyogawiwa. Inasemekana kwamba *kalonga* aliwateua viongozi kadhaa wa mbari za Wachewa-asili na kuwapatia madaraka makubwa katika dola lake. Wabanda walikuwa waangalizi wa madhabahu ya *kalonga* huko Mankhamba, na Wamwale waliongoza wapiganaji wa *kalonga*. Mapokeo yanaonyesha dhahiri ni kwa kiasi gani watu wasiokuwa Waphiri ama Wamaravi walihusishwa katika kufanya maamuzi yaliyohusiana na umiliki wa ardhi, ugawanyaji wa mali na uanzishwaji wa vita.

Kiwango cha uwezo wa *kalonga* binafsi kuendesha mambo ya ufalme wake huenda kilianza kupungua karibu na robo ya mwisho ya karne ya kumi na sita wakati dola lilipoanza kupanuka. Viongozi wa nasaba ndogo za Kiphiri walihama ukanda wa Manthamba-Mankhamba na kwenda kukalia nchi za jirani. Zikichukuliwa kwa pamoja, nchi zilizotawaliwa na *kalonga* na watemi hawa wasaidizi ndizo zilizounda kitovu cha mfumo wa dola la Wamaravi kama ulivyojitokeza katika karne ya kumi na saba.

Namua nyingine ya upanuzi wa Wamaravi ilihusisha uhamaji wa ndugu wakubwa wa karibu wa *kalonga* kwenda nchi za mbali kusini na kusini-magharibi mwa makao makuu. Huenda huu ulikuwa mpango wa makusudi wa ma-*kalonga* wa awali wa kuwaondoa watu ambao wangeweza kudai ufalme wa Manthimba. Kaphwiti na Lundu walihamia kwenye bonde la Shire chini na kulifanya koloni lao. Mwanzoni Kaphwiti alitawala bonde zima kabla ya kupoteza mamlaka yake mengi kwa *Lundu,* ambaye, baada ya kujiimarisha kwenye bonde la Shira chini, aliongoza upanuzi wa Wamaravi kuelekea nchi ya Walolo na Wamakua. Mchakato wa upanuzi wa Wamaravi katika eneo hili la Zambezia ya kaskazini ulianza katikati ya karne ya kumi na sita.

Uvamizi na ushindi wa Wamaravi dhidi ya nchi ya Walolo-Wamakua kwanza ulisaidiwa na ushabiki wa kupindukia wa mashujaa wa *lundu* ambao wanahistoria

wengine wa Afrika ya Mashariki wamewahusisha na Wazimba waliokuwa wanyang'anyi wakuu wa karne ya kumi na sita ambao *lundu* aliwaajiri. Ushindi wa uvamizi huu pia ulitokana na jamii za Walolo na Wamakua kutokuwa na dola. Mfumo wa kisiasa wa Walolo ulikuwa umechanguka; shughuli za kiserikali zilifanywa na majumbe wakisaidiwa na baraza la wazee. Wamakua nao walikuwa na mfumo wa kiserikali uliogatuka, lakini mara nyingine miongoni mwao, wakati wa matatizo, nasaba za ukoo mmoja ziliungana chini ya uongozi wa nasaba yenye nguvu zaidi. Hivyo, kutokana na shinikizo kutoka kwa Wareno, kulizuka temi zenye nguvu miongoni mwa Wamakua wa pwani mwishoni mwa karne ya kumi na sita.

Walolo na Wamakua walioshindwa na majeshi ya *lundu* walishirikishwa kwenye dola lililolipizwa kodi ambalo Wareno waliolowea Zambezi chini walilipatia jina la "Bororo." Matokeo yake yalikuwa kwamba ilipofika mwanzoni mwa karne ya kumi na saba, *lundu* alitawala eneo pana kaskazini mwa Zambezi, kutoka Shire chini huko magharibi hadi kufika karibu sana na Bahari ya Hindi kwa upande wa mashariki. Sio tu kwamba *lundu* alitambulika kama "mtu wa pili mwenye nguvu zaidi katika miliki ya Maravi (wa kwanza ni Kalonga)" bali kila baada ya kipindi fulani mashujaa wake waliingia eneo la pwani la Wamakua na kufanya uporaji kwenye makazi ya Wareno.

*Lundu* alishikilia pamoja miliki yake pana kwa msaada wa majenerali waaminifu wa kijeshi na vibaraka waliochukuliwa kutoka kwenye nasaba ndogo ndogo katika ukoo wake. Zaidi ya hayo, dola lake lilikuwa na msingi fulani wa kiuchumi kwa kuwa mbari tofauti zilizohusishwa katika dola hilo zilitegemea chumvi, chuma na nguo za pamba za *machila*, vitu ambavyo vilizalishwa na raia wa *lundu* wa Kimanganja walioishi kwenye bonde la Shire chini. Jambo jingine lililounganisha dola hilo ni dini ya Wamanganja. Teolojia ya dini hiyo iliyojikita kwenye madhehebu ya Mbona, ambayo madhabahu yake yalikuwa huko Khulubvi katika bonde la Shire chini, ilihusisha vipengele vingi vya upinzani wa makabwela dhidi ya matumizi mabaya ya mamlaka na hakipekee za kifalme. Matokeo yake ni kwamba madhehebu rasmi ya utemi mkuu wa *lundu* yalipata wafuasi wengi kwenye eneo pana, lililoanzia kwenye makao ya *lundu* katika bonde la Shire chini hadi kwenye delta ya Zambezi katika pwani ya mashariki.

Heshima kubwa aliyoipata *lundu* katika sehemu za mashariki ya muungano wa Wamaravi haikuepuka upinzani. *Kalonga* mwenyewe, aliyetawala eneo pana la nchi upande wa magharibi na mashariki mwa Ziwa Malawi na pia kandoni mwa Shire ya juu, alikuwa na wasiwasi mkubwa juu ya ongezeko la nguvu za *lundu*. Hivyo katika miaka ya 1620 na 1630 upanuzi wa Maravi kuelekea mashariki ulizorota kutokana na mvutano wa ndani kati ya *kalonga* na *lundu*. Baada ya hapo, upanuzi wa Maravi ulihama kutoka mashariki na kuelekezwa kusini-magharibi. Huko *undi* alianzisha miliki yake ambayo baadaye aliipanua.

Kulingana na tabdili mojawapo ya mapokeo yanayohusiana na kuanzishwa kwa miliki ya *undi,* mwasisi wake alitumwa na *kalonga* kwenda kukalia nyanda za kichanga karibu na nchi ya Wansenga. Hata hivyo tabdili nyingine inayoaminika

zaidi inadokeza kwamba kuondoka kwa *undi* kwenda kusini-magharibi kulisababishwa na mgogoro wa ndani ya ukoo-tawala wa Waphiri huko Manthimba.

Huko magharibi, *undi* na wafuasi wake walifanikiwa kulichukua eneo la mto Kapoche, uliokuwa kijito cha mto Zambezi. Kuanzia hapo walipanua mipaka ya ufalme wao unaoinukia kuelekea kwenye ndagano ya mito Zambezi na Luangwa. Kwenye eneo hilo wapiganaji wa *undi* walipambana na Watawara kandokando ya Zambezi na Wansenga kwenye ufukwe wa mashariki wa Luangwa chini. Lakini wanahistoria wanatofautiana kuhusu kiwango cha utawala wa Wamaravi juu ya Wansenga. Hata hivyo, kinachoweza kuhitimishwa kutokana na majadiliano haya ni kwamba katika awamu za upanuzi wake, dola la *undi* lilijumuisha temi kadhaa za Wansenga, lakini si zote. Kwa mfano, Wansenga wa kusini-magharibi karibu na Feira huko Zambia hawana mapokeo ya kwamba waliwahi kuwa sehemu ya "himaya" ya *undi*.

Bado lipo swali la jinsi *undi* alivyofanikiwa kuwa na kiwango fulani cha udhibiti wa kisiasa juu ya Wansenga. Hoja ya kimapokeo ni kwamba *undi* na wafuasi wake walitumia nguvu na kuanzisha uhusiano wa kudumu wa kindugu uliowafanya watemi wa Wansenga walioshindwa kutambuliwa kama "wana" au "mabinamu" wa watemi wa Wamaravi. Hata hivyo, siku za karibuni hoja nzito zaidi imezuka: Hoja hiyo ni kwamba huenda biashara na njaa vilichangia sana katika upanuzi wa athari za *undi* kwa jamii za jirani. Temi za Wansenga kandokando ya bonde la Luangwa zilipata mateso makubwa kutokana na njaa kali, na mara nyingi wenyeji wake walitafuta misaada kutoka nchi za *undi* ambazo zilikuwa na rutuba kuliko nchi zao. *Undi* pia alikuwa na ushawishi mkubwa na wafanyabiashara wa Kireno huko Tete, na jambo hili lilimwezesha kuwadhibiti wafanyabiashara wa jumuiya za jirani. Pia zipo dalili nyingi zenye kuonyesha kwamba *undi* na ndugu zake waliwaruhusu watemi wa Kinsenga walioingia kwenye twaa yao kuendelea kuendesha mambo yaliyohusu koo na maeneo yao ilimradi walilipa kodi yao ya pembe na watumwa kwenye makao makuu ya *undi*.

Wamaravi na Wachewa pia walipanuka kuelekea kaskazini na kuingia nchi ya Watumbuka. Miongoni mwa viongozi kutoka ukoo wa kifalme wenye asili ya Kimaravi waliohamia upande huo ni Chulu, Kaluluma, Kanyenda na Kabunduli.

Chulu na Kaluluma walihamia kwenye eneo la kusini ya Tumbuka lililojulikana kama Chimaliro pamoja na nyanda zilizolizunguka. Hapa waliwakuta Watumbuka, ambao walikuwa wanajitosheleza kiuchumi lakini wakiwa na mipangilio dhaifu kisiasa. Njia walizotumia Chulu na Kaluluma katika kuchukua madaraka ni suala lenye tafsiri zinazopingana katika mapokeo simulizi ya Wachewa na yale ya Watumbuka. Hata hivyo, inaonekana kana kwamba baada ya kipindi cha kuishi pamoja kwa amani, Watumbuka walijaribu kufanya upinzani lakini wakadhibitiwa kwa nguvu za kijeshi.

Kanyenda na Kabunduli walihamia eneo ambalo lilikuja kujulikana kama nchi ya Watonga. Kwa asili wote wawili walitoka kwenye kitovu cha himaya ya Wamaravi,

na kuhamia kwao kaskazini kuliwafikisha Khota Khota, mahali ambapo Kabunduli alitengana na Kanyenda na kuelekea kaskazini zaidi na kuingia nchi ya Watonga. Huko Kabunduli alijipatia sifa kubwa kwa kuviunganisha upya vikundi vya Watonga vilivyokuwa vimesambaratika ambavyo yaelekea kuwa alivishinda na kuviingiza chini ya udhibiti wake. Jinsi sifa zake zilivyoongezeka, ndivyo alivyozidi kufuatwa na familia kadha za watu wa kawaida kutoka ndani kabisa ya Uchewa.

Kuchanganyika huku kwa Wamaravi na wakazi wa asili wa nchi ya Watonga ndiko kunakoelezea upekee wa jamii ya Watonga kama tunavyoifahamu hii leo. *Chitonga*, lugha ya eneo hilo, ni kiungo kati ya Kitumbuka na lugha nyingine za Kichewa. Watonga pia ni kundi pekee kaskazini mwa Malawi lenye kuhesabu nasaba kukeni na kufuata desturi za urithi wa kukeni hadi leo hii.

Kwa jamii za Kichewa-Kimaravi, karne ya kumi na saba ilikuwa "enzi ya dhahabu," ambapo, kutokana na upanuzi wao wa nchi, waliibuka kama watu wenye nguvu zaidi kaskazini mwa Zambezi. Hata Wareno, waliokuwa wametulia kwenye makazi yao kandokando ya Zambezi, walilazimika kushirikiana nao. Hii ni kwa sababu Wamaravi hawakujifungia tu kwenye eneo la kaskazini mwa Zambezi. Kuanzia miaka ya 1590 hadi kwenye miaka ya 1630 waliingilia kwa vitendo katika eneo lililokuwa "twaa ya Wareno" kusini mwa Zambezi. Kwa vizazi viwili mwanzoni mwa karne ya kumi na saba, Wareno, kutoka Angoche kwenye pwani ya mashariki hadi Tete kwenye mto Zambezi, walitafuta namna ya kuwadhibiti Wamaravi kwa kushirikiana nao. Waliandikisha idadi kubwa ya Wamaravi kuwa askari katika jeshi lao ili kuwasaidia kwenye kampeni zao dhidi ya Wakaranga au Washona kusini mwa Zambezi, pia dhidi ya maadui wao walioishi karibu na makazi yao huko Zambezi.

Upanuzi wa Wamaravi ulikuwa na athari kadhaa. Kwa mfano, kuundwa kwa dola la *lundu* mashariki mwa bonde la Shire chini kuliwezesha madhehebu ya Mbona miongoni mwa Wamanganja kueneza athari zake kwa mapana zaidi. Labda athari za kiuchumi na za kiutamaduni zilikuwa na umuhimu pia. Katika eneo la muungano wa Wamaravi katika karne ya kumi na saba, biashara ya pembe ilishamiri. Matokeo yake ni kwamba Zambezia ya kaskazini ilikuwa na mwingiliano mkubwa na uchumi wa biashara ya kibepari. "Himaya" ya Wamaravi pia huenda ilijenga utamaduni wa namna moja miongoni mwa watu wanaofuata nasaba ya kukeni katika ukanda huo, maana wanatumia majina yaleyale ya kiukoo, na wana mfumo mmoja wa unasaba.

Wakati Wamaravi walikuwa wakipanuka kuelekea ukanda wa kusini katika karne za kumi na sita na kumi na saba, Wangulube, wahamiaji kutoka kaskazini-mashariki, walikuwa wakipenya na kuingia upande wa kaskazini. Hili ni tukio muhimu katika historia ya ukanda huu.

Kiongozi wa uhamiaji wa Wangulube, *mwaulambya*, alivuka mto Songwe kusini mwa vilima vya Misuku na kuingia sehemu iliyokuja kujulikana kama Ulambya. Hapo alianzisha koo za Wasikwese na Wachilima. *Mwaulambya* huyo alihakikisha kuwepo kwa udhibiti wa kisiasa kwa njia za amani zaidi kuliko *kyungu,* aliyevamia uwanda wa Karonga muda mfupi baadaye. Sababu mojawapo ya tofauti hizi ni

kwamba *mwaulambya* alikuwa na wafuasi wachache zaidi kuliko *kyungu*. Viongozi muhimu wa *mwaulambya* walitokana na familia za wenyeji, ambazo zilishirikishwa katika hadhi na nguvu za kisiasa za watawala hawa wapya. Vivyo hivyo, Wamsukwa walijitwalia madaraka ya kisiasa juu ya koo za Wasimwayi na Wasilumbu bila kutumia nguvu nyingi. Ulambya na Misuku ni tawala zilizoanzishwa kwa maelewano.

*Kyungu* Kameme na kundi lake walihamia kwenye uwanda wa Karonga kupitia Unyiha, Uiwa, Unamwanga na kisha Ulambya na Misuku huko magharibi. Kipindi kifupi baada ya kuwasili Karonga, Kameme alirejea na kufanya maskani yake upande wa magharibi karibu kabisa na Ulambya. Hapa alianzisha mamlaka ya kisiasa juu ya watu waliokuwa hasa na asili ya Kinyiha, ijapokuwa katika miaka ya baadaye Wamambwe na Wanamwanga wengi walihamia kwenye utemi wa Kameme. Haieleweki ni vipi Kameme alianzisha dola lake. Ni wazi dola lake lilikuwa dogo kuliko lile la kaka yake, *kyungu*, ambaye alianzisha ufalme wake kwenye dola ambalo tayari lilikuwepo, likitawaliwa na ukoo wa Wasimbowe.

Ukoo wa Wasimbowe ulitokea Unyiha katika Tanzania ya leo, na ulikuwa umejijenga kwenye kilima cha Mbande. Msingi wa nguvu za Simbowe haueleweki, lakini huenda alikuwa mfanyabiashara katika mtandao wa kibiashara ulioenea hadi pwani ya mashariki. Inaonekana kwamba uhusiano wa Simbowe na wenyeji asili haukuwa mzuri sana; baada ya kuwasili kwake, *kyungu* alianzisha ushirikiano na Wamwenekisindile waliokuwa walinzi wa madhabahu muhimu ya kidini yaliyohusishwa na madhehebu ya nyoka, na inaonekana kwamba Wamwenekisindile walimsaidia katika kuanzisha mashambulizi dhidi ya Simbowe. *Kyungu* alitwaa madaraka kwa nguvu huko Mbande, na polepole aliweza kuanzisha utaratibu mpya. Mara baada ya kutulia, ma-*kyungu* walidumisha ukuu wao juu ya raia wao wapya kwa kuanzisha kituo cha miviga ya madhehebu ya wahenga wa kifalme. *Kyungu* pamoja na maofisa wake walijiimarisha zaidi kwa kuoa miongoni mwa familia za wenyeji.

Kabla ya kuwasili kwa ukoo wa *Wakyungu* watu walikuwa wakiabudu mungu mkuu kupitia mizimu saidizi kama vile nyoka mtakatifu. *Wakyungu* waliwatumia wahenga wao kama watu wa kati katika kuabudu aina yao ya mungu mkuu, Ngulube. Polepole, jinsi watu walivyokuja kukubaliana na wazo la kuabudu wahenga na kuachana na madhehebu ya nyoka, waliukubali pia uungu wa *kyungu*. *Kyungu* alibadilika na kuwa mfalme-kuhani mwenye kuwasiliana na wahenga wa kifalme. Kwa Wangonde, *kyungu* akawa mwakilishi hai wa mungu. Afya yake iliukilia ustawi wao, na ili kulinda hali hii, alizuiliwa nyumbani mwake. Endapo *kyungu* alionyesha japo dalili ndogo ya ugonjwa, alikabwa roho na kuuliwa mara moja na washauri wake, *makambula*.

Maendeleo haya yalitokea wakati wa utawala wa ma-*kyungu* wanne wa mwanzo, kwa kukadiria kati ya 1600 na 1720. Mara baada ya kifo cha *kyungu* wa tatu, Mwakalosi, mtoto wake wa kiume na mrithi wake alikikataa kiti cha ufalme kwa vile alihofia kwamba endapo angaliugua *makambula* wangalimwua. Pia alikataa wazo la

watoto wake wote kuuawa isipokuwa mmoja, utaratibu uliokuwa ukifanyika ili kuepuka ushindani wa kugombea urithi. Mgogoro uliozuka kutokana na Mwakalosi kukataa kukalia kiti cha ufalme ulimalizika pale *malambula* walipompatia *ukyungu* kaka yake aliyeitwa Magemo.

Temi za Kameme, Mwaulambya na Msukwa pia ziliendeleza taratibu za kuabudu wahenga wa kifalme. Lakini hata hivyo kifalsafa na kilugha walifanana zaidi na Wanyiha, na vitendo vya kumkaba roho mfalme wao, kumzuilia ndani na kuua wanamfalme havikujitokeza kabisa katika historia yao. Hata hivyo, temi zote hizi zinawakilisha kuanzishwa, katika eneo hili, kwa aina mpya ya utaratibu wa kisiasa ambayo iliunganisha dini na siasa chini ya viongozi wenye heshima kubwa, na ambapo uhusiano miongoni mwa raia ulijengwa zaidi juu ya msingi wa kisiasa kuliko ule wa kindugu.

Mgogoro mpya wa kurithi ufalme ulitokea kwenye ufalme wa Wangonde baada ya kifo cha *kyungu* Magemo, ambaye mtoto wake wa kiume, Mwangonde, alikuwa mdogo mno kuweza kurithi ufalme. Mtoto wa kiume wa dada yake, Kasyombe, ndiye aliyekuwa *kyungu*. Baada ya Kasombe kuchukua uongozi, *makambula* walianza kupoteza baadhi ya madaraka yao, ambayo yalichukuliwa na *kyungu*. Kasyombe, ambaye baba yake alikuwa Mndali, alikulia Ngana, kaskazini mwa ufalme huo. Alisitisha ada ya kuwaua watoto wa kiume wa *kyungu*, idadi ya wanamfalme ikaanza kuongezeka na hivyo kuongeza nguvu za mfalme, hasa baada ya warithi wake wengine kuanza kuwakabidhi watoto wa kifalme maeneo ya ardhi, na hivyo kuhakikisha kwamba athari za *kyungu* zinafika katika eneo lote. Hakuna wasiwasi wowote kwamba ilipofikia 1800 ufalme wa Ngonde ulikuwa unajiamini vya kutosha kuweza kuanza kujiingiza katika siasa za ukanda mpana zaidi kusini mwa Wasongwe.

Kwa hiyo, katika kipindi cha kuanzia katikati ya karne ya kumi na tatu hadi katikati ya karne ya kumi na nane, eneo la kusini mwa mto Songwe lilikuwa limeendelea kupitia hatua kadhaa. Lilianzia kwenye mtandao wa awali wa madhabahu ya kidini yenye kuhusiana na madhehebu ya nyoka, likaingia kwenye mfumo uliotawaliwa na koo kubwa, na mwisho likaanzisha madola kadhaa: kaskazini kulikuwa na madola ya Ulambya, Kameme, Mikusu, Ungonde na Mwamphoka Mwambele; kusini kulikuwa na madola ya Kanyenda, Kabunduli, Kaluluma na Chulu. Huko kaskazini lugha ya Kyangonde ilikuwa imeanzishwa na waasisi wa Kingonde na Kinyakyusa kama lugha mpya, wakati huko kusini Chitonga kilikuwa kinaibuka kutokana na muungano wa jamii na lugha za Watumbuka na Wachewa. Sehemu ya kati ya ukanda huu ilitawaliwa na Watumbuka, ambao hawakuwa na serikali kuu, na ambao historia yao ya awali inaleta utata mwingi kuielezea.

Mabadiliko ya kidini yaliyotokea kutokana na kuanzishwa kwa dola la Wangonde yalijitokeza pia kwenye ukanda wa mamlaka ya Maravi. Mfumo wa dola la Maravi ulijumuisha mtandao wa madhabahu ya mvua ya kabla ya Wamaravi (yaani ya Wachewa-asili) uliokuwa umejikita huko Msinja, eneo ambalo kwa hivi sasa ni Lilongwe ya magharibi. Kila mjenzi wa dola la Kimaravi alijaribu kudhibiti

madhabahu yaliyoangukia kwenye utawala wake. Mjenzi huyo angetoa msaada na ulinzi, na, kwa kawaida, kufanya hija za kila mwaka kwenye madhabahu hayo. *Kalonga* na *undi* walijaribu kuchukua madaraka juu ya madhehebu ya Msinja, ilihali kwenye bonde la Shire chini *lundu* alifanikiwa kuanzisha kiasi kikubwa cha udhibiti juu ya madhabahu ya Mbona huko Nsanje. Kutokana na kiwango hiki cha ushiriki wa nasaba tawala katika madhehebu ya mvua, polepole teolojia yake ilianza kuwa changamani (ya mseto); ilianza kukubali ibada za mizimu ya wahenga wa kifalme, wakati visasili asilia vya Kichewa vilizuiwa. Hata hivyo mabadiliko muhimu ya kidini katika kipindi hicho yalitokea pale nasaba tawala ziliposhindwa kudhibiti madhehebu ya mvua. Hivyo nasaba hizo zilianzisha madhehebu yao zenyewe, ambayo moja ya kazi zake ilikuwa ni kuitukuza na kuiabudu familia ya kifalme.

Kuelekea katikati ya karne ya kumi na nane mfumo wa dola la Maravi ulianza kudidimia. Kudidimia huku kulichukua sura ya ama kujitenga ama upinzani dhidi ya utawala mkuu wa *kalonga, lundu,* na *undi*. Lakini hata hivyo sababu zilizoleteleza kudidimia kwa dola za Maravi haziko wazi. Kwa upande wa *undi* Wareno waliovamia miliki yake wakati wa kinyang'anyiro cha dhahabu cha miaka ya 1740 na ya 1750 walikuwa na dhima ndogo sana katika kudidimiza dola hilo. Pia hoja imetolewa ya kwamba mamlaka ya *undi* na ile ya *kalonga* zilidhoofishwa na kuongezeka kwa ukaidi wa Makewana, mdhibiti wa madhabahu makuu ya dini ya Kichewa huko Msinja, ambaye hakutaka kutumia nguvu zake za kidini kwa faida ya nasaba tawala. Makewana wa mwanzo walikuwa viungo muhimu vya umoja wa kidini wa tawala za *kalonga* na *undi*, lakini Makewana wa karne ya kumi na nane walianza kuwa na tamaa za kidunia na kujimegea maeneo yao wenyewe ya mamlaka. Huenda upinzani wao kwa *kalonga* na *undi* ulikuwa ni dalili ya jitihada za koo zao za Wachewa-asili kujaribu kurudisha utawala wao wenyewe.

Mwishowe tukio muhimu kabisa katika kudidimiza mamlaka ya dola la *lundu* mashariki ya mto Shire lilikuwa ni kuibuka kwa utaifa wa Wamakua-Walolo katika karne ya kumi na nane. Kimsingi utaifa wao ulikuwa umeelekezwa dhidi ya Wareno na washirika wao wa Kiafrika, kwa kuanzisha vita vikali vya kudhoofishana kuanzia 1749 hadi mwishoni mwa karne hiyo. Changamoto iliyotolewa na Wamakua wa pwani dhidi ya ubeberu wa Kireno kwenye pwani ya Msumbiji itakuwa iliwatia moyo Wamakua na Walolo wa bara hata wakaanzisha kampeni kama hizo dhidi ya utawala wa kigeni. Kwenye maeneo ya bara Wamaravi ndio waliokuwa walengwa wa chuki ya Wamakua-Walolo zaidi kuliko hata Wareno. Ukuu wa Wamaravi ulianza kutetereka kuanzia Kilimani kwa upande wa mashariki hadi kwenye Mlima Murambala huko Shire ya magharibi.

Katika kipindi kinachojadiliwa watu wa Zambezia ya kaskazini nao pia waliathirika sana na ongezeko la mahusiano ya kiuchumi kati yao na dunia ya nje. Mahusiano hayo yanarudi nyuma hadi kwenye kipindi cha utawala wa kibiashara wa Waarabu-Waswahili kwenye pwani ya mashariki na kandokando ya Zambezi kabla ya 1500, japo wakati huo yalikuwa ni ya kiasi tu. Hata hivyo baada ya kulowea kwa

Wareno kandokando ya Zambezi katika karne ya kumi na sita, mara kwa mara Wareno walisafiri kwa mashua kwenye mto Shire kuelekea kaskazini kuanzia Sena kununua vyombo vya chuma, nguo za *machila,* chumvi na pembe kutoka kwa Wamanganja, wao wakiwauzia nguo kutoka nje, shanga na vyombo vya sufuri (shaba nyeupe). Juu zaidi kufuata Zambezi, Wareno waliokuwa wameselelea Tete walianzisha uhusiano wa kibiashara na ufalme wa *undi* pamoja na makao makuu ya mfumo wa dola la Maravi hadi Shire juu na pwani ya kusini ya Ziwa Malawi. Baada ya kuanzishwa kwa *feira* (gulio kuu) katika Zumbo mnamo 1716, Wareno walipata mwanya wa kuyafikia masoko ya pembe katika jamii kadhaa kuelekea magharibi hadi kusini na katikati ya Zambia. Lakini kilicholeta mabadiliko ya wazi kwenye upanuzi wa athari za kibiashara za Wareno huko Zambezi kaskazini ni kukua na kuenea kwa *prazo* (ardhi "ya kifalme" iliyotolewa kwa wakulima wakubwa) huko Zambezia. *Prazo* hizo zilikuwa na dhima kubwa katika upanuzi wa athari ya kibiashara ya Wareno kaskazini mwa Zambezi.

*Prazo* ziliibuka wakati wakoloni wengi wa Kireno ama wa Kigoa walipojichukulia hadhi za kisiasa za watemi kwenye maeneo ya ardhi ambayo hapo awali yalikuwa mikononi mwa wenyeji Waafrika. Mchakato huu ulianzia huko Sena karibu na mwishoni mwa karne ya kumi na sita na taratibu ulienea kwenye maeneo mengine ya bonde la Zambezi chini kwenye karne ya kumi na saba. Mfalme wa Lisbon aliona kwamba kuruhusu kuanzishwa kwa *prazo* na masetla wa Kireno kungekuwa njia ya kuhimiza juhudi za watu binafsi katika kulikalia bonde la Zambezi, na pia alitumaini kwamba matarajio ya kupata ardhi yangewavutia wahamiaji kuselelea kwenye eneo hilo.

Katika karne ya kumi na nane, *prazo* zilitawala eneo zima la Zambezi chini kutoka Luabo au delta ya Zambezi huko mashariki hadi Chikoa upande wa magharibi. *Prazo* kubwa hazikuwa mashamba makubwa ya binafsi tu, bali pia zilikuwa ni maeneo ya kiutawala ambamo wamiliki wake, waliojulikana kama *prazeros,* walikuwa na mamlaka kamili kisheria, walianzisha vita, walitoza ushuru, na mara nyingi walijihusisha na vitendo vya ukatili mkubwa. Kati ya mambo muhimu yaliyowavutia wanahistoria kuhusu *prazo* hizi, mambo mawili yanajitokeza zaidi. Moja ni lile la uhusiano tata ulioendelezwa kati ya *prazo* hizi na dola jirani za Kiafrika; la pili ni lile la athari zake za kiuchumi juu ya sehemu zingine za ukanda wa Zambezia kaskazini.

Ma-*prazero* karibu wote walijihusisha katika mahusiano ya kidiplomasia na kijeshi na madola jirani ya Kiafrika kwa lengo la wazi la kuyanyonya rasilimali zao za kibinadamu. Kwa mfano, Wachikunda, waliowatumikia ma-*prazero,* walikuwa na uwezo wa kupata nguvukazi kutoka miongoni mwa Wamakua, Wamanganja, Wasena, Wakalonga, Watonga, Watawara, Wansenga, Watumbuka na wengineo. Kutokana na kuvutika kwao na biashara za pembe na dhahabu, ma-*prazero* walikuwa na dhima muhimu katika kuendeleza biashara kaskazini ya Zambezi. Kwa kuwatumia watumishi wao wa Kichikunda kama watu wa kati, waliauzisha mtandao wa

mahusiano ya kibiashara na jamii nyingi za Kiafrika katika ukanda huo: Wamanganja, Wachewa, Wansenga, Walenje pamoja na Walunda wa kusini. Watu hawa wa bara waliwapatia shaba nyekundu, pembe, nta na watumwa kwa kubadilishana na nguo za nje, shanga, vyombo vya sufuri, pombe kali na chumvi. Kuanzia kama mwaka 1740, ma-*prazero* walikuwa pia wanajihusisha katika kuchimba na kubadilishana dhahabu na Zambezi ya kaskazini, hasa katika miliki ya *undi*. Kiasi cha kilo 100 za dhahabu zilichimbuliwa kila mwaka kabla biashara hiyo haijadidimia kwemye miaka ya 1780.

Kinyang'anyiro hiki cha dhahabu kilisababisha ma-*prazero* na jumuiya za Wareno kwenye mto Zambezi kupoteza biashara ya pembe; biashara hiyo ilizidi kuingia mikononi mwa washindani wengine, hasa Wayao.

Wayao waliibuka kama taifa kuu la kibiashara mwishoni mwa karne ya kumi na saba na mwanzoni mwa karne ya kumi na nane, na walishiriki katika biashara za masafa marefu kote Afrika ya Mashariki na Kati. Kulingana na mapokeo simulizi ya Kiyao, wahunzi wa Kichisi ndio waliokuwa waanzilishi wa biashara ya kuelekea pwani. Wachisi walitegemea sana ujuzi wao wa kusana vyuma na biashara ya mazao yao ya vyuma ili kuendesha maisha yao. Hivyo upo uwezekano kwamba baada ya nchi ya Wayao kujitosheleza kwa bidhaa za chuma, Wachisi walipeleka bidhaa zao mbali zaidi na hivyo kuanzisha uhusiano na maeneo ya pwani. Maendeleo zaidi ya shughuli za kibishara za Wayao yalisaidiwa na kuanzishwa kwa soko imara la pembe huko Kilwa kati ya 1635 na 1698. Soko la pembe la Kilwa lilipoporomoka baada ya 1698 kutokana na migogoro kati ya Omani na Wareno, Wayao walipata soko kibadala huko Mossuril, mkabala na kisiwa cha Msumbiji. Yaelekea hadi wakati huo biashara ilikuwa tayari ni kitu cha lazima katika mtiindo wa maisha wa Wayao. Wayao walipeleka pembe zao hadi Msumbiji ama Kilwa, kufuatana na mahitaji yaliyokuwepo. Magharibi mwa nchi yao wenyewe, Wayao walikuwa na chanzo tajiri cha pembe kutoka nchi ya Wamaravi. Zaidi ya hayo, kuanzia kama mwaka 1750, walianza kupokea pembe zaidi kutoka kwa Wabisa wa kaskazini-mashariki mwa Zambia kwa ajili ya kuzisafirishwa kwenda Kilwa.

Kwa Wabisa, huenda biashara ilikuwa ni namna ya fidia kwa udhaifu wao wa kisiasa huko nyumbani kwao. Walikuwa wamebanwa katikati ya nguvu za upanuzi za falme za Walunda na Wabemba. Biashara na kusafiri vilikuwa ni njia muhimu ya kuwafikisha kwenye fursa zilizopatikana mbali zaidi. Wabisa walifungua njia nyingi mpya kati ya eneo la Luapula huko kaskazini-mashariki ya Zambia na pwani ya mashariki. Pia kati ya 1790 na 1830 walijaribu kuanzisha biashara kati ya ufalme wa Walunda na Wareno wa Zambezi. Walichukua pembe, shaba nyekundu na watumwa kutoka maeneo mbalimbali ndani ya bara la Afrika ya kati na kupeleka bidhaa hizo kwenye makazi huko pwani au kandokando ya Zambezi kwa kuzibadilisha kwa nguo, shanga, bunduki na baruti.

Moja ya matokeo ya biashara yao na pwani ni kwamba makazi yao wenyewe yalianza kuhama kuelekea mashariki kwenye bonde la Luangwa na hata ng'ambo

yake. Vijiji kadhaa vya Wabisa vilianzishwa kwenye bonde hilo kwenye miaka ya 1760, na hadi mwishoni mwa karne ya kumi na nane kulikuwepo na vijiji vya Kibisa kwenye eneo la magharibi la Malawi ya kati.

Kwa upande wa Wareno, kuporomoka kwa shughuli za uchimbaji wa dhahabu na kupoteza soko la pembe kwa Wayao na Wabisa ni miongoni mwa sababu za kujihusisha kwao kwa dhati katika biashara ya watumwa. Mwishoni mwa karne ya kumi na nane kulikuwa na mabadiliko kamili kwenye sura ya biashara miongoni mwa kanda mbalimbali za kaskazini mwa Zambezi. Watumwa wakawa ndio bidhaa muhimu ya biashara iliyoweza kuuzwa nje ya nchi. Mabadiliko haya yalikuwa dhahiri kiasi kwamba karne ya kumi na nane iliweza kubainishwa kwa biashara ya pembe na karne ya kumi na tisa kubainishwa kwa biashara ya watumwa. Kushiriki kwa Wareno katika biashara ya watumwa kulikuwa tayari ni kwa kiwango kikubwa kwenye miaka ya 1780, wakati watumwa kutoka Zambezia ya kaskazini waliposafirishwa kwenda kwenye visiwa vya kikoloni vya Wafaransa vya Maskarene katika Bahari ya Hindi.

Biashara ya watumwa iliposhamiri kuzidi biashara ya pembe, Wareno waliungwa mkono na Wayao na Wabisa. Soko la Kilwa lilianza kutawaliwa na biashara ya watumwa kuanzia miaka ya 1770 na kuendelea, na huenda wakati huo Wayao walianza kuchukua watumwa badala ya pembe katika misafara yao ya kutoka bara.

Eneo lote la ukanda wa kaskazini nalo pia liliingizwa kwenye mtandao wa biashara ya masafa marefu. Hadi kufikia karne ya kumi na nane, hakuna sehemu yoyote katika ukanda huu iliyokuwa imejihusisha na biashara ya masafa marefu, ijapokuwa kulikuwepo biashara kubwa ya wenyeji karibu na pwani ya Ziwa Malawi kuanzia nchi ya Tumbuka hadi nchi ya Nsenga pamoja na eneo la Uchewa kaskazini. Katika miongo minne ya kwanza ya karne ya kumi na nane eneo la Tumbuka lilikuwa limeunganishwa kwenye mtandao wa kibiashara ulioenea kutoka Katanga huko kaskazini-magharibi hadi Kilwa huko mashariki. Waliohusika na mabadiliko haya walikuwa wakuu wa kaya waliojulikana kama *balowoka* (wale waliovuka ziwa).

Mtu mashuhuri kati ya wote miongoni mwa hawa watu wapya ni Kakalala Musawila Gondwe, Mnyamwezi ambaye kwa kipindi fulani alikuwa amejihusisha na biashara ya kwenda pwani ya mashariki. Akiwa anatafuta pembe, Gondwe alivuka ziwa pale Chilumba na kuselelea kwenye nyanda za Nkamanga karibu na bonde la Luangwa, ambalo kwa wakati huo lilikuwa na idadi kubwa ya tembo. Alianzisha uhusiano na mkuu wa ukoo wa Luhanga na kisha akaoa kwa Waluhanga na kwa familia nyingine mashuhuri, na hivyo kujiingiza kikamilifu katika jamii ya Watumbuka.

Katumbi Mulindafya Chabinga alitoka kwenye nchi ya Wanyamwezi lakini baada ya kuvuka ziwa Chilumba alikwenda kwenye eneo la mlimani linalounganisha vilima vya Misuka na uwanda wa juu wa Nyika na kuselelea Chigoma huko Nthalire. Kutoka Chigoma Katumbi alipanua mahusiano yake ya kibiashara kuelekea Malambo kwenye bonde la Luangwa lilokuwa na utajiri mkubwa wa pembe.

Mfanyabiashara mwingine, Katong'ongo Mhenga, ambaye alitokea mkoa wa

Ubena-Uhehe, alivuka ziwa hilo muda mfupi baada ya kuselelea kwa Gondwe na Katumbi. Katong'ongo alikuwa akitafuta ardhi ambapo yeye na familia yake wangeweza kuishi, na ardhi hii aliipata kwenye bonde la Henga. Akiwa mwenye ujuzi mwingi, alifahamu namna ya kutengeneza chumvi, jambo ambalo lilimwezesha kudhibiti mashimo ya chumvi bora huko Kanembe. Yeye pia alioa katika familia za wenyeji na taratibu akapata umaarufu. Baadaye alikuja kujulikana kama Mwahenga, mmiliki wa eneo la Henga.

Wahamiaji hawa watatu walianza kutawala biashara ya karibu eneo lote la kusini mwa Songwe na mashariki ya bonde la Luangwa na waliishia kugongana wao kwa wao. Gondwe alihisi kwamba ilikuwa muhimu kwake kuwa na uhuru wa kutumia bure kivuko cha Chumba - kama sio kukimiliki - ili kusafirisha pembe zake kupeleka pwani ya mashariki. Kwa hiyo alijihusisha kwenye mgogoro wa urithi baada ya kifo cha Katumbi na kufanikiwa kuwashawishi watu wamkubali mgombea dhaifu kushika utemi. Kisha alifanya makubaliano na Mwahenga, ambaye alikubali kutokukwamisha biashara yake. Gondwe alifanya makubaliano kama hayo na watawala wa mashariki ya bonde la Henga. Hivyo ilipofikia mwaka 1800 Gondwe aliweza kudai ukiritimba wa biashara katika eneo lililokuwa katikati ya Luangwa na pwani ya magharibi ya Ziwa Malawi. Kwenye uwanda wa Nkamanga tayari alikwisha fanikiwa kupata mamlaka ya kisiasa, na hivyo kuweza kupanua miliki yake ya biashara.

Katika karne ya kumi na nane zilikuwepo pia tawala nyingine ndogo ndogo zilizoanzishwa na familia kutoka upande wa mashariki wa ziwa, na wengi wa waanzilishi wake walikuwa wafanyabiashara ya pembe kama walivyokuwa akina Gondwe na Katumbi. Kusini tu ya Ungonde, familia ya Mwafulirwa ilianzisha dola la Wafulira kwenye eneo lililokuwa limekaliwa na ukoo wa Mkandawire. Kisha ndugu wa Mwafulirwa walikwenda magharibi na kuselelea Zibang'ombe, mahali ambapo walianza kujenga dola la Wawenya, ambalo ilipofikia mwishoni mwa karne ya kumi na nane tayari lilikwisha panuka kuelekea kaskazini hadi mipaka ya kusini ya Ulambya. Kwa karibu kipindi hicho hicho, eneo la kusini-magharibi ya Uwenya liliangukia mikononi mwa utawala wa familia ya Mlowaka ya Mughogho. Eneo hili la Uyombe lilikuwa na tembo wengi sana, na miongo michache baadaye liliwavutia wasasi wengi.

Familia za wasasi zilivuka ziwa upande wa kusini zaidi na kuhamia sio mbali na eneo la sasa linaloitwa boma la Nkhata-Bay. Waliwaondoa watawala wa Kiphiri, na baada ya kizazi kimoja wakawa ndio familia inayotawala katika eneo hilo.

Kwa hiyo, katika karne ya kumi na nane, nchi ya Watumbuka ilitawaliwa kwanza na wasasi wa pembe, na kisha wafanyabiashara ambao, kwa kudhibiti utajiri, waliweza pia kupata mamlaka ya kisiasa. Ugatuzi wa madaraka ya kisiasa ulifutika na badala yake pakaingia mamlaka ya watemi wa kibiashara. Athari za kisiasa za aina hiyo hazikuwezekana katika madola ya kaskazini, ambayo yalibakia nje ya mtandao wa biashara ya masafa marefu kwa zaidi ya karne moja baada ya kuwasili kwa Watumbuka. Katika karne ya kumi na nane, himaya ya Wamaravi ilikuwa

inamomonyoka na madola ya ukanda wa pembezoni ya Watumbuka-Wachewa huko kusini yaliachiwa kudhibiti kabisa mambo yao wenyewe. Baada ya mwaka 1800 madola yote na jamii zote zilijihusisha kikamilifu kwenye enzi ya biashara ya pembe na, baadaye, watumwa; biashara ambayo matokeo yake yenye madhara makubwa yanafahamika.


Tarehe ya mwanzo katika juzuu hili hailandani na mpangilio wa vipindi vya kihistoria vya eneo hili. Enzi ya kihistoria katika ukanda wa kusini inafunguliwa t.1400 kwa kuwasili kwa Wamaravi, na kwenye ukanda wa kaskazini t.1600 kwa uhamiaji wa Wangulube. Hata hivyo, tarehe ya kufunga juzuu hili inasadifu, maana masuala mapya yalitawala karne ya kumi na tisa: kubadilika kwa biashara kutoka biashara ya pembe kwenda biashara ya watumwa, kuhusika kwa eneo zima la ukanda kwenye biashara iliyoendeshwa kutoka nje, kuanzishwa kwa temi za Wayao kwenye maeneo ambayo hapo awali yalikuwa chini ya Wamaravi, na mwishowe kuwasili kwa jamii mpya - Wanguni, Waswahili, Wakololo na Wazungu - ambao hatimaye waliwania kushika mamlaka ya kisiasa, bila kujali sababu tofauti tofauti zilizowaleta kwenye eneo hili.

# 22 Zambezia ya Kusini

Kipindi cha kutoka mwaka 1500 hadi 1800 huko Zambezia ya kusini kina kumbukumbu pungufu. Inabidi tutegemee zaidi maelezo ya wasafiri na wafanyabiashara wa Kireno ambao walipenya eneo hili katika muongo wa kwanza wa karne ya kumi na sita. Kwa hiyo, sura hii itajihusisha zaidi na madola matatu: himaya za Mutapa na Rozvi na madola ya mashariki mwa Shona. Madola ya Mutapa na Rozvi yalichipuka kutokana na utamaduni wa Zimbabwe Kuu (1200 - 1450, tazama UNESCO *Historia Kuu ya Afrika,* Juzuu la IV, Sura ya 21).

Zimbabwe Kuu ilififia polepole kuanzia katikati ya karne ya kumi na tano na kuendelea kadri uzalishaji wa dhahabu ulivyopungua. Kufifia kwa Zimbabwe Kuu kulisababisha kuibuka kwanza kwa dola moja ambalo halikujulikana sana lililoitwa Torwa au "Butwa" kulingana na nyaraka za Kireno. Mji wake mkuu wa kwanza, uliokuwa huko Khami na pengine ukiwa umeanzishwa katikati ya karne ya kumi na tano, uliteketezwa na moto katika nusu ya pili ya karne ya kumi na saba. Mji wake mkuu wa pili, huko Danangombe, ulikuwa mdogo kuliko ule ya kwanza. Mabaki ya kiakiolojia yanadokeza kwamba majengo yote ya mawe ya fahari katika dola la Torwa yalijengwa kabla ya mwaka 1650.

Maendeleo ya kisiasa ya pili muhimu baada ya kuporomoka kwa Zimbabwe Kuu yalikuwa ni kuibuka kwa himaya ya Mutapa mwanzoni mwa karne ya kumi na sita. Himaya ilikuwa na watu tofauti tofauti wasemao lugha ya Kikaranga. Kinadharia himaya hii ilienea kutoka ukingo wa kusini wa mto Zambezi hadi Bahari ya Hindi, lakini kimatendo watawala wa Mutapa walikuwa na mamlaka madogo nje ya nchi ya uwanda wa juu. Kuna ushahidi kwamba falme za Manyika, Uteve, Barwe na Danda zilijiondoa kwenye himaya katika karne ya kumi na sita, ingawa ziliendelea kutekeleza majukumu yao ya kimiviga na kutoa ushuru hadi kuibuka kwa *Changamire* (mtawala au mfalme) wa Dombo mwishoni mwishoni mwa karne ya kumi na saba. Imewahi kudokezwa kwamba *Machangamire* wenyewe walilipa ushuru wao mara chache chache kwa maliki wa Mutapa katika karne ya kumi na nane. Matukio kama hayo yalitokea huko Zambezi ya chini, ambako watawala wa Watonga na Wasena walifaulu kupinga juhudi zote za watawala wa Mutapa kulazimisha mamlaka yao ya kisiasa juu yao. Matukio haya yalipunguza himaya hadi kwenye kiini




**22.1** *Afrika ya kati na ya kusini-mashariki kwenye kipindi cha madola ya Mutapa na Torwa (kutoka S.I. Mudenge, 1988* A Political History of Munhumutapa t. 1400-1902; *na* Zimbabwe Epic, *National Archives of Zimbabwe, Harare, uk. 47)*

chake, pale kwenye eneo lililomomwa na nchi za Dande na Chidima.

Desturi ya kujenga majengo ya fahari kwa kutumia mawe katika himaya ya Mutapa pengine iliendelea hadi karne ya kumi na sita. Baadhi ya magofu ya awali kabisa, hususani yale ya Zwongombe, yaliwakilisha miji mikuu ya awali ya watawala wa Mutapa. Miji mikuu ya baadaye ilikuwa ya aina ya maboma ya urefu wa mita kadhaa kwenda juu.

Katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na nane watawala wa Mutapa walipoteza udhibiti wa moja kwa moja wa uwanda wa juu na kitovu cha himaya kikahamia kwenye mabonde ya kusini yaliyoko kati ya Zumbo na Tete. Upotevu huu wa udhibiti wa kisiasa ulikuwa hatima ya mlolongo mrefu wa kumeguka kulikoanza mnamo mwaka 1629, Wareno walipomshinda Mamvura Mutapa, na kumalizika mnamo mwaka 1917, dola la Mutapa lilipotoweka kabisa.

Kiutawala, himaya ilidhibitiwa katika ngazi tatu: mji mkuu, jimboni na kijijini. Mamutapa walikasimu mamlaka yao kwa machifu katika ngazi za kijiji na jimbo. Katika siku za awali za himaya, ni ndugu tu wa Mamutapa waliopewa nafasi hizo. Kwa mfano, ilikuwa ni desturi kwa mwana wa mfalme au anayetarajiwa kurithi kutawala nchi za Dande. Wale ambao, ingawa hawana uhusiano na Mamutapa, walisaidia katika hatua za kuteka himaya, pia waliteuliwa kwenye nafasi za mamlaka. Mamutapa walipoanza kujiamini zaidi katika karne ya kumi na saba, waliruhusu vijiji na majimbo kuwachagua viongozi wao. Katika mji mkuu, Mamutapa walisaidiwa na maofisa wa vyeo vya juu ambao walipewa ardhi kama malipo kwa huduma zao.

## *Imani na mbinu za udhibiti wa kiutawala*

Mamutapa walitumia taratibu kadhaa kudhibiti himaya. Mfano halisi ulikuwa ni tendo ambapo machifu wa nchi ilibidi waje na kuwasha mioto yao kutoka kwenye moto asilia wa mfalme na hivyo kuonyesha utii wao kwa mamlaka kuu. Mviga huu wa uaminifu ulirudiwa wakati wa kutawazwa kwa mtawala mpya wa Mutapa. Kushindwa kufanya mviga huu kulichukuliwa kuwa kitendo cha uasi na kutolewa adhabu kali.

Hii ilifanywa kwa kutumia jeshi madhubuti lililokadiriwa kuwa na wapiganaji 30,000 katika karne ya kumi na sita na askari 3,000 katika karne ya kumi na nane. Takwimu hizi zinaashiria kwamba kabla ya kufifia kwa himaya, watawala wa Mutapa walikuwa na uwezo wa kuwahamasisha wakulima wengi kujiunga na jeshi, lakini uwezo huo ulipungua pale himaya ilipoanza kufifia katika karne ya kumi na nane.

Mamutapa pia walitumia dini kuwadhibiti watawaliwa wao kwa njia ya mahusiano ya karibu baina ya tabaka tawala na dunia ya mizimu - ama mizimu ya mababu wa wafalme wenyewe, au makahini wanaowakilisha wamiliki asilia wa ardhi. Mfalme alitarajiwa kudumisha mawasiliano ya karibu na wafu wenye nguvu kwa niaba ya taifa. Mfumo wa ibada ya madhehebu ya makaburi ya kifalme pia uliboresha fahari ya maliki na kuimarisha udhibiti wake juu ya watu wake.

Wamiliki wa ardhi kama vile Wadzivaguru, walikuwa wagimba na maafisa wa miviga katika ikulu ya Mutapa. Kushiriki kwa maliki katika miviga ya ugimba kulionekana kuwa muhimu kwa ufanisi wa kiuchumi wa himaya. Dini ilikuwa utaratibu muhimu wa kudhibiti jamii katika uchumi ambao, kwa kiasi kikubwa, ulikuwa wa kilimo.

Mbinu ya kawaida kabisa ya udhibiti wa kisiasa ilikuwa ni ushuru uliotozwa na wafalme wa Mutapa kwa njia ya mazao ya kilimo, ngozi za simba na chui, manyoya ya mbuni, mifugo midogo na mikubwa, kidari cha kila mnyama aliyeuawa na, kuhusiana na tembo, pembe ambayo aliiangukia wakati akifa.

Ushuru pia ulikuwa wa namna ya kodi ya kazi. Kwa mujibu wa João de Barros, maafisa na watumishi wote wa mfalme na viongozi wa askari, kila mmoja na watu wake, ilibidi wamsaidie kulima mashamba yake au kufanya kazi nyingine kwa

siku saba katika siku thelathini. Utozaji wa kodi kwa kazi ulitumiwa pia na watawala watwawa (vibaraka).

Wakati wa kufungua migodi mipya watawala wa Mutapa, kwa kawaida, walituma mawakala wao wanaoaminika kukusanya kodi. Wachimba dhahabu walijenga sehemu kwa ajili ya wakusanya ushuru na vilevile kwa ajili ya kodi yenyewe. Hali ya mfumo wa kodi haielekei kama ilibadilika hadi kifo cha himaya ya Mutapa mwanzoni mwa karne ya ishirini.

Taratibu hizi mbalimbali za udhibiti kwa kiasi fulani zilifaulu katika kudumisha himaya kuu wakati ambapo umbali mkubwa ulifanya isiwezekane kwa machifu wa nchi kusimamia mambo kwa karibu. Kushindwa kwa jeshi kukabili kwa ufanisi uasi katika sehemu za mbali za himaya, njama za kisiasa za ndani walizonufaika nazo wafanyabiashara wa Kireno, na vita vya wenyewe kwa wenyewe, vyote vinaelezea kufifia polepole na kuanguka kwa himaya ya Mutapa.

## *Kipengele cha Wareno*

Ingawa Wareno walifika Sofala mnamo mwaka 1506, ilikuwa ni kuanzia mwaka 1550 hadi mwaka 1630 tu walipofanya majaribio ya dhati ya kudhibiti himaya ya Mutapa. Hadi mwaka 1540, biashara kati ya Wareno na Washona ilifanywa kwa msingi usiokuwa rasmi. Mnamo mwaka 1540, mahusiano ya kibiashara yalifanywa kuwa ya kawaida kwa kuanzishwa kwa kituo cha kidiplomasia na kibiashara katika makao ya kifalme ya Mutapa; kikiongozwa na afisa aliyeitwa "kiongozi wa malango." Majukumu yake yalikuwa ni kuwasilisha zawadi, maombi au malalamishi kutoka kwa wafanyabiashara wa Kireno kwenda kwa wafalme wa Mutapa na kinyume chake. Wareno waliwalipa watawala wa Mutapa kodi iliyoitwa *curva*.

Wakati wa kuanza kazi yake, kila kapteni mpya wa ngome ya Wareno ya Msumbiji alikuwa na wajibu wa kulipa kwa *monomutapa* kiasi sawa na kruzado elfu tatu cha nguo na shanga kwa miaka mitatu ya kipindi chake cha kazi. Kwa kubadilishana na kodi hiyo, wafalme wa Mutapa walitoa uhuru kwa wafanyabiashara kupita na kusafiri katika himaya yote. Kama ushuru haukulipwa katika muda ufaao, mfalme aliamuru kukamatwa kwa bidhaa zote katika himaya yake bila fidia. Hii kwa hakika ilitokea mnamo mwaka 1610 wakati Gatsi Rusere alipotangaza *mupeto* (kupokonya kwa nguvu) wa bidhaa za wafanyabiashara wa Kireno ambao ulisababisha kushambuliwa na kuuawa kwa wafanyabiashara wa Kireno.

Mfumo huu wa mahusiano ya ushuru uliendelea kwa mabadiliko kidogo tu hadi nusu ya pili ya karne ya kumi na sita, wakati Wareno walipoanza kuwadhibiti watawala wa Mutapa kutokana na vita vya uchokozi walivyopigana kusini mwa Zambezia kati ya mwaka 1569 na 1575, walipofaulu kujiimarisha katika falme za mashariki za Uteve na Manyika. Mwaka 1575 Wareno walifunga mkataba na mfalme wa Uteve ambapo kiongozi wa Sofala ilibidi alipe ushuru wa mwaka wa vipande 200 vya nguo kwa watawala wa Wateve. Kwa kubadilishana na ushuru waliolipa, wafanyabiashara wa Kireno walipata uhuru wa kupita katika ufalme wa Manyika,

ambako waliamini kuwa kuna dhahabu nyingi. Zaidi ya hayo, wakazi wa ngome ya Kireno ya Sofala waliruhusiwa kuingia ndani ya nchi kwa kufuata mto Sofala kwenda kununua vitu. Mkataba kama huo ulifungwa na mfalme wa Manyika mwaka 1573.

Mafanikio haya madogo yaliwashawishi Wareno kuzidi kujipenyeza katika himaya ya Mutapa. Maasi yaliyotokea huko kati ya mwaka 1590 na mwaka 1607 yaliwapa Wareno fursa ya kujiingiza katika uchangamani wa siasa za Mutapa. Mtawala mmoja wa Mutapa, Gatsi Rusere, alifunga mkataba nao wa msaada wa kijeshi, yeye akaahidi kuwaachia machimbo yote ya dhahabu, shaba, risasi na bati. Kwa hakika, mkataba huo ulitokea kuwa wa thamani ndogo kwa sababu Wareno hawakuwa na utaalamu wala wafanyakazi wa kuchimba migodi hiyo. Aidha, walimwacha Gatsi Rusere ashughulikie peke yake vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyoendelea hadi alipofariki mwaka 1624. Gatsi Rusere alirithiwa na mwanae Nyamba Kapararidze, ambaye uhalali wake ulipingwa na mjomba wake Mamvura. Katika vita vilivyofuata kati ya mahasimu hawa wawili, Mamvura alitafuta, na mnamo mwaka 1629 kupata, msaada wa kijeshi wa Wareno. Mkataba alioufunga na Wareno baada ya kutawazwa kwake ulimtaka Mamvura kuwapa uhuru wafanyabiashara wa Kireno kupita katika himaya yote, kuwafukuza wafanyabiashara wa Kiswahili na Kiarabu, na kuwaruhusu wamisionari wa Kidominika kuhubiri dini yao. Mkataba huo ulimtaka pia Mamvura kukomesha *curva,* na badala yake kulipa ushuru kwa Wareno kuanzia wakati huo na kuendelea. Baada ya mkataba huu, idadi ya wafanyabiashara na majasuri wa Kireno iliongezeka katika himaya ya Mutapa. Majasuri walipokonya ardhi ambayo baadaye ilitambuliwa na mfalme wa Kireno kama *prazos* (ardhi ya mfalme). Kutoka kuwa kwao wageni wa watawala wa Kiafrika, wafanyabiashara wa Kireno sasa karibu walikuwa wenye ardhi, lakini ubinafsi na vurumai zao zilisababisha kipindi cha machafuko na vurugu. Kwa hiyo, kujipenyeza kwa Wareno katika himaya ya Mutapa kulisambaratisha dola hilo, kuzua mfumo wa *prazo,* na kuchangia katika kuzaliwa kwa dola jipya, yaani himaya ya Rozvi.

## Mfumo wa *Prazo*

Kuchukuliwa kwa ardhi na majasuri wa Kireno kuliendelea karibu bila kuzuizi na matokeo yake yakawa ni kuundwa kwa *prazos da coroa* nyingi. Hizi zilimilikiwa na maafisa, wafanyabiashara, makundi ya kidini na waanzilishi wa makazi wa Kireno.

Mfumo wa *prazo* ulikuwa ni usanisi wa mifumo miwili ya kijamii na kiuchumi. Mfumo wa kwanza ulikuwa ni ule wa Washona ambao ulikuwa na tabaka la watawala na wakulima wazalishaji, na wa pili ambao ulilazimishwa juu ya ule wa Washona, ulikuwa na ma-*prazero*, waliotawala kama tabaka kuu juu ya *achikunda* (majeshi ya watumwa). Chifu wa Kiafrika aliendelea kutenda majukumu yake ya kijadi, lakini hakuwa tena na mamlaka yote, kwa kuwa *prazero* alijinyakulia hadhi ya kuwa mkuu juu yake.

Mahusiano ya uzalishaji katika *prazos* kimsingi, yalikuwa ya kikabaila. Chifu wa Kiafrika alimlipa *prazero* ushuru wa mali kama vile siagi, nguo iliyofumwa kienyeji,

asali, tumbaku, sukari, mifugo mikubwa na midogo, pembe za ndovu na mavumbi ya dhahabu. Katika nafasi yake kama chifu halisi, *prazero* aliamua kutumia desturi za kijamii ua za kidini za Kiafrika na kuoa katika familia za machifu ili kushinda udhaifu wake mkubwa - ule wa kukosa uhalali katika siasa za kijadi za Kiafrika.

Profesa Isaacman ametoa hoja kwamba *prazo* kama mfumo wa umilikaji ardhi wa Wareno ilibadilishwa na kuoanishwa na hali ya Kiafrika kiasi cha kuwa ya Kiafrika kabisa. Hata hivyo, hii nadharia ya kubadilika kwake kuwa ya Kiafrika kabisa ni vigumu kuitetea pale inapotambuliwa kwamba mfumo wa *prazo* wakati wote ulikuwa ukihusiana, kwa kiasi kikubwa au kidogo, na ubepari wa kibiashara, ma-*prazero* wakiwa watu wa kati katika biashara baina ya Msumbiji na India na baadaye Ulaya. Aidha muundo wa ndani wa *maprazo* ulikuwa na sifa ambazo ilikuwa vigumu kuziita za Kiafrika, mfano dhahiri ukiwa ni ule wa kuwepo sambamba kwa *colono* (walowezi) na *chikunda* (jeshi la watumwa). Kwa hakika, utaratibu kinyume, yaani ule wa kuondoshwa kwa Uafrika miongoni mwa jamii za kijadi za Kiafrika katika ma-*prazo*, ndio uliokuwa ukitokea. Kadiri mfumo wa *prazo* ulivyokabiliana na mahitaji ya ndani ya watumwa, ndivyo ma-*prazero* walivyowateka na kuwauza majirani wao wa Kiafrika na kuwaonea ma-*colono* na watumwa kwa namna ileile.

Isaacman ametoa hoja kwamba "katika utawala wa siku hadi siku wa ma-*colono*, nafasi ya *mambo* haikubadilika kabisa. Ni kweli kwamba *mambo* (mtawala wa kijadi) alikuwa na fahari na utii wa watu wake kutokana na uhusiano wake na ukoo wa waasisi. Lakini mwisho wa yote, *prazero* ndiye alikuwa na kauli ya mwisho katika kuamua mambo ya kisheria au uteuzi wa chifu mwenyewe wa Kiafrika. Hata haki ya kugawa ardhi ilitwaliwa na *prazero*. Haya yote yalibadilisha sana mfumo wa kisiasa wa kijadi. Ma-*prazo* yaliwakilisha awamu ya kwanza ya ukoloni wa Wareno huko Msumbiji: yalikuwa ni visehemu vya hapa na pale vya unyonyaji wa kisiasa na kiuchumi uliofanikishwa tu kwa kuzirekebisha asasi za kisiasa na kijamii za Kiafrika.

## Ueneaji wa ma-*prazo* kijiografia

Ma-*prazo* yalisambaa katika pande zote za mto Zambezi. Hata hivyo, kulikuwa na tofauti kubwa kati ya ma-*prazo* ya kusini mwa mto, ambayo yalikuwa mali ya mfalme wa Kireno na yale ya kaskazini, ambayo hayakuwa na hadhi hiyo. Kinadharia, *terra do coroa* ilitolewa tu kwa vizazi vitatu, ardhi iliweza kurithiwa tu kupitia mwanamke, haikuzidi urefu wa kilometa 14½, na mmiliki ilibidi alipe "kodi ya kuacha" ya mwaka. Wamiliki wa ma-*prazo* huko kaskazini hawakufungwa na masharti haya yote na walipata ardhi kwa kuwasiliana moja kwa moja na chifu wa mahali hapo.

Mfumo wa *prazo* ulidumishwa kwa kazi za makundi mbalimbali ya watumwa. Mtumwa wa ngazi ya juu alikuwa *chuanga*, aliyeteuliwa na *prazero* kwa sababu ya utii wake. Kila kijiji kilikuwa na *chuanga* wake, ambaye kazi yake kubwa ilikuwa ni kuwachunguza viongozi wa kijadi na kukusanya kodi na pembe za ndovu. Alikuwa pia na kazi ya kukusanya taarifa kuhusu idadi ya Waafrika waliokuwa katika *prazo*


ambayo ukubwa wake ulikuwa na umuhimu mkubwa kwa *prazero*. Ili kutekeleza mamlaka yake *prazero* alimtegemea *chikunda*, ambaye kazi yake kubwa ilikuwa ni kusimamia watu wa mahali hapo, kuhakikisha kwamba sheria za *prazero* zinafuatwa na kushughulikia pia matendo ya uasi. Jeshi la *chikunda* kwa kawaida, lilikuwa na watu kati ya 20 na 30 katika ma-*prazo* madogo, bali katika ma-*prazo* makubwa lingeweza kuwa na maelfu ya askari.

Katika ripoti yake ya mwaka 1766 kuhusu upwa wa Afrika, Antonio Pinto de Miranda alielezea mbinu zilizokuwa zikitumika kuwapata watumwa. Kwa mujibu wa maelezo yake, wawindaji wa watumwa waliwaiba watoto na kuwauza kwa wafanyabiashara wa Kireno, wafanyabiashara wa Kiswahili na wa Kiarabu na kwa mawakala wa Kiafrika. Baadhi ya watu waliuzwa kama watumwa au kutiwa rahani wakati wa njaa; na wahalifu waliotiwa hatiani, wafungwa wa kivita na walioshindwa kulipa madeni nao walikumbwa na janga hili. Picha inayoibuka kutokana na vyanzo vingine ni ile ya watu kuingia utumwani kwa hiyari.

## Kufifia kwa mfumo wa *prazo*

Mfumo wa *prazo* ulififia katika nusu ya pili ya karne ya kumi na nane kwa sababu kadhaa. Sababu ya kwanza ni ile ya mamlaka ya *prazero* kutodhihirika vema yakilinganishwa na yale ya utawala wa jadi wa Kiafrika. Mara nyingi hii ilimfanya *prazero* atumie vibaya mamlaka yake kwa kuwalazimisha wakulima wa Kiafrika kuuza mazao yao kwake peke yake na kwa bei za chini kwa makusudi. Aliwatoza pia kodi kubwa wakulima na kufanya ukatili bila wasiwasi wa kutiwa hatiani. Ma-*colono* yalijibu kwa kufanya uasi dhidi ya ma-*prazero* na hata kwa kuhama. Uasi na uhamaji huo ulisababisha kupungua kwa mazao ya kilimo, ukame na njaa. *Prazero* na jeshi lake la watumwa walitegemea chakula kilichozalishwa na wakulima; *chikunda* walitumia nguvu kupata vyakula kutoka kwa wakulima; na ma-*colono* yalijibu tena kwa kuhama kutoka kwa ma-*prazero* kwenda kutafuta chakula na usalama mahali kwingine.

Biashara ya watumwa ilikuwa kipengele kingine kilichosababisha kufifia kwa mfumo wa *prazo*. Biashara ya watumwa ya nchi za ng'ambo iliongezeka kwenye miaka ya 1640 kutokana na Wadachi kukalia Angola, kulikofanya Wareno wageukie kusini-mashariki ya Afrika kama chanzo kipya cha watumwa. Kuanzishwa kwa uchumi wa mashamba makubwa katika Visiwa vya Kifaransa vya Maskarene kwenye miaka ya 1730 kulisababisha mahitaji ya ziada ya watumwa. Lakini idadi ya watumwa waliosafirishwa nje kutoka kusini mwa Zambezia kufikia mwaka 1752, ilikuwa bado ndogo: yaani 300 kutoka Zambezia na 200 kutoka Sofala. Hata hivyo, kuelekea mwishoni mwa karne ya kumi na nane, biashara ya watumwa ilishika kasi kiasi cha kuwafanya ma-*prazero* huko katika bonde la Zambezi kuiona kama fursa ya kupata mali. Walipanga mashambulizi ya kuwateka watumwa katika nchi za Wachewa, Wansenga na Wamanganja. Pia walianza kuwauza watumwa waliokuwa katika mashamba yao na hivyo kudhoofisha msingi wa mfumo wa *prazo*. Hata hivyo,




**22.2** *Himaya ya Rozvi (kutoka D.N. Beach* Zimbabwe kabla ya 1900, 1984, uk. 38)

ng'ambo ya bonde la Zambezi, sehemu nyingine zilizobakia za Zambezia ziliathiriwa kidogo tu na biashara ya watumwa. Kufifia kwa mfumo wa *prazo* kusini mwa Zambezi kuliharakishwa na kuibuka kwa dola jipya kwenye nusu ya pili ya karne ya kumi na saba; yaani nasaba ya Kichangamire ya Rozvi.

## *Himaya ya Rozvi*

Asili ya himaya ya Rozvi bado haijawa dhahiri. Suala lenyewe limefanywa kuwa tata zaidi kutokana na jina *changamire* ambalo linahusishwa na muasisi wa himaya ya Rozvi mnamo nusu ya pili ya karne ya kumi na saba, lakini lilikwishatajwa katika karne ya kumi na tano. Hata hivyo, inaelekea kuna kukubaliana kuhusu mambo manne: la kwanza, kwamba Warozvi walikuwa sehemu halisi ya Wakaranga wa kihistoria wa himaya ya Mutapa hadi walipojitenga katika karne ya kumi na saba; pili, kwamba jina Rozvi lilitumiwa kwa mara ya kwanza kwa sehemu ya wale Wakaranga wa kihistoria waliohusishwa na kutwaa mamlaka kwa Changamire Dombo I kati ya mwaka 1684 na 1695; tatu, kwamba uundaji wa himaya ya Rozvi ulikuwa ni kazi ya Changamire Dombo I; na nne, kwamba jina Rozvi ambalo lilinyumbuliwa kutoka kitenzi cha Kishona *kurozva* (kuharibu), ama lilitumiwa na wafuasi wa Dombo kwa majivuno au walipewa kama jina la utani na walioathiriwa na matendo yao.

Kati ya mwka 1684 na mwaka 1695 Dombo Changamire polepole alichukua mamlaka huko kaskazini-mashariki. Bado haijawa wazi jinsi alivyotwaa mamlaka hayo. Alikuwa mchungaji wa wafalme wa Mutapa aliyeasi na kutoka na wafuasi wake, kwanza, hadi dola la Tarwa huko kusini-mashariki, na kisha hadi katika falme za Manyika na Uteve huko mashariki. Wafanyabiashara wa Kireno walifukuzwa mnamo mwaka 1684 kutoka ufalme wa Maungwe, kutoka nchi ya uwanda wa juu mnamo mwaka 1693 na kutoka ufalme wa Manyika mnamo mwaka 1695. Walikimbilia Zumbo, ambako walianzisha makazi mnamo mwaka 1710, kisha wakarudi katika makazi yao ya awali ya Masekasa huko Manyika. Hata hivyo, katika kila tukio, kulikuwa na maelewano ya kimya kimya kwamba walikuwa chini ya mamlaka ya makabaila wa Changamire wa Rozvi. Kwa njia hii watawala wa Rozvi waliweza kuunda himaya iliyoenea hadi Buhera, Bocha, Duma na nyanda za juu za kusini mashariki huko kusini, hadi katika udongo wa chumvichumvi huko kaskazini, na katika tambarare za chini huko kusini-magharibi. Kitovu cha himaya pengine kilienea katika eneo lilelile lililokuwa la Wandebele waliowarithi mnamo miaka ya 1840.

Wazo letu kuhusu mji mkuu wa Rozvi linatokana na maelezo ya karne ya kumi na tisa ya Wareno, ingawa pengine mji huo ulikuwa umebadilika kidogo tu tangu miaka ya 1600 na 1700. Makao ya mfalme, kulingana na maelezo haya, yalikuwa na nyumba tatu kubwa za mawe zilizozungukwa na kuta za pembe za ndovu. Changamire wa Rozvi alikuwa na bunduki nyingi alizopata kutoka kwa wafanyabiashara wa Kireno huko Sena.

Warozvi walidumisha utambulisho wao kama tabaka la juu la kigeni miongoni mwa watu walioshirikiana nao kizimu kilekile cha *moyo*, ambao walikwisha kuwa washirika wao wakati wa vita vya kuzitamalaki jamii zenye kuzungumza lugha ya Kikaranga, na vilevile jamii za dola la Tarwa.

## Utawala wa majimbo

Watawala wa Warozvi walitumia mbinu zinazofanana na zile za Mamutapa kudumisha himaya yao. Taratibu zake zilihusu ugawaji wa ardhi, ulipaji wa ushuru, dini na jeshi lililofunzwa vizuri.

Watawala wa Warozvi waligawa ardhi kwa machifu wapya na kuwatoza ushuru. Mfumo wao wa ushuru uliundwa kimsonge kama piramidi, kijiji kikiwa chini na makao ya mfalme katika kilele. Afisa mkuu na kiongozi wa jeshi walisimamia ukusanyaji wa ushuru katika himaya nzima, wakituma timu za wakusanyaji maalumu kwenda katika majimbo na vijiji mbalimbali.

Warozvi walibuni mfumo wa kidini uliokuwa tofauti kabisa na ule wa *mondhoro* ulioenea miongoni mwa Washona wa kaskazini na mashariki. Madhehebu ya Warozvi ya muungu-wa kikahini aliyeitwa Mwari, yalikitwa katika imani ya Mungu mkuu ambaye alijieleza kupitia katika tukio la asili kama vile umeme au tetemeko la ardhi. Maafisa wakuu wa kahini wa Mwari walikuwa ni Kinywa, Sikio na Jicho,

ambao madhumuni yao makubwa yalikuwa ni kukusanya taarifa. Madhehebu ya Mwari yalitumiwa na watawala wa Warozvi kwa malengo ya kisiasa.

Ufanisi uliovuma wa jeshi la Warozvi unahitaji maelezo ya ufafanuzi. Wachunguzi wa Kireno, katika karne ya kumi na nane, hawakuacha kuajabia nidhamu na ufanisi wa majeshi ya Warozvi, ambayo kwa jumla yalikuwa na pinde na mishale, sime, mikuki, mashoka ya kivita na marungu ya kutosha. Kama majeshi mengi katika jamii za Kiafrika za kabla ya ukoloni, majeshi ya Warozvi yalifanya miviga fulani iliyotia ujasiri na kujiamini kabla ya kwenda vitani. Wareno walitokea kuamini kwamba mfalme wa Warozvi alikuwa na "mafuta ya kichawi ambayo angeweza kuyatumia kumuua mtu yeyote kwa kumgusa tu nayo;" na hapana shaka kwamba imani hii ilikuwa na dhima kubwa katika ushindi wa Warozvi kijeshi, hususan ushindi wa *Changamire* wa Dombo dhidi ya Wareno katika vita vya Maungwe mnamo mwaka 1684.

Ujasiri wa majeshi ya Warozvi unaweza pia kuelezwa kwa mafunzo makini waliyopata askari. Majeshi ya Warozvi yalipangwa na kufunzwa kwa mtindo wa majeshi ya Wazulu, Wandebele na Wasotho ya mwanzoni mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa.

Hali nyingine ya jeshi la Warozvi ambayo imekuzwa sana ni ile ya kutoshindika. Kwa mfano, kushindwa kwa Wareno mwishoni mwa karne ya kumi na saba lazima kutazamwe katika muktadha wa kuwepo kwa Wareno katika Afrika Mashariki na Kati katika kipindi hiki. Wareno walikuwa wakipigana ili kujinusuru katika pwani ya Afrika Mashariki kutoka miaka ya 1650 hadi mwaka 1729, wakati ngome yao huko Mombasa ilipoharibiwa na sultani wa Oman. Kwa maneno mengine, kile walichokabiliana nacho *Machangamire* kusini mwa Zambezia hakikuwa nguvu kamili ya kijeshi ya Wareno.

Juhudi za kijeshi za Wareno kusini mwa Zambezia, kwa hakika, zilikitwa katika ma-*prazero*, ambao wenyewe walikuwa wametengana vibaya kutokana na maslahi ya kiuchumi yaliyogongana. Kama mambo haya hayatiliwi maanani, ni rahisi kukuza mno ufanisi wa chombo cha kijeshi cha Warozvi.

## *Uchumi*

Matawi makuu ya uzalishaji miongoni mwa jamii za Washona yalikuwa ni kilimo, ufugaji, uwindaji, ukusanyaji, uvuvi na ufuaji chuma pamoja na biashara ya masafa marefu na baina ya kanda.

### Kilimo

Washona walilima nafaka kuu tatu: ulezi, wimbi uliostahimili ukame na aina mbalimbali za mtama. Kitengo cha uzalishaji kilikuwa kaya, na hakuna ushahidi wa kutosha wa kuonyesha kwamba mgawanyo wa kazi ulikitwa katika tofauti za kijinsia. Ushahidi mdogo uliopo unadokeza kwamba hali ilitofautiana toka jamii hadi jamii. Katika baadhi ya jamii, wanaume walifanya kazi nzito na wanawake kazi nyepesi,

zaidi kwa moyo wa ushirikiano kuliko katika misingi ya mgawanyo wa kazi. Hata hivyo, katika jamii nyingine, kama ile ya Wahlengwe wa tambarare za chini, kulikuwa na mgawanyo wa kazi, watu wazima wanaume wakiwa wanatumia muda mwingi kutega na kuwinda wanyama hali vijana wakichunga mifugo na wanawake wakilima mashamba.

Majira ya kilimo yalianzia Septemba hadi Novemba, jembe ndilo lilikuwa zana kuu ya kilimo. Kulikuwa na kilimo cha kuhamahama, ambapo ardhi kongwe iliachwa pale ilipochoka na ardhi mpya kuanza kutumiwa. Kutumika kwa ardhi mpya kulifanyika kwa kufyeka vichaka na kuvichoma ili majivu yake yarutubishe udongo. Kilimo cha Washona, kama chumi nyingi za kilimo za kabla ya ukoloni, kilioanishwa na mazingira ya sehemu inayohusika.

Kipindi cha kutoka mwaka 1500 hadi mwaka 1800 kilishuhudia kuanzishwa kidogokidogo huko kusini mwa Zambezia kwa mazao mapya kutoka Ulaya na Asia, hasa katika mwambao na katika maeneo ambako Wareno walikuwa wamejenga makazi yao. Huko Sofala na katika Zambezi ya chini, wakulima wadogo wa Kiafrika walilima mpunga na viazi vikuu, ingawa hivi hakiwahi kuwa vyakula vyao vikuu. Pia walilima miwa kwa ajili ya kutafuna badala ya kutengeneza sukari, kwa kuwa walikosa utaalamu na vifaa. Wakulima wadogo wa Kiafrika pia walipanda miti mingi ya matunda kutoka India na Ureno kama vile mitini, minanasi, mipera, mipapai na michungwa; pia walipanda matikiti, matango, viazi vitamu na milimau. Kilimo cha matunda ya kigeni kilichochewa na mahitaji yake kutoka kwa wafanyabiashara wa kigeni waliosafirisha nje malimau hasa kupeleka huko India.

Kuna ushahidi kwamba ngano ilikuwa ikilimwa katika ufalme wa Manyika kwenye miezi ya Aprili na Mei, na kwamba kufikia mwaka 1778, karanga zilikuwa zikilimwa hapo. Aina mbili za jamii ya kunde - njugu mawe na kunde - zililimwa kila mahali.

Hakuna mazao yaliyoingizwa kutoka Ulaya na Asia yaliyowahi kutumiwa kama vyakula vikuu na Washona. Hali ilikuwa tofauti na mahindi ambayo yaliingizwa kusini mwa Zambezia katika karne ya kumi na nane. Zao hili polepole liliyafikia mazao ya ulezi na mtama na kuwa mojawapo ya vyakula vikuu vya Washona katika karne ya ishirini, hususani, miongoni mwa wakazi wa mijini.

## Nyanga na tambarare za chini

Uchumi wa kilimo wa Nyanga na maeneo ya tambarare za chini, kwa namna nyingi, ulikuwa tofauti na ule wa uwanda wa juu. Nyanda za juu za Nyanga zilikuwa na ardhi isiyo na rutuba na miinuko mikali. Sehemu kubwa ya Nyanga ya kaskazini iliwekewa matungazi ya kuta kavu za mawe za urefu wa mita moja. Matungazi haya yaliwekwa katika mitelemko na madhumuni yake yalikuwa ni kuhifadhi udongo na kuondoa mawe kwa unadhifu. Kuna ushahidi kiasi kwamba kiasi kidogo cha umwagiliaji kilifanyika, lakini kama nyongeza tu, kwani eneo la Nyanga likipata mvua ya kuridhisha kwa mwaka. Yaelekea kwamba umwagiliaji wa majira ya

kiangazı wa oustani za mboga, mahindi na migomba, ambao bado unafanyika katika eneo hili, ni desturi ya kilimo yenye asili ya karne ya kumi na nane.

## Uchumi wa tambarare za chini

Uchumi wa tambarare za chini ulikuwa tofauti. Hapa wenyeji, waliojulikana kama Wahlengwe, waliwinda, kukusanya (kuhemea) na kuvua, na kilimo kilifanyika kwa kiasi kidogo tu. Tambarare za chini zinapata mvua kidogo sana kwa mwaka, hivyo ukusanyaji ulikuwa na dhima muhimu sana katika uchumi wa tambarare za chini, kama ulivyo hata wakati huu. Matunda yaliyokusanywa yalikuwa ni *nkanyi* na *mahanga,* ambayo utomvu wake ulitumika kutengeneza mvinyo unaolewesha uliojulikana kama *kwaka,* na ubuyu. Matunda haya yalikusanywa na wanawake na watoto hali wanaume waliwinda wanyama wakubwa. Wanawake na watoto waliua panya na kukusanya viwavi wakubwa wa rangi ya fedha na nzige.

Wahlengwe walikuwa kama walivyo hadi leo, wawindaji wazuri; na kulikuwa na aina nyingi za wanyama katika tambarare za chini. Uvuvi pia ulikuwa kazi muhimu. Mito ya tambarare za chini, wakati huo na hadi sasa, ina samaki wengi. Eneo la Nyanga ni maarufu kwa samaki wake.

Uwindaji na uvuvi havikuwa ukiritimba wa Wahlengwe katika tambarare za chini. Katika sehemu mbalimbali za himaya ya Mutapa, wanaume waliwinda aina zisizohesabika za wanyama, wakiwemo simba, chui milia, chui, vifaru, tembo, nyati, ng'ombe mwitu, pofu na kongoni, kwa kuwataja wachache. Kanga walipatikana kwa wingi katika vichaka karibu na mashamba. Wawindaji wataalamu walitumia mitego na silaha za jadi (kama mikuki, rungu na pinde na mishale). Tangu kuingizwa kwa bunduki na Wareno mnamo karne ya kumi na sita, ufanisi wa wawindaji uliboreka.

Wahlengwe hawakuwa wawindaji tu. Uwezo wao wa kutofautisha aina mbalimbali za udongo unaonyesha kwamba walikuwa wakulima makini. Wahlengwe walitofautisha udongo kutokana na uwezo wake wa kuhodhi unyevu. Udongo wa kichanga walipojengea viunga vyao, waliuita *nthlava*. Udongo huu ulikuwa mzuri kwa kilimo cha matango, vibuyu, kunde, njugu mawe na karanga. Walilima pia ulezi na mtama hapo, lakini katika au karibu na mabonde. Udongo mweusi wa miamba ya volkano, waliuita *tsovolo*: huu ulikuwa udongo wenye rutuba unaohodhi unyevu kwa kipindi kirefu, na ambao waliutumia kulimia mahindi na aina mbalimbali za mboga. Yaelekea kwamba Wahlengwe hawakuwahi kukosa ardhi na walibanwa tu na mvua zisizokuwa za hakika.

Wachunguzi wa Kireno walitoa maoni yaliyohitilafiana kuhusu ufanisi wa chumi za kilimo za jamii za Washona kati ya mwaka 1500 na mwaka 1800, wakati wanahistoria wamekuwa na mwelekeo wa kutoa maelezo ya jumla kuhusu njaa katika eneo la kusini mwa Zambezia kabla ya na wakati wa ukoloni. David Beach ameeleza kilimo cha Washona cha kabla ya ukoloni kama "cha kufaa lakini kilichodumaa vibaya." Hii, kwa mujibu wa maelezo yake, ilikuwa ni kwa sababu hakukuwa na uchaguzi wa mazao na ardhi na utaalamu wa kubashiri *shangwa* (njaa) haukuwepo ili

kuepuka mabaa haya, yawe yale yaliyosababishwa na hali ya hewa, nzige au maafa mengine. Lakini jamii za Washona hazikuwa "zimetuama." Zilikuwa zina mawasiliano miongoni mwao na vilevile na jamii nyingine za Kiafrika zilizokuwa jirani kama vile Waswahili na Waarabu tangu karne ya kumi au mapema zaidi, na Wareno tangu mwanzoni mwa karne ya kumi na sita. Kwa Washona, mawasiliano haya yaliwakilisha juhudi za kurekebisha hali zao za kimaisha kwa njia ya mabadilishano ya bidhaa kwa bidhaa na biashara. Zaidi ya hayo, wakulima wadogo wadogo wa Kishona walikuwa wakipokea mazao mapya kwa kipindi chote tangu mwaka 1500 hadi mwaka 1800. Yote haya hufanya iwe vigumu kuueleza uchumi wa kilimo wa kabla ya ukoloni kuwa ulikuwa "umetuama." Historia ya kilimo ya kipindi cha kabla ya ukoloni ni hadithi ya ubunifu badala ya kutuama.

Aidha, wazo kwamba wakulima wadogo wadogo wa Kishona walikuwa hawajiwezi wakati wa ukame na njaa limepitwa na wakati. Kulikuwa na mbinu kadhaa za kupiga vita njaa kama vile kubadilishana chumvi, nyama, samaki, pembe za ndovu, mikeka, vyungu, vikapu, mikuki, mishale na vito kwa nafaka. Washona pia walipata nafaka wakati wa njaa kupitia mfumo ulioitwa *ukomondera,* ambapo mtu alikopa nafaka kwa maelewano kwamba ingerudishwa bila riba katika majira mazuri yanayofuata. Mwisho, uwindaji, uvuvi na ukusanyaji havikutoweka baada ya kuingizwa kwa mazao mapya, na viliendelea kuwa njia muhimu ya kuzuia njaa.

Richard Mutetwa ameonyesha kwamba tatizo la maghala ya kuhifadhi mazao halikuwa baya sana kwa sababu vyakula vikuu vitatu vya Washona, yaani ulezi, wimbi na mtama, viliweza kuhifahika kwa muda wa zaidi ya miaka mitatu au minne. Wakulima wadogowadogo wa Kishona pia walichukua hadhari ya kuhifadhi nafaka yao dhidi ya unyevu, kwa kukandika kwa uangalifu vilindo vyao vya nafaka na kuzuia hewa isiingie. Vilindo hivyo viliwekwa kwenye miamba au juu ya nguzo ndefu ili kuepuka mchwa. Kilimo cha Kishona cha kabla ya ukoloni kinapowekwa sambamba na hali ya ufanisi wa kilimo iliyokuwepo kwingineko Afrika, inaonekana kwamba hakuna sababu za kutosha za kudai kuwa kilimo cha Washona hakikuweza kutosheleza mahitaji ya wakulima wadogo wadogo.

## Ufugaji

Ufugaji ulikuwa tawi muhimu la uzalishaji katika himaya ya Mutapa na ile ya Warozvi. Ufugaji ulikuwa ni ule wa kondoo, mbuzi na ngombe. Hawa wanyama walitoa nyama, maziwa na mbolea ambayo wakulima ama walitumia au waliuza. Kumiliki ng'ombe nako kulikuwa na dhima ya kijamii ya kumpa hadhi mhusika. Nyaraka za Wareno zinasisitiza dhima kuu ya ng'ombe katika uchumi wa himaya ya Mutapa na wa himaya ya Rozvi. Makundi makubwa ya ng'ombe yalishamiri, hususani katika tambarare za juu ambako yalikuwa hayatishiwi na mbung'o. Kuna kila uwezekano kwamba watawala wa Mutapa na *Machangamire* wa Rozvi walihamisha ng'ombe kutoka tambarare za juu kwenda tambarare za chini wakati wa majira ya kiangazi wakati maji na chumvi vilikuwa pungufu na machungo

kutotosheleza katika tambarare za juu. Uhamishaji huu pia uliwawezesha wachungaji na wakulima kukutana na kubadilishana mazao yao: mazao ya mifugo kwa nafaka. Migogoro mara chache ilizuka baina ya wachungaji na wakulima pale ng'ombe walipoharibu mazao ya wakulima. Hii nayo ilisababisha kusogezwa kwa mzingo wa uhamishaji au uhamaji kwenda katika maeneo mapya kabisa - hivyo ndivyo namna wachungaji walivyoyakalia maeneo mapya.

Si akiolojia wala nyaraka za Waıeno zinatueleza ya kutosha kuhusu usimamizi wa ng'ombe na msambao wao tangu karne ya kumi na sita hadi mwishoni mwa karne ya kumi na nane. Vyanzo vya Wareno vimeendelea kutaja ukweli kwamba Zambezia ya kusini ilikuwa tajiri kwa ng'ombe na wanyama wengine. Mwanzoni mwanzoni mwa miaka ya 1500, Diogo de Alcacova aliandika kwamba ng'ombe 4,000 wasio na pembe walilipwa kama ushuru kwa mtawala wa Mutapa na mtawala wa Butwa huko kusini-magharibi. Mnamo mwaka 1569, Padri Monclaro alifananisha umbile kubwa la ng'ombe wa Butwa na lile la maksai wa Ufaransa.

Mbali na ng'ombe, wakulima wadogowadogo wa Kiafrika walifuga mbuzi, kondoo na kuku kwa ajili ya chakula na mabadilishano.

## Uchimbaji wa metali: chuma na shaba

Kiasi kikubwa cha chuma, shaba na risasi kilikuwa kikichimbwa kote katika himaya ya Mutapa na ya Rozvi, ingawa maandishi yaliyopo hufanya mtu aamini kuwa wakulima wadogowadogo walipendelea tu kuchimba dhahabu. Wakulima wadogowadogo wa Kiafrika walichimba chuma ambayo waliitumia kutengeneza vitu kama majembe, mikuki na mashoka. Wanjanja wa Wedza walipata sifa kama watengenezaji wa majembe, wakiuza majembe sehemu za mbali kama Manyika, Bocha, Burbera na nchi ya Nidau. Pia walichimba shaba ambayo waliitumia kutengeneza mabangili ambayo wanaume na wanawake walivaa mikononi na katika vifundo vya miguu. Uchunguzi wa kijiolojia uliofanywa mnamo mwaka 1952 ulionyesha kwamba tano kwa nne ya uzalishaji wote wa shaba huko Zimbabwe ulitoka Duma. Hata hivyo, kiasi kikubwa pia kilitoka Urungwe huko kaskazini-magharibi.

## Chumvi

Tasnia ya chumvi nayo ilikuwa muhimu sana kwa uchumi wa Washona kati ya mwaka 1500 na mwaka 1800, hususani katika maeneo ambayo hayakuwa na mvua za kutosha kulima mazao na kufuga ng'ombe kama vile Save ya kati. Eneo hili pia lilikuwa na udongo wa mfinyanzi mwingi, na wenyeji walinufaika na rasilimali hii kwa kubobea katika utengenezaji wa vyungu. Chumvi na vyungu vilibadilishwa kwa nafaka, hususani katika miaka ya njaa.

## Nguo

Uzalishaji wa nguo pia ulikuwa shughuli muhimu miongoni mwa wakulima wa

Kishona wa kusini mwa Zambezia. Ulimaji wa pamba na ufumaji ulishamiri zaidi katika ukingo wa mashariki wa mto Zambezi. Washona walifuma nguo kutokana na pamba hii na pia kutokana na gome la mbuyu. Eneo la tambarare za chini la ulimaji pamba lilijazilizwa na eneo la tambarare za juu ambalo lilikuwa na ng'ombe wengi, na hii kwa kiasi kikubwa ilibainisha ruwaza ya biashara kati ya maeneo.

*Dhahabu na fedha*

Kuwepo na kuchimbwa kwa fedha tangu karne ya kumi na sita hadi ya kumi na nane, ni jambo lililokisiwa kwa kukuzwa mno miongoni mwa mamlaka za Wareno, lakini katika kipindi chote kinachopitiwa au hata baadaye, hakuna migodi ya fedha iliyoonekana. Fedha kwa hakika ilipatikana kama pato la ziada la uchimbaji dhahabu, na kulikuwa na dhahabu nyingi katika tambarare za juu, huko Burwa sehemu za kusini magharibi na huko Manyika na Uteve sehemu za mashariki.

Kiasi cha dhahabu huko kusini mwa Zambezia kilikuwa kimekuzwa sana na Wareno katika karne ya kumi na sita. Kwa mfano, ilidaiwa kwamba "Mukaranga" yote haikuwa kitu kingine bali mgodi wa dhahabu na mtu alipaswa tu kuchimba kwa jembe na angepata dhahabu. Hata hivyo, kwa hakika kulikuwepo dhahabu nyingi katika himaya ya Mutapa, na mbali na yale waliyoyasema, Wareno waliona matumaini yao yakitimizwa hadi nusu ya pili ya karne ya kumi na saba.

Marejeo ya kihistoria yanadokeza kwamba uchimbaji madini haukuwa shughuli iliyoendeshwa kwa mwaka mzima kwa Washona, isipokuwa katika ufalme wa Manyika huko Mashariki, ambako uchimbaji ulifanywa kwa mwaka mzima kwa sababu mito iliyoko huko haikauki. Shughuli za uchimbaji madini za Washona zilifanyika katika miezi ya Agosti, Septemba na Oktoba, miezi ambamo ardhi ilisafishwa. Sababu nyingine ya kuchimba madini katika miezi hii ilikuwa kwamba wachimbaji wangeweza kuchimba kina kirefu kutokana na kushuka kwa usawa wa maji ya chini ya ardhi.

Shughuli za uchimbaji madini zilifuata ruwaza iliyoenea katika sehemu kubwa ya kusini mwa Afrika. Vyombo muhimu vilivyotumika kubomoa mgodi vilikuwa nyundomawe na mitaimbo ya chuma, na vilevile aina ya nondo iliyotengenezwa kwa kipande cha chuma kilichochomekwa kwenye ncha ya fimbo nzito. Mbinu ya uchimbaji wa mwamba wa dhahabu ilikuwa ni uwashaji moto, kama inavyoonekana kutokana na kiasi kikubwa cha mkaa ambao Roger Summers aliukuta katika migodi mingi ya kale. Katika mgodi mmoja alikuta vihori vyenye mkaa vikisimama katika uso wa mwamba. Kwa mujibu wa maelezo yake, vilifanya meko iliyoelekeza joto kwenye uso wa mwamba mgumu. Kwa kupoza mwamba uliotiwa joto kwa haraka kwa maji, Washona waliweza kupasua uso wa mwamba. Vipande vilivyokusanywa namna hiyo vililundikwa katika malundo ya kuni na kuokwa na baada ya hapo kwatzi iliyounguzwa ilipondwa na dhahabu kusafishwa kutokana nayo.

Kwa upande wa dhahabu ya tope, utaratibu wa kupatikana kwake ulikitwa vijijini. Katika majira ya uchimbaji madini, makundi ya wachimbaji 400 au zaidi na

wanawake na watoto wao, walikusanyika mahali palipoteuliwa wakiongozwa na mkuu wa kijiji. Walisafisha tope kwenye mabakuli yaliyotengenezwa kwa miti, na dhahabu iliyopatikana iliwekwa katika matete au manyoya tayari kwa kubadilishwa. Wakulima wadogowadogo walipendelea zaidi usafishaji dhahabu kuliko uchimbaji wa miambani kwa kuwa sehemu zilizochimbwa zilikuwa na kina kifupi na hazikuwa ghali. Wala sehemu hizo hazikuhatarisha maisha ya wachimbaji kama ilivyokuwa kwenye mashimo yalichimbwa katika udongo laini ambayo yaliporomoka mara kwa mara.

Watawala wa Mutapa na Warozvi waliweka udhibiti mkali katika uzalishaji wa dhahabu kwenye himaya zao. Imekadiriwa kwamba karibu asilimia 50 ya uzalishaji wa dhahabu katika himaya ya Mutapa ilichukuliwa moja kwa moja na tabaka la juu la watawala. Kama mtu aligundua mgodi wa dhahabu, alitakiwa kuufunika na kupeleka taarifa mara moja kwa chifu wa mahali hapo. Kushindwa kutii sheria hii adhabu yake ilikuwa kifo. Watawala wa Mutapa na Rozvi hawakutaka Wareno wajue ilipo migodi ya dhahabu, kwa kuwa hii ingewashawishi watake kutamalaki: aidha, udhibiti wa migodi uliwawezesha kupata maslahi mazuri zaidi katika biashara.

## Kupungua kwa uzalishaji wa dhahabu katika karne ya kumi na saba

Hali ya hatari ya uchimbaji dhahabu inaeleza ni kwa nini uzalishaji ulikuwa mdogo na kwa nini ulipungua katika karne ya kumi na saba. Aidha, usawa wa maji ardhini ulipofikiwa, haikuwezekana kuchimba chini zaidi bila msaada wa teknolojia mpya inayoweza kusukuma nje maji na tope. Mwisho, bei ambayo wafanyabiashara wa Kireno walilipa kwa dhahabu ilikuwa ya chini sana kuweza kuwashawishi wakulima kuhatarisha maisha yao.

Kipengele kimoja ambacho hakijachunguzwa kwa undani ni athari ya vita juu ya uzalishaji wa dhahabu. Nusu ya kwanza ya karne ya kumi na saba ilishuhudia kilele cha mashambulizi ya Wareno dhidi ya himaya ya Mutapa. Kuingilia kwa Wareno katika siasa za ndani za Washona kulisababisha vita miongoni mwa watawala wa Mutapa wenyewe na pia kati ya watawala wa Mutapa na watumwa wao. Vita hivi vilisababisha uhamaji wa muda na wa kudumu na njaa, hata katika maeneo yaliyokuwa na utajiri wa rasilimali na yenye ruwaza nzuri ya hali ya hewa. Nusu ya pili ya karne ya kumi na saba ilikuwa na vita vya *changamire* vya uharibifu zaidi ambavyo vilisababisha kujizatiti upya kwa watu kuunda madola kadhaa. Kwa hivyo, vita vinaweza vikalaumiwa kwa kuvuruga uzalishaji wa dhahabu katika nchi ya Washona katika karne ya kumi na saba kwa namna ile ile ambavyo mabaa ya asili yalivuruga kilimo kwa kupunguza kiasi cha ardhi kilichokuwepo.

Zaidi ya hayo, mbinu zilizotumiwa na wafanyabiashara wa Kireno ziliwatenga na wakulima ambao ndio walihusika zaidi na uzalishaji wa dhahabu. Mwanzoni mwanzoni mwa miaka ya 1500, wakulima wa Kiafrika walikuwa wakipeleka mazao yao moja kwa moja kwa ma-*feira* wa Kireno waliokuwa bara. Hata hivyo, baadaye katika karne hiyo, Wareno waliwatuma watu wa kati ndani ya nchi ambao walipeleka

bidhaa hadi milangoni mwa wakulima. Waliuza bidhaa kwa mkopo kwa wakulima ambao mara nyingi hawakulipa, matokeo yake yakawa ni mkwepaji kufanywa mtumwa. Mahusiano baina ya Wareno na wakulima wa Kiafrika yalizorota hadi kufikia kutishia maisha vijijini. Katikati ya miaka ya 1600, mfalme wa Uteve aliwaamuru watu wake wasichimbe dhahabu tena bali walime na kupanda mazao ya chakula ili wawe matajiri na kupata amani zaidi na utulivu. Kwa hiyo, vipengele vya kijamii pengine vilikuwa muhimu katika kufifisha uzalishaji wa dhahabu katika karne ya kumi na saba.

## Biashara

Kumbukumbu za biashara pia zinatoa ushahidi wa kihistoria wa tofauti katika chumi za wakulima wadogowadogo wa Kishona. Lengo kubwa la wakulima lilikuwa ni kuzalisha vitu vya matumizi badala ya bidhaa za mabadilishano. Lakini uzalishaji wa bidhaa ulilazimika kuwa wa mabadilishano ya mazao baina ya wakulima wenyewe na baina ya wakulima na mafundistadi, na hii ilisababisha kuibuka kwa biashara ya kikanda.

Wafanyabiashara wa Kiswahili walianzisha maduka kadhaa katika himaya ya Mutapa. Maduka ya kwanza huko Sofala na sehemu jirani pengine yalianzishwa katika karne ya kumi, wakati wafanyabiashara wa Kiswahili na Kiarabu walipoanza kufanya biashara na wakulima katika himaya ya Mutapa. Maduka yalifunguliwa siku za Jumatatu, wakulima wa Kiafrika wakibadilisha mazao yao ya kilimo kwa shanga, nguo na vitu vingine vya kigeni. Mahitaji ya vyakula lazima yaliongezeka Wareno walipoanzisha ngome huko Sofala mwaka 1506, ngome ambayo ilitokea kuwa kituo cha biashara ambapo wakulima wa Kiafrika walikuja kuuza mazao yao kwa wafanyabiashara wa Kireno.

Kuanzishwa kwa ngome hii lazima kutazamwe katika muktadha wa shughuli za kibiashara za Wareno tangu mwaka 1498. Lengo kuu la Wareno wakati huu lilikuwa ni kukalia sehemu zote muhimu katika Bahari ya Hindi. Ngome za Sofala na Kilwa zilijengwa mnamo mwaka 1506 kulinda biashara ya dhahabu, wakati ngome nyingine tatu zilijengwa kulinda biashara ya pilipili. Walipofika Sofala mwaka 1506, Wareno waliwakuta wafanyabiashara wa Kiswahili na Kiarabu wakiwa wamejiimarisha, na ushindani kati ya makundi haya mawili ambao ulikuwa umetokea mara kadhaa kijeshi, hatimaye ulikua. Wareno walishinda, na Waswahili na Waarabu walikimbilia kaskazini kwenye sehemu muhimu katika mto Zambezi ambako waliendelea kuhujumu shughuli za kibiashara za Wareno. Wareno walijibu kwa haraka kwa kuwafukuza kutoka katika idadi kubwa ya sehemu hizi na, mnamo mwaka 1531, wakaanzisha Sera na Tete kama vituo vyao vikubwa vya biashara. Kwa hiyo shughuli za kibiashara za Kireno zilisogea kaskazini, na hivyo kupunguza umuhimu wa eneo la Sofala.

Kushindwa kwa Waswahili mnamo mwaka 1512 na kukaliwa kwa Sera na Tete kulimaliza biashara huru ya Waswahili na Waarabu. Lakini kwa kuwa Wareno

hawakuwa na stadi wala watu waliohitajika, na kwa kuwa Waswahili na Waarabu walikuwa na shauku ya kuendelea kama wafanyabiashara katika eneo hilo, ushirikiano wa asili japo wa mashaka ulikua baina yao. Katika karne ya kumi na saba yote, Waswahili na Waarabu walikuwa mawakala wakubwa wa wafanyabiashara wa Kireno huko ndani ya nchi. *Vashambadzi* (wafanyabiashara) wa Kiafrika walikuwa watu wa kati muda mrefu kabla ya ujio wa Wareno, na dhima yao ilisimikwa rasmi katika ushirikiano.

Kushindwa kwa Waswahili na Waarabu kuliwaacha wafanyabiashara wa Kireno bila ushindani mkubwa katika njia ya biashara ya Zambezi na ndani ya nchi. Mwanzoni lengo la mfalme wa Wareno lilikuwa ni kuwa na ukiritimba wa biashara yote katika Sofala na ndani ya nchi, lakini hii haikuwezekana, kwa kuwa tamaa iliwapeleka wafanyabiashara bara kwenda kuweka mikataba huru na watawala wa Kiafrika.

Kama ilivyokuwa kwa wafanyabiashara wa Kiswahili na Kiarabu, wakulima wa Kiafrika walibadilishana mazao yao kwa vitu mbalimbali vya kigeni. Machimbo ya kiakiolojia ya Peter Garlake ya ma-*feira* ya Luanze, Dambarare na Rwinuka yanaashiria kwamba shanga zilikuwa bidhaa maarufu sana mwanzoni mwanzoni mwa karne ya kumi na sita. Shanga zilizokuwa zikitafutwa sana katika falme zote zilikuwa ni zile nyekundu na nyeusi zilizojulikana kama shanga za Kambay. Kulikuwepo pia shanga tofauti tofauti zilizoingizwa kutoka nje zikiwemo zile za marijani, fuwele, pyuta, jeti, kaharabu na kioo cha bluu cha Kivenisi, lakini hizi hazikupendwa sana. Kinyume chake, aina iliyotengenezwa kienyeji iliyojulikana kama *caracoes* (shanga ndogo za mawe) ilijaa sokoni kati ya mwaka 1516 na mwaka 1518. Nguo zilikuwa bidhaa nyingine muhimu za biashara, hususani nguo zenye rangi ya kung'aa zilizokuwa zikipimwa kwa urefu wa mkono.

Kwa kubadilishana na bidhaa hizi, Washona walileta katika soko la ngome au kwenye ma-*feira*, mtama mahindi, njugumawe, kunde, vikapu, mikeka, vyungu, mayai, asali, wanyama na ndege waliokamatwa kwa mitego na aina nyingi za mboga na matunda mwitu. Wahunzi wengi, wachonga vinyago na wachimba madini walibadilisha bidhaa ama miongoni mwao au na wafanyabiashara wa Kireno. Wakulima wakubwa walipata masoko kwa ajili ya ng'ombe, kondoo na nguruwe wao. Ngome ya Sofala na ma-*feira* ya bara yalijiimarisha sana katika jamii ya Washona na yakawa sehemu muhimu ya muundo wake wa kiuchumi na kijamii.

## Ma-*Feira* katika nchi ya Washona

Kipindi cha miaka ya 1575 hadi 1684 kilishuhudia mabadiliko katika ruwaza ya biashara baina ya wakulima wadogo wadogo wa Kiafrika na wafanyabiashara wa Kireno. Wafanyabiashara wa Kireno waliimarisha ushindi wao wa kibiashara na kijeshi juu ya Waswahili na Waarabu kwa kuchukua na kuyarekebisha na kuyageuza maduka (ya Waswahili na Waarabu) kuwa ma-*feira* ya Kireno. Baada ya muda, ma-*feira* yakawa sehemu muhimu katika mabadilishano ya Kiafrika na Kireno. Kila *feira*

lilikuwa na ngome, kikosi cha askari kumi hadi kumi na watano, kinadharia – kanisa na kasisi, na *capitão-mar* (wakala wa wafanyabiashara wa Kireno katika gulio kuu – *feira*). Ma-*feira* mengine yaliendeshwa na serikali ya Mito ya Sena, wakati mengine yalimilikiwa na watu binafsi. *Capitães-mores* (mawakala) walifanana na walinzi wa ma-*feira* wa Kireno wa enzi za kati. Nafasi ya *capitão-mor* katika nchi ya Manyika, Burwa na Karanga ililingana na ile ya *capitao-mor dos Banianes* katika kisiwa cha Msumbiji. Malipo yao yalichukuliwa tu kama ruzuku na ilikuwa sera ya watawala wa Kireno kuwateua tu watu matajiri kutoka makazi ya Kireno ya Sena kushika nafasi hiyo. Majukumu ya *capitães-mores* yalihusu utozaji kodi, udhibiti wa bei, usuluhishi baina ya wafanyabiashara wa Kireno na Kiafrika, kutoa leseni, kulinda misafara, kuandikisha askari na kutekeleza sheria kuhusu uzito na vipimo. Mamlaka na majukumu haya yalirekebishwa sana kadri *capitães-mores* walivyoingiliana na watawala mbalimbali wa Kiafrika.


## Ma-*feira* makuu

*Feira* ya Dambarare ilitangazwa kuwa ndiyo nzuri kupita ma-*feira* yote kwenye eneo la Mito ya Sena, ambako karibu wafanyabiashara matajiri wote wa Sena walifanyia biashara. Ilikuwa safari ya siku tatu kutoka Angwa, ambako kulikuwa na dhahabu nyingi lakini wakazi wachache, kwa kuwa ilikuwa mbali mno kutoka Sena na Tete.

Huko Uteve, Wareno walifanya *feira* ya mwaka huko Bandire kununua vifaa kutoka ndani ya nchi. *Feira* hii ilidumu tangu karne ya kumi na sita hadi ya kumi na nane, wakati mamlaka za Wateve zilipoisitisha. Mbinu zilizotumiwa na Wafalme wa Wateve kudhibiti biashara ya Wareno zilitofautiana kidogo na zile zilizotumiwa na jamii za Washona. Kwa mfano, huko Manyika, biashara ya *feira* ilidhibitiwa moja kwa moja na wafalme na mwana au binti mfalme wa eneo ambako *feira* ilifanyika. Lakini huko Uteve *feira* iliendeshwa kwa kiasi kikubwa na *inyamasango* (kiongozi wa kijiji) ambaye utawala wa Bandire ulikuwa chini ya mamlaka yake.

Wareno hawaelekei kuwa waliunda ma-*feira* yoyote kaskazini mwa Zambezi hadi mwanzoni mwanzoni mwa karne ya kumi na nane, wakati Zumbo na Michonga zilipoanzishwa. Sababu mbili zinaweza zikaeleza uanzishwaji wa baadaye wa ma-*feira* haya mawili ya mwisho: kugunduliwa kwa *bares* (migodi) kaskazini mwa Zambezi katika karne ya kumi na nane, na haja ya Wareno ya kutafuta sehemu nyingine kwa ajili ya biashara baada ya kufukuzwa kutoka nchi ya Washona na maliki wa Rozvi, Dombo Changamire kati ya mwaka 1693 na mwaka 1695.

Kufukuzwa kwa Wareno kutoka katika ma-*feira* yao na *changamire* kuliwalazimisha Wareno kugeukia mbinu za biashara walizotumia katika karne ya kumi na sita. Hata hivyo, waliweza kufufua *feira* ya Masekesa huko Manyika mnamo mwaka 1719, lakini si ile ya Uteve. Mfumo wa kuwa na afisa mmoja wa kuratibu mahusiano ya Wareno na watawala wa Kiafrika haukuwezekana tena kuhusiana na wafalme wa Mutapa, kwa kuwa hakukuwa na mamlaka kuu makini tena. Kwa hiyo ni lazima kuchunguza kwa ufupi mahusiano baina ya Wareno na baadhi ya watawala




**22.3** *Ma*-feira *makuu ya karne za kumi na sita na kumi na saba (imetokana na ramani ya 3 ya H.H. K. Bhila,* Trade and Politics in a Shona Kingdom. The Manyika and their African and Portuguese Neighbours, 1575-1902. *Imerekebishwa kwa idhini na hisani ya Longman Group, UK, Ltd)*

muhimu wa Kiafrika katika karne ya kumi na nane.

Huko mashariki, mfalme wa Uteve hakuwaruhusu Wareno kuchimba dhahabu katika migodi kwenye ufalme wake. Hata hivyo, raia wake waliweza kununua nguo na shanga kutoka kwa walowezi wa Kireno huko Sena. Hata katika biashara hii wafanyabiashara wa Kireno walitumia sehemu kubwa ya faida yao kujaribu kununua usalama. Sera ya Wateve katika karne ya kumi na nane ilikuwa dhidi ya Wareno. Katika ufalme wa Manyika, wafanyabiashara wa Kireno walipewa uhuru wa kupita kote nchini, lakini shughuli zao za kibiashara zilidhibitiwa vikali na watawala ambao *capitão-mor* na wafanyabiashara wa Kireno walikuwa wakiwalipa kodi.

Vilevile, ili kuweka *feira* ya Zumbo na njia ya biashara kwenda Butwa salama, wafanyabiashara wa Kireno walilipa ushuru mara kwa mara kwa *changamire*, ambaye alikuwa akituma wajumbe wake hadi katika *feira* ya Zumbo, akiomba zawadi zaidi ya kodi ya kawaida. Pamoja na matumizi haya yote, njia ya biashara kati ya Zumbo na Butwa haikuwa salama kabisa. Mashambulizi maarufu ya *changamire* ya mwaka 1756-1757 ambamo alinyang'anya mali ya thamani ya *pastas* 1,000 (*cruzados* 800.000) ulikuwa mfano wa hali hiyo. Biashara ya Zumbo pia ilivurugwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe vya kila mara na njaa katika miaka ya 1760. Lakini *changamire* bado walithamini biashara yao na Wareno. Watawala wa Rozvi walituma majeshi ya mashambulizi mara tatu kwenye miaka ya 1743, 1772 na 1781 kulinda *feira* ya Zumbo isishambuliwe na watawala jirani wa Kiafrika.

Hali ya mahusiano baina ya *Mutapa* na Wareno yaonekana ilibadilika kidogo katika karne ya kumi na nane. Wareno waliendelea kuweka kikosi cha askari 20, *capitão-mor*, luteni, kapteni-jenerali na mtawa wa Kidominika katika makao ya mfalme wa Mutapa. Pamoja na mipango hii, biashara baina ya Wareno na watawala wa Mutapa iliendelea kufifia katika karne ya kumi na nane. Kufifia huku kumeelezewa katika muktadha wa maendeleo ya kusini mwa Zambezia katika karne ya kumi na nane. Kwanza, kulikuwa na kakara za kutafuta dhahabu kaskazini mwa Zambezi, majasuri binafsi wa Kireno wakigundua *bares* na kuanza kuchimba dhahabu wenyewe. Pili, uzalishaji wa dhahabu takriban ulisimama kabisa katika karne ya kumi na nane. Tatu, wafanyabiashara wa Kiafrika na Kireno katika pande zote za mto Zambezi waligeukia uwindaji wa tembo kwa ajili ya meno yake.

Biashara ya meno ya tembo ilikuwa na dhima muhimu katika himaya ya Mutapa. Maelezo ya Wareno ya karne ya kumi na sita yanatuambia kwamba tembo walizoea kuranda katika kundi karibu kama kundi la ng'ombe na kwamba kiasi cha elfu nne au tano walikufa kila mwaka. Uwindaji wa tembo haukudhibitiwa sana na watawala wa Kiafrika kama walivyodhibiti dhahabu kwa kuwa uwindaji ulifanyika katika maeneo ya mbali. Hata hivyo, taarifa kidogo sana hujulikana kuhusu muundo wake; kuna baadhi ya mambo yanayoashiria kwamba uwindaji mkubwa wa tembo katika karne ya kumi na nane ulifanyika Buhera na Rimuka.

## *Hitimisho*

Kujipenyeza kwa Wareno kusini mwa Zambezia kulimomonyoa mamlaka ya matabaka tawala ya kienyeji na kuwezesha njia za moja kwa moja za kunyonywa kwa wakulima wadogowadogo na mtaji wa kibiashara wa Kireno, na baadaye mtaji wa kitasnia wa Kiingereza.

Wafanyabiashara wa Kireno walijihusisha zaidi na biashara ya dhahabu na meno ya tembo. Matokeo yake, bidhaa kuu za biashara ya eneo - chuma, chumvi na shaba - zikashuka daraja na kushika nafasi ya pili. Lakini biashara ya masafa marefu na biashara ya eneo zilistawishana, na hii ilisababisha kuibuka kwa tabaka la wafanyabiashara wa Kiafrika, waliojulikana kama *vashambadzi*. Kwa biashara ya masafa marefu kushamiri, ilibidi kuwepo dhahabu na meno ya tembo na wachukuzi, chakula cha kuwalisha hawa wabebaji, majembe ya kulima mazao na chuma cha kutengenezea majembe. *Vashambadzi* walisafirisha, si meno ya tembo tu na dhahabu, bali pia chumvi na majembe ya chuma, waliyobadilisha kwa chakula njiani. Wakulima wa Kiafrika walioishi karibu na njia za biashara walibadilishwa polepole kadiri walivyotoa mazao ya kilimo ya ziada kwa mauzo kwa wafanyabiashara na wachukuzi wao. Ni wazi kwamba, wakulima wadogowadogo, ambao wengi hawakujua thamani ya kimataifa ya bidhaa walizouza, walinyonywa kikatili na wafanyabiashara wa Kireno.

# 23 Utegemezi na kutegemeana kusini mwa Afrika 1500 - 1800

Baina ya 1500 na 1800, sehemu kubwa ya kusini mwa Afrika ilibadilishwa. Jumuiya mpya zilifanya mastakimu katika ukanda huo; jamii nyingi za awali zilibadili taratibu zao za maisha au makazi yao, na mahusiano yaliyoibuka ndani na baina ya jamii yalikuwa ni tofauti kabisa na yoyote yale yaliyokuwepo kabla. Mengi ya mabadiliko haya makubwa yalisababishwa na mabadiliko ya mahusiano ya nje ya kusini mwa Afrika. Mzungu wa kwanza, Vasco da Gama, alipozunguka Rasi ya Matumaini Mema *(Cape of Good Hope)* mwaka 1497, Kusini mwa Afrika kulikuwa na uhusiano dhaifu sana na dunia, lakini kufikia 1800 ukanda huo ulikwisha changanyika kabisa katika sulubu za dunia nzima za biashara na mikakati. Inafaa kufikiria mabadiliko ya mazingira ya kimataifa yenyewe kabla ya kujaribu kutathmini athari zake juu ya kusini mwa Afrika.

Kwenye mwaka 1500 Afrika ya kusini mwa Sahara na mabara ya Amerika yalikuwa hayajaingizwa katika mahusiano ya kawaida na sehemu nyingine za dunia. Biashara ya kimataifa ilihusika hasa na Ulaya na Asia, na karibu yote iliendeshwa kupitia bara, kwa gharama kubwa sana. Kwa Wareno, waliokuwa wa kwanza kuanzisha njia ya bahari kuzunguka Rasi, na kwa Waholanzi, Waingereza na Wafaransa, waliowafuata kupitia Rasi, Afrika ya Kusini sana sana ilikuwa ni janga kwa mabaharia. Kuchorwa kwa ramani ya upwa wake pole pole kulipunguza kutengwa kwake, lakini bado kuna haja ya kuchunguza kwa nini wafanyabiashara wa Kiarabu na wa Kizungu hawakuwa na shauku na eneo hili.

Wakati wa Enzi ya Chuma ya nyuma, nchi za uvuguvugu za kusini mwa dunia hazikuwa na mvuto sana kwa biashara ya kimataifa. Kutokana na kuwa na idadi ndogo ya watu na matumizi ya zana duni katika eneo hilo, ilikuwa ni vigumu kuzalisha ziada ya kawaida ya chakula, hata ndani ya kanda zilizoruhusu ukulima. Waarabu, walioendesha biashara iliyostawi kwenye mwambao wa Afrika, hawakushawishika kuelekea kusini zaidi, kwani dhahabu, pembe na watumwa - bidhaa zilizotunisha shehena yao - vilipatikana kwa urahisi zaidi kwenye pwani za kitropiki. Vivyo hivyo, Wazungu walisafiri kuzunguka Rasi kwa miaka 150 kabla ya kuwa na hamu ya haja na kusini mwa Afrika.

Kama miwasala kupitia baharini haikuwa mikubwa, miwasala ya nchi kavu


vilevile haikuwa na umuhimu zaidi. Jumuiya nyingi za kusini zilikuwa na mahusiano ya kihistoria na kiisimu na kaskazini, lakini mahusiano hayo yalikuwa na umuhimu mdogo katika maisha ya kila siku. Wakhoi, waliofuga wanyama, wakavua samaki na kukusanya chakula kwenye ukanda wa pwani ya kusini, hawakuwa na makutano kabisa na upande wa kaskazini. Hali kama hii iliwahusu pia Wasan, walioshi bara. Wasemaji wa lugha za Kinguni, zaidi zaidi mashariki ya safu ya milima inayougawa ukanda huo, walikuwa na makutano kidogo ya mara kwa mara na jirani zao wa kaskazini. Magharibi ya mbali (katika Namibia ya leo) Waherero na Waovambo walikuwa na mahusiano ya karibu ya kiisimu kati yao na pia na jirani zao wa kaskazini, ambapo Watswana na Wasotho, walioishi katikati, walifanya biashara kaskazini mara kwa mara. Hadi 1500, jamii hizi zilikuwa zimejitenga kabisa kabisa na dunia: mahusinao yao na nchi za nje yalikuwa ya hapa na pale na finyu.

Wazungu walipoanza kujishughulisha na jimbo hili, walifanya hivyo kikakamavu. Katikati ya miaka ya 1600, jumuiya mpya kabisa ilisimikwa katika Rasi na Kampuni ya Kiholanzi ya India Mashariki, ambayo iliendelea kuiona Afrika ya kusini kama kituo cha kupitia tu kuelekea Mashariki. Matokeo ya kikanda ya kuanzishwa kwa makazi katika Rasi yalikuwa makubwa zaidi kuliko wapangaji wa kampuni hiyo walivyokusudia. Ukanda huo kwa ujumla uliunganishwa imara na Ulaya na Asia, ingawa ilikuwa bado haijaamuliwa kama Waholanzi (walioshikilia Rasi tangu 1652 hadi 1795) au Waingereza (waliotwaa Rasi mwaka 1795) wangekuwa ndio mawakala wakuu. Kadri makazi mapya yalivyopanuka kuelekea bara, ndivyo yalivyoanzisha mahusiano mapya, yaliyonasibishwa na utawala na utegemezi. Hili liliashiria mwanzo wa mahusiano ya kibepari ya uzalishaji, pamoja na ukoloni na ubeberu, ambayo yalikuja kuigeuza Afrika ya kusini ghafla na kikwelikweli zaidi kuliko sehemu nyingine yoyote ya Afrika ya kusini mwa Sahara.

Inawezekana kuelezea hali na matukio ya karne ya kumi na sita, lakini ni vigumu kufanya hivyo bila upendeleo. Kila jumuiya ya wawindaji na wakusanyaji ilipogongana na wakulima katika karne mbili zilizopita, jumuiya hiyo iliangamizwa. Wakulima wamenusurika kwa idadi ya kutosha kiasi cha kuwalazimisha wanahistoria wawatambue: wafugaji hawakuwa na bahati hiyo.

Mahusiano ya kuvutia yalitawala Afrika ya Kusini katika karne ya kumi na sita ambayo yalikanusha dhana zote za kutoepukika kwa historia. Tofauti za kimazingira ziliruhusu kiasi fulani cha kubobea baina ya jamii. Wawindaji hawakuwa wanabadilika kuwa wafugaji, wala wafugaji kuwa wakulima, bali waliishi bega kwa bega, licha ya chuki ambazo mara kadhaa ziliambatana na maingiliano yao.

Nusu ya upande wa magharibi wa Afrika ya kusini, pamoja na Botswana na Namibia za sasa, hupata chini ya sm. 40 za mvua kila mwaka. Sehemu iliyo tofauti kabisa na hali hii ni bara ya musoma wa Rasi, ambayo hupata mvua uzuri ya kipindi cha baridi mara kwa mara. Katika karne ya kumi na tano, bila kujenga mabwawa na ufundi wa kuhifadhi chakula, wenyeji wa eneo hili wasingeweza kulima. Kujikita




**23.1** *Kusini mwa Afrika Karne ya kumi na sita na kumi na nane*

kwao kwenye uwindaji na ukusanyaji au kufuga ni ushahidi wa uchaguzi wa busara wa kuishi.

Asili na historia ya makundi ya wawindaji-wakusanyaji wa Kisan vimegubikwa katika visasili na kutokueleweka (*suitafahamu*). Tofauti kubwa ya aina za lugha zilizozungumzwa katika karne ya kumi na sita ni ushahidi wa karne nyingi za kujirekebisha ndani ya nusu ya magharibi ya Afrika ya kusini. Wasan walikuwa na njia za uhakika za kujikimu alimradi idadi ya watu haikuongezeka kushinda rasilimali za mazingira. Kuwinda na kukusanya kuliwafanya wasitegemee jamii nyingine, lakini waliingiliana na watu wengine. Wakati mwingine kundi la wawindaji walijishikiza kwa wafugaji kama wateja, wakijipatia mazao ya maziwa na kutoa wanyama pori au kutoa ushauri juu nyendo za wanyama. Aina hii ya maisha ilitegemea kabisa uzungukaji uliowekea mipaka ongezeko la watu na kufanya isiwezekane kuhodhi mali, kwani ingezuia kasi ya mwendo wa kikosi.

Kumiliki ng'ombe kulikuwa na maana kwamba Wakhoi walipaswa kung'ang'ania maeneo yaliyokuwa na maji ya kutosha badala ya kuzurura katika nyika kavu. Kwa kuwa ng'ombe waliweza kubeba mizigo, Wakhoi waliweza kujenga mahema na kuyasafirisha kila walipohama. Kuwako kwa wazee wasioweza kwenda au watoto

hakukuwa kikwazo kama ilivyokuwa awali. Mali ya binafsi iliweza kukusanywa pia, na ndani ya jamii hizi za wafugaji kiasi fulani cha tabaka kilijitokeza, kikiwatofautisha na Wasan waliokuwa wajamaa na wasiokuwa na mali. Haja ya kudhibiti jamii haikuwataka Wakhoi kujenga muundo rasmi wa mamlaka ya kisiasa; lakini watu binafsi waliweza kuwa na mamlaka kiasi ndani ya koo zao.

Ufugaji yawezekana ulitoa kiasi kikubwa zaidi cha chakula kuliko kuwinda wakati wa neema, lakini mifugo ilitishiwa na ukame na magonjwa ya mlipuko, pamoja na wizi na kuporwa wakati wa vita. Maafa kama hayo yalipotokea, Wakhoi aghlabu walianza kuwinda ili kupata riziki, angalau hadi hapo watakapokuwa wamepata makundi mapya ya mifugo. Karibu na musoma wa Rasi, ambako fursa za kuwinda zilikuwa finyu, wafugaji walionyang'anywa mifugo yao walielekea pwani kuanza kujikimu kwa kuvua samaki. Yawezekana maisha yalikuwa ya kuyumbayumba, lakini hawakuwa wachochole.

Hapangewezekana kuwako mpaka wa kiekolojia wa wazi baina ya Wakhoi na Waxhosa, kwani ukulima wa makazi na ufugaji vyote viliwezekana katika maeneo walikokutana. Kwa yakini kuingiliana kunaelekea kuwa kulikuwa kwa kawaida. Waxhosa - mmoja mmoja - waliacha kilimo cha makazi na kuanza kuchunga na wakati mwingine kuwinda. Kila baa lilipowatokea Wakhoi, waliweza kuwa wateja wa Waxhosa waliokwisha jijenga ujiranini, kwani mazao ya kilimo yaliibuka haraka baada ya njaa kuliko ufugaji. Robert Ross anaonyesha jinsi Wagonakwa, Wagkunukhwebe na Wantinde walivyokuwa Wakhoi kabla, kisha wakageuka kuwa wakulima wa mseto na kuingizwa kijumlajumla katika jamii ya Kixhosa. Ni kwa mtazamo wa kileo tu ndipo ufugaji wa Kikhoi unapoonekana kuwa ni wa kupita, na ni njia ya kujikimu iliyopitwa na wakati. Bali kwa takriban kipindi chote kilichohakikiwa, Wakhoi waliingiliana sana na jamii nyingine bobezi lakini bila kutelekeza mtindo wao wa maisha.

Enzi ya Chuma ya nyuma ilikwisha jijenga miongoni mwa Wanguni na Wasotho kufikia 1500. Chuma ilitumika sana na kufuliwa mahala pengi, ingawa si zana zote wala silaha zilikuwa za metali. Jamii za wawindaji na wafugaji walikuwa na mahitaji kidogo ya chuma na waliweza kutegemea kabisa mawe, mifupa, miti na ngwe. Iliwezekana pia kwa wakulima wa mchanganyiko kumudu maisha bila chuma. Katika kusini mwa Afrika, baadhi ya jumuiya walilima na kufuga kwa kutumia zana za chuma chache sana, kwa takriban miaka 1000. Hata hivyo, kupatikana kwa chuma kwa wingi katika Enzi ya Chuma ya nyuma hapana budi kulirahisisha shughuli zilizokuwapo na kuzalisha zaidi. Wakulima hufanya kazi kwa ufanisi zaidi pale zana za chuma zinapopatikana kwa kufyekea, na wanakuwa na muda wa ziada kwa kazi za mikono za nyumbani na kwa ufugaji wa mapana zaidi. Machimbo ya kiakiolojia yanaonyesha kuwa wanyama wa kufuga na ufinyanzi viliongezeka sana katika Enzi ya Chuma ya nyuma, na hiyo inafahamisha kuwako kwa kiwango kikubwa zaidi cha maisha ya starehe na mgawano wa kazi uliokuzwa ndani ya kila jumuiya.

Masimulizi ya wasafiri juu ya maisha ya jamii za Wanguni mashariki ya safu ya

mlima baina ya 1500 na 1800 hayalingani, na ufafanuzi wa matukio ya miaka hiyo unategemea uchunguzi wa mabaki ya data inayochangiwa na masimulizi machache yaliyosalia. Vitu vilivyokimu maisha vilikuwa nafaka na mifugo. Utegemezi wa kijadi kwenye mtama ulibadilishwa katika karne ya kumi na nane kwa kutumia mahindi, ambayo yalitoa mazao mengi zaidi. Ufugaji uliendeshwa vizuri sana kwa kutumia mchanganyiko wa malisho ya mahali pamoja na uhamishaji wa muhula wa wanyama ili kunufaika na malisho anuwai ya mbuga za kusini. Upungufu wa jumla wa mvua katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na nane, na ukame wa hatari mwishoni mwa karne, huenda vilishadidisha kupigania yale malisho ambayo yaliendelea kutumika hata katika miaka ya ukame.

Wingi wa watu unaelekea kuwa ulikuwa ni wa chini kuliko tulivyozoea sasa. Peires anakadiria kwamba walikuwepo watu 100,000 waliozugumza Kixhosa kufikia 1800, licha ya kuchanganyika na Wakhoi wa zamani. Haielekei kuwa palikuwa na shinikizo kubwa la msongamano wa watu kwenye ardhi wakati wowote baina ya 1500 na 1800. Jambo hili ni muhimu katika kuchunguza mfumo wa siasa uliorekodiwa kwa Wanguni. Muundo wao wa msingi, na kikundi chao cha chini kabisa cha kujitosheleza, kilikuwa ni kaya yenye kumiliki mifugo na kutumia ardhi. Kaya iliweza kuishi kama kikundi chao cha chini kabisa cha kujitosheleza, chenye kufanya biashara na kubadilishana bidhaa na wake na kaya nyinginezo, takriban bila kipingamizi chochote. Kimatendo, kila kaya iliunganishwa kupitia udugu wa ubaba kwenye nasaba, na hatimaye kwenye ukoo. Kiongozi wa ukoo wa kifalme, hata hivyo, alikuwa na madaraka kiasi ya kuendeshea mamlaka yake juu ya wasema Kixhosa wengine, isipokuwa kushughulikia mahusiano ya ndoa na zawadi. Uwezo wa kutoa wake, zawadi na ardhi hatimaye ulitegemea uwezo wa kaya ya mfalme kuzalisha zaidi ya kaya nyinginezo na koo. Lakini hapakuwa na kizuizi maalum kwa mtu wa kawaida kuwa tajiri wa mifugo na wake, hivyo ziada iliyompendelea chifu siku zote haikuwa kubwa. Juu ya tamaa ya machifu ya kugatiza kila kitu, watu wa kawaida pia walikuwa na tamaa zao. Mizozo isiyoisha ndani ya koo kuu za Kixhosa na, pengine, miongoni mwa jamii nyingine za Wanguni bila shaka ilichochewa na watu wa kawaida wapiga bongo ambao walitaka kuikwamisha mamlaka kuu. Vikwazo hivi juu ya kuzuka kwa utawala wa kidikteta havikuvunjwa hadi mwisho wa miaka ya 1700. Hadi hapo, maisha ya kila siku yanaelekea yalikuwa ya utulivu na kwa kawaida ya starehe, kama tutaamini ripori za nadra za Wazungu waliovunjikiwa na merikebu na kupata hifadhi miongoni mwa Wanguni.

Habari chache zaidi zinajulikana kuhusu Wasotho na Watswana magharibi ya Drakensberg, ambako mvua nyepesi ilihimiza msisitizo mkubwa zaidi juu ya ufugaji. Wasotho na Watswana lazima walikutana na Wakhoi, Wasan, Wangoni na Washona, kwani kulikuwa na mtandao wa biashara ndogo ndogo ndani ya maeneo haya.

Jumuiya za Kibantu za kusini, kama za Kisan na za Kikhoi, zilikutana na jumuiya nyingine zilizobobea lakini hazikugeuzwa na kukutana huku. Vikundi tofauti tofauti vya Kiafrika yaelekea viliweza kuishi pamoja kwa muda mrefu bila kikundi kimoja



**23.2** *Wakhoikhoi walitayarisha nafaka* (© The Mansell Collection, London)

kulazimisha mfumo wake wa uzalishaji juu ya kingine.

Historiografia ya kusini mwa Afrika imetawaliwa na maelezo ya historia na upanuzi wa makazi ya Waholanzi katika Cape Town. Kwa hakika, Wareno walikuwa Wazungu wa kwanza kujenga makazi ya kudumu katika jimbo hilo, na ni rahisi zaidi kuelewa hali ya kimapinduzi ya makazi ya Kidachi kama italinganuliwa na ile ya makazi ya awali ya Kireno.

Ureno katika karne ya kumi na sita ilikuwa ni nchi ya kikabaila, ndogo na maskini. Kupanuka kwake nje kuliongozwa na ufalme kama mkiritimba wa biashara katika India, na kuliungwa mkono na Kanisa, ambalo lilikuwa na athari kubwa juu ya utawala. Hadi 1510, makao makuu ya utawala wa nje yalikuwa Goa, na njia ya bahari ililindwa na ngome zilizolinda mlangobahari wa Msumbiji kuanzia Delagoa Bay hadi Tanzania ya leo. Wakiwa na meli bora na bunduki, Ureno haikuwa na shida katika kuziteka bandari za Waarabu na za Waswahili, lakini kulitakiwa zaidi ya ubora wa kijeshi kulitawala eneo hilo. Hii ilikuwa ni himaya ya majini, ambayo udhibiti wake ulikuwa ni wa kubabia. Pia, kimsingi ilikuwa himaya ya kikabaila ambamo ofisi muhimu na zenye ulua ziliuzwa na ufalme kwa malipo ya ada ya mwaka. Ilijazwa majangili ya Kireno, wafanya biashara wasio wa Kireno na majasuri. Faida ilipatikana kutokana na biashara ya dhahabu na pembe za ndovu, na baadaye biashara ya watumwa, kwa kutambua mamlaka ya watawala wa Kiafrika waliopo na kuibua ndani yao tabia zenye kugongana na maslahi ya jamii. Hadi mwisho wa karne ya kumi na sita himaya ya Wareno ndani ya Bahari ya Hindi ilikwisha tikiswa na ushindani kutoka mataifa mengine ya kibiabiashara ya Kizungu, na mlangobahari wa Msumbiji ukapoteza umuhimu wake wa kimkakati.

Unyonyaji wa Msumbiji haukuwa fanisi. Badala ya kuingiza njia mpya za uzalishaji, wafanyabiashara wa Kireno na wa Kihindi walikazania kuwa watu wa kati. Ardhi ilikatwakatwa mapande ya *prazos* na kukodishwa kwa *prazeros* na mashamba yalikuwa na sifa ya nyarubanja za kimwinyi za kijungujiko kuliko mashamba ya kuzalisha bidhaa. Ugavi wa nje wa bidhaa kuu - pembe, dhahabu na watumwa - ulitegemea wakusanyaji wenyeji. Ubepari wa kibiashara bila utaji, na ukoloni bila wakoloni-wakazi, kwa vyote vile ungevuruga Afrika mashariki ya kusini: kilichoshindikana kudhibiti ni mageuzi ya kudumu ya jamii za wakati huo.

Katika mapambano ya muda mrefu dhidi ya ukiritimba wa biashara wa Ureno, Kampuni ya Waholanzi ya India ya Mashariki iliundwa mwaka 1602, kwa kuungwa mkono na mfalme. Kampuni ilijitenga na makanisa yaliyorekebishwa, na kundi tawala la "Heren XVII" halikutetereka katika azima yake ya kutafuta faida za kibiashara. Kampuni iliweza kulipia matumizi makubwa ambayo yangeweza kufidiwa mbele ya safari. Ngome ya askari walinzi katika Rasi ulikuwa mfano halisi wa uwekezaji huo. Kilikuwa ni kituo cha mkakati kilichowekwa kwa misingi ya kuendelea na biashara ya Asia, mahala ambapo nyama mbichi na mboga viliweza kununuliwa kulisha msururu wa meli za Kidachi zenye kusafiri kwenda Botavia na kurudi. Wakhoi na wafanyakazi wa Kampuni waliposhindwa kuzalisha vyakula vya

kutosha Kampuni ilikimbilia kwenye mfumo wa uzalishaji wa kibepari uliorekebishwa ambapo watumishi wa Kampuni waliachiwa kama wakazi huru kujishughulisha na uzalishaji wa kibinafsi, Kampuni yenyewe ikijibakizia udhibiti wa soko.

Kama mataifa mengine ya Kizungu yaliyotanuka kuingia katika mbuga za jotojoto za nyasi zenye watu wachache, Waholanzi waligundua kuwa nyendo za makazi yao mapya zilikuwa tofauti na zile za makoloni yao ya nchi za tropiki. Kwa zaidi ya karne moja, mpaka kukutana na wakulima wa maskanini wa mazao mchanganyiko, tajriba yao ilikuwa ni sawa na ile ya Wahispania katika nyanda za majani za pampa (mbuga) za Amerika ya Kusini na tajriba ya Waingereza katika nyanda za majani za Amerika ya Kaskazini na kusini mashariki ya Australia.

Labda jambo la msingi lililoukilia makazi ya Rasi lilikuwa maendeleo ya pole pole na ya shida ya kilimo. Kwa miaka arobaini ya kwanza ya historia yake, makazi yaliagiza kutoka nje takriban chakula chake chote, licha ya hazina pana ya elimu ya kilimo waliyokuwa nayo walowezi. Jambo la pili kubwa la kuwezesha makazi lilikuwa ukosefu wa wenyeji wa kutumikisha. Pale ambapo Waindonesia waliweza kuelekezwa kwa wingi kwenye uzalishaji wa bidhaa kwa kuchezea miundo ya jamii iliyopo, haikuwezekana kuwageuza Wakhoi kuzalisha mahuruji bila kuangamiza kabisa jamii ya Kikhoi. Wakhoi wapya waliopona na kubakia ndani ya mipaka ya makazi waliungana na jamii nyinginezo kuunda jumuiya mpya - Wakhoikhoi (Wahotentot), ambao baadaye walikuja kuwa kitovu cha jamii ya machotara wa Rasi. Kampuni haikuweza kuwategemea Wakhoi kwa kazi, hivyo walipaswa kuingiza watumwa kutoka sehemu nyingine za Afrika na East Indies.

Sifa bainifu ya jamii mpya ilikuwa ni upanukaji daima. Katika Rasi, wafanyakazi walikuwa ghali na adimu, ambapo ardhi ilikuwa rahisi na nyingi; kwa hiyo njia ya wazi ya kufanikisha upanuzi wa ubepari ilikuwa si matumizi shadidi ya ardhi bali upanuzi wa maeneo. Kupanuka kwa kijiografia kwa makazi kulileta sura ile ile ya idadi ndogo ya watu waliosambaa iliyobainisha jamii ya Wakhoi. Hakika, ufugaji wa kibiashara haukuwa na maana zaidi ya kufuga karibu ng'ombe na kondoo walewale kwenye ardhi ileile kama zamani, wakati mwingine Wakhoi wakiajiriwa kama wachungaji. Hayakuwa matumizi ya ardhi hasa, bali mahusiano ya kijamii ambayo yalibadilishwa na utawala mpya. Mpakani mwa makazi ilikuwa vigumu hasa kwa walowezi wa Kidachi kudhibiti wafanyakazi wao; ilikuwa rahisi kwa wafanyakazi wasioridhika kukimbilia mashariki au kaskazini. Utumwa ulitoa sehemu tu ya jibu, maana watumwa walikuwa ghali na wangeweza kutoroka pia.

Katika karne ya kumi na nane, matilaba ya ufugaji mpana wa kibiashara yalijieleza yenyewe katika msururu wa mahusiano ya kijamii ambayo yanafanana fanana zaidi na yale ya pampa ya Amerika ya Kusini na ya Australia katika karne ya kumi na tisa kuliko sehemu nyingine za Afrika. Cape Town ilikuwa bandari ya kupitia, kitovu cha mahusiano yote ya biashara na makutano ya tamaduni na fikra za kimataifa. Maofisa wa Kampuni hawakuendesha makazi tu, bali pia aghalabu

walifanya biashara wenyewe, wakapatana na wamiliki ardhi matajiri zaidi, wafanyabiashara na wauza migahawa wa mjini, na kujitwaza juu ya jumuiya ya watumwa wenye nidhamu kali. Waliona bora kuliko wafugaji waliokuja mjini kwa nadra kuuza nyama, ngozi na shahamu. Wakizungumza Kiholanzi cha mitaani, wakiwa wenye kisomo cha kubabia na wakivaa magwanda ya kazi, wafugaji kweli walikosa ulimbwende wa mjini. Lakini walikuwa ndio mhimili wa uchumi wa kikoloni. Idadi ya watumwa iliendelea kuongezwa kila leo kwa kuingiza watumwa wapya kutoka nje, lakini idadi ya wafugaji iliongezeka haraka pia kwa uhamiaji na kwa kuzaana. Miaka mia moja na hamsini baada ya kuzinduliwa, makazi yalikuwa na wakazi huru zaidi ya 20,000 na watumwa zaidi ya 25,000.

Upanuzi wa maeneo ya makazi ulielekea kuwasambaza Wakhoi na Wasan kutoka upande wa magharibi wa bara. Wakati huo huo, ushikiliaji wa tabaka na nidhamu ndani ya jamii mpya ulielekea kuwatenga watumwa walioonyesha kujitegemea kimawazo, na Wakhoi wa zamani. Mara moja moja mlowezi wa Kizungu pia alikimbilia mpakani, ama kukwepa sheria, au kwa nia ya kutafuta utajiri wa haraka. Wakimbizi hawa wa Kikhoi na Kisan walikuwa sugu na wakali. Waliweza kutafuta na kupatiwa kazi na dola kama watekeleza sheria mpakani au kujaribu kuishi maisha ya maskani miongoni mwa wanampakani wa Kizungu, wakiwa waajiriwa walipwa mshahara au kama wafugaji huru. Ingawa kazi hii ya mwisho ilikuwa na matumaini ya kuvutia, ilikuwa vigumu, hasa kwa Wakhoi, kupata hati ya ardhi kwa majina yao. Mwisho, ilibakia njia ya tatu: kuwa hatua moja mbele ya mpaka wa upanuzi wa wafugaji wa Kizungu.

Eneo pana na kavu la upande wa kaskazini wa makazi ya Kampuni lilishuhudia kuibuka kwa jamii mpya, kama jamii za Kikora, Kigrikwa, na Kinama, ambazo kuanzia 1730 hadi karibu 1780 zilisumbuliwa kwa nadra na mamlaka ya Kampuni. Ili kujikimu, jamii hizi zilipora, zikafuga na kuuza ng'ombe, zikitegemea bunduki zilizopatikana kupitia makazi ya Kampuni. Uongozi ulikwenda kwa watu wa mpakani walioweza kuzungumza lugha ya Wazungu - wahalifu wa Kizungu na vizalia vya watumwa. Wengi wao, kama Wagrikwa, walikumbuka asili yao kutokana na makundi ya Wakhoi. Hata hivyo, hawa hawakuwa wakimbizi tu kutoka makazi ya Kampuni bali pia kutoka mipakani mwake. Walitamani kuwa na hadhi ya wafugaji huru wa biashara, lakini kwa kuwa walilazimika kuwatangulia washidani wao wa Kizungu, hawakuweza kukaa popote kwa muda mrefu. Hatimaye, mpaka "ulipofungwa" katika karne ya kumi na tisa kwa mchanganyiko wa hali ya mazingira na uimarishaji wa utawala wa kikoloni, siku ya Wagrikwa ilifikia mwisho wake.

Matukio kama haya yalitokea pia mashariki mwa mpaka, lakini huko mtiririko wa mambo ulikuwa wa haraka zaidi, na upeo katika miaka ya 1790 ulikuwa na mshindo zaidi, kwani haukuwahusu wafugaji Wazungu tu, mamlaka ya Cape Town na jumuiya za wakimbizi, bali pia Wabantu wa kusini kabisa.

Udhibiti wa kiasi fulani wa takriban Waxhosa wote yawezekana uliwekwa na mtawala Phalo, lakini kifo chake mwaka 1775 kilifungulia uhasama wa watoto wake

wa kiume, Rharhabe na Gealeka. Kifo cha Gealeka kiligawa majeshi ya wafuasi wake, na kifo vha Rharhabe mwaka 1782 pia kiliwagawa wafuasi wake, kati ya manaibu, Ndlamba na mrithi kijana, Ngqika. Kila moja ya makundi haya lilipania kutawala jumuiya nzima ya wasema Kixhosa na majirani zao Wakhoi, ambao waliorodheshwa kuwa ni marafiki. Kwa mtazamo wa makundi yote mawili, wafugaji wa Kizungu walielekea kuwa kama wafugaji wa kichotara - watu wanaoweza kuwa marafiki na wateja wa Waxhosa matajiri. Iliwachukua Waxhosa kizazi kimoja kuelewa sifa teule ya ufugaji wa *biashara*, na uchu wake wa malisho mapya wenye kuongezeka daima. Pamoja na hayo, waliendelea kutenda kana kwamba tishio lilikuwa liko mbali.

Wafugaji wa Kizungu polepole walifikia kuweka utaratibu wa kujilinda na kupanuka. Kampuni ilimlipia hakimu mkazi (*landdrost*) katika makazi makuu ya mjini, lakini yeye peke yake asingaliweza kudhibiti mambo. Katika shughuli zake za kisheria, *landdrost* alisaidiwa na wakazi - *heemraden* - ambao, katika mambo ya kijeshi, walijichukulia zaidi na zaidi mambo mikononi mwao. Kila mwanaume mtu mzima alikuwa, angalau kimsingi, babe (mzee wa kaya) wa jamii ndogo ya familia yake, watumwa wake, na wafanyakazi wake; na kila ubabe uliendesha mambo yake sana sana nje ya mfumo rasmi wa kisheria. Kwa hiyo vita vilipotishia, wababe walichagua kiongozi wa muda, na kitengo kilivunjwa mara ngawira ilipomalizika kugawanywa. Kadiri Wazungu walivyoongezeka mwishoni mwa kane ya kumi na nane, wakazi hawakuivumilia tena Kampuni. Mwaka 1795, walikana rasmi madaraka yake, na kutangaza jamhuri huru mbili za wababe wa Kizungu, jamhuri zilizodumu kwa muda mfupi za Swellendam na Graaf Reinet.

Wakati huohuo, maasi makubwa zaidi yalikuwa yanaandaliwa. Matokeo ya lazima ya kujipanua kwa wafugaji wa Kizungu yalikuwa ni kuwanyang'anya Wakhoi ardhi yao. Kwa Wazungu ilionekana ni sawa kwa Wakhoi kuwa watumishi wa mashambani badala ya kuwa wakulima huru, na kwa viongozi wa kundi la Waxhosa ilionekana ni sawa kabisa kwao kuwa wateja wa matajiri wa Kixhosa. Lakini Wakhoi waliikataa hali hii na mwaka 1799 wengi wao waligoma, wakijiimarisha kwa kuingiza Wakhoi wenye silaha waliokuwa wakitumikia serikali mpya ya Kiingereza. Yalikuwa ni mapinduzi chipukizi.

Wakati wa vita vya mapinduzi vya Kifaransa, askari wa maji wa Kiingereza walitwaa ngome nyingi dunia nzima ili kuimarisha ubora wao majini. Moja ya ngome hizo ilikuwa ngome ya Cape Town, iliyotekwa baada ya mapambano makali mafupi mwaka 1795. Jamhuri za wenyeji zilizimwa mara moja na Waingereza, lakini udhibiti wa wakazi juu ya ardhi ulithibitishwa.

Lakini uasi wa Wakhoi, hata hivyo, haukuweza kuzimwa kwa urahisi kiasi hicho. Akiwa na majeshi yasiyotosheleza kuendesha kampeni ya muda mrefu ya mpakani, Jenerali Dundas aliridhika kupoza mambo. Baadhi ya ardhi walipewa Wakhoi, mmoja mmoja; wengine walihimizwa kurudi kwenye ajira zao au kujiunga tena na kikosi cha Hottentot, na matatizo yaliachwa yatokote kwa miaka michache hadi

yalipolipuka tena mapema katika karne ya kumi na tisa.

Rasi, ambayo Waingereza waliitwaa mwishoni mwa miaka ya 1700, tayari ilikwisha kuwa na sifa nyingi ambazo zingeitofautisha katika karne ya kumi na tisa. Cape Town, ikiwa na wakazi 15,000 tu, ilikuwa bado ni bandari ya kupitia kwa biashara ya Asia na Ulaya; lakini pia ilikwishapata dhima kama njia ya kutolea bidhaa za uchumi mahuruji kutoka bara. Ndani ya koloni kwa jumla walikuwemo "Wakristo" wapatao 22,000, wengi wao wakiwa Wazungu na watu weusi wachache waliopewa uhuru. Wakhoi na Wasan walihesabiwa kuwa karibu 14,000, na watumwa karibu 25,000. "Wakristo" tu ndio waliweza kumiliki ardhi, ingawa Wakhoi walikuwa hawajatimuliwa kabisa kabisa; na watumwa tu ndio hawakuwa na haki ya uraia kabisa.

Zaidi na zaidi Wakhoi waliingizwa katika hali ya kuwa kati baina ya makazi (ya Wazungu) kwa upande mmoja na Waxhosa, Wasotho na Watswana kwa upande mwingine. Kwa kuwa ilikuwa Wakhoi - yaani jamii za Kikhoikhoi, Kigrikwa, Kinama na Kikora - ambao walipata kishindo cha upanuzi wa wafugaji kutoka magharibi ya Rasi, jumuiya nyingi za kilimo cha mchanganyiko za jimbo lote zilikuwa zimeathiriwa kiasi tu kufikia wakati huu. Miongoni mwa Wanguni wa kaskazini, uibukaji wa mashirikisho imara ambayo yaliendelea hatimaye kuunda madola ya Kizulu, kamwe haukuhusiana na matukio ya Rasi. Hata hivyo, hatimaye ilikuwa ni nguvu ya mageuzi ya ufugaji wa kibiashara, wenyewe ukichochewa na mageuzi ya kibepari ya Ulaya na Asia, ambayo ilithibitika kuwa nguvu ya kijamii ya kudumu kabisa ya karne ya kumi na tisa.


# 24

## *Pembe ya Afrika*

Katika historia ya kakazini-mashariki ya Afrika, karne za kumi na sita na kumi na saba ndizo zilizokuwa na vishindo vingi kuliko nyingine. Taifa kuu kisiasa na kijeshi, na maendeleo ya pekee ya kitamaduni ya himaya ya kikristo ya Ethiopia, yalisambaratika. Uvamizi wa mara kwa mara uliofanywa na maadui, licha ya kuangamiza idadi kubwa ya Wakristo, pia uliyatenganisha majimbo mazima mazima kwa vipindi virefu kutoka kwenye himaya. Kwa kitambo, himaya hii takatifu ilipoteza umaarufu wake wa zamani. Maliki Susenyos, ambaye aliingia Ukatoliki mwaka 1630 na kuufanya kuwa dini rasmi ya nchi alizusha machafuko ya kidini ambayo yalizidisha matata kutoka nje ya mipaka. Vita vikali vya wenyewe kwa wenyewe vilitanda kwenye himaya hii dhaifu na hatimaye kusababisha dini hii ngeni na waumini wake kutimuliwa. Baadaye kukafuata kipindi cha kuimarisha himaya na kufufua utamaduni wake. Ndipo kuanzia 1700 kipindi cha kumeguka kwa himaya kikaanza. Machafuko yaliyokuwa yakiongezeka yalikoma mwaka 1855, wakati Tewodros (Theodore) II alipoanzisha enzi ya Mamaliki wakuu ambao himaya ya Ethiopia inapaswa kuwashukuru kwa kuiwezesha kujiimarisha na kudumu wakati wote wa kipindi cha ukoloni.

Hata hivyo, kaskazini mashariki ya Afrika haikuwa na himaya ya Kikristo ya Uhabeshi pekee. Katika sehemu za mashariki na kati za bara hili dogo utamaduni wa Kiislamu pia nao ulifikia kilele katika miaka ya 1500, na Uislamu wenye kupenda vita ulikuwa ukikaribia kupata ushindi mkubwa. Akihamisishwa na moyo wa *jihadi* (vita vitakatifu) Ahmad Ibn Ibrahim al-Ghazi, aliyepachikwa jina la *Grãn* (Mashoto) katika tarihi za Wahabeshi Wakristo, alishinda vita moja baada ya nyingine. Mwaka baada ya mwaka, wakati wa kiangazi, majeshi yake yaliikamata Amhara na Tigre, yakilazimisha majimbo yote kusilimu. Lakini mara kiongozi huyu alipotoweka majeshi aliyokuwa ameyajaza ari yakaporomoka. Majeshi ya Kikristo yakaanza kujibu mapigo. Kuhamia kwa wingi kwa taifa kubwa la Waoromo (Wagalla) hatimaye kukaharibu jumuiya na tamaduni za jamii za Kiislamu za Uhabeshi ya kati bila kuacha mabaki.

Waoromo na Wasomali walifanya mambo ya muhimu yaliyobadili historia ya kaskazini mashariki ya Afrika. Mgeuko wao ulifuata njia zilizotofautiana kabisa.




**24.1** *Himaya ya Ethiopia na milki zake, t. 1550 (E. Haberland)*

Katika kuhamahama kwingi, Waoromo walisambaa kila upande. Waliyaingilia maeneo yaliyosaliwa na watu wachache kutokana na vita vya kidini, walitiisha na kusimilisha makabila mengi, lakini wakaiga utamaduni wao. Hawakujenga utamaduni wao halisi wa kitaifa.

Wasomali walikuwa tofauti. Kushiriki kwao kwa makundi makubwa makubwa katika vita vitakatifu vya *Grãn* na athari ya Uislamu vilisaidia sana katika kukuza mwamko mkubwa wa kitaifa. Ingawa Wasomali wamega wanyika katika makundi ya kikabila, wanajiona ni watu wa aina moja wenye utamaduni mmoja na dini moja.

Matukio ya kisiasa na kiutamaduni katika maeneo ya kaskazini, kati na mashariki mwa kaskazini-mashariki ya Afrika yalijulikana vizuri kihistoria, lakini historia ya magharibi na kusini-magharibi haikujulikana vizuri. Sasa tunafahamu kuwa wakati huu ulikuwa mwanzo wa ukuaji wa utamaduni wenye nguvu sana. Athari ya moja kwa moja kutoka kwenye himaya ya Kikristo ya kaskazini ilisababisha kukua kwa madola makubwa na tamaduni za kiwango cha juu zilizojitandaza kusini hadi kwenye mpaka asilia wa mwinuko wa nchi. Matukio muhimu zaidi ni kuanzishwa kwa madola ya Iraniya, Woloya, Dauro na madola madogo ya miinuko ya Gamo.

## *Himaya ya Kikristo ya Ethiopia kwenye miaka ya 1500*

Kufikia kama mwaka 1500, himaya ya Kikristo ya Ethiopia ilikuwa imefikia kiwango cha kisiasa na kiutamaduni ambacho haikuweza kukifikia tena kwa karne nyingi. Ilikuwa na hegemonia isiyopingika katika eneo la kaskazini-mashariki ya Afrika. Miji ya Kiislamu pembeni mwa mwambao wa Bahari ya Sham, ambako kwa sasa ni Eritrea, haikuwa na umuhimu kisiasa. Hata pwani ya Kiislamu-Kiarabu iliyozunguka Massawa ilikuwa sehemu ya himaya ya Uhabeshi. Nguvu za tawala nyingi ndogo ndogo za Kiislamu katika mashariki na katikati ya Ethiopia zilivunjwa kwa mapigo mazito ya Mamaliki wa Ethiopia wa karne iliyotangulia, na hasa mfalme Zera-Yakob (1434-68). Katika sehemu ya kusini na kusini-magharibi, athari ya himaya ya Kikristo ilikuwa na nguvu zaidi. Nchi mpya zilizoongozwa na tabaka-tawala la Kikristo zilianzishwa; na pia nchi na watu wa aina mbalimbali waliowahi kujitawala walilazimishwa kukubali mamlaka makuu ya himaya ya kaskazini katika siasa na utamaduni. Hati ya himaya ya Kiethiopia, *Kebra Nagast* (Utukufu wa Wafalme) ilihalalisha kiitikadi upanuzi uliokuwa ukifanywa na himaya.

Inawezekana kazi hii iliandikwa kama mwaka 1300, mara tu baada ya nasaba tawala kushika madaraka tena, na kujulikana kama nasaba ya Sulemani kuanzia hapo mpaka mwaka 1974. Visakale vya kijadi, na mapokeo ya kibiblia, Kitalmudi na Kikorani yaliunganishwa na kupatanishwa kwa mwito mmoja mtukufu wa wokovu. Rekodi za *Kebra Nagast* zinaeleza jinsi Malkia wa Sheba, hapa ikitambulishwa na Ethiopia, alivyofunga safari kwenda Yerusalem kujifunza hekima ya Sulemani. Aliingiliana na Sulemani na kupata mimba ya mtoto wa kiume, ambaye alimzaa baada ya kurejea. Mtoto huyo baadaye akawa mfalme wa kwanza wa Waethiopia.

Baadaye Menelik alipomtembelea baba yake Yerusalem alichukua Sanduku la Agano na kulileta Ethiopia. Tokea wakati huo lilihifadhiwa katika kanisa kuu mashuhuri la Aksum ambako wafalme wa Ethiopia walitawazwa. Kitabu kinamalizikia na tangazo la mgawanyiko wa kiroho wa dunia kati ya Himaya Takatifu kuu za Rumi na Ethiopia. Hadithi hii inawafanya Waethiopia wa Kikristo kuwa taifa teule la maagano yote mawili, la Kale na Jipya, kwani, tofauti na Wayahudi, wao wameikubali Injili. Uwezo wa Ethiopia wa kuhimili dharuba nyingi ulitokana hasa na jiografia yake yenye milima mingi. Lakini pia hisia ya kujiona kuwa taifa teule iliipa uthibitisho wa kiroho nia ya himaya ya kutanua mamlaka yake karibu katika sehemu yote ya kaskazini mashariki ya Afrika.

Wakati huo himaya ilikuwa katika hali ya utulivu mkubwa sana katika mambo yake ya ndani. Ripoti za Fransesco Alvares, ambaye kutoka mwaka 1520 hadi 1526 aliongozana na ujumbe wa Ureno kutoka Massawa hadi Shoa, akiwa padre wao, na kisha kutembelea maeneo mengi nchini kote, zilionyesha hali hii. Amani na usalama ulikuwepo, maagizo ya gavana yalitiiwa, na kauli ya mfalme ilikuwa na mamlaka kamili katika himaya yote ambayo ukubwa wake kutoka kaskazini mpaka kusini ulifikia kilometa elfu moja.

Himaya iliunganishwa na dhana ya Himaya Takatifu ya Kikristo, haki ya kutawala isiyopingika ya Nyumba ya Sulemani, na mwisho, imani ya Kikristo na utamaduni wa pamoja wa Kiamhara na Kitigrai. Utamaduni na lugha za makundi haya mawili zilikuwa na mvuto mkubwa wa kusimilisha mbari yalizokutana nazo. Hii ni dhahiri hasa katika makundi tofauti ya Waagawu, wenyeji wazawa wa kati na kaskazini ya Ethiopia, ambao nusura wote wasimilishwe na Waamhara na Watigrai. Pia, katika sehemu ya kusini ya jimbo la Shoa, ambalo sasa linakaliwa zaidi na Waoromo, sio Ukristo tu bali pia lugha ya Kiamhari na utamaduni wake ulienezwa juu ya ule wa makabila yaliyoishi sehemu ile.

Jaribio la Maliki Zera-Yakob la kugatisha utawala wa kisiasa wa himaya lilishindwa, lakini kauli yake bado ilitiiwa bila ubishi hata baada ya 1500. Tunaweza kuona kutokana na tarihi kuwa hali ilikuwa ni sawa na ile iliyopowepo katika karne za kumi na tisa na ishirini kuhusiana na uhuru wa kujitawala wa majimbo binafsi na swala la sheria ya ardhi. Ardhi nyingi ilikuwa ni masalio ya milki ya makabila na makundi ya familia ambayo yaliamua jinsi ya kuigawa kati yao wenyewe. Kanisa pia lilumiliki ardhi kubwa. Na mwishowe kulikuwa na ardhi ya dola ambayo mfalme aliweza kuwapatia kwa mapatano ya muda mfupi au mrefu wale aliowapenda, au kuitoa kwa shughuli maalumu. Ardhi hii ya kikabaila ilijulikana kama *gult*, neno ambalo pia lilitumika kubainisha haki ya kutoza ushuru na kudai huduma ambayo Maliki alimpa afisa wake.

Ufukuto usio wa kawaida wa jamii ya Kiethopia uliotawaliwa na dhana ya *telleck saw* (mtu mkuu), ambaye kila wakati ilimbidi kujijenga upya na ambaye alithaminiwa kwa ubora wa sifa na mafanikio yake tu, haukuweka msingi wa kuibuka kwa tabaka la waungwana. Kinadharia, mtu yeyote huru kutoka kwenye familia yenye

kuheshimika angeweza kuchaguliwa na bunge la wilaya kushika ofisi. Maliki alikuwa na mamlaka ya kuukubali au kuukataa uchaguzi huo. Hivyo mamlaka ya kifalme na uchaguzi wa kidemokrasia vilisaidiana, na hivyo kuzuia kuzuka kwa tabaka la waungwana kwa kuzaliwa lenye marupurupu ya kisiasa ambayo yangeweza kuyumbisha umoja wa himaya. Hali hii ilitokea baada ya 1700, wakati nguvu za Maliki zilikuwa zinazidi kufifia.

Barabara zilikuwa salama. Nyumba za wageni za kifalme zilikuwa nyingi na pia magulio ya kila wiki. Hali ya maisha kwa ujumla ilikuwa nzuri. Kodi zilizolipwa kwa kutoa mali zilimiminika kutoka kwenye majimbo na madola twawa hadi barazani kwa Maliki, ambako zilisambazwa upya. Ingawa hakukuwepo na sarafu au hati za kibiashara, hata hivyo ilikuwepo biashara kubwa ya masafa marefu, na bidhaa za matumizi ziliingizwa kutoka India na Mashariki ya Karibu.

Ethiopia iliunganishwa kwa karibu na nchi nyingi na hata zile za mbali kama Ulaya. Watawa wa Kihabeshi, watoaji wakuu wa elimu, sanaa na sayansi, walipata mafunzo yao Misri na kujihusisha katika utamaduni wa Kikhufu (Kikopti) na Kiislamu. Ingawa utunzi wa fasthi andishi ulijikita kwenye nyanja za dini na historia tu, lakini ulisitawi mpaka karibu ya 1650. Sanaa za maandishi, ambazo baadhi yake zimehifadhiwa katika michoro ya vitabu, zilichochewa na maingiliano na mashariki ya Kikristo na Ulaya. Kuwepo kwa magofu ya makanisa na ikulu nyingi ambazo habari zake hazijulikani sana ni ushahidi zaidi wa utajiri wa aina nyingi na ubunifu wa kisanii wa kipindi hiki.

## *Madola na tamaduni za Kiislamu: jihadi, Wasomali na Wahadiya*

Ilipofika 1300, kama sio kabla, Ukristo ulikuwa umekuza shughuli za kimisionari zenye nguvu katikati na kusini mwa Ethiopia. Ukristo, ukiwa ndio dini rasmi ya himaya ya Ethiopia, uliweza wakati wote kutegemea msaada wa dola - hata kwa moto kama ni lazima. Kinyume chake, kuenea kwa Uislamu kaskazini-mashariki mwa Afrika kulitegemea kusambaa kwa utamaduni wa Kiarabu na kuwepo kwa biashara na mawasiliano. Katika pwani ya kaskazini-mashariki mwa Afrika, athari za Uarabu na Uislamu zimekuwepo tokea zamani sana. Biashara kati ya rasi ya Uarabuni, pwani za Ethiopia na Somalia, ilisababisha kuanzishwa kwa miji mingi yenye jamii mchanganyiko lakini yenye athari kubwa ya Uarabu. Vituo muhimu sana kuanzia kaskazini vilikuwa: Massawa, visiwa vya Dahlak, Assab, Oboek, Tajura, Jibuti, Zayla, Berbera, Obbia, Mogadishu, Merka na Brava.

Ramani inayoonyesha kuenea kwa Uislamu katika karne za kumi na tano na kumi na sita inaonyesha waziwazi kuwa ulijizatiti kwenye pande zote za bonde la ufa - katika barabara kuu ya biashara hadi katikati ya Ethiopia. Kutoka pwani kwenda bara kulikuwa na madola kadha: Adal, lililokuwa kubwa kuliko yote, Dara, Dawaro, Bali, Arababni (au Aren), Sarha na Hadiya. Inawezekana kuwa athari ya Uislamu ilienea

magharibi kuvuka Bonde la Ufa. Kaskazini ya Bonde la Ufa, kwenye miteremko ya kusini ya milima ya Shoa, kulikuwa na madola mawili pacha ya Kiislamu ya Ifaf na Fatagari (Fatajari). Wakazi wengi wa madola haya hawakosi walizungumza lugha za Kisemiti ambazo zilienea sambamba na kuziua lugha za asili za Kikushi zilizokuwa zikizungumzwa mwanzoni. Lugha za Waharari, Wagurage wa mashariki na Waargobba ndizo pekee zilizosalia.

Madola haya yalijaa utamaduni wa Kiarabu-Kiislamu kutoka pwani, na masalio mengi ya utamaduni huo yanaonekana hadi leo. Mfano wa kuvutia zaidi kati ya makazi yaliyokuwepo wakati huo ni Harari, ambao ndio mji pekee asilia wa zamani katika nchi ya Ethiopia. Nyumba za ghorofa moja na mbili zilizojengewa kwa mawe na zenye mapaa bapa na vyumba vilivyonakishiwa vizuri, na makaburi mengi matakatifu yaliyojengewa kuta, yanaonyesha wazi athari ya Kiarabu. Athari ya Uarabu imeacha pia alama katika kujali sana utunzaji wa bustani ambao mpaka sasa unaendelea, na wingi wa mazao ya kula yaliyokuwa hayajulikani Ethiopia kama vile machungwa, malimau, mapichi, zabibu, ndizi na miwa. Ulimaji wa pamba, unywaji wa kahawa na utumiaji wa mirungi (*khat* au *kati*) (*celastrus*) pia unatokana na athari ya Waarabu. Katika sehemu mbalimbali za Ethiopia ya kati kunapatikana dhana tofauti za kidini, kaida na maneno yanayotokana na Kiarabu, ingawa Waislamu wa huko baadaye waliuacha Uislamu.

Kuenea kwa Uislamu na utamaduni wake kutoka mashariki hadi magharibi kulisababisha mgongano na himaya ya Kikristo. Hali hii ilitokea zaidi katika Ethiopia ya kati ambayo sasa inajulikana kama jimbo la Shoa, na upande wake wa mashariki. Sehemu hii pia ilikuwa uwanja wa mapambano makali kati ya mataifa haya mawili makubwa ambayo yaliendelea kwa karne nyingi bila upande wowote kushinda hadi nusu ya pili ya karne ya kumi na tano. Ingawa himaya ya Kikristo ilibakia kuwa ndiyo yenye nguvu kuliko zote katika eneo la kaskazini-mashariki ya Afrika, lakini ilishindwa kuyaondoa madola ya Kiislamu yaliyokuwa madogo kwake kwa eneo na hata idadi ya watu.

Hatufahamu kwa uhakika jambo lililobadilisha vita kati ya madola ya kibiashara ya Kiislamu na himaya ya Kikristo kuwa Vita Vitakatifu au *jihadi*, wala kwa nini utawala wa kisiasa wa masultani wa Adal, uliojulikana kama Walasma, ulihamishiwa kwa viongozi wa kidini (Maimamu). Na pia hatufahamu majeshi ya Kiislamu yalikopata mshikamano na ushabiki ulioyawezesha kukaribia kuisambaratisha himaya imara ya Kikristo. Sababu mojawapo iliyo wazi ni kuwepo kwa shujaa Ahmed ibn Ibrahim al-Ghazi (Ahmed Gran) aliyekuja kuwa kiongozi wa jihadi mwenye mvuto. Pia ni wazi kuwa nchi nyingine za Kiislamu duniani ambazo wakati ule ziliishikilia ipasavyo Somali ya kaskazini, ziliweza kukusanya askari wengi ukilinganisha na watu wachache waliokuwemo katika nchi za Kiislamu, kwa ajili ya majeshi yake nchini Ethiopia.

Vita na nchi ya Adal viliyoanzishwa na Wakristo, na vita muhimu ilivyoshinda katika eneo la Chercher wakati wa utawala mnyonge wa mfalme Lebna Dengel (1508-

40), havikuleta lolote jipya katika ugomvi wao. Lakini mwenendo wa vita ulibadili ghafla. Katika mapambano muhimu ya Sembera Kure (1529) katika ukingo wa magharibi wa Chercher, himaya ya Ethiopia ilipoteza jeshi lake lote pamoja na idadi kubwa ya watawala wake. Madhara ya vita hivyo yalikuwa ya kutisha. Hadi 1543, majeshi ya Kiislamu kila wakati wa kiangazi yalivamia kusini na kaskazini ya milima ya Ethiopia yakipata ushindi mkubwa na kutiisha jimbo moja hadi jingine. Katika majimbo ya Hadiya na Bali yaliyo kusini na mashariki ya Uhabeshi, watu walijiunga upande wa Waislamu, ambao mara nyingi walishiriki dini yao na kuwakaribisha kama wakombozi wao. Katika majimbo ya zamani ya Kikristo hali hii haikujitokeza, hasa katika maeneo yaliyokaliwa na Waamhara na Watigrai. Huko, wale ambao hawakuukubali Uislamu walichinjwa, hivyo wilaya zote zilisilimu, hata kama kwa jina tu. Makanisa na nyumba za watawa ziliharibiwa na kuporwa, na hazina iliyopatikana ikapewa majeshi ya Kiislamu. Hazina ya fasihi ya Kiethiopia na picha (picha ndogo ndogo kwenye vitabu na picha zilizochorwa kwenye kuta za kanisa) ziliharibiwa. Mwaka 1531 majimbo mawili makubwa na yenye watu wengi ya Dawaro na Shoa yaliyo kusini mashariki na katikati ya milima ya Ethiopia yalitiishwa. Amhara na Lasta, ambayo ni kati ya majimbo mawili yaliyo katikati ya dola, yalifuatia mwaka 1533. Mwaka huohuo Aksum, sehemu ya Ethiopia iliyo takatifu kuliko zote, iliteketezwa. (Mabao ya Sheria yaliokolewa na baadaye kurejeshwa Aksum ambako yako mpaka leo).

Lakini hata katika hali ya kukatisha tamaa, uimara wa Wakristo na nguvu ya dhana ya Utakatifu wa Himaya ya Ethiopia, ilikuwa wazi. Mara majeshi ya Kiislamu yalipoondoka wale walioshurutishwa kusilimu waliicha imani hiyo mpya. Majimbo yaliyokuwa yametawaliwa yalianzisha mapambano dhidi ya mabwana zao wapya. Hata mfalme dhaifu Lebna Dengel, ambaye wakati wote alikuwa akikimbia, alikataa kuoza binti yake kwa Mahammed Gran, licha ya kuahidiwa urafiki.

Lebna Dengel, akiwa mkimbizi anayetafutwa, alifariki mwaka 1540 kwenye nyumba moja madhubuti ya watawa ya Dabra Damo huko Tigre. Katika muda wa miaka michache kukawa na mabadiliko makubwa katika medani ya kisiasa. Kutawazwa kwa mfalme kijana Galawdewos (Claudius), mmoja kati ya watu mashuhuri sana katika historia ya Ethiopia, kulifuatiwa na kuundwa upya kwa himaya ya Ethiopia, kuwasili kwa kikosi cha kigeni cha Wareno na kushindwa kikamilifu kwa Waislamu.

Ilipofika karne ya kumi na sita, Ureno ilifikia kilele cha kukua kwa himaya yake. Bahari ya Hindi na ghuba zake ikawa ni bahari ya Kireno. Huko pwani ya Hormuz, Oman, Sokotra, Mombasa na kwingineko, ngome za Kireno ambazo hazikuwahi kutiishwa kikamilifu zilizuka upya. Kuja kwa manowari za Wareno Massawa, ambayo wakati huo ilikuwa chini ya himaya ya dola ya Ethiopia, mwaka 1541, ilikuwa ni nasibu ya kihistoria. Mwaka mmoja kabla, kikosi cha manowari za Kireno kutoka Goa, India, kilipelekwa bahari ya Shamu kuzuia upanuzi wa Waturuki, ambao baada ya kuishinda Misri walikuwa wakijipenyeza huko Arabia na hata Sudan.


Sehemu ya kikosi hicho ilitia nanga Massawa katika majira ya kuchipua ya 1541. Punde baadaye, *Bahar Nagas* (Mfalme wa Bahari) gavana wa jimbo la kaskazini kabisa ya himaya ya Ethiopia, alileta barua zikiomba msaada kwa ajili ya himaya ya Kikristo. Ilipofika Julai 1541, kikosi cha kujitolea cha watu 400 cha Kireno, kikiongozwa na mmoja wa watoto wa mwisho wa baharia mashuhuri Vasco da Gama, kiliingia katika milima ya Ethiopia. Mbinu zao za kupigana na silaha zao bora ziliwafanya kuwa wapinzani tishio kwa majeshi ya uvamizi ya Kiislamu kaskazini mwa Ethiopia. Waethiopia wengi walijitolea kuambatana na Wareno, ambao walilishinda vibaya mara mbili jeshi kali la Imamu Ahmad Gran. Imamu alifanikiwa kupata msaada wa aina mpya ya mizinga na walenga shabaha stadi kutoka kwa makamanda wa Kituruki wa Yemen. Kabla Wareno hawajaungana na jeshi la mfalme iliwabidi wapigane katika pambano la tatu na kushindwa. Hata hivyo Wakristo walikuwa na bahati. Jeshi la kifalme na mabaki ya jeshi la Kireno waliungana na ilipofikia Februari, 1543, jeshi la Kiislam liliangamizwa upande wa mashariki wa ziwa Tana na Imamu akauawa. Haijulikani kwa uhakika kama msaada uliotolewa na Ureno ndio uliosababisha ushindi katika vita hivi vya muda mrefu. Katika mapambano ya mwisho mizinga yao ilileta mlingano muhimu wa kimkakati. Misioni ya Kikatoliki iliyokuja nyuma ya askari wa Kireno ilikuwa na umuhimu mkubwa kwa Waethiopia (angalia chini). Awali ya yote hakukuwa na wasiwasi juu ya uwezo wa majeshi ya Kiislamu kuishinda Ethiopia kijeshi, lakini yalikuwa dhaifu mno kuweza kuyamiliki mataifa makubwa mawili ya Watigra na Waamhara wakati wote. Baada ya 1534, Wakristo waliibuka na ushindi katika kila pambano na katika miongo michache iliyofuata, himaya iliweza kurudisha ardhi iliyokuwa imetekwa. Nguvu za Uislamu zikawa zimevunjwa kwa karne nyingi zilizofuata.

## *Waoromo (Wagalla)*

Tangu katikati ya karne ya kumi na sita watu wa taifa kubwa la Waoromo, ambao awali walijulikana kama Wagalla, wamekuwa wakipenya katikati, mashariki na magharibi ya Ethiopia katika makundi yaliyokuwa yakiongezeka. Ujio, makazi na magomvi yao na makundi waliyoyakuta huko yalikuwa na athari kubwa kisiasa na kitamaduni. Himaya ya Ethiopia iliumia zaidi na kwa muda mrefu kutokana na watu hawa kuliko ilivyoumia kutokana na Waislamu, na ilipoteza milele majimbo mengi.

Ingawa bado sio rahisi kutaja sababu maalumu zilizowafanya Waoromo wahamehame sana, lakini tunafahamu kuwa kuhama kwao hakukusababishwa na kuwakimbia watu wengine wenye nguvu. Mapokeo ya Kioromo hayasemi lolote kuhusu jambo hili, ila yanasema kuwa walihama ili kutafuta malisho mapya kwa ajili ya watu wao waliokuwa wakiongezeka.

Bila kujali habari zilizojaa chuku za waandishi wa Kiamhara na Kizungu juu ya chimbuko lao, Waoromo ni Waethiopia halisi. Milima inayozunguka sehemu ambayo hivi leo ni jimbo la Bali ndiyo yaliyokuwa makazi yao na ni kutoka hapo ndipo waliondoka kwa wingi kwenda ndani kabisa ya milima ya Ethiopia na kusini ambako




24.2 *Uhamaji wa Waoromo kwenye karne ya kumi na sita.*

hivi leo ni Kenya na Bahari ya Hindi. Yote yale ambayo yameandikwa kuhusu utamaduni wao pia ni makosa. Walielezwa kuwa ni washenzi na wafugaji wasiostaarabika. Kumbe Waoromo ni watu wenye utamaduni wa kiwango cha juu na ulioendelea, wenye kusifiwa na majirani zao. Kuenea kwao kiasi kulikuwa ni matokeo ya uhodari wao: makabila mengine yalijiunga nao kwa sababu ya uhodari wao kijeshi na mfumo wao bora wa kijamii. Wahadiya, ambao waliishi kati ya Harari na Gurage, wanathibitisha ukweli huu, kwani karibu wote walijiunga na Waoromo.

Utamaduni wa Kioromo unatambulishwa na vitu vingi, hasa ule ukaribu wao na ng'ombe wao. Licha ya ng'ombe kuwa msingi wa riziki yao, vilevile ni kitu chenye umuhimu katika hisia na miviga yao. Utanzo huu wa ng'ombe na maadili yake ulienea katika utamaduni wao wote.

Waoromo walikuwa ni mchanganyiko wa mbari na koo zilizohusiana, na jinsi walivyozidi kuongezeka waligawanyika na kuanzisha makundi mapya yaliyokuwa huru kisiasa. Borana na Barentu (au Baraytu) walikuwa mababu wawili katika visasili na waanzilishi wa nusu mbili za wakazi wa asili ambao wamerithi majina yao. Baada ya kuanza uhamaji makundi haya yalitengana. Wabarentu zaidi wakasakini mashariki, na Waborana wakafanya makazi yao kusini, kati na magharibi. Mwishoni mwishoni mwa karne iliyopita, wakati Waoromo waliposhindwa na Maliki Menelik na kuingizwa kwenye himaya ya Ethiopia, waligawanyika katika makundi zaidi ya themanini ya ukubwa tofauti.

Mfumo wa *gada* ambao huwapanga watu katika marika kwa kutumia kanuni dhahania za tarakimu, ulikuwa msingi wa muundo wa kijamii na kisiasa wa Kioromo. Ilikuwa ni asasi iliyotawala maisha yao yote. Hakuna ambalo halikuhusishwa na sheria zake: uzazi, ubatizo, ndoa, jando, kuachana na mamlaka ya wazazi, ruhusa ya kuzaa na kulea watoto, kuandikishwa kwa ajili ya vita au uwindaji, wajibu wa kufanya matambiko, "kufariki kiraia" kwa kutengwa na mfumo, ada za mazishi na mambo elfu elfu ya maisha ya kila siku. Iliwakilisha jumla ya sheria zilizotawala maisha ya Waoromo. Baada ya miaka arobaini kupita tangu baba yake kupitia desturi hiyo, kila Muoromo mwanamume bila kujali umri wake ilimlazimu kupitia darasa la watoto. Kimsingi ilimlazimu kupitia madarasa kumi katika maisha yake, na kila moja lilichukua miaka minane. Wote walioingia shule pamoja walifanya kikundi cha *kigada* ambacho kilibakia kikundi cha wapiganaji kisichogawanyika maisha yote. Madarasa ya tano na ya sita yalikuwa ya uongozi wa vita. Kutokana na kuwa jamii ya watu huru na wenye haki sawa, hakukuwa na madaraja ya kijamii yaliyorithishwa. Kiongozi wa kabila, ambaye kwa kawaida alijiita *abba gada*, alichaguliwa miongoni mwa wale waliokuwa katika darasa la tano. Alisaidiwa na *wahayu* (majaji) ambao pia walichaguliwa kutoka kwenye darasa hili hili; na waheshimiwa wengine. Kanuni moja ya *gada* iliyokuwa na umuhimu mkubwa katika kujenga tabia ya uchokozi wa kivita wa Waoromo ni ile iliyoagiza kuwa angalao mara moja katika kipindi cha miaka minane cha utawala wa *gada* ilibidi ifanywe tabaro (safari ya mashambulizi ya kivita).. Ni yule tu ambaye amejipambanna kama askari na mwindaji shujaa

aliyeweza kushikilia wadhifa mkubwa katika jamii. Ingawa dhana ya kumwona muuaji na mwindaji kama shujaa ilikuwa imeenea miongoni mwa watu wote wa kaskazini-mashariki ya Afrika, lakini ni kati ya Waoromo pekee ambamo utanzo wa uuaji ulijikita mno katika mfumo wa maisha. Kila baada ya miaka minane wapiganaji wa Kioromo waliwavamia jirani zao ambao mpaka walipokuja kufahamu *mfumo wa kigada* walibakia kuchanganyikiwa na matukio haya ya kimsimu.

Dini ya Kioromo ilikuwa na uzito mkubwa. Imani juu ya mungu ambaye alikuwa muumbaji na baba wa mbinguni ilichukua mwelekeo wa Agano la Kale. Walikuwa na hazina kubwa ya fasihi simulizi iliyo takatifu na ya dunia, pamoja na sala na maombi kwa mungu, na pia mashairi ya mapenzi.

Mwanzoni mwa kuhamahama kwao Waoromo walibahatika kuwa na turufu nyingine zaidi ya umahiri wao wa kivita: walikuwa wakiingia kwenye majimbo yaliyokuwa na watu wachache mno baada ya vita vikali kati ya Waislamu na Wakristo. Hali hii ilijitokeza zaidi katika Ethiopia ya kati ambayo leo ni jimbo la Shoa, ambako majeshi ya Kiislamu yalipita kila mwaka yakielekea kaskazini. Kati ya 1530 na 1554 makundi ya wapiganaji wa Kioromo yalisogea kaskazini na katika 1554 yaliteketeza sehemu kubwa ya dola la Kiislamu la Adal. Ilikua wakati huu ambapo Waoromo walijifunza kupanda farasi na wakawa wapanda farasi hodari katika muda mfupi.

Mashambulizi yaliyofanywa na kikundi cha Kiharmufa cha Waoromo (1560-70) yaliwaathiri vibaya Wakristo pamoja na Waislamu. Walikuwa sasa wakivamia majimbo yaliyokuwa katikati ya dola ya Ethiopia, ambayo ndio kwanza yalikuwa yakipata afueni kutokana na maangamizo ya jihadi - majimbo ya Angot, Amhara na Bagemder. Wakati huo huo vikundi vingine vya Kioromo vilishambulia Adal, ambako kulikuwa na njaa na tauni ambayo ilimwangamiza hata Amir Nur mwenyewe. Mfalme Minas alipofariki theluthi moja ya dola la Ethiopia ilikuwa tayari imegeuzwa mastakimu ya kudumu ya Waoromo.

Lakini huu haukuwa mwisho wa upanuzi wa Waoromo. Hata kabla ya 1500, makundi mengine (Wagugi, Waborani na Waoroma) yalikuwa yamekwishaondoka kwenye milima iliyozunguka Bali kupitia nyika hadi kusini katika azma yao ya kufuata malisho mapya kwa mifugo yao. Hatimaye yalifika kwenye lango la mto Tana katika Bahari ya Hindi. Katika sehemu ya kati, Waarusi walifanya makazi yao karibu na lililokuwa jimbo la Bali na kuongeza mipaka yao zaidi upande wa magharibi. Wabarentu walienea katika sehemu iliyokuwa zamani majimbo ya Kiislamu ya Fatagari, Dawaro na Adal. Mji uliozungukwa na ngome wa Harari na kituo maarufu cha mahujaji cha Sek Hussen vilinusurika kama visiwa vya Kiislamu. Vikundi vya Kiamhara viliweza tu kujishikiza katika sehemu za joto na tambarare zilizokuwa rahisi kuzilinda, katika makorongo ya mito mikubwa na katika miinuko michache. Wawollo na Wayeggu Oromo walisambaa kwenye majimbo yenye rutuba ya Angoti na Amhara yaliyokaliwa awali na Wakristo. Licha ya Waoromo hao kuifanya lugha ya mahali hapo ya Kimhara kuwa lugha yao, waliendelea kuwa adui

wakubwa wa Wakristo kutokana na kusilimishwa kwao. Waoromo wengine walikaa kwenye nyanda za chini zenye rutuba kama wafugaji ng'ombe mashariki ya milima ya Ethiopia.

Mwanzoni mwa karne ya 17, wimbi la mwisho la Waoromo, likiwa na makundi kadhaa ya familia kubwa ya Makka, yalijitoma magharibi ambako leo ni majimbo ya Wallaga na Ilubabori, na hawakusita hadi walipofikia miteremko ya magharibi ya milima ya Ethiopia. Upande wa mashariki na kusini wa nchi hiyo walikutana na falme zilizojiendesha vizuri na zenye watu wengi zilizokuwa na uhusiano wa karibu na himaya ya Ethiopia iliyokuwa kaskazini, na ambazo baadhi ya watu wake walikuwa Wakristo. Upanuzi wa Waoromo uliendelea kwa nguvu licha ya upinzani uliofanywa na falme hizi, hasa kutokana na mawasiliano kati ya himaya na twawa zake zilizokuwa kusini mashariki kuwa mabovu sambamba na kudidimia kwa nguvu za himaya. Hivyo Bosa na Gumani zilipotea kwenye ramani ya kisiasa na zikawa makoloni ya Waoromo ya Gimma na Gumma. Hata hivyo jamii ya wazawa ilibakia na nguvu sana kiasi cha kuwafanya Waoromo waige utamaduni mwingi wa nchi waliyoishinda, hasa utaratibu wa kisiasa na ufalme, na kuufanya mfumo wa *kigada* upotee pole pole. Jimbo la Inariya ndilo lililokuwa la mwisho kusalimu amri; lilishindwa na Waoromo wa Limmu. Baada ya 1700 mfalme wake alikimbilia kusini, ambako falme za Kigonga na nyingi za Kiometo zilisimama imara dhidi ya Waoromo kutokana na umbile la nchi yao kuwa kinga asilia.

## *Wasomali*

Kwenye kipindi hicho hicho, kama sio mapema, Wasomali - taifa jingine lililokuwa mashuhuri - walianza upanuzi ambao ulikuwa na umuhimu mkubwa katika sehemu kubwa za mashariki ya Pembe ya Afrika.

Inasemekana kuwa nchi ya asili ya Wasomali ni nchi iliyo kaskazini ya mahali wanapoishi hii leo. Kutoka pale walisambaa kusini magharibi, pengine kuanzia karne ya kumi na moja na kuendelea. Wanajiografia wa Kiarabu wanazungumza juu ya makao ya Kisomali katika sehemu ya Merka kuelekea kusini mwa mji ambao hii leo unajulikana kama Mogadishu. Kama wachungaji wanaohamahama, idadi ya Wasomali ilivyozidi kuongezeka iliwasukuma kutafuta malisho mapya katika uelekeo wa milima ya Uhabeshi, na inawezekana walifika kwenye ukingo wa mashariki wa uwanda wa Harari karibu na mwaka 1500, na huko wakakutana na madola ya Kiislamu. Majina na taarifa za kishajara zilizoachwa na mtarihi Sihab Al-Din zinaonyesha kuwa Wasomali walichukua nafasi muhimu katika kuunga mkono jihadi ya Imamu Ahmad Grañ.

Athari ya Uarabu-Uislamu ya kuchechemua (kuzindua) na kuunganisha watu ilikuwa kubwa kwa Wasomali kuliko watu wengine wa kaskazini-mashariki ya Afrika. Uislamu ukawa ni kiungo kikubwa cha utamaduni wa Kisomali na imani yao iliendelea mara kwa mara kuchochewa na ujio wa wamisionari kutoka Arabia. Watu

hawa watakatifu ndio waliokuwa mababa waanzilishi wa Wasomali, kama vile Ismail Gabarti, mtu maarufu ambaye Wasomali wengi wametokana naye. Mvuto huu wa kitamaduni wa Kiarabu- Kiislamu pia uliwafanya Wasomali kujiona bora kiutamaduni na kuchochea uwezo wao wa kuyasimilisha makundi mengine waliyohusiana nayo katika eneo kubwa kati ya Ogadeni na Ziwa Turkana. Ni vigumu mno kuonyesha kwa uhakika hatua moja moja za upanuzi wa Wasomali kwa sababu makundi mengi yaliyojichomeka katika taifa la Kisomali yalificha ukweli kuhusu asili yao na kujichukulia nasabu za Kisomali.


Kutokana na athari ya Uislamu, utamaduni wa Kisomali, hasa kusini, ulibadilika. Wasomali, kwa hiyo, wakajifanya tofauti na kundi jingine lolote la jamii kubwa ya Waafrika wa kaskazini mashariki, ambao wameunganishwa nao na hali moja ya kihistoria, kiutamaduni na kijiografia. Athari iliyoletwa na mazingira ya kijiografia haifai kupuuzwa, kwani mbali na Waafari wanaoishi katika maeneo makame ya nchi yao, Wasomali ndio pekee wenyeji wa kaskazini- mashariki ya Afrika ambao nchi yao inaundwa na nyika kavu na nusu jangwa pekee. Mazingira haya ya ekolojia yaliwafanya wawe na utamaduni tofauti kabisa na ule wa watu wengine wa kaskazini-mashariki ya Afrika, ambao wengi wao wanaishi milimani.

## *Juhudi za himaya ya Ethiopia kujinusuru 1529-1632: kisa cha Wareno na kuzinduka tena kwa himaya baada ya 1632*

Kati ya 1529 (mwanzo wa jihadi) na 1632 (mwanzo wa kuzinduka) himaya ya Ethiopia ilikuwa ikijitahidi kujinusuru. Haukuwa wakati wa matukio makubwa ya kisiasa na kijeshi pekee, bali pia ulikuwa ni wakati wa mgongano mkubwa kifikra na kiutamaduni ambapo Ethiopia ilivamiwa na mawazo kutoka bara jingine.

Himaya ya Kikristo ilionyesha nguvu na uwezo usio wa kawaida wa kuhimili shinikizo kutoka kwa maadui wa nje na ndani. Ulikuwa wakati wa maliki Sansa Dengel (1563-97) ambapo himaya ilikuwa zaidi ya kufikirika akilini tu, ambapo nguvu ya kiroho ya dhana ya Himaya Takatifu ilidhihirika waziwazi. Waturuki walikuwa wakiimarisha utawala wao kwenye pwani ya Bahari ya Shamu; wakikamata bandari zote za Kihabeshi na kuingia ndani milimani hadi Tiara; katika majimbo ya kati ya Begender na Samen, vita vikali vya wenyewe kwa wenyewe vilikuwa vikiendelea dhidi ya Waethiopia wenye imani ya Kiyahudi, na uvamizi wa Waoromo ulikuwa umefikia kiwango cha kutia wasiwasi. Nguvu halisi za dola zilibakia mahali pale tu alipokuwepo Maliki na wanajeshi wake, lakini umilele wa "himaya ya Kinjili" haukuwa mashakani hata kidogo.

Ufalme ulipata bila shaka yoyote hasara kubwa ya nchi na watu katika jitihada hii kubwa ya kujilinda. Kutoka uzinduzi wa 1632, upanuzi wa kuelekea kusini, ambao ndio uliokuwa sera kuu ya kifalme katika karne zilizotangulia, haukuendelezwa.



**24.3** *Kasri ya Gondari, mji mkuu wa Ethiopia, iliyojengwa na Maliki Fasiladas ( © Werner Forman Archive, London)*

Kadiri nguvu za kifalme zilivyonyong'onyea, jitihadi zilielekezwa katika kudumisha utengemevu katika makao makuu. Uhamishaji wa makazi ya maliki kwenda Gondari mwaka 1636 ulikuwa ni ishara ya kujiondoa huku katika udhibiti wa himaya kwa jumla. Kabla ya hapa, Mamaliki, katika nchi hii ambayo haikuwa na miji, kila baada ya mwaka au nusu mwaka walihamisha makazi yao kwenda sehemu nyingine. Hii ilikuwa sheria ya lazima kufuatwa hata kama hakukuwa na ulazima wa kijeshi au wa kisiasa wa kufanya safari au kubadilisha makao. Hivyo haikuwa tu kukiuka jadi, lakini pia ishara ya kutangua sera zenye nguvu za Mamaliki waliomtangulia, pale Maliki Fasiladas alipojenga makao ya kudumu Gondari mwaka 1636, baada ya vita vikuu vya kidini vya mwisho vya wenyewe kwa wenyewe kumalizika. Gondari ikabakia kitovu cha masalia ya Ethiopia ya Kikristo hadi 1855.

Hivyo kati ya 1529, mwanzo wa jihadi, na 1597, kifo cha Maliki Sartsa Dengeli na mwanzo wa vita vya wenyewe kwa wenyewe, sera za kifalme zilijizatiti kwenye ulinzi. Maliki Galawdewos aliendelea na mapambano dhidi ya Waislamu, hasa wale wa jimbo la Adal Harari, kwa mafanikio makubwa. Mahusiano ya zamani na kusini-magharibi yakafufuliwa, athari ya utamaduni wa Kikristo-Kiamhari ikarejeshwa, na Waoromo wakarudishwa nyuma, japo kwa muda. Chini ya uongozi wa shujaa na mrithi mwenye kipaji cha siasa wa Ibrahim Grañ, Amiri Nur ibn Mugahidi, Waislamu wa Adal-Harari walijaribu tena kuikabili himaya ya Kikristo. Ingawa jeshi la Ethiopia, ambalo halikujiandaa vizuri kwa vita, lilipigwa na kurudishwa nyuma katika shambulio la Adal la mwaka 1559 na mfalme Galadewos kuuawa kwenye uwanja wa vita, huu ukawa mwisho wa nguvu za Kiislamu. Katika miongo michache madola ya Kiislamu na utamaduni wa Kiislamu ulipotea katika sehemu hii, kukabakia tu mji uliozungukwa na ngome wa Harari na usultani mdogo wa Awsa kwenye oasisi ya delta ya mto Hawasi. Maliki Minas (1559-63) zaidi alipambana na Waturuki ambao, kutoka kwenye vituo vyao kwenye bandari za Bahari ya Shamu, walijaribu kila mara kuweka vituo kwenye milima ya Ethiopia. Kutokana na Waoromo kutoiacha himaya kupumua, mtoto wa Minas, Sartsa Dengel (1563-97), ambaye alikalia kiti cha kifalme angali mtoto, alilazimika kuendesha mapambano pande zote bila kupumzika.

Vita vyenye ukatili wa kutisha vilianzishwa ili kuwamaliza Waethiopia wenye imani ya Kiyahudi katika milima ya kaskazini, hasa katika Sameni, Waggara, Dambiya, Belasa, Sallamt na Sagade, ambako hapo mwanzoni walikuwa na kiwango fulani cha kujitawala.

Inawezekana waliowatangulia waliingizwa kwenye Uzioni na wamisionari wa Kiyahudi kabla ya Ukristo kuanza. Tofauti na Wayahudi katika sehemu nyingine duniani, hawa waliingizwa kikamilifu katika utamaduni waliokuwa wakiishi nao kiasi kwamba hata vitabu vyao vitakatifu viliandikwa katika Kigeezi, lugha ya kifasihi na kidini ya Waethiopia, na sio kwa Kiyahudi.

Haijulikani kwa nini vita hivi vya kidini vilitokea wakati uleule ambao ufalme ulikuwa ukizongwa sana na maadui wa nje. Vita hivi, kama vile katika kizazi

kilichotangulia ambapo majeshi ya Kiislamu ya jihadi yaliwateketeza Wakristo, ni miongoni mwa vita vibaya sana katika historia ya Ethiopia. Wayahudi walikabiliwa na uchaguzi wa kuukumbatia Ukristo au kuuawa. Wayahudi wengi walikataa kubadili dini na hivyo wengi wao wakauawa. Wachache wao waliobaki walivuliwa haki zao za uraia na kunyang'anywa ardhi yao na wakashurutishwa kuwa mafundi mchundo; hivyo neno *Falasha* litumikalo kuwaelezea Waethiopia wenye imani ya Kiyahudi, likapata maana sawa na mfua chuma, mfinyanzi, fundi seremala au mfumaji - kwa hakika na kila aina ya kazi za ufundi wa mikono. Licha ya umuhimu wa kazi hizi, ziliendelea kudharauliwa, kwani jamii ilithamini mtu huru na mwenye kujitegemea bila kufanya kazi ya mshahara. Hivyo dharau ya kijamii iliambatana na uonevu wa kidini.

Inashangaza kuona jinsi himaya ya Ethiopia ilivyoweza kupata nguvu, baada ya karibu vizazi vitatu vya mapigano yasiyokwisha, sio tu dhidi ya Waturuki kwa upande wa kaskazini, Waislamu wa Kiadali huko mashariki na Waoromo huko kusini na kati, bali pia katika kampeni kubwa huko kusini-magharibi za kuilazimisha miji mikubwa ya Inariya, Bosa na Kaffa (Goma) kuwa tena na uhusiano wa karibu na kanisa la Kiethiopia na utamaduni wa Kiethiopia wa kaskazini. Mtunzi wa *Historia ya Wagalla* anaelezea jinsi mfalme Sartsa Dengel alivyoahidi kupunguza nusu ya ushuru uliolipwa na Inariya kwa sharti la wote kuwa Wakristo. Kutokana na shinikizo la Maliki, lakini pia akitilia maanani msaada uliotazamiwa dhidi ya Waoromo, Mfalme Badanko wa Inariya aliamua kubatizwa. Sherehe ilifanywa kwa heshima kubwa ikiwajumuisha mfalme na watu wake. Baada ya muda si mrefu mfalme wa Wabosa, majirani wa Wainariya, naye pia akabatizwa. Matukio haya ambayo yalitokea punde tu kabla ya 1600, yanawakilisha mwisho wa upanuzi wa himaya. Tunaweza kuhitimisha kutokana na mapokeo simulizi yaliyobakia ya watu wa Ethiopia ya kusini magharibi kuwa mahusiano yaliyofanywa wakati wa Sartsa Dengel yalikuwa ya kudumu na yenye kusisimua katika Ethiopia ya kusini na maendeleo ya utamaduni wake.

Hata hivyo, tukio muhimu zaidi kwa himaya ni mgongano wa kiitikadi na kanisa la Kikatoliki ambao ulichukua karibu karne nzima, yaani kutoka 1542 hadi 1632,.

Kwa kuanzisha Chama cha Yesu (Wayesu) mwaka 1540, Kanisa Katoliki lilipata chombo imara, sio tu cha kuendesha mapambano dhidi ya Mageuzi ya Kiprotestanti huko Ulaya, bali pia cha kuwaongoa "wapagani" na kurudisha makanisa yaliyoasi chini ya mamlaka ya Roma. Hata kabla ya 1540 mawasiliano yalikwishafanyika kati ya wafalme wa Kireno na wale wa Kiethiopia na mawasiliano haya sasa yaliendelezwa. Uamuzi muhimu bila shaka ulikuwa kuwepo nchini Ethiopia kwa baadhi ya askari wa jeshi la Ureno ambao walibakia nyuma pamoja na familia zao. Kabla ya 1557, Andrea da Oviedo alisimikwa uaskofu na kupelekwa Ethiopia na baadhi ya Wayesu wa Kireno kutayarisha kazi ya kuanzisha upya umoja wa Kanisa la Orthodox na Roma. Mazungumzo yake na mfalme Galawdewos yaliibua ufafanuzi wa welewa mkubwa wa dini ya Kiethiopia kupitia mdomo wa Maliki ambao unajulikana

katika historia kama "Ungamo la Imani la Galawdewos."

Kwa mara ya kwanza, sauti ilisikika Afrika ikisisitiza kuwa Ukristo ni dini isiyo na mipaka ya muda na mahali, na hakuna watu wowote ambao wanaweza kusema kuwa tasfiri yao ya Ukristo ndiyo pekee iliyo sahihi. Galawdewos anaonyesha kuwa badhi ya desturi na matendo ya Kanisa la Kiethiopia sio ya kipagani au Kiyahudi bali yana asili yake katika utamaduni wa Kiethiopia kama vile utamaduni wa Ulaya ulivyojidhihirisha katika Ukristo wa Kiulaya.

Chini ya Mfalme Sartsa Dengel, Wayesu walipewa Fremona, karibu na Adwa nchini Tigre, kuwa makao yao. Waliruhusiwa kuishi katika uhuru kamili na kujihusisha na kazi za umisionari. Mwaka 1603 Mhispania Pedro Paez alikuwa mkuu wa misioni. Alikuwa, bila shaka yoyote, mmisionari bora wa wakati ule na pia mwenye uvumilivu wa kupindukia. Hivyo Waethiopia wakawa na mazungumzo ya teolojia yaliyosisimua sana. Ili kuwafikia watu, kanisa liliweza hata kuendesha na kurekodi mazungumzo ya kidini katika Kiamhara. Badiliko hili lilikoma baada ya himaya kuundwa upya mwaka 1632 kwa kuanzishwa tena lugha maalumu ya kanisa, *Kigeezi,* ambayo Waethiopia wengi hawakuifahamu kama kilivyokuwa Kilatini kwa wakulima wa Kizungu wakati ule. Hata hivyo, mazuri yaliyosababishwa na uhusiano huu hayakudumu sana, na kongamano lililotoa mawazo bora likageuka na kuwa uadui wa wazi kati ya vikundi vya Ki-*Orthodox* na vya Kikatoliki.

Katika Ethiopia wakati huu fasihi ilipitia mwamko mkubwa, na kazi zilizoandikwa, nyingi zikiwa za teolojia na historia, ni miongoni mwa zilizo muhimu sana katika fasihi ya Kiethiopia. Kazi za teolojia zinazofaa kutajwa hapa ni *Fekkare Malakot* (Maelezo ya Uungu), *Mazgaba Haymanots* (Hazina ya Imani) na kazi inayojumuisha kila kitu ya *Haymanota Abaw* (Imani ya Mababa). Kazi hizi zilifasiriwa kutoka katika Kikhufu- Kiarabu. Ili kuwarudisha wale Wakristo ambao kwa kipindi kifupi walisilimu, *Mashafa Keder* (Kitabu cha Najisi) kiliandikwa kwa ajili ya ibada za kusafishwa. Enbakom (Habakuk), Muislam aliyebatizwa kuwa Mkristo, ambaye alipanda cheo hadi kufikia ngazi ya ukasisi wa Ethiopia, aliandika kitabu cha kipekee kiitwacho *Ankasa Amin* (Milango ya Imani), ambacho kinatetea Ukristo dhidi ya Uislamu. Zaidi ya hapo, kwa kufasiri *Barlaam* na *Josaphat*, Enbakom alifanikiwa kuifanya kazi mashuhuri ya fasihi ya mashariki kusomwa na Waethiopia.

Kazi tatu au kumbukumbu za historia zinasohusu enzi za wafalme Galawdewos, Sartsa Dengel na Susenyos, na *Historia Fupi ya Wagalla* kilichoandikwa na mtawa Bahrey, pia vinahesabiwa kuwa miongoni mwa kazi bora za maandishi za kipindi hiki.

Kutawazwa kwa Susenyos (1607) ni mwanzo wa awamu ya kata shauri katika makabiliano ya kanisa la Orthodox la Kiethiopia na Kanisa la Kimisionari la Kikatoliki. Mkuu wa Misioni ya Yesu, Pedro Paez, mwanateolojia, mhubiri, mwalimu na msanifu majengo, alikubaliwa kuingia kwenye baraza la Kifalme, na kutokana na haiba yake kubwa Maliki alianza kuegemea zaidi upande wa Ukatoliki.



**24.4** *Picha ya kuchora kwenye kitambaa ya Kikhufu ya karne ya 18 inayoonyesha Bikira (Mariamu) na Mtoto, Gondari*
*( © Werner Forman Archive, Makumbusho ya Addis Ababa)*

Kaka yake mwenye ushawishi mkubwa, Ras Seela Krestos, aliingia rasmi Ukatoliki mwaka 1612 na kuanzisha misioni ya Kikatoliki kwenye jimbo lake la Gojjam. Licha ya upinzani wa *abuna* (Uaskofu wa Kanisa la Ethiopia), mwaka 1632 mfalme mwenyewe pia akaingia imani ya Kikatoliki. Pedro Paez alifariki punde baadaye.

Mapambano kati ya imani na staarabu hizi mbili, ambayo hadi wakati huu yalifanyika kwa kutumia silaha za fikira na kwa kuheshimiana, sasa yaligeuka kuwa vita vya wazi. Tofauti na mtangulizi wake, Alphonso Mendex, askofu mpya wa Kihispania aliyeletwa na Papa, alikuwa mwenye imani finyu na mwenye kiburi. Chini ya ulinzi wa mfalme Mendez alianza kuliweka kanisa la Kiethiopia kama alivyoona yeye kuwa ndio mwelekeo sahihi. Mapadre wote wa Kihabeshi walitakiwa kupadirishwa upya, na makanisa yote kuwekwa wakfu upya. Kalenda ilifuata taratibu za Ulaya, tohara ilipigwa marufuku na Waethiopia wote walipaswa kubatizwa upya.

Maasi yaliongozana dhidi ya kanisa jipya lililochukiwa na kuwa makali zaidi katika majimbo ya kati ya Bagemderi, Lasta na Wag. Mfalme aliyeleta amani nchini, na ambaye awali alipendwa sana, sasa ilimbidi awatishe watu wake katika vita vilivyomwaga damu, ambapo ulokole wa Wayesu ulizidisha wasiwasi.

Mwaka 1632 kulikuwa na pambano kubwa ambamo licha ya Maliki kuibuka mshindi alikuwa mtu aliyekata tamaa. Aliachia ufalme, akawarudishia watu wake imani ya mababu zao na kuwaomba mapadri wa zamani kurudia liturgia yao.

Susenyos alifariki punde baadaye na misioni ya Kikatoliki ikafa. Watu wao kama walivyoingia katika dini mpya, walirudi kama kundi moja kwenye imani yao ya asili. Maliki mpya, Fasiladas, aliwafukuza Wayesu kutoka nchini. Polepole idadi ndogo ya Waethiopia waliong'ang'ania imani ya Kikatoliki walisakamwa, na viongozi wao wakuu, akiwemo Ras Seela Krestos, waliuawa. Fasiladas alidiriki hata kuwekeana mkataba na gavana wa Kituruki wa Massawa ambapo gavana alikubali kumuua mmisionari yeyote kutoka Ulaya anayeingia Massawa kwa mabadilishano ya fedha. Hivyo ndivyo ulivyokwisha, kutokana na makosa ya Wazungu, muwasala kati ya Afrika na Ulaya uliodumu kwa karibu ya miaka mia moja, ambao kwanza ulikuwa na manufaa lakini baadaye ukatumbuka nyongo.

Himaya ya Ethiopia sasa ikaanza kipindi cha kujitenga kwa makusudi kabisa na dunia iliyobakia na kufuata siasa ya kujiimarisha, lakini ilipofika mwisho wa karne siasa hii ikakwama. Kuanzishwa kwa makao ya kudumu ya kifalme huko Gondari, katika sehemu yenye usalama kijeshi, ni miongoni mwa mchakato huu. Ilikuwa sio rahisi tena kuendesha siasa ya uchokozi na yenye nguvu kutoka Gondari. Hivyo kuna matukio machache ya kisiasa ya kuripoti ya Ethiopia ya Kikristo katika nusu ya pili ya karne ya kumi na saba. Chini ya mfalme Yohannes (1667-82), Waethiopia Wakatoliki wachache waliobakia walipewa uchaguzi wa kuikubali imani ya Ki-*Orthodox* au kuondoka nchini. Waislamu waliokuwa bado wakiishi Ethiopia ya Kikristo, hasa wafanyabiashara, waliruhusiwa kuendelea na dini yao bila vikwazo vyovyote, ila waliwekwa katika makao tofauti ya kuishi.

Iyasu I (1682-1706) alikuwa Maliki wa mwisho. Alichukua hatua moja ya mwisho

iliyokuwa batili kurudisha uhusiano na Ethiopia ya kusini magharibi na hata kutembelea Inariya. Hakukuwepo na maadui wa ndani au wa nje kutishia usalama wa himaya. Bandari muhimu ya Massawa, ingawa kwa jina ilikuwa chini ya himaya wa Kituruki, ikisimamiwa na gavana wa Beja, ilikuwa wazi kwa biashara na Ethiopia. Punde baada ya kifo cha Iyasu, himaya ilianza kumomonyoka na kufikia hali ya kutokuwa na serikali baada ya 1755.

Katika kipindi hiki, maisha ya kitamaduni yalisitawi kwa mara ya mwisho chini ya ulezi wa baraza la kifalme huko Gondari. Kwa kiasi kikubwa kuliko wakati wowote ule, sanaa na sayansi zilionyesha kuwa ni uwanja wa tabaka dogo la waali tu. Ni vigumu hapa kueleza yote yaliyotokea kuhusu hali tofauti za maisha ya kisomi ya wakati huu. Hivyo tutatoa maoni yetu juu ya fasihi, usanifu majengo na uchoraji picha za rangi.

Tofauti na karne iliyopita, fasihi ilikosa uasili na kuchukua mwelekeo wa kimaadili, huku kazi nyingi zikiwa ni tafsiri kutoka Kikhufu-Kiarabu. Zinazostahili kutajwa ni *Faws Manfasawi* (Dawa ya Kiroho), kitabu cha ibada na utubio, na *Fetha Nagast* (Mamlaka ya Wafalme) mkusanyiko wa sheria na maelekezo kwa ajili ya kutumiwa na jamii za Kikhufu za Misri. Wakati huu ulishuhudia pia utungaji wa nyimbo za kidini za kumtukuza Mungu.

Sanaa za maandishi zina mahusiano ya aina hii na maisha ya kitalani. Makanisa yaliyochimbwa majabalini, ambayo ni miongoni mwa mambo asilia sana ya ustaarabu wa Ethiopia ya Kikristo, yalikuwa bado yakitengenezwa kwenye miamba mwishoni mwa karne ya kumi na tano, lakini aina hii ya ujenzi ilikwisha kabisa baada ya 1500, labda kutokana na vita vya kidini. Yaliyojitokeza baadaye katika Gondari na sehemu chache nyingine, kilikuwa kitu kingine tofauti kabisa - ngome kubwa, maktaba, makanisa na majengo yaliyounganishwa kwenye ikulu za Mamaliki na za wanafamilia ya kifalme. Muundo wa majengo haya kila mara ulionyesha ufundi wa kutoka nje. Mengi bila shaka yalijengwa na wajenzi wa Kihindi-Kireno ambao walikuja pamoja na wamisionari wa Kireno kutoka Goa. Kudidimia kwa taratibu kwa himaya, kuangamizwa kwa mji wa Gondari na Tewodros na madarweshi, na karne nyingi za kutotunzwa zimeondoa kabisa mvuto wa usanifu wa majengo haya na urembo wa gharama kubwa ulioyapamba kwa ndani. Yaliyobakia leo ni magofu au kuta ambazo zinaelezea kidogo tu juu ya kiwango cha ustaarabu wa wakati huo.

Michoro ya rangi ya Ethiopia ilijionyesha zaidi katika aina mbili: michoro ya rangi ya kuta za kanisa na michoro iliyokuwemo kwenye vitabu vya dini. Ingawa hakuna michoro mingi ya kanisa ya kabla ya karne ya kumi na saba iliyobaki, lakini miswada mingi ilyopo imetoka nyuma kwenye karne ya kumi na nne na inaonyesha kwa usahihi maendeleo ya aina hii ya michoro ya rangi. Karibu na mwaka 1500, michoro katika vitabu ilifikia kiwango cha juu kabisa sawa kabisa na kiwango cha ustaarabu wa Kikristo wa Kiethiopia. Hata nje ya matini iliyokusudiwa kuelezea, michoro hii ililenga katika kuwavutia watazamaji kwa nguvu ya taswira zake na kuimarisha imani yao. Michoro ya rangi ya nusu ya pili ya karne ya kumi na sita na

ile ya mwanzo wa karne ya kumi na saba, ni tofauti. Inaonyesha wingi wa athari kutoka nje ambazo sasa zinaingia Ethiopia. Mfano mzuri ni muundo wa msalaba ulioigwa na wachoraji wengi wa Kiethiopia - ambao ni nakala ya mchapo wa picha maarufu iliyochongwa kwenye muhuri wa ubao na kutolewa katika kitabu cha *Small Passion* na mchoraji na mwanavielelezo wa Kijerumani, Albrecht Durer. Picha zote hizi zinatoa ushahidi kuhusu uwezo mkubwa wa Waethiopia katika kuingiza miundo ya kigeni kwenye utamaduni wao. Pia ni kielelezo cha kipindi cha ghasia kilichotawaliwa na migogoro dhidi ya mambo ya nje ambayo hayakuweza kujioanisha na mtindo asilia wa sanaa ya Ethiopia.

Picha za (Urejesho) *Restoration* za Kipindi cha Gondari hatimaye zinajipambanua juu ya nyingine zote kutokana na uzuri wa kifahari na madaha ya maumbo yake. Zinaonyesha kupotea polepole kwa utukufu wa himaya, na zimechorwa kwa ajili ya jamii ya wapambe wa mfalme ambao hufurahia madaha na maumbo yake ya kidesturi. Katika kile kinachoitwa kipindi cha Pili cha Gondari, kuanzia kama mwaka 1700, msukumo wa ubunifu wa kisanaa ulianza kupotea hatua kwa hatua, na hatimaye kuishia katika kanuni za miundo inayojirudiarudia.

## *Kusini-magharibi mwa Ethiopia: kuibuka kwa utamaduni mpya na madola mapya*

Maandishi ya Kikristo na Kiislamu yanatufahamisha vizuri kuhusu mahusiano kati ya kusini-magharibi mwa Ethiopia na himaya ya Kikristo ya kaskazini kati ya 1500 na 1700, lakini hayatuwezeshi kukisia kiasi cha athari ambayo Ethiopia ilikuwa nayo zaidi ya utawala wa kisiasa na utozaji wa hongo.

Mapokeo simulizi yaliyosalia leo katika Ethiopia ya kusini yana utajiri wa maelezo ya kihistoria ambayo kwa bahati mbaya bado hayajaandikwa kwa ukamilifu. Mtiririko wa nasaba, mchanganuo wa tamaduni na matokeo ya akiolojia pia yanatoa madokezo muhimu na kuonyesha kuwa athari ya kaskazini juu ya kusini ilikuwa kubwa sana kiasi cha kusababisha kuibuka kwa utamaduni mpya.

Hali ya utamaduni ya Ethiopia ya kusini kabla ya karne ya kumi na tano, wakati kaskazini ilipoanza kuwa na athari, inaweza kufahamika kwa kuchunguza utamaduni wa sasa wa makundi ya kikabila ambayo hayakuguswa na athari hii mpaka hivi karibuni. Makundi ya aina hii yanapatikana miongoni mwa Wagimira, Waare na Wadizi, ambao hadi hii leo hawana miundo ya kidola wala asasi za kisiasa zilizokomaa.

Kabla ya kutokea kwa mabadiliko makubwa kutokana na kichocheo chenye kukua kilicholetwa na himaya ya Kikristo ya kaskazini, kiasi kikubwa cha koo ndogondogo huko kusini lazima ziliishi pamoja, zikiunganishwa na kiungo chepesi tu cha kuchangia lugha na utamaduni mmoja, kujitambua kama watu wa nasaba moja, na labda kumuenzi kuhani mkuu au mzee ambaye aliwakilisha uhusiano wa kidini wa kikundi. Mzee huyo alikuwa na hadhi fulani ya kidini kutokana na uhusiano wake wa

kinasaba na mwanzilishi wa kikundi, na pia alihusishwa na nguvu za kimiujiza, hasa juu ya mvua, mazao na mavuno. Kwa kulinganishwa na dhima yao ya kidini, dhima ya kisiasa ya waheshimiwa hawa ilikuwa kidogo mno. Waliohodhi nguvu za kisiasa ni koo huru, ambazo mwanzoni zikijitosheleza, na viongozi wake.

Washindi waliotokea kaskazini na dhana zao zisizobadilika kuhusu dola na ufalme, walivamia dunia hii isiyo na makuu ya wakulima wa kawaida. Ushindi na usimilishaji mara nyingi ulifanyika kwa amani; watu wa kusini wakiutambua utamaduni bora wa kaskazini. Hivyo ushindi wa jimbo ambalo baadaye lilikuja kuwa dola muhimu la Wolayta inasemakana ulitokana na ujanja wa kisiasa wa wavamizi. Katika mapambano ambayo yalihusisha vikundi vidogovidogo, watu wa kaskazini, badala ya kuwarushia mikuki wapinzani wao, waliwarushia vitambaa, shanga au vipande vya nyama. "Kama nyinyi ni matajiri na wenye nguvu kiasi cha kutupa ovyo mali namna hiyo, basi mtatutawala" wakasema Wawolayta. Hivyo wavamizi walichukua nchi ambayo chini ya athari yao waliweza kuibadilisha katika muda mchache kuwa dola lenye ari na uchokozi.

Ilikubalika mara nyingi bila ubishi kuwa madola yaliyoongozwa na wafalme, ambayo yalijisheneza silaha nzuri na kuwa na askari wa farasi, jambo lililokuwa halifahamiki asilani sehemu ya kusini, yalikuwa bora kuliko jamii zizoundwa kidemokrasia. Hivyo kuna taarifa ya vikundi kusalimu amri kwa kupenda kwao kwa wavamizi na kuwakubali viongozi wao kuwa watawala wao wapya.

Kwa njia hii mlolongo mzima wa madola mapya yalianzishwa, madola ambayo hayakuweza kusahau uhusiano wao na kaskazini, na ambayo matabaka tawala yao yalihifadhi na kuendeleza kwa uaminifu mila na asasi za kaskazini.

Na zaidi ya muundo rasmi wa nje wa mpangilio wa dola na maisha ya kitala, kisasili cha himaya ya Ethiopia pia kilichangia athari yake. Kisasili hicho kilidai kuwa wao walikuwa ndio taifa teule na ufalme wao ndio wa kweli, na kuwa walikusudiwa kutawala na kusimilisha majirani wote. Kama inavyojulikana kutokana na miaka 400 ya mapokeo simulizi, historia ya Ethiopia ya kusini ni hadithi ya utanuzi wa madola haya madogo yaliyoanzishwa karibuni, ambayo yaliongeza mipaka ya utawala wao kwa kuvichukua vikundi huru vidogo vidogo, na mara kwa mara yalichangia katika kuanzisha nasaba tawala miongoni mwa majirani zao. Mchakato huu ulifanyika kimzunguko. Hivyo kutokana na mapokeo simulizi, Inariya, dola la kwanza la Kigonga, ilianzishwa kabla ya 1500 na mhamiaji kutoka Tigre. Watu wa nasaba ya kifalme ya Busaso ya Inariya, kwenye karne za kumi na sita na kumi na saba, walianzisha milki nyingine: Bosa, ambayo ilimezwa na ufalme wa Kioromo wa Gimma katika karne ya kumi na tisa Kaffa; ambayo inasifika kuwa nchi iliyokuwa na nguvu zaidi kwa vizazi vingi katika Ethiopia ya kusini mashariki yote; na Sekko (Mocca) iliyo katika misitu asilia iliyopo kwenye ukingo wa magharibi wa milima ya Ethiopia.

Mapokeo simulizi yanaelezea kuwa hapo mwanzo ufalme wa Gangero ulianzishwa na wahamiaji Waislamu kuto ka Arabia. Baadaye nasaba asilia ya kifalme ya Kikristo

kutoka Gondari ikatawala. Maelezo yenye kufanana na hayo yanapatikana kuhusiana na eneo linalokaliwa na Waometo: yanasema kwamba huko Dawaro kikundi kingine cha wahamiaji waliojivunia asili yao ya Kigondari kilifanikiwa, baada ya miaka mingi ya mapambano, kuviunganisha vikundi vidogo vidogo vya wakazi wa asili kuwa dola lenye nguvu. Karibu na mwaka 1600 wazao wa mtu mmoja aliyeitwa Sum Tamben kutoka Tigre waliishinda Wolayta. Madola mengine, makubwa na madogo, pia yana mapokeo kama haya. Wana-nasaba ya kifalme ya Gosanaa, ambao huenda asili yao ni Ethiopia ya kaskazini, walianzisha jumla ya miliki kumi.

Katika Ethiopia ya kusini, mfumo wa jamii hapo awali ulikuwa ukiundwa kwa kuishi pamoja na kwa makubaliano miongoni mwa watu huru na sawa. Ni viongozi wa dini na mashujaa wa vita pekee waliopata marupurupu machache. Lakini katika nchi mpya zilizoundwa kutokana na athari ya dhana ya utawalamsonge wa kaskazini ya Kikristo, mambo yalikuwa tofauti. Mfumo tata wa msonge wa madaraja ya watu ulichukua nafasi ya usawa. Kileleni alikuweko mfalme mtukufu, asiyefikika na ambaye hakuwa rahisi kuonekana na watu wake. Familia yake tukufu ilipata marupurupu maalumu na mara kwa mara walishika nyadhifa muhimu za dola. Ufahari na itifaki zilizokithiri za nyumba za kifalme zilikuwa mara nyingi hazilingani na eneo dogo la nchi na watu wake. Kadiri falme zilivyozidi kuwa kubwa, ndivyo nyumba za kifalme nazo zilivyozidi, zikawa asasi huru zenye nguvu na mamia ya watu. Zilikuwa tofauti kabisa na zile za makuhani wakuu au viongozi wa koo ambao waliishi kwa jasho lao wenyewe na lile la familia zao, na zawadi za hiari kutoka kwa watu wengine.

Ukubwa ambao baraza la kifalme lingeweza kuwa nao unaonyeshwa na Wolayta, iliyoko kaskazini mwa Ziwa Abbaya. Hapa baraza la kifalme halikuwa tu kitovu cha maisha ya kisiasa bali pia wilaya takatifu, ikilindwa na wingi wa miviga na sheria za itifaki. Mfalme alipotoka hadharani, ama aliwekwa mbali na watu, ama alizungukwa na wafuasi wake. Baraza la kifalme lililindwa na ngome tatu na malango matatu, kila moja likiwa limefungwa kwa makomeo matatu. Ni mfalme tu aliyeweza kuchinja wanyama kwenye ardhi ya makazi yake matukufu, au kufanya aina yoyote ya ngono. Hivyo watumishi ambao walihudumia nafsi ya mfalme hawakushiriki katika ngono, na walikatazwa vikali, kama watumishi wa Maliki wa Ethiopia ya Kikristo, kutoka nje ya eneo la Ikulu na na kukutana na watu wengine. Ardhi ilipojengwa Ikulu ilikuwa tukufu sana kiasi kwamba ngono yoyote kati ya mwanamume - isipokuwa mfalme - na mwanamke ingesababisha kifo cha wakosaji na kuhamishia Ikulu mahali pengine.

Kutokana na athari ya kaskazini, alama za ufalme zilibadilishwa. Awali alama hizi zilikuwa vitu vya ishara visivyo ghali na vyenye muundo rahisi kama vile mkuki mtukufu, umma wenye ncha mbili au kamba ya majani. Nafasi ya vitu hivyo sasa ilichukuliwa na pete, hasa za vidoleni au mkononi, zilizotengenezwa kutokana na vito vya thamani vya dhahabu na fedha, ambavyo vilikuwa alama ya ufalme katika Ethiopia Kuu.

Athari ya Ethiopia Kuu ilikuwa na matokeo makubwa katika mfumo mzima wa jamii. Ingawa sehemu kubwa ya Waethiopia wa kusini walikuwa katika tabaka moja la watu wenye kulinganalingana, mfumo changamani wa madaraja uliofuata mtindo wa Ethiopia ya Juu ulichipuka. Mfumo huu ulijitambulisha na tanzo ya "thamani ya mtu" iliyoenea Ethiopia yote. Thamani ya mtu haikuweza kurithiwa kama vile utajiri au jina la kuheshimika, bali ilibidi itafutwe kwa juhudi ya kila mtu peke yake ili aweze kupata heshima aliyostahiki katika jamii. Kigezo kikuu kilikuwa ni mafanikio vitani na katika uwindaji wa wanyama wakali, na wajibu wa kuua alio nao mpiganaji. Ni yule tu aliyejipatia thamani kutokana na matendo yake ndiye angeweza kutaka achaguliwe kushika mojawapo ya nyadhifa nyingi za kuchaguliwa, ambazo upatikanaji wake ndicho kilikuwa kipimo cha hadhi ya mtu. Jina na cheo mara nyingi vilitajwa kwa neno lilelile, na kukosa jina kulikuwa sawa na kushindwa katika jamii. Hapa pia athari ya kaskazini iwazi, kwani majina ya vyeo hivi yamechukuliwa kutoka kwenye lugha ya Kiamhari au Kitigrai.

Kwa daraja, wukulima huru walifuatiwa na mafundi mchundo, ambao walikuwa katika matabaka-amali mahsusi na walikuwa katika daraja la chini zaidi kuliko wakulima. Licha ya umuhimu wao mkubwa wa kiuchumi, bado walipuuzwa. Hawakuruhusiwa kumiliki ardhi, walitakiwa kufuata kanuni zenye kuwadhalilisha, na, kwa muungwana, kugusana nao kimwili kulichukuliwa kuwa ni kujidhalilisha.

Chini kabisa walifuata watumwa, ambao, katika nchi nyingi, walikuwa zaidi ya theluthi moja ya watu wote. Wengi waliishi kama watwana katika mashamba ya mabwana zao, lakini waliweza kumiliki mali. Jasho lao na tija yao ndiyo iliwezesha kuwepo kwa tabaka tajiri lenye nguvu ambalo, mathalani huko Wolayta, ndilo lililoongoza vita vikubwa vya utamalaki.

Madola yote haya yalikuwa na watawala walioelimika waliochaguliwa na watu na kuthibitishwa kwenye kazi zao na mfalme. Madola yaligawanyika katika jumuiya, wilaya na majimbo. Yalikuwa na masoko ya umma ambayo yalisimamiwa na serikali na mtandao mzuri wa barabara. Ngome kubwa na kuta zenye milango yenye ulinzi ulio makini ziliwalinda na maadui wa nje.

Maendeleo ya vitu yaliyoletwa kutoka kaskazini hadi kusini tangu karne ya kumi na nne ni mengi. Inashangaza kwa kiwango fulani kuwa chombo muhimu kuliko vyote huko kaskazini, plau, hakikupata kukubalika kusini. Hata hivyo kilimo kilinufaika na mazao mengi yaliyoingizwa kutoka kaskazini. Ilikuwa labda baada ya karne ya kumi na nne au kumi na tano ambapo njegere, maharagwe mapana, dengu, vitunguu na vitunguu saumu viliingia kusini. Baadaye pakafuatia adesi na aina tofauti ya mbegu za mafuta, zikiwemo mbegu za kitani, ufuta, alizeti na *nogo,* zote kutoka Mashariki ya Karibu. Baadaye ikafuatia mimea ya Dunia Mpya iliyoletwa Afrika, labda na Wareno, kutoka Amerika baada ya zama za Kolumba (Christopher Columbus). Kati ya mimea hii, pilipili nyekundu, mahindi na tumbaku ni ya maana sana leo kiasi kwamba ni vigumu kufikiria maisha katika Ethiopia ya kusini bila mimea hiyo. Maboga, viazi vitamu, viazi mbatata na nyanya vilienea kwa kiwango kidogo.

Mpaka leo mbinu zinazotumiwa na dhuria wa mafundi michundo kutoka kaskazini bado zinaonyesha msukumo waliyoipatia sekta hii: ufumaji wa kutumia kifumio cha mdoshi *(treadle-loom)*, uhunzi wa dhahabu na fedha kwa kutumia vifaa vya kitaalamu, ushonaji wa ngozi kwa sindano, na urandaji wa mbao za kutengenezea mabamba ya milango, chano za mbao na mabakuli makubwa. Mwisho kuna haja ya kugusia kuingia kwa farasi katika sehemu ya kusini, ingawa hakukuwa na umuhimu wa kiuchumi, kwani alitumiwa kweye vita pekee na kwa kuonyesha ufahari tu.

Sasa tuangalie mvuto wa Kikristo: Je, ulikuwa na nguvu ya kutosha kuwa na athari ya kudumu huko kusini na kutoa mwelekeo wa kudumu? Hata hii leo ni dhahiri kuwa athari ya kitamaduni ilikuwa kubwa sana, mabaki yake yakiwa bado yanaonekana hadi kwenye mipaka ya Kenya na Sudan. Ni vigumu zaidi kutathmini athari za Ukristo katika mfumo wa maadili wa kila utamaduni wa kienyeji, katika desturi na matumizi yake, na katika maisha ya kiroho kwa jumla.

Kumbukumbu za Kikristo zenye kuvutia sana katika eneo hili, ambalo halikuhifadhi kumbukumbu nyingi za kazi za binadamu, ni misitu mitukufu mingi, hasa juu ya vilima na kwenye vilele vya milima, ikionyesha sehemu zilizokuwa na makanisa ya Kikristo kama majina yao yanavyoonyesha: *Kitosa* (Yesu) *Mairamo* (Mariamu) au *Gargisa* (George). Mali ghafi iliyotumiwa kuyajenga haikuwa ya kudumu, hivyo yote yametoweka. Hata hivyo maeneo hayo bado yanachukuliwa kama matukufu, na wazawa wa mapadre wa Kikristo wa zamani ambao wamekuwa wanachama wa koo zisizo za Kikristo bado wanaendesha sherehe ambazo ni tabdili za sadaka ya misa.

Bado utafiti wa uhakika haujafanywa ili kuona ni kwa vipi Ukristo, kama chombo cha kidini, na siyo kama mkusanyo tu wa viviga, uliathiri kiini cha maadili ya kidini ya Ethiopia ya kusini. Dhima isiyo ya kawaida ya Mariamu, ambayo inamweka nyuma Yesu Kristo, pia inahitaji utafiti. Jukumu la Mariamu, mungu mwenye kusaidia na kusamehe, hasa kwa upande wa wanawake, linaweza kuonekana katika Ethiopia ya kaskazini na kusini.

Kwa sura ya nje, kiasi kikubwa cha sheria na sherehe za Kikristo zilibakia huko kusini hadi hivi karibuni, wakati kanisa la Orthodox la Ethiopia lilipoanza tena kazi ya Umisionari. Kufunga katika siku maalumu kuliendelea, halikadhalika kuheshimu siku ya Sabato, ambapo kazi zote za shambani zilikatazwa, walau kwa warithi wa mapadre wa Kikristo wa zamani. Wiki ya Kikristo ya siku saba, iliyoratibu mpangilio wa siku za gulio, iliendelea kufuatwa. Jumapili za Kikristo sasa zimekuwa sikukuu za kiserikali, ambapo ma-*kesiga* (warithi wa mapadre wa Kikristo) wanakutanisha pamoja waumini wao na kufanya ibada fupi za kumwomba Mungu, Yesu na Mariamu, wakipiga alama ya msalaba na kuchoma nafaka badala ya ubani. Miongoni mwa sikukuu kubwa za Kikristo, Karamu ya Msalaba Mtakatifu (27 Septemba) ilikuja kuwa Karamu ya Mwaka Mpya, ambapo mashetani walikemewa na kulifanyika sherehe kubwa. Kristmasi na Epifania, siku zilizokuwa kuu kaskazini, zilisherehekewa na jamii chache za kusini, ambapo Pasaka iligeuzwa kuwa siku ya Mviga Mkuu wa Uwindaji


# 25 Afrika Mashariki: pwani

Karne za kumi na sita, kumi na saba na kumi na nane zilianza kwa kuja kwa Wareno katika miji ya Afrika Mashariki na kuishia na Waarabu wa Omani kujaribu kuanzisha aina fulani ya usultani katika pwani. Katika karne hizo tatu, miji ya pwani na jamii zake zilipitia katika mabadiliko makubwa ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.

## *Eneo la pwani mwanzoni mwa karne ya kumi na sita*

Mwaka 1500, pwani ilikuwa bado inajibwea katika "enzi yake ya fanaka." Masalio ya magofu na utamaduni wa vitu wa karne za kumi na tano na kumi na sita unatoa picha ya jumla ya mafanikio. Bali uchunguzi wa karibu zaidi unaonyesha kupitana kwa hali za ustawi wa kiuchumi na kimaisha.

Kilwa, ambayo ilikuwa ikistawi katika karne ya kumi na tano kutokana na kumiliki biashara ya dhahabu ya Sofala, iliyoidhibiti tangu mwanzo wa karne ya kumi na nne, ilikuwa ikionyesha dalili za awali za kuporomoka kwenye mkesha wa kuwasili kwa Wareno. Kufikia mwishoni mwa karne ya kumi na tano, Kilwa ilipoteza mamlaka juu ya Sofala, na athari yake ya kisiasa ilikuwa ikipungua kwenye upwa wa kaskazini, eneo lililokuwa muhimu kwake kiuchumi. Mabadiliko ya mserereko yaliyoipata - kiasi cha kuwa na watawala 13 kati ya 1442 na 1498 - yalikuwa kielelezo cha matatizo ya kisiasa ambayo yaliivunja nguvu. Aidha, mahusiano yake mabaya na Zanzibar yalionyesha udhaifu sugu wa miji ya Kiswahili wa kugombana wenyewe kwa wenyewe ambao ulirahisisha uvamizi wa mataifa ya nje. Mwaka 1454, Zanzibar ilikuwa ikijitahidi kumuweka mteule wake awe mfalme wa Kilwa. Hata hivyo Zanzibar, wakati huu, haukuwa mji wa pwani ulioongoza kisiasa au kiuchumi. Ulikuwa wenyewe umegawanyika katika karibu vitongoji vitano kila kimoja na mtawala wake. Hata hivyo Mombasa ilichuana na Kilwa na Malindi kama miji iliyoongoza. Wafanyabiashara wake waliongoza katika biashara ya pwani ya kusini hadi Angoche. Mji huu wa kisiwa pia ulianzisha mahusiano ya kibiashara na bara yake katika asali, nta na pembe, mahusiano ambayo yanaweza kuelezea kukua kwa ghafla kwa Mombasa hadi kuwa "jiji lenye nguvu kuliko miji yote ya pwani" wakati Wareno walipoingia (E.A. Alpers, 1975).




**25.1** *Pwani ya Afrika Mashariki* (A.I. Salim)

Malindi, ambao ulikuwa mpinzani mkubwa wa Mombasa, pia ulikuwa umeendelea ilipofika mwaka 1500. Biashara yake ilikuwa zaidi katika kusafirisha nje pembe na kiasi kidogo cha biashara nyingine kama ya nta, ambari na sandarusi. Tofauti na makazi mengine katika ukanda huu, hata katika karne ya kumi na sita Malindi ilikuwa na mashamba makubwa ya mtama na mpunga yaliyolimwa na watumwa.

Juu zaidi upande wa kaskazini sultani ndogondogo zilipatikana katika achipelago (funguvisiwa) ya Lamu, ambazo takribani zilikuwa katika ugomvi wa kudumu na hivyo kushindwa kuweka upinzani wa pamoja dhidi ya wavamizi wa Kireno. Hadi katikati ya miaka ya 1300, Lamu ilikuwa tayari ipo kwenye eneo lake la sasa, lakini ilianza kusitawi baada ya 1650.

Kati ya haya makazi makubwa ya biashara yalikuwepo mengi mengine madogo ambayo mara kwa mara yalijikuta yakitii amri za mojawapo ya miji mikubwa. Miji mikubwa ilijihusisha zaidi na biashara ya majini ya kimataifa kuliko ile midogo, iliyotegemea kilimo na uvuvi. Idadi ya makazi iliongezeka sana kati ya 1200-1800 - enzi ya fanaka ya pwani.

Ni vigumu kukadiria ukubwa wa makazi hayo kwa eneo na kwa watu. Inasemakana Malindi iliwahi kuwa na watu wanaokadiriwa kufikia 3,500 mwaka 1498 kutokana na nyumba 1,000 za mawe kukaliwa na watu, lakini idadi hii haiwahusishi wafanyakazi wa mashambani au maskini, ambao bila shaka waliishi katika vibanda vya udongo na nyasi. Kumomonyoka kwa pwani kisiasa kulifidiwa na umoja wa kidini na kitamaduni ambao ilipofika 1500 ulikuwa umejiimarisha vizuri. Makabila ya Kiafrika, Kiarabu na Kishirazi yaliingiliana kwa viwango tofauti kufanya kikundi kipya cha utamaduni kilichokuja kujulikana kama Waswahili (watu wa Mwambao). Waswahili ni jina la jumla ambalo watu wa mwambao walijiita hapo baadaye. Katika miaka ya 1500 walianzisha vikundi vya mijini ambavyo familia zake za waali na watawala, kwa sababu za ufahari, mara nyingi ziiidai bila sababu za msingi kuwa ni za asili ya Uarabuni au Ushirazi, hata kama zilikuwa zimechanganya mbari.

Wakati pwani ilikuwa imegawanyika kisiasa na wakazi wake walitokana na makundi tofauti, mambo mbalimbali yaliwaleta pamoja. Yaliyokuwa muhimu sana ni Uafrika wao na lugha ya Kiswahili, ambayo punde ilikuwa igeuke kuwa *lingua franca* (lugha-kiungo) ya pwani. Athari nyingine muhimu ni Uislamu, na kwa kiwango kidogo, athari ya Uarabu, ingawa hiyo ilikuja kutamalaki katika karne ya kumi na tisa tu.

Ukweli ni kuwa utamaduni wa Kiswahili ni mfano wa kikanda wa utamaduni wa Kiislamu. Ni wa kikanda kwa sababu uliathiriwa na utamaduni asilia wa Afrika Mashariki ambao kwa kiasi kikubwa uliingizwa ndani yake. Ingawa Kiswahili kwa miaka mingi kilichukua kiasi kikubwa cha maneno ya Kiarabu, lakini ndicho kipengele muhimu kuliko vyote kinachoonyesha mchango mkubwa wa Uafrika katika utamaduni wa Kiswahili. Mengine, na sio kusema sio muhimu, ni pamoja na miviga

inayohusiana na uzazi na ndoa, ibada za mazishi na usimikaji wa machifu, imani ya mizimu na ngoma za kijadi.

Ukwasi wa mali wa baadhi ya miji ya pwani mwaka 1500 ni wa kuajabia. Watawala waliishi katika makasri na waali katika makazi ya mawe yaliyokuwa na milango ya mbao iliyochongwa kiufundi. Maisha mazuri ya watu wa mjini yanaonekana katika uingizaji wa vitu vya anasa kama damaski, hariri, nguo za satini (zenye kung'aa), vitu vya shaba, vyombo vya udongo vya sini, vyombo vya kioo vya Mashariki ya Kati na shanga za kioo. Hata hivyo, ni wachache tu walioishi maisha ya ufahari, ambapo maskini na watumwa waliokuwa wengi waliishi katika vibanda vya udongo na nyasi.

Idadi kubwa ya watu walioishi katika makazi haya ni Waafrika na Waarabu wachache ambao idadi yao iliongezeka kwa kiasi kikubwa katika karne za kumi na nane na kumi na tisa. Ingawa watawala pengine walichukua, kwa usahihi, majina ya nasaba za Kiarabu, lakini walikuwa bila ubishi machotara na mara nyingi weusi. Rangi haikuwa na umuhimu wa kijamii au kisiasa; ukoo ndio uliomtofautisha mtu na kuonyesha nafasi yake na kiwango cha kujumuika kwake katika jamii hiyo.

## *Maingilio ya Wareno*

Wareno, kama majirani zao Wahispania katika rasi ya Iberia, walianza safari zao za upelelezi wakiwa bado wanakumbuka vita vyao dhidi ya Waislamu. Sababu za safari za Wareno zilikuwa ni kujaribu kuwazidi Waislamu kibiashara, kisiasa, kijeshi na kidini- kuvunja uhodhi wa Mamluki (baadaye Waturuki) wa njia za biashara kwenda Asia na China, na kuungana na Wakristo wengine kuondoa utawala wa Kiislamu popote utakapoonekana.

Mwanamfalme Henry, Mtunukiwa Mkuu wa Nishani ya Kristo, ndiye aliyebuni mkakati wa Wareno, na safara nyingi zilifanywa ili kutekeleza mpango wake. Januari, 1498 kundi la manowari za Vasko da Gama zilifika kwenye ukingo wa kusini kabisa wa pwani ya Waswahili kwenye mdomo wa mto Kilimani, ambapo Wareno waliyakuta makazi ya Waafrika-Waarabu ambayo yalikuwa na mawasiliano na nchi zilizotamaniwa sana za mashariki, ambazo ni kisiwa na mji wa Msumbiji, uliokuwa umeingia katika himaya ya Kilwa. Shehe wa pale aliwakaribisha mpaka alipogundua kuwa hawakuwa Waislamu, ambapo kutoaminiana kukasababisha migongano ya kwanza kati ya Waislamu na Wareno. Mapokezi ya Vasko da Gama Mombasa yalikuwa ya uhasama kwa sababu habari za mgongano uliotokea Msumbiji zilimtangulia. Katika hali tofauti Shehe wa Malindi alimpokea vizuri. Pande hizi mbili ziliunda umoja na Shehe wa Malindi aliitwa Mombasa mwishoni mwa karne ya kumi na sita. Safari ya Kwanza ya Vasko da Gama ilifaulu katika lengo lake la kufika India. Pia ilipata habari nyeti kuhusu biashara ya Waislamu katika pwani ya Waswahili na utajiri wa miji ya Kiswahili kama Msumbiji, Mombasa, Malindi uliwapendeza Wareno. Safari hii iliyokuwa hasa ya upelelezi ilifuatiwa na nyingine.

Safari moja mwaka 1501 iliwapa Wareno fununu kuhusu ukubwa wa Kilwa, lakini Shehe wake Ibrahim hakuweza kushawishika kusaidiana nao katika kuanzisha uwakala wa biashara katika Sofala.

Hivyo wakaamua kutumia nguvu. Mwaka uliofuata, vyombo vya Vasko da Gama huku vikisindikizwa na milio ya mizinga, viliingia kwenye bandari ya Kilwa. Ibrahim alikubali kulipa kodi ya mwaka na kuwa mtwawa wa Mfalme wa Wareno baada ya kutishiwa kuwa mji wake ungeteketezwa iwapo angekataa. Mwaka 1503, Ruy Lourenço Ravasko alifanya unyang'anyi na uharamia kwenye eneo linalozunguka Zanzibar kabla ya kuingia na kutumia nguvu kupata ushuru. Mwaka 1505, Dom Fransesko de Almeida, ambaye baadaye alikuwa gavana wa India, aliishambulia Kilwa kwa kisingizio kuwa mji ulikuwa nyuma katika malipo ya kodi na haukutundika bendera ya Kireno kama ishara ya utii.

Akitumia vizuri kutokuelewana miongoni mwa vikundi vilivyokuwepo, de Almeida alimsimika kibaraka wa Wareno Muhamad Ankoni kuwa mtawala, na Kilwa ikagharamia ujengaji wa ngome ya kwanza ya Kireno katika pwani ya Waswahili.

Mombasa ilimuonyesha Vasko da Gama uadui mwaka 1498, na Agosti 1505 ilikaribisha manowari za de Almeida kwa risasi za mzinga ulioopolewa kutoka kwenye merikebu ya Kireno iliyozamishwa. Mfalme wa Mombasa na watu wake waliwapa Wareno upinzani mkali lakini hatimaye mfalme alilazimishwa kusalimu amri. Kabla ya manowari kuondoka, mji uliporwa na kuchomwa moto. Inaelekea kuwa nia ya Wareno ilikuwa kuvunja nguvu ya Mombasa ili kuiongezea nguvu Kilwa, ambayo ingekuwa ngome yao kuu.

Kudhihirisha kuwa vitendo vya Wareno vilikuwa dhahiri vya kuadhibu, Mombasa ilishambuliwa tena mwaka 1528 na kumilikiwa kwa miezi minne. Umiliki huu mfupi, ambao uliisha kwa mji kuchomwa moto, haukuwapatia Wareno chochote isipokuwa upotevu wa maisha kwa wengi wao kutokana na mapigano na magonjwa.

Miaka kumi na sita kabla, kwenye mwaka 1512, Wareno walikuwa wamelazimika kuihama ngome yao ya Kilwa. Wakati huo Wareno walikuwa wamekwisha ng'amua kuwa kuna kiwango cha kodi ambacho mji ule ungeweza kukilipa na kuwa kiwango hicho kisingetosha kuhudumia kikosi cha askari wao. Walitarajia kuhodhi biashara ya dhahabu ya Sofala, lakini badala yake walifanikiwa kuivuruga kutokana maingilio yao na udhibiti wao wa kibiashara ambao haukufikiriwa kwa makini. Kufikia mwaka 1506 kikosi kilichokuwa Sofala kilikuwa hakifai tena kutokana na kukumbwa na magonjwa, na mwaka 1512 kikosi cha Kilwa kilihamishiwa India.

Biashara ya Kilwa iliongezeka sana baada ya Wareno kuondoka, ingawa mtawala wake alibakia kwa jina kuwa mtwawa wa Mfalme wa Ureno. Mpangilio wa biashara mjini hapo ulipata mabadiliko ya kuvutia. Wafanyabiashara wake sasa walikwepa Sofala iliyotawaliwa na Wareno na kutafuta uhusiano zaidi na pwani ya Angoche kusini mwa Msumbiji, ambayo ilikwisha kuwa, kwa muda mrefu, na mahusiano ya

kibiashara na bara ya Zambezi. Nia yao ilikuwa kudhoofisha mamlaka ya Wareno juu ya Sofala, na ili kuzuia mpango huu, Wareno waliingia bara na kuanzisha makazi Sena na Tete.

Kilwa ilitegemea sana biashara ya dhahabu na pembe ambayo wafanyabiashara wake waliileta kutoka Zimbabwe, kwani haikuwa na vitu vingi vya kuuza nje. Mara Sofala ilipotoka mikononi mwake, ilibidi Kilwa ianzishe mahusiano ya kibiashara na bara, na pembe ikawa biashara yake kubwa ya kusafirisha nje. Kubadilika huko kwa biashara ya Kilwa kulioana na upanuzi wa Wamaravi na Wayao.

Kwa kumalizia, ni kwamba Wareno walishindwa kubuni sera bayana ya uvamizi au utawala kwenye pwani ya Waswahili. Walikuwa na hamu ya kimamluki pekee ya kuhodhi nyendo zote za biashara. Hata katika hili waliweza kufanikiwa kwa kiwango kidogo. Kutokana na uvamizi wa Kireno kuwa mfupi sana, miji ya Kiswahili iliweza kuendelea na shughuli zao za kibiashara.

Wengi wanasema kuwa tokea mwanzo, maslahi ya Wareno yalikuwa mashariki; pwani ya Waswahili ilichukuliwa kama kisehemu tu cha *Estado de India* (dola la India), makao yake makuu yakiwa Goa, ambako gavana wa Kireno alikuwa na makao. Hata hivyo, Wareno walimteua "Kapteni wa Bahari ya Malindi," ambaye alikabidhiwa merikebu ndogo chache ili kufanya doria kwenye pwani ya Afrika Mashariki. Kadhalika, alikuwa na jukumu la kutoa vibali kwa vyombo na kuendesha karakana ya biashara ya Wareno iliyokuwako Malindi. Karakana hii iliingiza pamba na shanga kutoka India, ambavyo ilivibadilisha kwa vitu vya palepale kama sandarusi, ambari, pembe na makumbi ya nazi. Huu ni ushahidi wa shauku ya Wareno ya kushiriki katika biashara ya Kiafrika ya pwani na bara.

Mpaka ujio wa tabaro za Waturuki katika miaka ya mwisho ya 1500, vyanzo vya habari vinatoa maelezo finyu sana kuhusu pwani ya Waswahili. Inaelekea kuwa hali halisi ya mambo ilifanya makubaliano ya kisiasa na kiuchumi kuwezekana. Miji ya Waswahili ilibakia kuwa huru ilimradi hakukutokea mgongano wa kimaslahi na Wareno. Baadhi ya miji iliathirika vibaya kuliko mingine. Mombasa ilirudia hali yake ya kawaida baada ya kipigo ilichokipata kutoka kwa Wareno kwa kisingizio cha kulipiza kisasi, na mwaka 1569 ilielezewa na Padre Monclaro kuwa mji "mkubwa na wenye watu wengi"; lakini alikuta Kilwa ikiwa karibu haina watu kabisa, ingawa ikiendelea kufanya biashara ya pembe na visiwa vya Komoro na bara. Wakati huu jambo ambalo athari zake ni ngumu kupima kuliko lile la kuwepo kwa Wareno lilijitokeza: nyendo za watu katika bara na athari zake kwa miji ya Waswahili.

Mara walipoingia katika Bahari ya Hindi, Wareno walisababisha chuki, sio tu kutoka kwa watawala wenyeji wa Kiislamu, bali pia kutoka kwa Mamluki wa Misri. Baada ya kushindwa kwa Mamluki na Waturuki mwaka 1517, uongozi katika mapambano dhidi ya mvamizi Mreno ukamwangukia Sultani wa Kituruki wa Konstantinople. Mapambano kadhaa yalitokea katika pwani ya magharibi ya India na katika ghuba ya Uajemi. Ndipo, mwaka 1570-71, uasi ukatokea katika eneo lenye kudhibitiwa na Wareno la Hormuz, ambalo wakazi wake waliomba msaada kutoka

Uturuki. Uasi huo ulizimwa, lakini mfano wake uliigwa na miji mingine.

Mfalme wa Ureno alimshauri gavana mkuu wa Goa kukomesha tabia mbovu ya maofisa wa Kireno waliokuwepo katika pwani ya Waswahili, tabia ambayo mashehe wa Kiswahili waliilalamikia kwa mfalme. Mfalme aliogopa kuwa viongozi hawa wangeomba msaada wa Waturuki kuwasaidia kujikomboa kutokona na utawala wa Wareno. Matukio yaliyofuata yalidhihirisha kuwa woga huu ulikuwa na msingi. Wakati Mir Ali Bey alipotokea na merikebu moja mwaka 1585, alipokewa kwa furaha na miji yote ya Waswahili kati ya Mogadishu na Kilwa, isipokuwa Malindi. Aliondoka akiacha ahadi ya kurudi na jeshi lenye nguvu zaidi, baada ya kukusanya nyara na kuwachukua mateka askari wa Kireno hamsini pale Lamu. Wareno walijibu kwa kutuma jeshi la kuwashikisha adabu wenyeji, hasa wa Faza na Mombasa. Mwaka 1588 Mir Ali Bey alitimiza ahadi yake kwa kurudi na merikebu tano, na kwa mara nyingine akaungwa mkono na karibu miji yote isipokuwa Malindi, ambao uliweka pingamizi dogo tu. Ali Bey alipoanza kutekeleza azima yake ya kuufanya Mombasa kuwa kituo cha Kituruki, Wareno walijibu kwa kupeleka jeshi kubwa la majini mnamo Januari 1589.

Tishio la malipizo ya Wareno lilikuja wakati mmoja na majilio ya Wazimba wala watu kutoka bara, ambao waliitishia Mombasa. Wakazi wa mijini na waokozi wao Waturuki walijikuta wamenaswa kati ya maadui wawili. Kuangamizwa kwa jeshi la baharini la Waturuki na Wareno kuliwawezesha Wazimba kuingia Kisiwani, ambako walifanya uharibifu mkubwa. Baadaye Wazimba waliendelea kaskazini ambako walizuiwa na Wasegeju na hivyo kuinusuru Malindi nayo isipate kipigo. Wakati huohuo kikosi cha Wareno kiliendelea kaskazini na kuipa kipigo Lamu, ambayo ililipia aghali kitendo chake cha kuwaunga mkono Waturuki. Shehe na wakuu wengine walipelekwa Pate na kukatwa vichwa mbele ya masultani wa Pate, Faza na Siyu.

Ni vigumu kufahamu ni kwa kiasi gani uharibifu uliofanywa na Wazimba, kama ule wa Waoromo hapo baadaye, ulichangia katika kupunguza sana idadi ya watu na kuporomoka kwa baadhi ya miji ya Kiswahili. Yaelekea Mombasa ilidhoofishwa kiasi cha kumfanya adui wake wa siku nyingi, Malindi, kuuchukuwa mji huo kwa msaada wa Wasegeju. Hivyo ndivyo ulivyokwisha utawala wa nasaba ya kifalme ya Washirazi wa Mombasa ambao uliweka pingamizi wakati wote dhidi ya utawala wa Kireno. Nafasi yake ilichukuliwa na Sultani Ahmad, mtawala wa Malindi, ambaye alitunzwa kwa uaminifu wake kwa Wareno. Lakini athari za muda mrefu za kumhamishia Mombasa Kapteni wa kikosi cha Wareno, na makao ya mfalme wa Malindi, zilikuwa ni kudhoofika polepole kwa Malindi, ambako kuliendelea mpaka kwenye nusu ya pili ya karne ya kumi na tisa.

Kilifi, mji uliokuwa kati ya Mombasa na Malindi, pia ulikuwa na dhima katika matukio ya kipindi hiki. Inasemekana kuwa watawala wa Mombasa na Kilifi walikuwa ndugu. Mara baada ya kipigo cha Wazimba, Kilifi yaelekea ilipigana na Malindi kwa ajili ya Mombasa, pengine kutokana na mahusiano ya kinasaba kati ya

nasaba hizo mbili za utawala, pengine kutokana na tamaa. Malindi ililalamika kuhusu mashambulizi ya Kilifi na kuamua kuumaliza uchokozi wa Kilifi na pia madai yake yenyewe juu ya Mombasa. Baada ya ushinde huu yaelekea Kilifi ilididimia moja kwa moja.

Tabaro mbili za Waturuki zilionyesha udhaifu wa udhibiti wa Wareno kwenye upwa wa Uswahili. Ili kuimarisha udhibiti wao, Wareno waliamua kujenga ngome Mombasa na kuweka kikosi cha askari. "Ngome ya Yesu" *(Fort Jesus)* ilijengwa katika miaka ya 1593-4 na kikosi cha watu 100 kiliwekwa, chini ya kapteni ambaye mamlaka yake yalisambaa kutoka Brava kaskazini mpaka Rasi ya Delgado kusini. Lakini uimarishaji wa kuwepo kwa Wareno Mombasa hauonyeshi kuwa ulileta mabadiliko yoyote muhimu katika kuitawala pwani ya Kiswahili iliyobakia. Sehemu nyingine kuwepo kwao hakukudhihirika sana, na walichokitarajia ni malipo ya kodi tu kutoka kwa watawala wa miji. Kikosi cha Mombasa kiliwawezesha Wareno kupambana kwa haraka na majaribio yoyote ya upinzani na uasi ambayo yangetokea. Mwaka 1603, mtawala wa Pate alianzisha uasi wa silaha ambao ulisababisha ahukumiwe na kuuawa. Lakini adhabu hii haikuweza kuzuia maasi yaliofuatia ya Pate na miji mingine.

## Msambao wa watu na makazi katika pwani

Matukio kadhaa muhimu yalitokea katika karne ya kumi na saba. Mojawapo lilikuwa ni kuingia kwa Waholanzi na Waingereza katika Bahari ya Hindi kushindana na Wareno. Jingine lilikuwa la kudhoofika kwa mahusiano kati ya Wareno na watawala wapya wa Mombasa, washirika wao wa muda mrefu. La tatu lilikuwa usambaaji wa watu na makazi mapya katika pwani ambayo yalisababisha kuibuka kwa vikundi vipya.

Kupungua kwa usalama kulikoletwa kwa kiasi kikubwa na shinikizo la Waoromo kulisababisha vikundi vya Waswahili vya kaskazini kuhamia kwenye miji ya kusini. Pemba na Mombasa zote zilipokea wahamiaji, na ni wakati huu ambapo wahenga wa mataifa tisa (Mijikenda) ya Mombasa walihamia kisiwani. Vumba Kuu iliendelea zaidi na kuwa dola huru kwenye karne ya kumi na saba.

Tukio jingine lililokuwa muhimu kama hili ni kusambaa kusini kwa makundi kutoka Shungwaya (au Singwaya) ambayo baadaye yalikuja kuunda mataifa ya Miji Kenda na Wapokomo. Kwa mujibu wa T.T. Spear, makundi tofauti yalihamia kusini kutoka Shungwaya na kuishi katika vijiji vyenye maboma (makaya, umoja: kaya) katika vilima vilivyotazamana na miji ya Kiswahili kati ya Malindi na kusini kidogo ya Mombasa. Baada ya muda kupita, makaya yakawa zaidi ya makimbilio ya kujihami dhidi ya Waoromo na baadaye Wamasai, na kuwa na dhima kubwa katika maisha ya kijamii na kidini ya Mijikenda, dhima iliyodumu hata baada ya kipindi cha vijiji vyenye maboma.

## *Mgongano kati ya Ureno na Mombasa*

Baada ya uhamisho wa makao ya serikali kwenda Mombasa mahusiano ya kirafiki kati ya Wareno na Sultani Ahmed yalidumu kwa miaka mitatu au zaidi. Kapteni wa Mombasa hakuheshimu mikataba ya kiutawala na kifedha iliyofanywa na mshirika wake. Sultani alinung'unikia vikwazo vya biashara na merikebu ilivyowekewa Mombasa. Pia aliomba kutambuliwa kama mtawala wa Pemba, kisiwa ambacho yaelekea alikishinda kwa kutumia majeshi yake mwenyewe. Hatimaye Sultani Ahmed alipewa Pemba kwa mkataba wa kukodisha, malipo yake ya mwaka yakiwa magunia 300 -500 ya mchele.

Baada ya kufa kwa Sultani Ahmed mwaka 1609, mwanae al-Hasan aligombana na kapteni mpya wa Kireno, Manuel de Mello Pereira. Mahusiano kati yao yalikuwa mabaya sana hata kumfanya sultani atafute kimbilio Arabuja kuliko kukubaliana na uamuzi wa kushitakiwa Goa. Kwanza alipewa hifadhi na Wamusungolo (Waafrika wa bara), lakini baadaye walimsaliti na kumuua kwa malipo ya vipande vya nguo vilivyotolewa na Wareno.

Lisbon haikuhusika na usaliti huu, na ili kurekebisha mambo, ilisisitiza kuwa mtoto wa al-Hasan, Yusufu, baada ya kupata elimu Goa, afanywe mtawala. Akiwa huko Goa, Yusufu alibatizwa kuwa Mkristo na kupewa mke aliyekuwa chotara wa Kireno na Kiasia. Aliporudi Mombasa mwaka 1630, Wamombasa na Wareno hawakumkubali. Agosti 1631 Pedro Leitao de Gamboa, kapteni wa Kireno, aliamua kuwa tabia ya Yusufu ya kusali kwa mtindo wa Kiislamu kwenye kaburi la baba yake aliyeuawa ilikuwa sawa na kuikataa imani ya Kikristo na ilikaribia kuwa uhaini; akapanga kumrudisha Goa ili akashitakiwe. Yusufu akaamua kupigana.

Agosti 13, 1631, wakati wa sherehe ya Kireno ya Kalamu ya Kupazwa, aliingia *Fort Jesus* na wafuasi wake kwa kushitukiza, na Wareno wote isipokuwa wachache waliuawa. Yusufu alichukulia kurudi kwa vishindo katika Uislamu kama mwanzo wa jihadi ya kuwaondoa Wareno kutoka kwenye upwa wote. Mwito wake haukukubaliwa na hakuna mji mwingine uliokuja upande wake. Kutengwa huku kulimvunja moyo na akaenda Arabia - pengine kuomba msaada wa Waturuki.

Msaada haukuja, na Yusufu alirudi pwani ambako aliachochea uasi mdogo mdogo mpaka alipofariki mwaka 1637. Eneo la funguvisiwa la Lamu lilikuwa kaidi kuliko yote na Wareno walituma kikosi cha kuzitiisha Faza, Lamu, Manda na Pate mwaka 1636-37.

## *Wavamizi wa Kiingereza - Kiholanzi*

Kutokea kwa Waholanzi na Waingereza katika eneo hili tayari kulikwisha changia katika kufifia kwa mamlaka ya Wareno wakati wa uasi wa Yusufu. Kwa muda mrefu Waholanzi walihusika katika biashara ya Mashariki kama wakala, wakisafirisha kwa merikebu kwenda sehemu nyingine za Ulaya bidhaa za kikoloni zilizoletwa Lisbon.

Lakini Hispania na Ureno zilipoungana mwaka 1580, mfalme wa Hispania alipanga kuwaondoa Waholanzi, ambao walikuwa wakipigana tangu 1566 kujikomboa kutoka kwenye utawala wa Wahispania. Hii iliwafanya Waholanzi wajitahidi kwa uwezo wao wenyewe kufika Mashariki, na ilipofika mwisho wa karne ya kumi na sita merikebu zao ziliweza kushindana na za Wareno katika Bahari ya Hindi.

Wakati huohuo Waingereza tangu mwaka 1580 walianzisha mashambulizi ya kiharamia kwa merikebu za Wahispania, wakati umoja kati ya nchi mbili hizi za Kiiberia ulipohalalisha kuzishambulia milki za Wareno katika Bahari ya Hindi. Kabla ya mwisho wa karne, merikebu za Waingereza zilizunguka Rasi ya Matumaini Mema. Mwaka 1591 merikebu moja ilitua Zanzibar kabla ya kuendelea kueleka India, na mwaka 1608 nyingine ilitia nanga Pemba. Kuanzia hapo, iliwabidi Wareno wapigane na hawa wavamizi wa Ulaya katika Rasi ya Uajemi, kandokando ya pwani ya Malabar ya India na kuzunguka Sri Lanka. Si Mholanzi wala Mwingereza aliyetaka kumrithi Mreno kwa kumiliki mji wowote ule wa Afrika Mashariki kwa kudumu. Kutia nanga Zanzibar na Pemba kulikuwa kwa ajili ya mahitaji na maji tu. Hata hivyo, usumbufu wa Waingereza -Waholanzi ulipunguza sana uwezo wa Wareno, na Waingereza walipowasaidia wakazi wenyeji dhidi ya mabwana zao hali iliharibika zaidi.

Ingawa kirasmi Uingereza ilikuwa na amani na Hispania na Ureno, lakini mwaka 1622 manowari kadhaa za Kiingereza zilimsaidia Shah wa Uajemi kumwondoa Mreno kutoka kwenye kituo muhimu kimkakati cha bandari ya Hormuz. Wareno walirudi nyuma na kujizatiti Maskati, moja ya miji ya pwani ya Omani waliyoitawala tangu mwanzo wa karne ya kumi na sita. Kama walivyofanya Mombasa mara baada ya mashamublizi ya Waturuki mwaka 1588, Wareno walijenga ngome pale Maskati ili iwe kituo kikuu cha biashara ya India na Ghuba ya Uajemi.

## *Mwisho wa utawala wa Wareno katika Afrika Mashariki*

Mara baada ya Hormuz kutekwa na Waajemi, nasaba mpya ya kifalme ya Ya'rubi ilishika mamlaka katika Omani, ikidhamiria kuikomboa nchi kutoka kwenye himaya ya Kireno. Kati ya 1640 na 1650 Wareno walilazimishwa, baada ya kushindwa kijeshi, kuvunja ngome zao na kuondoka Maskati. Wakiwa na mamlaka juu ya mwambao huo, watawala wa Omani waliwatumia watu wao waliozoea kusafiri baharini kujenga jeshi la majini lenye nguvu ambalo lilianza kutoa upinzani kwa Wareno hata nje ya eneo la Ghuba.

Walipoikamata tena Mombasa baada ya uasi wa Yusufu, Wareno waliamua kubaki na kuutawala mji moja kwa moja. Wakati huu Pate ilionekana kuingia kipindi cha ufanisi na kusababisha Wareno kufungua ofisi ya forodha mwaka 1633. Lakini biashara ya mji iliifanya Pate kuwa na nguvu sana; Wareno wakaamua kuingilia kati, na uhusiano kati yao na Pate ukadorora. Wakati huo huo, malalamiko kutoka miji mingine kama Siyu, Pemba na Otondo, dhidi ya Wareno, hayakufika Lisbon tu bali

pia kwa watawala wapya wa Omani, ambao waliombwa msaada.

Katika kipindi cha pili cha karne ya kumi na saba kulifuata mapambano ya muda mrefu kati ya Wareno na Waarabu wa Oman katika miji ya Afrika Mashariki. Mwaka 1652 kikosi cha Omani kiliwashambulia Wareno Zanzibar. Wareno walijibu kwa kumfukuza malkia wa Zanzibar na mtoto wake, mtawala wa Otondo, kwa kuwatia shime Waarabu wa Omani. Mwaka 1660 jeshi la muungano kutoka Omani na Pate liliingia Mombasa na, inavyoelekea, liliteka makazi ya Wareno bila upinzani mkubwa. Mashambulizi mengine ya Omani yalifanywa kusini hadi kufikia Msumbiji (1669). Agosti, 1678 gavana mwenyewe aliongoza kikosi cha askari dhidi ya "Pate Yunga." Aliungwa mkono na utawala wa jirani wa Faza, ambayo ilikuwa na ugomvi na Pate. Kikosi hiki cha askari kiliondoka baada ya merikebu za Omani kutokea mwaka 1679, lakini washirika hao walipata nafasi ya kuwakamata watawala wa Pate, Siyu, Lamu na Manda, pamoja na watu wengine mashuhuri, ambao walikatwa vichwa. Hata hivyo, yaelekea Pate haikukubali kushindwa, kwani vikosi vingine vya askari vilipekekwa dhidi yake, kwa mfano mwaka 1687.

Juhudi ilifanywa kufikia mwafaka ambapo Shehe wa Pate angebaki na ufalme wake kwa sharti la kukubali kuwa chini ya Wareno. Lakini makubaliano haya ya muda yaliyofikiwa Goa yalikataliwa huko Lisbon. Wakati huo, Pate ilikuwa imeshindwa na Waomani na siku ya Noeli, katika jaribio la kutoroka kutoka ufungwani huko Panjim, mtawala mfungwa huyu na madiwani wake waliuawa.

Kwa miaka kadha vurugu za kiraia huko nyumbani zilikatiza mashambulizi ya Omani dhidi ya vituo vya Wareno katika Afrika Mashariki. Mashambulizi yalipoanza tena yalielekezwa Pemba, ambayo iliasi dhidi ya Wareno. Hata hivyo, mwaka 1694 Wareno waliweza kukomesha uasi huo na kuwafukuza Waarabu wa Omani. Lakini mwaka uliofuata ukinzani mkubwa sana ulikuja kutoka Omani. Machi 1696, merikebu saba za Omani, zikiwa na watu 3,000 na Shehe wa Lamu, zilitia nanga Mombasa. Walichukua mji na kisiwa kirahisi na kuzunguka ngome ya *Fort Jesus* mpaka Desemba 1698, ngome iliposalimu amri. Wakati kikosi cha askari wa Kireno kutoka Goa kilipowasili Mombasa Novemba 1698 na amri ya kumkabili adui, bendera nyekundu ya Omani ilikuwa tayari ikipepea juu ya ngome.

Kutoka 1728 hadi 1729 Wareno waliweza kurudi kwa muda mfupi Mombasa, wakitumia fursa ya kutokuwepo kwa Waomani wengi pwani na kukatishwa tamaa kwa Waswahili na Waarabu hao katika baadhi ya miji. Hakuna shaka kuwa mtawala wa Pate alikuwa haelewani na kikosi cha Waarabu kilichokuwepo mjini mwake. Wakati kikundi kidogo kilichoungwa mkono na Waomani kilipomuasi mtawala huyu, alitafuta msaada kutoka Goa mwishoni mwa mwaka 1727. Kutoka Pate kikosi cha Wareno kiliikabili Mombasa, ambako kikosi cha Omani kilichokuwemo ngomeni kiliomba msaada kutoka kwa mfalme wa Pate dhidi ya vikosi vingine vya Kiarabu vilivyolinda ngome ndogo ndogo Kisiwani. Mombasa na ngome yake ilisalimu amri kwa vikosi vya pamoja vya Wareno na Wapate.

Lakini kurudi kwa Wareno na ushirikiano wa Wareno na Wapate ulidumu kwa muda mfupi. Katika shauku yake ya kupata msaada dhidi ya wapinzani wake na marafiki zao wa Kiarabu, mtawala wa Pate alikuwa amewaahidi Wareno mambo mengi kuzidi uwezo wake, kama vile kuwalipa kodi na kuwapa ukiritimba wa biashara ya pembe. Katika muda wa miezi sita tu alikuwa tayari amekorofishana nao. Pambano la silaha lililotokea Juni 1729 liliwashawishi Wareno kuondoka Pate.

Wakati huo matata yalikuwa yakiwangojea Mombasa, Kikosi cha pamoja cha Wamombasa na Wamusungulo kilishambulia sehemu za Wareno mjini na kukizunguka kikosi kidogo kilichokuwemo ndani ya ngome. Novemba 1729, kikosi kilisalimu amri na kuruhusiwa kwenda kwa merikebu Msumbiji. Miji mingine, ikiwemo Zanzibar, Pemba na Mafia, ilifuata mfano wa Mombasa na kuwaua au kuwafukuza Wareno.

Kwa hiyo miji yenyewe ya Waswahili ndiyo ilihusika na hatima ya kufukuzwa kwa Wareno. Lakini mara baada ya kuondoka, Pate na Mombasa kwa mara nyingine zilikaliwa na Waomani, na pwani ya Waswahili ikaingia katika kipindi kipya katika historia yake.

Kushindwa kwa Wareno kulihusishwa na sababu nyingi: mfumo wao dhaifu na uliochanganyikiwa wa ukoloni; maofisa wasio na ujuzi na wenye tamaa, hali mbaya ya hewa isiyotabirika, na magonjwa miongoni mwa wakazi wa Kireno ambao tayari walikuwa wachache; na mwisho migongano ya wenyeji wenyewe kwa wenyewe ambayo mara iliwasaidia Wareno na mara haikuwasaidia. Karibu na mwisho wa kipindi hiki, uwezo wa Wareno ukawa mdogo mno kiasi cha kutoweza kumudu gharama za kuandaa kikosi cha kwenda kupigana.

Shughuli hizi za kijeshi zilifanyika katika muktadha wa matukio muhimu ya kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni katika mwambao. Upande wa kusini wa pwani, biashara muhimu kati ya Wayao na Kilwa ilianza ambayo, ilipofika mwisho wa karne ya kumi na saba, ilitawaliwa na kushamiri kwa biashara ya pembe. Biashara hii ilipata pigo la muda mfupi mwanzoni mwa miaka ya 1700 pale Wareno walipoipoteza Mombasa kwa Waomani. Kutokana na hali hii, Wayao walihamisha pembe zao kutoka Kilwa kwenda Msumbiji. Lakini kutawala kwa nasaba ya Busaidi huko Omani katikati ya miaka ya 1700 kulileta kipindi kingine cha ustawi kwa Kilwa.

Kaskazini zaidi, Vumba Kuu iliimarisha nafasi yake na mtawala wake alichukua cheo cha "Diwani." Familia tawala ya Kisharifu, Wabaalawi, ilichukua desturi mbalimbali za Kibantu ambazo iliziunganisha na ada za Kiislamu. Wasegeju na kikundi kimojawapo cha Miji Kenda, Wadigo, ambao waliishi ujiranini, walijenga uhusiano wa karibu na Vumba Kuu. Mvuto wa kidini wa familia za Kisharifu ambayo ilitawala Vumba Kuu ulisaidia kuwasilimisha, lakini walibakiza vipengele vya imani yao ya kidini, zikiwemo sherehe za kuleta mvua.

Katika funguvisiwa ya Lamu, Pate ilikuwa imefikia upeo wa juu wa ufanisi katika karne ya kumi na saba na ya kumi na nane. Ufanisi wake ulitokana na biashara ya majini, ambayo iliikamata vizuri wakati ambapo miji mingine kama Malindi,

Mombasa na Kilwa ilikuwa, muda mfupi kabla, imekumbwa na mashambulio ya jamii za bara kama vile Wazimba. Pate ilianzisha mahusiano yenye manufaa na Waoromo, ambao waliupatia mji ngozi za kuuza nje; aidha, ilifanya biashara ya pembe kutoka bara. Vyanzo vya kihistoria havielezei vya kutosha kuanguka kwa Pate, ambako kunaonekana kulitokea kwa haraka katika nusu ya pili ya karne ya kumi na nane.

## *Kichokoo cha Omani Afrika Mashariki*

Kuanguka kwa Pate kunatoa kisa cha moja ya tenzi maarufu katika Kiswahili, *Al-Inkishafi*. Mtunzi wake, Sayyid Abdallah bin Ali bin Nasir, alikuwa mmojawapo wa tabaka aali la Kisharifu la Pate. Masharifu ambao walilowea Pate wakawa wenyeji, pamoja na masharifu wa Lamu, walikuja kuchukua jukumu muhimu katika maendeleo ya jadi ya kifasihi na kidini ya Kiswahili. Mbinu za kufundisha Uislamu, vitabu vilivyotumika, madhehebu ya watakatifu, kustahiwa kwa masharifu na fani na maudhui ya tungo za kishairi ni sehemu ya urithi wa kitamaduni wa dhuria hawa wa Mtume Muhamadi, ambao hawakuishi tu katika funguvisiwa ya Lamu, bali pia sehemu nyingine za pwani, na kuchangia sehemu kubwa ya wasomi wake wa kidini.

Waomani walichangia sana katika kuibuka upya kwa uchumi wa Kilwa, kama ilivyofanya biashara ya watumwa. Biashara ya watumwa na biashara ya pembe ilitawala historia ya kiuchumi ya pwani ya mashariki kwa kipindi kirefu cha karne ya kumi na tisa. Biashara ilikuwa hasa kwa minajili ya kuwapatia Wafaransa watumwa waliowahitaji baada ya 1735, kwa ajili ya mashamba yao katika visiwa vya Maskarene: Ile-de-France (Mauritus) na Ile Bourbon (Reunion). Mwanzoni Wafaransa walinunua watumwa wao kwenye visiwa vya Wareno vya Msumbiji na Kerimba, lakini utawala wa Msumbiji ulianza kuporomoka katikati ya miaka ya 1700, sababu mojawapo ikiwa ni ushindani kutoka kwa wafanyabiashara wa Kiswahili na Kiarabu, ambao waliongeza shughuli zao katika ukanda wa pwani baada ya nasaba ya kifalme ya Busaidi kuimarisha mamlaka yake katika ufalme wa Omani. Kwa mara nyingine Kilwa ikawa kituo kikubwa cha biashara kilichowavuta wafanyabiashara ya watumwa na pembe kutoka bara.

Ilipofika 1785 umilikaji wa Msumbiji wa biashara ya pembe katika Afrika ya Kati na Mashariki ulikuwa umefifia kabisa, ingawa iliendelea kuitegemea biashara ya watumwa kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya watumwa katika makoloni ya Kifaransa katika Bahari ya Hindi. Wafanyabiashara wa Kiyao waliuza watumwa wengi zaidi na pembe huko Kilwa, ambayo ilikuja kuwa gulio kubwa kwa bidhaa zilizohitajika sana za kutoka Omani na Bara Hindi, kama vile nguo za surati. Ilipofika miaka ya 1780, Waswahili au wafanyabiashara walioswahilishwa walikuwa wakifanya safari za awali za biashara bara kupitia Ziwa Malawi.

Siasa na biashara mara nyingi havikutangamana: Waarabu wa Kiomani walifanya biashara na Kilwa, ingawa Sultani wa Kilwa aliulinda sana uhuru wake dhidi ya

Omani. Hata hivyo, kuanzia 1784, Imamu mpya wa Oman, Said bin Ahmed, alianza kampeni ya kijeshi ya kuitawala miji mingi ya pwani, ukiwemo Kilwa. Sultani wa Kilwa aliyekuwa anaanza kuzeeka, Hassan Ibrahim, aliweza kuweka upinzani hafifu. Alishurutishwa kukubali ubwana wa Imamu juu yake na kukubali kuwepo kwa gavana wa Omani na kikosi cha jeshi Kilwa. Lakini matukio haya ya kisiasa yaliweza tu kusaidia kufufua biashara katika pwani ya Kilwa kwa kuleta utulivu mkubwa na kuhimiza vitega uchumi vingi vya Kihindi. Bila shaka Maskati ilifaidika sana kutokana na mpango huu.

Kufikia mwisho wa karne, thamani ya kiuchumi ya sehemu chache ambamo waliwakilishwa ilionekana dhahiri kwa akina Busaidi. Jambo hili, pamoja na masuala mengine ya kisiasa na kiusalama, yalimfanya Sayyid Said bin Sultan (1804-56) kupanua mamlaka yake ya kifalme katika mwambao, na hatimaye kuanzisha makao yake makuu Zanzibar.

## *Himitisho*

Kati ya 1500 na 1800 kulikuwa na mabadiliko muhimu kwenye pwani ya mashariki ya Afrika. Miji mikubwa ya Waswahili, ambayo mpaka wakati huu ilikuwa huru ilikumbwa na uvamizi wa Wareno, wakati mwingine ukisaidiwa na njaa na ushindani wa wenyewe kwa wenyewe.

Utawala wa Wareno haukuwa na huruma. Wareno walikuwa wamedhamiria kuwapiga Waislamu kila mahali, kuchukua nchi zao na biashara, na hata kuwabadili, pamoja na waumini wa dini ya kijadi ya Kiafrika, kuwa Wakristo. Lakini Waislamu walikuwa wakaidi kwa Ukristo na ilipofika mwisho wa milki ya Wareno hakuna dalili zozote za Ukristo zilizobakia.

Kuhusu biashara na misafara ya kibiashara katika Bahari ya Hindi, Wareno walifanikiwa nusu tu. Miji ya Waswahili iliweza kubakia na kiasi kikubwa cha biashara, licha ya sheria zilizoanzishwa na Wareno. Tamaa na uzembe miongoni mwa maofisa wenyeji ndivyo vilivyosababisha matukio kama yale ya kuanguka kwa biashara ya dhahabu ya Sofala. Hata hivyo, pwani iliwatajirisha maofisa wa Kireno, hata kama haikumtajirisha mfalme wao.

Miji ya Waswahili ilipata faida zinazotofautiana. Unyambufu wa Mombasa uliiwezesha mara nyingi kurudia hali nzuri baada ya mashambulizi ya Wareno. Kilwa iliathirika vibaya zaidi, ingawa karibu na mwisho wa karne ya kumi na nane iliinuka kutokana na biashara ya watumwa. Miji mingine ya pwani ilipotea au kugeuka kuwa vijiji. Kuanguka kwao hakukusababishwa na Wareno; huenda sababu kubwa zaidi zilikuwa ni uvamizi wa Waoromo na Wazimba, ukichanganywa na mabadiliko ya mazingira. Pate pekee ilikuwa tofauti; ilifaidi kilele cha ufanisi wake, ambacho haikupata kukifikia kabla, kwenye karne ya kumi na saba na kumi na nane; kuanguka kwake kulianza mwishoni tu mwa karne ya kumi na nane. Utafiti zaidi unahitajika ili kuweza kujibu maswali mengi yaliyobakia kuhusu miji ya Waswahili, mambo yaliyosababisha kukua na kuendelea kwao, na hatimaye kuanguka kwao.

# 26

# *Ukanda wa Maziwa Makuu 1500 hadi 1800*

Kipindi hiki kinaweza kugawanywa katika sehemu tatu. Kipindi cha kwanza kinadumu takriban tangu 1500 hadi 1580, cha pili tangu 1580 hadi 1680, enzi ya ukame na njaa; na kipindi cha tatu, tangu miaka ya 1680 hadi 1800, wakati wa ujenzi wa madola na upanuzi. Kabla ya 1580, shughuli kuu ya maeneo ya kusini na kati ilikuwa uimarishaji wa madola yaliyofuata baada ya himaya ya Bachwezi, ambapo kaskazini, lilitokea dukizo la kwanza la watu wasemao Kiniloti cha Mashariki, pamoja na matokeo ya kiisimu yaliyoambatana nalo.

Kipindi cha pili kilitawaliwa na ukame na njaa. Pia kipindi hiki kilishuhudia hajira kubwa kabisa ya watu katika eneo hili ndani ya miaka elfu moja iliyopita. Kulikuwa na uhamaji mkuu toka Baar, Waluo walitawanyika, ambapo vamizi kabambe za Wanyoro zilifikia hata sehemu za Rwanda na Usukuma. Upande wa mashariki, ukame huu ulihusishwa na majilio ya Waniloti wa Kati-Mashariki, walioungana na wenyeji, pamoja na idadi kiasi ya watu waliohamia kusini.

Kipindi cha tatu kilijishughulisha na kujazana na kupanuka kwa asasi za madola. Kilianza na mgogoro wa kinasaba ndani ya Bunyoro, jambo lililoashiria kuanguka kwa himaya hiyo na kuleta uanzishwaji wa madola kemkem. Dola la Mpororo (?) lilianzishwa wakati huo na kisha kugawanyika vipande vipande. Kipindi kilimalizika na kuibuka na kupanuka kwa Buganda katika eneo la kati na Rwanda katika eneo la kusini, kama "Madola Makuu" mawili ya ukanda wa Maziwa Makuu, na kaskazini kuwekwa mipaka ya jumla ya mizingo ya sasa ya vikundi mbari vya Waniloti wa Mashariki ya Kati kama Waiteso, Wajie, Waluo wa Mashariki, Walango Omiro na Wakumam.

## *Maeneo ya Kaskazini na Kati*

### Kuundwa kwa vikundi na jamii mpya

Kabla ya mwaka 1000 wa enzi ya Kikristo, Wasudani wa Kati yawezekana ndio waliokuwa mashuhuri zaidi katika ukanda wote wa Maziwa Makuu. "Muru" lilikuwa ni jina la Kiluo la kuwatambulisha wenyeji wote hawa, na litatumika pale

ambapo mbari ya kundi fulani la Sudani ya Kati haijulikani, na hasa kuzitofautisha jamii za awali za jimbo hili na wahamiaji wa baadaye wa Kimadi, ambao pia walitokea Sudani ya Kati. Jamii nyingi za Sudani ya Kati ziliishi katika vikundi vikundi vilivyotawanyika, ambavyo vilitawaliwa na wazee. Walikuwa wakulima. Waliabudu Mungu wa ardhi na kutumia mawe ya mvua au mchanganyiko wa mafuta na maji kuleta mvua. Walikuwa na mfumo changamani wa vizimu na walizika wafu wao katika makaburi yenye mwanandani. Sana sana, walifahamika na wahamiaji wa baadaye kuwa walikuwa mabingwa katika ufuaji na uhunzi wa chuma. Hadi kufikia mwaka 1500 walikwisha mezwa na utamaduni wa Kibantu kusini mwa mpaka wa mto Nili-Kyoga, lakini bado walitamalaki kaskazini toka Nyanda za Juu za Alur hadi milima ya Karamoja.

Mnamo mwaka 1000, Dog Nam - mahali walipochimbuka Waniloti - palisambaratika. Kundi moja lilihamia Tekidi na kikundi kidogo kikahama toka Tekidi na kusakini Pakwac-Pawir. Kundi jingine kutoka Dog Nam likasakini Wipac (Rumbek). Katika nchi zote tatu za Waluo pekee, mamlaka ya kiurithi yaliyohusishwa na kizimu cha pongo yalikwishajijenga tangu kabla ya mwaka 1400.

Kipindi cha kuanzia 1400 hadi 1500 kilitumiwa kuimarisha mambo ndani ya madola yaliyorithi himaya na mbinu za kidiplomasia za mataifa makuu, yaani Bahinda na Babito. Watawala wapya waliwatambua baadhi ya machifu wenyeji, hasa wale wa Bwera na Buyaga. Palikuwa na mabishano machache tu juu ya kutwaa madaraka.

Kaskazini mwa mpaka wa Nili-Kyoga, mwaka wa 1500 ni muhimu, kwani inawezekana unapatana na majilio makubwa ya kwanza ya kundi la kaskazini la Waniloti wa Mashariki au tawi lao la jamii ya Wabari. Imetolewa hoja kuwa kundi hili lilihama makwao katika nyakati tatu kati ya mwaka 1490 na 1571. Kila kikundi kiliishambulia Tekidi kwa wakati wake mpaka makazi haya ya Kiluo yakavunjwavunjwa na uvamizi wa tatu wa Walotuho.

Data iliyopo inaonyesha kuwa Waniloti waliwaletea watu wa Sudani ya kati utaratibu wao wa rika, sherehe zao za moto, Mungu wa mbingu, mkuki na ngao, mkuki mtakatifu wa kuleta mvua, jembe lililonyooka na visingo (kofia maalumu za ngozi na mapambo mengine) vilivyonakshiwa. Maingiliano yao na watu wa Sudani katika maeneo mengi labda yalizaa temi na lugha yao ikawa lugha mpya ya biashara.

Uvamizi wa pili wa Waniloti wa Mashariki huenda uliathiriwa na Waoromo, walioacha makwao kaskazini mwa ziwa Turkana kati ya 1517 na 1544 na kushambulia Tekidi karibu wakati uleule walipoanza kuvamia Ethiopia ya kusini. Wahenga wa Wakakwa wa leo yawezekana walishiriki katika uhamaji huu.

Baar pakawa eneo la mchanganyiko mkubwa wa jamia kati ya Waniloti wa Mashariki na Wamadi. Inaonekana kuwa jamii mpya za Wapajuku, Wakakwa na Wakuku walitwaa lugha ya Waniloti wa Mashariki na kuchanganya Mungu wa mbingu na mkuki wa Kiniloti na Mungu wa ardhi wa Kisudani na uta na mshale. Yaelekea waliachana na utaratibu wa rika wa Kiniloti na kutwaa mavazi, desturi za

mazishi na mawe ya mvua ya Kimadi. Machifu wa kisiasa kwa jumla walitokana na Waniloti wa Mashariki ambapo mabingwa wa miviga walikuwa Wamadi. Wapajulu, Wakakwa na Wakuku walikuwa Wasudani kiutamaduni na Waniloti wa Mashariki kilugha.

Mchangamano wa Wabari ulikuwa wa aina hiyo hiyo, kiasi ukiwa na athari kubwa zaidi ya Kiniloti. Moja ya nduni kuu za jamii za Kibari na Kikuku ilikuwa ni kwamba *dupi* (tabaka la mahadimu) mara nyingine walitafoutiana kimaumbile na wazaliwa huru. Katika jamii za Kikakwa na Kipujulu *dupi* walikuwa ni wateja badala ya kuwa watwana au wajakazi. Kwa kuwa walitumiwa mara kwa mara kama wasaidizi katika miviga ya ugimba, na walikuwa wachimba madini na wafua chuma mashuhuri, inawezekana kuwa watu hawa walitoka Muru wala si Madi.

Uvamizi wa mwisho wa kundi la kaskazini la Waniloti wa Mashariki ulihusishwa na Walotuho, kufuatana na fasihi simulizi ya Waluo wa Tekidi. Walotuho waliyatwaa makazi ya Waluo ya Tekidi, na mfalme wake, Owiny Rac Koma (t. 1544-1571) akakimbia na wafuasi wake hadi makazi ya Waluo katika Pakwac-Pawir. Inaonekana kuwa kundi la Wasudani wa Kati, Waokarowok, walitumia lugha ya Waniloti wa Mashariki kutokana na athari za Walotuho.

Yaelekea kuwa Walotuho waliziingiza koo ndogo za Okarowok ndani ya koo zao nne kuu na kutumia miko ya vizimu ya Waokarowok. Walileta sherehe za kutengeneza moto, utaratibu wa marika, na, labda kutokana na hali yao ya kutotulia pamoja, wakajenga vijiji vilivyosongamana na kujaza watu sana katika eneo lililosifika kabla kwa kuwa na makazi yaliyotawanyika. Huu ni mweneo wa mbali kabisa kuelekea mashariki wa koo za vizimu na mawe ya mvua ambao labda unaonyesha mpaka wa mashariki wa jamii za Sudani ya Kati.

Wakati kundi la Waluo asili wakilazimishwa na uvamizi wa Waniloti wa Mashariki kuhamia eneo la Tediki, kundi jingine lilielekea kaskazini hadi Wipako Dwong' katika Rumbek. Kundi hili lilivunjika kati ya mwaka 1382 na 1418 na kwenda upande wa magharibi, kuelekea Mto Nili, na kuishi kwenye kingo za mto. Baadaye mkusanyiko huu uligawanyika tena, na kundi moja - Washilluk asili na washirika wao, walielekea kaskazini na kusakini huko kati ya 1490 na 1571. Mavamizi ya Waluo katika Baar yaliwakimbiza Wapanyimur, Waatyak na Wakoc-Pagak walioongozwa na Wamadi kuhamia kusini hadi eneo la Mlima Kilak. Kulifuata mapambano kati ya Wamadi na Waluo kwa ajili ya madaraka katika Pakwak-Pawir. Katika utemi wa Atyak ilibashiriwa kuwa wana wa kiume wa binti mfalme Nyilak (c 1517-1562) watamwua baba yake, mfalme, na kutwaa kiti cha ufalme. Matokeo yake, mfalme alimfungia binti yake, lakini msafiri wa Kiluo alimpa Nyilak mimba, akazaa mtoto wa kiume ambaye alimwua mfalme wa Madi kama ilivyobashiriwa. Kutokana na haya, labda madola mawili yaliibuka: Attyak (ambalo baadaye liliitwa Okoro), lililoongozwa na Waluo, na Acholi, lililoongozwa na Wamadi. Hadithi ya Nyilak in istiara (ambayo wahusika wake hubadilika kufuatana na simulio linalohusika) iliyokusudiwa kueleza kupinduliwa kwa utawala wa Kisudani

ama na Waluo upande wa kaskazini au Wabantu upande wa kusini.

Mnamo 1560 Wabotuho waliivamia Tekidi na kusababisha karibu wakazi wake wote pamoja na mfalme wao, kukimbilia Pakwac-Pawir. Utemi mkuu uliotokana na Walotuho ulikuwa Puranga. Kundi hili la Waluo lililoathiriwa mno na Waniloti wa Mashariki, linaweza kuitwa Waluo wa Mashariki. Walijenga umashuhuri miongoni mwa watu wa Acholi Mashariki, Labwor, Nyakwai na Lango, na pamoja na Waniloti wa Mashariki wakawa na athari mkataa juu ya lahaja zizungumzwazo katika maeneo haya.

## Kipindi cha ukame na njaa


Hakuna eneo la jimbo la Maziwa Makuu, wala lile la Afrika ya kati-mashariki, lililoepuka athari za baa la hali ya hewa la ukame lililofuatiwa na njaa mwishoni mwa karne ya kumi na sita na mwanzoni mwa karne ya kumi na saba. Katika kipindi hiki mvua katika maeneo ya kaskazini na kati ilikuwa ya wastani tu kwa miaka miwili. Miaka migumu kabisa ya ukame labda ilikuwa ni kati ya 1588 na 1590, 1601 na 1602, 1613 na 1617 hadi 1621. Katika kiangazi cha 1621 kina cha mto Nili cha majira ya joto kilifikia chini kabisa tangu mwaka 622 rekodi zilipowekwa kwa mara ya kwanza.

Kaskazini mwa Uganda kipindi chote kinajulikana kwa jina la *Nyarubanga*, neno la Kiluo lenye maana ya "Kilichotumwa na Mungu." Kipindi kilimalizika wakati wa Njaa Kubwa ya 1617 hadi 1621 ulioambatana na ugonjwa ulioteketeza makundi ya ng'ombe. Jinamizi hili la njaa ya wote linakumbukwa ndani ya mapokeo. Katika Misri maelezo yaliyopokelewa yanaogofya. Kula watu kulikuwa jambo la kawaida, na karibu nusu ya watu walikufa kwa njaa. Yaliyotokea huko Misri yawezekana yalitokea pia katika jimbo la Maziwa Makuu, hasa sehemu ya kaskazini.

Kama nusu ya wakazi walikufa wengi wa waliobaki walilazimika kuhama na kukimbia, wakikusanyika karibu na mito, maziwa, kwenye kingo za Mto Nili, pwani za Ziwa Nyanza (Victoria) na kwenye msururu wa maziwa kuelekea kusini hadi ndani ya Afrika ya kati. Masimulizi makuu kumi na mawili ya uhamaji wa wakati huu yamekusanywa.

*Nyarubanga* ilibadilisha jiografia ya kimbari na kisiasa ya sehemu kubwa ya ukanda wa Maziwa Makuu na pengine hata nje ya ukanda huo. Pengine ilikuwa ni pigo kubwa kwa uongozi uliojengwa juu ya dhana ya udhibiti wa nguvu za kimiujiza na hususa kwa wale waliodai kuwa na nguvu za kutengeneza mvua. Ikazaa aina mpya ya uongozi, uliotokana na wale walioongoza hajira na ambao ufundi wao kama makamanda, mashujaa na wawindaji, ulihakikisha uhai wa makundi makubwa ya watu. Mara baada ya tishio kuondoka, viongozi wa waliosalimika waliunda vitengo vipya vya kisiasa katika maeneo mapya ambayo huenda yalikuwa na wakazi wachache na wala hayakuwa na miundo yake yenyewe ya kisiasa.

Kwa hiyo, haishangazi kuona kuwa vyanzo vya mapokeo vinatoa picha kuwa kuanzia kama mwaka 1600 kulikuwa na mwanzo mpya. Katika maeneo yaliyo




**26.**1 *Nyarubanga na kuchenguka kwa Waluo, t. 1570-1720 (J.B. Webster)*

mengi, yalianza tena maingiliano ya mbari, makazi mapya na watawala wapya. Kama maelezo ya kabla ya 1600 ni mifupa mitupu na vungivu, hii ni kwa sababu *Nyambanga* iliharibu masimulizi ya mapokeo, ikifutilia mbali njia zake za kuyaeneza pamoja na takriban wazee wote ambao waliyahifadhi.

Uhamaji kutoka Baar uliharakishwa sana wakati wa *Nyarubanga*. Pakwac-Pawir pakawa makimbilio ya makundi makubwa ya watu wa lugha na tamaduni tofauti wenye kufa kwa njaa na kukata tamaa. Kumiminika kwa watu hawa ni dhahiri kuliharibu nafasi ya Wapaluo kaskazini mwa Nili, na kufanya suala la nani atawadhibiti Waluo na makundi mengine huko liwe na umuhimu mkubwa zaidi. Hali hii ilizaa mgogoro kati ya Chwa Nyabongo na Nyipir. Ugomvi huu unasimuliwa ndani ya mapokeo ya mkuki na ushanga. Nyipir na Tifool, ambao wafuasi wao walikuwa Waluo wa Owiny na Omolo, walihamia magharibi ya mto Nili mbali na nchi ya Chwa. Kufuatana na masimulizi ya mapokezi Nyipir alisimika shoka ndani ya mto mkavu wa Nili kama ishara ya utengano wa aushi. Akiwa kiongozi wa Attyak, Nyipir alianzisha ufalme wa Waalur wa Okoro ambapo Tifool alianzisha dola ambalo liligawanyika sehemu mbili, Nyiganda na Angal. Kundi kuu la Waowiny lilielekea kusini-mashariki, kupitia kaskazini mwa Ziwa Kyoga na kuungana na makambi ya Wabudola mashariki ya Busoga. Kufuatana na masimulizi ya Kijonam, Waluo waliobaki, wakiongozwa na Daka, walimpindua Abok na dola la Koch likagawanyika sehemu tatu; Koch Ragem magharibi ya mto Nili, Koch Labongo upande wa mashariki, na Koch Paluo iliyoongozwa na Wamadi.

Mluo mwanzilishi wa utemi wa Terego wa Walugbara yawezekana aliibuka kutokana na mtawanyiko kutoka Pakwac-Pawir. Banale na mpwa wake Raoule walifika nchi ya Madi wakiwa katika hali ya uchochole kabisa. Banale aliandamana na mwanamke mkoma wa Kimadi. Uhusiano wao wa siri ulipogundulikana baraza la wazee wa Madi likaamua kumkubali kuwa chifu. Akaanzisha Terego, utemi mkubwa kabisa miongoni mwa Walugbara au kusini mwa Madi. Wakati huo huo, Jaki na wanawe wenye wingi wa tamaa walikuwa wakitanua utawala wao juu ya nchi jirani ya Madi na inawezekana baraza la wazee walihiari kuongozwa na Banale kuliko kuingizwa ndani ya kundi la Jaki lenye kuongea Kiniloti cha Mashariki. Ni uamuzi huu uliowazezesha kuhifadhi lugha yao na kimsingi kubakia Wamadi kiutamaduni.

*Nyarubanga* ilisababisha hajira tatu kuelekea ukingo wa kusini-mashariki wa Ziwa Nyanza. Idadi kadha ya koo za Adhola ziliondoka Pakwac-Pawir na kuungana na Waowiny huko Kaberamaido. Mmoja wa viongozi wao alikuwa Amor, na ukoo wa Amor baadaye ulitokea Padhola na ngoma yao, mkuki mtakatifu na kizimu cha pongo. Makundi ya Adhola na Owiny yakaenda haraka kusini na kutamakani katika makambi hapo Budola mashariki mwa Busoga. Kundi jingine la koo ambalo lilikuwa sehemu ya mkusanyiko wa Waomolo ambao kwa asili walikuwa mchanganyiko wa Waluo-Wasudani, waliondoka Pakwac-Pawir, kwenda kaskazini hadi Tekidi na kusini kuelekea Mlima Elgon. Hivyo palikuwa na mwongezeko wa polepole wa walowezi wa Kiluo Mashariki mwa Uganda, ambao huenda waliungana na majilio ya

wakimbizi wa *Nyarubanga* kufanya vikundi viwili tafauti.

Hadi mwaka wa 1600, walowezi wa awali walikwishaungana na koo za wahamiaji kuunda angalau makundi manne: kundi la Waomolo katika makambi ya Banda, Waowiny-Adhola katika makambi ya Budola, koo mbili za baadaye za Adhola (Ramogi na Lakwar) ndani ya msitu wa Budama magharibi, na kundi la Busoga ya baadaye kaskazini mwa mto Mpologoma. Kati ya 1598 na 1650, makambi yote mawili ya Budola na Banda yalivunjika, labda kutokana na ukame mbaya wa miaka ya 1620 ulioashiria kuisha kwa *Nyarubanga.* Waowiny walielekea jimbo la Alego katika wilaya ya Siaya magharibi ya Kenya. Sehemu ya Waomolo ilifuata na makundi yote mawili yakaanza kugombana. Koo za Waadhola walikuwa wa mwisho kuondoka makambini mwao na kujiunga na ndugu zao magharibi ya Bundama.

Miongoni mwa wale waliobakiza lugha yao ya Kiluo magharibi ya Kenya, baadhi waliunda temi. Wengi wao, hata hivyo, walikuwa kama Wapadhola, waliosakini katika maeneo yasiyokaliwa na watu, na waliridhika na mfumo wa siasa usiokuwa na mkuu (yaani usio na kichwa), ambao uliendeleza amani kati ya koo thelathini na moja. Umoja wa kimbari uliendelezwa na kisasili kwamba koo zote zimetokana na wana na madhuria wa Adhola, mtemi aliyeongoza hajira kuu kutoka Kaberamaido hadi mashariki ya Budama. Wapadhola polepole walipata ardhi upande wa kusini na mashariki ya makazi yao ya awali. Baada ya 1650 walipigana pia na Wamaasai katika eneo la Tororo.

Koo nane za makusanyiko ya Waowiny na Waomolo zilihama kutoka makambi yao ya Budola na kuingia Busoga. Wote walitambulishwa na kizimu cha pongo (kulungu), na walikuwa na jadi ya kuwinda na kufuga, ingawa kundi la Owiny lilikuwa na jadi ya kulima pia. Koo zote za Owiny pamoja na Wakoli wa asili ya Omolo, zikawa koo tawala ndani ya Busoga. Waomolo, ambao walikuwa wafugaji zaidi, walisita kuweka makazi ya kudumu, na ni ukoo mmoja tu kati ya koo zao ulitawala.

Mara zilifuata hajira za Wapakoyo kutoka Pawir, kusini mwa Ziwa Kyoga, zilizoishia kuunda temi za Bagweri na Bugaya. Hajira za Waluo zilikusanya wafuasi wengi njiani kupitia ndoa za mchanganyiko, na pia kwa kuwa walitwaa madhabahu makuu, ambayo yaligeuzwa vituo vya miviga na hija za wafalme. Kila walikokwenda, Waluo haraka walitoa nafasi kwa miviga na asasi za kidini zilizokuwapo; uwezo wao wa kujirekebisha kidini ulikuwa ni moja ya silaha zao kuu za kisiasa.

Hadi 1750 madola tisa yalikwishaundwa. Kufika mwisho wa karne ya kumi na tisa madola haya yalikwisha vunjika vunjika na kufikia madola thelathini, na Wangoabi au ukoo wa pongo ukitawala karibu madola ishirini. Yale madola yaliyoendeleza urithi wa baba na mwana na kutumia watu wa kawaida kama watawala hayakupata matatizo ya kiurithi, na yalikuwa na vita vichache vya wenyewe kwa wenyewe. Kwa upande mwingine, wale waliotumia urithishaji wa ndugu kwa ndugu na kuwatumia wana wa wafalme kuendesha ofisi za utawala walikumbwa na magomvi

ya mara kwa mara ya kupigania kiti cha enzi, na vita vingi vya wenyewe kwa wenyewe. Nasaba zile zilizoshikilia misingi asilia ya Waluo zilitulia zaidi kuliko zile zilizoiga taratibu za urithi za raia zao wa Kibantu.

*Nyarubanga* na mhamo wa mkuki-na-ushanga ulioambatana nayo vilikuwa na umuhimu mkubwa kihistoria kwa Waluo, kwani viliamua msambao wao wa kijiografia wa leo. *Nyarubanga* pia ilianzisha uvamizi kabambe wa Wanyoro wa kusini, ukiongozwa na Wahima-Watutsi, na kupelekea matabaka ya washamba kujaribu kupindua utawala wa wafugaji. Hatua ya kwanza ya uvamizi iliongozwa na makundi ya waporaji wasiokuwa na mpango walioswaga jimbo lote la kusini, na hatimaye baadhi yao kusakini Buzinza, Burundi na hata mbali zaidi. Nao kwa upande wao wakachochea hajira nyingine zilizofuata msururu wa maziwa hadi katika Afrika ya Kati.

Kadiri ukame ulivyoshimikiza, ndivyo ng'ombe walivyoshambuliwa na ugonjwa ulioteketeza mifugo ya mfalme wa Kitara. Hali hii ilimchochea Chwa II kutuma majeshi yake kusini kupata mifugo ya kujazia mazizi yake na kuimarisha mamlaka ya kifalme. Wafugaji walikuwa ndio lengo la wazi la Wanyoro, na wakulima walikuwa ndio washirika wa kawaida wa Chwa.

*Nyarubanga* pia iliingiza kundi la kati la Waniloti wa mashariki katika medani ya Maziwa Makuu. Kihistoria, kundi hili, lililokuwa la mkusanyiko wa Wakarimojong-Teso, kimsingi, liligawanyika sehemu mbili: wakulima wa Kiisera waliofuga ng'ombe kiasi, na Wakoten, wafuga ng'ombe waliojishughulisha na kilimo kidogo. Ingawa Waisera na kundi la wafuga ng'ombe wote wanapatikana miongoni mwa watu wote wa kundi la kati la Waniloti wa Mashariki, makundi ya mbari yaliyotokana hasa na Waisera ni Waiteso, Watoposa na Wadodos. Makundi yaliyotokana na Wakoten ni Wakarimojong, Wajie na Waturkana.

Waokarowok (Ikarebwok) ni ukoo mkuu miongoni mwa kundi la kati la Waniloti wa Mashariki. Wanaelekea walitokea kwa mara ya kwanza katika jimbo la Agoro wakati Walotuho walipolazimisha lugha na desturi zao kwa Walukoya, watu wa Muru. Agoro kilikuwa kituo muhimu cha usambaaji wa Waisera-Omiro.

Hajira kubwa kuelekea kusini-mashariki ya Waluo zilizohusishwa na makundi ya Waowiny na Waomolo, nazo zilikuwa zimechanganyikana na Waisera, hususa Waomolo waliokwenda upande wa kusini kufuata ushoroba wa Angoro-Karamoja. Waowiry waliacha nyuma vikundi vya wasema Kiluo katika eneo ambalo baadaye lilikuja kuwa nchi ya Lango Omiro katika Amach kwenye kingo za kaskazini za Ziwa Kyoga. Sehemu muhimu ya wakazi ambao hatimaye walitambuliwa kama Waomolo labda walikuwa Waniloti wa Mashariki tangu awali. Wale waliofika magharibi ya Kenya walijulikana kwa Waluo kama Waomia – Lomia ukiwa moja ya koo nne kuu za Lotuho. Wimbi la mwisho la wahamaji kufika Siaya lilikuwa na makundi kutoka Uganda mashariki pia, kwa mfano Waowila, Wanatar na Bayuma. Inawezekana wote walikuwa Waisera-Omiro waliotokana na Wabako waliokuwa na asili ya Uhabeshi.

Pamoja na watu wa Sudani ya Kati na kundi la Kaskazini la Waniloti wa Mashariki Waisera walikuwa na koo za watu wa asili ya Kiluo na Kihabeshi miongoni mwao. Makundi haya bila shaka yaliimarishwa na wahamiaji kutoka Anywa, au Pari, na kutoka Baar na Pakwac-Pawir.

Kwa kipindi cha karne za kumi na saba na kumi na nane makundi haya ya wahamiaji waliishi pamoja na kuunda mikusanyiko iliyoitwa kwa majina ya mahali walipoishi, na wengine walikuwa na kiwango fulani cha kujitambulisha. Mikusanyiko mikubwa kabisa ilikuwa ni ya Wabako katika Jie ya kati, Waokii (au Wamiro) katika eneo la Mlima Moroto na Mto Omanimani la Karamoja ya kati, Waabwor katika Vilima vya Labwar, Wakumam mashariki ya Teso, pamoja na Waiworopo-Iteso (ambao walikuwa tofauti kwa sababu ya kukosa mshikamano ndani ya kundi lao) katika Karamoja ya kati na kusini. Makundi yote haya yalikusanya Waluo na Waniloti wa Mashariki katika uwiano unaotofautiana, na kufikia karne ya kumi na nane matumizi ya lugha mbili yalikuwa jambo la kawaida.

## Wafugaji na wakulima

Wanahistoria na Wananthropolojia wamekuwa na tabia ya kuzigawa jamii za ukanda wa Maziwa Makubwa katika sehemu mbili zisizoingiliana; wale wanaolima ardhi na wale wanaofuga wanyama. Lakini ukweli ulivyo hali ni changamani zaidi, yenye kufukuta na yenye kubadilika. Hajira za watu na mageuzi ya kijamii yalileta pamoja makundi ambayo mawazo yao na desturi zao aghlabu vilitofautiana. Kwenye kipindi chote hiki tunachokishughulikia hapa, vikundi vya wafugaji na wakulima wa mazao vyenye lugha tofauti viliendelea kuchanganyika na kufanya jamii mpya na zilizoshikamana vyema zaidi. Hapa pana mifano michache ambayo inaeleza vyema namna ya mabadiliko haya ya kijamii

Miongoni mwa Waniloti wa Mashariki Kati, makundi yaliyo mengi ya wafugaji yalitamakani katika eneo la vilima vya Mlima Koten-Magos la kaskazini-mashariki ya Karamoja. Ni dhahiri kuwa hawa watu wa Koten-Magos walikwishapata uzoefu wa ufugaji kabla ya kuja kusini. Hivyo basi, pamoja na kuwa walifika Karamoja na mifugo michache, mara moja waliendeleza uchumi mchanganyiko uliotegemea ufugaji, kilimo, uwindaji na ukusanyaji, utaratibu ambao ulichukuana vyema zaidi na hali ya hewa ya jimbo hilo, kuliko shughuli za uchumi za vikundi vingi zaidi vya kilimo. Matokeo ya mageuzi haya yalionekana kati ya 1680 na 1830 wakati makundi ya Koten-Magos yalipohamia katika makazi yao ya sasa, na kusababisha makundi ya wakulima ama yaungane nao na kuiga uchumi wao, au yakimbilie upande wa magharibi.

Mchakato huu ulianza kati ya 1680 na 1750 kwa kupanuka kwa makundi ya wafugaji kuelekea pande nne: Wangimonia waliambaa Mto Tarash na kufanya kitovu cha Waturkana; Wakorwakol walielekea magharibi hadi mto Longiro, na kuwa kundi muhimu la Wajie; kundi la tatu, lililojumuisha Wakarimojong na Wadodo wa baadaye, lilielekea kusini hadi mto Apule; na kundi la nne, Wangikora, lilihamia

kaskazini na kukaa katika Dodoth.

Hali ilitulia kwa muda, lakini shinikizo lililowekwa kwenye matumizi ya ardhi ya maeneo yaliyodhibitiwa na wafugaji pamoja na ukame wa 1780 na 1830 vikaanzisha harakati mpya za kuhama. Idadi kubwa ya watu waliohamia Nyakwai, Labwar, mashariki ya Acholi na Lango angalau walisema lugha mbili: Walisema lahaja ya Kiluo, na kwa kuwa wote waliunganishwa na wasema Kiluo kutoka magharibi ya mbali, walichukua lugha ya Kiluo. Hata hivyo, wale waliokwenda Teso walikuwa na Waluo wachache miongoni mwao kwa hiyo Waiteso wakatumia lugha ya Kiniloti cha Mashariki.

Mtiririko huu wa wakimbizi wakulima kuelekea magharibi ulichapushwa na upanukaji mpya wa wafugaji. Kwenye miaka ya 1780 makundi ya Wadodo-asili kwenye mto Apule yalikwenda kaskazini hadi Dodoth, wakailazimisha jumuiya ya Watoposa kusogea kaskazini mpaka kwenye nchi zao za sasa. Wafugaji wa Kidodo na wa Kitoposa wote walichanganyikana na idadi kadha ya makundi ya Waisera na hivyo kutwaa uchumi uliokuwa umeegemea zaidi kwenye kilimo kuliko ule wa ndugu zao wa kusini. Halafu, katika miaka ya 1820, Wakororwakol na Wajie Rengen waliungana kuteketeza jumuiya kubwa ya kilimo ya Wapoet walioishi kwenye Mto Kapoeta. Hatimaye, katika kipindi hiki hiki Wakarimojong-asili wa Mto Apule walijiingiza ndani ya makazi ya Waokii na Waiteso-Iworopom wa mwisho waliobaki, na kuwaingiza ndani ya jamii yao au kuwalazimisha kuondoka. Matukio haya, pamoja na ukame wa miaka ya 1830, yalichochea hajira kuu za mwisho kutoka katika eneo hili kuelekea magharibi.

Mfano wa Bunyoro-Kitara unaonyesha tena vizuri zaidi mahusiano kati ya wafugaji na wakulima. Kati ya 1760 na 1783 Bunyoro ilipokonywa ardhi nzuri ya malisho na Buganda. Pia kukua kwa mwelekeo wa kujitawala wa wafugaji wa jamii za Nkore, Buhweju na Buzimba kulilibania zaidi dola la Bunyoro kwenye ardhi za kilimo. Wafugaji waliishi miongoni mwa wakulima na kujenga pamoja jumuiya mpya ambamo ardhi badala ya ng'ombe ndiyo iliyokuwa msingi wa mamlaka ya kisiasa. Makundi mbalimbali, yaliyounganishwa na ndoa kemkem za mchanganyiko, yalitoa viongozi na wamiliki ardhi waliokusanya kodi kutoka kwa raia kwa ajili ya mfalme. Hivyo dola jipya la Bunyoro likazaliwa polepole katika karne ya kumi na nane.

## Asasi za kijamii na za kisiasa

Haikuwa lugha na uchumi tu vilivyotofautisha makundi ya wachungaji na yale ya Isera, na kuyatofautisha haya na makundi ya wasema Kiluo. Wafugaji walikamilisha taratibu zao za rika kama vyombo vya udhibiti wa kijerontolojia (wazee), na hizi zikawa asasi muhimu za kijamii na kisiasa katika jamii zao. Utaratibu wa marika pia ulikuweko ndani ya makundi ya Isera na jamii zilizoathiriwa nayo, japo si kwa ukamilifu. Asasi kuu katika jamii hizi zilikuwa mikusanyiko ya kimiviga ya koo kadha, iliyotumiwa kuamua magomvi na kutekeleza sherehe za kidini.

Katika mseto wa kimbari-kitamaduni kaskazini mwa mpaka wa Nili-Kyoga-Bisina, uchifu wa kurithi ulikuwa ni wazo la Waluo. Aina hii ya uongozi ilipingwa na Waluo wengi wa Mashariki na kukataliwa na wazee wao. Hata hivyo uongozi huo ulikuwa na athari fulani kwa asasi za kisiasa, si kwa vikundi vingi visemavyo Kiluo tu, bali pia kwa baadhi ya makundi ya Isera. Miongoni mwa wasema Kiluo, wale waliofuata machifu walielekea kuhamia mashariki mwa Acholi, ambako mawazo yao yaliimarishwa pale baadhi ya makundi ya Paluo yalipokuja kuungana nao kati ya 1680 na 1760. Katika Labwor, Lango, Nyakwac na Kumam, wananchi, kwa jumla, walikataa wazo la uchifu wa kurithi, na kupendelea utawala wa kimiviga wa wazee.

Licha ya haya, makundi haya wakati mwingine yaliwakabidhi viongozi binafsi mamlaka makubwa ya kisiasa. Karne za kumi na nane na kumi na tisa zilishuhudia ongezeko la vita miongoni mwa Waluo wa Mashariki na Waniloti wa Kati-Mashariki. Hili nalo liliongeza athari za viongozi wa majeshi na mabaraza yao, na za vijana, dhidi ya mfumo wa wazee. Hivyo, katika Lango, viongozi wakali wa vita waliunda mashirikisho mapana ya kijeshi ili kuteka nchi yao na kuandaa majeshi makubwa ya mamuluki yaliyopigana huko Bunyoro, Toro na Buganda. Mashirikisho kama haya yaliundwa huko Teso, Sebei (mlima Elgon), Kumam, na Padhola, lakini katika majimbo haya machifu walikuwa *emuron* (makuhani). Kutokana na wadhifa wao muhimu kabisa wa kijeshi, watu hawa walipata nguvu nyingi za kisiasa, lakini hakuna hata mmoja aliyeweza kupata hadhi ya kitemi kwa familia yake. Kuasisi *emuron* kuliingiza mamlaka mpya iliyotishia mabaraza ya vita na mamlaka ya wazee lakini haikuchanganyika kwa urahisi na utemi.

Waiteso waliosakini ndani ya "paja la ngombe" (eneo lililosheheni rutuba katika Ngora na Kumi pamoja na ardhi walizozitwaa kutokea hapo) walifanana sana sana na Waisera wa awali. Hawakuwa na taratibu za makundi ya rika, wala *etem* (makundi ya ukoo ya miviga) na hata *emuron.* Walitegemea koo tatu kuu zilizosifika kwa kusimilisha wageni, yaani Waatekok, Waikarebwok na Wairarak, waliohakikisha mshikamano wa jamii. Wakiwa wamekwisha changanyika zaidi tangu awali, Waiteso wa Kaskazini walikuwa na asasi zote hizi. Waiteso wengi walipenya ndani ya nchi ya Waluo na Wabantu kusini, kama watangulizi au mamuluki. Walikaribishwa kwa makusudi hasa katika baadhi ya madola ya Busoga ambako walisaidia kupunguza shinikizo la kijeshi na la kisiasa kutoka Buganda.

Katika eneo la kati, Buganda ilitofautiana kabisa na Bunyoro. Bila ya ukoo wa kifalme, lakini ikiwa na mfalme aliyeweza kuteua watumishi bila kujali mila, desturi au urithi, Buganda, kufikia mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, ilikuwa na tabaka chache zilizoasisiwa, unyumbufu usio wa kawaida wa kupanda ngazi na kiasi cha kiwango cha tofauti za kijamii kilichozidi kile cha Bunyoro lakini kidogo kuliko cha Rwanda.

Kisiasa na kijamii, Bunyoro-Kitara ilikuwa katikati Ukoo wa kifalme wa Babito awali ulikuwa wa wakulima ambao waliweka mifugo kiasi, lakini nasaba hii ikaendelea kutwaa tabia ya ufugaji zaidi na zaidi. Hata hivyo, matawi yasiyo ya

kifalme ya ukoo wa Babito yalipatikana katika matabaka yote za kiuchumi. Zaidi ya hapo wawakilishi wa matabaka mengine ya kijamii na makundi ya kirafiki waliteuliwa kushika ofisi mbalimbali za dola na baraza la mfalme kiasi kwamba tabaka la wafadhilika liliundwa ambao maslahi yake yalihusishwa na yale ya nasaba ya Babito.

*Mukama* wa Bunyoro alikuwa na mamlaka na utajiri kidogo zaidi kuliko *kabaka* wa Buganda; hii ni kwa sababu katika Bunyoro ufalme ulikuwa na utaratibu wa kugawa utajiri na ziada. Madaraka hayakulimbikizwa hapa; karibu nafasi zote zilikuwa za kurithiwa na *mukama* aliwathibitisha tu wale walioteuliwa. Matokeo yake, wakulima wachache sana walidiriki kupata ofisi ya juu. Zaidi ya hayo, ingawa katika Buganda zile koo thelathini zilikuwa na hadhi sawa, kinadharia, katika Bunyoro kulikuwa na tofauti ya wazi kati ya koo za hadhi ya juu na zile za hadhi ya chini. Waluo wa Kiniloti, walikuwako wale walioishi katika mfumo wa madola n

Miongoni mwa a wale waliokuwa na mfumo usio unganifu (bila utawala wa kati). Miundo ya madola ilikuwa myepesi mno kuliko katika Bunyoro au Buganda, na wafalme wa Kiluo waliingiza athari kiasi lakini walikuwa na mamlaka halisi kidogo tu. Ingawa baadhi ya nasaba zimedumu kwa karne kadha za nyuma, madola mengi ya Kiluo yalianza yamechelewa mno. Zaidi, ukame wa kujirudiarudia ulilazimisha hajira na mikusanyiko mipya ya jamii kiasi kwamba madola mengi, kama yanavyoonekana leo, yameanzishwa kuanzia kama mwaka 1680 au hata baadaye.

Hakuna hata dola moja miongoni mwa madola ya Kiluo lililonufaika na ardhi ya rutuba ya kilimo kama ya Buganda, Rwanda au madola ya Wahima. Wala hawakumiliki migodi sheheni ya chuma na chumvi kama ya maeneo ya Bunyoro au Busongora. Inaelekea Waluo walimiliki makundi tosha ya ng'ombe kabla ya *Nyurabanga,* lakini kufikia 1800 mifugo hii ilikwishateketezwa. Matokeo yake, dola la Kiluo halikuonyesha tofauti za utajiri wala hisia za kitabaka kama zile zilizoyatambulisha madola ya kusini-magharibi. Ndani ya madola yote ya Waluo, Waniloti wa Mashariki walikuwa mashuhuri sana, na idadi yao iliongezeka kutoka magharibi hadi mashariki na kufanya idadi kubwa kabisa ya wakazi wa Acholi ya mashariki. Walikuwa wajamaa sana katika mawazo yao ya kisiasa na ya kijamii na bila shaka ilikuwa vigumu kuwabadilisha na kuwaingiza kwenye mawazo ya uchifu na matabaka ya kurithiana. Katika majimbo ya mashariki, wafalme wa Kiluo walionekana zaidi na zaidi kama maraisi na wasemaji wa mabaraza ya wazee.

Katika madola ya Waluo, nadharia na matendo kuhusu matabaka ya watu vilitofautiana. Kinadharia, jamii za Waluo zimegawanyika katika matabaka mawili, wanamfalme na watu wa kawaida. Hata hivyo mnamo 1830 ainisho la tatu, kati ya wenye asili ya Kiluo na wasio na asili ya Kiluo likawa muhimu. Mara nyingi, wanaufalme walikuja kuhusishwa na Waluo na wasio Waluo kuhusishwa na watu wa kawaida. Kwa mawazo ya kawaida, watu wa kawaida wasio Waluo aghalabu wanapimwa kufuatana na zamani gani wahenga wao walichanganyika na jamii ya Waluo. Hata hivyo, mtu wa ukoo wa kifalme aliyetengana na uchifu kwa vizazi

kumi anatendewa tofauti kidogo tu na mtu wa nje ya ukoo ambaye wahenga wake waliingia ndani ya jamii ya Waluo vizazi kumi vilivyopita. Katika madola ya Waacholi ukoo wa kifalme unaoa nje ya ukoo, na watu wa nje husimilishwa haraka katika ukoo.

Mfumo wa tabaka wa Waluo unaweza kutazamwa kiuhalisi zaidi. Katika jumla ya maridhiano ya kisiasa yaliyofanywa kwa karne kadha, koo zisizokuwa za Kiluo zilishika nyadhifa au kufanya shughuli za miviga ambazo zilizipatia nasaba za wenye nyadhifa hizo hadhi kubwa. Kama kulikuwa na tabaka bora kabisa, basi lilikuwa ni lile la familia asili za mfalme, washauri wake, mamwinyi, na mabingwa wa miviga, wakiwemo wagimba na ma-*jago* (wakuu wasaidizi wa majimbo).

Waluo na Waniloti wa Kati-Mashariki, ambao hawakuwa na miundo ya kidola, hawakuwa na mfumo wa tabaka. Hapakuwa na machifu wala ofisi za kurithi. Tawala za wazee zilisimamiwa na wazee ambao maamuzi yao, iliaminiwa, yalibarikiwa na wahenga. Mifumo hii ya kihenga aghalabu ilijikusanyia makundi makubwa ya kijeshi ambamo chifu wa kivita na wasaidizi wake walitambuliwa na kuungwa mkono na *emuron* (kuhani). Palikuwa na mvutano kati ya wazee wanaotawala na wapiganaji vijana. Wazee waliweka udhibiti mkali hata wa kikandamizi juu ya vijana wa kiume, wakichelewesha matumaini yao ya ndoa na uhuru kwa kuhodhi vyote - wanawake na ng'ombe. Wakati mwingine vijana walihama kuepuka tafshani kama hizi.

Waluo wasio na mtawala mkuu na Waniloti wa Mashariki walionyesha mara nyingi tofauti kubwa za kiuchumi, zilizodhihirishwa na idadi ya ng'ombe waliowamiliki. Mali ilileta heshima na kuamsha matumaini ya ukarimu kochokocho lakini haikujenga tofauti za kijamii. Kwa yakini, ng'ombe waligawanywa kwa watu wengi kwa njia ya mahari.

### Mabadiliko katika uwiano wa mamlaka: kushuka kwa Bunyoro na kuinuka na kupanuka kwa Buganda

Baada ya *Nyarubanga*, matukio muhimu kabisa katika historia ya maeneo ya kaskazini na ya katikati ya jimbo la Maziwa Makuu yalikuwa ni zahama ndani ya Bunyoro, iliyoifanya ididimie hatimaye, na maendeleo ya ndani ya Buganda, yaliyoifanya iinuke na kupanuka hatimaye Mambo mawili haya yalisababisha mabadiliko ya ajabu katika uwiano wa mamlaka. Mgogoro wa Bunyoro ulianza na kifo cha Chwa wakati wa uvamizi wa kusini uliotokana na *Nyarubanga*. Mwana pekee wa Chwa, Winyi II, alitekwa, na Kitara kutawaliwa na mwakilishi, dada yake Chwa, Mashamba. Chwa hakuwa na wana kwa mke wake wa Kiluo ambao wangemrithi kufuatana na kanuni za jamii ya kifalme. Winyi II alimwua Mashamba na kutwaa ufalme. Baada ya hapo, desturi ya kale ambapo mrithi ilibidi azaliwe na mama wa Kiluo au Kipaluo, ikawa si kanuni tena bali tukio la nadra. Hivyo ugombeaji kiti cha enzi ukawa wazi kwa wanamfalme wote na magomvi ya urithi yakawa ya mara kwa mara na makali zaidi.

Chini ya nasaba ya kwanza, utemi wa Pawir ulikuwa na nafasi ya heshima ndani ya muundo wa himaya. Mfululizo wa "wafalme wa Kibantu," kama walivyoitwa na Wapaluo, ulikusudia kutumia vurugu la Pawir kuchochea hali ya utengano. Hili walilifanya kwa ufanisi kiasi kwamba utemi mdogo wa Pawir, ulioungana mwaka 1650, ulikwisha jigawa katika vijitemi sita kufikia mwaka 1750. Chini ya utawala wa Isana (t. 1733-1760), vijitemi hivi viliwekwa chini ya mamlaka ya mtemi wa nchi; hivyo nchi ya Paluo sasa ilipoteza hadhi yake ya kuwa nusu-huru na badala yake ikaingizwa ndani ya Bunyoro. Wapaluo waliendelea kukataa uteuzi wa Wabantu kwenye kiti cha enzi; baadhi walihamia kaskazini na mashariki kwa sababu ya kuzibiwa upeo wao wa kisiasa, kupoteza hadhi yao na kuteswa tu. Magomvi ya mara kwa mara ya urithi, yakichanganyika na ukinzani wa Kipaluo, yalidhoofisha mamlaka kuu ya Kitara.

Matokeo ya mara moja ya mgogoro ndani ya Bunyoro yalikuwa ni kuhama kwa mkupuo kwa Wapaluo-Pakoyo kukimbilia Acholi, Busoga kaskazini, Alur na hata Padhola na magharibi mwa Kenya. Wakati Wapaluo walieneza lugha yao kaskazini, Wapakoyo walijumuishwa kiisimu katika jamii ya Wasoga. Kaskazini, aina kuu ya uongozi wa kisiasa ilikuwa ni ya uzee au temi ndogo. Wapaluo walieneza ngoma ya kifalme, wakakuza heshima ya mtemi na kuingiza tawala ndogo ndogo ndani ya madola makubwa zaidi, huku wakiziruhusu kuendeleza uongozi wao wa urithi. Walianzisha madola mapya, kwa mfano, Lira Paluo na Paimol, na kukuza na kuunda upya madola mengine, kama Padile, Patongo, Alero na Koch. Puranga na Payera zilivutiwa na nadharia za Wapaluo na kusimilisha idadi kadha ya tawala ndogondogo katika mchakato wa kupanuka. Kujumuishwa katika jamii ya Kiluo kulifanyika ama kwa kusimilishwa ama kwa kugawanyika na kuwa na utitiri wa tawala ndogo ndogo za kisiasa. Lira Paluo ni mfano wa utaratibu wa kwanza (wa ujumuishi), Alur ni mfano wa utaratibu wa pili (wa kugawanyika).

Omukama (mfalme) Isansa alikuwa na dhima ya msingi katika kuanguka kwa Bunyoro kama alivyokuwa Kabaka Mawanda katika kuinuka kwa Buganda. Utawala wa Isansa ni mashuhuri kwa mchanganyiko wake wa ajabu wa ufanisi wa kijeshi na ushinde wa kisiasa. Kampeni aliyoongoza kusini ilikusudiwa kuonyesha mara nyingine tena nguvu za kijeshi za Bunyoro. Kwa kweli, Isansa alikuwa akigeuza sera ya kutawala nchi za pembezoni iliyofanya kazi kwa ukubalifu kwa karne tatu. Kosa lake kubwa kabisa la kisiasa lilikuwa kuishambulia ikulu ya Wamara, mkuu wa madhehebu ya Wa-Chwezi huko Bwera. Inawezekana Wamara alipinga nasaba ya pili ya Babito kwa sababu ilikiuka sheria za mila za urithi. Isansa akaamua kuvamia kijeshi. Kufuru hii ilikuwa kubwa kiasi kwamba miti "ilivuja damu" na Wamara alimwapiza Isansa, akitabiri kuwa Buganda ingeimeza Bunyoro. Utabiri ulisadifu kuwa kweli; Buganda haikutwaa sehemu kubwa ya Bunyoro tu bali madola madogo ya kusini hayakuwa salama pia. Yalikuwa mawindo muwafaka ya tamaa za kihimaya za Buganda, Nkore na Mpororo.

## Kuinuka kwa Buganda

Wakati wafalme wa Bunyoro wakijishughulisha na kuvunja mfumo wa siasa uliowahakikishia utawala wao kwa karne tatu, wafalme wa Buganda walikuwa wakisahihisha maovu mengi ya kisiasa yaliyokwamisha Buganda tangu ianzishwe. Tatizo la kwanza lilitokana na kuongezeka nguvu za ufalme na urasimu wake dhidi ya wakuu wa koo au viongozi wa Bataka. La pili lilihusishwa na utitiri wa wanamfalme wenye tamaa waliotafuta kila fursa ya kuvishawishi vikundi vya kisiasa vya koo kwa nia ya kutwaa kiti cha ufalme. Tatizo la tatu lilihusu magomvi ya kikatili ya urithi yaliyofuata vifo vya karibu wafalme wote. Magomvi haya yalileta uharibifu zaidi katika Buganda kuliko Kitara. Huko Kitara mapambano ya kiti cha enzi yaliweza kuwa makali lakini mara baada ya kuchaguliwa mfalme na kutawazwa aliuawa au kupinduliwa kwa nadra, ambapo katika Buganda mfalme aliweza kuuawa au kupinduliwa wakati wowote katika utawala wake.

Buganda ilikaa mahali pazuri kimazingira na kijiografia kuliko madola mengine makubwa ya Maziwa Makuu. Ukame haukutajwa popote ndani ya mapokeo yake marefu na yaliyoshehenezwa. Ilikuwa na msingi imara na anuwai wa kilimo ambao uliwapa uhuru wanaume kushiriki vita na siasa. Zaidi ya hayo, kwa kuwa ukingoni mwa Ziwa Nyanza, iliendesha biashara ya ziwani. Ilitengeneza nguo kutoka magamba ya miti ambazo zilithaminiwa sana na nchi za jirani. Katika utanuzi wake, Buganda ilifanikiwa kudhibiti migodi ya mbale (za chuma), rasilimali ambayo haikuwa nayo awali. Ukiondosha pengine madola ya Busoga ya kusini, hakuna madola mengine katika ukanda wa Maziwa Makuu yaliyomiliki kiunzi bora hivyo cha kijiografia na kiuchumi.

Lakini tofauti na madola mengine ya Maziwa Makuu, Buganda haikuwa na ukoo wa kifalme. Kila mwanamfalme alifuata ukoo wa mama yake, ambapo watu waliobaki walifuata kanuni za ubaba. Kwa hiyo kila ukoo ulikuwa na nafasi ya kutoa mfalme. Mfumo huu uliwapa watu wote hisia ya kuwa sehemu ya ufalme lakini, pia, uliutia moyo kila ukoo kumpatia *kabaka* mke, jambo ambalo lilizaa utitiri wa warithi watarajiwa wa ufalme.

Katika karne za kumi na sita na kumi na saba, Buganda ilikuwa kijidola tu, kama vingine vingi katika Busoga, vilivyovumilia urithi wa udugu na kutegemea watawala wa kifalme. Haikuwa imara na ilivunjwa vunjwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe visivyokwisha. Hata hivyo, utaifa wa Baganda ulikuwa na nguvu za kutosha kuzuia kujitenga na kugawanyika kwa dola.

*Kabaka* Tebandeke (t. 1644-1674) aliimarisha nguvu za ufalme kwa mashambulio fanisi dhidi ya maofisa wa miviga ya kidini, ambao matendo yao ya kupokonya yaliulemea sana ufalme na umma. Kufanikiwa kwake na kushindwa kwa Isansa kulitokana na tofauti za uongozi wa kidini katika falme mbili hizi. Katika Kitara madhehebu ya Wachwezi yalikuwa asasi gatifu, ambapo huko Buganda yaelekea kila ofisa wa miviga alikuwa akijitegemea.

Upanuzi wa nchi ya Buganda unahusishwa na wafalme watatu mashuhuri wa karne ya kumi na nane. Mawanda (t. 1674-1704) aliiteka Singo, akaivamia Kyaggwe na kutwaa Bulamogi kutoka Bunyoro. Kufuatana na ushindi mkubwa unaotokana na utekaji huu, kwa busara Mawanda alitelekeza mfumo wa zamani wa utawala fiche (usiokuwa wa moja kwa moja) na kuteua marafiki zake kutawala nchi zake mpya. Mawanda hakuwa na kipawa cha kijeshi tu, bali pia alikuwa mwanasiasa mwenye upeo wa mawazo na anasifika kwa haki kabisa kuwa baba wa mfumo wa sasa wa serikali ya Kiganda. Junju na Kamanya wote walitanua mipaka ya ufalme kati ya 1734 na 1794. Junju aliiteka Buddu na kulazimisha Kooki kuingia katika uhusiano wa ushuru. Kamanya alitwaa Buwekula kutoka Bunyoro. Hadi 1800 Buganda ilikwishajenga kikamilifu mamlaka yake juu ya Bunyoro.

Semakokiro, katikati ya karne ya kumi na nane, alijishughulisha na tatizo la wanamfalme. Alianza zoezi la kuwaua wapinzani walioshindwa, hata, kama hapana budi, wanamfalme. Aliwatimua wanamfalme (kutoka) kwenye utawala ili kuwazuia kutumia nafasi zao kula njama dhidi ya ufalme. Zoezi hili lilimpa mfalme mamlaka makubwa na kuandaa uanzishwaji wa ufalme wa kiimla ulioibuka katika karne ya kumi na tisa. Kwa kuzingatia vurugu la miaka ya awali ya siasa za Buganda, si ajabu kuutukuza mno ukubwa wa *kabaka* wa karne ya kumi na nane aliyefanya kazi ya kuunganisha dola. Lakini ni vyema kukumbuka kuwa utawala wa mabavu uliweza kufikiwa tu baada ya maasi ya muda mrefu, upinzani mkali kwa *kabaka*, ukatili mkubwa na ongezeko la wakimbizi kuelekea madola ya jirani.

Kwa karne nyingi, Buganda iliishi chini ya kivuli cha ubeberu wa Bunyoro, lakini, mwishoni mwa karne ya kumi na nane, ilikuwa tayari kuikabili hali hii. Buganda ilikwishajenga uzalendo mkali uliowawezesha wafalme wake kukusanya nguvu na kujenga mfumo imara wa kiutawala na kijeshi. Kufikia 1800 ilikwishakuwa na jamii shindani sana yenye kuwaruhusu watu kupanda ngazi na kujiendeleza kimaisha kuliko jamii yoyote ile katika ukanda wa Maziwa Makuu.

## *Falme za kilimo na kifugaji za Kusini*

Istilahi "utamaduni wa kati ya maziwa" iliyotumiwa kwa karibu karne nzima na wanaethnolojia wa mambo ya Kiafrika ilitokana na uchunguzi uliofanywa katika nusu ya kusini ya ukanda, hususan katika ufalme wa Rwanda ulioteuliwa kama mfano bora na waandishi kadhaa. Uundaji wa tanzo hii ya kitamaduni umekadiriwa kutukia katika kipindi cha karibuni hivi, kutoka karne ya kumi na sita hadi karne ya kumi na nane. Kazi iliyofanywa na wanahistoria kwa kipindi cha miaka ishirini iliyopita imesafisha taswira hii na kuziingiza katika muktadha wake wa kweli wa kihistoria jamii za watu zenye historia iliyosimikwa katika Zama za Chuma za kale, zenye kurudi nyuma angalao hadi mwanzoni mwa enzi ya Kikristo. Karne ya kumi na sita ni kipeo muhimu katika historia yao.

### Eneo la kijiografia - kiutamaduni

Umbile la kiasili la eneo hili na urithi wake wa kitamaduni unalipa madhari ya kinchi na

kijamii yaliyojaa tofauti nyingi. Magharibi safu ya Kabira - genge kubwa la mwatuko, lenye urefu wa mita 2000 kwenda juu, na linaloendelezwa kaskazini na volkano za Virunga- inatawala mabonde ya Ziwa Tanganyika na Ziwa Kivu. Mashariki vilima vya juu vya Rwanda na Burundi vinateremka pole pole kuelekea nyanda za juu zenye matutamatuta hadi pwani ya Ziwa Viktoria. Umbali wa nchi hii wa kilomita zaidi ya elfu moja kutoka Bahari ya Hindi ndio unaoupa ukanda huu kilimati (hali ya hewa) yake. Kadhalika, kutofautiana kwa sura ya nchi kunasababisha tofauti kubwa za viwango vya mvua. Nchi za juu za magharibi na pwani za Ziwa Viktoria zina mvua za mwaka za zaidi ya milimita 1500, ambapo bonde jembamba la Kagera linapata mvua chini ya milimita 1000.

Ruwaza ya kusambaa kwa lugha nayo ilikuwa na namna nyingi. Kanda zinazohusika zilikuwa na zoni mbili ambamo lugha za Kibantu zilisemwa. Watu waliweza kuelewana bila shida kubwa kutoka volkano za Viruga hadi Malagarazi ya chini, na kutoka Ziwa Lutanzige (Rwitanzige zamani Ziwa Albert) hadi kusini mwa Ziwa Viktoria. Katika eneo la awali, wafalme waliitwa *mwami* na katika yale ya pili *mukama* au *mugabe*. Hata hivyo, mipaka hii ya kijiografia na ya kitamaduni iliyokwisha jijenga kwa muda mrefu ilikuja kupoteza udhahiri wake kuanzia karne ya kumi na sita na kuendelea, kadiri falme zilivyoendelea kujijenga.

## Alama zilizoachwa na Ruhinda na Bachwezi.

Madola ya kusini yawezekana yalizuka kutokana na kusambaratika kwa ufalme wa kale, ulioanzishwa kati ya karne za kumi na sita na kumi na nane na mtekaji aliyeitwa Ruhinda - angalau hii ndiyo imani iliyokuwapo hadi miaka ya 1950. "Himaya ya Ruhinda" ilichukuliwa kuwa upanuzi, kuelekea kusini, wa "Himaya ya Bachwezi." ulioletwa na wimbi jipya la upanuzi la Wahima wafugaji. Sasa inafikiriwa kuwa tukio hili, kama kweli lilikuwepo, lilitokea mapema zaidi, mnamo karne ya kumi na tano. Ama kuhusu "kisakale cha Ruhinda." mapokeo mbalimbali yalirithisha maelezo yanayotofautiana sana. Huko Bunyoro na Nkore, shujaa Ruhinda anaelezewa kuwa ni mwanaharamu wa Wamara, "mfalme" wa mwisho wa Wachwezi, na mjakazi Njunaki, ambapo katika nchi ya Uhaya na Uzinza, baba yake anadaiwa kuwa alikuwa lgaba au Bugaba (Rugaba?), moja ya majina ya wenyeji ya Mungu Mkuu. Nasaba za Kihinda za Nkore, Karagwe, Kyamutwara, Ihangiro na Buzinza zilijichukulia kuwa waanzilishi wao walikuwa ama ndugu, mwana au mjukuu wa Ruhinda, ambaye anadaiwa kuwa alimpa kila mmoja wa waanzilishi hao nchi na ngoma.

Ushahidi wote unaonyesha kuwa kumbukumbu kuhusu Ruhinda inaakisi makutano ya mawimbi mawili ya mapokeo, yenye kuhusiana na makundi makuu mawili ya koo, Bahinda na Bayango, ambayo yalikwisha chukua mwiko mmoja, ule wa kima (*nkende*). Kuhusu kuanzishwa kwa nasaba za Kihinda, mapokeo yanahadithia kuwa hili lilitokea kizazi kimoja au viwili tu baada ya kizazi cha mshindi wa kwenye visakale. Labda jambo la kuvutia la kihistoria ni kuendelea kuwako kwa mapokeo ya Ruhinda, chimbuko la uhalali wa kisiasa, muda mrefu

baada ya karne ya kumi na sita. Ruhinda alitajwa katika karne ya kumi na nane huko Kyamutwara dhidi ya wanyang'anyi wa utawala kutoka ukoo wa Bahima wa Bankango; jina lake lilihusishwa katika karne ya kumi na tisa na kumbukumbu za utukufu wa zamani (katika Karagwe) na za umoja uliovunjwa (katika Buzinza). Mapokeo ya Ruhinda yalitumika katika karne ya kumi na tisa kuwaunganisha Wanyoro na Wahaya dhidi ya ubeberu wa Baganda.

Mapokezi kuhusu Ruhinda yalipata nguvu zake kutokana na uhusiano uliopo kati ya shujaa huyu wa hekayani na jusura za Bachwezi. Bila kujali ukweli wa kuwapo kwake, mapana yake na muda wake, "Himaya ya Kitara," kama kiunzi cha kijamii na kidini, ni dhahiri chimbuko lake lilikuwa katika nyanda za juu za Uganda ya magharibi. Hata hivyo, kusini ilichipuza visasili vyake mahususi, ambavyo kwavyo shughuli kuu zilitendwa na Wamara, Mugasha na Ryangombe. Miungu hii ni ile muhimu kabisa kati ya utitiri wa miungu thalathini au zaidi, iliyoendelea kuongezwa kufuatana na haja. Kila Mungu anahusishwa na eneo la shughuli fulani. Wamara anahusishwa na wafu, Mugasha na maji, mvua na maziwa, hivyo na uvuvi na kilimo, Irungu na nyika, hivyo na uwindaji na safari, Kagoro na radi na Ryangombe na ngo'mbe na uwindaji.

Ingawa Wamara, ambaye madhababu yake makuu yalikuwa katika Masaka, Bwera (Uganda), ni jina hai katika mapokeo ya Kitara, Nkore na Karagwe, athari za Mugasha yaelekea zilienea kutoka visiwa vya Sese, katika Ziwa Viktoria. Maelezo ya Ryangombe yanapatikana zaidi upande wa magharibi kutoka Rwanda hadi Ziwa Tanganyika. Dini hizi si asasi za kifalme tu, bali zinaonyesha kuwa na vyanzo vya kale ambavyo vinatangulia uanzishaji wa nasaba za kisasa.

Dini ya Bachwezi (au dini ya *Imandwa*) ilikuwa huru katika kuabudu na katika visasili vyake. Mashariki (katika Uhaya na Uzinza) familia hizo hizo ziliendeleza shughuli za kurithishwa kama *mbandwa* (makahini wa miungu), na zilihusika na utunzaji wa madhabahu. Upande wa magharibi (Rwanda, Burundi, Buha) kuingizwa katika *kubandwa* kulienea sana. Ishara na maneno yaelekea vilihusisha dini hii na ufalme wa Uhayani na Nkore, ambapo matendo ya ibada yaliyofanywa chini ya kivuli cha mti wa *mlinzi*, mti mtakatifu wa Ryangombe na Kiranga, yaelekea yalihusiana zaidi na umma. Lakini katika hali zote, haya yalikuwa ni matendo ya uzinduzi wa uaguzi na tiba, yenye kutoa kinga dhidi ya vitisho kutoka kwa wahenga wa karibu au matumizi mabaya ya madaraka.

## "Koo" au "tabaka-amali"?

Baada ya kukabiliwa na mapokeo andishi ambayo yaliipa umuhimu mkubwa nadharia ya "tabaka-amali" na hasa upinzani wa "kijamia" kati ya "malodi wa Kihima na Kitutsi" na "Bairu na watwana wa Kihutu," uandishi wa historia wa siku hizi umejishughulisha zaidi na muundo wa "ukoo". Licha ya kuwako katika ulimwengu wote wa utamaduni simulizi, ukoo hauna ufungamano sahili wa kikundi cha wanandugu, hata kama unahisiwa hivyo wakati mwingine. Nasaba, kwa maana halisi


ya neno hilo, zinaainishwa kwa vitengo vyenye kuwa na jina la jumla, kwa mwiko mmoja au miwili, na wakati mwingine kwa mapokeo yanayohusu asili yao au kwa kinga ya Mungu mmojawapo miongoni mwa Miungu wa Kichwezi, lakini hazikuwa na umoja wa kieneo. Baadhi ya koo zinatokea katika historia ndefu ya falme kadha za jimbo la Maziwa Makuu, mifano ikiwa ni Bayango wa Nkore wanaopatikana pia Buzinza, Bakimbiri wa Nkore na Buha ya kusini, na Basita wa Bunyoro na Bukerebe. Miiko wakati mwingine inahusu hata makundi makubwa zaidi: chura anaheshimiwa Rwanda na Bega, Bakono na Bahu (koo tatu kubwa ambazo zilitoa mama za malkia). Miongoni mwa mifano ya kuenea kwa mwiko wa *nkende*, mfano wa kustaajabisha ni ule wa Kiziba ambako mwiko huu unaheshimiwa na koo za kinasaba za Babito na Bahinda.

Usuli wa kihistoria wa koo u wazi katika Rwanda. Muundo wake hapa ni wa kipekee, kwani umefungiwa kwenye koo kuu kumi na nane ambazo zote zinahusisha Wahutu, Watutsi, na Watwa. Kwingineko, katika Burundi, Buha, Karagwe na nchi zenye kuambaa Ziwa Viktoria, kulikuwa na mamia ya koo lakini kila mmoja ulikuwa na aina tofauti ya ushirika, ama vitengo visivyooleana, au shirika zilizojengwa kwenye mahusiano ya utani au kula kiapo. Utambulisho aghalabu ulihusishwa kwa karibu na utekelezaji wa kazi za kisiasa au za kidini za uzito mkubwa au mdogo. Hadhi ya mtu ilitambulishwa na ukoo wake. Mapokeo ya kale kabisa yanashuhudia idadi kubwa ya dhima za kijanibu ambazo zilifanywa na koo maalumu, japo hili halimaanishi kuwa kila moja ya temi hizi ilikaliwa na watu wa aina moja.

Katika Rwanda, kuna vikundi vya kisiasa vingi vya kabla ya Wanyiginya, na idadi kadha ya vikundi hivi vimeendeleza dhima zake za miviga katika Rwanda ya sasa. Katika Burundi, hifadhi ya ngoma na majukumu ya kidini yaliyoshikiliwa na baadhi ya koo huenda vinaakisi mamlaka-tawala za zamani. Temi za koo hizi zote zilimezwa polepole kati ya karne za kumi na tano na kumi na saba (wakati mwingine baadaye) na nasaba mpya kama tutakavyoona. Licha ya mabadiliko na athari hizi za kikanda, vijikundi vidogo ndani ya ukanda viliendeleza upekee wake hadi karne ya ishirini.

Tofauti kati ya wafugaji na wakulima haiko wazi kabisa katika muktadha huu kiasi cha kusadikisha nadharia tete iliyopo ya mavamizi na migogoro. Si katika Rwanda tu ambako koo zimechanganyikana; hivi ndivyo ilivyo kwa asilimia 20 ya koo za Buhaya, zaidi ya asilimia 10 ya Bahutu, zaidi ya asilimia 50 ya Batutsi na asilimia 90 ya koo za Batwa katika Burundi. Koo nyingine ziko katika hatua ya kati au isiyo dhahiri, zikielezwa kama *Bairu* (walioenziwa) au *Bahutu* (wanaotoka katika familia nzuri). Basita wakati mwingine wanaitwa wafugaji (katika Rwanda kwa mfano), katika sehemu nyingine wanaitwa wafua vyuma-wakulima.

Ingawa nadharia tete kuhusu kukutana zama za kale kati ya makundi yasemayo Kibantu na makundi yasemayo Kikushi cha kusini au lugha za Sudani ya kati zinavutia, lakini zinahusu enzi za zamani sana (miaka elfu moja ya kwanza), hivyo haziwezi kutoa fununu ya hali halisi katika karne ya kumi na sita, hasa ikizingatiwa




*26.6 Eneo la kusini la Maziwa Makuu mwishoni mwa karne ya kumi na saba (J.P. Chrétien)*

kuchanganyika kwa tamaduni za watu hawa. Miainisho ya mbari ilitokea kwa misingi ya kikanda, kiukoo au kisiasa na kuakisi kategoria za Kihima/Kitutsi na Kiiru/Kihutu, ingwa itakuwa hatari kujaribu kueleza hasa kategoria hizi ziliwakilisha nini karne nne zilizopita. Jambo moja pekee laelekea kujitokeza - kiasi cha shughuli za ufugaji kwenye uwanda wa juu wa kati kutoka Nkore hadi Buha, kupitia Karagwe, Gisaka na Bugesera. Ushindi wa "Wahamiti," unaotajwa mara kwa mara kuhusiana na kipindi hiki, unatokea kuwa si chochote zaidi ya njia nyingine ya kuwasilisha sulubu za mahusiano ya kikanda na kisiasa-kiuchumi kati ya sekta iliyojikita katika ufugaji na sekta iliyojikita katika kilimo kati ya karne ya kumi na sita na karne ya kumi na nane.

## Uundaji wa falme za Kisasa: Uchunguzi wa kisiasa - kimazingira

*Matatizo ya kronolojia*

Utajiri wa vyanzo vya masimulizi unachangia katika tatizo changamani la kujenga upya kronolojia ya jimbo hili, kwani orodha za kinasaba na shajara za wanamfalme zinaonyesha tofauti nyingi, hasa kabla ya karne ya kumi na saba. Matukio mawili ya kupatwa kwa jua yanayotajwa mara kwa mara katika mapokeo yanatoa kumbukumbu mkata lakini kutambuliwa kwake kumesailiwa. "Mashambulizi" yaliyopangwa kuelekea kusini na wafalme wa Kibito wa Bunyoro pia yanaonekana kama athari unganishi tu kati ya falme mbalimbali, maana mapokezi yaliyokusanywa katika kila ufalme yanalipa tukio hili nyakati tofauti. Kwa yakini, Wanyoro lazima waliandaa mashambulizi mengi ya kupora ng'ombe. Hata hivyo, mawimbi matatu ya tabaro kubwa yanaainishwa:

(1) Katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na sita baada ya ushindi wa mwaka 1520 katika Nkore, Wanyoro wanasemekana kuwa waliivamia Rwanda mara mbili, wakiongozwa na mwanamfalme Chwa, mwana wa Nyabongo mrithi wa Olimi.

(2) Katika karne ya kumi na saba, ufalme mdogo wa Kiziba wa Kibito unaelekea ulipata mashambulizi ya mhami wake, Bunyoro, hasa wakati wa utawala wa Magembe Kitonkire. Karagwe iliathiriwa pia kipindi hiki hiki.

(3) Katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na nane mashambulizi mashuhuri yalitokea, yanayonasibishwa na *mukama* aliyeitwa Chwa au Kyebambe. Baada ya kuiteketeza nchi yote ya Buhaya kwa miaka kadha, mfalme huyu anasemekana alishindwa na kuuawa na mfalme Nyarubamba Kichumbu katika Ihangiro. Wakati huohuo kundi jingine la Wanyoro lilishindwa na Mugabe kutoka Nkore, ajulikanaye kama Kitabanyoro (Mwuaji wa Wanyoro). Falme za kusini hatimaye ziliondoshewa shughuli za Wabito, ambao athari yao, bila shaka, ilikuwa muhimu, hasa katika maongozi ya kijeshi ya falme hizi.

*Madola ya nyanda za juu za Kagera*

Jimbo hili la nyanda za nyasi liliwakilisha mwimo muhimu wa kisiasa - kijiografia, likitoa njia rahisi kutoka bonde la Kitonga hadi lile la Malagarazi. Bahati mbaya, historia yake ya kisiasa ndiyo iliyorekodiwa vibaya kabisa ndani ya ukanda huu, kutokana na matatizo yaliyozipata falme mbalimbali tangu karne ya kumi na tisa, na kusababisha mmomonyoko wa haraka wa mapokeo yao. Ni sehemu ya kaskazini tu, yenye kujumuisha Mpororo, Nkore na Karagwe, inayojulikana vizuri kwa wastani.

Licha ya vyanzo vyake vitukufu (nasaba ya Kisita), Karagwe ilianza kujionyesha nguvu zake kuanzia karne ya kumi na saba na kuendelea, ikitumia wimbi la kwanza la athari za Bunyoro. Ni machache yanayojulikana kuhusu akina Ntare na akina Ruhinda waliokuja baada yao, zaidi ya ukweli kwamba walikuwa na nguvu zaidi kuliko majirani zao upande wa mashariki. Walidumisha mahusiano mazuri na Gisaka na Rwanda, ambayo hata yaliingiza mashirikiano ya ndoa. Zahama katika karne ya kumi na nane, iliyochochewa na mashambulizi ya Wanyoro, ilisababisha upanuzi mpya na wa kasi, ukiongozwa na Ntare Kitabanyoro, na baadaye kuimarishwa kwa kuanzishwa kwa uhusiano wa kibiashara na nchi za Waganda na Wanyamwezi.

Mpororo, au Ndorma, ilirithi desturi thabiti ya serikali za kiukoo. Inasemekana kwamba Wakimbiri walitawaliwa na Ryangombe mwenyewe, na Wabaishekatwa na Malkia Kitami. Serikali nzima iliendeshwa na nasaba ya Wahima kutoka ukoo wa Washambo ambao walitumia kwa faida yao ombwe iliyotokana na kushindwa kwa Wanyoro huko Rwanda. Washambo walianzisha mashirikiano ya ndoa na Wahinda wa Nkore, ambao kwa wakati huo walikuwa dhaifu kuliko Washambo. Katikati ya karne ya kumi na saba, Mfalme Gahaya, mwana wa Ishemurari, alishambulia Gisaka na kuitia wasiwasi Rwanda. Kilele kilifikiwa mwanzoni mwa karne ya kumi na nane, lakini, miaka 50 baadaye, wakati Gahaya Rutindangyesi alipofariki, ufalme uligawanyika katika majimbo mawili yanayoshindana, na ngoma ya Murarwa ikafichwa karibu na Ziwa Bwinyoni katika milima ya magharibi.

Nasaba ya Gisaka ilidai kuwa na asili mbili za kiukoo; Wagesera na kundi la kizimu la *nkende* (nyani). Mwishoni mwa karne ya kumi na tano, Mfalme Kimenyi alitishia kuteka nchi ndogo ya *mwami* wa Rwanda aliyeitwa Ruganzu Bwimba. Katikati ya karne ya kumi na sita, Kimenyi Shumbusho alitumia fursa ya shambulizi la Wanyoro kuteka sehemu za kati za Rwanda za Bugunza na Bwanachyambwe. Rwanda haikuweza kurejesha sehemu hii iliyotekwa hadi karne moja baadaye.

Bugesera pia inaweza ikatazamwa kama mtangulizi wa nguvu za kisiasa ambazo baadaye ziliimarika katika milima ya magharibi. Nasaba ya Wahondogo ilikuwa ina uhusiano wa karibu na ile ya Wanyinginya wa Rwanda ya awali, na mashirikiano ya kindoa na kijeshi yaliipambanua historia ya nchi mbili hizi kutoka karne ya kumi na sita hadi ya kumi na nane. Hadi mwisho wa karne ya kumi na saba, Bugesera ilienea katika sehemu kubwa sana ya nchi kutoka mto Kanyarn hadi mto Ruvubu (theluthi nzima ya kaskazini ya Burundi ya leo), na, ikiwa na maeneo yake ya kunyweshea mifugo na kufanyia miviga, iliwakilisha makazi ya kawaida ya kichungaji. Matatizo

yalizuka kutokana na kukua kwa nasaba ya Baganwa huko Burundi, ambayo ilipendelea kushirikiana zaidi na Gisaka. Karne ya kumi na tisa ilianza na kugawanyika kwa nchi.

Kusini zaidi, falme kadhaa zilianzishwa katika bonde la Malagarazi. Kutoka karne ya kumi na sita. 'Buha ya kaskazini' inasemekana ilikuwa ikijumuisha Buyungu, Mahambwe, Ruguru, Buyogoma na hata Bushubi. Nasaba ya Wahumbi ilibakia kuwa na nguvu hadi karne ya kumi na nane. Hata hivyo, mapema zaidi, huko kusini mwa mto, Ruguru ikawa kituo cha dola jingine lililoundwa na Heru na Bushingo na kutawaliwa na nasaba ya Wakimbiri, ambayo, pamoja na jimbo la Wajiji huko Nkarinzi, ilianza kuielekea milima inayotazamana na kingo za mashariki za Ziwa Tanganyika. Ni katikati ya karne ya kumi tu Buha ilipoanza kuparaganyika.

*Madola yaliyopakana na Ziwa Viktoria*

Nchi hizi, ambazo zilikuwa na watu wengi zaidi, zilienea kwenye nyanda za juu za nyasi, nchi tambarare zenye unyevuunyevu na rutuba, na mabonde yenye maji yaliyojaa samaki. Utofautiano huu wa kijiografia uliathiri jumuiya na madola, na kwa kiasi fulani ulichangia katika kugawanyika kwa Kyamutwara na Buzinza katika karne ya kumi na tisa.

Kiziba, iliyopo kati ya Ziwa Viktoria na Mto Kagera, iligawanyika baina ya mahusiano yake ya kimapokeo na Kitara-Bunyaro naVisiwa vya Sese. Aidha, kila mara ilikuwa katika mgogoro na majirani zake wa kusini-magharibi, Kyamutwara na Karagwe, ambao walitumia migogoro ya kurithisha ufalme kwa faida yao. Tishio la Wanyoro ilifuatiwa mwishoni mwa karne ya kumi na nane na mashambulizi ya Waganda.

Katika Kyamutwara, utukufu wa Wahinda ulijengeka wazi na kukamilika katika karne ya kumi na saba na Mfalme Karemera. Ukatili wake wa kichaa inasemekana ulimfikisha kwenye hatua ya kuamuru mwanawe, Mukanbya, apofuliwe. Nasaba mpya ilianzishwa na Rugomora Mahe aliyeonekana kuwa shujaa na mstaarabishaji. Yeye na madhuria wake wakautumia udhaifu wa Kiziba na Ihangiro, angalau hadi mwisho wa karne ya kumi na nane, ambapo Kyamutwara nayo ilidhoofishwa na mfarakano wa ndani. Zaidi ya hayo, nasaba mbili za Bahima wa ukoo wa Bankango, waliotoka Buzinza katika utawala wa Kahigi Kasita, ziliendelea kupata nguvu za kijeshi na za kisiasa mnamo karne ya kumi na nane. Mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa waliweka serikali huru huko Bugabo, na kuanzisha "Kyamutwara ndogo" kwenye pwani ya Ziwa Viktoria, ambapo Wajerumani walikuja kuanzisha Bukoba mwaka wa 1890.

Ihangiro inaweza kugawanywa vyema katika jimbo tambarare la ziwa na uwanda wa juu wa ndani uitwao Mugongo. Migogoro ya urithi mwishoni mwa karne ya kumi na saba iliwapa fursa wafalme wa Kyamutwara, Rugomora na Kahigi, kuliingilia jimbo la uwanda wa juu. Uhalali wa ungiliaji huu uliweza kutolewa na uhusiano wa kinasaba. Mwishoni mwa karne ya kumi na nane, Nyarubamba II

aliwasihi Baganda kumsaidia kupata tena jimbo la uwanda wa juu kutoka kwa mwanamfalme mwasi. Kuanzia hapo na kuendelea kukazuka kile kinachoweza kuitwa ubeberu wa Kiganda katika mwambao wote wa magharibi ya Ziwa Viktoria.

Kwa upande wa Buzinza, tunaingia jimbo jingine la kitamaduni na kimbari ambapo athari za Waha, Wasukuma, na hata za Watatoga, ambao ni Waniloti, ziliingiliana. Jimbo hili pia lilikuwa makazi makuu ya Barongo wafuachuma. Baada ya tawala zilizogubikwa na visakale vya Ntare Muganganzara na Kabambo wa kwanza, kulikuwa na namna ya uanzilishi wa pili chini ya Kabambo Kinwa. Katika karne ya kumi na nane *Mugabe* Kakaraza ilibidi azime mashambulizi ya Waha kutoka magharibi na ya Watatoga upande wa mashariki. Mwanawe, Mwihahabi, alikuwa mtawala wa mwisho wa Buzinza iliyounganishwa: vita vya urithi viliishia katika kujitenga kwa Rusubi chini ya Ntare Muhire, na majimbo yote ya mwambao kuwa chini ya Ruhinda Mugangakyaro mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa.

Historia ya Bukerebe imesheheni athari changamani. Kitamaduni, nchi hii inayoundwa na kisiwa na peninsula, ni sehemu ya Uzinza. Hata hivyo, kwenye karne ya kumi na tisa nasaba ya Wasilanga ilidai kuwa na asili ya Kihinda (au hata ya Bunyoro). Mwanzilishi wake, Katobaha, anadaiwa kutokea Ihangiro katika karne ya kumi na saba. Kunako karne ya kumi na nane, wafalme *(Bakama)* polepole walijichukulia madaraka juu ya koo za Basita na Bakula, lakini tishio la Watatoga liliwalazimisha kujenga makao yao makuu kisiwani. Biashara muhimu ya pembe za ndovu iliendelezwa sana na ufalme huu mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa.

*Madola katika milima ya magharibi*

Ingawa upande wa mashariki fukuto za falme ziliisababisha uchenguzi, upande wa magharibi, tunaona muungano kwa manufaa ya tawala mbili - Rwanda na Burundi - kila moja ikihesabu zaidi ya wakazi milioni moja, kufikia mwisho wa karne ya kumi na tisa.

Utemi mdogo wa Kinyarwanda uliozuka katika karne ya kumi na nne kusini mwa Ziwa Mohazi (katika Buganza) ulifanikiwa kujijenga imara kwenye Mto Nyabarongo, kwa kusaidiwa na utawala mrefu wa Chyirima Rugwe aliyetwaa nchi za Wabongera. Lakini migogoro ya hatari ya karne ya kumi na sita ilikuja athiri utulivu wa ufalme huu. Vamizi mbili za Bunyoro zilizomfanya Mfalme Kigeri Mukobanya na Mfalme Mibambwe Mutabazi wakimbilie magharibi ziliishia katika kukihamishia Nduga kitovu cha nguvu za kisiasa, na nchi ya awali kutekwa na Gisaka. Baada ya utawala wa kivita wa Yuhi Gahima, magomvi ya urithi kati ya wanawe yalitumiwa na Bashi, Bahavu na watu wa Bugara upande wa magharibi kufanya maasi. Mfalme aliuawa, ngoma ya nasaba ya Rwoga ilishikwa. Licha ya mapokeo yanayoelekea kuhudhurisha mfululizo wa utawala usiokatizwa tangu mwanzo, inawezekana sana kuwa Ruganzu Ndori alianzisha nasaba mpya ya ngoma ya Kalinga mwanzoni mwa karne ya kumi na saba. Aliiteka tena Nduga, na kutoka hapo yeye pamoja na warithi wake wakapanua ufalme hadi kufika Ziwa Kivu na Mto Kanyarn, wakitwaa tena

Bwanachyambwe upande wa mashariki sawia. Kuinukia kwa nasaba mpya katika Burundi kulisitisha upanuzi huu mwishoni mwa karne, lakini ulianza upya katika karne ya kumi na nane kutokana na maongozi ya kijeshi ya pekee yaliyoandaliwa na Chyirima Rujugira na Kigeri Ndabarasa. Burundi na Gisaka zililazimika kurudi nyuma, Ndorwa ikasambaratika, Mubari ilitekwa na makazi pwani mwa Ziwa Kivu yakapanuliwa hadi Kinyaga. Mwishoni mwa karne ya kumi na nane, Bugesera, mshirika wa zamani, iligawanywa kati ya Rwanda na Burundi. Upanuzi huu uliendelea katika karne ya kumi na tisa, hasa katika kaskazini-magharibi na kusini-mashariki, lakini mamlaka za kale za Wahutu na Watutsi zilidhibiti uhuru wao kwa muda mrefu chini ya ulinzi wa aina fulani wa Banyiginya.

Kuna taarifa finyu kuhusu historia ya Burundi katika kipindi hiki. Mwanzoni mwa karne ya kumi na sita, nasaba tawala ya kwanza iliyoanzishwa na Ntare Karemera yaelekea ilisimikwa katika milima ya kaskazini-magharibi mpakani mwa ufalme wenye nguvu wa Bugesera. Halafu, mwishoni mwa karne ya kumi na saba, Ntare Rushatsi au Rufuku alianzisha nasaba ya Baganwa katika Nkoma na kuunganisha eneo la kusini, katikati na kaskazini (na hivyo kuunganisha mamlaka za kiukoo za ufalme wa zamani). Ntare vilevile aliamiri vita dhidi ya Bugesera, ambayo mfalme wake, Nsoro Nyabarega, ilibidi akimbilie Rwanda. Ni katika utawala mrefu wa Ntare Rugamba tu, kwenye nusu ya kwanza ya karne ya kumi na tisa, ufalme ulipotanuka kuelekea magharibi kufikia Mto Rusizi na mashariki hadi kufikia bonde la Malagarazi.

Magharibi zaidi, kandokando ya Ziwa Kivu, Bashi kwa upande mmoja, na Bafuriku na Bahavu kwa upande mwingine, wanarejelea asili moja katika jimbo la Nyindu (katika Lwindi). Mapokezi pia yanathibitisha juu ya historia ndefu ya mahusiano kati ya falme hizi ndogo na Burundi na Rwanda.

## Madola, chumi na jamii

Historia hii ya siasa na vita haipaswi kupuuza suala la miguro ya watu, kubadilika kwa mandhari za nchi na uzalishaji wa mazao, na mabadiliko ya kiasasi na hata ya kiitikadi.

### *Kukua kwa uhusiano kati ya ufugaji na ukulima*

Sababu za kijiografia zilitenga, tangu mwanzo, maeneo mawili, kila moja na shughuli zake: ufugaji kwenye uwanda wa juu wa Kagera, na kilimo kwenye pwani ya Ziwa Viktoria na milima ya magharibi. Katika kipindi kinachozungumziwa hapa, hata hivyo, shughuli zote mbili ziliendelea kutekelezwa zaidi na zaidi kwa pamoja katika jimbo lote. Kwa hakika, hazijapata kukingama: uhusiano wa nafaka za kale, wimbi na mtama, na ufugaji wa ng'ombe, waonekana kuwa ni mtindo wa zamani sana, kwa upande wa uzalishaji na pia kwa upande wa ulaji (ugali na maziwa). Karagwe ya kale ni mashuhuri, kufuatana na mapokeo, si kwa ng'ombe tu, bali pia kwa kulima na kwa pombe yake ya mtama. Maelezo ya awali yanataja matumizi ya mbolea, ambayo

umuhimu wake katika kilimo shadidi chenye mavuno mawili kwa mwaka katika maeneo chepechepe zaidi, kwa bahati mbaya haukutiliwa maanani.

Lakini kuelekea magharibi hasa, mambo kama ukame na njaa huenda yalisababisha kuongezeka kwa athari za wafugaji. Maafa ya aina hii yaliongezeka katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na saba na nusu ya pili ya karne ya kumi na nane, na kuwalazimisha wakulima kutafuta msaada wa wafugaji, ambao, kupitia utaratibu wa kuhamisha mifugo, waliweza kuhakikisha uhai wa ng'ombe wao. Katika karne ya kumi na saba, kuhama kwa vitovu vya nguvu za kisiasa kutoka maeneo ya mito Kagera na Malagarazi kwenda kwenye nyanda za juu za misitu za Kiriba, mkabala na Maziwa ya Kivu na Tanganyika, hakuwezi kuelezeka kwa kuangalia tabaro au mabadiliko ya nasaba tu, bali kulisababishwa pia na kukua kwa mfumo wa ushuru ulioyapendelea makundi ya wafugaji.

Katika Burundi au Rwanda, hata hivyo, itaonekana kuwa wale walionufaika na utawala uliosimikwa miaka 300 iliyopita waliwakilisha sehemu tu ya wamiliki mifugo, Watutsi matajiri na kikundi cha watawala kilichohusiana na ufalme. Kwa yakini, walikuwa ni wale waliofanikiwa, kwa matumizi halisi au ya kiishara ya ng'ombe, kujipatia udhibiti wa kisiasa juu ya uzalishaji wa kilimo. Kilimo hakikupewa umuhimu mkubwa na wanaethnolojia, ingawa umuhimu wake unajidhihirisha katika miviga na hata katika itikadi ya ufalme. Kwa mfano, katika Burundi, sherehe ya *muhamuro* ya mwaka, ambamo mamlaka ya ufalme yanatambuliwa upya, iliadhimisha kupanda mtama, na kuamua tarehe bora ya kupandia, katika nchi yenye msimu mrefu wa mvua. Zaidi ya hayo, kuhusu mazao ya chakula, kuingizwa kwa mimea ya asili ya Amerika (viazi vitamu, mahindi, na maharage) kuliwapatia wakulima fursa mpya ya kupanuka, kutoa uwezekano wa kupata mavuno mawili kwa mwaka, na kuwapa protini ya mimea.

Uhusiano kati ya walimaji na wachungaji, basi, hauna tabia ya kijumla isiyobadilika kama ambavyo mawazo chapwa ya kijamii-kibiolojia yangetaka tuamini. Mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na kinchi yaliyotokea kati ya karne ya kumi na saba na karne ya kumi na tisa yalikuza mahusiano ya Wahima-Wairu au Watutsi-Wahutu kutoka katika uhusiano wa biashara ya ndani hadi kuwa uhusiano changamano wa kimsonge, ambao unyumbufu wake ulitegemea madola yanayohusika au wakati maalumu katika kipindi kinachohusika.

*Uimarishaji wa nguvu za kifalme katika karne za kumi na saba na kumi na nane*

Kabla ya ukoloni, kila dola lilikuwa na mfumo wa kodi uliobadilika kufuatana na hali ya mazingira, urari kati ya nguvu mbalimbali za kuzalisha mali, sulubu za koo na aina za asasi zilizokuwepo. Kila mahali mfalme alidhibiti moja kwa moja maeneo ya kilimo yaliyokuwa karibu na makazi yake na kuwatuma machifu sehemu baki. Machifu hao aghalabu walikuwa wanamfalme wakisaidiwa na wajumbe ambao kwa kawaida walitokana na nasaba maarufu sana za mahali hapo. Kodi ililipwa katika mabaraza haya ama kwa nguvukazi au kwa mali. Hii iliwarnhusu makabaila

watawala kueneza athari zao kwa kugawanya kodi, hasa kwa vile anasa ilikuwa adimu. Mamlaka ya ufalme yaliimarishwa, hasa kuanzia karne ya kumi na nane na kuendelea, kwa njia nne zifuatazo:

*Unyonyaji wa uteja* Mahusiano yaliyojulikana kama *ubugabire* au *ubuhake* yaliendelea kuondolewa mikononi mwa watu binafsi na kutumiwa kwa madhumuni ya kisiasa: ulinzi ulihakikishwa kwa familia kwa matarajio ya kuwajibika zaidi. Katika Rwanda utaratibu wa *buhake* ulitumiwa zaidi hasa kutiisha koo za Wahutu mashuhuri katika majimbo ya pembezoni yaliyotekwa na Banyiginya, hususani kwenye miaka ya mwisho ya karne ya kumi na nane. Ni wakati huu huu ambapo mfumo wa ardhi wa *gikingi* ulianzishwa; mfumo huu ulitoa haki za kipekee za malisho kwa mfugaji muhimu zaidi ya wote, pamoja na haki za utawala juu ya familia zilizoishi ndani ya maeneo yake. Mtandao huu wa fadhila, wakati mwingine ukiitwa ukabaila, uliambatana na ongezeko kubwa la idadi ya mifugo katika Rwanda kutokana na utekaji wa karne ya kumi na nane.

*Mipangilio ya kijeshi* Rwanda ilijenga, hasa tangu wakati wa utawala wa Chyirima Rujugira, mfumo wa majeshi ya kudumu ya urithi, yenye vijana wa nasaba fulani walioishi katika makambi yaliyopigwa kwenye mipaka yenye kutishiwa na maadui. Wanamgambo hawa pia walichunga mifugo iliyomilikiwa au kulindwa na mfalme. Katika karne ya kumi na tisa, kazi ya asasi hii ilikuwa zaidi ya kukusanya kodi chini ya utumishi wa machifu muhimu. Umuhimu wa majeshi ulitambuliwa pia katika falme nyingine mwishoni mwa kipindi hiki.

*Uwezekano wa biashara* Hadi tarehe za karibuni, biashara ya kiasasi na ya ndani ya kubadilishana bidhaa ilikuwa muhimu zaidi katika biashara ya kawaida kuliko kwenye biashara maalumu. Pamoja na hayo, mazao ya jimbo kama chumvi, bidhaa za chuma au vikuku vya ukindu yalikuwa ndiyo mali ya wachuuzi wa kwanza kabisa. Bidhaa kutoka pwani ya Bahari ya Hindi, zikiwemo shanga za kioo au kombe za mapambo, zaonekana kuwa zilienea katika jimbo hili tangu karne ya kumi na saba. Shaba inadhaniwa ilikwisha kuwepo tangu karne ya kumi na nane na kuendelea katika Burundi, Karagwe na Buganda. Lakini ni katika karne ya kumi na tisa tu ambapo wafalme wa Rusubi, Karagwe na Rwanda walijaribu kudhibiti biashara hii ya bidhaa za anasa, kama ilivyokwisha kufanywa katika Buganda.

*Uthibiti wa kiitikadi* Mabadiliko yaliyoingizwa katika jamii kutokana na zahama za kilimo, vita vya utekaji vya karne za kumi na saba na kumi na nane na kuhama kwa watu, yaliendeleza uvunjikaji wa nasaba. Ufanisi wa dini ya Kichwezi katika karne ya kumi na saba unaeleweka, kwani ulitoa aina fulani ya kimbilio katika mazingira ya ukosefu wa utulivu. Kwa kiasi kikubwa uhalali wa falme mpya ulikuwa na mizizi ndani ya mvuvumko huu wa dini, kama inavyoshuhudiwa na visasili na miviga. Wafundwaji waliweza pia kuanzisha shughuli za mapinduzi miongoni mwa watu au

kuzuia matendo ya kifalme.

Hatimaye falme zilidhamiria kuidhibiti dini hii yenye makali kuwili na kuitumia kwa manufaa yao. Katika Kiziba, madhehebu ya wafalme waliokufa yalishindana na nguvu ya mizimu ya Bachwezi; huko Kyamutwara, ufalme, tangu wakati wa Rugomora Mahe na kuendelea, ulitegemea madhehebu ya Mugasha; katika Rwanda "mfalme wa *Imandwa*" alitawazwa barazani tangu utawala wa Chyirima Rujugira. Wakati huohuo ufalme wa Rwanda ulisimamia ukusanyaji rasmi wa ushairi wa tondozi (kusifu wafalme) na masimulizi ya kihistoria, makusanyo ambayo yalisambazwa na majeshi.

Vyanzo simulizi vya Rwanda vinaakisi hali ya pekee ya ugatizaji wa kisiasa nchini. Katika madola mengine, matabaka mbalimbali ya jamii yalibakia na kiasi kikubwa cha uhuru hadi kwenye mkesha wa ukoloni.

## *Hitimisho*


Hadi kufikia mwisho wa karne ya kumi na nane mpangilio wa sasa wa kiethnografia na kiisimu katika ukanda wa Maziwa Makuu ulikwisha kamilika. Hajira kuu za watu takriban zilikwishafikia mwisho, na makundi ya mwisho ya kimbari kuundwa katika ukanda (Wakiga, Waiteso na Walango Omiro) yalikuwa yakijiainisha, mchakato uliokamilika karibu na mwaka 1830. Pia, tukiondoa maeneo machache, enzi ya uundaji madola ilifikia mwisho, huku Rwanda ikiibuka kama dola lenye nguvu kuliko yote katika ukanda huu. Katika eneo la kati, Bunyoro iliendelea kushuka hadi kujitenga kwa Toro na nchi ya Paluo mwaka 1830. Hadi mwanzo wa karne ya kumi na tisa, Buganda ilikwishaibuka kama dola kuu katika eneo hili. Kuanzia hapo, mambo ya muhimu kwa mwanahistoria yanabadilika kutoka ukuaji wa mamlaka kuu kuelekea kwenye juhudi za machifu kudhibiti mamlaka ya mfalme. Katika karne ya kumi na tisa, utitiri wa mada mpya ulikuja kutawala historia ya Maziwa Makuu.

# 27 *Bara ya Afrika Mashariki: jamii za Kenya na Tanzania, 1500-1800*

Kipindi cha kuanzia 1500 hadi 1800 kilishuhudia kuinukia kwa jamii mbalimbali na mifumo ya kijamii na kiuchumi ambayo bado inajidhihirisha sana katika bara za Kenya na Tanzania. Pengine uanuwai wa tajiriba ndiyo sifa kuu ya eneo hili katika kipindi hiki. Sehemu ya kati ya eneo hili ilikaliwa na Wamaasai, Wachagga, Wapare, Washambala, Wagogo na Wahehe. Katika ukingo wa mashariki kulikuwa na Wakikuyu, Wakamba, Wa-Miji-Kenda, Wazigula na Wazaramo. Kaskazini-mashariki kulikuwa na Waluyia, Wakalenjin, Waluo, Wagusii na Wakuria; na katika upande wa kusini-magharibi ya Tanzania kulikuwa na jamii kama zile za Wasukuma, Wanyilamba, Wanyamwezi, Wazinza na Wakimbu.

Watu hawa wote, tukiacha zile jamii za pwani, bado walikuwa wametengwa na mwambao. Hakuna ushahidi wowote wa kimaandishi wa sehemu hizi za bara kuingiliwa na Waarabu au Waswahili kabla ya 1700; wala hakuna vyombo au vifaa vyovyote muhimu kutoka nje vilivyowahi kupatikana katika bara yoyote iliyo kaskazini ya Zambezi ambavyo ni vya kipindi cha kabla ya 1600. Hata hivyo, kuanzia kwenye miaka ya katikati ya 1600 inawezekana kuanza kuona kuibuka kwa temi na miundo rasmi ya kisiasa, na pia mabadiliko yanayoelekea kwenye uzalishaji ulioandamana na ulipaji kodi. Simulizi za mapokeo zinayaelezea maendeleo haya kama mojawapo ya utamalaki na usimilisho uliofanywa na wahamiaji waliokuwa na nguvu zaidi kuliko jamii za kienyeji. Kwa upande mwingine tunaweza pia kusema kwamba jamii za wenyeji polepole ziliwadhibiti watu ambao hadi wakati huo walikuwa wanomadi au wale ambao hawakuwa na makazi ya kudumu na ambao walikuwa wamejipenyeza ndani mwao.

Historia yote ni mpito kutoka hatua moja kwenda hatua nyingine. Katika karne zilizofuatia 1500, mbari bainifu tunazozifahamu hii leo, pamoja na sifa zake za pekee za kiisimu na kiutamaduni, zilikuwa tayari zanaanza kujitokeza katika jamii za bara ya Kenya na Tanzania. Shughuli ya uchumi iliyokuwa kubwa kushinda nyingine zote hapana shaka ilikuwa ni kilimo. Katika sehemu zote za kilimo zilizokuwa na makazi ya kudumu, watu walijaribu sana kutafuta mbinu za kujiweka sawa na mazingira yao na kwa urazini. Katika sehemu nyingine mbinu za juu zaidi za kilimo, kama vile kilimo cha tungazi, kubadili mazao kwa msimu, kutumia mbolea ya mimea, kilimo




**27.1** *Mbari za Tanzania na Kenya (kutokana na ramani iliyochorwa na M. Kivuva, Chuo Kikuu cha Moi, Kenya, kwa mujibu wa W.R. Ochieng')*

mchanganyiko na kilimo cha kwenye vinamasi vilivyokaushwa zilitumika

Wakati wakazi wengi wa Afrika Mashariki walikuwa wakulima, Wamaasai, Wapokot na Waturkana walikuwa zaidi ni wachungaji ambao waliipeleka mifugo yao kwenye malisho kuvuka nyanda za Kenya ya kati na Tanzania. Hata hivyo, hakuna hata wakati mmoja ambapo wakulima na wachungaji walifikiria kufuatilia shughuli moja pekee ya uchumi. Wakulima, kama vile Waluo na Wagusii, pia walifuga makundi makubwa ya mifugo, na wakati huo huo wafugaji, kama vile Wasamburu na Wamaasai wa Arusha, pia walikuwa na kiasi fulani cha kilimo. Wabaraguyu, Wakalenjin na Wakamba walikuwa nusu wakulima na nusu wafugaji.

Wasanye, Waokiek, Wasandawe na Wahazapi walibakia kuwa wawindaji na wakusanyaji; lakini hata kati yao pia kulitokeza namna fulani ya ruwaza ya kujishughulisha na kiasi fulani cha mazao ya chakula. Kwa mfano Waokiek walibadilisha asali kwa bidhaa za kilimo, na wawindaji wa Kidorobi na Kiathi walijiingiza katika biashara ya masafa marefu ya pembe za ndovu. Katika sehemu kubwa ya karne ya kumi na saba na kumi na nane, wakulima na wafugaji waligombea mbuga na nyanda za juu zenye rutuba na zenye maji mengi. Wakati huohuo waliingilia maeneo ya wawindaji na wakusanyaji, hali ambayo ilipelekea kumezwa, kuuawa kwa wingi au kutengwa kwa kundi hilo la mwisho.

## *Mageuko ya kiuchumi*

Hadi kufikia 1500, shughuli mbili kuu zilizowashughulisha watu wa bara ya Kenya na Tanzania zilikuwa ni kilimo na ufugaji wa ng'ombe. Kutokana na hali hii, basi, njaa ikajitokeza kama balaa dhahiri. Balaa hilo lilitokana na kuchoka kwa ardhi na mvua ambazo hazikuweza kutegemewa sana na ambazo ziliathiri mazao na malisho. Hata zile sehemu zenye hali nzuri sana kitabia-nchi nazo ziliathirika na baa la njaa. Yawezekana migomba ilisitawi huko Usambara lakini hata hivyo mapokeo yanazungumzia kuwepo kwa njaa walau mara moja kila baada ya miaka kumi na mitano. Mvua zilipokosekana, watu walikimbilia msituni kutafuta chakula, au wakati mwingine walibadilisha ng'ombe wao kwa nafaka kutoka kwa makundi yaliyobahatika kupata chakula zaidi.

Hata hivyo mbinu ya kwanza ya kujihami dhidi ya njaa ilikuwa ni ufundi wa mkulima. Kuanzia 1500 kulikuwa na majaribio ya mara kwa mara ya mazao ambayo yaliletwa mapema na Wabantu na Waniloti. Katika maeneo ya misitu kulikokuwa na mvua nyingi kilianzishwa kilimo cha migomba na mimea ya viazi badala ya mawele, ulezi na mtama. Baada ya 1500, mazao kadhaa kutoka Amerika na Ulaya, kama vile mahindi, karanga, viazi vitamu na mihogo, yaliletwa na Wareno. Vyakula vingine anuwai ikiwa ni pamoja na aina mbalimbali za mbaazi, maharage na njugu, navyo vililimwa na bado vinalimwa hadi hii leo.

Mkulima wa Afrika Mashariki alijaribu kila zao lililopatikana na akajisadifisha na mazingira yake. Wagusii waliotoka kwenye mbuga zilizopakana na Ghuba ya Winam

walipohamia kwenye nyanda za juu za kusini-magharibi ya Kenya kwenye miaka ya katikati ya 1700, na mavuno yao kuanguka ghafla, walikumbwa na njaa ambayo iliipunguza kwa wingi idadi yao. Walilazimika kupunguza kilimo chao cha aina anuwai za mitama na mazao mengine ya nyanda za chini na kuongeza kilimo cha ulezi na mazao ya tunguu yaliyoweza kustawi katika mazingira yao mapya. Kufikia mwishoni mwa karne ya kumi na nane maeneo ya bara za Kenya na Tanzania yalikuwa na mifumo mbalimbali ya kilimo. Pamoja na hayo kulikuwa na tabia moja iliyojitokeza sana mara kwa mara katika maeneo haya, nayo ilikuwa uchomaji moto wa mapori ili kusafisha ardhi kwa ajili ya kilimo. Baada ya majira kadhaa, ardhi ilipochoka, mkulima alihamia sehemu nyingine ili kuruhusu ardhi ipate kurutubika tena. Inaelekea kwamba mifumo yote ya kilimo katika bara zote za Kenya na Tanzania ilitegemea zaidi nguvukazi ya kaya, iliyotumia vifaa na zana zile zile sahili, yaani mashoka, majembe, mapanga na vitimbo.

Ufugaji wa ng'ombe, kuku, kondoo na mbuzi uliendelea kuwa shughuli muhimu ya kiuchumi na kiutamaduni katika bara ya Afrika Mashariki. Mbolea ya wanyama ilitumika katika kilimo. Mifugo ikawa ndicho chanzo cha kupatia mavazi, silaha na vyombo vya nyumbani. Kati ya wafugaji, kama vile Wamaasai na Waturkana, mifugo ndiyo iliyotawala taratibu za kila siku za maisha pamoja na mahusiano ya kiukoo, kwani maendeleo na mafanikio ya familia yalipimwa kwa kuangalia familia ilikuwa na mifugo kiasi gani. Katika jamii nyingi ambazo msingi wake ulikuwa ni kilimo, kama zile za Wakikuyu na Wagusii, kuwa na ng'ombe ilikuwa ni ishara muhimu ya utajiri na hadhi. Kati ya Waturkana, Waluo, Wakalenjin na Wamaasai, kulikuwa na desturi ya kukopa na kukopesha, bila masharti, ng'ombe, na pia kuwatumia kwa ajili ya mahari. Kwa njia hii ng'ombe wa kila familia walisambaa sana kati ya marafiki na jamaa ambao mara nyingi walikaa mbalimbali sana, jambo ambalo liliwanufaisha watu binafsi na jamii yote kwa ujumla.

Mbali na utajiri uliotokana na ng'ombe, watu ambao kazi yao kubwa ilikuwa ni ufugaji walikuwa pia na maeneo makubwa sana ya ardhi. Makundi kama vile Waoromo, Wasomali na Wamaasai yalipanua shughuli zao za uchungaji wa mifugo katika maeneo makubwa sana ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, kutokana na hadhi yake katika jamii, utajiri wake, ukubwa wake wa ardhi na nguvu zake za kisiasa na kijeshi, maisha ya ufugaji yalikuwa ndiyo muhimu zaidi na wengi waliyaonea wivu.

Uwindaji ulikuwa shughuli ambayo ilikamilishana na kilimo na ufugaji, yenyewe ikiwa ni njia mojawapo ya kupatia chakula na vilevile ikiwa ni njia ya kuyalinda mazao yasiharibiwe na wanyama. Mapokeo simulizi, hasa yale ya Waluo, Washambala, Wapare na Wakuria, mara kwa mara huelezea miguro ya watu kwa kuihusisha na jinsi kumfuatilia mnyama kulivyowapeleka katika sehemu nyingine ambako waliamua kulowea. Kisa cha kuzua cha asili ya ufalme wa Shambala kinaelezea hadithi ya Mbegha, mwindaji wa Kinguu, aliyekuwa akiwaua nguruwe mwitu (ngiri) waliokuwa wakiharibu mazao na akawa anawagawia watu nyama bure. "Washambala, katika kumsifia na kumshukuru, wakampa wake na kumfanya kuwa

mfalme wa Usambara yote." Kwa hiyo uwindaji ulikuwa ni shughuli muhimu na iliyoheshimika sana ya kiuchumi.

Umuhimu unaotolewa na mapokeo kwa kilimo, ufugaji na uwindaji unagongana vikali na hali ya kutopewa umuhimu wowote shughuli za uvuvi, isipokuwa miongoni mwa wakazi wa maeneo ya ukingoni mwa maziwa Turkana, Viktoria (Nyanza), Baringo, Eyasi na pwani ya Bahari ya Hindi. Samaki wa aina kadhaa walinaswa kwa ndoana, migono na madema. Samaki wakavu waliuzwa, na bado wanaendelea kuuzwa, kwa watu waishio mbali na maeneo ya uvuvi.

Mapokeo ya watu wengi wa Afrika Mashariki yanaonyesha kwamba kulikuwa na ujuzi wa utengenezaji chuma wa tangu zama za kale. Wanaakiolojia na wanaisimu pia wamethibitisha kwamba mbinu za teknolojia ya chuma ziliingizwa katika Afrika Mashariki na wa-Nilo-Sahara na Wabantu, pengine karne sita kabla ya Enzi za Ukristo. Maeneo ya mwanzo kabisa ya Enzi ya Chuma yako katika sehemu zinazozunguka Ziwa Nyanza (Victoria). Maeneo haya yaliknwa na sifa ya knwa na matanuru marefu ya mcheduara na mtindo wa ufinyanzi uliojibainisha sana. Kwa kawaida kazi za utengenezaji chuma zilikuwa zikifanywa na makundi machache tu ya watu, ziliknwa na hadhi sana na wakati mwingine ziliandamana na utajiri. Mapokeo kadhaa ya Ugweno yanatuambia kwamba kuelekea mwanzoni mwa karne ya knmi na sita, baadhi ya familia zilijishughulisha na kazi za kuyeyusha na kufua chuma tu. Nasaba kuu iliyokuwa maarufu kwa utengenezaji chuma, Washana, waliwahi kutawala katika nchi hiyo. Baadaye walitolewa na Wasuya ambao walibadilisha kaida za mafundo zilizokuwepo wakati huo kuwa asasi ya kitaifa yenye mamlaka ya udhibiti yasiyo na ukomo. Huko Kenya magharibi, Wagusii wanadai kuwa walikuwa wakitengeneza chuma tangu karne ya kumi na sita. Miongoni mwa Waluo wa kaskazini mwa ghuba ya Winam, wafua chuma wakuu walikuwa ni Walowa wa Yimbo. Walitengeneza majembe, vyembe vya mishale, mapambo, mashoka, mikuki, visu na nyembe. Shughuli nyingine muhimu za kikanda zilikuwa ni uchimbaji chumvi na kazi za ufundi kama vile utengenezaji ngoma, ujenzi wa mitumbwi na ufinyanzi. Kijadi, shughuli hizi zilikuwa chini ya ukiritimba wa koo fulani fulani tu. Hata hivyo ufundi kama ususi wa vikapu na ujenzi wa nyumba, hazikuwa kazi za wataalamu fulani pekee, bali zilifanywa na yeyote aliyekuwa na nafasi ya kuzifanya.

Kwa ufupi, ni muhimu kusisitiza kwamba kati ya 1500 na 1800 uzalishaji wa chakula lilikuwa jambo muhimu kabisa katika kuendelea kuishi na kupanuka kwa jamii. Kadri sehemu kubwa ya Afrika Mashariki ilivyotumika kwa kilimo na uchungaji mifugo, na kadri uzalishaji ulivyopanda na kuvuka mpaka wa mahitaji ya lazima tu, ndivyo watu walivyoanza kutumia muda wao kwa shughuli nyingine zaidi ya zile za kujikimu tu. Iliwezekana sasa kuwaondoa watu wengine katika shughuli za uzalishaji wa chakula ili washughulikie mambo mengine kama vile biashara, vita, kazi za kiserikali, sanaa, dini, tiba au falsafa, na kuboresha teknolojia.

## *Biashara*

Hadi kufikia miaka ya mwisho mwisho ya 1700, jamii nyingi katika bara za Kenya na Tanzania zilikuwa zikiendelea bila kutegemea nguvu za nje. Zilijitegemea kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Biashara, ubadilishanaji wa bidhaa kwa manufaa ya wote, ni kaida ya kilimwengu inayopatikana hata katika jamii zilizo sahili kabisa. Haijawahi kutokea hata kidogo kukuta makundi yote na maeneo yote kupewa njia (za uchumi) na rasilimali zile zile. Hivyo ni lazima kupata mahitaji muhimu kutoka kwa majirani. Kwa hali hiyo, wafugaji na wakulima walibadilishana mazao.

Mengi yameandikwa kuhusu mahusiano ambayo yamekuwepo, kwa karne na karne, kati ya Afrika Mashariki na Mashariki ya Mbali, lakini ni muhimu kusisistiza kwamba mahusiano muhimu ya kibiashara katika Afrika Mashariki hayakujibana katika biashara na masoko ya nje tu, bali pia yalihusisha mahusiano muhimu ya kiuchumi kati ya kanda mbalimbali za ndani. Biashara ya ndani ya Kiafrika ilikuwa na madhumuni na misukumo tofauti na ile ya Waarabu au Wazungu. Kutokana na hali hiyo, biashara hiyo ilikuwa ya vipindi bila mpangilio wa uhakika. Ilikuwa pia ni mbinu ya kujilimbikizia mali kwa njia ya mifugo na chakula.

Hebu tuangalie mifano kadhaa ya biashara hii. Mapokeo ya nchi ya Kikuyu huzungumzia mahusiano ya kale ya kibiashara kati ya Wakikuyu na jirani zao Wakamba na Wamaasai. Uchumi wa Wakikuyu ulikuwa wa aina anuwai. Ingawa kimsingi walikuwa wakulima, baadhi ya makundi yao, kwa mfano Watetu na Wamathira wa Nyeri, walikuwa na kiasi fulani cha uchumi wa kifugaji wakiishi maisha karibu sawa na jirani zao, Wamaasai. Kinyume chake, Wakikuyu wa Athi walijishughulisha na uwindaji na utafutaji wa bidhaa za msituni kama vile nta ya nyuki na asali. Kwa hiyo Wakikuyu waliwapa Wamaasai chakula na bidhaa za viwandani, Wamaasai nao wakavinunua vitu hivyo kwa ng'ombe, maziwa, ngozi, ngozi zilizofuliwa, migolole na huduma za sihiri. Ukikuyu vilevile iliwapa Wakamba masoko bora kuliko nchi nyingine baada ya mwaka 1760. Wakamba walinunua kutoka kwa jamii za Wakikuyu za Murang'a na Nyeri mazao ya chakula kama maharage, viazi vikuu, mahindi na *ndulu* (aina ya mboga ya majani ambayo wao waliipenda sana). Wakamba walinunua vitu hivyo kwa ngozi na uki (aina ya pombe iliyochachuka sana). Wakati mwingine pia waliuza nguvukazi zao, hasa wakati wa kipindi cha mavuno, kwa kufanya kazi za uvunaji, na wakapewa mazao ya chakula yaliyolingana na kazi zao.

Magharibi zaidi, upande wa upwa wa mashariki wa Ziwa Nyanza (Viktoria), kulikuwa na mtandao mkubwa wa biashara ulioziunganisha jamii mbalimbali. Wafanyabiashara walioshirikiana sana walikuwa ni Wagusii na Wajaluo. Wagusii waliwauzia Wajaluo mazao ya kilimo na bidhaa za chuma kama mashoka, mikuki, nyembe, na vyembe vya mishale; waliwauzia pia mawe ya talki, na ngozi za chui na nyani. Nao Wajaluo wakawapa ng'ombe, chumvi ya ngombe, ngozi, samli, maziwa,

samakı, vyungu na sumu.

Kusini zaidi katika Tanzania mapokeo kutoka Unyamwezi magharibi na Uvinza yanatueleza juu ya makundi ya wahamiaji wa kabla ya 1800 kutoka kaskazini ambayo yalikuwa yakibadilisha mazao ya nafaka kwa vyungu vya wakazi wa maeneo hayo wa mwanzo. Miongoni mwa Wanyamwezi, bidhaa za msituni pia ziliuzwa kati ya kijiji na kijiji, na zilihitajika sana katika nchi za kaskazini ambako Wanyilamba, Wasumbwa na Wasukuma waliishi. Katika Unyakyusa wanawake wengi walifanya kazi ya ufinyanzi, lakini wale walioishi katika maeneo ya volkano walikosa udongo mzuri wa mfinyanzi; kwa hiyo wakawategemea wafinyanzi wabobezi, kwa mfano wanawake wa Kikisi wa upwa wa Ziwa Nyasa, ambao walibadilishana vyungu vyao na bidhaa nyingine katika vijiji vya Unyakyusa; au watu wa Ngaseni ambao waliuza mitungi mikubwa ya (kuhifadhia) pombe kwenye barabara iliyozunguka miteremko ya juu ya Mlima Kilimanjaro.

Labda bidhaa mbili muhimu kabisa za biashara ya mwanzo katika Tanzania ya kati zilikuwa chuma na chumvi. Eneo kuu ambako ufuaji chuma ulifanywa lilikuwa kaskazini, miongoni mwa Waha na Wazinza. Upungufu wa chuma uliichapua biashara hiyo. Kote Tanzania chuma kilitumika kwa kutengenezea vitu anuwai: visu, majembe, mashoka, mikuki, vyembe vya mishale ya kuwindia, kuvulia samaki na kupigania. Wafanyabiashara wengi kutoka kaskazini na kusini walisafiri kwenda Uha na Uzinza kununua bidhaa hizi za chuma ambazo waliziuza tena nyumbani kwao. Kaskazini-mashariki Wachagga na Wamaasai walipata bidhaa za chuma kutoka kwa wafua chuma wa Upare, na mwishoni mwishoni mwa miaka ya 1700 utemi wa Mamba ulikuwa ndio kituo kikuu cha kazi za chuma kwa sehemu kubwa ya mkoa wa Kilimanjaro. Huko kusini, wafuachuma wa Kifipa walibadilisha bidhaa zao kwa nguo zilizotengenezwa katika bonde la Rukwa, ambapo Wanyakyusa walibadilisha bidhaa zao za chakula kwa bidhaa zilizotokana na majoko ya Wakinga. Chuma ilikuwa bidhaa adimu na yenye thamani sana; matajiri tu ndio walioweza kununua majembe ya chuma. Majembe yaliyotumika Kilimanjaro mwishoni mwishoni mwa karne ya kumi na nane yalikuwa na upana wa sentimeta chache tu, na Wasandawe waliyatumia hadi yalipobakia visagalima.

Chumvi ilikuwa bidhaa muhimu sana kwa watu wailioishi kwa kula vyakula vya mboga mboga. Machimbo makubwa ya chumvi yalikuwa katika Ugogo na huko Ivuna, Kanyene, Ziwa Balangida, Ziwa Singida na Ziwa Eyasi; pia huko Bukune, Buha na Uvinza. Vijito muhimu kabisa vya chumvi vilikuwa katika Buha na Uviuza. Vile vya Uvinza yaelekea vilianza kugemwa chumvi tangu karne ya kumi na moja. Tasniya hii ya chumvi ya Uvinza baadaye ilitiwa mwega na kuanzishwa kwa utemi wa asili wa Uvinza mwaka 1800.

Biashara kati ya Miji-Kenda ya kusini-mashariki ya Kenya na kaskazini-mashariki ya Tanzania kusema kweli ilianza kukua kuanzia mwanzoni mwa karne ya kumi na nane. Hiki kilikuwa kipindi ambapo watu wengi wa Miji-Kenda, ambao hapo awali walikuwa wamejitenga katika vijiji vilivyojengewa uzio, walianza kujipanua kwa

kutoka nje ya maeneo yao. Baadaye, idadi yao ikiwa sasa imeongezeka sana, walianza kuhama kwa mara ya pili, wakiweka makazi yao katika maeneo ya chini, yasiyo na rutuba, ya nchi yao iliyojaa vilima, na ambako mara kwa mara walipambana na Waomoro na Wamaasai.

Watu wa Miji-Kenda walikuwa zaidi ni wakulima wa mtama, mpunga na matunda. Katika kipindi chote cha karne ya kumi na nane walikuwa marafiki wakubwa wa Wamazrui, wakiwa ndio wagavi wakubwa wa makazi ya pwani wa bidhaa kama pembe za ndovu, sandarusi, asali, nta, tumbaku, nafaka, vyakula vingine, na mbao kwa ajili ya kuundia majahazi. Nao watu wa Miji-Kenda, kutokana na bidhaa zao hizo, walipata chumvi, shanga, nguo, majembe ya chuma na bidhaa nyingine. Katika biashara iliyotokea baina ya pwani na bara, walipeleka misafara yao kaskazini, katika nchi za Waoromo na Waborana, na kaskazini-magharibi katika nchi za Wakamba na Wachagga. Lakini udhibiti wao wa biashara ya bara haukudumu muda mrefu na kufikia miaka ya katikati ya 1700 nafasi yao ikawa imechukuliwa na Wakamba.

Yawezekana kwamba biashara kuelekea mikoa ya bara ya Kenya na Tanzania, hadi kufikia kwenye miaka ya 1700 au kabla, ilikwisha kuwa ya masafa marefu; hata hivyo ni kuanzia mwaka 1800 tu ambapo bara ya Afrika Mashariki ilianza kujishughulisha na biashara za masafa marefu na hivyo basi kuhusishwa na uchumi wa nje.

## *Shughuli za kisiasa na kijamii*

Asasi na mashirika ya kijamii na kisiasa yalikuwa na nafasi katika kuleta umoja katika jamii na ulinzi wa mali na biashara. Kati ya 1500 na 1800, jamii katika bara ya Afrika ilikuwa bado haijapata sura kamili. Bado kulikuwa na uhamaji mkubwa wa ndani kwa ndani katika maeneo ambayo ama yalikuwa yamekaliwa kidogo tu hapa na pale au hayakuwa yamekaliwa kabisa, na wakati mwingine, uhamiaji huo ukawa unawakutanisha watu wa lugha au lahaja mbalimbali, na wenye namna tofauti za kisiasa na kiuchumi. Migongano ya ndani ilizidi kadri koo zilivyopanuka. Katika baadhi ya maeneo makundi au familia zilizohamia huko zilileta uongozi wao wa kisiasa juu ya wenyeji waliokuwepo. Katika meneo mengine wahamiaji walimezwa na wenyeji. Katika pande zote uhamaji wa ndani kwa ndani ulianzisha mchakato wa kuchanganyika kwa tamaduni na siasa ambao uliendelea hadi wakati wa ukoloni.

Kwa hiyo, kipindi kati ya 1500 na 1800 kilikuwa na sifa kuu ya kuelekea kwenye ugatishaji wa kisiasa na kutokea kwa makundi makubwa makubwa ya kijamii na kiisimu. Kutokana na hali hiyo kukajitokeza, katika bara ya Afrika ya Mashariki, jamii anuwai; lakini jamii mbili kubwa ambazo zilitofautiana sana ni zile za wafugaji na wakulima.

Wafugaji, kama walivyokuwa wawindaji, walitegemea sana chakula cha nyama. Waliishi maisha ya kutangatanga, wakisafiri masafa marefu kutafutia mifugo yao

malisho. Walifuata ruwaza ya uhamaji ambayo takribani ilikuwa ileile kulingana na majira ya mwaka. Wafugaji walilazimika kulinda mifugo yao dhidi ya mashambulizi kutoka nje, yawe ni ya wanyama au binadamu. Maisha ya namna hiyo yalihitaji uongozi wenye mpangilio makini.

Historia ya kisiasa katika bara ya Kenya na Tanzania kwa kiasi fulani ilihusiana na kukua kwa idadi ya watu ambako, kwa upande mmoja, kuliletwa na maisha ya kukaa mahali pamoja ya wakulima na kwa upande mwingine kuliletwa na mpangilio wa kinidhamu wa kisiasa-kijeshi uliotakikana katika maisha ya ufugaji. Urari ulielemea zaidi upande mmoja au mwingine kati ya hawa wakinzani wawili kutegemeana na mabadiliko katika mipangilio na ufungamano wa kijamii; na pia kwa kutegemea maendeleo ya tekuolojia. Hadi kufikia 1800 wafugaji wakawa wanaanza kupoteza nguvu za kiuchumi na kijeshi kwa kulinganishwa na wakulima, ambao kwa haraka walikuwa wakifanya asasi zao za kisiasa kutengenea zaidi. Hasa wafugaji wa Kimaasai waliporomoka sana kijeshi na kiuchumi katika kipindi chote cha karne ya kumi na nane kutokana na magonjwa ya ng'ombe, magonjwa ya mlipuko na vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Kufikia 1700, katika bara ya Kenya na Tanzania kulikuwa na aina mbili kuu za mipangilio ya kisiasa-kijamii. Kwa upande mmoja kulikuwa na jamii za watu kama Wakikuyu, Miji-Kenda, Wakamba na Wamaasai, ambazo ziliishi katika makazi huru yaliyosambaa huku na huko na ambayo hayakuwa na aina yoyote ya utaratibu wa urasimu unganifu wa kijadi. Hata hivyo, ukosefu wa ugatishaji haukuwa na maana kwamba kulikuwa na mparaganyiko wa mambo au hapakuwa na mshikamano wa kisiasa na kijamii. Jamii hizi zilizogatuliwa zilikuwa na mabaraza ya familia, vijiji, na wilaya ambayo wajumbe wake walikuwa wazee. Watu wa kila familia, ukoo na wilaya waliunganishwa na taratibu za kimahusiano ambazo ziliamua na kutawala matendo ya kila mtu na kuainisha wajibati na haki za kila mtu.

Zilikuwepo pia jamii zilizogatishwa (au zilizokuwa zikiunda mfumo gati) kama vile Washambala, Wapare, Wasukuma Wanyamwezi na Wanga, ambao watemi wao walisimamia tawala chipukizi ambazo ziliweka kiunzi cha kijamii-kisiasa. Hadi kufikia mwisho wa karne ya kumi na nane baadhi ya makundi haya, kama Washambala na Wapare, yalikuwa yakitawaliwa na wafalme wa kiimla wenye nguvu au watemi wakuu.

Hebu tuangalie baadhi ya mifano ya maendeleo haya. Miongoni mwa Wapare, hatua ya kwanza ya maendeleo ya kisiasa ilifikiwa wakati kila ukoo ulipojiimarisha katika eneo lake na kumkubali kiongozi mmoja wa kimiviga na ambaye vizazi vyake viliweza kumrithi. Hii ina maana kwamba mahitaji ya kidini ya jamii hizi yalikuwa ndiyo kiini cha mabadiliko yao ya kisiasa. Baada ya kutamakani mahali fulani, kila kundi lilianzisha mahala pake patakatifu (*mpungi*) ambapo paliwaunganisha na wahenga wao na ambapo katika vipindi fulani maalumu watu wote walikusanyika kufanya ibada. Kadri idadi ya watu ilivyoongezeka ikawa lazima kuwaleta pamoja watu wa koo mbalimbali. Kipindi hiki cha kuanza kwa umoja wa jamii

kimevungwavungwa katika visasili, lakini kwa mujibu wa Isaria Kimambo, takriban "vizazi kumi na sita vilivyopita," koo nyingi za Kigweno zilimtambua mfuachuma mmoja wa Kishana kama mtemi wao. Baadaye Washana walipinduliwa na Wasuya ambao walianzisha dola unganifu. Mapinduzi hayo yalifanywa na Angovi, lakini mwanae wa kiume, Mranga, ndiye aliyelijenga na kuliimarisha dola la Ugweno; akazibadilisha mila na desturi za jando na unyago, ambazo hadi wakati huo zilikuwa za kiukoo, kuwa asasi changamani ya dola yenye mamlaka na nguvu kubwa. Katika kilele cha utukufu wake, dola la Ugweno lilikuwa na mtawala wake mkuu kabisa aliyejulikana kama *mangi mrwe* (mangi mkuu) ambaye alisaidiwa na baraza la mawaziri na *wamangi* (machifu wa wilaya).

Eneo jingine katika Tanzania ambako asasi za kitemi zilikuwa na nguvu ilipofikia 1600 lilikuwa ni Bukoba, ambako nasaba-tawala anuwai zilikuwa zimejitokeza kati ya jamii za wakulima. Mfumo wao wa kisiasa, ambao ulikuwa na utawala wa kati zaidi kuliko ilivyokuwa katika madola mengine ya Tanzania, ulihusisha umiliki wa ardhi na ng'ombe kwa namna ambayo mfumo wa ushuru uliokuwepo ulikuwa wa kinyonyaji zaidi. Madola haya yalikuwa katika ukanda wa Maziwa Makuu. Kusini zaidi tawala nyingi za kitemi zilijitokeza, zikiwa zinafananafanana kwa namna nyingi. Kila moja ilikuwa na kundi dogo la vijiji na maeneo jirani chini ya mtemi mmoja ambaye alichaguliwa na wanavijiji kutoka katika nasaba-tawala. Yeye ndiye aliyekuwa na regalia au nembo za utawala, kama vile mikuki mitakatifu. Alikuwa ndiye mlinzi wa moto wa kifalme ambao yasemwa ulitumika kuwashia moto yote katika utemi.

Andrew Roberts anatuambia kwamba temi nyingi za Unyamwezini pengine hazikutokana na mchakato mahsusi wa uhamaji au usambaaji, bali zilitokana na mazingira ya Unyamwezi yenyewe. "Tangu mapema sana," anasema, "baadhi ya watu waliheshimiwa kama waleta mvua na waganga, kama waanzilishi wa kufyeka misitu na kama wapatanishi." Utemi wa Unyamwezi ulitokana na chimbuko hili. Lakini tofauti na ilivyokuwa katika Upare ambako maendeleo haya yalielekea katika ugatishaji, temi ndogo ndogo za Unyamwezi zilikuwa zikiongezeka kiidadi. Ni katika karne ya kumi na tisa tu ambapo tunaona kunatokea ugatishaji wa haraka katika Unyamwezi kutokana na kupanuka kwa biashara na kutokea kwa wafanya biashara katili na waongozaji weledi wa umma kama Mirambo.

Miongoni mwa Wafipa wa kusini-magharibi ya Tanzania, visasili vya kale kabisa vinavyoelezea asili vinahusishwa na chimbuko la ufalme wa Ufipa *(Milansi)*. Kulingana na fasili moja iliyoandikwa na Roy Willis, "mtu wa kwanza duniani, ambaye aliitwa Ntatakwa, alidondoka kutoka mbinguni dunia ilipoanza, na akaanzisha nasaba tawala ya watemi wa Milansi." Watu wa kwanza kutamakani Ufipa walikuwa wakulima ambao waliishi katika vijiji vilivyokuwa vimejaa sana watu; hii ikawashawishi kuweka utaratibu wa ulinzi wa pamoja na kujenga ngome. Yaelekea watu wa ukoo-tawala walipata utawala wao kutokana na ufundi wao wa kufua chuma.

Baadaye, katika karne ya kumi na nane, mfumo wa siasa katika Ufipa ukabadilika

kutokana na uvamizi uliofanywa na wafugaji kutoka kaskazini ambao walianzisha kanuni za siasa ambazo hazikuwa tena zimekitwa kwenye mahusiano ya mfuatano wa mtemi-baba na mtemi-mwana, bali zikawa sasa zimekitwa kwenye uhusiano wa kibinafsi wa utii uliokuwepo baina ya mtawala na wafuasi wake. Wafuasi hao waliteuliwa na mtemi kutawala maeneo ya pembezoni, lakini hawakuwa na uhusiano wowote wa damu naye. Pengine paliwahi kutokea mapinduzi yaliyouondoa utawala wa Milansi wa nasaba-tawala na kuiweka madarakani nasaba-tawala ya Twa. Hata hivyo utawala wa Twa haukuwa na amani, kwani Ufipa ilivamiwa tena kuelekea mwishoni mwa karne ya kumi na nane. Safari hii walivamiwa na Wanyiha ambao walichoma vijiji vya Milansi. Kufikia 1800 vita vya wenyewe kwa wenyewe kati ya wapinzani wawili waliokuwa wakigombea kiti cha enzi cha Twa vilikuwa bado vinaendelea.

Idadi kubwa ya temi za viwango tofauti vya ukubwa na ugatishaji zilitokea Tanzania kati ya karne za kumi na sita na kumi na nane, kutokana na mahitaji ya kibinadamu, kisiasa na kiuchumi. Zilipewa sura mbalimbali na mazingira ya kimaumbile na kibinadamu. Ugatishaji na upanuzi wa uchumi ndiyo yaliyokuwa malengo ya madola mengi ya Tanzania, lakini mchakato wa kujenga utaifa mara nyingi ulionekana kuwa mgumu.

Huko magharibi ya Kenya yaelekea kwamba Wajaluo walijenga umoja wao kutokana na udugu, imani za kidini za mababu zao, na uongozi wa kurithi. Walipofika Nyanza walijenga mifumo ya kijamii-kisiasa ambayo ilikuwa imegatishwa na yenye matabaka zaidi kuliko ilivyokuwa katika jamii zao za awali. Ingawa koo na nasaba za Kijaluo zilikuwa sawa kwa namna nyingi, kuwepo kwa makundi ya watemi, viongozi wa dini na watu wa kawaida kuliashiria namna fulani ya kusigana katika usawa, hali ambayo ni vigumu kuipata katika jamii za Kenya.

Mchanganuo bora wa namna mfumo wa Kijaluo wa kijamii-kiuchumi ulivyofanya kazi katika kipindi hiki pengine ni ule uliofanywa na Petèr C. Oloo Aringo. Yeye anakubaliana na B. A. Ogot kwamba katika kiwango chake cha juu kabisa cha utaratibu wa kisiasa Wajaluo walikuwa wamegawika katika *ogendini* (makundi madogo ya mbari) kumi na tatu za ukubwa tofauti tofauti. Uanachama wa *ogenda* ulipatikana kupitia *gweng',* kundi la kisiasa na kieneo ambalo kwa kiasi fulani lilijitegemea. Kimsingi eneo la *gweng'* lilikuwa na wanachama kutoka ukoo ule ule, lakini pia mara nyingi sehemu ya eneo hilo liliazimwa na *jodak* (koo za nje).

Mkusanyiko mkuu kabisa wa kisiasa katika *gweng'* ulikuwa ni lile baraza la wazee. Baraza hilo la *gweng'* ndilo lililokuwa mlinzi mkuu wa eneo la ukoo. Liliendesha shughuli zote za miviga na ndilo lililoamua iwapo ilikuwa lazima ukoo uingie vitani au ufanye suluhu na *gweng'* nyingine. Maamuzi yao yalikuwa na nguvu ya sheria kwa raia wote. Wale ambao walikiuka taratibu zao au kukaidi maamuzi yao wangeweza kulaaniwa.

Juu ya *gweng'* kulikuwa na baraza la *oganda,* ambalo lilijadili mambo muhimu na makubwa ya siasa, sheria na uchumi, kama vile mauaji, wizi wa ng'ombe, kugombea

mipaka, njaa, magonjwa ya mlipuko, uvamizi, ulinzi, biashara na magomvi baina ya ukoo na ukoo au *gweng'* na *gweng'*.

Wakalenjin, ambao wameishi katika nyanda za juu za magharibi za Kenya kwa karne nyingi, walikuwa ni jamii iliyounganifuliwa kabisa kiutawala. Mamlaka yalihodhiwa na wazee na watu wenye utaalamu maalumu. Umbuji, uwezo wa kutoa mawazo muafaka katika mabaraza, na ujuzi katika mambo yaliyotokea nyuma na desturi za jamii zilikuwa ni sifa muhimu sana zilizotakikana kwa kiongozi wa siasa. Lakini zaidi ya yote mwanamume alipaswa kujidhihirisha kuwa yu mtu mwenye ndoa ya furaha na sifa njema katika jamii. Kati ya Wanandi, ambao ni tawi la Wakalenjin, kuna ushahidi unaoashiria kwamba kati ya karne ya kumi na nane na kumi na tisa mwelekeo mpya katika uongozi wa jamii ulianzishwa kwa kumweka kiongozi wa kiroho aliyejulikana kama *orkoiyot*. H. A. Mwanzi anasema kwamba ingawa mfumo wa kijamii-kisiasa wa jamii ya Wanandi ulibakia ule ule kwa kiasi kikubwa, mabaraza ya ukoo na ujirani yakiendelea na wajibu wao, hadi kufikia mwishoni mwa karne ya kumi na tisa *Orkoiyot* alikwisha wageuza Wanandi kuwa jamii iliyotawaliwa na viongozi wa kidini, na yeye mwenyewe akiwa ndiye mtawala mkuu.

Baada ya muda *Orkoiyot* akawa anadai sehemu ya ngawira iliyotekwa vitani, na akashinikiza mamlaka yake juu ya mabaraza mbalimbali kwa kuweka wawakilishi wake binafsi kuwa wajumbe wa kila baraza. Kutokana na hali hiyo likawa sasa limeanzishwa tabaka maalumu la maofisa, kati ya Wanandi, ambalo lilikuwa kiungo cha mawasiliano kati ya mabaraza mbalimbali na *Orkoiyot*. Maofisa hawa waliandamana na viongozi wa vita kwenda kwa *Orkoiyot* kuomba kibali chake ili kutekeleza mpango wa kuvamia sehemu fulani. Viongozi hao pia walikuwa wapelelezi wa siri wa *Orkoiyot*. Taratibu hizi polepole ziliigatisha jamii ya Wanandi katika nusu ya pili ya karne ya kumi na tisa.

## *Hitimisho*

Hadi kufikia mwaka 1800 idadi kubwa sana ya jamii za Waniloti, Wakushi na Wabantu zilikuwa zimetapakaa kote nchini Kenya na Tanzania. Ni katika maeneo ya Maziwa Makuu tu katika Afrika Mashariki ambako kulikwishajengeka dola na falme kubwa kubwa. Katika bara za Kenya na Tanzania umoja wa kawaida wa kijamii-kisiasa ulikuwa ni wa maeneo madogo madogo na uliokitwa katika utaratibu wa kiukoo. Wengi wa Wabantu walikuwa wakulima, ingawa pia pale ambapo iliwezekana walifuga mifugo yao wenyewe. Wafugaji kama Waturkana, Waoromo na Wamaasai waliishi katika jamii zenye ushari zaidi na kumiliki maeneo makubwa ya ardhi baina ya maeneo ya kilimo ya Wabantu. Pwani kulikuwa na miji-dola ya Kiswahili iliyotawaliwa na Waarabu wakazi wachache. Watu walioishi katika miji hii ya pwani walikuwa wa mchanganyiko, lugha yao kubwa ikiwa ni Kiswahili na sulubu za maisha yao zikiwa zatofautiana sana na zile za wakazi wa bara.

Mwisho wa karne ya kumi na nane ulikuwa mwisho wa maendeleo huru ya Afrika Mashariki. Mara tu baada ya 1800, watu huru wa Kenya na Tanzania wakakabiliwa

na uvamizi wa Waarabu na Wazungu. Sehemu kubwa ya ustaarabu wao wa kimapokeo ikawa ama imeathirika vibaya sana au ikazamishwa katika lindi la ghasia na fujo.


Wakati huu Afrika Mashariki haikuwa katika hali nzuri ya kuweza kuhimili nguvu za uvamizi huu uliotoka nje. Katika uzalishaji, Afrika kwa ujumla ilikuwa imebaki nyuma ya uwezo mkubwa sana wa sehemu nyingine za ulimwengu. Wakati ambapo baada ya mwaka 1500 Ulaya iliingia katika enzi kuu ya uvumbuzi wa kimakanika na kisayansi na ya maendeleo, bara la Afrika liliendeleza ustaarabu wake aste aste lakini bila kutetereka. Ustaarabu huu wa Enzi ya Chuma ulikuwa na mafanikio makubwa. Kulikuwa na maendeleo makubwa na ubunifu katika fani za maisha ya jamii, kuanzishwa kwa mazao mapya, kuenea kwa stadi za kazi za chuma, kukua kwa biashara na, zaidi ya yote, mbinu za kujitawala wenyewe na kulinda amani. Hapana shaka haya yalikuwa mafanikio muhimu sana, lakini hayakuweza kulingana na nguvu iliyokuwa ikiongezeka ya mataifa makubwa ya viwanda ya huko Ulaya. Kufikia mwaka 1800 uwezo wa kiufundi wa Wazungu ukawa umezidi sana ule wa Waafrika, na ilipofika mwaka 1900 pengo likawa ni kubwa sana. Kukosekana huku kwa urari ndiko kwa kiwango kikubwa kumekuwa sababu ya zahama iliyoanza kujitokeza kwenye miaka ya 1800.

# 28 Bukini (Madagascar) na visiwa vya bahari ya Hindi

## *Bukini*

Umbo la Bukini ya sasa limefinyangwa katika karne ya 19 wakati Wamerina wa bara hili walipoanzisha utawala wao wa kisiasa, na hivyo kuwa ni Wamalagasi pekee waliojulikana mbele ya macho ya watu wa nje. Hata hivyo, zaidi ya athari za matukio ya hivi karibuni, kuna historia tofauti na ndefu ambamo kipindi cha kati ya 1500 na 1800 kinajitokeza kwa namna ya pekee katika historia ya jumla ya Bukini. Upo ushahidi wa kutosha kuonyesha kwamba wenyeji wa Bukini waliungana katika karne hizi tatu kuunda vikundi vya kijamii, kidini, kiutamaduni na kisiasa ambavyo ndivyo vinavyounda watu wa leo wa Bukini: Waantakara, Waantandroy, Waantambahoaka, Waantanosy, Waantemoro, Waantesaka, Waantefasy, Wabara, Wabetsimisaraka, Wabetsileo, Wabezanozano, Wamerina, Wamahafaly, Wasakalava, Wasihanaka, Watanala na Watsimihety.

Ilipofikia katikati ya karne ya 16, ujio wa wahamiaji katika nchi hiyo ulisita, lakini wakazi kadhaa wa Bukini tayari walishakuwa na mahusiano na Wazungu, hasa Wareno; na angalau ukoo mmojawapo kati ya koo mashuhuri, *Wamaroserana,* ulikwisha anza kujijenga. Mwanzoni mwa karne ya 17, Bukini ilikuwa ni mkusanyiko wa falme ndogondogo ambazo kwa kiasi kikubwa zilijitegemea. Kabla ya kufikia mwishoni mwa karne, sehemu kubwa ya Bukini ya Magharibi iliungana chini ya himaya ya Sakalava, na falme kadhaa zilizuka katika sehemu za nyanda za juu. Katika karne hiyohiyo, mahusiano na Wazungu yalipanuka na kuongezeka zaidi, jinsi Waholanzi, Waingereza na makampuni ya Wafaransa huko Mashariki mwa India walivyozidi kuvutiwa na kisiwa hiki kikubwa cha Afrika. Biashara ya watumwa, ambayo hadi wakati huo ilikuwa ikipeleka watumwa Afrika ya Mashariki na Arabia, ilibadilisha mwelekeo na kuelekezwa kwenye Rasi (ya Afrika Kusini), Maskarene na Dunia Mpya, wakipakiwa kutokea maeneo kadhaa ya pwani ndefu ya Bukini. Silaha za moto zilianza kuenea na matokeo yake kuonekana kwenye ulingo wa siasa. Himaya ya Sakalava, na hasa ufalme wa Iboina, uliokuwa sehemu ya kaskazini ya himaya hiyo, ilifikia kilele chake katika karne ya 18, ilihali sehemu kubwa ya pwani ya




**28.1** *Mbari za Bukini* Chanzo: *Ramani ya Bukini kutoka kitabu cha* Falme za Kale za Bukini, 1500-1700, *iliyochorwa na Raymond K. Kent (Holt. Rinchart and Winston. Inc., 1970). Ramani imepatikana kwa ruhusa ya mchapishaji.*

mashariki iliungana kwa mara ya kwanza kuunda shirikisho la Betsimisaraka. Kabla ya kufikia mwishoni mwa karne, Wasakalava wa kaskazini na Wabetsimisaraka waliona nguvu zao zikipungua kwa kasi kubwa. Kinyume chake, Merina, iliyokuwa dhaifu na imegawanyika, ilifanikiwa kuongeza uzalishaji wa chakula chake, na idadi ya watu wake, na hivyo kuibuka upya kisiasa na kuwapatia Wamerina msingi imara wa upanuzi wa baadaye.

## Wageni na Miungano

Kabla ya karne ya 19 Waantemoro walikuwa tayari mashuhuri kama kundi pekee lililoweza kuandika kwa Kimalagasi (kwa kutumia hati za Kiarabu) na pia kutokana na uwezo wao maalumu katika uwanja wa sihiri na dini. Hakuna makubaliano kamili kuhusu ni lini na wapi walikofikia wahenga wa kwanza wa Waantemoro huko Bukini, wapi walikotokea, kiwango chao cha usilimishwaji au hata athari zao katika kisiwa hicho. Gustave Julien ni mwanazuoni wa kwanza kupendekeza kuwa chanzo chao kilikuwa ni Afrika ya Mashariki, hoja iliyoungwa mkono katika muongo uliopita. Jambo moja halina ubishi hata kidogo: Waantemoro walifikia kwenye ukingo wa mto Matitana huko kusini-mashariki, na ilikuwa tu baada ya kuchanganyika na *Watompon-tany* (mabwana wa ardhi, wenyeji asili wa kisiwani humo) ndipo walipounda jamii na dola. Hata hivyo inawezekana kuupa tarehe yenye uhakika kwa kiasi fulani uhamiaji wa watu hao kwenye ukingo wa Mto Matitana kutokana na ripoti za Wareno watatu, manahodha wa meli, waliotembelea eneo hilo kati ya 1507 na 1514. Ni mmoja tu kati yao ambaye alikuwa kwenye bonde la Matitana mwaka 1514 anayezungumza kuhusu "mji uliokaliwa na Wamoori (machotara wa Kiberiberi na Kiarabu)." Kwa vile wahenga wa Waantemoro ndio pekee wenye sifa ya kuitwa "Wamoori," basi koloni la Matitana lazima lilianza kati ya 1509 na 1513.

Mapokeo ya kimaandishi ya Waantemoro yanarekodi kukutana kwa Waantemoro na wale waliokalia pwani ya kusini-mashariki kabla ya kuwasili kwao. Mapokeo hayo yanatueleza kuhusu migongano ya mawazo kati ya wageni hawa na dhana zao za unasaba wa kuumeni na dhana za unasaba wa kuukeni za watu hawa wa asili, na yaelezea migogoro mingi iliyozuka miongoni mwa wageni hawa. Waantemoro walijiunga kwenye koo kubwa nne za kifalme na koo nne za kikasisi. Historia yao ya ndani ya hadi 1800 inaweza kuangaliwa kama mfululizo wa migogoro kati ya koo za kifalme za Waanteoni, Waantemahazo, Waanteisambo na Wazafikasinambo. *Andrianoni*, au mtawala mkuu wa Waantemoro wote, aliweza kutoka kwenye ukoo wowote kati ya zile koo nne. Koo za kikasisi ziliwania madaraka ya kuongoza shughuli za kidini na za kitamaduni. Kwa mfano Watsimeto, Wazafimbolazi, Waanakara na Waanterotri walitaka kuwa walinzi wa miswada *(sorabe)* mitakatifu ya Waantemoro, kuwa makuhani wakuu kwenye utawala, au kuwa karibu sana na ukoo wa Andrianoni. Mgawanyo huu ulififia katika karne ya 19 wakati koo za kikasisi za Waankara zilipohodhi mamlaka ya kidini na yale ya kisiasa.

Wakati Waantemoro walipojenga pwani mashariki ya Bukini, mbali na vikundi

kadhaa vya *Watompon-tany* vilivyokuwepo, walizikuta pia jumuiya nyingine zilizokuwepo pale kabla yao, kama vile Wazafindraminia, madhuria wa Raminia. Inakubalika kwa kawaida kwamba Raminia na wenzake waliwasili Bukini angalau kabla ya karne ya 15, lakini hakuna makubaliano kuhusu asili yao. Popote pale walipotokea, ikumbukwe kuwa Afrika ya Mashariki ndio iliyokuwa bandari muhimu ya njiani kuelekea Bukini.

Wakati Waantemoro walipofika, kwa jumla Wazafindraminia walikuwa na nafasi ya upendeleo miongoni mwa *Watompon-tany*; desturi *(sombili)* kwa wakati huo iliwaruhusu madhuria wa Warnminia peke yao kuchinja wanyama wafugwao. Wahenga wa Waantemoro walitafuta kuoana na wanawake wa Kizafindraminia na kulitokea hata ushindani miongoni mwao. Mwishowe, migogoro ilibakia kati ya vikundi viwili vya hawa wageni vilivyokuja kwa nyakati tofauti. Hali hii ilisababisha wasiwasi ambao ulielezewa katika simulizi za *Watompon-tany* kama pambano la "majitu" mawili. *Kilele cha* mgogoro huu wa jumla kilifikiwa kwa wakati mmoja na kuibuka kwa ukoo wa kifalme wa Wazafikasimambo kama watawala wapya wenye nguvu katika ukanda huo mnamo mwaka 1550. Shajara za Waantemoro hujaribu kwa taabu kuonyesha kwamba Wazafikasimambo walitokana na Waanteoni, ili kuwapatia asili ya kifalme ya palepale. Hata hivyo imefahamika kutoka chanzo cha kujitegemea cha miaka ya kati ya 1600 kwamba Wazafikasimambo walikuwa wahamiaji wa mwisho kutoka ng'ambo kuselelea kwenye ukingo wa mto Matitana, na kwamba jina lao lilitokana na mke wa *Kitompon-tany*. Walichukuliwa kama *ombiasa* (makasisi) na waandishi kutoka Maka waliotumwa ili kuwafundisha wenyeji wa huko. Kuanzia 1560 na kuendelea, Wazafikasimambo waliathiri mwelekeo wa jamii ya Waantemoro kwa namna ya kipekee. Walichukua kutoka kwa Wazafindraminia ukiritimba wa miviga ya *sombili* na kuutumia kama zana ya kiuchumi na kisiasa. Walipunguza uhuru wa wananchi wa kawaida na kuifanya dini kuwa kiini cha maisha ya kisiasa. Pia walisuluhisha migogoro kati ya Waantemoro na Wazafindraminia kwa kuwaua madhuria wa kiume na Waraminia kwa wingi iwezekanavyo na kuwafungia ndani wanawake na watoto wao. Inaweza kusemwa kwamba Wazafikasimambo waliunda ufalme wa kwanza wenye nguvu wa Waantemoro huko Matitana na kuukabidhi kwa Waandrianoni wawili wenye uwezo, yaani Rubesirana (t.1580-1615) na Andriapanolaha (t.1630-1660).

Vurugu zilizoikumba nchi ya Antemoro zilikuwa na athari hata kuvuka mipaka yake. Kwa mfano, zilisababisha tabia ya kuhama, jambo ambalo lilikuwa la kudumu katika jamii hiyo. Jinsi koo za kikasisi zilivyozidi kutoa wataalamu wengi kuliko walioweza kutumika katika jamii za ufalme wa Antemoro, ilitokea kuwa jambo la kawaida kwa *waombiasa* kuenea miongoni mwa jumuiya nyingine na kutoa ujuzi wao kwa wale waliouhitaji. Wakati huo huo walitenda kazi zao kwa mwelekeo wa kuleta mabadiliko ya kisiasa, yaani mpito kutoka temi ndogondogo zilizokaa mbalimbali na zenye kujali mambo yao tu na kuunda muungano mpana zaidi wa kisiasa. Misukosuko ya mara kwa mara kwenye ukingo wa Matitana pia ilisababisha kukimbia

kwa wajumbe kadha wa kadha wa tabaka la kifalme, na uuaji wa kikatili wa Wazafindraminia uliofanywa na Wazafikasimambo nao pia uliwafanya watu wengi kuhama kwa hiari kuelekea bara ya Bukini.

Kwa mujibu wa Etienne Flacourt, Wazafindraminia waliselelea miongoni mwa Waantanosy mwanzoni mwa karne ya 16, lakini hawakufanikiwa kuwalazimishia mamlaka yao. Waliingiza desturi ya *sombili* kwenye eneo hilo, wakajenga vibanda bora kabisa vya mbao, na wakajilimbikizia ng'ombe, ambao walikuwa chanzo chao kikuu cha utajiri. Aidha, walikuwa na hisia za udugu na utashi wa madaraka. Hivyo walijipatia nafasi ya upendeleo katika nchi za Waantanosy. Lakini uchu wao wa kupata mali, migogoro ya ndani na kushindwa kwao kupata ishara za kuwaunganisha Waantanosy wote, vilizuia kuanzishwa kwa dola moja lenye kutawaliwa na wafalme wa Kizafindramania. Badala yake, jamii mbili sambamba zilianzishwa, huku Wazandraminia wakiiga mfumo wa utawalamsonge wa *kitompon-tany*. Wafaransa walipoanzisha Fort Dauphin huko Antanosy mnamo 1643, jamii zote mbili zilikuwa zimeingiliana, sio tu kutokana na ndoanje, bali pia kwa sababu watu wa ngazi za juu kutoka pande zote mbili walikuwa wakielekea kwenye kuunda ugatishaji wa kisiasa. Hata hivyo, katika kipindi chake cha miaka thelathini kwenye janibu hizi (1643-1674), Fort Dauphin ilikomesha kabisa mchakato huu, na muungano wa kisiasa haukuweza kujiri.

Wazafindraminia hawakuwa wajenzi wa ufalme, na Waantemoro wanawakilisha tukio lisilo la kawaida la wageni walioanzisha jamii na dola lao wenyewe, lakini Wamaroserana wanatambulika kama familia muhimu ya ufalme wa nchi yote katika historia ya siasa ya Bukini. Hawa walikuja kutoa watawala kwa ajili ya Wamahafaly, Wasakalava wa Menabe na Boina, na kwa sehemu ya Waantandray na Wabara. Kama ilivyokuwa kwa wageni wengine, asili yao na kipindi chao cha kuibuka kimebakia kuwa suala la mabishano. Mapokeo ya Wamahafaly na Wasakalava yanatofautiana kuhusu ni nani wahenga asili na ni wapi walikotokea "Wamaroserana-asili." Fasihi simulizi zilizokusanywa wakati Wasakalava walipokuwa bado huru, kwa pamoja zinapendekeza vyanzo viwili tofauti kabisa. Waandrianalimbe kutoka ndani ya Bukini na Waandriamandazoala kutoka ng'ambo.

Mgongano huu wa mawazo unasaidia kuelezea madai ya waandishi kadhaa kwamba Wamaroserana, kwa mfano, asili yao ni huko kusini-mashariki ya Bukini, kwamba walikuwa Wahindi ambao walishukia karibu na Fort Dauphin ya leo kiasi cha mwaka 1300 na kuelekea kaskazini kuanzisha Zarabehava, familia ya kifalme ya Waantesaka, na kutoka huko wakaelekea magharibi. Nadharia hizi tete zimesahihishwa miaka ya hivi karibuni kwa kuzingatia vyanzo vya msingi. Kama mapokeo ya kifalme ya Waantesaka yanavyoonyesha, watawala wa Zarabehava walikuwa tawi la Wasakalava wa pwani ya magharibi waliounda Bukini kwenye kipindi fulani kati ya 1620 na 1650. Kwa hali hiyo hakukuweko na hajira ya nasaba ya Maroserana kutoka mashariki kwenda magharibi: nasaba hii iliundwa kusini-magharibi mwa Bukini. Zaidi ya hayo, hakuna ushahidi wowote wa kuthibitisha wazo

la asili ya Uhindi, hakuna masalia ya lugha ya Kihindi yaliyopatikana katika msamiati wa watawala wa Maroserana.

Mapokeo haya mawili ya Wasakalava yanayotofautiana kwa vyovyote vile hayapingani. Wageni waliotokea bara, waliowakilishwa na Bwana Mkuu Ali (Andrianalimbe), na wale wa kutoka ng'ambo waliowakilishwa na Andriamandazoala walikaribiana zaidi kwa mchakato wa miungano na migongano, kwa kufuata ruwaza ya kawaida iliyofuatwa na wageni walioingia Bukini. Upo uwezekano mkubwa kwamba wahenga wengine wa Wamaroserana walifika kusini-magharibi mwa Bukini kupitia baharini. Watawala wa Wamaroserana miongoni mwa Wasakalava walijulikana kama Wazafivolamena (watoto (wa kiume) wa dhahabu) wakati ambapo makaburi ya watawala wa Wamaroserana huko Mahafaly bado yanaitwa *volamena* (fedha nyekundu, yaani dhahabu). Kutokana na kwamba hakukuwepo na dhahabu yoyote kwenye nusu yote ya kusini ya Bukini, basi mapokeo hayo yanayoonyesha kwamba dhahabu iliagizwa kutoka nje ya eneo hilo yana ukweli mwingi. Vivyo hivyo, kwamba *volamena* ilikuja kuwa metali takatifu inaakisi wito wa ufalme wa nasaba zote wa wale waliongiza metali hiyo: Tunapofikiria ukaribu wa machimbo makubwa ya dhahabu ya Zimbabwe, na kuwepo kwa watu ambao wangeweza kuileta Bukini kwa kuvuka tu mara moja, pamoja na kuwepo kwa maneno kadhaa na mila zinazofanana kati ya Bukini na Zimbabwe, ni vigumu sana kuepuka kuhusisha Maroserana na Mwene Mutapa.

Mapokeo ya kuvutia sana yaliyokusanywa na kuchapishwa na Msakalava mwanzoni mwa karne ya 20 yalitoa mwanga kuhusu kuzaliwa kwa historia ya Wamaroserana. Mapokeo haya yanaashiria kwamba pale mwanzoni wageni waliofika kusini magharibi walishindwa kujijenga kisiasa na kuonyesha kwamba mafanikio ya kisiasa yasingewezekana bila kuanzishwa kwa muungano wa koo hizo na familia za watemi wenyeji. Pia yanaonyesha kwamba uwezo wa kubuni mambo mapya ulikuwa ni jambo lenye manufaa kwa Wamaroserana wa awali. Walikuwa na hisi za kupanua mipaka ya nchi yao, walianzisha ujenzi wa ngome na kujenga kwenye maeneo ya mwinuko; walitumia askari wa mgambo, walisuluhisha magomvi, walijua jinsi ya kuvutia wafuasi kwa kuwagawia chakula na mifugo, na walianza kutafuta msaada kutoka kwa watabiri waliokuwepo kuhusu mambo ya serikali. Walifuata njia ileile miongoni mwa Wamahafaly ambapo uhusiano wao na familia za kitemi za Waandrianisileliky uliwaletea ukuu wa kisiasa.

Ingefikiriwa kwamba mchanganyiko wa kiwango cha juu cha uzazi miongoni mwa Wamaroserana na jitihada za kutumia kanuni ya uwanambee (kurithiwa na mtoto wa kwanza wa kiume) katika urithi wa ufalme zingesababisha mlolongo usiokwisha wa matawi ya kiukoo na wanamfalme wasiokuwa na haki ya kutawala. Labda msako wa jibu la tatizo hili ndio uliowafanya waanze kutafuta ardhi mpya ili kuwapatia wanamfalme wasiokuwa na haki ya kutawala katika familia za kifalme vijiji vya kutawala. Hata hivyo tatizo hili liliendelea hadi kwenye karne ya 19, na kuleteleza uguraji wa hiari wa wenye asili moja, miungano ya urafiki na wapinzani wa

Wamaroserana na hata kuundwa kwa falme zinazoshindana.

## Watu wa nje na athari zao

Taarifa za Wazungu waliotembelea Bukini kabla ya kipindi cha ukoloni zimekuwa za thamani kubwa isiyopimika kwa mchango wake katika kujifunza historia ya nyuma ya kisiwa hicho. Kinyume chake ni kwamba kuwepo kwa Wazungu hadi mwaka 1800 kulileta athari chache zaidi za kusifika. Kijumla, Wareno walikuwa na athari hasi kwenye biashara iliyotawaliwa na Waislamu na mlango wake na vituo vyake magbaribi mwa Bahari ya Hindi. Vituo vya biashara vya kaskazini-magharibi vilikuwa kwenye visiwa vidogo kwenye ghuba za Mahajamba, Boina na Bombetoki. Vilidhibitiwa na kukaliwa na jamii za wazungumzaji wa Kiswahili ambao walijihusisha na biasharanje ya mchele na watumwa kwa kupeleka vitu hivyo huko Afrika Mashariki na Arabia. Kituo cha biashara cha kaskazini-mashariki kilichoitwa Iharana kilikuwa tofauti kwa namna nyingi. Waiharana waliishi bara, utamaduni wao wa siku nyingi ulikuwa wa asili, uliojizatiti kwenye ung'arishaji wa mawe na ufundi wa ujenzi. Hakuna shaka kwamba kuporomoka kwa Waiharana kulianza pale Ulaya ilipoingilia biashara ya Waislamu katika Bahari ya Hindi. Kuanzia 1700 na kuendelea, Iharana ilikuwa si chochote zaidi ya kivuli chake yenyewe cha zamani, na utamaduni wake ulitoweka bila kuacha hata dalili moja inayoonekana. Mwaka 1506, Wareno walikishambulia kituo kikuu cha biashara cha Waswahili huko kaskazini-magharibi na kuangamiza Boina, ila waliwahurumia Wabombetoki kwa vile Shehe wao alionyesha urafiki. Wareno walikutana na koloni kubwa la Waafrika kwa upande wa kaskazini zaidi, kwenye Ghuba ya Anorontsanga. Waafrika hawa waliofikia kiasi cha elfu mbili walijitayarisha kwa vita, kisha walibadilisha mawazo yao na kutokomea huko bara. Vibanda vyao vilichomwa moto na ilikuwa kama vile "mlima wote ulikuwa unaungua moto". Hata hivyo koloni hili halikuwa sehemu ya mtandao wa kibiashara wa Waislamu; Waafrika hawa walikuwa watumwa waliotoroka kutoka Malindi, Mombasa na Mogadishu.

Hata hivyo, baada ya mwanzo uliofanana na vita, huko Msumbiji Wareno walibadili msimamo wao na wakaanza kutuma merikebu moja kwa mwaka kwenda kaskazini-magharibi ya Bukini kuchukua mifugo, ambari, nguo za rafia (viramba) na watumwa. Zaidi ya kusababisha ongezeko la bidhaa za kuuza nje, Wareno walisababisha pia kuzuka kwa miungano kadhaa midogomidogo ya kisiasa huko kaskazini-magharibi mwa kisiwa, sio mbali kutoka vituo vya kibiashara vya Waswahili. Moja kati ya vituo hivi kiliongezeka kwa umaarufu chini ya mtawala ambaye cheo chake kilikuwa *Tingimaro*, ambaye "wakati wote alikuwa akipigana vita na majirani zake." Juni 1614, Tingimaro alitembelewa na Padri Luis Mariano wa shirika la Yesu huko Msumbiji kwenye mji wake mkuu Kuala. Padre huyu alitarajia kupata fursa ya kuanzisha dini yake kwenye nchi hiyo, lakini Tingimaro alikataa kuwekeana mkataba na Wareno na hakupenda kuruhusu shughuli za wamisionari ndani ya kisiwa hicho.

Katika miaka ya mwisho ya 1580, Wamoori wa Mazalagem walikataa kufanya biashara na Wareno, na padre wa shirika la Wadominika aliyekuwa akitafuta waumini wenyeji aliuawa. Vita viliepukwa tu kufuatia amri iliyotoka kwa mfalme wa Lisbon, lakini sio kabla ya kulipiza kisasi kwa Wamoori nje ya Bukini. Mwaka 1590 kaskazini-magharibi ya Bukini iliingizwa kwenye zoni ya biashara ya kisiwa cha Msumbiji. Kati ya 1614 na 1620, majaribio kadhaa ya kuanzisha kanisa kaskazini-magharibi ya Bukini yalifanywa.

Wareno walitiliana sahihi mikataba kadhaa na watawala waliokuwa kandokando ya pwani ya magharibi mwaka 1613, na ujumbe wa Wayesu ulitumwa kwenye ufalme wa Sadia, karibu na mto Manambolo, mwaka 1616-17. Ujumbe huu ulizua vita vya wenyewe kwa wenyewe ambavyo vilikuwa vinajiandaa kwa muda na ambavyo vilikuja kuwa na matokeo muhimu katika uanzishaji wa ufalme wa Wasakalava wa Menabe. Mwaka 1641 Wareno waliteka rasmi Afrika ya Magharibi katika mkataba baina yao na Waholanzi, jambo ambalo halikuwa na athari yoyote ya maana. Ni kweli, karibu na 1700 kaskazini-magharibi ya Bukini ilikuwa chini ya udhibiti wa Wasakalava-Maroserana; karne moja baadaye, Wamalagasi waliweza kushambulia sio tu vyombo vya Wareno peke yake katika mlango-bahari wa Msumbiji, bali pia vituo vyao kwenye visiwa vya Kwerimba na Ibo.

Inaonekana kwamba mwanzoni mwa miaka ya 1600 Wareno walichukua watumwa wachache zaidi kutoka Bukini kuliko washindani wao Waafrika na Waarabu. Wakati huohuo Visiwa vya Ngazija viligeuka kuwa kituo cha kati ambapo watumwa na bidhaa kutoka Bukini zilichukuliwa kwa ajili ya kupelekwa kwa merikebu huko Malindi, Mombasa, Mogadishu na Arabia. Mwaka 1614, Anzuani iliripotiwa kuwa ilikuwa imejaa watumwa wanaume na wanawake kutoka Bukini waliokuwa wakingojea kupelekwa Arabia ili kubadilishwa na pamba ya India na afyuni. Majahazi kutoka Shihir huko Ghuba ya Aden yalifanya safari za moja kwa moja kwenda Bukini kununua mchele, mtama na vijana wa kike na wa kiume. Ni wazi kwamba Wareno walikuwa wakipoteza mashiko yao huko Bukini na nafasi yao kuchukuliwa na wanunuzi wenyeji, na baada ya kama 1620 wanaonekana kupoteza moja kwa moja raghba yao kwenye kisiwa hicho.

Karne ya 17 ilipokuwa inajitoma kwenye nusu ya pili, wanunuzi wapya walijitokeza huko Bukini ambao hawakubanisha shughuli zao kaskazini-magharibi ya kisiwa hicho tu. Angalau merikebu nane zinafahamika kuwa zilikwa zikiwabebea Waholanzi huko Mauritius watumwa na mchele kutoka Bukini, hasa kutoka Ghuba ya Antongil, kati ya 1639 na 1647. Waholanzi walikuwa na migogoro ya mara kwa mara na Wamalagasi wa Mashariki hadi 1655 walipoanza kufanya safari za kwenda kisiwani humo kutokea kwenye Rasi; pia walishiriki kwenye migogoro ya wenyeji. Lakini pwani ya mashariki haikuwa imeungana, na kuwepo kwa Waholanzi hakukuonekana kuwa na athari ya kudumu. Hata hivyo, katika karne ya 18, Waholanzi pamoja na Wazungu wengine, waliyaathiri sana kibiashara maeneo kadhaa ya Bukini, na hasa kandokando ya pwani ya magharibi.

Vyombo vya baharini vya Waingereza vilifika Bukini mara mia nyingi kati ya 1600 na 1800; zaidi vilifika kwenye pwani za magharibi na hasa kwenye Ghuba ya Mt. Agostino. Kipijini cha Kiingereza, lugha ya biashara, kilijijenga chenyewe kwenye eneo hilo, na wenyeji kadhaa walichukua majina pamoja na vyeo vya Kiingereza. Mwaka 1645, Walokole (Ma-Puritani) wa Kiingereza walipelekwa kwenye Ghuba ya Mt. Agostino kuanzisha koloni, na miaka mitano baadaye jaribio jingine la ukoloni lilianzishwa kwenye visiwa vidogo vya Nosy Be huko kaskazini-magharibi.

Majaribio hayo mawili yalishindwa vibaya sana huku yakipoteza maisha ya watu wengi. Lakini tofauti na Wareno na Waholanzi, Waingereza hawakuanzisha vituo vyovyote huko Bukini, ila wao ndio waliokuwa wakijishughulisha zaidi na biasharanje ya watumwa wa Kimalagasi kwenda Dunia Mpya, hasa Barbados na Jamaika. Sensa iiyofanyika huko Barbados mwishoni mwa karne ya 17 ilionyesha idadi ya watumwa 32,473, nusu yao ikitokea Bukini. Maharamia walishiriki katika vita vya wenyeji, na kuchangia katika kupatikana kwa watumwa kwa ajili ya kusafirisha nje. Ilikuwa ni katika kipindi hiki cha maharamia ambapo mabadiliko mawili muhimu kuhusiana na biashara na bidhaa yalitokea. Kwanza, Wazungu walipoanza kushindana, watawala wa maeneo ya pwani walitumia vizuri fursa hiyo kuongeza bei zao. Pili, na huenda ni matokeo, Wazungu walianza kuuza silaha mbovu au zisizotumika tena, wakizibadilisha kwa watumwa waliohitajika sana. Mara nyingi silaha hizo zililipukia mikononi mwa wale waliozitumia.

Miongoni mwa mataifa ya Wazungu waliowania kuanzisha vituo vya kudumu huko Bukini, Ufaransa pekee ndiyo iliyoweza kufanikiwa kwa kiasi fulani huko Fort Dauphin, makazi yaliyolindwa kwa ngome kusini-mashariki mwa Bukini, ambayo yalidumu kwa zaidi kidogo ya miongo mitatu, kuanzia 1643 hadi 1674. Wanaume wengi wa Fort Dauphin waliwaoa wanawake wenyeji. Gavana wa kwanza wa Fort Dauphin, Pronis, alimwoa *Mrohandria* wa Kifindramania, na askari aliyepangwa jina la "la Case" alimwoa mrithi wa kike katika nchi ya Antanosy na kuwa shujaa wa kijeshi wa eneo hilo. Gavana aliyekuwa amesoma sana na wa muda mrefu huko Fort Dauphin, Etienne de Flacourt (1648-1658), mwandishi wa kazi mbili za msingi kuhusu Bukini, alibadilika kuwa mtawala wa kienyeji, na alilazimika kujihudumia mwenyewe kwa vile alipata msaada mdogo sana kutoka Ufaransa.

Kwa jumla, taathira ya Fort Dauphin haikutathiminiwa kwa uzito unaostahili: ilikuwa na unyeti wa kijanibu, lakini pia ilikuwa na matokeo mapana zaidi. Kwa mfano, Waantanosy walikuwa wamekaribia kupata muungano wao wa kisiasa, uliokuwa umeshindikana kwa muda mrefu, na Wazafindraminina, chini ya uongozi wa Dian Ramack, wakati Fort Dauphin ilipowawekea kizingiti. Wakati ambapo merikebu zilikuwa hazifiki tena kwenye ngome hiyo (1650-1654), vita vikali vya kugombea madaraka, vilitokea, upande mmoja ukiwa wa wageni, *Warohandria*, na upande wa pili maaskari wa Kifaransa. Ilipofikia 1653, Dian Ramack na *Warohandria* wengi walikuwa wamekufa, na watemi kadhaa waliapa kuwa waaminifu

*(mifaly)* kwa de Flacourt, ambaye hakuwa na raghba ya kujenga dola la kienyeji. Hali ilizidi kuwa mbaya baada ya kuondoka kwake, lakini hata hivyo Kampuni ya Pili ya Wafaransa ya India Mashariki ilifanya jitihada zaidi ya kuanzisha ukoloni huko Bukini. Vituo vya doria vilianzishwa Antongil, kwenye Mto Matitana na huko Sainte-Marie. Mwaka 1667 kiasi cha wakoloni 2000 hivi na maaskari wa Kifaransa walitua Fort Dauphin. Jambo hili lilianzisha mfululizo wa *mifaly,* jinsi watawala wa Antanosy walivyoendelea kujiondoa moja kwa moja kwenye mapambano hayo. Nje ya Antanosy, kuwepo kwa Wafaransa huko Fort Dauphin kulichapusha kuanzishwa kwa Menabe na mtawala wa Maraserana, Andriandahifotsy, ambaye aliunda ushirika na Fort Dauphin.. Fort Dauphin iliachwa mwaka 1674 na wakazi wake wa mwisho walihamishiwa Msumbiji, India na kwenye kisiwa cha Bourbon (sasa Réunion).

Uchumi wa mashamba makubwa ya visiwa vya jirani vya Maskarene, Bourbon na Ile-de-France (Mauritius, iliyohamwa na Waholanzi mwaka 1710) ulileta vurugu huko Bukini, hasa katika pwani ya mashariki, kwenye karne ya 18. Kwa kawaida inakubalika kwamba idadi kubwa ya watumwa walioingizwa katika visiwa vya Maskarene kati ya 1664 na 1766 walitokea Bukini, ila utawala wa kifalme wa Ufaransa, ambao ulinunua visiwa hivi kutoka Kampuni ya Ufaransa ya India ya Mashariki kwa zaidi ya pauni milioni 7.5, polepole uliwabadilisha Wamalagasi kwa watumwa kutoka Afrika. Hata hivyo isisahaulike kwamba uingizaji wa watumwa uliongezeka maradufu kati ya 1766 na 1788, na kwamba Wamaskarene, hata baada ya 1766, mara nyingi waliingilia sehemu ya kaskazini-mashariki mwa Bukini.

## Madola ya kaskazini na ya magharibi: Mahafaly, Sakalava, Antankara, Tsimihety

Baada ya ushindi wa awali wa kisiasa wa Wamaroserana huko kusini-magharibi, jamii mpya ilizuka kati ya mito miwili, Menarandra na Onilahy. Jina lake la Mahafaly (kutakatifuza) linahusishwa na utofautishaji wa kijamii na miviga ya kifalme. Kufuatana na mapokeo, Mmaroserana wa kwanza alijitenga kabisa na jamii, huku akishauriwa na kulindwa na *ombiasa* (kuhani) wa mtawala. Kwa vile alikuwa haonekani tena, alikuwa mtakatifu *(faly)*, na kwa mwendekezo huo, aliifanya ardhi pamoja na wakazi wake vilevile kuwa *maha-faly.* Wamaroserana walipochukua madaraka, jamii ya Mahafaly ilijumuisha waliopendelewa *(renilemy)*, na watu wa kawaida *(valohazomanga)*, na wale waliotokea kwingineko *(folohazomanga)*. Tabaka jipya la waali liliundwa na madhuria wa mtemi aliyekuwa na nguvu zaidi wakati wa kuundwa kwa jamii ya Wamaroserana (Tsileliki, asiyeshindika), raia wake wa awali, wale wote waliowasili wakifuatana na Wamaroserana wa asili, pamoja na wale waliokuwa wakitunukiwa mara moja moja.

Historia ya Wamahafaly kabla ya 1800 iliambatana na migogoro kati yao na majirani zao, kugawanyika katika falme nne huru, na kutekwa kwa ardhi iliyokuwa inamilikiwa na tawi la magharibi zaidi la Waantandroy. Wakati fulani katika miaka ya 1650, falme mbili za kwanza zilizojitenga, Menarandra na Sakatovo, zilianzishwa.

Baadaye kidogo, Manerandra ilizaa falme nyingine mbili, Linta (t.1670) na Onilay (t.1750). Mmoja wa wafalme wa Menarandra ndiye aliyeshinda na kuteka nchi za magharibi za Karimbola-Antandroy katika nusu ya kwanza ya karne ya 18. Athari za Waantemoro zinaweza kuonekana katika ufalme wa Onilahy, ambao mtawala wake wa kwanza alichukua cheo cha Antemoro cha Andrianoni kama jina lake. Kulikuwepo na watawala sita huko Sakatovu kabla ya 1800, saba huko Linta, watatu huko Menarandra na wawili huko Onilahy. Vikundi hivi vinaakisi mifarakano mingi ya ndani miongoni mwa Wamaroserana.

Ingawa Wamaroserana walipata ushindi wao wa kwanza miongoni mwa *tompontany* waliokuwa wakiishi kusini mwa Onilahy kwenye njia kuu zaidi ya majini ya kusini-magharibi, lakini nasaba tawala yao haikupata umaarufu wa kisiasa hadi pale wajumbe kadhaa kati yao walipokwenda kaskazini kwenye bonde la Fiherenana. Hapa ndipo walipozaliwa Wamaroserana-Volamena, na kutoka pale walivuka Mto Mangoky na kuunda nasaba tawala ya madola ya Sakalava ya Menabe na Iboina. Hakuna shaka kwamba Andriandahifotsy alianzisha nasaba ya Menabe, na huenda tawi lake la Volamena pia. Kuanzishwa kwa nasaba za Volamena na Menabe kuliambatana na nduni za kidini na kidunia. Kasisi wa kifalme aliyehusishwa na mamba, Ndriamboay (mamba mtukufu) alisifika kwa kuanzisha dhehebu la kuwatukuza wahenga *(dady)* miongoni mwa Wamaroserana, na hivyo kuwafanya watawala wawe *ampagnito-be* (wahenga wakuu wa kifalme, mababa wa umma). Kulingana na mapokeo mengine, Ndriamboay alimtoa kafara mke wa Andriandahifotsy, ambaye kutokana na damu yake kulipatikana majina mawili ya Volamena (almasi iliyogeuka kuwa nyekundu) na Menabe (nyekundu kuu). Mapokeo mengine yenye ukweli zaidi yanashikilia kwamba mke wa Andriandahifotsy alifanikiwa kumletea mumewe silaha za kwanza za moto wakati wa mapigano muhimu sana. Silaha hizo kumi zilikuja kuwa sehemu ya hazina ya kifalme na watoto wake wa kiume wakawa Wavolamena.

Wamaroserana walipokutana na jamii za Menabe, hawakuwa tena kwenye ardhi ya wafugaji wa kusini-magharibi. Ukanda wa pwani unaoenea, takribani, kati ya Majunga na Morondava, kwa karibu kilomita 650, ulikaliwa na wavuvi na wakulima waliokuwa wanafuga ng'ombe wachache. Isipokuwa kwa eneo la Sadia lililokuwa na msongamano wa watu, wakazi wengi waliishi kwenye jumuiya ndogondogo, na hawakuwa na silaha zozote. Kipande hiki cha pwani kilijulikana kama Bambala, na wakazi wake hawakuzungumza Kimalagasi bali lugha za Kibantu. Walikuwa Ma-*Cafre* na siyo Ma-*Buque*. Wasakalava walifika Sadia na kuunganika na Wamaroserana karibu na Mto Mangoky, labda kwenye kimojawapo cha vijito vyake vidogo kilichoitwa Sakalava. Mapokeo yote yanakubaliana kwamba Wasakalava ndio waliokuwa mashujaa hodari wa kipindi chao. Ndio waliokuwa silaha kuu ya mamlaka ya kisiasa ya watawala wa Volamena, lakini imani ya *dady* iliipatia mamlaka hii msingi wa kidini ambao haukuweza kutikiswa na mashujaa hao wa kutisha na madhuria wao. Fomula iliyowapatia wafalme hao majina hayo yenye kiambishi awali

cha *andria* (lodi, mheshimiwa) na kiambishi tamati cha *arivo* (elfu, maelfu) iliingizwa huko Manabe kutoka nje lakini labda haikuingizwa moja kwa moja na Wamaroserana. Fomula hii inaakisi lile wazo la kisiasa ya kwamba mfalme wa kweli lazima awe na raia wengi.

Manabe ya kusini ilikuwa inatawaliwa na Andriandahifotsy katika miaka ya mwanzoni ya 1670, wakati alipotembelewa na Mfaransa mfanyabiashara ya ng'ombe kutoka Fort Dauphin ambaye aliona jeshi lenye nidhamu la kiasi cha wanaume 12,000, na kupokea mafahali hamsini ya ng'ombe kama zawadi kwa ajili ya gavana wa ngome. Andriandahifotsy alifariki kama mwaka 1685. Migogoro ya kugombea urithi ilimwacha mmoja wa watoto wake wa kiume, Trimongarivo (aliyegeuza jina na kuwa Andriamanetriarivo) akiwa mkuu wa Menabe, ambayo aliipanua na kuiongezea raia wapya kutoka miongoni mwa wafugaji wa kusini-magharibi. Mdogo wake wa kiume, Tsimanatona (kwa *fitahina* Andrianmandisoarivo), alielekea kaskazini na kuanzisha Iboina. Ni vigumu kusema endapo Menabe ilikuwa na watawala wanne au sita kati ya 1720 na 1800, ila iliendelea kuimarika katika kipindi hiki, licha ya kuwepo ripoti kuhusu mauaji ya mfalme katika miaka ya 1730. Kwenye muongo uliofuatia, ushirika muhimu kati yao na watawala wa Andrevola wa bonde la Fiherenama ulifanyika kwa maafikiano ya damu ya kifalme ya Wafiherenama; ushirika huo uliiimarisha zaidi mipaka ya kusini ya Menabe. Huko Iboina, ikiwa imelindwa kwa upande wa kusini na dola-dada la Menabe, vituo vya biashara na wafanyabiashara wa Kiislamu walilazimishwa kuwa chini ya ulinzi wa mtawala wa Volamena. Majunga ilikua na kuwa mji mkuu wa Iboina, huku wafalme wake na kitala chao huko Marovoay wakipata ufahari usioweza kulinganishwa na mahali popote huko Bukini. Wakati wa kipindi cha Andrianinevenarivo (aliyejulikana kama Andrianbaga, alifariki 1752), Iboina ilikuwa katika kilele chake. Wahamiaji kutoka kaskazini, wakielekea kusini wakiwa na mifugo yao, polepole waliwameza wakazi wote wa Kibambala waliobakia. Hii haikumaanisha tu kutoweka kwa *watompon-tany* waliozungumza Kibantu, bali pia mabadiliko ya kinyumenyume kiuchumi wakati ambapo madola ya Sakalava yalihitaji wakulima zaidi. Jinsi ilivyozidi kuwa vigumu kupata nguvukazi ya kilimo kutoka maeneo mengine ya Bukini, Wasakalava walianza kuvamia visiwa vya Ngazija na hata kusini-mashariki mwa Afrika (ili kupata watumwa).

Katika theluthi ya mwisho ya karne ya 18, malkia Ravahiny (t.1767-1808) aliipatia Iboina serikali imara na iliyostawi kiuchumi. Hata hivyo Iboina ilianza kudidimia wakati wa utawala wa malkia huyo. Waislamu wa Iboina waliokuwa wameungana na Wasakalava ndio waliounda kikundi chenye ufukuto katika nchi hiyo kilichotaka kuchukua kiti cha enzi. Udhaifu mwingine uliojitokeza na ambao haukuwa waziwazi, ulianzia pwani ya mashariki mahali ambapo muadhamu mmoja wa Kipoli-Hungaria, *Count* Benyowsky, alikuwa amewashawishi watawala kadhaa wa Betsimisaraka kuacha kulipa ushuru kwa Waiboina. Wapiganaji waliotumwa mwaka 1776 kuwaadhibu walipa kodi hao wa zamani na kumwondosha Benyowsky

hawakufanikiwa katika lengo lao, na hivyo kudhihirisha kwa watu wa bara kwamba Waiboina walikuwa tayari wameshapoteza uwezo wao. Mwishowe, Ravahiny alifanya kosa katika sera ya nje kwa kuamua kuunga mkono mtawala wa Imerina ya kati, Andrianampoinimerina dhidi ya majirani zake walioshindana naye.

Wafalme wa Sakalava walikuwa madikteta na wapenda anasa. Maisha yao ya kila siku yalidhibitiwa na ma-*moasy* (makasisi) wa kifalme, na hakuna lolote lililoweza kufanywa bila ushauri wao. Kulikuwepo na Baraza la Kifalme lililoundwa na wazee sita, ambao waliishi kwenye kitala. Waziri wa kwanza, *manantany*, alihusika moja kwa moja na washauri maridhawa wa kifalme. Msaidizi wake, *fahatelo*, alichaguliwa kutokana na elimu yake kubwa kuhusu koo na unasaba pamoja na kujua mila za Sakalava. Kila kijiji kilikuwa na ofisa wake rasmi ambaye alihakikisha kwamba watu walifanya kazi siku nne kwa wiki kwenye mashamba ya mpunga ya mfalme, na kwamba mifugo ya kifalme ilihuishwa na kuongezwa kwa kuteka mifugo mipya, au kwa mfumo wa zawadi zilizokuwa zikitolewa kwa mgawo maalumu. Hakuna mfalme aliyewaza kutawala bila kuwa na *dady* wa kifalme (masalia ya wahenga wa Volamana), hasa kwa vile moja kwa moja mfalme mpya ndiye aliyekuwa kiungo kati ya walio hai na wahenga wa kifalme.

Watsimihety walitokana na vikundi vya wakimbizi visivyokuwa na viongozi kutoka pwani ya mashariki, ambao walikuwa wametoroka vita vya kuteka watumwa wakiwa na ng'ombe wao na kulowea kwenye uwanda mkuu wa Mandritsara. Huko kaskazini zaidi, kwenye eneo la miamba kisiwani humo, waliishi Waantankara (watu wa miambani). Hakuna hata moja kati ya jamii hizi iliyokuwa imeunda dola lake yenyewe; wote walikubali kutawaliwa na aila wa Wamaroserana, yaani Wavolafotsy, ambao kwa kushindwa kutawala miongoni mwa Wasakalava, walihamia bara upande wa kaskazini wakitafuta ufalme. Hata hivyo, punde Watsimihety waliwakataa Wavolafotsy (au Wavolamena) na kwa makusudi walichukua jina lao la pamoja *(tsi-mihety)* kuonyesha kwamba hawakuwa tayari kujitoa kwa utawala wa Wamaroserana. Kwa vile walishindwa kuanzisha ufalme unganifu, historia yao ya karne ya 18 haijulikani.

Waantankara waliichukulia hali hii tofauti kabisa. Wengine walijitoa kwa mwanzilishi wa Iboina na wengine walikuja kuwa chini ya udhibiti wa Wasakalava, katika kipindi kimoja au kingine katika karne ya 19. Hata hivyo, unasaba wa kifalme uliomrejelea Mvolafotsy aliyeitwa Kazobe, ulizuka miongoni mwao. Hata hivyo, ufalme unganifu kabisa wa Waantankara haukuanzishwa hadi katika kipindi cha binamu yake mkuu, Andriantsirotso, ambaye kufuatana na maandishi alitawala ama kuanzia t.1697 hadi 1710 au t.1710 hadi 1750. Alijenga mava ya kifalme huko Ambatosehana na kuanzisha ishara ya muungano ya ufalme wa Antankara iliyoitwa *saina*, bendera iliyokuwa na mwezi mwandamo na nyota. Alihusisha nguvu zake za utawala na *moasy* (kasisi) mwenye nguvu nyingi aliyetengeneza hirizi za kifalme. Alikuwa mshauri wa warithi wake wawili, na aliishi hadi kufikia umri wa zaidi ya miaka mia moja. Mtoto wake wa kiume na mrithi wake, Lamboina, alikuwa na

utawala mrefu kuliko zote nchini Bukini, uliojulikana zaidi kutokana na kutokuwepo na vita wakati wake. Waantankara walikopa utaratibu wa kisiasa kutoka kwa Waibona-Sakalava lakini hawakuchukua madhehebu yao ya *dady*.

## Madola ya Bara: Betsileo, Merina, Sihanaka, Bezanozana, Tanala na Bara

Wabetsileo walipata jina lao kutoka kwa mtawala aliyeitwa Besilau ambaye anajulikana kwa kupinga upanuzi wa Menabe kwenda nyanda za juu za huko bara katika miaka ya 1670 kulikofanywa na Wasakalava. Lakini hata hivyo, watu waliokuja kujulikana hapo baadaye kama Wabetsileo walianza kuwa chini ya serikali moja katika miaka ya 1800 kutokana na msukumo kutoka nje. Wakiwa ni mchanganyiko wa *watompon-tany* na wageni mbalimbali, Wabetsileo waligawanyika katika nchi kuu nne: Arindrano huko kusini, ikiungana na Ibara; Isandra ikiwa katikati, ikielekea magharibi na kwa Wasakalava; Lalangina ikiwa mashariki-kati, majirani zake wakiwa Watanala; na Manandriana huko kaskazini. Huenda Wabetsileo hawakuunda falme zozote kabla ya miaka ya 1650. Rasahamanarivo, mwanzilishi wa Lalangina, alilazimika kung'atuka na kumwachia kiti kaka yake kwa vile alikuwa na ukoma, lakini karibu na mwaka 1680 alikwenda Arindranao na kupokelewa na Wabetsileo wa kusini kama mtawala wao. Mapambano ya urithi na vita kati yake na majirani zake vilizuia ukuaji wa Lalangina ambayo, baada ya mauaji ya mfalme, iligawanyika katika mikoa minne. Hata hivyo, tawi la familia ya kifalme la Lalangina lililojitwalia madaraka, angalau lilitoa kiasi cha watawala watatu wenye nguvu katika karne ya 18: Roanimanalina, ambaye aliunganisha tena ufalme huo na kuanzisha jeshi la mgambo la taifa; Andrianonindranarivo aliyeleta mageuzi ya kiuchumi na ya kijamii; na Ramaharo aliyebadilisha jeshi la mgambo na kulifanya kiungo cha kiuchumi cha taifa kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mpunga. Ni kweli, katika karne ya 18 Wabetsileo walikuwa ndio wazalishaji wakuu wa mpunga huko Bukini.

Kufuatana na mapokeo yanayopingana, Zafimanarivo, ambaye alikuwa mhenga wa ukoo wa kifalme wa Isandra, alikuwa ama mwanamke kutoka Antemoro au mwana wa mfalme wa Maroserana aliyekuwa uhamishoni. Sababu za kijiografia zinapendelea mtangulizi kutoka Maroserana. Mzafimanarivo wa awali anahusishwa na istilahi *volamena* (dhahabu). Mtu asingeweza kuita Isandra nchi mashuhuri ya Betsileo hadi kwenye miaka ya 1750 wakati nchi hiyo ilipokuwa chini ya utawala wa mfalme mkuu, Andriamanalina I. Mara nyingine akiitwa "mfalme mcheshi" kutokana na uwezo wake wa kujadili hoja za kisiasa kwa ucheshi na kushinda. Andriamanaliana I alikuwa Mbetsileo wa kwanza kuzaa wazo la nchi moja iliyoungana. Diplomasia iliposhindwa, Andriamanalina I alitumia nguvu za kijeshi. Alipanua ufalme wake kuelekea magharibi na kuiingiza Betsileo kwenye mlundikano wa milima ya Midongy, na kuelekea Ibara huko kusini, ambapo alipata mtwawa muhimu, yaani mtawala wa Bara-Andriamanely II. Huku akibakiza miundo asili ya kila mkoa,

Andriamanalina I aliwaweka wanawe wa kiume kuongoza mikoa minne mipya walimoishi Wabetsileo wengi. Alipofariki 1790, Wabetsileo walikuwa kwenye upeo wa kisiasa. Ama kuhusu Manandriana, baada ya kuundwa mnamo 1750 ilikuwa na kipindi kifupi sana cha kuwa taifa huru, huku mtawala wake wa pili akijiweka kwa hiari yake mwenyewe chini ya Wamerina kwenye mwaka 1800.

Historia ya Merina kwa usahihi inaanza na utawala wa Ralambo, unaokadiriwa kuwa kati ya 1610 na 1640. Kabla ya hapo Merina haikuwa dola lenye mpangilio, ilikuwa na vijiji vingi vilivyotawaliwa na watemi, na wakazi wake walikuwa ama *watompon-tony*, Wavazimba au wahamiaji kutoka Hova. Mtawala wa kwanza wa nasaba ya Andriana alikuwa Andriamanelo, baba wa Ralambo. Yeye ndiye aliyeanzisha ngome huko Alosava na ndiye aliyeanza kutumia mikuki yenye ncha ya chuma badala ya ile yenye ncha ya udongo wa mfinyanzi.

Wakati wa Ralambo ndipo alipoibuka *sampy* (muungu wa kifalme) wa kwanza miongoni mwa ma-*sampy* kumi na wawili, yaani walinzi wa hirizi wa Imerina, mila ya kifalme ya tohara na kujamiina kwa maharimu, *fandraona* au ibada ya kila mwaka ya josho la kifalme, utabiri wa watawala waliokwisha kuondoka, matabaka ya waadhamu, wahunzi na masonara kwenye huduma za dola, kodi ya kichwa, ulaji wa nyama ya ng'ombe na jeshi dogo imara. Mwanae wa kiume na mrithi wake, Andrianjaka, alichukua hatua kadhaa za siasa ya ndani zilizowatia hofu wananchi wake, lakini hata hivyo alianzisha Antatanarivo na kutumia maeneo yenye kinamasi kupata mavuno mengi ya mpunga, na hivyo kuwafanya Wamerina kuwa wengi zaidi miongoni mwa Wamalagasi.


Ongezeko la watu huko Merina liliongeza tishio la njaa, na hivyo kulazimisha watawala wake kuendelea kupanua maeneo ya umwagiliaji maji. Wakati warithi watatu wa Andrianjaka walijitambulisha hasa kwa kuongezea urefu wa majina yao ya kifalme, kitukuu wake, Andriamasinavalona, alikuwa pia mfalme mkuu. Alishawishi kuanzishwa kwa sera ya upanuzi wa kichokozi na kuruhusu uhuru kiasi fulani kwa machifu wengi walioingia chini ya mamlaka yake. Aliongeza idadi ya koo za malodi kutoka nne na kuwa sita na kuwatuza malodi waliostahili kwa kuwapatia milki za mashamba na cheo cha *tompon-menakely* (mabwana wa mashamba). Akitaka kusuluhisha suala la mrithi wake wakati bado akiwa anatawala, aliigawa Imerina kwenye mikoa minne na kuweka wanawe wanne kutawala mikoa hiyo. Mara alijikuta akitawala falme huru nne. Isitoshe, alidhalilishwa na mwanawe mmojawapo kwa kuwekwa jela. Mfalme huyu mzee alifariki kwenye mwaka wa 1750 na Imerina iligeuka kuwa uwanja wa vita vya wenyewe kwa wenyewe, vita ambavyo hata wageni kutoka nje walishiriki. Ilipofikia kwenye 1770, Ambohimanga ilikuwa imeishinda Ambohitrabibly na kuonekana kuwa na nguvu zaidi chini ya mtawala wake, Andrianbelomasina. Mpwa wake, Ramboasalama, ambaye alikuwa mtawala wa Ambohimanga kwenye mwaka 1777-8, alikuja kutambuliwa kama mfalme muhimu zaidi wa Imerina.

Mfalme huyo aliyechukua jina la Andrianampoinimerina, kwanza alifanikiwa

kuleta amani kati yake na kaka zake wa kifalme waliokuwa wapinzani wake, na kisha kujenga ngome kuzunguka mipaka ya ardhi ya ufalme wake. Antatanarivo iliingia chini ya utawala wake mwaka 1797, ikifuatiwa mara na Ambohidratrimo, na maeneo mengine kadhaa ya Imerina kabla ya 1800. Hakuridhika na kuunganisha Merina, hivyo alianza kupeleka wajumbe kwa watawala wa maeneo mengine ya Bukini akiwashauri wakubali kuwa watwawa wake huku wakibakia na uhuru wao wenyewe, la sivyo, kama wakikataa kukubaliana na pendekezo hilo, wangeshuhudia nchi zao zikitekwa na Wamerina. Mara nyingine diplomasia ya namna hii ilifaulu, kwa mfano, miongoni mwa Wabetsileo wa Manadriana, Waandrantsay wa Betafo, na huko Imamo ya magharibi.

Ijapokuwa Wasihanaka na Wabezanozano hawakuchipuza miundo ya dola yenye nguvu, historia yao inabakia kuwa yenye kuvutia sana. Kundi la Wasihanaka lilianzia kwenye maeneo yaliyozunguka Ziwa Alaotra na Wabezanozano waliselelea eneo lililokuwa kati ya misitu ya mvua ya tropiki huko pwani ya mashariki na kwenye miteremko ya uwanda wa juu. Makundi haya mawili yalikuwa kwenye maeneo mazuri ilimopitia njia kuu ya biashara iliyounganisha Imerina na pwani ya mashariki, na hivyo wakawa watoaji wa watumwa kwa wafanyabiashara ya watumwa wa Maskarene. Wasihanaka na Wabezanozano walimiliki watumwa wengi kiasi kwamba mnamo 1768 walilazimika kuomba msaada kutoka kwa Wazungu ili kuzima maasi ya ndani yaliyosababishwa na watumwa. Mnamo 1767 wakati François Martin alipopenya na kuingia nchi ya Sihanaka, aliwakuta wenyeji wakikaa kwenye vijiji vyenye ngome za kuvikinga dhidi ya mashambulizi. Walikuwa na daraja pekee lililoonekana nchini Bukini hadi wakati huo, na pia walikuwa na silaha nyingi za pinde na mishale. Martin pia amethibitisha kwamba Wasihanaka walikuwa moja ya vikundi muhimu vya kibiashara huko visiwani, jambo ambalo lilimaanisha kuwa na utaratibu wa kutosha wa kisiasa. Hata hivyo hakuna ushahidi wowote wa kuonyesha kwamba walikuwa na mamlaka gati. Kusema kweli Wasihamaka walilipa ushuru kwa Iboina katika karne ya 18 lakini sio bila angalao jitihada moja kali ya kutaka kujikomboa kutokana na ushuru huo kwa kuanzisha mashambulizi makubwa ambayo hata hivyo hayakufaulu. Wabezanozano, ambao hapo mwanzoni ardhi yao iliitwa Ankay, nao pia walitawaliwa na watemi wenyeji na kuishi kwenye vijiji vilivyokingwa kwa ngome. Hata hivyo tofauti na Wasihanaka, wao angalau walikuwa na asasi iliyowaunganisha, ambayo ilikuwa katika sura ya hirizi zilizowakilisha miungu kumi na mmoja wa ulinzi waliosemekana kutokea kwenye ardhi ya Sakalava. Karibu na kufikia mwishoni mwa karne ya 18 Wabezanozano wanaelekea kuyakubali mamlaka ya Randrianomoina, mfalme wa kwanza, lakini hakuweza kutawala kwa muda mrefu, kwani Wamerina walimlazimisha kujisalimisha kwao.

Wakiwa wamebanwa kati ya nyanda za juu za Wabetsileo na Waantemoro wa pwani, Watanala walipata jina lao kutokana na mazingira yaliyowazunguka - "watu wa msituni." Baada ya muda si mrefu Watanala walikuwa watu waliochanganyikana sana kwa vile kiasi cha koo zao ishirini na tatu zilikuwa zikidai kuwa na chimbuko



**28.2:** *Mbari ya Wabara wa Ambusitra, kusini-mashariki mwa Bukini. Sanamu ya kumbukumbu inayoitwa* alualu, *inayojengwa wakati mtu anapokufa bila kuzaa mtoto wa kiume au iwapo maiti haikuzikwa kwenye makaburi ya familia. Sanamu hiyo ilizungushiwa nguzo zenye pembe za ng'ombe wa aina ya Zebu waliotolewa kafara kwenye sherehe za mazishi yake. Kanuni ilikuwa kwamba sanamu ya kike ndiyo iliyojengwa kwenye kaburi la mwanamume aliyekufa na inaashiria kiumbe aliyetarajiwa kuleta kizazi. Sanamu imetengenezwa kwa mti mgumu wa kafuri wenye urefu wa sentimeta 107 (© G. Berjonneau, ART 135, Boulogne-Billancourt)*

lao Betsileo. Hawakuwahi kamwe kuunda dola. Hata hivyo, wengine kati yao walijipambanua katika historia yao, kwa mfano Watanala wa Ikongo, jabali kubwa lililoweza kufikiwa tu kwa njia za kubahatisha. Likiwa limetengwa kabisa na nyanda za juu za Betsileo, eneo la Tanala-Ikongo lilikuwa ndio bara asili ya ukanda wa pwani, iliyofikika kwa usafiri wa majini tu kama vile Sandrananta, Faraony na Mto Matitana wa Antemoro. Kwa hivyo si jambo la kushangaza kwamba Waikongo-Tanala walipokea wahamiaji kutoka pwani ya mashariki na kwamba mmoja wao, Rambo, aliyesemekana kuwa Mmanteono-Antemoro, ndiye aliyekuwa baba wa nasaba-tawala ya kienyeji ya Zafirambo, iliyotajwa kwa mara ya kwanza na watu kutoka nje mwaka 1668. Kufuatana na mapokeo, Rambo alipata ufalme kwa sababu ya maarifa yake kuhusu talasimu za tiba na *sorabe*. Rambo anakumbukwa pia kama "mtoa-sheria." Sehemu kubwa ya karne ya 18 ni ya migogoro kati ya Ikongo-Tanala na Waantemoro, migogoro ambayo ilileteleza uvamizi wa kuangamiza uliofanywa na Tanala kwenye maeneo ya bondeni mwishoni mwa karne. Mwanzoni mwa karne ya 19, mmoja wa Wazafirambo, Andriamamohotra, aliungana na Andrianampoinimerina.

Wabara, ambao ndio waliokuwa wafugaji wakuu wa Bukini, na mara nyingi wakipewa asili ya Uafrika, wanaonekana kuwa wametokea kusini kabisa mwa nchi ya Arindrano, kandokando ya mto Ihosy. Kwa zile koo kubwa za Bara, Wabara-be, Wabara-Ianstsantsa na Wabara-Imamono, ziliongezeka koo mbili ndogo zaidi, Wavinda wa Ibara ya kusini-magharibi, na Waantivondro. Kulikuwepo na vipindi viwili vya nasaba-tawala katika mikoa ya ndani ya huko kusini (ambako Ibara ndiyo iliyokuwa miliki kubwa kuliko zote): kipindi kimojawapo, ambacho hata hivyo hakijulikani sana, kiliangukia wakati wa Wamaroserana wa asili; kile cha kisasa zaidi, yaani kipindi cha Zafimaneli, kilianza kama mwaka 1650. Kutokuwepo kabisa kwa utaratibu wa kurithishana utawala, na urahisi wa wapinzani kuweza kuhama na mifugo yao yote kwenda maeneo ya malisho mazuri zaidi, bila shaka kulirahisisha kusambaratika kwa mamlaka kuanzia mwaka 1640 na kuendelea, wakati mtawala wa Wamahafaly, Dian Manhelle, alipovamia eneo hilo na kuanza kuwaweka wajumbe wa familia yake kuwa watawala wa kijanibu. Baada ya kifo chake mwaka 1653, madhuria wake, Wazafimanely, polepole walichukua mamlaka ya utawala wa Ibara, lakini si aghalabu kwa manufaa ya Ibara. Kati ya 1650 na 1680, historia ya Ibara imetawaliwa na ushindani miongoni mwa wafalme wa Zafimanely kwa malengo ya kiuchumi zaidi kuliko ya kisiasa. Bila kuwa na mfumo wa ushuru wa kawaida, Wazafimanely waliweza tu kulinda nguvu zao kwa kutafuta utajiri kupitia maamuzi ya kisheria na zaidi kwa kushambulia na kuteka ng'ombe wa majirani zao. Mzunguko huu wa wasiwasi ulivunjwa tu baada ya 1800 na mfalme Raikitroka, ambaye anastahili kuchunguzwa kwa kina zaidi.

## Madola ya mashariki na kusini: Betsimisaraka, Antemoro, Antambahoaka, Antefasy, Antesaka, Antanosy na Antandroy

Wabetismisaraka, mara nyingi wakiwa wamegawanyika baina ya "Wakaskazini" (Antavaratra) na "Wakusini" (Antatsino), na katikati yao wakiwemo Wabetanimena, waliishi kandokando ya pwani ya mashariki ya Bukini, kwa kukisia kati ya Ghuba ya Antongil na Vatomandry. Kufuatana na vyanzo vingi, *watompon-tany* wa ukanda huu hawakuwa na miungano mikubwa ya kisiasa hadi mwanzoni mwa karne ya 18, na walibakia chini ya watemi *(filohany)* ambao kwa kawaida hawakutawala zaidi ya kijiji kimoja au viwili. Waantavaratra walipendelewa na maumbile ya asili, kwani walikuwa na bandari zote, wakati ambapo pwani ya Betanimena haikuwa na bandari hata moja. Jinsi Wamaskarene walivyozidi kutegemea Bukini ya mashariki kwa maduhuli yao, udhibiti wa bandari hizi uliwaletea *mafilohany* utajiri mkubwa. Hii pia ilikuwa ni sehemu ya Bukini ambayo kati ya 1680 na 1720 ilikuwa imekaliwa sana na Wazungu, hasa Waingereza na maharamia wa Marekani. Wengi wao walioana na Waantavaratra na kuzaa watoto machotara. Kama mwaka 1694, kutokana na moja ya miungano hiyo, alizaliwa mtu mmoja aliyeitwa Ratsimilahoe ambaye mabadiliko ya kisiasa miongoni mwa Waberanimena yalimwingiza kwenye jukwaa la siasa. Kwenye mwaka 1710 Wabetanimena (wakati huo wakijulikana kama *Sicoua* - "Wasikoua"), walimchagua mfalme wa Vatomandry kuwa mtawala mkuu ambaye angewaongoza kwenda bandari za kaskazini. Ratsimilahoe, licha ya ujana wake, alifanikiwa kuwaunganisha karibu Waantavaratra wote aliposimama imara dhidi ya uvamizi wa bandari hizo.

Ratsimlahoe aliteka upya Fénérive mnamo 1712, na kurudi nyuma kwa haraka kwa Wasikoua kuvuka mashamba ya udongo mwekundu wa mfinyanzi kukawapatia jina la *Be-tani-mena* (wengi wa udongo mwekundu). Ratsimilahoe alitunga jina la Betsimisaraka (wengi wasiogawanyika) ili kusisitiza hulka ya kudumu ya muungano wao wa kisiasa, na kuwatofautisha watu wake na Wabetanimena. Alileta amani kati yake na Wabetanimena kwa kumwachia mfalme wao bandari ya Tamatave, ila hatimaye yeye mwenyewe alichaguliwa kuwa mfalme wa Wabetsimisaraka wote na kupewa jina la Ramaroumanompou (bwana wa raia wengi) kwenye mji wake mkuu wa Foulpointe. Lakini amani hii ilidumu kwa miezi sita tu na Ratsimilahoe aliichukua tena Tamatave na kumfukuzia mfalme wa Betanimena kwenye eneo lisilofikika huko kaskazini zaidi. Kisha aliingia kwenye mapatano ya urafiki na Waantatismo na Wabezanozano. Ilipofikia kwenye 1730, Ratsimilahoe alikuwa mmoja wa watemi wenye nguvu huko Bukini, akishikilia pamoja muungano wa koo na familia zilizokuwa na uhuru wa kiasi fulani. Alifanikiwa kufanya jambo hilo kwa kuwaruhusu machifu wenyeji kuendelea kujitawala, na kujiamulia wenyewe kiasi cha ushuru cha kumlipa. ama kwa kutoa watumwa, ng'ombe au mchele. Alizifidia familia za *wafilohany* waliofia vitani walipokuwa wakipigana dhidi ya Betanimena na kuruhusu Waberanimena kukomboa ndugu zao waliochukuliwa mateka wakati wa ugomvi huo. Alitenda kwa haki kubwa kwa kuruhusu Mbetsimisaraka yeyote kukata

rufaa kwake. Huku akiwa na utambuzi wa nguvu kubwa za uchenguzi zilizotishia ufalme wake, Ratsimilaho alimwoa binti pekee wa mfalme wa Iboina ili kujifungamanisha na Wavolamena na himaya ya Sakalava. Alifariki mwaka 1754, baada ya kutawala kwa miaka arobaini. Kati ya wafalme watatu waliomfuata kati ya 1755 na 1803, yule wa pili, Iavy, alifanikiwa kupata sifa kuu kama mfanyabiashara mashuhuri wa watumwa huko Bukini. Katika nusu ya pili ya karne ya 18, nchi ya Betsimisaraka ilikuja kulandana na Angola wakati wa kilele chake cha mikasa ya utumwa katika sehemu ya mwanzo ya karne ya 17.

Hakuna shaka yoyote tena kwamba jamii za Waantesaka na Waantefasy wa kusini-mashariki ya Bukini kwa pamoja zilianzishwa na wahamiaji kutoka magharibi. Waantesaka ambao jina lao linaashiria asili ya Sakalava, waliondoka Menabe na kuishia Nosipandra (baadaye Vangaindrano) ambayo ilikuja kuwa mji wao mkuu. Inaonekana kwamba uhamaji wao ulikuwa umekwisha ilipofikia miaka ya 1650. Kwa Waantefasy, mapokeo yao yanashikilia kwamba mhenga wao wa kwanza, Ndretsileo, alitoka kwenye bara la Afrika, akafika kwenye Mto wa Menarandra na kuselea Ibara. Matatizo yao na Wazafimanely yalikuwa yamefikia pabaya wakati utawala wa mjukuu wake, Ndrembolanony, ulipoanza. Alimwoa binti wa mtawala wa Antevatobe, na mmoja kati ya watoto wake wa kiume, Marofela, alibuni jina la *Antefasy* (watu wa mchangani), akimaanisha, kwa mfano huo wa mchanga, kwamba ufalme wake ungekuwa na idadi kubwa ya watu.

Bila shaka mtawala aliyekuwa mashuhuri zaidi wa Antefasy kabla ya miaka ya 1800 alikuwa Ifara ambaye aliishi Ambaky (jina la zamani la Farafangana). Ifara alijipatia ukiritimba wa biashara na merikebu za kwanza za Wazungu kutembelea pwani yake, na alikuwa na nguvu nyingi kiasi kwamba wakati mmoja alionekana kama mmiliki pekee wa mto Manampatra. Mtawala mwingine wa Zarabehava anayekumbukwa sana ni Maseba, ambaye aliwakomboa Waantefasy kutoka kwenye utawala wa muda mfupi wa Antemoro. Kulingana na vyanzo vya Antemoro, migogoro kati ya Waantemoro na Waantefasy inaweza kurudi nyuma hadi kwenye miaka ya 1680. Migogoro hiyo iliendelea hadi kwenye miaka ya 1700 lakini vita vyenyewe havikuleta suluhisho Ia mkataa.

Waantesaka walikuwa na mtazamo wa kujali mambo yao ya ndani zaidi, na walikuwa na matatizo mengi ya urithi. Mapokeo yanaonyesha kwamba mmoja wa wafalme wao wa Kizarabehava, Ratongalaza, "ama aliwaua au kuwafukuza kaka zake wote". Mjukuu wake, Lengoabo, alikuwa ndiye mfalme wa mwisho katika karne ya 18, na alipanua mipaka ya Antesaka hadi upeo wake. Historia ya Waantambahoaka na Waantemoro kwa kipindi cha karne ya 18 haifahamiki; ijapokuwa Matitana inatajwa na taarifa za Wazungu kama mojawapo ya wasafirishaji nje wakuu wa mchele na watumwa, hasa baada ya 1724.

Kuwepo na Wazungu katika nchi ya Antenosy kulihimiliwa sio tu na uhusiano uliokuwepo na Fort Dauphin, bali pia na maendeleo ya uchumi wa mashamba makubwa ya Maskarene yaliyotokea baada ya 1720, pamoja na mahitaji makubwa

yasiyotoshelezeka ya watumwa, mchele na ng'ombe. *Count* wa Modave, gavana wa Kifaransa wa awamu ya pili katika Fort Dauphin (1767-1770), aligundua idadi ya watawala wasiopungua thelathini na watano kati ya bonde la Ambolo na Mto Mandrare. Hawa walipigana kugombea watumwa na ng'ombe na kusababisha raia wao kuhama mara kwa mara. *Count* Modave, ambaye alipinga biashara ya watumwa na kuibadilisha kwa biashara halali, alitelekezwa na Wafaransa na kuishia kuwa muuza watumwa ili kulipia madeni yake na kupata watumwa wa kufanya kazi kwenye mashamba yake mwenyewe huko Ile de France (Mauritius).

Ni lazima ikumbukwe kwamba Fort Dauphin ilijengwa wakati ardhi ya Antanosy ilikuwa ndilo eneo lililokaliwa na watu wengi zaidi huko Bukini; likiwa na ziada ya mazao ya kilimo na uwezekano mkubwa wa kuwa dola la muungano. Lakini muda mfupi baada ya kushindwa kwa azima ya Modave, msafiri mmoja wa Kifaransa aliielezea Antanosy kama "nchi maskini na ya kusikitisha kuliko zote" katika kisiwa hicho, ilichokaliwa na watu wachache sana na bila rasilmali ya aina yoyote.

Antandroy, nchi ya Bukini iliyokuwa kusini zaidi kuliko zote, ilijigawa katika sehemu mbili zilizojipambanua. Huko Antandroy magharibi, Wakarimbola hawana kumbukumbu ya kuhama. Antandroy ya mashariki kwanza ilikaliwa zaidi na Wamahandrovato, ambao baadaye walimezwa na ujio mkubwa wa wahamiaji kutoka Ibara na Antanosy wakitafuta usalama kwenye eneo kavu la kusini. Inaonekana kwamba nasaba tawala ya Wazafimanara ilizuka miongoni mwa Wamahandrovato na polepole utawala wao ukakubaliwa na Wakarimbola pia. Jina la pamoja, Antandroy, lilitolewa na Wazafimanara kwa watu wote walioishi kati ya mito ya Menarandra na Mandare, na linaakisi hisia ya muungano wa kisiasa na kuashiria kuwepo kwa "Muunganiko wa Zafimanara." Ilipofikia miaka ya 1790, Wazafimanara, waliotimuliwa na mafuriko na kushindwa kuhimili mabadaliko katika miliki yao ya awali, walilazimika kukimbilia kwenye uwanda wa juu wa Manombo. Kama ilivyokuwa kwa wakazi wengine wa Bukini, kumalizika kwa karne ya 18 hakukuashiria mema kwa Waantandroy.

## *Visiwa vya Ngazija: Komoro Kuu, Anzuani, Moheli na Mayotte*

Visiwa vya Ngazija, kwa kukadiria, viko katikati ya Bukini na Afrika. Komoro Kuu *(Grande Comore)* kiko karibu zaidi na bara la Afrika, Mayotte kinakabiliana na Bukini, wakati Anzuani na Moheli vipo katikati ya funguvisiwa. Yapo maafikiano ya kawaida kwamba visiwa vya Ngazija vilikaliwa na watu kutoka bara waliozungumza Kibantu ambao hawakuwa na kiungo chochote kilichofahamika cha Uislamu, kwamba dini hii kubwa iliingizwa visiwani na Waafroshirazi na kwamba ukuu wa Waislamu wa Sunni miongoni mwa Wangazija ni lazima uhusishwe na ushindi wa kisiasa wa Waislamu wa karibuni walioingia visiwani kutoka Afrika. Katika taarifa za mapokeo zilizokusanywa na Said Ahmad 'Ali, kipindi cha kabla ya Uislamu na kile cha

Washirazi vinahusishwa na watemi wa kale *(bedja)* na warithi wao *(fani)*, ambao watoto wao wa kike *(jumbe)* baadaye walioana na wageni wa Sunni. Kronolojia ya *Wabedja* na *fani* haikuwezekana kupatikana kutokana na ukosefu wa uchunguzi wa kina wa kiakiolojia, kiisimu na kihistoria. Uchunguizi wa aina hiyo ungetusogeza mbele katika kuyaelewa upya matukio makuu matatu: uhamaji wa wazungumzaji wa Kibantu, uhamiaji wa Waindonesia katika Afrika na Bukini, na kuchipuka kwa utamaduni wenyewe wa Kiswahili.

Ni dhahiri kufika kwa Waislamu wa mwisho kulitokea sambamba na dhana (mpya) ya kisiasa. Kwa mara ya kwanza zile "Komoro nne" zilionekana kama muungano mmoja na jitihada zilifanywa kuzileta chini ya mfalme mmoja (sultani) aliyekuwa anaishi Anzuani. Huenda kipindi cha usultani kilianza ama 1506 au labda kabla ya 1400. Komoro moja au mbili huenda zilikuwa chini ya udhibiti wa wafanyabiashara kutoka Msumbiji na Kilwa kabla ya kuwasili kwa "Waarabu Waislamu, wa kabila moja na wale walioanzisha Malindi," huko Komoro Kuu. Kila mara Mlima Kartala ulipofoka, Komoro Kuu iliweza kuonekana kutoka bara la Afrika.

Nasaba tawala ya kwanza ya Ngazija inasemekana kuwa ilianzia huko Anzuani, ijapokuwa mhenga wa kwanza alihamia Komoro Kuu. Mhenga wa pili, Hassan/Hassani, mwanzilishi halisi wa miliki, anaelezewa kama mjenzi mashuhuri wa misikiti huko Anzuani. Pia anafikiriwa kuwa mwenezaji mkuu wa ibada za Kishafii, na utawala wake unahusishwa kikamilifu na upokeaji wa Uislamu wa Sunni na watu wa Anzuani. Wanawe wa kiume walikuwa na majina mawili, moja la Kibantu na jingine la Kiarabu, na walipanua miliki ya Wahassanni hadi kwenye Komoro nyinginezo, labda wakiingiza imani ya dini mpya wakati huohuo. Lakini wakati Uislamu wa Sunni ulipoenea na kuliteka eneo la Ngazija, huku ukileta mfumo mpya wa haki ulioandamana na ma-*kadi na'ib* (makadhi wa vijijini) na *majilisi* (baraza la wazee) yake, upinzani wa kisiasa ulikuja kuwa jambo la mara kwa mara na lenye kuifukusa (kuitia msisimko) jamii ya Ngazija.

Taarifa za Wazungu pamoja na mapokeo ya wenyeji yanaonyesha kwamba historia ya Ngazija inatawaliwa sio na Komoro Kuu na Mayotte, bali na Anzuani na Moheli. Kuanzia mwanzoni mwa karne ya 17, wageni binafsi kutoka sehemu mbalimbali za Ulaya wanathibitisha kwamba ni kweli Anzuani ilikuwa na maliki -malkia - aliyetambulika kama kiongozi mkuu wa Komoro zote nne. Kulingana na vyanzo hivyo hivyo vya habari, kila kisiwa kilikuwa na mtawala wake, ambaye naye alimheshimu malkia wa Anzuani kama kiongozi wa nasaba tawala. Kwa mfano, mnamo 1602 Moheli ilitawaliwa na mfalme huru Mwislamu mwenye haiba ambaye aliwashangaza wageni wa Kizungu kwa umahiri wake mkubwa wa mambo ya kibaharia, elimu yake kubwa kuhusu Afrika na Arabia, na umilisi wake wa lugha ya Kireno. Mwaka 1614, wasafiri wa Kiingereza walikuta kwamba Komoro Kuu ilikuwa imegawanywa kwa "Malodi" kumi, kwamba malkia wa Anzuani ("Sultana mzee") alikuwa "amegawa" madaraka ya Moheli kwa watoto wake wawili wa kiume, na

kwamba bandari kuu ya Moheli ilikuwa chini ya gavana wa Fombony, mtu aliyekuwa na uwezo mkubwa. Mwaka huo huo, *fani* wa zamani wa M'samudu alijitangaza mwenyewe sultani huru na bwana wa Anzuani ya kaskazini, na malkia aliyeheshimiwa hakuwa tena mdhibiti wa kisiwa chake. Ilipofikia 1626, walikuwepo watu wawili walioshindania usultani wa Moheli, dhuria wa *fani* na "Mwarabu," na wote wawili walikuwa wamewaoa mabinti wa "Sultani wa mwisho."

Isipokuwa kwa wachache, watawala wa Ngazija walitafuta uhusiano mwema na Wazungu waliofika visiwani mwao. Karibu merikebu zote za Kiingereza zilizokuwa zikielekea Mocha, Ajemi na Sarat, zilitia nanga kwenye bandari ya Anzuani, na hivyo kujenga uhusiano wa muda mrefu kati ya Waingereza na watu wa Anzuani, urafiki ambao masultani wenyeji waliurejelea na kuutumia mara kwa mara. Kwa kipindi kirefu wafanyabiashara wa Ngazija walikuwa ni watu wa kati - kati ya Bukini, Afrika na Arabia - lakini hili halimaanishi kwamba visiwa vyenyewe vinne havikuwa na biashara ya kuuza nje. Vita vilivyokuwa vinatokea ndani ya kisiwa kimoja kimoja, kama vile vya Komoro Kuu mnamo 1620, na mashambulizi ya baharini ya mara kwa mara kutoka kisiwa kimoja hadi kingine, mara nyingi vilikuwa ni kwa lengo la kuteka watumwa wa kuuza nje. Kipindi kibaya kuliko vyote ni kile cha maharamia huko magharibi mwa Bahari ya Hindi (1680-1720), wakati uporaji na uanganizaji wa miji ya Ngazija ulipokuwa ni jambo la kawaida. Ilikuwa hasa kati ya 1700 na 1720 ambapo merikebu za kijeshi za Uingereza zilipoleta msaada wa vitendo kwa Anzuani na sultani wake. Msaada huu wa kijeshi uliakisi tamaa ya Anzuani ya kutaka kupanuka na kudhibiti kikamilifu zile Komoro nyingine, na (kwa upande wa Waingereza), kupata ridhaa ya sultani ya kutowasetiri maharamia. Ilipofikia 1720 nguvu za maharamia zilikuwa zimekoma, lakini kuingilia kwa vikosi vya silaha vya Uingereza kwa niaba ya Anzuani hakukukoma.

Kwa mujibu wa Said Ahmad Ali, mnamo 1736, Anzuani ilikuwa na mfalme mpya, Sultani Ahmad, ambaye aliamini kuwa Komoro zote zilitakiwa kuwa chini ya mtawala mkuu mmoja. Utawala wake ulikuwa mrefu lakini ulikumbwa na jaribio la "kupindua serikali" mnamo 1743, vita kamili vya kisiasa baina yake na Mayotte miaka michache baadaye, na zaidi ya yote, maasi makubwa ya ndani. Wakazi asili wa Anzuani (Wawamatsaha), wakiongozwa na mtu wa kawaida mwenye kipaji kikubwa aliyeitwa Tumpa, walifanya maasi mwaka 1775 dhidi ya viongozi wa Kiarabu, wakidai usawa kamili. Wahassani, waliokuwa wakisaidiwa na platuni ya majini ya Kiingereza, hawakupata tatizo lolote kumpiga risasi Tumpa. Kifo chake kilisitisha vuguvugu ambalo lingeweza kuleta athari kubwa zaidi kwa Anzuani na zile Komoro nyingine. Hata hivyo, karne ya 18 ilipokaribia kuisha, matatizo halisi yalikuwa ndiyo yanaanza kwa Komoro zote. Msururu wa mitumbwi kutoka Bukini, ikiongozwa na Wasakalava na Wabetsimisaraka, ilianza kuvamia na kupora watumwa kutoka visiwa vyote vinne na kutishia wenyeji hadi 1825. Zaidi ya hayo, misukosuko iliyosababishwa na upanuzi wa Wamerina huko Bukini ilikuwa na madhara yasiyotarajiwa. Kufuatia kuingia kwa wingi kwa Wasakalava waliokuwa wanaikimbia

Iboina, Mayote ilianza kuzungumza Kimalagasi, na ikapata masultani wa Kimalagasi. Kusema kweli hali katika Ngazija, eneo lililokuwa kati ya Afrika na Bukini, haikuwa nzuri hata kidogo.

## *Visiwa vya Maskarene: Reunion na Mauritius*

Tofauti na Bukini na Ngazija, visiwa vya Maskarene vilivyo mashariki mwa Bukini vilibaki bila kukaliwa na watu hadi pale Wazungu walipowasili katika Bahari ya Hindi. Réunion (Bourbon) na Mauritius (Ile de France) vilikuwa vituo vya manowari vilivyomilikiwa na makampuni makubwa ya baharini. Kuanzishwa kwa uchumi wa mashamba makubwa kwenye visiwa hivi hakukuathiri tu sehemu ya mashariki ya Bukini bali pia sehemu ya mashariki na kusini-mashariki ya Afrika pamoja na pwani ya India. Baada ya 1638 Waholanzi waliingiza nguvu zao zote huko Mauritius, wakivuna mbao zake na kuanzisha biashara ya watumwa na Bukini, ila mwaka 1710 walikitelekeza kisiwa hicho. Réunion ilipata walowezi wake wa kwanza kutoka Fort Dauphin kwenye miaka ya 1646 na 1654; hawa walikuwa ni Wafaransa na Wamalagasi walioiasi Kampuni ya Kwanza ya Wafaransa ya India ya Mashariki, ambayo hata hivyo ilifanikiwa kukifanya kisiwa cha Bourbon kuwa hifadhi yake kuanzia 1664 hadi 1719. Wafaransa walikuwa wameitwaa Mauritius kutoka Réunion, na ilipofikia 1721 visiwa vyote viliingia chini ya udhibiti wa Kampuni ya Pili ya India ya Mashariki na kuendelea hivyo hadi 1767, wakati Wamaskarene walipokabidhiwa kwa utawala wa kifalme. Wakiwa wameathiriwa na msukosuko kutokana na mapinduzi ya Ufaransa, watu wa Réunion na Mauritius walianza kudai aina fulani ya utaifa wa kijanibu, ambao ulikuwa kinyume na hatua zilizokuwa zikichukuliwa na makao makuu (huko Ufaransa), kama vile ukomeshaji wa utumwa ilipofikia 1794. Mwishoni mwa vita vya Napoleon, Mauritius iliingia mikononi mwa utawala wa Waingereza kwa kudumu, na upatikanaji wa watumwa ulisitishwa kwa muda.

Karibu na mwaka 1710, Réunion na Mauritius kwa pamoja vilikuwa na wakazi kiasi cha 2,000 na kati yao theluthi moja ikiwa ni ya watumwa. Ilipofikia katikati ya karne idadi ya watu ilikuwa imeongezeka kwa asilimia 300, lakini watumwa waliunda zaidi ya theluthi mbili ya ongezeko hilo.

Ilipokaribia mwishoni mwa karne ya 18 visiwa vyote viwili vilikuwa na wakazi 120,000, idadi iliyojumuisha watumwa 94,000. Kuanzia mwanzoni mwa karne ya 18 makundi matano ya kijamii yaliweza kuonekana wazi wazi: watu weupe waliokuwa madhuria wa kizazi cha kwanza cha wakoloni, wakrioli weupe, wakrioli machotara, wageni weupe wakazi na watumwa. Walikuwepo watumwa wachache waliokuwa wamepewa uhuru wao kabla ya 1797. Hata hivyo badiliko kubwa lilitokea miongoni mwa watumwa wakati wanunuzi wa Maskarene polepole walipogeuza uelekeo wao kutoka Bukini na kuelekea Afrika na India wakitafuta vibarua wapya. Badiliko hili linaweza kuelezwa hasa kwa kuzingatia imani iliyokuweko kuwa Wamalagasi

walikuwa na tabia ya kuanzisha makoloni ya watumwa watoro. Kwa hakika, wa-*marronnage* (watumwa watoro) huko Mauritius na Réunion, kama ilivyokuwa katika sehemu nyinginezo, walikuwa ni njia ya watumwa ya kujitoa utumwani, iliyosaidiwa na mazingira ya milima na misitu.

Ijapokuwa miwa ilikuwa inalimwa huko Mauritius tangu 1639, kiwanda cha kwanza cha sukari kilianzishwa na utawala wa Mahe de Labourdonnais (1735-1746). Mauritius haikuuza sukari nje hadi baada ya kufika kwa serikali ya kifalme ya Ufaransa, ambayo ilitupilia mbali vipingamizi vilivyokuwa vimewekwa na Kampuni ya Kifaransa ya India ya Mashariki, na hivyo kufungua visiwa hivyo kwa raia wote wa Ufaransa mwishoni mwa miaka ya 1760. Kahawa ililimwa kwa mara ya kwanza huko Réunion mnamo 1715 na kuwa zao lake kuu. Ilipata mavuno yake makubwa ya mwisho katika miaka ya mwanzo ya 1740. Ilipofikia 1767, na kutokana na mashindano kutoka Antilles, kilimo cha kahawa kilikuwa katika hali ya kuporomoka kiasi kwamba wakulima wa Réunion walijiingiza katika uzalishaji wa viungo vya chakula. Katika miaka thelathini iliyofuata, mvuto wa kibiashara ulihama kutoka Atlantiki kwenda Bahari ya Hindi, visiwa vya Maskarene vikawa ndivyo kituo kikuu cha mtandao huo ulioitwa (*"route des Iles"* (barabara ya visiwani). Mauritius, ambayo katika siku za Kampuni ilikuwa ikitembelewa na zaidi ya merikebu thelathini kwa mwaka, ilishuhudia ongezeko la mara kumi la vyombo vya baharini ilipofikia 1803. Kwenye 1800, wale wachache waliobahatika katika visiwa vya Maskarene walikuwa na kiwango cha juu cha maisha kilicholingana na, au labda kupita, kile cha nchi nyingine za kikoloni.

# 29 *Historia ya jamii za Kiafrika toka mwaka 1500 hadi 1800: hitimisho*

Majina mbalimbali yanatumika kuitia kipindi cha tangu mwaka 1500 hadi mwaka 1800 katika historia ya Afrika. Vitabu vingi vya historia hukiita "enzi ya biashara ya watumwa," vikikuza mno umuhimu wa tukio hili katika historia ya bara hili. Vinashindwa kuona ukweli kwamba huko Afrika Maghariki na Kati, biashara ya watumwa ilidumu hadi mwaka 1850, na huko Afrika Mashariki ilianza mnamo karne ya kumi na tisa, tukiachilia mbali biashara ya watumwa ya awali kuelekea nchi za Kiislamu. Jina hili pia halizingatii ukweli kwamba baadhi ya sehemu za bara kama vile Afrika Kusini, hazikupata kuguswa na biashara hiyo kabisa. Wanahistoria fulani, hasa wale wafuatao fikra mamboleo za Kimarx, huona kuunganishwa kwa Afrika katika uchumi wa kibepari wa dunia uliotawaliwa na Ulaya kuwa ndio sifa kuu ya kipindi hiki na hivyo kuyatilia uzito zaidi mahusiano ya nje ya Afrika kuliko mabadiliko yake ya ndani. Wanawaonyesha watu wa Afrika kama watu wenye bahati mbaya waliolaaniwa na kani za dunia ambazo hawana uwezo wa kuzielewa au kuzidhibiti. Wanahistoria wengine huchagua miguro ya watu na kukaliwa kwa dhati kwa bara kama sifa bainishi ya kipindi hicho. Ama kwa hakika, isipokuwa kwa matukio machache, yafaa izingatiwe kwamba hapakuwepo uhamaji mkubwa barani Afrika baada ya mwaka 1500. Watafiti wengine zaidi wangependekeza kuwasilisha historia ya karne hizi tatu kama mfululizo wa maangamizi ya kiekolojia na hufikiria ukame na njaa kuwa ndio vigezo vilivyoukilia kipindi hicho.

Kila moja ya majina haya hubeba ukweli fulani, lakini hakuna hata moja linalotilia maanani uchangamani na kanindani za karne hizi tatu za historia ya Afrika. Katika sura hii ya mwisho, tutajaribu kuchopoa dhamira kuu za mabadiliko ya kihistoria ya jamii za Kiafrika katika kipindi hiki kwa kutegemeza majadiliano yetu kwenye sura mbalimbali za juzuu hili.

Hebu tuanze kwa kuuliza swali la msingi la miguro ya watu. Sehemu kubwa ya Afrika ilikuwa imekwishakaliwa na watu kufikia mwaka 1500, na kile ambacho mapokeo simulizi hukiita uhamiaji kwa hakika kilikuwa ni kupanuka kwa idadi ya watu na misogeo. Ni Afrika kaskazini mashariki tu ndiyo iliyokuwa na miguro mikubwa ya watu katika kipindi hiki, miongoni mwa Waoromo, Wasomali, Waluo, Wakaramajong, Wakalenjin, Waturkana na Wamasai (rejea Sura ya 3).

Kitu kilicho muhimu zaidi ya uhamaji ni ukweli kwamba kipindi cha kati ya mwaka 1500 na mwaka 1800 kilikuwa cha maana sana kwa miundo mikuu ya kijamii na kisiasa barani. Katika karne hizi tatu ndipo wakazi wengi wa maeneo tofauti ya Afrika walipoungana katika makundi mapana ya kijamii, kiuchumi, kidini, kitamaduni na kisiasa yanayojenga jamii za sasa za Kiafrika.

Kadri jamii za Kiafrika zilivyobadilika kuwa mbari zenye maumbile ya pekee ya kiisimu na kitamaduni, sehemu kubwa ya Afrika ilikuwa ikibadilika kutokana na mahusiano yake ya nje. Wakati mnamo mwaka 1500 jamii nyingi za Kiafrika zilikuwa hazitegmei sehemu nyingine za dunia, kufikia mwaka 1800 sehemu kubwa ya Afrika ilikuwa imekwishajumuishwa katika duru za masoko ya dunia ambayo yalikuwa yamefungamanishwa na Ulaya, Amerika na Asia. Taratibu hizi za muungamko ziliwezeshwa na kuanzishwa kwa jumuiya mpya barani, kama vile walowezi wa Kiholanzi Kusini mwa Afrika; Wareno huko Angola na katika upwa wa Mashariki, na Waturuki huko Misri na Maghrib. Jamii nyingi za Kiafrika ilibidi polepole zibadilishe namna zilivyoishi au zigure au kufanya yote mawili. Punde mahusiano ya aina mpya kabisa yalijengeka ndani na baina ya jamii yaliyobainishwa na sifa za utawalaji na utegemezi ndani ya bara na katika mfumo wa dunia ambamo Ulaya ilitawalia.

Pathe Diagne amebainisha miundo mikuu ya kiuchumi iliyochipuka katika kipindi hiki (tazama Sura ya 2). Kwa mfano, uchumi wa kiporaji ulikuwa ni matokeo ya upanukaji wa Wahispania na Wareno. Uchumi huu ulivuruga kabisa mifumo midogo midogo ya Mediterania na Bahari ya Hindi na kufukarisha maeneo ya nchi ambayo baadaye yalitumbukizwa kwenye mzozo zaidi na biashara ya watumwa. Tabaka tawala la kijeshi liliibuka lililoishi kwa uharamia na mashambulizi kwa kutumia huduma za raia na watumwa.

Kama ilivyokuwa kwa uchumi wa kiporaji, uchumi wa vituo vya biashara ulijihusisha kwa kiasi kidogo sana na ugunduzi. Sehemu mpya za biashara katika njia za bahari zilikuwa ngome badala ya kuwa vituo vya biashara au viwanda. Katika pwaa za Guinea na Afrika ya Ikweta, huko Kongo, Angola na Senegambia, Wareno walipora vitu vingi kuliko walivyonunua. Kutoka mwaka 1650 hadi mwaka 1800, uchumi wa vituo vya biashara ulitegemea biashara ya watumwa ya kuvuka Bahari ya Atlantiki. Jamii zilizoathirika na uchumi wa vituo vya biashara zilibadilishwa polepole katika karne ya kumi na saba na ya kumi na nane. Huu ulikuwa utaratibu changamani uliohusisha mabadiliko makubwa na ambao sifa yake kubwa, hasa huko Afrika Magharibi na Kati, ilikuwa ni kushamiri kwa mitandao ya biashara juu ya madola yote (tazama Sura ya 18).

Kadri madola yalivyofifia, ndivyo na matabaka-tawala kongwe ya waali yalivyofifia na tabaka la wafanyabiashara kuinukia na kushika nafasi zao au kushirikiana nao. Kwa mfano kujipenyeza kwa Wareno kusini mwa Zambezia kulidhoofisha mno nguvu za tabaka tawala la kienyeji na kuwezesha kusimikwa kwa unyonyaji wa moja kwa moja wa wakulima wadogo wadogo na mabepari wa Kireno

(rejea Sura ya 22). Maendeleo kama hayo yaliibua raia waliochanganyika damu – *Mestizos* na Wakrioli wa Kasamansi, Guinea na Sierra Leone. Machotara wa Kiafrika-Kireno na Kiingereza-Kiafrika wa huko Seirra Leone waliunda makundi ya wafanyabiashara waliokuwa wakishika nafasi ya kati baina ya merikebu kutoka Ulaya na jamii za Kiafrika za bara.

Hata katika sultani za Funj na Fur ambako masultani walidhibiti na kulinda biashara ya masafa marefu iliyowaunganisha na Misri na Bahari ya Shamu, sehemu kubwa ya biashara ilikuwa mikononi mwa wafanyabiashara wa kati wa Kisudani *(jallaba)*, waliokuwa wakopeshaji wa fedha kwa ajili ya biashara ya nje.

Hivyo kutoka hali ya kutengwa mnamo mwaka 1500, jamii mbalimbali za Afrika polepole ziliunganishwa katika uchumi wa dunia. Mara nyingi, kuunganishwa huku kuliandamana na mabadiliko makubwa ya kijamii na kisiasa.

Pamoja na kuporomoka kwa madola makubwa huko Sudan Magharibi na Afrika ya kaskazini-mashariki mwanzoni mwa kipindi chetu hiki, eneo la nchi lililodhibitiwa na madola liliongezeka katika karne hizi tatu. Kipindi hiki pia kilikuwa na mifano mingi ya kujiimarisha kisiasa kulikotokana na upanuzi na ugatishaji wa asasi za kisiasa.

Huko Afrika ya kaskazini-mashariki mathalan, ingawa karne ya kumi na sita na ya kumi na saba zilishuhudia kuporomoka kwa himaya ya Ethiopia ya Kikristo, kulikuwa na upanuzi wa himaya hii kuelekea kusini, ambao ulichochea kukua kwa madola mapya kama vile Basa, Kaffa, Sekko, Wolayta na Dauro.

Ama kuhusu Bukini, tunaona mchakato kinyume wa ugatishaji. Kufikia mwanzoni mwa karne ya kumi na saba, Bukini ilikuwa bado ina temi ndogondogo zilizojitosheleza, lakini kufikia mwishoni mwa karne hiyo, himaya ya Sakalava ilikwisha jizatiti katika sehemu ya magharibi, na falme kadhaa kujitokeza hapo kisiwani. Himaya ya Sakalava ilifikia kilele chake kwenye karne ya kumi na nane, na upwa wa mashariki uliunganika kisiasa kwa mara ya kwanza kuwa mwunganiko wa Betsimisaraka. Kufikia mwaka 1800, madola haya mawili yalikuwa yakidhoofika na dola la Imerina, ambalo awali lilikuwa dhaifu na lenye mifarakano, lilipata nguvu.

Mchakato kama huu wa kuunganika na kugatisha mamlaka ulitokea kwenye upwa wa Guinea ya Chini. Kulingana na ramani ya mwaka 1629, kulikuwa na madola na falme thelathini na nane wakati huo katika eneo hilo, zilizoanzishwa na Waga na Waakan. Kutokana na madola haya ziliibuka himaya tatu kubwa za Aowin, Denkyira na Akwamu ambazo kufikia mwaka 1750 ziliungana kuunda himaya ya Asante.

Tukio la kisiasa lililoenea zaidi katika karne hizi tatu lilikuwa ni kwa dola lililodhoofika au kuporomoka kufuatiwa na madola kadhaa madogo au na mifumo ya kiuchumi. Hivyo, huko Afrika ya Kati, falme za Kongo, Tio, Lwango na Ndongo (zilizounda Angola baadaye) zilizokuwepo katika karne ya kumi na sita, zilianza kudhoofika kuanzia mwaka 1665, na nchi zikaunganishwa kuwa nchi kubwa kwa msingi wa matakwa ya kiuchumi yaliyoletwa na biashara ya watumwa.

Katika upwa wa Guinea ya Juu, madola mengine yalirithi himaya za Songhai na

Mali. Himaya ya Grand Foul iliibuka mnamo karne ya kumi na saba kutokana na kuporomoka kwa Songhai, lakini ikaiachia nafasi himaya ya Kaarta kwenye nusu ya pili ya karne ya kumi na nane. Kote katika mwambao mzima wa Bahari ya Atlantiki, nchi zote zilizoibuka kutokana na kuchenguliwa kwa Mali ziliunganishwa na Kaabu (Gabu) kwenye karne ya kumi na saba na ya kumi na nane, na kisha na Futa Jalon kwenye karne ya kumi na nane na ya kumi na tisa. Huko katikati, uibukaji mwingine ulitokea chini ya usimamizi wa Wabambara wa Segu, na huko kusini, Wajula (Wadyula) waliunda himaya ya Kong katika karne ya kumi na nane.

Mchakato kama huo unaweza kuonekana kusini mwa Zambezia. Kuporomoka kwa Zimbabwe Kuu kulipelekea kwanza katika kuibuka kwa dola la Torwa na baadaye kwa himaya ya Mutapa mwanzoni mwa karne ya kumi na sita. Kugawanyika na kufifia kwa dola la Mutapa kulianza mwaka 1629 lakini umbo la kisiasa la Mutapa halikutoweka kabisa hadi mwaka 1917.

Katika madola mengi mapya, mifumo ya asili ya serikali na utawala iliendelezwa. Kwa mfano, Dahomey iliwakilisha wazo jipya la dola. Mtazamo wa kimapokeo, uliochukulia dola kama familia kubwa, ulifuatiwa na dhana ya dola unganifu lenye nguvu linalotawaliwa na mfalme mwenye mamlaka kamili na anayetiiwa na raia wake wote.

Katika idadi kubwa ya madola haya, yaliibuka matabaka mbalimbali ya kijamii kama vile makabaila, makundi ya kijeshi, raia wa kawaida na watumwa. Hivyo jamii ya Kanuri huko Borno ilikuwa ya matabaka mengi sana. Katika nchi ya Wahausa, kadri makabaila na wafanyabiashara walivyotajirika, uainisho wa kitabaka ulihamishiwa kwenye kiwango cha kiuchumi - kukawa na *attajirao* (matajiri) na *talakawa* (mafukara).

Tabaka la makabaila (la kitawala na kijeshi) lilipata utajiri kwa kutumia njia mbalimbali za unyonyaji. Huko Misri, mathalan, himaya ya Waturuki ilipokuwa ikififia, mapambano ya ndani baina ya vijitabaka tofauti vya kijamii yalijitokeza. Hali mbaya ya kiuchumi iliakisi sera ya ukandamizaji ambapo idadi kubwa ya watu ilidhibitiwa na kunyonywa na tabaka dogo la wenye uwezo lililoundwa na Mamluki na wapambe wao. Hali hii ya ukandamizaji ilileteleza kuibuka kwa fasihi pendwa katika lugha ya Kiarabu iliyoeleza juu ya kunyonywa kwa wakulima wadogo.

Tawala hizi za kikandamizaji ziliwafanya wakulima wadogo kuasi katika sehemu nyingi za Afrika. Kuna haja ya kutafiti haraka matukio haya ya uasi ya wakulima wadogo katika karne ya kumi na saba na ya kumi na nane.

## *Biashara ya watumwa*

Je, biashara ya Watumwa ipewe umuhimu gani katika historia ya Afrika? Kwa maneno mengine tunavutiwa na nini, kama wanahistoria wa Kiafrika, kwenye biashara ya watumwa? Mataifa yote yamewahi kufanywa watumwa hapo kale: na neno lenyewe katika lugha ya Kiingereza linatokana na neno *slavs* lenye maana ya

watu wa Ulaya Mashariki. Lakini makundi mengine yamepata njia ya kuondosha wazo la utumwa katika utambuzi wao wa kihistoria. Waafrika hukuza mno umuhimu wa utumwa kwa kiasi kwamba hata neno "mtumwa" linachukuliwa kuwa karibu sawa na "Mwafrika." Kama D.B. Davis alivyokwisha kuonyesha waziwazi kwenye vitabu vyake, utumwa ni jambo muhimu katika itikadi ya dunia ya sasa ya nchi za Magharibi ambalo ni lazima tujaribu kulielewa.

Katika Sura ya 4, J.E. Inikori anajaribu kupima dhima ya utumwa wa watu weusi katika maendeleo ya kiuchumi ya nchi za Magharibi. Hili ni swali jingine la msingi ambalo ni lazima lichunguzwe kwa wazi na kwa undani. Marx na Engels wanadai kwamba ingawa utumwa mpaka sasa na daima umekuwa uovu mkubwa, bado umekuwa muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na hivyo ya kijamii. Bila utumwa, wanadai, kusingekuwa na ustaarabu wa Kiyunani wala Kirumi. Inikori anadai kwamba utumwa Afrika ulikuwa muhimu kwa uendelezaji wa mfumo wa kiuchumi, kijografia na kisiasa ulioelekezwa kwenye Bahari ya Atlantiki, na kwa ujenzi wa viwanda huko Ulaya Magharibi. Kwa upande mwingine, Fernand Braudel amewasilisha, katika majuzuu yake matatu ya *Civilization and Capitalism* (Ustaarabu na Ubepari), picha tofauti ya kuibuka kwa ubepari wa Ulaya hadi kuwa wenye nguvu kubwa duniani. Akianza na uchumi wa kimapokeo wa kujikimu kwa wakulima wadogo kupitia kwenye masoko, anaeleza jinsi hatimaye wenye mabenki na wafanyabiashara wachache walivyoweza, kwa kukiritimba biashara na kupata faida kubwa, kueneza nguvu iliyokuwa ikiongezeka ya ubepari wa Ulaya. Dhima ya utumwa wa Afrika katika mdahalo huu inahitaji kutathminiwa upya kabisa.

Katika Sura ya 5, J.E. Harris anauliza swali jingine muhimu kuhusu utumwa. Kutokana na ushahidi wote uliopo, ni wazi kwamba udhalilishaji wa Waafrika ulizidi kati ya mwaka 1500 na mwaka 1800 kutokana na kuongezeka kwa utumwa kuanzia mwaka 1619. Hata hivyo, ni biashara ya watumwa kati ya mabara, kuliko kitu kingine chochote, iliyowasambaza watu weusi duniani kote. Biashara hii ilisababisha diaspora (mtawanyiko) kubwa ya Waafrika, hasa katika Amerika na Karibian. Hapa ndipo mapambano ya kuwakomboa watu weusi yalikoanzia; mapambano ambayo ndiyo yalikuwa msingi wa Vuguvugu la Waafrika Wote *(Pan-African Movement)* kunako karne ya kumi na tisa na ya ishirini.

## *Kuingizwa kwa mazao mapya ya chakula*

Kuingizwa kwa mazao mapya ya chakula kutoka Amerika kumechukuliwa na waandishi wengi kama hali chanya ya biashara ya kuvuka Bahari ya Atlantiki. Wengine wamesisitiza kuwa mazao haya, yaliyopelekea kubadilika kwa mlo, yaliboresha afya ya Waafrika na hivyo kuchangia katika ongezeko la idadi ya watu. Lakini, kama alivyohoji M'Bokolo, athari za mabadiliko haya katika kilimo kwa Waafrika ni ngumu kuzifasiri. Anataja, mathalan, kwamba muhogo una thamani ndogo ya lishe na watu walioutegemea mno kama Watio na Wambosi, walisakamwa na utapiamlo mkali.

Mielekeo ya idadi ya watu mnamo karne ya kumi na saba na ya kumi na nane ni migumu kuimaizi kwa sababu kipindi hiki, ambapo biashara ya watumwa ilifikia kilele chake, kilihusika pia na kuingia barani Afrika kwa magonjwa mapya kama ndui, ambayo yalitokea kuwa mabaa ya mara kwa mara.

Hata hivyo, jambo lililo la hakika ni kwamba mazao mapya kutoka Amerika na Asia yaliyoingizwa na Wazungu katika maeneo mbalimbali ya Afrika kati ya mwaka 1500 na 1800, hasa mahindi mihogo, karanga, aina mbalimbali za maghimbi, viazi vitamu, matunda ya jamii ya machungwa, malimao na ndimu, nyanya, vitunguu na tumbaku, yalipanua uchumi wa kilimo barani. Ada ya sasa ya Waafrika kutegemea mno mahindi na mihogo kama vyakula vyao vikuu ilianza wakati huo.

Kwa mujibu wa M'Bokolo, kijamii, mapinduzi haya ya kilimo yalichangia sambamba na maendeleo ya biashara katika kuanzisha mgawano mpya wa kazi. Wanaume polepole waliwaachia wanawake na watumwa kazi nyingi za kilimo, wao wakipendelea zaidi biashara ambayo ilikuwa na faida kubwa. Kwa hiyo kuendelezwa kwa utumwa wa nyumbani na namna nyingine za utegemezi kulikuwa matokeo ya moja kwa moja ya mabadiliko haya katika kilimo (tazama Sura ya 18).

## *Maangamizi ya kiekolojia*

Majaribio yamekwisha kufanyika ya kuonyesha mahusiano thabiti kati ya vipindi vya ukame kama vile vinavyojadiliwa hapa na matukio makubwa ya kihistoria. Changanuzi hizi zinaelekea kuyapatia umuhimu mazingira kiasi kwamba Waafrika huonekana tu kama waathiriwa wa majanga ya asili wasiokuwa na uwezo wowote. Hakuna mahali popote ambako wanahistoria wanajadili hatua ambazo zimechukuliwa na Waafrika kukabiliana na madhara ya ukame wala jinsi ukame unavyoathiri na kuchangia kwenye mabadiliko katika mifumo ya uzalishaji na usambazaji, kuongezeka kwa thamani ya mazao ya vyakula na uendelezaji wa mbinu za kuhifadhi chakula.

Suala la ukame na njaa nalo huhusiana na suala kubwa la ufanisi wa kilimo cha Kiafrika katika kipindi cha kabla ya ukoloni. Kama anavyoonyesha Jan Vansina katika Sura ya 3, kipindi cha tangu mwaka 1500 hadi mwaka 1800 kilihusika na kuzuka kwa mbinu nyingi katika kutumia ardhi ambazo zilihimili msongamano mkubwa wa idadi ya watu. Katika sehemu nyingi za Afrika, mbinu za hali ya juu \za kilimo kama vile matuta ya mkingamo, mbadilishano wa mimea, mbolea ya majani, kilimo mchanganyiko na kilimo cha kwenye kinamasi zilitumika. Mada hizi zinahitaji kuzingatiwa zaidi na wanahistoria kuliko maoni ya jumla kuhusu njaa na ukame barani Afrika.

## *Ukristo na Uislamu*

Kipindi cha tangu mwaka 1500 hadi mwaka 1800, kilishuhudia kufifia kwa Ukristo barani Afrika, hasa huko Ethiopia, katika pwani ya mashariki na kwa kiasi kidogo

huko Kongo. Uislamu, kwa upande mwingine ulienea zaidi huko Afrika Magharibi, Sudan, Ethiopia na katika pwani ya mashariki.

Kwa mfano, katika pwani ya Guinea ya Chini, Ukristo ulimgizwa huko na Waholanzi na Waingereza. Walianza kwa kuanzisha shule za msingi katika ngome zao huko Cape Coast, El- Mina na Akkra. Baadaye, katika miaka ya 1750, wamisionari walitumwa Cape Coast na Chama cha Kutangaza Injili. Aidha, baadhi ya waumini wapya walitumwa ng'ambo kujipatia elimu zaidi na wengi wao walirudi nyumbani wakiwa walimu na wamisionari. Hivyo, msingi kwa ajili ya mapinduzi ya Kikristo yaliyokuja kutokea Afrika Magharibi katika karne ya kumi na tisa, uliwekwa katika kipindi hiki.

Huko Kongo, Ukristo uliingizwa na Wareno wakati wa utawala wa Alfonso wa I (1506-1545). Chini ya maelekezo ya mwanaye Henrique ambaye aliwekwa wakfu kama askofu huko Rumi, Mfalme huyo aliufanya Ukatoliki kuwa dini ya dola. Kwa kiasi kikubwa, dini hii ilikuwa ya waungwana wa mjini na uongozi wa kidini ulibakia kuwa wa Kireno. Lakini kutoka mwaka 1645 hadi mwaka 1700, wamisionari wa Kiitalia walianza kuwaongoa watu, hasa katika maeneo ya vijijini (tazama Sura ya 19).

Ukristo na Uislamu katika kipindi hiki zilikuwa ni imani za mseto. Kwa mfano, huko Kongo, Ukristo uliishi pamoja chanjari na dini za asili. Hata hivyo, majaribio yalifanywa kuunda makanisa huru. Huko Kongo, majaribio ya awali ya kuanzisha kanisa la kienyeji yalianza katika miaka ya 1630 na kufikia kilele chake mnamo mwaka 1704, wakati ambapo Dona Beatrice Kimpa Vita alianza kuhubiri Ukristo uliorekebishwa uliojulikana kama *Uantonia* uliowakana wamisionari na watu weupe. Kuanzia wakati huo, Ukatoliki wa kienyeji ulitapakaa Kongo.

Sasa tukiugeukia Uislamu, ni dhahiri kwamba upanuzi wake barani Afrika ni dhamira muhimu ya kipindi cha mwaka 1500 hadi mwaka 1800. Kwa mfano, katika pwani ya Guinea ya Chini, wafanyabiashara wa Kimande na wa Kihausa waliingiza Uislamu. Dini hiyo ilienea kwenye njia za biashara za kaskazini hadi kufika Asante na Baule kwenye miaka ya 1750. Kufikia mwaka 1800, Kumasi ilikuwa na makazi ya Kiislamu yaliyostawi, yenye chuo cha Kurani. Katika pwani ya Guinea ya Juu, Wafulbe na Wamande walihusika na uenezaji wa Uislamu. Hawa waliunda ushirikiano wa kidini wa Kifulbe na Kimalinke si tu kwa ajili ya kuwaongoa watu wa eneo hilo bali pia kwa ajili ya kuwatumikisha. Hivyo, kuenea kwa Uislamu kulihusishwa na nguvu za kisiasa katika maeneo mengi ya Afrika, kama hali katika Senegambia inavyoonyesha wazi. Hapa ukinzano kati ya uongozi wa Kiislamu na tawala za *ceddo* (au kiongozi wa vita) ndio unajenga usuli wa historia ya eneo. Huko Sudan, usilimishaji wa kaskazini ya nchi uliunda mpaka wa kiitakadi kati ya kusini na kaskazini mwa Sudan ambao bado unaonekana sana.

Kipindi hiki kilishuhudia uanzishwaji na upanuzi wa madola mawili ya Kiislamu katika nyika, yaani Sultani za Funj na Fur. Katika karne za kumi na nane na kumi na tisa, Uislamu uliendelea kuenea huko katika falme za Bambara, Mossi, Kong na

Gwirika, kupitia kwa wafanyabiashara, viongozi wa dini na hata kwa mabavu. Utaratibu kama huo wa upanuzi wa Uislamu unaweza kuonekana katika nchi ya Wahausa na huko Borno.

Mbali na ueneaji wa kijiografia wa Uislamu barani Afrika wakati huo, imani kali ya Kiislamu ilikuwa kipengele muhimu katika maeneo mengi. Kwa mfano, kulikuwa na harakati ya Nasir Al-Din iliyoanza huko Mauritania na kisha kuenea kuelekea kusini. Nia yake kwa kiasi ilikuwa ni masuala ya kiuchumi (ikitaka kudhibiti biashara ya nafaka na watumwa) na kwa kiasi mambo ya dini (kusafisha na kubadilisha Uislamu kwa kufanya uongozi wa dini ushike nafasi ya utawala dhalimu). Mwelekeo wa mabadiliko ya aina hiyo unaweza kuonekana miongoni mwa Waislamu katika nchi ya Wahausa, hasa katika karne ya kumi na nane. Jumuiya ya wanazuoni wa Kiislamu wenye usuli unaofanana wa kisiasa, kiuchumi na kidini, ilikua katika vituo mbalimbali na ikaanza kukosoa utawala uliowakilishwa na makabaila. Kadri utawala wa makabaila ulivyozidi kuwa wa kikandamizaji, ndivyo wanazuoni walivyoushambulia. Huu ndio usuli kwa jihadi ya karne ya kumi na tisa.

Kutokana na ukandamizaji wa wakulima wadogo wa Kiafrika uliofanywa na waali wa vijijini na mijini, hasa huko Sudan Magharibi, eneo la Niger na Chad, Misri, Sahara, Maghrib, Ethiopia na Kongo, viongozi wa Kiislamu na wa vuguvugu la kimasihi la Kikristo waliweza, kwa urahisi, kupata wafuasi wengi miongoni mwa wakulima wadogo.

Mwisho, yafaa izingatiwe kwamba Waafrika waliutazama Uislamu na Ukristo kimseto. Walipokea Uislamu hali wakati huo huo wakibakia kuwa waaminifu kwa dini zao za jadi. Dini hizi changamani baadaye zilikua pamoja na Ukristo barani Afrika na katika ibada za Waafrika wa Amerika huko Brazil, Haiti na Kuba (tazama Sura ya 12).

# *BIBLIOGRAFIA*

Wachapishaji wanapenda kueleza kuwa, ingawa kila jitahada imefanyika kuhakikisha kuwa bibliografia hii inakamilishwa kwa makini, makosa kadhaa yanaweza kujitokeza kutokana na ugumu na 'umataifa wa kazi yenyewe.


**Abbebe, B.** (1971) *Evolution de la propriété foncière au Choa* (Ethiopia) Paris: Imprimerie National et Librarie Orientaliste, P. Geuthner)

**Abdallah, Y. B.** (1919) *The Yaos* (ilipangwa, kuhaririwa na kutafsiriwa na M. Sanderson, Zomba; Tol. 2, London: Frank. Cass, 1973)

**Abitbol, M.** (1979) *Tambouctou et les Arma de la conquête marocaine du Soudan nigérien en 1591 à l'hégémonie de l'Empire du Maçina en 1833* (Paris: Maisonneuve & Larose), kur. 297

**Abraham, D. P.** (1969) 'The roles of Chiminuka and the Mhondoro cults in Shona political history', kwenye F. Stokes na R. Brown (wah.) kur. 28, 46

**Abun-Nasri, J. M.** (1975) A History of the Maghrib (Tol. 2, Cambridge: CUP), kur. 422

**Adams W. Y.** (1977) *Nubia - Corridor to Africa* ) London: Allen Lane), kur.797

**Ajayi, J. F. A** (mh.) (1989) *General History of Africa,* Juz. VI (Paris/Oxford/Berkeley: UNESCO/Heinemann/University of California Press, kur. 861.

**Ajayi, J. F. A.** na **Espie, J.** (wah.) 1965*) A Thousand Years of West African History* (Ibadan/ London: IUP/Nelson), kur. 543

**Ajayi, J. F. A. na Crowder, M.** (1971) *History of West Africa* (London: Longman; Tol. 2, 1976).

**Akinjogbin, I. A.** (1967) *Dahomey and* (wah.) *its Neighbours, 1708-1818* (Cambridge: CUP), kur. 234

**Alexandre, P.** na **Binet, J.** (1958) *Le groupe dit pahouin (Fang-Boulou-Beti)* (London/Paris: IAI/ PUF), kur. 152

**Alkali, M. B.** (1969) 'A Hausa community in crisis: Kebbi in the nineteenth century' (tasnifu ya MA, Ahmadu Bello, Chuo Kikuu cha Zaria)

**Allan, J.** (1965) *The African Husbandsmon* (London: Oliver na Boyd)

**Allbridge, T.J.** (1901) *The Sherbro and its Hinterland* (London: Macmillan), kur. 356

**Alpers, E. A.** (1975) *Ivory and Slaves in East Central Africa to the later Nineteenth Century* (London: Heinemann)

**Anquandab, J.** (1982) *Rediscovering Ghana's Past* (London: Longman), kur. 161

**Anttila, R.** (1972) *An Introduction to Historical and Comparative Linguistics* (New York: Macmillan) kur. 438

**Aptheker, H.** (1944) *American Negro Slave Revolts* (Chapa 2, New York: Columbia, University Press) kur. 409

**Arhin, K.** (1979) *West African Traders in Ghana in the Nineteenth and Twentieth Centuries*

(London: Longman), kur.146

**Arhin, K.** na **Goody, J.** (1965) *Ashanti and the Northwest* (Legon: Institute of African Studies, Chuo Kikuu cha Ghana)

**Atkins, G.** (mh. (1972) *Manding: Focus on an African Civilization* (London: SOAS)

**Austen, R. A.** (1968) *Northwest Tanzania under German and British Rule, 1889-1939* (New Haven:YUP)

**Avaro, J. A.** (1981) *Un peuple gabonais à l'aube de la colonisation: Le Bas Ogowe au XIXe siécle* (Paris: Karthala/CRA), kur. 290

**Axelson, E.** (1940) *South-East Africa, 1488-1530* (London: Longman) kur. 360

**Axelson, E.** (1973) *The Portuguese in South-East Africa, 1488-1600* ( Johannesburg, WUP), kur 276

**Barber, W.J.**(1964) *The Economy of British Central Africa: a Case Study of Economic Developmen in a Dualisti Society* (Lodnon: OUP, kur. 271

**Barry, B.** (1972) *Le royaume du Waalo: Le Sénégal avant la conquéte* (Paris: Maspéro), kur. 393

**Bastide, R.** (1971) *Les Amériques noires: les civilisations africaines dans le Nouveau Monde (Paris:* Payot) taf. *as African Civilizations in the New World* (London: Hurst,) kur. 232

**Bauer, P. T.** (1981) *Equality, the Third World and Economic Delusion* (London: George Weidenfeld na Nicolson)

**Behrens, C.** (1974) *Les Kroumen de la côte occidentale d'Afrique* (Talence: CNRS, Centre d'études de geographie tropicale), kur. 243.

**Bernstein, H.** (mh.) (1973) *Underdevelopment and Development: The Third World Today* (New York: Penguin Books).

**Berque, J.** (1982) *Ulemas, fondateurs, insurgés du Maghreb* (Paris: La bibliothèque arabe, Sindbad).

**Betoto, C.** (mh.) (1950) *Histoire de la royauté sakalava* (Paris: Ecole nationale de la France d'Outre-mer, typescript), kur. 1-32.

**Bhila, H. H. K.** (1982) *Trade and Politics in a Shona Kingdom. The Manyika and their Portuguese and African Neighbours, 1575-1902* (London: Longman).

**Binger, L.G.** (1982) *Du Niger au golfe de Guineé par le pays de Kong et le Mossi 1887-1889* (Juz. Paris: Hachette).

**Biobaku, S.O.** (mh.) (1973) *Sources of Yoruba History* (Oxford: Clarendon Press).

**Birmingham, D.** (1981) *Central Africa to 1870: Zambezia, Zaire and the South Atlantic* (Cambridge: CUP).

**Birmingham, D.** na **Gray, R.** (wah.) (1970) *Pre-colonial African Trade: Essays on Trade in Central and Eastern Africa before 1900* (London: OUP) kur. 308.

**Birmingham, D.** na **Martin, P.** (wah.) (1983) *History of Central Africa,* Juz.1 (London: Institute of Commonwealth Studies), kur. 314.

**Blackhurn, R.H.** (1982) *Kenya's peoples: Okiek* (London: Evants).

**Blake J. W.** (1942) *Europeans in West Africa, 1450-1560* (taf. na mh. J.W. Blake, London: kwa the Hakluyt Society, Tol. 2 Juz.2).

**Boahen, A.A.** (1964) *Britain, the Sahara and the Western Sudan, 1788-1861* (Oxford: Clarendon Press, Oxford Studies in African Affairs) , kur. 268.

**Boahen, A.A.** (1966) *Topics in West African History* (London: Longman).

**Bosman, W.** (1967) *A New and Accurate Description of the Coast of Guinea* (London: Frank Cass, reprint of 1705 Tol. 1, utangulizi na J.R. Willis).

**Boulègue, J.** (1968) *'La Sénégambie du milieu du Xve siècle au début du XVIIe siècle'* (PhD) tasnifu, 3[rd] cycle, Chuo Kikuu cha Paris).
**Bouquiaux, L.** na **Hyman, L.** (wah.) (1980) *L'expansion bantoue* (Juz.3 Paris: SELAF).
**Bovil, E. W.** (1958) *The Golden Trade of the Moors* (London: OUP, kur. 281, Tol. 2 (mh.) 1968, kur. 293 London: OUP).
**Boxer, C. R.** (1963) *Race Relation in the Portuguese Colonial Empire*, 1415-1825 (Oxford: Clarendon Press), kur. 136.
**Boxer, C. R.** (1969) *The Portuguese Seaborne Empire* (London: Hutchinson).
**Braudel, F.** (1981) *The Structure of Everyday Life: the Limits of the Possible* (taf. na kud. na S. Reynolds, London).
**Braudel, F.** (1984) *Civilization and Capitalism* (Juz.3, New York: Harper & Row).
**Burnham, P.** (1980) *Opportunity and Constraint in a Savanna Society* (London: Academic Press), uk. 324.
**Bynon, T.** (1977) *Historical Linguistics* (Cambridge: CUP) kur. 301.
**Cà da mosto, A da** (1937) *The Voyages of Cadamosto and Other Documents on Western Africa in the Second Half of the Fifteenth Century* (taf. na mh. G.R. Crone, London: Hakluyt Society), uk. 159.
**Caillié, R.** (1828) *Journal d'un voyage à Tomboucou et à Jenne* (Paris: Imprimerie Royale).
**Cairns, T.** (1971) *Barbarians, Christians and Muslims* (Cambridge: CUP).
**Calonne-Beaufaict, A. de** (1921) *Azande; introduction à une ethnographie générale des bassins de l'ubangi-Uele et de l'Aruwimi* (Brussels: M. Lamertin).
**Capron, J.** (1973) *Communautés villageoises bwa* (Mali, Haute-Volta) (Paris: Institut d'ethnologie, Mémoire na. 9), uk. 379.
**Carrette, E.** (1844) *Recherches sur la géographie et le commerce de l'Algérie méridionale* (Paris: Sciences historiques et géographiques).
**Castries, H. de** (1905-36) *Les sources inédites de l'histoire du Maroc de 1530 à 1845* (Juz. 18, Paris: Paul Geuthner).
**Centre de Civilisation burundaise** (mh.) (1981) *La Civilisation ancienne des peuples des Grands Lacs* (Paris: Karthala), kur. 495.
**Chaunu, H.** na **Chaunu, P.** (1955) *Séville et l'Atlantique, 1504-1650* (Juz. 11, Paris: Ecole des Hautes études).
**Chittick, H. N.** na **Rotberg, R.I.** (wah.) (1975) *East Africa and the Orient: Cultural Synthesis in the Pre-Colonial Times* (New York: Africana Publishing Company), kur. 343.
**Chrétien, J. P. (1977)** 'Les deux visages de Cham: points de vue français du XIXe siècle sur les races africaines d'après l'exemple de l'Afrique orientale', kwenye Guiral na E. Temime (wah.) *L'idée de race dans la pensée politique française contemporaine* (Paris: Editions du CNRS), kur. 171-99.
**Chrétien, J. P.** (mh.) (1983) *Histoire rurale de l'Afrique des Grands Lacs* (Paris: AFERA-Karthala), kur. 285.
**Cissoko, S. M.** (1968) *Histoire de l'Afrique occidentale* (Paris: PA), kur. 233.
**Clérici, M. A.** (1962) *Histoire de la Côte d'Ivoire* (Abidjan: CEDA).
**Coben, R.** (1970) 'Incorporation in Bornu', kwenye R. Cohen na J. Middleton (wah.), *From tribe to Nation in Africa* (Scranton: Chandler Int. Co.), kur.150-74.
**Commissariat, M. S.** (1957) *A History of Gujarat* (Calcutta).
**Cook, S.F.** na **Borah, W.** (1971-74) *Essays in population history, Mexico and the Caribbean* (Juz.2, Berkeley: UCP).

**Cornevin, R.** (1964) *Note sur l'histoire de Sansanné Mango* (London, Survey on African Chronology).

**Coupez,** A. na **Kamanzi, T.** (1962) *Récits historiques du Rwanda* (Tervuren: MRAC), kur. 327.

**Courtois, C.** (1955) *Les Vandales et l'Afrique* (Algiers: Arts et Métiers Graphiques), kur. 441.

**Crosby, C. A.** (1980) *Historical Dictionary of Malawi* (New York: Scarecrow Press), kur.169.

**Cruickshank, B.** (1853) *Eighteen years on the Gold Coast of Africa* (Juz. 2, London: Hurst na Blackett).

**Cuoq, J.** M. (1975) *Recueil des sources arabes concernant l'Afrique occidentale du VIIIe au XVIe siècle (Bilād al-Sūdān)* (Paris: editions du CNRS), kur. 490.

**Curtin P.** D. (mh.) (1967) Africa Remembered: Narratives by West Africans From the Era of the Slave Trade (Madison: UWP), kur.363.

**Curtin P.** D. (1969) *The Atlantic Slave Trade: A Census* (Madison: UWP), kur. 338.

**Curtin P.** D., **Feierman, S., Thompson, L.** na **Vansina, J.** (1978) *African History* (Boston/Toronto: Little Brown Company), kur. 612.

**Cuvelier, J.** na **Jadin, L.** (1954) *L'ancien royaume du Congo d'après les archives romaines, 1518-1640* (Brussels: ARSOM).

**Dampierre, E. de** (1968) *Un ancien royaume Bandia du Haut-Oubangui* (Paris: Plon, Recherches en sciences humaines, 24), kur. 601.

**Dantzig, A. van** (1978) *The Dutch and the Guinea Coast, 1674-1742: A Collection of Documents from the General State Archives at The Hague* (Accra: GASS), kur. 375.

**Dapper, O.** (1686) *Naukeurige Beschrijvinge der Afrikaensche gewestem van Egypten, Barbaryen, Libyen Biledulgerid...* (Amsterdam: Van Meurs); 1670 taf. ya Kiingereza, J. Ogilby, *Africa: Being an Accurate Description of the Regions of Aegypt, Barbary, Libya*, etc. (London; 1670 German taf. Beschreibung von Afrika... (Amsterdam: Van Meurs); 1686 taf.ya Kifaransa, *Description de l'Afrique...* (Amsterdam: Wolfgang, Waesberge, et al.).

**D'Arianoff, A.** (1952) *Histoire des Bagesera, souverains du Gisaka* (Brussels: Institut royal colonial belge), kur. 138.

**Davidson, B.** (1965) *The Growth of African Civilisation: A History of West Africa, 1000-1800* (London: Longmans), kur. 320.

**Davis, D.B.** (1984) *Slavery and Human Progress* (New York: OUP), kur. 374.

**Debourou, D.** M. (1979) *Commerçants et chefs de l'ancien Borgou, des origines à 1936* (Paris: Université de Paris 1, CRA).

**Debrunner, H. W.** (1965) *The Church in Togo: A Church Between Colonial Powers* (London: Lutterworth), kur. 368.

**Delafosse,** M. (1912) *Le Haut-Sénégal-Niger (Soudan français)* (Juz. 3, Paris: Larose).

**Delcourt, A.** (1952) *La France et les établissements français du Sénégal entre 1713 et 1763* (Dakar: Mémoires de l'IFAN No. 17), kur. 432.

**Denoon, D.** (1983) *Settler Capitalism: The Dynamics of Dependent in the Southern Hemisphere* (Oxford).

**Deschamps,** H. (1949/1972) *Les Pirates à Madagascar aux XVIIe siècles* (Tol. 2 1972, Paris: Berger-Levrault), Tol. I, kur. 244.

**Deschamps,** H. (1961/1965) *Histoire de Madagascar* (tol. 2 na 3, Paris: Berger-Levrault, Monde d'Outre-mer, Série Histoire) kur. 348.

**Deschamps,** H. na **Vianès, S.** (1959) *Les Malgaches du sud-est* (Paris: PUF), kur. 118.

**Diagne, P.** (1967) *Pouvoir politique traditionnel en Afrique occidentale: essai sur les institutions politiques Précoloniales* (Paris: PA), kur. 249.

**Diallo, T.** (1972) *Les institutions politiques du Fouta Djalon au XIXe siécle* (Dakar: IFAN, Initiations et études africaines), kur. 276.

**Dickson, K. B.** (1969) *A Historical Geography of Ghana* (Cambridge: CUP), kur. 379.

**Dike, K. O.** (1956) *Trade and Politics in the Niger Delta, 1830-1885: An Introduction to the Economic and Political History of Nigeria* (Oxford: Clarendon Press, Oxford Studies in African Affairs), kur. 250.

**Diop, A. B.** (1981) *La Société wolof, tradition et changement: les systèms d'inégalité et de domination* (Paris: Karthala), kur. 355.

**Diouf, M.** (1980) 'Le Kajoor au XIXe siècle et la conquète coloniale' (tasnifu ya PhD, Paris, Chuo Kikuu cha Paris).

**Dramani-Issifou, Z.** (1982) *L'Afrique noire dans les relations internationales au XVIe siècle: analyse de la crise entre le Maroc et le Sonrhai* (Paris: karthala), kur. 257.

**Dumestre, G.** (1974/1980) *La geste de Ségou* (Paris: A Colin) (Tol. 2, 1980); Tol. 1, kur. 579.

**Dunn, R. S.** (1972) *Sugar and Slaves: The Rise of the Planter Class in the English West Indies 1624-1713* (New York: Chapel Hill, UNCP).

**Dupire, M.** (1962) *Peuls nomades* (Paris: Institut d'ethnologie), kur. 336.

**Dupré, G.** (1982) *Un ordre et sa destruction* (Paris: ORSTOM), kur. 446.

**Ehret, C.** (1971) *Southern Nilotic History: Linguistic Approaches to the Study of the Past* (Evanston: NUP), kur. 200.

**Ehret, C.** na **Posnansky, M.** (wah.) (1982) *The Archaeological and Linguistic Reconstruction of African History* (Berkely: UCP), kur. 299.

**Evans-Pritchard, E. E.** (1940) The Nuer (Oxford: OUP), kur. 271.

**Evans-Pritchard E. E.** (1971) *The Azande: History and Political Institutions* (Oxford: Clarendon Press), kur. 444.

**Eyongetah, T.** na **Brain, R.** (1974) *A History of the Cameroon* (London: Longman), kur. 192.

**Equiauo, Olaudah** (1967) *Equiano's Travels*, (mh.) P. Edwards (London: Heinemann African Writers Series).

**Fage, J. D.** (1969) *A History of West Africa: An Introductory Survey* (Tol. 4 Cambridge: CUP), kur. 239, (chapisho la awali publ. As *An Introduction to the History of West Africa).*

**Fage, J. D.** na **Oliver, R.A.** (wah.) (1977) *The Cambridge History of Africa*, Juz. 3 (Cambridge: CUP), kur. 803.

**Farb, P.** (1969) *Man's Rise to Civilisation* (New York: Datton), kur. 332.

**Feierman, S.** (1974) *The Shambaa Kingdom: A History* (Madison: UWP), kur. 235.

**File, N.** na **Power, C.** (1981) *Black Settlers in Britain, 1555-1958* (London: Heinemann Educational Books).

**Fisher, A. G. B.** na **Fisher, H. G.** (1970) *Slavery and Muslim Society in Africa* (London: C. Hurst), kur. 182.

**Al-Fishtali, 'Abd al-Aziz** (1964) *Manahil al-Safia fi Akhbar al-Muluk al-Shurafa* (Rabat: Gunum Allan).

**Flint, J. E.** (mh.) (1976) *The Cambridge History of Africa*, Juz. 5 (Cambridge: CUP).

**Forde, C. D.** na **Jones, G. I.** (1950/1962) *The Ibo and Ibibio-speaking Peoples of South-Eastern Nigeria* (London: IAI, Ethnographic Survey of Africa, Part III), kur. 94.

**Forde, C. D.** na **Kaberry, P. M.** (wah.) (1967) *West African Kingdoms in the Nineteenth Century* (London:IAI/OUP), kur. 289.

**Forde, C. D.** (mh.) (1956) *Efik Traders of Old Calabar* (London: OUP).

**Fortes, M.** (1940) 'The political system of the Tallensi of the Northern Territories of the Gold coast' kwenye M. Fortes na E.E. Evans-Pritchard (wah.), *African Political Systems* (London: OUP), kur. 239-71.

**Franklin, J. H.** (1967) *From Slavery to Freedom: A History of American Negroes* (chapisho la kwanza 1956) (New York: Knopf), kur. 686.

**Freeman-Grenville, G. S. P.** (1962a) *The Medieval History of the Tanganyika Coast* (Oxford: Clarendon Press), kur. 238 (Tol. 2 1966), kur. 314.

**Freeman-Grenville, G. S. P.** (1962b) *The East African Coast: Select Documents from the First to Earlier Nineteenth Century* (Oxford: Clarendon Press), kur. 314.

**Freeman-Grenville, G. S. P.** (1963) 'The coast, 1498-1840', kwenye R. Oliver na G. Mathew (wah.), kur. 129-68.

**Freeman-Grenville, G. S. P.** (1965) *The French at Kilwa Island: An Episode in Eighteenth-Century East African History* (Oxford, Clarendon Press), kur. 243.

**Freeman-Grenville, G. S. P.** (mh.) (1980) *The Mombasa Rising against the Portuguese, 1631, from Sworn Evidence* (London: OUP), kur. 166.

**Frobenius, L.** (1911-13) *Und Africa Sprach* (Juz. 3, Berlin, Charlottenburg: Vita, Deutsches Verlagshaus, S.D.).

**Fyfe, C.** (1964) *Sierra Leone Inheritance* (London: OUP), kur. 352.

**Fyfe, C.** (1965) 'Peoples of the Windward Coast, A.D. 1000-1800', kwenye J.F.A. Ajayi na J. Espic (wah.), kur. 149-65.

**Fyfe, C.** na **McMaster, D.** (wah.) (1977 and 1981) *African Historical Demography* Juz. 1, 1977, kur. 473; Juz. 2, 1981 (Edinburgh: EUP).

**Gado, B.** (1972, ) *Gazetters of the Northern Province of Nigeria* Juz. 1 (London: Frank Cass).

**Garlake, P. S.** (1973) *Great Zimbabwe* (London: Thames na Hudson), kur. 224.

**Garrard, T. F.** (1980) *Akan Weights and the Gold Trade* (London: Longman), kur. 393.

**Godard, L.** (1859) *Le Maroc, notes d'un voyageur* (Algiers).

**Goody, J.** (1956) *Social Organization of the Lowili* (London: IAI/OUP), kur. 119.

**Gorju, J.** (1938) *Face au royaume hamite du Ruanda, le royaume frère de l'Urundi* (Brussels: Vromant), kur. 118.

**Gourou, P.** (1953) *La densité de la population du Ruanda-Urundi: Esquisse d'une étude géographique* (Brussels: Institut royal colonial belge), kur. 239.

**Grandidier, G.** (1942) *Histoire politique et coloniale* (de Madagascar), Juz. 5, (Paris).

**Grandidier, A., Charles-Roux, J., Delherbe, C., Froidevaux, H.** na **Grandidier, G.** (wah.) (1903-20) *Collections des ouvrages anciens concernant Madagascar* (Juz. 9, Paris, Comité de Madagascar).

**Grandidier, G.** na **Decary, R.** (1958) *Histoire politique et coloniale (de Madagascar)* Juz. 5, part 3 (Antananarivo).

**Gray, J. M.** (1962) *History of Zanzibar from the Middle Ages to 1856* (London: OUP), kur. 314.

**Gray, R.** (1961) *A History of the Southern Sudan* (London: OUP), kur. 219.

**Gray, R.** (mh.) (1975) *The Cambridge History of Africa*, Juz. 4 (Cambridge, CUP), kur. 738.

**Greenberg, J. H.** (1980) *'Classification of African Languages', General History of Africa*, Juz. 1, ch. 12 (Paris/London/Berkeley: UNESCO/Heinemann/University of California Press),

kur. 292-308.

**Grigg, D. B.** (1980) *Population Growth and Agrarian Change: An Historical Perspective* (Cambridge: CUP).

**Guillot, B.** (1973) *La Terre Enkou* (Paris: Mouton), kur. 126.

**Gutman, H. G.** (1976) *The Black Family in Slavery and Freedom* (New York: Pantheon Books), kur. 664.

**Guy, J.** (1979) *The Destruction of the Zulu Kingdom: The Civil War in Zululand, 1879-1884* (London:Longman), kur. 273.

**Hacquard, A.** (1900) *Monographie de Tombouctou* (Paris: Société des editions coloniales et maritimes), kur. 119.

**Hagenbucher Sacripanti, F.** (1973) *Les fondements spirituels du pouvoir au royaume de Loango, R. P. du Congo* (Paris: ORSTOM), kur. 214.

**Haig, Sir W.** (mh.) (1937) *The Cambridge History of India*, Juz. 3 (London: CUP).

**Hair, P. E. H.** (1974) 'From language to culture: some problems in the systematic analysis of the ethnohistorical records of the Sierra Leone region', kwenye R.P. Moss na R.J.A.R. Rathbone, *The Population Factor in African Studies* (London:ULP), kur.71-83.

**Hama, B.** (1967a) *Histoire du Gobir de Sokoto* (Paris: PA), kur. 167.

**Hama, B.** (1967b) *Histoire traditionnelle d'un peuple: les Zama-Songhay* (Paris: PA), kur. 273.

**Hama, B.** (1968) *Contribution à la connaissance de l'histoire des Peuls* (Paris: PA), kur. 362.

**Hama, B.** (1969) *Histoire traditionnelle des Peuls du Dallol Boboye* (Niamey: CRDTO), kur. 160.

**Hamani, D. M.** (1989) *Au carrefour du Soudan et de la Berbérie: le sultanat touareg de l'Ayar* (Juz. 2, Paris: Université de Paris I Panthéon-Sorbonne), kur. 521.

**Hanke, L.** (mh.) (1969) *History of Latin American Civilization: Sources and Interpretation* (Juz. 2, London: Methuen).

**Harms, R.** (1981) *River of Wealth, River of Sorrow: The Central Zaire Basin in the Era of the Slave and Ivory Trade, 1500-1891* (New Haven na London: YUP), kur. 277.

**Harris, J. E.** (1971) *The African Presence in Asia: Consequences of the East African Slave Trade*, (Evanston, Ill: NUP), kur. 156.

**Harris, J. E.** (1982) *Global Dimensions of the African Diaspora* (Washington DC:HUP).

**Hartwig, G. W.** (1976) *The Art of Survival in East Africa: The Kerebe and Long-distance Trade, 1800-1895* (New York/London: Africana Publishing), kur. 253.

**Hasan, Y. F.** (1967) *The Arabs and the Sudan* (Edinburgh: EUP), kur. 298.

**Herskovits, M. J.** na **Harwitz, M.** (wah.) (1964) *Economic Transactions in Africa* (London: Rout-ledge na Kegan Paul), kur. 444.

**D'Hertefelt, M.** (1971) *Les dans du Rwanda ancien: éléments d'ethnosociologie et d'ethnohistoire* (Tervuren: MRAC), kur. 85.

**Heuscb, L. de** (1972) *Le roi ivre ou l'origine de l'Etat* (Paris: Gallimard), kur. 331.

**Hill, A.** na **Kilson, M.** (wah.) (1969) *Apropos of Africa* (London: Frank Cass), kur. 390.

**Hilton, A.** (1985) *Family and Kingship* (Oxford: OUP).

**Holt, P. M.** (wah.) (1968) *Political and Social Change in Modern Egypt: Historical Studies from the Ottoman Conquest to the United Arab Republic* (London: OUP).

**Hopkins, A. G.** (1973/1975/1983) *An Economic History of West Africa* (London: Longman). (Tol. 1, (wah.) 1973, kur.337).

**Hopkins, J. F. P.** na **Levtzion, N.** (1981) *Corpus of Early Arabic Sources for West African*

*History* (Cambridge: CUP), kur. 492.

**Ingham, K.** (mh.) (1974) *Foreign Relations of African States* (London: Butterworth, Colston Paper, No. 75) kur. 344.

**Inikori, J. E.** (1979) 'The slave trade and the Atlantic economies, 1451-1870', in *The African Slave Trade from the 15th to the 19th Century: Reports and Papers of the Meetings of Experts Organized by UNESCO,* Port-au-Prince, Haiti, 31 January-4 February 1978, *The General History of Africa - Studies and Documents*, No. 2 (Paris: UNESCO), KUR. 56-87.

**Inikori, J. E.** (mh.) (1982) *Forced Migration: The Impact of the Export Slave Trade on African Societies* (London: Hutchinson University Library for Africa: New York: Africana Publishing Company), kur. 349.

**Isaacman, A. F.** (1969) 'The prazos da Coroa, 1752-1832: A functional analysis of the Portuguese system', *Studia*, 26, kur. 149-78.

**Izard, M.** (1981) *Histoire du Yatenga des origines à 1895* (Ouagadougou).

**Jackson-Haight, M.V.** (1967) *European Powers and South-east Africa, 1796-1856* (London: Routledge and Kegan Paul).

**Jadin, L.** na **Dicorato, M.** (1974) *Correspondence de Dom Afonso, roi du Congo*, 1506-1543 (Brussels: ARSOM 41-3), kur. 245.

**James, C. L. R.** (1963) *The Black Jacobins: Toussaint L'Ouverture and the San Domingo Revolution* (New York: Vintage).

**Johnston, H. H.** (1902) *The Uganda Protectorate* (Juz. 2 London: Hutchinson).

**Jones, A. H. M.** na **Monroe, E.** (1978) *A History of Ethiopia* (Oxford: OUP), kur. 196.

**Julien, C. A.** (1951-56) *Histoire de l'Afrique du Nord: Tunisie, Algérie, Masroc. De la conquète arabe à 1830,* Tol. 2, (Juz. 2, Paris: Payot).

**July, R.W.** (1974) *A History of the African People* (London: Faber), kur. 650.

**Kagame, A.** (1954) *Les organisations socio-familiales de l'ancien Rwanda* (Brussels: Académie royale des sciences coloniales), kur. 355.

**Kagame, A.** (1963) *Les milices du Rwanda Précolonial* (Brussels: Academic royale des sciences coloniales) kur. 196.

**Kagame, A.** (1972) *Un abrégé de l'ethno-histoire du Rwanda* (Butare: Editions universitaires du Rwanda), kur. 286.

**Kaira, O. Y.** (1970-71) 'A survey of the history of the Kaira Clan of Northern Malawi' (Student seminar paper, Chancellor College, Chuo kikuu cha Malawi).

**Kalinga, O. J. M.** (1985) *A History of the Ngonde Kingdom* (Berlin/New York: Mouton).

**Kaniki, M. H. Y.** (mh.) (1979) *Tanzania Under Colonial Rule* (London: Longman), kur. 391.

**Keen, B.** na **Wasserman, M.** (1980) *A Short History of Latin America* (Boston: Houghton Mifflin), kur. 574.

**Kent, R. K.** (1970) *Early Kingdoms in Madagascar, 1500-1700* (New York: holt, Reinhart na Winston).

**Kesteloot, L.** (1972) *Da Monzon de Ségou, épopée bambara* (Juz. 4, Paris: F. Nathan).

**Kesteloot, L.** (1983) *Biton Koulibaly, fondateur de l'empire de Ségou* (Dakar: NEA), kur. 96.

**Kieteglıa, J. B.** (1983) *L'or de la Volta Noire* (Paris: Karthala, CREA), kur. 247.

**Kimambo, I. N.** na **Temu, A.** (wah.) (1969) *A History of Tanzania* (Nairobi: EAPH), kur. 276.

**Kimble, D.** (1963) *A Political History of Ghana: The Rise of Gold Coast Nationalism, 1850-1928* (Oxford: Clarendon Press), kur. 587.

**Kirkman, J. S.** (1964) *Men and Monuments on the East African Coast* (London: Lutterworth Press), kur. 224.

**Ki-Zerbo, J.** (1978) *Histoire de l'Afrique noire* (Paris: Hatier), kur. 702.

**Klein, H. S.** (1967) *Slavery in the Americas: A Comparative Study of Virginia and Cuba* (Chicago: University of Chicago Press), kur. 270.

**Klein, M. A.** (1968) *Islam and Imperialism in Senegal Sine-Saloum, 1847-1914* (Edinburgh:EUP), kur. 285.

**Kouanda, A.** (1984) 'Les Yarse: fonction commerciale, religieuse et légitimité culturelle dans le pays moaga (Evolution historique)' (PhD) tasnifu, Chuo Kikuu cha Paris I.

**Kup, A. P.** (1961) *A History of Sierra Leone, 1400-1787* (London: CUP) kur. 212.

**Labarthe, P.** (1803) *Voyage à la Côte de Guinée* (Paris: Bossange, Masson na Besson), kur. 310.

**Laburthe-Tolra, P.** (1981) *Les seigneurs de la forét* (Paris: Publications de la Sorbonne), kur. 490.

**Lamb, V.** (1975) *West African Weaving* (London: Duckworth).

**Lamphear, J. E.** (1976) *The Traditional History of the Jie of Uganda* (Oxford: Clarendon Press, Oxford Studies in African Affairs), kur. 281.

**Lange, D.** (1977) *Chronologie et histoire d'un royaume africain* (Wiesbaden: Franz Steiner).

**Lara, O. D.** (1979) 'Negro resistance to slavery and the Atlantic slave trade from Africa to Black Americas' (working paper, Meeting of Experts organized by UNESCO on *The African Slave Trade from the 15th to the 19th Century*, Port-au-Prince, Haiti, 31 Januari-4 Februari 1978 1978. *The General History of Africa* – Studies and Documents, 2 (Paris: UNESCO), kur. 101-14.

**Laroui, A.** (1970) *L'histoire du Maghreb: un essai de synthèse* (Paris: Maspéro), kur. 390.

**Le Barbier, C.** (1916-17) 'Notes sur le pays des Bara-Imamono, région d'Ankazoabo', *BAM*, new series, 2, kur. 63-163.

**Lee, R. B.** (1979) *The Kung San: Men, Women and Work in a Foraging Society )* Cambridge: CUP), kur. 526

**Leo Africanus [Jean Léon l'Africain]** (1956) *Description de l'Afrique*, taf. A. Epaulard, maelezo na E. Epaulard, T. Monod, H. Lhote na R. Mauny Juz. 2, Paris: Maisonneuve)

**Lévi-Provinçial, E.** (1922) *Les Historiens des Chorfa* (Paris: Larose)

**Levtzion, N.** (1968) *Muslims and Chiefs in West Africa: A Study of Islam in the Middle Volta Basin in the Precolonial Period* (Oxford: Clarendon Press, Oxford Studies in African Affairs), kur. 228

**Lewis, I. M.** (mh) (1966) *Islam in Tropical Africa* (London: OUP, for the IAI) kur. 470

**Lewis, I. M.** (mh.) (1968) *Islam in Tropical Africa* (London: OUP for the IAI), kur. 470

**Lewis, I. W. A.** (1978) *The Evolution of the Internationa Economic Order* (Princeton: PUP)

**Little, K.** (1951) *The Mende of Sierra Leone* (London: Routledge na Kegan Paul) kur. 307

**Lombard, J.** (1965) *Structures de type 'feodal' en Afrique nore: étude des dynamismes internes et des relation sociales chez les Bariba du Dahomey* (Paris/The Hague:Mouton) kur. 544

**Lopes, R. S.** (1976) *The Commercial Revolution of the middle Ages, 950-1350* (Cambridge: CUP).

**Lougnon, A.** na **Toussaint, A.** (wah.) (1937) *Mémoire des Iles de France et de Bourbon* (Paris: Libraire Ernest Leroux), kur. 203

**Lovejoy, P. E.** (1983) *Transformations in Slavery: A History of Slavery in Africa* (Cambridge:CUP), kur. 349

**Lovejoy, P. E.** (1985) *Salt of the Desert Sun: A History of Salt Production and Trade in Central Sudan* (Cambridge:CUP), kur. 351

**Ly, A.** (1958) *La compagnie du Sénégal de 1673 à 1686* (Paris: PA), kur. 316

**MacMichael, H. A.** (1922) *A History of the Arabs in the Sudan* (Juz. 2 Cambridge: CUP)

**Madiega, G. Y.** (1978) 'Le Nord-Gulma precolonial (Haute-Volta) origine des dynasties, approche de la société (PhD tasnifu, Chuo Kikuu cha Paris 1)

**Mage, E.** (1968) *Voyage dans le Soudan occidental (1863-1866)* (Paris: Hachette). (Tol. Jipya Karthala, 1980, Frobenius Institute)

**Malzac, V.** (1921/1930) *Histoire du royaume Hova depuis ses origines jusqu a sa fin* (Antananarivo: Imprimerie catholique). (Chapa mpya 1930)

**Maquet, J. J.** (1954) *Le Syystéme des relations sociales dans le Ruanda ancien* (Tervuren:MRAC), kur. 221

**Marees, P. de** (1602/1605/1905) *A Description and Historical Declaration of the Golden Kingdom of Guinea,* tafsiri ya Kiingereza iliyofupishwa of 1602 chapa ya Kidachi kwenye S. Purchas (1613/1905), Juz.6, kur. 247-396; tafsiri ya Kifaransa 1605, *Descrition et récit historique du riche royaume d'or de Guinée* (Amsterdam: Classen)

**Martin, B. G.** (1971) 'Notes on some members of the learned classes of Zanzibar and East Africa in the nineteenth century', *AHS*, 4, 3, kur. 525-45

**Martin, G.** (1948) *Histoire de l'esclavage dans les colonies françaises* (Paris: Geuthner)

**Martin, P. M.** (1972) *The External Trade of the Loango Coast, 1576-1870: The Effects of Changing Commercial Relations on the Vili Kingdom of Loango* (Oxford: Clarendon Press, Oxford Studies in African Affairs, kur.193

**Marty, P.** (1972) *Les Chroniques de Ovalata et de Nema* (Paris: Genthner)

**Mauny, R.** (1970) 'Les navigations anciennes et les grandes découvertes', kwenye H. Deschamps (mh.), *Histoire generale de l'Afrique noire* (Paris: PUF), Juz. 1,Sehemu ya II, kur. 203-18

**Mauny, R. Thomas, L.V.** na **Vinsina, J.** (wah.) (1974) *The Historian in Tropical Africa* (London: OUP for the IAI), kur. 428

**Mauro, F.** (1960) *Le Portugal et l'Atlantique au XVIIe siécle, 1570-1670* (Paris: SEVPEN)

**M'Bokolo, E.** (1983) 'Histoire des maladies, histoire et maladie: l'Afrique;, kwenye M. Auge na S. Herzlich (wah.) *Le sens du mal* (Paris: Editions des Archives contemporaines)

**M'Bokolo, E.** (1981) Noirs et blancs en Afrique équatoriale: les sociétés côtières et la pénétration française (Paris/The Hague: Mouton, Civilisations et Sociétés, No.69), kur.302

**McCulloch, M., Littlewood, M.** na **Dugast, I.** (1954) *Peoples of the Central Cameroons* (London: IAI, Ethnographic Survey of Africa, Western Africa, Sehemu ya IX), kur. 177

**McLeod, M. D.** (1981) *The Asante* (London: British Museum Publications)

**Meek, R. L.** (1976) *Social Science and the Ignoble Savage* (Cambridge: CUP, Cambridge Studies in the History and Theory of Politics) kur. 249

**Meillassoux, C.** (mh.) (1975) *L'esclavage en Afrique précoloniale* (Paris: F. Maspero) kur. 582

**Mellafe, R.** (1975) *Negro Slavery in Latin America* (Berkeley, CA:UCP), kur. 172

**Merrick, T. W.** na **Grahm, D. H.** (1979) *Population and Economic Development in Brazil, 1800 to the present* (Baltimore: The Johns Hopkins Univesity Press)

**Mettas, J.** (1978) Répertoire des expéditions négrières françaises au XVIIIe siècle, (mh.) S. Daget (Nantes)

**Miers, S.** na **Kopytoff, I.** (wah.) (1977) *Slavery in Africa: Historical and Anthropological Perspectives* (Madison: UWP) kur. 474

**Miller, J. C.** (1973) 'Requiem for the Jaga,' *CEA*, 49, kur. 121-49 (Taz. pia *CEA*, 69 na 70).

**Miller, J. C.** (mh.) (1980) *The African Past Speaks: Essays on Oral Tradtion and History* (London: Hamden, Dawson na Archon) kur. 284

**Minchinton, W. E.** (mh.) (1969) *The Growth of English Overseas Trade in the17th and 18th Centuries* (London: Methuen)

**Mokhtar, G.** (mh.) (1981) *General History of Africa. Vol. II: Ancient Civilizations of Africa* (Paris/London/Berkeley: UNESCO/Heinemann/University of California Press)

**Monteil, C.** (1924) Les Bambara de Segou et du Kaarta (Paris: Larose), kur. 404 Tol. 2, 1977 (Paris: Maisonneuve), kur. 441

**Monteil, C.** (1932) *Une cité soudanaise, Djenné, métropole du delta central du Niger* (Paris: Société d'études géographiques, maritimes et coloniales) Tol. 2, 1971 (Paris: Anthropos)

**Morris, A.** (1981) *Latin America: Economic Development and Regional Differentiation* (London: Hutchinson), kur. 256

**Mudenge, S. I** (1974) 'An identification of the Rozvi and its implications for the history of Karanga', *RH*, 5, kur. 19-31

**Mutumba, M.** (1973) *Bulozi ünder the Luyana Kings. Political Evolution and State-Formation in Pre-Colonial Zambia* (London: Longman), kur. 278

**Mwaroha, E.** (1977) *Peuples et rois de l'Afriques des lacs* (Dakar: NEA), kur. 352

**Mwaroha, E.** (1981) 'Redevances et prestations dans les domaines royaux du Burundi précolonial', *Mélanges R. Mauny. Le sol, la parole et l'ècrit: 2000 ans d'histoire africaine* (Paris: SFHOM), kur. 751-68

**Nacanabo, D.** (1982) 'Le Royaume maagha de Yoko' (PhD tasnifu, Chuo Kikuu cha Paris 1)

**Nachtigal, G.** (1876) *Le Voyage de Nachtigal au Ouadai: Traduction de Van Vollenhoven* (Paris).

**Ndoricimpa, L.** (mh.) (1984) *L'arbre memoire. Traditions orales du Burundi* (Paris/Bujumbura: Editions Karthala/Centre de Civilisation Burundaise)

**Niane, D. T.** (1975a) *Recherches sur l'empire du Mali au Moyen-Age* (Paris: PA)

**Niane, D. T.** (1975b) *Le Soudan occidental au temps des grands empires, Xie-XVIe siécles* (Paris: PA)

**Niane, D. T.** )mh.) (1984) *General History of Africa Juz. IV Africa from the Twelfth to the Sixteenth Century* (Paris/London/Berkeley: UNESCO/Heinemann/University of California Press)

**Nicolas, G.** (1975) *Dynamique sociale et appréhension du monde au sein d'une société hausa* (Paris: Institut d'ethnologie, Travaux et mémoires de l'Institut d'ethnologie, No.78) kur. 661

**North, D.C.** (1981) *Structure and Change in Economic History* (New York:Norton)

**Northrup, D.** (1978) Trade Without Rulers: Precolonial Economic Development in South-Eastern Nigeria (Oxford: Clarendon Press) kur. 269

**Nsanze, A.** (1980) *Un domaine royal Burundi: Mbuye (1850-1945)* (Paris: SFHOM) kur. 93

**Nziziwe, I.** (1972) Studies in Ibo Political Systems: Chieftaincy and Politics in Four Niger States (London: Frank Cass), kur. 287

**Obeuga, T.** (1976) *La cuvette congolaise*: Les hommes et les structures (Paris:PA)

**Ochieng, W. R.** (1974a) *A Pre-Colonial History of the Gusii of Western Kenya 1500-1914* (Nairobi: EALB) kur. 257

**Ochieng', W. R.** (1975a) *A History of the Kadimo Chiefdom of Yimbo in Western Kenya* (Nairobi: EALB), kur. 78

**Ochieng', W. R.** (1975) 'Undercivilization in Black Africa', kwenye W. R. Ochieng', (mh.) 1975), The First Word (Nairobi; EALB), kur. 1 - 20

**O'Fahey, R. S.** (1980) 'State and Society in Dar Fur (London: Hurst)

**O'Fahey, R. S.** na **Spaulding, J. L.** (1974) *The Kingdoms of the Sudan* (London: Methuen), kur. 235

**Ogot, B.A** (1967) *A History of the Southern Luo, Juz. 1 Migration and Settlement 1500-1900* (Nairobi: EAPH)

**Ogot B.A.** (mh.) (1976a) *History and Social Change in East Africa* (Nairobi: EALB), kur. 235

**Ogot, B. A.** (mh.) (1976b) *Kenya Before 1900* (Nairobi: EAPH), kur. 291

**Oliver, R.** na **Mathew, G.** (wah.) (1963) *A History of East Africa*, Juz. 1 (Oxford: Clarendon Press), kur. 500

**Oliver, R.** (mh.) (1977) *The Cambridge History of Africa, Juz. 3, From c. 1050 to c. 1600* (Cambridge: CUP) kur. 803

**Oloo, P.C.** (1969) 'History of settlement: the example of Luo clans of Alego: 1500-1918' (tasnifu ya shahada ya kwanza , Chuo Kikuu cha Nairobi)

**Ott, T.O.**(1973) The Haitian Revolution (Knoxville: UTP) kur. 232

**Pachai, B.** (mh.) (1972) *The Early History of Malawi* (London: Longman) kur. 454

**Pageard, R.** (1963) *Civilisation mossi et Egypte ancienne* (Geneva: Institut africain)

**Pagés, A.** (1933) *Au Rwanda sur les bords du lac Kivu: Un royaume hamite au centre de l'Afrique* (Bussels: Institut royal colonial belge) kur. 703

**Palmer, H. R.** (1936) *The Bornu, Sahara and Sudan* (New York: Negro University Press, kur. 296

**Patterson, K. D.** (1975) *The Northern Gabon Coast to 1875* (Oxford: Clarendon Press), kur. 167

**Pélissier, P.** (1966) *Les paysans du Senegal: les civilisations agraires du Cayor a la Casamance* (Saint-Yrieix, Haute-Vienne: Imprimerie Fabregue),kur. 941

**Perman. M. L.** (1970) 'The traditional systems of stratification among the Ganda and the Nyoro of Uganda', kwenye A. Tuden na Plotnicov (wah.), *Social Stratification in Africa* (London: Macmillan), kur. 125-62

**Perrot. C. J.** (1982) *Les Anyi-Ndenye et le pouvoir politique aux XVIIIe siécles* (Abidjan/Paris: CEDA)

**Person, Y.** (1964) 'En quête d'une chronologie ivoirienne', kwenye J. Vansina, R. Mauny na 1. V. Thomas (wah.), *The Historian in Tropical Africa* (Oxford: OUP), kur. 322-38

**Person, Y.** (1970) 'Le Soudan nigérien et la Guinée occidentale', kwenye H. Deschamps, (mh.), *Histoire générale de l'Afrique noire, Juz. 1* (Paris: PUF), kur. 271-304

**Phillipson, D. W.** (1977) *The Later Prehistory of Eastern and Southern Africa* (London: Heinemann), kur. 323

**Piault, M. H.** (1970) Histoire Mawri: introduction à l'étude des processus constitutifs de l'Etat (Paris: Editions du CNRS), kur. 206

**Plancquaert, M.** (1971) *Les Yaka, essai d'histoire* (Tervuren: MRAC, Annales sciences humaines, Juz. 71)

**Pollock, N. C.** na **Agnew, S.** (1963) *A Historical Geography of South Africa* (London: Longman), kur. 242

**Porter, D. H.** (1970) *The Abolition of he Slave trade in England 1784-1807* (New York: Archon)

**Price, R.** (1976) *The Guiana Maroons: Historical and Bibliographical Introduction* (Baltimore:JHUP) kur. 184

**Priestley, M. A.** (1969) *West African Trade and Cost Society* (London:OUP), kur. 207

**Quarles, B.** (1961) *The Negro in the American Revolution* (Chapel Hill: UNCP), kur. 232

**Randles, W. G. L.** (1968) *L'ancien royaume du Congo des origines à la fin du XIXe siécle* (Paris/The Hague: Mouton), kur. 275

**Ranger, T. O.** (mh.) (1968) *Aspects of Central African History* (London/Nairobi: Heinemann/ EAPH), kur. 291

**Ranger, T.O.** (1979) *Revolt in Southern Rhodesia 1896-1897: A Study in African Resistance*, 1st jalada jepesi (London: Heinemann), kur. 403

**Rau, V.** (1966) 'Les marchands-banquiers étrangers au Portugal sous le régne de Joao III (1521-1557)' in Les aspects internationaux de la découverte océanique aux Xve et XVIe siécles (Paris).

**Rinchon, R. F. D.** (1964) *Pierre Ignace Liévin van Alstein, capitaine négrier: Gand 1733 – Nautes 1793* (Dakar: IFAN, Mémoire No.71), kur. 452

**Roberts, A. D.** (1976) *A History of Zambia* (London: Heinemann), kur. 288

**Roche, C.** (1976) *Conquête et resistance en Casamance* (Dakar: NEA)

**Rodney, W.** (1970) *A History of the Upper Guinea Coast 1545-1800* (Oxford: Clarendon Press), kur. 283

**Rodney, W.** (1972) *How Europe Underdeveloped Africa* (Dar es Salaam/London: TPH na Bodge L'Ouverture), kur. 316

**Rodney, W.** (1975) 'Africa in Europe and the Americas' kwenye J.D. Fage na R. Oliver (wah.), *The Cambridge History of Africa, Juz. 4* (Cambridge: CUP), kur. 578-651

**Rotberg, R.** na Mazrui, A. (wah.) *Protest and Power in Black Africa* (New York: OUP), kur. 1274

**Rout, L. B. Jr.** (1976) *The African Experience in Spanish America, from 1502 to the Present Day* (Cambridge: CUP), kur. 404

**Ryder, A. F. C.** (1969) *Benin and the Europeans, 1485-1897* (London: Longmans), kur. 372

**Salim, A. I.** (1980) 'Kenya, Muslims' in *Encyclopedia of Islam*, tol. jipya (Leiden/Paris: Brill/Maisonneuve et Larose)

**Sautter, G.** (1966) *De l'Alantique au fieuve Congo, une géographie du sous-peuplement* (Paris: Imprimerie nationale), kur. 1102

**Schove, D. J.** (1973) 'African droughts and the spectrum of time', kwenye D. Dalby na R. J. H. Church (wah.) *Droughts in Africa* (London:IAI), kur. 38-53; tol. 2, 1977

**Séré de Rivieres, E.** (1965) *Histoire du Niger* (Paris: Berger-Levrault), kur. 311

**Shaw, T.** (1978) *Nigeria: Its Archaeology and Early History* (London: Thames & Hudson)

**Shepherd, J. F.** na **Walton, G. M.** (1972) *Shipping, Martime trade, and the Economic Development of Colonial North America* (Cambridge: CUP)

**Shiroya, O.J.E** (haijachapishwa) 'The Lugbara: at the nexus of three worlds', kwenye J.B. Webseter (mh.), *Uganda before 1900*, Juz. 1

**Skinner, E. P.** (1964) *The Mossi of Upper Volta: The Political Development of a Sudanese People* (Stanford: SUP)

**Smaldone, J. P.** (1977) *Warfare in the Sokoto Caliphate* (Cambridge: CUP), kur. 228

**Southhall, A. W.** (1970) 'Rank and stratification among the Alur and other Nilotic peoples', kwenye A. Tuden and Plotnicov )wah.), *Social Stratification in Africa* (London: Macmillan), kur. 31-16

**Sow, A. I.** (1971) *Le filon du bonheur éternel par Mouhammadou Samba Mambeya* (Paris: Colin)

**Steinhart, E. I.** (1981) 'Herders and farmers', kwenye C.C. Steward na D. Crummery (mh.), *Modes of Production in Africa* (London: Sage Publications), kur. 115-56

**Stokes, E.** na **Brown, R.** (wah.) (1966) *The Zambezian Past: Studies in Central African History* (Manchester: MUP), kur. 427

**Sure-Canale, J.** (1970) *La Republique de Guinee* (Paris: Editions sociales), kur. 431

**Swartz, A.** (1971) *Tradition et changements dans la societe guere* (Paris: ORSTOM, Mémoires, Na. 52), kur. 259

**Tamrat, T.** (1977) 'Ethiopia, the Red Sea and the Horn', Cambridge *History of Africa*, Juz. 3 (Cambridge:CUP), kur. 98-182

**Tardits, C.** (1980) *Le royaume bamoum* (Paris: Armand Colin), kur. 1078

**Tardits, C.** (mh.) (1981) *Contribution de la recherche ethnologique á l'histoire des ciivilisations du Cameroun* (Juz. 2, Paris: Editions du CNRS), kur. 597

**Taylor, J. G.** (1979) *From Modernization to Modes of Production: A Critique of the Sociologies of Development and Underdevelopment* (London: Macmillan)

**Thomas, J. M. C.** (1979) 'Emprunt ou parentes', kwenye S. Bahuchet, *Pygmees de Centrafrique* (Paris), kur. 141-69

**Thompson, R. F.** na **Cornet, J.** (1982) *The Four Moments of the Sun: Kongo Art in Two Worlds* (Washington: National Art Gallery)

**Thornton, J.K.** (1983) *The Kingdom of Kong in the Era of the Civil Wars, 1641-1718* (Madison: UWP), kur. 193

**Tosh, J.** (1978) *Clan Leaders and Colonial Chiefs in Lango: The Political History of an East African Stateless Society, 1800-1939* (Oxford: Clarendon Press, Oxford Studies in African Affairs), kur.293

**Toure,M.** 91974) *Mande Influences in the Gyaman Kingdom,* Colloquium, Bonduku, Januari.

**Toussaint, A.** (1971) *Histoire des l'Iles Mascareignes* (Paris: PUF), kur. 128

**Trimingham, J. S.** (1970) *A History of Islam in West Africa* (Oxford: OUP), kur. 262

**Turnbull, C. M.** (1966) *Wayward Servants: The Two Worlds of the African Pygmies* (London: Eyre and Spottiswood), kur. 390

UNESCO (1963) *Nomades et nomadisme au Sahara* (Paris), kur. 195

UNESCO (1979) *The African Slave Trade from the Fifieenth to the Nineteenth Century, General History of Africa, Studies and Documents, Na. 2* (Paris: UNESCO), kur. 330

UNESCO (1980) *Historical Relations across the Indian Ocean, General History of Africa, Studies and Documents No. 3* (Paris: UNESCO), kur. 198

**Valensi, L.**(1969) *Le Maghreb avant la prise d'Alger,1790-1830* (Paris: Flammarion), kur. 141

**Valensi, L.** (1977) *Fellahs tunisiens: l'économie rurale et la vie des campagnes aux 18e et 19e siécles* (Paris/The Hague: Mouton), kur. 421

**Vansina, J.** (1961) *De la tradition orale ; essai de méthode historique* (Tervuren: MRAC, Mémoire No.36

**Vansina, J.** (1966) *Kingdoms of the Savanna: A History of Central African States until the European Occupation,* taf. ya Les *anciens royaumes de la savane* (Madison:UWP), kur. 364

**Vansina, J.** (1972) *La légende du passé: Traditions orales du Burundi* (Tervuren: MRAC, kur. 257

**Vansina, J.** (1973) *The Tio Kingdom of the Middle Congo, 1880-1892* (London: OUP), kur. 586

**Vansina, J.** (1978) *The Children of Woot: A History of the Kuba Peoples* (Madison: UWP), kur. 394

**Van Thiei, H.**(1971) *'Buzinza unter der Dynastie der Bahinda', Anthropos*, kur. 497-520

**Verin, P.** (1975) *Les échelles anciennes du commerce sur les côtes nord de Madagascar* (Juz. 2, Lille: Chuo Kikuu cha Lille)

**Wallerstein, I.** (1976) 'The three stages of African involvement in the world economy, kwenye P.C.W. Gutkind na I. Wallerstein (wah.), *The Political Economy of Contemporary Africa* (London: Sage Publications), kur. 30-57

**Walvin, J.** (1972) *The Blank Presence: A Documentary History of the Negro in England* (New York: Schocken Books)

**Walvin, J.** (1973) *Black and White: the Negro and English Society, 155-1945* (London: Allen Lane na Penguin Press), kur. 273

**Warren, R.** (1980) *Imperialism: Pioneer of Capitalism* (London: NLB na Verso)

**Webster, J. B.** (mh.) (1979) *Chronology, Migration and Drought in Interlacustrine Africa* (London: Longman na Dalhousie University Press), kur. 345

**Weiskel, T.C.** (1980) *French Colonial Rule and the Baule Peoples, 1889-1911* (Oxford: Clarendon Press), kur. 323

**Wilbour, C.M.** (1967) *Slavery in China during the Former Han Dynasty* (New York: Russel na Russell)

**Wilks, I.G.** (1975) *Asante in the Nineteenth Century: The Structure and Evolution of a Political Order* (Cambridge: CUP), kur. 800

**Williams, F.** (1970) *From Columbus to Castro: The History of the Caribbean, 1492-1969* (London: Andre Deutsch), kur. 576

**Williamson, K.** (1971) 'The Benue-Congo languages and Ijo', kwenye J.Berry na J. H. Greenberg (wah.), *Linguistics in Sub-Saharan Africa* (Mouton), kur. 245-306

**Wilson, M.** na **Thompson, L.M.** (wah.) (1969), 1971) *The Oxford History of South Africa* (Juz. 2, Oxford: Clarendon Press)

**Womersley, H.** (1984) 'Legends and the history of the Luba' kwenye T.Q. Reef (mh.) *Legends and History of the Luba* (Los Angeles: Cross Roads Press)

**Wright, J.** (1977) 'San history and non-San historian', kwenye *The Societies of Southern Africa in the 19th and 20th Centuries*, Juz. 8 (London)

**Zahan, D.**(1960 *Sociétes d'initiation bambara: le N'domo; le Kore* (Paris/The Hague: mouton), kur. 438

# *FAHARASA*


'Abd al-Rahman - 109
*Ab Shaykh*, - 108
Abd al-Kadir – 100, 101, 166, 167
Abd al-Karim ben Jame - 281
Abd al-Karim ibn Abu - 122
Abd al-Malik - 119
Abd al-Rahman - 108, 116
Abdallah - 98, 116
Abdu'l' Abbas al-Mansur - 20
Abdullah - 278
Abdullah al-Idkawi - 89
Abdullah al-Sha'rawi, - 90
Abdullah b. Lubekto - 278
Abdullahi - 98, 274
Abid, - 182
Abla Poku - 234
Abram Petrovich Hannibal - 71
Abron - 200
Abu Abd Allah - 114
Abu Abdallah Muhammad al-Dar's - 174
Abu Hassun - 123
Abu I-Abbas al-Mansur - 18
Abu Likaylik - 105
Abu Muhammad Abdallah, - 116
Abu Shanab - 87
Abu Yusufu - 20
Abu'I Kasim - 107
Abu'l-Kasim ben Ahmad Bukr - 107
*abusuapanin* - 226
Adar - 260
Adhola - 425
Adoe - 65
Adom - 232
*Affaitati* - 4
Afonso - 305
Afonso I – 304, 306, 314
Agabba – 257, 260
Agokoli - 226
*ahl-al Usul* - 101
Ahmad – 411, 482
Ahmad Bukr b.Musa - 107
Ahmad al Araj, - 116
Ahmad al Dardir, - 90
Ahmad al-Arj - 114
Ahmad al-Badawi - 89
Ahmad Ibn Ibrahim al-Ghazi - 380
Ahmad Karamanli - 139, 145
Ahmad Pasha - 81, 84
Ahmad, - 114, 122, 145
Ahmadu. – 173, 176
Ahmed - 413
Ahmed Gran - 385
Ait Atta Kabila - 125
Ajib I - 99
Akan – 228, 231, 232, 241, 242
Akkra - 232
Akwa - 293
Akwa Boni - 234
Akwamu, - 232, 487
al Ghalib Billah - 116
al Islam al-Fasi. - 128
al-Akbar - 102
Alawoma – 275, 276, 277
al-Bakri - 90
*al-Balad* – 90, 91, 93, 94
Albreacht Durer - 400
al-Dhahabi – 119, 129
Aleksander Pushkin - 71

al- Ayyashi - 120
Abu Abullahi b. Masani - 270
Abu Bakr - 90
Abu Bakr ibn Abd al-Karim - 122
Abu Bakr Kado - 258, 269
Abu Bakri b. Ahmad
Ali bey – 85, 90, 91, 93,143, 411
Ali Burghul, - 145
Ali Dundu, - 167
Ali Gaji – 272, 273, 274
Ali ibn Abdallah al-Rifi - 127
Ali Pasha - 143
Ali Sidi - 167
Alichandora, - 158, 159, 160
Aliyu - 259
al-Jabarti - 89
al-Jinn - 90
al-Kaim bi Amr Allah - 114
al-Khadr Ghaylan - 122
Al-Mahdiyya - 125
al-Mamura - 125
Al-Mansur – 120, 122, 127, 128, 170, 172, 177, 180, 278
al-Maslnkha - 117
al-Mukhtar. - 176
al-Mustafa al-Tazarkini - 174
al-Mustafa Gwani - 270
al-Mutawakkil Don Sebastian, - 117
Alpers - 405
Ahmad al-Mansur, - 119
Ahmad bin Muhriz, - 124
Ahmad Bukr - 108
Ahmad Grafi – 14, 391, 387
Ahmad ibin Muhriz - 125
- 160
*amanyamabo* - 250
Amari Ngoone Ndeela - 166, 167
Amari Ngoone, - 151, 152
Ambohimanga - 474
Ambriz - 317
amenokal - 177
Amir Ali - 276
Amir Nur - 390
Amiri Nuru ibn Mugahidi - 394
Anderea da Oviedo - 395
Andianampoinimerina - 472
Andirantsirotso - 472
Andrea Doria - 116
Andrevola - 471
Andrew Roberts - 456
Andriamanalina - 474
Andriamanalina 1 - 473
Andriamandazoala - 465
Andriamanelo - 474
Andriamanely II - 473
al-Ghalib Billah - 117
Al-Haji Umar - 204
al-Hasan - 413
al-Hasan ad-Dakhil - 122
Ali – 145, 270, 465
Ali b. Dunama – 272, 283
Ali b. Umar - 281
- 474
Andriandahifotsy - 469, 470, 471
Andrianjaka - 474
Andrianorri - 462
Andrianonindranarivo - 473
Andriaponolaha - 463
Angovi - 456
Anna - 306
Anquandah - 241
Antankara - 472
Antanosy - 469
Antatsino - 478
Antavaratra - 478
*Antefasy* - 479
Antemoro – 463, 470, 479
Antevatobe - 479
Antonio 1 - 309
Antonio Pinto de Miranda - 353
Anzuani – 481, 482
Aowin - 487
Aram, - 159
Arindrano – 473, 477
Arruj, - 135
Asante – 200, 487
*Asantehene* – 235, 241
*askiya* - 172
*askiya* Dawud - 257

Alphonso Mendex
- 398
al-Rashid - 108
al-Shirbini - 89
*al-Sudan* - 108
Alvarado - 65
al-Za'ri. - 174
Amadou Abel Sy.

Auwa - 261
*azalai* - 181
Azteki - 51

B.A. Ogot - 457
Babba Zaki - 260, 263
Babito - 432
Bachwezi - 435, 436, 446
Badanko - 395
Badi II Abu Dikn
- 100
Badi 111 - 101
Badi IV - 101, 105, 107
Badi Abu Shullukh
- 101
Badi Mwekundu,
- 101
Badri al-Hijazi - 89
Baganwa - 443
Bagweri - 425
Ba-Haddu b. Abu
-Bakr al-Dar'i
- 174
*Bahar Nagas* - 387
Bahavu - 442
Bahima - 441
Bahrey - 396
*Bairu* - 437

Andriamasinavalona
- 474
Andriana - 474
Andrianalimbe - 465
Andrianampoinimerina
- 474
Andrianbaga - 471
Andrianbelomasina
*Bakama* - 442
Bakir Pasha, - 87
Bakr al-Dalal. - 120
Bakr al-Shbani -122
*bakt* - 105
Bakula - 442
*balama* al-Saduk,
- 170
Bambara - 178, 184, 205
Banankoro - 188
Bandire - 365
Baukongo - 441
Banu 'Abd al-Wadid
- 133
Banu Maghfar, - 155
Banu Wattas. - 127
Banyiginya - 445
Baramangolo - 186, 187
Baraytu - 389
Barbak Shah - 73
Barbarossa - 20
Barentu - 389
Bari, - 163
Barwe - 347
Bashi - 442
Basita - 442
Baule - 234
Bawa - 270
Bawol. – 157, 168
Bayt al-Mal - 169
*bazales* - 5

*askiya* Muhammad
- 170, 257, 274
*Askiya* Muhammad II
- 257
askiya Nuh - 174
Assim - 246
Athman Bey - 129
Austen - 46
beecio – 158, 160
Behrens - 212
Bela - 293
Bell - 293
Bellum, - 159
*benangatoobe* - 19
Benefali – 186, 187
Benjamin Benneker
- 68
Beukan Kiriai - 257
Benyowsky - 471
Berba - 198
Besilau - 473
*bey* – 138, 139, 144, 145
*Beya* - 143
*beylerbey* - 135
*beylik* – 15, 16
Bibiana Vaz - 222
Bilad – 98, 108
*Bilad al-Makhzen*
- 134
Bilad al-Sudan - 105, 106, 273, 274, 277, 280, 281
Bilanga - 198
*Bin-Naaba* - 194
Biram Mansa - 161
Biton – 187, 220
Biton Kulibali – 175, 201
Bonaparte - 108
Borana - 389

Borgu - 198
Bororo - 336
Bosman - 241
Bosseyabe, - 166
Boukman - 68
Browne, - 112
Brue - 158
Bubakar Sire – 159, 166
Bubu Musa - 160
Bugaba - 435
Buganda - 432
Bugaya - 425
Bugesera - 443
Bnkr - 107
Bullom - 210
Bulsa, - 192, 198
Bunyoro - 439
Bure - 210
Busaidi - 416
Bushingo - 441
Busuma - 192
Cadiz - 47
Camara - 310
Carvalho Dias -321
Caulker - 223
Changamire - 24, 347, 354, 356, 365, 367
Charles 1 - 62
Charles V – 20, 134
Chibinda Ilunga - 321
Chigoma Katumbi - 344
*chikunda* - 352
Chinkhole - 335
*chiroma* - 281
Christelow - 47
Christopher Columbus - 42, 403
Chulu - 337
Chwa – 431, 439
Chwa II -.426
Chyirima Rugwe - 442
Chyirima Rujugira - 443, 445, 446
Claudius - 386
Cleveland, - 223
Corker - 223
Count Henry de Castries - 118
Count Modave - 480
Cruzado - 3
Cruzet - 48
Cuffy - 65
Curtin – 5, 46, 229
*curva* - 24

Daaku - 229
Dabra Damo - 386
Dagomba – 190, 191, 204
Dakin - 99
Damagram - 260
*damel* – 151, 156, 158, 159
Dan Gwarandume - 269
Danda - 347
Danyanke - 151
Dapper – 221, 289, 290
*Dar al-Islam*, - 134
Dauda - 263
David Beach - 358
David Reubeni - 99
Dawuda - 268
de Lacerda e Almeida - 327
Dengel - 392
Deniba Bo - 188
Denkoro – 187, 189
Denkyira – 232, 234, 235, 236, 487
Denyanke - 147, 152, 162, 166, 168, 183
Dervi - 89
*dey* – 138, 139, 144
Dey 'Ali Khoja - 144
Dhokoth; - 111
Dian Manhelle - 477
Dian Ramack - 468
Diogo de Alcacova - 360
Dirr - 100
Diwani - 416
Doka; - 101
*Dolphin* - 66
Dombo Changamire - 355, 365
Dombo I - 354
Don Sebastian – 118, 119
Dona Beatrice - 313
Dona Beatrice Kimpa Vita - 309
Donkuna - 188
Dorobe - 157
*dukowo* - 238
Dunama b. Muhammad - 274
Dundas - 378
Dunkula. - 109

E.de Dampierre - 288
*Ekpo* – 252, 253
Elizabeth 1 - 62
Eltis - 46
*emuron* – 429, 431
Enbakom - 396
Estervaniko - 65

*etem* - 429
Etienne Flacourt - 464, 468

fahatelo - 472
*Fakariya* – 85, 87
*fakih*, - 102
*Falasha* - 395
Famaghan Wattara - 201
fani - 482
Fante – 232, 233
Fara Kumba Mboji, - 156
Faraony - 477
*farinya* - 24
Fasiladas - 398
Fatagari - 385
*feira* – 364, 365, 367
Fernando Po - 290
Fetha - 399
*fia* - 238
Filipo II - 7, 117, 120
Filipo III - 127
Francesco d' Almeida - 22, 409
Francis - 6
Francois Martin - 475
Fransesco Alvares - 383
Fransisco Innocencio de Sousa Coutinho - 318
*Frescobaldi* - 4
*Fuggers* - 4
Fulakoro, - 187
Funji – 99, 100, 102, 103,105, 108, 111
Funji-Abdallabi - 101
Fur – 97, 103, 105, 106, 108, 487
Fyfe - 208

Ga, - 232
Gabarti - 392
Gabriel Prosser - 70
*gada* – 389, 391
Gahaya - 440
Gahaya Rutindangyesi - 440
Gajaaga – 162, 167
galadima - 281
Galawdewos – 386, 395, 396
Gangero - 401
*Gargisa* - 404
Garsia II – 309, 311, 312, 314
*gatari* - 262
Gatsi Rusere – 350, 351
Gealeka - 378
Gelowar - 158
Geogrges Madiega -197
George - 404
George Liele - 68
Gezo - 245
*ghazi* - 134
Gimma - 401
Gisaka - 442
Gobnangu - 198
Goncalo da Silveira, - 14
Gondwe – 344, 345
Gosanaa - 402
Grand Foul - 488
Granville Sharp - 62
Gulmanseba – 184, 198, 204, 205, 260
Gustave Julien - 462
Gustavus Vassa - 68
Gwiriko – 184, 204

Habakuk - 396
Habatit. - 176
Hair - 28
Hamadun al-Mazwar - 123
Hammadi Aissata, - 167
Hammadi Pate - 167
Hammiyuk - 176
Hammuda Pasha - 143
Hasan Pasha – 93,94, 96
Hash, 108
Hashimu Bazanfane, - 270
Hassan - 481
Hawwara – 91, 81
*Hazz al-Kuhuf* - 89
Hebbyabe - 166
Henrique - 305
Henry - 408
Heru - 441
Hilton - 304
Hormuz – 410, 414
Humam, - 91
Husayn b. Ali - 143

Iavy - 479
Ibini Okpube - 252
Ibn Abi Zayd al-Kayrawani - 102
Ibn al-Farid, - 89
ibn Haddu - 127
Ibn Hassun - 122
Iboina – 460, 475
Ibrahim - 409

Ibrahim al Bulad ibn Jabir - 102
Ibrahim al-Ghazi - 385
Ibrahim Badankari - 258
Ibrahim Bey – 90, 93, 94
Ibrahim Grafi - 394
Ibrahima Sambegu, - 163
Ibrahima Sory, - 164
Ibrim - 100
Idris - 102
Idris - Alawoma – 278, 273, 275, 276, 278, 279
Idris b. Ali – 273, 275, 280
Idris Katakarmabe - 274
Ifaf - 385
Ifara - 479
Ifranj Ahmad - 87
Igaba - 435
Ignatius Sancho - 68
Ikarebwok - 426
*ikta* - 79
Iktitiyar-ul-Mulk - 73
*iltizam* - 82
Ilunga mwindaji - 321
*Imandwa* - 436
Imerina – 472, 474
Inikori - 46
Inka - 51
Inkassa Ingwira - 231
Inkassa Kuu - 231
*innamne* - 262
Irungu - 436
Isaacman - 352
Isansa - 433
Isaria Kimambo - 456
Ishak II – 170, 172
Ishemurari - 440
Ismail - 392
Ismail Bey – 93, 94
Isna - 432
Iya Lamis - 261
Iyasu - 399
Iyasu I - 398
Iyasu II - 101
Ja'aliyyun - 102
Jab, - 198
Jaba - 197
Jabal Marra , - 106
Jakpangu - 198
Jal Joop - 167
Jallonke - 164
James Cleveland, - 223
James II - 124
Jamma - 98
Janga Kasanje - 306
Jawda - 283
*Jengu* - 253
Jeniseri Bashodabashi Kuchnk Mehmed. - 85
Jhujhar Khan - 73
Jicho - 355
Jimara, - 161
J. de Barros - 349
*jodaka* - 457
John Don - 134
jonya - 14
Joos – 158, 159
Jose Lopez de Moura - 222
Juan de Pareja - 62
Juan de Valladolid - 62
Judar Pasha – 3, 20, 170, 172
Junju - 434
*jurungul* - 279

Ka'id Uthman - 174
*Ka'im Makam* - 84
Kaabu - 147, 149, 150, 151, 161, 210, 216, 220
Kaarta – 175, 184, 186
*kabaka* - 430, 433, 434
Kabaka Mawanda - 432
*Kabaka* Tebandeke - 433
Kabambo - 442
Kabambo Kinwa - 442
Kabi - 260
Kabunduli – 337, 338
*Kabunga* - 302
Kadilo - 326
Kadiriyya – 102, 180, 183
Kahigi Kasita - 441
Kahya - 88
Kakalala - 344
Kakongo - 316
Kaladian Kulibali - 186
Kalala Ilunga - 321
Kalikstus III - 61
Kalinga - 442
*kalonga* – 335, 336, 341
Kaluluma - 337

Kamanya - 434
Kameme - 340
kangam - 158
Kanta Ahmadu - 257
Kanta Dawud - 257
*Kanun Name* – 81, 82
Kanyenda – 337, 338
Kaphwiti - 335
Kara Ibrahim Pasha, - 85
Karagwe - 441
Karamokho Alfa - 162, 163, 164
Karemera - 441, 443
Karrum al-Hajj - 122
Kasanje - 35
*Kashif* - 81, 83
Kasimiya. - 85
Kasyombe - 340
Katobaha - 442
Katong'ongo Mhenga - 344
Katumbi - 345
Katumbi Mulindafya Chabinga - 344
Kawa ag Amma - 177
Kawar - 268
Kayor, - 168
Kayra - 107
Kaytas Bey - 87
Kazembe – 318, 327
Kazobe - 472
*Kebra Nagast* - 382
Keita - 200
*kela yasku* - 279
*kente* - 241
Khalil ibn Ishak. - 102
khammasat - 16
*kharaj* - 22
Khayr al-Din - 20
Khayruddin - 135
Khyr Bey - 79
Kidervi - 89
Kidiawara, - 188
Kietegha - 201
Kigeri Mukobanya - 442
Kigeri Ndabarasa - 443
Kigonga - 391
*Kihabshi* - 73
Kikulughli – 139, 143, 145
Kilij - 135
Kimenyi - 440
Kimenyi Shumbusho - 440
Kimpa Vita - 314
Kinywa - 355
Kiranga - 436
Kisita - 440
Kitabanyoro - 439
Kitara - 436
Kitorode - 167
*Kitosa* - 404
Kogoro - 436
*kokani* - 262
Kolumba - 49
Koly Tengella – 149, 162, 151, 159
Konde Burama, - 164
Kong – 184, 187, 200, 201, 204
Kongolo - 321
Konko Bubu Musa - 160
Kooki - 434
Korogho - 200
Kristobal de Menesses - 62
Kristofa Kolumba - 42, 46
Kuala - 198
Kuchuk Mehmed - 86
Kulango - 200
Kulibali – 175, 188, 200, 220
*kulughli* - 138
Kumbari – 260, 264
Kunako - 257
Kupela - 198
Kurfai - 260
*kutama* - 37
Kutumbi - 259
Kwoja - 221
Kwotu, - 286
Kyamutwara – 441, 446
Kyebambe - 439
*Kyungu* Kameme - 339

L'Ouverture – 70, 76
*ladinos* - 5
*lamana* – 15, 26
Lamboina - 472
*lancados* – 221, 222
Lasta na Wag - 398
Lat Sukaabe Fall – 157, 158
Lebna Dengel – 385, 386
Lebu - 167
Lengoabo - 479
Leo Afrieanus, - 133, 228, 265
Leonardo Ortez - 62
Linta - 470
Lira Paluo - 432
Loggar – 158, 159
Lope Goncalves - 290

Lord Mansfield
- 64
Louis XIV – 124,
130
Lourenco Ravasko
-409
Luango – 302, 316
Luhanga - 344
Luis Mariano - 466
Lumpo, - 198
Lundu – 335, 336
Lwango - 487

Maa Ngala - 203
Maalik Sy - 162
maasi ya Mayeniseri
- 88
Maasi ya watumwa
- 65
maaskiya - 14
*madaki* - 261
Magembe Kitonkire
- 439
Magemo - 340
*Magho-Naaba* - 196
mah'alla - 144
Mahafaly - 469
Mahammad al-Amin
- 283
Mahammad Zaki - 269
Mahammadu Kanta
- 274
Mahammed Gran - 386
Mahe de Labourdonnais
- 484
Mahmud al-Ark, - 102
Mahmud Pasha - 172
Mahmud Zarkun - 172
*mai* - 258
*mailo* - 15
*Mairamo* - 404
*Mais* - 272
Majidhib. - 102
*makambula* - 339
Makewana - 341
Makhzen – 24, 137
Makoddu Kumba
Jaaring, - 159
makoko - 299
*malaguetta* - 209
Malam - 269
Malam Buhari - 269
Malam Jibril dan
Umaru - 270
malambula - 340
*Malik al-Umara* - 79
Malik Ambar - 73, 74
Maliki Akbar - 73
Maliki Fasiladas - 394
Maliki Galawdewos
- 394
Maliki Menelik - 389
Maliki Minas - 394
Maliki Petro Mkuu
- 71
Maliki Sartsa Dengeli
- 394
Maliki Susenyos
- 380
Maliki Zera-Yakob
- 383
Malixuri, - 158, 160
Malkia Kitami - 440
Malkia wa Sheba - 382
Maman Tukur dan Binta
- 270
Mamari Kulibali – 187,
188, 189
Mamprusi - 198, 204
Mamuel - 4
Mamutapa – 349,
355
Mamvura - 351
Mamvura Mutapa
- 348
Manabe - 471
Manandriana - 474
*manantany* - 472
Mande - 200
*Mande-Mani* - 221
*Mandi-Mansa* - 215
Manerandra - 470
Mani Luango - 290
*Manomutapa* - 350
Mansa – 216, 220
mansa Mahmud. - 172
Mansa Sulayman - 149
Mansa Tamba - 150
*mansaya* - 24
Manson Diarra - 187
Mansur b. Abd al-
Rahman - 174
Mansur b. Mas'ud al-
Za'ri - 174
*mantse* - 231
Manuel - 3
Manuel de Mello
Pereira - 413
Manyika – 347, 355,
357, 361, 367
Manzi - 192
Manzon 176
*marabouts* - 19
Maravi - 336
Mariamu - 404
*marisa* - 262
Marofela - 479
Maroserana – 465, 473
*marronnage* - 484

Maseba - 479
Masekesa - 365
Mashamba - 431
Massa - 186
Massa Maghan Keita - 187
Matamba - 307
Maungwe - 355
Mawanda - 434
Mawlay - 117
Mawlay Ismail - 128
Mawlay Abd al Malik, - 117, 118, 129
Mawlay Abdallah, - 130
Mawlay Abu Nasr, - 129
Mawlay Ahmad – 118, 125, 129
Mawlay Ahmad al-Dhahabi, - 129
Mawlay Ahmad al-Mansur - 169
Mawlay Ahmad, - 117
Mawlay al Mamun al-Kabir - 129
Mawlay al-Abbas - 122
Mawlay al-Harran, - 125
Mawlay Ali al -Sharif, -122
Mawlay al-Rashid - 122, 123, 124, 127, 177
Mawlay al-Sharif - 123
Mawlay Hafid - 129
Mawlay Hasham, - 125
Mawlay Ismail – 124, 125, 127, 129, 177, 182
Mawlay M'hammad, - 123
Mawlay Muhammad al-Alem - 129
Mawlay Sharif - 129
Mawlay Sulemani - 130
Mawlay Zaydan - 129
Maxan - 161
May Idris Alaoma, - 169, 170
Maya - 51
Mayeniseri – 139, 145
Mayotte – 481, 482, 483
*mbandwa* - 436
Mbanik, - 158
Mbanza Luango - 290
Mbegha - 450
Mbetsileo - 473
Mbushoong - 35
Mbwembe - 286
meen - 158
Mellakori - 211
Menabe - 467, 469, 470, 473, 479
Menarandra - 469
Mendez - 398
Menelik - 383
Merina - 474
*mestizos* – 221, 222
*mfekane* - 34
Mgamergu - 278
*Mgbe* – 252, 253
Mibambe Mutabazi - 442
Milansi – 456, 457
Miller - 317
Minas - 390
Mir Ali Bey - 411
Misuku - 339
Mkandawire - 345
Mlowaka Mughogho - 345
Mogho-Naaba - 204
Moheli – 481, 482
Monclaro – 360, 410
Monzon - 175
Mossi - 184
Mranga - 456
Msakalava - 465
Msukwa - 340
Mtu Muhammad - 89
Mtupa – 348, 365
Mubarak al-Dar'i - 174
*mugabe* – 435, 439, 442
Mugasha – 436, 446
Mughul – 73, 74
Muhammad Tayrab - 108
Muhammad – 117, 119
Muhammad Abu Likaylik – 101, 106
Muhammad al-Alem - 129
Muhammad al-Barnawi al-Kashinawi - 270
Muhammad al-Fadl - 109
Muhammad al-Haji, - 170
Muhammad al-Hajj al-Dila - 123
Muhammad Ali Pasha – 105, 112
Muhammad al-Maslakh, - 118
Muhammad al-Sabbagh

al-Kashinawi - 270
Muhammad al-Shaykh - 114, 116
Muhammad Ankoni - 409
Muhammad b. 'Uthman - 144
Muhammad ben al-Mubark - 257
Muhammad Bey - 93
Muhammad Bey Abu'l Dahab, - 91
Muhammad Dawra - 107
Muhammad ibn al-Kasim Alilish, - 128
Muhammad ibn M'Hammad - 120
Muhammad ibn M'Hammad ibn Abu - 120
Muhammad III, - 130
Muhammad Jawda, - 107
Muhammad Kisoki - 258, 274
Muhammad Kurra - 107, 108, 109
Muhammad na Uthman - 174
Muhammad Nazaki - 259, 268
Muhammad Sharif - 260
Muhammad Shashiri - 258
Muhammad Shaykh - 127
Muhammad Tayrab ibn Ahmad Bukr, - 107
Muhammad Wari - 258
Muhammad Zaki - 258, 259
Muhammad, - 108
Muhammad-Gao, - 172
*muhamuro* - 444
*Mukama* – 430, 435, 439
Mukanbya - 441
*munaki* - 313
Mungo Park, - 174
Murabiti Njaaya Sall - 156
Murad al-Malti - 139
Murad Bey – 93, 94
Murad III - 278
Musa Pasha - 84
Musawila Gondwe - 344
Mutapa – 333, 347, 349, 354, 355, 358, 359, 360, 361, 362, 363
*muteferrika*, 81
*mvant yav* - 327
Mvolafotsy - 472
Mwafulirwa - 345
Mwahenga - 345
Mwakalosi – 339, 340
*mwami* – 435, 440
Mwangonde - 340
*mwant Yav* – 321, 326
Mwanzi - 458
Mwari – 355, 356
Mwaulambya - 340
Mwene Mutapa – 14, 465
Mwihahabi - 442
*mwine Munza* - 321
*Mwine Munza Kalala* - 324

Na Bawa - 197
Na Garba - 191
Na Gbew - 190
Na Nyanghse - 190
Na Zangina, - 191, 204
*naaba* – 194, 196, 202
Naaba - Rawa - 190
Naaba Dulugu - 204
Naaba Kango – 193, 205
Naaba Koom - 192
Naaba Kuda – 191, 192
Naaba Kumdumye – 191, 205
Naaba Lambwega – 192,193
Naaba Manzi, - 192
Naaba Moatiba - 192
Naaba Namende - 192
Naaba Rawa - 192
Naaba Ruubo - 192
Naaba Saaga - 192
Naaba Wabri - 190
Naaba Warga – 192, 205
Naaba Wedraogo – 190, 197
Naaba Wende - 196
Naaba Wobgo, - 193

Naaba Wubri – 191, 192
Naaba Yadega – 190, 191, 192
Naaba Zombre –192, 204
Naaba Zungrana, - 190
*naabise* - 194
Naame - 161
Naatago – 158, 159
Nabii Muhamadi - 122
Nadega - 190
Nafana - 200
*nakid al-ashraf* - 90
*nakombse* - 194
Nana Tabiri - 241
*nangatoobe* - 19
Nanumba – 190, 191
Napanga Tenga - 196
Napoleon Bonaparte - 94
Napoleon. - 96
Nasir al-Din – 154, 155, 156, 161, 162, 166, 168
Nchare - 283
Ndlamba - 378
Ndongo - 487
Ndori - 442
Ndrembolanony - 479
Ndretsileo - 479
Ndriamboay - 470
Ngando - 293
*Ngola* – 302, 306
Ngolo - 187
Ngolo Diarra – 175, 188, 189, 202, 187
Ngome ya Yesu - 412
Ngoyo - 316
Ngqika - 378
Ngulube - 339
Nikki - 198
Nimi Lukeni - 302
Njaag Arm Bakar - 158
Njaajan - 149
Njaay, - 149
Njunaki - 435
Nkalany - 312
Noah - 61
Noeli - 115
Nsoro Nyabarega - 443
Ntare - 443
Ntare Kitabanyoro - 440
Ntare Muganganzara - 442
Ntare Muhire - 442
Ntare Rugamba - 443
Ntatakwa - 456
Nuh - 175
Nunbado - 198
Nungu - 198
Nyabongo - 439
*nyamankala* - 18
Nyamba Kapararidze - 351
Nyangolo, - 186
Nyarubamba II - 441
Nyarubamba Kichumbu - 439
*Nyarubanga* – 425, 426, 430, 431
Nzinga - 309
Nzinga Mbande - 306
Nzinga Nkuwa - 304
O'Hara - 159, 166
Oba - 243, 252
*obeah* - 66
Odak Ochollo - 110
Odienne - 200
Oduduwa - 246
*ogendini* - 457
Oghmor ag Ald - 176
*ojak* - 86, 87, 88, 90, 135,146
Okai Akwei - 232
Olaudah - 51
*Olaudah Equiano* - 68
Olimi - 439
*omanhene* - 233
Omolo - 425
Omukama - 432
Onilay - 470
Opoku Ware - 236
Opoku Ware, - 191
*Oranmiyan* - 248
Oranyan - 248
*Orkoiyot* - 458
Osei Tutu - 234, 236
Ottobah Cagoano - 68
Owiny - 425
Oyo - 245, 246, 248
Ozdemir - 100
Ozdemir Pasha, - 83

P.D Curtin - 8, 12
Paimol - 432
Pakana - 161
Palmer - 46, 258
Papa - 313, 398
Papa Nikolas V - 61
*pasha* - 135
pasha - 81, 85, 100, 138, 143, 174

pasha Abu Bakr. - 177
pasha Ba-Haddu - 176
Pathe Diagne - 486
Paul Cuffee - 67
Paulo Dias de Navaes - 306
Pawir - 432
Pedro II - 310
Pedro Leitao de Gamboa - 413
Pedro Navarro - 134
Pedro Paez - 396
Pedro Paez - 398
Peires - 373
Peter C. Oloo Aringo - 457
Peter Garlake - 364
Peukert - 246
Phyllis Wheatley - 68
Pieter de Marees - 229
Pietro della Valle, - 74
Pizarro - 65
Poron - 200
Prazo - 342, 351, 352, 353
Prince Hall - 67
Pronis - 468

*Quaqua* - 229
*quimbares* - 318

Raikitroka - 477
Ralambo - 474
Ralph Austen - 46
Ramadan b. Ahmadu - 270
Ramadhan - 125
Ramaharo - 473
Ramaroumanompou - 478
Rambo - 477
Raminia - 463
Randrianomoina - 477
Ras Seela Krestos - 398
Rasahamanarivo - 473
*Rasam Naaba* - 194
Ratongalaza - 479
Ratsimilaho - 479
Ratsimilahoe - 478
Ravahiny - 472
Ravahinya - 471
Raymond Mauny - 46
Rene Caillie - 174
Reombi-Mpolo - 291
*reth* - 111
Reth Bwoc - 111
Reth Dhokoth - 111
Reth Nyakwaa - 112
Rhrhabe - 378
Richard Allen - 67
Richard Brew - 239
Richard Mutetwa - 359
Ridhwan Bey - 85
Ridhwan Bey al-Fakari, - 84
Ridhwan Kahya - 88, 90
Ridhwan, - 88
rima - 193
Roanimanalina - 473
Robert Ross - 372
Roger Summers - 361
Rogers - 223
Roland Oliver - 109
Romboasalama - 474
Rout Jr - 46
Roy Willis - 456
Rozvi - 347, 351, 354, 355, 359, 360
Rubesirana - 463
Rueji - 321
Rugaba - 435
Ruganzu - 442
Ruganzu Bwimba - 440
Rugomora - 441
Rugomora Mahe - 441
Rugomora Mahe - 446
Ruhinda - 435, 436 440
Ruhinda Mugangakyaro - 442
Rukn-ud-din-Barbak - 72
Rumfa - 258
Ruy - 409
Rweej - 321
Rwoga - 442
Ryangombe - 436, 440

Sa'adi - 169, 177, 180
Saadi. - 114
Sadia - 467
Said Ahmad 'Ali - 480
Said Ahmad Ali - 482
Saint-Louis - 155, 156

157,154, 158
Sakalava - 460,470
471,472, 473,
475, 479, 487
Sakatovo - 469
Salah Ra'is - 135
Salih Bey - 90, 91
saliyane, - 81
Salum - 152,157,
159, 168
Sama, - 161
Samba - 160
Samba Gelaajo Jeegi - 160
Samba Lamu. - 152
*sampy* - 474
Sandrananta - 477
Sanduku la Agano
- 383
Sanwi - 233
*sarauta* - 261
*Sarki* - 267, 260
*sarkin* Azbin - 262
*sarkin* Fullani - 262
*Sarkin* Kano Abdullahi
- 258
*Sarkin lifidi* - 263
Sartsa - 392
Sartsa Dengel - 395,
396
*satiagi* - 155, 161
*saw* - 383
Sayyid - 73
Sayyid al Habshi Sultani
- 73
Sebamana - 175
Sebastian Gomez - 62
Sega - 167
Segu - 175, 174, 178,
184, 186, 190,
Seguela - 200
Sek Hussen - 390
Seku Ahmadu Barry
- 204
Seku Wattara - 201
Selim I - 77, 79, 81,
89
Semakokiro - 434
*Serdar*, - 84
Sereer - 159
Seville - 47
Shadhiliyya, - 102
Shah - 414
Shahzada, - 72
Shaihu - abdussalanri
- 269
Shaihu Ba-Tunashe
- 269
Sharif - 264, 271
shaykh al-Mukhtar,
- 175
Shaykiyya - 103
Shekarau - 259
Sherbro - 210
Shilluk Reth. 111
Shilluk: Abudhok
- 111
Sidi Bashir - 73
Sidi M'hammad - 128
Sidi M'hammad ibn
Abd al-Kadir al-
Kadir al-Fasi, - 128
Sidi Muhammad - 177
Sidi Muhammad ibn
Abdallah - 130
Sihab Al-Din - 391
Siin - 152, 157, 159,
168
Sikio - 355
Sila Makan Yero - 187
Simbowe - 339
Sinan Pasha - 20
Sira bo - 188
Soba - 259
*sombili* - 464
Sonni - 19
Sonni Ali - 170
*sorabe* - 477
Soriya - 164
Sory Mawdo - 164
Sourour - 130
*spahi*, - 84
Spear - 412
Stein - 46
Sube Njaay, - 161
Sulayman - 82, 100,
107, 130, 259
Sulayman Pasha, - 82
Sulayman Baal - 166
162
Sulayman ibn Ahmad
Bukr - 107
Sulayman Solongdungu
-106
Sulemani - 382, 383
Sum Tamben - 402
Sunsan - 186
Surur - 130
Susenyos - 398, 396

Ta'rikh - 182
Taj al-Din al-Bahari
- 102
Takali - 111
Tama - 269
Tankudgo - 198
Tatenga. - 192
Tauxier - 184
Tayrab - 107, 108
Tazarkini. - 174
Tegbesu - 245
Tejek - 158, 159
*telleck* - 383

Terrasse - 120
Tewodros - 380
Theodore II - 380
Thierno Molle - 167
Tighurt Pasha - 274
Tiguiton - 187
Tijaniyya - 180
Tingimaro - 466
Tio - 316, 487
Tirmaghan Traore, - 208
Togo - 111
Toussaint - 68, 76
Trimongarivo - 471
Tsileliki - 469
Tsimanatona - 471
Tucker - 223
Tugo - 111
Tuguri - 198
Tuman Bey - 89
Tumpa - 482
*tunka* - 160
Twa - 457

Uban Doro - 259
Ulad Abdallah - 166
*ulama* - 259
Ulambya - 339
Umar B. Idris - 272
Umar bi Idris - 281
*undi* - 337, 442
Uteve - 347, 355,361
Utham - 270
Uthman - 269, 270
Uthman Bey - 87,88
Uthman Nayinawa - 258

Vasco da Gama - 369, 387, 408, 409
Vatomandry - 478
*vodum* - 66
Volamana - 472
Volamena - 470
voodoo - 68

Waakan - 487
Waalo, - 168
Waantatismo - 478
Wachilima - 338
Wadabora - 188
Wadzivaguru - 349
Wafiherenama - 471
Waga - 487
Wahima - 440
Wajaga - 295
Wajula - 200
*Wakalimanjira* - 332
Wali Abu Abdullahi B. Masani - 269
Wamande Juula - 149
Wamara – 432, 436
*Wamaroserana* – 460, 471
Wambangala - 306
Wangara - 199
Waormani - 160
Waphiri - 337
Warren L. D'Azevedo - 210
Wasagone - 188
Wasakalava - 473
Wasape - 215
Wasikwese - 338
Wassa - 232
Watio - 306
Wattara - 200
Watyero Somono -187
Watyokosi, - 198
Waulad - 159
Wavolaotsy - 472
Wazaghawa, - 107
Winyi II - 431
*woloso* – 202
Xaaso - 167

Ya'rubi - 414
Yaasin Bubu - 156
Yaka – 40, 318
Ya-kub - 107
Yakub al-Mansur -122
Yamba Tiendrebeogo - 192
Yasif al-Yahudi - 86
Yatenga – 187, 193,194, 196, 199, 202
Yaye Hoola - 161
Yendabri - 198
Yenisari Kahya Ibrahim Kazdoghlu - 87
Yerim - 158
Yerim Kodne, - 156
Yirlabe - 166
Yohana II – 3, 4
Yohannes - 398
Yuhi Gahima - 442
Yusuf Karamanli-145
Yusufu – 145, 413, 414

Zafimanarivo - 473
Zafimaneli - 477
Zafirambo - 477
Zahir al-Umar - 93
Zahir Umar - 91
Zandoma - 192
Zarkun – 172, 174
Zaudai - 268
Zawila - 268
Zera-Yokob - 382
Zimbabwe Kuu - 347

# SHEREHE

[Kiswahili: Kiingereza/Kifaransa]
[Vifupisho: *n* = noun; *v* = verb]

## A. MAJINA YA WATU NA MAHALI

### A

**Abidjan:** Abijani
**Abyssinia/Uhabeshi:** Abyssinia
**Afrika Kusini:** South Africa
**Afrika Magharibi:** West Africa
**Afrika Mashariki:** East Africa
**Afrika ya Kusini:** Southern Africa
**Afrika ya Magharibi:** Western Africa
**Afrika ya Mashariki:** Eastern Africa
**Ajemi/Uajemi:** Persia
**Ajjer:** Adjdjer
**Akkra:** Accra
**Aksum:** Axum
**Aktika:** Arctic
**Amerika:** America
**Antaktika:** Antarctica
**Antiokia:** Antioch
**Asia Ndogo:** Asia Minor
**Assajen:** Assadjen
**Augustio:** Augustine
**Aurinyaki:** Aurignac
**Awjila:** Awdjila
**Azugui:** Azougui

### B

**Bahari ya Mediterania:** Mediterranean Sea
**Baleari, visiwa vya:** Balearic islands
**Bara Hindi/India:** India
**Barselona:** Barcelona
**Begemderi:** Begemder
**Bijay:** Bidjay
**Bizante:** Byzentium
**Bizasena:** Bizacena
**Bombetoki:** Bombetock
**Bonde la Ufa:** Lift Valley
**Buar: Bouar**
**Bukini/Madagaska:** Madagascar
**Bussura:** Boussoura

### C

**Chibinda:** Cibinda
**Chifinda:** Cifinda
**Chikoa:** Chicoa
**Chokwe:** Cokwe
**Chwa:** Cwa

### D

**Dacha:** Daca
**Daud:** Daoud
**Diula:** Dioula
**Duala:** Douala

E

**Efurata:** Ephrates
**Ekwado:** Equador
**Enkoje:** Encoje
**Ethiopia/Uhabeshi:** Ethiopia/Abbysinia

F

**Fatagari/Fatajari:** Fatagar/Fatadjar
**Filandia:** Flanders
**Fumban:** Foumban

G

**Garsia:** Garcia
**Grikwa:** Griqua
**Gwadalkivir:** Guadalquvir

H, I

**Hawasi:** Hawas
**Hijaz:** Hidjaz
**Hispania:** Spain
**Hungaria:** Hungary
**Irak:** Iraq

J

**Jabal:** Djabal
**Jadid:** Djadid
**Jadu:** Djadu
**Jaja:** Djadja
**Jalil:** Djalil
**Jalu:** Djalu
**Jalula:** Djalula
**Jama:** Djama
**Janet:** Djanet
**Jannan:** Djannan
**Jaret:** Djaret
**Jarid:** Djarid
**Javal:** Djaval
**Jerba:** Djerba
**Jibralta:** Gibraltar
**Jibuti:** Djibouti
**Jil:** Djil
**Jilmi:** Djilmi
**Judalla:** Djudalla
**Judham:** Djudham

K

**Kairo:** Cairo
**Kajor:** Cajor
**Kalabari:** Calabar
**Kalabria:** Calabria
**Kambay:** Cambay
**Kameruni:** Cameroon
**Kanari, visiwa vya:** Canary Islands
**Kanton:** Canton
**Kantor:** Cantor
**Karibiani:** Caribbean
**Karteji:** Carthage
**Kasamansi:** Casamance
**Kastile:** Castile
**Kilimani:** Quelimane
**Koch:** Koc
**Koloni la Rasi/Cape:** Cape Colony
**Komoro:** Comoro
**Kontonu:** Contonou
**Kordoba:** Cordoba
**Krete:** Crete
**Krioli:** Creole
**Kuba:** Cuba
**Kumbi:** Koumbi (mji)
**Kupros:** Cyprus
**Kushi:** Cush
**Kwala:** Cuala

**Kwanza:** Cuanza
**Kwerimba:** Querimba
**Kwotu:** Kuotu

L

**Laghwat:** Laghouat
**Levanti:** Levant
**Lwange:** Loange
**Lwango:** Loango

M

**Maka/Makka:** Mecca
**Maldive:** Maldives
**Marekani:** U.S.A
**Mashariki ya Karibu:** Near East
**Mashariki ya Mbali:** Far East
**Maskarene:** Mascarene
**Mbwembwe:** Mbuembue
**Memfisi:** Memphis
**Meroe:** Meroe
**Metuteki:** Mertoutek
**Mfundwaji:** Initiate (n)
**Misri:** Egypt
**Mmoori/Chotara wa kiberiberi:** Moor
**Monte Kassino:** Monte Cassino
**Moroko:** Morocco

N

**Najid:** Nadjd
**Ngazija/Komoro:** Comoro
**Nili:** Nile
**Njimi:** Ndjimi
**Nova Skotia:** Nova Scotia
**Nubia/Unubi:** Nubia
**Nyamina:** Niamina
**Nyani:** Niani
**Nyoro (ya Afrika magharibi):** Nioro

O, P, R

**Omani:** Oman
**Pasifiki, Bahari ya:** Pacific Ocean
**Pembe ya Afrika:** The Horn
**Punti:** Punt
**Rumi/Roma:** Rome

S

**Sabta:** Ceuta
**Saheli:** Sahel
**Saura:** Saoura
**Shamu, bahari ya:** Red Sea
**Shamu:** Syria
**Shelif:** Chelif
**Shiroda:** Schroda
**Silsile:** Silsileh
**Sirenaika:** Cyrenaica
**Sirta:** Cirta
**Sisilia:** Sicily
**Sokotra:** Socotra
**Songhai:** Songhay
**Sudani:** Sudan
**Suezi:** Suez
**Sulemani:** Solomon

T

**Tajura:** Tadjura
**Tanja:** Tangiers
**Tegdaust:** Tegdaoust
**Theba:** Thebes
**Tilimsan:** Tlemecen
**Tissukai:** Tissoukai
**Tondidaru:** Tondidarou
**Transoksania:** Transoxania

U, V

**Ubizenti:** Byzentium
**Udachi:** Germany

**Ugriki:** Greece (Modern)
**Uhabeshi:** Abyssinia
**Uholanzi:** Netherlands/Holland
**Ujerumani/Udachi:** Germany
**Ulasia:** Eurasia
**Ushelisheli:** Seychelles
**Ussuye:** Oussouye
**Uturuki/-a Kituruki:** Turkey/ Ottoman
**Uyunani:** Greece (Ancient)
**Vatikani:** Vatican

W

**Waafari:** Afar
**Waagawu:** Agaw
**Waasaki:** Asax (people)
**Waayubi:** Ayubids
**Wabinji:** Bindji
**Wadachi:** Germans
**Wafunji:** Funj
**Wagothi:** Goths
**Wahadiya:** Hadiyya
**Wahafsi:** Hafsids
**Wahiguya:** Ouahigouya
**Waholanzi:** Dutch; Hollanders
**Wajabal:** Djabals
**Wajaksanke:** Jaxaanke
**Wajuula:** Dyula/Juula (people)
**Wakelwi:** Kel Wi (people)
**Wakikonja:** Kikondja
**Walata:** Oualata
**Wamaliki/Kimaliki:** Maliki/Malikite
**Wamarini:** Marinids
**Wamethodi:** Methodists
**Wamoravi:** Almoravids
**Wan:** Ouan
**Waorima:** Ormas
**Waottoman:** Ottomans
**Warjilan:** Wardjlan
**Wasaffari:** Saffarids
**Wasanhaja:** Sanhadja (people)
**Wasenufu:** Senoufo people
**Wasirkassi:** Circassians
**Wassulu:** Ouassoulou
**Wattasi:** Wattasids
**Wavute:** Voute
**Wayesu:** Jesuits
**West Indies:** West Indies
**Wipako Dwong:** Wipaco Dwong'
**Wuri:** Wouri

XYZ

**Yerusalemu:** Jerusalem
**Zallaka:** Zallaca

**B. ISTILAHI**

**-a ardhini:** sub-terranean
**-a Asheuli (kipindi kilichotangulia enzi za kale za mawe):** Acheulian
**-a Ateri:** Aterian
**-a barafuto:** glacial
**-a baridi:** passive
**-a biashara:** merchantilist
**-a kadiri:** moderate
**-a Kafua:** Kafuan
**-a kale sana:** primeval
**-a kando ya mto:** riverine
**-a karibu na ikweta:** sub-equatorial
**-a karibu na tropiki:** sub-tropical
-a kati ya maziwa: interlacustrine
**-a kienyeji/kijanibu:** local
**-a kifahari/-a juu:** loft
**-a kiinjili:** evangelical
**-a kikaida:** stylized

**-a kina:** profound
**-a kiosteodontokerati:** osteodontokèratic
**-a kipindi cha tatu:** tertiary
**-a Kirumi:** romance
**-a Kiyunani:** Hellenic
**-a kudhuru pande zote:** internecine
**-a kukeni:** matrilineal
**-a kulazimisha/a kudhibiti/ -a mahavu:** coercive
**-a kupenda usawa:** egalitarian
**-a kupokezana:** relay
**-a kustakimu:** sedentary
**-a kuumeni:** patrilineal
**-a Lupemha:** Lupemban
**-a majini:** aquatic
**-a makali-kuwili:** biface
**-a maumbile:** physical
**-a mawe:** lithic/stone
**-a Mosteri:** Mousterian
**-a msingi:** rudimentary
**-a mviringo:** spheroid
**-a mvua nyingi:** pluvial
**-a mwisho:** terminal
**-a mzunguko:** cyclic
**-a mzunguko:** spiral
**-a namna moja/-a hali moja:** homogeneity
**-a ncha mbili:** two-pronged
**-a pande mbili:** bilateral
**-a Sango:** Sangoan
**-a siri/-a kificho:** clandestine
**-a siri:** covert
**-a sulubu:** arduous
**-a taaluma fungamano:** interdisciplinary
**-a titio:** tectonic
**-a uchokozi:** aggressive
**-a udongo mwekundu:** terracota
**-a Ulaya Magharibi/-a Magharibi/-a Kizungu:** Western
**-a uvuguvugu:** temperate
**-a wastani/-a kiliberali:** liberal
**-a wima:** vertical
**Abiri:** navigate
**Aboti:** Abbot (mkuu wa nyumba ya watawa)
**Adilifu, -enye haki:** impartial
**Afrocentric:** a mwelekeo wa Kiafrika
**Afynu:** opium
**Agoni:** argon
**Agua/uaguzi:** divine/divination
**Aila:** collateral (family branch)
**Aina awali:** prototype
**Akiki:** cornelian
**Akiolojia:** archaeology
**Akisi:** reflect
**Akropolis:** Acropolis
**Alabasta/jasi:** alabaster
**Alama:** sign
**Alluvial:** - kitope
**Amali/kazi:** career
**Amazoniti:** Amazonite
**Ambari:** ambergis
**Amiri(1):** Amiri/Emir
**Amiri(2):** Amirian
**Analojia:** analogy
**Anatomia:** analomy
**Anfa:** Anfatian
**Angahewa:** atmosphere
**Anthropolojia:** anthropology
**Anthropometa:** anthropometric
**Anza/anzisha:** embark
**Arabisha:** arabize
**Arami:** Aramaic
**Asheuli:** Acheuli
**Asilia/-a mapokeo:** orthodox
**Askari wa farasi:** cavalry
**Askari wa Kituruki:** janissary
**Askofu:** Bishop

**Ateri:** Aterian
**Athari:** implication
**Atlanthropo:** Atlanthropus
**Australopitheko:** Australopithecus

B

**Baa:** disaster
**Babe; babekaya:** patriarch
**Babu/mababu:** ançestor (s)
**Baganda/jamii ya Baganda:** Baganda
**Bahari Kuu:** ocean
**Bara(1)/kontinenti:** continent
**Bara(2):** hinterland/inland
**Barafuto:** glacier
**Barakala:** opportunist
**Barakoa:** cloth mask
**Baraza:** palaver/court
**Bari:** barium
**Basanti:** basalt
**Batli:** ship's log
**Bedui:** Beduin
**Bepari:** capitalist
**Biashara:** commerce; trade
**Biashara ya watumwa:** slave trade
**Biasharanje:** exports
**Bidaa:** innovation
**Bidhaa:** commodity
**Bidhaa:** goods
**Bidhaa za matumizi:** consumer goods
**Biokemia:** biochemistry
**Bluu iliyoiva:** indigo
**Bobari:** gouge
**Boma:** compound; kraal
**Bonde:** basin
**Bresia:** Breccia
**Bubalusi (aina ya paa):** bubalus
**Bubu:** boubou
**Buchari:** cleaver
**Buhuri:** frankincense
**Burini:** burin
**Busto (sanamu ya kichwa na kifua):** bust

C

**Chadanthropo:** Chadanthropus
**Chama/tapo/vuguvugu:** movement
**Changamani/ -a mseto:** syncretic (adj)
**Changamano/tanzo:** complex
**Changarawe za milimani:** scree
**Changuka:** disintegrate
**Chanzo/chimbuko:** origin; source
**Chavua:** pollen grains
**Chaza:** oyter
**Chenga, kipande:** fragment
**Chenguka, ku-:** to fragment
**Chifu:** chief (usually autonomous)
**Chimere:** Cimere
**Chochea:** agitate
**Chonge/jino la mbele:** incisor
**Choroa:** orynx
**Chotara:** mulatto
**Chotara wa Kiberiberi/Mmoori:** Moor

D

**Dalali:** broker
**Damaski:** Damask
**Darajia:** level
**Darubini:** telescope; binocular
**Demografia:** demography
**Dhahiri/thabiti:** tangible
**Dhanachapwa:** steriotype
**Dhalimu:** despot
**Dhibiti:** control

**Dhima/amali:** function
**Dhuria:** descendant
**Diabasi:** diabase
**Diaspora/sehemu za mtawayiko:** Diaspora
**Dini:** religion
**Dini ya kimasihi:** messianic religion
**Dioriti:** diorite
**Diskoidi:** discoid
**Dogma:** dogma
**Dola/ nchi/ jimbo:** State
**Dola/nchi twawa:** vassal state
**Dola unganifu:** centralized state
**Doleriti:** dolerite
**Duara:** circle
**Duhuli:** import
**Dukiza,ji-:** intrude
**Dukizo:** intrusion
**Dunia:** earth
**Durusu:** revise

E

**Ekolojia:** ecology
**Eledi:** shrewed
**Elektroni:** electron
**Elemeo:** tendency
**Endeleza(1):** protract
**Endeleza(2):** develop
**Endeleza(3)/kuza:** enhance
**Enea:** diffuse
**Eneolithi:** Aeneolithic
**Enye kudandia:** brachial
**Enye kuzunguka/tembezi:** itinerant
**Enye mabonde na miinuko:** undulating
**Enzi ya mawe:** stone age
**Enzi/zama (1):** age; era; epoch
**Enzi (2):** sway
**Enzi Mpya ya Mawe:** New Stone Age
**Enzi ya Chuma:** Iron Age
**Enzi ya Kati ya Mawe:** Middle Stone Age
**Enzi ya Mwanzo ya Mawe:** Early Stone Age
**Enzi ya Nyuma ya Mawe:** Late Stone Age
**Eosini:** eocene
**Epidemolojia:** epidemology
**Epidoti:** epidote
**Erevu, -epesi kung'amua:** astute
**Ethnografia:** ethnography

F

**Fahiwa:** sense
**Falsafa:** philosophy
**Falsafa ya sheria:** jurisprudence
**Famaliolojia:** pharmacology
**Famasia:** pharmacy
**Faraka:** sect
**Fasihi:** literature
**Fauna, wanyama:** fauna
**Fauresmithi:** Fauresmith
**Fedha/ajenti:** silver
**Fenomena:** phenomenon
**Fenza:** faience
**Ferikriti:** ferricrete
**Fidia(kt):** recoup
**Fidia(n):** restitution
**Fifia(1):** decline
**Fifia(2)/oza:** decay
**Fikia (upeo au hatua fulani):** culminate
**Filolojia:** philology
**Fizikia:** physics
**Fiziognomia:** physiognomy
**Fiziolojia:** physiology
**Flinti:** flint

**Flora:** mimea
**Foeniki:** Phoenician
**Fonolojia:** phonology
**Fuawe:** anvil
**Fundi-mchundo:** artisan
**Fundistadi:** craftsperson
**Fungu la/mfululizo wa milima:** massif
**Funguvisiwa:** archipelago
**Funo:** duiker
**Fununu:** clue
**Fuwawe:** punice stone
**Fuwele:** crystal

G

**Galena:** galena
**Gamblia:** Gamblian
**Gastropodi:** gastropod
**Gesi:** gas
**Geuza/badilisha:** reform
**Ghafi:** crude
**Gliseroli:** glycerol
**Gramina (aina ya nyasi):** gramineae
**Gudulia:** vase
**Gumba/baa la njaa:** famine
**Gunzi:** Günz

H

**Hadithi/masimulizi:** tale
**Hadubini:** microscope
**Hagiografia/uandishi kuhusu maisha ya watakatifu:** hagiography
**Hai:** active
**Hajira:** migration
**Hakiki:** vet
**Hakipekee:** prerogative
**Halijoto:** temperature
**Hali ya hewa:** climate
**Hamatani/pepo za kipupwe:** harmattan
**Hami/Wahami:** Hamite (s)
**Hangaiko/ uchungu wa moyoni:** chagrin
**Harakati/mapambano:** struggle
**Haram:** pyramid
**Haramia:** pirate
**Harimu:** Harem
**Harunia:** Harounian
**Hatarisha:** expose
**Hataza:** patent
**Hati unganishi:** cursive script
**Hati(1)/waraka:** document
**Hati(2) (ya maandishi):** script
**Hatua kwa hatua:** piece-meal
**Hawilisha:** transfer
**Hazimu:** appropriate (?)
**Heba/haiba kubwa:** charisma
**Hegemonia:** hegemony
**Hematiti:** hematite
**Hidrografia:** hidrography
**Hierografia/hatimchoro:** hieroglyphy
**Hilobatidi:** hylobatidae
**Himaya:** empire
**Himaya:** stronghold
**Himiza:** encourage
**Hirimu/rika:** age group
**Historiografia**: historiography
**Holosini:** Holocene
**Hominidi awali:** pre hominid
**Hominidi:** hominid
**Homo:** homo
**Homo faberi:** Homo faber
**Homo habili:** Homo habilis
**Homo sapi:** Homo sapiens
**Hongo, ushuru:** tribute

I

**Idilisha, chechemua:** stimulate
**Ikulu/jumba la mfalme/kitala:** palace
**Ikweta:** Equator
**Ilhamu/kariha:** inspiration
**Iliochanganywa:** compounded
**Iliyogawanyika:** segmentary
**Imani za kiroho:** mysticism
**Inadi/udogma:** dogmatism
**Ingilia (mali ya mtu mwingine):** encroach
**Ingiliana/mwingiliano:** interact/interaction
**Iosini:** Eocene
**Ishara:** symbol
**Isiodhahiri:** Indirect
**Isiokikomo:** timeless
**Isiokwisha/-a kurudiwarudiwa:** incessant
**Isiopevuka:** naive
**Isiyopenyeka/isiyoingilika:** impregnable
**Itale/graniti:** granite
**Itikadi:** ideology
**Itikeli:** ethics

J

**Jaala:** fate
**Jabrudia:** Jabrudian
**Jadeiti:** jadeite
**Jaha:** glory
**Jalizi:** auxiliary
**Jalizia:** supplement
**Jalo:** Djalo
**Jamaa:** relations
**Jamaa/jamii/familia:** family
**Jamia/mbari kuu:** race
**Jamii:** society
**Jamii ya kijadi:** traditional society
**Janibu:** locality
**Jarabati:** empirical
**Jasperi:** Jasper
**Jasuri:** adventurer
**Jenasi:** genus
**Jenetiki:** genetic
**Jeramna/Wajeramna:** Djeramna
**Jerontokrasia:** gerontocracy
**Jibu/jibizo/itiko:** reaction
**Jimbi:** cocoyam/taro
**Jimbo/mkoa:** canton
**Jinasibisha:** adapt oneself
**Jiolojia:** geology
**Jiomofolojia:** geomorphology
**Jiosumaku:** geomagnetic
**Jiwe la talki:** soapstone
**Jiwemoto:** silex
**Jumuishi:** encompassing
**Jumuiya:** community
**Juso/kizuizui/kinyago:** mask
**Jusura:** adventure
**Juula:** Dyula

K

**Kabaila:** aristocrat; big landowner
**Kabila/mbari/jamii:** ethnic group
**Kabla ya Sasa (KS):** Before Present (BP)
**Kaboni dioksidi:** carbon dioxide
**Kaburi:** Tomb
**Kadiria umri:** date
**Kafara:** sacrifice
**Kafiri:** infidel
**Kaharabu:** amber
**Kahini/mtabiri:** oracle
**Kainozoiki/senozoiki:** Cenozoic
**Kaka:** shell
**Kakara:** rush (n)
**Kalabria:** Calabrian

**Kalautala:** stereotype
**Kaledoni:** Caledonite
**Kali/potasi:** pottasium
**Kalisi(1):** calsium
**Kalisi(2):** chalice
**Kalisidoni:** chalcedony
**Kalsite:** calcite
**Kambi:** encampment; camp
**Kani:** force; energy
**kanindani, fukuto:** dynamics
**Kantara/penyezi:** bridgehead
**Kanuni:** principle; code
**Kanza, ku:** to smoke (dry in the smoke);
**Kanzi:** repository
**Kaolini:** kaolin
**Kapsia:** Capsian
**Kariha/muhu/uhamasisho/ msukumo:** inspiration
**Karne:** century
**Karnelia:** carnelian
**Kata nakshi:** engrave
**Katalogi:** catalogue
**Katarrina:** cartarrhina
**Kategoria:** category
**Kauri:** porcelain; ceramics
**Kaya:** homestead; household
**Kemia:** chemistry
**Kerkopitheko:** Cercopithecus
**Khalifa:** Caliph
**Khufu/Kopti:** Coptic
**Kiafrika-Kiasia:** Afro-Asiatic
**Kiafrikaana:** Africaans
**Kiambishi:** affix
**Kiambishi awali:** prefix
**Kiambishi-tamati:** suffix
**Kibantu-mama:** proto-Bantu
**Kibaraka:** collaborator; puppet; vassal
**Kibuyu:** calabash
**Kichocheo:** motivation
**Kichokoo/kipengele:** factor
**Kideni:** Danish
**Kidoko:** click
**Kifani:** model
**Kifinyange:** ceramic; pottery
**Kigange:** Ostracow
**Kigezo:** standard
**Kigoda:** stool
**Kigoda cha Dhahabu:** Golden Stool
**Kigumba:** arrow-head
**Kijikundi:** subgroup
**Kijisanamu:** figurine
**Kijitabaka:** strata
**Kijito:** tributary
**Kikiasi/kisifa:** quantitative/qualitative
**kikinga upepo:** wind break
**Kikoa/mwimo:** axis
**Kikombo:** scraper
**Kikwi/milenia:** millenium
**Kilimati:** climate
**Kilindi (cha bahari):** deep sea
**Kimelea:** parasite
**Kina:** rhyme
**Kinu:** mortar
**Kinubi:** lyre
**Kinyago:** mask; sculpture
**Kinyang'anyiro/kugombania:** scramble
**Kiolezo:** template
**Kionjo:** taste
**Kipindi kisichokuwa na mtawala:** interregnum
**Kipindi cha kati ya barafu:** interglacial period
**Kipindupindu:** cholera
**Kipiribao:** viper
**Kiramba, kishenshe:** palm/raffia cloth
**Kisakale:** legend

**Kisasili:** myth
**Kisawe/sinonimu:** synonym
**Kishoka/kichanjia:** chopper
**Kisifa:** qualitative
**Kisimbwi:** continental shelf
**Kisingo:** headdress (traditional)
**Kisukuku:** fossil
**Kiswidi:** Swedish
**Kita/imarisha:** entrench
**Kitala/Ikulu:** royal court
**Kitanguakimbunga:** anticyclone
**Kitenzi:** verb
**Kitimbo:** digging stick
**Kitovu:** focus
**Kitu yakinifu:** material thing
**Kituo cha kuhifadhi na kusambaza bidhaa:** entreport
**Kiunga:** plantation
**Kiunzi/skeletoni:** skeleton
**Kiunziakili:** mental framework
**Kiviga:** rite
**Kivinginyo/duara:** gyre
**Kivuli cha maana:** shade of meaning
**Kiwakilishi:** pronoun
**Kiwanda/shughuli ya biashara:** enterprise
**Kiwesley:** Wesleyan
**Kizalia/vizalia:** offspring
**Kizazi:** generation
**Kizimu:** totem
**Kizuizui:** mask
**Klaktonia:** Clactonian
**Kliori:** Creole
**Kodi isiyodhihirika/kodi ya kificho:** indirect tax
**Kola:** kola nut
**Koloni la kifalme:** crown colony
**Komesha/futa:** eradicate
**Kongamano:** symposium
**Konsonanti:** consonant
**Konstantini:** Constantine
**Korongo:** gorge
**Kosmogonia:** cosmogony
**Kotama:** sickle
**Kronolojia:** chronology
**Kronostratigrafia:** Chronostratigraphy
**Kufuru:** profane
**Kugawa/kuunganifua madaraka:** decentralization
**Kuingia kwa wingi:** influx
**Kuingilia/kujitia kati:** intervention
**Kujihini:** self denial
**Kujitanibu:** isolation
**Kujitawala:** autonomy; self rule
**Kujitawala/mamlaka/uhuru:** sovereignity
**Kukua/kubadilika/ukuo:** evolution
**Kundi la miungu:** pantheon
**Kupoteza imani:** disenchantment
**Kupri:** copper
**Kurani:** Quoran/Koran
**Kuruba:** curve
**Kusini mwa Sahara:** sub-Sahara
**Kutawaliwa/kuganganiizwa:** subjection
**Kutiisha/kutumikisha:** subjugation
**Kutotengemaa/kuyumbayumba:** instability
**Kuyumba/kutangaganga:** vacillation
**Kwa kuashiria:** indirectly
**Kwaga (mnyama kama pundamilia):** Qwagga
**Kwapua:** annex
**Kwatenari:** Quaternary
**Kwatzi:** quartz
**Kwatziti:** quartzite

**Kweli tupu/halisi:** down-to-earth

L

**Lahaja:** dialect
**Lamela:** lamella
**Latitudo:** Latitude
**Leksika:** lexical
**Lidianiti:** lydianite
**Linganifu:** consistent
**Linganishi:** comparative
**Liturujia/litujia:** liturgia
**Lodi:** Lord; nobleman
**Longitudo:** Longitude
**Lugha ambishi:** agglutinative language
**Lugha ya toni:** tonal language
**Luja:** wave

M

**Maada:** matter
**Maafa:** disaster
**Maarufu/mashuhuri:** prominent
**Maasi/uasi:** rebellion
**Maasi/upinzani:** insurrection
**Maathura/mwathirika:** victim
**Mabadiliko/evolusheni:** evolution
**Mabadiliko ya kupanda na kushuka:** fluctuations
**Mabaki:** vestiges; remains
**Mabishano/ubishani:** disputation/polemics
**Machezo/tamasha:** carnival
**Madhehebu/ada ya uzazi:** fertility cult
**Madodoso (ya awali):** overtures
**Maduhuli/bidhaa zinazoingia:** import(s)
**Maelezo/masimulizi:** account
**Maezi:** anchorage
**Mafundo:** initiation
**Mafunjo:** papyrus (reeds)
**Mafuta ya mawese:** palm oil
**Mageuzi:** reforms
**Mahitajio:** demands
**Mahuruji:** export(s)
**Maji ya kunde:** light skinned
**Majina:** nomenclature
**Majusi (1):** Zoroastrian
**Majusi(2)/msihiri:** magician
**Makabaila/malodi:** nobles
**Makabiliano ya ana kwa ana:** confrontation
**Makamu Mkuu wa Jeshi la Wanamaji:** Vice Admiral
**Maki:** layer
**Makimbilio:** refuge
**Makutano/ndagano:** confluence
**Malakite:** malachite
**Malale:** trypanosomiasis
**Malalo:** lair
**Maliki:** emperor
**Malodi:** nobility
**Mama:** proto
**Mama-Malkia:** Queen Mother
**Mamalia:** mammal
**Mame-Bantu: proto Bantu**
**Mamlaka** unganifu: centralized authority
**Mamlaka-pacha:** diarchy
**Mandhari:** terrain/ setting/landscape
**Manemane:** myrrh
**Mangani:** manganese
**Manju mtembezi:** troubadour
**Mapadre Weupe:** White Fathers
**Mapenzi juu ya binadamu/filantropia:** philanthropy
**Mapigano ya wenyewe kwa wenyewe:** civil conflicts

**Mapinduzi:** revolution
**Mapokeo huru:** independent tradition
**Mapokeo simulizi:** oral tradition
**Mapululu:** steppe
**Maridhiano:** compromise
**Masegego:** premolar
**Masihi/Kimasihi:** Messiah/Messianic
**Masihiya/-a Kikristo:** Christian
**Maslahi:** interest
**Matamanio/matakwa:** aspirations
**Matbaa/kiwanda cha uchapaji:** press (printing)
**Mateka:** captive
**Matilaba:** imperative(s)
**Matini simulizi:** oral text
**Matini:** text
**Mauaji (ya mtu mashuhuri):** assassination
**Mauaji ya baba:** patricidal
**Maudhui:** content
**Mawanda:** scope
**Mazingira ya kinamasi:** swampy habitat
**Mbandwa, kahini:** spirit medium
**Mbari kuu:** race
**Mbari/kabila:** ethnic group
**Mbinu za kujeya:** flaking techniques
**Mbirikimo:** Pygmy
**Mbuga (ya nyasi):** grassland
**Mbuga chachu:** sourveld
**Mbuga/pululu:** steppe
**Mbuga tamu:** sweetveld
**Mcha Mungu:** Murabit (holy man)
**Mchakato/wendo/mwendeleo:** process
**Mchanganıani:** syncretic (n)
**Mchanganyo:** compound
**Mchanguko:** disintegration
**Mchawi:** witch doctor
**Mchokozi:** aggressor
**Mchoro wa mapangoni/miambani:** rock painting
**Mdachi/Mjerumani:** German
**Mdeni, wa-:** Dane(s)
**Medani:** Theatre (of conflict)
**Melanini:** melanin
**Melezi/maezi:** anchorages
**Menyu:** pure
**Metalujia:** metallurgy
**Meza/funika kabisa:** engulf
**Mfalme mkuu:** paramount king
**Mfalme:** monarch/king
**Mfanano/mshabaha:** affinity
**Mfanya biashara/mchuuzi:** trader
**Mfanya biashara:** merchant
**Mfekane:** Mfecane
**Mfoko (wa wasiwasi):** upsurge
**Mfua:** smith
**Mfuasi:** disciple
**Mfugaji:** pastoralist
**Mfumo/mtandao:** network
**Mfumu/kahini:** oracle
**Mganga:** medicineperson; healer
**Mgimba/mganga wa mvua:** rain maker
**Mgogoro/zahama:** crisis
**Mgogoro/mgongano:** conflict
**Mhariji/wahariji:** exporter(s)
**Mhashamu:** Monsignor/Mgr
**Mhazeli:** hazel (plant)
**Mholanzi:** Dutch
**Mikrokemikali:** microchemical
**Mikrolithi:** microlithic
**Mila ya unyumba:** ritual intercourse
**Milenia/kikwi:** millennium

**Miosini:** miocene
**Mirathi:** legacy
**Mise/kokwa za mawese:** palm kernal
**Misri ya Chini:** Lower Egypt
**Misri ya Juu:** Upper Egypt
**Miwati:** wattle
**Mizengwe/kutawala kijanja:** manipulation
**Mjasirimali/mwekezaji:** entrepreneur
**Mji mkubwa/makao makuu:** metropolis
**Mjujube:** jujube plant
**Mkabala:** approach
**Mkataba:** treaty
**Mkazi:** burgher
**Mkingamo:** intersection
**Mkinzani/adui:** adversary
**Mkoa/jimbo:** province
**Mkongano:** cohesion
**Mkuo (wa shaba, dhahabu, n.k.):** bar, ingot, nugget (of copper, gold, etc)
**Mla mizoga:** scavenger
**Mlandano:** homogeneity
**Mlangobahari:** channel
**Mlangomto:** estuary
**Mlumba/mbugu:** bark cloth
**Mnara:** minaret
**Mnara wa ukumbusho/kumbukumbu:** monument
**Mnasaba:** symbiosis
**Mnasihi:** mentor
**Mnomadi/wanomadi/ walıamahamaji:** Nomad/Nomads
**Mnyweo:** evaporation
**Mode of production:** mtindo wa uzalishaji mali
**Modeli:** model
**Mofolojia:** mophology
**Momonyoa:** erode
**Monofisita:** Monophysite
**Monografia:** monography
**Morali:** morale
**Motifu:** motif
**Moyo wa kujituma:** initiative
**Mozarabi/Wa- :** Mozarabs
**Mpangilio/mtandazo:** layout
**Mpelelezi:** explorer
**Mpiganaji/askari:** warrior
**Mpini/kutia mpini:** haft, handle/to haft
**Mpito/uhawili:** transition
**Mporaji/mteka nyara:** marauder
**Mrindimo:** vibration
**Mrumi:** Roman
**Msamiati:** lexicon/vocabulary
**Msanii:** artist
**Msharasi:** awl
**Mshea:** shea tree
**Mshikamano:** solidarity
**Mshindani:** rival
**Msimamo:** stance
**Msimbo:** code
**Msimulizi/mtambaji:** narrator
**Msonge wa madaraka:** political hierachy
**Msukosuko:** upheaval; instability
**Msukumo, kichocheo:** impetus
**Mswidi, wa-:** Swede
**Mtabiri:** seer
**Mtafaruku/zahama:** crisis
**Mtaji, rasilmali:** capital
**Mtambaachi:** reptile
**Mtandao:** network
**Mtapo chuma:** iron ore
**Mtapo:** ore
**Mtarihi:** chronicler
**Mtawala mkuu:** central ruler
**Mtazamo:** outlook

**Mtemi:** traditional and autonomous chief
**Mtetemo:** vibration
**Mtindo wa uzalishaji:** mode of productiou
**Mtirangi**: dyewood
**Mtwawa:** vassal
**Muamala/mapatano ya biashara:** transaction
**Muda wa kumiliki/kushika cheo:** tenure
**Mujarabu:** tested
**Muktadha:** context
**Mumi:** mummy; maiti iliyohifadhiwa kwa kutiwa mumiani
**Mungu:** God; Allah
**Muongo:** decade
**Murabiti/warabiti:** marabout
**Muswada:** manuscript
**Muundo:** structure
**Muunganiko:** confederation
**Muungu:** deity
**Muwasala:** contact
**Mvinginyo:** gyration
**Mvutano/fadhaa:** tension
**Mvuvumko/mzinduko:** Renaissance
**Mwachano wa kijeni:** genetic drift
**Mwainisho:** classification
**Mwaloni:** oak
**Mwamba:** rock
**Mwamba masapo/tabaka:** sedimentary rock
**Mwamba wa volkano:** tuff
**Mwamili:** functionalist
**Mwana mapinduzi:** revolutionary; revolutionist
**Mwanamageuzi:** reformer
**Mwanana:** delicate
**Mwanashajara/mnasabu:** genealogist
**Mwanasilia/mwanajadi:** traditionalist
**Mwanazuoni:** scholar
**Mwangalizi:** regent
**Mwasho/mwako:** ignition
**Mwavi:** nettle tree
**Mwekezaji:** investor
**Mwelekeo pewa:** centrifugal
**Mwelekeo tovu:** centripetal
**Mwelezi:** cedar
**Mwendeleo:** continuum
**Mwiba wa kigumba/ndaka:** barb
**Mwimo:** column
**Mwinuko:** relief
**Mwinyi:** lord; aristocrat
**Mwondoko/mguro:** movement (moving)
**Myunani:** Ancient Greek
**Mzingiro:** siege
**Mzingo/pindi**: bend
**Mzozo/ugomvi:** wrangle

N

**Nadharia tete:** hypothesis
**Nasaba(1):** lineage
**Nasaba(2) (tawala):** dynasty
**Nasabu:** genealogy
**Natija**: outcome (?)
**Natiri:** sodium
**Natiri kabonati:** sodium carbonate
**Nchi:** country
**Nchi/tawala:** principality
**Ndagano/makutano**: confluence
**Nduni:** characteristic; aspect; feature
**Nembo:** emblem
**Neolithi/Zama Mpya za Mawe:**

Neolithic
**Neolithisha:** Neolithize
**Ngegu:** laterite
**Ngeu/ngegu:** ochre
**Nguvu/ari:** dynamism
**Nguvu za uzalishaji:** productive forces
**Nguvu-uzima:** vital force
**Nikeli/madini ya fedha:** nickel
**Nitrojeni:** nitrogen
**Nomino:** noun
**Nukuu/unukuzi:** transcribe/transcription
**Nusu-kipenyo:** radius
**Nutroni:** neutron
**Nyumha ya watawa:** monastery
**Nyumbu:** wildebeeste
**Nywele:** hair
**Nywele za singa:** straight hair
**Nywele za kitani/msokoto:** fuzzy hair
**Nywele za kipilipili:** wooly hair
**Nyweshea:** irrigate

O

**Oana kimseto:** intermarry
**Oasisi:** oasis
**Obsidi:** Obsidian
**Ojite:** Augite
**Ombwe:** void
**Onamastika:** onamastics
**Ottomani:** Ottoman

P

**Palae-:** pale-
**Paleakiolojia:** palaearchaeology
**Palebotania:** palaebotany
**Paleolithi:** paleolithic
**Paleontolojia:** palaeontology
**Paleosini:** Paleocene
**Palinolojia:** palynology
**Pambana:** contend
**Pampa, savana:** The Pampas
**Pangilia/panga/ratibu:** organize
**Papuri/karatasi za sisha:** papyrus (paper)
**Parishi/parokia:** parish
**Pedolojia:** pedology
**Pembezoni:** periphery
**Penyezi/kantara:** bridgehead
**Pepo za msimu:** monsoon (winds)
**Petroglafia:** petroglyph
**Pigo, mshtuko mkubwa:** brunt
**Pindi/mzingo:** Bend (of river)
**Piramidi/haram:** pyramid
**Pithekantropi:** Pithecanthropine
**Plani:** plan
**Planktoni:** plankton
**Platirrina:** Platyrrhina
**Plau:** plough
**Plaubembea:** swing plau
**Pleistosini:** Pleistocene
**Plioplestosini:** pliopleistocene
**Pliosini:** pliocene
**Plumbi sulfidi:** lead sulphide
**Pogo:** lopsided
**Polihedroni:** polyhedron
**Pongide:** pongidae
**Pongidi:** pongid
**Pongo:** bushbuck
**Pora/teka nyara:** plunder
**Potosha:** distort
**Primata:** primate
**Production:** uzalishaji mali
**Propaganda:** propaganda
**Prosimia:** pro-Simian
**Pundela:** pundela

R

**Radiografia:** radiography
**Radiokaboni:** radiocarbon
**Radiometa:** radiometre
**Raghba/sbauku:** interest
**Raghba, ari:** zeal; interest
**Raia:** subject
**Rasi:** cape/promontory
**Regalia/nembo:** regalia
**Rejesha (katika hali/maisha ya kawaida):** rehabilitate
**Rejimenti/kikosi:** regiment
**Rekebisha:** adapt
**Riba:** interest (bank, lending)
**Rika/hirimu:** age group
**Rikabu (wanyama wa kusafiria):** mount
**Rudisha hadhi:** rehabilitate
**Ruwaza/sulubu:** pattern

S

**Safari ndefu/treki:** trek
**Sagagego:** premolar
**Saikolojia:** psychology
**Saisi:** groom
**Sambaratika:** disintegrate
**Sanaa za maumbo:** plastic arts
**Sanaa ya ukutani:** mural
**Sanaajadiya/fanijadiiya:** folklore
**Sandarusi:** gum
**Sasisha/fanya ya kisasa:** modernize
**Satini:** satin
**Sawidi (kt):** draft (v)
**Sedimentolojia:** sedimetology
**Sekopithesidi:** Cercopithecidae
**Semiti/Wasemiti:** Semite (s)
**Sentimeta/sentimita:** centimeter
**Septa:** septum
**Serikali unganifu/ kuu:** central government
**Serikali ya wachache:** oligarchy
**Setla/mlowezi:** settler
**Shaba nyeusi:** bronze
**Shaba nyekundu/kupri:** copper
**Shadidi:** intensive
**Shahidi (wa imani):** martyr
**Shajara(1):** diary
**Shajara(2)/nasabu:** genealogy
**Shamba:** country; rural area; cultivated land
**Sharia:** Islamic law
**Shazia/msharasi:** awl
**Shehe/sheikh:** Shaykh
**Shellea:** Chellean
**Sheria za mila/jadi:** customery law
**Sheria:** lex (k.m. Lex Hadriana: Sheria ya Hadriana)
**Sheria:** law
**Shinda/tiisha/teka:** conquer
**Shindwa:** succumb
**Shirika, tarika:** religious order
**Shirikisho:** federation
**Shisti:** schist
**Sboka:** axe
**Shoka la mkono:** handaxe
**Shore:** crest
**Shujaa:** hero
**Siagi ya mshea:** sheabutter
**Sifa bainifu:** trait
**Silabi:** syllable
**Silikati:** silicate
**Simba:** codify
**Simbi/kauri:** cowry
**Simia:** Simian
**Similisha:** assimilate

**Simulizi:** oral
**-Siokalika:** uninhabitable
**-Siotokeza:** recessive
**Sisha:** papyrus pith
**Sitara:** shelter
**Sokota pamoja:** entwined
**Sokwe:** chimpanzee; ape
**Sokwe-mtu:** orangutang
**Sosiolojia:** Sociology
**Spektografia:** spectograph
**Spishi:** species
**Stratigrafia:** stratigraphy
**Sufii:** sufi; holy person; monk
**Sufuri/shaba nyekundu:** brass
**Suhula/nyenzo:** facility/facilities
**Suhulisha:** facilitate
**Sulubu/ruwaza:** pattern
**Susu:** cradle

T

**Taaluma ya Misri ya Kale/Misriolojia:** Egyptology
**Taamuli:** meditation
**Taathira:** impact
**Tabaka la wakwasi:** leisured class
**Tabaka la kiamali/tabaka-amili:** caste
**Tabaka (la dhahabu):** seam (of gold)
**Tabaka la makabaila:** aristocracy
**Tabakisha:** stratify
**Tabdili:** version
**Tafiri**: frustrate
**Tafsili:** interpretation
**Tahafifu/unafuu:** concession
**Taja:** cite; mention
**Tajiriba/uzoefu:** experience
**Takadiri:** destiny
**Takriban (t.):** circa (c.)
**Takua:** piety
**Tamadunisha:** acculturate
**Tamalaki/mtamalaki:** conquer/conqueror
**Tambulisha:** characterize
**Tangaza rasmi:** promulgate
**Tangua:** abrogate
**Tanzo/changamano:** complex
**Tao (dogo):** lobate arc
**Tapo/shule ya mawazo:** school of thought
**Tarihi:** chronicle
**Tarihia/kronolojia:** chronology
**Tarika/udugu:** brotherhood
**Tasnia:** industry
**Tasnia ya Wilton:** Wilton Industry, n.k.
**Tata:** complex
**Tawala:** dominant (mf. tabaka tawala)
**Tebo/jedwali:** table
**Teka/twaa:** annex
**Telegrafu/simu ya kuandika:** telegraph
**Tendeza:** activate
**Teokrasia:** theocracy
**Teolojia:** theology
**Terakota:** terracotta
**Thabiti:** strong; valid
**Thori:** thorium
**Tia akilini:** imbibe
**Tiba-jumui:** group healing
**Tiger:** chuimilia
**Timamu:** detail
**Timbe/mtapo:** ore
**Toa utumwani:** manumit
**Tohoa:** adapt
**Tokeo:** result
**Tondoti:** detail(s)
**Toni:** tone
**Tool:** zana

**Topografia:** topography
**Toponimia:** toponym
**Towashi:** eunuch
**Towe:** clay
**Trapezoidi:** trapezoid
**Tukio:** episode
**Tuliza:** placate
**Tumbawe:** coral
**Tumiliwa/tumilizi:** applied
**Tungamanisha:** integrate
**Tungazi:** terrace
**Ture:** Toure (name of person)
**Tuta la mchanga:** sand dune
**Twaa:** conquer (v)
**Twaa (n):** sphere of influence

U

**Uainishi:** typology
**Uamili:** functionalism
**Uamsho/mzinduko/mvuvumko:** Rennaisance
**Uasi/maasi:** rebellion
**Ubarakala:** opportunism
**Ubishani:** controversy
**Ubwe/mbwe:** pebbles
**Uchamungu:** piety
**Uchangamani:** syncretism
**Uchanganuzi:** analysis
**Uchanjaji chale:** scarification
**Uchifu:** chiefdom; chieftaincy
**Uchimbuzi:** excavation
**Uchochezi:** agitation
**Udhalimu:** despotism
**Udhanifu:** idealism
**Uelekeo:** direction
**Ufalme:** kingdom
**Ufalme Mkongwe (wa Misri):** Old Kingdom
**Ufalme wa Zama za Kati (wa Misri):** Middle Kingdom
**Ufalme Mpya (wa Misri):** New Kingdom
**Ufanano:** homogeneity
**Ufinyanzi/mfinyanzi:** pottery/potter
**Ufugaji:** pastoralism
**Ufuo:** shoreline
**Ugasumaku:** magnetic field
**Ugimba:** rain-making
**Uhai:** vitality
**Uhalisia:** realism
**Uharibifu mkubwa:** depredation
**Uhuru/kujitawala:** independence
**Uimara/ wepesi wa kujirekebisha:** resilience
**Ujeya (njeya):** flake(s)
**Ujirani:** proximity
**Ujumlisho:** generalization
**Ujusi/sihiri:** magic
**Ukabaila:** feudalism
**Ukadiri:** moderation
**Ukali/ukatili:** ferocity
**Ukali/mkazo:** intensity
**Ukanda/zoni:** zone
**Ukanda/eneo:** region
**Ukanindani:** dynamism
**Ukhalifa:** caliphate
**Ukilia:** determine
**Ukinzano:** contradiction
**Ukiritimba/uhodhi:** monopoly
**Ukaneshaji utumwa:** abolition (of slavery)
**Ukoo:** clan
**Ukuo/ukuzi:** evolution
**Ukwapuzi:** annexation
**Ukwasi:** opulence
**Ulikaji:** weathering
**Ulimwengu:** universe
**Ulinganifu:** equilibrium
**Ulokole:** fundamentalism
**Ulolo ntwawa:** vassalage

**Ulumbi/ufasaha wa lugha:** rhetoric
**Umiundo:** structuralism
**Umma:** populace
**Umoja:** unity
**Unasaba/udugu wa damu:** kinship
**Unasi:** populism
**Unda upya:** reconstruct
**Unda:** construct; manufacture
**Unganifu/enye mamlaka kuu:** centralized
**Unganifua:** de-centralize
**Ungaunga wa dhahabu:** gold dust
**Unyevuhewa:** humidity
**Uongozi:** helm
**Uowevu/unyevu:** moisture
**Upatanishi:** mediation
**Upungufu/uhaba:** dearth
**Urani:** Uranium
**Urari hafifu:** delicate balance
**Urasimi:** classicism
**Urazini:** consciousness
**Urea:** urea
**Urithi (wa utawala):** succesion
**Usawa:** equity
**Usawa wa bahari:** sea level
**Usemi:** saying
**Ushahidi/ushuhuda:** testimony
**Ushoroba:** corridor
**Ushuhuda simulizi:** oral testimony
**Usimilishaji:** assimilation
**Ustaarabu:** civilization
**Ustadi/ubunifu:** ingenuity
**Usuli:** background
**Utamaduni:** culture
**Utamaduni yanikinifu:** material culture (?)
**Utamakani wa watu:** peopling
**Utamalaki:** supremacy; conquest
**Utambulisho:** identity
**Utambuzi:** enlightenment
**Utando:** crust; patina
**Utando barafu:** ice sheet
**Utangamano:** harmony
**Utani:** joking relationship
**Utanzo:** complex
**Utanzu:** genre
**Utata:** ambiguity; complexity
**Utawala bayana:** direct rule
**Utawalafiche:** indirect rule
**Utawala wa kidini:** theocracy
**Utawala huria:** anarchy
**Utawalamsonge:** bureaucracy
**Utendi:** epic
**Utengemano/uthabiti:** stability
**Utengemano:** stability
**Utengenezaji/usindikaji:** processing
**Uteuzi asili:** natural selection
**Utondoti:** detail(s)
**Utumwa:** slavery
**Utumwa wa viungani:** plantation slavery
**Utwazi:** supremacy
**Uukilizi:** determinism
**Uundaji miji:** urbanization
**Uunganifishaji:** centralization
**Uvamizi wa ghafla:** incursion
**Uvamizi:** incursion
**Uwanda wa juu:** plateau
**Uwekezaji:** investment
**Uwili:** dual; duality
**Uzoefu/tajiriba:** experience

V

**Vekta:** vector
**Vertebrata:** vertebrate
**Viazi mishea:** tubers

**Vikundi (ndani ya kundi kubwa):** factions
**Vita vya msalaba:** crusade
**Vuguvugu la ukomeshaji utumwa:** abolitionist movement
**Vuka mpaka/kiuka:** transcend
**Vuruga:** disrupt
**Vurugu:** disruption

W

**Waali:** elite
**Wadhihisha:** weka wazi
**Wadi:** wadi
**Wahemeaji:** gatherers
**Wahka:** insecurity
**Wakati/wakaa:** duration
**Wakazi walowevu/wastakimu:** sedentary people
**Wangwa:** lagoon
**Waraka:** document
**Wari/waliofundwa:** initiates
**Wasta:** intermediary
**Wazawa:** autochtons; indegens
**Wekeza:** invest
**Wendo/machakato:** process
**Woto/mimea:** vegetation
**Yeli:** griot
**Zaka:** toolkit
**Zama za Mawe**: Stone Age
**Zambarau:** violet
**Zana:** Tool
**Zana ya wajihi tatu:** trihedral
**Zana za ujeya:** flaked tools
**Zebu:** smallhorned cattle
**Ziada:** surplus
**Zidua:** extract
**Zima/zuia:** suppress
**Zingia/zuia:** blockade
**Zinjanthropi:** Zinjanthrope
**Zinjantropus:** Zinjanthropo
**Zuio:** blockade
**Zumaridi:** emerald

## Historia Kuu ya Afrika

*Historia* hii inatoa mwanga juu ya umoja wa kihistoria wa Afrika pamoja na uhusiano wake na mabara mengine, hasa Amerika na Karibian. Kwa muda mrefu aina zote za taarifa za kubuni na hisia pendelevu zimeficha historia ya kweli ya Afrika kwa ulimwengu kwa jumla.

Kwa kujumuisha maarifa yetu juu ya Afrika, tukiweka bayana maoni mbalimbali kuhusu tamaduni za Afrika na kwa kupitia upya historia, *Historia* hii ina manufaa ya kutoa mwanga na uvulivuli na kueleza bayana tofauti za mawazo ambazo zinaweza kuwepo baina ya wasomi.

## Mapitio ya Majuzuu yote

"Mazao ya mwanzo ya UNESCO ni lazima yasifiwe kuwa ni mchango mkubwa wa kitaaluma."
Roland Oliver, *Times Literary Supplement*

"Ni mojawapo wa miradi mikubwa ya kitaaluma iliofanyika katika karne hii."
*West Africa*

"Majuzuu haya yametolewa kwa unadhifu mkubwa lakini yana bei nafuu sana ... Yanawakilisha matumizi mazuri kabisa ya pesa ambayo mnunuzi yeyote wa vitabu anaweza kuyapata ..."
Basil Davidson, *Third World Quarterly*

## V Afrika kuanzia Karne ya Kumi na Sita hadi ya Kumi na Nane

Juzuu la V linajadili historia ya Afrika mwanzoni mwa karne ya kumi na sita hadi mwishoni mwa karne ya kumi na nane. Mada kuu mbili zinajitokeza: kwanza mabadiliko ya ndani yanayoendelea ya nchi na tamaduni za Afrika wakati wa kipindi hiki. Pili, uongezekaji wa kujihusisha kwa Afrika kwenye biashara za nje - kukiwa na umuhimu mkubwa lakini ambao hautabiriki kwa dunia nzima.

Huko Afrika Magharibi, Waothomani waliwatamalaki Wamisri na kuanzisha Tawala zao huko Tripoli, Tunis na Algiers. Kusini mwa Sahara, baadhi ya nchi kubwa na za zamani zaidi zilianguka (Songhay Sudan Magharibi, Uhabeshi ya Kikristo), na vituo vipya vya madaraka vilijitokeza (Asante Dahomey, Sakalava). Miundo ya kisiasa na kiutawala ambayo ilikuwa ikiongozwa zaidi kutoka sehemu moja ilijitokeza na jamii zilizokuwa na matabaka ya wazi kijamii na, mara nyingi, yakiwa na mfumo wa ukabaila mkubwa. Dini za asili ziliendelea kuwepo pamoja na Ukristo (ukiwa unarudi nyuma) na Uislamu (ukiwa unaongezeka).

Pwani, hasa ya Afrika Magharibi, Wazungu walianzisha mtandao wa biashara ambao kwa kuanzishwa kwa kilimo cha mashamba makubwa huko New - World, ulikuwa ndio lengo kuu la biashara ya watumwa kimatiafa. Matokeo ya haraka ya biashara hii kwa Afrika yanaelezewa, na inafafanuliwa kuwa matokeo ya muda mrefu kwa dunia nzima ni pamoja na msingi wa uchumi wa dunia hivi sasa, pamoja na hali hiyo ya kutokuwepo na uwiano ndani yake.

TUKI • CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM • UNESCO
S.L.P 35110, Dar es Salaam

ISBN 9976 911 22 X